SHUHUDA KWA KANISA

2026 Edition

1 • 2 • 3 • 4 • 5 • 6 • 7 • 8 • 9



Uhamisho Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

MaarifaMtandaoni.com

RohoYaUnabii.Org

GOMBO LA 3

SAMARITAN LAYMEN MINISTRIES

Enendeni mtandaoni kote

SHUHUDA KWA KANISA

SHUHUDA KWA KANISA
2026 Edition, New Jersey, Marekani
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

2025 EDITION-Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo.

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)

KARIBUNI safari ya KUSIKILIZA NA KUSOMA SHUHUDA PAMOJA
SHUHUDA KATIKA SAUTI- SIKILIZA SHUHUDA
Shuhuda ni magombo tisa, yenye kurasa 4738 yaliyoanza kuandikwa mwaka 1855
Madhumuni, ushauri wa kiroho na ushauri wa kivitendo katika nyanja mbali mbali kama vile (Soma kurasa za 5TShuhuda 663-667)

Miaka 10 iliyopita tulikutana na watu wanaosoma Shuhuda kwa Kingereza (Testimonies for the Church-Revivalplan.com). Walitueleza umuhimu wa kuyasoma magombo haya na kutuhamasisha kuyasoma, hapo ndipo tulipoanza kuyasoma, tulikuwa tumesikia sura zake chache ila siyo sura zote. Tuling'amua kuwa hayakuwa na tafsiri ya Kiswahili. Nasi Tunashauri kila mtu asome magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua wiki 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com). Ukisoma au kusikiliza nusu saa kwa siku, itakuchukua miezi mine kumaliza magombo yote tisa. Tulianza kuyatafsiri kama marafiki miaka sita iliyopita, na ilituchukua muda wa mwaka, kisha tukaingia uhariri, na uhakiki.

Magombo ya Shuhuda tisa, ni kurasa 4738, ambazo zimetafsiriwa kwa ajili ya kila mwanadamu, na hasa wale watu wanaompenda Mungu na kutamani mabadiliko ya tabia. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili na kusambaza kwa

wengine kama zilivyo. Kwa nakala ya kidijitali ya vitabu hivi, tafadhali tembelea R***ohoYaUnabii.Org***, ***RohoYaUnabii.Net***, ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa*** au kwa Kingereza ***WhiteEstate.org***. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18,19 na Kumbukumbu la Torati 4:9.Enendeni Mtandaoni Kote duniani.

Shuhuda zina kila hali ya kusaidia uamsho na matengenezo na kufanya tabia zetu zifae.

Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...." Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu, na kuishi mtindo wa maisha anayotaka Bwana. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua ‘Google App’ ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

-Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze MUNGU na watu, katika muda ambao maadili yanayomomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili! Mpango huu kwa Kingereza utaupata katika Revivalplan.Com

Sambaza Machapisho Kwenye Kila Ardhi, Naam Nchini Kote au Mtandaoni (4Tsw 472)

‘Maelfu ya watu wataoongoka kwenye ile Kweli, katika saa ya kumi na moja, AMBAO wataupata na kuukubali Ukweli wa injili na Neno la Mungu na KUHUISHWA KWA harakati za Roho wa Mungu.—EGW’88 755 (1890). – {LDE 212.2}.’ Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanamwamini Mwenyezi Mungu na kubatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuongeza ladha bila kupoteza maana, wewe boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na maana iliyokusudiwa. Kila Shuhuda imeharirwa mara tano, binafsi

nimepitia mara tatu. Tumeweka Pointers (2Tsw 45.5) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapotaka. Sw inawakilisha, Kiswahili ambacho kinazidi kupanuka na kuwa moja za lugha za Wakristo wengi duniani. Niliona Machapisho ya Nuru kwa Kanisa ambayo sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa yenyewe kabisa kwa uzuri, japo yalichuja kurasa 4738 na kuwa 80 tu!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. Tuna idadi ya vitabu 130 sasa. Kama umeshiriki hii kazi na jina lako halikuweka, tafadhali tujulishe, Asante

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni ROHO MTAKATIFU, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika Mashariki wanahitaji pia kusoma Maandishi ya kalamu iliyovuviwa, kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la MUNGU limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 7000 kati ya 14,000, ambayo bado kufikiwa, angalia Joshuaproject.org na habari za ‘1040 window’

‘Sambaza Biblia kote,’ ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la MUNGU kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lolote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe chochote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto,

aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga ufalme wa Mungu, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandao ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu Afrika, basi tunabidishwa pia kuwa waandishi, Watunzi wa nyimbo, na watu wa kuhifadhi kumbukumbu zetu kwa miaka mingi, kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya Ya jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa umakini, nyimbo zilizoimbwa miaka kama 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu vya tenzi na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabuni, nasi hapa tuna nyimbo nzuri, ambazo zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu ya Biblia takatifu, na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto? Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa ‘Reverse Mission’-misheni iliyogeuka na kuwa kinyume cha kawaida. Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu. Watoto wetu na sisi mara zingine tunaona pengine tuwe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au tuwe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni ule waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je, viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila maandalizi hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba sio utamaduni wetu kuandika, ila sio utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Sio kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii, kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa muktadha wa Maandiko kwa Waamini ni vizuri tupatie watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti na asili ya kabila la mtu, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili, kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali, nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Shuhuda ni vitabu vya mashauri na maonyo. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na ROHO MTAKATIFU kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kiingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana waamini wengu wanaishi chini ya Sahara, ambao kuna wengi wanaozungumza Kiswahili. Kwa sasa, takwimu zinaonesha kuwa Afrika ina asilimia 50% ya waamini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Miaka kama 10 iliyopita, ni asilimia 3% tu ya Maandishi ya Roho ya Unabii ilikuwa imetafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza ‘fluently’ katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la MUNGU

3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni ROHO MTAKATIFU, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua ‘Google App’ ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua zama hizo kulikuwa na mambo gani, mfano mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK zilizozungumziwa; zitakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule utakapoingia katika tovuti. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila mtu magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Zifuatazo ni sentensi za Kalamu ya matumaini, kalamu iliyovuviwa kwa wamaani, ya Ellen

Sababu 18 muhimu, za kuzisoma Shuhuda.

1."Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa MUNGU. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na Zao wenyewe. MUNGU ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la MUNGU kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha MUNGU kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa shuhuda rahisi na za moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka. {5Tsw 664.3}

2.“Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za ROHO WA MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na haya yote yamechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa”. 5Tsw 217.2

3.“Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe WAKE. "Kazi yako," Alinielekeza “Ni kubeba Neno Langu... kuchukua Neno Langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kemea kutokana na Neno, matendo ambayo sio sawa ..... Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… “Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu.” RH, Julai 26, 1906

4.Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao, kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2Tsw 687.2}

5.“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu KUPITIA Shuhuda za Roho WAKE. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu WAKE kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…… Acha shuhuda Ipimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani…… Hakuna kazi ambayo ni nusu ya Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa ROHO WA MUNGU, au wa Shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za ROHO WA MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa Kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wa Sabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za ROHO WA MUNGU. Lt156-1903

6.“Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5Tsw 674

7.“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU … Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ya wengi ni kwamba wanafikiri kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5Tsw 217

8.“Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, na katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, ambazo, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

9.“Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake maradufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, uasi ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Shuhuda haipaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili Kwake, ili Ukweli mzuri wa kunyenyekesha uweze kuwavutia wote... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda….. Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia shuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa, na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili zituamshe na kuvutia akili zetu. Ili sote tusiwe na udhuru FLB: 295

10.“Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika Shuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU, hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyonenwa kupitia chombo CHAKE alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5Tsw 678

11."Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linalowabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili Yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

12."Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …….Watunze Watu, HAO kundi la malisho Yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.' SpM: 384

13."Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu WAKE, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye kutoa tahadhari, makaripio, na maonyo……. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu WAKE wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe KWAKE kwa kila mwale wa nuru ambao umeangazia njia yetu, ikiwa nuru hii imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo." 5Tsw 681

14."Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Nazijua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami….. "Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima yaonekane, na kuamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo zimewaleta watu katika hali mbaya sana, hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Watu Wa laodikia…. RH, Septemba 16, 1873

15."Hatupaswi kuogopa na kuuomba msamaha ulimwengu kwasababu ya kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo. Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi

mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9) kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wa Sabato hawawezi kufanya mapatano yoyote udunia. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Kweli za msingi za Neno la MUNGU … Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

16."Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri wanadamu, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa Ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo za kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo, Ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa. Wajibu wa mwanadamu kwa MUNGU na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la MUNGU, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali MUNGU kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa, na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5Tsw 665.1}

17. “Kiburi, kujipenda, ubinafsi, uchoyo, chuki, husuda na wivu vimefunika kwa ukungu, nguvu za ufahamu, na ile Kweli, ambayo ingewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu. Ile Kweli Imepoteza uwezo Wake-Bwana wa kuchangamsha moyo, na kudhibiti akili. Kanuni muhimu sana za ucha Mungu na ibada, hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na utakatifu wa maisha. Shuhuda hazijaletwa ili kulipuuzia Neno la MUNGU, bali kuliinua juu na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kugusa mioyo ya watu wote. {5Tsw 665.2}

18,"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la MUNGU linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo MUNGU amewawekea hizi kuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za MUNGU, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa MUNGU kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo ile nuru ambayo imekwishakutolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini ninyi hamjaithamini,

mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, ni wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo MUNGU ameridhika kuwapatia. {5Tsw 666.1}

Tunamshukuru sana Mungu kwa msaada Wake toka mwanzo. Tunawashukuru waso maji, wanamaombezi, wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafi ki, wajoli, ndugu katika safari ya kwenda mbinguni. Siku moja tutashangilia pamo ja tutakapoona mavuno!

1. Alex Ngamije -PreciousPresentTruth.org Rwanda
2. Stephen Letta-Masasi, Tanzania
3. Samuel Mhololo -Kigoma, Tanzania
4. Musa Budodi -Shinyanga Tanzania
5 Isack Msusu-Kigoma, Tanzania
6. Mr and Mrs Kumbuka Mlazi Misibo -Kigoma, Tanzania
7. Aimo Abayo –Morogoro, Tanzania
8. Zablon Mgonja -Arusha, Tanzania
9. Mwalimu Peter Marwa -Mwanza, Tanzania
10. Faustine Momadi Mkama -Dar Es Salaam,Tanzania
11. Paul Masaka -Oklahoma, Marekani
12. Ibrahimu Makamba-Tarime, Tanzania
13. Geoffrey Herman -Manyara, Tanzania
14. Pendo Makori -Visiga,Tanzania
15. Judi Mmari Mugane -Siha, Tanzania
16. Kikundi cha Mbaki/Ngulu Maombi -TAUS—USA
17. Women Prayer Warriors WPM -California, Marekani
18. Ezekiel Ojwang -Kiterere,Tanzania
19. John Mugane -Nakuru, Kenya
20. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
21. Eliphas Sambeke -Arusha, Tanzania
22. Stefano Kasiri -Kibaha, Tanzania
23. Gideon Christian - Ukerewe, Tanzania
24. Musa Muneja -Bariadi, Tanzania
25. Victoria Swai Mhololo -Arusha, Tanzania
26. Julius Letta -Morogoro, Tanzania

27. John Chilala Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
28. Milinje Bariki Momadi -Dar Es Salaam, Tanzania
29. Mbaraka Hamisi -Kilimanjaro, Tanzania
30. Rachel Akinyi Atandi-Nairobi, Kenya
32. Mbusi Mpagalushu -Bariadi, Tanzania
33. James Ongoro- Mara, Tanzania
34. Basanthi Thavamani-Lazar -Madras, India
35. Ndege Aruya-Rorya, Tanzania
36. Kwandu Kasiri -Pwani,Tanzania
37. Elinath Elisante Kukome -Kilimanjaro, Tanzania
38. Sharifa Athuman Seleman -Dar-es-Salaam, Tanzania
39. Jackson Musa Singano -Dar-es-Salaam, Tanzania
40. Daniel Masaka -Kisii, Kenya
41. Ellen Nyangoye- Nyagori-Rorya, Tanzania
42. Fares Ogilo-Rorya, Tanzania
43. Walter Nehemia -Dar Es Salaam, Tanzania
44. Gerard Nyafanga -Mara, Tanzania
45. Bilionea Wayoga-Rorya, Tanzania
46. Bettie Magesa Muasya-Machakos, Kenya
47. Kilango Makala -Kilimanjaro, Tanzania
48. Loyce Pima -Bunda, Tanzania
49. Niwaeli Mburuja -Hedaru, Tanzania
50. Cindy Tustch -Washington, Marekani
51. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
52. Sandra Barron -Kentucky, Marekani
53. John Ngasa -Mwanza, Tanzania
54. Methusela Mahumbi-Bariadi, Tanzania
55. Elmad Daudi Ndonga-Mombasa, Kenya
56. Luck Rahim Datoo -Arusha, Tanzania
57. Ruth Lilian Bango -Arusha, Tanzania
58. Mohammed Mboi -Kisii, Kenya
59. William Kalokaza-Rukwa, Tanzania
60. Eline Mrema-Kilimanjaro, Tanzania
61. Obed Lissi-Baraton, Kenya
62. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
63. Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania

64.Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania
65. Mr and Mrs Weber- Alaska, Marekani
66. Eliakim Mabula-Bariadi, Tanzania
67. Ngusa Mayunga-Rukwa, Tanzania
68. Evans Mobegi-Kisii, Kenya
69. Debbie Bisheli-Nairobi, Kenya
70. Yunus Tiras-Tarime, Tanzania
71.Sharon Ondieki-Nairobi, Kenya
72. Ibrahimu Ibare-Tarime, Tanzania
73. Ghati Matiko-Tarime, Tanzania
74. Haron Wamboa-Machakos, Kenya
75. Timothy Misungwi-Michigan, Marekani
76. Enoc Omosa-North Carolina, Tanzania
77. Filipo Lubua-Pittsburg, Marekani
78. Gibson Mujuni-Kagera, Tanzania
79. Lisa Lothian-New York, Marekani
80. Mickey Marr-Scranton, Marekani
81. Philemon Mswanyama-Texas, Marekani
82. Mapesa Kambira-Iowa, Marekani
83. Eduardo Punda-Beira, Mozambique
84. Robert Ndinayo-Goma, Congo
85. Aziz Jacob-Niassa, Mozambique
86.Daudi Jabez Masaka-Harrisburg, Marekani

Wenu katika huduma ya ***MaarifaMtandaoni.Com***, ***MaarifaMtandaoni.Africa*** ***RohoYaUnabii.Org***, ***RohoYaUnabii.Net***, ***RevivalPlan.Com*** na ***Tumaini Ughaibuni Youtube***

Shuhuda zina Kila hali au mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kumwona Mwokozi uso kwa Uso, na kuziona Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA
Wapendwa wa BWANA! Amina
Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

YALIYOMO

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI… 1

UTANGULIZI…. 4

NYAKATI ZA JUZUU YA TATU …. 10

SURA YA 1

WITO KWA WADHAMBI…. 14

SURA YA 2

UWEZO USIOTAKASWA…. 24

SURA YA 3

AKILI ZISIZO NA USAWA…. 33

SURA YA 4

URAFIKI WA KARIBU NA WALIMWENGU…. 39

SURA YA 5

KAZI MJINI NEW YORK 46
SURA YA 6
UZOEFU SI WAKUTEGEMEWA 61
SURA YA 7
UAMINIFU KATIKA KAZI ZA NYUMBANI 70
SURA YA 8
KIBURI NA MAWAZO MATUPU 72
SURA YA 9
KAZI HUKO BATTLE CREEK 75
SURA YA 10
MAFUMBO YA WALIOPOTEA 86
SURA YA 11
KAZI MAKANISANI 91
SURA YA 12
KWA WAZAZI MATAJIRI ..... 100~~101~~
SURA YA 13
ELIMU SAHIHI ..... 111~~112~~
SURA YA 14
MATENGENEZO YA AFYA 135
SURA YA 15
TAASISI YA AFYA 139
SURA YA 16
HATARI YA KUSIFIA, KUMPIGIA MTU MAKOFI, AU KUMSHANGILIA 154
SURA YA 17
KAZI KWA WAKOSAJI 155
SURA YA 18
SHULE YA SABATO 157
SURA YA 19
WATENDAKAZI OFISINI 159
SURA YA 20
UPENDO NA WAJIBU 163
SURA YA 21
KANISA LA BATTLE CREEK 164
SURA YA 22
KAZI YA UMISHONARI ..... 169~~168~~

SURA YA 23
ATHARI YA MAJADILIANO ..... 177~~176~~
SURA YA 24
HATARI NA WAJIBU WA VIJANA ..... 185~~184~~
SURA YA 25
WACHUNGAJI/WATUMISHI WAJITUNZAO WENYEWE (WAJIPENDAO WENYEWE) 189
SURA YA 26
KUPENDA FAIDA KULIKOPINDUKIA ..... 203~~202~~
SURA YA 27
KANISA LA LAODIKIA ..... 209~~208~~
SURA YA 28
MUSA NA HARUNI ..... 241~~240~~
SURA YA 29
KWA MCHUNGAJI KIJANA NA MKEWE ..... 251~~249~~
SURA YA 30
KUOTA NDOTO ZA MCHANA. ..... 269~~268~~
SURA YA 31
UASI MKUBWA ..... 276~~275~~
SURA YA 32
WITO KWA VIJANA ..... 294~~292~~
SURA YA 33
ZAKA NA SADAKA ..... 310~~307~~
SURA YA 34
UTOAJI KWA UKARIMU KWA MPANGO ..... 332~~329~~
SURA YA 35
UHURU WA MTU BINAFSI ..... 336~~333~~
SURA YA 36
UMOJA NDANI YA KANISA ..... 354~~349~~
SURA YA 37
USAFISHWAJI WA KWELI KATIKA HUDUMA ..... 373~~368~~
SURA YA 38
UMUHIMU WA KAZI ..... 380~~374~~
SURA YA 39
HALI YA ULIMWENGU ..... 383~~377~~
SURA YA 40

HALI YA KANISA 386380
SURA YA 41
KUIPENDA DUNIA 388382
SURA YA 42
KIBURI 392386
SURA YA 43
NGUVU YA UCHU WA CHAKULA 395389
SURA YA 44
UONGOZI 401395
SURA YA 45
MIITO KWA AJILI YA UCHANGISHAJI WA FEDHA/MALI 416409
SURA YA 46
WAJIBU KWA WANAOTESEKA 417410
SURA YA 47
WAJIBU WA MWANADAMU KWA WENZAKE 425418
SURA YA 48
DHAMBI YA TAMAA 443435
SURA YA 49
UCHAPAJI KAZI KATIKA HUDUMA 449441
SURA YA 50
WAZAZI KAMA WANAMATENGENEZO 457448
SURA YA 51 .....
"SIWEZI KUSHUKA" 465456

MWITO KWA MPENDWA MSOMAJI…

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu, ushauri, na Maombi yako msomaji. Wako watu wanaoishi nje ya Afrika wanahitaji pia kusoma kwa Lugha ya asili. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi karibu 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window'

'Sambaza Biblia po pote,' ndiyo kauli mbiu ya muumini; sambaza Neno la Mungu kote.

Jiunge nasi katika kuandika vitabu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ikiwa kuna kosa lo lote la kiuandishi au kiutafsiri, tafadhali wasiliana nasi na endapo ukiamua kuchapa, usibadilishe cho chote labda typos tu.

Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Kwa hapa Kwetu Afrika Mashariki, tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu; mada za afya, lishe, mahusiano kama ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake; haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, lakini kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwa sababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine.

Kwa nini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabu, nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu na kuelezea kisa fulani. Kwa nini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vitu vizuri, ikiwemo nyimbo za watoto?. Tuna wataalamu wengi wa nyimbo. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa

mazingira yetu na watoto wetu, na wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule.

Mfano mdogo sana ni, waandishi wengi wa nje huandika vitu vingine visivyoendana na muktadha wetu, mfano vyakula kama Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je viwanda vyetu hutengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana. Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk.

Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! tunaelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya!

Si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii; wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Kitabu cha Jando na Unyago kwa Waumini ni vizuri tupate watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti, na hii inafanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi.

Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio umma. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ikiwa ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani, tafadhali usisite kuutoa na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, fundisha wengine, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa Maandishi yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku.

UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

Back of the BOOK cover -Mkakati wa uamsho au Tumaini linalotiririka ni msaada mkubwa kwetu leo ambao hatuelewi vyema tufanye nini ili Maisha yetu yampendeze Mungu na watu, katika muda ambao maadili yanamomonyoka na ulimwengu hauna mafundisho mema au haufundishi kabisa. Mafundisho haya ni mazuri kwa kila binadamu anayeelewa Kiswahili!

“Nilichukua Biblia ya thamani, na kuizingira kwa “Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa,” zilizotolewa kwa ajili ya watu wa Mungu ili kusahihisha tabia zao. na "Hapa," nilisema na kuona kwamba, "karibu kesi za watu wote zinawakilishwa na maonyo haya waliyopewa watu hawa. Dhambi wanazopaswa kuepuka zimeonyeshwa. Shauri ambalo wangetamani linaweza kupatikana kuhusiana na jambo fulani la maisha yao, lipo hapa kwenye hizi shuhuda, limetolewa tayari, kwani kuna kesi zingine zinazofanana na zao wenyewe kabisa, na ambazo zitatatua tatizo lao wakifuata ushauri wake. Mungu amependezwa kukupa amri juu ya amri na kanuni juu ya kanuni Lakini wengi wenu hamyajui mashauri yaliyomo ndani ya Shuhuda, hamyafahamu Maandiko jinsi mnavyopaswa. Endapo mngelifanya Neno la Mungu kuwa Ndiyo mada kuu ya elimu/mafunzo kwenu, mkiwa na shauku ya kufikia vigezo vya Biblia na ukamilifu wa Kikristo, basi msingezihitaji Shuhuda. Ila ni kwa sababu mmepuuzia kujielimisha na Kitabu cha Mungu kilichovuviwa, yaani Biblia na ndio maana Yeye ametafuta kuwafikia kwa Shuhuda rahisi na nyofu, zinazolenga moja kwa moja mada, akivutia usikivu wenu/wako kwa Maneno yaliyovuviwa. ambayo mlikuwa mmepuuzia kuyatii, na kuwasihi mtengeneze maisha yenu kulingana na mafundisho Yake safi na yaliyotukuka." 5T 664.3

UTANGULIZI

Wapendwa vitabu hivi ni vyetu sote! Maana kila mtu anahitaji Mashauri. Kwenye wingi wa Ushauri hapaanguki jambo, na kuna usalama. Masihi Yu karibu kuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya na yatuchome sana, na kutuvutia tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Hivi ndivyo vitu pekee ambavyo tutaenda navyo mbinguni.

Shuhuda zimejaa mashauri, Makaripio na maonyo ya maisha ya kila siku kwa undani zaidi. Tumeambiwa kwenye maagizo kwamba shuhuda zina kila namna ya kukamilisha tabia zetu. Tulisikia kuhusu kuwepo kwa Shuhuda kwa Kanisa ila hatukujua sana kwamba zinahusiana na nini! Ila baada ya kuanza kusoma kila siku katika mpango wa kusoma Shuhuda Revivalplan.com kwa lugha ya Kingereza tuliona kuna haja kubwa ya kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili maana Divisheni yetu ambayo ina watu wengi wanaozungumza lugha ya Kiswahili, ndiyo Divisheni iliyo na watu wengi duniani (East-Central Africa Division of Seventh-day Adventists) kwa sasa, na takwimu zinaonesha kuwa Afrika sasa ina asilimia 50% ya waumini wanaotarajia marejeo ya YESU (Waadventista). Asilimia 3% ya Maandishi ya Roho ya Unabii yametafsiriwa Kiswahili.

Wana Marejeo wanaozungumza Kiswahili duniani sasa ni 11%. Kutokana na Google wale wanaozungumza Kingereza ‘fluently’ katika nchi za Kiswahilii ni asilimia ndogo sana kuliko tunavyofikiria! Tumepewa ulimwengu wa Kiswahili tuufikie. Hivyo Kutafsiri mambo haya ni jambo la dharura. Katika kutafsiri, Mambo manne ndiyo yalikuwa kwenye mawazo yetu kuliko mengine

1. Yesu Anarudi Upesi, inabidi shuhuda hizi ziwafikie watu mapema na kutayarisha tabia zetu na siku moja tusikie "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu...."

2. Kubeba ujumbe kama ulivyo ili watu wapate kilichonuiwa, bila kupotosha Neno la Mungu

3. Lugha rahisi itakayoweza kusomeka Kenya, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania

4. Sarufi ya lugha ya Kiswahili sanifu iwe imezingatiwa.

Maombi yetu makuu yawe matatu. Nayo ni Roho Mtakatifu, kujisalimisha kwa MUNGU na kuwa ndani Yake Naye ndani yetu. Haya manne yatakuja na baraka zote

tunazozihitaji tunaposoma Hizi shuhuda. Haya ni mausia ambayo yanatubidisha sote wenye mwili kuzisoma hizi shuhuda. Mambo mengine kwa kuelewa zaidi unaweza kupakua 'Google App' ya Roho ya Unabii kwa Kingereza.

Google imesaidia mambo kadhaa mfano Kujua mitindo na mavazi ya sketi za hoops miaka ya 1800BK; itakupa maoni waliyokuwa nayo wakati ule. Japo hekima haiongezeki kwa urahisi, maarifa yameongezeka, hivyo angalia mambo haya kwa kichujio cha Biblia zaidi ya teknolojia. Usiogope kurejelea kamusi, ndio kujifunza. Muumini daima ni mwanafunzi na anasaidiwa zaidi kukumbuka mambo mengi anapotumia machapisho zaidi ya njia zingine. Mengine ya Kingereza imebidi tuweke maana tunayatumia na hivyo utapata utambuzi wa jambo haraka, mfano mara nyingi hatusemi Jimbo, ila Konferensi/conference, majina ya magonjwa au mitindo n.k Tunashauri kila kanisa liwe na magombo yote haya tisa, na Kila kiongozi wa Kanisa na hata mshiriki afanye jitihada ya kuyasoma kwa mpango. Wengi wamechukua miezi 16 kwa kusoma Kurasa 10 kila siku (Revivalplan.com)

Wenu wadhamini, watafsiri, wahariri, washauri, wahakiki, marafiki, wajoli na ndugu katika safari ya kwenda mbinguni.

"Mashaka na hata kutokuamini shuhuda za Roho wa MUNGU, kunayachachua makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa iwe hivi. Wachungaji wanaohubiri ubinafsi badala ya Kristo wangependa iwe hivi. Shuhuda hazisomwi na wala hazithaminiwi. MUNGU amezungumza na wewe. Nuru imekuwa ikiangaza kutoka kwa Neno Lake na Kutoka kwa Shuhuda, na zote zimechukuliwa kwa urahisi na kupuuzwa." 5T 217.2

"Mwokozi wangu alinitangazia kwa mjumbe Wake. "Kazi yako," Alinielekeza "Ni kubeba Neno langu ... kuchukua Neno langu mbele ya wale wasioamini, na kwa kalamu na sauti kukemea kutokana na Neno matendo ambayo sio sawa ... Kwa ushawishi thabiti wa unyenyekevu, kwa sauti na kalamu, ujumbe nitakaoutoa utasikika kutoka kwa mtu ambaye hajawahi kujifunza shuleni… "Usimwogope mwanadamu, Sio wewe unayezungumza: ni Bwana Anayetoa jumbe kwa siku hizi za mwisho; nazo zitaandikwa katika vitabu, na zitasimama milele zote, ili kushuhudia dhidi ya wale ambao wameongozwa kuziacha kwa sababu ya ushawishi wa udanganyifu wa uovu." RH, Julai 26, 1906

Niliona kwamba wote wanapaswa kuchunguza mioyo na Maisha yao kwa ukaribu na kuona ikiwa hawakuwa wamefanya makosa yaleyale ambayo wengine walisahihishwa, na ikiwa maonyo yaliyotolewa kwa wengine hayakuhusu kesi zao wenyewe. Ikiwa ndivyo, wanapaswa kuhisi kwamba ushauri na maonyo yalitolewa haswa kwao na wanapaswa kufanya matumizi hayo kwao kana kwamba walikuwa wanaambiwa wao wenyewe. {2T 687.2}

“Zamani MUNGU alinena na wanadamu kwa kinywa cha manabii na mitume. Katika siku hizi Anazungumza na wanadamu kwa Shuhuda za Roho Wake. Hakukuwa na wakati ambapo MUNGU aliwafundisha watu Wake kwa bidii zaidi ya vile anavyowafundisha sasa juu ya mapenzi Yake na njia ambayo angewataka wafuate…. Acha Ushuhuda upimwe kwa matunda yake .... kwamba kazi hii ni ya MUNGU, au sio ya MUNGU. MUNGU hafanyi chochote kwa kushirikiana na Shetani… Hakuna kazi nusu ya 12 Shetani au nusu ya MUNGU katika jambo hilo. Ushuhuda ni wa Roho wa MUNGU, au wa shetani. Udanganyifu wa mwisho kabisa wa Shetani utakuwa ni kuzifanya Shuhuda za Roho wa MUNGU zisiwe na ushawishi. "Mahali ambapo hakuna maono, watu huangamia." Mithali 29:18. Shetani atafanya kazi kwa ustadi na kwa njia tofauti na kupitia wakala tofauti kutia mashaka imani ya watu wa MUNGU wa masalio katika Ushuhuda wa kweli…. FLB: 296 "Jambo moja ni hakika: Wale Waadventista Wasabato ambao wanachukua msimamo wao chini ya bendera ya Shetani kwanza wataacha imani yao katika maonyo na makaripio yaliyomo katika Shuhuda za Roho wa Mungu. Lt156-1903

“Ukikosa Imani katika Shuhuda utaondoka kwenye Ukweli wa Biblia. 5T: 674

“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu. BWANA hajatufungia mbingu, lakini njia yetu wenyewe ya kurudi nyuma imetutenga na MUNGU… Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ni kwamba kanisa linastawi na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi Wake na linarudi nyuma kuelekea Misri. Walakini ni wachache wanaochukua tahadhari dhidi ya uhitaji wao wa nguvu za kiroho… 5T: 217

“Nimeonyeshwa kuwa kutokuamini Shuhuda kumekuwa kukiongezeka kadiri watu wanavyorudi nyuma kutoka kwa MUNGU. Hali hii ipo katika safu zetu zote, katika nyanja zote. Lakini ni wachache wanaojua ni uzoefu gani kanisa linaenda kupitia. Niliona kwamba kwa sasa tuko chini ya uvumilivu wa BWANA; lakini hakuna anayejua ukubwa wa rehema ambayo imetolewa kwetu. Lakini ni wachache waliojitoa kwa MUNGU kwa moyo wote. Kuna wachache tu ambao, ni kama nyota katika usiku wenye dhoruba kali, huangaza hapa na pale kati ya wingu… RH, Agosti 30,1906

“Wakati Shuhuda, ambazo ziliaminiwa wakati mmoja, zinapotiliwa shaka na kuachwa, Shetani anajua waliodanganywa hawataachia hapo; na huongeza juhudi zake mara dufu hadi atakapowaingiza kwenye uasi wa wazi, ambao huwa hauwezi kupona na huishia katika uharibifu. "Ushuhuda haupaswi kuhafifisha Neno la MUNGU, bali kuliinua na kuzivutia akili kwake, ili Ukweli mzuri wa unyenyekevu uweze kuwavutia wote ... Ikiwa ungefanya Neno la MUNGU kuwa Somo lako, na

hamu ya kufikia Kiwango cha Biblia na kufikia kwa ukamilifu wa Kikristo, usingehitaji Shuhuda… Ukweli wa ziada haujatolewa: lakini MUNGU kupitia Ushuhuda amerahisisha Kweli kuu ambazo tayari zimetolewa na kwa njia Yake Mwenyewe aliyochagua amezileta mbele ya watu ili ziamshe na zivutie akili. ili wote wasiwe na udhuru FLB: 295

“Wengi sasa wanadharau maonyo ya uaminifu yaliyotolewa na MUNGU katika ushuhuda…. Lakini Upinzani dhidi ya vitisho vya MUNGU hautazuia utekelezaji wake. Kukataa Maneno ya Bwana, yaliyosemwa kupitia chombo Chake alichokichagua, itasababisha hasira Yake tu na mwishowe italeta uharibifu kwa mkosaji. 5T: 678

"Uelewa wa wale wanaodharau Shuhuda zilizo wazi za Neno la MUNGU, na kukataa kuamini kwa sababu ni jambo linawabugudhi au lisilovutia wengi kufanya, utatiwa giza; Ukweli utaonekana kwao kama uongo, na uongo utakubaliwa kama Ukweli…. Lakini upendo kwa Kristo na kwa roho ambazo alizifia kwa ajili yake, zitamwongoza mtumishi wa MUNGU kutoa maonyo na wito kwa uaminifu. SW, Juni 23, 1908

"Kupuuza Nuru ni Kuikataa." 13 Agizo nilipewa na Mwokozi, "Sio wewe ambaye wamekukataa, lakini Mimi, Mwokozi wao …… Wale ambao wamepuuza Jumbe ambazo nimempa mjumbe wangu kubeba wamemtukana YULE aliyetoa jumbe hizo. …Watunze Watu, kundi la malisho yangu, wasifundishwe na matabibu au walimu wanaokataa maonyo ambayo nimetoa kupitia mjumbe wangu.’ SpM: 384

"Wengi wanaenda kinyume kabisa na nuru ambayo MUNGU amewapa watu wake, kwa sababu hawasomi vitabu ambavyo vina nuru na maarifa yenye tahadhari, makaripio, na maonyo…. Nuru ya thamani sana, inayotoka kwenye kiti cha enzi cha MUNGU, imefichwa chini ya pishi. MUNGU atawafanya watu Wake wawajibike kwa uzembe huu. Hesabu lazima itolewe Kwake kwa kila mwale wa nuru ambayo imeangazia njia yetu, ikiwa imeboreshwa kwa maendeleo yetu katika mambo ya mbingu au imekataliwa kwa sababu ilikubalika kwao kufuata mwelekeo wa mambo.” 5T: 681

“Ushuhuda huu, ukipokelewa utaamsha utendaji, na kusababisha kujishusha, na kukiri dhambi. Shahidi wa Kweli anasema, "Najua kazi zako, ya kuwa hu baridi wala hu moto." Na tena, " Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." Halafu inakuja ahadi, “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami….. “Makosa na dhambi hizi, ambazo zimewaleta watu wa MUNGU katika hali yao ya unyonge, upofu, na umasikini, lazima zionekane, na zinaamsha toba ya bidii, na kuondoa dhambi hizi ambazo

zimewaleta katika hali mbaya sana. hali ya upofu na udanganyifu wa kutisha. Ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Na hii peke yake itajibu ujumbe kwa Walaodikia…. RH, Septemba 16, 1873

"Hatupaswi kuogopa na kuomba msamaha ulimwengu kwa kuwaambia Ukweli: Tunapaswa kudharau kuficha mambo.Dhihirisha rangi zako halisi ili kukidhi mahitaji ya wanadamu na malaika (1Wakor 4:9 kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu). Wacha ieleweke kwamba Waadventista Wasabato hawawezi kufanya mapatano yoyote. Kwa maoni yako na imani yako lazima kusiwe na kuonekana kidogo kwa kutetereka: ulimwengu una haki ya kujua nini cha kutarajia kutoka kwetu. - Sisi ni wamoja katika imani katika Ukweli wa kimsingi wa Neno la MUNGU… Tuna ujumbe kwaajili ya ulimwengu wote, Amri za MUNGU na Shuhuda za YESU KRISTO ni mzigo wa kazi yetu Ev: 16 na 179

"Niliichukua Biblia ya thamani na kuizingira kwa Shuhuda kadhaa kwa ajili ya Kanisa, zilizotolewa kwa ajili ya watu wa Mungu. Hapa, nilisema, kesi za karibu zote zinapatikana. Dhambi wanazopaswa kuacha zimeianishwa. Shauri wanalotaka linaweza kupatikana hapa, likitolewa kwa kesi zingine zinazofanana na wao wenyewe. Mungu ameridhika kuwapatia kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri. Lakini si wengi wenu ambao wanajua kwa hakika kile kilichomo katika Shuhuda. Hamyafahamu Maandiko. Laiti mngelifanya Neno la Mungu kuwa funzo kwenu, kwa shauku ya kufikia kiwango cha Biblia na kufikia ukamilifu wa Kikristo, msingehitaji Shuhuda. Ni kwa sababu mmepuuza kujifunza Kitabu cha Mungu kilichovuviwa ndio maana Yeye ametaka kuwafikia kwa ushuhuda rahisi na wa moja kwa moja, akiita usikivu wenu kwenye maneno ya uvuvio ambayo mlikuwa mmepuuza kuyatii, na kuwahimiza kuyatengeneza/kuyaumba maisha yenu kulingana na mafundisho yake safi na yaliyotukuka. {5T 664.3}

"Bwana anakusudia kuwaonya, kuwakaripia, kuwashauri, kupitia shuhuda zinazotolewa, na kuzivutia akili zenu kwa umuhimu wa ukweli wa Neno Lake. Shuhuda zilizoandikwa siyo kutoa nuru mpya, bali kusisitiza kwa uwazi kwenye moyo ukweli wa uvuvio ambao tayari umefunuliwa.Wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake umebainishwa waziwazi katika Neno la Mungu, lakini ni wachache miongoni mwenu wanaotii nuru iliyotolewa. Ukweli wa ziada haujatolewa; bali Mungu kupitia Shuhuda amerahisisha zile Kweli kuu zilizokwisha kutolewa na kwa njia Yake aliyoichagua Mwenyewe kuzileta mbele ya watu ili kuziamsha na kuzivutia akili, ili wote waachwe bila kisingizio. {5T 665.1}

“Kiburi, kujipenda, ubinafsi, chuki, husuda na wivu vimefunika nguvu za ufahamu, na Ukweli, ambao ungewafanya muwe na hekima ili kufikia wokovu, mmepoteza uwezo Wake wa kuvutia na kutawala akili. Kanuni muhimu sana za utauwa hazieleweki kwa sababu hakuna njaa na kiu ya ujuzi wa Biblia, usafi wa moyo, na

utakatifu wa maisha. Shuhuda si kwa ajili ya kulidharau Neno la Mungu, bali kuliinua na kuvutia akili, kwamba usahili mzuri wa Ukweli unaweza kuwavutia wote. {5T 665.2}

"Nilisema zaidi: Kama vile Neno la Mungu linavyozingirwa ndani ya vitabu hivi na vipeperushi, ndivyo ambavyo Mungu amewawekea ukuta kwa ajili ya maonyo, mashauri, makemeo na kutia moyo. Hapa mlipo mnalia mbele za Mungu, katika uchungu wa nafsi zenu, kwa ajili ya nuru zaidi. Nimeidhinishwa kutoka kwa Mungu kuwaambia kwamba hakuna mwale mwingine wa nuru kupitia Shuhuda utakaoangaza katika njia yenu mpaka muitumie kwa vitendo nuru iliyokwishatolewa. Bwana amewazingira kwa nuru; lakini hamjaithamini, mmeikanyaga, na wengine wameidharau nuru, wengine wameipuuza au kuifuata lakini kwa kutojali, wachache wameweka mioyo yao kuitii nuru ambayo Mungu ameridhika kuwapatia. {5T 666.1}

Shuhuda zina Kila mazingira ya kutusaidia Tabia zetu, Na Tabia za binadamu wenzetu. Hivi ndivyo vitu pekee yake tutakavyopaa navyo kwenda mbinguni kutoka hapa duniani! Na kuziona uso kwa Uso, Kovu za Mikono, miguu, na ubavu wa Yesu!

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana Yesu! Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa BWANA! Amina

NYAKATI ZA JUZUU YA TATU

MNAMO MWAKA 1872, SHUHUDA YA KWANZA YA JUZUU YA 3 ILIPOANDIKWA, JUHUDI ZA DHEHEBU LA WAADVENTISTA WASABATO ZILIELEKEZWA MAREKANI, KWA KIASI KIKUBWA ZILIJIKITA KATIKA JIMBO LA KATI NA JIMBO LA KASKAZINI-MASHARIKI. KULIKUWA NA WACHUNGAJI/WAHUDUMU THEMANINI NA SITA WALIOWEKWA WAKFU WENYE VIBALI VYA KUHUBIRI UJUMBE NA KUSIMAMIA KAZI. KANISA LILIMILIKI NA KUENDESHA NYUMBA MOJA YA UCHAPISHAJI NA TAASISI MOJA NDOGO YA AFYA, ZOTE ZIKIWA BATTLE CREEK, MICHIGAN. KATIKA KIPINDI CHA ROBO KARNE, MUNGU ALIWAONGOZA WATU WAKE KADIRI WALIVYOWEZA KUSONGA MBELE KWA UMOJA NA UMAHIRI, KWANZA KWA KUWA NA UELEWA MZURI WA MAFUNDISHO YA NENO, WAJIBU WA KUTANGAZA UJUMBE, MFUMO WA KANISA, NA KUENENDA KATIKA NJIA BORA ZA MTINDO WA MAISHA. LAKINI KULIKUWA NA UZOEFU MPYA NA FURSA KUBWA ZA MAENDELEO YA KANISA. MASHAURI YA JUZUU YA 3 YANAELEZEA KWA KINA MAMBO HAYA. [3Tsw 3.1]

MIAKA ISHIRINI NA MITANO ILIYOPITA, MZEE JAMES WHITE ALIKUWA AMEKUWA KIONGOZI WA KAZI MPYA. ALIKUWA AMEANZA KAZI YA UCHAPISHAJI, AKIFANYA KAZI KWA BIDII KWA AJILI YA UTARATIBU WA KANISA, ALIANZISHA SHUGHULI ZA KITABIBU, NA ALIKUWA KIONNGOZI MKUU KATIKA SAFU ZA UTAWALA NA UHARIRI. ALIONESHA NJIA KWA KUWA MWANZILISHI WA KAZI HII. KWA MAONO YAKE YA KIBIASHARA/KIUTAWALA NA BIDII YAKE YOTE KWA KANISA LINALOKUA, ALITAMBULIWA KAMA NDIYE KIONGOZI. KWA HALI HIYO, ILIKUWA NI KAWAIDA KWA WENGINE KUSHINDWA KUONA KWAMBA WANAPASWA KUWAJIBIKA KATIKA SHUGHULI MBALIMBALI ZA DHEHEBU HILI LINALOKUA. JUZUU HILI LINAFUNGUA MJADALA WA TATIZO HILI NA KUTOA WITO KWA WATENDA KAZI KUSHIRIKI PAMOJA KUITENDA KAZI YA KUBEBA MZIGO KATIKA MAKAO MAKUU GC, ILI KUMPUNGUZIA JAMES WHITE, MZIGO WA KAZI ULIOKUWA UKIMUELEMEA. ZAIDI YA YOTE, KUPITIA JUZUU HII, REJEA ZIMEFANYWA KWA KUANGALIA UKUAJI WA KAZI INAYOENDELEA, MAJUKUMU YANAYOONGEZEKA, NA HITAJI LA KUWATAKA VIJANA KUSHIRIKI KATIKA KUIFANYA KAZI. HATARI ZA KUMTAZAMA MTU MMOJA KAMA KIONGOZI MKUU ZILITAMKWA WAZIWAZI. [3Tsw 3.2]

UZOEFU WA KIPINDI HIKI NI SAWA NA ULE WA TAI ANAYEFUNDISHA WATOTO WAKE KURUKA KWA MARA YA KWANZA, AKIWA AMEMBEBA KINDA MGONGONI MWAKE NA KISHA KUMUACHA ILI AWEZE KUIMARISHA NGUVU ZAKE, HUKU MZAZI AKIWA DAIMA KARIBU ZAIDI, ILI KUTOA MSAADA PALE UNAPOHITAJIKA. AFYA YA JAMES WHITE ILIYODHOOFIKA, IMANI YAKE KUWA WENGINE WANAPASWA KUSHIRIKI KATIKA KUIINUA KAZI, NA WITO WA MARA KWA MARA KWAKE KUSHIRIKI KATIKA KAZI MAHALI TOFAUTI, YOTE HAYA YALIELEKEA KUMTENGANISHA NA KAZI ZA KIUTAWALA HUKO BATTLE CREEK. WAKATI BWANA NA BIBI WHITE WAKIENDELEA KUITUNZA NYUMBA YAO ILIYOKUWA KATIKATI YA KITUO KIDOGO CHA AFYA NA OFISI

ZA UCHAPAJI HUKO MAKAO MAKUU, MARA NYINGI WALIPATIKANA KATIKA MAENEO YA MBALI. KATIKA MSIMU WA JOTO MWAKA1872 NA 1873, WALITUMIA MUDA WAO KUPUMZIKA KATIKA MILIMA YA COLORADO, NA KWA MIEZI KADHAA WALIKUWA CALIFORNIA. MWAKA 1874, WALITUMIA MUDA MWINGI ZAIDI KATIKA PWANI YA MAGHARIBI, NDANI YA MUDA HUO MZEE
WHITE ALIANZA UCHAPAJI WA MAKALA IITWAYO ISHARA ZA NYAKATI. HIVYO WENGINE WALILAZIMIKA KUCHUKUA MAJUKUMU YA UONGOZI HUKO MAKAO MAKUU, NA KAZI ILIIMARIKA. [3T 3.3]

HIKI KILIKUWA KIPINDI KIGUMU PIA, KWANI, WAKATI AMBAPO KANISA LILIKUWA LIKITAFUTA UFUMBUZI KATIKA SUALA LA UONGOZI, WENGINE WALIJIKITA KATIKA USISITIZAJI WA UHURU WA MTU BINAFSI, NA WALIKUWA KATIKA HATARI YA KUURUDIA UZOEFU WA KORA, DATHANI, NA ABIRAMU WAKIPINGA MAMLAKA THABITI YALIYOWEKWA NA BWANA. MAMBO AMBAYO YAMEANDIKWA HAPA NA PALE KATIKA JUZUU YA 3 NI MASHAURI YANAYOTOA USHAWISHI ADILIFU KUPITIA UZOEFU HUU. ZIFUATAZO NI BAADHI YA KANUNI ZA SHIRIKA NA UONGOZI ZILIZOORODHESHWA KWA LUGHA NZURI HAPA NA PALE. [3Tsw 4.1]

KIPINDI CHA MIAKA MITATU CHA NYAKATI ZA JUZUU HII KILIASHIRIA MWISHO WA MUONGO WA KWANZA WA MAFUNDISHO NA MAZOEZI YA MATENGENEZO YA AFYA. USHAURI ULITOLEWA KUJILINDA DHIDI YA MAMBO YALIYOVUKA MIPAKA YAANI KUPITILIZA NA TOFAUTI MBALIMBALI. TENA NA TENA, KATIKA MAKALA ZA JUMLA NA SHUHUDA BINAFSI, ELLEN WHITE ALIELEKEZA KWENYE KANUNI KUU ZA KIASI NA KUISHI KWA UADILIFU, HUKU AKIWAITA WATU KUSONGA MBELE KATIKA UZOEFU WAO MPYA WA MATENGENEZO YA AFYA. [3Tsw 4.2]

YOTE HAYA YALIKUWA KWA AJILI YA KUWEKA MSINGI MZURI ILI KUKUA ZAIDI. ILIKUWA NI KATIKA KIPINDI HIKI AMBAPO WAUMINI WALIANZA KUPATA MTAZAMO WA ULIMWENGU MZIMA KAMA UWANJA WA KAZI. HUU ULIKUWA NI MTAZAMO WA KUSHANGAZA. ULILETA CHANGAMOTO. HAWAKUONA UMUHIMU WA SHULE NDOGO YA KANISA ILIYOANZISHWA HUKO BATTLE CREEK NA GOODLOE H. BELL, MWALIMU MZOEFU AMBAYE ALIUPOKEA UADVENTISTA KUPITIA UKARIBU NA WAUGUZI NDANI YA KITUO CHA TIBA RAHISI YAANI SANITARIUM, AKIWA MGONJWA. MAPEMA MWAKA 1872 MWANZONI MWA MAJIRA YA JOTO NDIPO ALIPOIANZISHA SHULE HIYO YA KWANZA. BAADAYE KIDOGO NDANI YA MWAKA HUO ILIWEKWA MIPANGO YA KWANZA, KWA AJILI YA SHULE KUBWA ZAIDI ILI KUTOA MAFUNZO KWA WATENDAKAZI YENYE MAMBO YA ZIADA. MWEZI DESEMBA, NDIPO SHUHUDA NA. 22 ILIPOWAFIKIA WATU WETU, WALIKUTA KATIKA UTANGULIZI KUNA WITO NA MAELEKEZO YA NAMNA YA SHULE NA JINSI YA KUIENDESHA. "ELIMU SAHIHI" NI KICHWA CHA MAKALA YA KURASA THELATHINI KINACHOONESHA MAONO MAKUU YA MSINGI JUU YA MAFUNZO YA VIJANA WETU. TUNGEWEZAJE KUUZUNGUKA ULIMWENGU NA UJUMBE WETU BILA KUWA NA WATENDA KAZI WALIYOELIMIKA? JE, TUNGEWEZAJE KUWA NA HUDUMA YA KUTOA ELIMU BILA KUWA NA SHULE?

WAKISIMAMA ILI KUTII MAAGIZO NA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA KITABU HIKI KURASA ZA 131-160, MABABU ZETU WALIANZISHA MFUMO WA ELIMU KWA KUANZA NA CHUO CHA BATTLE CREEK. JENGO LAKE KUU LILIWEKWA WAKFU MNAMO JANUARI 4, 1875.[3Tsw 4.3]

MIEZI MICHACHE TU KABLA YA TUKIO HILO KUBWA, MZEE JOHN N. ANDREWS, MMOJA WA WAHUDUMU WETU WAKUU, ALITUMWA USWISI KUWA MUASISI WA KUTANGAZA UJUMBE HUKO ULAYA. KATIKA MASHAURI YALIYOTOLEWA MIEZI MICHACHE KABLA, ELLEN WHITE ALIKUWA AMEANDIKA JUU YA HITAJI LA WAMISHENARI “KWENDA KATIKA MATAIFA MENGINE KUHUBIRI UKWELI KWA UANGALIFU MKUBWA.” UKURASA WA 204. MZEE ANDREWS ALISAFIRI MNAMO MWAKA 1874 KIPINDI CHA MAJIRA YA MAJANI KUPUKUIKA, WAADVENTISTA WA SABATO WALIANZA KUELEKEZA MACHO YAO KATIKA NCHI NYINGINE. [3Tsw 5.1]

MUDA AMBAO JUMBE ZA MASHAURI NA MAELEKEZO ZIMETUJIA NDANI YA MIAKA HII NI ZA KUSTAAJABISHA NA KUPENDEZA SANA. KUANZIA MWAKA 1859, WAADVENTISTA WASABATO WALIKUWA WAMEENDELEA KATIKA KUFANYA WAJIBU WAO KWA MUNGU WALIPOUTAMBUA UWAJIBIKAJI NA UWAKILI WAO KUPITIA UKARIMU WA MPANGO; LAKINI HAPO AWALI HAWAKUUTAMBUA WAJIBU KAMILI WA ZAKA, SEHEMU YA KUMI YA MAPATO. KATIKA VIFUNGU VIWILI, VYA MOYO WA JUZUU YA 3, HIVI SASA KATIKA MAKALA MBILI NDANI YA KIINI CHA JUZUU YA TATU KAMA MJUMBE WA BWANA ALIVYOANDIKA JUU YA "FUNGU LA KUMI LA" "MAPATO" NA "FUNGU LA TISA YA KUMI" INAYOBAKI. HADI MWAKA 1879 NDIPO DHANA HII PANA YA UTOAJI KWA UKARIMU ILIPOANZA KUKUBALIKA KUWA SEHEMU YA SERA YA MADHEHEBU, LAKINI HATUA HIYO ILIYOFANYA MENGI ILI KUHAKIKISHA MAPATO THABITI NA YANAYOHITAJIKA SANA KWA KAZI INAYOKUA ILIKUWA NA MIZIZI YAKE KATIKA MASHAURI YANAYOPATIKANA KWENYE SURA HIZI MBILI, “ZAKA NA SADAKA” NA “KUTOA KWA UKARIMU,” AMBAZO ZILICHAPISHWA MAPEMA MWAKA 1875. DHANA KAMILI YA UWAKILI WA KWELI ILITAMBULIWA KADIRI TULIVYOONGOZWA KUONA YA KWAMBA WITO WA UKARIMU WA MPANGO ULIKUSUDIWA NA MUNGU, SI TU KWA AJILI YA KUPATA PESA, BALI KAMA NJIA YA KUKUZA NA KUKAMILISHA TABIA YA MTOAJI. [3Tsw 5.2]

KAMA ITARAJIWAVYO, MPANGO WA UINJILISTI ULISABABISHA MZOZO NA VIKUNDI VINGINE VYA KIDINI, AMBAVYO MARA NYINGI VILITUPA CHANGAMOTO ZA MDAHALO NA MABISHANO. MIAKA KUMI ILIYOPITA MOSES HULL, MMOJA WA WAHUDUMU WETU, ALIIPOTEZA IMANI KWA KUJIUNGA NA UPANDE WA ADUI KUPITIA MIDAHALO YA AINA HIYO. SASA MASHAURI YALIYORUDIWARUDIWA YALITOA MWONGOZO HUKU YAKIONESHA HATARI NA FAIDA NDOGO ZA MAHUBIRI YA AINA HIYO. JUZUU YA 3 IMEJAA MASHAURI HAYO. [3Tsw 6.1]

KWA HIVYO MADA ZILIZOPO KATIKA JUZUU HII NI ZA TOFAUTI, ZIKITOA USHAURI KUANZIA KWA MKULIMA TAJIRI NA MKEWE ASIYE NA ELIMU HADI KWA

WAKURUGENZI NA WAHUBIRI. NAKALA ZA JUMLA ZINAJAZA SEHEMU KUBWA YA JUZUU HII. JUMBE BINAFSI, ZILIZOCHAPISHWA KWA MANUFAA YA WOTE ZINAPATIKANA KATIKA SEHEMU MBALIMBALI ZA JUZUU HII, KWA SABABU, KAMA ELLEN WHITE ALIVYOANDIKA, JUMBE NYINGI SANA ZINAHUSIANA NA MAMBO YALIYOZOELEKA "AMBAZO KATIKA MAMBO MENGI HUWAKILISHA MAMBO YA WENGINE." [3Tsw 6.2]

MAFUNUO MACHACHE BORA YANAUNDA MSINGI WA SEHEMU KUBWA YA KITABU HIKI. KATIKA KIPINDI HIKI MAONO YALIYOJIPAMBANUA YALIKUWA NI MACHACHE, LAKINI YA KINA ZAIDI. TENA NA TENA REJEA IMEFANYWA KWENYE MAONO YA KINA YA DESEMBA 10, 1871, NA JANUARI 3, 1875. MAONO HAYA YANAFAFANULIWA NA JAMES WHITE KATIKA MAELEZO YA CHINI KWENYE UKURASA WA 570. MAZINGIRA YA MAONO YA KWANZA YATAELEZWA KWA UKAMILIFU ZAIDI HAPA: ILIKUWA HUKO BORDOVILLE, VERMONT, MAONO HAYA YALIPOTOLEWA. RIPOTI YA MKUTANO ULIOFANYIKA MAHALI HAPO, DESEMBA 9 NA 10, ILITUMWA KWA AJILI YA KUFANYIWA MAPITIO NA MZEE A. C. BOURDEAU, AMBAYO YALIFANYIKA NYUMBANI KWAKE. KUPITIA HILI TUNAJIFUNZA KUWA BIBI WHITE ALIFANYA KAZI "HASA KWA AJILI YA KANISA." KATIKA MKUTANO MMOJA WA JIONI "SHUHUDA MAALUM ZILITOLEWA KWA WATU WALIOHUDHURIA; NA HAYA YALIPOIDHINISHWA [KWA WALE WALIOYASIKIA], NURU NA UHURU VILIINGIA NDANI YAO." JUMAPILI MCHANA WANA WAWILI WA MUUMINI NA MKE WA MMOJA KATI YA WALE WAUMINI WALIKUJA KUMUAGA BIBI WHITE. WALIKUWA "WAMERUDI NYUMA." KISHA MZEE BOURDEAU ANAELEZEA KILE KILICHOTOKEA: [3T 6.3]

"KATIKA HATUA HII, DADA WHITE ALIUHISI MZIGO HALISI WA MATATIZO YAO, NA SHAUKU YA PEKEE KWA AJILI YA WOKOVU WAO, AKAWAPA MAAGIZO TELE. KISHA AKAPIGA MAGOTI PAMOJA NAO NA KUWAOMBEA KWA SHAUKU KUBWA, IMANI, NA UIMARA, ILI WAWEZE KUMRUDIA BWANA. WALIKUBALI NA KUOMBA, WAKIAHIDI KUMTUMIKIA BWANA. ROHO WA BWANA AKAKARIBIA ZAIDI NA ZAIDI. DADA WHITE ALIKUWA HURU, NA PUNDE, BILA KUTARAJIA, ALIKUWA KATIKA MAONO. ALIBAKI KATIKA HALI HII KWA DAKIKA KUMI NA TANO. [3Tsw 7.1]

"HABARI HIZO ZILIENEA, NA PUNDE NYUMBA ILIJAA WATU. WADHAMBI WALITETEMEKA, WAUMINI WALILIA, NA WALIORUDI NYUMA WALIMRUDIA MUNGU. JAMBO HILI HALIKUWAHUSISHA WALE WALIOKUWEPO TU, KAMA TULIVYOJIFUNZA TANGU AWALI. BAADHI YA WALIOKUWA WAMEBAKI NYUMBANI WALIJIHISI KUWA NA HATIA SANA. WALIHISI KUWA WAMEFANYA JAMBO AMBALO HAWAKUWAHI KULIFANYA HAPO AWALI. MALAIKA WA MUNGU ALIKUWA ANATIKISA MAHALI PALE. MWISHO WA WAKATI, VITISHO, UKARIBU WA HUKUMU INAYOKUJA, WAKATI WA TAABU, AKILI ZA KIDUNIA KANISANI, UKOSEFU WA UPENDO WA KINDUGU, NA HALI YAO YA KUTOKUWA TAYARI KUKUTANA NA BWANA, VILIATHIRI SANA MAWAZO YA WOTE." THE REVIEW AND HERALD, DESEMBA 26, 1871. [3Tsw 7.2]

HIZO NDIZO NYAKATI ZA JUZUU YA TATU 3. [3Tsw 7.3]

Wadhamini wa machapisho ya Ellen G. White.

SURA YA 1

WITO KWA WADHAMBI

Ndugu Wapendwa Kaka na Dada: Ninahisi ninalazimika wakati huu kutekeleza jukumu ambalo lilipuuzwa kwa muda mrefu. {3Tsw 9.1}

Kwa miaka iliyotanguliwa na ugonjwa hatari na wa muda mrefu, mume wangu alikuwa anafanya kazi zaidi kuliko wanaume wawili walivyopasa kufanya kwa wakati mmoja. Hakuona wakati wowote ambao angeweza kupumzika kutoka kwenye shinikizo la utunzaji na kupata mapumziko ya akili na mwili. Kupitia ushuhuda alionywa kuhusu hatari yake. Nilioneshwa kwamba alikuwa akifanya kazi nyingi sana za kuuchosha ubongo. Nitanakili hapa ushuhuda ulioandikwa mnamo Agosti 26, 1855: {3Tsw 9.2}

"Nilipokuwa Paris, Maine, nilioneshwa kuwa afya ya mume wangu ilikuwa katika hali mbaya, kwamba hali ya kukosa utulivu wa akili ilikuwa kubwa sana kiasi cha uwezo wake kutostahimili. Wakati Ukweli wa leo ulipochapishwa kwa mara ya kwanza, aliweka jitihada sana na alifanya kazi bila kutiwa moyo hata kidogo au msaada kutoka kwa ndugu zake. Toka mwanzo alichukua mizigo juu yake ambayo ilikuwa ya kuchosha nguvu zake za mwili. {3Tsw 9.3}

“Mizigo hii, kama ingeshirikishwa kwa watu wote kiusawa isingekuwa ya kuchosha hivyo. Wakati mume wangu akichukua jukumu kubwa, baadhi ya ndugu zake katika huduma hawakuwa tayari kubeba chochote. Na wale walioyakimbia majukumu, hawakutambua mizigo yake, na hawakupendezwa na maendeleo hayo ya kazi na mradi wa Mungu kama ambavyo wangepaswa kufanya. Mume wangu alihisi upungufu huu na akaweka bega lake chini ya mizigo ambayo ilikuwa mizito sana na ambayo ilikuwa karibu imponde. Kama matokeo ya juhudi hizi za ziada roho zaidi zingeokolewa, lakini ni juhudi hizi hizi ambazo ziliharibu afya yake na kumnyima nguvu. Nimekuwa nikioneshwa kuwa anapaswa kwa kiasi kikubwa kuweka kando wasiwasi wake; Mungu yuko tayari kuruhusu afunguliwe kutoka kwa kazi hiyo ya kuchosha na kwamba anapaswa kutumia wakati mwingi katika kusoma Maandiko na katika jamii ya watoto wake, akitafuta kukuza akili zao. {3Tsw 9.4}

“Niliona kuwa halikuwa jukumu letu kujifadhaisha/kujichanganya wenyewe na majaribio ya mtu binafsi. Kazi kama hiyo ya mateso ya akili ilivumilia inayokuwepo kwa makosa ya watu wengine inapaswa kuepukwa. Mume wangu anaweza

kuendelea kufanya kazi kwa nguvu zake zote, kama ambavyo amekuwa akifanya na kama sehemu ya matokeo kujikuta akishuka kaburini, na kazi zake zikapotea kinyume cha kusudi la Mungu; au anaweza sasa aachiliwe, akiwa amebakiwa na nguvu kidogo, na akae zaidi, na kazi yake ikiwa na ufanisi zaidi.” {3Tsw 10.1}

Sasa nitanakili kutoka kwenye ushuhuda uliotolewa mnamo 1859: "Katika maono yangu ya mwisho nilioneshwa kwamba Bwana angefanya mume wangu ajitoe zaidi kwa kusoma Maandiko, ili aweze kuwa na sifa ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa neno na mafundisho, kwa njia zote mbili yaani kwa kuzungumza na kwa kuandika. Niliona kuwa huko nyuma tulikuwa tumejimaliza nguvu zetu kwa njia ya wasiwasi mwingi na uangalizi wa kulea kanisa na kuliweka katika nafasi nzuri. Kazi hii ya kuchosha katika maeneo mbali mbali, tukibeba mzigo wa kanisa, haihitajiki; kwa kuwa kanisa linapaswa kubeba mizigo yake lenyewe. Kazi yetu ni kuwafundisha katika Neno la Mungu, kuwahimiza juu ya umuhimu wa vitendo na kufafanua kwa usahihi zaidi nafasi yetu sahihi juu ya Ukweli. Mungu angetutaka tupaze sauti zetu kwenye mikusanyiko yetu juu mikubwa ya mambo muhimu kuhusiana na Ukweli wa leo. Mambo haya yanapaswa yawasilishwe kwa uwazi na kwa kudhamiria, na yanapaswa pia kuandikwa, ili wajumbe wa kimya waweze kuyapeleka mbele ya watu kila mahali. Kujitoa kukamilifu kwa kazi iliyo muhimu kunahitajika zaidi kwa upande wetu; tunapaswa kuwa wakweli ili kuishi katika nuru ya sura ya Mungu. Kama akili zetu zisingetekwa sana na mahangaiko ya kanisa zingekuwa huru zaidi kutumiwa juu ya masomo ya Biblia; na matumizi ya karibu ya Ukweli wa Biblia yangeizoesha akili kutembea katika welekeo huo, na hivyo tungekuwa tumefuzu kwa kazi tuliyokabidhiwa. {3Tsw 10.2}

“Nilioneshwa kwamba Mungu hakuweka juu yetu mizigo mizito ya aina hiyo kama tulivyofanya huko nyuma. Ni wajibu wetu kuzungumza na kanisa na kuwaonesha umuhimu wa kujifanyia kazi wao wenyewe. Wamekuwa wakibebwa sana. Sababu inayofanya tusihitajike kuchukua mizigo mizito na kushiriki katika kazi ya kujichosha ni kwamba Bwana ana kazi ya aina nyingine anayotaka tuifanye. Asingependa kuona tukiichosha miili yetu na nguvu za akili zetu, bali kuiweka akiba kwa wakati maalum, wakati msaada halisi utakapohitajika, na sauti zetu zitakaposikika.” {3Tsw 11.1}

“Niliona kwamba maendeleo muhimu yangepaswa kufanyika, ambayo yangehitaji ushawishi wetu kuyaongoza; mivuto hiyo ingeibuka, na makosa yangeletwa mara kwa mara kanisani, na ndipo ushawishi wetu ungehitajika. Lakini ikiwa tutakuwa tumechoshwa na kazi za hapo awali, tusingekuwa na hayo maamuzi yenye utulivu, busara, na kujitawala yaliyo muhimu kwa nyakati muhimu ambazo Mungu angetutaka tutende sehemu yetu muhimu. {3Tsw 11.2}

“Shetani amedhoofisha juhudi zetu kwa kuliathiri kanisa hata kusababisha tufanye kazi mara mbili ili tuweze kupata njia ya kupita kwenye giza na kutokuamini. Jitihada hizi za kuweka mambo sawa katika makanisa zimetumalizia nguvu zetu, na kufuatiwa na uchovu na udhaifu. Niliona kwamba tunayo kazi ya kufanya, lakini mpinzani wa roho zetu atapinga kila juhudi tunayojaribu kuifanya. Watu wanaweza kuwa katika hali ya kurudi nyuma, ili Mungu asiweze kuwabariki, na hili litakuwa ni jambo la kukatisha tamaa; lakini hatupaswi kuvunjika moyo. Tunapaswa kufanya wajibu wetu katika kuwasilisha nuru, na kuyaacha majukumu mikononi mwa watu.” {3Tsw 11.3}

Nitanakili hapa kutoka kwa ushuhuda mwingine, ulioandikwa Juni 6, 1863: "Nilioneshwa kuwa ushuhuda wetu bado unahitajika katika kanisa, ili tufanye kazi ya kujiokoa wenyewe kutoka kwenye majaribu na mahangaiko, na kwamba tunapaswa kuhifadhi mkao wa kiibada wa akili. Ni jukumu la wale walio ofisini kuzitumikisha zaidi akili zao ili mume wangu aitumikishe akili yake kidogo. Wakati mwingi unatumika na mume wangu kushughulika na mambo mbalimbali ambayo humchanganya na kumchosha akili, na kumuweka katika mazingira ambayo hayampi nafasi ya kusoma au kuandika, na hivyo kuzuia nuru yake isiangaze kama ilivyopaswa kuwa. {3Tsw 11.4}

“Akili ya mume wangu haipaswi kusongwa mno na kutumikishwa kupita kiasi. Lazima iwe na mapumziko, na lazima aachwe huru kuandika na kuzingatia mambo ambayo wengine hawawezi kufanya. Wale waliowekwa ofisini wangeweza kuinua kutoka kwake mzigo mzito wa uangalizi wa makanisa kama wangejitoa wenyewe kwa Mungu na kuhisi hamu kubwa ya kazi. Hakuna hisia za ubinafsi ambazo zingepaswa kuwepo miongoni mwa wale wanaofanya kazi ofisini. Ni kazi ya Mungu wanayoshughulika nayo, na watawajibika kwake kwa misukumo wanayoionesha na kwa jinsi sehemu hii ya kazi yake inavyofanywa. Wanapaswa kutiisha akili zao. Wengi wanahisi kuwa hapatakuwa na lawama itakayofungamanishwa na usahaulifu. Hili ni kosa kubwa. Kusahau ni dhambi. Kunapelekea kuboronga kwingi, machafuko mengi, na makosa mengi. Mambo yale yanayopaswa kufanywa yasisahauliwe. Akili lazima ipewe jukumu; ni lazima iadibishwe hadi ikumbuke. {3Tsw 12.1}

“Mume wangu amekuwa na uangalizi mwingi [wa makanisa], na amefanya mambo mengi ambayo wengine walipaswa kuyafanya, lakini ambayo aliogopa [kuwatuma] wafanye, isije, kwa kutotii kwao, wakafanya makosa ambayo isingekuwa rahisi kuyasahihisha na hivyo kuingia kwenye hasara kubwa. Hili limekuwa likisababisha mkanganyiko mkubwa kwenye kwa akili yake. Wale wanaofanya kazi ofisini wanapaswa kujifunza. Wanapaswa kusoma, na kufanya mazoezi, na kutumia akili zao wenyewe; kwa kuwa wanayo sehemu hii ya kazi wao wenyewe, wakati mume wangu ana majukumu ya idara nyingi za kazi. Kama mtendakazi akifanya makosa,

anapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wake kurekebisha uharibifu [uliosababishwa] kwa kutumia kipato chake mwenyewe, na kamwe pasiruhusiwe ofisi kupata hasara kupitia kwa uzembe wake. Asiache kutekeleza majukumu yake, lakini inampasa kujaribu tena, akiepuka makosa ya zamani. Kwa njia hii atajifunza kuwa na uangalifu ule ambao Neno la Mungu daima limekuwa likihitaji, na kwamba hatafanya zaidi ya wajibu wake. {3Tsw 12.2}

“Mume wangu angepaswa kuchukua muda kufanya mambo yale ambayo dhamira yake inamwambia yangehifadhi afya yake. Amedhani ya kwamba ilimpasa atupilie mbali mizigo na majukumu vilivyokuwa juu yake na kuiacha ofisi, au vinginevyo akili yake ingeweza kuvunjika. Nilioneshwa kwamba kama Bwana angemwachilia kutoka kwa wadhifa wake, angempa ushahidi wa wazi wa kuachiliwa kwake kama vile alivyompa [ushahidi huo] wakati alipomtwisha mzigo wa kazi juu yake. Lakini amebeba mizigo mingi sana, na wale wanaofanya kazi naye huko ofisini, na pia ndugu zake wanaomhudumia, wamekuwa wakiridhika kumuachia ayabebe. Kimsingi wamesimama nyuma ili wasibebe mzigo, na wamekuwa wakiwatuliza wale waliokuwa wakinung’unika dhidi yake, na kumuacha [mume wangu] akisimama peke yake akiwa amepinda na chini ya mzigo, hadi Mungu alipothibitisha kusudi lake mwenyewe. Kama tu wangechukua sehemu ya wajibu wao kwa ajili ya ule mzigo, mume wangu angepata unafuu. {3Tsw 13.1}

“Niliona kwamba Mungu sasa anatutaka tuchukue uangalifu maalum wa afya aliyotupatia, kwani kazi yetu bado haijakamilika. Ushuhuda wetu bado unapaswa kutolewa, nao utakuwa na ushawishi. Tunapaswa kuhifadhi nguvu zetu ili tuzitumie kwa kusudi la Mungu wakati kazi yetu itakapohitajika. Tunapaswa kuwa waangalifu kutochukua mizigo juu yetu, ile ambayo wengine wanaweza na wangepaswa kuibeba. Tunapaswa kuhimiza mkao wa akili wenye furaha, matumaini, na amani; kwa kuwa afya yetu kwa sehemu kubwa inategemea hali hiyo. Kazi ambayo Mungu anataka tufanye haizuii kujali afya zetu, ili tupone na athari za kazi nyingi tunazojitwisha. Afya zetu zinapokuwa kamili ndipo na kazi zetu zinapokuwa kamili zaidi. Tunapozichosha nguvu zetu, tunaishiwa nguvu, tunakuwa kwenye hatari ya kupata mafua, na katika nyakati kama hizo kunakuwepo hatari ya kupata magonjwa ya hatari. Tusiache wajibu wa kutunza afya zetu mikononi mwa Mungu, wakati Yeye ameweka wajibu huu mikononi mwetu.” {3Tsw 13.2}

Oktoba 25, 1869, nilipokuwa Adams Center, New York, nilioneshwa kwamba baadhi ya wachungaji kati yetu hushindwa kubeba jukumu lote ambalo Mungu angetaka wawe nalo. Ukosefu huu unatoa kazi ya ziada kwa wale walio wabeba mizigo, na hasa juu ya mume wangu. Wachungaji wengine hushindwa kutoka na kuhatarisha maisha yao kwa ajili kusudi na kazi ya Mungu. Maamuzi muhimu yanapaswa kufanyika; lakini kwa kuwa mwanadamu mwenye asili ya kufa hawezi

kuuona mwisho tangu mwanzo, wengine hukataa kujitosa na kusonga mbele kadiri majaliwa ya Mungu yanavyoongoza. Mtu fulani lazima asonge mbele; mtu fulani lazima ahatarishe maisha katika hofu ya Mungu, akitumainia kutoka Kwake. Wachungaji hao wanaokwepa aina hii ya kazi wanapoteza mengi. Wanakosa kuupata uzoefu ule ambao Mungu alipanga waupate ili kuwafanya imara, na kuwafanya watu wenye ufanisi wanaoweza kutegemewa katika dharura yoyote ile. {3Tsw 13.3}

Ndugu A, unaogopa kujiingiza katika hatari. Hauko tayari kujitosa pale unapokuwa huwezi kuona njia wazi kabisa. Hata hivyo ni lazima mtu fulani aifanye kazi hii; mtu fulani lazima atembee kwa imani, vinginevyo hakuna maendeleo yoyote yatakayofanyika, na hakuna kitakachokamilishwa. Hofu kwamba unaweza kufanya makosa na kwenda vibaya, na kisha ulaumiwe, inakufunga. Unajipatia udhuru wa kutochukua jukumu lolote kwa kuwa umeshawahi kufanya makosa huko nyuma. Lakini unapaswa kusonga mbele kulingana na dhamira yako njema, ukiweka tumaini la matokeo yako kwa Mungu. Mtu hapaswi kubeba majukumu haya yote yeye mwenyewe peke yake, lakini kwa tafakari nyingi na maombi ya dhati, [kazi hii] inapaswa kugawanywa kwa usawa kwa wote. {3Tsw 14.1}

Wakati wa mateso ya mume wangu, Bwana aliwajaribu na kuwathibitisha watu Wake kufunua yaliyokuwemo mioyoni mwao; na kwa kufanya hivyo aliwaonesha kile ambacho kilikuwa hakijagunduliwa ndani yao ambacho hakikuwa kulingana na Roho wa Mungu. Hali za kujaribu ambazo tuliwekwa chini yetu ziliitwa kutoka kwa ndugu yetu ambazo ambazo vinginevyo hazingefunuliwa. Bwana aliwathibitishia watu Wake kwamba hekima ya mwanadamu ni upumbavu, na kwamba isipokuwa wanamiliki uaminifu thabiti na kumtegemea Mungu, mipango yao na mahesabu yatathibitisha kutofaulu. Tunapaswa kujifunza kutoka kwa mambo haya yote. Ikiwa makosa yamefanywa, wao inapaswa kufundisha na kuongoza, lakini siyo kusababisha kuachana na mizigo na majukumu. Hawawezi kuweka kando mzigo na bado wawe wamefanya mapenzi ya Mungu. Baadhi ya wachungaji wana upungufu katika sifa zilizo za lazima kuyajenga makanisa, na hawapo tayari kuchangia kwa kusudi la Mungu. Hawana tabia ya kujitoa wenyewe kikamilifu kwa kazi, wakiwa na vipaumbele visivyogawanyika, ari isiyopungua, ustahimilivu na uvumilivu visivyochoka. Yakiwa na sifa hizi zilizo hai, makanisa yatakuwa katika viwango bora, na kazi ya mume wangu haiwezi kuwa nzito kiasi hicho. Wachungaji wote hawaweki akilini mwao wakati wote kwamba kazi za wote ni lazima zikaguliwe hukumuni, na kila mmoja kulipwa sawasawa na kazi yake ilivyo. {3Tsw 14.2}

Ndugu A, unalo jukumu la kubeba juu ya Taasisi ya Afya. [BAADAYE ILIJULIKANA KAMA BATTLE CREEK SANITARIUM]. Unapaswa kutafakari, unapaswa kuakisi. Mara kwa mara wakati unaoutumia kusoma ni wakati mzuri sana kwako kutafakari na kuchambua ni kipi kifanyike kuweka vitu kwenye mpangilio kwenye Taasisi na

ofisini. Mume wangu huichukua mizigo hii kwa sababu anaona kuwa kazi kwa taasisi hizi ni lazima zifanywe na mtu fulani. Kama wengine hawatimizi wajibu wao, yeye huingilia kati na kuziba mwanya uliopo na kuondoa upungufu. {3T 15.1} Mungu amemtahadharisha na kumuonya mume wangu kuhusiana na kuhifadhi nguvu zake. Nilioneshwa kwamba alifufuliwa na Bwana, na kwamba anaishi kama muujiza wa rehema - siyo kwa kusudi tena la kumlundikia juu yake mizigo ambayo hapo awali ilimwanngusha, bali ili watu wa Mungu wapate kufaidika na uzoefu wake katika kuendeleza masilahi ya jumla ya kazi, na kuhusiana na kazi ambayo Bwana amenipa, na mzigo ambao ameniwekea kubeba. {3Tsw 15.2}

Ndugu A, uangalifu mkubwa unatakiwa ufanyike na wewe, hasa hapo Battle Creek. Unapotembelea, mazungumzo yako ni lazima yawe juu ya masomo muhimu zaidi. Kuwa mwangalifu kuweka kielelezo bora. Hii ni hadhi iliyo muhimu sana na utahitaji uitendee kazi. Wakati uko hapa, unapaswa kuchukua muda kutafakari mambo mengi ambayo yanahitaji kufanywa na ambayo yanahitaji tafakari makini, umakini mkubwa, na maombi mengi na yenye bidii na imani. Unapaswa kuhisi kupendezwa sana na vitu vinavyohusiana na kazi katika Taasisi ya Afya na katika ofisi ya uchapishaji, kama vile mume wangu anavyohisi; wewe unapaswa kuhisi kuwa kazi ni yako. Huwezi kufanya kazi ambayo Mungu tayari ameshampa mume wangu aifanye, wala yeye kamwe hawezi kuifanya kazi ambayo Mungu amekupa wewe uifanye. Lakini ninyi wawili kwa pamoja, mkiunganishwa na kazi yenye uwiano, wewe ukiwa ofisini kwako, na mume wangu akiwa ofisini kwake, mnaweza mkafanikisha mengi. {3Tsw 15.3}

Kazi ambayo sisi sote tunapendezwa nayo ni kubwa; na wafanyakazi wenye ufanisi, wenye kuhiyari, na walio tayari kubeba mzigo ni wachache kweli kweli. Mungu atakupa nguvu, ndugu yangu, ikiwa utasonga mbele na kumngojea Yeye. Yeye atampa mume wangu na mimi mwenyewe nguvu katika kazi yetu ya pamoja, ikiwa tutafanya yote kwa utukufu wake, kulingana na uwezo na nguvu zetu alizotupatia. Unapaswa kuegemeza uzito wako wote juu ya Mungu na kumpa fursa ya kukufundisha, kukuongoza, na kukushawishi. Unahisi kupendezwa sana na kazi na kusudi la Mungu, na unapaswa kutafuta kutoka Kwake nuru na mwongozo. Atakupa nuru. Lakini, kama balozi wa Kristo, unatakiwa kuwa mwaminifu, kurekebisha makosa kwa upole na upendo, na juhudi zako hazitakuwa za bure. {3Tsw 16.1}

Kwa kuwa mume wangu amepona udhaifu wake, tumefanya kazi kwa juhudi sana. Hatukuendekeza starehe na raha zetu wenyewe. Tumesafiri na kufanya kazi katika mikutano ya makambi, na kuzichosha sana nguvu zetu, kiasi cha kutuletea udhaifu, kwa kuwa tulikosa muda wa kupumzika. Katika kipindi cha mwaka 1870 tulihudhuria mikutano kumi na mbili ya makambi. Katika idadi ya mikutano hii, mzigo wa kazi ulituelemea karibu sisi sote. Tulisafiri kutoka Minnesota hadi Maine, na hadi Missouri na Kansas. {3Tsw 16.2}

Mume wangu na mimi tuliunganisha juhudi zetu za kuboresha Matengenezo ya Afya [SASA INAITWA AFYA NJEMA/Good Health.] na kulifanya kuwa jarida la kupendeza na lenye faida, ambalo lingetakiwa, siyo tu na watu wetu, bali na watu wa madaraja yote. Huu ulikuwa mchosho mkali juu yake. Pia alifanya maboresho muhimu sana katika majarida ya Review na Instructor. Alifanya kazi ya watu watatu. Na wakati kazi hizi zote zikimuangukia katika tawi la uchapishaji la kazi, idara za fedha katika Taasisi ya Afya na Chama cha Uchapishaji vilihitaji kazi ya watu wawili ili kuwaondolea shida ya kifedha. {3Tsw 16.3

Watu wasio waaminifu ambao walikuwa wameaminiwa kwa kazi ofisini na katika Taasisi, walikuwa kupitia ubinafsi na ukosefu wa uadilifu, wameweka mambo katika hali mbaya zaidi. Kulikuwa biashara ambayo ilikuwa haijapata ufumbuzi ambayo ilitakiwa kushughulikiwa. Mume wangu aliingilia kati na kutumika kwa nguvu zake zote. Alikuwa anajichakaza. Tuliweza kuona kwamba alikuwa katika hatari; lakini hatukuweza kuona jinsi angeweza kuacha, hadi pale kazi hapo ofisini itakapomalizika. Karibu kila siku shida mpya mpya zingeibuka, shida mpya zilizosababishwa na ukosefu wa uaminifu wa watu ambao walikuwa wameisimamia kazi hiyo. Ubongo wake ulikuwa umechoshwa kwa kiwango cha juu. Lakini mashaka hayo mabaya zaidi sasa yamekwisha, na kazi inaendelea kwa mafanikio. {3Tsw 17.1}

Kwenye Konferensi Kuu (General Conference) mume wangu alisihi aachiliwe kutoka kwenye mizigo iliyokuwa juu yake; lakini, bila kuzingatia ombi lake mzigo wa kuhariri majarida ya Review na Reformer ulitwishwa juu yake akitiwa moyo kwamba watakaochukua mizigo na majukumu watatiwa moyo wakae battle Creek. Lakini hata leo bado hakuna msaada uliokuja kuondoa kutoka kwake mizigo ya kazi ya kifedha huko ofisini. {3Tsw 17.2}

Mume wangu anachakaa haraka. Tumehudhuria mikutano minne ya makambi ya Magharibi, na ndugu zetu wanatuhimiza tuhudhurie mikutano ya Mashariki. Lakini hatuthubutu kuchukua mizigo ya ziada juu yetu. Tulipotoka kwenye kazi ya mikutano ya makambi ya Magharibi mnamo Julai, 1871, tulikuta idadi kubwa ya kazi ambayo iliendelea kujilimbikiza wakati mume wangu alipokuwa hayupo. Hatujaona nafasi yoyote ya kupumzika bado. Mume wangu ni lazima afunguliwe kutoka kwenye mizigo iliyo juu yake. Kuna watu wengi wanaotumia ubongo wake kuliko wanavyotumia ubongo wao wenyewe. Kwa mtazamo wa nuru ambayo Mungu alipendezwa kutupatia sisi, tunawasihi ninyi, ndugu zangu, kumwachilia mume wangu. Mimi sipo tayari kudhihirisha matokeo ya yeye kuendelea kufanya kazi kwa namna anayofanya. Amewatumikia kwa uaminifu na bila ubinafsi kwa miaka mingi, na mwishowe akaanguka chini ya shinikizo la mizigo iliyowekwa juu yake. Ndipo na ndugu zake, ambao alikuwa amewaamini, wakamwacha. Wakamwacha

aangukie mikononi mwangu, na wakamtelekeza. Kwa karibu miaka miwili nilikuwa muuguzi wake, mhudumu wake, daktari wake. Sitaki kupita uzoefu huo kwa mara ya pili. Ndugu zangu, je! Mtaondoa mizigo hii kutoka kwetu, na kuturuhusu kuhifadhi nguvu zetu kama Mungu atakavyo, ili kazi iweze kunufaika kwa juhudi tunazoweza kufanya kwa Nguvu zake? Au mtatuacha tudhoofike/tulemae ili tuwe tusio na faida kwa kazi? {3Tsw 17.3}

Sehemu ya utangulizi ya wito huu ilisomwa kwenye mkutano wa makambi ya New Hampshire, Agosti, 1871. Tuliporudi kutoka Kansas mnamo vuli ya 1870, Ndugu B alikuwa nyumbani akiugua homa. Dada Van Horn, wakati huu, alikuwa hayupo ofisini kwa sababu ya homa iliyoletwa kwake na kifo cha ghafla cha mama yake. Ndugu Smith pia alikuwepo akitokea ofisini, huko Rochester, New York, akiendelea kupona homa. Kulikuwa na kazi nyingi ambazo hazikumalizika ofisini, lakini bado ndugu B aliacha majukumu ya wadhifa wake kuanza kujifurahisha kwa anasa zake mwenyewe. Ukweli huu katika uzoefu wake ni mfano wa mtu huyo. Wajibu mtakatifu uliwekwa kidogo sana juu yake. {3Tsw 18.2}

Ulikuwa ukiukwaji mkubwa wa uaminifu uliowekwa ndani yake kufanya hayo aliyoyafanya. Maisha haya yapo kinyume na maisha ya Kristo, aliye kielelezo chetu! Alikuwa ni Mwana wa Yehova, na Mwaanzilishi wa wokovu wetu. Alifanya kazi na kuteseka kwa ajili yetu. Alijikana nafsi Yake, na maisha Yake yote yalikuwa mfuatano wa magumu na ufukara. Kama angechagua kufanya hivyo, angeweza kupitisha siku zake katika ulimwengu wa uumbaji na ubunifu Wake mwenyewe, akiishi maisha rahisi na yenye uwingi wa vitu, akijilundikia raha na starehe zote ambazo ulimwengu ungeweza kumpa. Lakini hakufikiria urahisi wa maisha Yake Mwenyewe. Hakuishi ili kujifurahisha, bali alitenda mema na kutawanya baraka Zake juu ya wengine. {3Tsw 18.3}

Ndugu B alikuwa anaumwa homa. Ugonjwa wake ulikuwa mzito. Ili kuitendea haki kazi ya Mungu, nashawishika kusema ya kwamba ugonjwa wake haukuwa matokeo ya kujitoa bila kuchoka kwa ajili ya maslahi ya ofisi. Uzoefu usio na busara wa safari ya Chicago, kwa kufuata anasa zake mwenyewe, kilikuwa ndicho chanzo cha ugonjwa wake wa muda mrefu, wa kuchosha, na wenye mateso. Mungu hakumvumilia kwa kitendo chake cha kuacha kazi, wakati wengi ambao wangeweza kujaza nafasi muhimu katika ofisi walikuwa hawapo. Wakati ule ule ambao hakutakiwa kujiruhusu hata kwa saa moja, aliacha kazi yake ya uwajibikaji, na Mungu hakumsaidia. {3Tsw 18.4}

Hapakuwa na kipindi cha kupumzika kwetu, hata hivyo tulikihitaji sana. Majarida ya Review na Reformer, na Instructor yalikuwa ni lazima yaharirwe. Barua nyingi zilikuwa zimewekwa kando mpaka hapo tutakaporudi ili kuzikagua. Mambo yalikuwa katika hali ya huzuni pale ofisini. Kila kitu kilihitajika kuwekwa sawa. Mume wangu alianza kazi yake, na nikamsaidia kwa kadri nilivyoweza; lakini huo ulikuwa msaada kidogo tu. Alifanya kazi bila kukoma ili kunyoosha mambo ya kazi

yaliyokuwa yanatatanisha na kuboresha hali ya majarida yetu. Hakuweza kutegemea msaada kutoka kwa yeyote kati ya ndugu wanayehudumu naye. Kichwa, moyo, na mikono yake vilikuwa vimejaa. {3Tsw 19.1}

Hakutiwa moyo na Ndugu A na C, wakati wakijua kuwa alikuwa anasimama peke yake chini ya mizigo huko Battle Creek. hawakuitegemeza mikono yake. Waliandika kwa namna ya kukatisha tamaa juu ya afya zao mbaya, na kudai kwamba wao walikuwa katika hali ya kuchoka sana kiasi kwamba wasingeweza kutegemewa kumalizia kazi yoyote. Mume wangu aliona kuwa hapakuwa na kitu kinachoweza kutarajiwa kwa mwelekeo huo. Licha ya kufanya kazi mara mbili katika kipindi cha majira ya joto, bado hakuweza kupumzika. Na, bila kuangalia udhaifu wake, alijikaza kufanya kazi ambayo wengine walikuwa wameipuuzia. {3Tsw 19.1}

Mwanamatengenezo huyo alikuwa karibu kufa. Ndugu B alikuwa amekazia msimamo mkali wa Daktari Trall. Jambo hili lilimshawishi daktari kulisimamia swala la matengenezo kwa nguvu zaidi ya vile ambavyo angepaswa kufanya, kwa kuacha kutumia maziwa, sukari, na chumvi. Msimamao wa kuacha kutumia vitu hivi kabisa unaweza kuonekana ni sahihi kwa maelezo yake lakini muda ulikuwa haujafika wa kuchukua msimamo huu wa jumla kuhusiana na mambo haya. Na wale wanaochukua msimamo wao, na kutetea hoja ya kutotumia kabisa maziwa, siagi, na sukari, meza zao zingetakiwa ziwe huru na mambo hayo. Ndugu B, hata wakati anachukua msimamo huu na Daktari Trall kuhusiana na athari mbaya za chumvi, maziwa, na sukari, hakuwa anatekeleza mambo hayo aliyokuwa anayafundisha. Juu ya meza yake mwenyewe vitu hivi vilitumika kila siku. {3Tsw 19.2}

Wengi wa watu wetu walikuwa wamepoteza mvuto wa matengenezo, na barua zilikuwa zikipokelewa kila siku zikiwa na ombi hili la kukatisha tamaa: “Tafadhali niondoeni kwenye mpango wangu wa matengenezo.” Barua zilipokelewa kutoka Magharibi, ambako nchi ni mpya na matunda ni machache, ikiuliza: "Je! marafiki wa matengenezo ya afya wanaishije hapo Battle Creek? Je! Wanaacha kutumia chumvi kabisa? Kama ni hivyo, basi hatuwezi kuingia kwenye matengenezo ya afya kwa sasa. Tunachoweza kupata [hapa] ni matunda kidogo, wakati ambapo tumeacha matumizi ya nyama, chai, kahawa, na tumbaku; lakini lazima tuwe na kitu cha kudumisha uhai.” {3Tsw 20.1}

Tulikuwa tumetumia muda huko Magharibi, na tulikandua uhaba wa matunda, na tukawahurumia ndugu ambao walikuwa wakitafuta kwa dhamiri njema kulingana na kundi la Waadventista watunzao Sabato. Walikuwa wakikata tamaa, na wengine walikuwa wakirudi nyuma juu ya matengenezo ya kiafya, wakihofia kuwa watu wa huko Battle Creek walikuwa washika dini wenye misimamo mikali. Hatukupandisha kiwango cha kuvutia watu mahali popote huko Magharibi na hivyo kutopata wanaojisajili kwenye Matengenezo ya Afya. Tuligundua kuwa waandishi katika

jarida la Matengenezo walikuwa wakienda mbali na watu na kuwaacha nyuma. Kama tukichukua misimamo ambayo Wakristo waangalifu, na wana Matengenezo wa kweli, hawawezi kuipokea, tunawezaje kutarajia kunufaika na watu wa daraja hilo ambalo tunaweza kulifikia tu kwa njia ya Matengenezo ya Afya? {3Tsw 20.2}

Hatupaswi kwenda haraka zaidi kuliko tunavyoweza kuchukuliana na wale ambao dhamiri na akili zao vimeshawishika na ukweli tunaoutetea. Ni lazima tukutane na watu mahali walipo. Baadhi yetu tumechukuwa miaka mingi kufika katika nafasi yetu ya sasa katika matengenezo ya kiafya. Ni kazi ya polepole ili kupata mageuzi/matengenezo katika lishe. Tuna uchu wenye nguvu tunaopaswa kukabiliana nao; kwa kuwa ulimwengu umeenda kwenye ulafi. Kama tungeliwaruhusu watu muda wa kutosha kama tuliouhitaji kufikia hali yetu ya sasa ya maendeleo ya matengenezo, tungewavumilia, na kuwaruhusu kusonga mbele hatua kwa hatua, kama tulivyofanya, hadi miguu yao imeimarishwa juu ya jukwaa la matengenezo ya afya. Lakini tunapaswa kuwa waangalifu sana ili tusiendelee haraka sana, tusije tukalazimika kurudisha hatua zetu. Katika matengenezo ingekuwa bora tukapungukiwa alama moja kuliko kwenda mbele hatua moja zaidi. Na ikiwa kuna kosa hata kidogo, basi liwe katika jitihada za kuwakaribia zaidi watu. {3Tsw 20.3}

Zaidi ya yote, tusitetee misimamo kwa kalamu zetu ambayo hatuiweki katika vitendo huko kwenye familia yetu, na juu ya meza zetu. Huu ni udanganyifu, wenye aina ya unafiki. Huko Michigan twaweza kuishi vizuri zaidi bila chumvi, sukari, na maziwa kuliko watu wengi ambao wako katika Magharibi ya Mbali au Mashariki ya mbali, ambapo kuna uhaba wa matunda. Lakini kuna familia chache sana huko Battle Creek wasiotumia bidhaa hizi mezani mwao. Tunajua kwamba matumizi huru ya vitu hivi husababisha maumivu hivyo wasitumie nakala hizi kwenye meza zao. Tunajua kuwa matumizi huru ya vitu hivi hudhuru afya, na, mara nyingi, tunafikiria kwamba ikiwa hazitatumiwa kabisa, hali bora zaidi ya afya ingefurahia. Lakini kwa sasa mzigo wetu hauko juu ya vitu hivi. Watu wako nyuma sana kwa hilo tunaona ni kila kitu wanachoweza kuvumilia kutufanya tuweke mstari juu ya mapendezi yao mabaya na ya kuchochea mihadarati. Tunatoa ushuhuda chanya dhidi ya tumbaku, vileo vya pombe, ugoro, chai, kahawa, nyama za nyama, siagi, viungo (pilipili kali, siki na viungo visivyo vyema kwa mwili), keki tajiri kwa lishe (bidhaa za kusindikwa au kukobolewa kama mafuta, unga mweupe na sukari), mikate ya katakata (minced pies zilizokuwa zimeokwa na vitu vingine visivyo na afya), chumvi nyingi, na vitu vyote vya kusisimua vinavyotumiwa kama nakala ya chakula. {3Tsw 21.1}

Ikiwa tutafika kwa watu ambao hawajaangaziwa kuhusu matengenez ya kafya, na kuwasilisha yetu nafasi zenye nguvu mwanzoni, kuna hatari ya kuvunjika moyo wanapoona ni kiasi gani lazima watoe, ili wasifanye juhudi yoyote ya kufanya

mageuzi. Lazima tuongoze watu pamoja kwa uvumilivu na pole pole, tukikumbuka shimo refu ambalo sisi tulichimbwa ili kutoleewa humo. {3Tsw 21.2}

SURA YA 2

UWEZO USIOTAKASWA

Nimeoneshwa kuwa Ndugu B. anayo mapungufu makubwa katika tabia yake, ambayo yanamuondolea sifa ya kuwa mtu aliyeunganishwa kwa karibu na kazi ya Mungu pale ambapo majukumu muhimu yanatakiwa kubebwa. Anao uwezo wa kutosha wa akili, lakini moyo, na hisia, havijatakaswa kwa Mungu; kwa hiyo yeye hawezi kutegemewa kama mtu mwenye sifa kwa ajili ya kazi muhimu kama hiyo ya kuchapisha Ukweli katika ofisi ya Batlle Creek. Kosa au kupuuzia jukumu katika ofisi hii huwa vinaathiri kazi ya Mungu kwa ujumla. Ndugu B hajaona kushindwa kwake, kwa hivyo hawezi kubadilika. {3Tsw 22.1}

Ni kupitia kwa vitu vidogo vidogo ambapo tabia zetu zinaundwa na kuwa mazoea yenye uthabiti/uadilifu. Wewe ndugu yangu, umekuwa ukijipeleka katika kutothamini umuhimu wa matukio madogo madogo ya maisha ya kila siku. Hili ni kosa kubwa. Hakika, hakuna tukifanyacho kilicho kidogo. Kila tendo lina hesabu yake ya aina fulani, iwe katika upande wa wema/uzuri au katika upande wa ubaya. Ni kwa njia tu ya kuziishi kanuni katika mambo madogo madogo ya kawaida katika maisha tunapopimwa na tabia zetu zinapoundwa. Katika mazingira tofauti tofauti ya maisha tunapimwa na kudhibitishwa, na hivyo kupokea nguvu ya kusimama katika majaribu makubwa na yaliyo muhimu zaidi tunayoitwa kuyapitia na tunapata stahiki kujaza nafasi zilizo na umuhimu mkubwa zaidi. Akili ni lazima ifundishwe kwa njia ya mitihani ya kila siku ili kuunda tabia zenye uadilifu, na kuwa na hisia za madai ya haki na majukumu yaliyo juu ya mambo ya mielekeo, anasa na ya kujifurahisha. Akili iliyofundishwa hivyo huwa haiyumbi kati ya mema na mabaya, kama matete yanavyotetemeka na kuyumba wakati wa upepo; lakini mara tu jambo linapotokea mbele yao, hutambua mara moja kwamba kuna kanuni inayohusika, na mara moja huchagua jema bila kuchukua muda mrefu wa kujadiliana kuhusiana na hilo jambo. Watu wa namna hiyo ni watu waungwana/waadilifu kwa sababu wamejifunza wao wenyewe katika tabia za uaminifu na Ukweli. Kwa kuwa kwao waaminifu katika lile lililo dogo wanapata nguvu na huwa ni rahisi kwao kuwa waaminifu ao ni waaminifu kwa sababu wamejizoeza tabia za uaminifu na Ukweli. Kwa kuwa waaminifu katika lile lililo dogo, wanapata nguvu, na huwa ni rahisi kwao kuwa waaminifu katika mambo makubwa zaidi. {3T 22.2}

Elimu ya Ndugu B siyo ile ambayo inaweza kuimarisha zile sifa za juu za maadili ambazo zingemwezesha kusimama peke yake katika nguvu ya Mungu akiulinda Ukweli, katikati ya upinzani mkali, akiwa imara kama mwamba kwa kanuni, mkweli kwa tabia ya maadili, asiyeyumbishwa na sifa za mwanadamu, au lawama na tuzo, akiona ni bora kufa kuliko kuwa na dhamira iliyokiukwa. Uadilifu wa namna hiyo unahitajika katika ofisi za uchapaji, pale ambapo unyeti na Ukweli mtakatifu unapelekwa kwa watu, Ukweli ambao juu yake dunia itapimwa. {3T 22.3}

Kazi ya Mungu inawahitaji watu wenye nguvu za hali ya juu katika uadilifu ili kushiriki katika kazi ya kupeleka injili. Wanahitajiwa watu ambao mioyo yao ina mguso wa utakatifu. Watu wenye makusudi imara ambao hawayumbishwi kirahisi, ambao wanaweza kuweka kando mambo yao ya ubinafsi wanayoyapendelea na kutoa yote kwa ajili ya msalaba na taji. Kazi ya Ukweli wa leo inaumia kutokana na kukosekana kwa watu walio waaminifu kwa mambo ya haki na majukumu, ambao uadilifu wao ni imara, na ambao nguvu yao inafanana na mafunuo ya hekima ya Mungu. Sifa za namna hii zina thamani kubwa zaidi kuliko utajiri ambao hauelezeki ambao Mungu amewekeza katika kazi na katika kusudi Lake Mungu. Nguvu, uadilifu wa kiroho, na makusudi imara kwa ajili ya haki ni sifa ambazo haziwezi kupatikana kwa kiwango chochote kile cha dhahabu. Watu wenye sifa hizi watakuwa na ushawishi kila mahali. Maisha yao yatakuwa na nguvu zaidi kuliko ya yule mtu mwenye uwezo wa kuongea kwa ufasaha wa hali ya juu. Mungu anawaita watu wenye moyo, watu wenye akili mahiri, watu wenye uadilifu wa kiroho, ambao Yeye anaweza kuwafanya kuwa hazina ya Ukweli wake, watakaowakilisha kwa usahihi zaidi kanuni Zake takatifu katika maisha yao ya kila siku. {3T 23.1}

Kwa namna nyingine Ndugu B ana uwezo ambao wachache wanao. Kama moyo wake ungalitakaswa kwa kazi, angeijaza nafasi ya muhimu katika ofisi akiwa na ukubali wa Mungu. Anahitaji kuongolewa na kujinyenyekeza mwenyewe kama mtoto mchanga, na kutafuta usafi wa moyo, dini ya moyoni, ili kusudi mvuto wake ofisini, au kwa kazi ya Mungu mahali popote, uwe vile inavyopaswa kuwa. Kama ushawishi wake ulivyokuwa, umewajeruhi wote waliofungamanishwa na ofisi, na hasa vijana. Nafasi yake kama msimamizi ilimpa ushawishi. Hakuifanya kazi hiyo kwa hofu ya Mungu. Aliwapendelea baadhi ya watu kuliko wengine. Aliwapuuza wale ambao, kwa ajili ya uaminifu wao na uwezo wao, walistahili kutiwa moyo kwa namna maalum, na alileta hali ya kuvunjika moyo na mkanganyiko kwa wale ambao alipaswa kuwafanyia upendeleo maalum au kuguswa moyo juu yao. Wale wanaounganisha mapenzi yao na kuvutiwa na mtu mmoja au wawili, na kuchagua kupendelea wengine, wasibakie na nafasi zao kwenye ofisi hata kwa siku moja. Upendeleo huu kwa wale maalum watakaomridhisha msimamizi katika mawazo yake ya kufikirika (fanciful), kwa kuwapuuza wale wanaomcha Mungu, ambao

machoni pake ni wa thamani zaidi, siyo mtakatifu na ni kosa kwa Mungu. Kile ambacho Mungu anakithamini tunapaswa kukithamini. Mapambo ya mtu mnyenyekevu na Roho ya upole iliyotulia, Mungu huchukulia katika uthamani wa juu kuliko uzuri wa nje au mapambo ya nje, utajiri, au heshima ya ulimwengu. {3T 23.2}

Wafuasi wa Kweli wa Kristo hawatachagua urafiki wa karibu na wale ambao tabia zao zina mapungufu makubwa, na ambao mifano yao kwa ujumla haitakuwa salama kuifuata, wakati walikuwa na upendeleo wa kujifungamanisha na watu wanaotunza na wanaothamini majukumu katika kazi, biashara na katika dini katika dhamiri zao. Wale wanaopungukiwa na kanuni na mazoea ya ibada kwa ujumla, wanafanya ushawishi wenye mafanikio zaidi wa kufinyanga akili za rafiki zao wa karibu kuliko inavyofanywa na wale wanaoonekana kuwa na maisha yenye uwiano na wanaoweza kutawala na kushawishi wenye mapungufu katika tabia, yaani wale wanaopungukiwa hali ya kiroho na mazoea ya ibada. {3T 24.1}

Mvuto wa Ndugu B, ikiwa hautatakaswa, unahatarisha roho za wale wafuatao mfano wake. Mbinu zake za utayari wakati wote na ubunifu wake vinapendwa na kuthaminiwa sana, na huwaongoza wale walioungwa naye kumpa pongezi kwa sifa asizo kuwa nazo. Akiwa ofisini alikuwa mzembe wa muda. Ingekuwa hili limemuathiri yeye peke yake, basi lingekuwa jambo dogo tu; lakini hadhi yake kama msimamizi wa kazi ilimpa ushawishi. Kielelezo chake mbele ya wale wa ofisini hasa wale waliokuwa wanajifunza kazi haikuwa yenye busara na yenye uangalifu. Ukizingatia kipawa chake kikubwa cha akili, kama ndugu B angekuwa na hali ya juu sana ya kiroho na uadilifu, huduma yake ingekuwa yenye thamani pale ofisini. Kama kanuni zake zingekuwa ni zile ambazo hakuna lolote lingeweza kuziondoa kwenye jukumu lake la moja kwa moja, kwamba hakuna vivutio/ubembelezi ambao ungetolewa hata kuweza kuununua msimamo wake hadi kufanya tendo baya, mvuto wake ungesaidia kuunda tabia za wengine; lakini kupenda kwake starehe kumempumbaza hata kusahau jukumu lake. Kama angesimama katika nguvu za Mungu, bila kuyumbishwa na udanganyifu na lawama, akisimamia kanuni, mwaminifu kwa dhamira yake ya Ukweli na haki, angekuwa mtu mkubwa ambaye angejipatia mvuto kila mahali. Ndugu B hana hekima kuhusiana na uchumi. Anakosa hekima na uangalifu katika matumizi ya chakula, na katika kubana matumizi kwenye nyanja zote za maisha. Anapungukiwa na ujuzi ambao ungemwezesha kuchukuliana na fursa zilizofunguliwa na Mungu na kumfanya mtu aliye na utayari na wepesi kushugulikia mambo. Jambo ambalo lingemwezesha kujibadilisha na mwongozo wa ufunguzi wa Mungu na kumfanya mwepesi kushugulikia mambo. Anapenda sifa za wanadamu. Anayumbishwa na mazingira, na ni mwepesi wa kuingia majaribuni, na uadilifu wake siyo wa kutumainiwa. {3T 24.2}

Uzoefu wa kidini wa Ndugu B haukuwa mzuri au wa busara. Alikuwa akisukumwa na hisia na siyo kanuni. Moyo wake haukuwa unapatana na Mungu, na hakuweka mbele hofu ya Mungu na utukufu Wake. Mara nyingi alitenda kama mtu anayefanya biashara ya kawaida; na aliweka hisia kidogo sana juu ya utakatifu wa kazi ambayo anaifanya. Hakujizoeza kujikana nafsi na kujali uchumi au kubana matumizi, na kwa hiyo hana uzoefu katika mambo haya. Nyakati fulani alifanya kazi kwa bidii na kuonesha kupendezwa sana na kazi. Lakini mara akakosa umakini wa muda wake na kutumia wakati wa thamani katika mazungumzo yasiyo muhimu, akiwazuia wengine kutimiza majukumu yao na kuwaachia kielelezo cha uzembe na kukosa uaminifu. Kazi ya Mungu ni takatifu na inahitaji watu wenye uadilifu wa kiwango cha juu. Wanahitajika watu ambao akili zao za maamuzi na haki ni bora, hata katika mambo yaliyo madogo sana wanatafutwa ambao hisia zao za haki, hata katika mambo madogo kabisa, hayatawaruhusu kuingia wakati wao ambao siyo wa dakika na sahihi – wanaume ni nani atakayegundua kuwa wanashughulikia mali ya Mungu, na ni nani atakayefanya bila haki sahihi senti moja kwa matumizi yao wenyewe; wanaume ambao watakuwa waaminifu na wakamilifu kwa kinagaubaga, makini na wenye bidii, katika kazi yao, bila mwajiri wao kukosekana mbele yake, ikithibitisha kwa uaminifu wao kwamba wao siyo wapendezao tu watu, wahudumu wa macho tu, bali ni waangalifu, waaminifu, watendakazi wa Kweli, wanaotenda haki na kwa usahihi, si kwa sifa za kibinadamu, lakini kwa sababu wanapenda na kuchagua haki kutoka kwa hali ya juu ya wajibu wao kwa Mungu. {3T 25.1}

Wazazi hawajakamilika katika elimu ya watoto wao. Hawaoni umuhimu wa kufinyanga akili zao kwa kuwaadabisha-nidhamu. Wanawapatia elimu ya juu juu na hovyo, wakishughulika zaidi kwa ajili ya mapambo yao kuliko ile elimu halisi ambayo ingeweza kuwakuza na kuelekeza viungo vyao ili vitoe nguvu za roho, na kusababisha nguvu ya akili kupanuka na kuimarika kupitia mazoezi. Vitengo vya akili vinahitaji kukuzwa, ili vitumike kwa utukufu wa Mungu. Uangalifu mkubwa unahitajika utolewe kwa kuzingatia utamaduni wa akili, ili kusudi viungo mbalimbali vya akili vipate nguvu iliyo sawa kwa kuingizwa kwenye mazoezi, kila kimoja katika mahali pake. Ikiwa wazazi watawaruhusu watoto wao kufuata mwelekeo wa akili zao wenyewe na hivyo kuzipindisha kulingana na matamanio yao na starehe zao, na kupuuzia wajibu wao, tabia zao zitaundwa zikilingana na mfano huo na hawatakuwa na uwezo kwa ajili ya kazi yoyote watakayopewa maishani. Tamaa na mwelekeo wa vijana ni lazima zielekezwe, na tabia zao dhaifu ziimarishwe na mielekeo yao isiyo na tija ithibitiwe. {3T 25.2}

Ikiwa kitengo [cha akili] kimoja kinaumizwa hata kutotumika kabisa, au kimeondolewa kwenye njia yake sahihi, kusudi la Mungu halifanyiki. Vitivo vyote vinapaswa kuendelezwa vizuri. Utunzaji unapaswa kutolewa kwa kila kimoja, kwani kila kimoja kinavitegemea vingine, na vyote ni lazima vitumike ili akili iwe na uwiano/balansi. Ikiwa kitengo kimoja au viwili vinakuzwa na kuwekwa katika

matumizi ya kila wakati kwa sababu ni chaguo la watoto wako kuweka nguvu ya akili katika mwelekeo mmoja kwa kupuuza nguvu zingine za kiakili, watafikia utu uzima wakiwa wenye akili zisizo na usawa na tabia zisizo na uwiano. Watakuwa wenye kufaa na wenye nguvu katika mwelekeo mmoja, lakini wenye mapungufu sana katika mwelekeo mwingine ulio wa muhimu tu. Hawatakuwa wanaume na wanawake wenye uwezo. Upungufu wao utaacha alama, na utaharibu tabia yote. {3T 26.1}

Ndugu B amekuza mielekeo isiyoweza kutawalika kwa kupenda kusafiri/kutalii kwaajili ya starehe. Wakati na vyanzo vya mapato hupotea ili kutosheleza hamu yake ya kuvinjari kwaajili ya starehe. Kupenda kwake raha kwa ubinafsi kunapelekea kupuuzia majukumu yake matakatifu. Ndugu B anapenda kuhubiri, lakini hajawahi kuifanya kazi hii akisukumwa na hofu ya laana/ole itakayomwangukia ikiwa hatahubiri injili. Mara nyingi ameiacha kazi ofisini iliyohitaji uangalizi wake kazi hii kuhisi ole juu yake ikiwa hahubiri injili. Mara nyingi ameacha kazi ofisini ili kuitikia miito kutoka kwa baadhi ya ndugu zake wa makanisa mengine. Kama angehisi unyeti/utakatifu/uzito wa kazi ya Mungu kwa wakati huu, na kutoka akimfanya Mungu kuwa tumaini lake, na kujizoeza kujinyima, kujikana nafsi na kuuinua msalaba wa Kristo. Ikiwa angehisi sherehe ya kazi ya Mungu kwa wakati huu, na kwenda mbele kumfanya Mungu kuwa tegemeo lake, akifanya mazoezi ya kujikana, na kuinua msalaba wa Kristo, angekuwa ametimiza mema. Lakini mara nyingi alikuwa na ufahamu mdogo wa utakatifu wa kazi, hivyo alijiboreshea fursa ya kutembelea makanisa mengine ili kutengeneza mandhari ya kujiridhisha nafsi, kwa kifupi, safari ya raha- Pleasure trip -utalii . Ni tofauti gani kati ya mwenendo wake huu na ule ambao ulifuatwa na mitume, ambao walikwenda wakiwa na mzigo wa kazi ya Neno la uzima moyoni, na katika dhihirisho la Roho Mtakatifu walimhubiri Kristo aliyesulubiwa! Walionesha njia ya uzima kupitia kujikana na msalaba. Walikuwa na ushirika na Mwokozi wao katika mateso Yake, na hamu yao kubwa ilikuwa ni kumjua Kristo Yesu, na Yeye alisulubiwa. Hawakuona raha yao wenyewe, wala hawakuyahesabu maisha yao kuwa ya kupendeza kwao wenyewe. Waliishi siyo ili kufurahisha nafsi, bali kutenda mema, na kuokoa roho ambazo Kristo alizifia. {3T 26.2}

Ndugu B anaweza kuwasilisha hoja juu ya hoja za mafundisho ya imani (doctrines), lakini masomo ya vitendo ya utakaso, kujikana mwenyewe, na msalaba, yeye mwenyewe hana uzoefu nayo. Anaweza kusema kwa sikio, lakini hajahisi ushawishi wa utakaso wa Kweli hizi juu ya moyo wake, wala kuzitenda maishani mwake, anashindwa kuhimiza Ukweli moyoni/nyumbani juu ya dhamiri na hisia ya kina ya umuhimu wake na uzito/adhima kwa mtazamo wa hukumu/maamuzi, wakati kila kesi inapaswa kuamuliwa. Ndugu B hajafundisha akili yake, na mwonekano na

tabia yake ya nje ya mkutano havijawahi kuwa mfano mzuri. Mzigo wa kazi hauonekani kuwa juu yake, lakini amekuwa na michezo-michezo na kuwa kama kijana mdogo, na kwa mfano wake ameshusha kiwango cha dini. Vitu au mambo matakatifu na yale ya kawaida yamewekwa katika kiwango kimoja. {3T 26.2}

Ndugu B hajawahi kuvumilia kubeba msalaba kwa hiari yake mwenyewe; hajawahi kuwa tayari kumfuata Kristo kutoka horini hadi ukumbi wa hukumu na Kalvari. Amejiletea mateso mabaya kwa kutafuta starehe zake mwenyewe tu. Bado hajajifunza kwamba nguvu zake mwenyewe ni udhaifu na hekima yake ni upumbavu. Kama angetambua kuwa ameunganishwa kwenye kazi ya Mungu, na kwamba ana deni Kwake Yeye aliyempa muda na karama na ambaye alihitaji kwamba yote haya yaboreshwe kwa utukufu Wake, - kama angekuwa amesimama kwa uaminifu katika kituo chake cha ulinzi, - asingepata ugonjwa huo wa muda mrefu, na wenye kuchosha. Kuvinjari kwake katika hiyo safari kwaajili ya raha zake mwenye kulimsababishia mateso ya miezi na kungemsababishia kifo kama isingekuwa maombi ya bidii, ya imani ya imani yaliyowekwa kwa niaba yake na wale waliohisi kuwa yeye hakuwa tayari kufa. Ikiwa angekufa wakati huo, kesi yake ingekuwa mbaya zaidi kuliko ile ya mwenye dhambi asiye na mwanga. Lakini Mungu kwa rehema alisikia maombi ya watu Wake na akampa mkataba mpya wa maisha, ili apate nafasi ya kutubu kwa uaminifu Wake na kukomboa wakati. Mfano wake ulikuwa umeathiri wengi huko Battle Creek kwa mwelekeo usiofaa. {3T 27.2}

Ndugu B alipona ugonjwa wake, lakini ni vipi yeye au familia yake walihisi kuwa wanyenyekevu chini ya mkono ya Mungu. Kazi ya Roho wa Mungu, na hekima kutoka Kwake, havijadhihirishwa ili tufurahi na kuridhika sisi wenyewe, ili roho zetu zipate kufanywa upya katika maarifa na utakatifu wa Kweli. Ingekuwa bora kiasi gani kwa ndugu huyu ikiwa mateso aushida yake ingechochea kutafuta kwa uaminifu moyo, kugundua kutokamilika kwa tabia yake, ili aziweke mbali, na kwa Unyenyekevu wa roho atoke katika tanuru kama dhahabu iliyosafishwa, ikiakisi sura ya Kristo. {3T 28.1}

Ugonjwa ambao alikuwa amejiletea, kanisa lilimsaidia kuubeba. Watu wa kumwangalia alipewa, na gharama zake kiasi kikubwa zilibebwa na kanisa; lakini bado yeye na familia yake hawakuthamini ukarimu huu na kujali, na upole kwa upande wa kanisa. Walihisi kuwa wanastahili yote waliyotendewa. Ndugu B alipokuja kutoka kwa ugonjwa wake, alihisi vibaya kwa mume wangu kwa sababu hakukubaliana na mwenendo wake, ambao ulikuwa wa kushutumiwa sana. Aliungana na wengine kuumiza ushawishi wa mume wangu, na toka ameondoka ofisini hajajisikia sawa. Angeweza kusimama vibaya kwenye mtihani wa kuthibitishwa na Mungu. {3T 28.2}

Ndugu B bado hajajifunza somo ambalo atalazimika kujifunza ikiwa ataokoka mwishowe - kujikana mwenyewe, na kupinga tamaa zake kwa anasa. Atalazimika kuletwa juu ya ardhi hii tena na tena ili kujaribiwa kwa karibu zaidi, kwa sababu yeye alishindwa kuvumilia majaribu ya zamani. Amemchukiza Mungu kwa kujihesabia haki. Ana uzoefu kidogo tu katika ushirika wa mateso ya Kristo. Anapenda maonyesho na hana utashi unaohusu uchumi katika kutumia mali zake. Bwana anajua. Yeye Anapima hisia za ndani na nia ya moyo. Yeye Anaelewa wanadamu. Anajaribu uaminifu wetu. Anahitaji kwamba tumtumikie kwa kumpenda kwa akili yote, na moyo, na nguvu. Wapenda raha wanaweza kujivika mfano wa utauwa ambao unajumuisha kujinyima kwa aina fulani, na kujikana nafsi, na wanaweza kutoa dhabihu wakati na pesa, na bado ubinafsi usiwekwe chini, na bado wasiwe wameyatiisha mapenzi yao kwa mapenzi ya Mungu. {3T 28.3}

Ushawishi wa mabinti wa D ulikuwa mbaya sana huko Battle Creek. Hawakuwa wamefundishwa/kulelewa vyema. Mama yao alikuwa amepuuzia jukumu lake takatifu na hakuwazuia/hakuwadhibiti watoto wake. Hakuwalea katika hofu na maonyo ya Bwana. Walikuwa wameendekezwa na kulindwa kutoka kwa kubeba majukumu hadi hawakuwa na ladha na furaha kwa kazi wazi na rahisi za nyumbani. Mama alikuwa amewafundisha mabinti kufikiria kuhusu mavazi zaidi, lakini mapambo ya ndani hayakuinuliwa mbele yao. Wasichana hawa wadogo walikuwa na upuuzi/ubatili na kiburi. Akili zao zilikuwa najisi; mazungumzo yao yalikuwa ya kupotosha; na bado kulikuwa na kundi katika Battle Creek ambalo angeshirikiana na muhuri huu wa akili, na hawangeweza kushirikiana nao bila kuja chini kwenye kiwango chao. Wasichana hawa hawakushughulikiwa vikali kama vile kesi zao zilidai. Walipenda jamii ya vijana, na vijana wa kiume ndiyo imekuwa mandhari ya tafakari yao na mazungumzo yao. Wameharibu tabia, na wana ukaidi mwingi vichwani, kisha wanajiamini. {3T 29.1}

Familia nzima inapenda maonyesho. Mama si mwanamke mwenye busara, mwenye hadhi. Yeye hana sifa ya kulea watoto. Kuwavalisha watoto wake kufanya onesho ni jambo kubwa kwake kuliko mapambo ya ndani. Hajajitia nidhamu. Mapenzi yake hayajaletwa kulingana na mapenzi ya Mungu. Moyo wake hauko sawa na Mungu. Yeye ni mgeni kwa utendaji wa Roho Wake juu ya moyo, akileta tamaa na mapenzi ndani kulingana na utii wa Kristo. Yeye hana sifa za kuvutia za akili mahiri na hana utambuzi wa mambo matakatifu. Amewaruhusu watoto wake wafanye kama watakavyo. Uzoefu wa kutisha ambao amekuwa nao pamoja na watoto wake wawili wakubwa hayajagusa moyo kama hali ilivyodai. Amewazoeza watoto wake kupenda mavazi, ubatili, na upumbavu. Hajawanidhamisha wasichana wake wawili wadogo. AD, chini ya ushawishi mzuri, atakuwa kijana anayestahili; lakini ana mengi ya kujifunza. Anafuata mwelekeo badala ya wajibu. Anapenda kufuata mapenzi yake mwenyewe na anasa, na hana ujuzi sahihi wa majukumu

yanayomzunguka Mkristo. Hajaishinda tabia ya kuendekeza tamaa zake mwenyewe, na mwelekeo, wake mwenyewe, angetafsiri kwa furaha kuwa hiyo ndiyo wajibu. Haishinda tabia ya kujipendeza mwenyewe. Ana kazi kufanya kusafisha maono yake ya kiroho, ili apate kuelewa ni nini maana ya kutakaswa kwa Mungu, na kujifunza madai makuu ya Mungu juu yake. Kasoro kubwa katika elimu yake zimeathiri maisha yake. {3T 29.2}

Ikiwa, kwa sifa zake nzuri, Ndugu B angekuwa mwenye kiasi na msimamizi mwaminifu wa ofisi, kazi yake ingekuwa ya thamani kubwa ofisini, na angeweza kupata mshahara maradufu. Lakini kwa miaka iliyopita, kwa kuzingatia upungufu wake, na ushawishi usiowekwa wakfu, ofisi ingeweza kumudu kufanya bila yeye, hata kama huduma zake zingekuwa za bure. Ndugu na Dada B hawajajifunza somo la uchumi. Kujiridhisha kwao binafsi pamoja na tamaa ya anasa na kujionesha, vimekuwa na ushawishi wenye nguvu juu yao. Mshahara mdogo ungekuwa wa faida zaidi kwao kuliko mkubwa, kwani wangetumia yote kadri wapendavyo katika anasa mbalimbali. Wangefurahi kadri wanavyokwenda, na kisha dhiki inapowajia, wangekuwa hawajajiandaa kabisa. Dola ishirini kwa wiki zingetumiwa sawa na dola kumi na mbili. Laiti Ndugu na Dada B wangekuwa wasimamizi wazuri kiuchumi, wakijinyima wenyewe, wangeweza kuwa na nyumba yao wenyewe, na zaidi ya hayo wangekuwa na mali ya kutatua shida zao wenyewe wakati wa dhiki. Lakini hawajinyimi na kujibana kama wengine wanavyofanya, hadi kupelekea wakati mwingine kuwa tegemezi kwa wenzao. Ikiwa watapuuza kujifunza masomo haya, basi tabia zao zitaonekana kupungua katika siku ya Bwana. {3T 30.1}

Ndugu B amekuwa mtu anayependa sana somo la kujishusha kwa Kristo kutoka mbinguni na kuja duniani, na bado hajawahi kuhisi kwamba angeweza kuiga Mfano Mkuu. Katika maisha yake yote amedai kutafuta, fungu bora kuliko lile alilopewa Bwana wetu. Hajawahi kuhisi kina cha ujinga na dhambi ambacho Kristo ametaka kumwinua atoke humo na kumunganisha na asili Yake ya Uungu. {3T 31.1}

Ni jambo la kuogopesha kuhudumu katika mambo matakatifu wakati moyo na mikono si mitakatifu. Kuwa mtendakazi pamoja na Kristo kunahusisha majukumu mazito; kusimama kama mwakilishi wake si jambo dogo. Uhalisia wa kutisha wa hukumu utajaribu kazi ya kila mtu. Mtume alisema, "Hatujihubiri sisi wenyewe, bali Kristo Yesu Bwana; "Kwa maana Mungu, aliyeamuru nuru iangaze kutoka gizani, ameangaza ndani ya mioyo yetu, kutoa nuru ya ujuzi wa utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo." Utoshelevu wa mtume haukuwa ndani yake mwenyewe, bali katika neema ya Roho wa Kristo, aliyeijaza nafsi Yake na akaleta kila wazo chini ya utii kwa Kristo. Nguvu ya Ukweli iliyo ndani ya Neno linalohubiriwa itakuwa harufu ya uzima iletayo uzima au ya mauti iletayo mauti. Watendakazi wanapaswa kuwa mifano hai yenye Roho wa Kristo, barua zilizo hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Ninahuzunika na kutetemeka

ninapofikiria kuwa kuna wachungaji/wahudumu wengine, hata miongoni mwa Waadventista es Dabato, ambao hawajatakaswa na zile Kweli wanazozihubiri. Hakuna kitu chenye nguvu na kinachofanya kazi kwa haraka kama Roho wa Mungu aliye na kasi na Mwenye nguvu kufanya kazi ndani ya mioyo ya wajumbe Wake kutoa maarifa ya utukufu wa Mungu, ili kuwezesha kupata kwao ushindi. {3T 31.2}

Mahubiri ya Ndugu B hayajatiwa alama na kuidhinishwa na kushuka kwa Roho wa Mungu. Anaweza kuzungumza kwa ufasaha na kuweka hoja wazi, lakini mahubiri yake yamekosa mionjo ya kiroho. Miito yake anapotoa wito kwa watu, haijagusa mioyo ya watu kwa kujali na huruma nyororo ndani yake. Kumekuwa na safu ya maneno, lakini mioyo ya wasikilizaji wake haijawahi kuhuishwa na kuyeyushwa kwa hisia ya upendo wa Mwokozi. Wenye dhambi hawajasadikishwa na kuvutwa kwa Kristo kwa hisia kwamba "Yesu wa Nazareti anapita." Wenye dhambi wanapaswa kuwa na hisia wazi waliyopewa ya ukaribu na nia ya Kristo kuwapa wokovu wa sasa. Mwokozi anapaswa kuwasilishwa mbele ya watu, wakati moyo wa mzungumzaji unapaswa kutiishwa na kujazwa na Roho Wake. Toni za sauti, muonekano, maneno, inapaswa kuwa na nguvu isiyoweza kuzuilika ya kuihuisha mioyo na kudhibiti akili. Yesu anapaswa kupatikana katika moyo wa mtendakazi. Ikiwa Yesu Yuko katika maneno na sauti, ikiwa sauti inalainishwa na zabuni Yake ya upendo, itathibitisha baraka ya thamani zaidi kuliko utajiri wote, raha, na utukufu wa dunia; kwani baraka kama hizo hazitakuja na kupita bila kumaliza kazi. Usadikisho utakuwa wa kina, maoni yatatolewa, na swali litakuja kwa watu: "Je, nifanye nini ili niokolewe?" {3T 31.3}

SURA YA 3

AKILI ZISIZO NA USAWA/Balansi

Mungu amemkabidhi kila mmoja wetu amana takatifu, ambayo kutokana nayo atatuwajibisha. Kusudi Lake ni kwamba tuelimishe na kutumikisha akili zetu ili tuweze kutumia talanta alizotupatia katika namna ambayo itatimiza mema mengi zaidi na kuakisi utukufu wa Mpaji. Tuna deni kwa Mungu kwa sababu ya sifa zote za akili. Nguvu hizi zinaweza kukuzwa, na kwa busara kuelekezwa na kudhibitiwa ili kukamilisha kusudi ambalo kwalo zilitolewa. Ni wajibu kuelimisha akili ili kuleta nguvu za roho na kukuza kila kitivo. Wakati uwezo wote unapokuwa kwenye kuzoezwa, akili itakuwa ikiimarishwa, na kusudi ambalo kwalo vilitolewa litakuwa linakamilishwa. {3T 32.1}

Wengi hawafanyi kiwango kikubwa cha mema kwa sababu hutumia akili katika mwelekeo mmoja na kupuuza kutilia maanani uangalifu wa mambo yale ambayo wanadhani hawajaratibiwa kufanya. Baadhi ya vitivo vya akili ambavyo ni dhaifu vimeruhusiwa kukaa bila kutumika kwa kuwa kazi ile ambayo ingepaswa kuvitia katika utendaji, na hivyo kuvipatia nguvu, haifurahishi au ni ngumu. Nguvu zote za akili zinapaswa kuwa katika utekelezaji, na vitengo vyote kukuzwa. Utambuzi, uwezo wa kufanya maamuzi, kumbukumbu, na uwezo wote wa kufikiri wapaswa kuwa na nguvu sawa ili akili iweze kuwa msawaziko mzuri-balansi. {3T 32.2}

Ikiwa uwezo fulani wa vitivo unatumiwa kwa kupuuza vingine, mpango wa Mungu hautekelezwi kikamilifu ndani yetu; kwani vitivo vyote vina sababu ya kuweko au maana na vinategemeana. Mtu hawezi kutumika kwa ufanisi bila utendaji wake wote kutumika, ili usawa uweze kuhifadhiwa kwa uangalifu. Ikiwa umakini wote na nguvu hupewa kitivo kimoja tu, wakati vingine vimelala, maendeleo ya hicho kitivo yanakuwa na nguvu ndani yake kwa namna ya kupitiliza, kwa sababu nguvu zote hazijakuzwa na kupaliliwa. Akili zingine ni mbilikimo na hazina usawa. Akili

zote hazijaundwa sawa kwa asilia. Tuna akili tofauti; baadhi zina nguvu juu ya vipengele fulani na dhaifu sana kwa vingine. Upungufu huu, unaoonekana wazi, hauitajiki na haupaswi kuwepo. Ikiwa wale wanaozimiliki wangeimarisha alama dhaifu katika tabia zao kwa kuziendeleza na kuzifanyia mazoezi, wangekuwa na nguvu. {3T 33.1}

Inakubalika, ingawa siyo yenye manufaa zaidi, kutumia vile vitivo ambavyo kwa asili vina nguvu sana, huku tukivipuuzia vile ambavyo ni dhaifu, lakini ambavyo vinahitaji kuimarishwa. Vile vitivo vilivyo vidhaifu vingeangaliwa kwa umakini, ili kwamba nguvu zote za akili ziweze kuwa na msawaziko na vyote vifanye sehemu zake za kazi kama mashine iliyosimamiwa vizuri. Tunamtegemea Mungu kwa ajili ya kuhifadhi vitivo vyetu vyote. Wakristo wanawajibika Kwake kufundisha akili ili vitivo vyote viweze kuimarishwa na kukuzwa kikamilifu zaidi. Tukipuuza kufanya hivi, vitivo hivyo havitatimiza kusudi la kuundwa kwake. Hatuna haki ya kupuuza hata mojawapo ya nguvu ambazo Mungu ametupa. Tunaona hali ya kupendelea kufanya jambo moja tu huku mengine yakipuuziwa nchini kote (monomaniac). Mara nyingi panakuwepo akili timamu juu ya kila somo isipokuwa katika somo moja. Sababu ya hali hii kuwa hivi ni kwa kuwa kiungo kile kilichotumika kila wakati kimechakaa na kuugua, na vingine vikiachwa bila kutumika. Kiungo kile kinachotumika kila wakati huchakaa na kuwa dhaifu na hatimaye na mtu naye huwa chakavu/ameharibikiwa. Mungu hakutukuzwa kwa kufuata mwenendo huu. Kama angevitumia viungo vyote kwa usawa, vyote vingekuwa na makuzi yenye afya; kazi zote zisingebebeshwa kwa kiungo kimoja, na kwa hiyo hakuna kiungo ambacho kingeumia au kuharibikiwa. {3T 33.2}

Wachungaji wanapaswa kulindwa, ili wasije wakakwamisha kusudi la Mungu kutokana na mipango yao wenyewe. Wapo katika hatari ya kuipunguzia mapana/kasi ya kazi ya Mungu, na kuifungia kazi yao katika maeneo fulani fulani tu, bila kukuza shauku maalum kwa kazi ya Mungu katika idara zake zote mbalimbali. Kuna wale ambao hukaza akili zao juu ya jambo moja huku wakiyaweka kando mambo mengine yenye umuhimu sawa. Ni watu wenye mtazamo wa wazo moja tu. Nguvu zote za maisha yao zimejikita katika jambo ambalo akili inajishughulisha nalo wakati huo. Mambo mengine yote hayapewi umuhimu na hupotea machoni. Mada hii pendwa ndiyo iliyo mzigo wa mawazo yao na ajenda ya mazungumzo yao. Ushahidi wote kuhusiana na mada hiyo unashikiliwa kwa hamu na kuwekwa kwenye matumizi, na hata kuhangaikiwa kwa muda mrefu kiasi ambacho hata akili inachoka kufuatilia. {3T 34.1}

Mara nyingi wakati hupotezwa katika kuelezea mambo ambayo kiuhalisia siyo muhimu, na ambayo yangeweza kuchukuliwa kuwa yasiyohitaji uthibitisho kwa kuwa yako wazi. Lakini uhalisia ni kwamba mambo ya msingi ni lazima, yafanywe kuwa wazi na yatiliwe nguvu kwa kadri lugha na uthibitisho viwezavyo kufanya. Nguvu ya kubaki katika aina moja ya mawazo huku ukiweka kando mawazo mengine, inaweza ikaonekana kuwa ni nzuri lakini utendaji wa namna hiyo ulio

endelevu wa hicho kitengo cha akili huchakaza hivyo viungo ambavyo vilikusudiwa kutumika kwa ajili ya kazi hiyo. Zoezi hilo linavipa viungo hivyo kazi kubwa na matokeo yake ni kushindwa kukamilisha mema makubwa, na uchakavu mkubwa huja kwenye hicho kiungo wakati viungo vingine vinapokuwa vimelala na havitumiki. Kwa njia hiyo akili haiwezi kutumika kiafya na matokeo yake maisha hufupishwa. {3T 34.2}

Vitivo vyote vinapaswa kubeba sehemu ya kazi, vikifanya kazi kwa uwiano na mapatano na kuweka msawaziko unaotakiwa [balansi]. Wale wanaoweka nguvu zote za akili zao katika mada moja wana mapungufu sana kuhusiana na ule upande mwingine, kutokana na ukweli kuwa vitengo vyote vya akili havikuzwi kwa kulingana. Mada iliyo mbele yao inateka mawazo yao, na kuwaongoza mbele na mbele zaidi na kuwapeleka kwenye kina cha chini sana cha hilo jambo kwa kuendelea tena na tena. Wanayaona maarifa na nuru kwa kadri wanavyoendelea kuvutiwa na kuzama ndani zaidi. Lakini kuna akili chache sana zinazoweza kuwafuatilia, isipokuwa zimefikishwa kwenye kina hicho hicho cha uelewa wa somo. Kuna hatari ya watu kama hao kulima, na kupanda mbegu za Ukweli kwenye kina kirefu kiasi lile jani zuri na laini litashindwa kutokezea juu ya uso wa ardhi. {3T 34.3}

Mara nyingi kazi ngumu nyingi zimefanywa, ambazo hazitafurahisha watu kwani hazikupaswa kufanywa maana hazikuwa zinahitajika. Kama wale wenye msisitizo mkubwa watakuza kitengo hiki cha akili wakipuuza vitengo vingine vya akili, hawataweza kuwa na akili yenye uwiano ulio sawa. Watakuwa kama mashine ambayo seti moja tu ya magurudumu ndiyo inayofanya kazi kwa wakati mmoja. Wakati magurudumu mengine yakiota kutu kwa kutotumika, mengine yanachakaa kwa kutumika bila kupumzika. Watu wanaokuza kitivo/kitendo kimoja au viwili, na wakaacha kuvitumia vitengo vyote kwa uwiano ulio sawa, hawawezi kukamilisha hata nusu ya mema ambayo Mungu alikusudia wayatimize hapa ulimwenguni. Ni watu wenye mwelekeo wa upande mmoja; ni watu wa upande mmoja tu, wakitumia nusu ya uwezo ambao Mungu aliwapatia, wakati nusu nyingine ikiota kutu kwa kutotumika. {3T 35.1}

Ikiwa daraja hili maalum la akili lina kazi maalum, inayotaka kufikiri, lisitumie nguvu zake zote kuhusiana na jambo hili moja, huku likiweka kando mambo mengine yote. Wanapolichukua mada hiyo kama shughuli yao kuu, matawi mengine ya kazi ni lazima yawe na muda wa kushughulikiwa. Hili litakuwa bora zaidi kwao na kwa kusudi la kazi kwa ujumla. Tawi moja la kazi halipaswi kupewa umakini mkubwa na kupuuzia matawi mengine. Katika kuandikia watu makala, mengine yatahitaji kulindwa kwa muda wote yasije yakaelezwa kwa upungufu wakati yalikuwa na uwezo wa kuelezwa kwa uwazi zaidi, pale yatakapowasilishwa kwa hoja ambazo hazitakuwa na mvuto kwa msomaji. Ikiwa watakaa kwenye mada moja kwa muda mrefu, wakiitolea ufafanuzi unaoshawishi akili, kazi yao itakuwa karibu imepotea. Shauku ya msomaji haitakuwa ya kutosha kufuatilia mada hadi

mwisho wake. Mambo muhimu zaidi ya Ukweli yanaweza kufanywa kwa kuwekea uzito katika kila kipengele. Eneo kubwa limefunikwa au kushugulikiwa; lakini kazi ambayo juu yake juhudi kubwa inahiyotajika haijadadavuliwa na kushugulikiwa bado, ili kuweza kufanya kiasi kikubwa sana cha wema, kwa kuamsha hamu kwa jumla. {3T 35.2}

Katika enzi hizi, wakati hekaya za kuvutia zinachukua mkondo wake kuvutia akili, Ukweli uliowasilishwa katika mtindo rahisi, ukiungwa mkono na uthibitisho mchache wenye nguvu, ni bora zaidi kuliko kutafuta na kuleta lundo kubwa ya ushahidi; kwa kuwa ile hoja sasa haiwezi kusimama katika akili nyingi kabla ya pingamizi na ushahidi kuletwa mbele yao. Kwa wengine, madai mengi yatakwenda mbali zaidi kuliko mabishano marefu. Wanachukulia mambo mengi kama ya kawaida. Uthibitisho hauwezi kusaidia hoja hiyo akilini mwa watu kama hao. {3T 36.1}

Waadventista Wapinzani

Wapinzani wetu wenye machungu zaidi wanapatikana miongoni mwa Waadventista wa siku ya kwanza. Hawajihusishi na vita kwa uangalifu na kuonyesha heshima katika kazi ya Bwana. Watafuata njia yoyote, hata iwe isiyo na maana wala msimamo, ili kuficha Ukweli na kujaribu kuifanya sheria ya Mungu ionekane kuwa haina nguvu. Wanajidanganya wenyewe kwamba mwisho utahalalisha njia zao. Baadhi ya watu ambao hawakuwa na msimamo juu ya imani yao, wataanza matusi dhidi ya Sabato ya amri ya nne, na watadhihirisha misimamo yao mbele ya hadhira wakitumia maneno yao wenyewe, hata kama siyo ya kweli, au yasiyo ya haki, na hata ya kejeli, kama wanaweza kuwafanya wawe dhidi ya Ukweli wanaouchukia. 3T 36.2

Hatupaswi kuchochewa au kufadhaishwa na vita hivi visivyo vya haki kutoka kwa watu wasio na busara au sababu zenye maana. Wale wanaopokea, na kufurahishwa na, yale ambayo watu hawa wanazungumza na kuandika dhidi ya Ukweli si wale ambao wangesadikishwa na Ukweli au ambao wangeheshimu kazi ya Mungu ikiwa wataikubali. Wakati na nguvu vinaweza kutumika vizuri zaidi kuliko kukaa kwa muda mrefu juu ya ukosoaji na mabishano ya wapinzani wetu wanaoshujighulisha na kashfa pamoja na upotoshaji. Ingawa wakati wenye thamani unatumiwa katika kuwafuata wapotovu na wapinzani wasio waaminifu, watu ambao wako tayari kusadikishwa wanakufa kwa kukosa maarifa. Msururu wa mabishano ya kipumbavu ambayo Shetani mwenyewe ndiye mvumbuzi wake yamejazwa akilini mwa watu, huku watu wakilia kwa ajili ya chakula, kitoweo kulingana na majira yake. 3T 36.3

Wanahitajika wale ambao wamezoeza akili zao kupingana na Ukweli kutengeneza/kubuni mizozo mbalimbali. Na hatuna uwezo wala busara ya kuzichukua hizo ajenda kutoka mikononi mwao, na kuzipitisha kwa maelfu ya watu ambao hawangeweza kuzifikiria kama tusingezitangaza ulimwenguni. Hivi ndivyo

wapinzani wetu wanataka wafanye; wanataka watu wawatambue na tuwachapishie machapisho yao (tuwatangazie ajenda zao au falsafa zao). Hii ni kweli hasa kwa baadhi. Hili ndilo lengo lao kuu katika kuandika uongo wao na kupotosha Ukweli kwa watu wanaoipenda na kuitetea Kweli. Watakufa kwa upesi zaidi endapo watabaki pasipo kutambuliwa, pale watu watakapoyamaza na kuyadharau mafundisho yao ya uongo kimya kimya. Hawataki kuachwa peke yao. Upinzani ni kipengele ambacho wanakipenda. Kama isingekuwa jambo hilo basi watu hawa wangekuwa na ushawishi mdogo. 3T 37.1

Waadventista wa siku ya kwanza wakiwa kama kundi, ndio wagumu zaidi kuwafikia. Kwa ujumla wao huikataa Kweli, kama walivyofanya Wayahudi. Tunapaswa, kadri tuwezavyo, kusonga mbele kana kwamba hakuna watu kama hao miongoni mwetu. Wao hudhihirisha machafuko, na mmomonyoko wa maadili hudhihirika miongoni mwao kwa kiwango cha kutisha. Lingekuwa janga kubwa Zaidi na la kutisha kuwa na idadi kubwa ya watu kuukubali Ukweli. Wangelazimika kujifunza upya kila kitu la sivyo wangeleta na kusababisha matatizo makubwa. Kuna nyakati ambapo uwasilishaji wao mbaya tutalazimika kukabiliana nao. Wakati hali kama hii itakapowasili, itabidi kushugulikiwa mara moja na kwa haraka, ili tuweze kuendelea na kazi yetu. Mpango wa mafundisho ya Kristo unapaswa kuwa wetu. Yeye Alikuwa wazi na sahili/rahisi, akigusa moja kwa moja kwenye mzizi wa jambo, na kuyafikia mawazo na akili zote. 3T 37.2

Si sera njema sana kusema kwa uwazi juu ya kila jambo ambalo lingeweza kuwekwa bayana kwa urahisi, na wakati ambapo hoja chache tu zingeweza kufunika msingi na kutosha kwa madhumuni yote ya vitendo kuwashawishi au kuwanyamazisha wapinzani. Unaweza kuondoa kila wazo lenye kupinga leo na kuwanyamazisha wale wanaopinga ili wasiseme chochote, na bado kesho watapitia tena katika msingi au njia hiyo hiyo. Ndivyo itakavyokuwa, tena na tena, kwa sababu hawaipendi nuru na hawatakuja kwenye nuru, mpaka pale ambapo giza na makosa yao yatakapoondolewa kwao. Ni mpango bora kuweka akiba ya hoja kuliko kumwaga maarifa ya kina juu ya suala ambalo lingechukuliwa kuwa la kawaida bila mabishano ya kazi. Huduma ya Kristo ilidumu miaka mitatu tu, na kazi kubwa ilifanywa katika kipindi hicho kifupi. Katika siku hizi za mwisho kuna kazi kubwa ya kufanywa kwa muda mfupi. Wakati wengi wanajitayarisha kufanya jambo fulani, roho zitaangamia kwa ajili ya nuru na maarifa. 3T 37.3

Iwapo watu wanaojibidisha katika kuwasilisha na kutetea Ukweli wa Biblia, watachukua hatua za kuchunguza na kuonesha upotofu na kuwadhihirisha watu ambao siyo waaminifu ambao wanaigeuza Kweli kuwa uongo, Shetani atawachochea wapinzani wao na kuwawajibisha sana katika kuandika (kujitetea/kulumbana), na huku sehemu zingine za matawi ya kazi zikiachwa kuzorota. 3T 38.1

Inatulazimu sisi kuwa na roho ileile ambayo walikuwa nayo watu waliojibidisha na kujishughulisha katika ujenzi wa kuta za Yerusalemu wakati wa Nehemia. Tunafanya kazi kubwa, hatupaswi kushuka chini kutoka kwenye ukuta (Neh 6:3). Ikiwa Shetani anaona kwamba anaweza kuwafanya watu wa Mungu kujishughulisha tu na kujibu mashambulizi ya wapinzani, na hivyo kunyamazisha sauti zao, na kufanikiwa kuwazuia kufanya kazi muhimu zaidi kwa wakati huu, basi lengo lake litakuwa limetimizwa. 3T 38.2

Historia ya Sabato imewekwa mbali na watu kwa muda mrefu sana. Watu wanahitaji kazi hii ya thamani, hata kama si katika ukamilifu wake wote. Kamwe haitaweza kutayarishwa kwa namna ambayo itaweza kuwanyamazisha kabisa wapinzani wasio na msimamo, ambao wanayumbamba, kwa kutokuwa imara, na wanaopotosha Maandiko kwa ajili ya uharibifu wao wenyewe. Huu ni ulimwengu wenye pilikapilika nyingi. Watu wanaojibidisha na kujishughulisha na mambo ya ulimwengu huu hawana muda wa kutafakari, au hata kusoma Neno la Mungu vya kutosha kuelewa Ukweli wake wote wenye umuhimu katika Maisha yao. Ujengaji wa hoja refu zenye kuchosha katika mabishano utawavuta wachache sana; kwa kuwa wanapaswa wasome na kuelewa Maandiko wangali wanakimbia. Huwezi tena kuondoa mapingamizi yaliyopo kwenye amri ya Sabato kutoka katika akili za Waadventista wa siku ya kwanza kama ilivyokuwa kwa Mwokozi wa ulimwengu, kwa uwezo Wake mkuu na miujiza Yake, alivyoweza kuwashawishi Wayahudi kwamba Yeye Ndiye Masihi, kama walivyokuwa wamepanga kumkana na kumkataa. Kama ilivyokuwa kwa Wayahudi wakaidi, wasioamini, walivyochagua giza badala ya nuru, na hata kama malaika angezungumza nao kutoka kwenye nyua za mbinguni, wangaliweza kusema kuwa ni Shetani. 3T 38.3

Dunia inahitaji utendaji wa kazi sasa. Miito inasikika kutoka kila upande kama kilio cha Wamekedonia: “Njooni huku mtusaidie.” Hoja zilizo wazi, zikisimama kama nguzo zetu za ‘Kilomita’ barabarani ili kutuonyesha safari, zitafanya mengi zaidi katika kuwashawishi watu kwa ujumla, kuliko safu kubwa ya hoja ambazo zinajihusisha na mambo mengi, lakini ambazo hakuna mtu isipokuwa wenye hamu ya kuchunguza Maandiko ndio watakaoziatafutilia. Historia ya Sabato inapaswa kutolewa kwa watu. Ingawa toleo moja linaweza kuwa linasambazwa, na watu wakanufaika nalo, maboresho makubwa zaidi yanaweza kufanywa, hadi kila linalowezekana lifanyike ili kulileta chapisho kwenye ukamilifu. Mafanikio yetu yatakuwa katika kufikia watu wa kawaida. Wale walio na talanta na nafasi wameinuliwa juu ya usahili wa kazi, na wameridhika kiasi kwamba hawahisi haja ya kuufahamu Ukweli. Hapo ndipo walipokuwa Wayahudi, wenye kujihesabia haki, waliojitosheleza. Wao walijiona kuwa wakamilifu na wazima na wala hawana haja ya daktari. 3T 39.1

SURA YA 4

URAFIKI WA KARIBU NA WALIMWENGU

Desemba 10, 1871, nilioneshwa, Ndugu E, kwamba wewe na dada zako mlikuwa katika hali ya hatari sana; na kinachofanya msimamo wako kuwa hatari zaidi ni kwamba hutambui hali yako ya kweli. Nilikuona umefunikwa na giza. Giza hili halijakutanda kwa ghafla. Ulianza kuingia kwenye ukungu wa giza hatua kwa hatua, na karibu bila kuonekana, mpaka giza likawa Kweli kwako, lakini wingu hilo linazidi kuwa nene kila siku. Mara kwa mara niliona mng'ao wa nuru ukilitenganisha giza na wewe; lakini tena lingekufunga upya, kwa uimara na kwa unene zaidi kuliko hapo awali. 3T 39.2

Shule zako za uimbaji zimekuwa daima mtego kwako. Si wewe au dada zako walio na uzoefu wa kina ambao utakuwezesha kuwasiliana na athari unazokutana nazo katika shule zako za uimbaji, bila kuathiriwa. Inahitajika akili zenye nguvu, zenye uamuzi mkuu wa tabia kuliko nyinyi watatu, kuletwa katika jamii mliyomo na kutoathiriwa. Sikiliza Maneno ya Kristo: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kusitirika. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangazia wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Je, kielelezo chako na ushawishi wako umekuwa wa tabia hiyo nzuri ambayo imevutia na kusadikisha wenzako? Nadhani sivyo. Umejeruhiwa. Giza limetanda juu yako na kuhafifisha nuru yako ili isiwake

na mng'ao huo ili kuondoa giza juu ya wengine. Umekuwa ukijitenga zaidi na zaidi kutoka kwa Mungu. 3T 39.3

Wewe, ndugu yangu, una hisia kidogo tu ya kile ambacho umekuwa ukifanya. Umekuwa ukisimama moja kwa moja katikati ya njia ya maendeleo ya dada zako katika maisha ya mbingu. Wao, haswa zaidi F, wamenaswa na ujanja wa kurogwa, wa kishetani wa imani ya mizimu, na ikiwa ataondoa uchafu huu usio mtakatifu wa Shetani, ambao umepotosha hisia zake za mambo ya milele, itamlazimu kufanya juhudi kubwa. Itakuwa ni kuponyoka kwa kuponea chupuchupu- kwa upana wa nywele tu. Umepofushwa, umedanganywa, na umerogwa wewe mwenyewe. Hujioni mwenyewe. Ninyi nyote ni dhaifu sana, mpate kuwa hodari katika ile Kweli ya thamani, iokoayo, kuimarishwa, kusimikwa, na kutunzwa juu ya Mwamba Kristo Yesu. Moyo wangu unahisi jambo hil ikwa undani. Natetemeka kwa ajili yako. Ninaona majaribu kila upande unaokuzunguka, na ninyi ni wenye uwezo mdogo sana kuyapinga. 3T 40.1

Kaka E, nilioneshwa kuwa umepumbazwa na mahaba ya kufikirikia; unadanganywa kuhusu nia yako na makusudio halisi ya moyo wako. Nilikuona wewe katika jamii ya binti wa Kaka G. Binti huyu hajawahi kuukabidhi moyo wake kwa Kristo. Nilioneshwa kuathirika na kuhukumiwa. Lakini mwendo wako haukuwa wa tabia hiyo ili kuongeza usadikisho, au kumpa hisia kwamba kuna umuhimu wa pekee unaohusishwa na mambo haya. Unakiri kushikilia utakatifu wa wokovu wa roho, na Ukweli wa sasa. Msichana huyu haiheshimu Sabato kutokana na kanuni. Anapenda ubatili wa dunia na anafurahia fahari, kiburi cha maisha na maburudisho ya maisha. Lakini umekuwa ukiondoka polepole kutoka kwa Mungu, na kutoka kwenye nuru, hata huoni utengano ambao Ukweli huleta kati ya wale wanaompenda Mungu na wale wanaopenda anasa, kuliko kumpenda Mungu. Niliona kuwa umevutiwa na mahusiano/jamii yake. Mikutano ya kidini/kiroho na majukumu matakatifu yalikuwa ya umuhimu mdogo, wakati uwepo wa mtoto mdogo kama huyu, ambaye hana ujuzi wa Ukweli au wa mambo ya mbinguni, ulikuvutia kama sumaku. Mmepuuza kujikana nafsi na msalaba, ambao umelala chini moja kwa moja katika njia ya kila mfuasi wa Kristo. 3T 40.2

Nilioneshwa kwamba ikiwa ungekuwa unatembea katika nuru ungechukua msimamo wako juu ya uamuzi wa ile Kweli. Mfano wako ungeonesha kwamba ulizingatia Ukweli unaodai kuwa wa umuhimu huo, na kwamba mapenzi na moyo wako ungeweza kwenda tu mahali ambapo sura ya Kristo ilionekana. Kristo sasa anakuambia wewe: Kipi utachagua, Mimi au ulimwengu? Uamuzi wako unapaswa kufanywa hapa. Je, utafuata mwito na maongozi ya moyo usiotakaswa, kugeuka kutoka kwenye kujikana nafsi kwa ajili ya Kristo, na kuuruka msalaba bila kuinua? Au utainua msalaba huo, ingawa ni mzito, na kujidhabihu kwa ajili ya Ukweli? Hebu Mungu akusaidie kuona mahali ulipo, ili uweze kuweka makadirio ya kweli juu ya

mambo ya milele. Sasa una macho madogo sana ya kiroho kiasi kwamba yale matakatifu unayaweka kwenye kiwango cha kawaida. Una majukumu. Ushawishi wako unaathiri dada zako kwa kiwango kikubwa. Usalama wako pekee ni kujitenga na ulimwengu. 3T 41.1

Nilioneshwa wewe, ndugu yangu, ukichukua vijana pamoja nawe kwenye matukio ya burudani/matumbuizo wakati wa maslahi ya kiroho/kidini, na pia ukishiriki katika shule za kuimba na walimwengu ambao wote ni giza na ambao wana malaika waovu pande zote. Je, nuru yako ambayo ni hafifu inaonekanaje katikati ya giza hili na majaribu? Malaika wa Mungu hawakuhudhuria katika matukio haya. Umeachwa uende peke yako ukitumia nguvu zako mwenyewe. Shetani anapendezwa sana na msimamo/nafasi yako; kwa maana anaweza kukufanya uwe na ufanisi zaidi katika utumishi wake kuliko kama hukukiri kuwa Mkristo unayeshika amri zote za Mungu. Shahidi wa Kweli analihutubia kanisa la Laodikia: “Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; Basi, kwa kuwa una uvuguvugu, wala hu baridi wala hu moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi; na mavazi meupe, upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane; na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu." 3T 41.2

Umepofushwa na kupumbazwa na mawazo ya kufikirika. Umejisikia nguvu ulipokuwa dhaifu mwenyewe. Unaweza kuwa hodari ukimtegemea Yeye Aliye Mkuu. Unaweza kuwa chombo cha haki ikiwa uko tayari kuteseka kwa ajili ya Kristo. Wewe na dada zako mnaweza kukomboa wakati mkipenda, lakini itagharimu juhudi kubwa. Dada yako mdogo ameunganishwa na yule ambaye hastahili kupendwa naye. Kuna kasoro kubwa katika tabia yake. Hana kicho kwa vitu vitakatifu; moyo wake haujabadilishwa na Roho wa Mungu. Yeye ni mbinafsi, mwenye majivuno/kujigamba, na anapenda starehe kuliko wajibu. Hana uzoefu wa kujinyima na kunyenyekea. 3T 42.1

Katika kutengeneza urafiki, tahadhari kubwa yapasa itumike ili urafiki wa karibu usiingizwe na mtu ambaye mfano wake haungekuwa salama kuiga; kwa maana matokeo ya ukaribu kama huo ni kupotoshwa kutoka kwa Mungu, kutoka kwenye ibada na upendo wa Ukweli. Ni hatari sana kwako kuwa karibu na marafiki ambao hawana uzoefu wa kiroho/kidini. Iwapo mmoja wenu, au ninyi nyote watatu, mtafuata maongozi ya Roho wa Mungu, au kuthamini wokovu wa nafsi yako, hamtachagua watu kama hao kuwa marafiki zenu wa karibu sana, wale ambao hawazingatii mambo ya kidini kwa uzito, na wasiozingatia kuishi chini ya ushawishi wake kwa vitendo (mtindo wa maisha). Mawazo ya milele yanapaswa kuja kwanza kwako. Hakuna kitu kinachoweza kuwa na ushawishi wa hila na hatari chanya juu

ya akili, na kutumika kwa ufanisi zaidi kukomesha hisia kali na usadikisho wa Roho wa Mungu, kuliko kushirikiana na wale ambao ni wapuuzi, na wasiojali, na ambao mazungumzo yao ni juu ya ulimwengu na ubatili. Kadiri watu hawa wanavyoweza kujihusisha zaidi katika mambo mengine, ndivyo ushawishi wao unavyokuwa hatari zaidi kama masahibu, kwa sababu wanajihusisha na maisha yasiyo ya kidini hivyo na wana vivutio vingi vya kupendeza. 3T 42.2

Mungu ana madai juu yenu ninyi nyote watatu ambayo hamwezi kuyatupa kando kirahisi. Yesu amekununua kwa bei ya damu Yake Mwenyewe. "Ninyi si mali yenu wenyewe; kwa kuwa mmenunuliwa kwa thamani; basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho zenu ambazo ni za Mungu." Je, wewe huna dhabihu ya kumtolea Mungu? Majukumu makubwa yanasimama mbele yako na kila mmoja wenu katika maisha ya kila siku. Rekodi zako kila siku zinamfikia Mungu. Hatari kubwa zimefichwa kwenye njia yako. Kama ningeweza, ningekuchukua mikononi mwangu na kukubeba salama ili uvuke na kuwa juu ya hatari hizi; lakini hili siruhusiwi kufanya. Uko katika kipindi muhimu zaidi cha historia ya maisha yako. Ikiwa utaamsha nguvu za roho na kuzielekeza kwenye kupata vitu vya kupendeza vya milele, na ikiwa utafanya kila kitu kuwa chini ya hii, utafaulu kukamilisha tabia ya Kikristo. Nyote mnaweza kushiriki katika vita vya kiroho dhidi ya dhambi zinazowasumbua, na mnaweza, kupitia Kristo, kuwa washindi. Lakini halitakuwa jambo rahisi kama mchezo wa kitoto. Itakuwa ni vita vikali, vinavyohusisha kujikana nafsi na kubeba msalaba. Hatari ni kwamba wewe hutatambua kikamilifu kurudi nyuma kwako na hali yako ya hatari. Isipokuwa unayatazama maisha jinsi yalivyo, tupilia mbali mawazo mazuri ya kufikirika, na ujishughulishe na masomo ya kiasi na uzoefu, utakuja kuamka wakati umechelewa. Hapo utagundua kosa baya sana ulilofanya. 3T 43.1

Elimu yako haijawa ya aina hiyo ili kuunda wahusika madhubuti, kwa hivyo lazima upate elimu ambayo ulipaswa kuwa nayo miaka iliyopita. Mama yako alikuwa anakupenda sana. Mama hawezi kuwapenda watoto wake kwa kupindukia [lazima awapende], lakini anaweza kuwapenda bila hekima na kuruhusu mapenzi yake yampofushe hata asione masilahi yao bora. Umekuwa na mama mpole, mwenye kukuendekeza. Amewakingia kifua watoto wake kupita kiasi. Maisha yake yamekaribia kupondwa na mizigo ambayo watoto wake walipaswa kubeba, na ambayo wangeweza kubeba vizuri kuliko yeye. 3T 43.2

Ukosefu wa uimara na kujinyima kwa wahusika wako ni kikwazo kikubwa katika kupata uzoefu wa kweli wa kidini ambao hautakuwa mchanga wenye kuteleza. Uthabiti na uadilifu wa kusudi unapaswa kukuzwa. Sifa hizi ni muhimu kwa maisha ya Kikristo yenye mafanikio. Ukiwa na uadilifu wa nafsim hutayumbishwa kutoka kwenye haki na lile lililo sahihi. Hakuna nia itakayotosha kukusogeza kutoka kwenye mstari ulionyooka wa wajibu; utakuwa mwaminifu na mwenye

kumtegemea Mungu. Kusihi kwa mapenzi na upendo, matamanio ya urafiki, hayatakusukuma wewe kugeuka kutoka kwenye Ukweli na wajibu; hautaacha wajibu kwa sababu mvuto wenye mwelekeo wa chini. 3T 44.1

Ikiwa wewe, ndugu yangu, unashawishiwa kuunganisha maslahi yako ya maisha na msichana mdogo, asiye na uzoefu, ambaye ana upungufu wa elimu katika mambo ya kawaida ya kivitendo, na majukumu ya kila siku ya maisha, unafanya makosa; lakini upungufu huu ni mdogo ukilinganisha na ujinga wake kuhusiana na wajibu wake kwa Mungu. Hajakosa nuru; amekuwa na mapendeleo ya kidini, na bado hajahisi dhambi yake mbaya bila Kristo. Ikiwa, wewe katika kupenda kwako, unaweza kuacha tena na tena mikutano ya maombi, mahali ambapo Mungu hukutana na watu Wake, ili kufurahia jamii ya mtu ambaye hana upendo kwa Mungu na ambaye haoni vivutio katika maisha ya kiroho/kidini, Je, unawezaje kutarajia Mungu afanikishe ndoa/muungano kama huu? Usiwe na haraka. Ndoa za mapema hazipaswi kuhimizwa. Iwapo ama vijana wa kike au wa kiume hawataheshimu madai ya Mwenyezi Mungu, ikiwa watashindwa kuzingatia madai ambayo yanawafungamanisha na dini, kutakuwa na hatari kwamba hawatazingatia ipasavyo madai ya mume au ya mke. Tabia ya kuwa mara kwa mara katika jamii ya yule unayemchagua, na kwamba, pia, katika kutoa sadaka ya mapendeleo ya kidini na saa zako za maombi, ni hatari; unapata hasara ambayo huwezi kumudu. Tabia ya kukaa hadi usiku sana imekuwa ni desturi; ila haimpendezi Mungu, hata kama nyote wawili ni Wakristo. Saa hizi zisizofaa zinaumiza afya, hazifai akili kwa majukumu ya siku inayofuata, na zina mwonekano wa uovu. Ndugu yangu natumai utajiheshimu mwenyewe kiasi cha kuachana na aina hii ya uchumba. Ukiwa na jicho lililokita kwa utukufu wa Mungu, utasonga kwa tahadhari ya makusudi. Huwezi kuteseka na hisia za ugonjwa wa mapenzi yenye kupumbaza ili kupofusha maono yako hata huwezi kutambua madai ya juu ambayo Mungu anayo juu yako kama Mkristo. 3T 44.2

Vijana wapendwa, ninajielekeza kwenu watatu. Hebu liwe lengo lako kumtukuza Mungu na kupata mfano Wake wa maadili. Alika Roho wa Mungu awafiche wahusika wako. Sasa ni fursa yako nzuri ya kufua mavazi yako ya tabia na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Ninachukulia hii kama hatua ya kugeuka na kufanya mabadiliko katika hatima ya kila mmoja wenu. Utachagua lipi, asema Kristo, Mimi au ulimwengu? Mungu anatoa wito wa kujisalimisha bila masharti kwa moyo na mapenzi Kwake. Mkiwapenda rafiki, ndugu au dada, baba au mama, nyumba au mashamba kuliko Mimi, asema Kristo, hamnistahili Mimi. Dini huiweka nafsi chini ya wajibu mkubwa zaidi kwa madai yake, kutembea kwa kanuni zake. Kama vile sumaku ya ajabu inavyoelekeza upande wa kaskazini, ndivyo madai ya dini yanavyoelekeza kwenye utukufu wa Mungu. Umefungwa na viapo vyako vya ubatizo, kumheshimu Muumba wako na kujikana kwa uthabiti na kusulubisha

mapenzi na tamaa zako, na kuleta hata mawazo yako katika utiifu kwa mapenzi ya Kristo. 3T 45.1

Epuka kukimbilia majaribuni. Wakati majaribu yanapokuzingira, na huwezi kudhibiti hali zinazokuweka wazi kwayo, ndipo unaweza kudai ahadi ya Mungu, na kwa ujasiri na uwezo wa kufahamu utangaze: “Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.” Kuna nguvu kwenu nyote kwa Mungu. Lakini hutahisi kamwe hitaji lako la nguvu hizo ambazo pekee ndizo zinaweza kukuokoa, isipokuwa uhisi udhaifu wako na dhambi. Yesu, Mwokozi wako wa thamani, anakuita sasa kuchukua msimamo wako kwa uthabiti juu ya jukwaa la Ukweli wa milele. Ukiteseka pamoja Naye, Yeye atakupa taji ya utukufu katika ufalme Wake wa milele. Ikiwa uko tayari kutoa yote kwa ajili Yake, basi Yeye atakuwa Mwokozi wako. Lakini ukichagua njia yako mwenyewe utafuata gizani hadi utakapochelewa kupata thawabu ya milele. 3T 45.2

Je, upo tayari kuteseka kwaajili ya nini, kwa ajili ya Ukweli? Una kipindi kifupi sana cha kukuza sifa nzuri za wahusika wako. Ninyi nyote mmekuwa, kwa kiasi fulani, hamjaridhika na hamjafurahi. Mmekuwa na malalamiko mengi ya kufanya. Mmeongea kutokuamini na umewalaumu wengine. Hasa hii ni kweli kwa F na H. Mioyo yenu imejazwa na kiburi, na hata uchungu wakati mwingine. Vyumba na makabati yenu yamepuuzwa, na hamjapenda mazoezi ya majukumu ya kiroho/kidini. Kama mngekuwa mmevumilia katika juhudi zenu za kukua ndani ya Kristo, Kichwa chenu kilicho hai, sasa ungekuwa na nguvu, na uwezo wa kuwabariki wengine kwa ushawishi wako. Kama ungekuwa umekuza nishati thabiti isiyoyumba sasa ungekuwa na nguvu za kupinga majaribu. Lakini sifa hizi za thamani zinaweza kupatikana tu kwa kusalimisha nafsi kwa madai ya dini. Kisha nia na malengo yatakuwa ya juu, na akili na mapenzi yatasawazishwa na kanuni bora. Mungu atafanya kazi nasi ikiwa tu tutajihusisha na matendo yenye afya. Ni lazima tuhisi umuhimu wa kuunganisha juhudi zetu za kibinadamu na hatua ya ari na bidii na uwezo wa Mungu. Tunaweza kusimama mbele za Mungu, tukiwa na nguvu za kushinda. Wewe, Ndugu E, umeshindwa mno katika nishati ya kusudi la kufanya na kuvumilia. 3T 46.1

Ni kosa kubwa jinsi gani linalofanywa katika malezi ya watoto na vijana, katika kuwapendelea, kuwadekesha, kuwastarehesha, na kuwabembeleza. Wanakuwa wabinafsi na wasiofaa, na kukosa nishati katika vitu vidogo vya maisha. Hawajafunzwa kupata nguvu ya tabia kwa kufanya kazi za kila siku, ingawa wanaweza kuwa duni. Unapuuza kufanya kwa hiari na kwa furaha kile ambacho kiko mbele yako kufanya, na ambacho mtu lazima afanye. Kuna hamu kubwa na sisi sote kupata kazi kubwa zaidi, iliyotukuka zaidi. 3T 46.2

Hakuna anayestahili kwa kazi kubwa na muhimu isipokuwa amekuwa mwaminifu katika utendaji wa majukumu madogo-madogo. Ni kwa viwango kwamba mhusika huundwa na kwamba nafsi inayozoezwa kuweka juhudi na nguvu kulingana na kazi ambayo inapaswa kukamilishwa. Ikiwa sisi ni viumbe wa hali/mazingira, hakika tutashindwa kukamilisha tabia za Kikristo. Lazima umiliki mazingira/hali, na usiruhusu mazingira/hali zikudhibiti. Unaweza kupata nishati kwenye msalaba wa Kristo. Sasa unaweza kukua kwa viwango/digrii, na kushinda matatizo, na kushinda nguvu ya tabia. Unahitaji kuchochewa na nguvu ya uzima ya Yesu. Unapaswa kuvutiwa kwa Kristo na kuvikwa uzuri na ubora Wake wa Uungu. Binti wa kaka G ana elimu ya kupata; hana uwezo zaidi wa majukumu na ugumu wa maisha kama mke kuliko msichana wa shule mwenye umri wa miaka kumi. 3Tsw 46.3

Dini inapaswa kukuamuru, kukuratibu na kukuongoza katika harakati zako zote, na inapaswa kushikilia udhibiti kamili juu ya mapenzi yako. Ukijitoa bila kujibakiza mikononi mwa Kristo, ukifanya nguvu Zake kuwa nguvu yako, basi maono yako ya kimaadili yatakuwa wazi ili kutambua ubora wa tabia ili usije ukadanganywa na mwonekano na kufanya makosa makubwa katika urafiki wako. Nguvu zako za kimaadili lazima ziwe kali/makini na nyeti, ili ziweze kubeba majaribu makali na zisiharibiwe. Uadilifu wako wa roho/nafsi unapaswa kuwa thabiti hivi kwamba ubatili, maonesho, au kusifiwa kwa udanganyifu, kubembelezwa au kujipendekeza havitakuchochea. 3T 47.1

Lo, ni jambo kuu kuwa sawa na Mungu, roho kupatana na Muumba wake, ili, katikati ya maambukizo ya kielelezo kiovu, ambacho kwa kuonekana kwake kidanganyifu kungeweza kuivuta roho kutoka kwa wajibu, malaika waweze kutumwa kukuokoa! Lakini kumbuka, ukikaribisha majaribu mwenyewe, hutakuwa na usaidizi wa Mungu wa kukuzuia usishindwe. Wale watu watatu waliostahili walistahimili tanuru ya moto, kwa maana Yesu alitembea pamoja nao katika ule mwali wa moto. Lau wao wenyewe wangeingia motoni, wangeteketea. Ndivyo itakavyokuwa kwako. Usipotembea ukiazimia/kimakusudi katika majaribu, Mungu atakutegemeza jaribu likija. 3T 47.2

SURA YA 5

KAZI MJINI NEW YORK

Nikiwa Vermont, Desemba 10, 1871, nilioneshwa mambo fulani kuhusu New York. Sababu/kazi katika hali hiyo ilionekana kuwa katika hali ya kusikitisha. Kulikuwa na watenda kazi wachache tu, na hawa hawakuwa na ufanisi kama vile kukiri kwao kwa imani katika Kweli takatifu kwa wakati huu kulivyodai kufanya. Kuna wale katika Jimbo hilo waliohudumu kwa Neno na Mafundisho ya imani (Doctrines), ambao si watenda kazi wakamilifu, kazi zao ni nusunusu (not thorough). Ingawa wanaamini nadharia ya Ukweli, na wamekuwa wakihubiri kwa miaka mingi, hawatawahi kuwa watenda kazi hodari hadi wafanye kazi kwa mpango tofauti. Wametumia muda mwingi ndani ya makanisa, wakati hawana sifa za kuwafaidi. Wao wenyewe hawajawekwa wakfu mbele za Mungu. Wanahitaji roho ya uvumilivu kuteseka kwa ajili ya Kristo, “kukinywea kikombe,” na “kubatizwa kwa ubatizo,” kabla ya kuwa tayari kuwasaidia wengine. Watendakazi wasio na ubinafsi, waliojitolea wanahitajika, ili kuyainua mambo katika New York kwa kiwango cha Biblia. Watu hawa hawajawa katika mstari wa wajibu wao katika kusafiri kati ya makanisa. Ikiwa Mungu amewaita kwa kazi Yake, ya kuwaokoa wenye dhambi. Wanapaswa kujithibitisha wenyewe kwa kwenda nje katika mashamba mapya, ili wajue wenyewe kama Mungu amewakabidhi kazi ya kuokoa roho. 3T 48.1

Kama Ndugu Taylor, Saunders, Cottrell, Whitney, na Kaka na Dada Lindsay wangefanya kazi katika maeneo/nyanja mpya, sasa wangekuwa mbele sana kutokana na walivyo. Kukutana na upinzani wa wapinzani kungewasukuma kwenye Biblia zao kwa hoja za kutegemeza msimamo wao, na hilo lingeongeza ujuzi wao wa Maandiko na kuwapa utambuzi wa uwezo wao ndani ya Mungu wa kukabiliana na upinzani kwa namna yoyote ile. Wale wanaotosheka kwenda tena na tena kati ardhi ile ile ya makanisa, watakuwa na upungufu katika uzoefu wanaopaswa kuwa nao. Watakuwa dhaifu—wasiwe na nguvu ya kutaka, kufanya na kuteseka kwa ajili ya Ukweli. Watakuwa wafanyakazi wasio na tija. 3T 48.2

Wale walio na kazi ya Mungu mioyoni mwao na kuhisi upendo kwa nafsi za thamani ambazo Kristo alizifia, hawatatafuta raha au anasa zao wenyewe. Watafanya kama Kristo alivyofanya. Wataenda “kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.” Alisema: “Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi wapate kutubu.” 3T 49.1

Ikiwa watendakazi katika mji wa New York wangependa kulisaidia kanisa, hakuna njia bora zaidi wanayoweza kufanya hivyo kama kwenda katika maeneo/nyanja mpya na kufanya kazi ili kuleta roho katika Kweli. Kanisa linapoona kwamba wahudumu wote wanawaka na Roho ya kazi, kwamba wanahisi kwa kina nguvu ya Ukweli, na wanatafuta kuwaleta wengine kwenye ujuzi wake, litaweka maisha mapya na nguvu ndani yao. Mioyo yao itachochewa kufanya wawezavyo ili kusaidia katika kazi hiyo. Hakuna tabaka la watu ulimwenguni ambao wako tayari zaidi kujitolea mali zao kuendeleza kazi hiyo ya Bwana kuliko Waadventista Wasabato. Ikiwa wahudumu hawatawavunja moyo kabisa kwa uvivu wao, kukosa ufanisi na uzembe wao, na kwa kukosa kwao hali ya ukiroho, kwa ujumla wataitikia ombi au mwito wowote unaoweza kutolewa ambao unashawishi maamuzi/hukumu na dhamiri zao. Lakini wanataka kuona matunda. Na ni halali/haki kwamba ndugu waliopo mji wa New York wanapaswa kudai matunda ya wachungaji wao. Je, wamefanya nini? Je, wanafanya nini? 3T 49.2

Wachungaji/Watumishi huko New York walipaswa kuwa mbali kuliko jinsi walivyo. Lakini hawajajishughulisha na aina hiyo ya kazi ambayo ilileta bidii na upinzani mkali. Laiti wangefanya hivyo wangesukumwa kwenye Biblia zao na kwenye maombi ili kuweza kuwajibu wapinzani wao, na katika kutumia vipaji vyao vingeongezeka maradufu. Kuna wachungaji huko New York ambao wamekuwa wakihubiri kwa miaka mingi, lakini ambao hawawezi kutegemewa kutoa mipangilio ya mada za mahubiri [kozi] ya mihadhara. Wao ni duni, ni mbilikimo katika uwezo wao. Hawajazoeza akili zao katika kujifunza Neno na kukabiliana na upinzani, ili wawe na nguvu katika Mungu. Wangekuwa kama askari waaminifu wa msalaba wa Kristo, wangetoka “nje ya kambi,” wakimtegemea Mungu na nguvu zao wenyewe, badala ya kuegemea sana juu ya ndugu zao, wangepata uzoefu, na sasa wangepata stahiki/sifa za kushiriki katika kazi popote ambapo msaada wao unahitajika zaidi. Ikiwa wahudumu kwa ujumla katika jimbo la New York wangeyaacha makanisa ili wafanye kazi kwa ajili yao wenyewe, na wasingesimama katika njia yao, makanisa

na wahudumu wote wangekuwa sasa wameendelea zaidi katika hali ya kiroho na katika ujuzi wa Ukweli. 3T 49.3

Ndugu zetu wengi huko New York wamekuwa wakirudi nyuma juu ya matengenezo ya afya. Kuna idadi ndogo tu ya wanamatengenezo wa kweli wa afya katika jimbo. Nuru na ufahamu wa kiroho umetolewa kwa ndugu huko New York. Lakini Ukweli ambao umefikia ufahamu, nuru ambayo imeangaza juu ya roho, ambayo haijathaminiwa na kupendwa, itashuhudia dhidi yao katika siku ya Mungu. Ukweli umetolewa kuwaokoa wale ambao wangeamini na kutii. Kuhukumiwa kwao si kwa sababu hawakuwa na nuru, bali kwa sababu walikuwa na nuru na hawakuenenda ndani yake. 3T 50.1

Mungu amempa mwanadamu njia nyingi za kutosheleza hamu ya asili. Yeye Ameziweka mbele Yake, katika mazao ya ardhi, aina nyingi za chakula zenye ladha nzuri na zenye lishe bora kwa mfumo. Baba yetu wa mbinguni Mwenye fadhili anasema kwamba tunaweza ‘kula kwa uhuru. Tunaweza kufurahia matunda, mboga mboga, nafaka, bila kuharibu sheria za utu wetu. Vitu hivi, vilivyotayarishwa kwa njia rahisi na ya asili zaidi, vitaulisha mwili, na kuhifadhi nguvu zake za asili bila matumizi ya nyama. 3T 50.2

Mungu alimuumba mwanadamu kwa daraja la chini kidogo kuliko malaika na kumpa sifa ambazo, zikitumiwa ipasavyo, zitamfanya awe baraka kwa ulimwengu na kumfanya aakisi utukufu kwa Mpaji. Lakini ingawa ameumbwa kwa mfano wa Mungu, mwanadamu, kupitia kutokuwa na kiasi, amekiuka kanuni na sheria ya Mungu katika asili yake ya kimwili. Kutokuwa na kiasi kwa namna yoyote ile huharibu viungo vya utambuzi na hivyo kudhoofisha nguvu ya neva na ubongo kiasi kwamba mambo ya milele hayathaminiwi, bali yanawekwa kwenye kiwango, sawa na yale ya kawaida. Nguvu za juu za akili, ziliumbwa kwa madhumuni yaliyoinuliwa, huletwa katika utumwa wa tamaa mbaya. Ikiwa mazoea yetu ya kimwili si sawa, nguvu zetu za akili na maadili (roho) haziwezi kuwa na nguvu; Kwa maana uhusiano mkubwa unaohurumiana upo kati ya mwili na maadili. Mtume Petro alielewa jambo hilo na akapaza sauti yake ya onyo kwa ndugu zake: “Wapenzi, nawasihi kama wageni na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili, ambazo hupigana vita na Roho. 3T 50.3

Kuna nguvu ndogo sana ya maadili katika ulimwengu unaodai kuwa ni wa Kikristo. Mazoea mabaya yameendekezwa, na sheria za kimwili na utauwa na maadili vimepuuzwa mpaka kufikia hatua ya kuziweka sawa na viwango vya kidunia kwa ujumla. Mazoea ambayo hupunguza kiwango cha afya ya kimwili, hudhoofisha nguvu za kiakili na kimaadili. Kuendekeza/kuridhisha kwa tamaa za mwili na zisizo za asili hupelekea kuwapo na ushawishi unaotawala kwenye neva za ubongo. Viungo vya tabia za wanyama vinaimarishwa, wakati maadili yanaminywa kabisa. Haiwezekani kabisa kwa mtu asiye na kiasi kuwa Mkristo, kwa kuwa nguvu zake za juu/ubongo zinaletwa katika utumwa wa tamaa. 3T 51.1

Wale ambao wamekuwa na nuru juu ya mambo ya kula na kuvaa kwa usahili katika utii wa sheria za kimwili na za kimaadili, na ambao wanaiacha nuru inayoonesha wajibu wao, watakwepa wajibu katika mambo mengine. Wakizinyamazisha dhamiri zao ili kuepuka msalaba ambao itawabidi kuubeba ili kupatana na sheria ya asili, wao, ili kuepuka lawama, watakiuka Amri Kumi. Kuna uamuzi wa kutokuwa tayari kwa wengine kuvumilia msalaba na kudharau aibu. Wengine watachekwa kutokana na kanuni zao. Maridhiano na ulimwengu yanazidi kupata mizizi/msingi kati ya watu wa Mungu, wanaodai kuwa wasafiri, wapitaji na wageni hapa duniani, wakingojea na kutazama kutokea kwa Bwana. Kuna wengi miongoni mwa wanaodai kuwa washika Sabato huko New York ambao wamefunga ndoa kwa kifungo kizito zaidi na mitindo na tamaa za kiulimwengu kuliko walivyo na miili yenye afya, akili timamu, au mioyo iliyotakaswa. 3T 51.2

Mungu anawapima na kuwathibitisha watu binafsi huko New York. Yeye Ameruhusu wengine wawe na kiasi fulani cha ustawi/mafanikio ili kuendeleza yale yaliyo mioyoni mwao. Kiburi na upendo wa ulimwengu vimewatenganisha na Mungu. Kanuni za Ukweli karibia zote zimetolewa dhabihu, huku watu wakidai kupenda Ukweli. Wakristo wanapaswa kuamka na kutenda. Ushawishi unanena na kutengeneza maoni juu ya tabia za wengine. Watalazimika kubeba jukumu zito la kuamua kwa ushawishi wao hatima ya roho za wengine. 3T 51.3

Bwana, kwa Ukweli ulio karibu na wazi kwa siku hizi za mwisho, anawatenganisha watu kutoka katika ulimwengu na kuwatakasa kwa ajili yake Mwenyewe. Kiburi na mitindo isiyo ya afya, upendo wa kujionesha, upendo wa kukubalika—yote haya lazima yaachwe na ulimwengu ikiwa tungefanywa upya katika ujuzi sawa na mfano Wake Yeye aliyetuumba. “Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo inatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tukilitazamia tumaini lenye baraka na ufunuo wa utukufu wa Yesu Kristo, Mungu Mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi Yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake Mwenyewe ya kipekee, wale walio na juhudi katika matendo mema.” 3T 52.1

Kanisa katika ----- linahitaji kupepetwa. Uongofu kamili ni muhimu kabla ya kuwa katika mpangilio wa kufanya kazi. Ubinafsi, kiburi, husuda, dhulma, matusi, maovu, na masengenyo yametunzwa miongoni mwao, mpaka Roho wa Mungu amekuwa na uhusiano kidogo pamoja nao. Ingawa baadhi ya wanaodai kumjua Mungu wanabaki katika hali yao ya sasa, maombi yao ni chukizo machoni Pake. Hawaidhinishi imani yao kwa matendo yao, na ingekuwa afadhali kwa wengine wasingeweza kamwe kuukiri Ukweli kuliko kudharau kazi yao kama walivyofanya. Ingawa wanadai kuwa Wakristo na watumishi wa Kristo, wao ni watumishi wa adui wa haki; na matendo yao yanawashuhudia kwamba hawajamfahamu Mungu na kwamba mioyo yao haiendani na utiifu kwa mapenzi ya Kristo. Wanafanya utani

kama Watoto wadogo kuhusu dini (mambo ya kiroho); wanatenda kama watoto wadogo waliodekeshwa/walioendekezwa. 3T 52.2

Watoto wa Mungu, ulimwenguni kote, ni wenye undugu. Mwokozi wetu amefafanua waziwazi roho na kanuni zinazopaswa kutawala matendo ya wale ambao, kwa uthabiti, maisha yao matakatifu, wanajitofautisha na ulimwengu. Upendo wao kwa wao, na upendo mkuu zaidi kwa Baba yao wa mbinguni, unapaswa kuoneshwa katika mazungumzo na kazi zao. Hali ya sasa ya watoto wengi wa Mungu ni kama familia ya watoto wasio na shukrani na wagomvi. 3T 52.3

Kuna hatari ya hata wachungaji/wahudumu katika mji wa New York kuwa katika daraja hilo ambao daima wanajifunza ila hawawezi kamwe kufikia ujuzi wa Kweli. Hawajibidishi kutenda yale wanayojifunza. Wao ni wasikiaji tu wa Neno, lakini si watendaji. Wahudumu hawa wanahitaji uzoefu katika Ukweli ambao utawawezesha kufahamu tabia iliyotukuka ya kazi. 3T 53.1

Tunaishi katika wakati mzito/nyeti, muhimu sana katika historia ya dunia hii. Tunaishi ndani ya siku za hatari za mwisho. Matukio muhimu na ya kutisha yako mbele yetu. Ni muhimu kwa kiasi gani kwamba wote wanaomcha Mungu na kuipenda sheria Yake wanyenyekee mbele Zake, na kujitesa na kuomboleza, na kuungama juu ya dhambi ambazo zimewatenga na Mungu wao. Hii inapaswa kuchochea moyoni kengele kuu, ni kwamba hatuhisi au kuelewa hali yetu, hali yetu ya chini, na kwamba tunaridhika kubaki jinsi tulivyo. Tunapaswa kulikimbilia Neno la Mungu na kwa maombi, kila mmoja wetu akimtafuta Bwana kwa dhati na bidii, ili tumpate. Tunapaswa kufanya hii biashara/shuguli yetu ya kwanza. 3T 53.2

Washiriki wa kanisa wanawajibika kwa talanta zilizokabidhiwa kwa amana yao, na haiwezekani kwa Wakristo kutimiza wajibu wao isipokuwa wakizishikilia nafasi zilizoinuliwa mbele yao na ambazo zinaendana na Kweli zile takatifu wanazozikiri. Nuru inayoangazia njia yetu hutufanya tuwajibike kuiacha nuru hiyo iangaze kwa wengine kwa namna ambayo watamtukuza Mungu. 3T 53.3

Ndugu Katika Kanisa.

Maendeleo ya kanisa katika mambo ya kiroho katika kanisa-------- hayalingani na nuru iliyoangaza katika njia yao. Mungu ameweka dhamana ya kila talanta kuboreshwa kwa kuzitendea kazi kwa wachuuzi, ili Bwana ajapo awapokee walio wake pamoja na kundi lao. Kanisa la ---------- kwa kiasi kikubwa lina nyenzo za thamani, lakini washiriki wake wanashindwa kukifikia kiwango cha juu ambacho ndio fursa yao ya pekee. 3T 53.4

Nyenzo za kazi katika kanisa zinapatikana zaidi katika matawi ya familia tatu ambazo zimeunganishwa na ndoa. Kuna talanta nyingi zaidi kanisani, na nyenzo nyingi zaidi za kutengeneza watenda kazi wazuri, ambao wanaweza kuajiriwa kwa faida ya eneo husika. Kanisa zima halikui kiroho. Halipo katika hali nzuri kusitawisha nguvu kwa kutumia talanta ambazo Mungu amelipatia. Hakuna nafasi

kwa wote kufanya kazi. Kila mmoja anakatiza kwenye njia ya mwingine. Kuna ukosefu wa nguvu za kiroho. Endapo kanisa hili lingekuwa kama familia kila mmoja angeuhisi wajibu wake. 3T 54.1

Ikiwa talanta na ushawishi wa washiriki kadhaa vingetumiwa katika makanisa mengine, ambapo wangevutwa zaidi kutoa msaada mahali ambapo msaada unahitajika kweli, wangepata uzoefu wa thamani ya juu zaidi katika mambo ya kiroho, na kwa kubeba majukumu na mizigo katika kazi ya Mungu kungekuwa ni mbaraka kwa wengine. Huku wakishiriki katika kuwasaidia wengine, watakuwa wakimfuata Kristo kama kielelezo. Yeye Hakuja kuhudumiwa, bali kuhudumia wengine. Hakuwa mbinafsi au Mwenye kujipendeza Mwenyewe. Alijinyenyekeza, na kuishi kama mtumwa, huku akitumia maisha Yake katika kutenda mema. Masihi Angeweza kuzitumia siku Zake duniani katika starehe za maisha na kuishi kwa utajiri na vitu vingi na starehe za maisha haya, lakini hukuishi ili ajifurahishe, aliishi ili atende mema na kuwaokoa wengine katika mateso, na mfano Wake upo kwetu ili tuweze kuufuata. 3T 54.2

Ikiwa wangejiweka wakfu kwa Mungu, Ndugu I na J wangebeba majukumu makubwa zaidi ya waliyobeba. Wamefikiria kwamba wangekuwa wepesi zaidi katika kuuitikia wito wowote unaohusu fedha, na ya kwamba huo ndio mzigo/wito mkuu ambao walipaswa kubeba katika kazi ya Mungu. Lakini Mungu anahitaji kutoka kwao zaidi ya haya. Kama wangezifunza akili zao katika kulichunguza sana Neno la Mungu, ili wapate kuwa watendakazi katika kazi Yake, na kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wadhambi kama wanavyoonesha bidii kutafuta vitu vya maisha haya, wangekuza nguvu na hekima ya kushiriki katika kazi ya Mungu pale ambapo watenda kazi wanahitajika sana. 3T 54.3

Ndugu hawa, kwa kubaki katika jumuiya ya familia, hudumaa kiakili na kiroho. Si vyema kwa watoto wa familia moja, mbili, au tatu ambazo zimeunganishwa kwa ndoa, kuishi karibu-karibu (maili chache kutoka kwa kila moja wao). Jambo hili huleta ushawishi mbaya ndani ya hizo familia. Shuguli na Jukumu la mtu mmoja hugeuka kuwa la wote. Mifadhaiko na matatizo yanayoikumba kila familia yawe makubwa au madogo ambayo kwa hali yoyote ile yangepaswa yajulikane ndani ya familia husika tu, huenea kwa familia zote, na kufikishwa katika mikutano ya kiroho/kidini na kuathiri wengine. Yapo mambo yasiyopaswa kujulikana kwa mtu wa tatu, iwe ni rafiki au mtu wako wa karibu sana. Yanapaswa kubebwa na mtu binafsi au familia husika. Lakini uhusiano wa karibu uliyopo baina ya familia kadhaa, unaosababishwa na ushirikiano wa mara kwa mara, una tabia ya kuvunja hadhi/heshima ambayo inapaswa kudumishwa katika kila familia. Katika utekelezaji wa jukumu nyeti la kukemea na kuonya, yawezekana kukawa na hatari ya kuumiza hisia za mtu, isipokuwa litafanywa kwa upole, upendo mwanana, kujali na huruma nyororo na uangalifu mkubwa zaidi. Mifano ya tabia bora huwajibika katika makosa, na uangalifu mkubwa wapaswa kutekelezwa ili kwamba milima isifutuke kutoka kwenye matuta madogo madogo. 3T 55.1

Uhusiano kama huo wa kifamilia na kanisa kama ulivyo katika ---- hupendezesha sana hisia za asili; lakini sio bora, kwa kuzingatia mambo yote, na kwa ukuaji wa tabia zenye ukamilifu za Kikristo (kwa kawaida haisaidii tabia kuwa njema). Uhusiano wa karibu na ushirikiano uliozoeleka baina ya watu fulani, wakiambatana na kanisa, huhafifisha ukuaji wa kanisa. Heshima, kujiamini, na upendo unaofanya kanisa listawi hutoweka. Familia zote zitakuwa na furaha zaidi endapo hazitakuwa na ukaribu zaidi na familia nyingine na kutembeleana mara kwa mara, kisha ushawishi baina yao ungeongezeka mara kumi zaidi. 3T 55.2

Umoja uliopo baina ya familia hizi kupitia ndoa, na katika kuchangamana kwa urafiki uliokithiri au ukaribu wa makazi, kila mmoja huwa macho kuangalia makosa ya wenzake, na hujihisi kuwa na wajibu wa kuwarekebisha; na kwa sababu ndugu hawa wanapendana sana, uhuzunishwa na mambo madogo-madogo ambayo wasingeweza kuyaona kwa wale wasio na uhusiano nao wa karibu sana. Mateso makali ya akili huvumiliwa, kwa sababu hisia zitajitokeza kwa wengine ya kwamba hawajatendewa vizuri namna wanavyostahili kutendewa. Viwivu vidogodogo hutokea na vichuguu vya mchwa huwa milima. Malumbano haya na tofauti ndogo ndogo husababisha mateso makali ya akili kuliko yawezavyo mitihani/majaribu yanayotokana na vyanzo vingine. 3T 55.3

Mambo haya huwafanya wanaume na wanawake hawa wenye dhamiri na nia njema kushindwa kustahimili, na huipoteza tabia njema iliyokuwa ikikua ndani yao endapo wangeishi mahali tofauti. Wamedumazwa kiakili na kiroho. Hali hii hutishia kuuharibu manufaa/umuhimu yao. Kazi na masilahi yao yamejikita zaidi kwao wenyewe. Mvuto wao umepunguzwa wakati ulipaswa kukua zaidi na kuwa desturi, ili kwamba, kwa kuwekwa katika hali/mazingira mbalimbali, ili waweze kuutumia uwezo ambao Mungu amewapatia, kwa namna ambayo utauinua zaidi utukufu Wake. Vitivo vyote vya akili vina uwezo wa kuwa bora zaidi. Nguvu za nafsi zinahitaji kuamshwa na kuletwa katika vitendo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. 3T 56.1

Watendakazi Kwa BWANA

Mungu anawasihi na kuwaita wamishenari. Kuna watu wenye uwezo katika kanisa ----- ambao uwezo wao utakuzwa kwa ubora zaidi pale watakapotumia talanta zao katika kazi ya Mungu. Ikiwa ndugu hawa watajielimisha wenyewe na kulifanya kusudi la kazi ya Mungu kuwa kipaumbele au maslahi ya kwanza kwao, na kuziacha anasa za ulimwengu huu kwa ajili ya ile Kweli, basi baraka za Mungu zitakuwa juu yao. Ndugu hawa, wapendao Kweli, na ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakifurahi kwa sababu ya nuru inayoongezeka juu ya Maandiko, wanapaswa kuacha nuru yao iwaangazie wale walio gizani. Mungu atakuwa kwao hekima na nguvu, na atajitukuza Mwenyewe katika kufanya kazi pamoja na wale

wanaomfuata kikamilifu. Ikiwa “Mtu akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu.” Hekima na nguvu za Mungu zitatolewa kwa walio tayari na waaminifu. 3T 56.2

Ndugu katika ----- wamekuwa tayari kutoa mali zao kwa ajili ya shughuli mbalimbali, lakini wamejizuia. Hawakusema, Mimi hapa, Bwana; nitumie/nitume. Si kwa nguvu za kibinadamu ambazo huvifanya vyombo vya wanadamu kufanikiwa, bali ni nguvu na hekima Yake Yeye anayevitumia na kufanya kazi pamoja navyo ndivyo vinavyowafanya wanadamu wafanikiwe katika kufanya kazi ambayo ni muhimu kufanywa. Kwa kutoa mali zetu kwa Mwenye mbingu na nchi huku tukijizuia wenyewe (tusiwe pale kimwili), kamwe hatuwezi kupata ridhaa Yake wala kupata baraka Zake. Lazima kuwe na kanuni mioyoni mwa kaka na dada ---- kanuni kuhusu kutoa yote na hata kujitoa wao wenyewe, katika madhabahu ya Mungu. 3T 57.1

Watu bado wanahitajika katika mji wa Battle Creek ambao wako tayari na wataweza kuyaacha majukumu yao ili kuchukua majukumu ya Bwana na kufanya kazi. Wito huo umetolewa mara kwa mara tena na tena, lakini imekuwa vigumu kwa wengi kuitikia. Wengine wangeitikia wito huo kama maslahi yao ya kidunia yangeendelezwa kwa kufanya hivyo. Lakini kwa vile hakukuwa na matarajio ya kuongeza mali/uwezo wao kwa kuja Battle Creek, hawakuweza kuona wajibu wa kuja. "Kutii ni bora kuliko dhabihu." Na bila ya utii na upendo usio na ubinafsi, sadaka inayoonekana kuwa kubwa zaidi ni ndogo sana kuwasilishwa kwa Mmiliki wa vitu vyote. 3T 57.2

Mungu anawaita ndugu na dada katika ----- wanyanyuke na kuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu, ili awape nguvu dhidi ya adui (Waamuzi 5:23). Sababu inayofanya kuwe na nguvu ndogo sana miongoni mwa wale wanaodai Ukweli ni kwamba hawatumii uwezo ambao Mungu amewapa. Wengi sana wamefunga talanta zao kwenye leso/vitambaa na kuzificha ardhini. Ni kwa kutumia vipaji ndiyo wanaongezeka. Mungu atawapima na kuwathibitisha watu Wake. 3T 57.3

Ndugu Kaka na Dada I, wamekuwa wakifanya majukumu ya Mungu kwa uaminifu, na sasa watoto wao hawapaswi kusimama nyuma na kuacha majukumu kuwaelemea sana. Ni wakati ambapo nguvu za akili ambazo bado hazijachoshwa sana zilizo ndani ya watoto zinapaswa kuzoeshwa kufanya kazi zaidi haswa katika shamba la mizabibu la Bwana. 3T 57.4

Baadhi ya ndugu katika mji wa New York wamekuwa na wasiwasi kwamba Ndugu na Dada K, na haswa Dada K, anapaswa kutiwa moyo kufanya kazi miongoni mwa makanisa. Lakini hapo si mahali salama kwa wao kujidhihirisha. Ikiwa Mungu ameweka juu yao majukumu mbalimbali, basi si kwa ajili ya makanisa; kwa kuwa hayo ni ziada kwao. Kuna ulimwengu mbele ya Kaka na Dada K, ulimwengu unaolala katika uovu. Uwanja wao ni mkubwa/mpana. Wana nafasi nyingi ya kujaribu karama zao na kujaribu wito wao bila kuingia katika kazi za watu wengine

na kujenga msingi ambao wao hawakuuweka. Ndugu Kaka na Dada K wamekuwa wazito sana kupata uzoefu wa kujikana nafsi. Wamekuwa wazito katika kupokea na kutenda matengenezo ya afya zao katika Nyanja zake zote. Makanisa yako mbele yao zaidi katika swala la matengenezo juu ya vyakula. Hivyo hawatakuwa na faida sana kwa makanisa katika mwelekeo huu, lakini badala yake watakuwa kizuizi. 3T 57.5

Ndugu K hajawa baraka kwa kanisa lililoko -----, bali amekuwa mzigo mkubwa. Amesimama moja kwa moja katikati njia ya maendeleo yao. Hakuweza kuwa msaada pindi na mahali watu walipohitaji msaada zaidi. Hakuiwakilisha Imani yetu vyema; mazungumzo na maisha yake hayakuwa yenye utakatifu. Amekuwa nyuma sana, na hakuwa tayari kutambua na kuwa tayari kufanya miongozo ya usimamizi wa Mungu. Amesimama katika njia ya wakosaji; hajawa katika hali ambayo ushawishi wake ungependekeza imani yetu kwa wasioamini. 3T 58.1

Mfano wake umekuwa kizuizi kwa makanisa na kwa majirani zake wasioamini. Ikiwa Ndugu K angewekwa wakfu kabisa mbele za Mungu, kazi zake zingekuwa na matunda, na matokeo mengi ya mema yangedhihirika. Lakini kile ambacho hasa kinawatofautisha watu wa Mungu na mashirika ya kidini maarufu na yanayopendwa si taaluma zao pekee, bali tabia zao zenye kielelezo na kanuni zao za upendo usio na ubinafsi. Ushawishi wenye nguvu, unaotakasa wa Roho wa Mungu juu ya moyo, unaofanywa kwa maneno na matendo, huwatenganisha na ulimwengu na kuwataja kama watu wa pekee wa Mungu. Tabia na mwenendo wa wafuasi wa Kristo utakuwa kama wa Bwana wao. Yeye Ndiye kielelezo, ambacho ni kitakatifu na kikamilifu ambacho Wakristo wanapaswa kufuata. Wafuasi wa Kristo wa kweli watawapenda ndugu zao na kupatana nao. Watawapenda jirani zao kama vile Kristo alivyowapa kielelezo na watatoa dhabihu yoyote ikiwa wataweza na kwa kufanya hivyo kuzishawishi nafsi ziache dhambi zao na kuongoka kwenye ile Kweli. 3T 58.2

Ukweli, uliokita mizizi ndani ya mioyo ya waumini, utachipuka na kuzaa matunda ya uadilifu. Maneno na kazi zao ndizo njia ambazo kanuni safi za Ukweli na utakatifu hupitishwa kwa ulimwengu. Baraka za pekee na fursa ni kwa wale wanaopenda Kweli na kutembea kulingana na nuru ambayo wameipokea. Wakipuuza kufanya hivi, nuru yao itakuwa giza. Pindi watu wa Mungu wanapojiona kuwa hawamuhitaji Mungu, kwamba wamejitosheleza, Bwana huwaacha katika hekima yao wenyewe. Rehema na Ukweli zimeahidiwa kwa wanyenyekevu wa moyo, watiifu na waaminifu. 3T 59.1

Kaka K amesimama katika njia ya watoto wake. Ikiwa angewekwa wakfu kwa Mungu, akiwa na moyo wake katika kazi hiyo, na kuishi kwa kupatana na Ukweli aliodai, angehisi umuhimu wa kuiamuru nyumba yake baada yake, kama vile alivyotenda mtu wa Mungu ambaye ni mwaminifu Ibrahimu-Mwanzo 18. 3T 59.2

Ukosefu wa maelewano na upendo kati ya ndugu wawili K ni aibu katika kazi ya Mungu. Wote wawili wana makosa. Wote wawili wana kazi ya kufanya katika kujitiisha na kukuza neema za Kikristo. Mungu haheshimishwi kwa mifarakano, na sijakwenda mbali sana ninaposema chuki, iliyopo kati ya hawa ndugu wawili wa asili/kuzaliwa au wa damu. Ndugu A K ana makosa sana. Amethamini hisia ambazo hazijapatana na mapenzi ya Mungu. Anajua sura za kipekee za kaka yake, BK, kwamba ana tabia ya kufadhaika, kuudhika kirahisi, na isiyo na furaha. Mara kwa mara hawezi kuona mema hata kama yanadhihirishwa katika njia yake. Anaona uovu/ubaya tu na hukata tamaa kwa urahisi sana. Shetani anakuza kilima kidogo kuwa mlima mkubwa mbele yake. Unapozingatia mambo yote, Ndugu B K amefanya kazi ya kulaumiwa kwa kiwango kidogo kuliko ndugu yake, kwa sababu kazi yake imekuwa isiyo na madhara shambani mwa Bwana. 3T 59.3

Ndugu hawa wa damu/asili ni lazima wapatanishwe kikamilifu wao kwa wao kabla ya kuondoa lawama kutoka kwenye kazi ya Mungu ambayo mfarakano wao umesababisha. "Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao; Mtu asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake." "Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa." Wale wanaofanya kazi kwa ajili ya Mungu wanapaswa kuwa vyombo safi, vilivyotakaswa kwa matumizi ya Bwana. “Iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya BWANA. “Mtu akisema, nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona; Na amri hii tumepewa na Yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake pia.” 3T 59.4

Mabalozi wa Kristo wana kazi takatifu wanayopaswa yenye kuwajibisha sana. Ni ladha ya uzima iletayo uzima, au ya mauti iletayo mauti. Ushawishi wao unaamua hatima ya roho ambazo Kristo alizifia. Kaka na Dada K wote hawana uzoefu. Maisha yao hayajafikia utakatifu. Hawajapata ujuzi wa kina na kamili wa mapenzi ya Mungu. Bado hawajasonga mbele kwa uthabiti Kiroho kuelekea mbele na juu, ili kwamba uzoefu wao uweze kuwa wa thamani kwa kanisa. Mwenendo wao umelielemea kanisa kwa sehemu kubwa. 3T 60.1

Tabia za awali zilizodhihirishwa katika maisha ya awali ya Dada K hazikuwa na uzoefu ambao ungemfanya kuwa mbaraka kwa ajili ya wengine. Hajaishi kulingana kwa jinsi anavyosadiki katika Imani yake. Dhamiri yake imevunjwa mara nyingi sana. Amekuwa akitafuta na kufanya anasa kwa kiasi kikubwa na ametoa maisha yake kwa ajili ya ubatili, ufedhuli na mtindo mbalimbali ya kidunia, mbele ya nuru ya Ukweli ambayo imeangaza kwenye njia yake. Alijua njia, lakini alipuuza kutembea ndani yake. Bwana alimpa Dada K Shuhuda ya onyo na karipio. Aliamini na kuukubali ushuhuda na kujitenga na tabaka lile la watu waliokuwa wanapenda anasa kuliko kumpenda Mungu. Kisha, alipoyatazama maisha yake ya zamani, yaliyojaa sana kupuuzwa na makosa, alivunjika moyo, akacha kuamini na kuwa na huzuni nyingi. Kukata tamaa kulitandaza mbawa zake za giza juu yake. Ndoa yake

na Kaka K ilibadilisha mpangilio wa mambo kwa kiasi fulani, lakini toka hapo amekuwa na huzuni nyingi na kukata tamaa. 3Tsw 60.2

Dada K ana ufahamu mzuri wa unabii na anaweza kuufuatilia na kuzungumza juu yake kwa urahisi na utayari sana. Baadhi ya kaka na dada wamekuwa na shauku ya kuwahimiza Ndugu na Dada K watoke nje kama watenda kazi wenye bidii. Lakini kuna hatari ya kufanya kazi kwao kwa mtazamo mbaya. Faida za elimu za Dada K zimekuwa bora kuliko zile za wengi ambao amezungukwa nao. Kwa vile amefanya kazi hadharani, ametegemea nguvu zake mwenyewe zaidi kuliko Roho wa Mungu. Amekuwa na roho ya uhuru wa hali ya juu na amefikiri kwamba alistahili kufundisha badala ya kufundishwa. Kwa ukosefu wake wa uzoefu katika mambo ya kiroho, hayuko tayari kufanya kazi kati ya makanisa. Hana utambuzi na nguvu za kiroho zinazohitajika kuwajenga. Ikiwa yeye na mume wake wanashiriki katika kazi hii hata kwa namna ndogo kabisa, wanapaswa kuanza kwa kutoa ushawishi mzuri ndani ya kanisa lililopo -----. Kazi yao inapaswa kutolewa mahali ambapo kazi inahitaji kufanywa zaidi. 3T 60.3

Kuna kazi ya kufanywa katika maeneo mapya. Wenye dhambi ambao hawajasikia kamwe ujumbe wa onyo wanahitaji kuonywa. Hapa Kaka na Dada K wana nafasi ya kutosha ya kufanya kazi na kuthibitisha wito wao. Hakuna mtu anayepaswa kuwazuia katika juhudi zao ndani ya maeneo haya mapya. Kuna wenye dhambi wa kuokoa kila upande. Lakini wachungaji/wahudumu wengine wana mwelekeo wa kwenda tena na tena katika eneo lile lile kati ya makanisa, wakati kazi zao haziwezi kuwasaidia, na wakati wao unapotezwa. 3T 61.1

Tunatamani kwamba watumishi wote wa Bwana wangekuwa watenda kazi. Kazi ya kuonya roho haipaswi kufungwa kwa wachungaji/wahudumu peke yao, bali ndugu walio na ile Kweli mioyoni mwao, na ambao wamekuwa na ushawishi mzuri majumbani kwao, wanapaswa kutambua kuwa wanalo jukumu la kutenga muda wao na kwenda kuhudumu mbele za majirani wao na katika miji ya jirani ili kuwa wamishonari wa Mungu. Wanapaswa kubeba machapisho yetu na kushiriki katika mazungumzo na, katika roho ya Kristo, kusali pamoja na wale wanaowatembelea na kuwaombea. Hii ndiyo kazi itakayoamsha roho ya ari ya uchunguzi na matengenezo. 3T 61.2

Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akiwaita watu kufanya matengenezo ya afya zao. Hili ni moja ya tawi kuu ya kazi kwa ajili ya maandalizi ya ujio wa Mwana wa Adamu. Yohana Mbatizaji alifanya kazi akiwa na roho na nguvu za Eliya ili kuitayarisha njia ya Bwana na kuwageuza watu kwenye hekima ya wenye haki. Alikuwa mwakilishi wa wale wanaoishi katika siku hizi za mwisho ambao Mungu amewakabidhi Kweli takatifu, ili waziwasilishe mbele ya watu ili kuandaa njia kwa ajili ya ujio wa mara ya pili wa Kristo. Yohana alikuwa mwanamatengenezo. Malaika Gabrieli, moja kwa moja kutoka mbinguni, alitoa hotuba juu ya matengenezo ya afya kwa baba na mama wa Yohana. Alisema kwamba hapaswi

kunywa divai au kileo, na ili kwamba mtoto ajazwe na Roho Mtakatifu tangu kuzaliwa kwake. 3T 61.3

Yohana alijitenga na marafiki na lakshari/anasa za maisha. Usahili wa vazi lake, vazi lililofumwa kwa singa za ngamia, lilikuwa kemeo la kudumu kwa ubadhirifu na maonesho ya makuhani wa Kiyahudi, na ya watu kwa ujumla. Lishe yake, ilikuwa ni mboga-mboga tu (vegetables), nzige na asali ya mwituni, ilikuwa ni kemeo la tamaa ya kula na ulafi uliokuwa umeenea kila mahali. Nabii Malaki anasema hivi: “Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA, iliyo kuu na kuogofya; Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.” Hapa nabii anaelezea tabia ya kazi ya Bwana. Kuwa wale wanaopaswa kutayarisha njia kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo wanawakilishwa na Eliya mwaminifu, kama vile Yohana alivyokuja katika roho ya Eliya ili kuandaa njia kwa ajili ya ujio wa kwanza wa Kristo. Somo kuu juu ya matengenezo linapaswa kuchochewa, na mawazo ya hovyo yanapaswa kuondolewa. Ujumbe wa kiasi katika mambo yote unapaswa kujumuishwa ndani ya ujumbe, ili kuwageuza watu wa Mungu kutoka kwenye ibada yao ya sanamu, ulafi wao, tamaa na ubadhirifu wao wa mavazi na mambo mengine. 3T 62.1

Kujikana nafsi, unyenyekevu, na kiasi kinachohitajika kwa wenye haki, ambaye hasa Mungu huwaongoza na kuwabariki, kinapaswa kuwasilishwa kwa watu tofauti na tabia mbaya kupita kiasi, zinazoharibu afya za wale wanaoishi katika kizazi hiki chenye maadili ya mabaya/Uovu. Mungu amedhihirisha kwamba matengenezo juu ya afya yanahusiana kwa ukaribu na ujumbe wa malaika wa tatu kama vile mkono unavyohusiana na mwili. Hakuna mahali popote panapopatikana sababu kubwa ya kuzorota kimwili na kimaadili kama kupuuzwa kwa mada hii muhimu. Wale wanaojiingiza katika kuendekeza tamaa za ulaji na shauku mbaya, na kufumba macho yao juu ya nuru kwa kuhofu kuwa wataziona dhambi zao kwa uwazi huku hawako tayari kuziacha, wana hatia mbele za Mungu. Yeyote anayegeuka kutoka kwenye nuru kwa mfano mmoja huufanya moyo wake kuwa mgumu kutojali nuru juu ya mambo mengine. Yeyote anayekiuka wajibu wa kimaadili katika suala la kula na kuvaa hutayarisha njia ya kukiuka madai ya Mungu kuhusiana na maslahi ya milele. Miili yetu si yetu wenyewe. Mungu ana madai juu yetu ya kutunza makao Yake aliyotupa. Yeye Ametupa sisi ili tutoe miili yetu kwake iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kupendeza mbele Zake. Miili yetu ni ya Yeye Aliyeiumba, nasi tumefungwa katika wajibu wa kuwa na akili kuhusiana na njia bora ya kuihifadhi kutokana na kuharibika. Tukidhoofisha mwili kwa ajili ya anasa zetu wenyewe, na kwa kuendekeza uroho/ulafi, na kwa kuvaa kulingana na mitindo inayoharibu afya, ili kuendana na ulimwengu, tunakuwa maadui wa Mungu. 3T 62.2

Kaka na Dada K hawathamini nuru ipatikanayo katika matengenezo juu ya afya. Hawaoni muunganiko wake na nafasi yake kuhusiana na ujumbe wa malaika watatu. Uongozi wa Mungu au Majaliwa Yake, yamekuwa yakiwaongoza watu wa Mungu kutoka kwenye mazoea ya tabia mbaya za ulimwengu, mbali na kuendekeza

ulafi na tamaa, na kuweza kuwa na msimamo juu ya kujikana na kuwa na kiasi juu ya mambo yote. Watu ambao Mungu anawaongoza watakuwa wa kipekee. Hawatakuwa kama walimwengu. Lakini wakifuata miongozo ya Mungu watatimiza makusudi Yake, na watayatoa mapenzi yao ili kuongozwa na mapenzi Yake. Kristo atakaa moyoni. Hekalu la Mungu litakuwa takatifu. Mwili wako, asema mtume, ni hekalu la Roho Mtakatifu. Mungu hataki watoto Wake wajinyime/wajikane wenyewe ili waweze kuumia kutokana na nguvu za kimwili na nguvu zao. Anawahitaji kutii sheria ya asili, kuhifadhi afya ya kimwili. Njia ya asili ni njia Anayoiweka, na ni pana ya kutosha kwa Mkristo yeyote. Mwenyezi Mungu, kwa mkono wa kifahari na uliojaa ukarimu, Bwana ametujalia fadhila nyingi na mbalimbali kwa ajili ya riziki zetu na starehe. Lakini ili tufurahie hamu ya asili, ambayo itahifadhi afya na kuongeza muda wa maisha, Yeye huzuia/huratibu tamaa ya chakula. Anasema: Jihadharini; jizuieni, jinyimeni, kataeni, tamaa isiyo ya asili. Ikiwa tunajenga tamaa mbovu, tunakiuka sheria za utu wetu na kuchukua jukumu la kuitendea miili yetu ubaya na kujiletea magonjwa wenyewe. 3T 63.1

Roho na nguvu za Eliya zimekuwa zikichochea mioyo ya watu kufanya matengenezo na kuwaelekeza kwenye hekima ya wenye haki. Kaka na Dada K hawajaongoka kwenye matengenezo juu ya afya, ijapokuwa wamepokea ushahidi mwingi ambao Mungu ametoa juu ya somo hilo. Kujinyima au kujikana nafsi ni muhimu kwa dini ya Kweli. Wale ambao hawajajifunza kujikana wenyewe wamepungukiwa na utauwa wa maana na wa vitendo. Hatuwezi kutarajia kitu kingine chochote isipokuwa kwamba madai ya dini yatakutana na mapenzi ya asili na maslahi ya kidunia. Kuna kazi kwa kila mtu katika shamba la mizabibu la Bwana. Hakuna anayepaswa kuwa mvivu au mtu anayeishi bila kazi. Malaika wa Mungu wote wamechochewa, wakipanda mbinguni na kushuka duniani tena na ujumbe wa rehema na onyo. Wajumbe hawa wa mbinguni wanasonga juu ya akili na mioyo. Kuna wanaume na wanawake kila mahali, ambao mioyo yao inaweza kuvuviwa na Ukweli. Ikiwa wale walio na ujuzi wa Ukweli sasa wangefanya kazi pamoja na Roho wa Mungu, tungeona kazi kubwa ikikamilika. 3T 64.1

Maeneo mapya yamefunguliwa ambamo wote wanaweza kupima wito wao kwa juhudi za majaribio katika kuzitoa roho kutoka kwenye giza na makosa mbalimbali, na kuziweka juu ya jukwaa la Ukweli wa milele. Ikiwa Kaka na Dada K wanahisi kwamba Mungu amewaita kushiriki katika kazi Yake, wanayo ya kutosha kufanya ili kuwaita na kuwahubiri wenye dhambi ili waweze kufikiria toba; lakini ili Mungu afanye kazi ndani na kupitia kwao, wanahitaji uongofu kamili. Kazi ya kuwapa watu stahiki katika siku hizi za mwisho kwa ajili ya ujio wa Kristo, ni kazi takatifu zaidi, ya taadhima, na inawataka watenda kazi waliojitolea, wasio na ubinafsi. Wale walio na unyenyekevu, imani, nguvu, ustahimilivu, na uamuzi watapata mengi ya kufanya katika shamba la mizabibu la Bwana wao. Kuna majukumu yanayopaswa kufanywa, ambayo yanahitaji unyofu na bidii na nguvu zao zote. Ni

jambo la kutumika kwa hiari ambako Mungu anakukubali. Ikiwa Ukweli tunaokiri ni wa umuhimu usio na kikomo ambao unaamua hatima ya roho zetu, ni kwa kiasi gani basi, tunapaswa kuwa waangalifu katika uwasilishaji wake. 3T 64.2

“Njia ya wenye haki ni kama nuru ing’aayo, ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu.” Kaka na Dada K, kama mngetembea katika nuru ilipoangaza kwenye njia zenu, kama mngekuwa mnamkaribia Mungu zaidi, mkiamini Kweli kwa uthabiti na kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu katika nuru aliyotoa, sasa mngekuwa na uzoefu ambao ungekuwa na thamani isiyo na kifani. Ikiwa ungeboresha talanta ulizokopeshwa na Mungu, ungeangaza kama nuru ulimwenguni. Lakini nuru inakuwa giza kwa wale wote ambao hawatakwenda ndani yake. Ili tukubaliwe na kubarikiwa na Mungu kama baba zetu walivyokuwa, ni lazima, kama wao, tuwe waaminifu. Ni lazima tuboreshe/tuimarishe nuru yetu jinsi manabii wa kale, waaminifu walivyoboresha zao. Mungu anatuhitaji tutende kulingana na neema ambayo ametupa, na hatakubali pungufu ya vile anavyodai. Matakwa Yake yote ya haki lazima yatimizwe kikamilifu. Ili sisi tutekeleze wajibu wetu, ni lazima tusimame kwenye uwanja huo ulioinuka ambao utaratibu na maendeleo ya Kweli takatifu imetutayarishia. 3T 64.3

Ndugu L anashindwa kutambua nguvu ya Kweli ya utakaso inayopatikana toka kwa Mungu. Yeye si mvumilivu, mnyenyekevu, na mstahimilivu kama jinsi anavyopaswa kuwa. Anachochewa kwa urahisi; nafsi hujitokeza, na husema na kufanya mambo mengi bila kutafakari ipasavyo. Yeye hana wakati wote ushawishi wa kuokoa. Ikiwa angejazwa Roho wa Kristo, angeweza kwa mkono mmoja kumshika Mwenyezi Mungu, na mkongomwingine wa imani na upendo angemfikia maskini mwenye dhambi. Ndugu L anahitaji ushawishi wenye nguvu wa upendo wa Mungu; kwani hili litamuumba upya na kuusafisha moyo, na kutakasa maisha, na kumwinua na kumtukuza maisha yake yote. Ndipo maneno na matendo yake yatakuwa ladha na harufu ya mbinguni kuliko juu ya roho yake mwenyewe. 3T 65.1

Maneno ya uzima wa milele yakipandwa moyoni, matunda yatazaa kwa haki na amani. Roho ya kujitosheleza na kujiona kuwa muhimu ni lazima uishinde ndugu yangu mpendwa. Unapaswa kusitawisha roho ambayo iko tayari kufundishwa na kushauriwa. Chochote ambacho wengine wanaweza kusema au kufanya, unapaswa kusema: Hilo ni nini kwangu? Kristo ameniamuru mimi nimfuate.
Wewe unapaswa kusitawisha roho ya upole. Unahitaji uzoefu katika utauwa wa Kweli, na usipokuwa na haya, huwezi kushiriki katika kazi ya Mungu kwa ufahamu. Roho yako inapaswa kulainika na kutiishwa kwa kuletwa katika kutii mapenzi ya Kristo. Unapaswa wakati wote kudumisha hadhi ya unyenyekevu ya mfuasi wa Yesu. Mwenendo wetu, maneno na matendo yetu, huwahubiria wengine. Sisi ni nyaraka zilizo hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. 3T 65.2

Unapaswa kuwa mwangalifu usihubiri Ukweli kutoka kwenye ugomvi au mafarakano, kwani ukifanya hivyo bila shaka utageuza vita dhidi yako mwenyewe

na kujikuta ukiendeleza kazi ya adui kuliko ile Kweli ya Mungu. Kila wakati unaposhiriki katika shindano inapaswa kutoka kwenye hisia ya wajibu. Ukimfanya Mungu kuwa nguvu yako na kujitiisha, na kuiacha Kweli ilete ushindi, hila za Shetani na mishale yake yenye moto itaanguka juu yake mwenyewe, na utaimarishwa, utaepushwa na upotovu, na kulindwa na kila njia ya udanganyifu. Unahitaji kujifunza kuwa na tahadhari na si kukimbilia nguvu zako mwenyewe. Kazi ni muhimu na takatifu, na unahitaji hekima kubwa. Unapaswa kushauriana na ndugu zako ambao wamekuwa na uzoefu katika kazi. Lakini, zaidi ya yote, unapaswa kupata ujuzi kamili wa udhaifu wako mwenyewe na hatari, na unapaswa kuimarisha sehemu dhaifu katika tabia yako, ili usipoteze imani yako-usivunje imani. 3T 66.1

Tunaishi katikati ya hatari ya siku za mwisho, na ikiwa tuna roho ya kujitosheleza na kujitegemea tutaaanikwa kwenye hila za Shetani na kushindwa. Kujiona kuwa u-bora kuliko wengine ni tabia inayopaswa kuondolewa kwako, na ufichwe ndani ya mbawa za Mungu, ukimtegemea Yeye pekee Yake kwa ajili ya kukupatia nguvu. Makanisa hayahitaji kazi yako. Ikiwa umejiweka wakfu kwa Mungu, unaweza kufanya kazi katika nyanja mpya, na Mungu atafanya kazi pamoja nawe. Usafi wa moyo na wa maisha Mungu ataukubali. Chochote pungufu ya haya Yeye hatakizingatia. Ni lazima tuteseke pamoja na Kristo ikiwa tunataka kutawala pamoja Naye. 3T 66.2

Ndugu M angeweza kutimiza mema kama angaliweza, miaka mingi iliyopita, kutoa yote kwa ajili ya Kristo. Hajatakaswa kwa ile Kweli; moyo wake haujawa sawa/sahihi na Mungu. Ameficha talanta zake ardhini. Je, yeye ambaye ametumia talanta zake vibaya atasema nini wakati Bwana atakapomtaka atoe hesabu ya uwakili wake? Ndugu M hajaleta heshima kwa kazi ya Mungu. Ni hatari kushindana na majaliwa ya Mungu na kutoridhika karibu na kila kitu, kana kwamba kumekuwa na mpangilio maalum wa mazingira ili kujaribu na kuharibu. Kazi ya kupogoa na kutakasa ili kufaa kwa ajili ya mbingu ni kazi kubwa na itatugharimu mateso na majaribu mengi, kwa sababu nia zetu hazijatiishwa chini ya mapenzi ya Kristo. Ni lazima tupitie kwenye tanuru hadi moto uteketeze takataka na tusafishwe na kuakisi sura ya Mungu. Wale wanaofuata mielekeo yao na kutawaliwa na muonekano si majaji/waamuzi wazuri kwa kile Mungu anachofanya. Wamejawa na kutoridhika. Wanaona kushindwa pale palipo na ushindi, hasara kubwa palipo na faida; na, kama Yakobo, wako tayari kusema, “Mambo haya yote yako dhidi yangu,” wakati mambo yale yale wanayolalamika yanafanya kazi pamoja kwa manufaa yao. 3T 66.3

Hakuna msalaba, hakuna taji. Mtu anawezaje kuwa na nguvu katika Bwana bila majaribu? Ili kuwa na nguvu lazima tuwe na mazoezi juu ya kuimarisha nguvu zetu. Ili kuwa na imani yenye nguvu, ni lazima tuwekwe katika hali ambazo imani yetu itafanyiwa kazi na kuzoeshwa. Mtume Paulo, kabla tu ya kuuawa kwake, alimsihi

Timotheo hivi: “Uwe mshiriki wa mateso ya Injili kwa kadiri ya nguvu ya Mungu.” Ni kupitia dhiki nyingi ndipo tunapaswa kuingia katika ufalme wa Mungu. Mwokozi wetu alijaribiwa kwa kila njia inayowezekana kujaribiwa, na bado Alishinda katika Mungu daima. Ni fursa yetu kuwa hodari katika nguvu za Mungu chini ya hali zote na kujivunia msalaba wa Kristo. 3T 67.1

SURA YA 6

UZOEFU SI WAKUTEGEMEWA

Mpendwa Dada N,

Katika maono niliyopewa Desemba 10, 1871, naliona ya kwamba baadhi ya mambo yamekuwa ndio vizuizi vikubwa katika uponaji wako. Sifa zako za pekee zimekuzuia kupokea mema ambayo ungepaswa kuyapokea, na kuboresha afya yako kadri ulivyopaswa kuimarika. Una desturi zako maalum ambazo nawe haukubali kuziacha. Una maoni yako, ambayo huyatekeleza, na mara nyingi hayapatani na sheria za asili (physical laws), lakini ni maamuzi binafsi. 3T 67.2

Una akili na nia isiyopindishwa na zenye kudhamiria, hivyo unadhani ya kuwa unaelewa mambo yako vizuri zaidi kuliko wengine wanavyoelewa, kwa sababu unafuata hisia zako. Unaongozwa na hisia zako na unatawaliwa na uzoefu. Umejaribu mipango mingi ili kujiridhisha, na umeamua kuufuata uamuzi wako ndiyo bora. Lakini kipimo chako ni nini? Jibu: Hisia zako. Sasa, dada yangu, hisia zako zina uhusiano gani na Ukweli halisi katika jambo hili? Hakina ni kwa kiasi kidogo sana. Hisia ni kigezo duni, hasa zinapokuwa chini ya udhibiti wa mawazo yenye nguvu na nia thabiti. Una akili iliyodhamiria, na mwelekeo wako umeshauchorea ramani mbele yako, lakini huyatazami mambo yako kwa mtazamo sahihi. Maamuzi yako siyo salama kutumainiwa kuhusiana na kesi yako mwenyewe. 3T 68.1

Nilioneshwa kwamba umefanya maboresho (au umepata afueni), lakini sio sana, kwa haraka, au kwa kina, kama uwezavyo, kwa sababu haumhusishi mtu yeyote

katika mambo yako (unachukua maamuzi yote mikononi mwako). Kwa sababu hii, wapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wako kuongozwa na mashauri ya watu wenye uzoefu zaidi, nilitamani uje kwenye Taasisi ya Afya. Madaktari wa Taasisi ya Afya wanauelewa ugonjwa huu, sababu zake na matibabu sahihi, zaidi ya vile unavyoweza kufikiri; na ikiwa utayaweka kando mawazo uliyonayo kwa hiari, na kufuata mashauri yao, kuna tumaini la kupona. Lakini ukikataa kufanya hivi, sioni tumaini lolote la wewe kupona bila kupata matibabu sahihi. 3T 68.2

Kama nilivyoeleza hapo awali, wewe, dada yangu, unategemea uzoefu. Uzoefu wako unafanya uamue kufuata uelekeo fulani. Lakini yale ambayo wengi huyapitia si uzoefu hata kidogo; ni mazoea, kuendekeza anasa tu kw upofu na ,mara kwa mara ni kufuata ujinga, kwa azimio thabiti, lililowekwa, bila utashi au akili au uchunguzi unaohusiana na sheria zinazofanya kazi katika utimilifu wa matokeo. 3T 68.3

Uzoefu halisi ni aina mbalimbali ya majaribio makini yanayofanywa na akili iliyoondokana na ubaguzi na isiyodhibitiwa na maoni na mazoea yaliyoanzishwa hapo awali. Matokeo hutiwa alama kwa uangalifu na hamu ya kutaka kujifunza, kuboresha, na kurekebisha kila tabia ambayo haipatani na sheria za kimaumbile na kimaadili. Mawazo ya wengine kupinga kile ambacho umejifunza kutokana na uzoefu yanaonekana kwako kuwa upumbavu na hata ukatili. Lakini kuna makosa mengi yaliyopokelewa na kubakizwa kutoka katika mawazo potofu ya uzoefu kuliko vyanzo vingine vyovyote, kwa sababu hiyo kile kinachoitwa uzoefu kwa ujumla si uzoefu hata kidogo; kwa sababu kamwe hakuna jaribio la haki lililo halisi na lenye uchunguzi wa kina, linalohusisha ujuzi wa kanuni iliyohusika katika jaribio. 3T 69.1

Uzoefu wako ulioneshwa kwangu kuwa si wa kutegemeka, kwa sababu ni kinyume cha sheria ya asili. Unakinzana na kanuni zisizobadilika za asili. Dada yangu mpendwa, ushirikina hutokana na fikra potofu, ambao hupelekea migongano na sayansi pamoja na kanuni. Kipi kitelekezwe basi? Ubaguzi wako mkubwa na mawazo yaliyojikita sana katika kutafuta njia bora ya kuifuata kwa muda mrefu yamekutoa katika njia njema. Nimeielewa kesi yako kwa miaka mingi, lakini nimejihisi ya kuwa sitoweza kuliwasilisha jambo hilo kwa njia iliyo wazi na bora zaidi ambayo ungeweza kuiona na kuielewa, na kutumia kwa vitendo nuru uliyopewa. 3T 69.2

Wapo wengi vilema/wasiojiweza leo ambao watabaki hivyo kwa sababu hawataki kusadiki ya kwamba uzoefu wao sio wa kutegemeka. Ubongo ni mtaji wa mwili, makao ya nguvu zote za neva na matendo ya akili. Mishipa inayotoka kwenye ubongo inaenda mwilini. Kupitia mishipa ya ubongo, hisia za kiakili hupitishwa kwa neva zote za mwili kama waya za mawasiliano/telegrafu; na hudhibiti hatua

muhimu ya kila sehemu ya mfumo. Viungo vyote vinavyojongea hutawaliwa na mawasiliano yanayopokelewa kutoka kwenye ubongo. 3T 69.3

Ikiwa akili yako imevutiwa na imeaminishwa kwamba kuoga kutakudhuru, hisia ya akili huwasilishwa kwa mishipa yote ya mwili. Mishipa hudhibiti mzunguko wa damu; kwa hiyo damu, kwa kupitia fikra za akili, imejifungamanisha kwenye mishipa ya damu, na athari nzuri za kuoga hupotea. Yote haya ni kwa sababu damu huzuiliwa na akili kuzunguka kwa hiari kuelekea juu ili kuchochea, kuamsha, na kukuza mzunguko. Kwa mfano, kama unahisi ya kwamba ukioga mwili utapata baridi. Ubongo hutuma taarifa hii kwa mishipa ya damu, na mishipa ya damu, inayofanya kazi kwa kutii mapenzi yako, haiwezi kufanya kazi yake na kusababisha athari baada ya kuoga. Hakuna sababu katika sayansi au falsafa ya kwa nini kuoga mara kwa mara, kulikofanywa kwa uangalifu mkubwa, kufanye jambo lolote jingine, isipokuwa manufaa mazuri. Hili ndilo tendo linalohusisha zoezi dogo zaidi la kuifanya misuli izidi kufanya kazi na kusaidia mzunguko wa damu kupitia mfumo wake. Kuoga huiweka ngozi huru na mkusanyiko wa uchafu ambao hukusanywa mara kwa mara, na kuifanya ngozi kuwa ya unyevunyevu/moist na kunawiri/nyororo, na hivyo kuongeza na kusawazisha mzunguko wa damu. 3T 69.4

Watu wenye afya njema hawapaswi kupuuza kuoga. Wanapaswa kwa vyovyote kuoga mara nyingi zaidi ya mara mbili kwa wiki [Kwa hali ya maisha, na maji yaliyopo nk, mtu aoge kila siku] . Wale ambao hawana afya wana mchafuko wa damu, na ngozi zao hazina afya njema. Wingi wa vinyweleo, au matundu madogo, ambayo huuwezesha mwili kupumua huziba na kujaa uchafu. Ngozi inahitaji kusafishwa kwa uangalifu na kwa kina, ili vinyweleo vifanye kazi yake ya kutoa taka-mwili; kwa hiyo watu dhaifu ambao ni wagonjwa kwa hakika wanahitaji faida na baraka za kuoga mara nyingi zaidi ya mara mbili kwa wiki, na ni muhimu kuoga hata mara nyingi zaidi. Ikiwa mtu ni mgonjwa au mzima, atapumua kwa urahisi zaidi ikiwa ataoga. Kwa kufanya hivyo misuli huwa huru zaidi kunyumbulika, akili na mwili hutiwa nguvu, kisha akili itafanywa kuwa angavu, na kila kiungo kinakuwa hai. Kuoga hupoozesha/hutuliza mishipa. Husaidia kutoa jasho mwilini, huharakisha mzunguko wa damu, huzuia kuziba/vikwazo katika mfumo, na husaidia figo pamoja na mfumo wa mkojo. Kuoga husaidia tumbo, na ini, kwa kuvipatia nguvu na maisha mapya. Pia husaidia mmeng'enyo wa chakula, na badala ya mfumo kuwa dhaifu huimarishwa. Badala ya kuongeza uwezekano wa kuhisi baridi, uogaji mzuri, hukinzana na baridi kwa sababu mzunguko wa damu na viungo vya mfumo wa mkojo hurahisishwa; kwa kuwa damu husambaa kuelekea juu ya ngozi, kwa mtiririko rahisi zaidi na wa kawaida wa damu kupitia mishipa yote ya damu hupatikana. 3T 70.1

Uzoefu husemwa kuwa ndiyo mwalimu bora. Uzoefu wa kweli ni bora kuliko ujuzi wa kitabu. Lakini mazoea na desturi huwafunga wanaume na wanawake kama kwa

mikanda ya chuma, na kwa ujumla wao huhesabiwa haki kutokana na uzoefu, kulingana na uelewa wa kawaida wa neno hilo. Wengi sana wametumia vibaya uzoefu wenye thamani. Wameshikilia mazoea yao yenye kudhuru, ambayo kwa hakika yanaathiri afya ya kimwili, akili, na maadili; na unapotaka kuwaelekeza, wanaidhinisha njia yao kwa kurejelea uzoefu wao. Lakini uzoefu wa kweli huenda sambamba na sheria za asili pamoja na sayansi. 3T 71.1

Hapa ndipo tumekutana na matatizo makubwa sana katika masuala ya kidini. Mambo yaliyo wazi zaidi yanaweza kuwasilishwa, Kweli zilizo wazi zaidi, zinazoidhinishwa na Neno la Mungu, zinaweza kuletwa akilini; lakini sikio na moyo vimefungwa, na hoja yenye kusadikisha kwao ambayo ni : “uzoefu wangu mimi…..” Wengine watasema: “Bwana amenibariki katika kuamini na kufanya kama nilivyofanya; kwa hiyo siwezi kuwa nimekosea.”. Maneno "Uzoefu wangu" yameng'ang'aniwa,ila Kweli zinazoinua zaidi, zinazotakasa za Biblia zinakataliwa kwa kile wanachofurahia ili kuendana na uzoefu. Tabia nyingi za kutisha zaidi hufichwa chini ya kivuli cha uzoefu. Wengi wanashindwa kufikia uboreshaji huo wa kimwili, kiakili, na kimaadili ambao ni fursa na wajibu wao kuupata, kwa sababu hupigania na kuutegemea usalama wa uzoefu wao, ingawa uzoefu huo wa ulioamuliwa kwa kupotoshwa unapingana na Ukweli ulio wazi kabisa. Wanaume na wanawake ambao tabia zao mbaya zimeharibu katiba na afya zao watapatikana wakipendekeza uzoefu wao kama njia salama kwa wengine kufuata, wakati ni uzoefu huu huu ambao umewanyima nguvu na afya. Mifano mingi inaweza kutolewa ili kuonesha jinsi wanaume na wanawake wamedanganywa kwa kutegemea uzoefu wao. 3T 71.2

Bwana alimuumba mwanadamu akiwa mkamilifu tangu mwanzo. Aliumbwa akiwa na akili iliyo timamu na yenye msawaziko mzuri, ukubwa na nguvu za viungo vyake vyote vikiwa vimekuzwa kwa ukamilifu. Adamu alikuwa mwanamume mkamilifu. Ubora wa akili ulipangwa vyema kwa uwiano, kila kiungo kikiwa na kazi tofauti, na vyote vikitegemeana kwa matumizi kamili yanayofaa. Adamu na Hawa waliruhusiwa kula kutoka kwenye miti yote katika bustani, isipokuwa matunda yaliyo katika mti mmoja tu. Bwana akawaambia wawili hao-jozi: Siku mtakayokula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya, hakika mtakufa. Hawa alidanganywa na nyoka kuamini kwamba Mungu asingefanya kama alivyosema. “Hakika hamtakufa,” nyoka akasema. Hawa alikula na kuhisi kana kwamba amepata hisia za maisha mapya na ya kutukuzwa/kuinuliwa zaidi. Alimpelekea mumewe tunda, na jambo lililomshawishi Adamu kwa kiwango cha juu lilikuwa ni uzoefu wake Hawa. Nyoka alisema kwamba hatakufa, na hakuhisi madhara yoyote kutokana na lile tunda, hakuna kitu ambacho kingefasiriwa kuwa kifo, lakini, kama vile nyoka alivyosema, hisia ya kupendeza aliyoipata ilikuwa kama ya malaika. Uzoefu wake ukajipanga kichwani mwake kinyume cha amri chanya/thabiti ya Yehova na Adamu alikubali kushawishiwa na uzoefu wa mke wake. Ndivyo ilivyo

kwa ulimwengu wa kiroho/kidini kwa ujumla. Amri za Mungu zilizo wazi hukiukwa, na kwa sababu “hukumu ya uovu haifanyiki papo hapo, kwa hiyo mioyo ya wanadamu imeshamiri katika kutenda maovu.” 3T 72.1

Katika uso wa amri bora za Mungu, wanaume na wanawake hufuata muelekeo wao wenyewe kisha hudiriki kuliombea jambo hilo, ili Mungu akubali kuwaruhusu kwenda kinyume na mapenzi Yake dhahiri. Bwana hapendezwi na maombi ya aina hiyo. Shetani huja upande wa watu kama hao, kama vile alivyofanya kwa Hawa pale Edeni kwa kuziguza na kuzivutia akili zao, jambo hili hufanyika mara kwa mara akilini mwao na hatimaye huzoea, kisha huyasimulia kama shuhuda za ajabu ambazo Bwana amewapa. Uzoefu wa Kweli upo katika upatanifu kamili na sheria ya asili Mungu. Uzoefu wa uwongo huipinga sayansi na kanuni za Yehova. Ulimwengu wa kidini umefunikwa na giza totoro la maadili. Ushirikina na ushabiki/ushupavu hutawala akili za wanaume na wanawake, na hupofusha uamuzi wao ili wasiweze kutambua wajibu wao kwa wanadamu wenzao na wajibu wao wa kutii mapenzi ya Mungu bila ya kuuliza maswali. 3T 72.2

Balaamu alimuuliza Mungu kama angeweza kuwalaani Israeli, kwa sababu kwa kufanya hivyo aliahidiwa zawadi kubwa. Na Mungu akamwambia, “Usiende; lakini alisukumwa/alihimizwa na wale wajumbe, na kushawishiwa sana. Balaamu alikuwa ameoneshwa mapenzi ya Bwana katika jambo hili, lakini alikuwa na hamu sana ya kupokea motisha/vivutio/zawadi na kwa sababu hii alidiriki/alijitosa kumwomba Mungu mara ya pili. Bwana alimruhusu Balaamu kwenda. Kisha akapata uzoefu mzuri ajabu, lakini ni nani angetamani kuongozwa na jambo kama hilo? Kuna wale ambao huelewa wajibu wao kwa urahisi kabisa kama tu wajibu huo ungelikubaliana na mwelekeo wao wa asili au mapenzi yao. Hali ya mambo yanayotokea, mazingira na madhumuni huweza kuonesha wazi-wazi wajibu wao; lakini hali inapokuwa tofauti na mwelekeo wao wa asili, shuhuda hizi mara nyingi huwekwa kando. Ndipo watu hawa wanapowaza kumwendea Mungu ili kujifunza wajibu wao. Lakini Mungu hachezewi. Yeye Atawaruhusu watu kama hao kufuata matamanio ya mioyo yao wenyewe. Zaburi 81:11,12: “Lakini watu Wangu hawakuisikiliza sauti Yangu.” hivyo “Nikawaacha wakaenda kwa ukaidi wa mioyo yao, waenende katika mashauri yao.” 3T 73.1

Wale wanaotamani kufuata njia inayowapendeza mawazo yao ya kufikirika wako katika hatari ya kuachwa wafuate mielekeo yao, wakidhani kuwa ni uongozi ya Roho wa Mungu. Wajibu wa watu wengine unaoneshwa wazi kupitia mazingira na hali halisi na mambo kadha wa kadha yanayotokea; lakini, kwa kupitia ushawishi wa marafiki zao, na kukubaliana na mielekeo yao, wanauacha wajibu wao na kufuata mambo yao; kisha, kwa uangalifu mkubwa au dhamira kali, huomba kwa muda mrefu na kwa bidii kwa ajili ya nuru. Huwa na hisia za dhati katika jambo hilo, na wanafasiri hili kuwa ni Roho wa Mungu. Lakini wanadanganywa. Njia hii

ya kutenda, humhuzunisha Roho wa Mungu. Walikuwa na nuru na kwa sababu hiyo walipaswa kutambua fika wajibu wao; lakini vivutio vichache vyenye kuwashawishi, vinahamisha akili zao na kuzipeleka katika mwelekeo usio sahihi, kisha wanayamihiza mambo haya mbele za Bwana na kusisitiza hoja zao, Bwana huwaruhusu wafuate njia zao. Wana nia na mielekeo yenye nguvu katika kufuata njia zao, kiasi kwamba Mungu huruhusu wafanye hivyo ili wapate matokeo yake ambayo kwa kawaida huleta mateso. Watu hawa hufikiri kwamba wana uzoefu wa ajabu. 3T 73.2

Dada yangu mpendwa, uthabiti una nguvu kubwa ya kudhibiti ushawishi katika akili yako. Umejipatia nguvu ya kusimama na kupambana dhidi ya upinzani, na kuendesha shuguli ngumu za kutatanisha na kukanganya. Hupendi ugomvi. Wewe huchukulia mambo kwa njia nyeti sana na una mguso wa kina. Wewe u mwangalifu na mwenye dhamira kali sana, na maamuzi yako lazima yathibitishwe kabla ya kukubali maoni ya wengine. Endapo ungekuwa na afya njema, ungekuwa mwanamke bora na mwenye manufaa sana. Umekuwa mgonjwa kwa muda mrefu, na hii imeathiri mawazo yako na kuyafanya yawe ya kujifikiria nafsi, mawazo haya yameathiri mwili wako. Mazoea yako yamekuwa si nzuri katika mambo mengi. Chakula chako hakijaliwa kwa ugavi/wingi na ubora unaofaa. Unakula vyakula vingi na duni ambavyo haviwezi kumeng'enywa na kutengeneza damu nzuri katika mwili wako. Umelizoesha tumbo lako aina hii ya lishe. Uamuzi wako umekufundisha ya kuwa, njia hiyo ilikuwa bora zaidi, kwa sababu uliweza kukumbana na masumbufu au bughudha chache katika uamuzi huo. Lakini huo haukuwa uzoefu sahihi. Tumbo lako lilikuwa halipokei nguvu kutoka katika chakula ulichokula. Chakula chako kikiwekwa katika hali ya kimiminika hakitatoa nguvu ya kutosha na toni kwa mfumo wa mwili. Lakini unapobadilisha tabia hii, na kula zaidi vyakula vigumu zaidi na vimiminika kidogo, tumbo lako litahisi kusumbuliwa. Licha ya hili hupaswi kukata tamaa na kuachia mambo; bali unapaswa kulielimisha tumbo lako kubeba chakula kigumu zaidi. Unavaa nguo nyingi sana na kwa kufanya hivyo umeidhoofisha ngozi. Hajaupa mwili wako nafasi ya kupumua. Vinyweleo, au vitundu vidogo ambavyo huusaidia mwili kupumua, vinafungwa, na mfumo wa upumuaji unajaa uchafu. 3T 74.1

Tabia yako ya kutoka nje kwenye hewa safi na mwanga wa jua imekuwa na manufaa sana. Maisha yako ya kukaa nje yamekutegemeza kuwa mtu mwenye nguvu za kimwili kwa kiasi ambacho unazifurahia sasa. Lakini unapuuza mazoezi mengine ambayo ni muhimu zaidi kuliko haya. Unalitegemea gari lako sana, nawe, hulitumia mno, hata katika maeneo ya karibu zaidi. Unafikiri kwamba ukitembea umbali huo mdogo utaumia, na unajisikia kuchoka kufanya hivyo. Lakini katika hili uzoefu wako si wa kuaminika. 3T 75.1

Nguvu zile zile unazotumia kuingia na kutoka kwenye gari, na kupanda na kushuka ngazi, zingeweza pia kutumika katika kutembea na kutekeleza majukumu ya kawaida na ya lazima ya kila siku. Umekuwa mvivu sana katika kazi za nyumbani kana kwamba u mtu asiyejiweza. Hauhisi kuwa ni jukumu lako kutunza nguo za mume wako au kuandaa chakula chake. Sasa, dada yangu, kutokuweza kwako kupo zaidi katika mawazo yako kuliko uwezo halisi ulio nao. Unafikiri utachoshwa au kujipatia mzigo kama utafanya hayo; na ndivyo ilivyo. Lakini una nguvu ambayo ukiitumia kwa namna inayofaa kiuchumi ungetimiza mambo mengi mazuri na kukufanya uwe mwenye manufaa na mwenye furaha zaidi. Una hofu sana ya kuwa mnyonge hata usijiweze, kiasi kwamba
umeshindwa kutumia nguvu ambazo Bwana amekubariki. Katika mambo mengi umemsaidia mumeo, wakati huo huo ukiuelemea uvumilivu na mamlaka yake. Wakati akifikiri ya kwamba unaweza kubadili baadhi ya mazoea yako na kuwa bora au kupaa afueni, unadhani kuwa hakuelewi. Marafiki zako huhisi kuwa ungeweza kuwa mtu wa manufaa zaidi nyumbani kwako, yaani asiye mwenye kuhitaji msaada mara zote au asiyejiweza. Jambo hili hukuhuzunisha. Umedhani hawaelewi. Baadhi yao wameshinikiza maoni yao juu ya tabia yako pasipo kutumia busara, hili nalo, limekuhuzunisha. Umehisi ya kwamba Mungu, katika kujibu maombi, angekusaidia, na mara nyingi umesaidiwa kwa njia hii. Lakini bado hujapata nguvu za kimwili ambazo ni fursa yako kuzifurahia, kwa sababu hujatekeleza sehemu yako. Bado hujafanya kazi kwa ukamilifu na Roho wa Mungu. 3T 75.2

Bwana amekupa kazi ya kufanya ambayo Yeye hataki kuifanya kwa niaba yako. Unapaswa kuenenda kutokana na kanuni, na kujifungamanisha na sheria za asili, bila kujali hisia. Unapaswa kuanza kutenda kulingana na nuru ambayo Mungu amekupa. Huenda usiweze kufanya hivyo kwa wakati mmoja, lakini unaweza kufanya mengi kwa kutembea taratibu, hatua kwa hatua katika imani, ukiamini kwamba Mungu atakuwa Msaidizi wako, Naye atakutia nguvu. Unaweza kufanya mazoezi ya kutembea na kutekeleza majukumu rahisi ya kila siku, katika familia yako, na usiwe tegemezi sana kwa wengine. Kufahamu kwamba unaweza, kutakupa nguvu zaidi. Kama mikono yako ingetumika zaidi na ubongo wako utumiwe kwa udogo tu katika kuwapangia watu wengine, nguvu zako za kimwili na kiakili zingeongezeka. Ubongo wako sio mvivu, lakini hakuna kiungo kingine cha mwili kinachofanya kazi sambamba na ubongo. Mazoezi, ili yawe na manufaa kwako, yanapaswa kuratibiwa na kuletwa kwenye viungo vilivyodhoofika ili viweze kuimarishwa kwa matumizi. Tiba ya kutembea na kuviweka viungo katika mjongeo ina faida kubwa kwa kundi la wagonjwa ambao ni dhaifu sana kufanya mazoezi. Lakini wale walio wagonjwa wakitumaini tiba hii tu, na kuitegemea njia hii peke yake, wakati wanapuuzia kufanya mazoezi ya misuli, hufanya kosa kubwa. 3T 76.1

Maelfu ni wagonjwa na wanakufa miongoni mwetu, ambao wangeweza kupona na kupata afya na kuishi kwa hakika; lakini fikra zao zinawashikilia. Wanaogopa kwamba hali itakuwa mbaya zaidi ikiwa watafanya kazi au kufanya mazoezi, wakati haya ndiyo mabadiliko wanayohitaji ili wapone. Bila mazoezi haya hawawezi kamwe kupata nafuu. Wanapaswa kuzishugulisha nguvu za nia zao, na waweke kando maumivu na unyonge wao, kujihusisha na kazi yenye manufaa, na kusahau maumivu yao ya mgongo, mbavu, mapafu na kichwa. Kupuuza kufanya mazoezi ya mwili mzima, au sehemu ya mwili, hutaleta hali mbaya au za hatari kiafya. Kutotenda kazi kwa kiungo chochote cha mwili hupelekea kupungua kwa ukubwa na uimara wa misuli, na kusababisha damu kutiririka polepole katika mishipa ya damu. 3T 76.2

Ikiwa kuna majukumu ya kufanywa nyumbani, na haufikirii ya kuwa unaweza kuyafanya, lakini unategemea wengine wafanye. Wakati mwingine ni huwa ni usumbufu au hata ugumu kwako kupata msaada unaouhitaji. Mara kwa mara unatumia mara mbili ya nguvu zinazohitajika kutekeleza kazi hiyo, katika kupanga na kutafuta mtu wa kukufanyia kazi hiyo. Ikiwa tu utakubali akilini mwako, kufanya mwenyewe mambo haya madogo-madogo na majukumu ya familia, utabarikiwa na kuimarishwa, na ushawishi wako katika kazi ya Mungu utakuwa mkubwa zaidi. Mungu aliwaumba Adamu na Hawa katika Paradiso, na akawawekea kila kitu chema na cha kupendeza. Yeye Aliwapandia bustani nzuri. Hakuna mboga/mmea, maua wala mti ambao haukujitosheleza kwa matumizi ya aina yoyote ile iwe ni kwa mapambo n.k.

Muumba wa mwanadamu alijua kwamba kazi ya mikono Yake, au uumbaji Wake, hauwezi kuishi kwa furaha bila ya kufanya kazi. Paradiso ilifurahisha nafsi zao, lakini hii peke yake haikutosha; lazima wawe na kazi itakayovipa mazoezi ya viungo vya ajabu. Bwana aliuumba mwili ili utumiwe. Kama furaha ingehusisha kukaa bila ya kufanya kazi, basi mwanadamu, katika hali yake ya utakatifu, angeachwa pasina kazi. Ila Yeye Aliyemuumba mwanadamu alijua nini kingempa furaha, na pale alipomuumba tu, hakuchukua muda na kisha akampatia kazi. Ili wanadamu awe na furaha, lazima afanye kazi. 3T 76.3

Mungu ametupa sote kitu cha kufanya. Katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ambayo tunapaswa kuyafanya, ambayo yamo katika njia zetu, maisha yetu yatafanywa kuwa ya manufaa, na tutabarikiwa endapo tutayafanya. Sio tu kwamba viungo vya mwili vitaimarishwa na mazoezi, lakini akili pia itapata nguvu na maarifa kupitia utendaji wa viungo hivyo. Mazoezi ya msuli mmoja, huku mingine ikiwa haifanyi kazi, haitaimarisha ile isiyofanya kazi, isipokuwa mazoezi endelevu ya akili pia yataimarisha viungo ambavyo havitumiki. Kila kitivo cha akili na kila msuli una majukumu yake, na vyote vinahitaji kutumika ili viweze kukua ipasavyo na kudumisha afya yake. Kila kiungo na msuli huwa na ofisi/kazi bainishi

ya kufanya ndani ya mwili wa kiumbe hai. Kila gurudumu katika mashine lazima liwe hai, na linalofanya kazi nzuri na za ajabu za asili lazima ziwe endelevu ili kukamilisha yale yaliyo kusudiwa. Kila kitivo kina uhusiano na vitivo vingine, na vyote vinahitaji kufanya kazi ili kukua ipasavyo. Ikiwa msuli mmoja wa mwili utatumika zaidi kuliko mingine, ule unaotumiwa utakua mkubwa zaidi, na utaharibu upatanifu na uzuri wa ukuaji wa mfumo. Mazoezi mbalimbali hufanya misuli yote ya mwili itumike. 3T 77.1

Wale walio wanyonge na wavivu wasikubali mwelekeo wao wa kutofanya kazi au kukaa bila utendaji hai, hawapaswi kujinyima wenyewe hewa na mwanga wa jua, bali wanapaswa kujizoesha kufanya mazoezi ya nje wakitembea au kufanya kazi kwenye bustani. Watachoka sana, lakini jambo hili halitawaumiza. Dada yangu, utapata uchovu, lakini hautakuumiza; mapumziko yako yatakuwa mazuri baadaye. Kutokufanya kazi kunadhoofisha viungo ambavyo havifanyi mazoezi. Na wakati viungo hivi vinatumiwa, maumivu na uchovu hutokea, kwa sababu misuli imekuwa dhaifu. Sio jambo zuri kuacha baadhi ya misuli isifanye kazi kwa sababu tu itapata maumivu. Maumivu mara nyingi husababishwa na jitihada za asili kutoa uhai na nguvu kwa sehemu zisizo na uhai kwa sababu ya kutofanya kazi kwa muda mrefu. Utendaji kazi au kujongea kwa misuli hii ambayo haikuwa ikitumiwa kwa muda mrefu itasababisha maumivu, kwa sababu uwezo wa asili unaiamsha tena, ili iwe na utendaji hai. 3T 78.1

Kutembea, katika hali zote pale inapowezekana, ni dawa bora kwa miili yenye magonjwa, kwa sababu katika zoezi hili viungo vyote vya mwili hutumika. Wengi wanaotegemea tiba za kuvisogeza/kuvijongeza viungo kupitia watalaamu wenye mashine, wanaweza kufanikiwa zaidi kwa kufanya mazoezi ya misuli kuliko ambavyo wangeweza kusaidiwa na wataalamu na vifaa hivo. Katika baadhi ya matukio kutofanya mazoezi husababisha matumbo na misuli kudhoofika na kusinyaa, na viungo hivi ambavyo vimedhoofika kwa kutofanya kazi vitaimarishwa na mazoezi. Hakuna mazoezi ambayo yanaweza kuchukua nafasi ya kutembea. Kwa kufanya hivyo mzunguko wa damu huboreshwa zaidi. 3T 78.2

[Movement cure au tiba ya mjongeo ya 1900 iliyokuwa kama fiziotherapia au mama cheza, ilikuwa wataalamu wanamfanyia mtu mazoezi na massage na vyot maalumu, mtu aitwaye George Taylor na Injinia wa Sweden Goransson walitengeneza vyombo vya mazoezi ya mjongeo-patented movement cure aparatus.]

Matumizi endelevu ya viungo yatakuwa na faida kubwa kwako, Dada N. Umekuwa ukipata mawazo mengi au kuwa na imani nyingi nyingi, na kuwa mchangamfu na mwenye matumaini, hii imetokana na majeraha yako. ukiendelea kutowaamini matabibu, na kudhani ya kuwa unalielewa tatizo lako vizuri zaidi kuliko wao, hutofaidika kwa lolote bali utazidi kujeruhiwa, na matibabu yao. Madaktari wasipoaminiwa na wagonjwa wao kamwe hawatoweza kuwasaidia-mgonjwa

asipomsadiki daktari, hawezi kusaidiwa. Ikiwa utajielekeza, na kudhani kuwa unajua matibabu unayopaswa kupewa, kuliko wajuavyo matabibu, hutofanikiwa. Lazima usalimishe nia na maoni yako, na ujizuie kupinga uamuzi na ushauri wao katika shida yako. 3T 78.3

Bwana na akusaidie, dada yangu, usiwe na imani tu bali imani hii, iambatane na matendo. 3T 79.1

SURA YA 7

UAMINIFU KATIKA KAZI ZA NYUMBANI

Mpendwa dada O,

Ninahisi kuwa huna furaha. Ukiwa unatafuta kazi kubwa zaidi ya kufanya, unakosa umakini katika kazi ulizonazo kwa sasa ambazo zipo njiani mwako kabisa. Hauna furaha, kwa sababu unayaruka majukumu madogo ya kila siku ya maisha ukitazamia kupata kazi ya juu na kubwa zaidi kuliko unayofanya. Wewe haujatulia, hauna utulivu, na hauridhiki. Unapenda kuamrisha watu kuliko kutenda wewe mwenyewe. Unapenda sana kuwaambia wengine kwamba wafanye nini kuliko wewe mwenyewe, badala ya kuwa na uchangamfu ulio tayari katika kufanya jambo hilo kwa kupenda. 3T 79.2

Ungeifanya familia ya baba yako kuwa yenye furaha zaidi, endapo ungeyapa matakwa yako kipaumbele kidogo na furaha zaidi kwa wapendwa wako. Unaposhiriki katika majukumu ya kawaida katika maisha unashindwa kuweka moyo wako katika kazi yako. Akili yako inaenda mbele kule kwa kiwango cha juu zaidi, au yenye heshima kubwa. Binadamu yoyote anapaswa kufanya mambo kama haya ambayo hayafurahii wala kuyapenda. Majukumu haya ya kawaida, rahisi, yakifanywa kwa utayari na uaminifu, yatakupa elimu ambayo ni muhimu kwako kuipata itakayo kusaidia kuzipenda kazi za nyumbani.

Hapa kuna uzoefu wa muhimu sana unaotakiwa kuupata, lakini hutaupenda. Unalalamikia fungu lako, jambo linalowafanya watu walio karibu nawe kutokuwa na furaha, na unajikuta wewe binafsi unapoteza vitu vingi. Huenda kamwe usiitwe kufanya kazi ambayo itakuleta mbele ya umma. Lakini kazi zote tunazofanya ambazo ni za lazima kufanywa, iwe kuosha vyombo, kupanga meza, kuwakaribisha wagonjwa, kupika, au kufua, ni muhimu kimaadili; na usipoweza kufanya majukumu haya kwa uchangamfu na furaha hufai kwa majukumu makubwa na ya juu zaidi. Kazi za unyenyekevu zilizo mbele yetu zinapaswa kufanywa na mtu fulani (haziwezi kukaa bila kufanywa mfano kuosha choo cha umma, lazima mtu fulani afanye, asipofanya kutatokea shida); na wale wanaozifanya wanapaswa wajisikie kwamba wanafanya kazi ya muhimu na ya heshima, na kwamba katika utume wao, ingawa ni wa unyenyekevu, wanafanya kazi ya Mungu kwa hakika kama vile malaika Gabrieli alipotumwa kwa manabii. Wote wanafanya kazi kwa mpangilio katika maeneo/nyanja zao. Mwanamke nyumbani kwake, akifanya kazi rahisi za maisha ya kila siku ambazo lazima zifanyike, anaweza na anapaswa kuonesha uaminifu, utii, na upendo wa dhati kama malaika wafanyavyo katika duru/majukumu yao. Kuenenda sawa na mapenzi ya Mungu hufanya kazi yoyote kuheshimika. 3T 79.3

Unalohitaji ni upendo na vitendo vinavyoonyesha upendo na urafiki/mapenzi. Tabia yako inahitaji kufinyangwa. Wasiwasi wako lazima uwekwe kando, na badala yake lazima uuthamini upole, uungwana na upendo. Jinyime. Sisi hatukuumbwa kama Malaika, bali ni wa kiwango cha chini kuliko Malaika; na bado kazi yetu ni muhimu. Hatuko mbinguni, bali duniani. Tutakapokuwa mbinguni, ndipo tutakapostahili kufanya kazi ya juu na ya kuinua ya kimbingu. Ni katika ulimwengu huu lazima tujaribiwe na kuthibitishwa. Tunapaswa kuwa tayari, na kuimarishwa dhidi ya migogoro na wajibu wetu. 3T 80.1

Wajibu wa juu kabisa unaowahusu vijana upo katika nyumba zao wenyewe, kuwabariki baba na mama, kaka na dada, kwa mapenzi na maslahi ya Kweli. Hapa wanaweza kuonesha kujinyima, kukana nafsi na kuzisahau nafsi zao katika kujali na kuwatendea wengine. Kamwe mwanamke hatadhalilishwa kwa kazi hii. Hii ni ofisi takatifu zaidi, iliyoinuliwa anayoweza kuitumikia. Ni ushawishi wa namna gani anaoweza kuwa nao dada dhidi ya kaka zake? Ikiwa yuko sahihi anaweza kuamua tabia ya ndugu zake. Sala zake, upole, upendo na shauku yake inaweza kufanya

mengi katika familia. Dada yangu, sifa hizi adhimu haziwezi kuwasilishwa katika akili nyingine kabla hazijaonekana ndani yako kwanza. Kuridhika huko kwa akili/moyo, ule upendo, upole, na uchangamfu ambao utaufikia kila moyo, utaakisi kile ambacho moyo wako hutoa kwa wengine. Ikiwa Kristo hatawali moyo wako, kutakuwa na kutoridhika na upotovu wa maadili usiopendeza. Ubinafsi wako utakufanya ushurutishe wengine wakufanyie/wakupe kile ambacho wewen haupo tayari kuwapa wengine. Kama Kristo hayupo moyoni, hautakuwa na tabia na njema-utakuwa na tabia mbaya. 3T 80.2

Sio kazi ya heshima/kubwa wala vita/mapambano makubwa pekee ndiyo huijaribu roho na kuhitaji ujasiri. Maisha ya kila siku huleta mfadhaiko, majaribu, na kukatishwa tamaa. Ni kazi ya unyenyekevu ambayo mara nyingi huleta subira na ustahimilivu. Kujitegemea na maazimio thabiti ndiyo mambo ya muhimu ya kukutana nayo na kuyashinda magumu yote. Mshike Bwana kwa nguvu zote ili asimame pamoja nawe, kila mahali awe faraja yako. Unahitaji sana roho ya upole, utulivi na unyenyekevu, na bila hiyo huwezi kuwa na furaha. Acha Mungu akusaidie dada yangu, kutafuta unyenyekevu na haki. Wewe unamuhitaji Roho wa Mungu. Ikiwa uko tayari kuwa chochote au kutokuwa chochote-sifuri, Mungu atakusaidia na kukutia nguvu na kukubariki. Lakini ukipuuza majukumu madogo kamwe hutaaminiwa na kukabidhiwa majukumu yale makubwa zaidi. 3T 81.1

SURA YA 8

KIBURI NA MAWAZO YA UBATILI

Watoto wangu wapendwa P na Q: Mmedanganyika kuhusiana na nafsi zenu. Ninyi si Wakristo. Kuwa Wakristo wa Kweli ni kuwa kama Kristo. Mko mbali na alama katika suala hili; lakini natumaini kwamba hamtadanganyika hadi mtakapokuwa mmechelewa sana kuunda tabia kwa ajili ya mbinguni. {3T 81.2}

Mfano wenu haujawa mzuri. Hamjafikia hatua ya kutii maneno ya Kristo: “Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate Mimi.” Hapa kuna masomo ambayo hamjajifunza. Kujikana nafsi hakujawa sehemu ya elimu yenu. Mmepuuza kusoma maneno ya uzima. “Yachunguzeni Maandiko,”

kama alivyosema Mwalimu wa mbinguni. Yeye Alijua kwamba hili lilikuwa muhimu kwa wote ili wawe wafuasi wa Kweli wa Kristo. Mnapenda kusoma vitabu vya hadithi, lakini Neno la Mungu haliwavutii. Mnapaswa kujizuia usomaji wa hadithi na kukazania usomaji wenu wa Neno la Mungu na vitabu ambavyo ni vya tabia ya kiroho na yenye manufaa. Kwa kufanya hivyo mtafunga mlango dhidi ya majaribu, na mtabarikiwa. {3T 81.3}

Kama mngeboresha nuru ambayo imetolewa huko Battle Creek, sasa hivi mngekuwa mbali ya vile mlivyo katika maisha ya Kiungu/mbingu. Ninyi nyote wawili mna ubatili (mnashugulika na yale yaliyo bure kabisa) na mna kiburi. Hamjahisi kuwa lazima mtoe hesabu ya uwakili wenu. Mnawajibika kwa Mungu kwa fursa zenu zote na kwa mali zote ambazo hupita mikononi mwenu. Mmetafuta raha yenu wenyewe na kuridhisha/kuendekeza ubinafsi wenu kwa kupoteza dhamiri na idhini ya Mungu. Hamtendi kama watumishi wa Kristo, ambao wanawajibika kwa Mwokozi ambaye amewanunua kwa damu Yake ya thamani. "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki? Lakini Mungu na ashukuriwe kwa kuwa mlikuwa watumwa wa dhambi; mmeitii kutoka moyoni ile aina ya mafundisho mliyopewa. Baada ya kufunguliwa kutoka katika dhambi, mkawa watumwa wa haki." {3T 82.1}

Mnajiita watumishi wa Kristo. Je! mnajisalimisha KwakeYeye kwa utayari na utiifu wa hiari? Je, mnauliza kwa bidii jinsi mtakavyompendeza Yeye aliyewaita kuwa askari wa msalaba wa Kristo? Je! Nyote wawili mnauinua msalaba na kujisifu ndani yake? Jibuni maswali haya kwa Mungu. Matendo yenu yote, hata muwe mnafikiri ni siri kiasi gani, yako wazi kwa Baba yenu wa mbinguni. Hakuna kilichofichwa, hakuna kilichofunikwa. Matendo yenu yote na nia zinazowachochea ziko wazi machoni Pake. Ana ujuzi kamili wa maneno na mawazo yenu yote. Ni wajibu wenu kuyadhibiti mawazo yenu. Mtalazimika kupigana dhidi ya mawazo ya ubatili/hovyo. Mnaweza kufikiri kwamba hakuwezi kuwa na dhambi katika kuruhusu mawazo yenu yaende kama ambavyo yangefanya bila kujizuia. Lakini haikuwa hivyo. Mnawajibika kwa Mungu kwa kuendekeza mawazo yasiyofaa, ya ubatili; kwani kutokana na mawazo yasiyofaa hutoka kujisalimisha kwa dhambi, kufanya vitu ambavyo kwavyo akili imekaa. Simamieni/thibithini mawazo yenu, na itakuwa rahisi sana kutawala matendo yenu. Mawazo yenu yanahitaji kutakaswa. Paulo anawaandikia Wakorintho hivi: “Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.” Mnapokuja katika nafasi hii, kazi ya kujoweka wakfu itaeleweka vyema na ninyi nyote wawili. Mawazo yako yatakuwa safi, yaliyotakaswa, na yaliyoinuliwa; matendo yako safi na yasiyo na dhambi. Miili yenu itahifadhiwa katika utakaso na/hadhi/heshima, ili muwapatie "dhabihu iliyo hai,

takatifu, yenye kukubalika kwa Mungu, ndiyo ibada yenu yenye busara." Mnahitajika kujikana mwenyewe kwa vitu vidogo na vikubwa. Mnapaswa kujisalimisha kwa Mungu kikamilifu; hamjakubaliwa Naye katika hali yenu ya sasa. {3T 82.2}

Mmekuwa na ushawishi usiotakaswa kwa vijana walioko huko ----. Upendo wenu wa maonesho husababisha matumizi ya mali ambayo siyo sawa. Hamtambui madai ambayo Bwana anayo juu yenu. Hamjajua matokeo matamu/mazuri ya kujinyima. Matunda yake ni matakatifu. Kujitumikia wenyewe na kujifurahisha wenyewe umekuwa utaratibu wa maisha yenu. Kutumia mali yenu kukidhi kiburi yamekuwa mazoezi yenu. Oh, Laiti ingekuwa afadhali kiasi gani kama mngezuia tamaa zenu na kutoa dhabihu kwa ajili ya Ukweli wa Mungu, na kwa hivyo kukataa tamaa ya macho, tamaa ya mwili, na kiburi cha uzima kungewafanya muwe na kitu cha kuweka kwenye hazina ya Mungu! Badala ya kununua vitu visivyo na maana, wekeni vidogo mlivyonavyo katika benki ya mbinguni, ili ajapo Bwana mpate kupokea mtaji na faida. {3T 83.1}

Je, nyote wawili mmejifunza ni kiasi gani mngeweza kufanya ili kumheshimu Mkombozi wenu duniani? Lo, hapana! Mmekuwa radhi kujiheshimu na kupokea heshima ya wengine, lakini kujifunza ili kujionesha kuwa mmekubaliwa na Mungu hakujawa mzigo wa maisha yenu. Dini, safi na isiyo na unajisi, pamoja na kanuni zake zenye nguvu, ingewathibitishia kuwa ni nanga. Ili kujibu malengo makuu ya maisha lazima muepuke mfano wa wale ambao wanatafuta raha na anasa zao, na ambao hawana hofu ya Mungu mbele yao. Mungu ameweka masharti kwa ajili yenu ambayo ni ya kutosha. Ameandaa kwamba ikiwa mtatii masharti yaliyowekwa katika Neno Lake, na kujitenga na ulimwengu, mnaweza kupata nguvu kutoka Kwake kukandamiza kila ushawishi unaodhalilisha na kukuza yale bora, mazuri, mema, na ya kuinua. Kristo atakuwa ndani yenu "kisima cha maji kinachobubujikia uzima wa milele." Utashi, akili, na kila mhemko, vinapodhibitiwa na Kristo/dini, vina nguvu ya kubadilisha. {3T 83.2}

"Basi, mlapo au mnywapo, au chochote mfanyacho, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu." Hapa kuna kanuni ambayo iko kwenye msingi wa kila tendo, mawazo, na nia; kujitoa wakfu kwa ukamilifu, kwa mwili na akili, kwa udhibiti wa Roho wa Mungu. Nia isiyotakaswa na shauku lazima zisulubishwe. Hii yapaswa kuchukuliwa kama kazi muhimu na ngumu. Hata hivyo ni lazima ifanyike, vinginevyo mtasikia hukumu ya kutisha kutoka katika kinywa cha Yesu: "Ondokeni." Mnaweza kufanya mambo yote katika Kristo, awatiaye nguvu. Mko katika umri huo ambapo mapenzi/nia, uchu wa chakula, na shauku vinapiga mayowe kwa ajili ya anasa. Mungu ameyaweka haya katika asili yenu kwa malengo ya juu na matakatifu. Sio lazima kwamba yawe laana kwenu kwa kutumiwa vibaya. Yatakuwa hivi tu wakati mtakapotaa kutii udhibiti wa akili na dhamiri. Kujizuia, kujikana, kujinyima, ni

maneno na matendo ambayo hamna uzoefu nayo. Majaribu yamewayumbisha. Akili zisizotakaswa hushindwa kupokea nguvu na faraja hiyo ambayo Mungu amewaandalia. Akili hizi hazina utulivu na zina hamu kubwa ya kitu kipya, kitu cha kujiridhisha, kufurahisha na kusisimua akili; na hii inaitwa raha. Shetani ana mitego yenye kuloga/sumaku ya kuvutia ili kuhusisha mapenzi na kusisimua fikira za vijana hasa, ili aweze kuzifunga katika mtego wake. Mnajenga juu ya mchanga na Mnahitaji kulia kwa bidii: "Ee Bwana, nafsi yangu ya ndani ibadilishe." Mnaweza kuwa na ushawishi wa wema kwa vijana wengine, au mnaweza kuwa na ushawishi wa uovu. {3T 84.1}

Acheni Mungu wa amani awatakase kabisa, nafsi, mwili na roho. {3T 84.2}

SURA YA 9

KAZI HUKO BATTLE CREEK

Katika maono niliyopewa huko Bordoville, Vermont, Desemba 10, 1871, nilioneshwa kuwa nafasi ya mume wangu imekuwa mgumu sana. Shinikizo la masumbufu na kazi vimekuwa juu yake. Ndugu zake katika huduma hawajapata mizigo hii ya kubeba, na hawajaithamini kazi yake. Shinikizo la kila wakati juu yake limempa uchovu kiakili na kimwili. Nilioneshwa kuwa uhusiano wake na watu wa Mungu ulikuwa sawa, kwa njia zingine, na ule wa Musa kwa Israeli. Kulikuwa na manung'uniko dhidi ya Musa, wakati walikuwa katika hali mbaya, na kumekuwa na wanung'unikaji dhidi yake pia. {3T 85.1}

Hakujawa na mtu yeyote miongoni mwa watunza-Sabato ambaye angefanya kama ambavyo mume wangu amefanya. Amejitolea maslahi yake kwa ukaribu kabisa kwa ajili ya ujenzi wa kazi ya Mungu, bila kujali maslahi yake binafsi na kwa

kujitolea kwa raha ya kijamii na familia yake. Katika kujitolea kwake kwa kazi mara kwa mara amehatarisha afya na maisha yake. Amekuwa akilemewa sana na mzigo wa kazi hiyo, kiasi kwamba hajapata wakati unaofaa wa kujifunza, kutafakari, na kusali. Mungu hajamtaka awe katika nafasi hii, hata kwa maslahi na maendeleo ya kazi ya uchapishaji huko Battle Creek. Kuna matawi mengine ya kazi, maslahi mengine ya kazi hiyo, ambayo yamepuuzwa kupitia kujitolea kwake kwa kazi hii. Mungu ametupatia ushuhuda ambao utafikia mioyo. Amefungua mbele yangu njia nyingi za nuru, siyo tu kwa faida yangu, bali kwa faida ya watu Wake kwa ujumla. Amempatia mume wangu mwangaza mwingi juu ya masomo ya Biblia, siyo kwa ajili yake peke yake, bali kwa wengine. Niliona kwamba mambo haya yanapaswa kuandikwa na kuzungumzwa, na kwamba nuru mpya ingeendelea kuangaza juu ya Neno. {3T 85.2}

Niliona kwamba tunaweza kumaliza mara kumi zaidi ili kujenga kusudi la Mungu kwa kufanya kazi miongoni mwa watu wa Mungu, tukiwa na ushuhuda kadhaa wa kukidhi mahitaji ya kazi hiyo katika maeneo tofauti na chini ya hali tofauti, kuliko tunavyoweza kufanya tukibaki Battle Creek. Karama zetu zinahitajika katika kazi hiyo hiyo kwa maandishi/kunadika na kwa maneno. Wakati mume wangu anaelemewa sana, kama ambavyo amekuwa, na mkusanyiko wa mahangaiko na masuala ya kifedha, akili yake haiwezi kuzaa matunda katika Neno kama ambavyo ingekuwa vinginevyo. Na ana hatari/riski ya kushambuliwa na adui; kwani yuko katika nafasi ambayo kuna shinikizo kila wakati, na wanaume na wanawake watajaribiwa, kama Waisraeli, kulalamika na kunung'unika dhidi yake ambaye anasimama katika nafasi ya uwajibikaji zaidi katika kusudi na kazi ya Mungu. {3T 85.3}

Nikiwa nimesimama chini ya mizigo hii ambayo hakuna mtu mwingine angethubutu kuichukua, mume wangu wakati mwingine, chini ya shinikizo la masumbufu, amezungumza bila kuzingatia na kwa ukali dhahiri. Wakati fulani amewashutumu waliopo ofisini kwa sababu hawakujali. Na wakati ambapo makosa yasiyo ya lazima yametukia, yeye amehisi kwamba hasira kwa ajili ya kazi ya Mungu ilikuwa yenye haki ndani yake. Hatua hii ya kuzungumza nao haijawahi kupata kila wakati matokeo bora. Wakati fulani umetokea upuuziaji kwa upande wa wale waliokaripiwa kufanya mambo yale yale ambayo walipaswa kuyafanya; kwa maana waliogopa kwamba hawatawatendea haki; na basi wangelaumiwa kwa hilo. Basi kwaajili ambavyo kesi hii imekuwa, mzigo umemwangukia mume wangu. {3T 86.1}

Njia bora zaidi ingekuwa yeye kuwa mbali na ofisi zaidi kuliko ambavyo amekuwa, na kuacha kazi ili wengine wafanye. Na kama, baada ya kuhukumiwa kwa subira na haki, wangejidhihirisha kuwa si waaminifu, au hawakuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo, wangepaswa kutolewa, na kuachwa wafanye biashara ambapo kuboronga kwao na makosa yao vingeathiri maslahi yao binafsi na si kazi ya Mungu. {3T 86.2}

Kulikuwa na wale ambao walikuwa wakuu wa kazi ya Shirika la Uchapishaji ambao, kwa uchache kabisa, hawakuwa waaminifu. Na laiti wale waliohusishwa nao kama wadhamini wangejua na macho yao yasingepofushwa na hisia zao zisingepooza, watu hawa wangetengwa na kazi muda mrefu kabla ya hapo. {3T 86.3}

Mume wangu alipopona ugonjwa wake wa muda mrefu na mkali, alichukua kazi hiyo akiwa amechanganyikiwa na kwa aibu kwani iliachwa kwa watu wasio waaminifu. Alifanya kazi kwa azimio lote na nguvu ya akili na mwili aliyokuwa nayo kuileta kazi hiyo na kuikomboa kutoka katika mkanganyiko wa fedheha ambayo ilikuwa imeletwa ndani yake na wale ambao walikuwa na masilahi yao binafsi na ambao hawakuhisi kwamba kazi waliyohusishwa ilikuwa kazi takatifu. Mkono wa Mungu umenyooshwa katika hukumu juu ya hawa wasio waaminifu. Mwenendo wao na matokeo yanapaswa kuwa onyo kwa wengine kutofanya kama hawa walivyofanya. {3T 86.4}

Uzoefu wa mume wangu wakati wa ugonjwa wake ulikuwa wa usio mzuri-bahati mbaya kwake. Alikuwa amefanya kazi katika kusudi hili kwa shauku na kujitolea kuliko mtu mwingine yeyote alivyofanya. Alikuwa amejitokeza na kuchukua nafasi za mapema kama Mpaji alivyoongoza, bila kujali lawama au sifa. Alikuwa amesimama peke yake na kupigana na mateso ya mwili na akili, bila kuzingatia masilahi yake, wakati wale ambao Mungu aliwakusudia wasimame pamoja naye walimwacha kipindi alichohitaji msaada wao. Hakuwa tu ameachwa apigane vita na kuhangaika bila msaada wao na huruma, bali pia mara kwa mara ilimbidi akutane na upinzani na manung'uniko yao - manung'uniko dhidi ya mtu ambaye alikuwa akifanya mara kumi zaidi ya yeyote kati yao ili kujenga kusudi la kazi ya Mungu. Vitu vyote hivi vimekuwa na ushawishi wao; wamefinyanga akili ambayo hapo awali haikuwa na mashaka, yenye kutegemewa, na ya kuamini, na kumfanya apoteze imani kwa ndugu zake. Wale ambao wameshiriki katika kuleta kazi hii, kwa kiwango kikubwa, watawajibika kwa matokeo. Mungu angewaongoza ikiwa wangemtumikia kwa dhati na bidii na kwa kujitolea. {3T 87.1}

Nilioneshwa kwamba mume wangu alikuwa amewapatia ndugu zake ushahidi dhahiri wa kupendezwa kwake, na kujitolea kwa kazi ya Mungu. Baada ya kukaa miaka mingi ya maisha yake katika hali ya faragha na bila kukoma ili kuanzisha masilahi ya uchapishaji kwa hakika aliwazawadia watu wa Mungu kilicho chake na ambacho angeweza pia kutunza na kupokea faida kutoka kwa aliyemchagua kufanya hivyo. Kwa tendo hili aliwaonesha watu kwamba hakuwa akitafuta kujinufaisha mwenyewe, bali kuendeleza kazi ya Mungu. {3T 87.2}

Ugonjwa ulipomjia mume wangu, wengi walitenda kwa njia ile ile isiyo na hisia za huruma kama Mafarisayo walivyowatendea watu wenye bahati mbaya na walioonewa. Mafarisayo wangewaambia wale wanaoteseka kuwa shida zao zilitokana na dhambi zao, na kwamba hukumu za Mungu zimewajia. Kwa kufanya hivyo wangeongeza uzito wa mateso. Wakati mume wangu alipoanguka chini ya

mzigo wa masumbufu yake, kulikuwa na wale ambao hawakuwa watu katili wasio na huruma. {3T 88.1}

Alipoanza kupona, ili kwamba katika udhaifu wake na umasikini aanze kufanya kazi, aliwauliza wale ambao wakati huo walikuwa wakiongoza mambo ofisini kwa punguzo la asilimia 40 kwa oda ya dola mia moja kwa ajili ya vitabu. Alikuwa tayari kulipa dola sitini kwa vitabu hivyo ambavyo alijua vitakigharimu Chama dola hamsini pekee. Aliomba punguzo hili maalum kwa kuzingatia kazi yake ya zamani na dhabihu kwa niaba ya idara ya uchapishaji, lakini alinyimwa upendeleo huu mdogo. Aliambiwa bila tabasamu, kwa ubaridi kwamba wanaweza kumpa punguzo la asilimia 25. Mume wangu alifikiria jambo hili kwa uchungu sana, lakini akajaribu kuvumilia kwa njia ya Kikristo. Mungu mbinguni amerekodi uamuzi huo usio wa haki, na tangu wakati huo amechukua kesi hiyo kwa mikono Yake Mwenyewe, na amerudisha baraka zilizoondolewa , kama alivyofanya kwa Ayubu mwaminifu. Tangu wakati wa uamuzi huo usio wa kiungwana, Amekuwa akifanya kazi kwa ajili ya mtumishi Wake, na Amemwinua juu ya afya yake ya awali ya mwili, uwazi na nguvu ya akili, na uhuru wa roho. Na tangu wakati huo mume wangu amekuwa na furaha ya kupitisha machapisho yetu yenye thamani ya maelfu ya dola kwa mikono yake mwenyewe bila bei/kulipwa. Mungu hatawasahau kabisa wala hatawaacha milele wale ambao wamekuwa waaminifu, hata kama nyakati fulani wanafanya makosa. {3T 88.2}

Mume wangu amekuwa na usongo/bidii kwa Mungu na kwa Ukweli, na wakati mwingine ari hii imemwongoza kuzidi kuumia kwa nguvu ya mwili na akili. Lakini Bwana hajalichukulia hili kuwa dhambi kubwa kama kule kupuuza na kukosa uaminifu kwa watumishi Wake katika kukemea makosa kwa njia ambayo siyo ahihi. Wale ambao waliwasifu wasio waaminifu na kuwabembeleza (kuwasifia kwa udanganyifu) wale ambao hawajawekwa wakfu walikuwa washiriki katika dhambi yao ya kupuuza na uaminifu. {3T 88.3}

Mungu amemchagua mume wangu na kumpa sifa za pekee, uwezo wa asili, na uzoefu wa kuwaongoza watu Wake katika kazi. Lakini kumekuwa na manung'uniko kati ya Waadventista wanaotunza Sabato kama ilivyokuwa kati ya Israeli ya kale, na hawa wenye wivu, na shaka, kwa maoni na mapendekezo yao, wamewapa nafasi maadui wa imani yetu kutokuamini uadilifu wa mume wangu. Watu hawa wenye wivu wa imani hiyo hiyo wameweka mambo mbele ya makafiri katika nuru ya uwongo, na hisia zilizofanywa zisimame katika njia ya wengi kuukubali Ukweli. Wanamchukulia mume wangu kama tapeli mjanja, mtu mwenye ubinafsi, mwenye tamaa, na wanamwogopa yeye na Ukweli ulioshikiliwa na sisi kama waumini. {3T 89.1}

Wakati uchu chakula wa Israeli ya kale ulipozuiliwa, au wakati mahitaji yoyote ya lazima yalipoletwa juu yao, walimwangalia Musa, kwamba alikuwa mkali, kwamba alitaka kuwatawala, na kuwa mkuu juu yao, wakati alikuwa chombo tu mkononi

mwa Mungu kuwaleta watu Wake katika nafasi ya kunyenyekea na kutii sauti ya Mungu. {3T 89.2}

Israeli ya sasa wamenung'unika na kumwonea wivu mume wangu kwa sababu amesihi/ametoa mwito kwa ajili ya kazi ya Mungu. Amehamasisha ukarimu, amekemea wale wanaopenda ulimwengu huu, na amekemea ubinafsi. Ameomba michango kwa ajili ya kazi ya Mungu na, ili kuhimiza ukarimu kwa ndugu zake, ameongoza kwa michango ya ukarimu yeye mwenyewe; lakini kwa manung'uniko mengi, ya wenye wivu hata hili limefasiriwa kwamba alitaka kufaidika binafsi kwa njia ya ndugu zake na kwamba alikuwa amejitajirisha kwa gharama ya kazi ya Mungu; wakati ukweli katika suala hilo ni kwamba Mungu ameweka mikononi mwake nyenzo za kumwinua juu ya uhitaji ili kwamba asitegemee rehema/huruma za watu wanaobadilika, wanaonung'unika na wenye wivu. Kwa sababu hatujatanguliza maslahi yetu, bali tumemjali mjane na yatima, Mungu kwa uweza Wake ametenda kazi kwa niaba yetu na kutubariki kwa mafanikio tele na kwa wingi wa baraka. {3T 89.3}

Musa alitoa dhabihu ufalme uliotazamiwa, maisha ya heshima ya kiulimwengu na anasa katika makao ya kifalme, akichagua kuteseka zaidi pamoja na watu wa Mungu kuliko kufurahia anasa za dhambi kwa kitambo; maana alihesabu kushutumiwa Kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu, kuliko hazina zote za Misri. Kama tungechagua maisha ya raha na uhuru badala ya shughuli na masumbufu tungefanya hivyo. Lakini hili halikuwa chaguo letu. Tulichagua kufanya kazi kwa bidii kwa kusudi la Mungu, maisha ya kusafiri, pamoja na shida zake zote, upungufu/ufukara, na kuliko kujiweka katika maisha ya ugoigoi. Hatujaishi kwa ajili yetu wenyewe, ili kujipendeza wenyewe, bali tumejaribu kuishi kwa ajili ya Mungu, kumpendeza na kumtukuza. Hatukuifanya kazi ya Mungu kuwa chanzo cha kupata mali; bali Mungu ametimiza ahadi Yake kwa kutupatia mara mia katika maisha haya. Yeye Anaweza kututhibitisha kwa kuiondoa kutoka kwetu. Ikiwa ndivyo, tunasali tuwe na unyenyekevu ili kuhimili mtihani huo. {3T 89.4}

Ijapokuwa ameweka dhamana kwa vipaji vyetu vya pesa na ushawishi, tutajaribu kuviwekeza katika kazi Yake, kwamba ikiwa moto utateketeza na dhiki ikaipunguza, tunaweza kuwa na furaha ya kujua kwamba baadhi ya hazina zetu ziko mahali ambapo moto hauwezi kuziteketeza au dhiki kufagilia mbali. Kazi ya Mungu ni benki ya uhakika ambayo haiwezi kushindwa kamwe, na uwekezaji wa wakati wetu, mali/maslahi/shauku yetu, na uwezo wetu ndani yake ni hazina mbinguni ambayo haishindwi. {3T 90.1}

Nilioneshwa kwamba mume wangu amekuwa na shuguli mara tatu zaidi ya ile ambayo angepaswa kuwa nayo. Amejaribiwa kuhisi kwamba Ndugu R na S hawakumsaidia kubeba majukumu yake, na amejisikia huzuni kwa sababu hawakumsaidia katika masuala ya kazi kuhusiana na Taasisi na Chama cha Uchapishaji. Kumekuwa na maendeleo katika kazi ya uchapishaji tangu pale wale

wasio waaminifu walipotenganishwa nayo. Na kadri kazi ilivyozidi kuongezeka, kungepaswa kuwa na watu wa kushiriki majukumu; lakini wengine ambao wangeweza kufanya hivyo hawakuwa na shauku, kwa sababu isingeongeza mali zao kama vile biashara yenye faida zaidi ingeweza kufanya. {3T 90.2}

Hakuna talanta katika ofisi yetu ambayo inapaswa kuwepo. Kazi hiyo inadai watu waliochaguliwa zaidi na walio wengi zaidi kuishiriki. Kwa hali ya sasa ya mambo ofisini mume wangu bado atahisi shinikizo ambalo amepata, lakini ambalo hapaswi kulibeba tena. Ni kwa muujiza tu wa huruma ya Mungu kwamba amesimama chini ya mzigo kwa muda mrefu. Lakini sasa kuna mambo mengi ya kuzingatia. Ustahimilivu wake wa kudumu na kujitolea kwa kazi, vimeonesha kile ambacho kinaweza kufanywa katika idara ya uchapishaji. Watu walio na maslahi yasiyo ya ubinafsi pamoja na maamuzi/hukumu iliyotakaswa wanaweza kufanya kazi ya ofisi ifanikiwe. Mume wangu ameubeba mzigo huo peke yake kwa muda mrefu kiasi kwamba mzigo huo umepelekea kuleta jambo la kutisha kwa nguvu zake, na kuna ulazima chanya wa mabadiliko. Ni lazima aondolewe kutoka katika huduma kwa kiwango kikubwa, na bado anaweza kufanya kazi katika kusudi la Mungu katika kunena na kuandika. {3T 90.3}

Tuliporudi kutoka Kansas katika majira ya kupukutisha majani ya mwaka 1870, mimi na yeye tulipaswa kuwa na kipindi cha kupumzika. Majuma ya uhuru kutoka kwa huduma yalihitajika ili kuongeza nguvu zetu zilizochoka. Lakini tulipoona kwamba chapisho muhimu huko Battle Creek lilikuwa karibu kuachwa, tulihisi kulazimika kuchukua kazi hiyo kwa nguvu maradufu, na kufanya kazi zaidi ya nguvu zetu. Nilioneshwa kwamba mume wangu asisimamie hapo tena isipokuwa watakuwepo watu ambao watahisi uhitaji wa jambo hilo na kubeba mizigo ya kazi, huku yeye akitenda tu kama mshauri. Ni lazima aweke mzigo huo chini, kwa kuwa Mungu ana kazi muhimu afanye katika kuandika na kufundisha ile Kweli. Ushawishi wetu katika kufanya kazi katika uwanja mpana utaeleza zaidi kwa ajili ya kuijenga kazi ya Mungu. Kuna kiasi kikubwa cha ubaguzi katika akili nyingi. Kauli za uongo zimetuweka katika hali mbaya mbele ya watu, na hii inawazuia wengi kuukubali Ukweli. Wakifanywa waamini kwamba wale walio na nyadhifa za uwajibikaji katika kazi huko Battle Creek wanabuni na kuwa washupavu, wanahitimisha kwamba kazi yote ina makosa na kwamba maoni yetu kuhusu Kweli za Biblia lazima yasiwe sahihi, na wanaogopa kuchunguza na kupokea Ukweli. Lakini hatupaswi kwenda kuwaita watu watutazame; kwa ujumla hatupaswi kujisemea wenyewe na kutetea tabia zetu wenyewe; bali tunapaswa kusema Ukweli, kuinua Ukweli, kusema juu ya Yesu, kumtukuza Yesu, na hii, ilikihudhuriwa na nguvu ya Mungu, itaondoa ubaguzi na kutuliza upinzani. {3T 91.1}

Ndugu R na S wanapenda kuandika; vivyo hivyo mume wangu. Na Mungu ameacha nuru Yake iangaze juu ya Neno Lake, na amemwongoza kwenye uwanja wa mawazo tajiri ambayo itakuwa baraka kwa watu wa Mungu kwa ujumla. Wakati amebeba mzigo mara tatu, baadhi ya ndugu zake wanaomhudumia wameacha

jukumu limlemee sana, wakijifariji na wazo kwamba Mungu alikuwa amemweka Ndugu White kuwa kiongozi wa kazi hiyo na kumstahilisha kuifanya, na kwamba Bwana alikuwa hajawaandaa wao kwa nafasi hiyo; kwa hivyo hawajachukua jukumu na kubeba mizigo ambayo wangeweza kuibeba. {3T 91.2}

Lazima wawepo watu ambao wangehisi mzigo/shauku sawa na ambayo mume wangu amehisi. Hakuna wakati wowote muhimu katika historia ya Waadventista Wasabato kuliko sasa. Badala ya kazi ya uchapishaji kupungua au kurudi nyuma, uhitaji wa machapisho yetu unaongezeka sana. Kutakuwa na mengi ya kufanya badala ya kuwa machache. Mume wangu amekuwa akinung'unika sana, ameshindana na wivu na uwongo muda mrefu sana, na ameona uaminifu mdogo sana kwa watu, hata amekuwa na akimshuku karibu kila mtu, hata ndugu zake mwenyewe katika huduma. Ndugu wanaohudumu wamelihisi hili, na kwa hofu kwamba hawatasonga kwa busara, katika hali nyingi hawajasogea hata kidogo. Lakini wakati umefika ambapo watu hawa lazima wafanye kazi kwa umoja kuinua mizigo. Ndugu wanaohudumu hawana imani kwa Mungu. Wanaamini Ukweli, na kwa hofu ya Mungu wanapaswa kuunganisha juhudi zao, na kubeba mizigo ya kazi hii ambayo Mungu amewawekea. {3T 92.1}

Ikiwa, baada ya mmoja kufanya kila awezalo katika uamuzi wake, mwingine anafikiria anaweza kuona ni wapi angeboresha jambo hilo, anapaswa kwa uvumilivu, wema na upole kumpatia ndugu huyo faida ya uamuzi wake, lakini hapaswi kumlaumu wala kuhoji uadilifu wa kusudi lake mapema kuliko vile yeye mwenyewe asingetaka kushukiwa au kulaumiwa isivyo haki. Ikiwa ndugu anayehisi kusudi la Mungu moyoni ataona kwamba, katika jitihada zake za dhati za kufanya, ameshindwa, atahisi sana jambo hilo; kwa maana atakuwa na mwelekeo wa kutojiamini mwenyewe na kupoteza ujasiri katika hukumu yake mwenyewe. Hakuna kitakachodhoofisha ujasiri wake na utu wa utauwa kama kutambua makosa yake katika kazi ambayo Mungu amemteua aifanye, kazi ambayo anaipenda zaidi kuliko maisha yake. Basi, ni udhalimu kiasi gani, kwa ndugu zake ambao hugundua makosa yake kuendelea kushinikiza mwiba zaidi na zaidi ndani ya moyo wake, kumfanya ajisikie kwa uchungu zaidi, wakati kwa kila msukumo wanapunguza imani na ujasiri wake ndani yake wa kufanya kazi kwa mafanikio katika kuijenga kazi ya Mungu. {3T 92.2}

Mara kwa mara Ukweli na uhakika vinapaswa kusemwa wazi kwa wakosefu, ili kuwafanya waone na kuhisi makosa yao ili wafanye ukarabati/matengenezo. Lakini hili linapaswa kufanywa kila wakati kwa huruma, siyo kwa ukali/ujeuri au ukatili, bali kwa kuzingatia udhaifu wa mtu mwenyewe, asije akajaribiwa. Mwenye kosa anapoona na kukiri kosa lake, basi, badala ya kumhuzunisha, na kutafuta kumfanya ahisi kwa undani zaidi, faraja yapasa kutolewa. Katika mahubiri ya Kristo mlimani alisema: Msihukumu msije mkahukumiwa. Kwa maana hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. Mwokozi wetu alikemea hukumu ya haraka-haraka. "Kwa nini

unatazama kibanzi kilicho katika jicho la ndugu yako; ... na, wakati, boriti liko katika jicho lako mwenyewe?" Ni kawaida kwamba wakati mtu ana haraka ya kuona makosa ya ndugu zake, anaweza kuwa katika makosa makubwa yeye mwenyewe, lakini akawa kipofu kwa makosa hayo. {3T 93.1}

Wote ambao ni wafuasi wa Kristo wanapaswa kushughulika wenyewe kwa wenyewe jinsi tunavyotamani Bwana ashughulike nasi katika makosa na udhaifu wetu, kwa kuwa sisi sote tunakosea na tunahitaji huruma na msamaha Wake. Yesu alikubali kuchukua asili ya kibinadamu, ili apate kujua jinsi ya kuhurumia/kusikitikia watu, na jinsi ya kumsihi Baba Yake kwa niaba ya wanadamu wenye dhambi, wakosefu. Alijitolea kuwa Wakili wa mwanadamu, na Akajidhalilisha ili apate majaribu ambayo mwanadamu alikuwa amekumbwa nayo, ili aweze kuwasaidia wale ambao wangejaribiwa, na kuwa kuhani Mkuu Mwenye huruma na mwaminifu. {3T 93.2}

Mara kwa mara kuna umuhimu wa kukemea dhambi waziwazi na kukemea makosa. Lakini wachungaji/wahudumu ambao wanafanya kazi kwa wokovu wa wenzao hawapaswi kukosa huruma/rehema, wala kuyakuza makosa katika taasisi zao. Hawapaswi kufichua au kukemea udhaifu wao. Wanapaswa kuuliza ikiwa njia hiyo, inayofuatwa na mtu mwingine kuwaelekea wao wenyewe, ingeleta matokeo yanayotarajiwa; Je, ingeongeza upendo wao na kujiamini, kwa yule ambaye kwa njia hiyo alifanya makosa yao yawe maarufu? Haswa makosa ya wahudumu wanaojishughulisha na kazi ya Mungu yanapaswa kuwekwa ndani ya mduara mdogo kadri iwezekanavyo, kwani kuna wanyonge wengi ambao watafaidika ikiwa wanajua kuwa wale wanaohudumia kwa Neno na mafundisho wana udhaifu kama watu wengine. Na ni jambo la kikatili zaidi kwa makosa ya mchungaji/mtendakazi kufunuliwa kwa wasioamini, ikiwa mtendakazi huyo anahesabiwa kuwa anastahili kufanya kazi siku za usoni kwa ajili ya wokovu wa roho. Hakuna mema yanayoweza kutokana na mfiduo huo, isipokuwa ni madhara tu. Bwana anachukia njia hii, kwa kuwa inadhoofisha imani ya watu kwa wale anaowakubali kuendeleza kazi Yake. Tabia ya kila mtendakazi inapaswa kulindwa kwa wivu na ndugu na watendakazi wenzake. Mungu asema: "Usiwaguse watiwa-mafuta Wangu, wala msiwadhuru manabii Wangu." Upendo, kuaminiana na ujasiri vinapaswa kuzingatiwa. Kukosekana kwa upendo huu na kujiamini kwa mtumishi/mchungaji mmoja kwa mtumishi/mchungaji mwingine hakuongezi furaha ya yule aliyepungukiwa, bali anapomkosesha furaha ndugu yake anajikosesha furaha yeye mwenyewe. Kuna nguvu kubwa katika upendo kuliko ilivyowahi kupatikana katika kukosa na kulaumu. Upendo utayeyusha kupitia katika vizuizi, wakati lawama itafunga kila njia ya roho. {3T 93.3}

Mume wangu lazima awe na mabadiliko. Huenda hasara ikatokea kwenye ofisi ya uchapishaji kwa kukosa uzoefu wake wa muda mrefu, lakini hasara ya pesa haiwezi kulinganishwa na afya na maisha ya mtumishi wa Mungu. Mapato ya kazi yanaweza kuwa siyo makubwa kwa uhitaji wa wasimamizi wenye kujali uchumi; lakini ikiwa

mume wangu atashindwa tena, hilo litawavunja moyo ndugu zake na kudhoofisha mikono yao. Fedha haziwezi kuja kiasi kile kile. {3T 94.1}

Kuna mengi ya kufanywa. Wamishenari walio tayari wanapaswa kuwa shambani, na ikihitajika, kwenda katika nchi za kigeni ili kuwasilisha Kweli mbele ya wale walioketi gizani. Lakini kuna mwelekeo mdogo wa kujiweka wakfu kwa Mungu miongoni mwa vijana na kutumia talanta zao kumtumikia Yeye. Wako tayari kuachana na majukumu na mizigo. Hawapati uzoefu wa kubeba mizigo au ujuzi wa Maandiko ambao wanapaswa kuwa nao ili kuwafaa kwa kazi ambayo Mungu angeikubali mikononi mwao. Ni jukumu la wote kuona ni kiasi gani wanaweza kumfanyia Mwalimu ambaye amekufa kwa ajili yao. Lakini wengi wanatafuta kufanya kidogo kadri iwezekanavyo na wanathamini tumaini hafifu la kuingia mbinguni hatimaye. Ni bahati yao kuwa na nyota kwenye taji yao kwa sababu ya roho zilizookolewa kupitia wao. Lakini ole! Mazoea ya kukaa bila kazi na uvivu wa kiroho hutawala kila mahali. Ubinafsi na kiburi huchukua nafasi kubwa mioyoni mwao, na kuna nafasi ndogo ya mambo ya mbinguni. {3T 94.2}

Katika maombi ambayo Kristo aliwafundisha wanafunzi Wake lilikuwa ombi hili: Utusamehe makosa yetu kama sisi tunavyowasamehe wanaotukosea. Hatuwezi kurudia sala hii kutoka moyoni na kuthubutu kutosamehe, kwani tunamwomba Bwana atusamehe makosa yetu Kwake kwa njia ile ile ambayo sisi huwasamehe wale wanaotukosea sisi. Lakini ni wachache wanaotambua umuhimu wa Kweli wa sala hii. Ikiwa wale wasiosamehe wangefahamu undani wa maana yake, wasingethubutu kuirudia na kumwomba Mungu awashughulikie wanaposhughulika na wanadamu wenzao. Na bado roho hii ya ugumu na kukosa msamaha ipo hata miongoni mwa ndugu kwa kiasi cha kutisha. Ndugu ni mkali kwa ndugu yake. {3T 95.1}

Majaribio ya kipekee

Msimamo ambao mume wangu ameuchukua kwa muda mrefu katika kusudi na kazi ya Mungu umekuwa moja ya majaribio ya kipekee. Utendaji wake wa kuchukuliana na kazi na uwezo wake wa kuona mbele vimewafanya ndugu zake wachungaji kumwachia majukumu ambayo walipaswa kuyabeba wenyewe. Hii imefanya mizigo yake kuwa mikubwa sana. Na wakati ambapo ndugu zake hawajachukua sehemu yao ya mizigo, wamepoteza uzoefu muhimu ambao ilikuwa fursa yao kupata ikiwa wangetumia akili zao katika mwelekeo wa utunzaji, wa kuona na kuhisi kile ambacho lazima kifanyike kwa ujenzi wa kazi hiyo. {3T 95.2}

Majaribu makubwa yameletwa kwa mume wangu na ndugu zake wahudumu/wachungaji kwa kutosimama karibu naye wakati alipohitaji sana msaada wao. Kukatishwa tamaa ambako amekuwa nako mara kwa mara wakati wale aliowategemea walipomwacha katika nyakati za uhitaji mkubwa kumekaribia kuharibu uwezo wake wa kutumaini na kuamini uthabiti wa ndugu zake

wanaohudumu naye. Roho yake imejeruhiwa sana kiasi kwamba amejiona ana haki ya kuhuzunika, na ameruhusu akili yake kukita kwenye kukatishwa tamaa. Njia hii ya giza Mungu angemtaka aifunge, kwa sababu yuko katika hatari ya kuvunjikiwa meli ya imani hapa. Akili yake inapofadhaishwa, ni kawaida kwake kuleta yaliyopita na kuishi katika mateso yake ya zamani; na kutokuwa na maridhiano/mapatano kunashikilia roho yake, kwamba Mungu amemruhusu asumbuliwe na majaribu yasiyostahili. {3T 96.1}

Roho wa Mungu amehuzunishwa kwa sababu hajaweka kabisa njia zake kwa Mungu na kujiamini kabisa mikononi Mwake Bwana, na asiruhusu akili yake iingie katika njia ya mashaka na kutokuamini juu ya uadilifu wa ndugu zake. Kwa kuongelea mashaka na kukata tamaa hajarekebisha uovu, bali amedhoofisha nguvu zake mwenyewe na kumpa Shetani faida ya kumkasirisha na kumsumbua. Amekosea katika kuzungumzia mambo yanayomvunja moyo na kuzingatia sifa mbaya za uzoefu wake. Kwa kuzungumza hivi, anatawanya giza wala siyo nuru. Wakati fulani ameweka uzito wa kukatisha tamaa juu ya ndugu zake, jambo ambalo halikumletea msaada hata kidogo, bali liliidhoofisha tu mikono yao. Anapaswa kuishi kanuni ya kutozungumzia juu ya kutokuamini au kuvunjika moyo, au kuzingatia malalamiko yake. Ndugu zake kwa ujumla wamempenda na kumhurumia, na wametoa udhuru juu yake, wakijua shinikizo la taabu juu yake, na kujitolea kwake kwa kazi ya Mungu. {3T 96.2}

Mume wangu amejitahidi bila kuchoka ili kuyaleta maslahi ya uchapishaji hadi katika hali yake ya sasa ya ustawi. Niliona kwamba alikuwa na huruma na upendo zaidi kutoka kwa ndugu zake kuliko vile alivyofikiri kuwa. Wanaipekua karatasi hiyo kwa hamu ili kupata kitu kutoka kwenye kalamu yake. Ikiwa kuna sauti ya furaha ndani ya maandishi yake, ikiwa anazungumza kwa kutia moyo, mioyo yao hufurahi, na wengine hata hulia kwa hisia nyororo za shangwe. Lakini ikiwa huzuni na majonzi vimeoneshwa, nyuso za ndugu na dada zake, wanaposoma, huwa na huzuni, na roho ambayo huonesha maandishi yake huakisiwa juu yao. {3T 96.3}

Bwana anatafuta kumfundisha mume wangu kuwa na roho ya msamaha/kusamehe, na kusahau vifungu vya giza katika uzoefu wake. Kumbukumbu ya siku za nyuma zisizofurahisha huleta huzuni ya wakati wa sasa, na anaishi tena katika zile sehemu mbaya ya historia ya maisha yake. Kwa kufanya hivyo anashikilia giza na anasukuma mwiba zaidi ndani ya roho yake. Huu ni udhaifu wa mume wangu, na haumpendezi Mungu. Hii inaleta giza na sio mwanga. Anaweza kujisikia ahueni kwa wakati huo kwa kuelezea hisia zake; lakini hii inafanya hisia kali zaidi ya jinsi mateso na majaribu yake yalivyokuwa makubwa, mpaka yote yanapokuzwa katika mawazo yake, na makosa ya ndugu zake, ambao wamesaidia kuleta majaribu haya juu yake, yanaonekana kuwa mabaya sana hata makosa yao yanaonekana kwake kwamba hayawezi kubebeka/kuvumilika kamwe. {3T 97.1}

Mume wangu amelithamini giza hili kwa muda mrefu kwa kuishi maisha ya zamani yasiyo ya furaha kiasi kwamba ana nguvu kidogo ya kudhibiti akili yake wakati anapodumu katika vitu hivi. Mazingira na matukio ambayo mara moja asingeyafikiria, yanakuzwa mbele yake na kuwa makosa makubwa kwa upande wa ndugu zake. Amekuwa mwangalifu sana kwa makosa ambayo ameteseka kwayo kiasi kwamba ni muhimu awe kadri iwezekanavyo kwa uchache katika mazingira na Battle Creek, ambapo mambo mengi yasiyo furahisha yalitokea. Mungu ataiponya roho yake iliyojeruhiwa, ikiwa atamruhusu. Lakini kwa kufanya hivyo, atalazimika kuzika yaliyopita. Hapaswi kuyazungumzia hayo, au kuandika juu yake. {3T 97.2}

Mungu hapendezwi kabisa kwa mume wangu kusimulia magumu yake na malalamiko yake ya kipekee ya wakati uliopita. Ikiwa angeyatazama mambo haya kwa nuru kwamba hakutendewa yeye, bali Bwana, ambaye yeye ni chombo Chake, basi angepokea thawabu kubwa. Lakini amechukua manung'uniko ya ndugu zake kana kwamba amefanyiwa yeye mwenyewe na amejisikia kuitwa kuwafanya wote waelewe ubaya na uovu, na hivyo kumlalamikia wakati hakustahili lawama na unyanyasaji wao. {3T 97.3}

Kama mume wangu angehisi kwamba angeweza kuliacha jambo hili kwa Bwana, na kwamba manung’uniko yao na kupuuza kwao vilikuwa dhidi ya Bwana badala ya mtumishi katika utumishi wa Bwana, asingehuzunika sana, na asingeumizwa. Alipaswa kuyaacha kwa Bwana, ambaye yeye ni mtumishi Wake, ili apigane vita Vyake kwa ajili yake na kutetea haki yake. Ndipo hatimaye angepokea thawabu yenye thamani kwa mateso yake yote kwa ajili ya Kristo. {3T 98.1}

Niliona kwamba mume wangu hapaswi kukazia fikra katika mambo yenye kuumiza katika uzoefu wetu. Wala hapaswi kuandika malalamiko yake, bali ajiweke mbali nayo kadiri awezavyo. Bwana ataponya majeraha ya wakati uliopita ikiwa atageuza mawazo yake kutoka kwayo. "Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana; vile vinavyoonekana ni vya muda tu, lakini visivyoonekana ni vya milele. " Wakati ungamo linapofanywa na ndugu zake ambao wamekuwa wakikosea, anapaswa kukubali maungamo na kwa ukarimu, kwa heshima, atafute kuwatia moyo wale ambao wamedanganywa na adui. Anapaswa kukuza roho ya kusamehe na asifikirie juu ya makosa na maovu/makosa ya wengine, kwani kwa kufanya hivyo siyo tu kwamba anaidhoofisha nafsi yake mwenyewe, bali pia anatesa akili za ndugu zake ambao wamekosea, wakati ambapo wanaweza kuwa wamefanya yote wawezayo kufanya kwa kukiri kurekebisha makosa yao ya zamani. Ikiwa Mungu anaona ni muhimu kwamba sehemu yoyote ya hatua yao ya zamani iwasilishwe mbele yao, ili waweze kuelewa jinsi ya kujiepusha na makosa katika siku zijazo, atafanya kazi hii; lakini mume wangu hapaswi kujiamini kufanya hivyo, kwa kuwa hii inaamsha matukio ya zamani ya mateso ambayo Bwana angemtaka ayasahau. {3T 98.2}

SURA YA 10

MAFUMBO YA WALIOPOTEA

Kondoo Waliopotea

Nilielekezwa kwenye mfano wa kondoo aliyepotea. Kondoo tisini na kenda wameachwa nyikani, na msako unafanywa kumtafuta yule aliyepotea. Kondoo aliyepotea anapopatikana, mchungaji humwinua begani na kurudi kwa shangwe. Hakurudi akinung'unika na kumlaani/akimgombeza kondoo masikini aliyepotea kwa kuwa amemtaabisha sana, bali kurudi kwake na mzigo wa kondoo ni kwa furaha. {3T 99.1}

Na onesho kubwa zaidi la furaha linahitajika. Marafiki na majirani wameitwa kufurahi pamoja na mtafutaji, "kwa maana nimempata kondoo wangu aliyepotea." Upatikanaji huo ulikuwa mada ya furaha; upotevu haukuwa suala; kwani furaha ya kumpata ilizidi huzuni ya upotevu na taabu, kufadhaishwa. kuchanganyikiwa na hatari, iliyopatikana katika kumtafuta kondoo aliyepotea na kumrejeshea usalama. "Nawaambia, vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu." {3T 99.2}

Fedha Iliyopotea

Kipande cha fedha kilichopotea kimelenga kuwakilisha mkosaji, anayetangatanga. Uhangaikaji wa mwanamke ili kupata fedha iliyopotea ni kuwafundisha wafuasi wa Kristo somo kuhusu jukumu lao kwa wakosaji wanaopotoka kutoka njia ya haki. Mwanamke aliwasha mshumaa ili kuongeza mwanga wake, kisha akafagia nyumba, na kutafuta kwa uadilifu/bidii mpaka akaipata. {3T 99.3}

Hapa umeelezewa wazi wajibu wa Wakristo kwa wale wanaohitaji msaada kwa sababu ya kupotea kwao kutoka kwa Mungu. Wale wanaokosea hawapaswi kuachwa katika giza na makosa, bali kila njia inayopatikana inapaswa kutumiwa kuwaleta tena kwenye nuru. Mshumaa umewashwa; na, kwa maombi ya dhati ili nuru ya mbinguni ikidhi kesi za wale waliofunikwa na giza na kutokuamini, Neno

la Mungu linatafutwa kwa Ukweli ulio wazi, ili Wakristo waweze kuimarishwa na hoja kutoka kwa Neno la Mungu, na karipio zake, vitisho na faraja, ili waliokosea wafikiwe. Kutojali au kupuuza kutakutana na uso wa Mungu uliokunjamana. {3T 99.4}

Yule mwanamke alipoipata ile fedha, aliwaita marafiki zake na majirani zake pamoja, akisema: "Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimeipata fedha iliyopotea. Vivyo hivyo, nawaambia, kuna furaha mbele ya malaika na mbele ya Mungu juu ya mwenye dhambi mmoja atubuye. " Ikiwa malaika wa Mungu wanafurahi juu ya wakosaji ambao wanaona na kukiri makosa yao na kurudi kwenye ushirika wa ndugu zao, ni zaidi sana kiasi gani kwa wafuasi wa Kristo, ambao wenyewe wanakosea, na ambao kila siku wanahitaji msamaha wa Mungu na wa ndugu zao, wanapaswa kujisikia furaha kwa kurudi kwa ndugu au dada ambaye amedanganywa na udanganyifu/ujanja wa Shetani na kuchukua njia mbaya na kuteseka kwa sababu yake. {3T 100.1}

Badala ya kushikilia makosa, ndugu zao wanapaswa kukutana nao mahali walipo. Badala ya kutafuta makosa kwao kwa sababu wako gizani, wanapaswa kuwasha taa yao wenyewe kwa kupata neema zaidi ya Mungu na ujuzi ulio wazi zaidi wa Maandiko, ili waweze kuliondoa giza la wale walio katika upotovu kwa nuru wanayowaletea. Na watakapofaulu, na wakosaji kuhisi makosa yao na kujinyenyekesha kufuata nuru, wanapaswa kupokelewa kwa furaha, na sio kwa roho ya manung'uniko au juhudi ya kuwasisitizia juu ya dhambi zao kubwa, ambayo ilikuwa imewaletea maumivu, wasiwasi, na uchovu. Ikiwa malaika safi wa Mungu wanalisifia tukio hilo kwa furaha, ndugu zao wanapaswa kufurahi zaidi, ambao wenyewe wanahitaji huruma, rehema upendo, na usaidizi wanapokosea na katika giza lao wakiwa hawajui jinsi ya kujisaidia wenyewe. {3T 100.2}

Mwana Mpotevu

Usikivu wangu uliletwa kwenye mfano wa mwana mpotevu. Alitoa maombi kwamba baba yake ampe sehemu yake ya mali. Alitamani kutenganisha maslahi yake na ya baba yake, na kusimamia sehemu yake inayoendana na mwelekeo wake. Baba yake alitii/aliendana na ombi hilo, na kijana kwa ubinafsi aliondoka kwa baba yake, ili asisumbuliwe na ushauri wake au maonyo. {3T 100.3}

Kijana alifikiri kuwa anapaswa kufurahi kama angeweza kutumia sehemu yake kulingana na raha yake mwenyewe, bila kukasirishwa/kusumbuliwa na ushauri au kizuizi. Hakutaka kutatizwa na wajibu wa pande zote mbili. Kama alikuwa mmiliki wa mali pamoja na babaye (shea) basi baba yake alikuwa na madai juu yake kama mtoto. Ila yeye hakuhisi kuwa chini ya wajibu lolote kwa baba yake mkarimu, naye akaishikilia roho yake ya ubinafsi, ya uasi kwa wazo kwamba sehemu ya mali ya baba yake ilikuwa yake. Aliomba sehemu yake, wakati kwa haki asingeweza kudai chochote na hakupaswa kuwa na chochote. {3T 101.1}

Baada ya moyo wake wa ubinafsi kupokea hazina, ambayo hakuistahili kabisa, alienda mbali na baba yake, ili asahau kuwa alikuwa na baba. Alidharau kizuizi na aliazimia kikamilifu kupata raha kwa njia na namna yoyote aliyochagua. Baada ya kutumia mai yake katika dhambi yote ambayo baba yake alikuwa amempatia, nchi ilipatwa na njaa, na alihisi uhitaji mwingi. Kisha akaanza kujutia mwenendo wake wa dhambi wa kujifurahisha kupita kiasi, na ubaradhifu, kwani alikuwa fukara na alihitaji mali ambazo alikuwa amezitumia vibaya. Alilazimika kushuka kutoka katika maisha yake ya anasa ya dhambi hadi kwenye kazi ya chini ya kulisha nguruwe. {3T 101.2}

Baada ya kushuka chini kadiri ilivyowezekana akafikiria fadhili na upendo wa baba yake. Kisha akahisi hitaji la kuwa na baba. Alikuwa amejiweka katika nafasi ya upweke na uhitaji. Uasi na dhambi yake mwenyewe vilimfanya kujitenga na baba yake. Alifikiri juu ya upendeleo na fadhila tele ambazo watumishi wa nyumba ya baba yake walifurahia kwa hiari, wakati yeye ambaye alikuwa amejitenga na nyumba ya baba yake alikuwa akiangamia kwa njaa. Kwa fedheha iliyosababishwa na shida, aliamua kurudi kwa baba yake kwa kukiri kwa unyenyekevu. Alikuwa ombaomba, asiye na mavazi ya starehe au hata ya heshima. Alikuwa mnyonge kwa sababu ya shida na alikuwa amekonda kwa njaa. {3T 101.3}

Wakati kijana alipokuwa akingali mbali na nyumbani kwake, baba yake alimwona, na wazo lake la kwanza lilikuwa juu ya mwanaye huyo mwasi ambaye alikuwa amemwacha miaka mingi iliyopita na kufuata mwenendo wa dhambi ambayo hakuizuia. Hisia za baba zilichochewa. Pamoja na alama zote za unyonge wake baba alitambua sura yake mwenyewe. Hakungoja mtoto wake aje umbali wote kwake, bali aliharakisha kukutana naye. Hakumlaumu mwanawe, bali kwa upole na huruma nyingi, kwamba, kwa matokeo ya mwenendo wake wa dhambi, alijiletea mateso mengi sana, baba aliharakisha kumpatia uthibitisho wa upendo wake na ishara za msamaha wake. {3T 101.4}

Ijapokuwa mwanawe alikuwa amekonda na uso wake ulionesha wazi maisha machafu aliyokuwa amepita, ingawa alikuwa amevaa nguo za ombaomba na miguu yake iliyo pekupeku ikiwa imechafuliwa na vumbi la safari, huruma ya baba yake ilisisimka kwani mtoto huyo alianguka kifudifudi kwa unyenyekevu mbele yake. Baba hakusimama katika hadhi yake, hakuwa na ukali au madai. Hakuweka mbele ya mwanawe mwenendo wake wa zamani wa uovu na dhambi, ili kumfanya ahisi jinsi alivyokuwa amezama. Alimwinua na kumbusu. Alimchukua mwana muasi kifuani mwake na kumfunga vazi lake la kitajiri ili kuficha utupu wake. Alimweka kifuani mwake kwa uchangamfu mwingi, na kudhihirisha huruma kiasi kwamba ikiwa mtoto huyo alikuwa amewahi kutilia shaka wema na upendo wa baba yake, asingeweza kufanya hivyo tena. Ikiwa alikuwa na hisia ya dhambi yake alipoamua kurudi nyumbani kwa baba yake, alikuwa na hisia ya ndani zaidi ya mwenendo wake wa kukosa shukrani alipopokelewa hivyo. Moyo wake, kabla ya kutiishwa,

sasa ulikuwa umevunjika kwa sababu alikuwa amehuzunisha penzi la baba yake. {3T 102.1}

Mwana aliyetubu, ambaye akitetemeka alikuwa akiogopa sana kwamba atakataliwa, hakuwa amejiandaa kwa mapokezi kama hayo. Alijua hakustahili, na hivyo akakubali dhambi yake kwa kumwacha baba yake: "Nimekosa juu ya mbingu, na mbele yako, sistahili kuitwa mwana wako tena." Aliomba tu ahesabiwe kama mtumishi. Lakini baba huyo aliwaomba watumishi wake wamfanyie ishara maalum za heshima na kumvisha kana kwamba amewahi kuwa mwana wake mtiifu. {3T 102.2}

Baba alilifanya tukio la kurejea kwa mwanawe kuwa hafla maalumu ya furaha. Kijana wake mkubwa aliyekuwa shambani na hakujua kuwa mdogo wake amerudi, lakini alisikia maandamano ya jumla ya furaha na akawauliza watumishi maana ya hayo yote. Ilielezwa kwamba kaka yake, ambaye walidhani amekufa, alikuwa amerudi, na kwamba baba yake alikuwa amemchinjia ndama aliyenona kwa sababu alikuwa amempata tena kama ambaye alikuwa amekufa. {3T 102.3}

Ndugu huyo alikasirika na hakutaka kuingia ndani ili kumuona au kumpokea ndugu yake. Hasira yake iliguswa kwamba kaka yake ambaye hakuwa mwaminifu, ambaye alikuwa amemwacha baba yake na kumtupia jukumu zito juu yake la kutimiza majukumu ambayo yalipaswa kugawanywa na wote wawili, sasa anapaswa kupokelewa kwa heshima ya kiasi hicho. Ndugu huyu alikuwa amefuata mwenendo wa ubadhirifu, akipoteza mali ambazo baba yake alikuwa amempatia, mpaka akawa mhitaji, wakati kaka yake nyumbani alikuwa akifanya kwa uaminifu majukumu ya mwana; na sasa mfujaji huyu anakuja nyumbani kwa baba yake na kupokelewa kwa heshima na hadhi kuliko ambavyo yeye mwenyewe alikuwa amewahi kupata. {3T 103.1}

Baba akamsihi mwanawe mkubwa aende akampokee ndugu yake kwa furaha kwa sababu alikuwa amepotea, na sasa amepatikana; alikuwa amekufa katika dhambi na uovu, lakini sasa yu hai tena; amerudi kwenye fahamu zake za maadili na anachukia mwenendo wake wa dhambi. Lakini kijana wake mkubwa anasihi hivi: “Tazama, miaka mingi hii nimekutumikia, wala sikukosa amri yako wakati wowote; wala hukunipa mimi mwana-mbuzi, ili nifanye sherehe na rafiki zangu; amekuja mtoto, ambaye amekula mali yako pamoja na makahaba, nawe umemchinjia ndama aliyenona.” {3T 103.2}

Alimhakikishia mwanawe kwamba alikuwa pamoja naye sikuzote, na kwamba vyote alivyokuwa navyo vilikuwa vyake, lakini ilikuwa sawa kwamba wafanye tukio hili la furaha, kwa maana “ndugu yako alikuwa amekufa, naye yu hai tena; amepatikana." Ukweli kwamba waliopotea wanapatikana, waliokufa wako hai tena, lilizidi mazingatio yote ya baba. {3T 103.3}

Mfano/parablos huu ulitolewa na Kristo kuwakilisha njia ambayo Baba yetu wa mbinguni huwapokea wakosaji na wanaotubu. Baba Ndiye aliyekosewa; lakini

Yeye, kwa huruma ya nafsi Yake, amejaa rehema/sikitiko na msamaha, hukutana na mpotevu na kumuonesha furaha Yake kuu kwamba mtoto Wake, ambaye aliamini kuwa amekufa kwa upendo wote wa kimwana/kibaba, amekuwa na akili ya dhambi yake kubwa na kupuuzwa, na amerudi kwa baba yake, akithamini upendo wake na kukubali madai yake. Anajua kwamba mwanaye ambaye amefuata njia ya dhambi na sasa anatubu anahitaji huruma Yake na upendo Wake. Mtoto huyu ameteseka; amehisi hitaji lake, na anakuja kwa baba yake kama yeye pekee anayeweza kutoa mahitaji haya makubwa. Kurudi kwa mwana mpotevu kulikuwa chanzo cha furaha kuu. Malalamiko ya ndugu mkubwa yalikuwa ya asili, lakini sio sawa. Lakini hii ndiyo njia ambayo ndugu huifuata mara kwa mara dhidi ya ndugu. Kuna juhudi nyingi sana kuwafanya wale walio katika makosa kuhisi pale walipokosea, na kuendelea kuwakumbusha makosa yao. Wale ambao wamekosea wanahitaji huruma, wanahitaji msaada, wanahitaji huruma na upendo. Wanateseka kwa hisia zao, na mara nyingi hukata tamaa na kuvunjika moyo. Zaidi ya yote, wanahitaji msamaha wa huru/bure. {3T 104.1}



SURA YA 11

KAZI MAKANISANI

Katika kazi iliyofanywa kwa kanisa la huko Battle Creek katika kipindi cha joto cha 1870, hakukuwa na utegemezi wote kwa Mungu ambao wakati huo muhimu uliuhitaji. Ndugu R na S hawakumfanya Mungu kuwa tegemeo lao, na kwenda kwa nguvu Zake na kwa neema Yake, na kwa ukamilifu kama ilivyostahili. {3T 104.2}

Wakati Ndugu S anapofikiria kuwa mtu amekosea, mara nyingi huwa mkali sana. Anashindwa kuonesha huruma na kujifikiria ambavyo alipaswa kuonesha kama angekutwa kwenye mazingira hayo hayo. Yeye pia yuko katika hatari kubwa ya kufanya maamuzi mabaya na kukosea katika kushughulika na akili. Kazi hii ya kushughulikia akili, ni kazi njema sana na muhimu mno kuwahi kutolewa kwa binadamu. Wale ambao wanashiriki katika kazi hii wanapaswa kuwa na utambuzi wazi na nguvu nzuri za upambanuzi. Uhuru wa kweli wa akili ni jambo lililo tofauti kabisa na harara. Ubora ule wa uhuru ambao husababisha maoni yenye tahadhari, yenye maombi, na yenye uangalifu mkubwa hayapaswi kutolewa na kusalimishwa kirahisi, hadi pale ushahidi utakapokuwa na nguvu ya kutosha kuhakikisha kuwa tumekosea. Uhuru huu utafanya akili iwe shwari na isiyobadilika katikati ya makosa mengi yanayoendelea kutokea, na itawaongoza wale walio katika nafasi za uwajibikaji kutazama kwa uangalifu ushahidi wa kila upande, na kuwafanya wasibweteke au kupindishwa na ushawishi wa wengine, au na mazingira, na hivyo [kuwa katika hatari ya] kuunda hitimisho bila kushirikisha akili, au bila kuwa na ufahamu kamili wa hali zote. {3T 104.3}

Uchunguzi wa kesi huko Battle Creek ulikuwa kwa kiasi kikubwa ukifuata utaratibu ambao wakili humkosoa shahidi, na kulikuwa na kutokuwepo kwa Roho wa Mungu kulikokusudiwa. Kulikuwa na wachache walioungana katika kazi hii waliokuwa na ari na wenye bidii. Wengine walijihesabia haki na walijiona wamejitosheleza, na shuhuda zao zilitegemewa, na ushawishi wao uliyumbisha uamuzi wa Ndugu R na S. Kwa sababu ya mapungufu madogo, Dada T na U hawakupokelewa kama washirika wa kanisa. Ndugu R na S walipaswa kuwa na maamuzi na upambanuzi ili kuona kwamba pingamizi hizi hazikuwa na uzito wa kutosha kuwazuia dada hawa wasiingie kanisani. Wote wawili wamekuwepo kwenye imani kwa muda mrefu na

walikuwa waaminifu katika utunzaji wa Sabato kwa miaka kumi na nane au ishirini hivi. {3T 105.1}

Dada V, aliyeleta mambo haya, alipaswa kujihoji sababu nzito zaidi za kwa nini hakupaswa kuwa mshiriki wa kanisa. Je! yeye Hakuwa na dhambi? Je! Njia zake zote zilikuwa kamili mbele za Mungu? Je, alikuwa mkamilifu katika uvumilivu, kujikana mwenyewe, uungwana, subira, na utulivu wa hasira? Kama hakuwa na udhaifu wa kawaida wa wanawake, basi alikuwa na uhalali wa kutupa jiwe la kwanza. Wale wakina dada walioachwa nje ya kanisa walistahili kuwa na mahali pao ndani; walikuwa wapenzi wa Mungu. Lakini walishughulikiwa bila busara, na bila sababu ya kutosha. Kulikuwa na wengine ambao kesi zao zilishughulikiwa bila hekima ya mbinguni na bila hata uamuzi wenye busara. Maamuzi ya Ndugu S na nguvu za upambanuzi zimekuwa zikipotoshwa kwa miaka mingi sana kupitia ushawishi wa mkewe, ambaye amekuwa chombo bora zaidi cha Shetani. Kama angekuwa na sifa halisi ya uhuru, angekuwa anajiheshimu vizuri na kwa hadhi yake angejijengea nyumba yake mwenyewe. Anapoanza hatua iliyoundwa ili kudumisha heshima katika familia yake kwa jumla amelibeba jambo hilo kupita kiasi na amekuwa mkali na amezungumza kwa ukali na kwa jeuri kama dikteta. Anapotambua jambo hili baada ya muda kupita, basi huenda upande ule wa pili na kupitiliza kiasi cha kupoteza uhuru wake. {3T 105.2}

Katika hali hii ya akili angepokea taarifa kutoka kwa mkewe, na kuahirisha maamuzi yake, na kudanganywa kwa urahisi na ujanja wa mkewe. Wakati mwingine mkewe alikuwa akijifanya kuwa yeye ndiye ameteswa zaidi na angeelezea shida au ufukara ambao alikuwa amevumilia na jinsi alivyopuuzwa na ndugu zake, wakati mumewe hayupo. Kukwepa kwake mkewe kusema ukweli na sanaa za ujanja za kunyanyasa vibaya akili ya mumewe vimekuwa vikubwa. Ndugu S hajapokea kabisa nuru ambayo Bwana amempa katika nyakati zilizopita juu ya mkewe la sivyo asingeweza kudanganywa naye kama ambavyo amekuwa akidanganywa. Amekuwa akiletwa utumwani mara nyingi na roho ya mkewe kwa sababu moyo na maisha yake binafsi havijatakaswa kikamilifu kwa Mungu. Hisia zake ziliwaka juu ya ndugu zake, naye akawaonea. Ubinafsi ulikuwa haujasulubiwa. Anapaswa kutafuta kwa dhati na bidii kuyaleta mawazo na hisia zake zote kwa utii wa Kristo. Imani na kujikana kungekuwa wasaidizi hodari wa Ndugu S. Kama angejifunga/angezivaa silaha zote za Mungu na kutochagua utetezi mwingine zaidi ya ule ambao Roho wa Mungu na nguvu ya Ukweli vinampa, angekuwa hodari katika nguvu ya Mungu. {3T 106.1}

Lakini Ndugu S ni dhaifu katika mambo mengi. Kama Mungu angemtaka amfunue na kumhukumu jirani, kumkemea na kumsahihisha ndugu, au kupinga na kuwaangamiza maadui zake, ingekuwa kwake kazi ya kawaida na rahisi. Lakini vita dhidi ya ubinafsi, kushinda tamaa na mapenzi ya moyo wake mwenyewe, na kutafuta na kudhibiti nia za siri za moyo, ni vita ngumu zaidi. Yeye hayuko tayari

kuwa mwaminifu katika mashindano kama haya! Vita dhidi ya ubinafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa (kwa kila mtu!). Kujisalimisha mwenyewe, kukabidhi yote kwa mapenzi ya Mungu na kuvikwa unyenyekevu, kumiliki upendo huo ulio safi, wenye amani, na ulio rahisi kushawishiwa, na uliojaa upole na matunda mema, siyo jambo rahisi kulipata. Na bado ni upendeleo kwake na jukumu lake kuwa mshindi kamili hapa duniani. Nafsi ni lazima ijitiishe kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika maarifa na utakatifu wa Kweli. Maisha matakatifu na tabia ya Kristo ni mfano mwaminifu. Imani yake kwa Baba Yake wa mbinguni ilikuwa bila ukomo. Utii na unyenyekevu wake ulikuwa ule usiyopungua na mkamilifu. Yeye hakuja kuhudumiwa, bali kuhudumia wengine. Yeye hakuja kufanya mapenzi Yake Mwenyewe, bali mapenzi ya Yeye aliyemtuma. Katika mambo yote alijitiisha Mwenyewe Kwake Yeye ahukumuye kwa haki. Kutoka kwa midomo ya Mwokozi wa ulimwengu yalisikika Maneno haya: “Mimi siwezi kufanya neno Mwenyewe.” {3T 106.2}

Akawa masikini, na akajifanya Mwenyewe kuwa hana hadhi. Alikuwa na njaa na alikuwa na kiu mara kwa mara, na mara nyingi alikuwa amechoka katika kazi Zake; lakini hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Wakati, vivuli vya baridi vya usiku vilipokusanyika juu yake, mara kwa mara ardhi ndiyo iliyokuwa kitanda chake. Hata hivyo aliwabariki wale waliomchukia. Maisha ya ajabu kiasi gani! Ni uzoefu wa ajabu kiasi gani! Je! Sisi, tunaojidai kuwa wafuasi wa Kristo, tunaweza kuvumilia kwa uchangamfu upweke na mateso kama Bwana wetu, bila manung'uniko? Je! Tunaweza kunywa kikombe na kubatizwa kwa ubatizo huo? Ikiwa ndivyo, tunaweza kushiriki pamoja Naye utukufu Wake katika ufalme Wake wa mbinguni. Ikiwa sivyo, hatutakuwa na sehemu Naye. {3T 107.1}

Ndugu S ana uzoefu wa kujipatia, bila uzoefu huo kazi yake ingepata madhara makubwa. Anaathiriwa sana na kile wengine wanachomwambia juu ya mkosaji; Huamua kulingana na maoni yaliyomo akilini mwake, naye huyashughulikia makosa kwa ukali, wakati ambapo hatua ya kati ingekuwa bora zaidi. Hatilii maanani kwamba udhaifu wake mwenyewe, na ilivyo vigumu kwa mtu kuhoji mwenendo wake, hata anapokosea. Anapoamua kuwa kaka au dada amekosea yeye huwa na nia ya kupitisha jambo hilo kwa kushinikiza lawama yake, ingawa kwa kufanya hivyo anaumiza nafsi yake mwenyewe na kuhatarisha roho za wengine. {3T 107.2}

Ndugu S anapaswa kuachana na majaribu ya kanisa na haipaswi kuwa na chochote cha kufanya katika kutatua shida, ikiwa anaweza kuizuia. Ana karama ya thamani, ambayo inahitajika katika kazi ya Mungu. Lakini anapaswa kujitenga na ushawishi unaovuta huruma zake, unaochanganya maamuzi yake, na unaomwongoza kutenda bila busara. Hii haipaswi na haifai kuwa. Yeye ana imani ndogo sana kwa Mungu. Yeye hukaa sana juu ya udhaifu wake wa mwili na huimarisha kutokuamini kwa kukaa juu ya hisia mbaya. Mungu ana nguvu na hekima aliyoiweka akiba kwa wale wanaomtafuta kwa bidii, wakimwamini kwa imani. {3T 107.3}

Nilioneshwa kuwa Ndugu S ni mtu mwenye nguvu kwenye maeneo fulani, wakati katika maeneo mengine yeye ni dhaifu kama mtoto. Hatua yake katika kushughulika na wakosaji imekuwa na ushawishi wa kutawanya. Ana imani katika uwezo wake wa kufanya kazi katika kuweka mambo katika mpangilio pale anapodhani jambo hilo linahitajika, lakini halitupii jicho kwa umakini jambo hilo. Yeye huifumia kwenye kazi yake roho yake mwenyewe, na hapambanui mambo, na mara nyingi hufanya hivyo bila huruma na upole na kujali. Ana hali ya kutenda jambo kwa kuvuka mpaka (kupitiliza) hasa anapowatendea wengine. “Na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto; na wengine wahurumieni kwa hofu, mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili.” {3T 108.1}

Wajibu, wajibu mkali, anao dada mapacha, ambao ni wema/fadhila. Kama jukumu na wema vimechanganywa, faida iliyokusudiwa itapatikana; lakini ikiwa wajibu umetenganishwa na wema, ikiwa upendo mwororo hautachanganywa na wajibu, kutakuwa na kutofaulu, na madhara mengi yatakuwa ndiyo matokeo. Wanaume na wanawake hawataburuzwa, bali wengi wanaweza kupatikana kwa njia ya wema na upendo. Ndugu S ameshikilia juu mjeledi wa injili, na maneno yake mwenyewe mara kwa mara yamekuwa kama kile chuma kinachonyofoa nyama kinachofungwa mwisho wa mjeledi. Hali hii haikuwa ushawishi wa kuwachochea wengine kuwa na bidii zaidi na kuwafanya wafanye kazi nzuri, lakini imechochea mapambano/ugomvi ili kupunguza ukali wake. {3T 108.2}

Kama ndugu S angetembea nuruni, asingefanya makosa makubwa kama hayo na hivyo kufeli. “Mtu akienda mchana hajikwai; kwa sababu aiona nuru ya ulimwengu huu. Bali akienda usiku hujikwaa; kwa sababu nuru haimo ndani yake.” Njia ya utii ni njia ya usalama. “Aendaye kwa unyofu huenda salama; Bali apotoshaye njia zake atajulikana.” Tembea katika nuru, na “Ndipo utakapokwenda katika njia yako salama, Wala mguu wako hautajikwaa.” Wale ambao hawatembei katika nuru watakuwa na dini dhaifu, iliyodumaa. Ndugu S anapaswa kuhisi umuhimu wa kutembea katika nuru, haijalishi ataisalimisha nafsi yake kwa kiasi gani. Ni juhudi ya dhati, inayosukumwa na upendo kwa ajili ya roho, ambayo huimarisha moyo na kukuza neema. {3T 108.3}

Ndugu yangu, asili yako unajiona uko huru na uliyejitosheleza mwenyewe. Unakadiria uwezo wako wa kutenda, katika viwango vya juu sana kuliko uwezavyo kubeba. Unamwomba Bwana akunyenyekeze ili ufae kwa kazi yake na anapojibu maombi yako na kukuweka chini ya majaribu yaliyo muhimu ya nidhamu na utimilifu wa kitu hicho, mara nyingi unatilia mashaka na kukata tamaa, na unadhani una sababu ya kuvunjika moyo. Wakati Ndugu W alipokuonya na kukuzuia usijishughulishe na shida za kanisa, mara nyingi umehisi kuwa alikuwa akikuzuia. {3T 109.1}

Nilioneshwa kazi zako huko Iowa. Kulikuwapo na kushindwa kwa makusudi ya kukusanya pamoja na Kristo. Uliwavuruga, uliwachanganya, na kuwatawanya

kondoo masikini. Ulikuwa na usongo/juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. Kazi yako haikuwa kwa upendo, lakini ya ukali na isiyo na huruma. Ulikuwa mwenye kudai ukamilifu, mkali na usiyechukuliana na mapungufu. Haukuwatia nguvu wagonjwa na kuwafunga vilema. Ukali wako usiofaa uliwachochea wengine kutoka kwa zizi ambao hawawezi kufikiwa na kurudishwa. Maneno yanayosemwa wakati ufaao ni kama tofaa (apo Mithali 25:11) za dhahabu katika picha za fedha. Maneno yasiyosemwa vizuri ni kinyume chake. Ushawishi wako utakuwa kama mvua ya mawe yenye kuleta uharibifu/ukiwa. {3T 109.2}

Umejihisi kutotulia chini ya vikwazo wakati Ndugu W amekuonya, amekutahadharisha, amekushauri, na kukukemea. Umedhania kuwa kama ungeweza kuwa huru na kuifanya kazi hiyo wewe mwenyewe, basi ungeweza kufanya kazi njema na bora zaidi. Lakini ushawishi wa mke wako umepunguza sana kufaa kwako. Hujatawala/hujasimamia vizuri nyumba yako mwenyewe; umeshindwa kuamuru kaya yako. Umedhania kwamba unajua jinsi ya kusimamia mambo yako ya nyumbani. Lakini jinsi umedanganywa! Mara nyingi umefuata msukumo wa roho yako mwenyewe, ambayo imesababisha mashaka na kukatishwa tamaa, na hizi zimetia giza utambuzi wako na kukudhoofisha kiroho kiasi kwamba kazi zako ziwe na kutokamilika sana. {3T 109.3}

Kazi za Ndugu R na S katika ----- zilikuwa changa. Ndugu hawa walikuwa na uzoefu wao wa zamani wenye makosa uliokuwa mbele yao, ambao ungetosha kuwalinda wasijihusishe na kazi ambayo hawakustahili kuifanya. Kulikuwa na mengi ya kutosha yaliyokuwa yanahitaji kufanywa. Palikuwa mahali pagumu kuanzisha kanisa. Mvuto wa upinzani uliwazunguka kote kote. Kila hatua iliyofanywa ilipaswa kuwa kwa tahadhari na maombi mengi. {3T 110.1}

Hawa ndugu wawili wamekuwa wakionywa na kukemewa mara kwa mara kwa kufanya maamuzi yasiyo na busara, na kwamba hawakupaswa kuchukua majukumu kwa namna walivyoyachukua. Ah, ingekuwa bora zaidi kwa kazi ya Mungu katika _____ kama wangekuwa wakifanya kazi katika maeneo mapya! Kiti cha Shetani kiko -----, na pia katika miji mingine miovu, naye ni adui mjanja tunayepaswa kushindana naye. Kulikuwa na vitu visivyo na mpangilio kati ya watunza Sabato huko ---- ambavyo vilikuwa kikwazo kwa kazi. Lakini kuna wakati unaofaa wa kuongea na kutenda, fursa ya thamani/dhahabu ambayo itaonesha matokeo bora ya kazi iliyofanyika. {3T 110.2}

Kama mambo yangeachwa yakue na kufikia ukomavu kabla hayajaguswa, kungekuwa na utengano wa wale wasio na utaratibu, wasiojitoa, na hakungekuwepo kikundi cha upinzani. Jambo hili linapaswa kuepukwa kwa kadri inavyowezekana. Ni afadhali kanisa lipate uchungu mwingi, na kupitia uzoefu wenye uvumilivu mwingi, kuliko kufanya haraka, katika kuendesha mambo, na kuchochea roho ya malumbano. Wale walioupenda hasa ukweli, kwa ajili ya kuutetea Ukweli huo, walipaswa kufuata msimamo wao wakiwa na utukufu wa

Mungu akilini mwao na kuiruhusu nuru ya Ukweli iangaze mbele ya wote. {3T 110.3}

Wanaweza kutarajia kuwa mambo ya kuchanganyikiwa na kutoridhika kati yao yangewaletea shida. Shetani hangekaa kimya na kuona kundi likiinuka katika ----- ili kudhihirisha Ukweli na kuondosha udanganyifu na makosa. Hasira yake ingewashwa, na angeanzisha vita dhidi ya wale wanaoshika amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu. Lakini hii haikupaswa kuwafanya waumini waaminifu kukosa subira au kuvunjika moyo. Vitu hivi vinapaswa kuwa na ushawishi wa kumfanya mwamini wa Kweli alindwe zaidi, kukesha, na kusali - zaidi ya huruma, sikitiko, na upendo kwa wale ambao walikuwa wakifanya kosa kubwa sana kuhusu vitu vya milele. Kama Kristo alivyovumilia, na anavyoendelea kuchukuliana, na makosa yetu, kutokuwa na shukrani kwetu, na upendo wetu dhaifu, ndivyo tunavyopaswa kuchukuliana na wale wanaojaribu na kupima uvumilivu wetu. Je! Wafuasi wa Yesu anayejikana, anayejitolea muhanga watakuwa tofauti na Bwana wao? Wakristo wanapaswa kuwa na mioyo ya fadhili na uvumilivu.
{3T 110.4

Mpanzi wa Injili

Fumbo la mpanzi wa injili, ambalo Kristo aliliwasilisha mbele ya wasikilizaji Wake, lina somo ambalo tunapaswa kujifunza. Wale ambao wanahubiri Ukweli wa Leo na kutawanya mbegu nzuri watatambua matokeo yaliyo sawa na ya mpanzi wa injili. Madaraja yote yataathiriwa zaidi au kwa upungufu na uwasilishaji wa Ukweli ulio wazi na wenye kusadikisha. Wengine watakuwa wasikilizaji wa njiani. Wataathiriwa na Ukweli uliosemwa; lakini kwa kuwa hawajakuza nguvu za maadili, wamefuata mwelekeo badala ya wajibu, na tabia mbaya zimefanya mioyo yao kuwa migumu hadi imekuwa kama barabara ngumu, iliyokanyagwa-kanyagwa sana. Hawa wanaweza kudai kuuamini Ukweli; lakini hawana hata hisia tu ya tabia yake takatifu, iliyoinuliwa. Hawajitengi kutoka kwenye urafiki wa wapenda anasa na jamii fisadi/mbovu; lakini hujiweka mahali wanapojaribiwa kila wakati, na wanaweza kuwakilishwa na uwanja ambao haujafungwa uzio. Wanaalika vishawishi vya adui na mwishowe hupoteza utambuzi ambao walionekana kuwa nao kwa Ukweli wakati mbegu nzuri ilipoangushwa ndani ya mioyo yao. {3T 111.1}

Wengine ni wasikiaji waliopandwa kwenye mawe (Mat 13). Wanapokea kwa urahisi chochote kipya na cha kufurahisha. Neno la Ukweli wanalipokea kwa furaha. Wanazungumza kwa bidii, na kwa dhati kuhusiana na imani na matumaini yao, na wanaweza hata kutoa karipio kwa wale wenye uzoefu wa muda mrefu kwa upungufu fulani au kwa ukosefu wao wa shauku. Lakini wanapojaribiwa na kudhibitishwa na joto la mateso na majaribu, wakati kisu cha kupogoa cha Mungu kinatumiwa, ili waweze kuzaa matunda kwa ukamilifu, bidii/ari yao inakufa, sauti zao huwa kimya. Hawajivunii tena nguvu na uwezo wa Ukweli. {3T 111.2}

Daraja hili linadhibitiwa na hisia. Hawana kina na utulivu wa tabia. Kanuni haifikii kina kirefu, ikizingatia chemchemi za matendo. Wameuinua Ukweli kwa Neno, lakini siyo watendaji wa hilo Neno. Mbegu ya Ukweli haijaweka mizizi chini kabisa. Moyo haujafanywa upya kwa ushawishi wa kubadilisha wa Roho wa Mungu. Na wakati Ukweli unapohitaji wanaume na wanawake wanaofanya kazi, wakati dhabihu zinapaswa kutolewa kwa ajili ya Ukweli, wako mahali pengine; na majaribu na mateso yanapokuja, huanguka kwa sababu hawana kina cha udongo. Ukweli, Ukweli ulio wa wazi, usiopindapinda, na ulio karibu, huletwa juu ya moyo na kufunua ulemavu wa tabia. Wengine hawatastahimili mtihani huu, lakini mara nyingi hufumbia macho kutokamilika kwao; ingawa dhamiri zao zinawaambia kwamba Maneno yaliyonenwa na wajumbe wa Mungu, ambayo hubeba karibu sana tabia zao za Kikristo, ni Kweli, lakini hawatasikiliza sauti. Wamekasirishwa kwa sababu ya Neno na huuondoa Ukweli badala ya kujisalimisha kwa kutakaswa nao. Wanajifariji kwamba wanaweza kwenda mbinguni kwa njia rahisi. {3T 112.1}

Bado lipo kundi lingine linalowakilishwa katika fumbo hili. Wanaume na wanawake wanaolisikiliza Neno wanashawishika na Ukweli na wanalikubali bila kuona dhambi ya mioyo yao. Upendo wa ulimwengu unashikilia nafasi kubwa katika mapenzi yao. Katika biashara wanapenda kuchukua lile fungu bora zaidi baada ya kubembelezana kwenye bei. Wanazuia, na kwa njia ya udanganyifu na ulaghai wanajipatia mali ambayo itathibitisha kuwa mwiba kwao; kwa kuwa itaangusha malengo na nia zao njema. Mbegu nzuri iliyopandwa mioyoni mwao husongwa. Mara kwa mara wamejawa na masumbufu ya maisha na wasiwasi, wakihofia kuwa hawatapata mali, au kwamba watapoteza kile walichopata, na kwamba hufanya mambo yao ya kidunia kuwa ya msingi. Hawairutubishi ile mbegu njema. Hawahudhurii kwenye mikutano ambayo mioyo yao ingeweza kuimarishwa kwa upendeleo mbalimbali wa kidini. Wanahofia kukutana na upoteaji wa mambo ya kidunia yaliyo ya muda mfupi tu. Udanganyifu wa utajiri unawaongoza kujifariji na kujidanganya kuwa ni jukumu lao kujitaabisha na kupata kila wawezacho/mali, ili wasaidie kazi ya Mungu; na bado wanavyozidisha utajiri wao wa kidunia ndivyo mioyo yao inavyokuwa migumu kuwa mbali na hazina zao, mpaka mioyo yao igeuke kabisa kutoka kwa Ukweli waliopenda. Mbegu nzuri husongwa kwa sababu imejaa wasiwasi wa kilimwengu na wasiwasi usiyohitajika - na upendo kwa anasa za ulimwengu na heshima ambazo utajiri hutoa. {3T 112.2

Ngano na Magugu

Katika fumbo jingine ambalo Yesu aliwasilisha kwa wanafunzi Wake, aliufananisha ufalme wa mbinguni na shamba ambalo mtu alipanda mbegu njema, lakini ambalo, wakati akiwa amelala, adui alipanda magugu. Swali liliulizwa na watumwa wa mwenye nyumba: “Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu? Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye? Akasema, La; msije

mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo. Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu." Kama uaminifu na umakini vingehifadhiwa, kama kusingekuwa na kulala au uzembe wa aina yeyote, adui asingekuwa na nafasi nzuri ya kupanda magugu kati ya ngano. Shetani huwa halali kamwe. Anaangalia, na kuboresha kila fursa na kuwaweka mawakala wake ili wasambaze makosa, ambayo hupata udongo mwema katika mioyo mingi isiyotakaswa. {3T 113.1}

Waumini wa dhati wa Ukweli wanahuzunishwa, na majaribu, na huzuni zao zimeongezeka sana, kutokana na vitu vinavyowaudhi, vinavyowavunja moyo, na vinavyowakatisha tamaa katika juhudi zao. Lakini Bwana angewafundisha waja Wake somo la uangalifu mkubwa katika nyendo zao zote. "Viacheni vyote vikue pamoja." Using'oe magugu kwa kuyavuta kwa nguvu yasije katika kung'oka kwake yale majani mateke yakalegea. Wachungaji na washiriki wa kanisa wote kwa pamoja wanapaswa kuwa waangalifu sana, wasije wakawa na juhudi isiyolingana na maarifa. Kuna hatari ya kufanya mengi ili kuponya magumu yaliyo katika kanisa, ambayo, kama yangeachwa yenyewe, yangeweza kujifanyia tiba yenyewe. Ni sera mbovu kushughulikia mambo katika kanisa ambayo hayajakomaa vya kutosha. Tunapaswa kuwekeza uangalifu mkubwa, uvumilivu, na kujitawala nafsi katika kuchukuliana na mambo haya, ili tusiende kufanya kazi kwa roho zetu wenyewe kwa nia ya kuyaweka sawa. {3T 113.2}

Kazi iliyofanywa ----- ilifanywa kabla haijakomaa na ilisababisha utengano wa mapema kwenye lile kanisa dogo. Kama watumishi wa Mungu wangeweza kuhisi nguvu ya somo la Mwokozi wetu katika mfano wa ngano na magugu, wasingeifanya kazi kwa namna walivyoifanya. Kabla hatua za kuwatoa wale ambao hawafai kabisa hazijachukuliwa, muda utolewe wa wao kutoa malalamiko yao juu ya kuondolewa kwao kanisani, na jambo hilo daima lifanyike kwa uangalifu mkubwa na maombi mengi ya dhati. Hatua zilizochukuliwa huko ----- zilizalisha vikundi vya upinzani. Wengine walikuwa kama wale wasikiaji wa njiani, wengine walikuwa wasikiaji wa kwenye mwamba, na wengine walikuwa wake kundi lililopokea Ukweli wakati moyo ulikuwa na ukuaji wa miiba ambayo iliiisonga mbegu nzuri - hizi hazingeweza kukamilisha wahusika wa Kikristo. Lakini kulikuwa na wachache ambao wangeweza kulishwa na kutiwa nguvu, na kuwasaidia kusimama katika Ukweli. Lakini nafasi zilizochukuliwa na Ndugu R na S zilileta shida ya mapema, halafu kulikuwa na ukosefu wa hekima na uamuzi katika kusimamia kikundi. {3T 114.1}

Kama watu wanastahili kutengwa na kanisa kama Shetani alivyotengwa kutoka mbinguni, watakuwa na watu wanaowaunga mkono na kuwahurumia. Daima kuna watu wa kundi linaloathiriwa zaidi na watu binafsi kuliko wanavyoshawishiwa na Roho wa Mungu na kanuni nzuri; na, katika hali yao ya kutoongoka, hawa huwa tayari kusimama upande wa makosa na kuonesha huruma na kuwasikitikia wale

ambao hawakustahili. Hawa wahurumiaji wana ushawishi mkubwa na wengine; mambo huonekana katika nuru iliyopotoka, madhara makubwa yamefanyika, na roho nyingi zimeharibiwa. Shetani katika uasi wake alichukua theluthi moja ya malaika. Waligeuka kutoka kwa Baba na kutoka kwa Mwanawe, na kuungana na mchochezi wa uasi. Tukiwa na Ukweli huu mbele yetu tunapaswa kusonga mbele kwa tahadhari kubwa. Tunatarajia nini isipokuwa majaribu na kuchanganyikiwa katika uhusiano wetu na wanaume na wanawake wa akili za kipekee? Tunapaswa kutambua hili na kuepuka ulazima wa kung'oa magugu, isije ngano nayo ikang'oka. {3T 114.2}

"Ulimwenguni mnayo dhiki," asema Kristo; lakini ndani Yangu mtakuwa na amani. Majaribu ambayo Wakristo wanakabiliwa katika huzuni, shida, na aibu ni njia iliyoteuliwa na Mungu kutenganisha makapi na ngano. Kiburi chetu, ubinafsi, tamaa mbaya, na kupenda raha za ulimwengu lazima vyote vishindwe; kwa hivyo Mungu hututumia mateso ili kutujaribu na kututhibitisha, na kutuonesha kuwa maovu haya yapo katika tabia zetu. Lazima tushinde kupitia nguvu na neema Yake, tupate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, tukiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. "Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu," asema Paulo, "yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." Mateso, misalaba, majaribu, shida, ufukara na majaribu yetu mbalimbali ni wafanyakazi wa Mungu kutusafisha, kututakasa, na kutufanya tufae kwenye ghala la mbinguni. {3T 115.1}

Madhara yaliyofanywa kwa kazi ya Ukweli kwa hatua za mapema zisizongoja mambo kukomaa haziwezi kurekebishwa kabisa. Kazi ya Mungu katika ----- haijasonga mbele kama ilivyotakiwa, na haitasimama kama taa nzuri mbele ya watu kama ilivyotakiwa kuwa kabla kazi hii haijafanywa. Mara kwa mara kuna watu kati yetu ambao ushawishi wao unaonekana kuwa ni ujinga tu kwenye upande wa haki. Maisha yao yanaonekana kuwa yasiyo ya faida; lakini wacha wawe waasi na wapambanaji, na wanakuwa wafanyakazi wenye bidii wa Shetani. Kazi hii kwa kiasi kikubwa inategemea hisia za moyo wa asili. Kuna haja kubwa ya kujichunguza mwenyewe na kuwa na maombi ya faragha. Mungu ameahidi hekima kwa wale wanaomuomba. Kazi ya umishenari mara kwa mara huingiwa na wale ambao hawajajiandaa kwa kazi hiyo. Bidii ya nje huchochewa, wakati sala ya faragha ikipuuzwa. Wakati hali ni hiyo, madhara mengi hufanywa, kwa kuwa kazi hizi hutafuta kurekebisha dhamiri za wengine kwa kutumia kanuni/sheria yao wenyewe. Kujitawala nafsi kunahitajika sana. Maneno ya haraka huchochea ugomvi. Ndugu S yuko katika hatari ya kuingiza roho ya ukosoaji mkali. Hili haliwafanyi kuwa wahudumu wa haki. {3T 115.2}

Ndugu S, una mengi ya kujifunza. Umekuwa na mwelekeo wa kuyaelekeza mashtaka ya kushindwa kwako na kukatishwa tamaa kwako kwa Ndugu W, lakini uchunguzi wa karibu wa nia yako na hatua za mwenendo wako utafunua sababu

zingine zilizo ndani yako kutokana na hali hii ya kukatishwa tamaa. Kufuatia mwelekeo wa moyo wako mwenyewe wa asili hukuleta katika hali ya utumwa. Roho kali, ya kutesa ambayo wakati mwingine umekuwa ukiiendekeza huondoa mvuto wako. Ndugu yangu, una kazi ya kujifanyia mwenyewe ambayo hakuna mwingine anayeweza kukufanyia. Kila mmoja lazima atoe hesabu yake mwenyewe kwa Mungu. Yeye Ametupatia sheria Yake kama kioo ambacho twaweza kukitazama na kugundua mapungufu yalyo katika tabia zetu. Hatupaswi kuangalia kioo hiki kwa kusudi la kuona makosa ya jirani yetu yanavyoonekana, au kuangalia ili kuona kama mwingine anafikia kiwango hicho, lakini kuangalia ili kuona kasoro zilizo ndani yetu, ili tuweze kuziondoa. Maarifa siyo yote tunayohitaji; tunapaswa tufuate nuru. Hatuachwi kuchagua wenyewe na kutii yale ambayo yanakubalika kwetu na kutotii pale inapoonekana inachukuliana na hali zetu. Utii ni bora kuliko dhabihu. {3T 116.1}

SURA YA 12

KWA WAZAZI MATAJIRI

Kwenye mkutano wa kambi huko Vermont, mnamo 1870, nilihisi nikihimizwa na Roho wa Mungu kutoa ushuhuda ulio wazi kuhusiana na jukumu la wazazi wazee na wazazi matajiri kuhusiana na mali zao. Nilioneshwa kwamba wanaume wengine

ambao ni wajanja/hila, wenye busara, na walio makini kwa shughuli za biashara kwa ujumla, wanaume wanaotambulika kwa wepesi na usahihi, kuhusiana na matumizi bora ya mali zao wakati wa uhai wao, hawajui ni mapema kiasi gani mlango wao wa rehema waweza kufungwa; na bado wanavuka mwaka hadi mwaka mwingine huku biashara zao zikiwa hazijawekwa kwa usawa/utulivu, na mara nyingi maisha yao hukoma wakiwa hawajatumia hawana uwezo wa maamuzi. Au wanaweza kufa ghafla, bila kuwapo kwa onyo lolote, na mali zao kutumika katika namna ambayo wao wenyewe wasingeiafiki. Hawa wana hatia ya uzembe; hawa ni mawakili wasiyo na uaminfu. {3T 116.2}

Wakristo wanaoamini Ukweli wa leo wanapaswa kudhihirisha hekima na uwezo wa kuona mbali. Hawapaswi kupuuza mwelekeo wa mali zao, wakitarajia fursa nzuri ya kurekebisha biashara zao wakati wawapo kwenye ugonjwa wa muda mrefu. Biashara zao zinapaswa kuwa katika hali ambayo, kama wangetakiwa kuziacha wakati wowote, na kama hawangekuwa na sauti katika mpangilio wake, zingeweza kuendelea vizuri kwa namna ile ile ambayo ingekuwa kama wangekuwa hai. Familia nyingi katika hali ya kutokuwa waaminifu zimeibiwa mali zao zote na kukumbwa na umaskini kwa sababu kazi ambayo ingeweza kufanywa vizuri kwa saa moja imekuwa ikipuuzwa. Wale wanaotengeneza wosia wao wasiogope kupata maumivu au gharama ili kupata ushauri wa kisheria ili wawe katika hali ambayo itawaasa kulishinda jaribu hili. {3T 117.1}

Niliona kwamba wale wanaodai kuamini Ukweli wanapaswa kuonesha imani yao kwa matendo yao. Wanapaswa, pamoja na matajiri wasio waadilifu, kufanya urafiki, ili mwishowe wapokewe katika makao ya milele. Mungu amewafanya wanadamu kuwa wasimamizi wa mali. Yeye Amewapa mikononi mwao pesa za kuendeleza kazi kuu ya wokovu wa roho ambao kwa ajili ya huo, Kristo aliacha makao Yake, utajiri Wake, utukufu Wake, na kuwa maskini ili, kwa kujishusha Kwake na kujitoa Kwake Mwenyewe, awalete wana na binti wengi wa Adamu kwa Mungu. Katika majaliwa Yake Bwana ameagiza kwamba kazi katika shamba lake la mizabibu idumishwe kupitia mali iliyokabidhiwa mikononi mwa wasimamizi Wake. Kupuuzia kwa upande wao kujibu wito wa kazi ya Mungu katika kutekeleza kazi Yake kunawaonesha kuwa ni watumishi wazembe, wasio na maadili na wavivu. {3T 117.2}

Nilioneshwa baadhi ya mambo kuhusiana na kazi kule Vermont, lakini hasa kule Bordoville na ujirani. Haya yafuatayo ni kutoka Shuhuda kwa Kanisa namba 20: {3T 118.1}

“Kuna kazi inayotakiwa kutekelezwa kwa wengi waishio Bordoville. Niliona kwamba adui alikuwa akifanya kazi kwa bidii ili kuendeleza makusudi Yake. Watu ambao Mungu amewapa talanta za utajiri wamezihamishia kwa watoto wao jukumu ambalo Mbingu ziliwapatia la kuwa mawakili wa Mungu. Badala ya kumpa Mungu vitu ambavyo ni Vyake, wanadai kwamba kila walichonacho ni chao, kana

kwamba ni kwa uweza wao na kwa nguvu zao na kwa hekima zao wamepata mali zao." {3T 118.2}

"Wengine huweka mali zao mahali wasipoweza kuifikia kwa kuiweka mikononi mwa watoto wao. Nia yao ya siri ni kujiweka katika nafasi ambayo hawatahisi kuwajibika kutoa mali zao kueneza Ukweli. Hawa hupenda kwa Neno, lakini si kwa matendo na Kweli. Hawatambui kuwa zile pesa wanazoshikilia ni za Bwana, na siyo zao wenyewe." {3T 118.3}

"Wazazi wanapaswa kuwa na hofu kubwa katika kuwakabidhi watoto wao talanta za mali ambazo Mungu ameziweka mikononi mwao, isipokuwa pale wanapokuwa uhakikisho mkubwa na ushahid kwamba watoto wao wana hamu kubwa, wanapenda, na kujitoa kwa ajili ya Mungu kuliko wao wenyewe, na kwamba watoto hawa watakuwa wenye juhudi zaidi, unyofu na bidii katika kupeleka mbele kazi ya Mungu, na ukarimu/wema zaidi katika kuendeleza mbele shughuli mbali mbali zilizounganishwa nayo ambazo zinahitaji mali. Lakini wengi huweka mali zao mikononi mwa watoto wao, na hivyo hutupa juu yao jukumu la uwakili wao wenyewe, kwa kuwa Shetani huwahimiza kuifanya. Kwa kufanya hivyo wanaweka mali hiyo katika safu ya adui. Shetani hufanya jambo hilo ili kukidhi makusudi yake mwenyewe na huiweka mbali na kazi ya Mungu mali iliyohitajika, ili iweze kutekelezwa vizuri kazi yake mwenyewe-adui." {3T 118.4}

"Wengi waliokiri imani kwa juu juu wana upungufu katika matendo mema. Kama wangeonesha imani yao kupitia matendo yao wangeweza kuwa na ushawishi mkubwa upande wa Ukweli. Lakini hawakuzi talanta za mali waliyoazimwa na Mungu. Wale wanaofikiria kupunguza ukali wa dhamiri zao kwa kuwamilikisha mali zao watoto wao, au kwa kuzizuia zisifanye kazi ya Mungu na kuzipitisha mikononi mwa watoto wasioamini, na wazembe ili wazifuje, kuzizuia, na kuziabudu, watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu; wao ni mawakili wasiyo waaminifu wa pesa za Bwana wao. Wanamruhusu Shetani kuwatawala kupitia watoto hawa, ambao akili zao ziko chini ya udhibiti wake. Madhumuni ya Shetani yametimizwa kwa namna nyingi, wakati mawakili wa Mungu wanaonekana wameshikwa na butwaa na kupooza; hawatambui jukumu lao kubwa na hesabu ambayo watapaswa kuitoa hivi karibuni." {3T 118.5}

Nilioneshwa kwamba mlango wa rehema kwa baadhi katika maeneo ya karibu ya ---- ulikuwa karibu ufungwe, na ilikuwa muhimu kwamba kazi yao ikamilike katika viwango vya kukubaliwa na Mungu, ili kwamba katika makazi ya mwisho waweze kusikia sauti "Vema mtumwa mwema" kutoka kwa Bwana mkubwa. Nilioneshwa pia kutokuwa na uthabiti kwa wale wanaodai kuamini Ukweli wakizuia mali zao kwa kazi ya Mungu, ili waiache kwa watoto wao. Baba na mama wengi ni maskini katikati ya ukwasi. Wanajinyima, kwa kiwango kikubwa, starehe zao za binafsi na mara nyingi hujikana mambo ambayo ni muhimu kwa starehe (comfort) za maisha na afya, wakati walikuwa na uwezo wa kujiamulia mambo hayo. Wanadhani

hairuhusiwi, kama ilivyokuwa, kutumia mali zao kwa starehe zao au kwa makusudi ya kutoa msaada. Wana kusudi moja mbele yao, na kusudi hilo ni kuokoa mali ili wawaachie watoto wao. Wazo hili ni lenye kipaumbele sana, lililofungamanishwa sana na matendo yao yote, kwamba watoto wao hufunza kutarajia wakati ambapo mali hii itakuja kuwa yao. Wanangojea kwa hamu kuhusu mali hiyo, na matarajio haya yana ushawishi muhimu lakini siyo mzuri kwa tabia zao. Wengine wanakuwa wanyang'anyi wa matumizi, wengine huwa wabinafsi na wenye tamaa, na wengine wanakua wavivu na wazembe. Wengi hawakuzi tabia za uchumi; hawatafuti kuwa watu wanaojitegemea. Hawana malengo, na wana utulivu mdogo wa tabia. Mivuto iliyopokelewa utotoni na katika kipindi cha ujana inaletwa katika uundaji wa tabia na kuwa kanuni kuu ya matendo katika maisha ya utu uzima. {3T 119.1}

Wale waliozoea kanuni za Ukweli wanapaswa kufuata kwa karibu Neno la Mungu kama mwongozo wao. Wanapaswa kumpa Mungu vile vilivyo vya Mungu. Nilioneshwa kuwa kuna baadhi huko Vermont walikuwa wakifanya kosa kubwa kwa kuzitumia vibaya mali ambazo Mungu alikuwa amewakabidhi. Walikuwa wakipuuza madai ya Mungu juu ya kila kitu walicho nacho. Macho yao yalipofushwa na adui wa haki, na walikuwa wakichukua mwenendo ambao ungewasababishia madhara wao wenyewe na watoto wao wapendwa. {3T 120.1}

Watoto walikuwa wakishawishi wazazi wao kuacha mali zao mikononi mwao ili wazitumie kulingana na maamuzi yao. Licha ya mwanga wa Neno la Mungu, kuwa wazi na dhahiri kuhusiana na pesa zilizosimamiwa na wasimamizi/mawakili na yakiwapo maonyo ambayo Mungu ametoa kupitia Ushuhuda juu ya utafutaji wa mali – hata ikiwa, baada ya nuru yote hii kuwa mbele yao wote, watoto kwa njia ya moja kwa moja au kwa kupitia njia nyingine isiyo ya moja kwa moja huwashawishi wazazi wao wawagawie mali zao wakiwa hai, au kuandika wosia kwamba mali hizo ziwekwe mikono mwao mara tu baada ya kifo cha wazazi wao, wanachukua juu yao wenyewe jukumu la kutisha. Watoto wa wazazi waliozeeka wanaodai kuuamini Ukweli wanapaswa, kwa hofu ya Mungu, kuwashauri na kuwasihi wazazi wao kuwa waaminifu kwa madai yao ya imani, na kuchukua hatua ambazo Mungu ataridhia, kuhusu mali zao. Wazazi hawapaswi kujizuia kuweka hazina yao wenyewe mbinguni na kujitwalia fedha zao wenyewe badala ya kufanya maendeleo ya kazi ya Mungu. Hawapaswi kujizuilia wao wenyewe hazina ya mbinguni kwa kuacha ziada ya mali kwa wale walio na mali za kutosha; kwani kwa kufanya hivyo siyo tu wanajinyima fursa ya thamani isiyoshindwa ya kuweka hazina mbinguni, bali wanaiibia hazina ya Mungu. {3T 120.2}

Nilisema kwenye mkutano wa makambi kwamba wakati mali inapoandikiwa wosia kuwa ya watoto, wakati hakuna inayotengwa kwa kazi ya Mungu, au, ikiwa ipo, basi ni pesa ndogo ambayo haistahili kutajwa/kuorodheshwa, mali hii itageuka kuwa laana kwa watoto watakaoirithi. Itakuwa chanzo cha majaribu na ingefungua

mlango ambao kupitia huo wangekuwa katika hatari ya kuanguka katika tamaa nyingi za hatari. {3T 120.3}

Wazazi wanapaswa kutumia mamlaka/haki ambayo Mungu amewapa. Aliwakabidhi talanta ambazo angewataka wazitumie kwa utukufu Wake. Watoto hawakupaswa kuwajibika kwa talanta za baba. Ingawa wana akili timamu na maamuzi ya busara, wazazi wanapaswa, kwa kuzingatia kwa njia ya maombi, na kwa msaada wa washauri sahihi ambao wana uzoefu katika Ukweli na ujuzi wa mapenzi ya Mungu, kupanga mali yao. Ikiwa wana watoto wanaoteseka au wanaohangaika katika umasikini, na ambao wangetumia mali kwa busara, hawa wangepaswa kufikiriwa hao. Lakini ikiwa wana watoto wasioamini ambao wana utajiri mwingi wa ulimwengu huu, na ambao wanautumikia ulimwengu, wanafanya dhambi dhidi ya Bwana, aliyewafanya kuwa mawakili Wake, kwa kuweka mali mikononi mwao kwa sababu tu ni watoto wao. Madai ya Mungu hayapaswi kuchukuliwa kwa wepesi. {3T 121.1}

Na inapaswa kueleweka wazi kuwa, kwa sababu wazazi wameandika wosia wao, hii haitawazuia kutoa mali kwa kazi ya Mungu wakati wa uhai wao. Hili wanapaswa kulifanya. Wanapaswa kuridhishwa na jambo hilo hapa, na kupata thawabu ya baadaye, kwa kuratibu ziada ya mali yao wakati wakiwa hai. Wanapaswa kufanya sehemu yao ili kuendeleza kazi ya Mungu. Wanapaswa kutumia mali waliyoazimwa na Bwana kutekeleza kazi ambayo inahitaji kufanywa katika shamba Lake la mizabibu. {3T 121.2}

Upendo wa fedha upo kwenye mzizi wa karibu uhalifu wote uliofanywa ulimwenguni. Akina baba ambao kwa ubinafsi huzuia mali zao ili kuwatajirisha watoto wao, na wasiyoona mahitaji ya kazi ya Mungu na kuyashughulikia, hufanya makosa ya kutisha. Watoto wanaofikiria kuwabariki na mali zao hulaaniwa na mali hizo. {3T 121.3}

Fedha iliyoachwa kwa watoto mara nyingi huwa mzizi wa uchungu. Mara nyingi watoto hugombana juu ya mali waliyoachiwa na ikiwa kuna wosia, mara chache wote kuridhika na mgawanyo uliofanywa na baba. Na badala ya mali iliyoachwa kuibua shukrani na ucha Mungu inapokumbukwa, husababisha kutoridhika, kunung'unika, wivu, na kutoheshimiana. Kaka na dada waliokuwa na amani miongoni mwao wakati wa nyuma, hutofautiana, na mifarakano ya familia mara nyingi huwa ni matokeo ya mali za kurithi. Utajiri unatamanika kama tu njia ya kusaidia kukidhi mahitaji ya sasa na kama njia ya kuwatendea mema wengine. Lakini utajiri wa kurithi mara nyingi huwa mtego kwa aliye nao, kuliko kuwa mbaraka. Wazazi hawapaswi kuwafanya watoto wao wakutane na vishawishi ambavyo wanawasababishia kwa kuwaachia mali ambayo wao wenyewe hawakufanya juhudi yoyote kuipata. {3T 121.4}

Nilioneshwa kuwa baadhi ya watoto wanaodai kuamini Ukweli, kwa njia isiyo ya moja kwa moja, wangemshawishi baba kuweka mali zake kwa watoto wake badala

ya kuzitumia kwa kazi ya Mungu wakati wa uhai wake. Wale waliomshawishi baba yao kuhamishia uwakili wake kwao, (masikini!) hawajui wanachofanya. Wanajikusanyia wenyewe jukumu maradufu, lile la kupindisha akili ya baba yao ili asitimize kusudi la Mungu katika kutumia mali alizoazimwa na Mungu ili azitumie kwa utukufu Wake, na jukumu la ziada la kuwa mawakili wa mali ambayo ilipaswa kutolewa kwa wabadilishaji na baba, ili Bwana mkubwa aweze kupokea iliyo yake na riba. {3T 122.1}

Wazazi wengi hufanya kosa kubwa katika kutoa mali zao kutoka mikononi mwao na kuweka mikononi mwa watoto wao wakati wao wenyewe wakiwa na jukumu la matumizi mabaya ya talanta waliyoazimwa na Mungu. Wazazi wala watoto huwa hawafurahishwi na uhamishaji huu wa mali. Na wazazi, kama wataishi miaka michache zaidi, kwa ujumla watajutia tendo hili kwa upande wao. Upendo wa wazazi kwa watoto wao hauongezwi kwa hatua hii. Watoto hawahisi kuongezeka kwa moyo shukrani na wajibu kwa wazazi wao kwa ukarimu wao. Laana huonekana kuwa kwenye mizizi ya jambo lenyewe, ambalo huzaa tu ubinafsi kwa upande wa watoto na kutokuwa na furaha na hisia mbaya za utegemezi ulio finyu kwa upande wa wazazi. {3T 122.2}

Kama wazazi, wakati wa uhai wao, wangewasaidia watoto wao kujisaidia (elimu, mtaji, ardhi n.k), ingekuwa bora kuliko kuwaachia kiasi kikubwa [cha mali hadi] wakati wa mauti. Watoto ambao wameachwa kutegemea zaidi/rasilimali na juhudi zao, hufanya vyema kuliko wanaume na wanawake na hujiweka katika mazingira bora zaidi ya maisha halisi kuliko watoto wale waliotegemea mashamba ya baba zao. Watoto walioachwa wategemee rasilimali zao wenyewe kwa kawaida hunoa uwezo wao, huboresha fursa/upendeleo wao, na hukuza na kuelekeza vitivo vyao ili kukamilisha kusudi maishani. Mara nyingi hukuza stadi za kazi ya bidii na tabia za kazi za mikono, kubana matumizi, kujiwekea akiba, na thamani ya maadili, ambavyo ndiyo msingi wa mafanikio katika maisha ya Kikristo. Wale watoto ambao wazazi wao hufanya zaidi, mara nyingi huwa na hisia za chini za wajibu kwa [wazazi wao]. Makosa ambayo tumekuwa tukiyazungumza yamekuwepo katika----Wazazi wamehamisha uwakili wao juu ya watoto wao (watoto wawafanyie uamuzi wa mali zao badala ya kufanya wajibu wao kwa Mungu). {3T 122.3}

Kwenye mkutano wa makambi huko -----, 1870, nilitoa wito kwa wale waliokuwa na mali kutumia mali hizo kwa kazi ya Mungu kama mawakili Wake waaminifu, na kutoiacha kazi hii kwa watoto wao. Ni kazi ambayo Mungu amewaachia ili wafanye, na wakati Bwana atakapowataka kutoa hesabu, wanaweza, kama mawakili waaminifu, kumrudishia yale aliyowaazimisha, yaani mtaji na faida. {3T 123.1}

Ndugu X, Y, Z waliwasilishwa mbele yangu. Watu hawa walikuwa wanafanya makosa katika kupanga matumizi ya mali zao. Baadhi ya watoto wao walikuwa wanatoa ushawishi katika kazi hii, na walikuwa wakikusanya juu ya nafsi zao majukumu ambayo hawakuwa tayari kuyabeba. Walikuwa wakifungua mlango na

kumkaribisha adui aingie na vishawishi vyake ili kuwasumbua, kuwanyanyasa na kuwaangamiza. Wana wawili wadogo wa Ndugu X walikuwa katika hatari kubwa zaidi. Walikuwa wakishirikiana na watu wenye mtindo wa tabia ambayo haingeweza kuwainua, bali ingewashusha. Ushawishi wa hila wa ushirikiano huu ulikuwa unazidi kupata ushawishi usiyoonekana kirahisi juu ya vijana hawa. Mazungumzo na namna ya ushirika wa uovu vilikuwa vya tabia ile inayowatenganisha na ushawishi wa dada zao na waume wa dada zao. Nilipokuwa nikiongea juu ya mada hii kwenye mkutano wa makambi nilipata hisia za kina sana. niliwatambua watu waliokuwa mbele yangu niliokuwa nimewaona kwenye maono. Niliwahimiza wale ambao walinisikia umuhimu wa kujitolea kabisa kwa Mungu. Sikuita majina, kwa sababu sikuruhusiwa kufanya hivyo. Ilibidi nizingatie kanuni, nisihi/nivute mioyo na dhamiri, na kuwapa wale ambao walidai kumpenda Mungu na kushika amri Zake nafasi ya kukuza tabia. Mungu angewatumia maonyo na maonyo, na ikiwa kweli walitamani kufanya mapenzi Yake walipata fursa. Nuru ilipewa, na kisha tulilazimika kusubiri na kuona ikiwa watakuja kwenye nuru. {3T 123.2}

Niliondoka kwenye mkutano wa makambi nikiwa na mzigo wa wasiwasi akilini mwangu kwa kurejelea watu ambao hatari yangu nilikuwa nimeoneshwa. Katika miezi michache habari zilitufikia juu ya kifo cha Ndugu Y. Mali yake iliachwa kwa watoto wake. Mnamo Desemba iliyopita tulikuwa na miadi ya kufanya mikutano huko Vermont. Mume wangu alikuwa mgonjwa na hakuweza kwenda. Ili kujipunguzia kukatishwa tamaa kukubwa sana, nilikubali kwenda Vermont nikishirikiana na Dada Hall. Nilizungumza na watu na uhuru fulani, lakini mikutano yetu ya konferensi haikuwa ya bure. Nilijua kwamba Roho wa Bwana hangeweza kuwa na uhuru mpaka maungamo yatolewe na kuwe na kupondeka/kuvunjika kwa moyo mbele za Mungu. Sikuweza kukaa kimya. Roho wa Bwana alikuwa juu yangu, na nilielezea kwa kifupi kiini cha kile nilichoandika. Niliita majina ya wengine waliokuwepo ambao walikuwa wamesimama katika njia ya kazi ya Mungu. {3T 124.1}

Matokeo ya kuacha mali kwa watoto kwa mapenzi, na pia ya wazazi kuhamishia jukumu la usimamizi wao juu ya watoto wao wakati wazazi walikuwa wakiishi, ilikuwa imethibitishwa mbele yao. Tamaa ilikuwa imesababisha wana wa Ndugu Y kufuata njia mbaya. Hii ilikuwa kweli hasa kwa mmoja wa wanawe. Nilifanya kazi kwa uaminifu, nikisimulia vitu ambavyo nilikuwa nimeona akimaanisha kanisa, haswa kwa wana wa Ndugu Y. Mmoja wa ndugu hawa, yeye mwenyewe akiwa baba, alikuwa ameharibika moyoni na maishani, na kuwa laumu kwa kazi ya thamani ya Ukweli wa leo; viwango vyake vya chini vya maadili vilikuwa vinaharibu vijana. {3T 124.2}

Roho wa Bwana alikuja kwenye mikutano, na maungamo ya unyenyekevu yalifanywa na baadhi, yaliyoandamana na machozi. Baada ya mkutano huo

nilikuwa na mahojiano na watoto wadogo wa Ndugu X. Niliwasihi, na kuwahimiza kwa ajili ya wokovu wa roho zao, wajitenge na ushirika wa wale ambao walikuwa wakiwaongoza kwenye uharibifu, na kutafuta mambo yatakayosababisha amani yao. Nilipokuwa nikiwasihi vijana hawa, moyo wangu ulivutwa kuwaelekea, nami nilikuwa na shauku ya kuwaona wakimtii Mungu. Niliwaombea, na kisha nikawasihi wajiombee wao wenyewe. Tulikuwa tunapata ushindi; walikuwa wanaelekea kujitoa. Sauti ya kila mmoja ilisikika ikipaa kwa maombi ya unyenyekevu, ya toba, na nilihisi kwa kweli amani ya Mungu ikituama juu yetu. Malaika walionekana kutuzunguka, na nilikuwa nimefungwa katika maono ya utukufu wa Mungu. Hali ya kazi kule ----- ilioneshwa tena kwangu. Niliona kwamba baadhi yao walikuwa wamerudi nyuma mbali na Mungu. Vijana walikuwa katika hali ya kurudi nyuma. {3T 124.3}

Nilioneshwa kwamba wana wawili wadogo wa Ndugu X walikuwa kwa asili ni wenye dhamiri na moyo mwema, vijana wenye bidii, lakini ambao Shetani alikuwa amewapofusha mtazamo wao. Mafungamano yao hayakuwa ya watu ambao wangeimarisha na kuboresha maadili yao au kuongeza uelewa wao na upendo kwa Ukweli na vitu vya mbinguni. “Lakini mkosaji mmoja huharibu mema mengi.” Dhihaka na mazungumzo mabaya ya masahaba hawa yalikuwa na athari yake ya kuondoa alama za dhati za kidini. {3T 125.1}

Ni makosa kwa Wakristo kushirikiana na wale ambao maadili yao ni ya kiwango cha chini. Kujuana kwa undani, na ukaribu wa kila siku unaochukua muda usiyochangia kwa lolote nguvu za akili au za kimaadili/kiroho ni jambo la hatari. Ikiwa mazingira ya kimaadili/kiroho yanayowazunguka watu siyo safi na yasiyotakaswa, bali yaliyochafuliwa na ufisadi, wale wanaopumua hali hii watagundua kuwa hufanya kazi akilini na moyoni ili kutia sumu na kuharibu. Ni jambo la hatari kuzungumza na wale ambao akili zao kwa kawaida huchukua misimamo inayoelekea chini (maadili mabaya). Taratibu na bila wao kutambua, wale ambao kwa asili wana dhamiri zilizo hai na wanapenda usafi wa moyo watakuja katika kiwango hicho hicho na kushiriki pamoja na kuhurumia ukosefu wa adabu na utasa wa kimaadili wanaokutana nao katika mawasiliao ya kila wakati. {3T 125.2}

Ilikuwa muhimu kwamba ushirikiano na vijana hawa ungebadilika. “Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema.” Shetani amefanya kazi kupitia mawakala kuwaharibu vijana hawa. Hakuna kitu kinachoweza kuzuia kwa ufanisi zaidi au kuzuia hisia kali na matamanio mema kuliko kushirikiana na watu batili, wapuuzi, wazembe, na wenye nia mbaya. Haijalishi ni vivutio gani watu hawa wanaweza kumiliki kwa kutumia busara zao, kejeli, kushushua na kufurahisha, ule ukweli kwamba wanaichukulia dini (mambo ya kiroho) kwa wepesi na kwa kutoijali ni sababu tosha ya kwa nini tusishirikiane nao. Wanapojishughulisha zaidi katika mambo mengine, ndivyo ushawishi wao unavyopaswa kuogopwa kama wenzi, kwa

sababu wanaleta mvuto usiyo wa kidini na mivuto mingine mingi ya hatari. {3T 125.3}

Vijana hawa wanapaswa kuchagua watu wa kushirikiana nao kutoka kwa wale wanaopenda usafi wa Ukweli, ambao maadili yao hayajatiwa doa, na ambao tabia zao ni safi. Lazima wazingatie masharti yaliyowekwa katika Neno la Mungu, ikiwa kweli watataka kuwa wana wa Mungu, washiriki wa familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni. “Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha.” Mungu anawapenda hawa vijana, na kama watafuata maongozi ya Roho Wake, na kutembea katika shauri Lake, Yeye atakuwa nguvu yao. {3T 126.1}

Mungu amempa Ndugu A Y uwezo mzuri, mitazamo ya haraka, na ufahamu mzuri wa Neno Lake. Kama moyo wake ungekuwa umetakaswa, angeweza kuwa na ushawishi mzuri kwa ndugu zake, hali kadhalika na majirani zake na wale anaoshirikiana nao. Lakini upendo wa pesa umeishika sana nafsi yake, na umefungamanishwa sana na shughuli zote za maisha, hivi kwamba ameungamanishwa na ulimwengu badala ya kubadilishwa kwa kufanywa upya kwa akili. Nguvu zake zimepotoshwa na kuharibiwa na mapenzi mabaya ya faida, ambayo yamemfanya awe mbinafsi, bahili, na mtu anayelazimisha mambo. Kama sifa zake bora zingekuwa zikitumika kikamilifu katika utumishi wa Bwana Wake, kuliko kutumiwa kutimiza masilahi yake binafsi, kama malengo na makusudi yake vingekuwa kumekita katika kutenda mema na kumtukuza Mungu, ubora wa akili ambao Mungu alikuwa amempa ungeingiza kwenye tabia yake nguvu, unyenyekevu, na ufanisi ambavyo visingeshindwa kumletea heshima na vingempatia ushawishi juu ya wote alioshirikiana nao. {3T 126.2}

Nilioneshwa kuwa mali iliyoachwa na baba kwa kweli imekuwa mzizi wa uchungu kwa watoto wake. Amani na furaha yao, na kuaminiana baina yao, kwa kiwango kikubwa kumevurugwa na mali hiyo. Ndugu A Y hakuhitaji mali ya baba yake. Alikuwa na talanta za kutosha kusimamia yale ambayo Mungu alikuwa ameyakabidhi kwake ili ayasimamie. Kama tu angetumia vyema kile alichokuwa nacho, angalau angekuwa miongoni mwa wale waliokuwa waaminifu katika yale yaliyo madogo sana. Ongezeko la usimamizi wa mali ya baba yake, ambalo alikuwa akilitamani kwa shauku kubwa, lilikuwa jukumu zito kuliko vile ambavyo angeweza kulisimamia vyema. {3T 127.1}

Kwa miaka kadhaa upendo wa pesa umekuwa uking’oa upendo wa wanadamu na upendo wa Mungu. Na kwa kuwa mali za baba yake zilikuwa katika uwezo wake wa kuzifikia, alitamani kuhodhi yote yaliyowezekana mikononi mwake mwenyewe. Alifuata njia ya ubinafsi kuwaelekea ndugu zake kwa sababu alikuwa na upendeleo na angeweza kufanya hivyo. Ndugu zake hawakuwa na hisia sahihi. Walikuwa na uchungu naye. Katika kushughulikia jambo hilo alijipendelea kuliko wengine hadi

mwenendo wake ikaitukanisha kazi ya Mungu. Amepoteza uwezo wa kujitawala. Lengo lake kuu limekuwa ni kupata faida, na ni faida ya kibinafsi (mchoyo). Upendo wa pesa moyoni ulikuwa mzizi wa uovu huu wote. Nilioneshwa kwamba kama angegeuza nguvu zake ili kufanya kazi kwenye shamba la mizabibu la Bwana angefanya mema mengi, lakini sifa hizi zinapopotoka zinaweza kuleta madhara makubwa. {3T 127.2}

Wakina kaka B hawajapata msaada waliopaswa kuwa nao. AB amefanya kazi kwa hasara kubwa. Amechukua mizigo mingi sana juu yake, ambayo imelemaza kazi zake hivi kwamba hajaongezeka nguvu za kiroho na ujasiri kama ambavyo ilipaswa. Kanisa, lenye nuru ya Ukweli, na ambalo lilipaswa kuwa na nguvu katika Mungu katika kunia, na kufanya, na kujitoa kafara, kama ingekuwa lazima, kwa sababu ya Ukweli, limekuwa kama watoto dhaifu. Wamehitaji wakati na kazi ya Ndugu AB kutatua shida ambazo hazipaswi kuwapo kamwe. Na shida hizi zinapotokea kwa sababu ya ubinafsi na mioyo isiyotakaswa, zingeweza kuondolewa kwa saa moja, kama kungekuwa na unyenyekevu na roho ya kukiri. {3T 127.3}

Wakina kaka B wanafanya makosa kwa kubaki katika -----. Wanapaswa kubadilisha eneo lao na wasiwe wanalitembelea eneo lao zaidi katika kipindi cha mwaka. Wangekuwa na uhuru mkubwa katika kutoa ushuhuda wao. Ndugu hawa hawajapata uhuru wa kusema Ukweli na mambo ya dhahiri katika kipindi walichoishi. Kama wangeishi mahali pengine, wangekuwa huru zaidi na mizigo, na ushuhuda wao ungekuwa na uzito mara kumi zaidi wakati walipolitembelea kanisa hili. Wakati Ndugu AB amelemewa na majaribu madogo-madogo ya kanisa na kuwekwa katika ----, angepaswa awe anafanya kazi nje ya nchi. Amekuwa mhudumu wa meza/ofisi ya kusaidia wenye mahitaji hadi akili yake imetiwa giza asielewe nguvu na uwezo wa Ukweli-Mdo 6:1-3. Hajaamshwa na mahitaji halisi ya kazi ya Mungu. Amekuwa akipoteza hali ya kiroho na ujasiri. Kazi ya kudumisha utoaji wa mpango imepuuzwa. Baadhi ya ndugu, ambao shauku yao yote ilikuwa wakati mmoja katika kuendeleza kazi ya Mungu, wamekuwa wakikuza ubinafsi na ubahili badala ya kuwa wenye kujitolea zaidi na wenye kuongezeka katika viwango vyao vya kuupenda Ukweli na ibada. Wamekuwa wakipungua katika mambo ya ibada na kuzidi katika mambo ya ulimwengu. Baba C ni mmoja wa watu hawa. Anahitaji uongofu mpya. Ndugu C amepata upendeleo mkuu na marupurupu ya hali ya juu, na haya yasipoboreshwa, hukumu na giza zitafuata kulingana na nuru aliyokuwa nayo, kwa kutoboresha talanta alizopewa na Mungu ili aziboreshe. {3T 127.4}

Ndugu huko Vermont wamemhuzunisha Roho wa Mungu kwa kuruhusu upendo wao kwa Ukweli na shauku yao katika kazi ya Mungu kupungua. {3T 128.1}

Ndugu DB alizichosha nguvu zake msimu uliopita alipokuwa akifanya kazi katika maeneo mapya akitumia hema na bila kuwa na msaada unaofaa. Mungu hataki

huyu ndugu, au yeyote kati ya watumishi Wake, waumize afya zao kwa kujiweka kwenye mazingira magumu au kwa kazi ya mateso. Ndugu huko ----- walipaswa kuhisi kupendezwa ambako kungeoneshwa na kazi zao. Wangeweza kupata msaada kama wangekuwa macho na kuvutiwa na kazi ya Mungu na kutambua thamani ya roho. Wakati Ndugu DB alipata hisia ya kina ya kazi ya Mungu na thamani ya roho, ambayo ilidai bidii endelevu, kanisa kubwa huko ----- na shida zao ndogo zilimzuilia Ndugu AB kumsaidia kaka yake. Ndugu hawa wanapaswa kuja na ujasiri mpya, wakijipukutisha wenyewe kutoka kwa majaribu na kukatishwa tamaa vilivyowashikilia huko ----- kiasi cha kudhoofisha ushuhuda wao, na wanapaswa kudai nguvu kutoka kwa yule Mwenye Nguvu. Walipaswa kubeba ushuhuda wa wazi, na ulio huru, kwa Ndugu X na Y, na kuhakikisha unapokelewa na kufanya wawezavyo ili hawa ndugu wagawanye mali yao kwa usahihi. Ndugu AB, kwa kuchukua mizigo mingi hivi, anapunguza nguvu yake ya akili na mwili. {3T 128.2}

Kama Ndugu C angekuwa akitembea katika nuru kwa miaka michache iliyopita, angetambua thamani ya roho. Kama angekuza upendo kwa Ukweli angekuwa amefuzu kufundisha Ukweli kwa wengine. Huenda angemsaidia ndugu DB katika kazi yake ya hema. Angeweza angalau kubeba mizigo ya kanisa la nyumbani. Kama angekuwa na upendo kwa ndugu zake, na kama angekuwa ametakaswa na Kweli, angeweza kuwa mpatanishi wa amani badala ya kuwa mchochezi wa magomvi, ambayo, pale yalipoungana na shida zingine, yalimtoa Ndugu AB kutoka upande wa kaka yake katika wakati muhimu zaidi na kuwasababishia Ndugu DB kufanya kazi kupita uwezo wao. Na hata hivyo, baada ya Ndugu DB kufanya kila awezalo, kazi haikutimizwa ambayo ingeweza kufanywa ikiwa kungekuwa na shauku ambayo ingekuwa katika ----- kusambaza msaada wakati ilikuwa inahitajika sana. Jukumu la kutisha liko juu ya kanisa hilo kwa kupuuza kwao wajibu. {3T 129.1}

Nilioneshwa kuwa hatua ya Ndugu X katika kugawanya mali yake miongoni mwa watoto wake ilikuwa ikiwabebesha jukumu ambalo hakupaswa kuliachia. Sasa ametambua kuwa matokeo ya hatua hii hayakumletea ongezeko la mapenzi kutoka kwa watoto wake. Hawajahisi kuwa chini ya wajibu kwa wazazi wao kwa kile ambacho wamewafanyia. Watoto hawa walikuwa wadogo na wasiyo na uzoefu. Hawakuwa na sifa ya kubeba jukumu lililowekwa juu yao. Mioyo yao haikuwa imejitoa wakfu, na marafiki wa kweli walitazamwa nao kama wanaoandaa maadui, wakati wale ambao wangewatenganisha na marafiki zao hasa walikubaliwa. Mawakala hawa wa Shetani walikuwa daima wakipendekeza maoni ya uwongo kwa akili za vijana hawa, huku mioyo ya kaka na dada, baba na mama, ilikuwa imetofautiana. {3T 129.2}

Baba X alifanya makosa. Kama angewaambia zaidi waume wa binti zake, ambao walipenda Ukweli kwa unyofu, na angekuwa tayari zaidi kusaidiwa na ushauri wa watu hawa wa uzoefu, makosa makubwa yangeweza kuzuiwa. Lakini hii ndiyo njia

ambayo adui kwa ujumla hufanikiwa kusimamia mambo kuhusiana na matumizi ya mali. {3T 130.1}

Maswala haya yote yaliyotajwa yalibuniwa na kuendelezwa na Mungu ili wote wapate kuona athari ya udanganyifu wa utajiri juu ya moyo. Matokeo katika maswala haya, yanayoonekana kwa wote, yanapaswa kutoa onyo kwa wakina baba na mama na kwa watoto wenye tamaa. Neno la Mungu hufafanua uchoyo kama ibada ya sanamu. Haiwezekani kwa wanaume na wanawake kushika sheria ya Mungu na kupenda pesa. Mapenzi ya moyo yanapaswa kuwekwa juu ya vitu vya mbinguni. Hazina yetu inapaswa kuwekwa mbinguni, maana pale hazina yetu ilipo, ndiko pia moyo wetu utakuwapo. {3T 130.2}

SURA YA 13

ELIMU SAHIHI

Kazi nzuri kabisa iliyowahi kutolewa kwa wanaume na wanawake duniani ni ile ya kushugulikia akili za ujana/vijana. Uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa katika elimu ya vijana ili kutofautisha njia ya mafundisho ili kuibua nguvu za kiwango cha juu na nzuri za akili. Wazazi na walimu wa shule hakika wanakosa sifa ya kuwafundisha watoto vizuri ikiwa wanakuwa hawajapata kwanza somo la kujitawala nafsi, uvumilivu, subira, uungwana na kuhusiana na wengine ipasavyo, na upendo. Hii ndiyo nafasi iliyo muhimu kwa wazazi, walezi, na waalimu! Kuna wachache sana ambao hugundua mahitaji muhimu zaidi ya akili na jinsi ya kuelekeza akili inayokua, mawazo yanayokua na hisia za ujana. {3T 131.1}

Kuna wakati wa kufundisha watoto na wakati wa kuelimisha vijana, na ni muhimu kwamba huko shuleni hizi zote ziunganishwe kwa kiwango kikubwa. Watoto wanaweza kufundishwa kwa huduma ya dhambi au kwa huduma ya haki. Elimu ya

mapema ya vijana huunda tabia katika maisha yao ya kidunia na katika maisha yao ya kidini. Sulemani anasema: “Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha hata atakapokuwa mzee.” Lugha hii ni chanya. Mafunzo ambayo Sulemani anaamuru ni yale ya kuelekeza, kuelimisha, na kukuza. Ili wazazi na waalimu wafanye kazi hii, lazima wao wenyewe waelewe “njia” ambayo mtoto anapaswa kuiendea. Hii inahusisha zaidi ya kuwa na ujuzi wa vitabu. Inahusu kila kitu kilicho chema, chenye fadhila. chenye huruma, chenye haki na kitakatifu. Inazingatia mazoezi ya kiasi, uchaji Mungu/utauwa, wema wa kindugu, na upendo kwa Mungu na kwa kila mmoja. Ili kufikia jambo hili, elimu ya watoto ya mwili, akili, maadili, na dini lazima vizingatiwe. {3T 131.2}

Elimu ya watoto, nyumbani au shuleni, haipaswi kuwa kama mafunzo ya wanyama bubu; kwa kuwa watoto wana nia yenye akili, ambayo inapaswa kuelekezwa kudhibiti nguvu zao zote. Wanyama bubu wanahitaji kufundishwa, kwani hawana uwezo wa kufikiri na akili. Lakini akili ya mwanadamu lazima ifundishwe kujitawala. Lazima ipewe elimu ya kumtawala mwanadamu, wakati wanyama wanatawaliwa na mabwana zao na wamefundishwa kuwatii. Bwana ndiye husimama badala ya akili, maamuzi, na nia ya mnyama. Mtoto anaweza kuzoeshwa, kama ilivyo kwa mnyama, ili asiwe na nia yake mwenyewe. Hata upekee wa nafsi yake unaweza kuunganishwa kwa yule anayesimamia mafunzo yake; ili nia yake, na makusudi yake yote, viwe chini ya nia ya mwalimu. {3T 132.1}

Watoto walioelimika kwa njia hiyo watakuwa na upungufu wa nguvu ya maadili na uwajibikaji wa mtu binafsi. Hawajafundishwa kujiongeza kwa kutumia akili na kanuni; nia zao zinatawaliwa na mwingine, na akili haijaanza kushughulishwa, ili iweze kupanuka na kuimarishwa kwa mazoezi. Hawajaelekezwa na kutiishwa/kunidhamishwa kwa kuzingatia mila zao za kipekee na uwezo wa akili zao, kutoa nguvu zao kali wakati inahitajika. Walimu hawapaswi kukomea hapa, bali wanapaswa kuzingatia ukuzaji wa viungo vilivyo dhaifu, ili nguvu zote ziweze kuletwa katika kufanyiwa mazoezi, na kutolewa kutoka hatua moja ya nguvu hadi nyingine, ili akili ipate utimamu/uwiano unaofaa. {3T 132.2}

Kuna familia nyingi za watoto ambao wanaonekana wamefundishwa vizuri wakati wa mafunzo ya kuadabisha; lakini wakati ule mfumo anaowashikilia kutunza sheria unapovunjika, huonekana kuwa hawawezi kufikiria, kutenda, au kuamua wenyewe. Watoto hawa ambao wamekuwa kwa muda mrefu chini ya sheria ya chuma/kikandamizaji, hawaruhusiwi kufikiri na kutenda kwa kujitegemea wao wenyewe katika mambo yale ambayo ilikuwa sahihi sana kama wangefanya wao wenyewe, na matokeo yake yamekuwa kukosa kujiamini kufanya maamuzi yao wenyewe yanayotokana na maoni yao wenyewe. Na wanapotoka kwa wazazi wao ili waende wakatende wenyewe, wanaongozwa kwa urahisi na uamuzi wa wengine katika njia mbaya. Hawana utulivu wa tabia. Hawajazoezwa kufanya maamuzi yao

wenyewe kwa haraka na kwa kadri inavyowezekana, na kwa hivyo akili zao hazijakuzwa vizuri na kuimarishwa. Kwa muda mrefu wamedhibitiwa kabisa na wazazi wao kiasi kwamba huwategemea kikamilifu moja kwa moja; wazazi wao husimama badala ya akili na maamuzi yao. {3T 132.3}

Kwa upande mwingine, vijana hawapaswi kuachwa wafikiri na kutenda bila kujali maamuzi ya wazazi na walimu wao. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu maamuzi yenye uzoefu na kuwa tayari kuongozwa na wazazi na walimu wao. Wanapaswa kuelimika kiasi kwamba akili zao zitaunganishwa na akili za wazazi na waalimu wao, na kuelekezwa ili waweze kuona uhalali wa kutii ushauri wao. Na ndipo wanapoondoka kwenye mkono uliokuwa ukiwaongoza wa wazazi wao na waalimu, tabia zao hazitakuwa kama mwanzi unaotetemeshwa na upepo. {3T 133.1}

Mafunzo makali ya vijana, bila kuwaelekeza vizuri kufikiri na kutenda kwa kujitegemea wenyewe kama uwezo na akili zao zitakavyoruhusu, na kwamba kupitia kwa njia hii wanaweza kuwa na ukuaji wa mawazo, hisia za kujiheshimu wenyewe, na kujiamini kuwa katika uwezo wao wenyewe wanaweza kufanya kitu, kutazalisha daraja la watu dhaifu katika nguvu ya akili na maadili. Na watakaposimama ulimwenguni kufanya kwa uwezo wao watafunua ukweli kwamba walikuwa wamefundishwa kama wanyama, na hawakuelimishwa. Nia zao, badala ya kuongozwa, zililazimishwa kutiishwa na nidhamu kali ya wazazi na waalimu. {3T 133.2}

Wale wazazi na waalimu wanaojivunia kuwa na uthibiti kamili wa akili na nia za watoto walio chini ya uangalizi wao wangeacha kujisifu kwao kama wangeyaangalia maisha ya baadaye ya watoto ambao kwasasa wanatiishwa kwa nguvu au kwa hofu. Hawa ni kama hawajajiandaa kabisa kushiriki katika majukumu magumu ya maisha. Wakati vijana hawa wanapokuwa hawapo tena chini ya uangalizi wa wazazi na waalimu wao, na wanalazimika kufikiria na kujifanyia kazi, wanakuwa katika uhakika wa kufuata njia mbaya na kujitupa kwenye nguvu ya majaribu. Hawafanyi maisha haya yafanikiwe, na upungufu huo unaonekana katika maisha yao ya kidini. Laiti kama waalimu wa watoto na vijana wangeweza kuona matokeo ya baadaye ya nidhamu yao potofu ikiwa imeanikwa mbele yao, wangebadilisha mpango wao wa elimu. Darasa hilo la waalimu ambao wamejiridhisha kuwa wana udhibiti kamili wa nia za wanafunzi wao siyo darasa la waalimu waliofanikiwa zaidi, ingawa muonekano kwa wakati huu waweza kudanganya. {3T 133.3}

Mungu kamwe hakuwahi kupanga kuwa akili moja ya mwanadamu ilazimike kuwa chini ya uthibiti kamili wa mtu mwingine. Na wale wanaokazana kufanya nafsi za wanafunzi wao ziungane na nafsi zao na wao wenyewe kuwa akili, nia, na dhamira

kwa ajili yao, wanajichukulia jukumu la kutisha. Wasomi hawa katika nyakati fulani fulani wanaweza kuonekana kama askari waliokamilika kimafunzo. Lakini kizuizi kitakapoondolewa, kutaonekana uhitaji wa matendo yaliyo huru kutoka kwa kanuni thabiti iliyopo ndani yao. Wale wanaopanga kuwa na lengo la kuwaelimisha watoto waone na kuhisi nguvu iliyomo ndani yao, na kutengeneza wanaume na wanawake wenye kanuni, wawezao kumudu nafasi yoyote maishani, ndiyo walimu wanaofaa na wenye mafanikio ya kudumu. Kazi yao inaweza isioneshe faida nzuri kwa watazamaji wazembe, na kazi zao zaweza zisithaminiwe sana kama zile za waalimu wanaoshikilia akili na nia za wanafunzi wao wakizitawala kwa mamlaka; lakini maisha ya baadaye ya wanafunzi hao yataonesha matunda ya mpango bora wa elimu. {3T 134.1}

Kuna hatari ya wazazi na waalimu kuamuru na kuagiza sana, wakati wakishindwa kuja kwa kiwango cha kutosha katika uhusiano wa kijamii na watoto au wanafunzi wao. Mara nyingi hujizuia sana [wasiwasogelee watoto], na hutumia mamlaka yao kwa njia ya ubaridi, na isiyo na huruma ambayo haiwezi kushinda mioyo ya watoto na wanafunzi wao. Kama wangewakusanya watoto karibu nao, na kuwaonesha kuwa wanawapenda, na wangewaonesha kupendezwa na juhudi zao zote na hata kwenye michezo yao, wakati mwingine hata kujifanya watoto miongoni mwao, wangewafurahisha watoto na wangepata upendo wao na kuwafanya wawaamini. Na watoto kwa haraka sana wangeheshimu na kupenda mamlaka ya wazazi na waalimu wao. {3T 134.2}

Tabia na kanuni za mwalimu zinapaswa kuzingatiwa kuwa za umuhimu mkubwa kuliko hata sifa zake za kisomi. Ikiwa yeye ni Mkristo wa dhati atahisi umuhimu wa kuvutiwa katika elimu ya mwili, akili, maadili, na kiroho ya wanafunzi wake. Ili kuwa na ushawishi sahihi, anapaswa kuwa na uthibiti kamili juu yake mwenyewe, na moyo wake mwenyewe unapaswa kujazwa na upendo kwa wanafunzi wake, utakaoonekana katika sura, maneno, na matendo yake. Anapaswa kuwa na uthabiti wa tabia, ndipo anaweza kuunda akili za wanafunzi wake na pia kuwafundisha sayansi. Elimu ya mapema ya ujana kwa ujumla huunda tabia wao kwa maisha yote. Wale ambao hushughulika na vijana wanapaswa kuwa waangalifu sana kukuza ubora wa akili, ili wapate kujua vizuri jinsi ya kuelekeza nguvu zake ili ziweze kutumika katika viwango vilivyo bora zaidi. {3T 135.1}

Acha Kufungia Watoto Shuleni-Watoto wasifungiwe kwenye vyumba vya shule au nyumbani, bali waachwe kwenye hewa bora Mfumo wa elimu uliokuwa ukitumika kwa vizazi vya nyuma umekuwa mbaya kwa afya na hata kwa maisha yenyewe. Watoto wengi wadogo wametumia masaa matano kila siku katika vyumba vya shule visivyo na hewa ya kutosha inayozunguka, na ambavyo si vikubwa kwa kutosha malazi yenye afya ya wanafunzi. Hewa ya vyumba kama hivyo mara hugeuka na kuwa sumu kwa mapafu yanayoivuta. Watoto wadogo, ambao miguu, mikono na

misuli yao haina nguvu, na ambao akili zao hazijakua vyema bado, wamewekwa ndani ya nyumba na kuwaletea madhara. Wengi huwa hawana kitu cha kuwashikilia maishani kifaacho kuanza nacho. Kufungiwa shuleni siku hadi siku huwafanya [wanafunzi] wawe na wasiwasi na magonjwa. Miili yao imedumaa kwa sababu ya hali ya uchovu wa mfumo wa neva. Na ikiwa taa ya uzima itazimwa, wazazi na waalimu hawatazingatia kwamba walikuwa na ushawishi wowote wa moja kwa moja katika kuzima cheche muhimu. Wakati wamesimama karibu na makaburi ya watoto wao, wazazi wanaoteseka wanaangalia kufiwa kwao kama kipindi maalum cha majaliwa ya Mungu, wakati, kwa ujinga usiyo na sababu, hatua zao wenyewe zimeharibu maisha ya watoto wao. Kutoa mashitaka kwamba kifo chao kuwa ni mapenzi ya Mungu, ni kufuru. Mungu alitaka watoto wadogo waishi na wawe na nidhamu, ili wawe na tabia nzuri na wamtukuze katika ulimwengu huu na wamsifu katika ulimwengu ule ulio bora. {3T 135.2}

Wazazi na waalimu, kwa kuchukua jukumu la kuwafundisha watoto hawa, hawahisi uwajibikaji wao mbele za Mungu kwa kujuua mwili (elimu yake), ili waweze kutibu miili ya watoto wao na wanafunzi kwa njia ya kuhifadhi maisha na afya. Maelfu ya watoto hufa kwa sababu ya ujinga wa wazazi na walimu. Akina mama watatumia masaa mengi kufanya kazi isiyo ya lazima kwenye nguo zao na za watoto wao ili kukidhi matakwa ya maonesho, na kisha watasihi kwamba hawapati muda wa kusoma na kupata habari muhimu ya kutunza afya za watoto wao. Wanadhani haina shida kuisalimisha miili yao kwa madaktari na kuuacha mzigo huo kwa huyo tabibu. Ili kuchukuliana na mitindo na desturi, wazazi wengi wameitoa mhanga afya na maisha ya watoto wao. {3T 136.1}

Ili kuufahamu mwili wa ajabu wa mwanadamu, mifupa, misuli, tumbo, ini, utumbo, moyo, na matundu ya ngozi, na kuelewa utegemezi wa kiungo kimoja juu ya kingine kwa ajili ya matendo ya kiafya ya viungo vyote, ni utafiti na somo ambalo akina mama wengi hawavutiwi nalo. Hawajui chochote juu ya ushawishi wa mwili juu ya akili na akili juu ya mwili. Hawaelekei kuelewa chochote kuhusu akili, ambayo huunganisha ya muda kitambo na yale ya umilele. Kila kiungo cha mwili kiliumbwa kiwe mtumwa wa akili. Akili ni mtaji na kitovu kikuu cha mwili-head quarters and capital-City. Watoto wanaruhusiwa kula nyama, viungo, siagi, jibini, nyama ya nguruwe, keki yenye virutubisho vingi, na vikolezo vingi vya kutia ladha kwenye chakula. Wanaruhusiwa pia kula wakati wowote na katikati ya milo vyakula visivyo vya afya. Vitu hivi hufanya kazi yake ya kuvuruga tumbo, kusisimua neva kwa namna isiyo ya asili, na kudhoofisha akili. Wazazi hawatambui kuwa wanapanda mbegu ambayo italeta magonjwa na kifo. {3T 136.2}

Watoto wengi wameharibiwa maisha yao yote kwa kukazania kuitumia akili zaidi na kupuuza kuimarisha nguvu za mwili. Wengi wamekufa utotoni kwa sababu ya hatua iliyofuatwa na wazazi na walimu wa shule bila busara kwa kuwalazimisha

watoto wao wanaosoma, kwa kubembeleza au kwa kuwatia hofu, wakati walikuwa wadogo sana kuweza kuingia ndani ya chumba cha shule. Akili zao zimeelemewa na masomo wakati hawakupaswa kuitwa shuleni, bali kuzuiliwa hadi viungo vya miili viwe na nguvu ya kutosha kuvumilia mikiki mikiki ya kiakili. Watoto wadogo wanapaswa kuachwa huru kama kondoo wadogo ili wakimbie-kimbie huko nje, wakiwa huru na wenye furaha, na wanapaswa kuruhusiwa fursa nzuri zaidi ya kuweka msingi wa viungo sawasawa. {3T 137.1}

Wazazi wanapaswa kuwa waalimu pekee wa watoto wao hadi watakapofikisha umri wa miaka minane au kumi. Mara tu akili zao zinapoweza kupambanua, wazazi wanapaswa kufungua mbele yao kitabu kikuu cha maumbile/uumbaji/nature cha Mungu. Mama anapaswa kuwa na upendo kidogo kwa vitu bandia ndani ya nyumba yake na katika kuandaa mavazi yake ya kutoka nayo nje, na anapaswa kupata wakati wa kukuza, yeye mwenyewe na watoto wake, upendo kwa miche inayochipuza na maua yanayofunguka. Kwa kuwaelekeza watoto wake kwa rangi tofauti tofauti na aina mbalimbali za maumbo na viasilia, anaweza kuwafanya wafahamiane na Mungu, ambaye alifanya vitu vyote vizuri vinavyovutia na kufurahisha. Anaweza kuongoza mawazo yao kwa Muumba wao na kuamsha katika mioyo yao michanga upendo kwa Baba yao wa mbinguni, ambaye ameonesha upendo mkubwa sana kwao. Wazazi wanaweza kumshirikisha Mungu na kazi Zake zote alizoumba. Chumba pekee cha shule cha watoto wa kuanzia umri wa miaka minane hadi kumi kinapaswa kuwa kwenye uwanja uliojawa na hewa ulio katikati ya maua yanayofunguka na mandhari nzuri ya asili. Na kitabu chao cha pekee kinapaswa kuwa hazina za maumbile. Masomo haya, yaliyowekwa kwenye akili za watoto wadogo katikati ya mandhari mazuri na ya kupendeza ya maumbile, hayawezi kusahauliwa katika siku za hivi karibuni. {3T 137.2}

Ili watoto na vijana wawe na afya, uchangamfu, ucheshi, na misuli na ubongo uliokuzwa vyema, wanapaswa kuwa kwenye eneo la wazi lenye hewa ya kutosha na maburudisho n kazi inayoratibiwa vizuri. Watoto na vijana waliohifadhiwa mashuleni na waliofungwa kwenye vitabu, hawawezi kuwa na viungo vizuri vyenye afya ya mwili. Zoezi la ubongo katika kusoma, lisilo na ulinganifu na mazoezi ya mwili, lina mwelekeo wa kuivuta damu kwenye ubongo, na mzunguko wa damu kupitia mfumo huwa katika hali isiyo na usawa. Ubongo hujawa na damu nyingi wakati maeneo ya pembezoni mwa mwili huwa na damu kidogo. Kunatakiwa kuwepo sheria zinazoratibu masomo yao kwa masaa kadhaa, na kisha sehemu ya wakati wao inapaswa kutumiwa katika kazi ya mwili. Na ikiwa tabia zao za kula, kuvaa, na kulala zitalingana na sheria za mwili, wanaweza kupata elimu bila kuitoa mhanga afya ya mwili na akili. {3T 137.3}

Mwelekeo wa Kwenda Hini

Mwelekeo wa kwenda chini wa Miili ya Jamii ya Wanadamu Kitabu cha Mwanzo kinatoa maelezo kamili juu ya maisha ya kijamii na ya mtu binafsi, na bado hatuna kumbukumbu ya kuzaliwa kwa mtoto mchanga akiwa kipofu, kiziwi, mlemavu, au utindo wa ubongo. Hakuna kumbukumbu ya kuwepo kifo cha kawaida katika umri wa watoto wachanga, umri wa utoto, au katika umri wa mapema wa ujana. Hakuna maelezo ya wanaume na wanawake waliokufa kwa magonjwa. Tangazo au taarifa za msiba, za watu waliokufa katika kitabu cha Mwanzo zinasomeka hivi: “Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini, naye akafa.” “Siku zote za Sethi ni miaka mia kenda na kumi na miwili, akafa.” Kuhusu wengine, kumbukumbu zinasema: Aliishi katika uzee mwema naye akafa. Ilikuwa ni nadra sana kwa mtoto kufa kabla ya baba yake na kama ingetokea tukio kama hilo lilihesabiwa kustahili kuwekwa kwenye kumbukumbu: "Na Harani alikufa kabla ya baba yake Tera.” Harani alikuwa baba kabla ya kifo chake. {3T 138.1}

Mungu alimjalia mwanadamu nguvu kubwa muhimu sana kuweza kukabili mkusanyiko wa magonjwa yaliyoletwa kwenye jamii ya wanadamu kama matokeo ya tabia zilizopotoka, na ameendelea [kumjalia hivyo] kwa miaka elfu sita. Ukweli huu wenyewe unatosha kutuhakikishia nguvu na uwezo wa kiumeme ambavyo Mungu alimpa mwanadamu wakati wa uumbaji Wake. Ilichukua zaidi ya miaka elfu mbili ya uhalifu na kuridhisha hamu ya mambo duni na tamaa, ili kuleta magonjwa ya mwili katika jamii ya wanadamu kwa kiwango kikubwa. Kama Adamu, wakati wa uumbaji Wake, hangekuwa amepewa nguvu muhimu mara ishirini kuliko ile ya watu wa sasa, jamii ya wanadamu, na tabia zao za sasa za kuishi kwa kukiuka sheria ya asili, ingekuwa imetoweka. Wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo jamii ya wanadamu ilikuwa imeshuka kwa kasi kubwa kiasi kwamba ongezeko la magonjwa lilikikandamiza kizazi hicho, na kuingiza wimbi la dhiki na uzito wa mateso usiyoelezeka. {3T 138.2}

Hali mbaya ya ole ya ulimwengu kwa wakati huu imewasilishwa mbele yangu. Tangu anguko la Adam jamii ya wanadamu imekuwa ikizidi kuporomoka. Baadhi ya sababu za hali mbaya ya sasa ya wanaume na wanawake, walioumbwa kwa mfano wa Mungu, zilioneshwa kwangu. Na hisia ya kiasi gani inapaswa kufanyika ili kupunguza kasi, hata kwa kiwango [kidogo], mmonyoko huu wa mwili, akili, na maadili, ilisababisha moyo wangu kuwa mgonjwa na kuzimia. Mungu hakuiumba jamii ya wanadamu katika hali yake dhaifu ya sasa. Hali hii ya mambo haitokani na kazi ya Majaliwa au mipango ya Mungu, bali ni kazi ya mwanadamu; iliyoletwa kwa njia ya tabia mbaya na dhuluma, kwa kukiuka sheria ambazo Mungu ameziunda kutawala uwepo wa mwanadamu. Kupitia jaribu la kukidhi hamu ya kula, Adamu na Hawa kwanza walianguka kutoka kwa hali yao ya juu, takatifu, na yenye furaha. Na ni kupitia jaribu lilelile ambapo jamii ya wanadamu

imedhoofishwa. Wanadamu wameruhusu hamu, tamaa na uchu kuchukua kiti cha enzi, na kuyatiisha maamuzi na akili. {3T 139.1}

Ukiukaji wa sheria ya asili, na kusababisha, mateso ya wanadamu, vimekuwepo kwa muda mrefu sana kiasi kwamba wanaume na wanawake wanaangalia hali ya sasa ya ugonjwa, mateso, unyonge, na kifo cha mapema kama mambo ambayo wanadamu walipangiwa nayo. Mwanadamu alikuja kutoka mikononi mwa Muumba wake akiwa mkamilifu na mzuri wa umbo, na aliyejazwa nguvu muhimu kiasi kwamba ilichukua zaidi ya miaka elfu moja kabla ya hamu yake mbaya na tamaa zake, na ukiukaji wa jumla wa sheria za mwili, havijajidhihirisha katika jamii ya wanadamu. Vizazi vya hivi karibuni vimehisi shinikizo la udhaifu na magonjwa kwa kasi kubwa zaidi [vikitokea] baada ya kila kizazi. Nguvu muhimu zimedhoofishwa sana na hamu na shauku ya matamanio. {3T 139.2}

Wazee wa imani kutoka Adamu hadi Nuhu, isipokuwa wachache tu, waliishi karibu miaka elfu moja. Tangu siku za Nuhu urefu wa maisha umekuwa ukipungua. Waliokuwa wakiugua magonjwa waliletwa kwa Kristo kutoka kila jiji, mji, na kijiji ili awaponye; kwa kuwa walikuwa wanaumwa kila aina ya magonjwa. Na magonjwa yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kupitia vizazi kwa vizazi mfululizo tangu kipindi hicho. Kwa sababu ya ukiukaji wa sheria za maisha ulio endelevu, vifo vimeongezeka kwa kiwango cha kutisha. Miaka ya mwanadamu imefupishwa, ili kizazi cha sasa kiende kaburini, hata kabla ya umri ambao vizazi vilivyoishi miaka michache ya kwanza ya elfu moja baada ya uumbaji, havijafikia hatua ya kuonesha vitendo. {3T 139.3}

Ugonjwa umeambukizwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto, kutoka kizazi hadi kizazi. Watoto wachanga wasio na uwezo wa kutembea bado wanaumizwa vibaya kwa sababu ya dhambi za wazazi wao, ambazo zimepunguza nguvu zao muhimu. Tabia zao mbaya za kula na kuvaa, na za kutapanya mali, hupitishwa kama urithi kwa watoto wao. Wengi wanazaliwa wakiwa na maradhi ya akili, wenye ulemavu, vipofu, viziwi, na sehemu kubwa sana [ya hao watoto] huwa na upungufu wa akili. Kukosekana kusiko kwa kawaida kwa kanuni inayoelezea kizazi hiki, na inayooneshwa katika hali yake ya kutotambua sheria za maisha na afya, ni jambo linaloshangaza. Ujinga unatawala juu ya somo hili, wakati nuru inaangaza pande zote. Kwa walio wengi, hofu yao kuu ni, nini watakachokula? Nini watakachokunywa? Na nini watakachovaa? Pamoja na yote yaliyosemwa na kuandikwa kuhusu jinsi tunavyopaswa kuishughulikia miili yetu, hamu ya kula ni sheria kuu inayotawala wanaume na wanawake kwa ujumla. {3T 140.1}

Nguvu za maadili zimedhoofishwa kwa kuwa wanaume na wanawake hawaishi kwa kutii sheria za afya na kufanya somo hili kubwa kuwa jukumu la kibinafsi. Wazazi huwarithisha watoto wao tabia zao zenye kupotoshwa, na magonjwa yenye

kuchukiza huharibu damu na kudhooisha nguvu ya ubongo. Wengi wa wanaume na wanawake hubaki katika ujinga wa sheria [zinazotawala mwili] uwepo wao, na hujishughulisha na hamu na uchu unaopoteza akili na maadili, na huonekana kuwa tayari kubaki katika ujinga wa matokeo ya ukiukaji wao wa sheria za asili. Wanajiingiza katika hamu mbaya ya matumizi ya sumu [inayoua] polepole ambayo huharibu damu na kudhoofisha nguvu za neva, na matokeo yake hujiletea magonjwa na kifo. Rafiki zao huita matokeo ya hatua hii majaliwa ya Mungu/Mpaji -au kipindi cha maongozi ya Mungu. Katika hili wanaitukana Mbingu. Waliasi sheria za asili na wakapata adhabu kwa kutumia sheria Zake vibaya. Mateso na vifo sasa vinatawala kila mahali, haswa kati ya watoto. Kuna tofauti kubwa kiasi gani kati ya kizazi hiki na wale walioishi wakati wa miaka elfu mbili za kwanza! {3T 140.2}

Umuhimu wa Mafunzo ya Nyumbani- Niliuliza ikiwa wimbi hili la ole halingeweza kuzuiwa na kitu kifanyike kuokoa vijana wa kizazi hiki kutoka kwa uharibifu unaowatishia. Nilioneshwa kuwa sababu moja kubwa ya hali ya kusikitisha iliyopo ni kwamba wazazi hawahisi kuwa chini ya wajibu wa kuwalea watoto wao kufuata sheria za mwili. Akina mama wanapenda watoto wao kwa upendo wa ibada ya masanamu na huendekeza hamu yao wakati wanajua kuwa itaumiza afya zao na kwa hivyo itawaletea magonjwa na kutokuwa na furaha. Ukarimu huu wa kikatili umeoneshwa kwa kiwango kikubwa katika kizazi cha sasa. Tamaa za watoto zinaridhishwa kwa kupoteza afya na kuepuka hasira kwa kuwa ni rahisi kwa wakina mama, kwa wakati huu, kuwaridhisha [watoto wao] kuliko kuwazuia yale wanayoyalilia. {3T 141.1}

Kwa hivyo akina mama wanapanda mbegu ambayo itakua na kuzaa matunda. Watoto hawajafundishwa kukataa hamu zao na kuzuia matakwa yao. Nao wanakuwa wabinafsi, wagumu/wakali, wasiyotii, wasiyo na shukrani, na wasiyo watakatifu. Akina mama ambao wanafanya kazi hii watavuna kwa uchungu matunda ya mbegu waliyopanda. Wamefanya dhambi dhidi ya Mbingu na dhidi ya watoto wao, na Mungu atawawajibisha. {3T 141.2}

Kama elimu kwa vizazi vya nyuma ingefanywa juu ya mpango ulio tofauti kabisa, vijana wa kizazi hiki cha sasa wasingekuwa wapotovu sana na wasiyo na thamani. Wasimamizi na waalimu wa shule walipaswa kuwa wale ambao walielewa fiziolojia na ambao walikuwa na hamu, siyo tu ya kuwafundisha vijana katika sayansi, bali pia kuwafundisha jinsi ya kuhifadhi afya ili watumie maarifa yao kwa mambo mazuri baada ya kuipata. Ufundishaji huu ungetakiwa uwe umeunganishwa na shule, iliyoudwa ili kubeba matawi mbalimbali ya kazi, ili wanafunzi wapate ajira na mazoezi muhimu nje ya masaa ya shule. {3T 141.3}

Kazi ya wanafunzi na maburudisho vilipaswa kuwa vimeratibiwa kwa kuzingatia sheria ya mwili na zingetumika kuwahifadhia sauti/toni yenye afya ya nguvu zote

za mwili na akili. Kisha maarifa ya vitendo ya biashara yangeweza kupatikana wakati elimu yao ya nadharia ikipatikana. Wanafunzi shuleni wangepaswa kuwa na hisia za kimaadili zilizoamshwa kuona na kuhisi kuwa jamii ina madai juu yao na kwamba wanapaswa kuishi kwa kutii sheria ya asili ili waweze, kwa uwepo wao na ushawishi, kwa amri/kanuni na mfano, kuwa faida na baraka kwa jamii. Inapaswa kuingizwa [kwenye akili za] vijana kwamba wote wana ushawishi unaoiambia jamii mara zote kuboresha na kuinua au kushusha na kupunguza. Somo la kwanza la vijana linapaswa kuwa kujitambua wenyewe na jinsi ya kuweka miili yao katika afya [anatomy and fiziolojia nk]. {3T 142.1}

Wazazi wengi huwaweka watoto wao shuleni karibu mwaka mzima. Watoto hawa hupitia utaratibu wa kusoma kama mtindo tu, lakini hawahifadhi yale wanayojifunza. Wengi wa wanafunzi hawa wa kudumu wanaonekana wenye kupungukiwa maisha ya kielimu. Ukiritimba wa kuendelea kusoma unachosha akili, na hiyo huwafanya wasivutiwe na masomo yao; na kwa wengi matumizi ya vitabu huwa yenye uchungu. Hawana upendo wa kina wa mawazo na hawana hamu ya kupata maarifa. Hawajitii moyo wao wenyewe katika kutafakari, utafiti na kuchunguza. {3T 142.2}

Watoto wanahitaji sana elimu sahihi ili waweze kutumiwa ulimwenguni. Lakini juhudi yoyote inayoinua utamaduni wa kielimu juu ya mafunzo ya maadili inaelekezwa vibaya. Kufundisha, kukuza, kung'arisha, na kusafisha vijana na watoto vinapaswa kuwa mzigo mkubwa kwa wazazi na waalimu. Wale wanaotafakari kwa kina na wanaofikiri kwa mantiki ni wachache kutokana na ukweli kwamba mivuto ya uongo imeingilia kati maendeleo ya akili. Dhana ya wazazi na waalimu kwamba usomaji wa kudumu ungeimarisha akili kumethibitika kuwa si kweli, kwani katika hali nyingi imekuwa na athari zilizo kinyume. {3T 142.3}

Katika elimu ya awali ya watoto wazazi na waalimu wengi hushindwa kuelewa kwamba umakini mkubwa unahitaji kutolewa kwa viungo vya mwili, kwamba hali ya afya ya mwili na ubongo vyaweza kulindwa. Imekuwa kawaida kuhimiza watoto kuhudhuria shule wakiwa watoto wachanga tu, wanaohitaji utunzaji wa mama. Wakiwa kwenye umri teke-teke, mara nyingi hujazana katika vyumba vya shule visivyo na hewa nzuri, ambapo hukaa katika mkao mbaya kwenye mabenchi/mimbari iliyojengwa vibaya, na matokeo yake maungo madogo na mateke ya baadhi yao hupata ulemavu. {3T 143.1}

Mwelekeo na tabia za ujana vina uwezekano wa kudhihirika katika utu uzima. Unaweza kuinamisha mti mchanga kulingana na umbo lolote utakalochagua, na ukibaki na kukua kwa namna ile uliyouinamisha, utakuwa mti wenye kasoro na utatoa daima somo kwa watu juu ya majeraha na dhuluma uliyopokea mkononi

mwako. Unaweza, baada ya miaka ya ukuaji, kujaribu kunyoosha mti, lakini juhudi zako zote zitathibitisha kutozaa matunda. Daima utakuwa mti uliolemaa. Hivyo ndivyo ilivyo kwa akili za vijana. Wanapaswa kufundishwa kwa uangalifu na kwa upole katika utoto. Wanaweza kufundishwa katika mwelekeo sahihi au mwelekeo wenye makosa, na katika maisha yao ya baadaye watafuata hatua ambayo walielekezwa katika ujana. Tabia zilizoundwa katika ujana zitakua sambamba na ukuaji na kuimarika sambamba na nguvu, na kwa ujumla zitakuwa zile zile katika maisha ya baada ya kufa yaani katika maisha ya milele, na zitaendelea tu kuwa na nguvu. {3T 143.2}

Tunaishi katika wakati ambao karibu kila kitu ni cha juu juu. Kuna utulivu na uthabiti wa tabia kidogo sana, kwa kuwa mafunzo na elimu ya watoto kutoka utoto wao ni ya kijuu juu tu. Tabia zao zimejengwa juu ya mchanga unaoteleza. Kujikana nafsi na kujitawala havijaundwa pamoja kwenye tabia zao. Wamedekezwa na kuendekezwa, wakiachiliwa hadi wameharibika wasifae kwa maisha halisi. Kupenda starehe kunatawala akili, na watoto huchelewesha na kuingizwa kwenye uangamivu wao. Watoto wanapaswa kufundishwa na kuelimishwa kwamba watarajie majaribu na wajiandae kukabili shida na hatari. Wanapaswa kufundishwa kujitawala wenyewe na kwa heshima kushinda matatizo; na ikiwa hawataki kuingia shidani, wasijiweke katika njia ya majaribu kwa kupanga; ikiwa wataepuka mivuto miovu na makundi mabaya, halafu wanalazimika kuwa katika makundi hatarishi, watakuwa na nguvu ya tabia [itakayowawezesha] kusimama katika haki na kulinda kanuni, na wataondoka kwa nguvu ya Mungu na maadili yao yakiwa hayajawekwa ulema au kuchafuliwa. Ikiwa vijana ambao wameelimishwa vyema watamfanya Mungu kuwa tumaini lao, nguvu zao za kimaadili zitalishinda jaribu lenye nguvu zaidi. {3T 143.3}

Lakini ni wazazi wachache wanaotambua kuwa watoto wao wako vile ambavyo mfano na nidhamu zao zimewatengeneza, na kwamba wanawajibika kwa tabia ambazo watoto wao wanazikuza. Ikiwa mioyo ya wazazi wa Kikristo ingetii mapenzi ya Kristo, wangetii agizo la Mwalimu wa mbinguni: “Bali utafuteni kwanza ufalme Wake, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Ikiwa wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangefanya tu hili, wagetoa, siyo tu kwa watoto wao, bali kwa ulimwengu ambao hauamini, mifano ambayo ingeweza kuwakilisha dini ya Biblia. {3T 144.1}

Ikiwa wazazi Wakristo waliishi kwa kutii matakwa ya Mwalimu wa mbinguni, wangetunza unyenyekevu katika kula na katika kuvaa, na wangeishi zaidi kulingana na sheria ya asili. Hawangeweza kutumia wakati mwingi sana kwa maisha ya bandia/feki, wakijihangaisha wenyewe na mizigo ambayo Kristo hajaweka juu yao, lakini ambayo amewaagiza kabisa waiepuke. Kama ufalme wa Mungu na haki yake vingetiliwa maanani na kupewa kipaumbele na wazazi, hakuna

muda mdogo wenye thamani ambao ungepotezwa kwa mapambo ya nje yasiyo ya lazima wakati akili za watoto wao, zikiwa katika hali ya kupuuzwa kabisa. Wakati wa thamani ambao wazazi wengi huutumia kuwavalisha watoto wao ili wakajioneshe katika matamasha yao ya maburudiko, ingekuwa bora, na bora zaidi, [kama wakati huo] ungetumika kukuza akili zao wenyewe ili waweze kuwa na uwezo wa kufundisha watoto wao vizuri. Siyo muhimu kwa wokovu au furaha ya wazazi hawa kwamba watumie wakati mzuri wa kipindi cha kupimwa ambacho Mungu amewapatia, [na kuutumia] katika kuvaa, kutembelea, na kusengenya. {3T 144.2}

Wazazi wengi wanasihi kwamba wana shughuli nyingi za kufanya hivi kwamba hawana wakati wa kuboresha akili zao, kuwaelimisha watoto wao kwa maisha ya vitendo, au kuwafundisha namna wanavyoweza kuwa kondoo wa zizi la Kristo. Ni hadi kwenye makao ya mwisho, wakati kesi za wote zitakapoamuliwa, na matendo ya maisha yetu yote yatakapowekwa wazi machoni petu, mbele za Mungu na Mwana-Kondoo na malaika wote watakatifu, ndipo wazazi watakapotambua thamani isiyo na kipimo ya wakati wao uliotumika vibaya. Wengi sana watatambua kwamba njia yao mbaya imeamua hatima ya watoto wao. Siyo tu wameshindwa kujipatia wao wenyewe Maneno ya pongezi kutoka kwa Mfalme wa utukufu, “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu . . . ingia katika furaha ya bwana wako,” lakini wanasikia kutangazwa juu ya watoto wao shutuma mbaya, “Ondokeni!” Jambo hili linawatenganisha watoto wao na furaha na utukufu wa mbinguni milele, na kutoka kwenye uwepo wa Kristo. Nao wenyewe pia wanapokea laana: Ondoka, “Wewe mtumwa mbaya na mlegevu.” Yesu kamwe hatasema “Vema” kwa wale ambao hawajashugulikia “Umefanya vizuri” kwa maisha yao ya uaminifu ya kujikana nafsi na kujitoa mhanga kuwafanyia wengine mema na kukuza utukufu Wake. Wale ambao huishi kwa kanuni/kusudi la kujipendeza wenyewe badala ya kuwatendea wengine mema watakabiliana na hasara ya milele. {3T 145.1}

Kama wazazi wangeweza kuamshwa na hisia ya jukumu la kuogofya ambalo liko juu yao katika kazi ya kuwafundisha watoto wao, muda wao mwingi ungetolewa kwa maombi na siyo kwa onesho lisilo la lazima. Wangeweza kutafakari na kusoma na kuomba kwa dhati na bidii kwa Mungu ili wapate hekima na msaada wa Masihi wa kuwafundisha watoto wao na ili wakuze tabia ambazo Mungu atazikubali. Wasiwasi wao haungekuwa ni kwa jinsi gani wanaweza kuwasomesha watoto wao ili wasifiwe na kuheshimiwa na ulimwengu, lakini ni jinsi gani wanaweza kuwaelimisha kuunda tabia nzuri ambazo Mungu atazikubali. {3T 145.2}

Mafunzo mengi, kusoma na kuomba kwa bidii kwa ajili ya hekima ya mbinguni kunahitajika ili kujua jinsi ya kushughulika na akili za ujana, kwani inategemea sana mwongozo ambao wazazi hutoa kwa akili na mapenzi ya watoto wao. Kusawazisha (balance) akili zao katika mwelekeo sahihi na kwa wakati unaofaa ni

kazi muhimu zaidi, kwani hatima yao ya milele inaweza kutegemea maamuzi yaliyofanywa wakati fulani wa dharura. Ni muhimu kiasi gani basi, kwamba akili za wazazi ziwe huru kadiri inavyowezekana kutoka kwenye mifadhaiko, kuhangaikia mambo ya kidunia, ili waweze kufikiria na kutenda kwa kuzingatia utulivu, hekima, na upendo, na kufanya wokovu wa roho za watoto wao kuwa jambo la kwanza na la juu kabisa! Kusudi kubwa ambalo wazazi wanapaswa kutafuta kulifikia kwa ajili ya watoto wao wapenzi ni mapambo ya ndani. Wazazi hawawezi kuthubutu kuruhusu wageni na watu wasiyowajua kudai umakini/usikivu wao, na kwa kuwanyang'anya muda, ambao ni mtaji mkubwa wa maisha, na kufanya isiwezekane wao kuwapa watoto wao kila siku maagizo ya subira ambayo inawapasa kuwa nayo ili kutoa mwelekeo sahihi kwa akili zao zinazokua. {3T 146.1}

Muda huu wa maisha ni mfupi sana kiasi cha kutoweza kufujwa bure katika mambo madogo, katika kutembeleana/ziara zisizo na faida, kwa mavazi yasiyo ya lazima kwa ajili ya kujionesha, au katika burudani za kujifurahisha. Hatuwezi kumudu kutumbua wakati tuliopewa na Mungu ili [kuutumia] kuwabariki wengine na kujiwekea hazina mbinguni. Hatuna wakati mwingi sana wa kutekeleza majukumu muhimu. Tunapaswa kutoa wakati kwa elimu/utamaduni/desturi za mioyo yetu na akili zetu ili tuweze kufuzu kwa kazi yetu ya maisha. Kwa kupuuza majukumu haya muhimu na kufuata tabia na desturi za jamii ya mazoea, ya kimitindo ya ulimwengu, tunajifanyia sisi wenyewe na watoto wetu kosa kubwa. {3T 146.2}

Akina mama wenye akili za ujana za kufundisha na wenye tabia za watoto zinazohitaji kuundwa hawapaswi kutafuta msisimko wa ulimwengu ili kuwa wachangamfu na wenye furaha. Wana kazi muhimu ya maisha, na hawawezi kutumia muda kwa njia isiyo na faida. Wakati ni moja ya talanta muhimu ambazo Mungu ametukabidhi na ambazo Yeye atatutaka tuutolee mahesabu. Kupoteza wakati ni kupoteza akili. Nguvu za akili ni rahisi kukabiliwa na ukuzwaji wa juu. Ni jukumu la akina mama kukuza na kupalilia akili zao na kuweka mioyo yao safi. Wanapaswa kuboresha kila njia iliyo karibu nao kwa ajili ya uboreshaji wao wa kiakili na kimaadili, ili waweze kuhitimu katika kuboresha akili za watoto wao. Wale wanaojiingiza kwenye tabia ili kuyaridhisha makundi yao, hivi karibuni watahisi kutotulia hadi watakapotembelea au kuburudisha wageni. Watu kama hawa hawana nguvu ya kukabiliana na mazingira. Hawapendelei kujichunguza au kujiadabisha. Akili huwa na njaa ya mionekano ya maisha mbalimbali ya kidunnia; watoto hupuuzwa kwa ajili ya kuridhishwa na mambo yenye viwango duni; na malaika wanaochukua kumbukumbu huandika: “Watumishi wasiyo na faida.” Mungu alikusudia kuwa akili zetu zisiwe zisizo na makusudi, bali zile zinazopaswa kutimiza mema katika maisha haya. {3T 146.3}

Kama wazazi wangehisi kuwa ni jukumu zito lililowekwa juu yao na Mungu kuwafundisha watoto wao ili wafae katika maisha haya; kama wangelipamba

hekalu la ndani la roho za wana na binti zao kwa maisha ya kutokufa, tungeshuhudia mabadiliko makubwa na yaliyo bora katika jamii. Pasingeshuhudiwa hali ya kutozingatiwa uchaji Mungu wa vitendo, na isingekuwa vigumu sana kuamsha hisia za maadili za watoto kuelewa madai ambayo Mungu anayo juu yao. Lakini wazazi huwa wazembe zaidi na zaidi katika kuelimisha watoto wao katika matawi/mambo muhimu. Wazazi wengi huruhusu watoto wao kuunda tabia mbaya na kufuata mwelekeo wao, na wanashindwa kutia akilini mwao hatari ya kufanya hivi na umuhimu wa kudhibitiwa na kanuni. {3T 147.1}
Mara nyingi watoto huanza kipande cha kazi kwa shauku, lakini, wakichanganyikiwa au kuchoshwa nacho, hutamani kubadilisha na kuanza kitu kingine kipya. Kwa njia hiyo waweza kushika mambo kadhaa, na wakikutana na changamoto ndogo, hukata tamaa, na hivyo huacha kazi moja na kuiendea nyingine, bila kukamilisha chochote. Wazazi hawapaswi kuruhusu kupenda mabadiliko kuwatawale watoto wao. Wasijishughulishe sana na vitu vingine kiasi cha kukosa muda wakiadabisha kwa uvumilivu akili zinazokua. Maneno machache ya kutia moyo, au msaada kidogo kwa wakati unaofaa, vyaweza kuwabeba juu ya shida na kuvunjika moyo kwao, na kuridhika watakopata kutokana na kuona kazi waliyoifanya na iliyokamilika itawachochea kufanya juhudi zaidi. {3T 147.2}

Watoto wengi, kwa kukosa maneno ya kutia moyo na msaada kidogo katika juhudi zao, wanakata tamaa na hubadilika kutoka kitu kimoja kwenda kingine. Na wanabeba mapungufu haya ya kusikitisha hadi katika maisha ya utu uzima. Wanashindwa kufanikiwa kwa chochote wanachoshiriki, kwani hawajafundishwa kuvumilia chini ya hali za kukatisha tamaa. Kwa hivyo maisha yote ya wengi huthibitisha kutofaulu, kwa sababu hawakuwa na nidhamu sahihi wakati wa utoto/ujana. Elimu inayopatikana katika utoto na ujana huathiri taaluma yao yote ya biashara katika maisha ya utu uzima, na uzoefu wao wa kidini hubeba alama inayolingana nayo. {3T 148.1}

Kazi za mikono (mwili) kwa Wanafunzi

Pamoja na kuwepo kwa mpango wa sasa wa elimu mlango wa jaribu umefunguliwa kwa vijana. Ingawa kwa ujumla wana masaa mengi ya kusoma, wana masaa mengi yasiyo na chochote cha kufanya. Saa hizi za burudani hutumiwa mara kwa mara kwa njia ya hovyo. Ujuzi wa tabia mbaya huwasilishwa kutoka kwa mmoja hadi mwingine, na uovu huongezeka sana. Vijana wengi sana ambao wamefundishwa kwa njia ya dini ya nyumbani, na ambao huenda shuleni wakiwa hawana hatia na wema, wanaharibikiwa kwa kushirikiana na wenzao waovu. Wanapoteza heshima binafsi na huzitoa mhanga zile kanuni bora. Ndipo hujiandaa kufuata njia ya kuelekea/kushuka chini, kwa kuwa wametumia vibaya dhamiri zao hata dhambi haionekani kuwa kubwa mno. Uovu huu, ambao upo katika shule ambazo zinaendeshwa kulingana na mpango wa sasa, unaweza kurekebishwa kwa kiwango

kikubwa ikiwa masomo na kazi zinaweza kuunganishwa. Uovu ule ule upo katika shule za juu, ila kwa kiwango kikubwa; kwani vijana wengi wamejielimisha wenyewe katika uovu, na dhamiri zao zimeunguzwa. {3T 148.2}

Wazazi wengi hupuuza uimara na sifa nzuri za watoto wao. Hawaonekani kufikiria kuwa [watoto wao] wataingizwa katika ushawishi wa udanganyifu wa vijana watukutu. Wazazi huwa na hofu pale tu wanapowapeleka [watoto wao] shule za mbali, lakini wanajifariji kwamba, kwa kuwa wamekuwa na mifano mizuri na mafundisho ya kidini, watakuwa wakweli kwa kanuni katika maisha yao ya shule zao za masomo ya juu (sekondari, au chuo). Wazazi wengi wana uelewa mfinyu juu ya kiwango gani cha uasherati kilichopo katika taasisi hizi za mafunzo. Katika matukio mengi wazazi wamefanya bidii na wamepata shida nyingi hata kukosa chakula na mahitaji muhimu kwa kusudi la kutaka kuwapatia watoto wao hatima ya elimu iliyo bora. Na baada ya juhudi zao zote, wengi wana uzoefu mchungu wa kupokea watoto wao kutoka kwa hatua zao za masomo wakiwa na tabia mbaya na mwenendo ulioharibiwa. Na mara nyingi huwa hawaheshimu wazazi wao, na huwa wasiyo na shukrani, na wasiyo watakatifu. Wazazi hawa wanaonyanyaswa, wanaozawadiwa hivi na watoto hawa wasiyo na shukrani, hulalamika kwamba waliwatuma watoto wao kutoka kwao ili wakaingizwe kwenye vishawishi na kurudi kwao wakiwa wameharibika mwili, akili, na maadili. Wakiwa na matumaini yaliyokatishwa tamaa na mioyo iliyokaribia kuvunjika wanawaona watoto wao, ambao walikuwa na matarajio makubwa, wakifuata njia ya uovu huku wakiendesha maisha mabaya na ya huzuni. {3T 149.1}

Lakini kuna wale wenye kanuni zilizo thabiti ambao hujibu/huitikia matarajio ya wazazi na waalimu. Wanapitia hatua ya kusoma wakiwa na dhamiri safi na hutoka na mwenendo nzuri na maadili yasiyotiwa doa na ushawishi mbaya. Lakini hawa wa aina hii ni wachache. {3T 149.2}

Wanafunzi wengine huweka maisha yao yote katika masomo yao na kuziwekea mkazo akili zao juu ya kusudi la kupata elimu. Wanaushughulisha ubongo, lakini hawaruhusu nguvu za mwili kubaki zikiwa hazifanyi kazi. Ubongo umefanyishwa kazi kupita kiasi, na misuli huwa dhaifu kwa sababu ya kutotumiwa. Wanafunzi hawa wanapohitimu, ni dhahiri kwamba wamepata elimu yao kwa hasara ya maisha. Wamesoma usiku na mchana, mwaka baada ya mwaka, wakiziweka akili zao kila wakati kwenye mtanuko, wakati wakiwa wameshindwa kufanya mazoezi ya kutosha ya misuli yao. Wanatoa kafara yote kwa ajili ya kupata ujuzi wa sayansi, na hivyo hujiweka tayari kuelekea kwenye makaburi yao. {3T 149.3}

Mabinti mara nyingi hujitolea kusoma huku wakipuuza mikondo mingine ya elimu muhimu zaidi kwa maisha ya vitendo kuliko usomaji wa vitabu. Na baada ya kupata elimu yao, mara nyingi hudhihirika kuwa elimu hiyo huwaletewa ulema wa namna

fulani au kutokuwa na manufaa katika maisha. Walipuuza afya zao kwa kubaki sana ndani ya nyumba, kujinyima hewa safi ya mbinguni na mwangaza wa jua unaotolewa na Mungu. Mabinti hawa wachanga wangeweza kutoka kwenye shule zao wakiwa na afya, kama wangejumuisha kwenye masomo yao kazi za nyumbani na mazoezi ya nje ya nyumba. {3T 150.1}

Afya ni hazina kubwa. Ndiyo utajiri mkubwa zaidi wanadamu wafao wawezao kumiliki. Utajiri, heshima, au masomo hununuliwa kwa gharama kubwa, hata kwa kupoteza nguvu ya afya. Hakuna yoyote katika mafanikio hayo inayoweza kukupa furaha, kama afya itakuwa imetindika/haipo au kuna ugonjwa. Ni dhambi mbaya kutumia vibaya afya ambayo Mungu ametupatia; kwani kila matumizi mabaya ya afya hutudhoofisha maisha yote na kutufanya tushindwe, hata kama tungepata kiwango chochote cha elimu. {3T 150.2}

Katika matukio mengi wazazi ambao ni matajiri hawahisi umuhimu wa kuwapa watoto wao elimu inayoendana na majukumu ya maisha na inayoendana pia na sayansi. Hawaoni umuhimu, kwa faida ya akili na maadili ya watoto wao, na kwa faida yao ya baadaye, kuwapa uelewa kamili wa kazi inayofaa. Hii ni kwa kuwa watoto wao, kama wangepatwa na bahati mbaya au janga/shida, wangeweza kusimama katika uhuru mzuri, wakijua kutumia mikono yao. Ikiwa wana mtaji wa nguvu hawawezi kuwa masikini, hata ikiwa hawana senti. Wengi ambao katika ujana walikuwa katika hali tajiri wanaweza kuibiwa utajiri wao wote na kuachwa na wazazi na kaka na dada wanaowategemea. Basi ni muhimu sana kiasi gani kwamba kila kijana aelimishwe kufanya kazi, ili aweze kujiandaa kwa hali ya dharura yoyote! Utajiri kwa kweli ni laana pale wenye kuumiliki wanapouruhusu kusimama katika njia ya wana na binti zao [na kuwazuia] kupata maarifa ya kazi inayofaa na yenye manufa, itakayowawezesha kufuzu kwa maisha ya vitendo. {3T 150.3}

Wale ambao hawalazimiki kufanya kazi, mara nyingi hawana mazoezi ya kutosha ya afya ya mwili. Vijana, kwa kushindwa kuzifanya akili na mikono yao kutumika katika kazi ya vitendo iliyo hai, wanapata tabia ya uvivu na mara nyingi hupata kile kinachotisha zaidi, elimu ya mitaani/barabarani – wakizururazura madukani, wakivuta sigara, kunywa pombe, na kucheza karata. {3T 150.4}

Mabinti watasoma riwaya, wakijitolea udhuru wa kutofanya kazi ngumu kwa kwa kisingizio kuwa wana afya dhaifu. Udhaifu wao ni matokeo ya kukosa mazoezi ya misuli ambayo Mungu amewapa. Wanaweza kudhani kuwa wao ni dhaifu sana kufanya kazi za nyumbani, ila wanapenda kushona, kutarizi na kujipamba kwa urembo nyusoni mwao na mikononi, na hivyo kuhifadhi uteke-teke wa mikono na nyuso zao zinakuwa zimepauka bila kuwa na rangi nzuri ya kuonyesha damu inatiririka vizuri kama inavyopaswa kiafya (pale), huku mama zao wenye kulemewa wakijitahidi sana kuosha na kupiga pasi nguo zao. Mabinti hawa siyo

Wakristo, kwa sababu wanakiuka amri ya tano. Hawawaheshimu wazazi wao. Lakini mama ndiye anayepaswa kulaumiwa zaidi. Amewadekesha binti zake na kuwaachilia wasitekeleze sehemu yao ya majukumu ya nyumbani, mpaka kazi imekuwa na ladha mbaya kwao, na wanapenda na kufurahia uvivu na kukaa bila kazi. Wao hula, na kulala, na kusoma riwaya, na kuzungumza juu ya mitindo/fasheni, wakati maisha yao hayana maana/manufaa. {3T 151.1}

Umaskini, katika hali nyingi, ni mbaraka; kwa kuwa unazuia vijana na watoto kuharibiwa na kutojishughulisha na kazi. Nguvu za mwili na akili pia zinapaswa kupaliliwa na kukuzwa vizuri. Huduma ya kwanza na ya mara kwa mara ya wazazi inapaswa kuwa kuona watoto wao wakiwa na viungo/afya imara, ili waweze kuwa wanaume na wanawake wenye busara wenye hali ya maisha bora. Haiwezekani kufikia hali hii bila mazoezi ya mwili. Kwa afya yao ya mwili na maadili mema, watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi, hata ikiwa hakuna ulazima wowote kwa kuwa wamejitosheleza kwa mahitaji yote. Kama wangekuwa na tabia safi na njema wanapaswa kuwa na nidhamu ya kazi iliyoratibiwa vyema, ambayo ingeipatia mazoezi misuli yote. Kuridhika ambako watoto watajipatia, kwa kutumika kwao, na kwa kujinyima ili kuwasaidia wengine, watakuwa ni wenye raha yenye afya zaidi waliyowahi kuifurahia. Kwa nini matajiri na watoto wao wajikoseshe mbaraka huu mkubwa? {3T 151.2}

Enyi wazazi, kutoshughulisha kwa kazi za mikono/mwili ni laana kubwa kabisa ambayo imewahi kuja juu ya ujana. Binti zako hawapaswi kuruhusiwa kulala kitandani asubuhi na mapema, wakiyatumia masaa ya thamani waliyopewa na Mungu kwa makusudi yasiyo bora na ambayo watalazimika kuyatolea hesabu. Mama huwaumiza watoto wake wa kike kwa kubeba mizigo ambayo walipaswa kushiriki naye kwa faida yao ya sasa na ya baadaye. Hatua ambayo wazazi wengi hufuata kwa kuwaruhusu watoto wao kuwa wavivu na kutosheleza hamu yao ya kusoma hadithi za mahaba haiwafai kwa maisha halisi. Usomaji wa riwaya/tamthiliya na hadithi ni maovu makubwa zaidi ambayo vijana wanaweza kujiingiza. Usomaji wa riwaya na vitabu vya hadithi za mapenzi ni maovu makuu ambayo vijana wamejitumbukiza kwayo na huwafanya wasiwe wakina mama wanaoweza kushiriki katika maisha ya utendaji na manufaa. Wao ni wajenzi wa majumba makubwa hewani, wanaoishi katika ulimwengu usiyo halisi, ulimwengu wa kufikirika. Wanakuwa wepesi wa kuvutwa na hisia za mahaba/mapenzi na na ulimwengu wa kufikirika wenye matamanio ya kujidanganya. Maisha yao ya bandia/feki yanawaharibu na kuwafanya wasifae kwa kitu chochote muhimu. Wamedumazwa akili, japo wanaweza kujidanganya kuwa wao ni bora katika akili, mwenendo, haiba na tabia. Mazoezi katika kazi za nyumbani ni yenye faida kubwa kwa wasichana wadogo. {3T 151.3}

Kazi ya mwili/mikono haizuii ukuzwaji wa akili. Mbali na hilo. Faida ipatikanayo kwa kazi ya mwili/mikono itamweka mtu katika uwiano na kuzuia akili

kufanyishwa kazi kupita kiasi. Mateso yanayotokana na ile kazi yataingia kwenye misuli na kuutuliza ubongo uliochoka. Kuna wasichana wengi wasiotulia, wasiyo na manufaa ambao wanachukulia kuwa si jambo linalowastahili wanawake kufanya kazi ngumu. Lakini tabia zao ni wazi sana kuweza kuwadanganya watu wenye busara kwa kuzingatia kutokuwa na thamani kwao. Wanatabasamu kwa njia ya ujinga na kuudhi watu wakitakata kusifu watu na kujaribu kuwa wazuri kwao na kucheka-cheka huku wakiwa na wasiwasi na tabia yao inakuwa isiyo na uhalisia (feki) iliyo na maigizo tu ya kuvuta umakini wa watu uende kwao katika vitendo vyaoau matamshi (simpering and gigling and all affectations). Wanaonekana kana kwamba hawangeweza kusema maneno yao sawasawa na kwa kunyoka, kama vile wana kithembe, wana tabasamu za kipumbavu, lakini chambua yote wayasemayo kwa kutamka maneno vibaya kutokana na kutengeneza midomo au ulimi kama wana ‘kithembe’ na kutabasamu kusiko kwa kweli au kwa kujikomba (tabasamu za plastiki au feki). Je! hawa ni wanawake/mabinti? Hawakuzaliwa wapumbavu, lakini wameelimishwa kuwa hivyo. Hapahitajiki mtu dhaifu, jambo lisilo na msaada, uvaaji wenye mapambo mengi au kuzungumza kwa madaha ya kithembe ili kumfanya mwanamke. Mwili ulio na afya nzuri unahitajika ili kuwa na akili na busara bora. Mwonekano mzuri na elimu ya vitendo ya majukumu muhimu ya nyumbani haviwezi kuwa kipingamizi kwa akili iliyokuzwa vyema; yote mawili ni muhimu sana kwa mwanamke. {3T 152.1}

Nguvu zote za akili zinapaswa kutumiwa na kukuzwa ili wanaume na wanawake wawe na akili zenye uwiano/utimamu. Ulimwengu umejaa wanaume na wanawake wenye mwelekeo wa upande mmoja ambao wamekuwa kama hivyo kwa sababu seti moja ya viungo vyao ilipaliliwa wakati seti ya upande mwingine ilidumazwa kwa kutotumika. Elimu ya sehemu kubwa ya vijana imeshindwa. Wamesoma kupita kiasi, huku wakipuuzia kile kinachohusiana na shughuli za maisha halisi. Wanaume na wanawake huwa wazazi bila kuzingatia majukumu yao, na watoto wao hushuka chini katika mizani ya mapungufu ya mwanadamu kuliko wao wenyewe walivyo. Katika hali hiyo jamii ya wanadamu hushuka kwa kasi kubwa. Maombi ya kudumu ya kujiunga na masomo-kusajili, kama yanavyofanyika sasa mashuleni, hayawaandai vijana kwa maisha halisi. Akili ya mwanadamu inahitaji kushughulishwa. Kama haishughulishwi katika welekeo sahihi, itajishughulisha katika mwelekeo usiyo sahihi. Ili kudumisha uwiano wa akili, kazi na masomo ni lazima viunganishwe shuleni. {3T 152.2}

Mpango ulipaswa uwe umewekwa katika vizazi vilivyopita kwa ajili ya elimu katika vipimo vikubwa. Katika shule hizo palipaswa kuanzishwa vitengo vya kilimo na viwanda au miradi ya kazi zenye kumshugulisha mtu. Pangepaswa pia kuwepo waalimu wa kazi za nyumbani. Na sehemu ya muda wa shule kila siku ulipaswa kutumika kwa kazi za mikono, ili uwezo wa akili na mwili viweze kutumika kwa

uwiano ulio sawa. Kama shule zingeanzishwa juu ya mpango tulioelezea, leo hii kusingekuwa na akili nyingi zisizo na uwiano ulio sawa. {3T 153.1}

Mungu aliandaa kwa ajili ya Adamu na Hawa bustani nzuri [hakuwaweka ghorofani au mjini]. Aliwapatia kila kitu ambacho matamanio yao yalikihitaji. Aliwapandia miti izaayo matunda ya kila aina. Kwa mkono wenye ukarimu aliwazungushia kwa fadhila zake. Miti yenye manufaa na mizuri, na maua ya kupendeza ambayo yalichipuka yenyewe na kushamiri kwa wingi mwingi karibu nao, hayakujua chochote juu ya kuoza. Adamu na Hawa walikuwa matajiri kweli kweli. Walimiliki Edeni. Adam alikuwa bwana katika miliki yake mzuri. Hakuna ambaye angeweza kuhoji ukweli kwamba alikuwa tajiri. Lakini Mungu alijua kwamba Adamu hangekuwa na furaha hadi atakapopewa kazi ya kufanya. Kwa hiyo akampa kazi ya kufanya; alipewa kazi ya kutunza bustani. {3T 153.2}

Kama wanaume na wanawake wa kizazi hiki kilichopotoka wana kiasi kikubwa cha hazina ya kidunia, ambacho, kikilinganishwa na kile cha Paradiso yenye uzuri na ya kitajiri aliyopewa bwana mkubwa Adamu, huonekana si chochote, wanawezaje kujihisi kuwa juu ya kazi za mikono na kuwaelimisha watoto wao kuiangalia kazi ya mikono kama kitu cha kudhalilisha? Wazazi matajiri kama hao, kwa mafundisho na mifano wanayoonesha, wanawaelekeza watoto wao kuwa pesa humfanya mtu kuwa binadamu muungwana na mwanamke mtanashati [wa kuheshimiwa lady and gentleman]. Lakini wazo letu la muungwana na mwanamke wa kuheshimiwa hupimwa kupitia akili na thamani ya maadili [aliyonayo mtu]. Mungu hakadirii kwa mavazi. Shauri la mtume Petro aliyevuviwa ni: “Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usiyoonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.” Roho ya upole, unyenyekevu na utulivu huinuliwa juu ya heshima au utajiri wa dunia. {3T 153.3}

Bwana anafundisha kwa vitendo jinsi anavyowakadiria matajiri wa kilimwengu wanaoinua roho zao kwa ubatili kwa sababu ya mali zao za kidunia, na tajiri anayebomoa ghala zake na akajenga kubwa zaidi, ili apate nafasi zaidi ya kuweka mali zake. Akimsahau Mungu, alishindwa kutambua mali zake zote zilitoka wapi. Hakuna shukrani zilizopanda kwa mfadhili wake mwema. Alijipongeza hivi: “Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi.” Bwana Mfadhili, ambaye alikuwa amemkabidhi utajiri wa kidunia kwa ajili ya kuwabariki wenzie na kumtukuza Muumba wake, alikasirika kwa haki juu ya kutokuwa na shukrani kwake na akasema: “Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.” Hapa tuna kielelezo cha jinsi Mungu asiye na mwisho/ukomo anavyomkadiria mwanadamu. Utajiri mkubwa, au kiwango chochote cha utajiri, hautapata

upendeleo wa Mungu. Fadhila na baraka hizi zote hutoka Kwake ili kuthibitisha, kupima, na kukuza tabia ya mwanadamu. {3T 154.1}

Wanadamu wanaweza kuwa na mali isiyo na mipaka; lakini ikiwa hawajajitajirisha kwa Mungu, na ikiwa hawapendelei kujiwekea hazina ya mbinguni na hekima ya Mungu, wanahesabiwa kuwa wapumbavu na Muumba wao, na sisi tunawaacha pale pale Mungu alipowaacha. Kazi ni mbaraka. Haiwezekani tukafurahia afya bila kufanya kazi. Viungo vyote ni lazima viingizwe kwenye matumizi ili viweze kukuzwa vyema na ili wanaume na wanawake wawe na akili zenye uwiano ulio sawa. Kama vijana wangekuwa wamepewa elimu kamili katika mikondo mbalimbali ya kazi za mikono katika matawi mbalimbali kama wangekuwa wamefundishwa kazi za mikono kama walivyofundishwa sayansi, elimu yao ingekuwa ya faida kubwa kwao. {3T 154.2}

Mkazo wa kudumu kwenye ubongo wakati misuli haifanyi kazi, hudhoofisha mishipa, na wanafunzi huwa na hamu isiyoweza kudhibitiwa ya mabadiliko na burudani za kutumbuiza na kusimumua. Na wanapoachiliwa, baada ya kushikiliwa kwenye masomo kwa masaa kadhaa kila siku, huwa na tabia kama za wanyama pori. Wengi hawajawahi kuthibitiwa wakiwa nyumbani. Wameachwa kufuata mwelekeo wao, nao hufikiri kwamba kizuizi cha masaa ya kusoma ni mwelemeo mkubwa juu yao; na kwa kuwa hawana chochote cha kufanya baada ya masaa ya kusoma, Shetani hupendekeza mchezo na mambo yenye madhara ili kuleta mabadiliko. Ushawishi wao juu ya wanafunzi wengine unavunja moyo. Wale wanafunzi waliowahi kunufaika na mafundisho ya dini nyumbani, na ambao hawajui maovu ya jamii, mara nyingi huwa wanazoeana zaidi na wale ambao akili zao zimetelekezwa katika hali duni, na ambao kunufaika kwao juu ya utamaduni wa akili na mafunzo ya dini kulikuwa kudogo sana. Na wapo katika hatari, kwa kuchanganyika katika jamii ya watu wa daraja hili na kwa kupumua mazingira ambayo hayainui bali ambayo yana mwelekeo wa hushusha na kudhalilisha maadili, nao huzama kwa kiwango cha chini sawa na wenzao. Ni furaha ya sehemu kubwa ya wanafunzi wa kundi hili, katika masaa yao yasiyo ya kazi, kuwa na wakati mzuri. Na wengi wa wale waondokao majumbani mwao wakiwa hawana hatia na safi huharibiwa na makundi yao wakiwa shuleni. {3T 155.1}

Nimeongozwa kuuliza: Je! Ni lazima mambo yote yale yenye thamani katika ujana wetu yateketezwe ili kupata elimu ya shuleni? Kama kungekuweko na vitengo vya kilimo na viwanda vilivyounganishwa na shule zetu, na vikawa na waalimu mahiri walioajiriwa kufundisha vijana katika mikondo mbalimbali ya masomo ya nadharia na kazi za mikono, wakitumia sehemu ya siku nzima kukuza akili, na sehemu nyingine ya siku kukuza kazi za mikono, leo hii kungekuwa na daraja la vijana lililoinuliwa zaidi ambao wangejitokeza hadharani na kuonesha vitendo ambavyo vingekuwa na ushawishi katika kuijenga jamii. Vijana wengi ambao wangehitimu katika taasisi kama hizo wangetoka wakiwa na uimara wa tabia. Wangekuwa na

ustahimilivu, ushupavu, na ujasiri kushinda vizuizi, na kanuni ambazo zingewafanya wasiyumbishwe na ushawishi mbaya, hata kama ni ule unaopendwa na watu kiasi gani. Pangetakiwa kuwa na waalimu wazoefu wa kutoa masomo kwa mabinti kwenye idara ya mapishi. Mabinti hawa wangepewa maelekezo ya namna ya kutengeneza mavazi/kushona, namna ya kukata, namna ya kushona, na namna ya kurekebisha mavazi, na hivyo kuwa wameelimishwa kwa ajili ya majukumu halisi ya maisha. {3T 155.2}

Kwa wavulana pangepaswa kuwepo na vituo ambapo wangeweza kujifunza stadi mbalimbali ambazo zingeleta mazoezi ya misuli yao na nguvu zao za akili. Kama vijana wangekuwa na uchaguzi katika kuwa na elimu ya aina moja tu (yaani 1.elimu ya kazi za mikono, au 2.ile ya vitabu na madarasani tu), ni ipi basi ambayo ingekuwa na matokeo bora katika hizo kwenye mabano? Elimu ya sayansi ya vitabuni, – pamoja na hasara zake zote kwa afya na maisha, au elimu ya kazi za mikono kwa ajili ya maisha halisi? Tunajibu bila kusita: ile ya pili. Kama kuna elimu inayopaswa kupuuzwa ni ile ya kusoma vitabu. {3T 156.1}

Kuna wasichana wengi walioolewa na wenye familia ambao wana ujuzi mdogo tu wa majukumu uwezao kumkuza mke na mama. Wanaweza kusoma, na kutumia ala za muziki; lakini hawawezi kupika. Hawawezi kutengeneza ugali/mkate mzuri, ambao ni muhimu sana kwa afya ya familia. Hawawezi kukata na kushona nguo, kwani hawakujifunza jinsi ya kufanya hivyo. Walichukulia mambo haya kuwa yasiyo ya lazima, na katika maisha yao ya ndoa wanategemea mtu kuwafanyia mambo haya kama watoto wao wenyewe wadogo. Huu ni uzembe usiosameheka unaohusu majukumu ya lazima ya maisha ambayo hufanya familia nyingi kuwa zisizo na furaha. {3T 156.2}

Dhana kwamba kazi inadhalilisha maisha ya kisasa ya mitindo/fasheni imeweka maelfu kaburini ambao wangeweza kuwa bado wanaishi. Wale wanaofanya kazi ya mikono peke yake mara nyingi hufanya kazi kupita kiasi na bila kujipa vipindi vya kupumzika; wakati darasa la wasomi lenyewe huutumikisha sana ubongo na huteseka kutokana na kupungukiwa na nguvu yenye afya ambayo hupatikana kwa kufanya kazi za mikono. Kama wasomi au watu wenye akili mahiri wangeshirikiana kubeba mzigo wa darasa la wafanyao kazi za mikono na hivyo kuimarisha misuli yao, wale wafanyao kazi za mikono wangefanya kazi kidogo na kutumia sehemu kubwa ya wakati wao kukuza utamaduni wa akili na maadili. Wale wa tabia ya kukaa tu kivivu na kujifunza kwa nadharia wanapaswa kufanya mazoezi ya mwili, hata ikiwa hawana haja ya kufanya kazi kwa kuwa wamejitosheleza kwa mahitaji ya kifedha. Afya inapaswa kuwa ushawishi wa kutosha kuwaongoza kuunganisha kazi ya mwili na kazi ya akili. {3T 156.3}

Maadili, akili na utamaduni wa mwili vinapaswa kuunganishwa ili kuwapata wanaume na wanawake waliokuzwa vizuri, na wenye uwiano ulio usawa. Baadhi wamehitimu kutumia nguvu kubwa ya kiakili kuliko wengine, wakati wengine

wakiwa na mwelekeo wa kupenda na kufurahia kazi ya mikono. Makundi haya yote mawili yanapaswa kutafuta kuboresha mahali pale penye mapungufu, ili waweze kumletea Mungu, miili mikamiliu ili iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Yeye, inayokubaliwa Naye, iliyo ibada yao yenye maana. Tabia na desturi za jamii ya kimtindo hazipaswi kupima mwenendo wa matendo yao. Mtume Paulo aliyeongozwa/aliyevuviwa na roho ya Mungu anaongeza: “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” {3T 157.1}

Akili za watu wanaofikiri hufanya kazi kwa bidii sana. Mara nyingi hutumia nguvu zao za kiakili kwa kutotumia hekima kama mwana mpotevu, wakati kuna tabaka lingine ambalo lengo lake kubwa maishani ni kazi zinazotumia nguvu za mwili. Tabaka hili la pili haliizoezi akili. Misuli yao hutumika wakati bongo zao zikiwa zimenyang’anywa nguvu ya kiakili, kama ilivyo kwa akili za watu wanaofikiri zinafanyishwa kazi wakati miili yao inaporwa nguvu na uwezo kwa kupuuzia kuzoeza misuli yao. Wale wanaoridhika kuyatumia maisha yao kwa kazi za mwili/mikono na kuwaachia wengine wafikiri kwa ajili yao, huku wakiendeleza kutekeleza yale ambayo bongo zingine ziliyaandaa, watakuwa na nguvu za misuli bali wenye akili dhaifu. Ushawishi wao wa mambo mema ni mdogo ukilinganisha na vile ambavyo ingekuwa kama wangetumia bongo zao kwa kiwango sawa na misuli zao. Watu wa tabaka hili huanguka kirahisi wanaposhambuliwa na maradhi; mfumo hutiwa uhai kwa nguvu za umeme wa ubongo kukinga maradhi. {3T 157.2}

Watu wenye nguvu nzuri za mwili wanapaswa kujielimisha wao wenyewe kufikiri sambamba na kutenda, na wala wasiwategemee wengine kuwa ubongo ulio mbadala wao. Ni kosa linalofanywa na watu wengi kudhani kuwa kazi ni jambo linaloshusha hadhi. Na hiyo ndiyo sababu inayofanya vijana wengi kuwa na hofu na kuamua kujielimisha ili waje kuwa waalimu, makarani, wanasheria, na kushika nafasi nyingine yeyote ambayo haihitaji kazi za nguvu. Mabinti huichukulia kazi ya nyumbani kuwa inayodhalilisha. Na ingawa mazoezi ya mwili huhitajika pale mtu afanyapo kazi ya nyumbani, na mazoezi hayo ikiwa siyo makali sana, huratibu katika kukuza afya, lakini bado [watu] hutafuta elimu itakayowafaa kuwa walimu au makarani, au watajifunza biashara ambayo itawashikilia ndani ya nyumba kwa ajira ya kuketi kwenye viti. Mwonekano wa kiafya hupotea kutoka mashavuni mwao-damu haitembei vizuri, na magonjwa hujikusanya juu yao, kwa kuwa wameporwa mazoezi ya viungo na hivyo tabia zao zimepotoshwa kwa ujumla. Yote hii ni kwa sababu ya kuiga mitindo! Wanafurahia maisha laini, ambayo ni dhaifu na yaliyooza. {3T 158.1}

Ni kweli kuna udhuru kwa mabinti kutochagua kazi za nyumbani kama ajira, kwa sababu wale ambao huajiri wasichana wa jikoni kwa kawaida huwachukulia kama watumishi. Mara kwa mara waajiri wao hawawaheshimu na wanawachukulia kana kwamba hawastahili kuwa sehemu ya familia. Hawawapi maslahi.marupurupu

wanayowapa washonaji, watoa nakala, na walimu wa muziki. Lakini hapawezi kuwa na ajira muhimu zaidi kuliko ile ya kazi za nyumbani. Ili kupika vizuri, kuwasilisha chakula chenye afya mezani kwa nama inayovutia, panahitajika akili na uzoefu. Yule aandaaye chakula kipaswacho kuwekwa matumboni mwetu, ili kigeuzwe damu na kurutubisha mfumo, anachukua nafasi muhimu na ya juu sana. Nafasi ya mtoa nakala za kuchapa, mshonaji, au mwalimu wa muziki haiwezi kuwa sawa kwa umuhimu na ile ya mpishi {3T 158.2}

Maelezo yaliyotangulia ni taarifa ya kile kinachoweza kufanywa na mfumo sahihi wa elimu. Wakati ni mfupi sana sasa kuweza kukamilisha kile ambacho kingeweza kufanywa katika vizazi vilivyopita; lakini tunaweza kufanya mengi, hata katika siku hizi za mwisho, kurekebisha maovu yaliyopo katika elimu ya vijana. Na kwa sababu wakati ni mfupi, tunapaswa kuwa dhati na bidii na kufanya kazi kwa dhati kuwapa vijana elimu ambayo inaambatana na imani yetu. Sisi ni wanamatengenezo. Tunatamani watoto wetu wasome kwa faida iliyo bora zaidi. Ili kufanya haya, wanapaswa kuingizwa kwenye kazi ya mikono itakayoifanya misuli kuingia kwenye mazoezi. Kila siku, kazi ya yenye mfumo na iliyoratibiwa, inapaswa kuwa sehemu ya elimu ya vijana, hata katika kipindi hiki cha mwisho. Mengi sasa yanaweza kupatikana kwa kuunganisha kazi za mikono na shule. Katika kufuata mpango huu wanafunzi watatambua unyoofu wa roho, unyumbulifu na nguvu ya mawazo, na wataweza kukamilisha kazi nyingi zaidi za akili kwa wakati maalum kuliko vile ambavyo wangeweza kufanya kwa kusoma peke yake. Na watakapoondoka shuleni watakuwa na viungo ambavyo havijaharibika, wenye nguvu na ujasiri wa kuvumilia katika nafasi yoyote ambayo uweza wa Mungu unaweza kuwapatia. {3T 158.3}

Kwa sababu wakati ni mfupi, tunapaswa kufanya kazi kwa uadilifu na bidii na kwa nguvu maradufu. Watoto wetu wanaweza wasiingie kamwe vyuoni kamwe, lakini wanaweza kupata elimu katika mikondo hiyo muhimu ambayo wanaweza kuigeuza katika matumizi ya vitendo na yatakayoipa akili utamaduni mpya na kufanya nguvu yake ilete matokeo katika maisha. Wanaweza kuwa na jina la kuwa na elimu ya chuo kikuu, lakini kiuhalisia wao ni mambumbu waliosoma tu bila ya kuelimika. {3T 159.1}

Kuna vijana wengi ambao Mungu angekubali huduma zao kama wangejiweka wakfu Kwake kikamilifu. Kama wangetumia nguvu hizo za akili katika kumtumikia Mungu kama wanavyotumia sasa katika kujihudumia wenyewe na kupata mali, mashamba nk, wangefanya kazi ya mikono kwa dhati, kwa uvumilivu, na kwa mafanikio makubwa shambani mwa Bwana. Vijana wetu wengi wanapaswa kuelekeza mawazo yao kwa kusoma Maandiko, ili Mungu awatumie katika kazi Yake. Lakini hawajawa na akili katika maarifa ya kiroho kama walivyo katika mambo ya kitambo; hivyo wanashindwa kufanya kazi ya Mungu ambayo wangeweza kufanya katika viwango vya kukubalika. Kuna wachache wanaoonya wenye dhambi na kuongoa roho kwa Kristo, wakati ambapo wangepaswa kuwa wengi. Vijana wetu

kwa ujumla ni wenye busara katika maswala ya kidunia, lakini siyo wenye akili katika mambo ya ufalme wa Mungu. Wanaweza kugeuza akili zao na kuzielekeza mbinguni kwa Bwana, na kwenye njia ya Mungu na kutembea kwenye nuru, wakiendelea kutoka kwa kiwango kimoja cha nuru na nguvu hadi kingine ili waweze kuwageuza wadhambi kwa Kristo na kuwaongoza wasiyoamini na waliokata tamaa kwa njia ing'arayo ielekeayo mbinguni. Na vita vitakapomalizika, wanaweza kukaribishwa kwa furaha ya Bwana wao mbinguni. {3T 159.2}

Vijana hawapaswi kuingia kwenye kazi ya kufafanua Maandiko na kutoa hotuba juu ya unabii wakati hawana ujuzi wa Kweli muhimu za Biblia wanazojaribu kuzifafanua kwa wengine. Wanaweza kuwa na mapungufu katika mikondo ya kawaida ya elimu na kwa sababu hiyo kushindwa kufanya kiwango cha mazuri ambacho wangeweza kufanya kama wangekuwa wamesoma kwenye shule nzuri. Ujinga hautaongeza unyenyekevu au hali ya kiroho ya yeyote anayedai kuwa mfuasi wa Kristo. Ukweli wa Neno la Mungu unaweza kuthaminiwa zaidi na Mkristo msomi aliye na akili bora sana. Kristo anaweza kutukuzwa zaidi na wale wanaomtumikia huku wakitumia akili mahiri. Lengo kuu la elimu ni kutuwezesha kutumia nguvu ambazo Mungu ametupatia kwa njia ambayo itawakilisha vyema dini ya Biblia na kukuza utukufu wa Mungu. {3T 160.1}

Tunadaiwa na Yeye aliyetupatia uhai, kwa talanta zote tulizoaminiwa; na ni wajibu tunaodaiwa kwa Muumba wetu kukuza, kupalilia na kuboresha talanta alizotukabidhi. Elimu itaadabisha akili, itakuza nguvu zake, na kwa ufahamu itaziongoza, ili tuweze kutumika vizuri katika kukuza utukufu wa Mungu. Tunahitaji shule ambayo wale wanaoingia tu kwenye huduma wanaweza kufundishwa angalau mikondo ya kawaida ya elimu na ambapo wanaweza pia kujifunza Ukweli wa Neno la Mungu la wakati huu. Katika shule hizi, mihadhara inapaswa kutolewa juu ya unabii. Wale wenye uwezo mzuri hasa na ambao Mungu atakubali wafanye kazi katika shamba Lake la mizabibu watanufaika sana na maelekezo ya miezi michache tu katika shule ya namna hiyo. (161) {3T 160.2}

SURA YA 14

MATENGENEZO YA AFYA

Desemba 10, 1871, nilioneshwa tena kuwa matengenezo ya afya ni tawi moja la kazi kubwa itakayowaandaa watu kwa kuja kwa Bwana. Imeunganishwa kwa karibu na ujumbe wa malaika wa tatu kama vile mkono ulivyo kwa mwili. Sheria ya Amri Kumi imechukuliwa kwa wepesi na wanadamu, lakini Bwana asingekuja kuwaadhibu wahalifu wa sheria hiyo bila kuwatumia kwanza, ujumbe wa onyo. Malaika wa tatu anatangaza ujumbe huo. Laiti kama watu wangewahi kutii sheria ya Amri Kumi, wakitekeleza maishani mwao kanuni za maagizo hayo, laana ya magonjwa ambayo sasa imeifurikisha/imeigharikisha dunia isingekuwepo. {3T 161.1}

Wanaume na wanawake hawawezi kukiuka sheria ya asili kwa kuendekeza hamu mbaya na tamaa mbaya, bila kuvunja sheria ya Mungu. Kwa hivyo Yeye ameruhusu nuru ya matengenezo ya afya kutuangazia, ili tuweze kuona dhambi yetu katika kuvunja sheria alizoziweka katika uhai wetu. Starehe zetu zote au mateso vyaweza kugunduliwa kwamba vimetokana na utii au uvunjaji wa sheria ya asili. Baba yetu wa mbinguni Mwenye neema anaona hali ya kusikitisha ya watu ambao, wengine kwa kujua lakini wengi kwa kutojua, wanaishi kwa kukiuka sheria ambazo ameweka. Na kwa upendo na huruma kwa jamii ya wanadamu, Yeye husababisha nuru kuangaza juu ya matengenezo ya afya. Bwana Anaandika sheria Yake na adhabu ambayo itafuata ukiukaji wake, ili wote wapate kujifunza na kuwa waangalifu kuishi kwa amani na sheria ya asili. Bwana Anatangaza sheria Yake kwa uwazi kabisa na kuifanya iwe ionekane/maarufu sana kiasi kwamba ni kama mji uliowekwa juu ya kilima. Viumbe wote wenye uwajibikaji wanaweza kuielewa ikiwa watataka. Watu waliozaliwa na utindio wa ubongo, au shida ya maradhi ya akili (idiots) hawatawajibika. Kuweka wazi sheria ya asili, na kuhimiza utii wake, ni kazi inayoambatana na ujumbe wa malaika wa tatu kuandaa watu kwa kuja kwa Bwana. {3T 161.2}

Adamu na Hawa walianguka kwa hamu ya kula. Kristo alikuja na kuhimili jaribu kali la Shetani na, kwa niaba ya jamii ya wanadamu, alishinda hamu ya kula, akionesha kwamba mtu anaweza kushinda. Kama Adamu alivyoanguka kupitia hamu ya kula na kupoteza Edeni yenye raha/pleasure, watoto wa Adamu wanaweza, kupitia Kristo, kushinda hamu ya kula na kwa kujizuia katika vitu vyote kuipata tena Edeni. {3T 161.3}

Ujinga siyo udhuru sasa kwa uvunjaji wa sheria. Nuru inaangaza wazi, na hakuna anayehitaji kuwa mjinga, kwani Mungu Mkuu Mwenyewe Ndiye mkufunzi wa mwanadamu. Wote wamefungwa na majukumu matakatifu zaidi kwa Mungu; kutii falsafa bora na ya hekima na uzoefu halisi ambao sasa anawapatia kupitia matengenezo ya afya. Yeye Anapanga kwamba somo kuu la matengenezo ya afya

lichochewe na akili ya jamii ivurugwe sana na kutaka kuchunguza; maana itadhaniwa ni kitu kisichowezekana kwa wanaume na wanawake, wakiwa na tabia zao zote za dhambi, zinazoharibu afya, na zenye tabia ya kudhoofisha ubongo, kugundua na kuuelewa Ukweli mtakatifu, ambao kupitia huo wanapaswa kutakaswa, kusafishwa, kuinuliwa, na kufanywa kufaa kwa jamii ya malaika wa mbinguni katika ufalme wa utukufu. {3T 162.1}

Wakazi wa ulimwengu wa Nuhu waliangamizwa kwa kuwa walikuwa wameharibikiwa tabia kwa njia ya hamu ya chakula ya kupotosha. Sodoma na Gomora ziliharibiwa kwa sababu ya kufurahia hamu ya chakula isiyo ya asili, iliyopumbaza akili sana kiasi kwamba hawakuweza kutambua tofauti kati ya madai matakatifu ya Mungu na mayowe ya hamu ya kula akilini mwao. Hamu ya chakula iliwatumikisha, na wakawa wakali na wenye ujasiri katika machukizo yao ya kuchukiza kiasi kwamba Mungu asingewavumilia waishi duniani. Mungu anauelezea uovu wa Babeli kuwa ulikuwa ulafi na ulevi wake. {3T 162.2}

Mtume Paulo analihimiza kanisa: “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.” Basi, watu wanaweza kuifanya miili yao kuwa siyo mitakatifu kwa njia ya tamaa ya dhambi. Wasipokuwa watakatifu wanakuwa hawajajiandaa kuwa watu waabuduo wa kiroho na hawastahili mbinguni. Ikiwa mtu atathamini nuru ambayo Mungu kwa huruma anampa juu ya matengenezo ya afya, anaweza kutakaswa kupitia Ukweli na kustahili kutokufa. Lakini ikiwa anapuuza nuru hiyo na kuishi kwa kukiuka sheria ya asili lazima alipe adhabu. {3T 162.3}

Mungu alimuumba mwanadamu mkamilifu na mtakatifu. Lakini mwanadamu alianguka kutoka katika makazi yake matakatifu kwa sababu alikiuka sheria ya Mungu. Tangu anguko kumekuwa na ongezeko la kasi la magonjwa, maumivu, mateso, na vifo. Lakini bila kujali kwamba mwanadamu amemtukana Muumba wake, upendo wa Mungu bado umeelekezwa kwa jamii ya wanadamu; Naye anaruhusu nuru kuangaza ili mwanadamu atambue kwamba ili kuishi maisha makamilifu ni lazima aishi kwa amani na sheria hizo za asili zinazotawala nafsi yake. Kwa hivyo ni jambo lenye umuhimu mkubwa zaidi ajue namna ya kuishi ili nguvu zake za mwili na akili zitumike kwa utukufu wa Mungu. {3T 162.4}

Haiwezekani kwa mtu kuutoa mwili wake kama dhabihu iliyo hai, takatifu, na ya kumpendeza Mungu kwa kuwa ni kawaida kwa ulimwengu kufanya hivyo, basi naye anajiingiza katika mazoea ambayo yanapunguza nguvu ya mwili, akili, na maadili. Mtume anaongeza: “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” Yesu, aliketi juu ya Mlima wa Mizeituni, akiwapa wanafunzi Wake maagizo juu ya ishara ambazo zinapaswa kutangulia kuja Kwake. Alisema: “Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa

kuja Kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu." {3T 163.1}

Dhambi hizo hizo zilizoleta ghadhabu ya Mungu juu ya ulimwengu katika siku za Nuhu zipo katika siku zetu. Wanaume na wanawake sasa huendesha ulaji na unywaji wao kwa ulafi na ulevi. Dhambi hii inayotawala, ya kuendekeza tamaa iliyopotoka ya chakula, iliyochochea tamaa za wanadamu katika siku za Nuhu na kusababisha ufisadi wa jumla, hadi ukatili, uovu na uhalifu wao ukafika mbinguni, na Mungu akaiosha dunia kwa gharika kutokana na uchafuzi wake wa maadili. {3T 163.2}

Dhambi zile zile za ulafi na ulevi zilipunguza hisia za maadili za wakazi wa Sodoma ili uhalifu uonekane kuwa furaha ya wanaume na wanawake wa mji huo mwovu. Kwa hivyo Kristo anauonya ulimwengu: "Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku Zake Mwana wa Adamu. Walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakioa na kuolewa, hata siku ile Nuhu aliyoingia katika safina, gharika ikashuka ikawaangamiza wote. Na kadhalika, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga; lakini siku ile Lutu aliyotoka Sodoma kulinyesha moto na kibiriti kutoka mbinguni vikawaangamiza wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu." {3T 163.3}

Kristo hapa ametuachia somo muhimu zaidi. Hahimizi uvivu katika mafundisho Yake. Mfano Wake ulikuwa kinyume cha hilo. Kristo alikuwa mtendakazi dhati na Mwenye juhudi. Maisha Yake yalikuwa ya kujikana nafsi, bidii, uadilifu, uvumilivu, uchapakazi, na ujasiriamali. Ameweka mbele yetu hatari ya kufanya kula na kunywa kuwa jambo la kipaumbele. Anaonesha matokeo ya kuendekeza hamu ya kula. Nguvu za maadili zinafubazwa ili dhambi isiyonekane kuwa mbaya. Uhalifu unafumbiwa macho, na tamaa duni kabisa zinatawala akili hadi ufisadi wa jumla unang'oa kanuni na misukumo mizuri, na Mungu anafanyiwa kufuru. Haya yote ni matokeo ya kula na kunywa kupita kiasi. Hii ndiyo hali ya mambo ambayo Bwana anatangaza itakuwepo wakati wa kuja Kwake mara ya pili. {3T 164.1}

Je! Wanaume na wanawake wataonyeka? Je! Watathamini nuru, au watakuwa watumwa wa hamu ya kula na tamaa za maadili machafu yanayoelekea chini? Kristo anatupatia kitu cha juu cha kukihangaikia kuliko tu kuhangaikia tutakula nini, na tutakunywa nini, na tutavaa nini. Kula, kunywa, na kuvaa huhangaikiwa kupita kiasi hivi kwamba vinakuwa uhalifu, na hizi ni miongoni mwa dhambi zilizotajwa za siku za mwisho, na ni ishara ya kuja kwa Kristo upesi. Muda, pesa, na nguvu, ambavyo ni vya Bwana, lakini ambavyo ametukabidhi, vinafujwa kwa mitindo ya mavazi isiyo ya lazima na starehe zinazoandamana na hamu ya kupotosha ya chakula, ambayo hupunguza nguvu na kuleta maumivu na

uchakavu/uozo. Haiwezekani kuitoa miili yetu kama dhabihu iliyo hai kwa Mungu wakati imejazwa na uharibifu na magonjwa vinavyotokana na tamaa yetu ya kuendekeza mazoea ya dhambi. {3T 164.2}

Ujuzi ni lazima upatikane kuhusiana na namna ya kula na kunywa na kuvaa ili kuhifadhi afya. Ugonjwa husababishwa na kukiuka sheria za afya; ni matokeo ya kukiuka sheria ya asili. Wajibu wetu wa kwanza, ambao tunadaiwa na Mungu, kwetu wenyewe, na kwa wenzetu, ni kutii sheria za Mungu, ambazo ni pamoja na sheria za afya. Tukiwa wagonjwa tunawalemea rafiki zetu, na kujiweka kwenye mazingira ya kutofaa kutimiza majukumu yetu kwa familia na majirani zetu. Na wakati kifo cha mapema kinapotokea kama matokeo ya uvunjifu wa sheria za asili, tunawapelekea wengine huzuni na mateso; na kuwanyima majirani zetu msaada ambao tunapaswa kuwapa katika kuishi; na tunaziibia/tunazinyima familia zetu faraja na msaada tunaoweza kuwapa, na tunamnyang'anya Mungu huduma anayotudai ili kuendeleza utukufu Wake. Je! kwa hali hiyo, sisi si wavunjaji wa sheria ya Mungu? {3T 164.3}

Lakini Mungu ni mwingi wa huruma, Mwenye neema, na mpole, na wakati nuru inapokuja ili kuonesha ni nani walioumiza afya zao kwa tamaa za dhambi, na wanaposadikishwa kuwa wenye dhambi, na kutubu na kutafuta msamaha, Yeye hupokea sadaka ya kinyonge aliyopewa, na kuwapokea. Ah, ni huruma nyororo kiasi gani kwamba hakatai mabaki ya maisha yaliyotumika vibaya ya mwenye kuteseka, na mwenye dhambi anayetubu! Katika huruma Zake zenye neema na ukarimu, huziokoa roho hizi kutoka motoni. Lakini ni dhabihu duni na ya kusikitisha kama nini, kumtolea Mungu aliye safi na mtakatifu! Viungo vya thamani, na bora vimepoozeshwa na tabia mbaya za anasa za dhambi. Matarajio yamepotoshwa, na roho na mwili vimechafuliwa. {3T
165.1}

SURA YA 15

TAASISI YA AFYA

Kazi kubwa ya matengenezo ni lazima iendelee mbele. Taasisi ya Afya imeanzishwa huko Battle Creek ili kupunguza wanaoteseka/waathirika, kusambaza nuru, kuamsha roho ya uchunguzi, na kuendeleza matengenezo. Taasisi hii inaendeshwa kwa kanuni ambazo ni tofauti na zile za taasisi nyingine yoyote ya usafi katika nchi. Pesa siyo lengo kuu pamoja na marafiki na waendeshaji wake. Wanaiendesha [taasisi] kutoka kwa dhamiri, ya mtazamo wa kidini, wakilenga kutekeleza kanuni za usafi wa Biblia. Taasisi nyingi za aina hiyo zimewekwa juu ya kanuni tofauti na ni za kihafidhina, wakilifanya lengo lao kuwa kufikia viwango vya daraja linalopendwa angalau kwa nusu na kutengeneza hatua zao ili kuwafanya kupokea ufadhili mkubwa na fedha nyingi. {3T 165.2}

Taasisi ya Afya huko Battle Creek imeanzishwa juu ya kanuni thabiti za kiroho/kidini. Waendeshaji wake wanamtambua Mungu kama mmiliki halisi. Waganga na wasaidizi wanamtafuta Yeye kwa mwongozo, na wanalenga kusonga mbele kwa uangalifu, katika hofu yake. Kwasababu hiyo inasimama kwa msingi wa uhakika. Wakati watu dhaifu, na vilema wanaoteseka wanapojifunza juu ya kanuni za wakurugenzi, wasimamizi, waganga, na wasaidizi katika Taasisi ili waone kama wana hofu ya Mungu mbele yao, watajisikia salama huko kuliko kwa zile taasisi maarufu. {3T 166.1}

Kama wale wanaofungamana na Taasisi ya Afya huko Battle Creek watashuka kutoka kwa kanuni safi, zilizoinuliwa za Ukweli wa Biblia na kuiga nadharia na mazoea ya wale walio wakuu wa taasisi zingine, ambako magonjwa ya watu wasiyojiweza hutibiwa, kwa pesa tu, wahudumu wakiwa hawafanyi kazi kwa mtazamo wa juu, wa kidini, baraka maalum ya Mungu haingekuwa juu ya Taasisi. Taasisi hii imeundwa na Mungu kuwa moja ya msaada mkubwa katika kuandaa watu kuwa wakamilifu mbele za Mungu. Ili kufikia ukamilifu huu, wanaume na wanawake lazima wawe na nguvu ya mwili na akili kuthamini Ukweli ulioinuliwa wa Neno la Mungu na kuletwa katika nafasi ambayo watatambua kutokamilika kwao katika tabia zao za maadili. Wanapaswa kuwa na bidii ya kufanya matengenezo, ili wawe na urafiki na Mungu. Dini ya Kristo haipaswi kuwekwa nyuma na kanuni zake takatifu ziliwekwa ili kukidhi tabaka lolote, hata kama ni maarufu. kama kiwango cha Ukweli na utakatifu kitashushwa, kusudi la Mungu halitatimizwa katika taasisi hii. {3T 166.2}

Lakini imani yetu ya kipekee haipaswi kujadiliwa na wagonjwa. Akili zao hazipaswi kusisimuliwa bila sababu juu ya masomo ambayo tunatofautiana, isipokuwa kama wao wenyewe watapenda; na kisha tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa kutosumbua akili kwa kuwahimiza kuipokea imani yetu ya kipekee. Taasisi ya Afya siyo mahali pa kukimbilia kuingia kwenye majadiliano juu ya maoni ya imani yetu ambayo tunatofautiana na ulimwengu wa kidini kwa ujumla. Mikutano ya maombi hufanyika katika Taasisi ambayo wote wanaweza kushiriki ikiwa wanachagua, lakini kuna mengi ya kuzungumzia kuhusiana na dini ya Biblia yasiyohitaji kugusa tofauti zenye kutatanisha. Ushawishi wa kimya utafanya makubwa zaidi ya mabishano ya wazi. {3T 166.3}

Katika kuhimiza kwenye mikutano ya maombi baadhi ya watunza Sabato wamehisi kuwa imewapasa kuingiza Ujumbe wa Sabato na wa malaika wa tatu vinginevyo wangekosa kuwa na uhuru. Hii ni tabia ya akili finyu. Wagonjwa ambao hawajui imani yetu hawajui nini maana ya ujumbe wa malaika wa tatu. Kuanzishwa kwa maneno haya bila ufafanuzi wazi juu yake kunajeruhi tu. Lazima tukutane na watu mahali walipo, na bado hatuhitaji kuitoa mhanga kanuni moja ya Ukweli. Mkutano wa maombi utathibitisha baraka kwa wagonjwa, wasaidizi, na matabibu. Vipindi vifupi na vya kupendeza vya sala na ibada ya kijamii itaongeza ujasiri wa wagonjwa kwa wadaktari na wasaidizi wao. Wasaidizi hawapaswi kunyimwa mikutano hii kwa sababu ya kazi zao isipokuwa pale ambapo ni lazima kabisa. Wanawahitaji na wanapaswa kufurahi pamoja nao. {3T 167.1}

Kwa kuanzisha mikutano ya kawaida, wagonjwa huiamini Taasisi na wanahisi wako nyumbani zaidi. Na hivyo njia huwa imeandaliwa kwa mbegu ya Ukweli kuota mizizi katika baadhi ya mioyo. Mikutano hii inavutia sana wale wanaodai kuwa Wakristo na hujenga hisia nzuri kwa wale ambao siyo Wakristo. Kuaminiana kunaongezeka kati yao, na chuki hupunguzwa na katika hali nyingi huondolewa kabisa. Halafu kunakuwepo wasiwasi au hofu ya kuhudhuria mkutano wa Sabato. Pale, katika nyumba ya Mungu, ni mahali pa kuongea maoni yetu ya kimadhehebu. Hapo mchungaji anaweza kuzungumzia kwa uwazi juu ya mambo muhimu ya Ukweli wa leo na kwa roho ya Kristo, na kwa upendo na upole, kusisitiza mioyoni juu ya hitaji la utii kwa mahitaji yote ya Mungu, na kuuacha Ukweli ushawishi mioyo. {3T 167.2}

Nilioneshwa kuwa kazi kubwa inaweza kukamilishwa ikiwa kuna madaktari waungwana wa viwango sahihi vya akili ambao walikuwa na utamaduni sahihi na uelewa kamili wa kila sehemu ya kazi inayompasa daktari. Waganga wanapaswa kuwa na sehemu kubwa ya uvumilivu, ustahimilifu, upole, sikitiko na huruma; kwani wanahitaji sifa hizi katika kushughulikia wagonjwa wenye maumivu, wennye magonjwa mwilini, na ambao wengi wao wanaugua vyote viwili mwili na akili. Siyo jambo rahisi kupata daraja sahihi la wanaume na wanawake, wale wanaofaa mahali husika na ambao watafanya kazi kwa mapatano, kwa bidii, na bila ubinafsi kwa faida ya mgonjwa anayeteseka. Wanaume wanatafutwa katika Taasisi ambao

watakuwa na hofu ya Mungu mbele yao na ambao wanaweza kuhudumia akili za wagonjwa na kudumisha matengenezo ya afya kwa mtazamo wa kidini. {3T 167.3}

Wale ambao hufanya kazi hii wanapaswa kuwekwa wakfu kwa Mungu na kamwe kusudi lao kuu lisiwe kushughulikia mwili ili tu kutibu magonjwa, kwa hivyo kufanya kazi sawa na mtazamo wa madaktari wale mashuhuri na wanaopendwa, lakini kuwa mababa wa kiroho, kuhudumia akili zilizougua, na kuielekeza roho inayougua dhambi kwa tiba/dawa isiyoshindwa, Mwokozi aliyekufa kwa ajili yao. Wale wanaosumbuliwa na magonjwa huteseka kwa maana zaidi ya moja. Wanaweza kustahimili maumivu ya mwili vizuri zaidi kuliko wanavyoweza kuvumilia mateso ya akili. Wengi hubeba dhamiri iliyovunjwa na inaweza kufikiwa tu na kanuni za dini ya Biblia. {3T 168.1}

Wakati maskini, mgonjwa aliyepooza alipoletwa kwa Mwokozi, dharura/uharaka wa kesi hiyo ulionekana kutoruhusu ucheleweshwaji wa wakati, kwani tayari umauti ulikuwa unafanya kazi yake juu ya mwili. Wakati wale waliomchukua kitandani kwake walipoona kuwa hawawezi kuja moja kwa moja mbele ya Kristo, mara moja, walifumua paa na kuteremsha kitanda alichokuwa amelala mgonjwa wa kupooza. Mwokozi wetu aliona na kuelewa hali yake kikamilifu. Alijua pia kwamba mtu huyu mnyonge alikuwa na ugonjwa wa roho uliokuwa unamsumbua zaidi kuliko mateso ya mwili. Alijua kuwa mzigo mkubwa aliokuwa amebeba kwa miezi ulikuwa umetokana na dhambi. Umati wa watu ulingoja kwa kimya kisichoruhusu kupumua ili kuona jinsi Kristo atakavyoshughulikia kesi hii, inayoonekana kuwa haina matumaini, na walishangaa kusikia Maneno ambayo yalidondoka kutoka midomoni Mwake: "Mwanangu, jipe moyo; umesamehewa dhambi zako." {3T 168.2}

Haya yalikuwa Maneno ya maana sana ambayo yangeweza kusikika kwa sikio la mgonjwa yule aliyekuwa anateseka, kwani mzigo wa dhambi ulikuwa umemlemea sana kiasi kwamba hakuweza kupata afueni hata kidogo. Kristo anauinua mzigo uliomkandamiza sana: “Jipe moyo;” Mimi, Mwokozi Wako, nilikuja kusamehe dhambi. Uso wa mgonjwa anayeteseka ulibadilika kwa haraka kiasi gani! Matumaini yalichukua mahali pa giza la kukata tamaa, na amani na furaha ikichukua mahali pa mashaka yanayosumbua na kiza kilichojaa. Akili ikirejeshwa kwenye amani na furaha, mwili unaoteseka sasa uliweza kufikiwa. Kisha Maneno haya yakaja kutoka kwenye midomo ya Masihi: “Umesamehewa dhambi zako;” “Inuka, na utembee.” Katika juhudi za kutii nia, mikono hiyo isiyo na uhai, na isiyo na damu inahuishwa; mkondo wenye afya wa damu unatiririka kupitia mishipa; rangi ya risasi yaani kijivu ya mwili wake inapotea, na mwanga mwekundu wa afya unachukua nafasi yake. Viungo ambavyo kwa miaka mingi vimekataa kutii nia sasa vimehuishwa, na yule aliyepooza aliyeponywa anabeba kitanda chake na anatembea katikati ya umati kwenda nyumbani kwake, akimtukuza Mungu. {3T 168.3}

Jambo hili lipo kwa ajili ya kutufundisha. Waganga watakaofanikiwa katika matibabu ya magonjwa wanapaswa kujua jinsi ya kuhudumia akili iliyo na ugonjwa. Wanaweza kuwa na ushawishi mzuri kwa mema ikiwa watamfanya Mungu kuwa tumaini lao. Wagonjwa wengine na walemavu wanahitaji kuondolewa maumivu yao kabla akili haijafikiwa. Baada ya msaada kuingia mwilini, daktari anaweza mara kwa mara na kwa mafanikio makubwa zaidi kushughulikia dhamiri, na ndipo moyo huwa na mwelekeo wa kuvutwa na ushawishi wa Ukweli. Kuna hatari ya wale wanaofungamana na Taasisi ya Afya kupoteza mtazamo juu ya kusudi la taasisi kama hiyo kuanzishwa na Waadventista wa Sabato, na kuanza kufanya kazi kwa mtazamo wa walimwengu, wakizifuata taasisi zingine. {3T 169.1}

Taasisi ya Afya haikuanzishwa kati yetu kwa kusudi la kupata pesa, ingawa pesa ni muhimu sana kuendesha taasisi hiyo kwa mafanikio. Uangalifu katika matumizi ya pesa unapaswa kutekelezwa na wote katika kutumia mali, ili kwamba pesa zisitumike pasipo lazima. Lakini panapaswa kuwepo mali za kutosha kuwekeza katika yote yanayopunguza usumbufu wowote ambao utafanya kazi ya wasaidizi au kuleta faraja [convinience], na haswa ya madaktari, kuwa rahisi iwezekanavyo. Na wakurugenzi wa Taasisi wanapaswa kujipatia kila kituo ambacho kitasaidia katika kutibu wagonjwa kwa mafanikio. {3T 169.2}

Wagonjwa wanapaswa kutibiwa kwa huruma, kujali, upendo na upole mkubwa zaidi. Na bado waganga wanapaswa kuwa na msimamo imara na wasiyoruhusu, katika matibabu yao ya wagonjwa, kutawaliwa na mgonjwa na kupewa maelekezo kutoka kwa wagonjwa. Msimamo imara kwa upande wa madaktari ni wa lazima kwa faida ya wagonjwa. Lakini msimamo unapaswa kuchanganywa na uungwana/staha na adabu na heshima. Hakuna daktari au msaidizi anayepaswa kushindana au kulumbana na mgonjwa, au kutumia maneno makali ya ujeuri au yenye kuudhi, yanayokasirisha, au hata maneno yasiyo ya fadhili/we,a, haijalishi mgonjwa awe na mchokozi/uchokozi wa kupita kiasi-wa kiasi gani. {3T 170.1}

Moja ya makusudi makuu ya Taasisi yetu ya Afya ni kuelekeza roho za wagonjwa kwa Mganga Mkuu, Chemchemi ya uponyaji ya Kweli, na kuwaelekeza kwenye umuhimu wa matengenezo kutoka kwa mtazamo wa kidini, kwamba hawavunji tena sheria ya Mungu kwa msamaha wa dhambi. Ikiwa hisia za maadili za watu wasiyo na uwezo zinaweza kuamshwa na wanaona kuwa wanamkosea Muumba wao kwa kujiletea magonjwa na kwa hamu ya kula na tamaa mbaya, watakapoondoka kwenye Taasisi ya Afya hawataacha kanuni zao nyuma, lakini watazichukua pamoja nao na zitakuwa watengenezaji/warekebishaji/waratibu wa Kweli wa afya nyumbani. Kama hisia za maadili zinaamshwa, wagonjwa wataazimia kutekeleza ushawishi wa dhamiri; na kama watauona Ukweli watautii. Watakuwa na uhuru wa Kweli, na mzuri utakaowasukuma kuuweka kwenye vitendo Ukweli ambao wanaukubali. Na ikiwa akili itakuwa na amani na Mungu, hali za mwili zitakuwa nzuri zaidi. {3T 170.2}

Jukumu kubwa kuliko yote lipo juu ya kanisa lililoko Battle Creek kuishi na kutembea katika nuru, na kuhifadhi unyenyekevu na kujitenga na ulimwengu, ili ushawishi wao uweze kutangaza kwa nguvu ya kishawishi kwa wageni kwa Ukweli wanaohudhuria mikutano yetu. Ikiwa kanisa huko Battle Creek ni mwili usiyo na uhai, uliojaa kiburi, uliojiinua juu ya unyenyekevu wa utauwa wa Kweli, na unaoegemea ulimwenguni, mvuto wake utakuwa wa kutawanya kutoka kwa Kristo na kufanya Ukweli nyeti na ulio wa lazima wa Biblia upoteze nguvu. Washiriki wa kanisa hili wana fursa za kufaidika na mihadhara kutoka kwa waganga wa Taasisi ya Afya. Wanaweza kupata habari juu ya mada kubwa ya matengenezo ya afya ikiwa watataka. Lakini kanisa huko Battle Creek, lenye kudai kuwa na Ukweli mkubwa, lipo nyuma sana ukilinganisha na makanisa mengine ambayo hayajabarikiwa na faida ambazo wanazo. Kupuuzia kwa kanisa kuishi kulingana na nuru waliyopewa juu ya matengenezo ya afya ni jambo la kuvunja moyo kwa waganga na marafiki wa Taasisi ya Afya. Kama kanisa lingeonesha kupendezwa zaidi na matengenezo ambayo Mungu mwenyewe amewaletea ili kuwaandaa kwa ujio Wake, ushawishi wao ungekuwa mara kumi kuliko ulivyo sasa. {3T 170.3}

Wengi wa wale wanaodai kuamini Shuhuda wanaishi kwa kupuuza nuru iliyotolewa. Matengenezo ya mavazi yanachukuliwa na wengine kwa upuuzaji mkubwa na wengine kwa dharau, kwa kuwa kuna msalaba unaoambatana nayo. Kwa msalaba huu, mimi namshukuru Mungu. Hicho ndicho tunachokihitaji kutofautisha na kutenganisha watu wa Mungu wanaoshika amri na wale wa ulimwengu. Matengenezo ya mavazi yanatoa jibu kama ilivyokuwa utepe wa samawati/bluu kwa Israeli ya kale. Watu wenye kiburi, na wale wasiyo na upendo kwa Ukweli mtakatifu, ambao utawatenganisha na ulimwengu, watauonesha kwa matendo yao. Mungu katika majaliwa Yake ametupa nuru juu ya matengenezo ya afya, ili tuielewe katika fani zake zote, tufuate nuru inayoletwa nayo, na kwa kujihusisha kikamilifu na maisha tuwe na afya ili tumtukuze Mungu na kuwa baraka kwa wengine. {3T 171.1}

Kanisa kwa ujumla huko Battle Creek halijaiendeleza au kuitegemeza Taasisi hiyo kwa mfano wanaoonesha. Hawajaheshimu nuru ya matengenezo ya afya kwa kuitekeleza katika familia zao. Magonjwa yaliyozitembelea familia nyingi huko Battle Creek hayakutakiwa kuwepo ikiwa kama wangefuata nuru ambayo Mungu amewapa. Kama Israeli ya kale hawakuzingatia/wamepuuza nuru na hawakuona umuhimu wowote wa kuzuia hamu yao ya chakula kuliko walivyofanya Israeli wa kale. Wana wa Israeli walikuwa na nyama na wakasema, kama wengi sasa wasemavyo: Tutakufa bila nyama. Mungu aliwapa Israeli iliyoasi nyama, lakini laana yake ilikuwa pamoja nayo. Maelfu yao walikufa wakati nyama waliyoitamani ilipokuwa kati ya meno yao. Tunao mfano wa Israeli ya zamani ambao ni onyo kwetu sisi kwamba tusifanye kama wao. Historia yao ya kutokuamini na uasi imeachwa kwenye kumbukumbu kama onyo maalum kwamba hatupaswi kufuata mfano wao wa kunung'unika kwa mahitaji ya Mungu. Twawezaje kupita bila kujali,

tukichagua mwenendo wetu wenyewe, tukifuata maono ya macho yetu wenyewe, na kwenda mbali zaidi na Mungu, kama Waebrania? Mungu hawezi kuwafanyia watu Wake mambo makubwa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao na kutokuamini kunakotokana na dhambi. {3T 171.2}

Mungu hana upendeleo; lakini katika kila kizazi wale wanaomcha Bwana na kutenda haki wanakubaliwa Naye; wakati wale wanaonung'unika, wasiyoamini, na waasi hawatapata kibali Chake wala baraka zilizoahidiwa kwa wale wanaopenda Ukweli na wanaotembea ndani yake. Wale ambao wana nuru na hawaifuati, lakini wanapuuza matakwa ya Mungu, watakuta kwamba baraka zao zitabadilishwa kuwa laana na rehema zao kuwa hukumu. Mungu angependa tujifunze unyenyekevu na utii tunaposoma historia ya Israeli ya kale, ambao walikuwa watu Wake waliochaguliwa na wa pekee, lakini ambao walijiletea uharibifu wao wenyewe kwa kufuata njia zao wenyewe. {3T 172.1}

Dini ya Biblia haileti hatari kwa afya ya mwili au ya akili. Ushawishi wa Roho wa Mungu ni dawa bora kabisa ambayo inaweza kupokelewa na mwanamume au mwanamke mgonjwa. Mbingu imejaa afya tupu peke yake, na kadiri mvuto wa mbinguni unavyotambuliwa kwa undani ndivyo hakika zaidi kutakuwa kupona kwa mgonjwa au mlemavu anayeamini. Katika taasisi zingine za afya wanahimiza maburudisho, michezo ya kucheza, na kucheza ili kupata msisimko, lakini wanaogopa kufanya hivyo kwa sababu za kidini. Nadharia ya Dk Jackson katika suala hili siyo tu ni yenye makosa lakini ni hatari. Hata hivyo amezungumza haya kwa njia ambayo, ikiwa maagizo yake yangezingatiwa, wagonjwa wangeongozwa kufikiria kwamba kupona kwao kunategemea kuwa na mawazo machache juu ya Mungu na mbingu kwa kadri iwezekanavyo. Ni kweli kwamba kuna watu wenye akili zisizo na utimamu/uwiano wanaojiona kuwa waumini sana na ambao huweka kipaumbele kufunga na kuomba huku wakiumiza afya zao. Nafsi hizi zinajiletea maumivu na kukubali kudanganywa. Mungu hajahitaji jambo kama hili kutoka kwao. Wana haki ya kifarisayo, ambayo haitokani na Kristo, bali hutoka kwao. Wanaamini kuwa kazi zao nzuri zaweza kuwaletea wokovu na wanatafuta kununua mbingu kwa kazi zao nzuri badala ya kutegemea, kama ambavyo kila mwenye dhambi anapaswa, juu ya sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Kristo na utauwa wa Kweli, leo na hata milele, itakuwa afya kwa mwili na nguvu kwa roho. {3T 172.2}

Wingu ambalo limesimama juu ya Taasisi yetu ya Afya linainuka, na baraka ya Mungu imehudhuria juhudi zilizofanywa katika kuiweka kwenye misingi sahihi na kurekebisha makosa ya wale ambao kwa kukosa uaminifu walileta aibu kubwa juu yake na kuvunjika moyo kwa marafiki zake kila mahali. {3T 173.1}

Wale ambao wamepeana riba kwenye matumizi ya misaada ya Taasisi riba, au kwenye gawio, la hisa zao, wamefanya jambo zuri, ambalo litawaletea thawabu. Wale wote ambao hawajafanya hivyo, ambao wana uwezo wa kufanya hivyo,

wanapaswa, kwa nafasi yao ya kwanza, kugawa yote au sehemu, kama wengi wa wenye hisa walivyofanya. Na kama kuongezeka kwa faida/maslahi na kufaa kwa taasisi hii kunavyodai, wote, hasa kwa wale ambao hawajafanya hivyo, wanapaswa kuendelea kuchukua hisa ndani yake. {3T 173.2}

Niliona kwamba kulikuwa na idadi kubwa ya mali ya ziada kati ya watu wetu-ongezeko, sehemu ambayo inapaswa kuwekwa katika Taasisi ya Afya. Niliona pia kuwa kuna maskini wengi wanaostahiki kati ya watu wetu ambao ni wagonjwa na wanaoteseka, na ambao wamekuwa wakitafuta Taasisi kupata msaada, lakini ambao hawawezi kulipa bei za kawaida za bodi/bweni na chakula, matibabu, n.k Taasisi imejitahidi kupambana kwa taabu na madeni miaka mitatu iliyopita na haikuweza kutibu wagonjwa kwa kiwango chochote bila malipo kamili. Ingempendeza Mungu kwa watu wetu wote wanaoweza kufanya hivyo kuchukua hisa kwa wingi katika Taasisi ili kuiweka katika hali ambayo inaweza kusaidia maskini wanyenyekevu na wanaostahili wa Mungu. Kuhusiana na hili niliona kwamba Kristo anajitambulisha upande mmoja na ubinadamu unaoteseka, na kwamba tuliyoyafanya kwa hata watoto Wake wadogo, ambao Yeye anawaita ndugu Zake, tulikuwa tunamfanyia Mwana wa Mungu. {3T 173.3}

“Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono Wake wa kuume, Njoni ninyi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininywesha; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona Wewe una njaa, au una kiu, au U mgeni, au U uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Ndipo Bwana atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kwa vile hamkumhudumia mmojawapo wa hawa walio wadogo, hamkumtendea Mimi. Na hao wataenda katika adhabu ya milele; bali wenye haki watapata uzima wa milele." {3T 174.1}

Kuinua Taasisi ya Afya kutoka hali yake ya chini katika msimu wa kupukutisha majani wa 1869 hadi hali yake ya sasa ya kufanikiwa, hali ya matumaini ilihitaji dhabihu na juhudi ambayo marafiki zake wa nje ya nchi walijua kiasi kidogo. Halafu ilikuwa na deni ya dola elfu kumi na tatu na kulikuwa na wagonjwa wanane

tu waliokuwa wanalipia. Na kilichokuwa kibaya zaidi, ni kuwa hatua ya mameneja wa zamani ilikuwa kama ya kuwakatisha tamaa marafiki wa Taasiisi kwamba hawakuwa na moyo wa kuingiza mali za kuondoa deni au hata kuwahimiza wagonjwa kuilinda Taasisi hiyo. Ilikuwa ni katika wakati huu wa kukatisha tamaa ambapo mume wangu aliamua akilini mwake kwamba mali ya Taasisi lazima iuzwe ili kulipa deni, na salio, baada ya malipo ya deni, kurudishiwa kwa wenye hisa kulingana na kiwango cha hisa ambazo kila mmoja alikuwa nazo. Lakini asubuhi moja, wakati akiomba kwenye madhabahu ya familia, Roho wa Mungu alimshukia alipokuwa akiomba mwongozo wa Mungu katika maswala yanayohusu Taasisi, naye akasema, huku akiinama kwa magoti: “Bwana atathibitisha kila neno alilolisema kupitia maono kuhusiana na Taasisi ya Afya, na itainuliwa kutoka kwa hali yake ya chini na kufanikiwa kwa utukufu.” {3T 174.2}

Kuanzia wakati huo tuliichukua kazi hiyo kwa bidii na tumefanya kazi bega kwa bega na Taasisi hiyo kukabiliana na ushawishi wa watu wenye ubinafsi ambao walileta aibu juu yake. Tumetoa mali zetu, na hivyo kuweka mfano kwa wengine. Tumehimiza matumizi mazuri na utedaji kazi kwa upande wa wote waliounganishwa na Taasisi na tumewasihi kwamba waganga na wasaidizi wafanye kazi kwa bidii kwa malipo kidogo mpaka taasisi itakapokuwa imejiimarisha tena kwa kiwango kitakachorejesha imani/matumaini kwa watu wetu. Tumetoa ushuhuda wazi dhidi ya udhihirisho wa ubinafsi kwa mtu yeyote aliye na uhusiano na Taasisi na tumeshauri na kukemea makosa. Tulijua kwamba Taasisi ya Afya haingefaulu mpaka pale baraka ya Bwana itakapokuwa juu yake. Kama baraka Yake ingeandamana nayo, marafiki wa kazi hiyo wangekuwa na ujasiri/uhakika kuwa ilikuwa kazi ya Mungu na wangejisikia salama kutoa mali ya kuifufua biashara, ili iweze kufanikisha kusudi la Mungu. {3T 175.1}

Waganga na wasaidizi wengine walienda kufanya kazi kwa bidii. Walifanya kazi kwa bidii katika mazingira ya kukatishwa tamaa sana. Dk. Ginley, Chamberlain, na Lamson walifanya kazi kwa nguvu na bidii, kwa malipo kidogo, ili kujenga taasisi hii inayozama. Na, asante Mungu, deni la awali limeondolewa, na nyongeza kubwa za makazi ya wagonjwa imefanyika na kulipwa. Mzunguko wa jarida la *Health Reform*- Matengenezo ya Afya, ambao uko katika msingi wa mafanikio ya Taasisi, umeongezeka mara mbili, na limekuwa ni jarida lililo hai. Kujiamini katika Taasisi kumerejeshwa kikamilifu katika akili za watu wetu wengi, na kumekuwa na wagonjwa wengi katika Taasisi hiyo, karibu mwaka mzima, kwa kuwa waliweza kupatiwa malazi na kutibiwa vizuri na waganga wetu. {3T 175.2}

Ni jambo la kusikitisha sana kwamba mameneja wa kwanza wa Taasisi hiyo wanapaswa kuchukua hatua ya kuizamisha taasisi hii, kwa deni na kukata tamaa. Lakini upotevu wa kifedha ambao wamiliki wa hisa wamehisi na kujuta umekuwa mdogo kulinganisha na kazi, shida, masumbufu, na utunzaji ambao mimi na mume wangu tumebeba bila malipo, na ambayo waganga na wasaidizi wamebeba kwa ujira mdogo. Tumeingiza hisa katika Taasisi kiasi cha dola elfu kumi na tano,

ambazo “zimetengwa,” lakini ambayo ni ndogo ikilinganishwa na uchakavu ambao tumeupitia kama matokeo ya mameneja wa zamani wazembe na wasiotulia. Lakini kama Taasisi sasa inasimama juu ya sifa na uangalizi kuliko hapo awali, na kama mali ni ya thamani zaidi kuliko pesa zote ambazo zimewekeza, na kama makosa ya zamani yamerekebishwa, wale ambao wamepoteza imani yao hawana udhuru wa kuendeleza hisia za ubaguzi. Na ikiwa bado wanaonesha ukosefu wa ari, itakuwa kwa sababu wanachagua kuthamini ubaguzi badala ya kuongozwa na busara. {3T 176.1}

Katika majaliwa na uongozi wa Mungu, Ndugu A ameonesha kuvutiwa kwake na kuelekeza nguvu zake kwa Taasisi ya Afya. Amekuwa na maslahi/shauku isiyo na ubinafsi kuendeleza masilahi ya Taasisi na hajajizuia au kujipendelea. Ikiwa anamtegemea Mungu na kumfanya kuwa nguvu na mshauri wake anaweza kuwa baraka kwa waganga, wasaidizi, na wagonjwa. Ameunganisha masilahi yake kwa kila kitu kilichounganishwa na Taasisi na amekuwa baraka kwa wengine kwa kubeba mizigo kwa uchangamfu ambayo haikuwa michache wala myepesi. Amewabariki wengine, na baraka hizi zitaonekana tena juu yake. {3T 176.2}

Lakini Ndugu A yuko katika hatari ya kuchukua mizigo ambayo wengine wanaweza na wanapaswa kuibeba. Hapaswi kujichosha kwa kufanya mambo ambayo wengine, ambao muda wao hauna thamani kubwa, na wangeweza kufanya. Anapaswa kutenda kama mkurugenzi na msimamizi. Anapaswa kuhifadhi nguvu zake, ili kwa uamuzi wake wa uzoefu aweze kuelekeza wengine nini cha kufanya. Jambo hili ni muhimu ili aweze kudumisha nafasi ya ushawishi katika Taasisi. Uzoefu wake katika kutawala hekima na uchumi ni muhimu. Lakini yuko katika hatari ya kutenganisha masilahi yake sana kutoka kwa familia yake, na kuzama sana katika Taasisi, na kuchukua mizigo mingi juu yake, kama mume wangu alivyofanya. Masilahi ya mume wangu kwa Taasisi ya Afya, Chama cha Uchapishaji, na kazi kwa ujumla ilikuwa kubwa sana kiasi kwamba alielemewa/alitindikiwa na kazi na amelazimika kustaafu kazi kwa muda, na laiti kama angefanya machache zaidi kwa taasisi hizi na kugawa upendo wake kwa familia yake, asingekuwa na msongo wa kudumu kuelekea upande mmoja, na angeweza kuhifadhi nguvu zake na kuendelea na kazi zake za mikono bila kukatizwa [amevunjika]. Ndugu A ndiye mtu sahihi kwa mahali hapo. Lakini hapaswi kufanya kama mume wangu alivyofanya, hata ikiwa mambo hayako katika hali nzuri kama vile alivyotumia nguvu zake zote kwao. Mungu hajahitaji ama mume wangu ama Ndugu A wajinyime raha ya familia, waachane na nyumba na familia, kwa ajili ya masilahi ya taasisi hizi muhimu.
{3T 176.3}

Katika kipindi cha miaka mitatu au minne iliyopita watu kadhaa wamevutiwa na Taasisi ya Afya na wamefanya juhudi kuiweka katika hali nzuri. Lakini wengine wamekosa utambuzi na uzoefu. Maadamu Ndugu A anafanya sehemu isiyo ya

ubinafsi na kushikamana na Mungu, Yeye atakuwa msaidizi Wake na mshauri Wake. {3T 177.1}

Madaktari wa Taasisi ya Afya hawapaswi kuhisi kuwa wanalazimika kufanya kazi ambayo wasaidizi wao wanaweza kuifanya. Hawapaswi kutumika bafuni au kwenye chumba chenye mizunguko mingi, wakitumia nguvu zao kwa kufanya kile ambacho wengine wangeweza kukifanya. Hapapaswi kuwa na ukosefu wa wasaidizi wa kuuguza wagonjwa na kuangalia walio dhaifu wanaohitaji waangalizi. Matabibu wanapaswa kuhifadhi nguvu zao kwa ufanisi wa kufanikisha majukumu yao ya kitaalam. Wanapaswa kuwaambia wengine nini cha kufanya. Ikiwa kuna uhaba wa wale ambao wanaweza kuwasaidia kufanya mambo haya, watu wanaofaa wanapaswa kuajiriwa na kuelekezwa vizuri, na kulipwa vizuri kwa huduma zao. {3T 177.2}

Watu wasiajiriwe kama vibarua isipokuwa wale ambao watafanya kazi bila ubinafsi kwa masilahi ya Taasisi, na watu kama hao wanapaswa kulipwa vizuri kwa huduma zao. Lazima kuwe na timu [ya watumishi] ya kutosha, hasa msimu wa magonjwa mengi wa majira ya joto, ili asiwepo atakayeelemewa kwa kufanya kazi kupindukia. Taasisi ya Afya imeshinda aibu zake; na waganga na wasaidizi hawapaswi kulazimishwa kufanya kazi ngumu, na kupata shida kama hiyo ya ufukara, kama wakati ilipoaibika sana kama matokeo ya watu wasio waaminifu, waliokaribia kuidondosha chini. {3T 178.1}

Nilioneshwa kuwa matabibu katika Taasisi yetu wanapaswa kuwa wanaume na wanawake wenye imani na wa kiroho. Wanapaswa kumfanya Mungu kuwa tumaini na tegemeo lao. Kuna wengi wanaokuja kwenye Taasisi ambao, kwa utoshelevu wao wenyewe wa dhambi, wamejiletea magonjwa ya karibu kila aina. Watu wa daraja hili hawastahili huruma ambayo wamekuwa wakiihitaji mara kwa mara. Na ni jambo lenye maumivu kwa waganga kutumia wakati na nguvu kwa ajili ya watu wa daraja hili, waliojiharibu kimwili, kiakili, na kimaadili. Lakini kuna daraja ambalo, kwa njia za ujinga, liliishi kwa kukiuka sheria za maumbile. Wamefanya kazi bila kiasi na wamekula bila kiasi, kwa sababu ilikuwa ni kawaida kufanya hivyo. Wengine wamepata mateso mengi kutoka kwa waganga wengi, lakini hawajapata nafuu yoyote, isipokuwa hali imeendelea kuwa mbaya zaidi. Mwishowe wametengwa kutoka kazini, kutoka kwenye jamii, na kutoka kwa familia zao; na kama suluhisho lao la mwisho wanakuja katika Taasisi ya Afya na matumaini dhaifu kwamba wanaweza kupata afueni. Daraja hili linahitaji huruma. Wanapaswa kutibiwa kwa upole zaidi, na uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa ili kuweka wazi kwenye uelewa wao kuhusu sheria ya kuwepo kwao, ili waweze, baada ya kuacha kuzivunja, na kwa kujitawala wao wenyewe, kuepuka maumivu na magonjwa, ambavyo ni adhabu ya kuvunja sheria za asili. {3T 178.2}

Dk B siyo mtu bora zaidi anayefaa kubadilishwa ili kujaza nafasi kama daktari katika Taasisi. Anawaona wanaume na wanawake walioharibiwa viungo, walio

dhaifu katika nguvu ya kiakili na kimaadili, na anafikiria ni kupoteza wakati kushughulikia kutibu kesi kama hizo. Ndiyo inaweza kuwa hivyo katika kesi nyingi. Lakini hapaswi kuvunjika moyo na kuchukizwa na wagonjwa na wenye shida. Hapaswi kupoteza huruma yake, na subira yake, na kuhisi kuwa maisha yake hayatumiki vizuri anapowafanyia wale ambao hawawezi kamwe kutambua huduma wanayopokea, na ambao hawatatumia nguvu zao, ikiwa watapona, kubariki jamii, lakini watafuata njia ile ile ya kujiridhisha nafsi waliyopitia walipopoteza afya. Dk. B haipaswi kuchoka au kukata tamaa. Anapaswa kumkumbuka Kristo, ambaye alikuja moja kwa moja (ana kwa ana) na kuungana na wanadamu wanaoteseka. Ingawa, mara nyingi, waliougua walikuwa wamejiletea magonjwa kwa njia yao ya dhambi kwa kukiuka sheria ya asili, Yesu aliwasikitikia udhaifu wao, na walipokuja Kwake na magonjwa yenye kuchukiza zaidi, Yeye hakujitenga mbali kwa roho ya ubaridi kwa kuogopa kuambukizwa; Aliwagusa na kuamuru ugonjwa uwatoke. {3T 178.3}

“Na alipoingia katika kijiji kimoja, alikutana na watu kumi wenye ukoma; wakasimama mbali, wakapaza sauti wakisema, Ee Yesu, Bwana mkubwa, uturehemu! Alipowaona aliwaambia, Enendeni, mkajioneshe kwa makuhani. Ikawa walipokuwa wakienda walitakasika. Na mmoja wao alipoona kwamba amepona, alirudi, huku akimtukuza Mungu kwa sauti kuu; akaanguka kifudifudi miguuni Pake, akamshukuru; naye alikuwa Msamaria. Yesu akajibu, akanena, Je, Hawakutakaswa wote kumi? Je, wale kenda wa wapi? Je! Hawakuonekana waliorudi kumpa Mungu utukufu ila mgeni huyu? Akamwambia, Inuka, enenda zako, imani yako imekuokoa.” {3T 179.1}

Hapa pana somo kwa ajili yetu sote. Wakoma hawa walikuwa wameharibiwa sana na ugonjwa kiasi kwamba walikuwa wametengwa na jamii wasije wakawaambukiza wengine. Mipaka yao ya kutembea ilikuwa imeamriwa na mamlaka. Yesu anakuja mbele ya macho yao, na katika mateso yao makubwa wanamlilia Yeye ambaye Ndiye pekee aliye na uwezo wa kuwasaidia. Yesu anawaamuru wakajioneshe kwa makuhani. Wana imani ya kuanza safari yao, wakiamini nguvu ya Kristo imewaponya. Wanapoendelea na njia yao wanagundua kuwa ugonjwa wa kutisha umewatoka. Lakini ni mmoja tu aliye na hisia za moyo wa shukrani, ni mmoja tu anayehisi deni lake la kina kwa Kristo kwa kazi hii kubwa aliyomfanyia. Huyu mtu mmoja, anarudi akimsifu Mungu, na kwa fedheha kubwa huanguka miguuni pa Kristo, akikiri kwa shukrani kazi aliyofanyiwa. Na mtu huyu alikuwa mgeni; wengine tisa walikuwa Wayahudi. {3T 179.2}

Kwa ajili ya mtu huyu mmoja, anayetumia vizuri baraka ya afya, Yesu aliwaponya wale wote kumi. Wale tisa walipita bila kuthamini kazi iliyofanyika, na hawakutoa shukrani yoyote kwa Yesu kwa kufanya kazi hiyo. {3T 180.1}

Hivi ndivyo juhudi za waganga wa Taasisi ya Afya zitakavyolipwa. Lakini ikiwa, katika kazi yao ya kusaidia wanadamu wanaoteseka, mmoja kati ya ishirini 1/20,

atatumia vizuri faida zilizopokelewa na kutambua juhudi zao kwa niaba yake, madaktari wanapaswa kuhisi moyo wa shukrani na walioridhika. Ikiwa mtu mmoja kati ya kumi ameokolewa, na roho moja kati ya mia moja imeokolewa katika ufalme wa Mungu, wote walio na uhusiano na Taasisi watalipwa kwa juhudi zao zote. Mashaka yao yote na masumbufu havitapotea kabisa. Ikiwa Mfalme wa utukufu, Mwenye enzi wa mbinguni, alifanya kazi kwa wanadamu wanaoteseka, na ni wachache waliothamini msaada Wake wa kimbingu, waganga na wasaidizi katika Taasisi hiyo wanapaswa kuona haya kulalamika ikiwa juhudi zao dhaifu hazitathaminiwa na wote na zinaonekana kutupiliwa mbali na baadhi yao. {3T 180.2}

Nilioneshwa kuwa wale tisa ambao hawakurudi kumpa Mungu utukufu, wanawawakilisha kwa usahihi Watunza Sabato wanaokuja kwenye Taasisi ya Afya kama wagonjwa. Wanapewa ukaribisho wa kipekee na wanapaswa kutambua mashaka na kukata tamaa wanakokuwa nako waganga, na wangepaswa kuwa wa mwisho wa kuwasababishia masumbufu yasio wa lazima na mzigo. Hata hivyo najuta kusema kwamba mara nyingi wagonjwa ambao ni wagumu sana kuwasimamia katika Taasisi ya Afya ni wale wa imani yetu. Wanajisikia kuwa huru kutoa malalamiko kuliko kundi jingine lolote. Watu wa mataifa, na wanaodai kuwa Wakristo wa madhehebu mengine, wanathamini juhudi zilizofanywa kwa ajili ya kupona kwao zaidi ya watunza Sabato wengi. Na warudipo majumbani kwao hupeleka mvuto wenye nguvu unaoisema vizuri Taasisi ya Afya kuliko wanavyofanya Watunza Sabato. Na wengine walio huru sana kuhoji, na kulalamika juu ya usimamizi katika Taasisi, ni wale ambao wametibiwa kwa kupunguziwa bei. {3T 180.3}

Jambo hili limekuwa likiwavunja moyo waganga na wasaidizi; lakini wanapaswa kukumbuka kuwa Kristo, Ndiye Mfano wao mkuu, na wasichoke katika kufanya vizuri. Ikiwa mmoja kati ya idadi kubwa anashukuru na anatoa ushawishi mzuri, wanapaswa kumshukuru Mungu na kupata ujasiri. Mtu huyo anaweza kuwa mgeni au mtu baki kabisa, na swali linaweza kutolewa: Wako wapi wale tisa? Kwa nini watunza Sabato wote wasivutiwe na hii maslahi na kuiunga mkono, huku wakiisema vizuri Taasisi ya Afya? Baadhi ya Watunza Sabato wanavutiwa kidogo sana [na Taasisi ya Afya] kiasi kwamba, wakati wakihudumiwa katika Taasisi hiyo bila malipo, huzungumza kwa dharau kwa wagonjwa juu ya mali zilizotumika kuwawezesha wagonjwa kupona. Natamani watu kama hawa kutafakari njia zao. Bwana anawaona kama alivyowaona wale wenye ukoma tisa ambao hawakurudi kumpa utukufu. Wageni hufanya wajibu wao na wanafurahia na kuthamini juhudi zilizofanywa ili kupona, wakati hawa wengine huleta ushawishi dhidi ya wale ambao wamejaribu kuwafanyia mema. {3T 181.1}

Dk. B anahitaji kukuza uungwana, staha, adabu na wema asije akaumiza hisia za wagonjwa. Yeye ni mkweli na mwenye moyo ulio wazi, mwangalifu, mwenye

dhamiri iliyo kali, mkweli, na mchangamfu. Ana uelewa mzuri wa magonjwa, lakini anapaswa kuwa na maarifa kamili jinsi ya kutibu wagonjwa. Kwa ujuzi huu anahitaji utamaduni wa kibinafsi, uboreshaji wa tabia, na kuchagua zaidi maneno na vielelezo katika mazungumzo yake ya chumba cha kuhudumia wagonjwa. {3T 181.2}

Dr B ni mwepesi sana wa kukwazika na ana asili ya hasira ya haraka, ya mlipuko. Yeye huenda sana juu kwenye mambo yanayotugawa kwa wakati huu. Amefanya juhudi za kurekebisha roho yake ya haraka na kushinda mapungufu yake, lakini bado ana kazi kubwa anayotakiwa kufanya zaidi. Kama ataona mambo yakimuendea mrama hukurupuka haraka sana kuwaambia wale waliokosea anachofikiria, na yeye hatumii maneno yanayofaa zaidi kwa hadhira hiyo. Wakati mwingine huwakwaza na kuwachukiza wagonjwa kiasi kwamba wanamchukia na [matokeo yake] huisusa Taasisi hiyo huku wakiwa na hisia ngumu, kwa hasara ya wote; wao wenyewe na Taasisi. Jambo la kuzungumza kwa kuwakosoa wagonjwa wanaoumwa mwili na akili, huleta matokeo mazuri mara chache sana. Lakini ni wachache waliohamia jumuiya za kiulimwengu, na wanaoyaangalia mambo kutoka kwenye mtazamo wa kilimwengu, walio tayari kupokea taarifa ya Ukweli inayowahusu wao wenyewe pale inapowasilishwa mbele yao. Ukweli siyo wa kuzungumzwa wakati wote. Kuna wakati, fursa na nafasi inayofaa kuzungumza ambapo maneno hayo hayawezi kukwaza. Waganga hawapaswi kufanya kazi kupita kiasi hadi mifumo yao ya neva ishindwe, kwani hali hii ya mwili haitakuwa nzuri kwa akili tulivu, mishipa thabiti, na roho iliyochangamka, na yenye furaha. Dk B amebanwa sana na Taasisi. Alipaswa kuwa na mabadiliko. Anapaswa kutoka Battle Creek mara kwa mara na kupumzika na kuvinjari, siyo kila mara kufanya ziara za kitaaluma, lakini kutembelea mahali ambapo anaweza kuwa huru na ambapo akili yake haitakuwa na wasiwasi juu ya wagonjwa. {3T 181.3}

Faida ya kutoka kwenye Taasisi ya Afya wakati mwingine inapaswa kutolewa kwa madaktari wote, haswa kwa wale wanaobeba mizigo na majukumu. Ikiwa kuna uhaba wa msaada ambao unazuia jambo hili kufanywa, msaada zaidi unapaswa kupatikana. Kuwa na madaktari wanaofanya kazi kupita kiasi, na hivyo kutostahiki kutekeleza majukumu ya taaluma yao, ni jambo la kuogopwa na ni kengele ya tahadhari. Linapaswa kuzuiwa pale inapowezekana, kwani linaleta mvuto mbaya dhidi ya masilahi ya Taasisi. Waganga wanapaswa kuendelea vizuri. Hawapaswi kuugua kunakotokana na kufanya kazi kupita kiasi au kwa ujinga wowote ulio upande wao. {3T 182.1}

Nilioneshwa kuwa Dk. B huvunjika moyo kwa urahisi sana. Kutakuwepo siku zote mambo yanayosababisha mtu kukasirika, kuchanganyikiwa, na kuupima utahimilivu wa waganga na wasaidizi. Lazima wawe tayari kwa hili na wasiwe na msisimko au kuyumbishwa na kukosa msawaziko/utimamu. Lazima wawe watulivu na wenye upendo kwa chochote kinachoweza kutokea. Wanafanya ushawishi

utakaoakisiwa na wagonjwa katika majimbo mengine na utakaoitangaza Taasisi ya Afya kwa mema au kwa ubaya. Wanapaswa kuzingatia kila wakati kuwa wanashughulika na wanaume na wanawake wenye akili zilizo na ugonjwa, ambao mara nyingi huona vitu kwa njia potovu na huku wakijiamini kuwa wanaelewa mambo kikamilifu. Waganga wanapaswa kuelewa kuwa jibu laini hubadilisha ghadhabu. Sera lazima itumike katika taasisi ambayo wagonjwa wanatibiwa, ili kufanikiwa kudhibiti akili za wagonjwa na kuwanufaisha wagonjwa. Ikiwa waganga wanaweza kubaki watulivu katikati ya dhoruba ya maneno yasiyowafikiria wengine, yenye jazba, ikiwa wanaweza kutawala roho zao wenyewe wanapokasirishwa na kudhalilishwa, hapo watakuwa washindi kweli kweli. “Na mtu aitawalaye roho yake ni bora kuliko mtu atekaye mji.” Kuitiisha nafsi, na kushusha tamaa chini ya udhibiti wa nia, ndio ushindi mkubwa zaidi ambao wanaume na wanawake wanaweza kupata. {3T 182.2}

Dk B siyo kipofu kwa tabia yake ya kipekee. Anaona mapungufu yake, na wakati anahisi shinikizo juu yak,e huwa anarudi nyuma na kuugeuzia mgongo uwanja wa mapigano. Lakini hatapata chochote kwa kufuata hatua hii. Yeye yuko mahali ambapo mazingira yake na shinikizo la hali vinakuza nguvu katika tabia yake, sehemu ambazo ukali wa tabia unahitaji kuondolewa, ili aweze kutakaswa na kuinuliwa. Kitendo cha yeye kukimbia mapambano hakutaondoa kasoro. Hata angekimbia kutoka kwenye Taasisi hiyo, hangeondoa au kushinda kasoro za tabia yake. Ana kazi mbele yake, kushinda kasoro hizi ikiwa anataka kuwa miongoni mwa watu ambao watasimama bila kosa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, akiwa ametoka kwenye dhiki kuu, na akiwa ameosha mavazi yake ya tabia na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Nafasi imewekwa kwa ajili yetu ili tuoshwe. Chemchemi imeandaliwa kwa gharama isiyo na kipimo, na mzigo wa kuosha uko juu yetu, sisi ambao si wakamilifu mbele za Mungu. Bwana hapendekezi kuondoa madoa haya ya unajisi bila sisi kufanya chochote kwa upande wetu. Lazima tuoshe nguo zetu katika damu ya Mwana-Kondoo. Tunaweza kushikilia sifa za damu ya Kristo kwa imani, na kupitia neema na nguvu Zake, tunaweza kuwa na nguvu ya kushinda makosa yetu, dhambi zetu, kutokamilika kwetu kwa tabia, na tukawa washindi, baada ya kuosha mavazi yetu katika damu ya Mwanakondoo. {3T 183.1}

Dk. B anapaswa kutafuta kuongeza kila siku kwenye maarifa yake na kukuza adabu, uungwana, staha na uboreshaji wa tabia. Katika mazungumzo yake ya chumba cha wagonjwa ajizoeze kushuka kwa kiwango cha chini; [wagonjwa] hawana ushawishi wa kuwainua. Anapaswa kuzingatia kwamba yeye anashughulikia tabaka zote za akili na kwamba mvuto anaoutoa utaenda hadi kwenye majimbo mengine na utaakisi hali ya Taasisi hiyo. Kushughulika na wanaume na wanawake ambao akili zao pamoja na miil ina ugonjwa ni kazi nzuri. Hekima kubwa inahitajika na waganga katika Taasisi ili kuponya mwili kupitia akili. Lakini ni wachache wanaotambua nguvu ambayo akili inayo juu ya mwili. Magonjwa mengi

yanayosumbua wanadamu yana asili yake katika akili na yanaweza kuponywa tu kwa kuirudisha akili kwenye afya. Kuna wengi sana kuliko tunavyofikiria ambao ni wagonjwa kiakili. Ugonjwa wa moyo husababisha mara nyingi hali ya kutomeng'enywa chakula tumboni na kuvimbiwa [dyspectic], kwani shida ya akili ina ushawishi wa kupooza kwa viungo vya mmeng'enyo. {3T 183.2}

Ili kufikia daraja hili la wagonjwa, daktari lazima awe na utambuzi, uvumilivu, wema fadhili, na upendo. Moyo mgumu, na mgonjwa, na akili iliyokata tamaa, vinahitaji matibabu mepesi, na ni kupitia huruma nyororo, kujali, na upendo kwamba daraja hili la akili vinaweza kuponywa. Waganga wanapaswa kupata hali ya kuaminiwa nna wagonjwa, na kisha wawaelekeze kwa Daktari anayeponya kikamilifu. Ikiwa akili zao zinaweza kuelekezwa kwa Mbebaji wa Mzigo, na wanaweza kuwa na imani kwamba atapendezwa nao, tiba ya miili na akili zao zilizo na ugonjwa zitakuwa na hakika. {3T 184.1}

Taasisi zingine za afya zinaangalia kwa jicho la wivu Taasisi ya Afya huko Battle Creek. Wanafanya kazi kwa mtazamo wa ulimwengu, wakati mameneja wa Taasisi ya Afya wanafanya kazi kwa mtazamo wa kiroho/kidini, wakimkubali Mungu kama mmiliki wao. Hawafanyi kazi kwa ubinafsi kwa ajili ya kujipatia mali peke yake, bali kwa ajili ya Kristo na ubinadamu. Wanatafuta kuwanufaisha wanadamu wanaoteseka, kuponya akili inayougua pamoja na mwili unaoteseka, kwa kuwaelekeza wagonjwa kwa Kristo, Rafiki wa wenye dhambi. Hawaweki dini kando katika shughuli zao, lakini humfanya Mungu kuwa tumaini na tegemeo lao. Wagonjwa wanaelekezwa kwa Yesu. Baada ya waganga kufanya kile wanachoweza kwa niaba ya wagonjwa, wanamwomba Mungu afanye kazi na juhudi zao na kuwarejesha wagonjwa watesekao kwenye afya. Jambo hili [Mungu] amelifanya katika baadhi ya matukio, kwa kujibu maombi ya imani. Na hili ataendelea kulifanya kama watakuwa waaminifu na kuweka tumaini lao Kwake. Taasisi ya Afya itafanikiwa, kwani Mungu anaitegemeza. Na kama baraka Zake zitaandamana na Taasisi, itafanikiwa na itakuwa njia ya kufanya mema tele/mengi. Taasisi zingine zinajua kuwa kiwango cha juu cha maadili na ushawishi wa kidini vilivyopo katika Taasisi yetu. Wanatambua kwamba wahudumu wake hawajasukumwa na kanuni za ubinafsi, za ulimwengu, na wanaionea wivu kutokana na mvuto wake katika kusimamia na kuongoza. {3T 184.2}

SURA YA 16

HATARI YA KUSIFIA, KUMPIGIA MTU MAKOFI, AU KUMSHANGILIA

Nimeoneshwa tahadhari kubwa itumike, hata pale inapobidi kuondoa mzigo wa dhuluma kutoka kwa wanaume na wanawake, wasije wakaegemea hekima zao na kushindwa kumfanya Mungu kuwa tegemeo lao la pekee. Si salama kuwasifia watu au kuinua uwezo wa mchungaji wa Kristo. Katika siku ya Mungu [ya hukumu], wengi sana watapimwa katika mizani na kukutwa wamepungua kwa sababu ya kuinuliwa. Ningewaonya kaka na dada zangu kamwe msiwasifie wanadamu kwa kupitiliza au udanganyifu (au kutia chumvi kuhusu uwezo wao), au kuwapigia makofi kwa sababu ya uwezo wao, kwani hawawezi kustahimili hilo. Ubinafsi huinuliwa na matoleo yake, watu hupoteza uwezo wa kusimama. Ninasema tena kwa kaka na dada zangu: Ikiwa mnependa roho zenu ziwe safi kutokana na damu ya watu wote, kamwe msimpambe mtu au kujikomba au kujipendekeza kwake, kamwe msisifu juhudi za wanadamu wafao; maana hiyo yaweza kuthibitisha uharibifu wao. Si salama, kwa maneno na kwa matendo yetu, kumwinua kaka au dada, hata kama tabia yake itaonekana ni ya kinyenyekevu kiasi gani. Ikiwa kweli wana roho ya upole na ya unyenyekevu ambayo Mungu anaithamini sana, wasaidie kuihifadhi. Hili halitafanywa kwa kuwakemea wala kwa kupuuza kuwapa thamani yao halisi inayowastahili. Lakini ni wachache ambao wanaweza kubeba sifa bila kujeruhiwa/kuumizwa. {3T 185.1}

Baadhi ya wachungaji wenye uwezo ambao sasa wanahubiri Ukweli wa leo, wanapenda kutambuliwa. Makofi huwasisimua na kuwachochea, kama vile glasi ya divai inavyofanya kwa mnywaji. Waweke wachungaji hawa mahali ambapo wana

kusanyiko dogo lisiloahidi msisimko wa pekee na ambalo halisababishi upinzani wowote, na watapoteza shauku/tamaa yao na bidii yao, na wataonekana kuwa wanyonge katika kazi kama vile mtu asiye na akili timamu anaponyimwa kiasi kidogo cha pombe yake. Watu hawa watashindwa kufanya kazi ya Kweli, na halisi mpaka pale watakapojifunza kufanya kazi bila msisimko wa makofi. {3T 185.2}

SURA YA 17

KAZI KWA WAKOSAJI

Ndugu C na D walishindwa katika mambo fulani katika usimamizi wao wa mambo ya kanisa pale Battle Creek. Walifanya mambo kwa haraka kupita kiasi katika kutumia roho zao na hawakumfanya Mungu kuwa tegemeo lao lote. Walishindwa kutimiza wajibu wao kwa kutoliongoza kanisa kwa Mungu, Chemchemi ya maji ya uzima, ambapo wangeweza kutimizia mahitaji yao na kutosheleza njaa ya nafsi zao. Ushawishi wa kufanywa upya, wa kutakasa wa Roho Mtakatifu, ambao ungetoa amani na tumaini kwa dhamiri iliyosumbuka, na kurejesha afya na furaha kwa nafsi, haukufanywa kuwa wa kipaumbele cha yote. Kitu kizuri walichokuwa nacho hakikufikiwa. Ndugu hawa walikuwa na roho ya ukosoaji usio baridi na huruma kwa wingi katika kuwachunguza watu ambao walijitolea kuwa washiriki wa kanisa. Roho ya kulia pamoja na wale waliao na kufurahi pamoja na wale wafurahio haikuwa ndani ya mioyo ya ndugu hawa wahudumu jinsi inavyopaswa kuwa. {3T 186.1}

Kristo alijitambulisha na mahitaji ya watu Wake. Mahitaji yao na mateso yao yalikuwa Yake. Anasema: Nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; Nalikuwa kifungoni, nanyi mkanijia. Wachungaji wa Mungu wanapaswa kuwa na mioyo ya upendo mwororo, kujali na upendo wa Kweli kwa wafuasi wa Kristo. Wanapaswa kudhihirisha upendo huo wenye kina ambao Kristo anauonesha katika utunzaji wa mchungaji kwa kondoo waliopotea; wanapaswa kufuata kielelezo

kilichotolewa na Kristo na kudhihirisha huruma na upole uleule, na upendo ule ule wenye huruma nyororo na kujali, upole, rehema/huruma ambayo Yeye ametuonesha. {3T 186.2}

Nguvu kuu za maadili za roho ni imani, tumaini, na upendo. Ikiwa hizi hazifanyi kazi, mchungaji anaweza kuwa na bidii na aliyejitoa sana, lakini kazi yake haitakubaliwa na Mungu na haiwezi kuwa na matokeo mazuri kwa kanisa. Mchungaji wa Kristo anayebeba ujumbe mzito kutoka kwa Mungu kwenda kwa wanadamu, daima anapaswa kutenda haki, kupenda rehema, na kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Roho ya Kristo ndani ya moyo itaelekeza kila nguvu ya nafsi, kulisha na kulinda kondoo wa malisho Yake Bwana, kama mchungaji mwaminifu na wa Kweli. Upendo ni mnyororo wa dhahabu ambao hufunga mioyo ya waumini baina yao wenyewe kwa wenyewe katika vifungo vya hiari vya urafiki, huruma nyororo, kujali, upendo mwanana, na uthabiti wa uaminifu, na ambao hufunga roho kwa Mungu. Kuna ukosefu wa makusudi wa upendo, huruma nyororo, sikitiko, na kujali miongoni mwa ndugu. Wachungaji wa Kristo ni baridi sana na hawana mioyo yenye huruma. Mioyo yao yote haiwaki kwa huruma nyororo na upendo wa dhati. Ibada iliyo safi na iliyoinuka zaidi kwa Mungu ni ile inayodhihirika katika tamaa na juhudi za dhati kabisa za kuleta roho kwa Kristo. Sababu inayofanya wahudumu wanaohubiri Ukweli wa leo wasifanikiwe zaidi ni kwamba wana upungufu, wamepungukiwa sana, katika imani, tumaini, na upendo. Kuna taabu na migogoro, kujinyima nafsi na majaribu ya siri ya moyo, ambayo sote tunapaswa kuyakabili na kuyabeba. Kutakuwa na huzuni na machozi kwa ajili ya dhambi zetu; kutakuwa na mapambano endelevu na kukesha mara kwa mara, yakichanganyika na majuto na aibu kwa sababu ya mapungufu yetu. {3T 187.1}

Hebu wahudumu wa msalaba wa Mwokozi wetu mpendwa wasisahau uzoefu wao katika mambo haya; lakini wakumbuke siku zote kwamba wao ni watu tu, wanaoweza kukosea, na wana mihemko/shauku/jazba/tamaa sawa na ndugu zao, na kwamba ikiwa watawasaidia ndugu zao lazima wawe wavumilivu katika juhudi zao za kuwatendea mema, mioyo yao ikiwa imejawa na huruma/sikitiko na upendo. Ni lazima waje kwenye mioyo ya ndugu zao na kuwasaidia pale walipo dhaifu na wanapohitaji msaada zaidi. Wale wafanyao kazi katika neno na mafundisho wanapaswa kuvunja mioyo yao migumu, yenye majivuno, na isiyoamini kama wangependa kuyashuhudia hayo kwa ndugu zao pia. Kristo amefanya yote kwa ajili yetu kwa sababu tulikuwa wanyonge; tulifungwa katika minyororo ya giza, dhambi, na kukata tamaa, na kwa hiyo hatukuweza kufanya lolote kwa ajili yetu wenyewe. Ni kwa kutumia imani, tumaini, na upendo ndipo tunapokaribia zaidi na zaidi kiwango cha utakatifu mkamilifu. Ndugu zetu wanahisi hitaji lile lile la huruma la usaidizi ambalo nasi tumelihisi. Hatupaswi kuwalemea kwa karipio lisilo la lazima, lakini tunapaswa kuliruhusu pendo la Kristo litubidishe kuwa wenye

huruma na wapole sana, ili tuweze kulia kwaajili ya wakosaji na wale waliomwasi Mungu. Nafsi ina thamani
isiyo na kikomo. Thamani yake inaweza kukadiriwa tu kwa bei iliyolipwa ili kuikomboa. Kalvari! Kalvari! Kalvari! Itaeleza thamani halisi ya nafsi/roho/mwanadamu. {3T 187.2}

SURA YA 18

SHULE YA SABATO

Utauwa ulio muhimu kwa maisha ni kanuni inayopaswa kusitawishwa. Nguvu za Mungu zinaweza kututimizia yale ambayo mifumo yote ya ulimwengu haiwezi kufanya. Ukamilifu wa tabia ya Kikristo unategemea kabisa neema na nguvu zinazopatikana peke yake katika Mungu. Bila kuwepo kwa nguvu ya neema juu ya moyo, inayosaidia juhudi zetu na kutakasa kazi zetu, tutashindwa kuokoa roho zetu wenyewe na kuokoa roho za wengine. Mfumo na utaratibu ni muhimu sana, lakini hakuna anayepaswa kupokea hisia kwamba hizi zitafanya kazi bila neema na nguvu za Mungu zinazofanya kazi kwenye akili na moyo. Moyo na mwili vingeshindwa katika mzunguko wa kaida/sherehe, na katika utekelezaji wa mipango yetu, bila uwezo wa Mungu wa kuhamasisha na kutoa ujasiri wa kufanya. {3T 188.1}

Shule ya Sabato katika Battle Creek ilifanywa kuwa mada kuu ya kupendeza na Ndugu E. Ilivuta akili za vijana, huku majukumu mengine ya kidini yakipuuzwa. Mara kwa mara, baada ya shule ya Sabato kufungwa, msimamizi, na idadi fulani ya walimu, na idadi kubwa ya wasomi walikuwa wakirudi nyumbani kupumzika. Walihisi kwamba mzigo wao wa siku hiyo umeisha na kwamba hawakuwa na wajibu

zaidi. Kengele ilipolia saa ya Huduma kuu ikawa imewadia, na watu wakaacha nyumba zao na kwenda kwenye nyumba ya ibada, na huko wangekutana na sehemu kubwa ya [jumuia ya] shule wakielekea kwenye nyumba zao. Na hata kama mkutano ungekuwa wa muhimu kiasi gani, mvuto wa sehemu kubwa ya shule ya Sabato usingeweza kuamshwa ili kufurahia mafundisho yaliyotolewa na mchungaji kuhusu mambo muhimu ya Biblia. Ingawa watoto wengi hawakuhudhuria Huduma kuu, wengine waliobaki hawakufaidika na Neno lililonenwa; kwa maana waliona kuwa ni jambo linalochosha. {3T 188.2}

Ni lazima pawe na nidhamu na utaratibu katika shule zetu za Sabato. Watoto wanaohudhuria shule hizi wanapaswa kuthamini upendeleo wanaoufurahia na wanapaswa kutakiwa kuzingatia kanuni za shule. Na hata uangalifu mkubwa zaidi unapaswa kuchukuliwa na wazazi kuona kwamba watoto wao wana masomo yao ya Biblia kuliko juhudi inayochukuliwa katika kuhakikisha kwamba masomo yao ya shule ya kutwa yametayarishwa. Masomo yao ya Biblia yanapaswa kusomwa kikamilifu zaidi kuliko masomo yao katika shule za kawaida. Ikiwa wazazi na watoto hawaoni umuhimu wa masomo haya, basi ni bora watoto wabaki nyumbani; kwa maana shule ya Sabato itashindwa kutoa baraka kwao. Wazazi na watoto wanapaswa kufanya kazi kwa kupatana na msimamizi na walimu, na hivyo kutoa uthibitisho wa kwamba wanathamini kazi iliyofanywa kwa ajili yao. Wazazi wanapaswa kupendezwa na kuwa na shauku na elimu ya kidini ya watoto wao, ili wapate ujuzi kamili zaidi wa Maandiko. {3T 189.1}

Kuna watoto wengi ambao wanalalamika kuhusu ukosefu wa muda kama sababu kwa nini hawakujifunza masomo yao ya shule ya Sabato, lakini ni wachache ambao hawangeweza kupata muda wa kujifunza masomo yao kama wangekuwa wana matamanio nayo. Wengine hutumia wakati wa maburudisho na kuosha macho kwa kuona mambo au utalii [sighseeing]; wengine kwa [kutumia muda huo] kushona isivyo lazima mavazi yao kwa ajili ya maonesho, na hivyo kusitawisha kiburi na ubatili. Saa za thamani zinazotumiwa kwa hila ni wakati wa Mungu, ambao ni lazima watoe hesabu Kwake. Saa zinazotumiwa katika mapambo yasiyo na maana au katika burudani na mazungumzo ya bure, pamoja na kila kazi, zitaletwa hukumuni. {3T 189.2}

SURA YA 19

WATENDAKAZI OFISINI

Wale walio katika ofisi wanaodai kuamini Ukweli wanapaswa kuonesha nguvu ya Ukweli katika maisha yao na kuthibitisha kwamba wanafanya kazi kwa kwenda mbele na juu zaidi kutoka kwenye msingi wa kanuni. Wanapaswa kuwa wanatengeneza maisha na tabia zao kufuatisha Yeye aliye Kielelezo kamili. Kama wote wangeweza kutazama kwa jicho la utambuzi uhalisi wa ajabu wa umilele, ni utisho ulioje wa hukumu ungewapata baadhi ya wale walio ofisini ambao sasa hupita tu wakionekana kutojali, ingawa wametengwa na matukio ya milele kwa nafasi finyu sana. Maonyo mengi yametolewa, na kuufikia moyo kwa hisia kali na maombi ya dhati na bidii, ambayo kila moja limesajiliwa mbinguni kwa uaminifu, kusawazisha mahesabu ya kila mmoja katika siku ya upelelezi wa mwisho. Upendo usiochoka wa Kristo umefuata wale wanaojishughulisha na kazi Yake ofisini. Mungu amewafuata kwa baraka na maombezi/kusihi/mwito, lakini anachukia dhambi na ukosefu wa uaminifu unaoshikamana nao kama ukoma. Kweli za kina na za dhati ambazo wale walio katika ofisi wamepata fursa ya kuzisikiliza zinapaswa kushikilia

huruma zao na kuwaongoza katika kuthamini kwa kiwango cha juu nuru ambayo Mungu amewapatia. Ikiwa watatembea katika nuru, itarembesha na kuyatukuza maisha yao kwa pambo la mbinguni, usafi na wema wa Kweli. {3T 190.1}

Njia imefunguliwa mbele ya kila mtu katika ofisi kujihusisha kutoka moyoni moja kwa moja katika kazi ya Kristo na wokovu wa roho/wanadamu. Kristo aliiacha mbingu na kifua cha Baba Yake ili kuja kwenye ulimwengu usio na urafiki, uliopotea ili kuokoa wale ambao wangeokolewa. Yeye Alijihamisha Mwenyewe kutoka kwa Baba Yake na kubadilisha ushirika safi wa malaika kwa ule wa wanadamu walioanguka, wote waliochafuliwa na dhambi. Kwa huzuni, maombolezo na mshangao, Kristo anashuhudia ubaridi, kutojali na kupuuzwa, ambako wale wanaojiita wafuasi Wake katika ofisi wanashughulikia nuru na jumbe za maonyo na upendo alizowapa. Kristo ametoa mkate na maji ya uzima kwa wote wenye njaa na kiu. {3T 190.2}

Bwana anawataka wote walio katika ofisi kufanya kazi kwa nia ya juu. Katika maisha Yake Mwenyewe, Kristo amewapa kielelezo. Wote wanapaswa kufanya kazi kwa matamanio/mapenzi, kwa kujitolea, na kwa imani kwa ajili ya wokovu wa roho. Ikiwa wote katika ofisi watafanya kazi kwa makusudi yasiyo na ubinafsi, wakitambua utakatifu wa kazi hiyo, baraka za Mungu zitakuwa juu yao. Ikiwa wote wangechukua mizigo yao kadhaa kwa furaha na bashasha, uchakavu na fadhaa haingekuja kwa uzito sana juu ya mume wangu. {3T 190.3}

Ni sala chache jinsi gani za dhati na bidii zimetumwa kwa Mungu kwa imani kwa ajili ya wale waliofanya kazi katika ofisi ambao hawakuwa katika Kweli kikamilifu! Ni nani ambaye amehisi thamani ya nafsi ambayo Kristo aliifia? Ni nani wamekuwa wafanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana? Niliona kwamba malaika walihuzunishwa na mambo madogo-madogo na michezo ya wale waliodai kuwa wafuasi wa Kristo waliokuwa wakishughulikia mambo matakatifu ofisini. Wengine hawana hisia zaidi ya utakatifu wa kazi na huifanya kama ambavyo wangeifanya kazi [nyingine] ya kawaida. Mungu sasa anawaita wale wanaoisumbua/wanaoichosha ardhi, wasiozaa matunda wajiweke wakfu Kwake na kukita/kuweka mapenzi na matumaini yao Kwake. {3T 191.1}

Bwana angetamani wote waliounganishwa na ofisi kuwa walezi na wabeba mizigo. Ikiwa ni wapenda raha, wasipojizoeza kujinyima, hawafai mahali pa ofisi. Wafanyakazi wa ofisi hiyo wanapaswa kuhisi kwamba wanapoingia humo kwamba ni mahali Patakatifu, mahali ambapo kazi ya Mungu inafanywa katika uchapishaji wa Ukweli ambao utaamua hatima ya roho/wanadamu. Hili halihisiwi au kutambulika kama inavyopaswa kuwa. Kuna mazungumzo katika idara ya uchapaji ambayo hugeuza akili kutoka kwa kazi. Ofisi si mahali pa kutembelea, au pa kupalilia/kuendekeza roho ya kutafuta wachumba/kutongozana, au mahali pa maburudisho au ubinafsi. Wote wanapaswa kuhisi kwamba wanafanya kazi kwa

ajili ya Mungu. Yeye anayepepeta nia zote na kusoma mioyo yote anathibitisha, na kujaribu, na kuwapepeta watu Wake, hasa wale walio na nuru na ujuzi, na ambao wanajishughulisha na kazi Yake takatifu. Mungu ni mchunguzi wa mioyo na mjaribu hatamu, na hatakubali chochote isipokuwa kujitoa kabisa kwa kazi na kujitoa Kwake Mwenyewe. Wote katika ofisi wanapaswa kufanya kazi zao za kila siku kana kwamba [wanafanya] mbele za Mungu. Hawapaswi kuridhika kwa kufanya kile wanachodhani kinatosha, na kupokea ujira wao; lakini wote wanapaswa kufanya kazi mahali popote ambapo wanaweza kusaidia zaidi. Kaka White anapokuwa hayupo, kunakuwepo baadhi ya watu walio waaminifu; kuna wengine ni wachungaji wa macho yaani hufanya kazi mtu akiwa anawatazama au watumishi wa mshahara. Ikiwa wote katika ofisi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangekuwa waaminifu katika utendaji wa kazi ofisini, kungekuwa na badiliko kubwa kuelekea ubora. Vijana wa kiume na wa kike wamezama sana katika jamii ya kila mmoja wao, wakizungumza, mizaha na kejeli, na malaika wa Mungu wamefukuzwa ofisini. {3T 191.2}

Marcus Lichtenstein alikuwa kijana aliyemcha Mungu; lakini aliona kanuni ndogo sana ya kidini ya Kweli kwa wale waliokuwa kanisani na wale wanaofanya kazi ofisini hivi kwamba alifadhaika, na kukatishwa tamaa, na kuchukizwa. Alijikwaa juu ya ukosefu wa uangalifu katika kushika Sabato uliodhihirishwa na baadhi ya watu ambao bado walidai kuwa washika amri. Marcus alikuwa na heshima kubwa kwa kazi katika ofisi; lakini ubatili, upuuziaji, michezo-michezo, na ukosefu wa kanuni vilimkwaza. Mungu alikuwa amemwinua na katika majaliwa yake alimuunganisha na kazi Yake katika ofisi. Lakini kuna mambo machache sana yanayojulikana kuhusu akili na mapenzi ya Mungu na baadhi ya wanaofanya kazi katika ofisi hivi kwamba waliitazama kazi hii kuu ya kuongoka kwa Marcus kutoka katika dini ya Kiyahudi kuwa haina umuhimu wowote. Uzito/Thamani yake haikuthaminiwa. Aliumizwa mara kwa mara na kufukuzwa kwa F na wengine ofisini; na alipojaribu kuwakemea, maneno yake yalipokelewa kwa dharau kwamba asijihatarishe kwa kuwaelekeza. Uongeaji wake uliokuwa na ulema ulikuwa tukio la mzaha na kufurahisha watu fulani. {3T 192.1}

Marcus alijawa na hisia za kina sana juu ya swala la F, lakini hakuona jinsi ambavyo angeweza kumsaidia. Marcus asingeweza kuondoka ofisini kama vijana hao wangekuwa waaminifu kwa taaluma yao. Iwapo ataiharibu imani yake, damu yake itaonekana kwenye ncha za nguo za vijana wanaomkiri Kristo, lakini ambao kwa matendo yao, maneno yao na mwenendo wao husema waziwazi kwamba wao si wa Kristo, bali wa ulimwengu. Hali hii ya upuuziaji unaopaswa kushutumiwa, hali ya kutojali na kutokuwa na uaminifu, lazima ikome; mabadiliko ya kina na ya kudumu lazima yafanyike katika ofisi, au wale ambao wamekuwa na nuru nyingi na mapendeleo makubwa wanapaswa kufutwa kazi na wengine kuchukua nafasi zao, hata kama ni makafiri. Ni jambo la kutisha kujidanganya. Malaika alisema, akiwaonesha wale walio katika ofisi: “Haki yenu isipozidi haki ya waandishi na

Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.” Taaluma haitoshi (Au kukiri kwa mdomo tu haitoshi). Lazima kuwe na kazi iliyoingizwa katika nafsi na kufanywa katika maisha. {3T 192.2}

Upendo wa Kristo unafika kwenye kina kirefu cha taabu na ole wa kidunia, la sivyo haungekutana na kesi ya mwenye dhambi mbaya zaidi. Pia unafikia kiti cha enzi cha Milele, vinginevyo mwanadamu asingeweza kuinuliwa kutoka katika hali yake duni, na mahitaji yetu yasingetimizwa, matamanio yetu yasingetoshelezwa. Kristo ameongoza njia kutoka duniani hadi mbinguni. Yeye Anaunda kiungo cha kuunganisha kati ya ulimwengo na mbingu-two worlds-mwalimwengu mawili. Analeta upendo na unyenyekevu wa Mungu (kwa kushuka chini na kuja kwetu) kwa mwanadamu, na humleta mwanadamu juu kupitia sifa zake ili kukutana na upatanisho wa Mungu. Kristo Ndiye njia, Kweli na uzima. Ni kazi ngumu kufuata, hatua kwa hatua, kwa uchungu na polepole, kuendelea na kwenda juu, katika njia ya usafi na utakatifu. Lakini Kristo amefanya maandalizi ya kutosha ili kutoa nguvu mpya na nguvu za mbingu/Mungu katika kila hatua ya mapema katika maisha ya mbingu. Huu ndio ujuzi na uzoefu ambao mikono katika ofisi yote inataka, na lazima iwe nayo, au kila siku wanaleta aibu juu ya kazi ya Kristo. {3T 193.1}

Kaka G anafanya makosa katika maisha yake. Anajiwekea makadirio ya juu sana. Hajaanza kujijenga kwa njia sahihi ili kufanikiwa maishani. Anajenga juu, lakini msingi haukuwekwa sawa. Msingi lazima uweke chini ya ardhi, na kisha jengo linaweza kwenda juu. Anahitaji nidhamu na uzoefu katika majukumu ya kila siku ya maisha ambayo sayansi haitatoa; elimu yake yote haitampa mazoezi ya mwili ili afundishwe na ugumu wa maisha. {3T 193.2}

Kutokana na kile ambacho Nimeoneshwa, lazima kuwe na uteuzi makini wa msaada katika ofisi. Vijana na wasiojaribiwa na wasiojiweka wakfu hawapaswi kuwekwa hapo, kwa kuwa wanakabiliwa na majaribu na hawana tabia maalum. Wale ambao wameunda tabia zao, ambao wana kanuni zisizobadilika, na ambao wana Ukweli wa Mungu moyoni hawatakuwa chanzo cha mara kwa mara cha matunzo/masumbufu na wasiwasi, bali msaada na baraka. Ofisi ya uchapishaji ina uwezo wa kutosha wa kufanya mipango ya kupata wasaidizi wazuri, wale ambao wana uwezo na kanuni. Na kanisa, kwa upande wake, lisitafute kujinufaisha senti moja kutoka kwa wale wanaokuja ofisini kufanya kazi na kujifunza kazi zao. Kuna nafasi [walizoshikilia] ambazo wengine wangeweza kupata mishahara mizuri kuliko [wanayoipata] ofisini, lakini hawawezi kamwe kupata nafasi muhimu zaidi, yenye heshima zaidi ua ya nyadhifa ya juu, au iliyotukuka zaidi kuliko kazi ya Mungu ya hapo ofisini. Wale wanaofanya kazi kwa uaminifu na bila ubinafsi watapewa thawabu. Kwao kuna taji ya utukufu iliyotayarishwa, ikilinganishwa nayo heshima zote za kidunia na anasa ni kama mavumbi madogo ya mizani. Hasa watabarikiwa wale ambao wamekuwa waaminifu kwa Mungu katika kuangalia ustawi wa kiroho wa wengine katika ofisi. Masilahi ya kifedha na ya muda, vinapolinganishwa na hii,

huzama chini na kuonekana kitu kidogo. Katika mizani moja kuna vumbi la dhahabu; na kwa mizani nyingine, ni nafsi ya mwanadamu yenye yenye hiyo thamani hiyo na heshima hiyo, utajiri, na utukufu vilivyotolewa na Mwana wa Mungu ili kuikomboa kutoka katika utumwa wa dhambi na kukata tamaa kusiko na tumaini. Nafsi ina thamani isiyo na kikomo na inadai umakini wa hali ya juu. Kila mtu anayemcha Mungu katika nafasi hiyo ya ofisi anapaswa kuacha mambo ya kitoto na ya ubatili, na, kwa ujasiri wa Kweli wa kimaadili, asimame wima katika hadhi ya utu wake, akiepuka mahusiano/mazoea ya chini [low familiarity], lakini akifunga moyo kwa moyo katika kifungo cha maslahi na upendo wa Kikristo. Mioyo inatamani huruma na upendo, na inaburudishwa, inafanya upya na kuimarishwa navyo kama vile maua yanavyopata mvua na mwanga wa jua. {3T 193.3}

Biblia inapaswa kusomwa kila siku. Maisha ya kidini, ya ujitoaji kwa Mungu, ndiyo ngao bora zaidi kwa vijana wanaokabili majaribu katika makundi yao huku wakipata elimu. Neno la Mungu litatoa kiwango sahihi cha mema na mabaya, na kanuni za maadili. Kanuni isiyobadilika ya Ukweli ndiyo ulinzi pekee kwa vijana. Madhumuni yenye nguvu na uthabiti yatafunga milango mingi iliyo wazi kwa majaribu na mivuto ambayo haifai kwa kudumisha tabia ya Kikristo. Roho dhaifu, isiyo na msimamo iliyojiingiza katika maisha ya wavulana na vijana itafanya maisha ya taabu na mapambano ya kudumu kwa kuwa uamuzi na kanuni thabiti havipo. Watu kama hao watakutana na vikwazo katika kufaulu maisha haya, na watakuwa katika hatari ya kupoteza maisha bora. Itakuwa salama kuwa mkweli kwa ajili ya haki. Jambo la kwanza la kuzingatia linapaswa kuwa kumheshimu Mungu, na la pili, kuwa mwaminifu kwa wanadamu, kutekeleza majukumu ambayo kila siku huyaleta, kukabiliana na majaribu yake na kubeba mizigo yake kwa uthabiti na moyo thabiti. Jitihada ya dhati na isiyochoka, iliyounganishwa na kusudi dhabiti na kumtumaini kwa ukamilifu Mungu, vitasaidia katika kila dharura, vitawastahilisha maisha yenye manufaa katika ulimwengu huu, na kuandaa mazingira ya kufaa kwa maisha yasiyo na kufa. {3T 194.1}

SURA YA 20

UPENDO NA WAJIBU

Upendo una dada pacha, ambaye ni wajibu/jukumu. Upendo na wajibu vinasimama bega kwa bega. Upendo unaotekelezwa huku wajibu ukipuuzwa utawafanya watoto kuwa wakaidi, wabinafsi, wapotoshaji, wabinafsi, na wasiotii. Ikiwa jukumu kali litaachwa kusimama peke yako bila upendo kulilainisha na kushinda, litakuwa na matokeo yale yale. Wajibu na upendo lazima vichanganywe ili watoto wapate nidhamu ifaayo. {3T 195.1}

Hapo zamani, makuhani walipewa maagizo: “Nao watawafundisha watu Wangu tofauti iliyopo kati ya vitu vitakatifu na vitu vya sikuzote, na kuwafundisha kupambanua kati ya yaliyo machafu na yaliyo safi. Na katika mashindano

watasimama ili kuamua; wataamua sawasawa na hukumu Zangu.” “Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi neno la kumwonya mtu huyo, aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe umejiokoa roho yako.”{3T 195.2}

Hapa wajibu wa wahudumu/wachungaji wa Mungu unawekwa wazi. Hawawezi kusamehewa kutoka katika utekelezaji wa uaminifu wa wajibu wao wa kukemea dhambi na makosa katika watu wa Mungu, ingawa inaweza kuwa kazi isiyopendeza/isiyokubalika na haiwezi kupokelewa na yule ambaye ana makosa. Lakini katika visa vingi yule aliyekaripiwa angekubali onyo hilo na kutii karipio laiti kama wengine wangesimama njiani. Wanakuja wakiwa wenye huruma na kumsikitikia yule anayekaripiwa na kuhisi kwamba ni lazima wamtetee. Hawaoni kwamba Bwana amechukizwa na mkosaji, kwa sababu njia ya Mungu imejeruhiwa na Jina Lake limetukanwa. Nafsi zimegeuzwa kando kutoka kwenye Ukweli na zimevunjikiwa imani kama tokeo la njia mbaya inayofuatwa na yule mwenye makosa; lakini mtumishi wa Mungu ambaye utambuzi wake umegubikwa na hukumu yake inasukumwa na mivuto mibaya angechukua msimamo/utambuzi wake wa upesi pamoja na mkosaji ambaye ushawishi wake umefanya madhara mengi, kama vile mkarimu wa uovu na dhambi, na kwa kufanya hivyo hakika anasema kwa mwenye dhambi: “Usifadhaike, usisononeke moyo na kujiangusha chini ; hata hivyo wewe bado upo sawa.” Hawa humwambia mwenye dhambi: Itakuwa heri kwako. {3T 196.1}

Mungu anawataka watendakazi/wachungaji Wake watembee katika nuru na kutofunika macho yao ili wasiweze kutambua utendaji kazi wa Shetani. Hebu wawe tayari kuwaonya na kuwakemea walio hatarini kwa hila zake. Shetani anafanya kazi kwa mkono wa kuume na wa kushoto ili kupata nafasi nzuri yenye kumpa faida. Yeye hapumziki. Anavumilia. Yeye yu macho na mjanja kutumia kila hali na kuigeuza kuwa upande wake katika vita vyake dhidi ya Kweli na masilahi ya ufalme wa Mungu. Ni jambo la kusikitisha kwamba wachungaji wa Mungu hawako macho kuona hila za Shetani kama inavyopaswa kuwa. Na badala ya kumpinga Shetani ili aweze kuwakimbia, wengi wanaelekea kufanya maridhiano na nguvu za giza. {3T 196.2}

SURA YA 21

KANISA LA BATTLE CREEK

Kuna pingamizi kubwa la kuwa na shule hiyo iliyoko Battle Creek. Kanisa ni kubwa, na kuna idadi kubwa ya vijana wanaohusishwa nalo. Ikiwa ushawishi ambao mshiriki mmoja anao juu ya mwingine katika kanisa kubwa sana ungekuwa wa

tabia ya kuinua, inayoongoza kwa usafi na wakfu kwa Mungu, basi vijana wanaokuja Battle Creek wangekuwa na faida kubwa zaidi kuliko kama shule ingekuwa mahali pengine. Lakini ikiwa ushawishi katika Battle Creek utakuwa katika siku zijazo jinsi ulivyokuwa kwa miaka kadhaa iliyopita, ningewaonya wazazi kuwaweka watoto wao mbali na Battle Creek. Ni wachache tu katika kanisa hilo kubwa ambao wana mvuto unaowavuta watu kila mara kwa Kristo; ilhali kuna wengi ambao, kwa mfano wao, watawaongoza vijana mbali na Mungu na kuupenda ulimwengu. {3T 197.1}

Pamoja na uwingi wa makanisa katika Battle Creek kuna ukosefu mkubwa wa kuhisi wajibu wao. Wale ambao wana dini ya vitendo watahifadhi utambulisho wao wa tabia chini ya hali yoyote. Hawatakuwa kama mwanzi unaotetemeka katika upepo. Wale walioko mbali wanahisi kwamba wangepewa upendeleo mkubwa sana, kama wangeweza kupata fursa ya kuishi Battle Creek, kati ya kanisa lenye nguvu, ambapo watoto wao wangeweza kufaidika na shule ya Sabato na mikutano. Baadhi ya ndugu na dada zetu katika nyakati zilizopita wamejikana nafsi ili watoto wao waishi huko. Lakini wamekatishwa tamaa katika karibu kila jambo. Kulikuwa na wachache tu katika kanisa wa kudhihirisha kupendezwa bila ubinafsi kwa vijana hawa. Kanisa kwa ujumla lilisimama kama wageni wa kifarisayo, wakiwa wamejitenga na wale waliohitaji msaada wao zaidi. Baadhi ya vijana waliounganishwa na kanisa, ambao walidai kuwa wanamtumikia Mungu, lakini wakipenda anasa na ulimwengu zaidi, walikuwa tayari kufahamiana na wageni wachanga waliokuja kati yao, na kuwa na ushawishi mkubwa juu yao ili kuwaongoza kwenye ulimwengu badala ya kuwa karibu na Mungu. Wakati wanafunzi hawa walipokuwa wanarudi nyumbani, [walijikuta] wako mbali zaidi na Ukweli kuliko wakati walipofika Battle Creek. {3T 197.2}

Wanaume na wanawake wanatakiwa katika moyo wa kazi ambao watakuwa baba na mama wauguzi, wakuzaji na walezi katika Israeli, watakaokuwa na mioyo inayoweza kubeba mengi kuliko ‘mimi’ na ‘yangu’ tu. Wanapaswa kuwa na mioyo ambayo itawaka upendo kwa vijana wapendwa, iwe ni washiriki wa familia zao au watoto wa jirani zao. Wao ni washiriki wa familia kuu ya Mungu, ambayo Kristo alikuwa na shauku kubwa sana kwao hivi kwamba alitoa kila dhabihu ambayo iliwezekana Kwake kufanya ili kuwaokoa. Kristo Aliacha utukufu Wake, ukuu Wake, kiti Chake cha enzi na mavazi ya kifalme, akawa maskini, ili kwa umaskini Wake watoto wa wanadamu wapate kuwa matajiri. Hatimaye aliimwaga nafsi yake hadi kifo, ili aweze kuokoa jamii ya wanadamu kutoka katika taabu isiyo na matumaini. Huu ni mfano wa ukarimu usio na ubinafsi, na usiojifikiria ambao Kristo ametupa sisi ili tuuige. {3T 198.1}

Katika majaliwa maalum ya Mungu vijana wengi na pia wale waliokomaa wametupwa katika mikono ya kanisa la Battle Creek kusudi wabariki na nuru kuu

ambayo Mungu amewapa, na kwamba, kupitia juhudi zao zisizo na ubinafsi, wapate pendeleo la thamani la kuwaleta kwa Kristo na kwa Kweli. Kristo anawatuma malaika Wake kuwahudumia wale wanaoletwa chini ya ushawishi wa ile Kweli, kulainisha mioyo yao na kuwafanya wawe rahisi kuathiriwa na mivuto ya Ukweli Wake. Wakati Mungu na malaika Wake wanafanya kazi yao, wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanaonekana kutojali. Hawafanyi kazi kwa umoja na Kristo na malaika watakatifu. Ingawa wanadai kuwa watumishi/wachungaji wa Mungu wanatumikia maslahi yao wenyewe na kupenda raha zao wenyewe, na roho zinaangamia karibu nao. Nafsi hizi zinaweza kusema kweli: “Hakuna mtu anayejali nafsi yangu.” Kanisa limepuuza kuboresha mapendeleo na baraka zilizo katika uwezo wao, na kwa kupuuza kwao wajibu, wamepoteza nafasi za thamani/dhahabu za kuleta roho kwa Kristo. {3T 198.2}

Wasioamini wameishi kati yao kwa muda wa miezi, na hawajafanya juhudi maalum ili kuwaokoa. Je, Bwana mkubwa atawachukuliaje wachungaji kama hao? Wanadamu wasioamini wangekuwa wameitikia kwa juhudi zilizofanywa kwa niaba yao kama ndugu na dada wangekuwa wameishi kulingana na taaluma zao zilizotukuzwa. Kama wangekuwa wanatafuta nafasi ya kazi kwa faida ya Bwana wao, wangeweza kutafuta nafasi za kuwaombea,kutenda wema na kuomba nao, na wangeweza kujihisi kuwa na jukumu zito lililo juu yao [linalowataka] kuonesha imani yao kwa njia ya matendo, kwa mfano, na kwa kuwa kielelezo. Kupitia zana zao roho hizi zingeweza kuokolewa na kuwa kama nyota katika taji la furaha yao. Lakini, mara nyingi, nafasi dhahabu/adimu zimepita na kamwe hazitaweza kurudi. Roho zilizokuwa kwenye bonde la kukata maneno zimechukua nafasi zao kwenye katika jeshi la adui na kuwa maadui wa Mungu na Ukweli. Na kumbukumbu ya kukosa uaminifu ya wafuasi wa Yesu wasio waaminifu imepanda hadi mbinguni. {3T 198.3}

Nilioneshwa kwamba kama vijana wa Battle Creek wangekuwa waaminifu kwa taaluma yao, wangeweza kushinikiza ushawishi mkubwa wa wema kwa vijana wenzao. Lakini sehemu kubwa ya vijana katika Battle Creek wanahitaji uzoefu wa Kikristo. Hawamjui Mungu kwa ujuzi wa uzoefu na majaribio. Hawana uzoefu wa kibinafsi katika maisha ya Kikristo, na lazima waangamie pamoja na wasioamini isipokuwa kama watapata uzoefu huu. Vijana wa daraja hili hufuata mivuto na mwelekeo badala ya wajibu. Wengine hawatafuti kuongozwa na kanuni. Hawasumbuki kuingia kwenye mlango ulio mwembamba, wakitetemeka kwa hofu wasije wakashindwa. Ni watu wenye kujiamini, wenye majivuno, wenye kiburi, wasiotii, wasio na shukrani, na wasio watakatifu. Tabaka kama hili huongoza roho katika njia pana kwenye uharibifu. Ikiwa Kristo hayumo ndani yao, hawawezi kumwiga Yeye katika maisha na tabia zao. {3T 199.1}

Kanisa la Battle Creek limekuwa na nuru kuu. Kama watu wamependelewa kipekee na Mungu. Hawajaachwa katika ujinga kuhusiana na mapenzi ya Mungu kuhusu wao. Wangepaswa kuwa mbali kuliko pale walipo kwa sasa, kama imani yao inavyowadai, endapo wangetembea katika nuru. Hawatofautiani sana na dunia, hawana upekee maalumu, na utakatifu kama vile imani yao inavyowahitaji kuwa, na kama vile Mungu anavyo taka watoto wa nuru waenende. Wao si watiifu na wenye uchaji Mungu kama nafasi yao ilivyotukuka na wajibu wao mtakatifu wa kuwa watoto watembeao nuruni unavyowahitaji wawe. Ujumbe mzito zaidi wa rehema ambao umewahi kutolewa kwa ulimwengu umekabidhiwa kwao. Bwana amefanya kanisa hilo kuwa hifadhi ya amri Zake kwa namna ambayo hakuna kanisa lingine limewahi kufanyiwa. Mungu hakuwaonesha upendeleo Wake wa kipekee kwa kuwakabidhi Kweli Yake takatifu ili wao tu-peke yao, ndiyo wafaidike na nuru iliyotolewa, bali kwamba nuru iliyoangaziwa juu yao kutoka mbinguni iwaangazie wengine na kuangaziwa tena kwa Mungu na wale wanaopokea Ukweli unaomtukuza. Wengi katika Battle Creek watakuwa na hesabu ya kutisha ya kutoa katika siku ya Mungu kwa ajili ya kupuuza huku kwa wajibu kidhambi. {3T 199.2}

Wengi wa wale wanaodai kuamini Ukweli katika Battle Creek wanapinga imani yao kwa matendo yao. Wao ni kama wasioamini, na walio mbali na kutimiza matakwa ya Mungu na kutoka kwenye kukiri imani yao, kama lilivyokuwa kanisa la Kiyahudi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo. Kama Kristo angetokea katikati yao, akionya na kukemea ubinafsi, kiburi, na kupenda urafiki wa ulimwengu, kama alivyofanya wakati wa kuja Kwake kwa mara ya kwanza, ni wachache wangemtambua kama Bwana wa utukufu. Picha ya kupuuza kwao wajibu wao ambayo angeionesha mbele yao hawangeipokea, lakini wangemwambia usoni Mwake: “Wewe umekosea kabisa; sisi tunastahili kuinuliwa sana kwa ajili ya matendo yetu mema.” {3T 200.1}

Wayahudi hawakuingia gizani mara moja. Ilikuwa kazi ya taratibu, hadi waliposhindwa kutambua karama ya Mungu katika kumtuma Mwanawe. Kanisa la Battle Creek limekuwa na manufaa bora zaidi, nao watahukumiwa kwa nuru na mapendeleo waliyo nayo. Mapungufu yao, kutokuamini kwao, ugumu wa mioyo yao, na kupuuza kwao kuthamini na kuifuata nuru si mambo madogo ukilinganisha na yale Wayahudi waliyopendelewa, waliokataa baraka ambazo wangeweza kuzikubali, nao wakamsulubisha Mwana wa Mungu. Wayahudi sasa ni mshangao/mshtuko na lawama kwa ulimwengu. {3T 200.2}

Kanisa la Battle Creek ni kama Kapernaumu, ambayo Kristo anaiwakilisha kama iliyoinuliwa mbinguni kwa nuru na mapendeleo ambayo walikuwa wamepewa. Ikiwa nuru na mapendeleo ambayo walikuwa wamebarikiwa nayo yangetolewa kwa Sodoma na Gomora, wangeweza kusimama hadi leo. Ikiwa nuru na maarifa ambayo

kanisa katika Battle Creek yamepokea yangepewa mataifa walioketi gizani, wangeweza kuwa mbele sana ya kanisa hilo. {3T 200.3}

Kanisa la Laodikia liliamini Kweli, na kufurahia baraka za injili, na walidhani walikuwa matajiri katika upendeleo wa Mungu, wakati Shahidi wa Kweli aliwaita maskini, uchi, vipofu, na wenye huzuni. Hii ndiyo hali ya kanisa la Battle Creek na sehemu kubwa ya wale wanaodai kuwa watu wa Mungu kwa kuzishika amri. Bwana haangalii kama mwanadamu aonavyo. Mawazo Yake na njia Zake si kama njia zetu. {3T 201.1}

Maneno na sheria ya Mungu, iliyoandikwa katika nafsi, na kuoneshwa katika maisha yaliyowekwa wakfu, matakatifu, vina mvuto wenye nguvu wa kuhukumu ulimwengu. Tamaa, ambayo ni ibada ya sanamu, na husuda, na kupenda dunia, vitang'olewa kutoka katika mioyo ya wale wanaomtii Kristo, na itakuwa furaha yao kutenda haki, kupenda rehema, na kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu - Mika 6. Lo, ni kiasi gani mambo haya yanajumuishwa, kwa kutembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu! Sheria ya Mungu, ikiwa imeandikwa moyoni, itavuta akili na utashi chini ya utii wa Kristo. {3T 201.2}

Imani yetu ni ya kipekee. Wengi wanaodai kuwa wanaishi chini ya sauti ya ujumbe wa mwisho wa rehema hawajatenganishwa katika mapenzi yao na ulimwengu. Wanasujudu mbele ya urafiki wa ulimwengu na kuitoa mhanga nuru na kanuni ili kupata upendeleo wake. Mtume anafafanua watu waliopendelewa na Mungu kwa maneno haya: “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.” {3T 201.3}

SURA YA 22

KAZI YA UMISHONARI

Desemba 10, 1871, nilikuwa nimeoneshwa kuwa Mungu angetimiza kazi kubwa kupitia ile Kweli kama watu waliojitoa wakfu, na wenye kujikana nafsi wangejitoa wenyewe bila kinyongo kwa kazi ya kuziwasilisha kwa wale walio gizani. Wale ambao wana ujuzi wa ile Kweli ya thamani na ambao wamejiweka wakfu kwa Mungu ni lazima wajiweke wenyewe kwenye kila nafasi inayofunguka ili kupenyeza Ukweli. Malaika wa Mungu wanatembelea na kusogea katika mioyo na dhamiri za watu wa mataifa mengine, na roho zile aminifu waaminifu zinasukwasukwa zinaposhuhudia dalili za nyakati katika hali ya mataifa ambayo bado hawajatulia. Maswali yanaibuka mioyoni mwao: Nini itakuwa mwisho wa mambo haya yote? Wakati Mungu na Malaika wapo kazini kuishawishi mioyo, watumishi wa Kristo wanaonekana kuwa wamelala. Lakini wachache wapo kazini kwa kwenda sambamba na wajumbe wa mbinguni. Wanaume na wanawake wote walio Wakristo kwa kila Neno hilo linavyomaanisha, wanapaswa kuwa watendakazi shambani mwa Bwana. Wanapaswa kuwa macho sana, wakifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wa wenzao, na wanapaswa kuiga mfano ambao Mwokozi wa ulimwengu amewapa katika maisha Yake ya kujinyima, kujitoa kafara, uaminifu, na kufanya kazi kwa dhati na bidii. {3T 202.1}

Kumekuwa na roho kidogo tu ya umishonari kati ya Waadventista Washika Sabato. Kama wachungaji na watu wangeamshwa vya kutosha, hawangepumzika hivyo bila kujali wakati Mungu amewaheshimu kwa kuwafanya wahifadhi wa sheria yake kwa kuichapa katika akili zao na kuiandika mioyoni mwao. Kweli hizi zenye umuhimu mkubwa zitaipima na kuijaribu dunia; na bado katika nchi yetu wenyewe kuna miji, vijiji, na miji ambayo haijapata kusikia ujumbe wa onyo. Vijana wanaohisi kusumbuliwa na miito ambayo imefanywa kwa kuomba msaada katika kazi hii kuu ya kuendeleza kazi ya Mungu wamechukua hatua fulani za kusonga mbele, lakini hawajapokea mzigo wa kazi hiyo juu yao vya kutosha ili kutimiza kile ambacho wanaweza. Wapo tayari kufanya kazi ndogo ambayo haihitaji jitihada maalum. Kwa hiyo hawajifunzi kuweka tegemeo lao lote/kamili kwa Mungu na kwa imani iliyo hai kuchota kutoka kwenye Chemchemi kuu na Chanzo cha nuru na nguvu ili kwamba jitihada zao zipate kufanikiwa kabisa. {3T 202.2}

Wale wanaofikiri kwamba wana kazi ya kumfanyia Bwana, hawapaswi kuanza juhudi zao kati ya makanisa; wanapaswa kwenda nje katika nyanja mpya na kuthibitisha karama zao. Kwa njia hii wanaweza kujipima wenyewe na kutatua suala hilo kwa kujiridhisha wao wenyewe, ikiwa kweli Mungu amewachagua kwa kazi hii. Watahisi umuhimu wa kujifunza Neno la Mungu na kusali kwa bidii kwa ajili ya hekima ya mbinguni na msaada wa Mungu. Kwa kukutana na wapinzani wanaoleta pingamizi kwa mambo muhimu ya imani yetu, wataletwa pale ambapo

watapata uzoefu wenye thamani zaidi. Watahisi udhaifu wao na kuelekezwa kwenye Neno la Mungu kwa kasi na kwa maombi. Katika zoezi hili la karama zao watakuwa wakijifunza na kuziboresha, na kupata kujiamini, ujasiri, na imani, na hatimaye watakuwa na uzoefu wa thamani. {3T 203.1}

Wakina kaka H walianza moja kwa moja katika kazi hii. Katika utumishi wao hawakuenda kati ya makanisa, bali walikwenda katika maeneo mapya. Walianza kwa unyenyekevu. Walikuwa wadogo machoni pao wenyewe na waliona umuhimu wa utegemezi wao wote kwa Mungu. Ndugu hawa, hasa AH, sasa wako katika hatari kubwa ya kujitegemea/kujitosheleza wenyewe. Alipolumbana na wapinzani, ukweli ulipata ushindi, na akaanza kujisikia nguvu ndani yake. Mara tu anapokuwa juu ya kazi, kazi zake hazitainufaisha kazi ya thamani ya Mungu. Hapaswi kuhimiza kupenda mijadala, lakini anapaswa kuyaepuka haya wakati wowote anapoweza. Mashindano haya na nguvu za giza katika debate/mjadala mara chache huleta matokeo bora zaidi kwa maendeleo ya ukweli wa leo. {3T 203.2}

Kama vijana wanaoanza kufanya kazi katika kazi hii wangekuwa na roho ya umishenari, wangetoa uthibitisho kwamba kwa kweli Mungu amewaita kwenye kazi hiyo. Lakini wasipotoka kwenda mahali papya, bali kuridhika kwenda kutoka kanisa hadi kanisa, wanatoa uthibitisho kwamba mzigo wa kazi hauko juu yao. Mawazo ya wahubiri wetu vijana si mapana vya kutosha. Bidii yao ni dhaifu sana. Kama vijana wangekuwa macho na waliojitoa kwa Bwana, wangekuwa na bidii kila dakika ya wakati wao na wangetafuta sahiki/kufaa kuwa watenda kazi katika uwanja wa umishenari badala ya kuwa wapambanaji. {3T 203.3}

Vijana wanapaswa kujipatia sifa (kujistahilisha) wenyewe kwa kuzifahamu lugha nyingine, ili Mungu apate kuwatumia kama daraja la kuwasilisha Ukweli Wake unaookoa kwa wale wa mataifa mengine. Vijana hawa wanaweza kupata ujuzi wa lugha nyingine hata wakiwa wanafanya kazi kwa ajili ya wenye dhambi. Ikiwa watautumia vizuri muda wao wanaweza kuboresha akili zao na kujipatia sifa/stahiki kuwa wenye manufaa zaidi. Ikiwa wasichana ambao wamebeba jukumu kidogo wangejitoa wenyewe kwa Mungu, wangeweza kustahili kupata manufaa kwa kujifunza na kufahamu lugha nyinginezo. Wangeweza kujishughulisha na kazi ya kutafsiri. {3T 204.1}

Machapisho yetu yanapaswa kuchapishwa katika lugha nyinginezo, ili mataifa ya kigeni yaliyo mbali, yaweze kufikiwa. Mengi yanaweza kufanywa kupitia vyombo vya habari, lakini bado mengi zaidi yanaweza kutimizwa ikiwa mvuto wa kazi ya mhubiri aliye hai utaenda na machapisho yetu. Wamishenari wanahitajika ili kwenda katika mataifa mengine kuhubiri Kweli katika hali iliyolindwa na yenye uangalifu. Kazi ya Ukweli wa leo inaweza kupanuliwa sana kwa jitihada za kibinafsi. Mgusano wa akili ya mtu binafsi na akili nyingine ya mtu binafsi utafanya mengi zaidi kuondoa ubaguzi, ikiwa kazi ni ya busara, kuliko yale machapisho yetu pekee yawezavyo kufanya. Wale wanaojihusisha na kazi hii hawapaswi

kushauriana/kusikiliza uvivu, raha zao au mwelekeo wao; wala hawapaswi kupenda umaarufu au maonesho. {3T 204.2}

Wakati makanisa yanapoona vijana wakiwa na bidii ya kustahili kueneza kazi zao kwenye miji, vijiji, na miji ambayo haijawahi kuamshwa kwa ile Kweli, na wamishenari wakijitolea kwenda mataifa mengine ili kuwapelekea Ukweli, makanisa yatatiwa moyo na kutiwa nguvu zaidi kuliko kwa wao wenyewe kupokea utendaji wa vijana wasio na uzoefu. Wanapoona mioyo ya wahudumu wao yote inawaka kwa upendo na bidii kwa ajili ya ile Kweli, na kwa tamaa ya kuokoa roho, makanisa yataamka yenyewe. Hawa kwa ujumla wana karama na uwezo ndani yao wenyewe kuweza kujibariki na kujiimarisha wenyewe, na kukusanya kondoo na wana-kondoo zizini. Wanahitaji kutupwa juu ya rasilimali zao wenyewe, ili karama zote ambazo zimelala, ziweze kuitwa kutumika katika huduma hai. {3T 204.3}

Makanisa yanapoanzishwa, inapaswa kuwekwa mbele yao kwamba hata kutoka miongoni mwao ni lazima watu wachukuliwe ili kupeleka Ukweli kwa wengine na kuinua makanisa mapya; kwa hiyo ni lazima wote wafanye kazi, na kusitawisha kwa ukamilifu talanta ambazo Mungu amewapa, na kuwazoeza akili zao kushiriki katika utumishi wa Bwana wao. Ikiwa wajumbe hawa ni wasafi wa moyo na mtindo wa maisha, ikiwa mfano wao ndio ule upaswao kuwa, kazi zao zitakuwa na mafanikio makubwa; kwa kuwa wana Ukweli wenye nguvu zaidi, ulio wazi na unaoshikamana/uliofungamanishwa, na ambao una hoja zenye kusadikisha katika kuupendelea. Wana Mungu upande wao na malaika wa Mungu hufanya kazi kwa juhudi zao. {3T 205.1}

Sababu inayofanya kuwe na utimilifu mdogo sana na wale wanaohubiri Kweli siyo kuwa Ukweli wanaobeba haupendwi, lakini kwa sababu watu wanaobeba ujumbe hawajatakaswa na zile Kweli wanazohubiri. Mwokozi anaondoa tabasamu Lake, na uvuvio wa Roho Wake hauko juu yao. Uwepo na uwezo wa Mungu wa kumhukumu mwenye dhambi na kumsafisha na udhalimu wote hauonekani. Maangamizi/Uharibifu wa ghafula umewajia watu, na bado hawatishiki kwa woga au tahadhari. Wahudumu wasiojitoa wakfu hufanya kazi kuwa ngumu sana kwa wale wanaokuja nyuma yao na ambao wana mzigo na roho ya kazi juu yao. {3T 205.2}

Bwana amewagusa watu wa lugha nyingine na kuwaleta chini ya ushawishi wa Ukweli, ili waweze kufuzu kufanya kazi katika kazini mwake. Yeye Amewaleta hadi kwenye ofisi ya uchapishaji, ili wasimamizi Wake waweze kujinufaisha na huduma zao kama wangekuwa macho na matakwa ya kazi hiyo. Machapisho yanahitajika katika lugha zingine ili kuongeza shauku na ari ya uchunguzi kati ya mataifa mengine. {3T 205.3}

Kwa namna ya ajabu sana Bwana alitenda juu ya moyo wa Marcus Lichtenstein na kuelekeza njia ya kijana huyu hadi Battle Creek, ili aweze kuletwa chini ya ushawishi wa Ukweli na kuongoka; ili apate uzoefu na kuunganishwa na ofisi ya

uchapishaji. Elimu yake katika dini ya Kiyahudi ingemfanya astahili kutayarisha machapisho ya Kiebrania. Ujuzi wake wa Kiebrania ungekuwa msaada kwa ofisi hiyo katika utayarishaji wa machapisho ambayo kupitia kwayo kungeweza kupatikana kwa daraja ambalo lisingeweza kufikiwa. Haikuwa zawadi duni ambayo Mungu aliipa ofisi katika Marcus. Tabia yake na uangalifu wake ulikuwa kwa mujibu wa kanuni za Kweli za ajabu alizokuwa anaanza kuziona na kuzithamini. {3T 205.4}

Lakini ushawishi wa baadhi ya watu katika ofisi ulimhuzunisha na kumkatisha tamaa Marcus. Wale vijana ambao hawakumheshimu kama alivyostahili, na ambao maisha yao ya Kikristo yalikuwa kinyume na kazi yao na kukiri kwao, walikuwa njia ambayo Shetani alitumia kutenganisha kutoka kwa ofisi karama ambayo Mungu alikuwa ameipatia. Alienda zake akiwa amechanganyikiwa, akiwa na huzuni, na aliyevunjika moyo. Wale ambao walikuwa na uzoefu wa miaka mingi, na ambao walipaswa kuwa na upendo wa Kristo mioyoni mwao, walikuwa wametengwa mbali sana na Mungu kwa ubinafsi, kiburi, na upumbavu wao wenyewe hivi kwamba hawakuweza kutambua kazi maalum ya Mungu katika kumuunganisha Marcus na ofisi. {3T 206.1}

Kama wale waliounganishwa na ofisi wangekuwa macho na si walemavu wa kiroho, Ndugu I angekuwa ameunganishwa zamani na ofisi na angeweza sasa kuwa tayari kufanya kazi nzuri ambayo inahitaji kufanywa. Alipaswa kujishughulisha na kufundisha vijana wa kiume na wa kike, ili sasa wawe na sifa za kustahili kuwa wafanyakazi katika nyanja za umishenari. {3T 206.2}

Wale wanaoshiriki katika kazi hiyo wamekufa karibu theluthi mbili kwa sababu ya kukubali mivuto mibaya. Wamekuwa mahali ambapo Mungu hangeweza kuwashawishi kwa Roho wake Mtakatifu. Na, loo, jinsi moyo wangu unavyoumia ninapoona kwamba wakati mwingi umepita, na kwamba kazi kubwa ambayo ingeweza kuwa imefanywa imeachwa bila kufanywa kwa sababu wale walio katika nyadhifa muhimu hawajatembea kwenye nuru! Shetani amesimama tayari kuwahurumia watu walio katika wadhifa mtakatifu na kuwaambia kwamba Mungu hataki kwao bidii nyingi na utendaji kazi usio na ubinafsi, wa kujitoa kama vile Ndugu White anavyotazamia; na wanatulia chini bila kuwa na umakini kwenye kiti cha starehe cha Shetani, na adui aliye macho daima na mvumilivu anawafunga minyororo ya giza huku wakidhani kwamba wako sawa. Shetani hufanya kazi kwa mkono wao wa kulia na kushoto kwao, na pande zote zinazowazunguka; na wao hawajui. Wanaita giza nuru, na nuru, giza. {3T 206.3}

Ikiwa wale walio katika ofisi ya uchapishaji wanashiriki kweli katika kazi takatifu ya kutoa ujumbe mzito wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu, wanapaswa kuwa waangalifu jinsi gani wanatekeleza katika maisha yao kanuni za ile Kweli wanayoishughulikia. Wanapaswa kuwa na mioyo safi na mikono safi. {3T 207.1}

Watu wetu walio na uhusiano na ofisi hawajawa macho kuboresha upendeleo ulio katika uwezo wao wa kuufikia na kupokea talanta na mvuto wote ambao Mungu

amewapatia. Pamoja na karibu wote kushikamana na ofisi kuna kushindwa sana kutambua umuhimu na utakatifu wa kazi. Kiburi na ubinafsi vipo kwa kiwango kikubwa sana, na malaika wa Mungu hawavutiwi na ofisi kama ambavyo wangepaswa kuwa kama mioyo ingekuwa safi na katika mawasiliano/ushirika na Mungu. Wale wanaofanya kazi katika ofisi hawajapata kuhisi waziwazi kwamba Kweli walizokuwa wakishughulikia zilikuwa za asili ya kimbingu, zilizokusudiwa kutimiza kazi fulani na ya pekee, kama vile kuhubiri kwa Nuhu kabla ya Gharika kulivyokuwa. Kama vile mahubiri ya Nuhu yalivyoonya, yalivyowapima, yalivyowajaribu, na kuwathibitisha wakaaji wa dunia kabla ya gharika ya maji kuwaangamiza kutoka juu ya uso wa dunia, ndivyo Ukweli wa Mungu kwa siku hizi za mwisho unafanya kazi sawa ya kuonya, kujaribu na kuuthibitisha ulimwengu. Machapisho yanayotoka ofisini yana muhuri wa Milele. Yatawanywa kote nchini na wanaamua hatima ya roho za watu. Watu wanahitajika sana sasa wanaoweza kutafsiri na kutayarisha machapisho yetu katika lugha nyingine ili ujumbe wa onyo upate kwenda kwa mataifa yote na kuwapima wanadamu kwa nuru ya Kweli, ili wanaume na wanawake, kadiri waionavyo nuru, wageuke kutoka katika uasi na kuwa watii wa sheria ya Mungu. {3T 207.2}

Kila upendeleo/fursa inapaswa kuboreshwa ili kueneza Ukweli kwa mataifa mengine. Hii itafanyika kwa gharama kubwa, lakini gharama hazipaswi kwa namna yoyote ile kuzuia utendaji wa kazi hii. Mali ni za thamani tu zinapotumiwa kuendeleza maslahi ya ufalme wa Mungu. Bwana amewaazima wanadamu mali kwa kusudi hili hili, ili wazitumie katika kupeleka Ukweli kwa wanadamu wenzao. Kuna kiasi kikubwa cha mali za ziada katika safu ya Waadventista Wasabato. Na kuizuia kwa ubinafsi ili isitumike kwa kazi ya Mungu ni kupofusha macho yao kwa umuhimu wa kazi ya Mungu, na kuwafanya wasiweze kupambanua ukuu wa nyakati tunazoishi, au thamani ya utajiri wa milele. Hawaioni Kalvari katika nuru ifaayo, na kwa hiyo hawawezi kufahamu thamani ya nafsi ambayo kwayo Kristo alilipa bei hiyo isiyo na upeo. {3T 208.1}

Watu watawekeza mali katika kile wanachokithamini zaidi na ambacho wanadhani kitawaletea faida kubwa zaidi. Wakati watu watadiriki kuingia katika hatari kubwa na kuwekeza sana katika biashara za kidunia, lakini hawako tayari kujitosa au kuwekeza sana katika kusudi la kazi ya Mungu ya kupeleka Ukweli kwa wanadamu wenzao, wanathibitisha kwamba wanathamini sana hazina yao ya kidunia kuliko mbinguni kama kazi zao zinavyoonesha. {3T 208.2}

Kama watu wangeweka hazina yao ya kidunia juu ya madhabahu ya Mungu, na wangefanya kazi kwa bidii ili kupata hazina ya mbinguni kama walivyofanya ili kupata ile ya kidunia, wangewekeza mali kwa uchangamfu na kwa furaha popote pale ambapo wangeweza kuona fursa ya kutenda mema na kusaidia kazi ya Bwana wao. Kristo amewapa ushahidi usio na shaka wa upendo na uaminifu Wake kwao, Naye amewakabidhi mali za kuwajaribu na kuthibitisha uaminifu wao Kwake. Yeye

Aliacha mbingu, utajiri Wake na utukufu, na kwa ajili yao akawa maskini, ili kwa umaskini Wake wapate kuwa matajiri. Baada ya kujishusha hivyo ili kumwokoa mwanadamu, Kristo hahitaji machache kutoka kwa mwanadamu zaidi ya kwamba ajikane nafsi yake mwenyewe-kujinyima na kutumia mali ambayo amemwazima katika kuwaokoa wanadamu wenzake, na kwa kufanya hivyo atoe uthibitisho wa upendo wake kwa Mkombozi wake na kuonesha kwamba anathamini wokovu ulioletwa kwake kwa dhabihu hiyo isiyo na kikomo. {3T 208.3}

Sasa ni wakati wa kutumia mali kwa ajili ya Mungu. Sasa ndio wakati wa kuwa matajiri katika matendo mema, tukijiwekea akiba yetu msingi mzuri kwa wakati ujao, ili tuushike uzima wa milele. Nafsi/roho moja iliyookolewa katika ufalme wa Mungu ina thamani kuliko utajiri wote wa duniani. Tunawajibika kwa Mungu kwa ajili ya roho za wale wanadamu ambao tunakutana nao, na kwa kadri uhusiano wetu unavyokuwa wa karibu na wanadamu wenzetu na majukumu yetu yanaongezeka. Sisi ni undugu mmoja mkubwa, na ustawi wa wanadamu wenzetu unapaswa kuwa shauku/maslahi yetu makubwa. Hatuna dakika moja ya kupoteza. Ikiwa tumekuwa wazembe katika jambo hili, ni wakati muafaka sasa tuwe na bidii kuukomboa wakati, isije ikapatikana damu ya roho kwenye nguo zetu. Kama watoto wa Mungu, hakuna hata mmoja wetu ambaye amesamehewa kushiriki katika kazi kuu ya Kristo katika wokovu wa wanadamu wenzetu. {3T 209.1}

Itakuwa kazi ngumu kushinda ubaguzi na kuwaaminisha wanadamu wasioamini kwamba jitihada zetu za kuwasaidia hazipendezi. Lakini hii haipaswi kuzuia kazi yetu. Hakuna agizo katika Neno la Mungu linalotuambia tuwatendee wema wale tu wanaothamini na kuitikia juhudi zetu, na kuwanufaisha wale tu ambao watatushukuru kwa hilo. Mungu ametutuma kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu. Ni kazi yetu kufanya yote tuwezayo. “Asubuhi panda mbegu zako, wala jioni usiuzuie mkono wako; Tuna imani ndogo sana. Tunamuwekea mipaka/kikomo Mtakatifu wa Israeli. Tunapaswa kushukuru kwamba Mungu anajinyenyekeza na kushuka chini hata kumtumia yeyote kati yetu kama chombo Chake. Kwa kila maombi ya dhati yanayowekwa kwa imani kwa lolote, majibu yatarudishwa. Huenda yasije kama tulivyotarajia; lakini yatakuja, si labda kama tulivyopanga, lakini wakati ule tunapoyahitaji sana. Lakini, loo, kutokuamini kwetu kumekuwa dhambi jinsi gani kwetu! "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa." {3T 209.2}

Vijana wanaojishughulisha na kazi hii hawapaswi kuamini sana uwezo wao wenyewe. Hawana uzoefu na hivyo wanapaswa kutafuta kujifunza hekima kutoka kwa wale ambao wamekuwa na uzoefu wa muda mrefu katika kazi na ambao wamepata fursa za kujifunza tabia. {3T 209.3}

Badala ya ndugu zetu kuwahudumia watu wanaofanya kazi kati ya makanisa, Mungu anapanga watawanyike huko nje ya nchi na kazi yetu ya umishenari ipanuliwe zaidi kwa kadri tunavyoweza kumiliki eneo/ardhi ili kuweza kwenda kila

upande kuibua makundi mapya. Tunapaswa daima kubakiza kwenye mawazo ya wanafunzi wapya hisia ya umuhimu wa utume wetu. Kadri watu wenye uwezo wanavyoongokea Ukweli, hawahitaji watendakazi watakaopeperusha bendera yao ya [inayoashiria] imani hai; lakini watu hawa lazima waone umuhimu wa kufanya kazi katika shamba Lake Bwana. Kadri makanisa yanavyotegemea wafanyakazi kutoka nje ya nchi kuimarisha na kuhimiza imani zao, hayatawezakuwa na nguvu zao wenyewe. Wanapaswa kuelekezwa kwamba nguvu yao itaongezeka ikiwiana na juhudi zao binafsi. Kwa kadri tunavyoufuata kwa karibu zaidi mpango wa kazi za umishenari wa Agano Jipya ndivyo juhudi tunazozitumia zinavyokuwa na mafanikio zaidi. {3T 210.1}

Tunapaswa kufanya kazi kama Mwalimu wetu wa mbinguni, tukipanda mbegu za Kweli kwa uangalifu, mahangaiko, na kujinyima/kujikana nafsi. Ni lazima tuwe na nia ya Kristo ikiwa hatutachoka katika kutenda mema. Maisha Yake yalikuwa maisha ya dhabihu ya daima kwa manufaa ya wengine. Ni lazima tufuate mfano Wake. Ni lazima tupande mbegu ya Ukweli na kumtumaini Mungu ili kuihuisha. Mbegu ya thamani inaweza kulala kwa muda fulani bila kuota, wakati neema ya Mungu inaweza kuuthibitisha moyo na mbegu iliyopandwa kuamshwa kwenye uzima na kuchipua na kukua na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Wamishenari katika kazi hii kuu wanatafutwa kufanya kazi bila ubinafsi, kwa bidii, na kwa kudumu kama watenda kazi pamoja na Kristo na malaika wa mbinguni katika wokovu wa wanadamu wenzao. {3T 210.2}

Wachungaji wetu wanapaswa hasa kujihadhari na uvivu na majivuno, ambayo huwa na kawaida ya kukua kutoka kwa fahamu kwamba tuna ‘sisi tuna Ukweli na hoja zenye nguvu ambazo wapinzani wetu hawawezi kukabiliana nazo’; na ingawa Kweli tunazoshughulikia ni kuu kwa kubomoa ngome za nguvu za giza, kuna hatari ya kupuuza uchaji-Mungu wa kibinafsi, usafi wa moyo, na kujitolea kikamilifu kwa Mungu. Kuna hatari ya kujidhania kwamba wao ni matajiri wenye maongezo ya mali, huku wakiwa hawana sifa muhimu za Wakristo. Wanaweza kuwa wanyonge, maskini, vipofu, wasio na furaha, na uchi. Hawahisi umuhimu wa kuishi kwa kumtii Kristo kila siku na kila saa. Kiburi cha kiroho kimekula mambo muhimu ya kidini. Ili kuhifadhi unyenyekevu, ingekuwa vyema kukumbuka jinsi tunavyoonekana machoni pa Mungu mtakatifu, ambaye anasoma kila siri ya nafsi, na jinsi tunavyopaswa kuonekana mbele ya wanadamu wenzetu kama wangetujua kwa namna ile Mungu atujuavyo. Kwa sababu hii, ili kutunyenyekeza, tunaelekezwa kukiri makosa yetu, na kuboresha fursa hii ya kusalimisha majivuno yetu. {3T 210.3}

Wachungaji hawapaswi kupuuza mazoezi ya mwili. Wanapaswa kutafuta kujifanya kuwa wa manufaa na kuwa wa msaada pale wanapotegemea ukarimu wa wengine. Hawapaswi kuruhusu wengine wawangojee wakiwahudumia au kuwatumikia, bali wanapaswa kupunguza mizigo ya wale ambao, wakiwa na heshima kubwa sana kwa

huduma ya injili, wangejiweka kwenye usumbufu mkubwa kuwafanyia kile ambacho wanapaswa kujifanyia wenyewe. Afya duni ya baadhi ya wachungaji wetu ni kwa sababu ya kupuuza kwao mazoezi ya viungo katika kufanya kazi zenye manufaa au muhimu na kazi za mikono-wanataka kutumikiwa. {3T 211.1}

Kwa sababu jambo hilo limetokeza, Nilioneshwa kwamba ingekuwa afadhali kama akina Ndugu J wangefanya wawezavyo katika utayarishaji wa vijizuu ili visambazwe kati ya Wafaransa. Kama kazi hizi hazingetayarishwa katika utimilifu wake wote, zingeweza kuenezwa vyema zaidi, na Wafaransa wangeweza kupata fursa ya kuchunguza uthibitisho wa imani yetu. Kuna hatari kubwa katika kuchelewa. Wafaransa walipaswa kuwa na vitabu vinavyoeleza sababu za imani yetu. Ndugu J hawakuwa tayari kufanya haki na uadilifu kwa kazi hizi, kwa kuwa walihitaji kuwa wa kiroho na kuhuishwa wao wenyewe au vitabu vilivyotayarishwa vingekuwa na muhuri wa akili zao. Walihitaji kusahihishwa, isije ikawa mahubiri yao na maandishi yao yakawa ya kuchosha. Walihitaji kujielimisha ili waje mara moja kwenye vipengele muhimu na kuelezea tabia/sifa muhimu za imani yetu zionekane wazi mbele ya watu. Kazi imezuiliwa na Shetani, na mengi yamepotea kwa sababu kazi hizi hazikutayarishwa wakati zinapaswa kutayarishwa. Ndugu hawa wanaweza kufanya mema mengi kama watajitoa kikamilifu kwa kazi na ikiwa watafuata nuru ambayo Mungu amewapa. {3T 211.2}

SURA YA 23

ATHARI YA MAJADILIANO

Desemba 10, 1871, Nilioneshwa hatari za Ndugu K. Ushawishi wake juu ya kazi ya Mungu si vile inavyopaswa kuwa au inavyoweza kuwa. Anaonekana kuwa katika upofu kuhusu matokeo ya mwenendo wake; hatambui ni aina gani ya changamoto anayoacha nyuma yake. Hafanyi kazi kwa namna ambayo Mungu anaweza kukubali. Niliona kwamba alikuwa katika hatari kubwa kama alivyokuwa kwa Moses Hull kabla ya kuiacha Kweli. Alijiamini mwenyewe. Alifikiri alikuwa wa thamani kubwa sana kwa kazi ya Ukweli kwamba kazi hiyo haikuweza kutendekea bila yeye, hivyo wasingeweza kumfukuza. Kaka K amejisikia vivyo hivyo. Anategemea sana nguvu na hekima yake mwenyewe. Laiti angeuona udhaifu wake jinsi Mungu anavyouona hangejidanganya na kujisifia mwenyewe kamwe au kuhisi hata kupata ushindi. Na asipomfanya Mungu kuwa tegemeo lake na nguvu zake ataivunja meli ya imani kama alivyofanya Musa Hull. {3T 212.1}

Yeye katika kazi yake hapokei nguvu kutoka kwa Mungu. Anategemea msisimko ili kuamsha matamanio yake ya ukuuk. Katika kufanya kazi na wachache, ambapo hakuna msisimko maalum wa kuchochea, anapoteza ujasiri wake. Wakati kazi inapokuwa ngumu na anapokuwa hajabebwa na mhemko/msisimko huu wa pekee, basi hajishikilii imara zaidi kwa Mungu na kuwa dhati na bidii zaidi ya kuvuka giza na kupata ushindi. Ndugu K, mara kwa mara unakuwa katika hali ya kitoto, dhaifu, na usiyefaa kwa wakati ule unapopaswa kuwa na nguvu zaidi. Hii inapaswa kuwa ushahidi kwako kwamba bidii yako na matendo yako havitoki katika chanzo sahihi kila wakati. {3T 212.2}

Nilioneshwa kuwa hapa kuna hatari ya wachungaji vijana wanaojihusisha na majadiliano. Wanageuza mawazo yao kwenye kujifunza Neno ili kukusanya mambo makali, na wanakuwa wenye kejeli (wanashushua watu) na, katika jitihada zao za kukutana na mpinzani, mara nyingi sana wanamwacha Mungu nje ya swali-nje ya akili na utendaji wao. Msisimko wa mjadala hupunguza hamu yao katika mikutano ambapo msisimko huu maalum huwa haupo. Wale wanaoshiriki katika debate/mijadala sio vibarua waliofaulu zaidi na waliorekebishwa vyema ili kuijenga kazi. Kwa wengine, majadiliano yanatamaniwa, na wanapendelea aina

hii ya kazi kuliko nyingine yoyote. Hawajifunzi Biblia kwa unyenyekevu wa akili, ili wapate kujua jinsi ya kuufikia upendo wa Mungu; Kama Paulo asemavyo: “Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani, mkiwa na shina na msingi katika upendo, mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; upendo wa Kristo, upitao maarifa yote, mjazwe utimilifu wote wa Mungu.” {3T 212.3}

Wahubiri wachanga wanapaswa kuepuka mazungumzo yenye mijadala (debate), kwa kuwa hayaongezi hali ya kiroho au unyenyekevu wa akili. Katika baadhi ya matukio inaweza kuwa muhimu kukutana na mtu mwenye kiburi dhidi ya Ukweli wa Mungu katika mjadala wa wazi; lakini kwa ujumla mijadala hii, iwe ya mdomo au ya maandishi, husababisha madhara zaidi kuliko mema. Baada ya majadiliano jukumu kubwa zaidi liko juu ya mchungaji kuendeleza shauku ya watu na siyo mjadala tu. Anapaswa kujihadhari na mwitikio unaoweza kutokea baada ya msisimko wa kidini, na asikubali kuingia katika kujikatisha tamaa yeye mwenyewe. {3T 213.1}

Watu ambao hawatakubali madai ya sheria ya Mungu, ambayo ni wazi sana, kwa ujumla watachukua mkondo usio na sheria; kwani kwa muda mrefu wamechukua upande wa yule mwasi mkuu katika kupigana na sheria ya Mungu, ambayo ndiyo msingi wa serikali yake mbinguni na duniani, nao wamejizoeza katika kazi hii. Katika vita vyao hawatafungua macho yao au dhamiri zao kwa nuru. Hufumba macho yao wasije wakaangazwa. Kesi yao haina tumaini sawa na ile ya Wayahudi ambao hawangeiona nuru ambayo Kristo aliwaletea. Ushahidi wa ajabu aliowapa juu ya Umasihi Wake katika miujiza aliyoifanya, katika kuponya wagonjwa, kufufua wafu, na kufanya kazi ambazo hakuna mtu mwingine aliyezifanya au angeweza kuzifanya, badala ya kuyeyusha na kuitiisha mioyo yao, na kushinda ubaguzi wao mbaya, uliwachochea wawe na chuki na hasira ya kishetani kama vile Shetani aliyokuwa nayo alipofukuzwa kutoka mbinguni. Kadiri walivyokuwa na nuru kubwa na ushahidi, ndivyo chuki yao ilivyokuwa kubwa zaidi. Waliazimia kuizima nuru kwa kumwua Kristo. {3T 213.2}

Wachukiao sheria ya Mungu, ambayo ni msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani, wanamiliki ardhi sawa na Wayahudi wasioamini. Nguvu zao za ukaidi zitafuata wale wanaozishika amri za Mungu, na kiasi chochote cha nuru kitakataliwa nao. Dhamiri zao zimevunjwa kwa muda mrefu sana, na mioyo yao imekuwa migumu sana kwa kuchagua giza badala ya nuru, hata wanahisi kuwa ni wema ndani yao, ili kulifikia lengo lao, hutoa ushahidi wa uongo au kuinama karibia kila hatua iliyo sawa au yenye udanganyifu, kama walivyofanya Wayahudi katika kumkataa Kristo. Wanatoa hoja kwamba matokeo huhalalisha njia iliyotumika. Kwa hakika wanaisulubisha sheria ya Baba, kama Wayahudi walivyomsulubisha Kristo. {3T 213.3}

Kazi yetu inapaswa kukumbatia kila fursa ya kuwasilisha Ukweli katika usafi na usahili wake mahali pale ambapo kuna hamu au shauku yoyote ya kusikia sababu za imani yetu. Wale ambao wamekazia zaidi unabii na mambo ya kinadharia ya imani yetu wanapaswa bila kukawia kuwa wanafunzi wa Biblia juu ya masomo ya vitendo. Wanapaswa kuchukua rasimu ya kina zaidi kwenye chemchemi ya Ukweli wa mbingu. Wanapaswa kujifunza kwa uangalifu maisha ya Kristo na masomo Yake ya utauwa wa kivitendo, yaliyotolewa kwa faida ya wote na kuwa kanuni ya kuishi kwa haki kwa wote wanaopaswa kuamini Jina Lake. Wanapaswa kujazwa na roho ya Kielelezo wao mkuu na wawe na hisia ya juu ya maisha matakatifu ya mfuasi wa Kristo. {3T 214.1}

Kristo alikutana na kesi ya kila daraja katika masomo na namna ya mafundisho Yake. Alikula na kukaa pamoja na matajiri na maskini, na akalichukua Mwenyewe kufahamu masilahi na kazi za wanadamu, ili apate kuifikia mioyo yao. Wale wasomi na wenye akili nyingi zaidi walifurahishwa na kuvutiwa na hotuba Zake, na bado zilikuwa wazi na sahili kiasi cha kueleweka na akili za unyenyekevu zaidi. Kristo alijitolea Mwenyewe kila nafasi ya kuwapa watu mafundisho juu ya yale mafundisho ya mbinguni na maagizo ambayo yangepaswa kuingizwa katika maisha yao na ambayo yangewatofautisha na wanadini wengine wote kwa sababu ya tabia yao takatifu, iliyoinuliwa. Masomo haya ya mafundisho ya Mbingu hayaletwi kubeba dhamiri za watu jinsi inavyopaswa kuwa. Mahubiri haya ya Kristo huwapa wachungaji wanaoamini Ukweli wa leo unaowasilisha kwa hotuba ambazo zitafaa kwa karibu kila tukio. Hapa kuna sehemu ya kujifunza kwa mwanafunzi wa Biblia, ambayo hawezi shauku/kupendezwa nayo bila kuwa na roho ya Mwalimu wa mbinguni ndani ya moyo wake mwenyewe. Hapa kuna masomo ambayo Kristo aliwasilisha kwa tabaka zote. Maelfu ya watu wa kila aina ya tabia na kila daraja la jamii walivutwa na kuvutiwa na jambo lililoletwa mbele yao. {3T 214.2}

Wachungaji wetu wetu ambao wamekuwepo kwenye kazi ya kuhubiri Ukweli wa leo wamefanya makosa makubwa katika utendaji wao. Wamejielimisha kama wapiganaji/wagomvi. Wamekuwa wakijifunza mada zinazobishaniwa kwa lengo la kujadiliwa, na masomo haya ambayo wameyatayarisha wanapenda sana kuyatumia. Ukweli wa Mungu uko wazi, wazi, na unaojihitimisha wenyewe. Unapatana na, upo kinyume na makosa, na unaangaza kwa uwazi na kwa uzuri. Kupatana kwake kunauweka hukumuni kila moyo usiojaa chuki/ubaguzi. Kwa muda mrefu wahubiri wetu wanatoa hoja juu ya Ukweli, ambao umewekwa tayari kwa ajili yao, na, kama hakuna vikwazo, Ukweli huondoa ushindi. Lakini Nilioneshwa kwamba katika hali nyingi chombo duni [mtu] kinachukua sifa ya ushindi uliopatikana, na watu, ambao ni wa kidunia zaidi kuliko kiroho, wanasifu na kuheshimu chombo, wakati Ukweli wa Mungu hauinuliwi kwa ushindi uliopata. {3T 215.1}

Wale wanaopenda kushiriki katika majadiliano kwa ujumla hupoteza hali yao ya kiroho. Hawamwamini Mungu jinsi inavyopaswa. Wana nadharia ya Ukweli iliyoandaliwa kumtandika viboko mpinzani. Hisia za mioyo yao wenyewe isiyotakaswa zimetayarisha vitu vingi vikali, vya karibu vya kutumia kama mjeledi wao ili kumchukiza na kumkasirisha mpinzani wao. Roho wa Kristo hana sehemu katika hili. Huku kukiwa na mabishano madhubuti, mtoa mada kwenye mjadala anafikiri kwamba ana nguvu za kutosha kumshinda mpinzani wake, na Mungu anaachwa nje ya jambo hilo. Baadhi ya wachungaji wetu wamefanya malumbano kuwa ndiyo kibarua chao kikubwa. Wakiwa katikati ya msisimko unaoibuliwa na malumbano, wanaonekana wamesisimka na kuhisi kuwa na nguvu na kuzungumza kwa nguvu; na katika msisimko huo mambo mengi hupita huku watu wakidhani wapo sawa, jambo ambalo kwao wenyewe ni kosa na ni aibu kwa yule ambaye alikuwa na hatia ya kutamka maneno ambayo hayafai kwa mhudumu/mchungaji Mkristo. {3T 215.2}

Mambo haya yana uvutano mbaya juu ya wahudumu wanaoshughulikia Kweli takatifu, zilizoinuliwa, Kweli ambazo zitathibitika kuwa harufu ya uzima iendayo uzima, au ya kifo kuelekea kifo, kwa wale wanaozisikia. Kwa ujumla ushawishi wa malumbano juu ya wachungaji wetu ni ule wa kuwafanya wajitegemee na kujitosheleze wenyewe na wajitukuze katika makadirio yao wenyewe. Hii haikubaliki. Wale wanaopenda mijadala hawafai kuwa wachungaji wa kundi. Wamezoeza akili zao kukutana na wapinzani na kusema maneno ya kejeli/kushushua, na hawawezi kushuka chini ili kukutana na mioyo yenye huzuni na inayohitaji kufarijiwa. Pia wamekazia sana mabishano hivi kwamba wamepuuza mambo yanayofaa ambayo kundi la Mungu linahitaji. Wana ujuzi mdogo tu wa mahubiri ya Kristo, ambayo yanaingia katika maisha ya kila siku ya Mkristo, na wana mwelekeo mdogo tu wa kuyasoma. Wameinuka juu ya unyenyekevu wa kazi. Walipokuwa wadogo machoni pao wenyewe, Mungu aliwasaidia; malaika wa Mungu waliwahudumia na kufanya kazi zao zifanikiwe sana katika kuwasadikisha wanaume na wanawake kuhusu ile Kweli. Lakini katika mafunzo ya akili zao kwa ajili ya majadiliano mara nyingi huwa wakorofi, jeuri na wakali. Wanapoteza hamu na huruma nyororo ambayo inapaswa kuandamana na juhudi za mchungaji wa Kristo. {3T 216.1}

Wachungaji/wahudumu wa mijadala kwa ujumla hawastahili kulisaidia kundi linalohitaji sana msaada. Wakiwa wamepuuza dini ya vitendo katika mioyo na maisha yao wenyewe, hawawezi kulifundisha kundi. Isipokuwa kuna mihemko/msisimko, hawajui jinsi ya kufanya kazi; wanaonekana kupungukiwa na nguvu zao. Ikiwa wanajaribu kuzungumza, inaonekana hawajui jinsi ya kuwasilisha somo linalofaa kwa tukio hilo. Wakati wanapopaswa kuwasilisha somo ambalo litalisha kundi la Mungu, na ambalo litafikia na kuyeyusha nyoyo, wanarudi kwenye

baadhi ya mambo ya kale yaliyozoeleka na kupitia hoja zilizopangwa, zenye unyanyapaa, ambazo ni kavu na zisizovutia. Kwa hivyo, badala ya nuru na uzima, wanaleta giza kwa kundi na pia kwa roho zao wenyewe. {3T 216.2}

Baadhi ya wahudumu wetu hushindwa kukuza/kusitawisha ari/hali ya kiroho, lakini huhimiza maonesho ya dhati na shughuli fulani zilizojengwa juu ya msingi usio na hakika. Wachungaji wenye kutafakari kwa utulivu, wenye mawazo na wapendao ibada, wenye dhamiri na imani, vilivyounganishwa na shughuli na ari/bidii, wanatafutwa katika enzi hii. Sifa mbili, mawazo na hali ya kupenda ibada, shughuli na bidii, vinapaswa kwenda pamoja. {3T 217.1}

Wachungaji wa debate/mijadala ndiyo wasiotegemewa zaidi miongoni mwetu, kwa sababu hawawezi kutegemewa kazi inapokuwa ngumu. Wapeleke mahali wanapopendezwa kidogo tu, nao wataonesha kwamba wanataka ujasiri, bidii, na kupendezwa kikweli. Wanategemea zaidi kusisimshwa na kutiwa nguvu na msisimko unaoletwa na mjadala au upinzani kama anavyofanya yule anayelewa kwenye pombe yake. Wachungaji hawa wanatakiwa kuongoka upya. Wanahitaji kunywa ndani kabisa ya vijito visivyokoma vinavyotoka kwenye Mwamba wa milele. {3T 217.2}

Hali njema ya milele ya wenye dhambi ilidhibiti na kuratibu mwenendo wa Yesu. Alikwenda huku na huko akifanya mema. Ukarimu ulikuwa uzima wa nafsi Yake. Hakuwatendea wema tu wale wote waliomjia wakiomba rehemaYake, bali aliwatafuta kwa kudumu. Hakuwahi kufurahishwa na kusifiwa/makofi au kukata tamaa kwa kulaumiwa au kukatishwa tamaa. Alipokutana na upinzani mkubwa na kutendewa kikatili zaidi alikuwa na ujasiri mzuri-alikuwa na uchangamfu na kutiwa moyo. Hotuba muhimu sana ambayo Uvuvio umetupatia, Kristo aliihubiri kwa msikilizaji mmoja tu. Alipokuwa ameketi juu ya kisima ili apumzike, kwa maana alikuwa amechoka, mwanamke Msamaria akaja kuteka maji; Aliona fursa ya kuifikia akili yake, na kupitia kwake kufikia akili za Wasamaria, waliokuwa katika giza kuu na upotofu/makosa. Ingawa alichoka, aliwasilisha Kweli za ufalme wake wa kiroho, ambao ulimvutia mwanamke wa kipagani na kumfanya amstaajabie Kristo. Akatoka nje akitangaza habari hii: “Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa Ndiye Kristo?” Ushuhuda wa mwanamke huyu uliwaongoa wengi na kuwaingiza kwenye imani katika Kristo. Kupitia taarifa yake wengi walikuja kumsikiliza Kristo wao wenyewe na kuamini kwa sababu ya neno lake mwenyewe. {3T 217.3}

Ijapokuwa idadi ya wasikilizaji wanaopendezwa inaweza kuwa ndogo, ikiwa mioyo yao inafikiwa, na uelewa unasadikisha, wanaweza, kama yule mwanamke Msamaria, kubeba taarifa ambayo itainua kiwango cha watu wenye shauku/kupendezwa kwa mamia nao watachunguza wao wenyewe. Wakati

wakifanya kazi katika maeneo ili kuinua kiwango cha wanaovutiwa, kutakuwa na mambo mengi ya kukatisha tamaa; lakini ikiwa mwanzoni inaonekana kuwa na shauku/maslahi kidogo tu, huo siyo ushahidi kwamba umekosea wajibu wako na mahali pa kazi. Ikiwa maslahi yanaongezeka kwa kasi, na watu wanasonga kwa uelewa, na wala haitokani na msukumo, lakini ni kutokana na kanuni, maslahi ni afya zaidi na ya kudumu kuliko pale ambapo msisimko mkubwa na shauku huanzishwa kwa ghafla, na hisia husisimua kwa kusikiliza mjadala, mchuano mkali kwa pande zote mbili za swali, ama kwa kuunga mkono Ukweli au kwa kuwa kinyume cha Ukweli. Kwa hivyo upinzani mkali unaundwa, misimamo inachukuliwa, na maamuzi ya haraka hufanywa. Na matokeo yake ni hali ya homa ya mambo. Kuzingatia kwa utulivu na kufanya maamuzi kunahitajika/hakupo. Wacha msisimko huu utulie, au acha mwitikio ufanyike kwa usimamizi usio na busara, na maslahi hayawezi kuoneshwa tena. Hisia na huruma za watu zilichochewa; lakini dhamiri zao hazikusadikishwa, na mioyo yao haikuvunjika na kunyenyekezwa mbele za Mungu. {3T 217.4}

Katika uwasilishaji wa Ukweli usiopendwa (usio maarufu) na watu wengi, unaohusisha msalaba mzito, wahubiri wanapaswa kuwa waangalifu kwamba kila Neno liwe kama vile Mungu mwenyewe angelifanya. Maneno yao yasiwe yanayokata-kata kamwe. Wanapaswa kuwasilisha Ukweli kwa unyenyekevu, kwa upendo wa ndani kabisa kwa roho na hamu ya dhati ya wokovu wao, na kuacha Ukweli wenyewe ukate. Wasiwadharau wachungaji wa madhehebu mengine na kutaka kuibua mjadala. Hawapaswi kusimama katika nafasi kama ile ya Goliathi alipoyatukana majeshi ya Israeli. Israeli hawakumtukana wala kumpa changamoto ya uthubutu Goliathi, lakini Goliathi alifanya majivuno yake dhidi ya Mungu na watu Wake. Kukaidi, kujisifu, kutukana mamlaka, kutoa uthubutu na matusi lazima yatoke kwa wapinzani wa Ukweli, wanaotenda kama Goliathi. Lakini hakuna hata mmojawapo wa roho hiyo inayopaswa kuonekana ndani ya wale ambao Mungu ametuma kutangaza ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu unaoangamizwa. {3T 218.1}

Goliathi aliamini silaha zake. Aliyatia hofu majeshi ya Israeli kwa majivuno yake ya ukaidi, ya kikatili, huku akifanya maonesho ya kustaajabisha ya silaha zake, ambazo zilikuwa nguvu zake. Daudi, katika unyenyekevu na bidii yake kwa Mungu na watu wake, alipendekeza kukutana na mtu huyu mwenye majigambo/majivuno. Sauli alikubali na kuweka silaha zake za kifalme juu ya Daudi. Lakini hakukubali kuzivaa. Alizivua silaha za mfalme, kwa maana hakuwa amezithibitisha. Alikuwa amemthibitisha Mungu na, kwa kumtumaini Yeye, alikuwa amepata ushindi maalum. Kuvaa silaha za Sauli kungetoa hisia kwamba yeye ni shujaa wa vita, wakati yeye alikujwa kijana mdogo tu, yaani Daudi aliyechunga kondoo. Hakutaka imaanishwe/imaanishe kwamba silaha za Sauli zipewe sifa, kwa maana tumaini lake lilikuwa kwa Bwana, Mungu wa Israeli. Alichagua vijiwe/kokoto chache kutoka kwenye kijito, na kwa kombeo na fimbo,

silaha yake pekee, akatoka kwa Jina la Mungu wa Israeli kukutana na shujaa mwenye silaha. {3T 218.2}

Goliathi alimdharau Daudi, kwa kuwa sura yake ilikuwa ya kijana tu ambaye hajafundishwa mbinu za vita. Goliathi alimtukana Daudi na kumlaani kwa miungu yake. Alihisi kwamba ilikuwa ni dharau juu ya hadhi yake kuwa na kijana mdogo tu, asiye na silaha nyingi, kuja kumkabili. Alijisifu kwa yale ambayo angemfanyia. Daudi hakukasirika kwa sababu alionwa kuwa duni sana, wala hakutetemeka kwa vitisho vyake vya kutisha, bali alijibu hivi: “Ndipo Daudi akamwambia yule Mfilisti, Wewe unanijia mimi na upanga, na fumo, na mkuki, bali mimi ninakujia wewe kwa Jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli uliowatukana.” Daudi anamwambia Goliathi kwamba kwa Jina la Bwana atamfanyia mambo yale yale ambayo Goliathi alikuwa ametishia kumfanyia Daudi. “Nao jamii ya watu wote pia wajue ya kwamba Bwana haokoi kwa upanga wala kwa mkuki; maana vita ni vya Bwana, Naye atawatia ninyi mikononi mwetu.”{3T 219.1}

Wachungaji wetu hawapaswi kutukana na kuwatishia watu kwa uthubutu, na kuzusha mijadala. Acheni wenye kukaidi wawe upande wa wapinzani wa Kweli ya Mungu. Nilioneshwa kwamba Ndugu K na wahudumu wengine wametenda sana sehemu ya Goliathi. Na kisha baada ya kuthubutu na kuchochea majadiliano wameamini katika mabishano yao yaliyotayarishwa, kama ambavyo Sauli alitaka Daudi atumainie silaha zake. Hawajamtumainia Mungu wa Israeli kama Daudi mnyenyekevu, na kumfanya Yeye kuwa nguvu zao. Wameenda wakiwa na ujasiri na majivuno, kama Goliathi, wakijitukuza na kutojificha nyuma ya Yesu. Walijua Ukweli ulikuwa na nguvu, na kwa hiyo hawajanyenyekeza mioyo yao na kwa imani kumtumainia Mungu kuipa Kweli ushindi. Wamefurahishwa na kupoteza msimamo wao, na mara nyingi majadiliano hayajafaulu, na matokeo yake yamekuwa ni madhara kwa nafsi zao na kwa nafsi za wengine. {3T 219.2}

Nilioneshwa kwamba baadhi ya wachungaji wetu vijana wanapata shauku ya kufanya mijadala (mabishano), na kwamba, wasipoona hatari yao, hii itathibitisha mtego kwao. Nilioneshwa kwamba Ndugu L yuko katika hatari kubwa. Anaifundisha akili yake katika mwelekeo mbaya. Yuko katika hatari ya kupanda juu ya usahili wa kazi. Anapovaa silaha za Sauli, akiwa, kama Daudi, ana hekima ya kuzivua kwa sababu hajazithibitisha, anaweza kupona kabla hajaenda mbali sana. Wahubiri hawa wachanga wanapaswa kusoma mafundisho ya kivitendo ya Kristo pamoja na ya kinadharia, na kujifunza juu ya Yesu, ili wapate neema Yake, upole Wake, unyenyekevu Wake na kujishusha kwa akili. Ikiwa wao, kama Daudi, wameletwa katika nafasi ambayo kusudi la Mungu kwa Kweli linawaita wakutane na mtukanaji na mtu anayejigamba kwa Israeli, na kama wanakwenda katika nguvu za Mungu, wakimtegemea Yeye kabisa, Yeye atawabeba na kusababisha Ukweli Wake ushinde kwa utukufu. Kristo ametupa mfano. “Lakini Mikaeli, malaika mkuu, aliposhindana

na Ibilisi, na kuhojiana naye kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kumshitaki kwa kumlaumu, bali alisema, Bwana na akukemee.” {3T 220.1}

Mara tu mhubiri anaposhuka kutoka kwenye nafasi ambayo mchungaji hapaswi kamwe kuwa nayo, na kushuka kwenye kichekesho ili kuunda kicheko juu ya mpinzani wake, au anapokuwa na kejeli na mkali na kumtukana, anafanya kile ambacho Mwokozi wa ulimwengu hakuthubutu kufanya; kwa maana anajiweka juu ya ardhi ya adui. Wahudumu wanaoshindana na wapinzani wa Kweli ya Mungu si lazima wakutane na wanadamu tu, bali Shetani na jeshi lake la malaika waovu. Shetani hutafuta nafasi ya kupata faida kutoka kwa wachungaji wanaotetea Ukweli, na wanapoacha kuweka imani yao yote kwa Mungu, na maneno yao hayako katika roho na upendo wa Kristo, malaika wa Mungu hawawezi kuwaimarisha na kuwaangazia. Wanawaacha kwa nguvu zao wenyewe, na malaika waovu wanashinikiza giza lao; kwa sababu hii wapinzani wa Ukweli nyakati fulani wanaonekana kuwa na faida, na majadiliano, yana madhara zaidi kuliko manufaa halisi. {3T 220.2}

Wachungaji wa Mungu wanapaswa kumkaribia zaidi. Ndugu K, L, M, na N wanapaswa kuwa wakitafuta kusitawisha uchaji-Mungu wa kibinafsi-utauwa binafsi, badala ya kuhimiza upendo wa malumbano. Wanapaswa kutafuta kuwa wachungaji wa kundi, badala ya kufaa wenyewe kuunda msisimko kwa kugeuza hisia za watu. Ndugu hawa wako katika hatari ya kutegemea zaidi umaarufu wao na mafanikio yao kwa watu kama wabishanaji werevu kuliko kuwa wanyenyekevu, watenda kazi waaminifu na wafuasi wa Kristo waliojitoa, wanyenyekevu, watenda kazi pamoja Naye. {3T 221.1}

SURA YA 24

HATARI NA WAJIBU WA VIJANA

Imetumwa kwa Vijana Wawili

Desemba iliyopita Nilioneshwa hatari na majaribu ya ujana. Wana wawili wadogo wa Baba O wanahitaji kuongoka. Wanahitaji kufia nafsi zao kila siku. Paulo, mtume mwaminifu, alikuwa na uzoefu mpya kila siku. Anasema: “Mimi hufa kila siku.” Huu ndiyo uzoefu hasa ambao vijana hawa wanahitaji. Wako katika hatari ya kupuuza wajibu wa sasa na kupuuza elimu ambayo ni muhimu kwa maisha ya vitendo. Wanaiona elimu katika vitabu kuwa jambo muhimu zaidi linalopaswa kushughulikiwa ili kufanya maisha kuwa yenye mafanikio. {3T 221.2}

Vijana hawa wana kazi za nyumbani ambazo hawazizingatii. Hawajajifunza kuchukua wajibu na kubeba majukumu ya nyumbani ambayo ni wajibu wao kuyabeba. Wana mama mwaminifu, mwenye utendaji, ambaye amebeba mizigo mingi ambaye watoto wake hawakupaswa kubeba. Katika hili wameshindwa kumuenzi mama yao. Hawajashiriki mizigo ya baba yao kama ilivyokuwa wajibu wao, na wamepuuza kumheshimu baba inavyopaswa. Wanafuata mwelekeo badala ya wajibu. Wamefuata njia ya ubinafsi maishani mwao, katika kuepuka mizigo na taabu, na wameshindwa kupata uzoefu wenye thamani ambao wasingeweza kumudu kunyimwa kama wangefanikisha maisha. Hawajahisi umuhimu wa kuwa waaminifu katika mambo madogo, wala hawajahisi wana wajibu kwa wazazi wao wa kuwa wakweli, kamili, na waaminifu katika majukumu ya unyenyekevu na duni ya maisha ambayo yamo moja kwa moja katika njia yao. Wanaangalia juu ya matawi ya kawaida ya ujuzi, hivyo ni muhimu sana kwa maisha ya vitendo. {3T 221.3}

Kama vijana hawa wangekuwa baraka mahali popote, basi mahali hapo palipaswa kuwa nyumbani. Kama wataachilia mwelekeo, badala ya kuongozwa na uamuzi wa uangalifu wa sababu yenye kiasi, uamuzi mzuri wenye busara, na dhamiri iliyoelimika, hawawezi kuwa baraka kwa jamii au kwa familia ya baba zao, na matazamio yao katika ulimwengu huu na katika ulimwengu bora zaidi yanaweza kuwa hatarini. Vijana wengi hupokea fikra kwamba maisha yao ya utotoni hayakuundwa kwa ajili ya utunzaji/utumishi/kazi, bali kumangamanga katika michezo ya bure, katika mzaha, katika dhihaka, na anasa za kipumbavu. Huku wakishiriki katika upumbavu na kujifurahisha kwa hisia, wengine hawafikirii chochote ila kuridhika kwa kitambo kulikounganika nako. Tamaa yao ya kujifurahisha, upendo wao kwa jamii na kupiga soga na kucheka, huongezeka kwa

kujifurahisha, kujiridhisha na wanapoteza furaha yote kwa ajili ya hali halisi ya maisha, na majukumu ya nyumbani yanaonekana kutokuvutia. Hakuna mabadiliko ya kutosha kukabiliana na akili zao, na wanakuwa wasiotulia, wanyonge, na wenye kukasirika. Vijana hawa wanapaswa kuhisi kuwa ni wajibu wao kupafanya nyumbani kuwa pa furaha na palipochangamka. Wanapaswa kuleta mwanga wa jua ndani ya makao, badala ya kivuli kwa njia ya kulalamika kusiko na sababu na hali ya kutoridhika inayoondoa furaha. {3T 222.1}

Vijana hawa wanapaswa kukumbuka kwamba wanawajibika kwa upendeleo wote walioufurahia, na kwamba wanawajibika kwa uboreshaji wa wakati wao na lazima watoe hesabu kamili kwa ajili ya uboreshaji wa uwezo wao. Wanaweza kuuliza: Je, tusiwe na tafrija au maburudisho? Je, tufanye tu kazi, kazi, kazi, bila kubadilisha mandhari na kufanya jambo jingine? Matumbuizo yoyote ambayo wanaweza kushiriki katika kuomba baraka za Mungu juu yake kwa imani haitakuwa hatari. Lakini tafrija/matumbuizo yoyote ambayo huwanyima sifa ya kusali kwa faragha, na kufanya ibada kwenye madhabahu ya sala, au kushiriki katika mkutano wa maombi si salama, bali ni hatari. Mabadiliko kutoka kwenye kazi ya kimwili ambayo imetoza nguvu nyingi inaweza kuwa muhimu sana kwa muda, ili waweze kujishughulisha tena na kazi, wakiweka juhudi kubwa ili kupata mafanikio makubwa zaidi. Lakini mapumziko yote huenda yasiwe ya lazima, au hata kuandamana na matokeo bora zaidi kadri nguvu zao za kimwili zinavyohusika. Hawahitaji, hata wakiwa wamechoka na aina moja ya kazi, kuchezea na kupoteza nyakati zao za thamani. Kisha wanaweza kutafuta kufanya jambo ambalo si la kuchosha sana, lakini ambalo litakuwa baraka kwa mama na dada zao. Katika kupunguza mahangaiko yao kwa kujitwika mizigo mizito zaidi wanayopaswa kubeba, wanaweza kupata burudiko lile ambalo linatokana na kanuni na ambalo litawaletea furaha ya Kweli, na wakati wao ukiwa hautumiki katika mambo madogo madogo au katika kujifurahisha kwa ubinafsi. Wakati wao unaweza kutumika kwa faida daima, na wanaburudishwa kila wakati kwa namna tofauti tofauti, na huku bado wakiukomboa wakati, ili kila wakati utumike kwa kumbukumbu njema kwa ajili ya mtu fulani. {3T 222.2}

Umefikiria kuwa ilikuwa muhimu zaidi kupata elimu katika sayansi. Hakuna wema katika ujinga, na ujuzi hautapunguza ukuaji wa Kikristo; lakini ukiitafuta kutokana na kanuni, ukiwa na lengo sahihi mbele yako na kuhisi wajibu wako kwa Mungu katika kutumia uwezo wako kuwatendea wengine mema na kukuza utukufu Wake, ujuzi utakusaidia kutimiza lengo hili; itakusaidia kutumia nguvu ambazo Mungu amekupa, na kuzitumia katika utumishi Wake. {3T 223.1}

Lakini, vijana, mkipata maarifa mengi sana na bado mkashindwa kuyatumia maarifa hayo kwa vitendo, mnashindwa kutimiza lengo lenu. Ikiwa, katika kupata elimu, mnajishughulisha sana na masomo yenu hata mkapuuza sala na upendeleo wa kidini, na kuwa wazembe na kutojali ustawi wa roho yenu, ikiwa mtaacha

kujifunza katika shule ya Kristo, mnauza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza kwaajili ya supu ya dengu iliyojaa mkanganyko. Kusudi la kupata elimu halipaswi kusahaulika kwa muda. [Elimu] inapaswa kukuza na kuelekeza uwezo wenu ili uweze kuwa muhimu zaidi na kuwabariki wengine kwa kiwango cha juu cha uwezo wenu. Iwapo kwa kupata elimu mnaongeza kujipenda kwenu wenyewe, na mwelekeo wenu wa kutojihusisha kubeba majukumu, ingekuwa bora muwe hivyo hivyo bila elimu. Iwapo mnapenda na kuabudu vitabu, na kuviruhusu viingie kati yenu na wajibu wenu, ili mhisi kusita kuacha masomo yenu na kusoma kwenu ili kufanya kazi muhimu ambayo mtu fulani lazima aifanye, mnapaswa kuzuia hamu yenu ya kusoma na kukuza upendo kwa kufanya mambo ambayo sasa hamyapendelei. Mtu aliye mwaminifu katika lililo dogo zaidi atakuwa mwaminifu katika mambo makubwa zaidi. {3T 223.2}

Mnahitaji kusitawisha upendo na shauku kwa wazazi wenu na kwa ndugu na dada zenu. “Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu; kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana; kwa tumaini, mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; katika kusali, mkidumu; kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu; katika kukaribisha wageni mkijitahidi.” Vijana, hamwezi kumudu kuyatoa mhanga maisha yenu ya milele kwa ajili ya masomo yenu ya shule. Waalimu wenu wanaweza kuwachochea kwa kuwasifia, na kuwapigia makofi na mnaweza kudanganywa na ujanja wa Shetani. Mnaweza kuongozwa hatua kwa hatua kutafuta kufaulu na kupata ukubali wa waalimu wenu, lakini ujuzi wenu katika maisha ya mbingu, katika dini ya vitendo, utakua ukishua chini, na chini zaidi. Majina yenu yatasimama yakiwa yameandikwa mbele ya malaika watakatifu, walioinuliwa na mbele ya Muumba wa ulimwengu na Kristo, na Mkuu wa mbinguni, katika mwanga mbaya sana. Pembeni yao kutakuwa na kumbukumbu ya dhambi, makosa, kushindwa, kupuuza, na ujinga kama huo katika maarifa ya kiroho kwamba Baba na Mwanawe, Yesu Wakili wetu, na malaika wanaohudumu wataona haya kuwamiliki ninyi kama watoto wa Mungu-kusema kwamba ninyi ni wa kwao. {3T 224.1}

Katika kuhudhuria shule mnakabiliwa na majaribu mbalimbali ambayo msingekabiliwa nayo nyumbani katika nyumba ya baba zenu, chini ya uangalizi wa wazazi wanaomcha Mungu. Ikiwa nyumbani kwenu mlisali peke yenu mara mbili au tatu kwa siku kwa ajili ya neema ya kuepuka maovu yaliyomo duniani kwa njia ya tamaa, mnapaswa kusali zaidi mnapokuwepo mashuleni katika kizazi hiki kilichopotoka, kwa kuwa mazingira yenu hayafai zaidi katika malezi ya tabia ya Kikristo. {3T 224.2}

Vijana hawa hawana nguvu za kutosha za tabia ya Kikristo; hasa ndivyo hali ilivyo kwa A O. Hajatulia, hana mizizi, na hajajikita katika Ukweli. Mshiko wake kwa Mungu umekuwa madogo sana hata amekuwa hapokei nguvu na nuru kutoka juu,

bali amekuwa akikusanya giza kwenye nafsi yake. Amesikia kutokuamini kukizungumzwa sana na amependezwa kidogo sana na Kweli hivi kwamba hayuko tayari kutoa sababu ya tumaini lake. Yeye hana utulivu kama mwanzi unaotetemeshwa na upepo. Yeye ni mkarimu moyoni, bado anapenda vichekesho na kupata raha/fun, uvivu, na ushirika wa marafiki zake wachanga. Amejiingiza katika mwelekeo huu kwa gharama ya kutoa mhanga maslahi ya nafsi yake. Ni muhimu ndugu yangu kuepuka kujichanganya sana katika jamii ya vijana wasio na dini. Utamaduni wa akili na moyo wako, kuhusiana na majukumu ya kivitendo ya maisha, unahitaji kwamba sehemu kubwa ya wakati wako itumike katika jamii ya wale ambao mazungumzo na imani yao itaongeza imani na upendo wako kwa Ukweli. {3T 225.1}

Umejaribu kutupilia mbali kizuizi ambacho imani ya ile Kweli imekiweka, lakini haujathubutu kuwa na ujasiri sana katika kutoamini kwako. Mara nyingi sana walawi wa dunia, na jamii ya wale ambao kwao ushirika na dini vimetengwa, yamekuwa chaguo lako, na umekuwa, kwa nia na makusudio yote, ukihesabiwa pamoja na tabaka hilo linalouletea Ukweli dharau/laumu. Huna nguvu za kutosha katika imani au katika kusudi hadi uwe katika jamii kama hiyo. Ili kupoteza wakati umejiingiza katika roho ya mazungumzo ya kipuuzi, ambayo yamekuletea jeraha chanya kwa kuihafifisha dhamiri yako. Unapenda kupongezwa na kukubalika. Ukipata hayo kwa njia ya heshima, si dhambi sana; lakini uko katika hatari ya kujidanganya mwenyewe na wengine; unahitaji kulindwa katika hatua hii na kuona kwamba unapata idhini yote unayopokea. Ikiwa umeidhinishwa kwa sababu ya kanuni zako nzuri za busara/utimamu na thamani ya maadili, hii ndiyo faida yako. Lakini ikiwa unabembelezwa, kusifiwa kwa kutia chumvi, na kudekeshwa na kusifiwa na kupongezwa kwa sababu unaweza kutoa hotuba zenye kung'aa na maneno ya kufaa, na kwa sababu wewe ni mchangamfu, unaifanya hotuba kuwa na maneno ya kuchekesha/kuburudisha/werevu, na mwenye akili, na si kwa sababu ya uthamani wa kiakili na kimaadili, utaonwa na wanaume na wanawake wenye busara, wacha Mungu na wenye akili timamu kama kitu cha kuhurumiwa badala ya kuonewa wivu. Unapaswa kulindwa dhidi ya kusifiwa kwa kutia chumvi. Yeyote aliye mpumbavu kiasi cha kukusifu wewe kwa kupitiliza hawezi kuwa rafiki yako wa kweli. Marafiki zako wa kweli watakuonya, kukusihi, na kukukemea, kukaripia na kuyafunua makosa yako. {3T 225.2}

Umefungulia akili yako kwa giza la kutokuamini. Ifunge kwa kumcha Mungu. Tafuta ushahidi, nguzo, za imani yetu na uzishike kwa uthabiti. Unahitaji ujasiri huu katika Ukweli wa leo, kwa kuwa utathibitisha nanga kwako. Itaweka kwenye tabia yako nguvu, ufanisi, ubora, uungwana, na hadhi nzuri ambayo itaamuru heshima. Himiza mazoea ya ujasiriamali. Unapungukiwa sana hapa. Wewe na ndugu yako mna mawazo mazuri sana ya kufanikiwa, lakini kumbuka kwamba kwa Mungu ni tumaini lenu la pekee. Matarajio yako wakati fulani yanaweza kuonekana kuwa ya kujipendekeza kwako au kukudanganya, lakini matarajio yanayokuinua juu ya kazi

rahisi, duni za nyumbani, na juu ya majukumu ya kidini, yatathibitisha kushindwa. Ninyi, marafiki zangu wapendwa, mnahitaji kunyenyekea mioyo yenu mbele za Mungu na kupata uzoefu mzuri na wa thamani katika maisha ya Kikristo kwa kufuata kumjua Bwana na kuwabariki wengine kwa maisha ya kila siku ya usafi usio na doa, uadilifu uliotukuka, wa utimilifu katika maisha ya kila siku na utendaji wa wajibu wa Kikristo na wajibu wa maisha ya vitendo. Una majukumu ya kufanya nyumbani; una majukumu ya kubeba ambayo bado hujayainua. {3T 226.1}

Kile mnachopanda mtavuna pia. Vijana hawa sasa wanapanda mbegu. Kila tendo la maisha yao, kila Neno linalosemwa, ni mbegu ya mema au mabaya. Kama mbegu ilivyo, ndivyo na mazao yatakavyokuwa. Watu wakiendekeza pupa, tamaa mbaya, matamanio potovu au kuacha kukidhi haja ya chakula au mwelekeo wa mioyo yao isiyotakaswa; ikiwa watakuza kiburi au kanuni zisizo sahihi na kuthamini tabia za kutokuwa waaminifu au upotovu-ulevi, uasherati, uchafu, watajipatia mavuno mengi ya majuto, aibu, na kukata tamaa. {3T 226.2}

Malaika wa Mungu wanatafuta kuwaongoza vijana hawa kumlilia Bwana kwa unyofu: “ Bwana na Uwe kiongozi wa ujana wangu.” Malaika wanawaalika na kutafuta kuwavuta kutoka katika mitego ya Shetani. Mbingu inaweza kuwa yao ikiwa watatafuta kuipata. Taji ya utukufu usioweza kufa itakuwa yao ikiwa watatoa yote kwa ajili ya mbinguni. {3T 227.1}

SURA YA 25

WACHUNGAJI/WATUMISHI WAJITUNZAO WENYEWE (WAJIPENDAO WENYEWE)

Ndugu R, ushawishi wako haujawa ule wa tabia inayoleta heshima kwa kazi ya Ukweli wa leo. Ungekuwa umetakaswa na Ukweli unaowahubiria wengine, ungekuwa na faida mara kumi zaidi [10x] kwa kazi ya Mungu kuliko ulivyokuwa. Umetegemea sana juu ya kuunda hisia na umeamini kwamba bila hiyo utakuwa na ujasiri mdogo tu. Msisimko huu mkubwa na faida zake ndivyo vimekuwa nguvu yako na utukufu na mafanikio kama mtendakazi, lakini haya hayampendezi Mungu. Kazi yako katika mwelekeo huu ni nadra na umekuwa ukijidanganya mwenyewe kuwa yapo sawa. {3T 227.2}

Uchunguzi wa kina na karibu unaonesha Ukweli kwamba kuna miganda michache sana itakayokusanywa baada ya mikutano hii maalum ya kusisimua. Hata hivyo, kwa kutumia uzoefu wote wa nyuma, haujajifunza kubadilisha utaratibu wako wa kazi. Umekuwa mzito kujifunza jinsi ya kuunda kazi zako za baadaye katika namna ya kufuta makosa ya zamani. Sababu ya hali hii ni kuwa, kama mlevi, unapenda mihemko ya mikutano hii yenye kusisimua; na unaitamani kama mlevi anavyotamani glasi ya pombe ili kuamsha nguvu zake zilizofifia. Mijadala hii, ambayo husababisha msisimko, imekosewa kwa kudhaniwa kuwa italeta bidii kwa Mungu na upendo kwa Ukweli. Umepungukiwa na Roho wa Mungu wa kufanya Naye kazi katika juhudi zako. Kama ungekuwa na Mungu pamoja nawe katika harakati zako zote, na kama ungehisi mzigo kwa roho na ungekuwa na hekima ya kusimamia kwa ustadi misimu hii ya kusisimua kushinikiza roho kuingia katika ufalme wa Kristo, ungeona matunda ya kazi yako, na Mungu angetukuzwa. Nafsi yako yote inapaswa kuwashwa na roho ya zile Kweli unazoziwasilisha kwa wengine. Baada ya kutenda kazi ya kuithibitisha mioyo madai ambayo sheria ya Mungu inayo juu yao, ukiwafundisha kutubu kwa Mungu na imani katika Kristo, basi kazi yako hapo ndipo tu imeanza. Wewe pia mara kwa mara unajitolea udhuru kumaliza kazi na kuacha mzigo mzito ili wengine wauchukue katika kumaliza kazi ambayo unapaswa kufanya. Unasema kuwa huna stahiki kumaliza kazi hiyo. Halafu unajiambia, basi wapata ufuzu haraka katika kumaliza kubeba mapema mzigo wa mchungaji wa kondoo, au mchungaji wa watu, na mchungaji wa kundi, nayo itakuwa bora zaidi. {3T 227.3}

Kama mchungaji wa Kweli unapaswa kujitawala mwenyewe unaposhughulika na akili na kumpa kila aliye kwenye kundi la Mungu sehemu yake ya chakula kwa wakati wake. Unapaswa kuwa mwangalifu na ujifunze kuwa na masomo ya vitendo uliyoyachunguza na ambayo unaweza kuzama ndani yake kwa roho na kuwasilisha kwa njia ya wazi, na yenye nguvu kwa watu kwa wakati na mahali panapohitajika. Hujajikimu kikamilifu katika Neno la Uvuvio kwa ajili ya kazi zote nzuri. Wakati kundi linapohitaji chakula cha kiroho, wewe umekuwa ukitoa mada kadhaa za ubishani/malumbano ambazo hazikuwa zinafaa kulingana na hali iliyokuwepo bali yalikuwa mazungumzo juu ya mambo ya kitaifa. Ikiwa utajipa jukumu na kuelimisha akili yako kwa maarifa ya somo ambalo Neno la Mungu limekupatia,

unaweza kujenga kusudi la Mungu kwa kulisha kundi na chakula ambacho kingefaa na ambacho kingetoa afya ya kiroho na nguvu kama mahitaji yao yanavyotaka. {3T 228.1}

Bado haujajifunza kazi ya mchungaji wa Kweli. Utakapoelewa hili, kusudi na kazi ya Mungu vitakaa juu yako kwa uzito mkubwa kiasi kwamba hautakuwa na mwelekeo wa mizaha na utani, na hutashiriki mazungumzo mepesi na ya kijinga. Mhudumu wa Kristo mwenye mzigo sahihi wa kazi na mwenye hisia za juu za tabia iliyoinuliwa na utakatifu wa utume Wake hatapendelea kushughulikia mambo mepesi na kuzungumzia mambo hafifu na wana-kondoo wa kundi. {3T 228.2}

Mchungaji wa Kweli atapendezwa na yote yanayohusiana na ustawi wa kundi, kuwalisha, kuwaongoza, na kuwatetea. Atajibeba kwa hekima kubwa na atadhihirisha upole kwa wote, akiwa mwenye adabu, uungwana, staha na mwenye huruma kwa wote, haswa kwa waliojaribiwa, walioathirika na waliokata tamaa. Badala ya kulipatia kundi hili huruma ambayo shida zao maalum zinadai na ambazo udhaifu wao umekuwa ukizihitaji, wewe, ndugu yangu, umelikwepa kundi hili, huku ukiwavuta wengine kwa huruma. “Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi Yake iwe fidia ya wengi.” “Amin, amin, nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka.” “Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu.” “Basi imetupasa sisi tulio na nguvu kuuchukua udhaifu wao wasio na nguvu, wala haitupasi kujipendeza wenyewe. Hebu kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema, akajengwe. Kwa maana Kristo Naye hakujipendeza Mwenyewe; bali kama ilivyoandikwa, Malaumu yao waliokulaumu Wewe yalinipata Mimi.” {3T 228.3}

Siyo kazi ya mhudumu wa injili kujifanya kuwa bwana juu ya milki ya Mungu na kuwabamiza watu, bali kwa unyenyekevu wa akili, kwa upole na ustahimilivu, kukaripia, kukemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Je! Maandiko yaliyotangulia yatalinganaje na maisha yako ya zamani? Umekuwa ukikuza tabia ya ubinafsi karibu maisha yako yote. Ulioa mwanamke mwenye nia yenye nguvu-mkaidi [strong set will]. Tabia yake ya asili ilikuwa ya ubinafsi sana. Nyie wote wawili mlikuwa wenye kupenda ubinafsi, na kuunganisha matamanio yenu hakujasaidia shida ya yeyote kati yenu, lakini iliongeza hatari ya wote wawili. Wala hamkuwa waangalifu wote, na hofu ya Mungu haikuwa mbele yenu kwa kiwango cha juu. Kujipenda, kujiridhisha, imekuwa kanuni inayowatawala. Wote wawili mmekuwa na kujitoa wakfu kudogo sana kwa Mungu kiasi kwamba hamjanufaishana. Kila mmoja wenu ametaka njia yake mwenyewe; kila mmoja wenu ametaka kubembelezwa, kudekezwa na kusifiwa na kusubiriwa/kutumikiwa. {3T 229.1}

Bwana aliona hatari zako na mara kwa mara alikutumia maonyo kupitia Ushuhuda kwamba masilahi yako ya milele yalikuwa hatarini isipokuwa kama utaishinda hali yako ya kujipenda nafsi, na kuifanya nia yako ipatane na nia ya Mungu. Kama ungesikiliza maonyo na makemeo kutoka kwa Bwana, kama ungegeuka kabisa, na kubadilika kabisa, mke wako asingekuwa sasa katika mtego wa adui, akiwa amechwa na Mungu na kuuamini udanganyifu mkubwa wa Shetani. Laiti kama ungefuata nuru ambayo Mungu alitoa, hivi sasa ungekuwa mfanyakazi hodari, mwenye nguvu na mwenye ufanisi katika kazi ya Mungu, mwenye sifa ya kutimiza mara kumi zaidi ya vile unavyoweza kufanya sasa. Umekuwa dhaifu kwa sababu umeshindwa kutunza nuru. Mara chache sana umeweza kutambua sauti ya Mchungaji wa Kweli iliyo tofauti na ile ya mgeni au mtu baki. Kupuuza kwako kutembea katika nuru kumeleta giza juu yako, na dhamiri yako, ambayo kwa kukiukwa mara nyingi, imekufa ganzi. {3T 229.2}

Mke wako hakuamini na kufuata nuru ambayo Bwana kwa huruma alimtumia. Alidharau karipio, na yeye mwenyewe akafunga mlango ambao sauti ya Bwana ilisikika ikimshauri na kumuonya. Shetani alifurahi, na hakukuwa na chochote cha kumzuia kujishughulisha na ujasiri wake, na, kwa udanganyifu wake wa kupendeza na madanganyo, na yanayobembeleza, akamfanya kuwa mateka kwenye nia yake. {3T 230.1}

Bwana alikupa ushuhuda kwamba mke wako alikuwa kikwazo kwako katika kazi zako na kwamba haupaswi kuambatana naye hadi utakapokuwa na ushahidi wa kutosha zaidi kuwa amekuwa mwanamke aliyeongoka, aliyebadilishwa na aliyefanywa upya kwa akili yake. Kisha ukahisi kuwa una kisingizio cha kuomba nyumba; ukafanya ushuhuda huu udhuru wako na ukafanya kazi ipasavyo, ingawa hukuwa na haja ya nyumba yako mwenyewe. Mkeo alikuwa na majukumu ya kufanya kwa wazazi wake ambayo alikuwa amepuuzia maisha yake yote. Ikiwa angechukua jukumu hili lililopuuzwa kwa muda mrefu kwa roho ya uchangamfu basi sasa hangeachwa mateka kwa Shetani kutimiza nia yake na kuharibu moyo na roho yake katika utumishi wake. {3T 230.2}

Matakwa yako ya kuhitaji nyumba yalikuwa ya kufikirika, kama yalivyo matakwa yako mengi unayodhani. Ulipata nyumba ambayo ubinafsi wako ulitamani, na ungeweza kumwacha mke wako akiwa katika hali nzuri ya faraja/starege. Lakini Mungu alikuwa akimwandalia mtihani wa mwisho kwake. Mateso ya mama yake yalikuwa ya hali ambayo ingeamsha huruma moyoni mwake kama [moyo] haungekuwa umeshikwa kabisa, na kufanywa sugu na kuunguzwa kwa ubinafsi. Lakini majaliwa haya ya Mungu yalishindwa kuamsha upendo wa kifamilia wa binti kwa mama yake anayeteseka. Hakukuwa na nyumba inayojali iliyo tayari kusimama katika njia yake, hakuna watoto wa kushiriki upendo na matunzo yake, na umakini wake masikini! ukajielekeza kwa ubinafsi wake. {3T 230.3}

Mzigo wa masumbufu/utunzaji ambao baba yake alilazimika kuubeba ulikuwa mzito sana kwa umri wake na nguvu zake, na alikuwa amechoka kwa mateso makali. Ni hakika basi, kama binti angekuwa na eneo nyeti moyoni mwake, asingeweza kujizuia kuhisi na kuamsha hisia ya wajibu wake kushiriki mizigo ya dada yake na mume wa dada yake. Lakini alifunua hali ya moyo wake, kwa kutokujali kwake alikoonesha, na kwa kujiepusha na utunzaji na mzigo wote ambao angeweza kunyanyua, kwamba moyo wake ulikuwa mgumu kama jiwe. {3T 231.1}

Kuwa karibu na wazazi wake na bado kuonesha kutojali kulitosha kuelezea moyo wake ulivyo. Aliwasiliana na mumewe hali ya mambo. Ndugu R alikuwa mbinafsi kama mkewe, na alituma ombi la dharura ili [huyo mama] aje kwake. Ni kwa namna gani malaika wa Mungu, Je, malaika wale wenye huruma nyororo, kujali, upole na wenye upendo, wanaohudumia, walivyoliona tendo hilo? Binti aliwaacha wageni kufanya kazi kwenye ofisi hizo nyeti ambazo angepaswa kushirikiana kwa furaha na dada yake aliyelemewa. Malaika walitazama kwa mshangao na huzuni kwenye eneo hilo na kugeuka kutoka kwa mwanamke huyu mwenye ubinafsi. Malaika wabaya walichukua nafasi za hawa, na akachukuliwa mateka na Shetani kwenye nia yake adui. Alikuwa wakala wa Shetani na kwa hivyo alionekana kuwa kizuizi kikubwa kwa mumewe; kazi yake ilikuwa yenye umuhimu kidogo tu. {3T 231.2}

Kazi ya Mungu ingesimama juu zaidi huko ----- kama efoti/juhudi ile ya mwisho isingefanyika, maana kazi haikukamilika. Kuvutiwa kulifufuliwa/kuliamshwa, lakini iliendelea kuzama kwa namna ambayo isingeweza kuinuliwa tena. Ninakuuliza, Ndugu R, ulinganishe maandiko yaliyonukuliwa hapo awali kuhusiana na kazi na huduma ya Kristo na mwenendo wako kupitia kazi yako kama mhudumu wa injili, lakini haswa katika mfano niliyotaja, ambako jukumu lilikuwa wazi sana kwa mtu kuweza kufanya kosa lolote, kama dhamiri na nia visingekuwa vimepoozwa na mwendo mrefu wa ibada ya sanamu inayoendelea. {3T 231.3}

Kwa sababu ya kuwaacha wazazi wako katika mateso yao wakati walihitaji msaada, kanisa lililazimika kuchukua mzigo huu na kuwaangalia washiriki wa mwili wa Kristo waliokuwa wanateseka. Kwa kutojali huku, Mungu hachukulii kwa wepesi mambo kama hayo kwani yanamkasirisha. Yamewekwa kwenye kumbukumbu na malaika. Mungu hawezi kufanikisha wale ambao huenda moja kwa moja kinyume na wajibu ulio wazi kabisa uliowekwa katika Neno Lake, jukumu la watoto kwa wazazi wao. Watoto wanaojihisi kutowajibika kwa wazazi wao wa kidunia kuliko vile ulivyofanya wewe, lakini wanaweza kujiondoa kirahisi kutoka kwenye majukumu yaliyo juu yao, hawatakuwa na heshima inayostahili kwa Baba yao wa mbinguni; hawataonesha uchaji au kuheshimu madai ambayo Mungu anayo juu

yao. Ikiwa hawawaheshimu wazazi, yaani wanawadharau wazazi wao wa kidunia hawatamheshimu na kumpenda Muumba wao. Kwa kutowajali wazazi wake, mke wako alivunja amri ya tano ya Amri Kumi: “Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.” Hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi. Wale wasiowaheshimu au wasiowastahi wazazi wao hawapaswi kutarajia kwamba baraka ya Mungu itawajia. Wazazi wetu wana madai juu yetu kiasi kwamba hatuwezi kuyatupilia mbali au kuyapuuza. Lakini watoto ambao hawajafundishwa na kudhibitiwa katika utoto, na ambao wameruhusiwa kujifanya wenyewe kuwa mada kuu ya uangalizi wao -kitovu, kwa ubinafsi wakitafuta raha zao wenyewe na kujiepusha na mizigo, huwa na mioyo isiyo na huruma na hawaheshimu madai ya wazazi wao, waliowaangalia katika utoto wao. {3T 232.1}

Ndugu R, umekuwa mbinafsi katika vitu hivi mwenyewe na umejipunguzia sana majukumu. Umehitaji uangaliwe na utunzwe, lakini wewe mwenyewe hujawarudishia [wazazi wako mambo hayo unayodai]. Umekuwa mbinafsi na mkali, na mara nyingi umekuwa hauna busara na umempa nafasi ya majaribu mke wako. Wote wawili mmekuwa msiotakaswa na wenye ubinafsi wa kushangaza. Umejitoa muhanga kidogo kwa sababu ya Ukweli. Wewe, pamoja na mke wako, mmeepuka mizigo, na mmejichukulia nafasi ya kusubiriwa kuliko kujaribu kuwa mzigo mwepesi kwa wengine, kwa kadri iwezekanavyo. {3T 232.2}

Wachungaji/wahudumu wa Kristo wanapaswa kuhisi ni wajibu unaowahusu/unaowafunga, ikiwa watapokea ukarimu wa ndugu zao au marafiki, kuacha baraka kwenye familia kwa kutafuta kuhamasisha na kuimarisha washiriki wake. Wasipuuzie majukumu ya mchungaji, wanapotembelea nyumba kwa nyumba. Wanapaswa kufahamiana na kila mshiriki wa familia, ili waweze kuelewa hali ya kiroho ya wote, na kutofautisha aina yao ya kazi ili kukidhi mahitaji ya kila mmoja. Wakati mchungaji anayebeba ujumbe mzito wa onyo kwa ulimwengu anapopokea tabia za ukarimu za marafiki/wenyeji na ndugu, na anapuuza majukumu ya mchungaji wa kondoo na hajali katika mfano wake na tabia yake, akishirikiana na vijana katika mazungumzo ya upuuzi au hovyo, katika mizaha na utani, na katika kuelezea masimulizi/vihadithi vya kuchekesha ili kuunda kicheko/anectodes, hastahili kuwa mhudumu wa injili na anahitaji kuongoka kabla ya kukabidhiwa utunzaji wa kondoo na kondoo. Wachungaji walio wapuuziaji wa majukumu yanayowahusu wachungaji waaminifu hutoa ushahidi kwamba hawajatakaswa na Ukweli wanaowasilisha kwa wengine na hawapaswi kutegemezwa au kudumishwa kama watendakazi shambani mwa Bwana mpaka watakapokuwa na hali ya juu ya utakatifu wa kazi ya mhudumu wa Kristo. {3T 232.3}

Wakati kunapokuwapo mikutano ya jioni tu ya kuhudhuria, kuna wakati mwingi ambao unaweza kutumiwa kwa faida kubwa katika kutembelea nyumba kwa nyumba, na kukutana na watu mahali walipo. Na ikiwa wahudumu wa Kristo wana neema za Roho, ikiwa wataiga Mfano Mkuu, watapata ufikiaji wa mioyo na wataongoa roho kwa Kristo. Baadhi ya wachungaji wanaobeba ujumbe wa mwisho wa rehema wako mbali sana. Hawaboreshi fursa walizonazo za kupata kuaminika na watu wasioamini, kwa tabia zao zenye kupigiwa mfano, kwa kuvutiwa kwao kusiko na ubinafsi kwa ustawi wa wengine, kwa wema wao, kwa uvumilivu wao, kwa unyenyekevu wao wa akili, na kwa adabu yao yenye heshima/uungwana. Matunda haya ya Roho yatatoa ushawishi mkubwa zaidi kuliko mahubiri mimbarani bila juhudi za kibinafsi katika [kutembelea] familia. Lakini kuhubiriwa kwa Ukweli unaopima na ulionyoka kwa watu, vikiandamana na juhudi binafsi, ya ziara ya nyumba kwa nyumba, katika kukazia juhudi za kwenye mimbari, vitapanua kwa kiasi kikubwa ushawishi kwa wema, na roho zitaongolewa kwa Ukweli. {3T 233.1}

Baadhi ya wachungaji wetu hubeba majukumu mepesi mno, huku wakikwepa uangalizi na mizigo yao; kwa sababu hii hawahisi uhitaji wa msaada kutoka kwa Mungu, msaada ambao wangeuhitaji kama wangeinua mizigo ambayo kazi ya Mungu na Imani yetu inahitaji waiinue. Wakati mizigo katika kazi hii itakapobebwa, na wakati wale wanaoibeba watakapopelekwa katika sehemu zenye shida, watahisi hitaji la kuishi karibu na Mungu, ili wawe na ujasiri wa kumpa njia zao Bwana na kwa imani wadai msaada huo ambayo Yeye peke Yake Ndiye Mwenye uwezo wa kuutoa. Kisha watakuwa wakipata uzoefu wa kila siku katika imani na tumaini, ambavyo ni vya thamani kubwa kwa wahudumu wa injili. Kazi yao ni nzito na takatifu kuliko wahudumu kwa ujumla wanavyotambua. Wanapaswa kutembea na ushawishi uliotakaswa. Mungu anahitaji wale wanaohudumu katika mambo matakatifu wawe watu wanaohisi wivu kwa kazi Yake. Mzigo wa kazi yao unapaswa kuwa wokovu wa roho. Ndugu R, hajahisi kama nabii Yoeli anavyoelezea: “Hao makuhani, wahudumu wa Bwana, na walie Kati ya Patakatifu na madhabahu, Na waseme, Uwaachilie watu wako, Ee Bwana, Wala usiutoe urithi wako upate aibu, Hata mataifa watawale juu yao; Kwani waseme kati ya watu, Yuko wapi Mungu wao?” “Wapandao kwa machozi Watavuna kwa kelele za furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, Azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, Aichukuapo miganda yake.” {3T 234.1}

Ndugu R, nilioneshwa kuwa mwendo wako wa kazi umekuwa kinyume cha matakwa ya Neno la Mungu. Umekuwa mzembe kwa maneno yako na kwa tabia yako. Kondoo wamekuwa na mzigo wa kumtunza mchungaji, kuonya, kukaripia, kuhimiza, na kulia juu ya mwenendo wa hovyo wa mchungaji wao, ambaye, kwa kukubali ofisi yake, anakubali kuwa yeye ni mnenaji wa Mungu. Hata hivyo anajijali yeye mwenyewe zaidi kuliko anavyojali kondoo masikini. Hujahisi mzigo wa roho.

Hujaenda kazini kwako ukilia na kuomba kwa ajili ya roho ili wenye dhambi waweze kuongoka. Kama ungefanya hivyo ungekuwa unapanda mbegu ambayo itakua baada ya siku nyingi na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Unapokuwa huna kazi unayoweza kufanya katika mazungumzo ya kuota moto jioni wakati familia inapokusanyika kwa sala, unapaswa kuonesha ujasiriamali na matumizi mazuri ya wakati, na ujifunze kubeba majukumu kwa kujishughulisha, yenye manufa. {3T 234.2}

Wewe na mke wako mngeweza kuwa mmejiokoa na mambo yanayogeuka ghafla kuwa mabaya, na mngekuwa wachangamfu na wenye furaha kama msingekuwa mmetafuta maisha yasiyo na sulubu na kama mngechanganya kazi za mikono na masomo yenu. Misuli yako ilitengenezwa ili itumike, siyo kuwa ikae bila kutumika. Mungu aliwapa Adamu na Hawa katika Edeni kila kitu wanachotaka; lakini Baba yao wa mbinguni alijua kwamba wanahitaji kazi ili kudumisha furaha yao. Ikiwa wewe, Ndugu R, utafanya mazoezi ya misuli yako kwa kufanya kazi na mikono yako sehemu fulani ya kila siku, ukichanganya kazi za mikono na masomo, akili yako ingekuwa na uwiano ulio sawa, mawazo yako yangekuwa ya tabia iliyo safi na iliyoinuka zaidi, na usingizi wako ungekuwa wa asili zaidi na wenye afya. Kichwa chako kingekuwa kinachanganyikiwa mara chache zaidi na kisingewaza ujinga kwa sababu ya ubongo uliosongamana. Mawazo yako juu ya Ukweli mtakatifu yangekuwa wazi zaidi, na nguvu zako za maadili kuwa na nguvu zaidi. Hupendi kazi; lakini ni kwa faida yako kuwa na mazoezi zaidi ya mikono/mwili kila siku; kwa maana itachangamsha damu iliyozubaa ili ifanye shughuli za kiafya, na itakuvusha juu ya hali ya kutoridhika na udhaifu. {3T 235.1}

Haupaswi kupuuza kusoma na kujifunza kwa bidii, lakini unapaswa kuombea nuru kutoka kwa Mungu ili akufungulie ufahamu wako hazina za Neno Lake, ili upate kutoshelezwa kwa kazi zote njema. Kamwe hautakuwa katika nafasi ambayo haitakuwa lazima kwako kukesha na kuomba kwa dhati na bidii ili kushinda vitu vinavyokukera na kukusumbuasumbua. Utahitaji kulindwa kila wakati ili ubinafsi usionekane. Umehimiza tabia ya kujifanya uonekane/maarufu sana, ukizungumzia shida za familia yako na afya yako mbaya. Kwa kifupi, habari ya nafsi yako ndiyo imekuwa ndiyo mada ya mazungumzo yako na mada hiyo umekuja kukaa kati yako na Mwokozi wako. Unapaswa kujisahau mwenyewe na kujificha nyuma ya Yesu. Hebu Mwokozi mpendwa atukuzwe, lakini nafsi yako ipotee. Unapoona na kuhisi udhaifu wako hautaona kuwa kuna kitu ndani yako kinachostahili kutambuliwa au kupewa uzito. Watu hawajachoshwa tu, bali wamechukizwa, na utangulizi wako kabla ya kuwasilisha mada yako. Kila wakati unapozungumza na watu na kutaja majaribu ya familia yako, unajishusha wewe mwenyewe kwenye makisio yao na kupendekeza watu kukushuku kuwa haupo sawa (kuna shida fulani). {3T 235.2}

Una mfano wa wachungaji waliojiinua wenyewe na waliotamani sifa kutoka kwa watu. Walidekeshwa, walisifiwa-sifiwa na kubembelezwa nao ni wasio na busara hadi wakajiinua na kujiona wanajitosheleza, na, wakitumaini hekima yao wenyewe, na kuzamisha imani yao. Walifikiri walikuwa wanapendwa na maarufu sana kiasi kwamba wangeweza kuchukua hatua yoyote na bado wahifadhi umaarufu wao. Hii imekuwa dhana yako. Wakati mhudumu wa Kristo anapokuwa na tabia ya kutoa mambo ya masengenyo/uvumi kama mada ya kujadili, na maadili yake yanapohojiwa sana, hapaswi kuita huo kuwa ni wivu au kashfa. Unapaswa kuwa mwangalifu jinsi unavyotia moyo mafunzo ya mazoea ya fikra, ambako tabia zinaundwa ambazo zitathibitisha uharibifu wako. Tia alama wale ambao mwendo wao unapaswa kuchukia, na kisha usichukue hatua ya kwanza katika mwelekeo ambao wameenda nao. {3T 236.1}
Umekuwa ukijiona unajitosheleza na umepofushwa na kudanganywa na Shetani hata huwezi kutambua udhaifu wako na makosa mengi. “Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.” {3T 236.2}

Nilioneshwa uwanja wa kazi. Miji, majiji, na vijiji kila mahali vinapaswa kusikia ujumbe wa onyo; kwani wote watajaribiwa, watapimwa na kuthibitishwa na ujumbe wa Ukweli wa leo. Kazi kubwa inapaswa kufanywa, lakini wafanyakazi wanaoingia kwenye uwanja huu wanapaswa kuwa watu wa busara wanaojua jinsi ya kushughulika na akili. Wanapaswa kuwa watu wavumilivu, wema, waungwana na wenye adabu na wenye hofu ya Mungu mbele yao. {3T 236.3}

Mara nyingi unapata kuaminiwa na watu; lakini ikiwa, kwa tabia isiyofaa au kwa mwenendo mbaya wa uzembe, kwa ukali au roho ya kutojizuia na kutaka kuwatawala kwa mabavu, utapoteza kuaminika kwako, na imani yao, madhara zaidi yatatokea kwa kazi ya Mungu kama hakutakuwa na juhudi yoyote iliyofanywa. Madhara makubwa yametokea kwa kazi ya Mungu na wachungaji wanaoendeshwa na mihemko/hisia. Wengine hukereka kwa urahisi na hukasirika mara kwa mara; na, wakinyanyaswa, wanalipiza kisasi. Hivi ndivyo Shetani anavyofurahia kuwasababisha watende. Maadui wa Ukweli hushinda udhaifu huu kupitia kwa mchungaji/mhudumu wa Kristo, kwani ni aibu kwa kazi ya Ukweli wa leo. Wale wanaoonesha udhaifu huu wa tabia hawawakilishi Ukweli au wahudumu wa imani yetu. Ukosaji wa busara wa mchungaji mmoja hutupa wingu la tuhuma juu ya wote na hufanya kazi za wale wanaomfuata kuwa ngumu sana. {3T 236.4}

Ndugu R, unapoenda kufanya kazi katika uwanja mpya unapenda kuzungumzia mambo ya mabishano, kwa sababu umefundisha akili yako kwa aina hii ya kazi. Lakini kazi yako haijawahi kuwa na thamani ya moja ya kumi ya vile ilivyotakiwa kuwa kama wewe ungefuzu kuwa na uzoefu wa vitendo na kuwapa watu hotuba

juu ya masomo ya vitendo. Unahitaji kuwa mwanafunzi katika shule ya Kristo, ili uweze kupata utauwa wa vitendo. Unapokuwa na nguvu ya kuokoa ya Kweli kwenye nafsi yako mwenyewe huwezi kujizuia kulisha kundi la Mungu na Ukweli ule ule wa vitendo ambao umeufanya moyo wako mwenyewe ufurahi kwa Mungu. Matendo na mafundisho ya imani vinapaswa kuunganishwa ili kuishawishi mioyo na umuhimu wa kujitoa kwa madai ya Ukweli baada ya ufahamu kusadikishwa na uzito wa ushahidi. Watumishi wa Kristo wanapaswa kuiga mfano wa Bwana katika namna ya utendaji kazi wao. Wanapaswa daima kuweka mbele za watu, katika namna bora zaidi ya inayoeleweka kwao, umuhimu wa utauwa wa vitendo, na wanapaswa kuwaleta, kama alivyofanya Mwokozi wetu katika mafundisho yake, kuona umuhimu wa kanuni ya kidini na haki katika maisha ya kila siku. Watu hawalishwi na wahudumu wa makanisa maarufu, na roho zina njaa ya chakula ambacho kitarutubisha na kuzaa maisha ya kiroho. {3T 237.1}

Maisha yako hayana alama ya unyenyekevu wa akili na upole wa tabia. Unampenda Mungu kwa Neno, lakini siyo kwa tendo na kwa Ukweli. Heshima/hadhi yako inaumizwa kirahisi. Wachungaji wanapaswa kwanza kuhisi ushawishi utakasao wa ukweli juu ya mioyo yao na katika maisha yao wenyewe, na kisha juhudi zao za mimbarini zitatekelezwa na mfano wao wanaouonesha nje ya mimbari. Wachungaji wanahitaji kulainishwa na kujitakasa wenyewe mbele za Mungu kwa namna ya pekee kabla Mungu hajafanya kazi na juhudi zao. {3T 237.2}

Umeacha nafasi ya thamani/dhahabu ya kukusanya mavuno ya roho ikuponyoke kwa sababu haikuwezekana kwa Mungu kufanya kazi na juhudi zako, kwani moyo wako haukuwa sawa Naye. Roho yako haikuwa safi mbele Zake Yeye aliye Mfano wa usafi na utakatifu. Kama utazingatia uovu moyoni mwako, Bwana hatasikia maombi yako. Mungu wetu ni Mungu Mwenye wivu. Yeye anajua mawazo na taswira na udanganyifu wa moyo. Umefuata maamuzi yako mwenyewe na umeshindwa vibaya wakati ambapo ungeweza kufanikiwa. Kuna hatari kubwa katika juhudi hizi, kufanya kazi hiyo kwa uzembe au kwa kutozingatia hatari. Nafsi zinajaribiwa juu ya Ukweli muhimu, wa milele, na kile unachoweza kusema au kukifanya kitakuwa na ushawishi wa kusawazisha katika kuamua ikiwa wataamua kwa kuupokea Ukweli au dhidi ya Ukweli. Wakati ulipaswa kuwa katika unyenyekevu mbele za Mungu, ukimsihi afanye kazi sambamba na juhudi zako, akihisi uzito wa kazi na thamani ya roho, umechagua jamii ya mabinti, bila kujali utakatifu wa kazi ya Mungu na ya ofisi yako kama mchungaji wa injili ya Kristo. Ulikuwa umesimama kati ya walio hai na wafu; lakini bado ulijishughulisha na mazungumzo mepesi na ya kipuuzi, katika utani na mizaha. {3T 238.1}

Je, Malaika wanaohudumia wanawezaje kukuzunguka, wakiangazia mwanga juu yako na kukupa nguvu? Wakati unapaswa kutafuta njia, mbinu na uwezo wa kuangaza akili za wale walio katika upotofu na giza, nawe unajifurahisha mwenyewe na umekuwa mbinafsi sana kushiriki katika kazi ambayo huna

mwelekeo wowote nayo au huna upendo nayo. Kama msimamo wetu unalaumiwa na wale wanaokuchunguza, una uvumilivu kidogo nao. Mara nyingi unawapa jibu fupi la mkato na kali, kana kwamba hawakustahili kukuchunguza kwa karibu, lakini ni lazima wachukue yote yaliyowasilishwa kama Ukweli, bila kuchunguza wao wenyewe. Katika kazi yako ya huduma umegeuza roho nyingi kutoka kwenye Ukweli kutokana na namna ulivyowatendea. Siyo kwamba kila wakati utakuwa usiye na subira na usiyefikiwa; unakapojisikia utachukua muda wa kujibu maswali kwa uwazi; lakini mara kwa mara unakosa uungwana/adabu na mwenye hasira, mkali na mwenye mambo ya kipuuzi, nawe hukasirika kama mtoto. {3T 238.2}

Kabari la dhahabu lililofichwa na vazi la Babeli lilisumbua kambi yote ya Israeli. Hasira ya Mungu ilikuja juu ya watu kwa sababu ya dhambi ya mtu mmoja. Maelfu walishindwa vita na wakauawa kwenye uwanja wa vita kwa sababu Mungu hangebariki na kufanikisha watu ambao miongoni mwao kulikuwa na hata mwenye dhambi mmoja, ambaye alikuwa amekiuka Neno Lake. Dhambi hii haikuwa katika ofisi takatifu, lakini Mungu mwenye wivu hakuweza kwenda kupigana na majeshi ya Israeli wakati dhambi hizi zilizofichwa zilikuwa kambini. {3T 239.1}

Licha ya onyo la mtume kuwa mbele yetu “jitengeni na ubaya wa kila namna.” wengine wanaendelea kufuata mwendo usiokubaliana na Wakristo. Mungu anataka watu Wake wawe watakatifu, wajiweke mbali na matendo ya giza, wawe safi moyoni na maishani, na wasio na mawaa na ulimwengu. Watoto wa Mungu, kwa imani katika Kristo, ni watu Wake wateule; na watakaposimama juu ya ardhi takatifu ya Ukweli wa Biblia, wataokolewa kutoka kwa ushirika na matendo yasiyokuwa na matunda ya giza. {3T 239.2}

Ndugu R, umesimama moja kwa moja katika njia ya kazi ya Mungu na umeleta giza kubwa na kuvunjika moyo juu ya kusudi Lake. Umepofushwa na Shetani; umetafuta kufanya kazi ili watu wakusikitikie, na kweli huruma uliyoitaka umeipata. Kama ungekuwa umesimama kwenye nuru ungeweza kugundua nguvu ya Shetani akifanya kazi ili kukudanganya na kukuangamiza. Watoto wa Mungu hawali na kunywa ili kufurahisha hamu, lakini kuhifadhi maisha na nguvu ya kufanya mapenzi ya Bwana wao. Wanajivika kiafya, siyo kwa kuonesha au kuendana na mabadiliko ya mitindo. Tamaa ya jicho na kiburi cha maisha vimetengwa kutoka kwenye makabati yao ya nguo na kutoka majumbani mwao, kutoka kwa kanuni. Wanaondoka kutoka kwa udhati wa Bwana, na mazungumzo yao yameinuliwa na ya kimbinguni. {3T 239.3}

Mungu ni Mwenye huruma sana, kwani anaelewa udhaifu wetu na majaribu yetu; na tunapokuja Kwake na mioyo iliyovunjika na roho zilizopondeka, Yeye anakubali toba yetu, na anaahidi kwamba, kama tutashikilia nguvu Zake na kufanya amani Naye, tutafanya amani naye. Ah, ni shukrani kiasi gani, furaha kiasi gani, tunapaswa kuhisi kuwa Mungu ni Mwenye huruma! {3T 239.4}

Umeshindwa kutegemea nguvu za Mungu. Umekaa juu yako mwenyewe na umejifanya mada ya mawazo na mazungumzo. Majaribu yako yametukuzwa kwako mwenyewe na kwa wengine, na akili yako imegeuzwa kutoka kwa Ukweli, kutoka kwa Mfano ambao tunatakiwa kuiga, ili kumdhoofisha Ndugu R. {3T 240.1}

Unapokuwa nje ya mimbari unapaswa kuwa umehisi thamani ya roho na umekuwa ukitafuta nafasi za kuwasilisha Ukweli kwa watu binafsi, lakini haujahisi jukumu linalomhusu mhudumu wa injili. Yesu na haki hazikuwa mada zako, na fursa nyingi zimepotea ambazo, kama zingeboreshwa, zingeweza kuamua alama zaidi za roho zilizo tayari kutoa yote kwa ajili ya Kristo na Ukweli. Lakini mzigo huu hukuubeba. Kazi ya kichungaji ilihusisha msalaba, na wewe hukujihusisha katika huo. {3T 240.2}

Niliona malaika wa Mungu wakitazama maoni yako na matunda unayotoa nje ya mkutano, na ushawishi wako wa jumla kwa waamini na wasioamini. Niliwaona malaika hawa wakizifunika nyuso zao kwa huzuni na kwa huzuni wakigeuka bila kusita kutoka kwako. Mara kwa mara ulikuwa ukijishughulisha na mambo madogo-madogo, na wakati ulikuwa na juhudi za kufanya ambazo zinahitaji nguvu ya uwezo wako wote, fikira wazi, na sala ya bidii, ulifuata raha yako na mwelekeo wako, na uliamini nguvu zako na hekima yako kukutana, si na watu peke yao, bali enzi na nguvu, Shetani na malaika zake. Hii ilikuwa ni namna ya kuifanya kazi ya Mungu kwa uzembe na kuweka Ukweli na kazi ya Mungu hatarini, na kuhatarisha wokovu wa roho. {3T 240.3}

Mabadiliko kamili ni lazima yatendeke ndani yako kabla ya kukabidhiwa kazi ya Mungu. Unapaswa kuzingatia maisha yako kama Ukweli ulio halisi na siyo kama ndoto ya uvivu na kupoteza muda. Kama mlinzi juu ya kuta za Sayuni, wewe ni mtu anayeweza kuzuiwa kwa roho za watu. Unapaswa kukaa ndani ya Mungu. Unahama bila kuzingatia, kutokana na mhemko/msukumo badala ya kanuni. Hujahisi ulazima mzuri wa kufundisha akili yako, wala ya kumsulubisha ndani yako yule mtu wa kale na nia na tamaa zake. Unahitaji kusawazishwa na uzito wa Roho wa Mungu, na harakati zako zote kuthibitiwa na huyo. Sasa huna uhakika katika yote unayofanya. Unafanya na kufuta; unajenga na kisha kubomoa; unawasha shauku halafu kutokana na ukosefu wa kujitoa na hekima ya Bwana, unaizima. Hujatiwa nguvu, hujaimarishwa, na hujatulia. Umekuwa na imani kidogo tu; haujaishi maisha ya maombi. Unahitaji sana kuunganisha maisha yako na Mungu, na kisha hutapanda kwa mwili na kuvuna uharibifu mwishowe. {3T 240.4}

Mzaha, utani, na mazungumzo ya kidunia ni ya ulimwengu. Wakristo ambao wana amani ya Mungu mioyoni mwao watakuwa wachangamfu na wenye furaha bila kujishughulisha na upuuzi au mambo mapesi au ujinga. Wakati wakikesha kwa maombi watakuwa na utulivu na amani ambayo itawainua juu ya vitu vingi. Siri ya utauwa, iliyofunguliwa kwa akili ya mhudumu wa Kristo, itamwinua juu ya

starehe za kidunia, na mambo ya kijuu-juu [feki], uasherati, maadili ya kuelekea chini na msisimko. Atakuwa mshirika wa tabia ya Uungu, akiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Mawasiliano yaliyofunguliwa kati ya Mungu na nafsi yake yatamfanya kuzaa matunda katika maarifa ya mapenzi ya Mungu na kufungua mbele yake hazina ya masomo ya kivitendo ambayo anaweza kuwasilisha kwa watu, ambayo hayataleta purukushani au mfanano na tabasamu, lakini italeta umakini katika akili, itagusa moyo, itaamsha hisia za maadili kwa madai matakatifu ambayo Mungu anayo juu ya ushawishi na maisha. Wale ambao hufanya kazi kwa Neno na mafundisho wanapaswa kuwa watu wa Mungu, safi moyoni na maishani. {3T 241.1}

Wewe uko katika hatari kubwa zaidi ya kuleta aibu juu ya kazi ya Mungu. Shetani anajua udhaifu wako. Malaika zake wanawawasilishia pointi zako dhaifu wale wanaodanganywa na maajabu yake ya uwongo, na tayari wanakuhesabu wewe kama mmoja wa idadi yao. Shetani anafurahi wewe kufuata njia isiyo ya busara kwa sababu unajiweka chini ya ardhi yake na kumpa faida juu yako. Adui anajua vizuri kwamba uzembe wa watu wanaotetea sheria ya Mungu utazigeuza roho kutoka kwenye Ukweli. Hujachukua juu ya roho yako mzigo wa kazi na umefanya kazi kwa uangalifu na kwa bidii faraghani ili kuishawishi akili kuhusiana na Ukweli. Wewe pia mara nyingi hukosa subira, hukasirika, na kuwa mtoto, na unajitengenezea maadui kwa tabia zako za ghafla. Ni mpaka utakapokuwa kwenye uangalifu wako, utakuwa unadhuru roho dhidi ya Ukweli. Ni mpaka utakapokuwa mtu aliyebadilishwa, na uliyefanya maishani mwako kanuni za Kweli takatifu unazowasilisha kwenye mimbari, kazi yako itaishia kuwa ndogo sana tu. {3T 241.2}

Uzito wa jukumu upo juu yako. Ni wajibu wa mlinzi kuwa katika zamu yake kila wakati, akizilinda roho kama mmojawapo wa wale watakaopaswa kutoa hesabu. Ikiwa akili yako imechepuka kutoka kwa kazi kubwa na imejazwa na mawazo yasiyo matakatifu; kama mipango ya ubinafsi na miradi inanyang'anya usingizi, ambayo husababisha nguvu ya akili na mwili kupungua, unafanya dhambi dhidi ya nafsi yako mwenyewe na dhidi ya Mungu. Utambuzi wako umekuwa butu, na vitu vitakatifu vimewekwa katika kiwango sawa na vitu vya kawaida. Mungu anaaibishwa, kazi Yake inashutumiwa, na kazi nzuri ambayo ungeifanya pale ambapo ungemfanya Mungu kuwa tumaini lako inaharibiwa. Kama ungehifadhi nguvu ya uwezo wako na kuweka nguvu ya ubongo wako na mwili wako wote katika kazi muhimu ya Mungu bila kujizuia, ungekuwa umetambua kazi kubwa zaidi, na kazi hii ingefanywa kikamilifu zaidi. {3T 242.1}

Kazi zako zimekuwa na kasoro. Mfanyakazi hodari huwashirikisha watu wake kumfanyia kazi nzuri sana na yenye thamani ambayo inahitaji kuchunguza na kufikiria kwa umakini. Wanapokubali kuifanya kazi hiyo wanajua kwamba, ili kuifanikisha kazi hiyo sawasawa, vitivo vyao vyote vinahitaji kuamshwa na kuwekwa katika hali yake bora kabisa. Lakini mtu mmoja wa kundi hilo hutawaliwa

na hamu mbaya ya chakula. Anapenda pombe kali. Siku baada ya siku yeye hukidhi hamu yake ya vichocheo, na, wakati akiwa chini ya ushawishi wa kichocheo hiki, ubongo hujazwa ukungu, mishipa ya fahamu hudhoofika, na mikono yake huwa haipo sawa. Huendelea na kazi yake siku kwa siku na hukaribia kuiharibu kazi iliyokabidhiwa kwake. Mtu huyo hupoteza mshahara wake na hufanya madhara yasiyorekebishika kwa mwajiri wake. Kupitia ukosefu wake wa uaminifu anapoteza imani ya bwana wake na pia ya wafanyakazi wenzake. Alikabidhiwa jukumu kubwa, na kwa kukubali tumaini hilo walilomwekea, alikubali kuwa alikuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo kulingana na maagizo yaliyotolewa na mwajiri wake. Lakini kupitia kujipenda mwenyewe, na kuendekeza hamu ya kula naye akavuna matokeo yake. {3T 242.2}

Shida yako, Ndugu R, ni sawa na hii. Lakini uwajibikaji wa mhudumu/mchungaji wa Kristo, ambaye amewekwa ili auonye ulimwengu juu ya hukumu inayokuja, ni muhimu zaidi kuliko ule wa mfanyakazi wa kawaida kwani vitu vya milele ni vya maana zaidi kuliko vya kitambo. Ikiwa mchungaji/mhudumu wa injili hujitosa kwenye mwelekeo wake badala ya kuongozwa na wajibu, ikiwa anaitia nafsi kwa gharama ya kupoteza nguvu za kiroho, na matokeo yake husonga mbele bila busara, roho zitasimama katika hukumu kumhukumu kwa kutokuwa mwaminifu. Damu ya roho itapatikana kwenye mavazi yake. Inaweza ionekane kwa mchungaji asiyeongoka kuwa ni jambo dogo linalofaa, kujenga, na kisha kubomoa; kuvunja moyo, kufadhaisha, na kukatisha tamaa roho zile zilizoongolewa na Ukweli aliouwasilisha. Ni jambo la kusikitisha kupoteza ujasiri/tumaini la wale ambao amekuwa akifanya kazi ili kuwaokoa. Lakini matokeo ya njia isiyo ya busara iliyofuatwa na mchungaji haitaeleweka kikamilifu hadi pale mchungaji atakapoweza kuona kama Mungu aonavyo. {3T 243.1}

SURA YA 26

KUPENDA FAIDA KULIKOPINDUKIA

Ndugu S, nilioneshwa, Desemba 10, 1871, kwamba kuna kasoro kubwa katika tabia yako, ambayo, kama haitaonekana na kuthibitiwa, itathibitisha uharibifu wako; na hautapimwa tu katika mizani ya mahali Patakatifu, na kuonekana umepungua, lakini ushawishi wako utaamua hatima ya wengine. Ama utakuwa unakusanya pamoja na Kristo ama utakuwa unatawanyika kila kona. {3T 243.2}

Nilioneshwa kuwa una upendo wa kina kwa ulimwengu. Upendo wa pesa ni shina la mabaya yote. Unajidanganya mwenyewe kuwa upo sahihi, wakati siyo ilivyo. Mungu huona sivyo kama mwanadamu aonavyo. Huuangalia moyo. Njia Zake siyo njia zetu, wala mawazo Yake siyo mawazo yetu. Masumbuko yako makubwa na wasiwasi wako ni kupata mali. Shauku hii ya kunyonya imekuwa ikiongezeka juu yako mpaka inauzidi nguvu upendo wako wa Ukweli. Nafsi yako inaharibiwa kwa kupenda pesa. Upendo wako kwa Ukweli na maendeleo yake ni dhaifu sana. Hazina yako ya kidunia inadai na inashikilia matamanio yako. {3T 243.3}

Una maarifa juu ya Ukweli; wewe si mbumbumbu wa madai ya Maandiko; unajua mapenzi ya Bwana wako, kwa kuwa ameyafunua wazi wazi kwako. Lakini moyo wako hauelekei kufuata nuru inayoangaza juu ya njia yako. Una kipimo kikubwa cha kujikweza na kujidanganya mwenyewe. Upendo wako kwako ni mkubwa kuliko upendo wako kwa kazi ya Ukweli wa leo. Kujiamini kwako na kujitosheleza kwako hakika kutathibitisha uharibifu wako isipokuwa kama utaweza kuona udhaifu wako na makosa, na kufanya mabadiliko. Wewe ni jeuri na hutabiriki. Una nia yako mwenyewe unayotaka kuidumisha, na ingawa maoni ya wengine yanaweza kuwa sahihi, na uamuzi wako siyo sahihi, lakini wewe siyo mtu wa kukubali jambo na kujisalimisha (au kushindwa na kukubali mawazo ya wengine). Unashikilia maoni yako kwa hali ya juu, bila kujali maamuzi ya wengine. Natamani ungeona hatari ya kuendelea na hatua ambayo umekuwa ukiifuata. Kama macho yako yangeangazwa na Roho wa Mungu, ungeona vitu hivi wazi. {3T 244.1}

Mke wako anaupenda Ukweli, na yeye ni mwanamke wa vitendo, mwanamke wa kanuni. Lakini huitambui thamani yake. Amefanya kazi kwa bidii kwa faida ya kawaida ya familia, lakini haujampa ukubali wako. Hujashauriana naye kama ulivyo wajibu wako. Unafanya mambo yako kuwa siri yako mwenyewe; hupendi

kufungua moyo wako kwa mke wako na kumjulisha kile akili yako inachofikiria, na nini hisia zako na imani yako hasa. Wewe ni msiri. Mkeo hana nafasi ya heshima katika familia yako ile anayostahili kuwa nayo na ile aliyo na uwezo wa kuijaza. {3T 244.2}

Unadhani mkeo hapaswi kuingilia mipango na mikakati yako, na wewe pia mara nyingi huweka mapenzi na mipango ya utendaji kinyume chake. Unafanya mambo kana kwamba utambulisho wa mkeo ugezamishwa ndani ya utambulisho wako (identity/individuality), na yeye asiwe na utambulisho wake mwenyewe. Mungu atamwajibisha yeye kwa yale aliyotenda kwa nafsi yake. Wewe huwezi kumuokoa, naye hawezi kukuokoa. Ana dhamiri yake mwenyewe ambayo lazima aongozwe nayo. Unaonekana kutamani uwe dhamiri kwake, na wakati mwingine kwa watoto wako. Mungu anayo madai ya juu dhidi ya mke wako kuliko wewe ulivyo na madai juu yake. Mkeo anapaswa kujiundia tabia yake mwenyewe, na atawajibika kwa Mungu kwa tabia hiyo anayoiunda. {3T 244.3}

Unatakiwa kuunda tabia, na utawajibika kwa Mungu kwa tabia ile unayoikuza. Una mvuto wa kulazimisha na kutawala na roho ya kidikteta ambavyo havipatani na mapenzi ya Mungu. Lazima uache kuwa mkali sana na bainishi. Umejivuna kwamba wewe ndiwe chaguo bora zaidi la shirika/kundi lenu. Una maoni mazuri, lakini hujayaingiza maoni haya ya viwango na mazuri kwenye tabia yako na katika mwonekano wako. Umeshindwa kukamilisha tabia yenye uwiano. Una maoni mazuri yaliyopangiliwa, lakini sifa hizi zote nzuri za akili zimedhoofishwa na kuwa butu, na hali ya upotoshaji. Hujafuata masharti yaliyowekwa katika Neno la Mungu kwa wewe mwenyewe kuwa mwana wa Mungu. Ahadi zote za Mungu ziko juu ya masharti. “Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike. Basi, kwa kuwa tunayo ahadi hizi, wapenzi wangu, na tujitakase na uchafu wote wa mwili na roho, tukikamilisha utakatifu katika kumcha Mungu.”Uzoefu huu bado wewe hujaupata, nawe wapaswa uwe nao. Unapenda kuingia katika makundi ya wasioamini na kuwasikia wakiongea, na wewe mwenyewe pia kuchangia mazungumzo. Yesu hawezi kutukuzwa kwa mazungumzo yako na laiti kama ungekuwa na roho ya Yesu usingekuwa sana katika jamii ya wale ambao hawakuwa na upendo kwa Ukweli wa Mungu. {3T 245.1}

Umehisi kuwa kulikuwa na vizuizi kwa watoto wako kuwa Wakristo, na umehisi kuwa wengine wanapaswa kulaumiwa. Lakini usijidanganye kuhusu jambo hili. Ushawishi wako kama baba ulikuwa unatosha, kama kusingekuwa na kitu kingine chochote cha kuzuia, au kusimama katika njia yao. Mfano wako na mazungumzo yako vimekuwa vyenye tabia ambayo watoto wako hawakuweza kuamini kuwa ilikuwa inapatana na taaluma yako (kukiri kwako kwa mdomo). Mazungumzo yenu na wasioamini yamekuwa ya hali ya chini sana, mepesi, yaliyojaa mzaha na utani,

kiasi kwamba ushawishi wako hauwezi kuwainua kamwe. Ushirikiano wako na wengine [deal] daima hayajakuwa ya kiuaminifu kabisa. Hujampenda Mungu kwa moyo wako wote, kwa akili yako yote, na kwa nguvu zako zote, na jirani yako kama nafsi yako. Kama ingekuwa ni uwezo wako, ungejifaidisha wewe mwenyewe dhidi ya jirani zako. Kila senti/dola inayokujia kwa njia hii itabeba laana ambayo utahisi mapema au hivi punde. Mungu hutunza kumbukumbu ya kila kitendo cha dhuluma, kiwe kimetendwa kwa muumini au kafiri, na kamwe Yeye hatakidharau au kukiruka. Tabia yako ya kuwa na tamaa ni mtego kwako. Ushirikiano wako na wanadamu wenzako hauwezi kuhimili mtihani wa hukumu. {3T 246.1}

Tabia yako ya Kikristo imegundulika kuwa na madoa ya uchoyo. Madoa hayo itabidi yaondolewe, vinginevyo utakosa uzima wa milele. Kila mmoja wetu ana kazi ya kufanya kwa Mwalimu; kila mmoja wetu ana talanta za kuboresha. Yule mnyenyekevu na aliye maskini zaidi wa wanafunzi wa Yesu aweza kuwa mbaraka kwa wengine. Wanaweza wasitambue kuwa wanafanya tendo lolote maalum lililo jema au kubwa, lakini, kwa ushawishi wao wa kimya kimya, wanaweza kuanzisha mawimbi ya baraka ambayo yatapanuka na kuongezeka, na kamwe hawatajua matokeo ya furaha ya maneno yao na tabia thabiti hadi hatua ya mwisho ya ugawaji wa thawabu. Hawajisikii au hawajui kuwa wanafanya jambo lolote kubwa. Hawatakiwi kujichosha na wasiwasi juu ya mafanikio. Wanapaswa kusonga mbele tu, si kwa maneno mengi na kujitukuza na kujisifu, lakini kwa utulivu, wakifanya kwa uaminifu kazi ambayo uongozi wa Mungu umewapa, na hivyo hawatapoteza tuzo yao. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwako. Kumbukumbu ya uhai wako itaandikwa katika kitabu cha kumbukumbu; na kama utakuwa mshindi hatimaye, kutakuwapo na roho zilizookolewa kwa juhudi zako, kwa kujikana kwako, kwa maneno yako mazuri na kwa maisha thabiti ya Kikristo. Na wakati tuzo zitakapokuwa zikigawanywa kwa wote kama kazi zao zilivyokuwa, roho zilizokombolewa zitakuita heri, na Bwana atasema: “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu,” “ingia katika furaha ya Bwana wako.” {3T 246.2}

Ulimwengu umejawa na haraka kubwa, na kiburi, ubinafsi, uchu, ukatili na vurugu; na inaweza kuonekana kwetu kuwa ni kupoteza muda na pumzi kuwa katika msimu na nje ya msimu, na kwa nyakati zote kujiweka tayari kusema maneno ambayo ni ya upole, safi, yenye kuinua, yasiyo na doa, na takatifu, mbele ya kimbunga cha machafuko, zogo, na ugomvi. Na bado maneno yaliyosemwa vizuri, yakitoka kwa mioyo na midomo iliyotakaswa, na kudumishwa na tabia ya Kikristo na ya kiucha-Mungu, yatakuwa kama tofaa la dhahabu kwenye picha za fedha. Umekuwa kama mmoja wa wanenaji walio na ubatili na umeonekana kama mmoja wa walimwengu. Wakati fulani umekuwa mzembe katika maneno yako na mzembe katika mazungumzo yako na umejishusha kama Mkristo kwa maoni ya wasioamini. Wakati fulani umeuzungumza Ukweli; lakini maneno yako hayajabeba mvuto makini wenye kusukasuka, wenye kuhangaisha ambao ungeathiri moyo.

Yameambatanishwa na maneno mepesi, yasiyo na maana ambayo yangewaongoza wale unaozungumza nao kuamua kwamba imani yako si ya kweli na kwamba huziamini Kweli unazozikiri. Maneno ya kupendelea Ukweli, yanayosemwa katika kujiamini kwa utulivu, bila harara kwa kusudi lililo sawa na kutoka kwa moyo safi, yatafanya mengi kuondoa upinzani na kuongoa roho. Lakini roho ya ukali, ya ubinafsi, ya kushutumu itafukuza zaidi roho kutoka kwenye Kweli na kuamsha roho ya upinzani. {3T 247.1}

Hutakiwi kusubiria matukio makubwa-makubwa, au kutarajia uwezo wa ajabu, kabla hujafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Mungu. Haupaswi kufikiria vile walimwengu watakavyochukulia juu yako. Kama maingiliano yako na wao na mazungumzo yako ya kiucha Mungu ni ushuhuda ulio hai kwao juu ya usafi na udhati wa imani yako, na wanashawishika kuwa unatamani hasa kuwafaidisha, maneno yako hayatapotea kabisa juu yao, lakini yatakuwa yenye kuzaa mema. {3T 247.2}

Mtumishi wa Kristo, katika kitengo chochote cha huduma ya Kikristo, kwa maneno na kwa vitendo atakuwa na mvuto wa kuokoa juu ya wengine. Mbegu nzuri iliyopandwa inaweza kulala kwa muda mfupi katika moyo baridi, wa kidunia, wa ubinafsi bila kudhibitisha kwamba imekita mizizi; lakini mara kwa mara Roho wa Mungu hufanya kazi juu ya moyo huo na kuimwagilia na umande wa mbinguni, na mbegu iliyofichwa kwa muda mrefu huota na mwishowe huzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Hatujui katika kazi yetu ya maisha ni mbegu ipi itafanikiwa, ni hii au ile. Haya siyo mambo ya kutushughulisha sisi wanadamu masikini tunaokufa mwishowe. Tunapaswa kufanya kazi yetu, na kuacha Mungu ashughulikie matokeo. Kama ungekuwa gizani na kwenye ujinga, usingekuwa na hatia. Lakini umekuwa na nuru kubwa, umesikia Ukweli mwingi; na bado umekuwa si mtekelezaji wa Neno. {3T 248.1}

Maisha ya Kristo ni mfano kwetu sisi sote. Mfano Wake wa kujikana, kujitoa kafara, na ukarimu usio na ubinafsi ni mambo tunayotakiwa kuyaiga. Maisha Yake yote ni dhihirisho lisilo na mwisho la upendo Wake mkuu na kujishusha kumwokoa mwanadamu mwenye dhambi. “Pendaneni, kama vile Mimi nilivyowapenda ninyi,” asema Kristo. Ni kwa namna gani maisha yetu ya kujinyima, kujitolea, na ukarimu yatalinganishwa na maisha ya Kristo? “Nyinyi ni,” anasema Kristo, akiwaambia wanafunzi Wake, “nuru ya ulimwengu.” “Ninyi ni chumvi ya dunia.” Ikiwa huu ndiyo upendeleo na wajibu wetu pia, nasi tu miili ya kiza na kutokuamini, tunachukua jukumu zito kiasi gani! Twaweza kuwa mifereji ya nuru au ya giza. Ikiwa tumepuuza kuboresha nuru ambayo Mungu alikuwa ametupa, na tumeshindwa kuendeleza katika maarifa na utakatifu wa Kweli kama ambavyo nuru ilielekeza njia, tuna hatia na tuko gizani kulingana na nuru na Ukweli tuliopuuzia kuuboresha. Katika siku hizi za uovu na hatari tabia na kazi za wale

wanaodai kuwa Wakristo kwa ujumla hazitahimili mtihani wala kuvumilia kuumbuliwa wakati wa kuchunguzwa na nuru ambayo sasa inawaangazia. Hakuna mapatano kati ya Kristo na Beliali; hakuna ushirika kati ya nuru na giza. Je! Roho ya Kristo na roho ya ulimwengu vyawezaje kupatana? Bwana Mungu wetu ni Mungu mwenye wivu. Yeye Anahitaji mapenzi ya dhati na kujitoa kusikosazwa kwa wale wanaodai wanampenda. Mwandishi wa Zaburi anasema: “Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.” {3T 248.2}

Umesimama moja kwa moja ukizinga njia ya wokovu wa watoto wako. Unaweka kutokujali kwao kwa mambo ya kidini juu ya sababu zingine badala ya zile za Kweli. Mfano wako ni kikwazo kwao. Wanajua kwa matunda yako, kwa maneno na matendo yako, kwamba hauamini juu ya kuja Kwake Kristo hivi karibuni. Baadhi yao hawasiti kufanyia mzaha wazo la kuja kwa hivi karibuni kwa Kristo na ufupi wa wakati uliobaki. Wanaridhishwa sana unapobembeleza wafanya biashara kushusha bei za bidhaa zao kwenda chini zaidi [bargain], hata ikiwa ni kwa senti ndogo tu mradi wewe ujinufaishe. Wanafikiri kuwa baba anapenda sana biashara na kwamba hakuna mtu anayeweza kumshinda, na wanafuata nyayo zako. Imani bila matendo imekufa, ikiwa imani hiyo itakuwa peke yake. Pesa imekupa nguvu, na umetumia nguvu hiyo kujinufaisha kwa mahitaji ya wengine. Mawazo yako katika maisha ya biashara hayakuwa ya uaminifu, hukuwa mwenye haki na wanadamu wenzako. Kwa biashara yako umepoteza sifa yako kama Mkristo na kama mtu mwaminifu. Kwa biashara ya haki, mali hazikuingia katika milki yako haraka vya kutosha kutosheleza kiu yako ya kupata faida, na mara nyingi umefanya mizigo ya yule maskini iwe mizito zaidi kwa kutumia fursa ya uhitaji wake ili kujiongezea mali yako. Angalia kwa uangalifu, Ndugu S. Unapata hasara za kutisha ili kupata faida ya kidunia. Unapoteza uadilifu wa kibinadamu na fadhila ya kimbingu, katika saa ya jaribu. Je, hii ni faida au hasara? Je, wewe ni tajiri au maskini kwa maongezo yote hayo? Kwako ni hasara ya kutisha, kwani inachukua kiasi kingi tu kutoka kwa hazina ambayo unaweza kuwa umejikusanyia huko mbinguni. {3T 249.1}

Kila fursa ya kumsaidia ndugu aliye na shida, au kusaidia kazi ya Mungu katika kueneza Ukweli, ni lulu ambayo wewe unaweza kuituma mapema na kuiweka katika benki ya mbinguni kwa utunzaji ulio salama. Mungu anakujaribu na kukuthibitisha. Yeye Amekuwa akikupa baraka Zake kwa mkono wa ukarimu na sasa anaangalia kuona ni matumizi gani unayoyatumia, kuona ikiwa utawasaidia wale wanaohitaji msaada na ikiwa utahisi thamani ya roho na ufanye kile unachoweza na mali ambazo Yeye amekukabidhi. Kila fursa kama hiyo iliyoboreshwa huongeza hazina yako ya mbinguni. Lakini kujipenda mwenyewe kumesababisha upende mali za kidunia hata kwa gharama ya mali za mbinguni. Unachagua hazina ambayo nondo na kutu huharibu kuliko zile ambazo zinadumu kama umilele udumuvyo. Ni fursa yako kuonesha huruma nyororo ya kweli, kujali

na kubariki wengine; lakini macho yako yamepofushwa sana na mungu wa ulimwengu huu kiasi kwamba huwezi kugundua kito hiki cha thamani – baraka ya kupokelewa kutokana na kutenda mema, kwa kuwa tajiri wa matendo mema, kwa kuwa tayari kusambaza, kwa kuwa tayari kuwasiliana, kwa kujiwekea msingi mzuri dhidi ya wakati ujao, ili uweze kushikilia uzima wa milele. Unahatarisha nafsi yako kwa kupuuza kutumia fursa za thamani kupata hazina ya mbinguni. Je! umekuwa tajiri kweli kweli kwa ubahili wako, na kwa kusimamia mali zako kwa uchoyo? Mungu anakujaribu, na ni juu yako kuamua ikiwa utatoka dhahabu au taka isiyo na thamani. Je! Mlango wako wa rehema ungefungwa usiku wa leo, kumbukumbu yako ya maisha ingesimamaje? Hakuna hata senti/dola moja ya kile ulichojikusanyia ambacho ungeweza kuondoka nacho. Laana ya kila tendo lisilo la haki ingekuhudhuria. Ukali wako katika biashara wa kujipatia pesa, unapoonekana kwenye kioo ambacho Mungu atawasilisha mbele yako, hautasababisha kujipongeza. Tamaa ni ibada ya sanamu. {3T 249.2}

Tumaini lako pekee ni kuunyenyekeza moyo wako mbele za Mungu. “Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?” Ninakusihi: Usifumbe macho yako kwa hatari yako. Usiwe kipofu wa matamanio ya juu zaidi ya roho kwa kukimbilia matarajio ya heri na yenye utukufu ya maisha yaliyo bora. Watafutaji wenye mashaka, na waliolemewa na faida ya ulimwengu ni vipofu na wendawazimu. Wanageuka kutoka hazina isiyokufa, isiyoweza kuharibika, kwenda kwa ulimwengu huu. Kumeremeta na mapambo vya ulimwengu huu huvutia hisia zao, na vitu vya milele kutothaminiwa. Wanafanyia kazi kile ambacho hakishibishi na kutumia pesa zao kwa ajili ya kile ambacho siyo mkate/chakula, wakati Yesu anawapa amani na tumaini na baraka nyingi, kwa maisha ya utii. Hazina zote za dunia zisingeweza kuwa na utajiri wa kutosha kununua zawadi hizi za thamani. Hata hivyo wengi bado ni wendawazimu na wanageukia mbali kutoka kwa vivutio vya mbinguni. Kristo atatunza majina ya wote wasiohesabu kuwa ni dhabihu ya gharama kubwa sana iliyotolewa naye juu ya madhabahu ya imani na upendo. Yeye Alitoa dhabihu yote kwa ajili ya ubinadamu ulioanguka. Majina ya watiifu, wanaojitolea muhanga, na waaminifu yatachorwa kwenye viganja vya mikono Yake; hawatatapikwa midomoni Mwake, bali watachukuliwa midomoni Mwake, na Yeye atasihi kwa niaba yao mbele ya Baba. Wakati wabinafsi na wenye kiburi wanasahauliwa, wao watakumbukwa; majina yao hayatakufa. Ili tuwe na furaha sisi wenyewe, lazima tuishi kuwafurahisha wengine. Ni vizuri sisi kutoa mali zetu, talanta zetu, na mapenzi yetu kwa kujitolea kwa shukrani kwa Kristo, na kwa njia hiyo kupata furaha hapa na utukufu wa milele hapo baadaye. {3T 250.1}

Usiku mrefu wa kukesha, wa kutumika na kazi ngumu, unakaribia kupita. Kristo Yu karibu kuja. Jitayarishe. Malaika wa Mungu wanatafuta kukuvuta kutoka kwako na kutoka kwa vitu vya kidunia. Wacha wasifanye kazi hiyo bure. Imani, imani iliyo

hai, ndicho unachohitaji; Imani itendayo kazi kwa upendo na kutakasa roho. Kumbuka Kalvari yenye kutisha, na pale dhabihu isiyo na kikomo ikatolewa kwa ajili ya mwanadamu. Sasa Yesu anakualika uje Kwake vile ulivyo na kumfanya Yeye awe nguvu yako na Rafiki wa milele. {3T 251.1}

SURA YA 27

KANISA LA LAODIKIA

Ujumbe kwa kanisa la Laodikia ni masuto na ufunuo wa kustusha, na yanawahusu watu wa Mungu waishio wakati huu. {3T 252.1}

“Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa Kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa Changu. Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi.” {3T 252.2}

Bwana hapa anatuonesha kuwa ujumbe unaopaswa kupelekwa kwa watu Wake na wachungaji/wahudumu ambao amewaita kuonya watu siyo ujumbe wa amani na usalama. Siyo tu wa kinadharia, bali ni wa kivitendo kwa kila jambo. Watu wa Mungu wanawakilishwa katika ujumbe kwa Walaodikia kama walio katika hali ya usalama wa kimwili. Wako katika raha/starehe/wamebwetela, wakiamini kuwa wako katika hali ya juu ya mafanikio ya kiroho. “Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. {3T 252.3}

Ni udanganyifu gani mkubwa unaoweza kuja juu ya akili za wanadamu kuliko imani kwamba wapo sawa na wakati wakiwa wamekosea mno! Ujumbe wa Shahidi Mwaminifu unawakuta watu wa Mungu katika udanganyifu wa kusikitisha, lakini walio waaminifu katika udanganyifu huo. Hawajui kuwa hali yao ni ya kusikitisha mbele za Mungu. Wakati wale waliohutubiwa wakijifariji wenyewe kwamba wako kwenye hali ya kiroho iliyoinuliwa, ujumbe wa Shahidi Mwaminifu huvunja usalama wao kwa ufunuaji au kuanikwa nje kwa masuto ya kusitusha ya hali yao halisi ya upofu wa kiroho, umaskini, na unyonge. Ushuhuda, huo mkali na unaokata, hauwezi kuwa wenye makosa, kwa kuwa ni Shahidi Mwaminifu Ndiye anayezungumza, na ushuhuda Wake ni lazima uwe sahihi. {3T 252.4}

Ni vigumu kwa wale wanaojisikia salama katika mafanikio yao, na ambao wanajiamini kuwa matajiri katika maarifa ya kiroho, kupokea ujumbe unaotangaza kwamba wamedanganywa na wenye uhitaji wa kila namna ya neema ya kiroho. Moyo usiotakaswa ni “mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha.” Nilioneshwa kuwa wengi wanajidanganya wenyewe kwamba wao ni Wakristo wazuri, ambao hawana hata mwale wa nuru kutoka kwa Yesu. Hawana uzoefu wa maisha kwa ajili yao wenyewe katika maisha ya uchaji-Mungu. Wanahitaji kazi kamili na yenye kina ya kujidhili mbele za Mungu kabla ya kuhisi hitaji lao la dhati na la bidii, za kudumu kupata neema za thamani za Roho. {3T 253.1}

Mungu huwaongoza watu Wake hatua kwa hatua. Maisha ya Kikristo ni maisha ya mapambano na gwaride la kusonga mbele daima. Hakuna kupumzika vitani. Ni kwa juhudi za kudumu, zisizokoma ndipo tunapoweza kudumisha ushindi juu ya majaribu ya Shetani. Kama kundi la watu tunashinda katika uwazi na nguvu ya Ukweli. Tunadumishwa kikamilifu katika nafasi zetu kutokana na idadi kubwa ya ushuhuda ulio wazi wa Maandiko. Lakini tunapungukiwa sana na unyenyekevu wa Biblia, uvumilivu, imani, upendo, kujikana, kukesha, kuwa macho, kuwa makini na roho ya dhabihu Tunahitaji kukuza utakatifu wa Biblia. Dhambi inatawala miogoni mwa watu wa Mungu. Ujumbe wazi unaokemea wa Walaodikia haujapokelewa. Wengi hushikilia mashaka yao na dhambi zao pendwa/vipenzi wakati wakiwa katika udanganyifu mkubwa sana wa kuongea na kuhisi kama watu wasiohitaji chochote. Wanadhani ushuhuda wa Roho wa Mungu katika kukemea hauhitajiwi kuja kwao kwani ni makosa wao kupewa au haukuwamaanisha wao. Watu kama hao wapo katika hitaji kuu la neema ya Mungu na utambuzi wa kiroho ili wapate kugundua mapungufu yao ya maarifa ya kiroho. Wanakosa karibu kila sifa iliyo muhimu kukamilisha tabia ya Kikristo. Hawana maarifa halisi ya Kweli ya Biblia, ambayo ingepelekea wao kuwa na maisha ya unyenyekevu yanayolandanisha mapenzi yao na mapenzi ya Kristo. Hawaishi kwa kutii matakwa yote ya Mungu. {3T 253.2}

Haitoshi tu kudai kuuamini Ukweli. Askari wote wa msalaba wa Kristo kwa Kweli hujipa jukumu la kuingia kwenye krusade/vita dhidi ya adui wa roho, kuhukumu makosa na kudumisha haki. Lakini ujumbe wa Shahidi Mwaminifu unafunua Ukweli kwamba udanganyifu wa kutisha uko juu ya watu wetu, jambo linalolazimisha kuwaendea kwa maonyo, ili kuvunja usingizi wao wa kiroho, na kuwaamsha kwa vitendo vyenye maamuzi. {3T 254.1}

Katika maono yangu ya mwisho nilioneshwa kuwa hata ujumbe huu maalum wa Shahidi Mwaminifu haujakamilisha mpango wa Mungu. Watu bado wanasinzia katika dhambi zao. Wanaendelea kujitangaza wao wenyewe kuwa ni matajiri na wasio na haja ya kitu chochote. Wengi huuliza: Hivi kwa nini makemeo haya yote yalitolewa? Kwa nini Ushuhuda unaendelea kutushutumu kwa kurudi nyuma na kwa

dhambi za kuhuzunisha? Tunapenda Ukweli; tunafanikiwa; hatuna haja ya shuhuda hizi za onyo na karipio. Lakini hebu wanung'unikaji hawa waichunguze mioyo yao na kulinganisha maisha yao na mafundisho halisi ya Biblia, hebu wanyenyekeze roho zao mbele za Mungu, hebu neema ya Mungu iangaze giza, na magamba yatadondoka kutoka kwenye macho yao, na watatambua umaskini wao wa kweli wa kiroho na unyonge. Watahisi umuhimu wa kununua dhahabu, ambayo ni imani safi na upendo; mavazi meupe, ambayo ni tabia isiyo na doa iliyosafishwa katika damu ya Mkombozi wao mpendwa; na dawa ya macho, ambayo ni neema ya Mungu, ambayo itatoa utambuzi wazi wa mambo ya kiroho na kugundua dhambi. Mafanikio haya ni ya thamani zaidi kuliko dhahabu ya Ofiri. {3T 254.2}

Nimeoneshwa kuwa sababu kubwa kwa nini watu wa Mungu sasa wanapatikana katika hali hii ya upofu wa kiroho ni kwamba hawataki kupokea masahihisho. Wengi wamedharau makemeo na maonyo waliyopewa. Shahidi Mwaminifu analaani hali ya uvuguvugu ya watu wa Mungu, ambayo humpa Shetani nguvu kubwa juu yao katika wakati huu wa kungoja, na kukesha. Wabinafsi, wenye kiburi, na wapendao dhambi daima wanashambuliwa na mashaka. Shetani ana uwezo wa kupendekeza mashaka na kupanga pingamizi kwa Shuhuda ulio wazi ambao Mungu huutuma, na wengi hudhani ni wema na dalili ya akili kwao, wanapoonesha kutoamini na kuhoji na kubisha. Wale wanaotamani kutilia shaka watapata nafasi nyingi. Mungu hakusudii kuondoa mazingira yote yanayoweza kuleta hali ya kutoamini. Yeye Hutoa ushahidi, ambao ni lazima uchunguzwe kwa uangalifu na akili nyenyekevu na roho inayofundishika, na wote wanapaswa kuamua kutokana na uzito wa ushahidi. {3T 255.1}

Uzima wa milele ni wa thamani isiyo na kikomo na itatugharimu yote tuliyonayo. Nilioneshwa kuwa hatuwekei makisio sahihi juu ya mambo ya milele. Kila kitu kinachostahili kumilikiwa, hata katika ulimwengu huu, lazima kipatikane na kutunzwa kwa juhudi, na wakati mwingine kwa kafara yenye uchungu zaidi. Na hii inafanyika ili kupata hazina inayoharibika tu. Je! Hatutakuwa tayari kuvumilia mizozo na taabu, na kufanya bidii na kujitolea sana, ili kupata hazina ambayo ina thamani isiyo na kikomo, na maisha yenye kipimo sawa na kile cha umilele? Je! mbingu itatugharimu mno? {3T 255.2}

Imani na upendo ni hazina za dhahabu, vitu ambavyo vinakosekana sana miongoni mwa watu wa Mungu. Nimeoneshwa kuwa kutokuwa na imani na shuhuda zenye maonyo, zenye kutia moyo, na kukemea kunazima nuru kutoka kwa watu wa Mungu. Kutoamini kunawafunga macho ili wasitambue hali yao halisi. Shahidi Mwaminifu anaelezea upofu wao hivi: "Nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi." 3T 255.3}

Imani katika Kristo ajaye upesi hivi karibuni inafifia. “Bwana wangu anakawia” haisemwi tu kimoyo-moyo, bali inaoneshwa kwa maneno na kwa kukusudiwa hasa kwenye vitendo. Upumbavu katika wakati huu wa kukesha unaziba hisia za watu wa Mungu kuhusu ishara za nyakati. Uovu wa kutisha unaoongezeka unaalika kazi kubwa na ushuhuda ulio hai, ili kuibana dhambi ibaki huko-huko, nje ya kanisa. Imani imekuwa ikipungua kwa kiwango cha kutisha, na ni kwa njia tu ya kuifanyia mazoezi ambapo inaweza kuongezeka. {3T 255.4}

Katika kuinuka kwa ujumbe wa malaika watatu, wale walioshiriki katika kazi ya Mungu walipaswa wajitose; kulikuwa na kafara ya kutoa. Walianza kazi hii kimaskini, taabu na kupata mateso makubwa na kukabiliwa na ufukara mkubwa na aibu. Walikabiliana na upinzani uliodhamiria, uliowasukuma kwa Mungu kwa ajili ya mahitaji yao na hivyo kusababisha Imani yao kuwa hai. Mpango wetu wa sasa wa utoaji wa ukarimu kwa mpango unawategemeza wachungaji [systematic benevolence], na hakuna uhitaji na hakuna wito wa zoezi la kuimarishwa kiimani. Wale wanaoanza sasa kuhubiri Ukweli hawana chochote cha kupoteza. Hawana hatari ya kukimbia, hawana kafara maalum ya kutoa au cha kujitosha. Mfumo wa Ukweli umewekwa tayari mikononi mwao, na machapisho hutolewa kwao, yakithibitisha Ukweli wanaouendeleza. {3T 256.1}

Baadhi ya vijana huanza tu wakiwa hawana hisia halisi ya tabia iliyoinuliwa ya kazi ya Mungu. Hawana ufukara, hawana magumu, au mizozo mikubwa ya kukutana nayo, ambayo ingehitaji matumizi ya imani. Hawakuzi hali halisi ya kujikana nafsi-kujinyima kwa vitendo na kuthamini roho ya kujitolea. Wengine wanajivuna na kuinuliwa, na hawana mzigo wowote wa kazi juu yao. Shahidi Mwaminifu anazungumza na wachungaji hawa akisema: “Uwe na bidii, ukatubu.” Baadhi yao wameinuliwa sana kwa majivuno kiasi kwamba wamekuwa kikwazo na laana kwa kazi ya thamani ya Mungu. Watu hawa hawashinikizi ushawishi unaookoa kwa wengine. Watu hawa wanahitaji kuongolewa kikamilifu kwa Mungu mwenyewe na kutakaswa na Ukweli wanaowasilisha kwa wengine. {3T 256.2}

Ushuhuda Unaolikemea Kanisa

Wengi sana huhisi kutotulia na wivu kwa sababu mara nyingi husumbuliwa na maonyo na makemeo ambayo huweka dhambi zao mbele yao. Shahidi Mwaminifu anasema: “Nayajua matendo yako.” Nia ya moyo, makusudi, lengo, kutokuamini, tuhuma na wivu vinaweza kufichika machoni pa wanadamu, lakini siyo kwa Kristo. Shahidi Mwaminifu anakuja kama mshauri: “Ninakupa ushauri wewe, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu,

na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami. Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi." {3T 256.3}

Wale wanaoshutumiwa, na kukemewa na Roho wa Mungu hawapaswi kuinuka dhidi ya chombo kinyenyekevu. Ni Mungu, na siyo mwanadamu mwenye makosa, aliyesema nao ili kuwaokoa kutoka kwenye uharibifu. Wale wanaodharau onyo wataachwa katika upofu ili wajidanganye wenyewe. Ila wale wanaoendelea kushughulika na kujitenga na dhambi zao, ili wawe na neema zinazohitajika, watakuwa wakifungua milango ya mioyo yao ili Mwokozi mpendwa aingie na kukaa nao. Watu wa daraja hili daima utawakuta wakiwa katika maelewano kamili na ushuhuda wa Roho wa Mungu. {3T 257.1}

Wachungaji wanaohubiri Ukweli wa leo hawapaswi kupuuza ujumbe mzito kwa Walaodikia. Ushuhuda wa Shahidi Mwaminifu siyo ujumbe laini. Bwana hawaambii, Wewe ni mwenye haki; umepokea adhabu na maonyo ambayo hukustahili kamwe; umekatishwa tamaa bila sababu yoyote kwa njia ya ukali; basi wewe huna hatia ya makosa na dhambi unazokemewa. {3T 257.2}

Shahidi Mwaminifu anatangaza kwamba unapodhani upo kwenye hali nzuri ya ustawi unakuwa upo kwenye uhitaji wa kila kitu. Haitoshi kwa wachungaji kuwasilisha masomo ya nadharia; wanapaswa pia kuwasilisha masomo yale ambayo ni ya vitendo. Wanahitaji kusoma masomo ya vitendo ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake na kuyatumia kwa karibu sana kwa ajili ya roho zao na kwa ajili ya watu. Kwa kuwa Kristo anatoa ushuhuda huu wa kukemea, je! hiyo inamaanisha kuwa ana upungufu wa upole kwa watu Wake? La, hapana! Yeye aliyekufa kumkomboa mwanadamu kutoka mautini, anapenda kwa upendo wa Mungu, na wale anaowapenda anawakemea. "Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi." Lakini wengi hawataupokea ujumbe ambao Mbingu kwa rehema inawatumia. Hawawezi kuvumilia kuambiwa juu ya kupuuza kwao wajibu na makosa yao, ubinafsi wao, kiburi chao na kupenda kwao ulimwengu. {3T 257.3}

Nilioneshwa kwamba Mungu ameweka kwa mume wangu na kwangu kazi maalum, ili kutoa ushuhuda ulio wazi kwa watu Wake, na kupiga kelele kwa sauti kubwa, bila kuachilia, kuwaonesha watu makosa yao na nyumba ya Israeli dhambi zao. Lakini kuna daraja la watu ambalo halitapokea ujumbe wa karipio, nao watainua mikono yao kuwakinga wale ambao Mungu angependa kuwakemea na kuwasahihisha. Hawa hupatikana hata wakiwahurumia wale ambao Mungu angewafanya wahisi umaskini wao wa kweli. {3T 258.1}

Neno la Bwana, lililonenwa kupitia watumishi Wake, linapokelewa na wengi kwa maswali na hofu. Na wengi watasitisha utii wao kwa onyo na karipio zinazotolewa, wakingojea mpaka kila kivuli cha kutokuwa na uhakika kitakapoondolewa akilini mwao. Kutokuamini kunakodai maarifa kamili hakutapokea kamwe ushahidi ambao Mungu Yuko radhi kuutoa. Yeye Anahitaji kutoka kwa watu Wake imani ambayo inategemea uzito wa ushahidi, siyo juu ya maarifa kamili. Wafuasi hao wa Kristo wanaokubali nuru ambayo Mungu hutuma lazima watii sauti ya Mungu anapoongea nao wakati kunapokuwepo sauti zingine nyingi zinazopiga kelele dhidi ya sauti hiyo. Panahitajika utambuzi ili kutofautisha sauti ya Mungu. {3T 258.2}

Wale ambao hawatachukua hatua wakati Bwana anapowaita, lakini ambao wanasubiri ushahidi dhahiri zaidi na fursa nzuri zaidi, watatembea gizani, kwani nuru itaondolewa. Ushahidi uliotolewa siku moja, ikiwa utakataliwa, hautaweza kurudiwa kamwe. {3T 258.3}

Wengi wanajaribiwa kuhusu kazi yetu na wanaihoji kwa maswali. Wengine, katika hali zao za majaribu, malipo mashaka na mashaka ya watu wa Mungu kwa ushuhuda wa kukemea kwamba tumewapa. Wanafikiria shida ni kwa wale wanaobeba ujumbe wa onyo, wanaozisonda dhambi za watu na kusahihisha makosa yao. Wengi hudanganywa na adui wa roho. Wanafikiri kwamba kazi za Ndugu na Dada White zingekubalika kama hawangekuwa wakiendelea kulaani makosa na kukemea dhambi. Nilioneshwa kuwa Mungu ameiweka kazi hii juu yetu, na wakati tunapozuiliwa kukutana na watu Wake na kutoa ushuhuda wetu na kukinzana na maono na wivu wa wale ambao hawajawekwa wakfu, ndipo Shetani hushinikiza majaribu yake kwa nguvu sana. Wale ambao daima wamekuwa kwenye upande wa wanaohoji, upande wa mashaka wanajisikia huru kushauri mashaka yao kupenyeza kutokuamini kwao. Wengine wanajifanya watakatifu na wanaonekana kuwa waangalifu na wacha Mungu wenye mashaka sana, ambao huachilia kwa tahadhari, lakini ambao wana nguvu zaidi ya mara kumi ya kuimarisha wale walio na makosa, na kupunguza ushawishi wetu na kudhoofisha imani ya watu wa Mungu katika kazi yetu, kuliko kama wangefanya hivyo kwa uwazi zaidi. Nafsi hizi masikini, niliona, zilidanganywa na Shetani. Wanajifariji kwa kujidanganya kwamba wako sawa, kwamba wanamuunga mkono Mungu na ni matajiri katika utambuzi wa kiroho, wakati ni masikini, vipofu na wanyonge. Wanafanya kazi ya Shetani, lakini wanafikiria wana bidii kwa Mungu. {3T 258.4}

Wengine hawatapokea ushuhuda ambao Mungu ametupatia ili kuupeleka, wakijifariji wenyewe kuwa tunaweza kudanganyika, na wao wanaweza kuwa sahihi. Wanadhani ya kwamba watu wa Mungu hawahitaji kushughulikiwa na kukemewa waziwazi, kwani Mungu Yuko pamoja nao. Hawa wanaojaribiwa, ambao roho zao zimekuwa katika vita na kukemewa kwa dhambi kuliko kwa uaminifu, hulia: Nena nasi mambo laini-laini. Ni tabia gani zitaundwa na ujumbe huu wa

Shahidi Mwaminifu kwa Walaodikia? Hakuwezi kuwa na udanganyifu hapa. Ujumbe huu ni lazima upelekwe kwa kanisa lenye uvuguvugu na watumishi wa Mungu. Ni lazima uamshe watu Wake kutoka kwenye hali yao ya kujidhania wapo katika usalama na udanganyifu wao wa hatari kuhusiana na msimamo wao halisi mbele za Mungu. Ushuhuda huu, kama utapokelewa, utawaamsha kuchukua hatua na kusababisha kujidhili na kuungama dhambi. Shahidi Mwaminifu anasema: “Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto.” Na tena, “Wote niwapendao Mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.” Ndipo huja ahadi: “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami.” “Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti Changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi.” {3T 259.1}

Watu wa Mungu lazima waone makosa yao na waamke na kufanya toba ya bidii na kuweka mbali dhambi hizo ambazo zimewaleta katika hali mbaya ya umaskini, upofu, unyonge, na udanganyifu wa kutisha. Nilionyeshwa kuwa ushuhuda ulio wazi lazima uishi kanisani. Hili pekee ndilo litajibu ujumbe kwa Walaodikia. Makosa yanapaswa kukemewa, lazima dhambi iitwe dhambi, na uovu lazima ushughulikiwe kisawasawa na kwa udhati, na uweke mbali nasi kama watu. {3T 260.1}

Kupambana na Roho wa Mungu

Wale wenye roho ya upinzani kwa kazi ambayo kwa miaka ishirini na sita tumekuwa tukisukumwa na Roho wa Mungu kuifanya, na ambao wangevunjilia mbali ushuhuda wetu, niliona hawapambani dhidi yetu bali dhidi ya Mungu, aliyeweka juu yetu mzigo wa kazi ambao Yeye hajawapa watu wengine. Wale wanaohoji na kupinga na kubishana, na kudhani ni fahari kutilia shaka, na ambao wamekuwa ni wenye kukatisha tamaa, wale ambao wamekuwa sababu ya kuifanya kazi yetu kuwa ngumu wakidhoofisha imani yetu, matumaini yetu, na ujasiri wetu, wamekuwa ni hao hao wenye kuleta dhana kuwa kuna uovu, na kuingiza kwa hila mashtaka yenye kushuku, kijicho na kutafuta kwa wivu fursa ya kuwa kinyume chetu. Wanachukulia kirahisi kwamba kwa vile tuna udhaifu wa kibinadamu basi ni ushahidi mzuri kwamba sisi tuna uwezekano wa kufanya makosa na kwamba wao wapo sahihi. Ikiwa wanaweza kupata mfano wa kitu chochote wanachoweza kutumia kutuumiza wanafanya hivyo kwa roho ya ushindi na wapo tayari kuilaani kazi yetu ya kukemea mabaya, na kuiona [kazi yetu ya] kukemea dhambi kama iliyofanywa kwa roho ya ukali, na ya kidikteta. {3T 260.2}

Lakini wakati tukiwa hatuikubali njozi yao kuhusu kazi yetu kama sababu ya shida zetu, wakati tukishikilia kuwa Mungu ametuteua kwa kazi yenye majaribu kuliko za wengine, tunakiri kwa moyo wa unyenyekevu na kwa toba kuwa imani yetu na ujasiri wetu vimejaribiwa kwa ukali sana, na kwamba nyakati fulani tumeshindwa

kutumainia kikamilifu kwa Yeye aliyetuteua kwa kazi Yake. Lini unakusanya ujasiri tena, baada ya kukatishwa tamaa na majaribu, tunajuta sana kwamba hatujawahi kuamini Mungu, alitoa njia ya udhaifu wa kibinadamu, na kuruhusu kuvunjika moyo kufifisha imani yetu na kupunguza yetu imani kwa Mungu. Nimeoneshwa kuwa watumishi wa Mungu wa kale walipata kukatishwa tamaa na kuvunjika moyo na vile vile sisi maskini binadamu. Tulikuwa katika ushirika/kundi zuri; hata hivyo hii haikufanya hivyo ili kupata udhuru. {3T 260.3}

Kwa kuwa mume wangu amekuwa akisimama kando yangu kunitegemeza katika kazi yangu na ametoa ushuhuda ulio wazi unaolingana na kazi ya Roho wa Mungu, wengi wamehisi kuwa ni yeye mwenyewe aliyekuwa akiwaumiza wao, wakati ni Bwana aliyemwekea mzigo na ambaye, kupitia mtumishi Wake alikuwa, akiwakemea wao na kutafuta kuwaleta mahali ambapo wangetubu makosa yao na kupata kibali cha Mungu. {3T 261.1}

Wale ambao Mungu amewachagua kwa kazi muhimu daima wamekuwa wakipokelewa bila imani na kwa kutiliwa mashaka. Zamani, wakati Eliya alipotumwa na ujumbe uliotoka kwa Mungu ukiwaendea watu, watu wale hawakutii onyo. Walimdhania kuwa ni mkali kupita kiasi. Hata walimdhania kuwa amepotelewa akili yake kwa kuwa aliwashutumu, watu wa Mungu waliopendelewa, kama wenye dhambi, na uhalifu wao kama ulio mbaya sana kiasi kuwa hukumu ya Mungu itaamka dhidi yao. Shetani na majeshi yake wamekuwa daima wakijipanga dhidi ya wale wanaobeba ujumbe wa onyo na wanaokemea dhambi. Utashi usiotakaswa utaungana pia na adui wa roho kuifanya kazi ya watumishi waaminifu wa Mungu iwe ngumu kadri iwezekanavyo. {3T 261.2}

Ikiwa mume wangu ameshinikizwa kupita kiasi na amevunjika moyo na kukata tamaa, ikiwa sisi wakati mwingine hatujaona chochote cha kuvutia maishani ambacho tunapaswa kukichagua, hiki siyo kitu cha kushangaza au kipya. Eliya, mmoja wa manabii wakubwa na hodari wa Mungu, alipokimbia kuokoa maisha yake kutokana na ghadhabu ya Yezebeli mwenye hasira kali, mkimbizi, akiwa amechoka na amechakaa kwa safari, alitamani kufa kuliko kuishi. Kukata tamaa kwake kwa uchungu juu ya uaminifu wa Israeli kulikuwa kumeuvunja moyo awke, na yeye alihisi kuwa hangeweza tena kumtumaini mwanadamu. Katika siku ya mateso na giza la Ayubu, anatamka maneno haya: “Na ipotelee mbali ile siku niliyozaliwa mimi. {3T 261.3}

Wale ambao hawajazoea kupata hisia za kina, ambao hawajasimama chini ya mzigo kama gari ya kukokotwa chini ya miganda, na ambao masilahi yao hayajawahi kufungamanishwa kwa karibu na kazi ya Mungu hata ionekane kama sehemu ya miili yao na iliyo bora kwao kuliko uhai, hawawezi kuthamini hisia za

mume wangu kama vile Israeli walivyoshindwa kuthamini hisia za Eliya. Sisi tunajutia sana hali ya kuvunjika moyo, kwa hali yoyote ile. {3T 262.1}

Suala la Ahabu ni Onyo

Chini ya utawala uliopotoka wa Ahabu, Israeli walimwacha Mungu na kuharibu njia zao mbele Zake. “Ahabu mwana wa Omri akafanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana kuliko wote waliomtangulia. Ikawa, kama ingalikuwa neno dogo tu kuyaendea makosa ya Yeroboamu mwana wa Nebati, akamwoa Yezebeli binti Ethbaali, mfalme wa Wasidoni, akaenda akamtumikia Baali, akamsujudia. Akamjengea Baali madhabahu katika nyumba ya Baali, aliyoijenga huko Samaria. Ahabu akaifanya Ashera; Ahabu akazidi kumghadhibisha Bwana, Mungu wa Israeli, kuliko wafalme wote wa Israeli waliomtangulia” 3T 262.2}

Ahabu alikuwa dhaifu katika nguvu za maadili. Hakuwa hakuwa akili yenye kujali mambo matakatifu; alikuwa mbinafsi na mtu asiye na kanuni/msimamo. Muungano wake na ndoa na mwanamke aliye na tabia iliyoamuliwa na haiba, iliyokuwa imejitolea kabisa kwa ibada ya sanamu, na hii ikawafanya wote wawili kuwa mawakala wa kipekee wa Shetani, na kuwaongoza watu wa Mungu katika ibada ya sanamu na uasi mbaya. Roho iliyodhamiriwa na Yezebeli iliunda tabia ya Ahabu. Asili yake ya mfalme ya ubinafsi haikuwa na uwezo wa kuthamini rehema za Mungu kwa watu Wake na wajibu Wake kwa Mungu kama mlezi na kiongozi wa Israeli. Hofu ya Mungu ilikuwa ikinywea kila siku katika Israeli. Ishara za ibada zenye upofu za sanamu na kufuru zilikuwa zinaonekana kati ya Israeli wa Mungu. Hakukuwa na mtu aliyethubutu kufunua maisha yao kwa kusimama waziwazi kinyume na ibada ya sanamu yenye makufuru iliyoshamiri. Madhabahu za Baali, na makuhani wa Baali ambao walitoa dhabihu kwa jua, mwezi, na nyota, zilikuwa zimejaa/maarufu kila mahali. Walikuwa wameweka wakfu mahekalu na mashamba ambayo kazi ya mikono ya wanaume iliwekwa kwa kuabudiwa [sanamu]. Faida ambazo Mungu aliwapa watu hawa hazikuleta moyo wa shukrani kwenda Kwake Yeye, Aliye Mtoaji. Neema na zawadi tele zote za mbinguni, mito, vijito vya maji yaliyo hai, umande laini, manyunyu ya mvua ambayo yaliburudisha ardhi na kusababisha mashamba yao kuzaa kwa wingi, vyote hivyo walisema vilitokana na neema ya miungu yao, walitoa sifa kwa miungu-[feva ya Mungu wao]. {3T 262.3}

Nafsi aminifu ya Eliya ilihuzunishwa. Hasira yake iliamka, naye alikuwa na wivu kwa utukufu wa Mungu. Aliona kwamba Israeli ilikuwa imetumbukia katika uasi wa kutisha. Na alipokumbuka mambo makubwa Mungu aliyokuwa amewafanyia, alielemewa na huzuni na mshangao. Lakini yote haya yalikuwa wamesahaulika na watu wengi. Alikwenda mbele za Bwana, na huku roho yake ikikamuliwa na uchungu, akimsihi awaokoe watu wake kama inawezekana kupitia hukumu hiyo. Alimsihi Mungu awazuilie watu Wake wasio na shukrani umande na mvua, hazina

za mbinguni, ili kusudi Israeli yenye uasi iweze kuiomba miungu yao, sanamu zao za dhahabu, mbao, na mawe, jua, mwezi, na nyota, kwamba imwagilie maji na kuitajirisha nchi, na kuzalisha kwa wingi mazao, na hatimaye ione kwamba, hakika hakuna mafanikio kwa miungu hiyo. Bwana alimwambia Eliya kuwa amesikia maombi yake na atazuia umande na mvua visiwafikie watu wake mpaka watakapomrudia Yeye kwa toba. {3T 263.1}

Dhambi ya Akani na Adhabu Yake

Mungu kwa umakini alikuwa amewalinda watu Wake dhidi ya kujichanganya na watu wa mataifa ya waabudu sanamu waliowazunguka, isije mioyo yao ikadanganywa na mashamba ya miti, madhabahu na mahekalu ya kuvutia, yaliyokuwa yamepangwa kwa namna ya gharama kubwa ya kuishawishi na kuipotosha hisia/akili ili Mungu awekwe chini katika mawazo ya watu namiungu hii iwe mbadala wa Mungu wa mbinguni. {3T 263.2}

Jiji la Yeriko lilikuwa limejiachia kwa ibada ya sanamu ya kupindukia mno. Wakazi walikuwa matajiri sana, lakini utajiri wote ambao Mungu alikuwa amewapatia waliuhesabu kama zawadi kutoka kwa miungu yao. Walikuwa na dhahabu na fedha kwa wingi; lakini, kama watu walioishi kabla ya Gharika [antedeluvians], walikuwa waovu na wenye kukufuru, na walimtukana na kumkasirisha Mungu wa mbinguni kwa matendo yao maovu. Hukumu za Mungu ziliamshwa dhidi ya Yeriko. Ilikuwa ngome. Lakini Kapteni/Generali wa jeshi la Bwana Mwenyewe alikuja kutoka mbinguni kuongoza majeshi ya mbinguni katika shambulio juu ya mji. Malaika wa Mungu walishika kuta kubwa na kuziangusha chini. Mungu alikuwa amesema kwamba mji wa Yeriko unapaswa kulaaniwa na kwamba wote wanapaswa kuangamia isipokuwa Rahabu na watu wa nyumbani mwake. Familia ya Rahabu walipaswa kuokolewa kwa sababu ya neema ambayo Rahabu aliwaonesha wajumbe wa Bwana. Neno la Bwana kwa watu lilikuwa: “Na ninyi, msikose kujiepusha na kitu kilichowekwa wakfu; msije mkakitwaa kitu kilichowekwa wakfu, baada ya kukiweka wakfu; nanyi hivyo mtayafanya matuo ya Israeli kuwa yamelaaniwa na kuyafadhaisha.” Naye Yoshua akawaapisha kiapo wakati ule, akasema, Na alaaniwe mbele za Bwana mtu yule atakayeinuka na kuujenga tena mji huu wa Yeriko; ataweka msingi wake kwa kufiliwa na mzaliwa wa kwanza wake, tena atayasimamisha malango yake kwa kufiliwa na mtoto wake mwanamume aliye mdogo.” 3T 264.1}

Mungu alikuwa makini sana kuhusu Yeriko, ili watu wasije watu wakalogwa na kupendezwa kwa vitu ambavyo wenyeji walikuwa wameviabudu na mioyo yao ikageuzwa kutoka kwa Mungu. Aliwalinda watu Wake kwa amri zilizokuwa nzuri

sana; lakini pamoja na maagizo ya Mungu kwa kinywa cha Yoshua, Akani alijitosa kukiuka. Tamaa yake ilimpelekea kuchukua hazina ambazo Mungu alikuwa amekataza wasiziguse kwa sababu laana ya Mungu ilikuwa juu yao. Na kwa sababu ya dhambi ya mtu huyu, Israeli wa Mungu walikuwa dhaifu kama maji mbele ya adui zao. {3T 264.2}

Yoshua na wazee wa Israeli walikuwa katika dhiki kubwa. Walilala mbele ya Sanduku la Agano la Mungu katika hali ya unyenyekevu mkuu uliopoteza matumaini, kwa sababu Bwana alikuwa na hasira na watu Wake. Waliomba na kulia machozi mbele za Mungu. Mungu Bwana akamwambia Yoshua, “Haya! Inuka, mbona umeanguka kifudifudi hivi? Israeli wamefanya dhambi, naam, wamelivunja Agano Langu nililowaagiza; naam, wametwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu; tena wameiba, tena wameficha na kuvitia pamoja na vitu vyao wenyewe. Ndiposa wana wa Israeli hawawezi kusimama mbele ya adui zao; wakawapa visogo adui zao, kwa sababu wamelaaniwa; Mimi sitakuwa pamoja nanyi tena, msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu.” {3T 264.3}

Jukumu la Kukemea Dhambi

Nimeoneshwa kuwa Mungu hapa anaelekeza kwa vitendo jinsi anavyoichukulia dhambi miongoni mwa wale wanaodai kuwa watu Wake washikao amri. Wale aliowaheshimu kwa namna maalum sana wakishuhudia maonesho ya nguvu Zake, kama aliyofanya kwa Israeli ya kale, na ambao hujihatarisha kwa kutotambua mwelekeo Wake alioutamka wazi, watakuwa wahanga wa ghadhabu Yake. Atawafundisha watu Wake kwamba kutotii na dhambi ni jambo linalomchukiza mno na ambalo halipaswi kupuuzwa au kuchukuliwa kiholela. Yeye Anatuonesha kuwa wakati watu Wake wanapopatikana katika dhambi mara moja wanapaswa kuchukua hatua zilizodhamiriwa ili kuiweka mbali nao dhambi hiyo, na ili uso wa hasira Yake isiwe juu yao wote. Lakini ikiwa dhambi za watu zinapitwa bila kushughulikiwa na wale walio katika nafasi za uwajibikaji, mkunjo wa sura Yake utakuwa juu yao, na watu wa Mungu, kama kanisa, watawajibika kwa dhambi hizo. Katika kushughulika Kwake na watu Wake katika siku za nyuma Bwana ameonesha umuhimu wa kulitakasa kanisa kutoka kwenye makosa. Mtenda dhambi mmoja aweza kueneza giza ambalo litaondoa nuru ya Mungu kutoka kwa mkutano wote. Wakati watu wanapogundua kuwa giza linatanda juu yao, na hawajui sababu, watamtafuta Mungu kwa bidii, kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kujidhili, mpaka makosa ambayo humhuzunisha Roho Wake yafutwe na kuwekwa kando. {3T 265.1}

Ubaguzi na chuki isiyo na sababu iliyoelekezwa kwetu kwa kuwa tumekemea mabaya ambayo Mungu alikuwa amenionesha kuwa yalikuwepo, na kilio ambacho kiliinuka kijeuri, ukali na kikatili havikuwa halali. Mungu anatuhimiza tunene, nasi hatutanyamaza. Ikiwa makosa yapo dhahiri miongoni mwa watu wake, na ikiwa

watumishi wa Mungu wanayapita bila kujali, watakuwa kama wanamtegemeza na kumhalalisha mwenye dhambi, na kwa hali hiyo nao wana hatia sawa na huyo mdhambi na kwa hakika watapokea hasira ya Mungu; kwa kuwa watawajibika kwa dhambi za wenye hatia. Nikiwa kwenye maono nilielekezwa kwenye matukio mengi ambapo ghadhabu ya Mungu ilipatikana kutokana na upuuziaji kwa upande wa watumishi Wake katika kushughulikia makosa na dhambi vilivyopo katikati yao. Wale waliohalalisha au kutoa udhuru kwaajili ya makosa haya wamefikiriwa na watu kuwa wanadamu wazuri sana na wa kupendeza kwa tabia, kwa sababu tu waliepuka kuchukua hatua kwa mujibu wa Maandiko. Kazi haikukubaliana au kupendeza katika hisia zao; kwa hivyo waliiepuka. {3T 265.2}

Roho ya chuki iliyokuwepo na baadhi kutokana na makosa yaliyokemewa yaliyo miongoni mwa watu wa Mungu yameleta upofu na udanganyifu wa kutisha juu ya nafsi zao, na kufanya isiwezekane kwao kutofautisha kati ya mema na mabaya. Wamejipaka dawa ya macho ya kiroho ya kwao wenyewe. Wanaweza kushuhudia makosa, lakini hawajisikii kama Yoshua alivyojisikia na kujinyenyekeza wenyewe kwa kuwa hatari ya roho zimehisiwa nao. {3T 266.1}

Watu wa kweli wa Mungu, walio na roho ya kazi ya Bwana na wokovu wa roho mioyoni mwao, daima wataiona dhambi katika tabia yake halisi. Daima watakuwa upande wa waaminifu na watashughulikia kwa uwazi dhambi ambazo zimekuwa zikiwakumba/zikiwazinga watu wa Mungu kwa urahisi. Hasa katika kufungwa kwa kazi ya kanisa, katika wakati wa kutiwa muhuri kwa wale mia na arobaini na nne elfu ambao watasimama bila kosa mbele za kiti cha enzi cha Mungu, watahisi kwa undani zaidi makosa ya watu wanaodai kuwa wa Mungu. Jambo hili limeelezwa kwa msisitizo kwa mfano aliouonesha nabii wa kazi ya mwisho chini ya kivuli cha watu ambao kila mmojawapo alikuwa na silaha ya kufisha/kuua mkononi mwake. Mtu mmoja kati yao alikuwa amevaa bafta, naye ana kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. “Bwana akamwambia, Pita kati ya mji, kati ya Yerusalemu, ukatie alama katika vipaji vya nyuso vya watu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yote yanayofanyika kati yake.” {3T 266.2}

Je, ni nani wasimamao katika shauri la Mungu wakati huu? Je! Ni wale wakaribiao kutoa udhuru kati ya watu wanaojidai ni wa Mungu na ambao hunung'unika mioyoni mwao, wala siyo kwa wazi, dhidi ya wale ambao wangetaka kukemea dhambi? Je! Ni wale wanaochukua msimamo wao dhidi yao na kuwahurumia watendao dhambi/makosa? Hapana, kwa kweli! Kama wasipotubu, na kuacha kazi ya Shetani katika kuwakandamiza wale ambao wana mzigo wa kazi na kwa kuinua mikono ya wenye dhambi katika Sayuni, hawatapokea muhuri wa Mungu wa ukubali. Wataanguka katika uharibifu wa jumla wa waovu, uliowakilishwa na kazi ya wanaume watano waliobeba silaha za kuchinja watu. Chunga jambo hili kwa uangalifu: Wale wanaopokea alama safi ya Ukweli, iliyotengenezwa ndani yao kwa

nguvu ya Roho Mtakatifu, iliyowakilishwa na alama ya mtu aliyevaa bafta, ni wale "wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yote yanayotendeka." kanisani. Upendo wao kwa Usafi na heshima na utukufu wa Mungu ni za kiwango hicho, na wana mtazamo ulio wazi juu ya hali ya dhambi iliyokithiri, kiasi kwamba wanawakilishwa kama watu wenye uchungu na maumivu makali, na walio katika hali ya kuugua na kulia. Soma sura ya tisa ya Ezekieli. {3T 267.1}

Lakini mauaji ya jumla ya wale wote ambao hawaoni tofauti kubwa iliyopo kati ya dhambi na haki, na hawahisi kama wahisivyo wale wanaosimama katika shauri la Mungu na kupokea alama, imeelezwa kwa njia ya utaratibu kwa watu watano wenye silaha za kuchinja watu. “Piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachilie, wala msione huruma; Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu yeyote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika Patakatifu Pangu.” {3T 267.2}

Katika kisa cha dhambi ya Akani Mungu alimwambia Yoshua: “Mimi sitakuwa pamoja nanyi tena, msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu.” Mfano huu unalinganishwaje na mwendo unaofuatwa na wale ambao hawatapaza sauti zao dhidi ya dhambi na uovu, lakini ambao huruma zao daima hupatikana kwa wale wanaosumbua kambi ya Israeli kwa dhambi zao? Mungu alimwambia Yoshua: wewe “Huwezi kusimama mbele ya adui zako, hata mtakapokiondoa kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu.” Alitangaza adhabu ambayo ingefuata uvunjaji wa Agano Lake. {3T 267.3}

Kisha Joshua akaanza msako wa bidii ili kujua aliye na hatia. Aliwachukua Waisraeli kwa makabila yao, kisha kwa familia zao, na baadaye kwa mtu mmoja mmoja; na Akani akatwaliwa kama yule mwenye hatia. Lakini ili jambo hilo liweze kuwa wazi kwa Waisraeli wote, na ili kwamba pasiwepo nafasi ya kunung'unika na kusema kwamba asiye na hatia ameumizwa Yoshua alitumia sera. Alijua Akani alikuwa ni mkosaji na kwamba alikuwa ameficha dhambi yake na kumkasirisha Mungu dhidi ya watu Wake. Kwa busara Yoshua alimshawishi Akani kufanya toba ya dhambi yake, ili heshima na haki ya Mungu ithibitishwe mbele ya Waisraeli. “Yoshua akamwambia Akani, mwanangu, nakusihi, umtukuze Bwana, Mungu wa Israeli, ukaungame Kwake; uniambie sasa ulilolitenda; usinifiche.” {3T 268.1}

“Akani akamjibu Yoshua, akasema, kweli nimefanya dhambi juu ya Bwana, Mungu wa Israeli, nami nimefanya mambo haya -na haya. Nilipoona katika nyara joho nzuri ya Babeli, na shekeli mia mbili za fedha, na kabari ya, uzani wake shekeli hamsini, basi nalivitamani nikavitwaa; tazama, vimefichwa mchangani katikati ya hema yangu, na ile fedha chini yake. Basi Yoshua akatuma wajumbe wakapiga mbio mpaka hemani; na tazama, vile vitu vilikuwa vimefichwa hemani mwake, na ile fedha chini yake. Wakavitoa kutoka hapo katikati ya hema, wakavileta kwa

Yoshua, na kwa wana wa Israeli wote, nao wakaviweka chini mbele za Bwana. Kisha Yoshua, na Israeli wote pamoja naye, wakamtwaa Akani, mwana wa Zera, na ile fedha, na Lile joho, na ile kabari ya dhahabu, na wanawe, na binti zake, na ng'ombe zake, na punda zake, na kondoo zake, na hema yake, na vitu vyote alivyokuwa navyo, wakavileta juu hata bonde la Akori. Yoshua akasema, Mbona umetufadhaisha hivi? Bwana atakufadhaisha wewe leo. Ndipo Israeli wote wakampiga kwa mawe, kisha wakawateketeza kwa moto, na kuwapiga kwa mawe." {3T 268.2}

Bwana alimwambia Yoshua kwamba Akani hakuwa amechukua tu vitu ambavyo alikuwa amewaamuru kwa msisitizo kuwa wasivichukue, wasije wakalaaniwa, lakini alikuwa ameiba na na kisha amedanganya. Bwana alisema kuwa Yeriko na nyara zake zote vinapaswa kuteketezwa isipokuwa dhahabu na fedha, ambavyo ingetengwa kwa hazina ya Bwana. Ushindi wa kuuteka Yeriko haukupatikana kupitia vita, uzoefu au ujuzi wa watu. Nahodha wa jeshi la Bwana alikuwa ameongoza majeshi ya mbinguni. Vita vilikuwa vya Bwana; Yeye Ndiye aliyepigana vita. Wana wa Israeli hawakupiga pigo lolote. Ushindi na utukufu vilikuwa vya Bwana, na nyara zilikuwa Zake. Yeye Aliagiza zote ziteketezwe isipokuwa dhahabu na fedha, ambazo alivitenga kando kwa ajili ya hazina Yake. Akani alielewa vizuri akiba iliyotengenezwa na kwamba hazina za dhahabu na fedha alivyovitamani vilikuwa vya Bwana. Aliiba kutoka hazina ya Mungu kwa faida yake mwenyewe. {3T 268.3}

Tamaa Miongoni mwa Watu wa Mungu

Niliona kwamba wengi wa wale wanaodai kuzishika amri za Mungu wanatumia mali kwa matumizi yao wenyewe mali/vitu ambavyo Bwana amewakabidhi na ambazo zinapaswa kuingia katika hazina Yake. Wanamwibia Mungu katika zaka na katika sadaka. Wanazielekeza kwingine na kuzizuia kutoka kwake kwa maumivu yao wenyewe. Wanajiletea hali ya kukonda na umasikini juu yao na giza kwa kanisa kwa sababu ya tamaa yao, wanajifanya, na kujidanganya kwao, na kumwibia Mungu katika zaka na katika matoleo. {3T 269.1}

Niliona kwamba roho nyingi zitazama gizani kwa sababu ya tamaa yao. Ushuhuda wa wazi na ulionyoka, ni lazima uishi kanisani, la sivyo laana ya Mungu itakaa juu ya watu Wake kama vile ilivyokuwa juu ya watu Wake Israeli ya kale kwa sababu ya dhambi zao. Mungu anawawajibisha watu Wake, kama kanisa, kwa dhambi zilizomo kwa mtu mmoja mmoja walio miongoni mwao. Ikiwa viongozi wa kanisa watapuuza kutafuta kwa bidii dhambi zinazoleta hasira kwa Mungu juu ya kanisa, watawajibika kwa dhambi hizo. Lakini kushughulika na akili, ndiyo kazi nzuri kabisa ambayo wanadamu waliwahi kupewa. Wote hawawezi kusahihisha makosa. Hawana hekima ya kutenda kwa haki, wakati huo huo wakipenda rehema. Hawana

mwelekeo wa kuona umuhimu wa kuchanganya upendo na huruma nyororo, kujali, na upendo unaojali pamoja na maonyo ya uaminifu. Wengine huwa wakali bila sababu ya msingi, na hawahisi umuhimu wa agizo la mtume: “Wahurumieni wengine walio na shaka, na wengine waokoeni kwa kuwanyakua katika moto.” {3T 269.2}

Kuna wengi ambao hawana busara ya Yoshua na ambao hawana jukumu maalum la kutafuta makosa na kushughulikia mara moja dhambi zilizopo kati yao. Hebu watu wa namna hiyo wasiwazuie wale walio na mzigo wa kazi hii juu yao; wasisimame katika njia ya wale ambao wana jukumu hili la kufanya. Wengine huifanya hoja ya kuuliza na kutilia shaka na kupata sababu ya kutoa makosa kwamba wengine wanafanya kazi ambayo Mungu hajaweka juu yao. Hawa husimama moja kwa moja katika njia kuwazuia wale ambao Mungu amewawekea mzigo wa kukemea na kusahihisha dhambi zilizoenea ili hasira yake igeuke kutoka kwa watu wake. Kama kesi ya Akani ingekuwa kati yetu, kuna wengi ambao wangewashtaki wale ambao wangechukua jukumu hilo la Joshua kwa kuwasuta kuwa na roho hiyo ya kumtafuta mbaya, kumpata huyo mbaya, na kumwajibisha kwa makosa. Mungu si wa kuchezewa na maonyo Yake hayawezi kupuuzwa bila adhabu na watu wapotovu. {3T 270.1}

Nilioneshwa kuwa njia ya kutubu ya Akani ilikuwa sawa na maungamo ambayo wengine kati yetu tumekuwa tukifanya na tutakuwa tukifanya. Wanaficha makosa yao na hukataa kukiri kwa hiari, hadi Mungu anapowafunua, na ndipo hukiri dhambi zao. Watu wachache huvuka hatua hiyo ya kufanya mabaya hadi kuwa wagumu [wa mioyo]. Wanaweza hata kutambua kwamba kanisa linaelemewa na mzigo, kama Akani alivyojua kwamba Israeli walikuwa dhaifu mbele ya adui zao kwa sababu ya hatia yake. Hata hivyo dhamiri zao haziwahukumu. Hawatalipa unafuu kanisa kwa kuinyenyekeza mioyo yao yenye kiburi na uasi mbele za Mungu na kwa kuweka mbali makosa yao. Hasira ya Mungu iko juu ya watu Wake, na Yeye hatadhihirisha nguvu Zake katikati yao wakati dhambi zikiwamo miongoni mwao na zinalelewa na wale walio katika nafasi za uwajibikaji. {3T 270.2}

Wale wanaofanya kazi kwa hofu ya Mungu ili kuliondoa kanisa kwenye vizuizi na kurekebisha makosa mabaya, ili watu wa Mungu waone umuhimu wa kuchukia dhambi na kufaulu katika usafi/utakaso, na ili Jina la Mungu litukuzwe, watakutana daima na mivuto yenye kupinga kutoka kwa wale wasiojitakasa na kujiweka wakfu. Sefania anaielezea hali ya kweli ya watu wa daraja hili na hukumu za kutisha zitakazokuja juu yao: {3T 270.3}

“Kisha itakuwa wakati ule, nitauchunguza Yerusalemu kwa taa; Nami nitawaadhibu watu walioganda juu ya sira zao; wasemao katika mioyo yao, Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya.” “Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu;

I karibu, nayo inafanya haraka sana; Naam, sauti ya siku ya Bwana; Shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko! Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, Siku ya mawingu na giza kuu, Siku ya tarumbeta na ya kamsa, Juu ya miji yenye maboma, Juu ya buruji zilizo ndefu sana. Nami nitawaletea wanadamu dhiki, hata watakwenda kama vipofu, kwa sababu wamemtenda Bwana dhambi; na damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi. Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya Bwana; bali nchi yote pia itateketezwa kwa moto wa wivu Wake; maana atawakomesha watu wote wakaao katika nchi hii, naam, ukomo wa kutisha." {3T 271.1}

Toba Iliyofanywa kwa Kuchelewa Sana

Wakati matatizo hatimaye yatakapokuja, kama ambavyo kwa uhakika yatatokea, na Mungu akiongea kwa niaba ya watu Wake, wale waliotenda dhambi, wale waliokuwa wingu la giza na waliosimama kinyume na namna Mungu anavyowatendea kazi watu Wake, wanaweza kustushwa kwa urefu walioenda katika kunung'unika na kuleta machafuko kwa kusudi la kazi ya Mungu; na, kama Akani, baada ya kutishwa na kupata hofu, wanaweza kukubali kuwa wamefanya dhambi. Lakini toba yao itakuwa imechelewa sana na siyo ya kiwango kinachofaa kuwanufaisha, ingawa yaweza kuleta unafuu kwa kazi ya Mungu. Watu kama hao hawafanyi toba yao kwa sababu ya kushawishiwa na hali yao ya kweli na kwa uelewa wa namna mwenendo wao ulivyomchukiza Mungu. Mungu aweza kuwapatia watu wa kundi/daraja hili mtihani mwingine, uthibitisho mwingine, ili kuwapa nafasi waoneshe kuwa hawajajiandaa vizuri kusimama huru kutoka kwenye uasi wote na dhambi kuliko kabla ya kukiri kwao. Wamependa kuning'inia upande wa ubaya zaidi. Na wakati wito unapotolewa kwa wale ambao watakuwa upande wa Bwana kuchukua uamuzi uliothibitika kuthibitisha haki, wataonesha msimamo wao wa Kweli. Wale ambao kwa karibu maisha yao yote kudhibitiwa na roho aliye wa kigeni kwa Roho wa Mungu kama ilivyokuwa kwa Akani watakuwa kimya na ni wabaya sana wakati utakapokuja wa kufanya maamuzi kwa kila mtu. Hawatadai kuwa upande wowote. Nguvu za Shetani zimewashikilia kwa muda mrefu hivi kwamba wanaonekana wamepofushwa na hawana mwelekeo wa kusimama na kuitetea haki. Ikiwa hawachukui maamuzi upande ule usiofaa, siyo kwa sababu wana hisia wazi juu ya kipi kilicho sawa, lakini n kwa sababu hawathubutu. {3T 271.2}

Mungu hatachezewa. Ni wakati wa vita/mgogoro ambapo rangi za Kweli zinapaswa kuonekana zikipepea kuelekea kule bendera inakopeperushwa na upepo. Hapo ndipo ambapo ujuzi wa kila mbeba kiwango unatakiwa kuwa thabiti na kuruhusu msimamo wao halisi ujulikane wazi. Ni hapo tu ambapo ujuzi sahihi wa kila askari wa kweli na wa haki unapopimwa. Wale watu ambao hukwepa wajibu, kamwe

hawezi kuvikwa taji la ushindi. Wale walio wakweli na waaminifu hawataficha Ukweli, lakini wataweka moyo na nguvu zao kazini, na kujitosa katika jitihada zao zote katika mapambano, haijalishi vita vitageuka kuwa vya namna gani. Mungu ni Mungu anayechukia dhambi. Na yule anayemtia moyo mwenye dhambi, akisema, Ni heri kwako, yaani mambo yako yapo vizuri sana, Mungu atamlaani. {3T 272.1}

Kutubu kwa dhambi kulikofanywa kwa wakati unaofaa ili kuwapa nafuu watu wa Mungu kutakubaliwa Naye. Lakini kuna wale kati yetu watakaofanya toba, kama alivyofanya Akani, wakiwa wamechelewa sana kuweza kujiokoa. Mungu aweza kuwapima na kuwapa jaribu lingine, kwa nia ya kuwashuhudia watu Wake kwamba hawawezi kumudu jaribu/mtihani mmoja, moja litakalowathibitisha kwa Mungu. Hawapatani na haki. Wanadharau ushuhuda wa moja kwa moja unaofikia moyo, na wangefurahi kuona kila mtu anayetoa maonyo akinyamazishwa. {3T 272.2}

Eliya Amkemea Ahabu

Watu wa Israeli walikuwa wamepoteza hofu na heshima kwa Mungu hadi Neno Lake kupitia Yoshua likawa halina uzito nao. “Katika siku zake, Hieli Mbetheli akajenga Yeriko; akatia misingi yake kwa kufiwa na Abiramu mzaliwa wake wa kwanza, na kuyaweka malango yake kwa kufiwa na mwana wake mdogo Segubu; sawasawa na Neno la Bwana alilolinena kwa Yoshua mwana wa Nuni.” 1Wafalme 16 {3T 273.1}

Wakati Israeli ilipokuwa ikiasi, Eliya alibaki kuwa nabii mwaminifu na wa Kweli wa Mungu. Nafsi yake aminifu ilikuwa alisumbuka sana alipoona kuwa kutokuamini na ukafiri ulikuwa ukiwatenganisha haraka wana wa Israeli na Mungu, na aliomba kwamba Mungu awaokoe watu Wake. Aliomba kwamba Bwana asiwatupe kabisa watu Wake watendao dhambi, lakini kwamba kwa njia ya hukumu ikiwa ni lazima awaamshe katika toba na asiwaruhusu kwenda mbali zaidi katika dhambi na hivyo kumfanya awaangamize kama taifa. {3T 273.2}

Ujumbe wa Bwana ulimjia Eliya, kwenda kwa Ahabu na maonyo ya hukumu zake kwa sababu ya dhambi za Israeli. Eliya alisafiri mchana na usiku mpaka alipofika kwenye kasri la Ahabu. Hakuomba kibali cha kuingia, na hakusubiri kutangazwa rasmi. Ghafla bila Ahabu kutarajia, Eliya alikuwa anasimama mbele ya mfalme wa Samaria aliyepigwa na mshangao akiwa amevalia vazi la ngozi ya wanyama ambalo kwa kawaida huvaliwa na manabii. Haombi msamaha kwa kuingia kwake kwa ghafla, bila mwaliko; lakini huku akiinua mkono wake mbinguni, anathibitisha kwa kicho kwa Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu na nchi, hukumu ambazo zingekuja kwa Israeli: “Kama Bwana, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele Zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, ila kwa neno langu. {3T 273.3}

Tangazo hili la kushtua juu ya hukumu za Mungu kwa sababu ya dhambi za Israeli ilianguka kama radi nzito juu ya mfalme aliyeasi. Alionekana kupooza kwa mshangao na hofu; na kabla hajaweza kupona kutokana na mshangao wake, Eliya, bila kusubiri kuona athari ya ujumbe wake au kabla hajapona kutokana na ule mashangao, Eliya alitoweka kwa ghafla kama alivyokuja. Kazi yake ilikuwa kuongea Neno la ole kutoka kwa Mungu, naye akaondoka mara moja. Neno lake lilikuwa limefunga hazina za mbinguni, na Neno lake lilikuwa ndiyo funguo pekee ambayo ingeweza kuzifungua tena. {3T 273.4}

Bwana alijua kuwa hakuna usalama kwa mtumishi Wake kuwemo kati ya wana wa Israeli. Asingeweza kumweka pamoja na Israeli aliyeasi, lakini alimtuma kupata kimbilio/hifadhi kati ya taifa la kipagani. Akamwagiza aende kwa mwanamke ambaye alikuwa mjane na ambaye alikuwa katika umasikini mkubwa sana, aliyekuwa masikini sana kiasi kwamba hakuweza kutegemeza maisha isipokuwa kwa kuishi maisha kwa chakula kidogo mno-kipato kidogo. Mwanamke mpagani anayeishi kwa nuru bora aliyokuwa nayo alikuwa katika hali inayokubalika zaidi na Mungu kuliko wajane wa Israeli, waliokuwa wamependelewa kwa upendeleo maalum na nuru kubwa, na bado hawakuishi kulingana na nuru ambayo Mungu alikuwa amewapa. Kama Waebrania walivyokataa nuru, wao waliachwa gizani, na Mungu hangemwacha mtumishi Wake awe miongoni mwa watu Wake, ambao walikuwa wameichokoza hasira ya Kiungu. {3T 274.1}

Sasa kulikuwa kuna nafasi kwa mwasi Ahabu na Yezebeli wa kipagani kujaribu nguvu ya miungu yao na kuthibitisha Neno la Eliya kuwa la uwongo. Manabii wa Yezebeli wapo kwa mamia. Dhidi yao hao wote anasimama Eliya, peke yake. Neno lake limeifunga mbingu. Ikiwa Baali anaweza kutoa umande na mvua, na kusababisha mimea kustawi; ikiwa anaweza kusababisha mito na vijito kutiririka kama kawaida, bila kutegemea hazina za mbinguni katika manyunyu ya mvua, basi acha Israeli na mfalme imwabudu huyu mungu Baali na watu waseme kwamba yeye ndiye Mungu. {3T 274.2}

Eliya alikuwa mtu mwenye hali ya kianadamu kama sisi tulivyo-shauku-hisia nk. Utume wake kwa Ahabu, na shutuma zake za kutisha kwake kuhusu hukumu za Mungu, kulihitaji ujasiri na Imani. Akiwa njiani kuelekea Samaria mito inayotiririka daima, vilima vilivyofunikwa na majani, misitu ya miti maridadi inayostawi, – kila kitu ambacho jicho lake lilitua kwacho kilikuwa katika hali ya kustawi kwa uzuri na utukufu, – na katika hali yake ya maumbile vilikuwa vinashawishi hali ya kutoamini [hivi kweli vingekoma?]. Inawezekanaje vitu hivi vyote vilivyo katika maumbile, ambavyo kwa sasa vinastawi sana, viunguzwe na ukame? Inawezekanaje chemichemi hizi zinazoinywesha nchi ambazo hazijawahi kuonekana zikikoma kutiririsha maji yake, ziwe kavu? Lakini Eliya hakuendekeza hali ya kutoamini. Aliendelea na utume wake akihatarisha maisha yake. Aliamini

kikamilifu kwamba Mungu atawanyenyekeza watu Wake walioasi na kwamba kupitia kutembelewa na hukumu Zake kungewaletea aibu na kuwaongoza katika toba. Alitoa kila kitu kwa utume uliokuwa mbele yake. {3T 274.3}

Wakati Ahabu anapopona kwa kiwango fulani kutoka kwenye mshangao wake kwa Maneno ya Eliya, nabii huyo anakuwa ameshatoweka. Anafanya uchunguzi kwa bidii kwa ajili yake, lakini hakuna mtu aliyemwona au anayeweza kutoa habari yoyote kumhusu. Ahabu anamjulisha Yezebeli Neno la ole ambalo Eliya ametamka mbele yake, na chuki yake dhidi ya nabii inaelezewa kwa makuhani wa Baali. Wanaungana naye katika kumshutumu na kumlaani nabii wa Yehova. Habari za kulaani kwa nabii zilienea katika nchi yote, na kuamsha hofu ya wengine na hasira ya wengi. {3T 275.1}

Baada ya miezi michache dunia, ikiwa haijanyeshewa kwa umande au mvua, ikaanza kuwa kavu, na mimea kukauka. Mifereji ambayo haijawahi kujulikana kukomesha mtiririko wake, inapungua [kutiririsha maji], na vijito vinakauka. Manabii wa Yezebeli wanatoa dhabihu kwa miungu yao na kuwaita usiku na mchana kuiburudisha dunia kwa umande na mvua. Lakini kuimba na kurudiarudia maneno ya uchawi/kunuiza, na nyimbo za sala kwa Baali na udanganyifu uliokuwa ukifanywa na wao hapo awali kudanganya watu haukubali kuitikia makusudi hayo sasa [incantations to Baal]. Makuhani wamefanya kila kitu kutuliza hasira ya miungu yao na kujaribu kumfurahisha; kwa uvumilivu na bidii inayostahili kazi hiyo bora wamekaa karibu na madhabahu zao za kipagani, wakati moto wa dhabihu ukiwaka juu ya mahali pote pa juu, na mayowe ya vilio vya kuogofya na maombi ya makuhani wa Baali yanaendelea kusikika usiku baada ya usiku kupitia Samaria iliyolaaniwa. Lakini mawingu hayaonekani mbinguni kukatilia mbali miale ya jua linalochoma. Neno la Eliya linasimama kidete, na hakuna kitu ambacho makuhani wa Baali wanaweza kufanya kitakachobadilisha. {3T 275.2}

Mwaka mzima unapita, na mwingine unaanza, na bado hakuna mvua. Dunia imekauka utadhani moto ulikuwa umepita juu yake. Mashamba yanayostawi vizuri ni kama jangwa linalowaka moto na kuunguza. Hewa inakuwa kavu na inayomfanya mtu asipumue vizuri, na tufani ya vumbi inayapofusha macho na kukaribia kusimamisha upumuaji. Bustani za Baali zimebaki bila majani, na miti ya misitu haitoi kivuli, lakini imebaki kuwa kama mifupa mikavu tu. Njaa na kiu vinamuelemea mwanadamu na mnyama kwa ogofyo la vifo vya kutisha. {3T 275.3}

Ushahidi huu wote wa haki na hukumu ya Mungu hauwaamshi Israeli kutubu. Yezebeli amejazwa na wendawazimu. Hatainama wala kujishusha kwa Mungu wa mbinguni. Manabii wa Baali, Ahabu, Yezebeli, na karibu Israeli yote, wanaelekeza mashitaka yao mabaya yote kwa Eliya- kwa viapo. Ahabu alikuwa ametuma kwa kila ufalme na taifa kumtafuta nabii huyo wa ajabu na alikuwa amewapa kiapo

falme na mataifa ya Israeli yaliyodai kwamba hawajui chochote kumhusu. Eliya alikuwa amefunga mbingu na Neno lake na alikuwa amechukua ufunguo pamoja naye, naye hakuweza kupatikana popote. {3T 276.1}

Ndipo Yezebeli akaamua kwamba kwa kuwa hawezi kumfanya Eliya ahisi nguvu yake ya kuua, atalipiza kisasi kwa kuwaangamiza manabii wa Mungu katika Israeli. Hakuna mtu aliyedai kuwa nabii wa Mungu atakayeishi. Mwanamke huyu aliyedhamiria, na mwenye hasira, anatekeleza kazi yake yenye ukichaa/wazimu kwa kuwaua manabii wa Bwana. Makuhani wa Baali na karibu Israeli wote wamedanganyika mno kiasi kwamba wanaona kuwa ikiwa manabii wa Mungu wangeuawa, basi msiba wanaoupitia ungekoma. {3T 276.2}

Lakini mwaka wa pili unapita, na mbingu zisizo na huruma hazitoi mvua. Ukame na njaa vinatekeleza kazi yao ya kusikitisha, na bado Waisraeli waasi hawashushi mioyo yao yenye majivuno, na dhambi mbele za Mungu; lakini wao wananung'unika na kulalamika juu ya nabii wa Mungu aliyewaletea hali hii ya kutisha. Akina baba na mama wanaona watoto wao wakiangamia, bila uwezo wa kuwasaidia. Na bado watu wapo katika giza mbaya sana la namna hiyo kiasi kwamba hawawezi kuona kuwa haki ya Mungu imeamshwa juu yao kwa sababu ya dhambi zao na kwamba msiba huu mbaya hutumwa kwa huruma kwao kuwaokoa kusudi wasimkane kabisa na kumwacha Mungu wa baba zao. {3T 276.3}

Iligharimu Israeli mateso na uchungu mkubwa kuletwa kwa toba hiyo ambayo ilikuwa muhimu katika ili kupata tena imani yao iliyopotea na hisia wazi ya uwajibikaji wao kwa Mungu. Uasi wao ulikuwa zaidi ya kutisha kuliko ukame au njaa. Eliya alisubiri na kuomba kwa imani kwa miaka mingi ya ukame na njaa ili mioyo ya Israeli, kupitia mateso yao, igeuzwe kutoka kwa ibada yao ya sanamu na kuwa utii kwa Mungu. Lakini pamoja na mateso yao yote, walisimama kidete katika ibada zao za sanamu na kutazama juu ya nabii wa Mungu kama sababu ya msiba wao. Na kama Eliya angekuwa chini ya himaya yao wangemkabidhi kwa Yezebeli, ili aweze kutosheleza kisasi chake kwa kutwaa/kuondoa maisha yake. Kwa kuwa Eliya alithubutu kutamka Neno la ole ambalo Mungu alimwamuru, alijifanya yeye mwenyewe kuwa mtu wanayemchukia. Hawakuweza kuona mkono wa Mungu katika hukumu ambazo walikuwa wakiteseka kwa sababu ya dhambi zao, lakini lawama zote hizo walizielekeza kwa yule mtu Eliya. Hawakuzichukia dhambi zile zilizowaleta chini ya fimbo ya Bwana ya kuadhibu, lakini walimchukia nabii mwaminifu, chombo cha Mungu cha kukemea dhambi zao na msiba. {3T 276.4}

“Ikawa baada ya siku nyingi, Neno la Bwana likamjia Eliya, katika mwaka wa tatu, kusema, Enenda, ukajioneshe kwa Ahabu; Nami nitaleta mvua juu ya nchi.” Eliya hasiti kuanza safari yake ya hatari. Kwa miaka mitatu alikuwa akichukiwa, na kuwindwa kutoka mji hadi mji kwa agizo la mfalme, na taifa lote limetoa kiapo

kuwa hawezi kupatikana-hawawezi kumpata. Na sasa, kwa Neno la Mungu, anapaswa kujitokeza mbele ya Ahabu. {3T 277.1}

Wakati wa uasi wa Israeli yote, na wakati bwana wake ni mwabudu Baali, gavana wa Ahabu nyumba ameonekana kuwa mwaminifu kwa Mungu. Kwa kuhatarisha maisha yake mwenyewe amewahifadhi manabii wa Mungu kwa kuwaficha kwa hamsini katika pango na kuwalisha. Wakati mtumishi wa Ahabu akitafuta kwenye ufalme wote chemchemi na vijito vya maji, Eliya anajihudhurisha mwenyewe mbele yake. Obadia alimheshimu nabii wa Mungu, lakini Eliya alipomtuma ujumbe kwa mfalme, aliogopa sana. Anaiona hatari na vifo vinavyomkabili yeye mwenyewe na Eliya. Anaomba sana kwamba maisha yake yasitolewe kafara; lakini Eliya anamhakikishia kwa kiapo kwamba atamwona Ahabu siku hiyo. Nabii huyo hataenda kwa Ahabu hivi hivi lakini kama mmoja wa wajumbe wa Mungu, mwenye kuamuru heshima, na anatuma ujumbe kwa Obadia: “Tazama, Eliya yupo.” Kama Ahabu anataka kumuona Eliya, sasa anayo fursa ya kuja kwake. Eliya hataenda kwa Ahabu. {3T 277.2}

Kwa mshangao uliochanganyika na woga mfalme anasikia ujumbe kwamba Eliya ambaye anamwogopa na anamchukia, sasa anakuja kumlaki. Kwa muda mrefu amemtafuta nabii huyo ili amwangamize, na yeye anajua kwamba Eliya hangeweka wazi maisha yake na kuja kwake isipokuwa kama analindwa au kwa shutuma zenye vitisho. Anakumbuka mkono uliopooza wa Yeroboamu na anaamua kwamba sio salama kuinua mkono wake mkono dhidi ya mjumbe wa Mungu. Na kwa hofu na kutetemeka, na akiwa na wafuasi wengi na onyesho kubwa la jeshi lenye nguvu, anaharakisha kukutana na Eliya. Na anapokutana uso kwa uso na mtu ambaye yeye amemtafuta kwa muda mrefu, hathubutu kumdhuru. Mfalme, mwenye jazba kali sana, na aliyejaa chuki dhidi ya Eliya, anaonekana kuwa hana nguvu na hana mtu mbele yake. Anapokutana na nabii hawezi kujizuia kunena kwa lugha ya moyoni mwake: “Je! Ni wewe, Ewe mtaabishaji wa Israeli?” Eliya, akiwa amekasirika, na aliyejaa wivu kwa heshima na utukufu wa Mungu, anajibu mashtaka ya Ahabu kwa ujasiri: “Si mimi niliyewataabisha Israeli; bali ni wewe, na nyumba ya baba yako, kwa kuwa mmeziacha amri za Bwana.” {3T 278.1}

Nabii, kama mjumbe wa Mungu, alikuwa amekemea dhambi za watu, akitangaza juu yao hukumu za Mungu kwa sababu ya uovu wao. Na sasa, akisimama peke yake katika hali ya fahamu ya kutokuwa na hatia, akiwa imara katika uadilifu wake, akizungukwa na kundi la watu wenye silaha, Eliya haoneshi woga, wala haoneshi kicho kwa mfalme. Mtu ambaye Mungu amezungumza naye, na ambaye ana ufahamu wa wazi wa jinsi Mungu anavyomchukulia mwanadamu katika upotovu wake wa dhambi, hana jambo la kutoea udhuru au kuomba msamaha kwa Ahabu wala kumwabudu/kumwinamia. Kama mjumbe wa Mungu, Eliya sasa anaamuru na Ahabu mara moja anatii kana kwamba Eliya ndiye mfalme na yeye ndiye raia. {3T 278.2}

Dhabihu juu ya Mlima Karmeli

Eliya anadai mkutano huko Karmeli wa Waisraeli wote na pia wa manabii wote wa Baali. Taadhima ya kutisha katika sura ya nabii inampatia mwonekano wa mmoja asimamaye kwenye uwepo wa Bwana Mungu wa Israeli. Hali ya Israeli katika uasi wao inataka mwenendo-mwonekano thabiti, hotuba kali, na mamlaka ya kuamuru. Mungu huandaa ujumbe unaoendana na wakati na tukio. Wakati fulani huweka Roho Wake juu ya wajumbe Wake ili kutoa mlio wa tahadhari usiku na mchana, kama alivyofanya mjumbe wake Yohana: “Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake.” Ndipo tena watu wa vitendo huhitajiwa ambao hawatayumbishwa kutoka kwenye jukumu lao, lakini ambao nguvu zao zitainuka na kudai, “Ni nani aliye upande wa Bwana?” hebu na aje pamoja nasi. Mungu atakuwa na ujumbe unaofaa kukutana na watu Wake katika hali zao mbalimbali. {3T 279.1}

Wajumbe wepesi hutumwa katika ufalme wote wakiwa na ujumbe kutoka kwa Eliya. Wawakilishi wanatumwa kutoka majiji, miji, vijiji, na familia. Wote wanaonekana kuwa na haraka kujibu miito, kana kwamba kuna muujiza mzuri unaokwenda kutendeka. Kulingana na amri ya Eliya, Ahabu anakusanya manabii wa Baali huko Mlima Karmeli. Moyo wa kiongozi mwasi wa Israeli umejawa na hofu, na mshangao na anatetemeka kufuatia maelekezo ya nabii mkali wa Mungu. {3T 279.2}

Watu wanakusanyika juu ya Mlima Karmeli, mahali pa uzuri wakati umande na mvua zilipokuwa zikinyesha juu yake vilisababisha kustawi; lakini sasa uzuri wake umeangamia kwa laana ya Mungu. Juu ya mlima huu, uliokuwa na uzuri wa miti na maua, manabii wa Baali walikuwa wamejenga madhabahu kwa ibada yao ya kipagani. Mlima huu ulikuwa mahali panapoonekana dhahiri; ikiziangalia kwa chini nchi zilizo karibu na ukiwa mbele ya sehemu kubwa ya ufalme. Kama Mungu alivyokuwa akidharauliwa kwa ishara na ibada ya sanamu zilizokuwa zinaendelea hapa, Eliya alichagua hapa kama mahali pazuri zaidi kwa onesho la nguvu za Mungu na kudhihirisha anavyostahili heshima. {3T 279.3}

Manabii wa Yezebeli, wapatao mia nane hamsini kwa idadi- 850, kama Kikosi cha wanajeshi waliojiandaa kwa vita, walitembea kwa makundi wakiongozwa na muziki wa ala na onesho la kuvutia. Lakini kuna mtetemo mioyoni mwao wanapofikiria kuwa kwa Neno la nabii huyu wa Yehova nchi ya Israeli imekosa umande na mvua kwa miaka mitatu. Wanahisi kuwa kuna kengele ya tahadhari na mgogoro wa kutisha unanyemelea. Walikuwa wameiaminia miungu yao, lakini hawakuweza kutengua Maneno ya Eliya na kuthibitisha kuwa alikuwa muongo. Miungu yao haikuweza kubadilika licha ya kilio chao cha kusikitisha, sala, na dhabihu. {3T 279.4}

Eliya, asubuhi na mapema, anasimama juu ya Mlima Karmeli, akizungukwa na Israeli waasi na manabii wa Baali. Ni mtu pekee katika umati huo mkubwa,

anayesimama bila hofu. Yeye ambaye ufalme wote amemshtaki kwa uzito wake wa ole/laana ulio mbele yao, yeye asiyetishika na asiyetumikiwa na majeshi yanayoonekana na onesho lenye kuvutia. Anasimama, akiwa amevaa vazi lake refu, akiwa na taadhima ya kutisha usoni mwake, kana kwamba anaufahamu kabisa utume wake mtakatifu kama mtumishi wa Mungu [aliyetumwa] kutekeleza amri Zake. Eliya anayaelekeza macho yake juu ya kilele cha milima mahali palipokuwa pamesimama madhabahu ya Yehova wakati mlima ulipokuwa umefunikwa na miti na maua yaliyostawi. Laana ya Mungu sasa iko juu yake; hali yote ya ukiwa ya Israeli inaonekana wazi juu ya madhabahu ya Yehova iliyopuuzwa na kubomolewa, na madhabahu zinaonekana mbele ya Baali. Ahabu anasimama mbele ya makuhani wa Baali, na wote wanangoja kwa matarajio ya hofu-wasiwasi na utisho juu ya maneno ya Eliya. {3T 280.1}

Katika mwangaza kamili wa jua, akiwa amezungukwa na maelfu, - watu wa vita, manabii wa Baali, na mfalme wa Israeli, - anasimama mtu asiye na ulinzi, Eliya, anayeonekana yuko peke yake, lakini siyo peke yake. Mwenyeji wa mbinguni Mwenye nguvu zaidi anamzunguka [pande zote]. Malaika wenye nguvu zaidi wamekuja kutoka mbinguni kumkinga nabii mwaaminifu na mwenye haki. Kwa sauti ya ukali na ya kuamuru Eliya analia: “Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa Ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni Yeye. Wale watu hawakumjibu neno.” Hakuna hata mmoja katika mkutano huo mkubwa aliyethubutu kusema neno moja kwa Mungu na kuonesha uaminifu wake kwa Yehova. {3T 280.2}

Ni udanganyifu wa kushangaza na upofu wa kutisha kiasi gani, kama wingu jeusi, lilikuwa limeifunika Israeli! Upofu huu na uasi ulikuwa haujawafunga kwa ghafla; ulikuja juu yao pole pole kwa kuwa hawakulisikia Neno la kukemea na onyo Bwana alilolituma kwao kwa sababu ya majivuno na dhambi zao. Na sasa, katika mgogoro huu wa kutisha, mbele ya makuhani waabudu-sanamu na mfalme aliyeasi, wakakaa katikati (njia panda-neutral). Ikiwa Mungu anachukia dhambi moja kuliko nyingine, ambazo watu wake wamekutwa na hatia, haitabadilisha chochote katika nyakati hizi za dharura. Kutoonesha tofauti na kutokuwa na upande wowote nyakati za migogoro ya kidini inachukuliwa na Mungu kama uhalifu mkubwa na ulio sawa na aina mbaya kabisa ya uadui dhidi ya Mungu. {3T 280.3}

Israeli yote ipo kimya. Sauti ya Eliya inasikika tena ikiwaambia, “Ndipo Eliya akawaambia watu, mimi nimesalia, mimi peke yangu, nabii wa Bwana; lakini manabii wa Baali ni watu mia nne na hamsini-450. Kwa hiyo na watutolee ng'ombe wawili; wao na wajichagulie ng'ombe mmoja, wamkate-kate na kumweka juu ya kuni, wasitie moto chini; nami nitamtengeza huyo ng'ombe wa pili, na kumweka juu ya kuni, wala sitatia moto chini. Nanyi ombeni kwa jina la mungu wenu, nami nitaomba kwa Jina la Bwana; na Mungu Yule ajibuye kwa moto, na awe Ndiye Mungu. Watu wote wakajibu wakasema, Maneno haya ni mazuri. Eliya akawaambia

manabii wa Baali, Jichagulieni ng'ombe mmoja, mkamtengeze kwanza; maana ninyi ndio wengi; mkaliitie jina la mungu wenu, wala msitie moto chini. Wakamtwaa yule ng'ombe waliyepewa, wakamtengeza, wakaliitia jina la Baali tangu asubuhi hata adhuhuri, wakisema, Ee Baali, utusikie. Lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu. Nao wakaruka-ruka juu ya madhabahu waliyoifanya. Ikawa, wakati wa adhuhuri, Eliya akawafanyia dhihaka, akasema, Mwiteni kwa sauti kuu; maana ni mungu huyo; labda anazungumza, au ana shughuli, au anasafiri, au labda amelala, sharti aamshwe. Wakapiga kelele, wakajikatakata kwa visu na vyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika. Ikawa, wakati wa adhuhuri ulipopita, walitabiri hata wakati wa kutoa dhabihu ya jioni; lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu, wala aliyeangalia." {3T 281.1}

Pendekezo la Eliya ni la busara. Watu hawathubutu kulikwepa, na sasa wanapata ujasiri wa kujibu: Neno ni zuri. Manabii wa Baali hawathubutu kupinga au kukwepa jambo hilo. Mungu ameelekeza jaribio hili na limeleta mkanganyiko kwa waasisi wa ibada ya sanamu na ishara ya ushindi kwa ajili ya Jina Lake. Makuhani wa Baali hawathubutu kufanya vinginevyo kuliko kukubali masharti. Wakiwa na utisho na hatia mioyoni mwao huku wakijitahidi kujionesha wakakamavu na wajasiri kwa nje, wanatengeneza madhabahu yao, wanaweka kuni juu yake na yule mnyama wa kuchinjwa, na kisha kuanza matamko yao, kuimba kwao na kupiga kelele, mambo yanayoandamana na ibada zao za kipagani. Vilio vyao vikali vinasikika tena kupitia misitu na milima: "Ee Baali, utusikie." Makuhani wanakusanyika kwa makundi karibu na madhabahu zao, na kwa kurukaruka, na kung'ata, na kupiga kelele, na kukanyaga kwa kishindo, na kwa ishara zisizo za asili, na kung'oa nywele zao, na kukata nyama zao, wanadhihirisha umakini wao katika kile wanachokiamini. {3T 281.2}

Asubuhi inapita na adhuhuri inakuja, na bado hakuna mwendo wa miungu yao kuwahurumia makuhani wa Baali, waabudu sanamu waliodanganywa. Hakuna sauti inayojibu kilio chao cha wasiwasi. Makuhani wanaendelea kubuni jinsi, kwa udanganyifu, watakavyoweza kuwasha moto juu ya madhabahu na kumpa Baali utukufu. Lakini jicho thabiti la Eliya linaangalia kila mwendo/mjongea. Sauti mia nane zenye makelele zinachosha koo na kulikwaruza. Nguo zao zimetapakaa damu, na bado msisimko wao ulijaa hofu hauishi. Maombi yao yamechanganyika na laana kwa mungu wao jua asiyetuma moto kwenye madhabahu zao. Eliya anasimama tu, akiangalia kwa jicho la tai usije udanganyifu wowote ukatumika; kwa kuwa anajua kama, kwa njia yeyote ile, wangeweza kuwasha moto kwenye madhabahu, naye angesambaratishwa kwa kuraruliwa vipande vipande pale pale. Anapenda kuwaonesha watu upumbavu mashaka yao na hali yao ya kusita sita katikati ya mawazo mawili wakati wana kazi nzuri za uweza wa Mungu kwa niaba yake na dhibitisho zisizohesabika za rehema Zake zisizo na kipimo na upendo uliojaa adhili kwao.
{3T 282.1}

“Ikawa, wakati wa adhuhuri, Eliya akawafanyia dhihaka, akasema, Mwiteni kwa Baali kwa sauti kuu; maana ni mungu huyo; labda anazungumza, au ana shughuli, au anasafiri, au labda amelala, sharti aamshwe. Wakapiga kelele, wakajikata-kata kwa visu na nyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika. Ikawa, wakati wa adhuhuri ulipopita, walitabiri hata wakati wa kutoa dhabihu ya jioni; lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu, wala aliyeangalia.” {3T 282.2}

Ni kwa furaha kiasi gani Shetani, aliyeanguka kama umeme kutoka mbinguni, angewasaidia wale ambao amewadanganya, wale ambao akili zao amezithibiti, na ambao wamejitoa kikamilifu kwa Huduma yake. Kwa furaha angeweza kutuma umeme na kuwasha dhabihu zao; lakini Yehova ameweka mipaka ya Shetani. Yeye Amezuia nguvu zake adui, na hila zake zote haviwezi kuleta hata cheche moja ya moto kwa madhabahu za Baali. Jioni inaanza kuchwa. Manabii wa Baali wamechoka, wamezimia, na wamechanganyikiwa. Mtu mmoja anapendekeza hili, mwingine anapendekeza lile hadi juhudi zao zinakoma. Kelele na laana zao hazisikiki tena juu ya Mlima Karmeli. Kwa udhaifu na kukata tamaa wanajiondoa mashindanoni. {3T 282.3}

Watu wameshuhudia majaribio ya kutisha ya makuhani wasio na busara, waliojaa hofu. Wameshuhudia kurukaruka kwao juu ya madhabahu kana kwamba walitaka miale inayowaka kutoka kwenye jua irukie madhabahu zao. Wamechoka na maonesho ya kishetani/kipepo, ya ibada ya sanamu ya kipagani; na sasa kwa dhati wanatamani kusikia Eliya atasema nini. {3T 283.1}

Zamu ya Eliya sasa ikafika. “Eliya akawaambia watu wote, Nikaribieni mimi. Watu wote wakamkaribia. Akaitengeneza madhabahu ya Bwana iliyovunjika. Eliya akatwaa mawe kumi na mawili, kwa hesabu ya kabila za wana wa Yakobo, aliyejiliwa na Neno la Bwana na kuambiwa, jina lako litakuwa Israeli. Naye akaijenga madhabahu kwa mawe hayo katika Jina la Bwana; akafanya mfereji, kama wa vipimo viwili vya mbegu, ukiizunguka madhabahu. Kisha akazipanga zile kuni, akamkata yule ng'ombe vipande vipande, akaviweka juu ya kuni. Akasema, Jazeni mapipa manne maji, mkayamwage juu ya sadaka ya kuteketezwa, na juu ya kuni. Akasema, Fanyeni mara ya pili. Wakafanya mara ya pili. Akasema, Fanyeni mara ya tatu. Wakafanya mara ya tatu. Yale maji yakaizunguka madhabahu; akaujaza mfereji maji. Ikawa, wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya nabii akakaribia, akasema, Ee Bwana, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa Wewe Ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi Wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa Neno lako. Unisikie, Ee Bwana, unisikie, ili watu hawa wajue ya kuwa Wewe, Bwana, Ndiwe Mungu, na ya kuwa Wewe umewageuza moyo wakurudie. Ndipo moto wa Bwana ukashuka, ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni, na mawe, na mavumbi, ukayaramba

yale maji yaliyokuwamo katika mfereji. Na watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi; wakasema, Bwana Ndiye Mungu, Bwana Ndiye Mungu.” {3T 283.2}

Eliya wakati wa saa ya dhabihu ya jioni anatengeneza madhabahu ya Mungu ambayo uasi wa Israeli umeruhusu makuhani wa Baali kuibomoa. Hamwiti mmoja wa watu amsaidie katika kazi yake ngumu. Madhabahu za Baali zote zimetayarishwa; lakini anageukia madhabahu ya Mungu iliyovunjika, ambayo ni takatifu zaidi na ya thamani kwake katika magofu yake yasiyopendeza kuliko madhabahu zote nzuri za Baali. {3T 284.1}

Eliya anaheshimu agano la Bwana na watu Wake, pamoja na kuwa wamemwasi. Kwa utulivu na kwa kicho anakarabati madhabahu iliyovunjika yenye mawe kumi na mawili/12, kulingana na hesabu ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Makuhani wa Baali waliokatishwa tamaa, waliochoka baada ya juhudi zao za wendawazimu, zilizosheheni ghadhabu, wameketi au wamelala chini kabisa ardhini, wakingojea kuona Eliya atafanya nini. Wamejawa na hofu na chuki dhidi ya nabii kwa kupendekeza jaribio ambalo limefunua udhaifu wao na uzembe wa miungu yao na kukosa kwao ufanisi. {3T 284.2}

Watu wa Israeli wamesimama wakiwa wamepigwa na butwaa, waliokwajuka, wenye wasiwasi, na waliokumbwa na hofu, wakati Eliya anapomwita Yehova, Muumba wa mbingu na dunia. Watu wameshuhudia, ghadhabu ya unafiki na isiyo mashiko ya manabii wa Baali. Kwa kulinganisha sasa wamebahatika kushuhudia utulivu, na mwonekano wa uhuisho na kutisha wa Eliya. Anawakumbusha watu juu ya upungufu wao, ambao umeamsha ghadhabu ya Mungu juu yao, halafu anawataka wanyenyekeze mioyo yao na kumrudia Mungu wa baba zao, ili laana Yake iondolewe kutoka kwao. Ahabu na makuhani wake waabudu sanamu wanaangalia kwa mshangao uliochanganyika na hofu. Wanasubiri matokeo kwa ukimya wenye wasiwasi, na utulivu. {3T 284.3}

Baada ya mnyama wa kafara kuwekwa juu ya madhabahu, anawaamuru watu wafurikishe dhabihu na madhabahu kwa maji, na kujaza mfereji pande zote za madhabahu. Kisha kwa heshima anainama mbele za Mungu asiyeonekana, anainua mikono yake kuelekea mbinguni, na kutoa sala ya utulivu na rahisi, isiyoambatana na matumizi ya nguvu zenye jeuri, ukatili au misisimko ya kimwili. Hakuna mayowe ya vilio juu ya vilele vya Karmeli. Ukimya wa kicho, unaowanyanyasa makuhani wa Baali, unakaa juu ya wote. Katika sala yake, Eliya hatumii muonekano usio wa kawaida. Anamwomba Yehova kana kwamba alikuwa karibu, akiishuhudia tukio zima, na kusikia sala yake ya dhati, ya bidii, lakini iliyo rahisi. Makuhani wa Baali wamepiga kelele/mayowe, na kutoa povu mdomoni, wakirukaruka, na wakiomba, kwa muda mrefu - tangu asubuhi mpaka jioni. Maombi ya Eliya ni mafupi sana, ya dhati, yenye adabu na yanayotoka moyoni. Mara tu sala hiyo ilipotolewa kulikuwa

na miali ya moto inayoteremka kutoka mbinguni kwa njia wazi na tofauti tofauti, kama umeme mkali, ikiwasha kuni za kafara na kuteketeza mnyama wa kafara, ikilamba maji kwenye mfereji na kulamba/kuteketeza hata mawe ya madhabahu. Mng'aro wa moto unaangaza mlima na ni wenye kuleta maumivu katika macho ya umati wa watu. Watu wa ufalme wa Israeli ambao hawakukusanyika juu ya mlima wanaangalia kwa hamu wale waliokusanyika hapo. Kadri moto ulivyokuwa ukishuka, wanaushuhudia na wanashangaa kwa kile wanachokiona. Inafanana na nguzo ya moto kwenye Bahari Nyekundu, ambapo usiku ilitenganisha watoto wa Israeli na jeshi la Wamisri. {3T 284.4}

Watu walio juu ya mlima wanasujudu kwa hofu bila kushurutishwa na kwa mshangao mbele za Mungu asiyeonekana. Hawawezi kuuangalia moto mkali unaoteketeza uliotumwa kutoka mbinguni. Wanahofia kwamba wanaweza kuangamizwa katika uasi na dhambi zao, hivyo wanalia kwa sauti moja, ambayo inatoa mwangwi kwenye nyanda zilizo chini kwa sauti ya kutisha iliyosikika wazi wazi: "Bwana Ndiye Mungu, Bwana Ndiye Mungu." Israeli hatimaye imeamshwa na haiwezi kudanganywa tena. Wanaona dhambi zao na jinsi walivyomvunjia Mungu heshima. Hasira zao zimeamshwa dhidi ya manabii wa Baali. Kwa hofu, makuhani wa Ahabu na Baali wanashuhudia udhihirisho wa nguvu za Yehova. Kwa mara nyingine tena sauti ya Eliya inasikika kwa maneno ya kushtua ya kuamuru watu: "Wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja." Watu wako tayari kutii neno lake. Wanawakamata manabii wa uwongo waliowadanganya, na kuwaleta kwenye kijito cha Kishoni, na huko, kwa mkono wake mwenyewe, Eliya anawaua hawa makuhani waabudu masanamu. {3T 285.1}

Hukumu za Mungu zikiwa zimetekelezwa juu ya makuhani wa uwongo, watu wakiwa wamekiri dhambi zao na kumtambua Mungu wa baba zao, laana inayokausha/ukame ya Mungu sasa inapaswa kuondolewa, naye apaswa kufanya upya baraka Zake kwa watu Wake na kuiburudisha dunia kwa umande na mvua. {3T 286.1}

Eliya anamwambia Ahabu: "Haya! Inuka, ule, unywe; kwani pana sauti ya mvua tele." Wakati Ahabu akienda kusherehekea, Eliya anapanda kutoka kwenye dhabihu ya kutisha kwenda juu ya Mlima Karmeli kuomba. Kazi yake ya kuwaua makuhani wa kipagani haikuwa imeacha kumuandaa kwa zoezi zito la maombi. Alikuwa ametimiza mapenzi ya Mungu. Baada ya kutimiza mapenzi ya Mungu, yeye kama chombo cha Mungu, alifanya kile awezacho, kuondoa kisababisho cha uasi wa Israeli kwa kuwaua makuhani waabudu sanamu, hata alipokuwa hawezi kufanya zaidi. Kisha anaomba kwa niaba ya Israeli iliyotenda dhambi na iliyoasi. Katika mkao wenye maumivu zaidi, uso wake ukiinamishwa katikati ya magoti yake, kwa dhati kabisa anamsihi sana Mungu alete mvua. Mara sita mfululizo anamtuma mtumishi wake ili aangalie ikiwa kuna ishara yoyote inayoonekana kuonesha kuwa Mungu amesikia maombi yake. Hawi mtu asiye na uvumilivu au asiye na imani kwa

kuwa Bwana hatoi ishara kuwa maombi yake ya dhati yamesikilizwa. Anaendelea kuomba kwa bidii, akimtuma mtumishi wake mara saba ili kuona ikiwa Mungu ametoa ishara yoyote. Mtumishi wake anarudi mara ya sita kutoka kuangalia welekeo wa baharini na taarifa ya kukatisha tamaa kwamba hakuna ishara ya mawingu yanayojikusanya huko mawinguni. Mara ya saba anamjulisha Eliya kuwa kuna wingu dogo linaloonekana, lenye ukubwa wa kiganja cha mtu. Hii ilitosha kuridhisha imani ya Eliya. Hasubiri hadi wingu jeusi lijikusanye ili kujipatia uhakika wa jambo. Katika wingu hilo dogo linaloinuka imani yake husikia sauti ya wingi wa mvua. Matendo yake ni sawa na imani yake. Anatuma ujumbe kwa Ahabu na mtumishi wake: “Tandika farasi, ushuke, mvua isikuzuie.” {3T 286.2}

Unyenyekevu wa Eliya

Unyenyekevu wa Eliya Hapa Eliya alionesha alijitosa kwa jambo fulani juu ya imani yake. Hakungojea ili aone. “Ikawa, muda si muda, mbingu zikawa nyeusi kwa mawingu na upepo, ikanyesha mvua nyingi. Ahabu akapanda garini, akaenda zake Yezreeli. Mkono wa Bwana ulikuwa juu ya Eliya; akajikaza viuno, akapiga mbio mbele ya Ahabu mpaka kuiingia Yezreeli.” {3T 287.1}

Eliya alikuwa amepitia msisimko mkubwa na kazi wakati wa mchana; lakini Roho wa Bwana alikuja juu yake kwa sababu alikuwa mtiifu na alikuwa ametenda mapenzi Yake katika kuwaua makuhani waabudu sanamu. Baadhi watakuwa tayari kusema: Eliya alikuwa mtu mgumu na katili kiasi gani! Na yeyote anayetetea heshima ya Mungu kwa gharama yoyote ile atapokea lawama na hukumu juu yake mwenyewe kutoka kwa walio wengi. {3T 287.2}

Mvua ilianza kushuka chini. Ilikuwa usiku, na mvua ya upofu ilimzuia Ahabu kuona njia yake. Eliya, akiwa ametiwa moyo [amehuishwa] na Roho na uweza wa Mungu, alijifunga vazi lake refu na kumkimbilia Bwana gari la Ahabu, akiongoza njia yake hadi lango la jiji. Nabii wa Mungu alikuwa amemdhalilisha Ahabu mbele ya watu wake. Alikuwa amewaua makuhani wake waabudu sanamu, na sasa alitaka kuonesha kwa Israeli kwamba yeye alimkubali Ahabu kama mfalme wake. Kama kitendo cha heshima/ibada maalum aliongoza gari lake, akikimbia mbele yake kwenda mlango wa lango la mji ili kumwongoza mfalme. {3T 287.3}

Hapa kuna somo kwa vijana ambao wanadai kuwa ni watumishi wa Mungu, wanaobeba ujumbe Wake, walioinuliwa katika makadirio yao wenyewe. Hawawezi kufuatilia chochote cha maana katika uzoefu wao, kama Eliya, lakini wanajiona hawawezi kutekeleza majukumu ambayo kwao yanaonekana duni. Hawatashuka kutoka kwa hadhi yao ya kichungaji ili kufanya huduma inayohitajika, wakiogopa kuwa watakuwa wakifanya kazi ya mtumishi. Watu wa aina hiyo wote wanapaswa kujifunza kutoka kwa mfano wa Eliya. Neno lake lilifunga hazina za mbinguni, umande na mvua, kutoka duniani miaka mitatu. Neno lake peke yake lilikuwa ufunguo wa kufungua mbingu na kuleta manyunyu ya mvua. Aliheshimiwa na

Mungu wakati akitoa ombi lake rahisi mbele ya mfalme na maelfu ya Israeli, kwa kujibu ombi, moto uliwaka kutoka mbinguni na kuwasha moto juu ya madhabahu ya kuteketeza. Mkono wake ulitekeleza hukumu ya Mungu kwa kuwaua makuhani wa Baali mia nane na hamsini 850; na bado, baada ya kazi ngumu, kali na ya ushindi wa siku hiyo, yeye ambaye angeweza kuleta mawingu na mvua na moto kutoka mbinguni alikuwa tayari kufanya huduma ya unyonge na kukimbia mbele ya gari la Ahabu katika giza na upepo na mvua, kumtumikia yule mfalme ambaye hakuogopa kumkemea usoni pake, kwa sababu ya dhambi zake na uhalifu. Mfalme alipita katikati ya malango. Eliya akajifunga vazi lake na kulala juu ya ardhi tupu. {3T 287.4}

Eliya Katika Hali Ya Kukata Tamaa Kukubwa

Baada ya Eliya kuonesha ujasiri huo usio na hofu katika mashindano kati ya maisha na kifo, baada ya kuwa ameshinda dhidi ya mfalme, makuhani, na watu, kwa kawaida tungetarajia kwamba hangeweza kamwe kukaribisha kukata tamaa au kutishwa na woga. {3T 288.1}

Baada ya kuonekana kwake kwa kwanza kwa Ahabu, alipokuwa akitamka juu yake hukumu za Mungu kwa sababu yake na uasi wa Israeli, Mungu alielekeza mwendo wake kutoka kwa nguvu ya Yezebeli hadi mahali pa usalama milimani, kwenye kijito cha Kerith. Huko alimheshimisha Eliya kwa kumpelekea chakula asubuhi na jioni kwa njia ya malaika wa mbinguni. Kisha, kijito kilipokauka, alimpeleka kwa mjane wa Sarepta, na akafanya muujiza kila siku ili kuiwezesha familia ya mjane na Eliya kuwa na chakula. Baada ya kuwa amebarikiwa na ushahidi wa upendo wa jinsi hiyo na matunzo kutoka kwa Mungu, tungedhani kwamba Eliya hataacha kumtumaini kamwe Bwana. Lakini mtume anatuambia kwamba alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, na anayeshawishiwa na majaribu kama sisi. {3T 288.2}

Ahabu alimsimulia mkewe matukio ya kushangaza ya siku hiyo na maonesho mazuri ya nguvu ya Mungu yaliyoonesha kuwa Yehova, Muumba wa mbingu na dunia, alikuwa Mungu; pia kwamba Eliya alikuwa amewaua manabii wa Baali. Kwa hili, [la kuwaua manabii] Yezebeli, aliyekuwa amefanywa mgumu katika dhambi, alikasirika sana. Shupavu, mkaidi, na aliyedhamiria katika ibada yake ya sanamu, alimtangazia Ahabu kwamba Eliya hapaswi kuishi. {3T 288.3}

Usiku huo mjumbe alimwamsha nabii aliyechoka na kumpatia neno lililotoka kwa Yezebeli, alilopewa katika jina la miungu yake ya kipagani, kwamba kwenye uwepo wa Waisraeli atamfanyia Eliya kama alivyowatendea makuhani wa Baali. Eliya alipaswa kukutana na tishio hili na kiapo hiki cha Yezebeli kwa kusihi ulinzi kutoka kwa Mungu wa mbinguni, aliyemwagiza afanye kazi aliyoifanya. Alipaswa kumwambia mjumbe kwamba Mungu ambaye alimwamini atakuwa mlinzi wake dhidi ya chuki na vitisho vya Yezebeli. Lakini imani na ujasiri wa Eliya vikaonekana

kummwacha. Anainuka na kuanza kutoka kwenye usingizi wake akiwa amefadhaika. Mvua inanyesha kutoka mbinguni, na giza liko kila upande. Anapoteza uwepo wa Mungu na kukimbia kuponya maisha yake kana kwamba mlipizaji wa damu alikuwa karibu nyuma yake. Anamuacha mtumishi wake nyuma wakiwa njiani, na asubuhi anakuwa yupo mbali na makazi ya wanadamu, kwenye jangwa lenye ukame, akiwa peke yake. {3T 289.1}

“Naye alipoona hayo, aliondoka, akaenda aihifadhi roho yake, akafika Beer-sheba, mji wa Yuda, akamwacha mtumishi wake huko. Lakini yeye mwenyewe akaendelea katika jangwa mwendo wa siku moja, akaenda akaketi chini ya mretemu. Akajiombea roho yake afe, akasema, Yatosha; sasa, Ee Bwana, uiondoe roho yangu; kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu. Naye akajinyosha akalala chini ya mretemu; na tazama, malaika akamgusa, akamwambia, Inuka, ule. Akatazama, kumbe! Pana mkate umeokwa juu ya makaa, na gudulia la maji, kichwani pake. Akala, akanywa, akajinyosha tena. Malaika wa Bwana akamwendea mara ya pili, akamgusa, akasema, Inuka, ule; maana safari hii ni kubwa mno kwako. Akainuka, akala, akanywa, akaenda katika nguvu za chakula hicho siku arobaini mchana na usiku hata akafika Horebu (Sinai), mlima wa Mungu. Akafika kunako pango, akalala ndani yake. Na tazama, Neno la Bwana likamjia, naye akamwambia, Unafanya nini hapa, Eliya? Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu, waiondoe. Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. Ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika mavazi yake, akatoka, akasimama mlangoni mwa pango. Na tazama, sauti ikamjia, kusema, Unafanya nini hapa, Eliya?” {3T 289.2}

Eliya alipaswa kumtumaini Mungu, aliyekuwa amemuonya ni wakati gani wa kukimbia na mahali gani pa kupata hifadhi kutoka kwa chuki ya Yezebeli, mahali palipo salama kutokana na utafutaji wa bidii wa Ahabu. Bwana hakuwa amemwonya wakati huu kwamba akimbie. Hakuwa amemngojea Bwana azungumze naye. Alisogea kwa kasi. Angekuwa amesubiri kwa imani na uvumilivu, Mungu angemkinga mja Wake na angempa ushindi mwingine wa ishara katika Israeli kwa kutuma mapigo yake juu ya Yezebeli. {3T 290.1}

Akiwa amechoka na akiwa ameanguka chini, Eliya anakaa chini kupumzika. Amekata tamaa na akiwa na hisia za kunung'unika. Anasema. “Ee Bwana, uiondoe roho yangu; kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu.” Anahisi kuwa maisha

si ya kutamanika tena. Alitarajia kuwa baada ya kuonesha ishara ya nguvu ya Mungu mbele ya Israeli wangekuwa wakweli na waaminifu kwa Mungu. Alitarajia kwamba Yezebeli hangekuwa na ushawishi tena juu ya akili ya Ahabu na kwamba kungekuwa na mapinduzi ya jumla katika ufalme wa Israeli. Na wakati ujumbe wa kutisha kutoka kwa Yezebeli ulipofikishwa kwake, alisahau kwamba Mungu alikuwa ni Yule Yule Mwenye nguvu zote na Mwenye huruma Mungu yule yule aliyemwomba moto ukatoka mbinguni, ukaja, na aliyemwomba mvua, ikawa. Mungu alikuwa amejibu kila ombi; lakini Eliya bado ni mkimbizi aliyekimbia mbali na nyumba za watu, na asiyetamani kamwe kumtazama mwanadamu tena. {3T 290.2}

Je, Mungu anamwangaliaje mtumishi Wake anayepitia mateso? Je! humwacha kwa sababu hali ya kukata tamaa na kukosa matumaini imemkumba? Lo, hapana. Eliya alianguka chini kutokana na kuvunjika moyo. Siku nzima alikuwa amejitaabisha bila chakula. Wakati akiliongoza gari la Ahab, akikimbia mbele ya gari hilo hadi kwenye lango la jiji, alikuwa na ujasiri. Alikuwa na matumaini makubwa kwamba Israeli kama taifa itarudi kwenye utii wake kwa Mungu na kurejeshwa katika upendeleo na neema yake. Lakini mara nyingi matokeo yanayofuatia baada ya kuinuka kwa imani na mafanikio yanayoacha alama na utukufu na ushindi, vilikuwa vinamuelemea Eliya. Alinyanyuliwa hadi juu ya Pisga, na baadaye kujikuta akidhalilishwa hadi bonde la chini kabisa kwa imani na hisia. Lakini jicho la Mungu lilikuwa bado juu ya mtumishi Wake. Hakupunguza kumpenda wakati alipohisi kuvunjika moyo na aliyeachwa na Mungu na mwanadamu kuliko wakati ule, alipomjibu kwa maombi yake, wakati moto ulipowaka kutoka mbinguni ukiangaza Karmeli. {3T 290.3}

Wale ambao hawajabeba majukumu mazito, au ambao hawajajizoeza kujihisi vibaya, hawawezi kuelewa hisia za Eliya na hawatakuwa tayari kumpa kujali, upendo na huruma zao nyororo anazostahili. Mungu anajua na anaweza kusoma uchungu wa moyo ulio chini ya majaribu na mzozo mkali. {3T 291.1}

Wakati Eliya analala chini ya mti wa mretemu, mguso laini na sauti ya kupendeza ilimwamsha. Anainuka mara moja kwa hofu yake, kama anayetaka kukimbia, kama anayefuatiliwa na adui anayetafuta maisha yake na ambaye sasa amekwishampata. Lakini katika uso wa huruma wa upendo uliomwinamia haoni uso wa adui, lakini wa rafiki. Malaika ametumwa na chakula kutoka mbinguni kumsaidia mtumishi mwaminifu wa Mungu. Sauti yake inamwambia Eliya: "Amka ule." Baada ya Eliya kutumia kiburudisho cha chakula kilichoandaliwa kwa ajili yake, alilala tena. Mara ya pili malaika wa Mungu anahudumia mahitaji ya Eliya. Anamgusa mtu aliyechoka, na kwa huruma anamwambia: "Amka ule; kwa sababu safari ni kubwa kwako." Eliya aliimarishwa na akaendelea na safari yake hadi Horebu. Alikuwa jangwani. Usiku alikaa katika pango kwa usalama/ulinzi kutoka kwa wanyama wa porini. {3T 291.2}

Hapa Mungu, kupitia mmoja wa malaika Zake, alikutana na Eliya, na kumwuliza: "Je, unafanya nini hapa, Eliya? "Nilikutuma kwenye kijito cha Keriti, nilikutuma kwa mjane wa Sarepta, nilikutuma Samaria na ujumbe kwa Ahabu, lakini ni nani aliyekutuma safari hii ndefu kwenda jangwani? Na Je, una ujumbe gani hapa? Eliya anaomboleza uchungu wa roho yake kwa Bwana: "Akasema, Nimekuwa na wivu sana kwa ajili ya Bwana, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano Yako, na kuziangusha madhabahu Zako; na kuwaua manabii wako kwa upanga; na mimi, hata mimi peke yangu, nimebaki; nao wanatafuta uhai wangu, ili wauondoe. Akasema toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunjavunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. Ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika mavazi yake, akatoka, akasimama mlangoni mwa pango. Na tazama, sauti ikamjia, kusema, Unafanya nini hapa, Eliya? Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano Yako, na kuzivunja madhabahu Zako, na kuwaua manabii Wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu waiondoe. {3T 291.3}

Kisha Bwana anajidhihirisha Mwenyewe kwa Eliya, akimwonesha kuwa tumaini la utulivu na kumtegemea Mungu kwa uthabiti kutampatia msaada wa haraka wakati wa uhitaji. {3T 292.1}

Nimeoneshwa kuwa mume wangu amekosea kwa kukata tamaa na kwa kutomwamini Mungu. Mara kwa mara Mungu amejifunua kwake kwa ushahidi wa ajabu wa utunzaji Wake, upendo, na nguvu. Lakini wakati alipoona kuwa masilahi yake na wivu wake kwa Mungu na kwa kazi yake havijaeleweka au havijathaminiwa, kwa nyakati fulani amevunjika moyo na kukata tamaa. Mungu amempa mume wangu na mimi kazi maalum na muhimu ya kufanya katika kusudi Lake, kukemea na kushauri watu Wake. Tunapoona maonyo yetu yanahafifishwa, tunatukanwa na kulipwa kwa chuki badala ya huruma, basi mara nyingi tumeruhusu imani yetu na tumaini kwa Mungu wa Israeli viende kombo; na, kama Eliya, tumevunjika moyo na kukata tamaa. Hapa kumekuwa na kosa kubwa katika maisha ya mume wangu - kukata tamaa kwake kwa sababu ya ndugu zake kumeleta majaribu juu yake badala ya kumsaidia. Na ndugu zake wanapoona, huzuni na kukata tamaa kwa mume wangu, kama athari za kutokuamini kwao na ukosefu wa huruma, wengine huwa tayari kushangilia/kushinda juu yake na kuchukua faida ya hali yake ya kukata tamaa, na kuhisi kwamba, baada ya yote, Mungu hawezi kuwa na Ndugu White au vinginevyo asingeonesha udhaifu katika mwelekeo huu. Ninarejelea kazi ya Eliya na hali ya kuvujwa moyo na kukata tamaa. Eliya, ingawa alikuwa nabii wa Mungu, alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi.

Wanadamu tuna udhaifu wa hisia za mauti tunazopaswa kushindana nazo. Lakini kama tutamtegemea Mungu, Yeye Hatatuacha kamwe wala kututelekeza. Katika hali zote, sisi tunaweza kuwa na imani thabiti kwa Mungu, kwamba hatatuacha wala kututelekeza wakati tunatunza uadilifu wetu. {3T 292.2}

Mume wangu anaweza kupata ujasiri katika shida yake, kwamba ana Baba wa mbinguni Mwenye huruma anayesoma nia na kuelewa madhumuni ya roho. Wale ambao wanasimama mbele ya vita, na ambao wamefanywa upya na Roho wa Mungu kumfanyia kazi maalum, mara nyingi watahisi athari wakati shinikizo linapoondolewa, na kukata tamaa wakati mwingine kunaweza kuwashinikiza sana na kutikisa imani ya kishujaa zaidi na kudhoofisha akili zilizodumu imara kwa muda mrefu. Mungu anaelewa udhaifu wetu wote. Anaweza kuhurumia na kupenda wakati mioyo ya wanadamu yaweza kuwa migumu kama jiwe. Kusubiri kwa subira na kumtumaini Mungu wakati kila kitu kinaonekana giza ni somo ambalo lazima mume wangu ajifunze kikamilifu. Mungu hatamwangusha katika uadilifu wake. {3T 293.1}

SURA YA 28

MUSA NA HARUNI

Haruni alifariki na kuzikwa katika mlima Hori. Musa, ndugu yake Haruni, na Eleazari mwanawe wakamsindikiza kwenda mlimani. Musa alipewa jukumu chungu la kumvua mavazi yake ya kikuhani kaka yake Haruni na kumvalisha mpwa wake Eleazari, kwa maana Mungu alikuwa amesema Kijana wake angemrithi Haruni kazi ya ukuhani. Musa na Eleazari walishuhudia kifo cha Haruni; Na Musa akamzika huko

mlimani. Tukio hili katika mlima Hori linarudisha akili zetu kwenye matukio mengine ya kushangaza maishani mwa Haruni. {3T 293.2}

Haruni alikuwa mtu mwenye tabia nzuri, ambaye Mungu alimchagua kusimama na Musa na kuzungumza kwa ajili yake; kwa kifupi, kuwa kinywa cha Musa. Mungu angeweza kumchagua Haruni kama kiongozi; lakini Yeye anayeijua mioyo, anayeelewa tabia, alijua kuwa Haruni alikuwa mwepesi kupindishwa kukiwa na mkazo au shinikizo na hakuwa na ujasiri wa kusimama na kutetea haki na maadili bila kujali matokeo. Shauku ya Haruni ya kuridhisha watu wakati mwingine ilimwongoza kufanya makosa makubwa. Mara nyingi alikubaliana na kusihi kwao, kwa kufanya hivyo alimvunjia Mungu heshima. Ni ukosefu huo huo wa uthabiti wa mamlaka kwenye familia yake ulisababisha kifo cha wanawe wawili wa kiume. Haruni alikuwa mashuhuri kwa uchaji-Mungu na utumishi wa kazi, lakini alipuuzia kuadabisha familia yake. Badala ya kufanya kazi hiyo ya kuelimisha watoto wake wamheshimu Mungu na wawe na kicho aliwaruhusu kufuata njia zao. Hakuwaadabisha kuheshimu mamlaka ya wazazi na kujikana nafsi, ila alikubaliana na matwaka yao. Baba ndiye alikuwa mtawala sahihi wa familia yake maadamu alikuwa bado hai, mamlaka yake yasingekoma, hata baada ya watoto wake kuwa watu wazima na kuwa na familia zao wenyewe. Mungu Mwenyewe alikuwa mfalme wa taifa, Naye alidai utii na heshima kutoka kwa watu. {3T293.3}

Utaratibu na mafanikio ya ufalme yanategemea utaratibu mzuri wa kanisa. Na ustawi, maelewano, na mpangilio wa kanisa ulitegemea utaratibu mzuri na nidhamu kamili ya familia. Mungu huadhibu wazazi wasio waaminifu, ambao amewapa jukumu la kudumisha kanuni ya sheria za serikali za wazazi, ambazo ndiyo msingi wa nidhamu ya kanisa na ustawi wa taifa. Mtoto mmoja asiye na nidhamu mara nyingi ameharibu amani na maelewano ya kanisa, na kuchochea taifa kunung'unika na kuasi. Kwa mkazo mzito kabisa Bwana amewapa watoto wajibu wa kuwaheshimu wazazi wao. Na kwa upande mwingine, Yeye anahitaji wazazi wawafundishe watoto wao kwa bidii bila kukoma, kuwaelimisha yahusuyo usimamizi wa madai ya sheria Yake Mungu na kuwafundisha katika ufahamu na hofu ya Mungu. Amri hizi ambazo Mungu aliwapa Wayahudi kwa hafla kubwa zenye kicho, zina uzito sawa kwa wazazi Wakristo wa leo. Wale ambao wanapuuzia nuru na maagizo ambayo Mungu ametoa katika Neno kuhusiana na kufundisha Watoto na kuziamuru nyumba zao baada yao- Mwanzo 18, watatoa hesabu ya kutisha. Kosa la jinai la Haruni kule kupuuzia kuwaadabisha Watoto wake wawe na heshima, kuwaamuru na hili lilisababisha kifo cha wanawe {3T 294.1}

Mungu alimtofautisha Haruni kwa kumchagua yeye na kizazi chake cha watoto wa kiume kwenye ukuhani. Wanawe walihudumu kwenye ofisi takatifu, Nadabu na Abihu walishindwa kuheshimu amri ya Mungu ya kutotoa moto usio mtakatifu juu ya vyetezo vyake na ubani mbele Zake. Mungu alikuwa amewakataza, kuleta moto

mgeni kwenye vyetezo kwani kungeleta maumivu ya kifo kwa watoto hao {3T 295.1}

Hapa tunaona nidhamu isiyo na mashiko (legevu). Hawa wana wa Haruni walionekana kutofundishwa kuheshimu amri za baba yao, walipuuzia mamlaka ya wazazi na hawakugundua umuhimu wa kufuata maagizo ya Mungu kwa umakini. Wakiendekeza hamu yao ya kunywa kileo, na walipo kuwa chini ya ushawishi wa kichocheo cha pombe, akili yao ikiwa imetanda ukungu, hawakuweza kutambua tofauti kati ya vitu vitakatifu na vile vya kawaida. Walienenda kinyume na mwongozo wa wazi wa Mungu, na kumvunjia heshima Bwana kwa kuleta moto wa kawaida badala ya moto mtakatifu [moto mgeni]. Mungu aliwazuru kwa ghadhabu Yake; moto ukatoka mbele Zake na kuwaangamiza. {3T 295.2}

Haruni aliubeba uchungu wake mkali kwa uvumilivu na unyenyekevu. Huzuni na uchungu mkali uliikumba roho yake. Dhamira yake iliguswa kwa kupuuzia jukumu. Alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu sana, alikuwa akifanya upatanisho wa dhambi za watu. Alikuwa kuhani wa nyumba yake, lakini alikuwa ameendelea kuchukuliana na upumbavu wa watoto wake-akipuuzia au kuruka upumbavu huu. Alikuwa amepuuzia jukumu lake la kuwalea na kuwafundisha utii, kujikana nafsi na kuheshimu mamlaka ya wazazi. Kwa hisia za kujiridhisha vibaya, hakufanikiwa kufinyanga tabia za watoto wake ziwe zenye kicho kwa vitu ambavyo ni vya milele. Haruni, kama wazazi wengi Wakristo walivyo leo alikuwa na upofu, hakuona kwamba mapenzi yake yaliyowekwa vibaya na kuwaendekeza watoto wake kwa makosa lilikuwa jambo baya lililowaanda watoto hawa kwa ghadhabu fulani ya Mungu na kwa ghadhabu Yake aliwaangamiza hao watoto. Wakati Haruni alishindwa kutumia mamlaka yake, haki ya Mungu iliamka dhidi yao. Haruni ilibidi ajifunze kwamba upole wake, bila kuwa na uthabiti wa kuweka kizuizi kama mzazi na huruma isiyo ya busara kwa wanawe ulikuwa ukatili usio na kipimo. Mungu alichukua haki mikononi Mwake Mwenyewe na kuwaangamiza wana wa Haruni. {3T 295.3}

Mungu alipomwita Musa apande mlimani, alikuwa na siku sita kabla ya kupokelewa ndani ya wingu, ili awe mbele ya uwepo wa Mungu wa karibu. Kilele cha mlima kilikuwa kimeangaziwa nuru ya utukufu wa Mungu. Na japo wana wa Israeli walikuwa wameona utukufu huu kwa macho yao, kutokuamini ilikuwa kawaida yao kiasi kwamba walianza kunung'unika kwa kutoridhika kwa sababu Musa hakuwepo nao. Wakati utukufu wa Mungu ulionesha uwepo Wake mtakatifu juu ya mlima, na kiongozi wao alikuwa akiongea kwa karibu sana na Mungu, wao wangepaswa kujitakasa kwa kujipeleleza mioyo yao, kujinyenyekeza, na kuwa na hofu ya Mungu. Mungu alikuwa amemwacha Haruni na Huri kuchukua nafasi ya Musa. Kwa kutokuwepo kwake Musa, watu walipaswa kushauriana na kujadiliana na hawa watu wawili walioteuliwa na Mungu. {3T 296.1}

Mapungufu ya Haruni yakaonekana hapa kama kiongozi au gavana wa Israeli. Watu walimshambulia wakisema awatengenezee miungu ya kuwaongoza mbele yao kurudi Misri. Hii ilikuwa fursa kwa Haruni kuonesha imani yake na kutoyumbishwa katika kumwamini Mungu, na kwa uthabiti/ujasiri na msimamo kukabiliana na matakwa ya watu inavyopaswa. Lakini tabia yake ya kupendeza watu kwa kuruhusu wafanye wanachotaka ndiyo iliyomwongoza kumvunjia Mungu heshima. Aliwaomba walete mapambo yao kwake, naye akawatengenezea ndama wa dhahabu, na akatangaza mbele za watu: "Hii ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa kutoka nchi ya Misri." Na kwa huyu mungu asiye na utashi/maana alitengeneza madhabahu na kutangaza kesho yake siku kuu kwa Bwana. Vizuizi vyote vilionekana vimeondolewa kutoka kwa watu. Walitoa sadaka za kuteketezwa kwa ndama wa dhahabu, na hali ya kutokuwa na umakini, ya michezo-michezo ikawaingia. Walijiingiza kwenye ghasia za aibu na ulevi; walikula, wakanywa, na wakainuka kucheza. {3T 296.2}

Zilikuwa zimepita wiki chache tu tangu walipokuwa wamefanya agano adhimu na Mungu kwa sauti Yake. Walikuwa wamesikiliza Maneno ya sheria ya Mungu, yaliyozungumzwa kwa utukufu wa kutisha kutoka mlima wa Sinai, katikati ya ngurumo za radi na umeme na tetemeko la ardhi Kutoka 20. Walikuwa wamesikia matangazo kutoka midomoni mwa Mungu Mwenyewe: "Mimi ni Bwana Mungu wako, niliyekutoa kutoka nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa usiwe na miungu mingine isipokuwa Mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao. "{3T 296.3}

Haruni na wanawe walikuwa wameinuliwa kwa kuitwa mlimani ili kushuhudia utukufu wa Mungu. "Wakamwona Mungu wa Israeli; chini ya miguu Yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti samawi, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi Wake" {3T 297.1}

Mungu alikuwa amemteua Nadabu na Abihu kwa kazi takatifu zaidi, kwa hivyo alikuwa amewaheshimu kwa namna ya ajabu. Aliwapa mtazamo wa utukufu Wake bora, kwamba madhari ambayo walikuwa wameshuhudia mlimani ingekaa nao na kuwafaa zaidi katika ubora wa huduma Yake, na kumpa Yeye kipaumbele cha heshima za watu ambayo ingesaidia watu kuwa na maoni yaliyo wazi kuhusu tabia Yake na kuamsha ndani yao heshima na utii unaomstahili na heshima kwa matakwa Yake yote. {3T 297.2}

Kabla Musa hajawaacha watu wake kwenda mlimani, aliwasomea Maneno ya agano ambalo Mungu alifanya pamoja nao, nao kwa sauti moja walijibu: "Yote ambayo Bwana amesema tutayafanya na kuwa watiifu." Jinsi dhambi ya Haruni ilivyokuwa kubwa kwa kiasi gani? Ilikuwa ya kumkasirisha Mungu kwa kiasi gani? {3T 297.3}

Wakati Musa alipokuwa akipokea sheria za Mungu mlimani, Bwana alimjulisha dhambi ya uasi ya wana Israeli na akamwomba Musa amruhusu ili aende kuwaangamiza. Lakini Musa alifanya maombezi mbele za Mungu kwa ajili ya watu hawa. Ingawa Musa alikuwa mtu mpole na mnyenyekevu zaidi ya wote walioishi kabla yake, lakini wakati masilahi ya watu ambao Mungu alikuwa amemteua kuwa kiongozi yalipokuwa hatarini, alipoteza woga wake wa asili na kwa kutokata tamaa akiwa na nia moja na ujasiri wa ajabu, akamsihi Mungu kwa niaba ya Israeli. Hakukubaliana na wazo la Mungu la kuangamiza watu Wake, japo Mungu aliahidi kwamba atakapowaangamiza, atampandisha Musa na kumwinulia kizazi cha watu bora kuliko Israeli. {3T 297.4}

Musa alishinda. Mungu alikubali ombi lake la dhati la kutowafuta watu Wake usoni pa nchi. Musa akayatwaa yale mawe mawili ya agano, sheria ya amri kumi, na akashuka kutoka mlimani. Roho ya machafuko, sherehe za ulevi za kucheza za wana wa Israeli zilifika masikioni mwake muda mfupi kabla ya kufika kambini. Alipoona ibada yao ya sanamu, na kwamba walikuwa wamevunja njia za Maneno ya agano kwa kiasi kikubwa, huzuni kuu ya kufadhaisha na alitekewa na ghadhabu iliyomwingia kuhusiana na ibada yao ya sanamu. Kuchanganyikiwa na aibu kwa ajili yao kukamwingia, na hapo ndipo alitupa mawe yale ya amri kumi na akayavunja. Kama vile ambavyo walikuwa wamevunja agano lao na Mungu, Kwa kuvunja yale mawe mawili, Musa alikuwa ameashiria kwao vile vile pia Mungu Naye alikuwa amevunja agano nao. Mawe ambayo yaliandikwa sheria za Mungu yalikuwa yamevunjwa. {3T 298.1}

Haruni na tabia yake ya kushawishiwa kirahisi, na kujisalimisha [amiable, mild, pleasing], isiyo na ukali na yenye kupendeza, alitafuta kumpatanisha Musa na watu, kana kwamba hakuna dhambi kubwa iliyo kuwa imetendwa na watu ambayo Musa anaichukulia kwa uzito mkubwa hivyo. Musa aliuliza kwa hasira akamwambia Haruni watu hawa wamekufanya nini hata ukaleta dhambi hii kuu juu yao? Haruni akasema, hasira ya bwana wangu isiwake, wewe unawajua watu hawa, ya kuwa wamejielekeza kwa mabaya. Maana waliniambia, katufanyie miungu, itakayo kwenda mbele yetu, kwa maana mtu huyo Musa, aliyetutoa katika nchi ya Misri, hatujui yaliyompata. Nikawaambia, mtu yeyote aliye na dhahabu na aivunje; basi wakanipa, nami nikaitupa ndani ya moto, akatoka ndama huyu."Haruni alitaka Musa afikirie kwamba muujiza wa ajabu umetokea nao umebadilisha mapambo yao ya dhahabu na kuwa umbo la ndama. Hakumwelezea Musa kwamba yeye pamoja na wafanya kazi wengine, walikuwa wametengeneza sanamu hii {3T 298.2}

Haruni alikuwa anafikiria kuwa Musa alikuwa mgumu katika kusikiliza matakwa ya watu. Alifikiria kwamba Musa angepunguza uthabiti wake, na apunguze kutoa maamuzi wakati mwingine na hivyo angepatana na watu na kuridhisha matakwa yao, angekuwa na shida chache, na hivyo kungekuwepo na amani na maelewano zaidi katika kambi ya Israeli. Haruni hapa alikuwa anajaribu sera hii mpya. Alitumia hulka yake ya asili kwa kuafikiana na matakwa ya watu, akitaka kuondoa kutoridhika kwao na kuhifadhi mapenzi yao mema, na hivyo kuzuia uasi, ambao alidhani ungekuja ikiwa hangefanya walivyotaka. Lakini kama Haruni angesimama imara bila kuyumba kwa ajili ya Mungu; kama angejibu pendekezo la watu la kuwatengenezea miungu ya kuwaongoza kuelekea Misri kwa ghadhabu ya haki na kuchukizwa inayostahili pendekezo hilo la watu; endapo angeweza kuwakumbusha vitisho vya sinai, pale ambapo Mungu alikuwa amenena sheria Zake katika utukufu na ukuu wa ajabu; kama angewakumbusha juu ya agano lao zito na Mungu kwamba wangepaswa kutii yote aliyokuwa amewaamuru; kama angewaambia kwamba hatakubali kujitolea maisha yake, kwa kukubaliana na matakwa yao, angekuwa na ushawishi kwa watu na kuzuia uasi mbaya wa imani. Pale Musa alipokuwa hayupo alipaswa kutumia ushawishi wake katika njia sahihi, alipaswa kusimama kwa uthabiti kama Musa, na kuwazuia watu wasifuate njia ya dhambi, ushawishi uliegemea upande usiofaa. Alikuwa hana nguvu kwenye ushawishi utakaomletea Mungu heshima kwa kushika sheria Yake takatifu. Bali kwenye upande usiofaa alikuwa na ushawishi mkubwa.
Aliwaongoza tu watu nao, wakamtii. {3T 298.3}

Haruni alipochukua hatua ya kwanza mbaya, roho ambayo ilikuwa imewashawishi watu ilimwingia, na hii ndiyo ilimwongoza na kumwamrisha kama jemedari wa jeshi, na watu walikuwa na umoja na kutii. Hapa Haruni alitoa idhini iliyopelekea kutenda dhambi mbaya zaidi, kwa vile ilikuwa rahisi kwake kusimama kuliko kutetea haki. Alipoondoka kutoka kwenye uadilifu kwa kuwapa watu ruhusa katika dhambi, alionekana kuhamasishwa na uamuzi huo, akawa na bidii na usongo mpya. Woga wake ulionekana kutoweka ghafla na akawa na ari/bidii ambayo hakuionesha katika kusimamia na kutetea heshima ya Mungu dhidi ya makosa ya kufanya dhahabu kwenye sura ya ndama. Aliamuru madhabahu ijengwe, kwa uhakikisho wa makusudi bora zaidi, aliwatangazia watu kwamba kesho kutakuwa na siku kuu kwa Bwana. Wapiga tarumbeta walichukua maneno kutoka kinywani mwa Haruni na wakatoa matangazo kutoka kwa kikundi kwenda hadi kikundi cha majeshi ya Israeli. 3T 299.1

Uhakikisho potofu wa Haruni uliolekea njia yenye uovu, ulimpa Haruni mvuto mkubwa kwa watu kuliko ule ambao Musa alikuwa nao katika kuwaongoza watu kwenye njia sahihi na katika kutuliza uasi. Ni upofu wa jinsi gani uliokuwa umemjia

Haruni kwa kuweka mbele ya watu kuwa- nuru ndiyo giza na giza ndiyo nuru! Ni dhana mbaya kiasi gani aliyochukua kwa kutangaza siku kuu ya Bwana juu ya ibada yao ya sanamu iliyokuwa na mfano wa dhahabu! Hapa zinaonekana nguvu alizo nazo Shetani juu ya akili ambazo hazijatawaliwa kabisa na Roho wa Mungu. Shetani alikuwa amesimamisha bendera yake katikati ya Israeli, nayo ilitukuzwa kama bendera ya Mungu. {3T 300.1}

"Haya," Haruni alisema bila kusita wala aibu, " hii ndiyo miungu yako, Israeli, iliyokuleta kutoka nchi ya Misri. "Haruni aliwashawishi wana wa Israeli kwenda mbali zaidi katika ibada ya sanamu kuliko ilivyokuwa imengia akilini mwao. Hawakufadhaishwa tena, au kusumbuliwa moyo kwamba pengine utukufu unaowaka kama moto juu ya mlima ungeweza kummaliza kiongozi wao Musa. Waliona walikuwa na jemedari aliyewafaa, na walikuwa tayari kufanya chochote ambacho aliwapendekezea. Walimtolea dhabihu mungu wao wa dhahabu; walitoa sadaka na kujitolea kwa anasa, vurugu, na ulevi. Walikuwa wameshaamua kwenye akili zao wenyewe kwamba matatizo mengi yaliyokuwepo sababu yake haikuwa dhambi walizofanya nyikani; ila shida kubwa kati ya zote, ilikuwa ni kiongozi wao. Hakuwa mtu aliyestahili kuongoza. Alikuwa mtu mgumu, asiyepinda hata kidogo na daima akiwakumbusha dhambi zao, akiwatahadharisha, akiwakemea, na kuwatishia kuhusu hasira ya Mungu. Mpangilio mpya wa mambo ulikuwa umefika, na wakimfurahia Haruni na nafsi zao wenyewe walifikiri: Laiti Musa angekuwa mpole na asiye mgumu kama Haruni, kungekuwa na amani na maelewano kwa jinsi gani katika kambi ya Israeli! hawakujali tena kama Musa angerudi lini kutoka mlimani au asingerudi. {3T 300.2}

Musa alipoona ibada ya sanamu ya Israeli na hasira yake ilipowaka sana kwa aibu yao ya kumsahau Mungu, aliyatupa yale mawe yenye amri kumi, Haruni alisimama kwa upole, akichukulia ukosoaji wa Musa kwa uvumilivu wenye sifa. Watu walipendezwa na roho nzuri ya Haruni na walichukizwa na harara ya Musa. Lakini Mungu haoni kama vile mwanadamu aonavyo. Yeye Hakulaani ukali na ghadhabu ya Musa dhidi ya uasi wa sheria za msingi za Mungu. {3T 300.3}

Kiongozi haswa, au jemedari anachukua msimamo wake kwa Mungu. Ametoka moja kwa moja kwenye uwepo wa Bwana, ambako alimsihi Bwana aondoe ghadhabu Yake kutoka kwa watu Wake waliomkosea. Na sasa ana kazi nyingine ya kufanya kama mhudumu wa Mungu, kutunza heshima ya Mungu mbele ya watu Wake, na kufanya waone dhambi ni dhambi, na haki ni haki. Ana kazi ya kufanya katika kuondoa ushawishi mbaya wa Haruni. "Ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. Na hao wana wa Lawi wakafanya kama

vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu-3,000. Musa akasema, jiwekeni wakfu kwa Bwana leo, naam, kila mtu juu ya mwanawe na juu ya ndugu yake; ili awape baraka leo."{3T 301.1}

Hapa Musa anafafanua kujitoa wakfu kwa uhalisi kwa kumtii Mungu, kusimama katika kuitetea haki na kuonesha utayari wa kutenda kusudi la Mungu katika majukumu yasiyofurahisha kabisa, kwa kufanya hivyo alionesha kuwa madai ya Mungu ni juu ya madai ya marafiki au maisha ya jamaa wa karibu. Wana wa Lawi walijiweka wakfu kwa Mungu kusimamia haki Yake dhidi ya uhalifu na dhambi. {3T 301.2}

Haruni na Musa wote walitenda dhambi kwa kutompa Mungu utukufu na heshima kwenye maji ya Meriba. Wao wote wawili walikuwa wamechoshwa na kukasirishwa na malalamiko ya kila wakati ya wana wa Israeli, wakati ambapo Mungu alipotaka kuonesha kwa rehema Zake utukufu Wake, kulainisha na kuongoza mioyo yao kutubu, Musa na Haruni walidai walikuwa nguvu za kuwapasulia mwamba. “Sikieni sasa, enyi waasi; je! tuwatokezee maji katika mwamba huu?” Hii ilikuwa nafasi nzuri sana/dhahabu, ya kumtukuza Bwana Mungu katikati yao, kwa kuwaonesha uvumilivu wa Mungu na huruma yake nyingi kwao. Walikuwa wamewanung'unikia Musa na Haruni kwa sababu hawakuweza kupata maji. Musa na Haruni walichukua manung'uniko haya kama majaribu makubwa na wakajivunjia heshima na kisha wakasahau kuwa watu walikuwa wakimhuzunisha Mungu na wala sio wao. Ni Mungu ambaye walikuwa wakimtendea dhambi na kumvunjia heshima, na wala sio wale ambao walikuwa wameteuliwa na Mungu kusimamia kazi Yake. Walikuwa wakimtukana Rafiki yao mkubwa kwa kuwatupia Musa na Haruni dhiki zao; walikuwa wakinung'unikia uongozi, majaliwa au utoaji wa Mungu. {3T 301.3}

Dhambi ya hawa viongozi wa pekee ilikuwa kubwa. Maisha yao yangeweza kupendeza hadi mwisho. Walikuwa wametukuzwa sana na Bwana; lakini Mungu hatoi udhuru wa dhambi za wale walio katika nafasi zilizoinuka kwa urahisi zaidi ukilinganisha na wale walio katika nafasi za hali ya chini na unyenyekevu Watu wengi wanaojiita wakristo huwaangalia wale ambao hawawakemei au kulaani ubaya kama wacha Mungu na Wakristo kweli, ila wale ambao husimama kwa ujasiri kwa kutetea haki, na wasiokubaliana na ushawishi usiotakaswa, huwaona kana kwamba hawana uchaji wa Mungu na roho ya Kikristo. {3T 302.1}

Wale wanaosimamia kutetea heshima ya Mungu na kudumisha usafi wa Kweli kwa gharama yoyote watapata majaribu mengi, kama alivyopata mwokozi wetu kule jangwani kwenye majaribu. Isipokuwa wale wenye tabia za kufuata mkumbo kirahisi, wasio na ujasiri wa kulaani makosa, kwa kukaa kimya wakati wa ushawishi wa mwovu watakuwa mikononi mwa shetani. Unahitajika kusimama katika kutetea haki dhidi ya shinikizo lolote, hivyo kuepuka maumivu mengi ya moyo na wasiwasi

mwingi, ambavyo hupelekea kupoteza zawadi kubwa sana, na hata ile ya kupoteza roho yako na za wengine. Wale wanaoafikiana na Mungu, na kupitia kwa imani Kwake hupokea nguvu dhidi ya kupinga uovu na kuitetea haki, daima watakuwa na mizozo mikali, kila mara watalazamika kubaki peke yao. Lakini ushindi wa thamani utakuwa pamoja na Mungu kuwa tegemeo lao. Neema Yake itakuwa nguvu kwao. Umakini wao wa maadili kwa Mungu utakuwa wa thamani, wazi, na nguvu zao za maadili zitaweza kustahimili ushawishi mbaya. Uadilifu wao, utakuwa kama wa Musa, wenye tabia safi zaidi. {3T 302.2}

Roho ya upole na unyenyekevu ya Haruni, pamoja na shauku yake ya kuwafurahisha watu na kufuata mkumbo, kwa kuwapendeza watu, ilimpofusha macho yake kuona dhambi zao na uzito mkubwa wa uhalifu ambao alikuwa ameuidhinisha. Kitendo chake cha kuchochea watu kwa uovu na dhambi katika Israeli kilisababisha vifo vya wanaume elfu tatu. Kuna utofauti kati ya tabia ya Haruni na tabia ya Musa. Baada ya Musa kuwathibithishia watu kwamba hawawezi kumdharau Mungu bila kujipatia adhabu; baada ya kuwaonesha hasira za Mungu kwa sababu ya dhambi zao, kwa kutoa amri mbaya ya kuua marafiki au jamaa ambao waliendelea katika uasi wao; baada ya kazi ya haki ya kuondoa ghadhabu ya Mungu, bila kujali hisia zao za huruma kwa marafiki wapendwa na jamaa ambao waliendelea kuwa wagumu katika uasi wao-- baada ya haya, Musa alikuwa tayari kwa kazi zingine. Alithibitisha kuwa nani alikuwa rafiki wa Kweli wa Mungu na watu. {3T 303.1}

"Hata asubuhi yake Musa akawaambia watu, mmetenda dhambi kuu; na sasa nitakwenda juu kwa Bwana, labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi yenu. Musa akarejea kwa Bwana akasema, Aa! watu hawa wametenda dhambi kuu wamejifanyia miungu ya dhahabu. Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao- na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika. Bwana akamwambia Musa, mtu yeyote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu Changu. Basi sasa uende ukawaongoze watu hawa mpaka mahali pale; tazama, Malaika wangu atakutangulia; pamoja na hayo siku nitakayowajilia nitawapatiliza kwa ajili ya dhambi yao. Bwana akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama, ambayo Haruni aliifanya." {3T 303.2}

Musa alimwomba Mungu kwa niaba ya wana Israeli wenye dhambi. Hakujaribu kuipunguza dhambi yao kuwa ndogo mbele za Mungu; hakutoa udhuru wa dhambi. Alikiri waziwazi kuwa walikuwa wametenda dhambi, dhambi kubwa na walikuwa wamejifanyia miungu ya dhahabu. Halafu anapoteza upole wake na kisha maslahi ya Israeli yanaunganishwa kwa karibu kiasi cha kupata ujasiri wa kuja kwa Mungu na kumwomba awasamehe watu Wake. Na ikiwa dhambi yao ni kubwa sana kiasi kwamba Mungu hawezi kuwasamehe, ikiwa ni lazima majina yao yatolewe kutoka kitabuni Mwake, anamsihi Bwana afute jina lake pia. Wakati Bwana anafanya upya ahadi Yake kwa Musa, kwamba Malaika Wake ataenda mbele yake na kuwaongoza

watu kwenda nchi ya ahadi, Musa alijua kwamba ombi lake lilikuwa limekubaliwa. Lakini Bwana alimhakikishia Musa kwamba ikiwa angekasirika na kuwazuru watu kwa makosa yao, hakika angewaadhibu kwa dhambi hii mbaya pia. Lakini endapo wangetii tangu sasa, Yeye angeifuta dhambi yao hii kubwa katika kitabu Chake. 3T 303.3

SURA YA 29

KWA MCHUNGAJI KIJANA NA MKEWE

Mpendwa ndugu na Dada A: Kwa miezi kadhaa nimehisi kuwa wakati umefika wa kuwaandikia mambo kadhaa yanayowahusu ambayo Bwana alipendezwa kunionesha miaka kadhaa iliyopita. Kesi zenu zilionеshwa kwangu kuhusiana na wale ambao walionekana kuhitaji kufanya kazi kwa ajili yao wenyewe ili waweze kufaa katika kazi ya kuwasilisha Kweli. Nilionеshwa kuwa nyote wawili mlikuwa na upungufu wa sifa muhimu na ikiwa hizi hazitapatikana, kufaa kwenu na wokovu wa roho zenu wenyewe utakuwa hatarini. Mna makosa katika tabia zenu ambayo ni muhimu sana yasahihishwe. Mkipuuza kushika kazi hii kwa uthabiti na bidii, makosa haya yatazidi kuwa makubwa na kulemaza ushawishi wenu, njia za utumishi na kazi ya Mungu, na mwishowe kusababisha kutengwa kwenu na kazi ya kuhubiri Kweli, ambayo ninyi mnaipenda sana. {3T 304.1}

Katika maono niliyopewa kuhusiana na B, nilionеshwa kuwa hali ya tabia isiyo nzuri kabisa. Alikuwa hajaadabishwa, na hulka/jazba yake haikuwa imethibitiwa. Alikuwa amemeruhusiwa kujifanyia anachotaka na mara nyingi alijifanyia alivyopenda. Alikuwa na upungufu wa kicho kwa Mungu na heshima kwa watu. Alikuwa na roho kaidi yenye ubinafsi isiyotaka kujisalimisha lakini yenye fikira dhaifu na zisizo sahihi kuhusiana na kuwashukuru wale ambao wanasaidia kwa bidii. Alikuwa mbinafsi mno {3T 304.2}

Nilionеshwa roho ya kujitegemea. dhamira thabiti ya kutotaka kuelekezwa, kukosa kicho na heshima ikiweka alama katika tabia yako Dada A. Ikiwa hutakuwa mwangalifu na kushinda kasoro hizi katika tabia yako hakika utashindwa kukaa na Kristo katika kiti Chake cha enzi. {3T 305.1}

Kuhusiana na Ndugu A, nilionеshwa kuwa mambo mengi yaliyotajwa kwenye Shuhuda kwa B yalihusika nawe pia. Nilielekezwa kwenye maisha yako ya nyuma. Nikaona tokea utoto umekuwa ukijiamini, mkaidi, na mwenye kutaka kufanya mapenzi yako mwenyewe, na ukifuata akili yako mwenyewe. Una roho ya kujitegemea mwenyewe, na hivyo imekuwa vigumu sana kwako kumsikiliza au kujisalimisha kwa mtu yeyote. Wakati ulipowajibika kuacha njia yako unayofuata na kufuata matakwa ya wengine, ungefanya mambo utakavyo na kwa pupa. Umejiona kwamba una uwezo wa kufikiri na kutenda unavyotaka mwenyewe, umeukubali Ukweli na kuupenda, nao umekufanyia mambo mengi mema, lakini haujaleta mabadiliko yote yaliyo muhimu na ya lazima kwenye ukamilifu wa tabia ya Kikristo. Wakati ulipoanza kufanya kazi ya Mungu ulikuwa na unyenyekevu zaidi na ulikuwa tayari kushauriwa na kuongozwa. Lakini ulipoanza kufanikiwa kwa kiwango fulani, kujiamini kwako kuliongezeka, na unyenyekevu wako ukapungua na ukanza kujitegemea mwenyewe zaidi. {3T 305.2}

Ulipoangalia kazi ya Ndugu na Dada White uliona kwamba kuna sehemu ambazo ungeweza kufanya vizuri zaidi kuliko wao. Hisia za kuwa dhidi yao zimependwa na kuthaminiwa moyoni mwako. Kwa asili wewe ni mwenye hisia za wasiwasi, na ukafiri. Jinsi unavyoendelea kuiona kazi yao, na kusikia maonyo wanayowapa wale ambao walikuwa wamekosea, umejiuliza kama wewe binafsi ungezichukuliaje shuhuda hizo nyofu. Uliamua kwamba hungeweza kuzipokea, na ukaanza kujiimarisha kupinga njia ambazo wanafanya kazi hiyo, na hivyo ukafungua mlango moyoni mwako wa tuhuma kwao (kuwashuku), mashaka, na wivu kwa kazi yao. {3T 305.3}

Ulikuwa na hisia za ubaguzi dhidi ya kazi yao. Ukaangalia, na ukasikiliza, na ukakusanya kila ulichoweza, na kuwanenea mabaya. Kwa vile Mungu amekupa kiwango fulani cha mafanikio, ulianza kuweka uzoefu wako mdogo na kulinganisha na kiwango cha kazi cha Ndugu White. Ukajidanganya moyoni kwamba, ungekuwa mahali pake ungeweza kufanya kazi hiyo vizuri zaidi kuliko yeye. Ukaanza kuchukua uzoefu wako mfupi na huduma zako na kuzilinganisha na huduma za ndugu White na kujitanua. Ukajidanganya kuwa laiti ungekuwa katika nafasi yake ungefanya kwa ubora zaidi kuliko yeye. Ukaanza kujiona bora machoni pako mwenyewe ukafikiria kwamba maarifa uliyonayo ni mapana na ya thamani kuliko ilivyo kweli. Kama ungekuwa tu na sehemu ya miaka ya uzoefu katika mazingira halisi ya kazi, shuguli zake, mifadhaiko yake, na kubeba mzigo katika kazi ambayo Ndugu White amekuwa akiifanya, ungeweza kuelewa vizuri kazi yake na kuwa tayari zaidi kumwonea huruma katika kazi yake, badala ya kunung'unika na kushuku na kumwonea wivu. {3T 306.1}

Wapaswa kuwa na wivu kwako mwenyewe kuhusiana na kituo chako cha kazi ili usije ukashindwa kufanya kazi ya kukubalika mbele za Mungu, na kisha ukashindwa kuheshimu kazi ya Mungu unapotumika. Unapaswa uwe na kujidhili kwa roho, jisikie: “Ni nani basi aliyemkamilifu kufanya kazi hiyo?" Kinachowafanya ninyi wawili kuwa tayari kukosoa na kunena mabaya kuhusu kazi ya Ndugu White ni kwa sababu mnafahamu machache sana kuhusu kazi hiyo. Ni wachache sana mlio na mzigo halisi unaowauma kwenye mioyo yenu, na hivyo mna uchungu mdogo sana wenye uhalisia ambao unagusa mioyo yenu katika kazi ya Mungu, mmekuwa na fadhaa kidogo na kubeba dhiki chache sana kwa ajili ya wengine, kiasi kwamba hamko tayari kuthamini kazi yake kuliko ambavyo mtoto wa miaka kumi angethamini utunzaji, mifadhaiko, na taabu za kazi za kuchosha za babaye mwenye kulemewa na mzigo. Mtoto huyu anaweza kutembea akiwa na furaha moyoni kwa sababu hana uzoefu wa mzigo wa babaye mwenye uchovu. Anaweza kushangaa kuhusu hofu na mahangaiko ya babaye, ambayo yanaonekana kuwa siyo ya lazima kwake; lakini miaka ya uzoefu inapoongezwa maishani basi atajua na kubeba uhalisia wa mizigo yake, ndipo ataweza kutazama nyuma katika maisha ya baba yake na kuelewa kile ambacho kilikuwa fumbo la kushangaza kwenye ujana wake; kwani uzoefu mchungu umempa maarifa. {3T 306.2}

Nilioneshwa kuwa uko katika hatari ya kuondoka kwenye unyenyekevu wa kazi na kujiweka juu ya kilele. Unaona kuwa hauhitaji maonyo na ushauri, na lugha ya moyo wako ni: "Ninao uwezo wa kuhukumu, kufanya maamuzi, kutofautisha vitu, na kujua kati ya jema na baya, sitaki haki zangu zikiukwe. Hakuna mtu atakayeniamrisha. Ninao uwezo wa kufanya mipango yangu ya utendaji [plan of action]. Nafanya vizuri kama mtu mwingine yeyote tu. Mungu Yuko pamoja nami na ananipa mafanikio katika juhudi zangu. Je, ni nani aliye na mamlaka ya kuniingilia? "maneno haya nilikusikia ukiyasema suala lako lilipokuwa likipita mbele yangu, hukusema haya kwa yeyote, lakini ilikuwa kana kwamba unajizungumzia mwenyewe. Malaika wangu aliyenihudumia alirudia maneno haya akiwasonda ninyi wawili: " Nawahakikishieni kwamba msipobadilika na kuwa kama watoto wadogo, kamwe hamtaingia katika ufalme wa mbinguni. Kwa hivyo mtu yeyote anayejinyenyekeza akawa kama huyu mtoto, huyo ndiye aliye mkuu kuliko wote katika ufalme wa mbinguni."{3T 306.3}

Niliona kuwa nguvu ya watoto wa Mungu iko katika unyenyekevu wao. Pale wanapojiona ni dhaifu machoni pao wenyewe, Yesu atakuwa nguvu na haki yao, na Mungu atafanikisha kazi zao. Nilioneshwa kuwa Mungu atamthibitisha Ndugu A. Angempa kiwango cha ustawi; na ikiwa atastahimili jaribio, na ikiwa atazitumia baraka za Mungu na uwakili mzuri, bila kujitwalia heshima kwake na kutoinuliwa juu, na kuwa na ubinafsi, na kujiamini mwenyewe, Bwana angeendeleza baraka Zake kwa ajili ya Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake Mwenyewe. {3T 307.1}

Nimeona, Ndugu A, kuwa ulikuwa katika hatari kubwa ya kuinuliwa, na kujiona mwenye haki, uliyejitosheleza na ukijisikia kuwa u tajiri na kutohitaji kitu chochote. Isipokuwa utajilinda kwa hivi vidokezo, Bwana atakuruhusu uendelee hivyo mpaka udhaifu wako udhihirishwe wazi wazi kwa wote na uletwe katika nafasi ambazo utajaribiwa sana endapo wengine hawatakuchukulia katika mwangaza unaojiona kuwa upo umejiona kwamba umeinuliwa na una uwezo ulio juu. Nilioneshwa kuwa haukuwa tayari kabisa kubeba ustawi na mafanikio makubwa, Uongofu kamili peke yake utafanya kazi inyohitajika katika suala lako. {3T 307.2}

Nimeoneshwa kuwa nyote wawili ni wachoyo/wabinafsi kwa asili. Mko hatarini daima, msipojihusisha kwa kuwa waangalifu kwa yale mnayofikiria na kutenda. Mtaweka mipango inayowaridhisha ninyi, bila ya kufikiria jinsi wengine watakavyoathiriwa kwa njia hasi. Mna tabia ya kutekeleza mawazo na mipango yenu bila ya kuheshimu maoni au hisia za wengine. Wote wawili mwapaswa kujifunza kuwaheshimu wengine na kuwa na adabu/uungwana. {3T 308.1}

Ndugu A, umefikiri kuwa kazi yako ni ya umuhimu mkubwa sana, kiasi kwamba huwezi kushuka chini na kujihusisha na kazi za nyumbani. Hupendi majukumu haya. Uliyapuuzia ukiwa mdogo/kijana. Lakini majukumu haya madogo ambayo unayapuuzia ni ya muhimu katika kujenga tabia iliyo bora. {3T 308.2}

Nimeoneshwa kuwa wachungaji wetu kwa jumla wana mapungufu ya utumishi katika familia ambazo wanazitembelea. Wengine hutumia bongo zao kusoma muda wote kwa sababu wanapenda kufanya vile. Hawaoni kuwa Mungu amepanga kwamba wachungaji hawa wachungaji wawe mbaraka pia katika familia za wenyeji wao, ila wengi huweka akili zao kwenye vitabu na hujifungia kutoka kwenye hizo familia wala wasizungumze na hao wenyeji juu ya mada za Ukweli. Masilahi ya kidini katika familia hayatajwi sana. Haya ni makosa. Wachungaji ambao hawana mzigo au shughuli inayohusiana na uchapishaji, na wale ambao hawana mahangaiko na shuguli nyingi za makanisa yote, hawapaswi kufikiri kuwa kazi yao ni ngumu kupita kiasi. Wanapaswa kuwa na shauku kubwa, kujali kwa undani zile familia wanazo zitembelea; hawapaswi kuhisi kwamba ni lazima wabembelezwe na kusubiriwa na kutumikiwa wakati ambapo hawana malipo ya kuwapa watu hao. Kuna jukumu lililopo katika familia za Kikristo kuwakaribisha wahudumu wa Kristo na pia kuna jukumu kwa wachungaji wengi wanafikiria kwamba wangepewa kipaumbele kuliko watu wengine na kusubiriwa na wanajeruhiwa mara kwa mara na utumishi wao hulemazwa kwa kudekezwa kama wanyama wa kufugwa ambao ni vipenzi kwa watu (pets). {3T 308.3)

Ndugu na Dada A, wakati mko kati ya ndugu zenu mara kwa mara mmekuwa na mazoea ya kufanya mipango inayokupendeza/inayokubaliwa nanyi wenyewe na mnachukua hatua ya kuvuta usikivu wa watu kwenu, bila kufikiria faida, usumbufu au hasara za wengine. Mna hatari ya kujifanya ninyi kuwa ndio wa muhimu (kiini). Mmepata usikivu na umakini wa wengine wakati ambapo, kwa faida ya roho zenu na zile za wengine, mngeweka umakini kwa wenyeji wenu mnaowatembelea kwenye majumba yao. Mkifanya hivyo mngekuwa na mvuto mkubwa zaidi, na mngebarikiwa kwa kusaidia kuongoa roho kwa kuzileta kwenye Kweli. {3T 309.1}

Ndugu A, una uwezo wa kuwasilisha Ukweli kwa wengine. Una akili ya uchunguzi/udadisi; lakini una mapungufu makubwa katika tabia yako, ambayo nimeyaorodhesha na ambayo ni lazima uyashinde. Unapuuza staha/uungwana na maadili yanayohusu kujali na uungwana kwa sababu unajifikiria mwenyewe sana kiasi kwamba hauelewi usikivu wa mambo haya madogo kuwa ni wajibu wako. Mungu asingependa uwape wengine mzigo wakati wewe unapuuzia kuona na kufanya vile ambavyo mtu anapaswa kuvifanya. Haimpunguzii hadhi mchungaji anayeshughulikia injili kukusanya kuni na kuchota maji wakati ambapo inahitajika au kufanya shughuli ambazo zinahitajika kufanywa katika familia ya wenyeji wako ambao wanafanya maisha yako yawe na furaha. Kwa kutoyaona majukumu haya muhimu na kuboresha nafasi za kuyafanya, unajinyima baraka za kweli na pia unawanyima wengine mema ambayo ni upendeleo na baraka kwao kupokea toka kwako {3T 309.2}

Baadhi ya wachungaji wetu hawana mazoezi ya mwili ya kutosha yanayoendana na utumiaji wa bongo zao. Matokeo yake, wanasumbuliwa na unyonge. Hakuna

sababu nzuri kwa afya za wachungaji wanaotekeleza majukumu ya kawaida, afya zao kuwa mbaya. Akili zao hazielemewi kila wakati na mashuguli yenye wasiwasi na majukumu muhimu na mazito ya taasisi zilizopo miongoni mwetu. Niliona kuwa hakuna sababu ya maana ya kushindwa katika kipindi hiki muhimu cha misheni na kazi ikiwa watatilia umakini nuru ambayo Mungu amewapa kuhusiana na jinsi ya kufanya kazi, jinsi ya kufanya mazoezi, na wakiweka umakini unaotakiwa kuhusu lishe yao {3T 309.3}

Baadhi ya wachungaji wetu hula chakula kingi sana na kisha hawafanyi mazoezi ya kutosha kuyeyusha chakula na kutoa uchafu ambao hujilimbikiza kwenye mfumo. Wanakula na kisha wanatumia wakati wao mwingi kukaa chini kusoma, kujifunza, au kuandika, wakati sehemu ya wakati wao inapaswa kuelekezwa kwa mpangilio fulani kwenye kazi za mikono. Wahubiri wetu hakika wataharibikiwa na afya wasipokuwa waangalifu katika kujaza matumbo yao na chakula kingi, hata kile kilicho na afya si vizuri kikiwa kingi. Niliona kwamba ninyi, Ndugu na Dada A, Nyote wawili mlikuwa hatarini na kipengele hiki. Ulaji wa kupita kiasi unazuia mtiririko mzuri wa mawazo na maneno, na kiwango fulani cha hisia ni muhimu sana katika kusisitiza Ukweli kwenye moyo wa msikiaji injili. Kutokuwa na kiasi kuhusiana na kuridhisha hamu ya chakula hufunika na kufunga akili, na kuzifanya ziwe butu kwa mionjo mitakatifu ya Roho. Nguvu za akili na maadili ya baadhi ya wahubiri wetu zimedhoofishwa na ulaji usiofaa na kutofanya mazoezi ya mwili. Wale walio na hamu ya kula chakula kingi hawapaswi kuendekeza tamaa yao ya chakula, ila wafanye mazoezi ya kujinyima na kukana nafsi zao, nao watakuwa na mbaraka wakutunza misuli iliyo na nguvu na akili zisizosumbuliwa kupita kiasi. Ulaji wa kupindukia hufanya mawazo ya mtu kuwa duni kwa kuchukua nguvu zinazotoka kwenye mifumo mingine (Mfumo wa ubongo) ili zikafanye kazi ya kuyeyusha chakula tumboni. {3T 310.1}

Kushindwa kwa wachungaji wetu kuvipa viungo vyao mazoezi yanayotakiwa hufanya viungo vichakae, na vingine viwe dhaifu kwa kutotumiwa inavyopasa. Ikiwa kiungo kimoja au misuli vitaachwa kitumike sana, kile kinachotumiwa zaidi lazima kichoshwe zaidi na kudhoofishwa sana. Kila kitivo cha akili, na kila msuli, kina kazi tofauti na vyote kwa usawa vinahitajika kufanyiwa mazoezi ili viendelee ili viendelee na kuendelea kuwa na nguvu yake ya afya. Kila kiungo cha mwili kina kazi yake maalumu katika mwili wa binadamu, kila gurudumu la mashine ya mwili lazima liwe hai na likifanya kazi vyema, vitivo vyote vinahusiana na kimoja kinaathiri kingine na vyote vinahitaji kupata mazoezi ili viweze kuendelezwa vyema. {3T 310.2}

Ndugu na Dada A, hakuna hata mmoja kati yenu ninyi wawili anayefurahia kazi za mikono na zile nyumbani. Wote mnahitaji kukuza upendo kwa kazi ambazo ni majukumu ya kawaida ya maisha [practical life skills]. Elimu hii ni muhimu kwa afya na itaongeza manufaa kwenye utumishi wako. Unawaza mno kuhusu kile

utakachokula. Usiguse vile ambavyo vitafanya damu yako iwe duni; nyote wawili mna ugonjwa wa kuvimba unaotokana na maambukizo (pengine kifua kikuu). {3T 310.3}

Ndugu A, kupenda kwako kujisomea na kutopenda kazi za mikono, wakati unazungumza na kulifanyisha mazoezi koo lako, hufanya iwe rahisi kwako kupata magonjwa ya koo na mapafu. Unapaswa kuwa mwangalifu na kisha usizungumze kwa haraka, usichoshe sehemu ya juu ya viungo vya sauti kwani utavichakaza na kuvikera na itakuwa msingi wa kujiletea ugonjwa. Kitendo cha kutoa sauti kinapaswa kuja kutoka kwenye misuli ya tumbo. Mapafu na koo viwe ni mfereji tu wa kuleta sauti lakini havipaswi kufanya kazi yote. {3T 311.1}

Nilioneshwa kuwa mtindo wa kula ambao wewe na mke wako mnautumiam utawaletea magonjwa, ambayo yakiingia, itakuwa vigumu kuyaondoa. Mnaweza mkachuliana nayo kwa miaka mingi, na wala msioneshe dalili za kuumwa, lakini athari/matokeo hufuata matendo hayo kwa hakika. Mungu hatafanya muujiza wa kutunza afya na maisha yenu. Lazima mle na kusoma na kufanya kazi kwa uelewa, mkiifuata dhamira iliyoelimishwa. Wahubiri wetu wawe na matengenezo ya dhati, na wasifanye matengenezo kwa sababu wengine hufanya hivyo, bali wafanye kutokana na kanuni, kwa kulitii Neno la Mungu. Mungu ametupa nuru kubwa juu ya matengenezo ya afya, ambayo anataka sote tuheshimu. Yeye Hatumii nuru ili ikataliwe au kupuuzwa na watu Wake bila kuleta matokeo yenye mateso. {3T 311.2}

Waanzilishi wa Kazi

Nilioneshwa nyote wawili hamjitambui. Ikiwa Mungu angemwachilia adui juu yenu, kama alivyo mfanyia mtumishi wake Ayubu, asingepata ndani yenu ile roho ya uadilifu iliyo kuwa thabiti kama aliyokutwa nayo mtumishi Wake Ayubu, badala yake angepata roho ya manung'uniko na ya kutokuamini. Ungekuwa huko Battle Creek wakati wa ugonjwa wa mume wangu, wakati wa migogoro ya ndugu na dada zetu huko, wakati shetani alikuwa na nguvu maalumu juu yao huko, nyote wawili mngekuwa mmekunywa kwa kina roho yao ya wivu na ya kutafuta makosa kwa wengine. Ungekuwa miongoni mwa wale wenye jazba, kama wengine, ya kumfanya awe, mgonjwa, aliyepooza, na mkosaji kwa Neno. {3T 311.3}

Una tabia ya kuhesabu mapungufu yako kuwa madogo kwa kukuza na kushugulikia makosa ambayo unafikiri yapo kwa Ndugu na Dada White; na ungekuwa na fursa kama ile waliyokuwa nayo watu wa Battle Creek, ungepania kwenda mbali zaidi kuliko baadhi yao waliofanya vita vyao viovu dhidi yetu; kwa maana unayo imani kidogo na heshima ndogo kuliko wengine wao, na usingepunguza kuiheshimu kazi na wito wetu. {3T 312.1}

Nilioneshwa kuwa, licha ya wewe kuwa na uzoefu wa kuhuzunisha wa mfano wa wengine ambao wamechanganyikiwa na walinung'unika na kutulaumu na kutuonea

wivu, utashindwa kuonywa na mifano yao, na Mungu atajaribu uaminifu wako na kufunua siri za mioyo yenu. Kutokuamini kwako, tuhuma zako, na husuda yako zitafunuliwa, na udhaifu wako utawekwa wazi, ili uweze kuuona na kujielewa, ikiwa ungeamua kufanya hivyo. {3T 312.2}

Nilikuona ukisikiliza mazungumzo ya waume na wake, na nikaona kwamba ulifurahia kukusanya mitazamo na maoni yao ambayo ilikuwa miiba, kuhusiana na kazi zetu. Wengine walilaumu kwa jambo hili, na wengine wakatafuta lawama kuhusu jingine, kama miongoni mwa wana Israeli walivyonung'unika wakati Musa alikuwa kiongozi wao. Wengine walikuwa wakishutumu mwendo wetu, wakisema kwamba hatukuwa (tumeacha vitu vya dunia- hatukuwa wahafidhina/conservative) wa kizamani vile tulivyopaswa kuwa-; hatukuwapendeza watu kwa kadiri tulivyoweza; tulizungumza wazi wazi mno; tulikemea sana. Wengine walikuwa wakizungumza juu ya mavazi ya Dada White, wakichambua vitu visivyo vya maana- kama vile kuchuma nyasi [picking straw]. Wengine walikuwa wakionesha kutoridhika na njia ambayo Ndugu White alikuwa akifuata, na maneno yalikuwa yakipita kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, wakihoji mwenendo wao na kutafuta makosa. Malaika alisimama mbele ya watu hawa, ila wao hawakumwona, akiwa na bidii ya kuandika maneno yao katika kitabu ambacho kitafunguliwa mbele za Mungu na malaika. {3T 312.3}

Wengine wanatafuta kwa hamu kitu cha kulaumu kuhusiana na Ndugu na Dada White, ambao wamejipatia mvi sasa katika utumishi wao kazini mwa Mungu. Wengine huelezea maoni yao kwamba Ushuhuda wa mama White hauwezi kuaminika. Mambo haya yanapendwa na wale wasiojiweka wakfu ushuhuda wa maonyo umechunguza ubatili wao na kiburi, endapo wangeachwa wafanye watakavyo, wangeendelea tu kwenye mambo yote yahusianayo na fasheni na kiburi Mungu atawapa wote fursa ya kujithibitisha na kukuza tabia yao ya kweli. {3T 312.4}

Miaka kadhaa iliyopita niliona kwamba bado tutalazimika kukutana na roho ile ile iliyoibuka Paris, Maine, na ambayo haijaweza kupona kabisa. Imesinzia, ila haijafa. Mara kwa mara roho hii ya manung'uniko na uasi uliodhamiriwa imejitokeza kwa watu tofauti ambao waliwahi kutiwa chachu na roho hii mbaya ambayo imetufuata kwa miaka kadhaa. Dada A, roho hii imethaminiwa nawe kwa kiwango fulani, na imekuwa na ushawishi wa kuunda maoni na hisia zako. Uovu wa kujiona wewe ni mtakatifu umekuwa ukikua polepole akilini mwa ndugu C, na sasa sio rahisi kwake mwenyewe kuiondoa roho hii. Roho hiyo-hiyo iliyodhamiriwa ilimshikilia D na wengine huko Maine kwa udanganyifu wa ushabiki kwa muda mrefu, dhidi ya kila mvuto wa kuwaongoza kwenye Ukweli, nayo imekuwa na nguvu pamoja na ushawishi, wa kudanganya akili ya E katika ---, na ushawishi huo umekuathiri wewe. Ulikuwa na roho iliyotulia, yenye uthabiti, isiyotii, ambayo adui angeweza kuiathiri, na matokeo yale yale, ila kwa kiwango kikubwa zaidi,

yataonekana kwenye mvuto wako, kama kuna makosa, kama yalivyoonekana kwa dada E. {3T 313.1}

Hisia za tuhuma, wivu, na kutokuamini kwa miaka kadhaa zimekua zikipata nguvu akili mwako. Unachukia kuonywa. Kila kitu ni nyeti kwako, na huruma zako zinaibuka mara moja kwa mtu yeyote anayekemewa. Hizi sio hisia zilizotakaswa, na hazichochewi na Roho wa Mungu. Ndugu na Dada A, mimi nilioneshwa kuwa wakati roho hii ya kutafuta makosa na manung'uniko inapoendekezwa, kukuzwa ndani yako, wakati inadhihirishwa na chachu ya kutoridhika, wivu, na kutokuamini ambayo imelaani maisha ya E na mumewe na ikaonekana, tutakuwa na kazi ya kukabiliana nayo jinsi inavyopaswa na tusiipe nafasi; mpaka itakapokua, sasa hivi napaswa ninyamaze, kwani kuna wakati wa kusema na wakati wa kunyamanza. Niliona kwamba, endapo mafanikio ya kweli yangeambatana na ndugu A, basi pasipo yeye kuwa mtu alieongoka kikamilifu, yupo hatarini kupoteza roho yake. Hana heshima inayopaswa kuhusiana na nafasi na kazi za wengine; anajiona kuwa hakuna anayeweza kulinganishwa naye {3T 313.2}

Nilioneshwa kwamba majaribu yataendelea kuongezeka kuhusiana na kazi za Ndugu na Dada White. Kazi yetu ni kazi ya pekee, ina tabia tofauti na zingine zinazofanywa kwenye shamba la Bwana. Mungu hawaiti wachungaji ambao hufanya kazi katika Neno na mafundisho tu, na wala hatuiti sisi tufanye kazi yao. Kila mmoja wetu, kwa namna fulani ana kazi maalumu. Imempendeza Mungu Kunifunulia siri za maisha ya ndani na dhambi zilizofichwa za watu Wake. Wajibu huu usio wa kufurahisha umewekwa juu yangu, kukemea makosa na kufichua dhambi zilizofichwa. Wakati nilipolazimishwa na Roho wa Mungu kukemea dhambi ambazo wengine hawakujua zipo, imechochea hisia za asili katika mioyo ya wale ambao hawajatakaswa. Wakati wengine wamejinyenyekeza mioyo yao mbele ya Mungu, na kwa toba na kukiri wameacha dhambi zao, wengine wamehisi roho ya chuki zikiinuka ndani ya mioyo yao. Kiburi chao kimeumizwa wakati mwenendo wao umekemewa. Hupenda kufikiria mawazoni kwamba ni Dada White ndiye anayewaumiza, badala ya kushukru kwamba Mungu kwa rehema Zake, amezungumza nao kupitia chombo Chake dhaifu, kuwaonesha hatari zao na dhambi zao, zilizokuwa zimeonekana ili waachane nazo kabla ya kuchelewesha makosa hayo kusahihishwa. {3T 314.1}

Wengine wako tayari kuuliza: Je, ni nani aliyemwambia Dada White mambo haya? Hata wengine wameniuliza: Je! Kuna mtu alikuambia mambo haya? Ningeweza kuwajibu: Ndio; malaika wa Mungu amenena nami. Lakini wanachomaanisha ni: Je! Ndugu na dada wamekuwa wakikufunulia makosa yao kwako? Siku za usoni sitazichukulia kwa udogo hizi shuhuda ambazo Mungu amenipa, kwa kujaribu kutoa maelezo ili ni waridhishe watu hawa wenye akili finyu. Bali nitayachukulia maswali yote kama tusi/kashfa kwa Roho wa Mungu. Mungu ameona kuwa ninafaa kuwekwa kwenye sehemu niliyopo, ambayo hajampa mtu yoyote katika wale

tunaofanya nao kazi. Yeye Ameniwekea mzigo wa kukemea ambao hajampa mtu mwingine yeyote. Mume wangu amesimama kando yangu kudumisha Shuhuda na kutoa sauti yake kuendana na Shuhuda zenye karipio. Amelazimika kuchukua msimamo ulioamuliwa kupinga kutokuamini na uasi ambao umekuwa na ujasiri na ukaidi, ambao ungeweza kutupilia mbali ushuhuda wowote ambao ningeweza kutoa, kwa vile wale waliokemewa na Shuhuda walichomwa na kuhisi makaripio haya waliyopewa kwa kina. Hivi ndivyo vile Mungu alivyokuwa amepanga haswa. Yeye Alitaka Shuhuda iwachome mioyo. Ilikuwa ni lazima uwaingie moyoni kabla ya mioyo yao yenye kiburi kuachana na dhambi zao na ifishe mioyo yao na maisha yao kutoka kwenye uovu wote. {3T 314.2}

Katika kila hatua ambayo tumesonga mbele ambayo Mungu ametuongoza kuifanya, kumekuwa na zana tayari za shetani kati yetu, zikisimama nyuma yetu na kupendekeza mashaka na kutokuamini, na kutupa vizuizi katika njia yetu, kudhoofisha imani yetu na ujasiri. Tumelazimika kusimama kama mashujaa wa vita, tukiwa na utayari wa kusonga mbele na kupigana dhidi ya upinzani ulioletwa. Hii imefanya kazi yetu kuwa ngumu mara kumi kuliko ambavyo ingekuwa. Tumelazimika kusimama kwa uthabiti na kuwa imara kama mwamba. Ukakamavu huu umetafsiriwa kuwa ugumu wa moyo na utashi/nia. Mungu hakupanga kamwe tuyumbeyumbe, kwanza tuanze kwenda kulia na kisha kushoto, ili kuziridhisha akili za ndugu wasiojitoa wakfu. Yeye Alibuni kwamba njia yetu kuwa ya moja kwa moja. Mtu mmoja na mwingine wamekuja kwetu, wakidai kuwa wana mzigo mkubwa kwetu kwenda njia hii au ile, kinyume na vile nuru ya Mungu imetuelezea. Je! Ingekuwaje ikiwa tungeifuata hii mianga ya uongo na maoni ya mashabiki? Hakika watu wetu hawapaswi kutuamini endapo tutafanya hivi. Imebidi tusimame dede kama jiwe la gumegume na kisha tuendelee kufanya kazi na wajibu tuliopewa. {3T 315.1}

Wengine kati yetu wamekuwa tayari kuchukulia mambo kwa kupitiliza, wamepitiliza mipaka. Wameonekana kutokuwa na nanga. Hiyo imeumiza Kweli sana. Kuna wengine ambao wanaonekana kutokuwa na uwezo wa kuwa thabiti na uhakika, wa kwenda vitani endapo Mungu ataita askari waaminifu wapatikane kwenye vituo vya kazi. Kuna wale ambao hawapo tayari kumkimbiza adui watakapotakiwa kufanya vile na Mungu. Hawatafanya chochote mpaka wengine wapigane vita na kupata ushindi kwa ajili yao, na kisha wao watakuwa tayari kushiriki nyara. Je! Mungu anawezaje kuwategemea askari kama hao? Wanahesabiwa kama waoga katika kazi Yake. {3T 315.2}

Kundi hili, niliona, halikupata uzoefu wao wenyewe kuhusu vita dhidi ya dhambi na Shetani. Walielekea kuwa tayari kupigana na askari waaminifu wa Kristo kuliko kuwa dhidi ya Shetani na jeshi lake. Kama wangevaa silaha na kujitahidi kwenda vitani, wangepata uzoefu muhimu ambao ilikuwa fursa yao kuupata. Lakini hawakuwa na ujasiri wa kupigania haki, kujitosa katika mambo ya vita, na kuona

jinsi ya kumshambulia Shetani na kuchukua ngome yake. Wengine hawana mawazo ya kudiriki/kuthubutu katika kazi au kujitosa kwenye jambo lolote. Lakini ni lazima watu wathubutu, yabidi mtu fulani ajitose katika kazi hii; mtu anaweza kukutana na hatari katika hii kazi. Wale ambao hawatajitosa na kukumbana na hatari ya kukosolewa watasimama tayari kuwaangalia wale wanaobeba majukumu, na watakuwa tayari kutafuta mwanya wowote unaoonekana ili kuwakosoa makosa yao na kuwaumiza endapo wangeweza. Huu umekuwa uzoefu wa Ndugu na Dada White katika kazi zao. Shetani na jeshi lake wamejipanga dhidi yao, lakini haya hayakuwa yote; wakati wale ambao wangesimama karibu nao katika vita vya kazi walipowaona wakilemewa na kushinikizwa kupita kiasi, walisimama tayari kuungana na Shetani katika kazi yake ya kuwavunja moyo na kuwadhoofisha, na, ikiwezekana, wawafukuze mbali ili watoke shambani mwa Bwana. {3T 316.1}

Ndugu na Dada A, nimeoneshwa kuwa mlipokuwa mnasafiri, watu wamewaangalia kwa kuwaweka kwenye viti vya juu, na kuwapa heshima kubwa, na hali iliyo juu kuliko ilivyokuwa kwa faida yenu. Huna kawaida ya kuheshimu wengine ambao wamechukua mzigo wa kazi ambao Mungu aliwaagiza. Nyote wawili hampendi kujishugulisha hampendi mbadilishiwe au msumbuliwe na jambo lolote. Mnapenda vitu viende jinsi mnavyotaka kwa faida na faraja yenu yenu. Mna ubinafsi na maoni yaliyoinuliwa kuhusiana na mafanikio yenu. Hamjakuwa na shuguli zenye kufadhaisha na mizigo ya kubeba, na maamuzi muhimu ya kufanya yanayo husiana na maslahi ya kazi ya Mungu, hayo yameangukia upande wa mume wangu. Mungu amemfanya mume wangu kuwa mshauri kwa watu wake, kuwashauri na kuwaongoza vijana kama wewe, kama watoto wake katika Kweli. Vijana kama wewe mwenyewe, kama watoto katika Kweli. Na unapochukua nafasi hiyo ya unyenyekevu ambao ndiyo nafasi yako halisi ambayo yafaa uongozwe kuichukua, utakuwa tayari kushauriwa. Ni kwa sababu umekuwa ukibeba majukumu madogo na hivyo hauelewi ni kwanini Ndugu White anapaswa kuhisi kwa uzito kuhusu kazi hii kuliko wewe. Kuna tofauti hii tu kati yako na yeye katika suala hili. Yeye amewekeza miaka thelathini ya maisha yake bora kwa kazi ya Mungu, wakati wewe umewekeza miaka michache tu ya uzoefu na kwa ulinganifu, hakuna yoyote yaliyo magumu uliyoyapitia ukijilinganisha naye. {3T 316.2}

Baada ya waanzilishi wa kazi hii kufanya kazi kubwa ili kuandaa Ukweli na kuileta kazi hii mikononi mwako, wewe unaubeba na kwenda kufanya kazi, ukiwasilisha hoja zenye thamani ambazo wengine kwa shauku isiyoelezeka wamezichunguza kwa ajili yako. Ulipokuwa umepata maslahi mazuri na posho, mshahara wako wa kila wiki umekuwa wa uhakika, ukawa hauna sababu ya kufadhaika katika nyanja hii, ila waanzilishi/painia wa kazi hiyo walijinyima kwa kila aina-kujikana nafsi. Hawakuwa na uhakika wa chochote. Walimtegemea Mungu na wale wachache wenye mioyo ya Kweli waliopokea matunda ya kazi zao. Wakati wewe sasa una ndugu wanaokuonea huruma, wanaokutunza na kuonesha shukrani kwa kazi yako watenda kazi wa kwanza katika kazi hii walikuwa na watu wachache sana

waliokuwa karibu nao kuwasaidia. Wote wangeweza kuhesabiwa kwa dakika chache tu. Tulijua maana ya kuwa na njaa na kuteseka na baridi kwa kukosa mavazi yanayofaa. Tumesafiri usiku wote na kutembelea ndugu, kwa sababu hatukuwa na njia ya kulipia gharama za nyumba ya wageni. Tumesafiri maili nyingi kwa miguu, mara kadha wa kadha kwa sababu hatukuwa na pesa ya kukodi gari la farasi. Ni Jinsi gani Kweli ilivyokuwa ya thamani kwetu! Jinsi zilivyokuwa za thamani roho zilizonunuliwa kwa damu ya Kristo! {3T 317.1}

Hatuna malalamiko ya kusema kuhusu mateso yetu katika siku hizo ambazo tulikuwa na uhitaji na kuchanganyikiwa, ambazo zilifanya zoezi la imani liwe lazima kwetu. Zilikuwa siku zenye furaha zaidi katika maisha yetu. Hapo tulijifunza imani kama ya mtoto mdogo. Hapo, wakati wa shida tulimjaribu na kumthibitisha Bwana. Yeye Alikuwa faraja yetu. Yeye alikuwa kwetu kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi ya uchovu (jangwa). Ni bahati mbaya kwako, ndugu yangu, na kwa wachungaji walio vijana kwa ujumla, kwamba wewe na wao hamjapata uzoefu huo wa dhiki, majaribu na uhitaji uzoefu wa namna hiyo ambao ungekufaa zaidi ya nyumba au ardhi, dhahabu au fedha. {3T 318.1}

Tunapozungumzia uzoefu wetu wa zamani wa kazi nyingi na dhiki za umasikini, na kufanya kazi kwa mikono yetu ili tujisaidie kupata gharama za kuchapisha Ukweli tulipoanza kazi, baadhi ya vijana wachungaji wetu, vijana wenye uzoefu wa miaka michache kazini wanaonekana kukasirishwa na wanatuhukumu kwa kujivunia kazi zetu wenyewe. Sababu ya kufanya hivi, ni kwamba maisha yao yamekuwa huru sana kutokana masumbufu, uchovu na kazi ngumu, ufukara, na kujitolea kabisa kiasi ambacho hawajui jinsi ya kutuhurumia, na ulinganifu huo hawaukubali katika mafikara yao. Kuwaletea uzoefu wa wengine ambao ni tofauti kabisa na uzoefu wao wenyewe haifanyi utumishi wao kuonekana katika mwangaza mzuri kama ambavyo wangetaka iwe. {3T 318.2}

Tulipoanza kazi hii sote wawili tulikuwa na afya dhaifu. Mume wangu alikuwa na shida ya tumbo [dyspeptic]; na bado mara tatu kwa siku, kwa imani, tulimwomba Mungu atupe nguvu. Mume wangu aliingia kwenye shamba la nyasi za kulisha ng'ombe na mundu wake [sickle and hay], na kwa nguvu ambayo Mungu alimpa kama jibu la maombi yetu ya bidii, alilipwa kwa kukata nyasi, na tukapata pesa za kununulia mavazi safi ya kawaida, na pia gharama ya nauli yetu kwenda kwenye jimbo jingine la mbali kuwasilisha Ukweli kwa ndugu zetu. {3T 318.3}

Tunayo haki ya kurudi nyuma kuangalia yale yaliyopita, kama mtume Paulo alivyofanya. Nami nilipokuwa pamoja nanyi na kuhitaji sikumlemea mtu. Maana hao ndugu waliokuja kutoka Makedonia walinipa kadiri ya mahitaji yangu; nami katika mambo yote najilinda nafsi yangu nisiwaelemee hata kidogo; tena najilinda. Kama vile ile Kweli ya Kristo ilivyo ndani yangu, hakuna mtu atakayenifumba kinywa katika kujisifu huku, katika mipaka ya Akaya. "Kwa kurejelea mwisho wetu wa zamani, tunafanya himizo la mtume kwa Waebrania: "Kumbuka siku zile za

mwanzo baada ya kupokea mwanga, jinsi mlivyovumilia mapambano makali na mateso. Wakati mwingine mlitukanwa na kuteswa hadharani; wakati mwingine mlikuwa radhi kuungana na wale walioteswa hivyo."{3T 318.4}

Maisha yetu yamesukwa pamoja na kazi ya Mungu. Hatuna maslahi tofauti kando na kazi hii. Na tunapoona kazi ilivyoendelea kutoka kwenye mwanzo mdogo sana, ikiinuka polepole, lakini kwa uhakika kwa nguvu na mafanikio; tunapoona mafanikio ya kazi ambayo tumeshiriki kwa bidii, na kuteseka, na ilikaribia sana kwa maisha yetu kutolewa mhanga, ni nani anayeweza kutuzuia au kutukataza kujisifu kwetu kwa Mungu? Uzoefu wetu kwenye hii kazi ni wa thamani kwetu. Tumewekeza kila kitu ndani yake. {3T 319.1}

Musa alikuwa mwanadamu mpole zaidi kuliko wote walioishi; lakini, kwa sababu ya manung'uniko ya wana wa Israel, alilazimishwa kurudia kuleta mienendo yao ya dhambi baada ya kutoka Misri na kuthibitisha mwenendo wake kama kiongozi wao. Kabla tu ya kuondoka Israeli, wakati alikuwa anakaribia kufa, alirudia kusoma mbele yao mwenendo wao wa uasi na manung'uniko tokea walipotoka Misri, na jinsi shauku/maslahi yake na upendo wake kwao ulivyokuwa mkubwa na ukamwongoza kumsihi Mungu kwa niaba yao. Akawaelezea jinsi alivyomsihi sana Bwana amruhusu avuke mto Yordani na kuingia nchi ya ahadi; “Na Bwana alinikasirikia mimi kwa ajili yenu, akasema, wala wewe hutaingia humo. Musa akawasilisha mbele yao dhambi zao, na kuwaambia “Mmekuwa na uasi juu ya Bwana tokea siku nilipowajua ninyi……" Aliwasimulia ni mara ngapi yeye alikuwa amemsihi Mungu na kuinyenyekeza roho yake kwa uchungu kwa sababu ya dhambi zao. {3T 319.2}

Ilikuwa mpango wa Mungu kwamba Musa awakumbushe Israeli mara kwa mara juu ya makosa yao na uasi, ili wanyenyekeze mioyo yao mbele ya Mungu kwa ajili ya dhambi zao. Bwana hakutaka wasahau makosa na dhambi ambazo zilikuwa zimesababisha hasira Yake dhidi yao. Kurudia kutajwa kwa makosa yao, na rehema na wema wa Mungu kwao, ambavyo hawakuwa wamevithamini, kulikuwa hakukubaliani na hisia zao. Hata hivyo, Mungu aliagiza kwamba hili ni lazima lifanywe. {3T 320.1}

Nimeoneshwa kuwa vijana kama wewe, ambao mna uzoefu wa miaka michache, isio mikamilifu kuhusiana na Kweli ya leo, sio wale ambao Mungu atawaamini kubeba majukumu mazito na kuongoza kazi hii. Hawa watakuwa bado wachanga kwa kuchukua nafasi ambazo zitapingana na maamuzi na maoni ya wale wenye uzoefu uliokomaa, ambao maisha yao yamesukwa na kazi ya Mungu kwa miaka mingi ambayo inalingana na ile miaka ambayo wale wachungaji vijana wameishi na wale ambao wamekuwa sehemu ya kazi kuanzia kwenye mwanzo wake mdogo. Mungu hatachagua watu wenye uzoefu mdogo na wanaojiamini sana kuongoza katika kazi hii takatifu, na muhimu. Kuna mengi yaliyo hatarini hapa. Watu ambao wana uzoefu mdogo katika mateso, majaribu, upinzani na uvumilivu wa kuleta

kazi katika hali yake ya ustawi ilivyo leo, hawa watu lazima wawe na wivu kwa ajili yao wenyewe {3T 320.2}

Vijana ambao sasa wanashiriki katika kazi ya kuhubiri Ukweli lazima wakuze sifa za kiasi, staha, uungwana na unyenyekevu. Wanapaswa kuwa waangalifu jinsi wanavyoinuliwa, wasije wakapinduliwa. Watatoa hesabu kwa nuru wazi ya Ukweli ambayo inawaangazia sasa. Niliona kwamba Mungu amekasirika na tabia ya kunung'unika dhidi ya wale waliopigana vita vizito [mapambano mazito] kwa ajili yao nao walivumilia sana katika mianzo, wakati kazi ilikuwa kubwa na ngumu. {3T 320.3}

Wafanya kazi wenye ujuzi, wale ambao walifanya kazi zikiwa nzito na mizigo ilipokuwa ya kukandamiza wakiwa wachache tu kuibeba, Mungu hujali jambo hili; na ana wivu kwa wale ambao wameonekana kuwa waaminifu. Yeye Hafurahii wale ambao wapo tayari kutafuta makosa na kuwashutumu watumishi wa Mungu ambao wamejipatia mvi katika kuijenga kazi ya Ukweli wa leo. Lawama na manung'uniko yenu, vijana, hakika itasimama dhidi yenu katika siku ya hukumu. Kama Mungu hajaweka majukumu mazito juu yako, wewe usijichukulie nafasi isiyo yako na kutumainia uamuzi wako mwenyewe na kujichukulia majukumu ambayo hustahili. {3T 320.4}

Ndugu na dada mpendwa, mnapaswa kukuza ukeshaji, kuwa macho/umakini na unyenyekevu, na kuwa na bidii katika maombi. Kwa kadri mnavyoishi karibu na Mungu, ndivyo mtakavyobaini kwa wazi zaidi udhaifu wenu na hatari zenu. Mtazamo halisi wa sheria ya Mungu, utambuzi wazi wa kazi ya upatanisho wa Kristo, itawafanya mjitambue na kuwaonesha ni wapi mmeshindwa kuwa na tabia kamilifu ya kikristo. Kwa kifupi, ninyi nyote wawili mnahitaji uzoefu wa kila siku wa mapenzi ya Mungu yawahusuyo ninyi. Unapoona upungufu wako mkubwa wa kiroho utagundua kweli kwamba upotovu wa kibinadamu, kama ulivyooneshwa katika Neno la Mungu, ni hakika katika uzoefu wako. Ninyi nyote mna tabia ya kifarisayo, na mpo hatarini kubaki hapo kwa hiari na kwa hofu katika giza kuhusiana na hatari zenu na msimamo wenu wa Kweli mbele za Mungu. {3T 321.1}

Wote mnapaswa kujifunza kuhusu majukumu yanayohusiana nanyi katika hali mbalimbali na mahusiano ya maisha. Mmepuuzia majukumu yenu kwa Mungu na kwa wanadamu. Mnahitaji sana maarifa ya kujitambua wenyewe, hili ni muhimu sana. Ujinga wa mioyo yenu wenyewe unawaongoza kupuuzia uzoefu wa Kweli wa kila siku kuhusiana na maisha ya kimbingu Kwa kiwango fulani, unapuuza umuhimu wa kuwa na ushawishi wa Bwana/mbingu pamoja nawe kila wakati. Hii Ni muhimu sana katika kufanya kazi ya Mungu. Ikiwa utapuuza hili, na kulipitisha tu kwa kujiamini na kujitosheleza, utaishia kufanya makosa mengi sana-utaboronga mambo. Daima unahitaji kuthamini unyenyekevu wa akili na roho ya kumtegemea Mungu. Yeye ambaye anahisi udhaifu wake mwenyewe ataangalia juu ya pale alipo, na daima atahisi kuhitaji nguvu kutoka juu. Neema ya Mungu itamwongoza

kuonesha na kuthamini roho ya shukrani kila wakati. Yeye anayefahamu vyema udhaifu wake mwenyewe atajua kwamba ni neema isiyo na kifani ya Mungu peke yake tu, ndiyo ambayo itashinda juu ya uasi wa moyo. {3T 321.2}

Unahitaji kuvijua vipengele dhaifu na vyenye nguvu katika tabia yako, ili ulindwe kila wakati na usije ukajishughulisha na biashara, na kuchukua majukumu, ambayo Mungu hajawahi kukupa. Haupaswi kulinganisha matendo yako na kuyapima maisha kutokana na viwango vya kibinadamu, lakini kwa sheria inayotuwajibisha iliyofunuliwa katika Biblia. Mnayo kazi ya kuifanya kwa ajili yenu wenyewe, Ndugu na Dada A, ambayo hamkuwahi kuwazia kwamba hili lilikuwa muhimu. Kwa miaka mmekuwa mkiendekeza majaribu ya kuwa na wivu kuhusiana nasi na kazi yetu. Hii haimpendezi Mungu. Mnaweza kufikiria kuwa mnaamini shuhuda ambazo Mungu ametoa, lakini kutokuamini kwamba zinatoka kwa Mungu kumeanza kupata mwanya kwenu {3T 322.1}

Kazi yako, Ndugu A, ingekuwa na matokeo mazuri katika kugeuza roho kuelekea Kweli ikiwa ungekita kwenye vitendo na nadharia vile vile, kuwa na mambo hai, yenye vitendo katika moyo wako mwenyewe na kuyafanya katika maisha yako mwenyewe. Unahitaji kushikilia mbingu kwa uimara zaidi. Unategemea zaidi mazingara yako yalivyo. Ukiwa una washiriki wengi, unajiinua, na unatamani kuwahutubia hao. Lakini wakati mwingine washiriki wanapopungua, roho yako inanyongonyea, na unakuwa na ujasiri mdogo kufanya kazi. Hakika kuna upungufu wa namna fulani. Haujamshikilia Mungu kwa uthabiti wa kweli. Kati ya mafundisho ya Kristo ya Kweli yaliyo ya muhimu zaidi ni yale yaliyohubiriwa kwa mwanamke mmoja msamaria ambaye alikuja kuteka maji na akamkuta yeye akiwa amechoka, na kuketi kisimani. Chemchemi ya maji ya uzima ilikuwa ndani yake. Chemchemi ya maji ya uzima lazima iwe ndani yetu, ikirusha maji ili kuburudisha wale ambao wamewekwa chini ya ushawishi wetu. {3T 322.2}

Kristo aliwatafuta watu popote walipokuwepo- kwenye barabara za umma, kwenye nyumba za watu binafsi, katika masinagogi, na kando ya bahari. Alifanya kazi kwa bidii siku nzima, akihubiria umati na kuponya wagonjwa walioletwa Kwake; na mara kwa mara, baada ya kuwaaga watu ili warudi majumbani kwao kupumzika na kulala, alitumia usiku mzima kwa maombi, ili aje na nguvu mpya za kufanya kazi asubuhi yake. Ewe kaka na dada, ninyi hamjui lolote linalohusiana na uhalisia wa kujikana nafsi na kujitolea kwa ajili ya Kristo kuhusiana na Kweli. Lazima umtegemee Mungu Kwa ukamilifu zaidi na kupunguza kuzitegemea akili zako. Unahitaji kujificha kwa Mungu. {3T 322.3}

Ndugu unaelekea, kuwa mkali unapokaripiwa na kuja na hitimisho lako mwenyewe kuhusu watu binafsi, haswa ikiwa wamekatiza njiani pako; na, kulingana na maoni yako ya jambo hilo, wakati mwingine unashughulika nao kwa njia iliyo ya ukali bila ya kuwahurumia. Haukuwa mpole, mwenye kujali, mwenye moyo wa huruma, mwenye uungwana, kama Mfano wako ulivyo (Yesu). Unahitaji kuwa mwenye

huruma, mkarimu na mwema, unahitaji kuleta roho yako karibu na ushirika na Mungu kwa maombi ya dhati yaliyochanganywa na imani hai. Kila sala inayotolewa kwa imani humwinua mwombaji kuhusiana na mashaka ya kukatisha tamaa za kibinadamu. Maombi huleta nguvu na kuleta upya mapambano na nguvu za giza huchukuliana na majaribu kwa uvumilivu, na kuvumilia magumu kama askari wazuri wa Kristo. {3T 323.1}

Wakati unashauriana na mashaka na hofu zako, au kujaribu kutatua kila kitu ambacho haukioni kabla ya kuwa na imani, mashaka yako yatazidi kuongezeka. Unapokuja kwa Mungu, ukijisikia mnyonge na ukimtegemea, jinsi ulivyo, na kwa maombi ya unyenyekevu haja zako zijulikane kwake Yeye ambaye ana hekima isiyo na kikomo, anayeona kila kitu kwenye uumbaji na anaongoza kila kitu kwa mapenzi na Neno Lake, anaweza kusikia na kukujibu kilio chako, na atamulika nuru moyoni mwako na karibu nawe; kwa kupitia maombi ya dhati, roho yako iletwe na kuunganishwa na akili isiyo na kikomo. Unaweza usiwe na ushahidi wa kushangaza wakati uso Wake Mwokozi unakuinamia kwa huruma na upendo, lakini hivi ndivyo ilivyo. Unaweza usione mkono Wake ukikugusa, lakini mkono Wake upo juu yako kwa upendo na huruma zenye masikitiko {3T 323.2}

Mungu anawapenda nyote wawili na anahitaji kuwaokoa na wingi wa wokovu Wake. Lakini haipaswi kuwa katika njia mnayotaka ninyi, bali njia aliyoichagua Mungu Mwenyewe. Lazima uzingatie masharti yaliyomo kwenye Maandiko ya Kweli, na Mungu hakika atatimiza sehemu Yake kama vile kiti Chake cha enzi kilivyo hakika. Kwa sababu maonyo ambayo Mungu hutuma kwa watu Wake hudhalilisha asili ya kibinadamu, Ndugu usienende dhidi ya makaripio na maonyo haya. Unahitaji kufia nafsi kila siku, kupata uzoefu wa kusulubishwa kwa nafsi yako. {3T 323.3}

Kutokana na nuru ambayo Mungu amenipa katika maono, uovu na udanganyifu unaongezeka kati ya watu wa Mungu wanaodai kuzishika amri Zake. Macho ya kiroho ya kuona dhambi kama ilivyo, na kisha kuitoa nje ya kambi, yanapungua kati ya watu wa Mungu; na upofu wa kiroho unawajia haraka. Ushuhuda ulionyooka lazima ufufuliwe, na utawatenganisha wale kutoka Israeli wale ambao wamewahi kupigana vita na njia ambazo Mungu ameziweka ili kuzuia uovu/ufisadi usiingie kanisani. Uovu lazima uitwe uovu. Dhambi zenye kusikitisha lazima ziitwe kwa jina lake halisi. Watu wote wa Mungu wamkaribie na kuosha mavazi yao ya tabia katika damu ya Mwana-Kondoo. Kisha wataona dhambi zao katika nuru ya Kweli na watatambua jinsi zilivyo chukizo mbele za Mungu. {3T 324.1}

Wazazi wetu wa kwanza waliona ni jambo dogo walipojaribiwa kukiuka amri ya Mungu katika tendo moja dogo na kula zao la mti ambalo lilikuwa zuri kwa macho na la kupendeza kwa ladha. Kwa mkosaji hili lilikuwa tendo dogo tu, lakini liliharibu uaminifu wao kwa Mungu na kufungua mafuriko ya huzuni na hatia ambazo zimeudhuru ulimwengu hata leo. Ni nani awezaye kujua, wakati jaribu

linapokuja, kwamba matokeo mabaya yataingizwa kwa hatua moja tu mbaya ya haraka/harara! Usalama wetu pekee ni kulindwa na rehema ya Mungu kila wakati, na sio kutazama kwa macho yetu wenyewe ya kiroho na kisha mabaya tukayaita mazuri na mazuri mabaya. Bila kusita au mabishano, lazima tufunge na kulinda njia za moyoni dhidi ya uovu. {3T 324.2}

Itatugharimu juhudi kupata uzima wa milele. Ni kwa bidii tu, bidii zenye uvumilivu wa muda mrefu, nidhamu na vita vikali, tutashinda. Lakini tukivumilia na kunuia, katika Jina la Bwana Mshindi aliyeshinda kwa niaba yetu huko jangwani kwenye majaribu, na tushinde kama alivyoshinda, tutapata thawabu ya milele. Jitihada zetu, kujikana kwetu nafsi, kutokata kwetu tamaa, lazima vilingane na thamani ile idumuyo ya kile ambacho tunakitafuta. {3T 324.3}

Haupaswi kuruhusu kujihurumia kwako mwenyewe kukuzinge wewe na wengine kufanya makosa kwa sababu huoni kitu kilicho waziwazi kinachokushutumu. Mungu anaona; Yeye Anaweza kusoma nia na madhumuni ya moyo. Ninakusihi kwa Jina la Bwana wetu, ambaye ametuita na kutupa kazi tunazozifanya, toa mikono yako (usijihusishe) na utuache tufanye kazi ambayo Mungu ametupa kuifanya. Kaa na maneno yako ya huruma na sikitiko kwa wale ambao wanayastahili haswa, wale wanaosukumwa na Roho wa Mungu kuwaonesha watu Wake maovu yao na nyumba ya Israeli dhambi zao. Makosa na dhambi yanakumbatiwa katika siku hizi za mwisho kuliko Kweli na haki. Maaskari wa msalaba wa Kristo wanatakiwa sasa kuvaa silaha za Kikristo na kurudisha nyuma giza la maadili linalofurika duniani. {3T 325.1}

Mungu atawapa ninyi wawili ushindi wa thamani ikiwa mtajisalimisha kikamilifu Kwake na mwache neema Yake itawale na kutiisha mioyo yenu yenye kiburi. Kujihesabia haki kwako hakutafaulu lolote kwa Mungu. Hakuna kitu kinachopaswa kutapatapa (kama kifafa) na kuanza kwa roho ya harara. Makosa hayawezi kusahihishwa, wala matengenezo ya tabia kupatikana kwa juhudi ndogo za vipindi. Utakaso sio kazi ya siku moja au mwaka, lakini ya maisha yote. Bila juhudi za kila wakati na shughuli za kudumu, hatuwezi kuwa na maendeleo katika maisha ya kimbingu, hakuna kupata taji ya mshindi. Tunafanya kazi ya kujitayarisha na hukumu, na hatutakuwa salama tukifanya kazi kwa kutegemea hekima yetu wenyewe na kutumaini maamuzi yetu wenyewe. Roho ile ya kujiamini mliyonayo sasa ninyi wawili, haiwezi kuwapa furaha mbinguni; maana huko wote, hata malaika walioinuliwa, wako chini ya mamlaka-wanatii. Lazima mjifunze kutii na kujinyenyekeza. Kwa neema ya Mungu ninyi nyote wawili. {3T 325.2}

Dada A, niliona kuwa lazima uwe mwangalifu ili usifungue mlango wa majaribu kwa mumeo ambayo huwezi kuufunga hata ukitaka. Ni rahisi kumkaribisha adui mioyoni mwenu kuliko kumfukuza akishapata mwanya. Kiburi chako kinaumizwa haraka, na unahitaji kumkaribia Mungu zaidi, na utafute neema kwa dhati na bidii, neema ya mbingu, kustahimili magumu kama askari mzuri wa Yesu Kristo. Mungu

Ndiye msaidizi wako ikiwa utamchagua Yeye kama nguvu yako. Wote wawili mnapaswa kujitoa wakfu kwa Mungu zaidi. Njia pekee ya kukesha Kwa unyenyekevu ni kukesha kwa maombi. Msifikirie hata kidogo kwamba mnaweza kukaa chini na kufurahi, na mkiangalia jinsi ya kujifurahisha na kuwa na maisha rahisi, yasiyo na usumbufu. Maisha ya Kristo ni mfano wetu. Yeye Alikuwa mtu mwenye huzuni na ajuaye sikitiko Alijeruhiwa, na Alipigwa. Umeridhika sana na nafasi/maisha yako. Unahitaji kukesha kila wakati, ili Shetani asikudanganye kwa ujanja wake. Akileta mawazo ya kifisadi na awaongoze kuwa kinyume cha kazi na giza kuu. Umakini wako lazima uhusishwe na roho ya kumtegemea Mungu kwa unyenyekevu. Haipaswi kufanywa kwa kiburi, na roho ya kujitegemea, bali kwa hali ya kina ya kujua udhaifu wako na kuwa na imani kama ya mtoto katika ahadi za Mungu. {3T 325.3}

Kwa sasa kuna urahisi na furaha ya kuhubiri Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, kuliko wakati ule ujumbe ulipoanza, wakati watu walikuwa wachache na tulionekana kama tu watu wanafiki/washabiki wale waliobeba jukumu la kazi, ilipoanza kuinuka na kuendelea siku zile za awali za kupeleka ujumbe ndio waliojua ni nini maana ya migogoro, dhiki, na maumivu ya moyo, mzigo ulikuwa mzito kwao usiku hata mchana. Hawakufikiria mapumziko, kutokuwa na usumbufu au raha yao hata walipokuwa wanakumbwa na mateso na magonjwa. Muda uliokuwa mfupi ulihitajika kufanya kazi, na watenda kazi walikuwa wachache {3T 326.1}

Mara kwa mara, tulipoletwa kwenye mazingira yenye dhiki, usiku mzima ulitumika kwa maombi ya bidii, na uchungu tukitokwa machozi kwa kuomba msaada na nuru kutoka kwa Mungu ili kutuangazia juu ya Neno Lake. Wakati nuru imefika na mawingu yamerudishwa nyuma, ni furaha na tabasamu la shukurani ya jinsi gani lililokuja kwa wale waliotafuta kwa dhati na bidii Ukweli! Shukrani zetu kwa Mungu zilikuwa kamilifu kama jinsi juhudi zetu za kilio cha matamanio ya nuru kilivyokuwa. Usiku mwingine hatukuweza kulala kwa sababu mioyo yetu ilifurika upendo na shukrani kwa Mungu. {3T 326.2}

Watu ambao huenda kuhubiri Ukweli siku hizi wana mambo mengi ambayo wameshatayarishiwa tayari. Hawawezi kupata ule uzoefu wa dhiki/umasikini kama watenda kazi wa Ukweli wa leo, walivyovumilia kabla yao. Ukweli umeletwa waziwazi, kipande hadi kipande mpaka umetengeneza mnyororo uliokamilika/uliounganishwa. Ili kuleta Ukweli nje kwa namna iliyo wazi na maelewano imebidi utafiti wa makini ufanyike. Upinzani, wenye uchungu sana na ulioidhamiriwa uliwapeleka watumishi wa Mungu kwa Bwana na kwenye Biblia zao. Nuru iliyotoka kwa Mungu hakika ilikuwa ya thamani sana {3T 327.1}

Nimeonesha kwamba sababu ya wengi kutojua lile lililo sawa ni kwa kuwa muda mrefu wamekuwa wakimwendekeza adui, ambaye amefanya kazi nao bega kwa bega, nao hawakutambua nguvu zake. Wakati mwingine inaonekana vigumu

kusubiri kwa uvumilivu mpaka kufikia wakati wa Mungu kutetea haki. Lakini nimeoneshwa kuwa tukikosa subira tunapoteza tuzo ya thamani. Kama watunzaji waaminifu wa shamba kubwa la Bwana, lazima tupande kwa machozi na tuwe na subira na tumaini. Lazima tukutane na shida na huzuni, majaribu, kazi za kuchosha zitatabisha roho zetu, lakini lazima tusubiri kwa uvumilivu kwa imani ili tuvune kwa furaha. Katika ushindi wa mwisho, Mungu hataweza kuwatumia wale watu ambao hawaonekani wakati wa shida na hatari, wakati nguvu, ujasiri, na ushawishi wa wote huhitajika kumshambulia adui. Wale ambao husimama kama askari waaminifu kupigana dhidi ya uovu, na kutetea haki, kupigana na enzi na mamlaka, dhidi ya watawala wa giza la ulimwengu huu, dhidi ya uovu wa kiroho kwenye mahali pa juu, kila mmoja atapokea pongezi kutoka kwa Bwana: "Vema, mtumishi mwema na mwaminifu. … ingia katika furaha ya Mola wako. "{3T 327.2}

Kamwe hakujakuwepo wakati wa hitaji kubwa la makaripio na maonyo ya uaminifu, na kufanya kazi kwa karibu kama ilivyokuwa wakati huu. Shetani ameshuka chini kwa nguvu kubwa, akijua kuwa wakati wake ni mfupi. Analundika ulimwenguni hadithi za kupendeza (hekaya), na watu wa Mungu wanapenda waambiwe mambo laini-laini, dhambi, na uovu havichukizi. Nilioneshwa kuwa watu wa Mungu lazima waimarike zaidi, wafanye juhudi za kurejesha (kurudisha) nyuma giza linaloingia. Kazi ya Roho wa Mungu inahitajika kwa karibu kwenye mioyo kuliko hapo awali. Upumbavu lazima upepetwe, lazima tuamke kutoka kwenye uchovu ambao utaleta uharibifu kwetu tusipoupinga. Shetani ana nguvu, na ushawishi wa kutawala/kudhibiti akili. Wachungaji na walei wapo katika hatari ya kuwa upande wa nguvu za giza. Hakuna kitu kama kusimama katikati (vuguvugu). Sisi sote tunaamua kwa upande wa haki au upande wa ubaya Kristo alisema: "Yeye ambae hayuko Nami Yu dhidi Yangu; na yeye asiyekusanya pamoja Nami hutapanya. " {3Tsw 327.3}

Daima kutakuwepo wale ambao watawahurumia wale ambao wamekosea. Shetani alikuwa na malaika waliomhurumia mbinguni, na alichukua idadi kubwa ya malaika hao pamoja naye. Mungu na Kristo na malaika wa mbinguni walikuwa upande mmoja na Shetani upande mwingine. Pamoja na nguvu isiyo ya kawaida na kipimo cha ukuu wa Mungu na Kristo, malaika walishindwa. Ujanja wa Shetani ulianza, na wakaanza kuamini kwamba Baba na Mwana walikuwa maadui zao na kwamba Shetani alikuwa mfadhili wao. Shetani ana nguvu hiyo sasa na anamiliki juu ya akili, ila sasa imeongezeka mara mia kwa ajili ya uzoefu, utendaji na mazoezi (experience and practice).

Wanaume na wanawake leo wamedanganywa, wamepofushwa na dhana na hila zake, na wasijue. Kwa kutoa nafasi ya mashaka na kutokuamini kuhusu kazi ya Mungu, na kwa kuthamini hisia za kutokuaminiana na wivu wa kikatili, wanajiandaa kwa udanganyifu kamili. Wanainuka juu na hisia zenye uchungu dhidi

ya wale ambao wanathubu tu kusema juu ya makosa yao na kukemea dhambi zao. {3Tsw 328.1}

Wale ambao katika hofu ya Mungu walijitokeza na kujitosa kukutana na uongo na dhambi, wakiuita kwa jina lake, wamefanya jukumu lisilopendwa wakipata mateso mengi kwenye hisia zao; ila wana huruma za wachache na kutelekezwa na wengine. Wenye huruma wako upande usio sahihi, na hutimiza makusudi ya Shetani kwa kupinga mpango wa Mungu. {3Tsw 328.2}

Makemeo daima huumiza asili ya binadamu. Roho nyingi zimeharibiwa na huruma zisizokuwa na busara za ndugu zao; kwa vile, ndugu waliwahurumia, wakadhania lazima iwe kweli kwamba walinyanyaswa, na kwamba mkemeaji alikuwa amekosea kila kitu na alikuwa na roho mbaya. Tumaini pekee la wenye dhambi katika Sayuni ni kuona dhambi zao zilivyo haswa na kuachana nazo. Wale ambao wanaoshugulika na kuharibu makali ya karipio ambayo Mungu hutuma, wakisema kwamba mwonyaji alikuwa na makosa kwa kiasi fulani na aliyeonywa hakuwa sahihi kabisa, wanamfurahisha adui. Njia yoyote ile ambayo Shetani anaweza kutengeneza ili kufanya karipio lisiwe na athari/matunda yanayotakiwa hukamilisha mipango yake. Wengine watamlaumu yule ambaye Mungu amemtuma na ujumbe wa maonyo, wakisema, Yeye ni mkali sana; na kwa kufanya hivyo wanawajibika kwa nafsi ya yule mwenye dhambi ambaye Mungu alitaka kumwokoa, na kwa sababu Mungu alimpenda, basi alimtumia marekebisho, ili apate kunyenyekeza nafsi yake mbele za Mungu na aachane na dhambi zake. Watu hawa wenye huruma ya uongo watatoa hesabu kwa Bwana siku ya hukumu kwa kazi yao ya mauaji. {3T 329.1}

Kuna wengine wanaodai kuamini Kweli ambao hawaoni hatari yao wenyewe. Wanaendekeza uovu mioyoni mwao na kuutenda maishani mwao. Marafiki zao hawawezi kusoma mioyo yao, na mara nyingi wanafikiria wapo sawa tu. {3T 329.2
Black Hawk, Colorado
Augsut 12, 1873.

SURA YA 30

KUOTA NDOTO ZA MCHANA [Day-dreaming].

Dada E Mpendwa nimeoneshwa kwamba unahitaji kuongoka kikamilifu. Umeukubali Ukweli, lakini hujapokea baraka ambayo huletwa na Kweli, kwa

sababu hujapata uzoefu wa nguvu yake inayobadilisha. Upo hatarini kupoteza sehemu zote mbili usipofanya kazi kamilifu ya neema moyoni mwako. Lazima mapenzi yako yaletwe kwenye nia na mapenzi ya Kristo. {3T 329.3}

Hauko sasa kwenye njia sahihi ya kupata hiyo amani na furaha ambayo yule anayeamini Kweli, mnyenyekevu, na anayebeba msalaba ana uhakika wa kuipata . Una muhuri wa tabia ya baba yako. Una tabia ya ubinafsi; hutambui hili, lakini ni kweli. Mawazo yako makuu yapo kwako mwenyewe, kujipendeza mwenyewe, kufanya vitu vinavyokubalika kwako mwenyewe, bila kujihusisha na furaha ya wale walio karibu nawe. Unafanya makosa katika kuitafuta furaha. Ukiipata, itahusika na kuwajibika na kusahau nafsi yako. Huwezi kuwa na furaha ikiwa mawazo yako yanahusiana zaidi na wewe mwenyewe. {3T 329.4}

Unapuuzia kufanya kazi ambayo Mungu amekupa uifanye kwa ucheshi. Unapuuzia majukumu ya kawaida, yaliyo rahisi njiani mwako, na akili yako hutangatanga kwenda kwenye kazi kubwa zaidi, ambayo unafikiria inapendeza ladha yako zaidi, na ambayo unafikiria itajaza mapungufu katika maisha yako, na utupu wa nafsi yako. Hakika utasikitishwa na kukatishwa tamaa hapa. Kazi ambayo Mungu amekuachia uifanye ni kutekeleza majukumu yale ya kawaida, ya kila siku ambayo yapo karibu nawe na kufanya kazi rahisi, za nyumbani za maisha kwa uchangamfu, usizifanye bila kufikiri, lakini moyo wako uwe katika kile unachofanya, ukifanya kwa moyo wako kama vile ufanyavyo na mikono yako, majukumu rahisi ambayo yako mbele yako. {3T 330.1}

Hujifunzi kuwapendeza na kuwapa furaha wengine; macho yako hayajafunguka, ili ujaribu kuangalia mambo gani madogo ambayo unaweza kuyafanya, na tahadhari gani ndogo katika maisha ya kila siku zinazoonesha kujali wazazi na familia yako. Umejisikia kwamba ni fadhila kubwa kwako kujifungia mbali na familia, na kulea mawazo yasiyo na furaha na uzoefu usio na furaha, ukichuma miiba, na ukiridhishwa kuitumia kukujeruhi mwenyewe. Unaendekeza tabia ya ndoto za mchana, ambayo ni lazima iachwe, unaacha kufanya majukumu yako. Kazi ambayo unapaswa kufanya ili kuwapunguzia wengine mzigo unaipuuzia kwa kufurahia kudekesha/kutafakari mawazo yasiyo na furaha. Haujitambui. Shika majukumu yako. Amka! na ushike majukumu ambayo umeyapuuzia. Komboa muda uliopita kwa uaminifu wa siku zijazo. Shika kazi iliyo mbele yako, na, kwa utendaji kazi wa uaminifu, utajisahau mwenyewe na hutakuwa na muda wa kujifikiria na kuona unakosa furaha na kuwa na huzuni. {3T 330.2}

Una karibu kila kitu cha kujifunza kwenye uzoefu wa kikristo. Hubadiliki kwa haraka jinsi inavyopaswa, na ikiwa utapata uzima wa milele, muda huu ndiyo wa kutengeneza tabia ya mbinguni au tabia ambayo itakuzuia kuingia mbinguni. Umefanya nia na mawazo yako kujifikiria mwenyewe kupindukia kiasi kwamba haujatambua unapaswa kufanya nini ili kuwa mfuasi wa Kweli wa Yesu, Yeye aliye mpole na mnyenyekevu, umepuuzia majukumu yako ya nyumbani. Umekuwa wingu

na kivuli katika familia, wakati ilikuwa fursa yako kutoa nuru na kuwa mbaraka kwa wapendwa wanao kuzunguka. Unajishugulisha na vitu vidogo vidogo vya upuuzi, ukikasirishwa, na kukosa furaha. Wakati katika uhalisia, hakuna la maana linalofanya uwe na tabia hiyo. Hujazinduka na kuangalia jinsi unavyoweza kumtua mama yako mzigo na kubariki wazazi wako kwa njia zote. Umetazamia wazazi na dada zako kukusaidia kuwa na furaha, kukuhudumia wewe, na kukutumikia wewe, wakati mawazo yako yamekuwa na ubinafsi. Hujapata neema ya Mungu ndani ya moyo wako, wakati umejidanganya mwenyewe kwa kufikiria kwamba ulikuwa umesonga mbele sana kuhusiana na kujua mapenzi ya Mungu. Unapenda kujihusisha kwenye mazungumzo na wale ambao sio wa imani zetu, wakati hukuweza kuwapa sababu yenye utashi kuhusu imani yetu mbele zao. Katika hili huwakilishi Kweli unavyopaswa na badala yake unaumiza Kweli badala ya kuitendea mema. Endapo ungezungumzia machache kuhusiana na uthibitisho wa imani yetu na uchukue muda kujifunza Biblia yako na uache matendo yako, haiba na tabia yako kukushuhudia kwamba mvuto wa Ukweli u mzuri juu ya moyo wako na maisha yako, ungefanya mengi zaidi mema kuliko porojo tu, wakati unakosa uaminifu katika mambo mengi. {3T 331.2}

Unapokuwa mwangalifu kufuata mfano wa Mkombozi wetu asiye na ubinafsi, na anayejitoa mhanga, ambaye daima alitafuta kufanya mema na kuwabariki wengine, wala sio kujitafutia maisha rahisi, anasa na furaha kwa ajili yako mwenyewe, ndipo utabariki wengine na ushawishi wako. Tunapojichanganya kwenye jumuiya katika familia au katika mahusiano ya maisha tulipowekwa, kwenye mazingira madogo yenye mipaka au makubwa kuna njia nyingi ambazo tunaweza kushuhudia kuhusu Bwana wetu na njia nyingi ambazo tunaweza kumkana. Tunaweza kumkana kwa maneno yetu, kwa kusema wengine vibaya, kwa kuzungumza kwa upumbavu, mzaha na utani, kwa maneno yasiyo na maana na yasiyo na fadhila, au kwa kunyamaza, na kusema kinyume cha Kweli. Kwa maneno yetu tunaweza tukakiri Kristo hayumo ndani yetu. Kwa tabia zetu tunaweza kumkana kwa kupenda anasa/raha zetu, kwa kukwepa majukumu na mizigo ya maisha ambayo lazima mtu mwingine atabeba ikiwa tutayaepa, kwa kupenda raha ya dhambi. Tunaweza pia kumkana Kristo kwa kiburi cha mavazi na kufanana na ulimwengu, au kwa tabia isiyokuwa uungwana, staha na upole. Tunaweza kumkana kwa kupenda maoni yetu wenyewe na kwa kujaribu kudumisha na kuhalalisha ubinafsi wetu. Tunaweza pia kumkana kwa kushugulisha akili kukimbia kwenye mkondo wa ugonjwa wa hisia za mapenzi/mahaba na kufikiria juu ya magumu na shida zetu. {3T 331.3}

Hakuna kabisa mtu ambaye anayeweza kumkiri Kristo mbele ya ulimwengu mpaka nia na roho ya Kristo iishi ndani yake. Hatuwezi kuwasilisha kile ambacho hatuna. Mazungumzo na matendo lazima yawe halisi na yanayoonekana wazi kuhusiana na neema na Ukweli uliomo ndani. Ikiwa moyo umetakaswa, umejisalimisha na una unyenyekevu, matunda yataonekana kwa nje na yatakuwa yenye matokeo zaidi

katika kumkiri Kristo. Maneno na kukiri kwa mdomo tu haitoshi. Wewe, dada yangu, lazima uwe na zaidi ya haya. Unajidanganya mwenyewe. Moyo wako, tabia yako, na matendo yako hayaoneshi roho ya upole, kujinyima, na upendo wenye kutoa. Maneno na kukiri kwa mdomo kunaweza kuonesha unyenyekevu na upendo; lakini ikiwa mwenendo hautasimamiwa kila siku na neema ya Mungu, hautashiriki zawadi ya mbingu, haujaacha vitu vyote kwa ajili ya Kristo, hujasalimisha mapenzi yako mwenyewe na raha zako ili uwe mwanafunzi Wake. {3T 332.1}

Unafanya dhambi na kumkana Mwokozi wako kwa kukita kwenye mambo ya huzuni, kwa kujikusanyia mwenyewe shida. Unajikopesha shida za kesho leo, na kuleta uchungu moyoni mwako, na kuleta mzigo na wingu kwa wale walio karibu nawe, kwa kujizalishia majaribu. Muda wa thamani wa rehema ambao Mungu amekupa ili kutenda mema na kuwa tajiri wa matendo mema, wewe huna busara kabisa kwa kuutumia kufikiria mawazo kufikiria ya huzuni na kujenga majumba/kasiri hewani una shida ya mawazo ambayo yanafikiria mada ambazo hazitaleta afueni au furaha. Ndoto zako za mchana zinazinga njia yako katika namna ya kupata afya na uzoefu wa akili bora katika mambo ya Mungu na maadili bora kwa maisha bora. {3T 332.2}

Ukweli wa Mungu uliopokelewa moyoni una uwezo wa kukufanya uwe na hekima hata upate wokovu. Katika kuuamini na kuutii utapokea neema ya kutosha kutekeleza majukumu na kushinda majaribu ya leo. Neema ya kesho hauhiitaji, unapaswa kuhisi kushugulikia neema ya leo tu. Pata ushindi wa mambo ya leo; Jikane nafsi yako kwa leo kesha na omba kwa ajili ya leo, jipatie ushindi kwa uwezo wa Mungu leo. Yale yahusuyo maisha na mazingira yetu, matukio yanayotuzunguka, na Maandiko ya Neno la Mungu yanayotambua na kupima vitu vyote-- haya yanatosha kutufundisha wajibu wetu na yale tu tunayopaswa kufanya, siku kwa siku. Badala ya kutesa akili yako kukimbia kwenye njia ya mawazo ambayo haina faida yoyote, ungechukua muda kusoma maandiko kila siku na kutekeleza majukumu ya kila siku ambayo sasa yanaonekana kukukera lakini ambayo lazima yafanywe na mtu fulani 3T 333.1

Uzuri wa asili/uumbaji una ndimi ambayo inazungumza na hisia zetu bila kukoma. Moyo ulio mkunjufu huvutiwa na upendo na utukufu wa Mungu kama unavyoonekana katika kazi za mkono Wake. Sikio linalosikia linaweza kusikia na kuelewa mawasiliano ya Mungu kupitia kazi za maumbile. Kuna somo katika mwale wa jua na katika vitu mbalimbali vya asili ambavyo Mungu ameviwasilisha mbele yetu. Mashamba ya kijani kibichi, Miti mirefu, vikonyo chipukizi vya miti na maua, wingu linalopita, mvua inayoanguka, kijito kinachotiririka, jua, mwezi, na nyota mbinguni, vyote vinakaribisha usikivu wetu na tafakari, na kutusihi tumfahamu Mungu, aliyeumba vyote. Masomo ya kujifunza kutoka kwa vitu anuwai vya ulimwengu wa asili ni haya: vinatii mapenzi ya muumba wao; kamwe havimkani Mungu, kamwe havikatai kutii maneno yoyote ambayo ni mapenzi Yake. Viumbe

vilivyoanguka peke yao ndiyo vinavyokataa kutoa utii kamili kwa muumba wao. Maneno na kazi zao zinapingana na Mungu na zinapingana na kanuni Ya serikali Yake. {3T 333.2}

Mawazo yako hayakuinuliwa. Kuna mambo mengi katika asili vya kukuongoza kumpenda na kumuabudu muumba wako. Kuna lishe ya kiroho bila kujifungia mwenyewe ukijilisha matumaini yaliyokatishwa tamaa na fikra potofu. Usiwe mwepesi kuzungumza na wasio amini na kuingia kwenye mabishano na wale wanaopinga Ukweli, kwani hawajajikimu kwa maandiko kiasi cha kufanya hivi. Umepuuzia kusoma Biblia yako. Unaweza kupendekeza Ukweli kwa njia bora kwa upole wa maisha yako na uaminifu katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku. Ikiwa unadhamiria kwa umakini kufanya sehemu yako, na kuwa mwaminifu na mwenye udhati na bidii kuona ni kipi unaweza kufanya kwa wale ambao unajaribu kuwafikia katika kazi ya Bwana, basi utawakilisha Ukweli kwa njia bora. Njia bora ya kuwashawishi watu kuhusiana na Ukweli si kwa mabishano, au mazungumzo, lakini kwa kuiishi Kweli kila siku, kwa kuongoza maisha thabiti, yenye kiasi, yenye staha, maisha ya unyenyekevu kama mwanafunzi wa Kristo. {3T 334.1}

Ni jambo la kusikitisha kutoridhika na mazingira yetu au mazingira ambayo tumewekwa ambapo majukumu yetu yanaonekana kuwa ya unyenyekevu na yasiyo na umuhimu. Wajibu wa kibinafsi na unyenyekevu hayakufurahishi huna pumziko, huna raha, huna kuridhika, haujatulia. Yote haya yanatokana na ubinafsi. Unajifikiria zaidi mwenyewe kuliko wengine wanavyo kufikiria. Unajipenda mwenyewe kuliko unavyowapenda wazazi wako, dada zako, na ndugu zako, na kuliko unavyompenda Mungu. Unatamani kazi za aina inayokufurahisha, ambazo unafikiri zinakufaa vyema zaidi. Hauko tayari kufanya kazi na kusubiri katika mazingira yenye unyenyekevu mahali ambapo Mungu amekuweka mpaka atakapo kuhakiki na kukujaribu, na uoneshe uwezo wako na kufaa katika nafasi za juu zaidi. Heri wapole; maana watairithi nchi. "Roho ya upole sio roho ya kutoridhika, lakini ni kinyume chake. {3T 334.2}

Wale ambao wanaojiita Wakristo ambao daima hunung’unika na kulalamika, na huonekana kufikiria kwamba furaha na uso wa ucheshi ni dhambi, hawana vazi la Kweli la dini. Wale ambao wanaangalia juu ya mandhari nzuri ya asili kama wanavyoangalia picha ya kifo, wanaochagua kutazama majani yaliyonyauka badala ya kuchuma maua mazuri, ambao hufurahi kwa huzuni na kila kitu ambacho kimenyong’onyea katika lugha inayozungumzwa kwao na ulimwengu wa asili, ambao hawaoni uzuri katika mabonde yaliyovikwa na kijani kibichi na sura ya mlima mzuri uliovikwa na mimea mipya, ambao hufunga hisia zao kutoka kwenye sauti za furaha ambazo zinazungumza nao kwenye uumbaji na ambazo zina muziki mtamu kwenye sikio la msikilizaji–hawa hawamo ndani ya Kristo. Hawatembei katika nuru, lakini wanalikusanya kwao giza na huzuni, wakati ambapo wangeweza

pia kuwa na mwangaza na baraka za Jua la Haki linalowazukia mioyoni mwao na uponyaji katika mihimili Yake. {3T 334.3}

Dada yangu mdogo, unaishi maisha ya kufikirika. Huwezi kugundua au kuona baraka katika chochote. Unafikiria shida na majaribu ambayo hayapo; unatia chumvi shida ndogo -ndogo ili zionekane ni shida nzito. Huu sio upole/unyenyekevu ambao Kristo anaubariki. Ni kutoridhika kusikotakaswa kutokuwa na kawaida. Upole na unyenyekevu ni neema ya thamani, iliyo tayari kuteseka kimya, iliyo tayari kuvumilia shida. Upole na unyenyekevu una uvumilivu na unafanya kazi kuwa na furaha katika hali zote upole/unyenyekevu daima hushukuru na hutengeneza nyimbo zake za furaha, nyimbo moyoni mwa mwana wa Mungu. Upole/unyenyekevu utakutana na kukatishwa tamaa kutendewa mabaya na hautalipiza kisasi. Upole/unyenyekevu sio kunyamaza kimya na kuzira moyoni. Kukasirika ni kinyume cha upole/unyenyekevu; kwani hujeruhi na kuleta maumivu kwa wengine, na upole/unyenyekevu hautafuti kujipendezesha nafsi. {3T 335.1}

Ndiyo tu umeingia katika shule ya Kristo. Una karibu kila kitu cha kujifunza. Hauvai nguo kwa kutokuwa na kiasi au ubaradhifu wakati huu ila una mtazamo wa kiburi unatamani uvae bila kuwa na kiasi. Unafikiria kuhusu mavazi zaidi ya unavyopaswa. Kristo anakualika Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi. Salimisha shingo yako kwenye nira ambayo Kristo ameweka na utapata katika huu usalimishaji, furaha ambayo umejaribu kujipatia kwa njia yako mwenyewe. {3T 335.2}

Unaweza kuwa mcheshi endapo utaleta mawazo yako chini ya mapenzi ya Kristo. Usichelewe, lakini chunguza moyo wako kwa ukaribu na ufishe nafsi kila siku. Unaweza kuuliza: Je! nitawezaje kutawala matendo yangu mwenyewe na kudhibiti hisia zangu za ndani? wengi ambao hawakiri kumpenda Mungu hudhibiti roho zao kwa kiwango kikubwa bila msaada wa neema maalum ya Mungu. Wanakuza kutawala nafsi. Kwa kweli hili ni kemeo kwa wale ambao wanajua kwamba kutoka kwa Mungu wanaweza kupata nguvu na neema, na bado hawaoneshi neema za Roho. Kristo Ndiye kielelezo chetu. Yeye Alikuwa mpole na mnyenyekevu. Jifunze kutoka Kwake, na uige mfano Wake. Mwana wa Mungu hakuwa na kosa. Lazima tunuie huu ukamilifu na kushinda kama Yeye alivyoshinda, ikiwa tunataka kuketi mkono Wake wa kuume. {3T 336.1}

Una sifa za tabia ambazo zinahitaji kuadabishwa kwa ukali na kudhibitiwa kwa kudhamiria kabla ya kuingia kwenye ndoa kwa usalama, hivyo ndoa lazima itolewe kwenye mawazo yako mpaka ushinde kasoro hizo kwenye tabia yako, kwani hutaweza kuwa mke mwenye furaha. Umepuuzia kujielimisha kuhusiana na utaratibu wa kazi za nyumbani. Hujaona ulazima wa kuwa na tabia za kazi ya bidii,

tasnia na uzalishaji na uadilifu. Tabia ya kufurahia kazi zenye manufaa, inapojengwa kwa mara ya kwanza, haipotei kamwe. Na unakuwa tayari umeandaliwa kuwekwa katika hali zote za maisha na utastahili kuwekwa katika nafasi fulani. Utapenda kujishugulisha. Kama unapenda kazi zenye kuleta manufaa, akili yako itashughulishwa na ajira yako, na hutapata wakati kuendekeza mawazo kwenye ndoto za kufikirika za mambo unayodhani ni mazuri yanayoelea hewani. {3T 336.2}

Ujuzi wa kazi muhimu utaipa nguvu akili yako yenye kuhangaika na isiyoridhika, ufanisi, na uzuri, hadhi ya kuwa na kiasi, na itafanya watu wa kuheshimu. Unajifahamu mwenyewe kwa udogo sana; hujui udanganyifu wa moyo wako mwenyewe. Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wakufisha, chunguza moyoni mwako kwa uangalifu, na pata muda wa kutafakari na kuomba. Usipoona mapungufu ya tabia yako na kwa unyofu wenye bidii usahihishe makosa yako, huwezi kuwa mwanafunzi wa Kristo. {3T 336.3}

Unapenda kufikiri na kuzungumzia kuhusiana vijana wa kiume. Unatafsiri tabia zao njema na za adabu kwa watu ni umakini wao wa hali ya juu kwako. Unajidanganya kwamba unaheshimiwa nakutaminiwa kwa hali ya juu kuliko vile ilivyo. Hebu mazungumzo yako yawe kwenye mada zenye faida, zinazoboresha na za kukuinua juu. Mtoto wangu mpendwa, haujengi tabia njema yenye Ukweli na kutokuwa na hila-unyofu. Moyo wako hauko sawa. Ushawishi wako sio mzuri kwa wale walio wadogo kwako, kwa kuwa huna nia ya Kristo; lakini unajidanganya kwamba umepiga hatua katika maisha ya Kikristo. {3T 337.1}

Matengenezo lazima yaanze katika familia ya baba yako. Unabeba muhuri wa tabia ya baba yako. Unapaswa kujitahidi kuachana na makosa yake na kuchukua mambo kwa kupitiliza. Endapo u mwanafunzi wa Kweli wa Kristo, utaona kazi muhimu ya kufanya nyumbani mwako. Kila familia inaweza kuwa shule ya kudumu. Dada mkubwa anaweza kuwa na mvuto mkubwa wa ushawishi kwa wadogo zake kwenye familia. Wale wadogo wakijionea mfano wa wakubwa wao, watatawaliwa na kanuni ya kuiga zaidi kuliko maagizo yanayorudiwa mara kwa mara. Binti mkubwa anapaswa kuhisi kwamba ni jukumu la Kikristo linalomkabili kumsaidia mama mizigo yake mingi na mizito inayomkabili. Kugaragara kitandani kulala, au, kufikiria mambo ya huzuni wakati mabega ya wengine katika familia yanainama katika kubeba mizigo inayotesa ni jambo baya zaidi ya kupoteza wakati. {3T 337.2}

Mabinti wakubwa wawe msaada katika kusaidia kuelimisha wadogo zao katika familia. Hapa kuna nafasi nzuri kwako kuonesha fadhili, bidii, na kuwa na hofu ya Bwana mbele zako, kwa kufundisha wale ambao wanajua machache zaidi yako, unaweza kupokea upendo kutoka kwa wale ambao unajaribu kuwasaidia. Hapa unaweza kuwa na mafunzo bora ya kujipatia mazoezi ya neema za kikristo. Hupendi watoto. Ni jambo la kweli kwamba haupendi watoto, na kwa jumla hupendi chochote kinachohitaji ufanye bidii, uwajibike, na uvumilivu. Hupendi

kuwa na uthabiti. Unapenda mabadiliko na mambo tofauti na daima unatafuta yale yanayokuridhisha na kukuletea furaha mwenyewe. Unahitaji elimu binafsi (kujielimisha), na unaweza kufanya hili sasa kuliko wakati ujao. Unahitaji kufanya karibu kila badiliko linalopaswa kufanywa maishani mwako, na acha Mungu akusaidie kushikilia kazi hiyo bila kuchelewa. Ni wale tu walio safi, wema, na watakatifu ndio watakaokaa pamoja na Kristo atakapokuja kwenye ufalme wake. {3T 337.3}

Huwezi kuipata mbingu bila bidii ya dhati, bidii ya kudumu. Kama inavyoonekana katika nuru ya mbinguni, maisha yako mpaka sasa yamekuwa hayana malengo na karibu yote yamekuwa hayana manufaa. Sasa unayo nafasi ya kukomboa wakati na kuosha vazi lako la tabia katika damu ya Mwana-Kondoo. Mungu atakusaidia ukihisi kuhitaji msaada Wake. Haki yako haina thamani kwa Mungu. Ni katika kupitia sifa za Kristo tu ndipo utakuwa mshindi hatimaye. Kama utakuwa miongoni mwa wale ambao watakaookolewa na kupata wokovu wa milele, mbingu itakuwa rahisi sana kuipata {3T 338.1}

SURA YA 31

UASI MKUBWA

Kora, Dathani na Abiramu waliasi dhidi ya Musa na Haruni, na hivyo dhidi ya Bwana. Bwana alikuwa ameweka majukumu maalum juu ya Musa na Haruni katika kuwachagua kwa ukuhani na kwa kuwapa heshima na mamlaka ya kuongoza mkutano wa Israeli. Musa aliteswa na kuendelea kuasi kwao Waebrania. Kama kiongozi aliyechaguliwa na anayeonekana wa Mungu, alikuwa ameunganishwa na Waisraeli katika nyakati za hatari, na alikuwa amebeba kutoridhika kwao, wivu wao, na manung'uniko yao, bila kulipiza kisasi na bila kutaka kulipiza kisasi au kutolewa kutoka kwa nafasi yake yenye kujaribu. 3T 339.1

Wakati Waebrania walipokuwa katika matukio ya hatari, au ambapo tamaa/shauku zao hazikutimizwa, badala ya kumtumaini Mungu, ambaye alikuwa amewafanyia miujiza mikubwa, walinung'unika dhidi ya Musa. Mwana wa Mungu, ingawa hakuonekana na mkutano, alikuwa kiongozi wa Waisraeli. Uwepo wake ulikwenda mbele yao na kufanya safari zao zote, wakati Musa alikuwa kiongozi wao anayeonekana, akipokea maagizo yake kutoka kwa Malaika, ambaye alikuwa Kristo. 3T 339.2

Msingi wa Ibada ya Sanamu

Kwa kutokuwepo kwa Musa kusanyiko lilimtaka Haruni awafanyie miungu ya kwenda mbele yao na kuwaongoza kurudi Misri. Hili lilikuwa tusi kwa kiongozi wao mkuu, Mwana wa Mungu asiye na mwisho. Wiki chache tu kabla, walikuwa wamesimama wakitetemeka kwa hofu na woga mbele ya mlima, wakisikiliza Maneno ya Bwana: "Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Utukufu uliotakasa mlima wakati sauti ilisikika ambayo ilitikisa mlima huo toka katika msingi wake, bado ulikuwa juu yake, ukitembea mbele ya mkutano; lakini Waebrania waligeuza macho yao na kuomba miungu mingine. Musa, kiongozi wao anayeonekana, alikuwa akiongea na Mungu mlimani. Walisahau ahadi na onyo la Mungu: “Tazama, namtuma Malaika mbele yako, akulinde njiani, na kukuleta mahali ambapo nimetayarisha. Jihadharini Naye, na kutii sauti Yake, usimkasirishe; kwa maana hatasamehe makosa yenu, kwa maana Jina Langu liko ndani Yake.” 3T 339.3

Waebrania walikuwa wagumu na wajeuri katika kuamini na wasio na shukrani kabisa katika ombi lao baya lisilo na kicho: "Tutengenezee miungu, ambayo itatuongoza." Ikiwa Musa hakuwepo, uwepo wa Bwana bado ulibaki; hawakuachwa wenyewe. Mana iliendelea kuanguka, na walilishwa na mkono wa Mungu asubuhi na jioni. Nguzo ya wingu wakati wa mchana na nguzo ya moto usiku ilionesha uwepo wa Mungu, ambayo ilikuwa ukumbusho hai mbele yao. Uwepo wa Mungu haukutegemea uwepo wa Musa. Lakini wakati huo huo alipokuwa akimsihi Bwana katika mlima kwa niaba yao, walikuwa wakikimbilia kwenye makosa ya aibu, katika uvunjaji wa sheria iliyotolewa hivi karibuni kwa ukuu/utukufu. 3T 340.1

Hapa tunaona udhaifu wa Haruni. Angekuwa amesimama kwa ujasiri katika Ukweli wa maadili na kwa ujasiri angewakemea viongozi katika ombi hili la aibu, maneno yake ya wakati unaofaa yangeokoa uasi huo mbaya. Lakini hamu yake ya kupendwa na mkutano na kuwa maarufu, na hofu yake ya kusababisha kukasirika kwao, ilimwongoza kutoa kafara ya utii wa Waebrania katika wakati huo wa uamuzi. Aliinua/alijenga madhabahu, akatengeneza sanamu ya kuchonga, na akatangaza siku ambayo wataifanya takatifu sanamu hiyo kama kitu cha kuabudiwa na kutangaza mbele ya Israeli wote: Hawa ndio miungu waliokuongoza/waliokutoa kutoka Misri. Wakati kilele cha mlima bado kikiangazwa na utukufu wa Mungu, anashuhudia kwa utulivu shangwe na kucheza kwa sanamu hii isiyo na maana; na

Musa ameteremshwa kutoka mlimani na Bwana kuwakemea watu. Lakini Musa hakukubali kuondoka mlimani hadi maombi yake kwa niaba ya Israeli yasikilizwe, na ombi lake kwamba Mungu awasamehe limejibiwa. 3T 340.2

Mbao za Sheria Zavunjwa [Amri Kumi]

Musa alikuja kutoka mlimani na kumbukumbu nzuri mikononi mwake, ahadi ya Mungu kwa mwanadamu kwa sharti la utii. Musa alikuwa mtu mpole zaidi duniani, lakini alipoona uasi wa Israeli alikuwa na wivu na hasira kwa utukufu wa Mungu. Katika ghadhabu yake alitupa chini ahadi ya thamani ya Mungu, ambayo ilikuwa ya kipenzi kwake kuliko maisha. Aliona sheria imevunjwa na Waebrania, na kwa bidii yake kwa Mungu, kuichafua sanamu ambayo walikuwa wakiabudu, alitoa kafara mbao za mawe. Haruni alisimama karibu, kwa utulivu, kwa uvumilivu akibeba lawama kali za Musa. Yote hii ingeweza kuzuiwa na neno kutoka kwa Haruni kwa wakati unaofaa. Uamuzi wa Kweli ulio bora na wa haki katika saa ya hatari ya Israeli ungekuwa umesawazisha akili zao katika mwelekeo sahihi. 3T 341.1

Je! Mungu anamhukumu Musa? Hapana, hapana; wema mkuu wa Mungu husamehe uamuzi wa haraka na bidii ya Musa, kwa sababu yote ilikuwa kwa sababu ya uadilifu wake na kukatishwa tamaa na huzuni mbele ya macho yake katika ushahidi wa uasi wa Israeli. Mtu ambaye angeweza kuwaokoa Waebrania katika saa ya hatari ni mtulivu. Haoneshi ghadhabu kwa sababu ya dhambi za watu, wala hajilaumu mwenyewe na kudhihirisha kujuta chini ya hali ya makosa yake; lakini anatafuta kuhalalisha mwenendo wake katika dhambi mbaya. Anawafanya watu wawajibike kwa udhaifu wake katika kukubali ombi lao. Hakuwa tayari kuvumilia manung'uniko ya Israeli na kusimama chini ya shinikizo la kelele zao na matakwa yasiyofaa, kama Musa alivyofanya. Aliingia katika roho na hisia za watu bila kujibu, na kisha akataka kuwafanya wawajibike. 3T 341.2

Kusanyiko la Israeli lilidhani Haruni ni kiongozi mzuri zaidi kuliko Musa, kiongozi wao wa sasa. Hakuwa mgumu sana asiyepindishwa kirahisi. Walifikiri kwamba Musa alionesha roho mbaya sana ya kutokubaliana, na huruma zao zilikuwa kwa Haruni, ambaye Musa alimkemea sana. Lakini Mungu alisamehe ujinga aliofanya kwa dhati/unyofu wa kweli kwa Musa [kuangusha mbao za Amri Kumi], wakati alimwajibisha Haruni kwa udhaifu wake wa dhambi na ukosefu wa uadilifu wakati wa shinikizo la hali. Ili kujiokoa, Haruni alitoa dhabihu za maelfu ya Waisraeli. Waebrania walihisi adhabu ya Mungu kwa tendo hili la uasi, lakini kwa muda mfupi walikuwa wamejaa kutoridhika na uasi tena. 3T 341.3

Watu Wanung’unika

Wakati majeshi ya Israeli yalipofanikiwa, walijichukulia utukufu wote kwao wenyewe; lakini walipojaribiwa na kukabiliwa na njaa au vita

walimtwika/walimpachika Musa taabu zao zote. Nguvu ya Mungu ambayo ilidhihirishwa kwa njia ya kushangaza katika kukombolewa kwao kutoka Misri, na kuonekana mara kwa mara katika safari yao yote, ingepaswa kuwatia moyo na kuimarisha imani yao na kuziba vinywa vyao kwa kuwa na semi hata moja ya kukosa shukurani. Lakini woga mdogo tu wa uhitaji, hofu ndogo ya hatari kutokana na sababu yoyote, ulipelekea ulinganifu usio sawa wa faida kwa upande wao, na kuliwasababisha kupuuza baraka zilizopatikana katika nyakati zao za hatari kubwa. Uzoefu waliopitia katika suala la kuabudu ndama wa dhahabu ulipaswa kuwa na maoni ya kina juu ya akili zao kama kamwe kutofutwa. Lakini ingawa alama za kukasirika kwa Mungu zilikuwa bado mpya mbele yao kwa kuwa na safu iliyovunjika [jeshi lililopungua] na kukosekana kwa idadi ya watu kwa sababu ya makosa yao ya mara kwa mara dhidi ya Malaika aliyekuwa akiwaongoza, hawakuchukua haya masomo kwa moyo na kwa utii mwaminifu kukomboa kushindwa kwao huko nyuma; na mara nyingine walishindwa na majaribu ya Shetani. 3T 342.1

Jitihada bora za mtu mpole na mnyenyekevu zaidi duniani hazikuweza kuwafanya wawe watiifu. Shauku ya Musa isiyo na ubinafsi ilizawadiwa wivu, kushukiwa, na kusingiziwa uongo. Maisha yake manyenyekevu ya mchungaji yalikuwa ya amani na furaha zaidi kuliko nafasi yake ya sasa kama mchungaji wa mkutano huo mkubwa wa roho za misukosuko. Wivu wao usiokuwa na sababu ulikuwa mgumu kudhibiti kuliko mbwa mwitu wakali wa nyikani. Lakini Musa hakuthubutu kuchagua njia yake mwenyewe na kufanya apendavyo mwenyewe. Alikuwa ameacha fimbo ya uchungaji kwa amri ya Mungu na mahala pake alikuwa amepokea fimbo yenye nguvu. Yeye hakuthubutu kuweka fimbo hii ya enzi chini na kujiuzulu wadhifa wake mpaka Mungu amfukuze/amtoe kazini. 3T 342.2

Ni kazi ya Shetani kujaribu akili. Atapendekeza maoni yake ya ujanja na atachochea mashaka, kuhoji, kushuku, kutokuamini, na kuwa na mashaka na maneno na matendo ya yule anayesimama chini ya majukumu na anayetafuta kutekeleza akili ya Mungu katika kazi zake. Ni kusudi maalum la Shetani kumwaga juu na karibu na watumishi wa chaguo la Mungu, shida, mashaka, fadhaa na upinzani, ili washindwe kufanya kazi yao na, na ikiwa inawezekana, wakate tamaa. Wivu, ugomvi, na hisia mbaya zitapambana, vitapinga kwa kiwango kikubwa, sawasawa na juhudi bora kabisa ambazo watumishi wa Mungu, walioteuliwa kwa kazi maalum, wanaweza kuwekeza. 3T 343.1

Mpango wa Shetani ni kuwafukuza kutoka kazini kwa kufanya kazi kupitia mawakala. Wote ambao anaweza kuwafanya kutokuwa na imani, au kushuku atawatumia kama vyombo vyake. Nafasi ya Musa katika kubeba mizigo aliyobeba kwa waisraeli wa Mungu haikuthaminiwa. Hii ipo ndani ya asili ya mwanadamu, wakati wasipokuwa chini ya uongozi wa moja kwa moja wa Roho wa Mungu, tabia ya tamaa, kijicho, wivu, na uaminifu wa kikatili, ambao, ikiwa hautashindwa,

utasababisha hamu ya kudhoofisha na kubomoa wengine, wakati roho za ubinafsi zitatafuta kujijenga juu ya upotovu wao. 3T 343.2

Kora, Dathani na Abiramu

Kwa uteuzi wa Mungu wanaume hawa walikuwa wamepewa wadhifa/heshima maalum. Walikuwa katika idadi hiyo ambayo, pamoja na wazee sabini, walipanda pamoja na Musa mlimani na kuuona utukufu wa Mungu. Hawa wawili, waliona nuru tukufu iliyofunika sura ya Mungu ya Kristo. Chini ya wingu kulikuwa na muonekano kama "kazi ya jiwe ya samawi iliyochongwa, na kama mwili wa mbinguni katika uhalisi Wake." Watu hawa walikuwa mbele ya utukufu wa Bwana na walikula na kunywa bila kuangamizwa na usafi na utukufu usio na kifani ambao ulionekana juu yao. Lakini mabadiliko yalikuja. Jaribu, lilikuwa dogo mwanzoni, lilikuwa limehifadhiwa moyoni; na jinsi lilivyohimizwa likawa limeimarishwa mpaka pale mawazo yalipodhibitiwa na nguvu ya Shetani. Hawa watu juu ya upumbavu mdogo na wa kijinga zaidi walijitokeza kwenye kazi yao ya kutokujua. Mwanzoni walidokeza na kuonesha mashaka/kushuku, ambayo yalichukua kwa urahisi akili nyingi na walijitokeza zaidi. Na kwa kupata uhakika zaidi na zaidi, kwa watu kuafikiana nao katika tuhuma zao kwa neno kutoka kwa mtu mmoja na mwingine, kila mmoja akielezea kile alichofikiria juu ya vitu kadhaa ambavyo vilikuwa chini ya taarifa yake, roho hizi zilizodanganywa kwa kweli ziliamini kuwa zilikuwa na bidii kwa Bwana katika jambo hilo na kwamba hawatasamehewa isipokuwa watekeleze kikamilifu kusudi lao la kumfanya Musa aone na kuhisi msimamo wa kijinga aliokuwa nao kwa Israeli. Chachu kidogo ya kutokuamini na kisha mafarakano, tamaa, na wivu ilikuwa ikitia chachu ya kambi ya Israeli. 3T 343.3

Kora, Dathani, na Abiramu walianza kazi yao katili kwa watu ambao Mungu alikuwa amewakabidhi majukumu matakatifu. Walifanikiwa kuwatenga wakuu mia mbili na hamsini 250, watu ambao walikuwa maarufu katika mkutano, wanaume mashuhuri. Wakiwa na hawa wanaume wenye nguvu na ushawishi upande wao, walihisi kuwa na uhakika wa kufanya mabadiliko makubwa katika mpangilio wa mambo. Walifikiri wangeweza kuibadilisha serikali ya Israeli na kuiboresha sana kutoka kwa utawala wake wa sasa. 3T 344.1

Kora hakuridhika na nafasi yake. Alikuwa ameunganishwa na huduma ya hema, lakini alitaka kuinuliwa mbele, kwenye ukuhani. Mungu alikuwa amemweka Musa kama kiongozi mkuu, na ukuhani ulipewa kwa Haruni na wanawe. Kora alidhamiria kumlazimisha Musa abadilishe utaratibu wa mambo, ili apandishwe hadhi ya ukuhani. Ili kuwa na hakika zaidi ya kutimiza kusudi lake, aliwavuta Dathani na Abiramu, wazao wa Reubeni, katika uasi wake. Hawa walifikiri kwamba, wakiwa wazao wa mtoto wa kwanza wa Yakobo, mamlaka kuu, ambayo Musa alijinyakulia, ilikuwa yao; na, pamoja na Kora, waliazimia kupata ofisi ya ukuhani. Hawa watatu walikuwa na usongo sana katika kazi mbaya na waliwashawishi wanaume mashuhuri mia mbili na hamsini [250] waliokuwa na nafasi kwenye jumuiya, ambao

pia walikuwa wameazimia kushiriki katika ukuhani na serikali, kujiunga nao. 3T 344.2

Mungu alikuwa amewaheshimu Walawi kufanya huduma katika hema kwa sababu hawakushiriki katika kutengeneza na kuabudu ndama wa dhahabu na kwa sababu ya uaminifu wao katika kutekeleza agizo la Mungu juu ya waabudu sanamu. Kwa Walawi pia walipewa ofisi ya kusimamisha maskani na kupiga kambi kuzunguka pande zote, wakati majeshi ya Israeli yakipiga hema zao mbali nayo. Na walipokuwa safarini, Walawi walishusha maskani na kuibeba, Sanduku la Agano na vyombo vyote vitakatifu. Kwa sababu Mungu aliwaheshimu Walawi hivi, wakaanza kuwa na matamanio ya ukuu kuhusiana na nafasi ya juu zaidi, ili wapate ushawishi mkubwa kwa mkutano. Ndipo “Wakajikusanya pamoja kinyume na Musa na Haruni, na kuwaambia, Mmechukua kila kitu kuwa juu yenu, angalia mkutano wote ni watakatifu, kila mmoja wao, na Bwana Yu kati yao; kwanini sasa mnajiweka peke yenu kuwa juu ya mkutano wa Bwana? ” 3T 345.1

Kubembeleza, Kumdanganya mtu kwa Kumsifia na Huruma ya Uongo

Hakuna kitu ambacho kitawapendeza watu zaidi kuliko kusifiwa kwa kupitiliza kwa kuweka chumvi na kubembelezwa wanapokuwa gizani na wamekosea, na wanastahili kukemewa. Kora alifanikiwa kupata masikio na ukubali wa watu, na huruma yao, kwa kumwakilisha Musa kama kiongozi jeuri. Alisema kuwa alikuwa mkali sana, muonevu sana, mwenye mabavu sana, na kwamba aliwakemea watu kana kwamba walikuwa wenye dhambi wakati walikuwa watu watakatifu, waliotakaswa kwa Bwana, na Bwana alikuwa kati yao. Kora alisoma matukio hayo katika uzoefu wao katika safari zao nyikani, ambapo walikuwa wameletwa katika maeneo yenye dhiki, na ambapo wengi wao walikuwa wamekufa kwa sababu ya manung'uniko na kutotii, na kwa akili zao zilizopotoka walidhani na waliona wazi kabisa kwamba shida zao zisingekuwepo ikiwa Musa angefuata njia nyingine. Alikuwa mgumu asiyetaka kuthibitiwa au kupindishwa, mkali sana, na waliamua kwamba majanga yao yote jangwani yalikuwa juu yake. Kora, roho iliyoongoza, alidai hekima kubwa katika kugundua sababu ya kweli ya majaribu na mateso yao. 3T 345.2

Katika kazi hii ya kutoridhika, kulikuwa na maelewano makubwa na umoja wa maoni na hisia kati ya mambo haya ya kutatanisha kuliko ilivyokuwa ikijulikana kuwapo hapo awali. Mafanikio ya Kora katika kupata sehemu kubwa ya mkutano wa Israeli upande wake yalimfanya ahisi kujiamini kuwa alikuwa na busara na sahihi katika hukumu, na kwamba Musa alikuwa akinyakua mamlaka ambayo yalitishia ustawi na wokovu wa Israeli. Alidai kwamba Mungu alikuwa amemfunulia jambo hilo na kumwekea mzigo wa kubadilisha serikali ya Israeli kabla tu mambo hayajachelewa. Alisema kwamba kutaniko halikuwa na kosa; walikuwa wenye haki; kwamba kilio hiki kikubwa juu ya manung'uniko ya mkutano ulioleta juu yao

ghadhabu ya Mungu ilikuwa makosa; na kwamba watu walitaka tu kuwa na haki zao; walitaka uhuru wa mtu binafsi. 3T 346.1

Kama hisia ya uvumilivu wa kujitolea wa Musa ungewarudia kwenye kumbukumbu zao, na kama juhudi zake zisizo na ubinafsi kwa niaba yao walipokuwa katika bonde la utumwa zingekuja mbele yao, dhamiri zao zingeguswa/zingeamshwa. Wengine hawakuwa na Kora kabisa kwa maoni yake juu ya Musa na walitaka kusema kwa niaba yake. Kora, Dathani, na Abiramu ilibidi wawape sababu watu kwa nini Musa alionesha kupendezwa sana kwa kusanyiko la Israeli kutoka mwanzo. Akili zao za ubinafsi, ambazo zilishushwa kama vyombo vya Shetani, zilidokeza kwamba mwishowe wamegundua kitu cha nia inayoonekana ya Musa. Alikuwa amekusudia kuwafanya wazururе nyikani hadi wote, au karibu wote, waangamie, kisha awe mmiliki wa mali zao. 3T 346.2

Kora, Dathani, na Abiramu, na wakuu mia mbili na hamsini ambao walikuwa wamejiunga nao, kwanza walianza kuwa na wivu, kisha tamaa/kijicho, na baadaye wakaasi. Walikuwa wamezungumza kwa niaba ya nafasi ya Musa kama mtawala wa watu mpaka wakafikiri kwamba huo ni msimamo wenye kutamanika sana ambao yeyote kati yao angeweza kuujaza yeye kama yeye. Na wakajiweka katika mkao wa kutokuridhika mpaka walipojidanganya na kudhani kwamba Musa na Haruni wamejiweka katika nafasi ambayo walikuwa wanashikilia Israeli. Walisema kwamba Musa na Haruni walijiinua juu ya mkutano wa Bwana kwa kuchukua ukuhani na serikali, na kwamba ofisi hii haipaswi kupewa nyumba yao peke yao. Walisema kwamba ilitosha kwao ikiwa wangekuwa sawa na ndugu zao; kwani hawakuwa watakatifu zaidi ya watu, ambao walipendelewa na kuwa na kibali sawa na uwepo na ulinzi wa pekee wa Mungu. 3T 346.3

Tabia Yajaribiwa

Musa aliposikiza maneno ya Kora, alijawa na uchungu na akaanguka kifudifudi mbele ya watu. “Akanena na Kora na watu wake wote, akisema, Hata kesho Bwana ataonesha ni nani aliye Wake, na ni nani aliye mtakatifu; Naye atamleta karibu Naye; hata yeye aliyemchagua atamfanya karibu Naye. Fanya Hivi; chukua vyombo vyako vya kufukizia, Kora na watu wako wote; na weka moto ndani yake, na tia uvumba ndani yake mbele za Bwana kesho; na itakuwa, huyo mtu atakayemchagua Bwana, atakuwa mtakatifu. Mnachukua mengi sana juu yenu, enyi wana wa Lawi. Musa akamwambia Kora, Tafadhali, sikieni, enyi wana wa Lawi; ni jambo dogo kwenu, ya kuwa Mungu wa Israeli amewatenga ninyi na mkutano wa Israeli, ili awakaribishe Kwake ili mtumikie kwenye maskani ya Bwana, na kusimama mbele ya mkutano ili kuwahudumia? Naye amekuleta karibu Naye, na ndugu zako wote, wana wa Lawi pamoja nawe; je! Unatafuta ukuhani pia? Kwa sababu hii wewe na mkutano wako wote mmekusanyika pamoja kumpinga Bwana; na Haruni ni nini, hivi kwamba mnanung'unika dhidi yake? ” Musa aliwaambia kwamba Haruni

hakuchukua cheo chochote yeye mwenyewe, kwamba Mungu alikuwa amemweka katika ofisi takatifu. 3T 347.1

Dathan na Abiram walisema: “Je! Ni jambo dogo kwamba umetuleta kutoka nchi yenye mtiririko wa maziwa na asali, kutuua jangwani, isipokuwa ujifanye mkuu juu yetu? Tena hukutuleta katika nchi itiririkao maziwa na asali, wala hukutupa urithi wa mashamba na mizabibu; je! Utawatoa macho watu hawa? hatutakuja. ” 3T 347.2

Walimshtaki Musa kuwa ndiye sababu ya wao kutoingia Nchi ya Ahadi. Walisema kwamba Mungu hakuwa amewashughulikia hivi, na kwamba hakuwa amesema kwamba watakufa nyikani, na hawataamini kamwe kwamba Bwana alikuwa amesema hivyo; Musa ndiye aliyesema haya, wala si Bwana; na yote yalipangwa na Musa kamwe kutokuwaleta katika nchi ya Kanaani. Walisema juu ya kuwaongoza kwake kutoka nchi ambayo inabubujika maziwa na asali. Katika uasi wao na upofu, walisahau mateso yao huko Misri na mapigo ya uharibifu yaliyoletwa juu ya nchi. Nao sasa wakamshutumu Musa kwa kuwaleta kutoka nchi nzuri ili awaue jangwani, ili apate kutajirika na mali zao. Wakamwuliza Musa, kwa njia ya dharau, ikiwa alifikiri kwamba hakuna hata mmoja wa jeshi la Israeli aliye na hekima ya kutosha kuelewa nia yake na kugundua udanganyifu wake, au ikiwa alifikiri wote wangenyenyekea ili awaongoze kama vipofu kama alivyopenda, wakati mwingine kuelekea Kanaani, kisha kurudi tena kuelekea Bahari ya Shamu na Misri. Walisema maneno haya mbele ya mkutano, nao wakakataa kabisa kukubali mamlaka ya Musa na Haruni. 3T 348.1

Musa aliguswa sana na mashtaka haya yasiyo ya haki. Alimwomba Mungu mbele ya watu ikiwa amewahi kutenda kiholela, na akamsihi awe hakimu wake. Watu kwa ujumla hawakushawishiwa na waliathiriwa na uwongo wa Kora. “Musa akamwambia Kora, kesho wewe na mkutano wako wote uwe mbele za Bwana, wewe, na wao, na Haruni; na kila mtu atwae chetezo chake, na kuweka uvumba ndani yake, mkamletee Bwana kila mtu chetezo chake, vyetezo vyao mia mbili hamsini; wewe pia, na Haruni, kila mmoja chungu chake. Kila mtu akachukua chetezo chake, na kuweka moto ndani yake, na kuweka uvumba juu yake, wakasimama mlangoni pa hema ya kukutania pamoja na Musa na Haruni. 3T 348.2

Kora na wafuasi wake, ambao kwa kujiamini kwao walitamani ukuhani, hata walichukua vifuniko vya moto na kusimama kwenye mlango wa hema na Musa. Kora alikuwa akithamini tamaa yake na uasi wake hadi alipojidanganya mwenyewe, na kweli alifikiri kwamba mkutano huo ni watu wenye haki sana na kwamba Musa alikuwa mtawala dhalimu, akiendelea kukaa juu ya matakwa ya kutaniko kuwa takatifu, wakati hakukuwa na haja yake, kwa kuwa walikuwa watakatifu. 3T 349.1

Hawa waasi walikuwa wamewadanganya/wamewabembeleza watu kwa jumla kuamini kwamba walikuwa sahihi na kwamba shida zao zote zilitokana na Musa,

mtawala wao, ambaye alikuwa akiwakumbusha kila mara dhambi zao. Watu wakadhani kwamba ikiwa Kora angewaongoza na kuwatia moyo kwa kuzingatia matendo yao ya haki badala ya yule ambaye aliwakumbusha makosa yao, wangekuwa na safari yenye amani na ufanisi sana, na bila shaka angewaongoza, sio kwenda nyuma na kisha kwenda mbele katika jangwa, lakini kuingia Nchi ya Ahadi. Wakasema ni Musa aliyewaambia kuwa hawawezi kuingia katika nchi, na kwamba Bwana hakuwa amesema hivi. 3T 349.2

Waasi Waangamia

Kora, kwa kujiamini kwake kulikoinuliwa, alikusanya mkutano wote wa Israeli dhidi ya Musa na Haruni, “mlangoni pa hema ya kukutania; na utukufu wa Bwana ukaonekana kwa mkutano wote. Bwana akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia, Jitengeni wenyewe kati ya mkutano huu, ili niwaangamize kwa muda mfupi. Wakaanguka kifudifudi, wakasema, Ee Mungu, Mungu wa roho za wote wenye mwili, je! Mtu mmoja atatenda dhambi, Nawe utakasirikia mkutano wote? 3T 349.3

“Bwana akanena na Musa, na kuwaambia, Nena na mkutano, ukisema, Ondokeni karibu na maskani ya Kora, Dathani na Abiramu. Musa akainuka, akaenda kwa Dathani na Abiramu; na wazee wa Israeli wakamfuata. Akaongea na mkutano, akisema, Tafadhali, ondokeni kutoka katika hema za watu hawa waovu, wala msiguse kitu chao, msije mkaangamizwa katika dhambi zao zote. Basi wakakwea kutoka katika maskani ya Kora, na Dathani, na Abiramu, pande zote; na Dathani na Abiramu wakatoka, wakasimama mlangoni pa hema zao, na wake zao, na wana wao, na watoto wao wadogo. Musa akasema, Hivi ndipo mtakapojua ya kuwa Bwana amenituma kufanya kazi hizi zote; kwa kuwa sikuyafanya kwa akili yangu mwenyewe. Ikiwa watu hawa watakufa kifo cha kawaida cha watu wote, au ikiwa watatembelewa baada ya kujiliwa na watu wote, basi Bwana hakunituma. Lakini ikiwa Bwana atafanya jambo jipya, na ardhi ikifunua kinywa chake, na kuwameza, pamoja na kila kilicho chao, nao watashuka shimoni haraka; ndipo mtakapoelewa ya kuwa watu hawa wamemkasirisha Bwana.” Musa alipoacha kusema, ardhi ilifunguliwa, na hema zao, na vitu vyao vyote vilimezwa. Walishuka wakiwa hai shimoni, ardhi ikawafunika, na wakaangamia kutoka kwa mkutano. 3T 349.4

Wana wa Israeli waliposikia kilio cha wale waliopotea, walikimbia umbali mrefu kutoka kwao. Walijua kwamba walikuwa na hatia, kwa sababu walikuwa wamepokea mashtaka dhidi ya Musa na Haruni, na waliogopa kwamba wao pia wataangamia pamoja nao. Lakini hukumu ya Mungu ilikuwa bado haijakamilika. Moto ulitoka katika wingu la utukufu na kuwateketeza wale watu mia mbili na hamsini waliotoa uvumba. Hawa walikuwa wakuu-koo za kifalme; Hao ni, watu kwa ujumla wenye uamuzi mzuri na wenye ushawishi katika kutaniko, wanaume mashuhuri. Walioheshimiwa sana, na uamuzi wao mara nyingi ulikuwa umetafutwa

katika mambo magumu. Lakini waliathiriwa na ushawishi mbaya, na wakawa na kijicho, tamaa, wivu, na waasi. Hawakuangamia pamoja na Kora, Dathani, na Abiramu kwa sababu hawakuwa wa kwanza katika uasi. Walikuwa wa kwanza kuona mwisho wa viongozi katika uasi, na walikuwa na nafasi ya kutubu uhalifu wao. Lakini hawakupatanishwa na uharibifu wa watu hao waovu, na hasira ya Mungu iliwajia na kuwaangamiza pia. 3T 350.1

“Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Nena na Eleazari, mwana wa Haruni kuhani, kwamba aondoe vyetezo vyake kutoka motoni, nawe uwatawanye moto huko mbele; kwa kuwa wametakaswa. Vyombo vyake vya kufukizia watenda dhambi hawa dhidi ya nafsi zao, na wazifanyie sahani pana za kufunika kifuniko cha madhabahu; kwa kuwa walizitoa mbele za Bwana, kwa hiyo zimetakaswa; nazo zitakuwa ishara kwa wana wa Israeli. ” 3T 350.2

Uasi Haukuponywa

Baada ya maonesho haya mabaya ya hukumu ya Mungu watu walirudi kwenye mahema yao. Waliogopa, lakini hawakuwa wanyenyekevu. Walikuwa wameathiriwa sana na roho ya uasi na walikuwa wamepongezwa kwa kudanganywa na Kora na wafuasi wake kuamini kwamba walikuwa watu wazuri sana na kwamba walidhulumiwa na kudhalilishwa na Musa. Akili zao zilikuwa zimejaa kabisa roho ya wale ambao walikuwa wameangamia, hivyo ilikuwa ngumu kujiondoa kutoka katika upotofu wa chuki zao. Ikiwa wangekubali kuwa Kora na wafuasi wake wote walikuwa waovu na Musa alikuwa mwadilifu, basi wangelazimika kupokea Neno la Mungu kitu ambacho hawakutaka kuamini, kwamba hakika wote watakufa nyikani. Hawakuwa tayari kunyenyekea katika hili na walijaribu kuamini kwamba yote ni udanganyifu, kwamba Musa alikuwa amewadanganya. Watu waliopotea walikuwa wamesema maneno mazuri kwao na walikuwa wameonesha maslahi/shauku ya pekee na upendo kwao, na walidhani Musa ni mtu anayebuni vitu visivyo halali. Waliamua kuwa hawawezi kukosea; kwamba, baada ya yote, wale watu waliopotea walikuwa watu wazuri, na Musa kwa njia fulani alikuwa sababu ya kuangamizwa kwao. 3T
351.1

Shetani anaweza kuongoza roho zilizodanganywa kwa umbali mrefu. Adui anaweza kupotosha hukumu yao, macho yao, na kusikia kwao. Ilikuwa hivyo kwa Waisraeli. "Lakini siku iliyofuata mkutano wote wa wana wa Israeli walinung'unika dhidi ya Musa na juu ya Haruni, wakisema, Mmewaua watu wa Bwana." Watu walifadhaika na kukatishwa tamaa kwamba jambo hilo lilitokea likitoa upendeleo kwa Musa na Haruni. Kuonekana kwa Kora na wafuasi wake, wote wakitumia vibaya ofisi ya makuhani na vyombo vyao vya kufukuzia, iliwashangaza watu na kuvuta akili zao. Hawakuona kwamba wanaume hawa walikuwa wakidiriki kutoa dharau kali kwa Ukuu wa Mungu. Walipoangamizwa, watu walitishika sana; lakini baada ya muda

mfupi wote walimjia Musa na Haruni kwa fujo, na kuwashtaki kwa damu ya wale waliopotea kwa mkono wa Mungu. 3T 351.2

“Ikawa, mkutano ulipokuwa umekusanyika dhidi ya Musa na dhidi ya Haruni, walitazama kuelekea Hema ya Kukutania; na tazama, wingu liliifunika, na utukufu wa Bwana ukaonekana. Musa na Haruni wakafika mbele ya Hema ya Kukutania. Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Ondokeni kati ya mkutano huu, ili niwaangamize mara moja. Wakaanguka kifudifudi. ” Licha ya uasi wa Israeli na mwenendo wao wa kikatili kwa Musa, bado alionesha kuwajali sawa na hapo awali. Akaanguka kifudifudi mbele za Bwana, akamsihi Yeye awaachilie watu. Wakati alikuwa akiomba Bwana asamehe dhambi za watu Wake, Musa alimwomba Haruni afanye upatanisho wa dhambi zao wakati yeye alibaki mbele za Bwana, ili sala zake ziweze kupanda na ubani na kukubalika kwa Mungu, na kwamba mkutano wote wasiangamie katika uasi wao. 3T 352.1

“Musa akamwambia Haruni, Chukua chetezo, kisha weka moto ndani yake kutoka kwa madhabahu, na weka uvumba, na uende haraka kwa mkutano, ukafanye upatanisho wao; kwa kuwa ghadhabu imetoka kwa Bwana; na pigo limeanza. Haruni akachukua kama vile Musa alivyoamuru, akaenda mbio katikati ya mkutano, na tazama, pigo lilikuwa limeanza kati ya watu; akaweka ubani, akafanya upatanisho wa watu. Akasimama kati ya wafu na walio hai; pigo likazuiliwa. Basi wale waliokufa kwa tauni walikuwa elfu kumi na nne na mia saba [14,700 + 250], kando na wale waliokufa kwa habari ya Kora. Haruni akamrudia Musa mlangoni pa hema ya kukutania; na lile pigo likazuiliwa.” 3T 352.2

Somo kwa Wakati Wetu

Katika kisa cha Kora, Dathani, na Abiramu tuna somo la maonyo ili tusije tukafuata mfano wao. “Wala tusimjaribu Kristo, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaangamizwa na nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyonung'unika, na kuangamizwa na Mwangamizi. Sasa mambo haya yote yaliwapata kwa mifano; na yameandikwa ili kuwaasa, ambao mwisho wa dunia umefika juu yao. ” 3T 353.1

Tunao ushahidi katika Neno la Mungu juu ya dhima ya watu Wake kudanganywa sana. Kuna matukio mengi ambayo yanaweza kuonekana kuwa jitihada ya dhati na ari kwa heshima ya Mungu ina asili yake ya kuacha roho isiyolindwa kwa adui kuijaribu na kupendeza na kugusa akili na hisia potofu ya hali halisi ya mambo. Na tunaweza kutarajia vile vile katika siku hizi za mwisho, kwa maana Shetani yuko na juhudi sana sasa kama vile alivyokuwa katika kusanyiko la Israeli. Nguvu ya ukatili na ubaguzi haieleweki. Baada ya mkutano huo kuwa na ushahidi baada ya kuona kwao kuharibiwa kwa viongozi hawa katika uasi, nguvu ya kushuku/mashaka na kutokuamini ambayo ilikuwa imeruhusiwa katika roho zao haikuondolewa. Waliona ardhi imefunguliwa na viongozi wa uasi wakishuka kwenda ndani ya

matumbo ya dunia-kaburi. Maonesho haya ya kutisha hakika yalipaswa kuwaponya na kuwaongoza kwenye toba ya ndani kabisa kwa unyanyasaji wao kwa Musa. 3T 353.2

Hapa Mungu aliwapa Israeli wote fursa ya kuona na kuhisi dhambi ya mwenendo wao, ambayo ilipaswa kuwaongoza kutubu na kuungama. Aliwapatia waliodanganywa ushahidi mwingi kwamba walikuwa wenye dhambi na kwamba mtumishi Wake Musa alikuwa sahihi. Walikuwa na upendeleo wa kutumia usiku mmoja kwa kutafakari juu ya ugeni wa kutisha wa Mbinguni ambao walikuwa wameushuhudia. Lakini hekima/maamuzi yalikuwa yamepotoshwa. Kora alikuwa amechochea uasi huo, na wakuu mia mbili na hamsini walikuwa wamejiunga naye katika kueneza kutokuelewana. Kusanyiko lote, kwa kiwango kikubwa au kidogo, liliathiriwa na kijicho/wivu uliopo, hisia mbaya, na chuki dhidi ya Musa, ambayo ilileta hasira ya Mungu kwa njia ya kutisha. Walakini Mungu wetu Mwenye neema anajionesha Mwenyewe kuwa Mungu wa haki na rehema. Alitofautisha kati ya wachochezi-viongozi katika uasi-na wale waliodanganywa au kuongozwa nao. Alihurumia ujinga na upumbavu wa wale waliodanganywa. 3T 353.3

Mungu alizungumza na Musa kuamuru kusanyiko liache mahema ya watu ambao walikuwa wamewachagua badala ya Musa. Watu ambao uharibifu wao walitayarisha walikuwa vyombo mikononi mwa Mungu vya kuokoa maisha yao katika hafla hiyo. Musa akasema: "Ondokeni kutoka karibu na maskani ya Kora." Wao pia walikuwa katika hatari ya kutisha ya kuangamizwa katika dhambi zao na ghadhabu ya Mungu, kwani walikuwa washiriki katika uhalifu wa watu ambao walikuwa wamewapa huruma yao na ambao walikuwa wamejiunga nao. 3T 354.1

Ikiwa wakati Musa alikuwa akitoa jaribio mbele ya mkutano wa Israeli, wale ambao walikuwa wameanza uasi wangetubu na kutafuta msamaha wa Mungu na wa mtumishi Wake aliyejeruhiwa, kisasi cha Mungu hata wakati huo kingekomeshwa. Lakini huko katika hema zao kwa ujasiri alisimama Kora, mchochezi wa uasi, na wale waliomwunga mkono, kana kwamba ni wakaidi wa ghadhabu ya Mungu, kana kwamba Mungu hakuwahi kufanya kazi kupitia mtumishi Wake Musa. Na zaidi sana hawa waasi walitenda kana kwamba walikuwa wamepewa heshima ya hivi karibuni na Mungu kwa kuletwa na Musa karibu moja kwa moja katika uwepo Wake, na kuuona utukufu Wake usiokuwa na kifani. Watu hawa walimwona Musa akishuka kutoka mlimani baada ya kupokea zile mbao za pili za mawe na wakati uso wake ulikuwa uking'aa sana na utukufu wa Mungu, hata watu hawakumkaribia, lakini walimkimbia. Aliwaita, lakini walionekana kutishika.
Aliwasilisha vibao vya mawe na kusema: Nimewasihi kwa niaba yako na nimeondoa ghadhabu ya Mungu kutoka kwako. Nilihimiza kwamba, ikiwa Mungu lazima aachwe na kuharibu kutano Lake, jina langu pia linaweza kufutwa kutoka kwa kitabu Chake. Tazama, amenijibu, na hizi mbao za mawe ambazo nimeshika

mkononi mwangu ndio amana niliyopewa ya upatanisho wake na watu Wake. 3T 354.2

Watu wanaona kuwa ni sauti ya Musa; kwamba, ijapokuwa amebadilika na kutukuzwa, yeye ni Musa bado. Wanamwambia kuwa hawawezi kumtazama usoni mwake, kwani nuru inayong'aa katika uso wake inaleta maumivu makali sana kwao. Uso wake ni kama jua; hawawezi kuuangalia. Musa anapogundua shida, hufunika uso wake kwa mtandio/pazia. Hawasihi kwamba nuru na utukufu juu ya uso wake ni onesho la utukufu wa Mungu aliouweka juu yake, na kwamba watu lazima wauchukue kama ulivyo, lakini anafunika utukufu wake. Dhambi ya watu hufanya iwe chungu kuutazama uso wake uliotukuzwa. Ndivyo itakavyokuwa wakati watakatifu wa Mungu watakapotukuzwa kabla tu ya kutokea kwa Bwana wetu mara ya pili. Waovu wataondoka na watajificha mbali na macho yao, kwani utukufu katika sura za watakatifu utawaumiza. Lakini utukufu huu wote juu ya Musa, muhuri huu wote wa Mungu uliyoonekana juu ya mtumishi mnyenyekevu wa Mungu, ulisahaulika. 3T 354.3

Rehema Kidogo

Waebrania walikuwa na nafasi ya kutafakari juu ya mambo ambayo walikuwa wameshuhudia wakati wa kutembelea ghadhabu ya Mungu juu ya wale walio maarufu katika uasi huu mkubwa. Wema na rehema za Mungu zilionesha kwa kutowaangamiza kabisa watu hawa wasio na shukrani wakati ghadhabu yake iliwaka dhidi ya wale waliowajibika zaidi na tukio hili. Aliwapa mkutano ambao walikuwa wamejiruhusu kudanganywa, nafasi ya toba. Ukweli kwamba Bwana, Kiongozi wao asiyeonekana, alionesha uvumilivu mwingi na rehema katika kisa hiki imeandikwa wazi kama ushahidi wa utayari Wake Bwana, wa kuwasamehe wakosaji wakubwa wakati wanahisi dhambi zao na kurudi kwake na toba na udhalilishaji/kujidhili. Mkutano huo ulikuwa umekamatwa katika mwendo wao wa kiburi kwa kuoneshwa kisasi cha Bwana; lakini hawakushawishika kuwa walikuwa wenye dhambi kubwa dhidi Yake, watu wanaostahili ghadhabu Yake kwa njia yao ya uasi. 3T 355.1

Haiwezekani kwa wanaume kutoa tusi kubwa kwa Mungu kuliko kudharau na kukataa watu/vyombo ambavyo ameviteua kuwaongoza. Hawakuwa wamefanya hivi tu, lakini walikuwa wamekusudia kuwaua wote Musa na Haruni. Watu hawa walikimbia kutoka kwa hema za Kora, Dathani, na Abiramu kwa kuogopa uharibifu; lakini uasi wao haukupona. Hawakuwa katika huzuni na kukata tamaa kwa sababu ya hatia yao. Hawakuhisi athari ya dhamiri iliyoamka, iliyosadikishwa kwa sababu walikuwa wametumia vibaya upendeleo wao wa thamani na walitenda dhambi dhidi ya nuru na maarifa. Hapa tunaweza kujifunza masomo muhimu ya uvumilivu wa Yesu, Malaika aliyewatangulia Waebrania jangwani. 3T 355.2

Kiongozi wao asiyeonekana angewaokoa kutokana na uharibifu wa aibu. Msamaha ulikuwa umetulia na kuendelea kukaa juu yao. Inawezekana kwao kupata msamaha ikiwa hata sasa watatubu. Kisasi cha Mungu sasa kimewakaribia na kuwapa wito wa kutubu. Uingiliaji maalum, usioweza kushikiliwa kutoka mbinguni umekamata uasi wao wa kiburi. Ikiwa sasa wataitikia uingiliaji na majilio ya Mungu wanaweza kuokolewa. Lakini toba na udhalilishaji wa mkutano lazima ulingane na makosa yao. Ufunuo wa nguvu ya ishara ya Mungu umewaweka zaidi ya kutokuwa na uhakika. Wanaweza kuwa na ujuzi wa msimamo wa Kweli na wito mtakatifu wa Musa na Haruni ikiwa wataikubali. Lakini kupuuza kwao kuzingatia ushahidi ambao Mungu alikuwa amewapa ilikuwa ni hatari ya kufisha/kifo. Hawakutambua umuhimu wa hatua za haraka kwa upande wao kutafuta msamaha wa Mungu kwa dhambi zao za kutisha na kuleta huzuni. 3T 356.1

Usiku huo wa majaribu kwa Waebrania haukupita kwao kwa kuungama na kutubu dhambi zao, lakini kwa kubuni njia fulani ya kupinga ushahidi uliowaonesha kuwa wao ni wakosaji na wenye dhambi. Bado walithamini chuki yao yenye kijicho kwa watu walioteuliwa na Mungu na kujiimarisha katika mwendo wao wa wazimu wa kupinga mamlaka ya Musa na Haruni. Shetani alikuwa karibu kupotosha hukumu na kuwaongoza wakiwa wamefungwa macho katika uharibifu. Akili zao zilikuwa zimetiwa sumu kabisa na kutoridhika, na walikuwa wameweka jambo hilo bila swali katika akili zao kwamba Musa na Haruni walikuwa watu waovu, na kwamba walihusika na kifo cha Kora, Dathani, na Abiramu, ambao walidhani wangeweza kuwa wakombozi wa Waebrania kwa kuleta utaratibu mzuri wa mambo, ambapo sifa ingechukua mahali pa kukaripia, na amani mahali pa wasiwasi na malumbano/mizozo. 3T 356.2

Siku moja kabla, Waisraeli wote walikuwa wamekimbia kwa hofu kwa kengele ya tahadhari kilio cha wenye dhambi waliotiwa hatia ambao walishuka shimoni; kwani walisema: "Isije ikawa nchi itatumeza sisi pia." "Lakini kesho yake mkutano wote wa wana wa Israeli walinung'unika dhidi ya Musa na juu ya Haruni, wakisema, Mmewaua watu wa Bwana." Kwa ghadhabu yao walikuwa tayari kuweka mikono ya vurugu juu ya watu wa uteuzi wa Mungu, ambao waliamini wamefanya kosa kubwa kwa kuwaua wale ambao walikuwa wazuri na watakatifu. 3T 357.1

Lakini uwepo wa Bwana unadhihirishwa katika utukufu Wake juu ya maskani, na Israeli waasi wanakamatwa katika mwendo wao wa ujuvi na wendawazimu, wa kudhani na wa kimbelembele. Sauti ya Bwana kutoka kwa utukufu Wake wa kutisha sasa inazungumza na Musa na Haruni kwa Maneno yale yale ambayo walikuwa siku moja kabla waliamriwa kuliambia mkutano wa Israeli: “Ondokeni kati ya mkutano huu, ili niwaangamize mara moja.” 3T 357.2

Hapa tunapata maonesho ya kushangaza ya upofu ambao utazunguka akili za wanadamu ambazo zinageuka kutoka kwenye nuru na ushahidi. Hapa tunaona nguvu ya uasi uliotulia, na jinsi ilivyo vigumu kutiishwa/kujisalimisha. Hakika

Waebrania walikuwa na ushahidi wenye kusadikisha zaidi katika kuangamizwa kwa watu ambao walikuwa wamewadanganya; lakini bado walisimama kwa ujasiri na kwa uasi, na ukaidi, wakawashtaki Musa na Haruni kwa kuua watu wazuri na watakatifu. "Kwa maana uasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama uovu na ibada ya sanamu." 3T 357.3

Musa hakuhisi hatia ya dhambi na hakuharakisha kwenda kwa Neno la Bwana na kuliacha kusanyiko kuangamia, kama Waebrania wavyokuwa wamekimbia kutoka kwa hema za Kora, Dathani, na Abiramu siku iliyotangulia. Musa alikawia; kwani hangekubali kuutoa umati huo mkubwa kwenye uharibifu/kuangamia, ingawa alijua kwamba walistahili kisasi cha Mungu kwa uasi wao wa kudumu. Alisujudu mbele za Mungu kwa sababu watu hawakuona ulazima wa kudhalilishwa; aliwaombea/aliwapatanisha na Mungu kwa sababu hawakuona haja ya kuomba kwa niaba yao wenyewe. 3T 357.4

Musa hapa anamuwakilisha Kristo. Wakati huu muhimu na wa dharura, Musa alionesha masilahi ya Mchungaji wa Kweli kwa kundi lake analolitunza. Aliomba kwa kuugua na kusihi, kwamba ghadhabu ya Mungu aliyekosewa isiwaangamize kabisa watu wa chaguo lake. Na kwa maombezi yake alishikilia mkono wa kisasi, kwamba mwisho kamili haukufanywa na Israeli asiye mtiifu, mwasi. Alimwelekeza Haruni jinsi ya kufanya katika shida ile ya kutisha na ya dharura, wakati hasira ya Mungu ilikuwa imetoka na tauni/pigo limeanza. Haruni alisimama na chetezo chake, akikipungia mbele za Bwana, wakati maombezi ya Musa yalipaa na moshi wa ubani. Musa hakuthubutu kusitisha maombi yake. Alishika nguvu ya Malaika, kama vile Yakobo katika mapigano yake, na kama Yakobo alishinda. Haruni alikuwa amesimama kati ya walio hai na wafu wakati jibu la neema lilipokuja: Nimesikia sala yako, sitawaua watu hawa wote-sitawakomesha kabisa. Wanaume wale ambao kusanyiko liliwadharau na kuwa tayari kuwaua, ndio waliowaombea kwa niaba yao kwamba upanga wa kisasi cha Mungu uweze kuondolewa na Israeli wenye dhambi waokolewe. 3T 358.1

Wenye Kudharau Karipio

Mtume Paulo anasema wazi kwamba uzoefu wa Waisraeli katika safari zao umeandikwa kwa faida ya wale wanaoishi katika zama za ulimwengu huu, wale ambao miisho ya ulimwengu imekuja kwao. Hatufikiri kuwa hatari zetu ni kidogo kuliko zile za Waebrania, lakini ni kubwa zaidi. Kutakuwa na majaribu ya wivu na manung'uniko, na kutakuwa na uasi wa wazi, kama ilivyoandikwa kwa Israeli ya kale. Kutaendelea kuwa na roho ya kuinuka wakati wa kukemea dhambi na makosa. Lakini je! Sauti ya kukemea itanyamazishwa kwa sababu ya hii? Ikiwa ndivyo, hatutakuwa katika hali nzuri kuliko ilivyo kwa madhehebu mbali mbali katika nchi yetu ambao wanaogopa kugusa makosa na dhambi za watu zinazoshamiri. 3T 358.2

Wale ambao Mungu amewatenga kuwa wahudumu wa haki wana majukumu yaliyo wakfu/mazito yaliyowekwa juu yao kukemea dhambi za watu. Paulo alimwamuru Tito hivi: “Sema mambo haya, na kutia, na kukemea kwa mamlaka yote. Mtu yeyote asikudharau.” Kuna wale ambao watamdharau yule anayethubutu kukemea dhambi; lakini kuna wakati lazima karipio litolewe. Paulo anamuamuru Tito kukemea tabaka fulani kwa ukali, ili waweze kuwa wazima katika imani, wenye busara ya kiroho. Wanaume na wanawake ambao, pamoja na mashirika yao tofauti, wameletwa pamoja katika nafasi ya kanisa wana upungufu na makosa. Kadri hizi tabia zinavyokuzwa, zitahitaji kukemewa. Ikiwa wale ambao wamewekwa katika nafasi muhimu hawajawahi kukemewa, wala kukemea, hivi karibuni kutakuwa na hali ya kuvunjika moyo kwa mambo ambayo yangemvunjia Mungu heshima sana. Lakini je! Karipio litatolewaje? Wacha mtume ajibu: "Kwa uvumilivu wote na Mafundisho ya imani." Kanuni inapaswa kuletwa kwa yule anayehitaji kukemewa, lakini kamwe makosa ya watu wa Mungu hayapitwi bila kujali-hayarukwi kwa uzembe. 3T 358.3

Kutakuwa na wanaume na wanawake wanaodharau kukaripiwa na ambao hisia zao zitakuwa kinyume na karipio. Haipendezi kuambiwa makosa yetu. Karibu katika kila kisa ambapo kukemea ni muhimu, kutakuwa na wengine ambao hupuuza kabisa Ukweli kwamba Roho wa Bwana amehuzunishwa na shutuma imetolewa kwa kusudi Lake. Hawa watawahurumia wale ambao walistahili kukemewa, kwa sababu hisia binafsi zimeumizwa. Huruma hii yote isiyotakaswa inawaweka wapatanishi ambapo ni washiriki katika hatia ya yule aliyekaripiwa. Katika visa tisa kati ya kumi ikiwa aliyekemewa alikuwa ameachwa chini ya hisia ya makosa yake 9/10, angeweza kusaidiwa kuyaona na kwa hivyo kurekebishwa. Lakini wale wanaoingilia mambo kati, wasaidizi wasiotakaswa huweka ujenzi mbaya kabisa juu ya kusudi la mkemeaji na asili ya karipio lililotolewa, na kwa kumhurumia yule aliyekemewa husababisha ahisi kwamba amenyanyaswa kweli-kweli; na hisia zake huinuka kwa uasi dhidi ya yule ambaye ametimiza tu wajibu wake. Wale ambao kwa uaminifu hufanya majukumu yao yasiyofurahisha/yasiyopendeza chini ya hisia ya uwajibikaji wao kwa Mungu watapata baraka Yake. Mungu anataka waja Wake wawe dhati na wenye bidii daima kufanya mapenzi Yake. Katika agizo la mtume kwa Timotheo anamhimiza "lihubiri Neno; uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiofaa, karipia, kemea na kuonya kwa uvumilivu wote na Mafundisho ya imani.” 3T 359.1

Waebrania hawakuwa tayari kujisalimisha kwenye maagizo na masharti ya Bwana. Walitaka tu njia yao wenyewe, kufuata mwongozo wa akili zao wenyewe, na kudhibitiwa na uamuzi wao wenyewe. Je! Wangeweza kuachwa huru kufanya hivyo, Je, hakuna malalamiko ambayo yangefanywa kwa Musa?; lakini hawakuwa na utulivu chini ya vizuizi. 3T 360.1

Mungu angewataka watu Wake wanidhamishwe/waadabishwe na kuletwa katika upatanifu na utendaji kazi wa matendo, ili waweze kuona kwa macho yao kabisa na kuwa na nia moja na hukumu moja. Ili kuleta hali hii ya mambo, kuna mengi ya kufanywa. Moyo wa matendo ya kimwili lazima ushuke na ubadilishwe. Mungu ameunda kwamba kutakuwa siku zote naShuhuda hai kanisani. Itakuwa muhimu kukemea na kuhimiza, na wengine watahitaji kukemewa vikali, kama kesi inavyodai. Tunasikia ombi: "Ah, mimi ni mwepesi kuathiriwa hisia (hisia zangu ni nyeti), siwezi kuvumilia hata tafakari! (au kukemewa)" Ikiwa watu hawa wangesema kesi hiyo kwa usahihi, wangesema hivi: “mimi ni mtu mwenye nia yenye ukaidi, ninasikia nimejitosheleza, ninajivuna sana, siwezi kuamriwa; Mimi sitakemewa na mtu. Nadai haki ya uamuzi wa mtu binafsi; Nina haki ya kuamini na kuongea nitakavyo. ” Bwana hatatutaka sisi tuondoe upekee au utambulisho wetu. Lakini ni mtu gani ambaye ni hakimu mzuri wa, ni kwa namna gani suala hili la uhuru wa kibinafsi linapaswa kuchukuliwa? 3T 360.2

Petro anawahimiza ndugu zake: “Vivyo hivyo, ninyi vijana, watiini wazee. Naam, nyinyi nyote nyenyekeaneni, na kuvaa mavazi ya unyenyekevu: kwa maana Mungu huwapinga wenye kiburi, na huwapa neema wanyenyekevu.” Mtume Paulo pia anahimiza ndugu zake wa Filipi kwa umoja na unyenyekevu: “basi ikamilisheni furaha yangu kwa kuwa na nia moja, mkiwa na upendo huo moja, mkiwa wa roho na kusudi moja. Msitende jambo lolote kwa nia ya kujitukuza wala kujivuna, bali kwa unyenyekevu kila mtu amhesabu mwingine bora kuliko nafsi yake. Kila mmoja wenu asiangalie faida yake mwenyewe tu, bali pia ajishughulishe kwa faida ya wengine. Iweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu.” Tena Paulo anawahimiza ndugu zake tena: “Mapenzi na yawe yasiyo na unafiki. Chukia yaliyo mabaya; shikamana na yaliyo mema. Pendaneni kwa upendo wa kindugu; kwa heshima mkipendana.” Kwa kuwaandikia Waefeso anasema: "Kujitiisha nyinyi kwa nyinyi kwa kumcha Mungu." 3T 360.3

Historia ya Waisraeli inaweka mbele yetu hatari kubwa ya udanganyifu-kujidanganya. Wengi hawana maana ya asili ya dhambi zao na neema ya msamaha. Wako katika giza la asili, wanakabiliwa na majaribu na udanganyifu mkubwa. Wako mbali na Mungu; lakini wanapata kuridhika sana katika maisha yao, wakati mwenendo wao unachukiwa na Mungu. Kundi hili litapigana vita na uongozi wa Roho wa Mungu, haswa kwa kukaripiwa. Hawataki kusumbuliwa. Wakati mwingine wana hofu ya ubinafsi na madhumuni mazuri, na wakati mwingine mawazo na wasiwasi; lakini hawana uzoefu wa kina, kwa sababu hawajaelekezwa kwa Mwamba wa milele. Kundi hili kamwe halioni umuhimu wa Shuhuda ya wazi [Plain Testimony]. Dhambi haionekani kuwa mbaya sana kwao kwa sababu hiyo kwamba hawatembei katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru. 3T 361.1

Bado kuna kundi lingine ambalo limekuwa na nuru kubwa na usadikisho maalum, na uzoefu wa Kweli katika utendaji wa Roho wa Mungu; lakini majaribu mengi ya

Shetani yameyashinda. Hawathamini nuru ambayo Mungu amewapa. Hawazingatii maonyo na makaripio kutoka kwa Roho wa Mungu. Wako chini ya hukumu. Hawa watakuwa wanapingana na Shuhuda iliyo nyofu [Straight Testimony] kwa sababu unawahukumu. 3T 361.2

Mungu hutengeneza kwamba watu Wake watakuwa kitu kimoja, kwamba wataona macho kwa macho na kuwa na nia moja na hukumu moja. Hii haiwezi kutimizwa bila ushuhuda ulio wazi, ulio hai kanisani. Ombi la Kristo lilikuwa kwamba wanafunzi Wake waweze kuwa kitu kimoja kwani Yeye alikuwa mmoja na Baba Yake. “Wala siwaombei hawa peke yao, bali pia wale ambao wataniamini kupitia neno lao; ili wote wawe kitu kimoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, na Mimi ndani yako, ili wao pia wawe kitu kimoja ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini kwamba Wewe umenituma. Na utukufu ulionipa nimewapa; ili wawe kitu kimoja, kama vile sisi tulivyo mmoja: Mimi ndani yao, na Wewe ndani Yangu, ili wawe wakamilifu katika mmoja; na ulimwengu ujue ya kuwa Wewe umenituma, na uliwapenda, kama vile ulivyonipenda Mimi. ” 3T 361.3

SURA YA 32

WITO KWA VIJANA

Wapendwa Vijana.

Mara kwa mara Bwana amenipa shuhuda za onyo kuhusu ninyi. Yeye Amewapatia faraja ikiwa mtaweka mioyo yenu katika uzuri na utakatifu zaidi Kwake. Wakati Maonyo haya yakiuhishwa kwa wazi mbele yangu, ninahisi hali ya hatari yako ambayo najua wewe hauihisi. Shule iliyoko Battle Creek inaleta pamoja vijana wengi wa aina tofauti wewe kiakilii. Kama vijana hawa hawatajiweka wakfu kwa Mungu na kutii matakwa yake na hawatajinyenyekesha katika njia za Amri zake kuwepo kwa shule hii ya Battle Creek katika mahali hapa kutathibitisha maana kubwa ya kukatishwa tamaa kwa kanisa. Shule hii yaweza kuwa baraka au laana. Ninawaomba ninyi mnaoitwa kwa Jina la Kristo kujitenga na uovu na kujenga tabia ambayo Mungu atapendezwa nayo. {3T 362.1}

Ninauliza: Je! Unaamini kwamba ushuhuda wa karipio ambao umepewa ni wa Mungu? Ikiwa unaamini kweli kwamba sauti ya Mungu imezungumza na wewe, ikionesha hatari zako, je! wewe unatii mashauri yaliyotolewa? Je! Unaweka shuhuda hizi za onyo unaziweka upya akilini mwako kwa kuzisoma mara nyingi kwa mioyo ya maombi? Bwana ameongea nanyi watoto na vijana tena na tena lakini mmekuwa si wepesi kwa tahadhari na maonyo mliyopewa. Ikiwa haujatia uasi moyoni dhidi ya maoni ambayo Mungu ametoa juu ya tabia zako na hatari zako, na dhidi ya njia uliyopewa kufuata, baadhi yenu mmekuwa hamna umakini kwa mambo yanayoohitajika myafanye kwenu ili muweze kupata nguvu ya kiroho na kuwa baraka shuleni, kanisani, na kwa wote mnaoshirikiana nao. 3T 362.2

Vijana wa kiume na wa kike mnawajibika kwa Mungu kwa nuru aliyowapatia ninyi. Nuru hii na maonyo haya yasipotiiwa yataletwa katika hukumu dhidi yenu. Hatari zako zimesemwa wazi; umeonywa na unalindwa kila upande, umezingirwa na maonyo. Katika nyumba ya Mungu umesikiliza Kweli nzito/adhimu, zinazochunguza moyo zilizowasilishwa na watumishi wa Mungu kwa kuoneshwa na Roho. Je Ukweli huu una uzito gani mioyoni mwenu? Je, maonyo yana ushawishi gani juu ya tabia zako? Utawajibika kwa kila moja ya wito na maonyo. Haya

yatainuka katika hukumu kuwashtaki wale ambao waliishi maisha ya ubatili, tamaa na kiburi. {3T 363.1}

Wapendwa marafiki vijana, kile unachopanda, ndicho utakachovuna pia. Sasa ni wakati wa kupanda kwako. Je, mavuno yatakuwa nini? Je, unapanda nini? Kila neno unalotamka, kila tendo unalofanya, ni mbegu ambayo itazaa matunda mazuri au mabaya na itasababisha furaha au huzuni kwa mpazi. Kama vile mbegu zilizopandwa, ndivyo pia mazao. Mungu amekupa nuru kubwa na upendeleo mwingi. Baada ya nuru hii kutolewa, baada ya hatari zako kuwasilishwa wazi mbele yako, jukumu linakuwa lako. Namna unavyoshughulikia nuru ambayo Mungu hukupa itageuza mizani/kiwango cha furaha au ole. Unajitengenezea hatima yako mwenyewe. 3T 363.2

Ninyi nyote mnaushawishi kwa mema au mabaya kwenye akili na tabia za wengine. Na ushawishi ambao unaufanya umeandikwa katika Kitabu cha Kumbukumbu mbinguni. Malaika anayekuhudumia anachukua kumbukumbu ya maneno na matendo yako. Unapoamka asubuhi, je! Unahisi kukosa msaada kwako nahitaji lako la nguvu kutoka kwa Mungu? na je, kwa unyenyekevu, kwa moyo wote unamjulisha Baba yako wa mbinguni mahitaji yako? Ikiwa ndivyo, malaika huweka alama kwenye maombi yako, na ikiwa sala hizi hazijatoka nje ya midomo ya uwongo, wakati uko katika hatari ya kufanya vibaya bila kujua na kutoa ushawishi ambao utasababisha wengine kufanya vibaya, malaika wako mlinzi atakuwa kando yako, kukuhamasisha wewe kuipitia njia bora, kukuchagulia maneno, na kushawishi matendo yako. 3T 363.3

Ikiwa huhisi hatari yoyote, na ikiwa hautoi maombi ya msaada na nguvu ya kupinga vishawishi, utakuwa na uhakika wa kupotea au kurandaranda; kupuuza kwako wajibu kutawekwa alama katika kitabu cha Mungu mbinguni, na utapatikana ukiwa umepunguka katika siku ya kujaribu. Kuna wengine karibu yako ambao wamefundishwa mambo ya kidini/kiroho, na wengine ambao wamedekeshwa, wamebembelezwa, wameendekezwa, na kusifiwa mpaka wameharibiwa uhalisia wa maisha yao kwa kivitendo. Ninazungumza kuhusu watu ninaowajua. Mienendo yao imepotoka sana kwa kujifurahisha/kujiridisha, kujiendekeza, na uvivu kiasi kwamba hawana manufaa kwa maisha haya. Na ikiwa tabia haina faida kwa sasa kuhusu maisha haya, tunaweza kutumaini nini kwa maisha hayo ambayo yote ni ya usafi na utakatifu, na ambapo wote wana mienendo yenye upatano? Nimewaombea watu hawa; Nimezungumza nao mwenyewe. Niliweza kuona ushawishi ambao wangefanya juu ya akili zingine katika kuwaongoza katika ubatili, kupenda mavazi, na uzembe katika kuzingatia masilahi yao ya milele. Tumaini pekee kwa tabaka hili ni kwao kuzingatia njia zao, kunyenyekeza mioyo yao ya kiburi, ya ubatili mbele za Mungu, kufanya ungamo la dhambi zao, na kuongoka. 3T 364.1

Ubatili katika mavazi na vile vile upendo wa burudani ni jaribu kubwa kwa vijana. Mungu ana madai matakatifu juu yetu binadamu wote. Yeye Anadai moyo wote, roho yote, mapenzi yote. Jibu ambalo wakati mwingine wanajibu hapa ni: "Ah, mimi wala sikiri kuwa ni Mkristo!" Je! Vipi ikiwa wewe haukiri kuhusu kuwa Mkristo? Je! Si Mungu huyo huyo aliye na madai hayo hayo juu yako kama yale anayodai juu ya yule anayedai kuwa mtoto Wake? Kwa sababu wewe ni jasiri katika kupuuza kwako vitu vitakatifu, Je! Dhambi yako ya kupuuza na uasi inarukwa au kupuuzwa tu na Bwana? Kila siku unapojali madai ya Mungu, kila fursa ya rehema inayodharauliwa, inadaiwa kwa akaunti yako na itaongeza orodha ya dhambi dhidi yako siku ambayo hesabu za kila roho zitachunguzwa. Ninazungumza wewe, vijana wa kiume na wa kike, unayekiri au usiyekiri kwa mdomo wako: Mungu anataka mapenzi yenu, kwa utii wenu wa furaha na kujitolea kwake. Sasa una muda mfupi wa majaribio, na unaweza kuboresha nafasi hii kufanya kujisalimisha kwa Mungu bila masharti (muda mfupi wa mlango wa rehema kufungwa). 3T 364.2

Utii na kujisalimisha kwa matakwa ya Mungu ni masharti yaliyotolewa na mtume Paulo, aliyevuviwa ili tuwe watoto wa Mungu, washiriki wa familia ya kifalme. Kila mtoto na kijana, kila mwanamume na mwanamke, Yesu amemwookoa kwa damu Yake Mwenyewe kutoka kwenye lindi la uharibifu ambao Shetani alikuwa akiwalazimisha waende. Kwa sababu wenye dhambi hawatakubali wokovu unaotolewa kwao bure, je! Sasa wamefunguliwa au kuwekwa huru kutoka kwa majukumu yao? Chaguo lao la kubaki katika dhambi na makosa ya kijasiri hayapunguzi hatia yao. Yesu alilipa bei yao, nao ni mali Yake. Wao ni mali Yake; na ikiwa hawatatoa utii kwa Yeye ambaye ametoa uhai Wake kwa ajili yao, lakini wakatoa wakati wao na nguvu na talanta zao kumtumikia Shetani, watapata mshahara wao, ambao ni kifo. Utukufu usiokufa na uzima wa milele ni thawabu ambayo Mkombozi wetu anatoa kwa wale ambao watakuwa watiifu Kwake. Yeye Amewafanya waweze kukamilisha tabia ya Kikristo kupitia Jina Lake na kushinda kwa sababu yao wenyewe kama Yeye alivyoshinda kwa niaba yao. Yeye Amewapa mfano katika maisha Yake Mwenyewe, akiwaonesha jinsi wanavyoweza kushinda. “Mshahara wa dhambi ni mauti; lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.” 3T 365.1

Madai ya Mungu yana mashiko sawa kwa binadamu wote. Wale wanaochagua kupuuza wokovu mkuu unaotolewa kwao bure, ambao huchagua kujitumikia wenyewe na kubaki maadui wa Mungu, maadui wa Mkombozi aliyejitolea sana kwa dhabihu yake, wanapata mshahara wao. Wanapanda kwa mwili na mapenzi ya tamaa za mwili huvuna uharibifu. Wale ambao wamemvaa Kristo kwa ubatizo, kwa kitendo hiki huonesha kujitenga kwao na ulimwengu na kwamba wamefanya agano la kutembea katika maisha mapya, hawapaswi kuweka sanamu mioyoni mwao. Wale ambao waliwahi kufurahiya ushahidi wa dhambi kusamehewa, ambao

wameonja upendo wa Mwokozi na ambao huendelea kuungana na maadui wa Kristo, kukataa haki kamili ambayo Yesu huwapa na kuchagua njia ambazo amezikataza, watahukumiwa vikali zaidi kuliko wapagani/makafiri ambao hawajawahi kupata nuru na hawajawahi kumjua Mungu au sheria Yake. Wale ambao wanakataa kufuata nuru ambayo Mungu amewapa, wakichagua burudani, ubatili, na upumbavu wa ulimwengu, na kukataa kufuata mwenendo na matakwa ya haki na matakatifu ya sheria ya Mungu, wana hatia ya dhambi nzito zaidi machoni pa Mungu [aggravating sins]. Hatia yao na mshahara wao utalingana na nuru na nafasi ya upendeleo ambayo wamekuwa nayo. 3T 365.3

Tunaona ulimwengu ukifyonzwa na matumbuizo yao. Mawazo ya kwanza na ya juu zaidi ya sehemu kubwa, haswa ya wanawake, yanaoneshwa. Upendo wa mavazi na raha unaharibu furaha ya maelfu. Na baadhi yao wanaodai kupenda na kuzishika amri za Mungu huliakisi tabaka hilo kwa karibu kadri wawezavyo na kuhifadhi jina la Kristo. Baadhi ya vijana wana hamu ya kujionesha kiasi kwamba wako tayari hata kuliacha Jina la Kristo/Kikristo ikiwa wanaweza tu kufuata mwelekeo wao wa ubatili wa mavazi na kupenda raha. Kujikana kwa mavazi ni sehemu ya jukumu letu la Kikristo. Kuvaa wazi, kujiepusha na maonesho ya vito na mapambo ya kila aina, ni sawa na imani yetu. Je! Sisi ni wale ambao tunaona upumbavu wa walimwengu katika kujiridhisha na ubadhirifu wa mavazi na pia kupenda maburudisho? Ikiwa ndivyo, tunapaswa kuwa tabaka la wale ambao huepuka kila kitu kinachotoa idhini kwa roho hii ambayo inamiliki akili na mioyo ya wale wanaoishi kwa ulimwengu huu tu na ambao hawafikirii au kujali yajayo. 3T 366.1

Vijana wa Kikristo, nimeona ndani ya baadhi yenu upendo wa mavazi na maonesho ambayo yameniumiza. Ndani ya wale ambao wamefundishwa vizuri, ambao wamekuwa na upendeleo/fursa za kiroho/kidini tangu utoto wao, na ambao wamemvaa Kristo kwa ubatizo, na hivyo kudai kuwa wamekufa kwa ulimwengu, nimeona ubatili katika mavazi na kuchukulia mambo kirahisi kwa mizaha na kutojali katika mwenendo ambao umemsikitisha Mwokozi mpendwa na umekuwa aibu kwa kusudi la Mungu. Nimeweka alama kwa maumivu ya kupungua kwako katika dini na tabia yako ya kukata na kupamba mavazi yako. Wengine wamekuwa na bahati mbaya hata kumiliki mikufu ya dhahabu au pini, au yote mawili, na wameonesha ladha mbaya katika kuvionesha hivi, na kufanya vivutie ili wapate umakini wa watu. Lakini naweza kuhusisha tabia hizi na tausi ambaye ana mambo ya kipuuzi, anayeonesha manyoya yake mazuri ili kusifiwa. Ni kwamba ndege huyu masikini anapaswa kuvutia, kwa kuwa sauti yake na umbo lake sio la kuvutia tu. 3T 366.2

Vijana wanaweza kujitahidi katika kutafuta mapambo ya roho ya upole na utulivu, kito cha thamani isiyo na kifani ambacho kinaweza kuvaliwa na neema ya mbinguni. Mapambo haya yatamiliki vivutio kwa wengi katika ulimwengu huu, na

yatathaminiwa kwa bei kubwa na malaika wa mbinguni, na zaidi ya yote na Baba yetu wa mbinguni, na yatawastahilisha wavaaji kwa kukaribishwa kama wageni katika nyua za mbinguni. 3T 367.1

Vijana wana vitivo ambavyo, kwa ukuzaji unaofaa au bora, vingeweza kustahili karibu nafasi yoyote ya uaminifu/dhamana. Ikiwa wangefanya hivyo kuwa lengo lao kupata elimu ya kufanya mazoezi na kukuza nguvu ambazo Mungu amewapa ili ziweze kunufaisha na kudhihirisha baraka kwa wengine, akili zao hazingekuwa duni kwa kiwango cha chini vile. Wangeonesha kina cha mawazo na uthabiti wa kanuni, na wangeamuru ushawishi na heshima. Wanaweza kuwa na ushawishi wa kuinua juu ya wengine, ambao ungeongoza roho kuona na kutambua nguvu ya maisha ya Kikristo yenye hekima/akili mahiri. Wale ambao wanajali sana mapambo kwa ajili ya maonesho kuliko kuelimisha akili na kutumia nguvu zao kwa faida kubwa, ili wamtukuze Mungu, hawatambui uwajibikaji wao kwa Mungu. Watakuwa na mwelekeo wa kuwa watu wa juu juu katika yote wanayofanya na watapunguza manufaa yao na kudhoofisha akili zao. 3T 367.2

Ninahisi uchungu sana moyoni kwa baba na mama wa vijana hawa, na pia kwa watoto. Kumekuwa na ukosefu wa mafunzo ya watoto hawa, ambayo inaacha jukumu mazito mahali pengine. Wazazi ambao wamedekesha au wamewabembeleza na kuwaingiza watoto wao badala ya kuwazuia kwa kanuni za busara, wanaweza kuona tabia walizozitengeneza. Kama mafunzo yalivyokuwa, ndivyo tabia zilivyopindishwa. 3T 367.3

Ibrahimu Mwaminifu

Akili yangu inarudi nyuma kwa Ibrahimu mwaminifu, ambaye, kwa kutii amri ya Mungu aliyopewa katika maono ya usiku huko Beersheba, anaendelea na safari yake na Isaka akiwa kando yake. Anaona mbele yake mlima ambao Mungu alikuwa amemwambia atamwonesha kwa ishara Kama sehemu anayotakiwa kutoa kafara juu yake. Anaondoa kuni kutoka kwenye bega la mtumishi wake na kuziweka juu ya Isaka, yule atakayetolewa sadaka. Anajifunga nafsi yake kwa ukakamavu na ushupavu wenye uchungu mkali, tayari kwa kazi ambayo Mungu anamtaka afanye. Kwa moyo uliovunjika na mkono ambao unatetemeka au kuvunjika moyo, anachukua moto, wakati Isaka anauliza: Baba, moto uko hapa na kuni; lakini hiyo sadaka iko wapi? Lakini, oh, Ibrahimu hawezi kumwambia sasa! Baba na mwana wanajenga madhabahu, na wakati mbaya sana unakuja kwa Ibrahimu kumjulisha Isaka yale ambayo yameumiza moyo wake katika safari hiyo ndefu, kwamba Isaka mwenyewe ndiye kafara. Isaka sio kijana mdogo; ni kijana aliyekua mtu mzima. Angeweza kukataa kutii mpango wa baba yake ikiwa angechagua kufanya hivyo. Hamshtaki baba yake kwa uwendawazimu, wala hatafuti kubadilisha kusudi lake. Anatii. Anaamini katika upendo wa baba yake na kwamba hangetoa kafara hii ya

kutisha ya mwanawe wa pekee ikiwa Mungu hakumwamuru afanye hivyo. Isaka amefungwa na mikono inayotetemeka, yenye upendo ya baba yake mwenye huruma kwa sababu Mungu amesema. Mwana hujisalimisha kwa kafara kwa sababu anaamini uadilifu wa baba yake. Lakini kila kitu kinapokuwa tayari, wakati imani ya baba na utii wa mtoto vimejaribiwa kabisa, malaika wa Mungu anazuia mkono ulioinuliwa wa Ibrahimu ambao uko karibu ya kumuua mwanawe na kumwambia kuwa sasa inatosha. "Sasa najua ya kuwa unamcha Mungu, kwa kuwa hukunizuia mwanao, mwanao wa pekee Kwangu." 3T 368.1

Tendo hili la imani kwa Ibrahimu limeandikwa kwa faida yetu. Linatufundisha somo kuu la kujiamini/kujitumainisha kwa Mungu katika mahitaji yote, hata yawe ya kufunga na ya kuumiza; na inafundisha watoto kujitiisha kikamilifu kwa wazazi wao na kwa Mungu. Kwa utii wa Ibrahimu tunafundishwa kuwa hakuna kitu cha thamani sana kwetu tusichoweza kumtolea Mungu. 3Tsw 368.2
Isaka alikuwa mfano wa Mwana wa Mungu, ambaye alitolewa kafara kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Mungu angeweka mkazo kwa Ibrahimu wa injili ya wokovu kwa mwanadamu. Ili kufanya hivyo, na kuufanya Ukweli huu kuwa halisi kwake pamoja na kujaribu imani yake, Alimtaka amuue mpenzi wake Isaka. Huzuni na uchungu wote ambao Ibrahimu alivumilia wakati wa jaribio hilo la giza na la kutisha, ulikuwa kwa kusudi la kusisitiza sana juu ya uelewa wake katika mpango wa ukombozi kwa mwanadamu aliyeanguka. Alifanywa kuelewa katika uzoefu wake mwenyewe jinsi ambavyo kujikana kwa Mungu asiye na mwisho kwa kumtoa Mwanawe mwenyewe afe ili kumwokoa mwanadamu kutoka kwa uharibifu kabisa hakuwezi elezeka. Kwa Ibrahimu hakuna mateso ya akili ambayo yangeweza kuwa sawa na yale ambayo alivumilia kwa kutii amri ya Mungu ya kumtoa kafara mwanawe [mental torture]. 3T 369.1

Mungu alimpa Mwanawe maisha ya fedheha, kujikana, umaskini, taabu, lawama, na kifo cha maumivu ya kusulubiwa. Lakini hakukuwa na malaika wa kubeba ujumbe huu wa furaha kwa Masihi kwamba: “Inatosha; Hauhitaji kufa, Mwanangu mpendwa.” Vikosi vya malaika vilikuwa vikingojea kwa huzuni, wakitumai kwamba, kama ilivyokuwa kwa Isaka, Mungu atazuia kifo Chake cha aibu wakati wa mwisho. Lakini malaika hawakuruhusiwa kupeleka ujumbe wowote kama huo kwa Mwana mpendwa wa Mungu. Udhalilishaji katika ukumbi wa mahakama na katika njia ya kuelekea Kalvari uliendelea. Alidhihakiwa, alichekwa, na kutemewa mate. Alivumilia kejeli, dhihaka, na matusi ya wale waliomchukia, mpaka juu ya msalaba alipoinamisha kichwa na kufa. 3T 369.2

Je! Mungu anaweza kutupa uthibitisho wowote mkubwa wa upendo Wake kuliko ule wa kumtoa Mwanawe kupita katika tukio hili la mateso? Na kama zawadi ya Mungu kwa mwanadamu ilivyokuwa zawadi ya bure, upendo Wake hauna kikomo, kwa hivyo madai yake juu ya ujasiri wetu, utii wetu, moyo wetu wote, na utajiri

wa mapenzi yetu hayana kikomo vilevile. Yeye Anahitaji yote ambayo yanawezekana kwa mwanadamu kutoa. Utii kwa upande wetu lazima ulingane sawa na zawadi ya Mungu; ni lazima uwe kamili na usiopunguka chochote. Sisi sote ni wadeni kwa Mungu. Yeye Ana madai juu yetu ambayo hatuwezi kuyalipa bila kujitoa kikamilifu na kuwa dhabihu ya hiari. Bwana Anadai utii wa haraka na wa hiari, na hakubali kitu chochote pungufu ya hiki. Tuna nafasi sasa kupata upendo na upendeleo wa Mungu. Mwaka huu unaweza kuwa mwaka wa mwisho katika maisha ya wengine waliosikia au kusoma ujumbe huu. Je! Kuna yeyote kati ya vijana ambao amesikia/amesoma wito huu ambao wangechagua raha za ulimwengu kabla ya amani hiyo ambayo Kristo humpa mtafutaji dhati na mwenye bidii na mtendaji wa mapenzi Yake? 3T 369.3

Mungu anazipima tabia zetu, mwenendo wetu, na nia zetu katika mizani ya Patakatifu. Itakuwa jambo la kuogofya kutamkwa tukitaka kwa upendo na utii kwa Mkombozi wetu, ambaye alikufa msalabani ili kusogeza mioyo yetu Kwake. Mungu ametupa zawadi kubwa na ya thamani. Yeye Ametupa nuru na ujuzi wa mapenzi Yake, ili kwamba tusipotee au kutembea gizani. Kupimwa katika mizani na kupatikana umepungua katika siku ya mwisho na thawabu litakuwa jambo la kutisha, kosa baya ambalo haliwezi kurekebishwa kamwe. Marafiki wadogo, je! Kitabu cha Mungu kitatafutwa/kitachunguzwa bure kwa majina yenu? (na yasipatikane?)3T 370.1

Mungu amekuteuwa kufanya kazi yake ambayo itakufanya uwe mtendakazi pamoja naye. Karibu na wewe kuna roho za kuokoa. Kuna wale ambao unaweza kuwatia moyo na kuwabariki kwa juhudi zako za dhati. Unaweza kugeuza roho kutoka dhambini kwenda katika nuru. Unapohisi uwajibikaji wako kwa Mungu utahisi hitaji la uaminifu katika maombi na uaminifu katika kujilinda dhidi ya majaribu ya Shetani. Utakuwa, ikiwa kweli wewe ni Mkristo, utahisi kuomboleza juu ya giza la kimaadili la ulimwenguni kuliko kujiridhisha katika kuendekeza katika mizaha na kiburi cha mavazi. Utakuwa kati ya wale wanaougua na kulia kwa machukizo yanayofanywa katika nchi-Ezek 9. Utapinga vishawishi vya Shetani vya kujiridhisha na kuendekeza ubatili, kukata vito na mapambo ya maonesho. Akili ni finyu na ufahamu umepungua ambao unaweza kuridhishwa na vitu hivi vya ujinga hadi kupuuzia majukumu ya hali ya juu. 3T 370.2

Vijana katika siku zetu wanaweza kuwa watendakazi na Kristo ikiwa watatataka hivyo; na katika kufanya kazi, imani yao itaimarika na maarifa yao kuhusu Mungu yataongezeka. Kila kusudi la Kweli na kila tendo la kutenda sahihi litarekodiwa katika Kitabu cha Uzima. Natamani ningewaamsha vijana kuona na kuhisi dhambi ya kuishi kwa kujiridhisha na kudhoofisha akili zao kwa vitu visivyo na thamani na vya ovyo tu, vya ubatili vya maisha haya. Ikiwa wangenyanyua mawazo na maneno

yao juu ya vivutio vya kijinga vya ulimwengu huu na kufanya malengo yao kumtukuza Mungu, amani Yake, inayopita ufahamu wote, ingekuwa yao. 3T 370.3

Fedheha ya Kristo

Je! Yeye Aliye mfano wetu hakuiendea njia ngumu, ya kujikana nafsi, kujitolea dhabihu, na ya unyenyekevu kwa ajili yetu ili kutuokoa? Yeye Alikumbana na magumu, taabu, uzoefu wa kukatishwa tamaa, unyenyekevu, aibu na mateso katika kazi Yake ya kutuokoa. Na Je! sisi Tukatae kufuata pale ambapo Mfalme wa utukufu ameongoza njia? Je! Tulalamike tu juu ya shida na majaribu katika kazi ya kuyashinda kwa ajili yetu wenyewe, wakati tunakumbuka mateso ya Mkombozi wetu katika jangwa la majaribu, katika Bustani ya Gethsemane, na Kalvari? Haya yote yalistahimiliwa ili kutuonesha njia na kutuletea msaada wa Mungu ambao ni lazima tuwe nao au tuangamie. Ikiwa vijana wangepata maisha ya umilele, wasingehitaji kutarajia kufuata mwelekeo wao wenyewe. Tuzo itawagharimu kitu, ndio, kila kitu. Wanaweza sasa kuwa na Yesu au ulimwengu. Vijana wapendwa wangapi watapata shida, uchovu, taabu, na wasiwasi ili kujihudumia wenyewe na kupata kitu katika maisha haya! Hawafikirii kulalamika juu ya shida na ugumu wanaopitia ili kutumikia maslahi na matakwa yao. Kwa nini, basi, wajiepushe na magomvi, migogoro, kujikana nafsi, au kujitoa ili kupata uzima wa milele? 3T 371.1

Kristo alikuja kutoka katika nyua za utukufu kuja katika ulimwengu huu uliochafuliwa na dhambi na kujinyenyekeza hadi ubinadamu. Yeye Alijitambulisha Yeye Mwenyewe kwa udhaifu wetu na alijaribiwa katika kila hali na vipengele vyote kama sisi. Kristo alikamilisha tabia ya haki hapa duniani, si kwa sababu Yake Mwenyewe, kwa kuwa tabia Yake ilikuwa safi na isiyo na doa, bali kwa mwanadamu aliyeanguka. Tabia Yake atampatia mwanadamu ikiwa atakubali. Mdhambi, kupitia toba ya dhambi zake, imani katika Kristo, na utii wa sheria kamilifu ya Mungu, anakuwa na haki ambayo Kristo ameithibisha Kwake; inakuwa haki yake, na jina Lake linaandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo. Anakuwa mtoto wa Mungu, mwanachama wa familia ya kifalme. 3T 371.2

Yesu alilipa bei isiyo na kikomo ili kuukomboa ulimwengu, na jamii za watu aliopewa mikononi Mwake; wakawa mali Yake. Yeye Alitoa dhabihu hadhi/heshima Yake, utajiri Wake, na nyumba Yake tukufu katika nyua za kifalme na kuwa mtoto wa Yusufu na Mariamu. Yusufu alikuwa mmoja wa wafanyakazi wa chini kabisa wa siku hizo. Yesu pia alifanya kazi; aliishi maisha ya shida na taabu. Wakati huduma Yake ilipoanza, baada ya Ubatizo wake, Alivumilia mfungo mchungu wa karibu wiki sita. Haikuwa tu maumivu ya njaa ambayo yalifanya mateso Yake kuwa mazito sana, bali taabu ya hatia ya dhambi za ulimwengu zilizoweshinikizwa juu yake kwa ukali. Yeye ambaye hakujua dhambi alifanywa kuwa dhambi kwa ajili yetu. Kwa

uzito huu mbaya wa hatia juu Yake kwa sababu ya dhambi zetu Alipinga jaribio la kutisha juu ya hamu ya kula, tamaa na juu ya kupenda ulimwengu na heshima, na kiburi cha kuonekana/kujionyesha kinachopelekea kudhania ujuvi [presumption]. Kristo alivumilia majaribu haya matatu makubwa na akashinda kwa niaba ya mwanadamu, akamfanyia tabia ya haki, kwa sababu alijua mtu hangeweza kufanya haya mwenyewe. Alijua kwamba juu ya mambo haya matatu, Shetani alitaka kushambulia jamii za watu. Alikuwa amemshinda Adamu, na alibuni kuendelea mbele na kazi Yake hadi amalize uangamivu/uharibifu wa mwanadamu. Kristo aliingia shambani kwa niaba ya mwanadamu na kumshinda Shetani kwa ajili yake kwa sababu Aliona kuwa mwanadamu hangeweza kushinda kwa niaba yake mwenyewe. Kristo aliandaa njia ya ukombozi wa mwanadamu kwa maisha Yake Mwenyewe ya mateso, kujinyima, kujikana nafsi, na kujitolea, na kwa fedheha Yake na kifo Chake cha mwisho. Alileta msaada kwa mwanadamu ili, kwa kufuata mfano wa Kristo, apate kushinda mwenyewe, kama vile Kristo alivyoshinda kwa ajili yake. 3T 372.1

Je! hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, na ninyi si mali yenu? kwa kuwa mmenunuliwa kwa bei; kwa hivyo mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na kwa roho zenu ambazo ni za Mungu. " “Hamjui ya kuwa ninyi ni hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Mtu yeyote akilinajisi hekalu la Mungu, Mungu atamharibu; kwa kuwa hekalu la Mungu ni takatifu, ninyi ndio hekalu.” “Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; Kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana mapatano gani kati ya Kristo na Beliali? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na asiyeamini? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, Nitakaa ndani yao, Nami nitatembea kati yao; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wana wangu na binti zangu, asema Bwana Mwenyezi.” 3T 372.2

Ni kwa neema, ukarimu, wema na kwa upole wa kiasi gani kwamba Baba yetu wa mbinguni anashughulika na watoto Wake! Yeye Anatulinda sisi kutokana na hatari elfu moja zisizoonekana kwetu na anatulinda na udanganyifu na hila zilizojificha za Shetani, tusije wakaangamizwa. Kwa sababu ulinzi wa Mungu kupitia malaika Wake hauonekani na maono yetu mepesi, hatujaribu kutafakari na kuthamini nia ya uangalizi ambayo Muumba wetu Mwenye fadhili, mkarimu na mwema anayo katika kazi ya mikono Yake; na hatushukuru kwa wingi wa rehema anazotupa kila siku. 3T 373.1

Vijana ni wajinga, hawajui hatari nyingi ambazo wanapata kila siku. Hawawezi kuzifahamu zote kikamilifu; lakini ikiwa watakuwa waangalifu na wenye maombi, Mungu atazifanya dhamiri zao kuwa makini na mitazamo yao wazi, ili waweze kutambua utendaji wa adui na kuimarishwa dhidi ya mashambulio yake. Lakini vijana wengi kwa muda mrefu wamefuata mielekeo yao kwamba wajibu ni neno lisilo na maana kwao. Hawatambui majukumu ya juu na matakatifu ambayo wanaweza kufanya kwa faida ya wengine na kwa utukufu wa Mungu; na wanapuuza kabisa kuyafanya. 3T 373.2

Ikiwa vijana wangeweza kuamka na kuhisi hitaji lao la kina, la dhati la nguvu kutoka kwa Mungu kupinga vishawishi vya Shetani, ushindi bora ungekuwa wao, na wangepata uzoefu muhimu katika vita vya Kristo. Ni wachache tu wa vijana wanaofikiria himizo la mtume Petro aliyevuviwa: “Kuwa wenye kiasi, kuwa macho; kwa sababu adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze, nanyi mpingeni huyo mkiwa thabiti katika imani.” Katika maono aliyopewa Yohana aliona nguvu ya Shetani juu ya wanadamu na akasema: "Ole wa nchi na bahari! kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu, mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache” 3T 373.3

Usalama pekee kwa vijana ni katika kukesha bila kukoma na sala ya unyenyekevu. Hawana haja ya kujidanganya kwamba wanaweza kuwa Wakristo bila haya. Shetani anaficha vishawishi vyake na hila zake chini ya kifuniko cha taa, kama vile alipomkaribia Kristo jangwani. Wakati huo alikuwa akionekana kama mmoja wa malaika wa mbinguni. Adui wa roho zetu atatujia kama mgeni wa mbinguni, na mtume anapendekeza tuwe na kiasi na umakini katika kukesha kama usalama wetu pekee. Vijana wanaoendekeza na kujiridhisha katika uzembe, vichekesho, mizaha na mivuto, na wanaopuuza majukumu ya Kikristo, wanaendelea kuanguka chini ya majaribu ya adui, badala ya kushinda kama Kristo alivyoshinda. 3T 374.1

Huduma ya Kristo sio yenye kuhenyesha na ngumu kwa roho iliyowekwa wakfu kikamilifu. Utii kwa Mwokozi wetu hauondoi furaha yetu na raha ya Kweli katika maisha haya, lakini una nguvu ya kubadilisha, kutakasa, kuboresha na kuinua tabia zetu. Utafiti/ujifunzaji wa kila siku wa maandiko ya thamani ya maisha yanayopatikana katika Biblia huimarisha akili na kutoa ujuzi wa matendo makuu na matukufu ya Mungu kwa uhalisia kwenye asili/uumbaji. Kupitia kusoma Maandiko tunapata maarifa sahihi ya jinsi ya kuishi ili kufurahiya kiwango kikubwa cha furaha ambayo isiyo na mawaa, na ile ambayo hatujawahi kuipata. Mwanafunzi wa Biblia pia amepewa hoja za Maandiko ili aweze kukukabiliana mashaka ya wasioamini na kuyaondoa kwa mwangaza wazi wa Ukweli. Wale wanadamu ambao wamechunguza Maandiko wanaweza kuimarishwa dhidi ya majaribu ya Shetani; sisi tunaweza kupatiwa ukamilifu kabisa ili tupate kutenda

kila tendo jema na kuwa tayari kumpa kila mtu anayetuuliza sababu ya tumaini lililo ndani yao [2Tim 3:17]. 3T 374.2

Maoni mara nyingi huachwa akilini kwamba dini ni ya kudhalilisha mtu na kwamba ni kujishusha chini au kujinyenyekeza kwa watenda dhambi kukubali kiwango cha Biblia kama kanuni/sheria yao ya maisha. Wanafikiri kuwa mahitaji yake hayayamfanyi mtu kuwa bora na mwungwana, aliyesatakaswa na kwamba, kwa kuikubali, lazima waachilie ladha zao zote, na kufurahiya kile kilicho kizuri, na badala yake lazima wakubali udhalilishaji na uharibifu-kushushwa chini. Shetani huwa hafanyi udanganyifu mkubwa juu ya akili kuliko huu. Dini safi ya Yesu inahitaji wafuasi Wake wawe na usahili na uzuri wenye unyenyekevu wa asili na uboreshaji wa usafi wa asili na utakasaji ulioinuliwa, badala ya feki/bandia na uwongo. 3T 374.3

Ingawa dini safi huonekana kuwa ngumu katika matakwa/mahitaji yake na, haswa kwa vijana, ikilinganishwa vibaya na mapambo ya uwongo na vivutio vya ulimwengu, mahitaji ya Bibilia yanazingatiwa kama mitihani ya kudhalilisha, ya kujikana nafsi, ambayo huchukua starehe za maisha kutoka kwao. Lakini dini la Biblia daima huwa na mwelekeo wa kuinua na kusafisha. Na laiti wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangefanya kanuni za dini iliyo safi katika maisha yao, dini ya Kristo ingekubalika kwa akili bora/zilizosafishwa zaidi. Dini ya Biblia haina kitu ndani yake ambacho kingeweza kuzingatia hisia nzuri zaidi. Hakika katika maagizo na mahitaji yake yote, dini ya Biblia ni safi kama tabia ya Mungu na imeinuliwa kama kiti Chake cha enzi. 3T 375.1

Mkombozi wa ulimwengu ametuonya dhidi ya kiburi cha maisha, lakini sio dhidi ya neema Yake na uzuri wa asili. Yeye Alielekeza kwa uzuri wote unaong'aa wa maua ya kondeni na kwa maua ya yungiyungi/lily yaliyopumzika katika usafi wake bila doa kifuani mwa ziwa na akasema: “Tafakari maua ya kondeni, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti; lakini bado nawaambia, Hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa uzuri kama mojawapo ya hayo.” Hapa anaonesha kwamba licha ya watu wanaweza kuwa na uangalifu mkubwa, na wanaweza kufanya kazi kwa uchovu kujifanyia wenyewe vitu vya kupendeza na mapambo yao ya nje na maonyesho, mapambo yao yote ya bandia, ambayo wanayathamini sana, hayatalingana na maua sahili/rahisi ya shamba kwa uzuri wa asili. Hata maua haya rahisi, na mapambo ya Mungu, yangeangalia mavazi mazuri ya Sulemani kwa uzuri. "Hata Sulemani katika fahari yake yote hakuwa amevalishwa kama moja ya haya." 3T 375.2



Hapa kuna somo muhimu kwa kila mfuasi wa Kristo. Mkombozi wa ulimwengu anazungumza na vijana. Je! wewe Utasikiliza Maneno Yake ya mafundisho ya mbinguni? Anawasilisha mbele yako mandhari ya mawazo ambayo yatakuza, kuinua, kusafisha, na kutakasa, lakini ambayo hayatadhalilisha au kudhoofisha akili. Sauti Yake inazungumza nawe: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Jiji lililowekwa juu ya mlima haliwezi kufichwa. ” "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu Aliye mbinguni." Nuru ya Mungu ikiwa ndani yako, itawaangazia wengine. Haiwezi kamwe kufichwa. 3T 376.1

Vijana wapendwa, tabia iliyo ndani yako ya kuvaa kulingana na mitindo, na kuvaa mapambo yenye utepe na dhahabu na vitu bandia kwa ajili maonesho, haitapendekeza kwa wengine dini yako au Ukweli ambao unakiri. Watu wenye utambuzi wataangalia kujaribu kwako kujipendezesha kwa nje kama uthibitisho wa akili dhaifu na mioyo yenye kiburi. Mavazi sahili/rahisi ya wazi, yasiyometameta yatakuwa mapendekezo kwa dada zangu vijana. Kwa njia bora zaidi unaweza, wewe kuruhusu nuru yako iangaze kwa wengine kuliko katika usahili wako wa mavazi na mwenendo/hulka. Unaweza kuonesha hayo yote,

ukiyalinganisha na vitu vya milele, unaweka thamani halisi juu ya vitu vya maisha haya. 3T 376.2

Sasa ni fursa yako ya pekee, na thamani/dhahabu, kutengeneza tabia safi na takatifu ya mbinguni. Hauwezi kumudu kujitolea wakati huu wa thamani katika mapambo ya nguo/vitambaa na kukosa mpangilio na kujipendezesha kwa nje kwa kupuuza mapambo ya ndani. Hebu “Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje yaani kusuka nywele, na kujitia dhahabu, au kuvaa mavazi; lakini na iwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.” 3T 376.3

Mungu, aliyeumba kila kitu chema na kizuri ambacho jicho huvutiwa, ni mpenda uzuri. Yeye Anakuonesha wewe jinsi Anavyowekea viwango vya thamani kwenye uzuri halisi. Mapambo ya roho ya upole na utulivu yana thamani kubwa machoni pake. Je! Sisi Hatutaki kutafuta kwa dhati na bidii kupata kile ambacho Mungu anakionesha kuwa cha thamani zaidi kuliko mavazi ya gharama kubwa au lulu au dhahabu? Mapambo ya ndani, ukarimu na neema ya upole, roho inayopatana na malaika wa mbinguni, haitapunguza hadhi ya Kweli ya tabia au kutufanya tusipendeze hapa ulimwenguni. 3T 376.4

Dini, safi na isiyo na unajisi, humpa sifa mmiliki wake. Utapata kila wakati kwa Mkristo wa Kweli uchangamfu uliothibishwa na wenye alama, imani takatifu, yenye furaha kwa Mungu, na kujisalimisha kwa huduma Yake, ambayo inaburudisha na kufurahisha roho. Kwa Mkristo, upendo wa Mungu na wenma/fadhili zinaweza kuonekana katika kila fadhila anayopokea. Uzuri katika maumbile ni mada ya kutafakari. Katika kujifunza uzuri wa asili unaotuzunguka, akili huchukuliwa kupitia maumbile kwa Mtunzi wa yote yanayopendeza. Matendo yote ya Mungu yanazungumza na hisia na akili zetu, yakikuza nguvu Zake, yakinyanyua hekima Yake. Kila kitu kilichoumbwa kina zawadi inayomvutia na kumchangamsha mtoto wa Mungu na hutengeneza ladha yake kwa kuzingatia ushahidi huu wa thamani wa upendo wa Mungu juu ya kazi ya stadi ya mwanadamu. 3T 377.1

Nabii huyu, kwa Maneno ya hamasa inayong'aa, humtukuza Mungu katika kazi Zake zilizoumbwa: "Wakati ninapozitazama mbingu , kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota, ulizoziweka; Mtu ni nini hata umkumbuke? na mwanadamu hata umtembelee? “Ee Bwana Bwana wetu, Jina Lako ni lililo bora duniani kote! Nitakusifu, ee Bwana, kwa moyo wangu wote; Nitaonesha maajabu Yako yote Zaburi 8. [How Excellent is your work] ” 3T 377.2

Ukosefu wa dini ndio hufanya njia ya maprofesa wengi wa dini iwe ya kivuli [wale wanaoikiri dini kwa mdomo au watu feki, huleta kivuli/huzuni]. Kuna wale ambao wanaweza kuonekana kana kwamba ni Wakristo lakini hawastahili jina hilo.

Hawana tabia ya Kikristo. Wakati Ukristo wao unapojaribiwa, udanganyifu wake hujidhihirisha.
Dini ya Kweli inaonekana katika mwenendo wa kila siku. Maisha ya Mkristo yanajulikana kwa kufanya juhudi za dhati na bidii, na zisizo na ubinafsi kufanya kazi nzuri kwa wengine na kumtukuza Mungu. Njia yake sio ya giza na ya huzuni. Mwandishi aliyevuviwa alisema: “Lakini njia ya wenye haki ni kama nuru iangazayo, inayoangaza zaidi na zaidi hata mchana mkamilifu. Njia ya waovu ni kama giza; hawajui ni kitu gani kiwakwazacho.” 3T 377.3

Na Je! Vijana wataishi maisha ya ubatili, yasiyo na thamani na yasiyo na fikra ya mitindo na ujinga, wakifanya akili zao kuwa fupi katika mambo ya mavazi na kutumia wakati wao kwa raha na tamaa za mwili? Wakati hawajawa tayari, Mungu anaweza kuwaambia: "Usiku huu upumbavu wako utaisha." Yeye Anaweza kuruhusu ugonjwa wa mauti uje juu ya wale ambao hawajazaa matunda kwa utukufu Wake. Wakati wanakabiliwa na uhalisia wa milele, wanaweza kuanza kutambua thamani ya wakati na maisha waliyopoteza. Wanaweza basi kuwa na hisia fulani ya thamani ya roho. Wanaona kwamba maisha yao hayajamtukuza Mungu kwa kuwaongoza wengine kwenda mbinguni kwa kuwaangazia njia yao. Wameishi kwa kujitukuza. Na wakiharibiwa na maumivu na uchungu wa roho hawawezi kuwa na dhana wazi ya vitu vya milele. Wanaweza kutazama maisha yao ya zamani, na kwa majuto yao kila mmoja anaweza kulia: "Sijamfanyia chochote Yesu, ambaye amenifanyia kila kitu mimi. Maisha yangu yamekuwa kufeli kukubwa au kwa kutisha (maanguko).” 3T 377.4

Unapoomba, kijana mpendwa, kwamba usiingie kwenye majaribu, kumbuka kuwa kazi yako haiishii katika maombi. Lazima basi ujibu sala yako mwenyewe kwa kadiri inavyowezekana kwa kupinga majaribu, na uache yale ambayo huwezi kujifanyia mwenyewe kwa Yesu ili akufanyie. Huwezi kulindwa sana kwa maneno yako na katika mwenendo wako, usije ukamwalika adui kukujaribu. Vijana wetu wengi, kwa kupuuza kwao maonyo na ushauri waliopewa, hufungua mlango wazi kwa Shetani aingie. Pamoja na Neno la Mungu kuwa mwongozo wetu na Yesu kama Mwalimu wetu wa mbinguni hatuhitaji kuwa wajinga wa maagizo Yake au hila za Shetani na kushindwa na majaribu yake. Haitakuwa kazi isiyopendeza kuwa watiifu kwa mapenzi ya Mungu tunapojitoa kikamilifu kuongozwa na Roho Wake. 3T 378.1

Sasa ni wakati wa kufanya kazi. Ikiwa sisi ni watoto wa Mungu, maadamu tunaishi katika ulimwenguni huu, Yeye atatupa kazi yetu. Hatuwezi kamwe kusema kuwa hatuna cha kufanya maadamu kuna kazi ambayo bado haijafanyika. Ninatamani kwamba vijana wote wangeweza kuona, kama nilivyoona, kazi ambayo wanaweza kufanya na kwamba Mungu atawawajibisha kwa kuipuuza. Kazi kubwa zaidi iliyowahi kutimizwa ulimwenguni ilifanywa na Yeye ambaye alikuwa mtu wa

huzuni na anayejua huzuni. Mtu mwenye nia ya mizaha au michezo-michezo kamwe hatatimiza mema. 3T 378.2

Udhaifu wa kiroho wa vijana wa kiume na wa kike katika kizazi hiki ni wa kushutumiwa/kusikitisha kwa sababu wangeweza kuwa wakala wenye nguvu kwa mema ikiwa wangejitoa wakfu kwa Mungu. Ninaomboleza sana ukosefu wa uimara/utulivu kwa vijana. Hili tunapaswa sote kulishutumu/kulipinga. Inaonekana kuna ukosefu wa nguvu ya kutenda haki, ukosefu wa bidii ya kutii wito wa wajibu kwa dhati, badala ya ule wa mwelekeo. Inaonekana kuna nguvu lakini kidogo ya kupinga majaribu kwa wengi. Sababu ya kwa nini wamedumaa katika mambo ya kiroho yaani ni mbilikimo wa kiroho, ni kwa sababu hawafanyi mazoezi ya kuwa wenye nguvu kiroho. Wao husimama mahali pamoja wakati wanapaswa kusonga mbele. Kila hatua katika maisha ya imani na wajibu ni hatua kuelekea mbinguni. Nataka sana kusikia juu ya matengenezo katika mambo mengi kama yale ambayo vijana hawakuwahi kuyafahamu hapo awali. Kila vishawishi/vivutio ambavyo Shetani anaweza kubuni vinawekwa juu yao kuwafanya wasiojali na wazembe kuhusu mambo ya milele. Ninashauri kwamba juhudi maalum zifanywe na vijana kusaidiana kuishi kwa uaminifu kwa nadhiri zao za ubatizo na kwamba waahidi kwa dhati mbele za Mungu kuondoa mapenzi yao kwa mavazi na maonesho. 3T 379.1

Ningewakumbusha vijana ambao hupamba nafsi zao na huvaa manyoya kwenye kofia zao kwamba, kwa sababu ya dhambi zao, kichwa cha Mwokozi wetu kilivishwa taji ya aibu ya miiba. Unapotumia wakati wa thamani sana kupamba mavazi yako, kumbuka kwamba Mfalme wa utukufu alikuwa amevaa kanzu sahili/rahisi, isiyo na mshono. Ninyi mnaojichosha katika kupamba utu wenu, tafadhali kumbukeni kwamba Yesu mara nyingi alikuwa amechoka kutokana na taabu endelevu na kujikana nafsi na kujitoa sadaka kuwabariki wanaoteswa na wahitaji. Alitumia usiku mzima akiomba juu ya milima yenye upweke, sio kwa sababu ya udhaifu Wake na mahitaji Yake, lakini kwa sababu Aliona, Alihisi, udhaifu wa tabia zako kupinga vishawishi vya adui juu ya maeneo ambayo sasa wewe umeshindwa. Yeye Alijua kwamba utakuwa mtu asiyejali kuhusu hatari zako na usingehisi hitaji lako la maombi. Ilikuwa kwa sababu yetu kwamba Yeye alimwaga maombi Yake kwa Baba Yake kwa kilio kikali na machozi. Ilikuwa ni kutuokoa kutoka katika kiburi na upendo wa ubatili, starehe na raha ambayo sasa tunaendekeza, na ambayo inazuia upendo wa Yesu, kwamba machozi hayo yalimwagika na kwamba uso wa Mwokozi wetu uligubikwa na kuharibika na huzuni na uchungu kuliko yeyote wa wana wa watu. 3T 379.2

Je! Ninyi, marafiki wachanga, mtainuka na kuukunguta/kuupukutisha ujinga na usingizi huu mbaya na upumbavu/ujinga ambao umewafananisha na ulimwengu? Je! Mtasikiliza sauti ya onyo ambayo inakuambia kwamba uharibifu uko katika njia

ya wale ambao wamebweteka kwa starehe katika saa hii ya hatari? Uvumilivu wa Mungu hautakusubiri wewe kila wakati, wewe masikini, mwenye roho iliyodanganya na mwenye mizaha, na usiyejali. Yeye anayeshikilia hatima zetu mikononi Mwake hatadharauliwa/hatachezewa kila wakati. Yesu anatutangazia kuwa kuna dhambi kubwa kuliko ile iliyosababisha uharibifu wa Sodoma na Gomora. Ni dhambi ya wale ambao wana nuru kuu ya Ukweli katika siku hizi na ambao hawasukumwi kutubu. Ni dhambi ya kukataa nuru ya ujumbe mzito/adhmu kabisa wa rehema kwa ulimwengu. Ni dhambi ya wale wanaomwona Yesu katika jangwa la kujaribiwa, ameinama chini kwa uchungu wa mauti kwa sababu ya dhambi za ulimwengu, na bado hawasukumwi kutubu kabisa-kikamilifu. Alifunga karibu wiki sita ili kushinda, kwa niaba ya mwanadamu, anasa ya hamu ya chakula na ubatili, na hamu ya kujionesha na heshima ya ulimwengu. Yeye Amewaonesha jinsi wanavyoweza kushinda kwa sababu yao wenyewe kama Yeye alishinda; lakini haivutii au kupendeza kwa asili yao kuvumilia mzozo na aibu, kejeli na aibu, kwa ajili ya Yeye mpendwa. Haikubaliki kwao kujikana mwenyewe na kuwa daima katika kutafuta kuwatendea wengine mema. Haitoi furaha kwao kushinda kama Kristo alivyoshinda, kwa hivyo wanageuka kutoka katika Mfano wazi waliopewa kuiga na kukataa kuufuata mfano huo ambao Mwokozi alikuja kutoka nyua za mbinguni kuwaachia. 3T 380.1

Itakuwa rahisi na bora zaidi kwa Sodoma na Gomora katika siku ya hukumu kuliko kwa wale ambao wamepata upendeleo na nuru kuu inayoangaza katika siku zetu, lakini ambao wameacha kufuata nuru na kutoa mioyo yao kikamilifu kwa Mungu. 3T 380.2

SURA YA 33

ZAKA NA SADAKA

Utume wa kanisa la Kristo ni kuokoa wenye dhambi wanaoangamia. Ni kuwajulisha wanadamu upendo wa Mungu na kuwavuta kwa Kristo kupitia upendo huo. Ukweli kwa wakati huu ni lazima upelekwe katika pembe za giza za dunia, na kazi hii inaweza kuanzia nyumbani. Wafuasi wa Kristo hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi; lakini, wakiwa wamejazwa na Roho wa Kristo, wanapaswa kufanya kazi pamoja Naye kwa upatano. 3T 381.1

Kuna sababu za ubaridi uliopo sasa na kutokuamini. Upendo wa ulimwengu na kujali maisha hutenganisha roho na Mungu. Maji ya uzima lazima yawe ndani yetu, na yakitiririka kutoka kwetu, yakibubujikia kwenye maisha ya umilele. Ni lazima tukifanyie kazi kile ambacho Mungu amekifanyia na anakifanyia kazi ndani. Ikiwa Mkristo atafurahia nuru ya uzima, lazima aongeze bidii yake kuwaleta wengine kwenye maarifa ya Ukweli. Maisha yake yanapaswa kuhusisha bidii kali na kujitolea kuwafanyia wengine mema; na kisha hakutakuwa na malalamiko ya ukosefu wa furaha. 3T 381.2

Malaika huendelea kufanya kazi kwa furaha ya wengine daima. Hii ndio furaha yao. Hiyo ambayo mioyo ya ubinafsi inaweza kufikiri ni huduma ya kufedhehesha, kuwahudumia wale ambao wanatisha kwa kuwa duni na walio dhaifu katika tabia na daraja, ni kazi ya malaika safi, wasio na dhambi katika nyua za kifalme za mbinguni. Roho ya upendo wa kujitoa dhabihu nafsi wa Kristo ni roho ambayo imeenea mbinguni na ndio kiini cha furaha Yake. 3T 381.3

Wale ambao hawahisi raha maalum katika kutafuta kuwa baraka kwa wengine, kwa kufanya kazi, hata kwa kujitoa dhabihu, kuwafanyia mema, hawawezi kuwa na roho ya Kristo au ya mbinguni; kwa kuwa hawana umoja na kazi ya malaika wa

mbinguni na hawawezi kushiriki katika raha inayowapa furaha iliyoinuliwa. Kristo alisema: "Shangwe itakuwa mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja atubuye, zaidi kuliko watu tisini na tisa waadilifu au wenye haki, ambao hawahitaji toba." Ikiwa furaha ya malaika ni kuona wenye dhambi wakitubu, Je! Haitakuwa furaha ya wenye dhambi, waliookolewa na damu ya Kristo, kuona wengine wakitubu na kumrudia Kristo kupitia utumikaji wao? Kwa kufanya kazi kwa usawa na Kristo na malaika watakatifu, tutapata furaha ambayo haiwezi kupatikana kando na kazi hii. 3T 381.4

Kanuni ya msalaba wa Kristo huwaleta wote wanaoamini chini ya majukumu mazito ya kujikana nafsi zao wenyewe, kusambaza nuru kwa wengine, na kutoa uwezo wao kusambaza nuru. Ikiwa wameuanganishwa na mbingu watahusika katika kazi hiyo sawa na malaika. 3T 382.1

Kanuni ya walimwengu ni kupata kila wawezacho katika vitu vinavyoharibika vya maisha haya. Upendo wa ubinafsi kwa kujipatia faida mwenyewe ndiyo kanuni tawala katika maisha yao. Lakini furaha safi kabisa haipatikani katika utajiri au mahali ambapo tamaa inapiga mayowe ya kutamani kila wakati, lakini ambapo utoshelevu unatawala na ambapo upendo wa kujitoa ndio kanuni inayotawala. Kuna maelfu ambao wanapitisha maisha yao kwa kujiendekeza/kujifurahisha na ambao mioyo yao imejaa kutoridhika na malalamiko. Wao ni waathirika wa ubinafsi na kutoridhika katika juhudi za bure kuridhisha akili zao na anasa na kujiridhisha. Lakini kutokuwa na furaha kumepigwa muhuri juu ya nyuso zao, na nyuma yao kuna jangwa, kwa sababu njia yao haizai matunda kwa kazi nzuri. 3T 382.2

Kwa kadiri upendo wa Kristo unavyojaza mioyo yetu na kudhibiti maisha yetu, tamaa, ubinafsi/uchoyo, na kupenda starehe vitashindwa, na itakuwa furaha yetu kufanya mapenzi ya Kristo, ambaye tunadai kuwa watumishi Wake. Furaha yetu itakuwa sambamba na kazi zetu zisizo na ubinafsi, zinazohamasishwa na upendo wa Kristo. 3T 382.3

Hekima ya Mungu imetoa nafasi, katika mpango wa wokovu, sheria ya utekelezaji na mwitikio [action and reaction], na kuifanya kazi ya uaminifu, katika matawi yake yote, ibariki maradufu. Yeye anayetoa kwa wahitaji huwabariki wengine, na kisha anajibariki mwenyewe kwa kiwango kikubwa zaidi. Mungu angeweza kufikia lengo Lake katika kuokoa wenye dhambi bila msaada wa mwanadamu; lakini Alijua kwamba mwanadamu hangefurahi bila kuhusika katika kazi kubwa ambayo atakuwa anakuza kujinyima, kujikana nafsi na ukarimu. 3T 382.4

Mtu huyo asipoteze matokeo yaliyobarikiwa ya ukarimu, Mkombozi wetu aliunda mpango wa kumsajili mwanadamu kama mtendakazi-mwenza. Kwa mlolongo wa hali ambayo ingeamsha sadaka yake, Yeye humpa mwanadamu njia bora ya kukuza

wema na ukarimu na humfanya awe na mazoea ya kutoa kusaidia maskini na kuendeleza kazi Yake. Yeye Anawatuma maskini Wake kama wawakilishi Wake. Kwa mahitaji yao, ulimwengu ulioharibiwa unavuta kutoka kwetu talanta na njia za ushawishi wa kuwasilisha kwao Ukweli, ambao wanauhitaji sana kwani wanaangamia. Na tunapotii miito hii kwa dhati na bidii na kwa vitendo vya ukarimu tunajiunga na utamaduni wa mfano Wake Yeye ambaye kwa sababu yetu alikua masikini. Katika kutoa tunabariki wengine, na kwa hivyo kukusanya utajiri wa Kweli. 3T 382.5

Kumekuwa na ukosefu mkubwa wa ukarimu wa Kikristo kanisani. Wale ambao walikuwa na uwezo bora wa kufanya kwa maendeleo kwa ajili ya Mungu wamefanya kidogo tu. Kwa rehema Mungu amelileta kundi hili kwenye ujuzi wa Ukweli, ili wapate kuthamini thamani yake isiyokadirika ikilinganishwa na hazina za kidunia. Yesu amewaambia: "Nifuateni Mimi." Yeye Anawajaribu na mwaliko wa karamu aliyoiandaa. Anaangalia kuona ni tabia gani watakayoiendeleza, ikiwa masilahi yao ya ubinafsi/uchoyo yatazingatiwa kama ya thamani kubwa kuliko utajiri wa milele. Wengi wa ndugu hawa wapendwa sasa kwa vitendo vyao wanapanga visingizio vilivyotajwa katika mfano ufuatao: 3T 383.1

Ndipo akamwambia, Mtu mmoja alifanya karamu kubwa, akaalika wengi; akamtuma mtumwa wake wakati wa chakula cha jioni kuwaambia wale walioalikwa, Njoni; kwa maana mambo yote sasa yako tayari. Na wote kwa ridhaa moja wakaanza kutoa udhuru. Wa kwanza akamwambia, Nimenunua kipande cha shamba, na lazima niende nikakione; nakuomba unisamehe. Mwingine akasema, Nimenunua ng'ombe jozi tano, na nakwenda kuzijaribu; nakuomba unisamehe. Na mwingine akasema, nimeoa mke, na kwa hivyo siwezi kuja. Basi yule mtumwa akaenda, akampa Bwana wake habari ya mambo haya. Ndipo mwenye nyumba alipokasirika akamwambia mtumishi wake, Nenda upesi kwenye barabara na vichochoro vya mji, na ulete hapa maskini, vilema, viwete, na vipofu. 3T 383.2

Mfano huu unawakilisha kwa usahihi hali ya wengi wanaodai kuamini Ukweli wa sasa. Bwana amewatumia mwaliko wa kuja kwenye karamu ambayo Yeye amewaandalia kwa gharama kubwa Kwake; lakini shauku/masilahi ya kidunia yanaonekana kuwa na umuhimu mkubwa kuliko hazina ya mbinguni. Wanaalikwa kushiriki katika mambo yenye thamani ya milele; lakini mashamba yao, ng'ombe wao, na masilahi yao ya nyumbani yanaonekana kuwa ya umuhimu mkubwa zaidi kuliko kutii mwaliko wa mbinguni kwamba yanashinda kila kivutio cha Mungu, na vitu hivi vya kidunia vinafanywa kisingizio cha kutotii kwao amri ya mbinguni, "Njoo; kwa maana mambo yote yako tayari sasa.” Ndugu hawa wanafuata kwa upofu mfano wa wale waliowakilishwa katika mfano huo. Wanaangalia mali zao za kidunia, na kusema: Hapana, Bwana, siwezi kukufuata Wewe; "Nakuomba unisamehe-unipe udhuru." 3T 383.3

Baraka hizo ambazo Mungu amewapa watu hawa kuwathibitisha, kuona ikiwa watampa "Mungu yaliyo ya Mungu," wanazitumia kama kisingizio kwamba hawawezi kutii madai ya Ukweli. Wamezikumbatia hazina yao za kidunia mikononi mwao na kusema, “Lazima nitunze vitu hivi; Sipaswi kupuuza mambo ya maisha haya; vitu hivi ni vyangu. ” Kwa hivyo mioyo ya watu hawa imekuwa migumu kama barabara kuu inayopitwa/inayokanyagwa mara kwa mara. Wanafunga mlango wa mioyo yao kwa mjumbe wa mbinguni, ambaye anasema, "Njoo; kwa kuwa vitu vyote viko tayari sasa, ”na kuacha wazi,wakialika kuingia kwa masumbufu ya dunia na kujali masumbufu ya biashara, na Yesu anabisha bure ili akaribishwe. 3T 384.1

Mioyo yao imeshonana miiba iliyoota na masumbufu na wasiwasi wa maisha haya kiasi kwamba vitu vya mbinguni haviwezi kupata nafasi ndani yao. Yesu anawaalika waliochoka na wenye kulemewa na ahadi ya kupumzika ikiwa watamjia Yeye. Anawaalika wabadilishe nira yenye uchungu ya ubinafsi na kutamani, ambayo inawafanya watumwa wa fedha/mali, kwa kuwa nira Yake, Anasema ni rahisi, na mzigo Wake, ambao ni mwepesi. Anasema: “Jifunzeni kutoka Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu.” Bwana Angewataka waachilie mbali mizigo mizito ya kujali dunia na kuchanganyikiwa, na kuchukua nira Yake, ambayo ni kujinyima na kujitolea dhabihu kwa ajili ya wengine. Mzigo huu utathibitika kuwa mwepesi. Wale ambao wanakataa kukubali unafuu ambao Kristo huwapa, na wanaendelea kuvaa kongwa lenye uchungu la ubinafsi, wakizihenyesha nafsi zao jukumu kubwa katika mipango ya kujilimbikiza pesa kwa furaha ya ubinafsi, hawajapata amani na mapumziko yanayopatikana katika kubeba nira ya Kristo na kuinua mizigo ya kujinyima, kujikana nafsi na ukarimu na upendo usiojifikiria wenyewe ambao Kristo amebeba kwa niaba yao. 3T 384.2

Wakati upendo wa ulimwengu unachukua nafasi ya moyo na kuwa upendeleo unaotawala, hakuna nafasi inayoachwa ya kumwabudu Mungu; kwa nguvu za juu za akili hujisalimisha kwa utumwa wa utajiri, na hauwezi kuhifadhi mawazo ya Mungu na ya mbinguni. Akili hupoteza kumkumbuka Mungu na hupunguzwa na kudumaa kwa ukusanyaji wa pesa. 3T 385.1

Kwa sababu ya ubinafsi na kupenda ulimwengu, watu hawa wamekuwa wakipita kwa hisia kidogo na kidogo juu ya ukubwa wa kazi kwa siku hizi za mwisho. Hawajaelimisha akili zao kufanya biashara ya kumtumikia Mungu. Hawana uzoefu katika mwelekeo huo. Mali yao imefyonza mapenzi yao na kuzinga/kupuuza ukubwa wa mpango wa wokovu. Wakati wanaboresha na kupanua mipango yao ya kidunia, hawaoni umuhimu wa kukuza na kupanua kazi ya Mungu. Wanawekeza fedha/mali zao katika vitu vya muda lakini sio katika vitu vya milele. Mioyo yao ina matamanio ya mali zaidi. Mungu amewafanya hawa kuwa amana ya sheria

Yake, ili waweze kuiruhusu nuru kwa neema ili iwaangazie wengine. Lakini wameongeza zaidi kujali kwao masumbufu/mifadhaiko kiasi kwamba hawana muda wa kuwabariki wengine kwa ushawishi wao, kuzungumza na majirani zao, kuomba nao na kwa ajili yao, na kutafuta kuwaleta kwenye ujuzi wa Ukweli. 3T 385.2

Watu hawa wanawajibika kwa mema wanayoweza kufanya, lakini ambayo hawafanyi sababu ya kujali ulimwengu na mizigo, ambayo inachukua akili zao na kunyonya upendo wao. Nafsi ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake zinaweza kuokolewa kwa juhudi zao binafsi na Mfano wao wa Mbinguni. Nafsi zenye thamani zinaangamia kwa nuru ambayo Mungu amewapatia wanadamu ili imulike juu ya njia ya wengine. Lakini nuru hiyo ya thamani imefichwa chini ya pishi, na haitoi mwanga kwa wale waliomo ndani ya nyumba. 3T 385.3

Kila mtu ni wakili wa Mungu. Kwa kila mtu Bwana amekabidhi mali Zake, lakini mwanadamu anadai mali hizo kuwa zake. Kristo anasema: "Fanya kazi mpaka nitakapokuja." Wakati unakuja ambapo Kristo atahitaji iliyoyake na riba. Atamwambia kila mmoja watumishi Wake: "Toa hesabu ya utumishi wako." Wale ambao wamezificha pesa za Bwana wao katika leso katika ardhi, badala ya kuzitoa kwa wenye kubadilishana, na wale ambao wamefuja pesa za Bwana wao kwa wachuuzi/kuzitumia kwa vitu visivyo vya lazima, badala ya kuzitoa ili kupata riba kwa kuziwekeza katika kazi Yake, hawatapokea kibali kutoka kwa Bwana, lakini hukumu. Mtumishi asiye na faida katika mfano huo alileta talanta moja kwa Mungu, na akasema: “Nilijua wewe ni mtu mgumu, unavuna mahali usipopanda, na kukusanya mahali ambapo haukutawanya: nikaogopa, nikaenda. na kuificha talanta yako ardhini; tazama, hiyo unayo yako.” Bwana wake akamwambia: "Wewe mtumishi mwovu na mvivu, ulijua kwamba mimi huvuna mahali ambapo sikupanda, na kukusanya mahali ambapo sikutawaya; Ilikupasa basi kuiweka pesa yangu kwa wabadilishaji, halafu wakati wa kuja Kwangu ningepaswa kupokea yangu na riba.” 3T 385.4

Mtumishi huyu asiye na faida hakuwa mjinga wa mipango ya Mungu, lakini alijiweka imara kukwamisha kusudi la Mungu, akimshtaki kwa ukosefu wa haki katika uhitaji wa kukuza talanta alizokabidhiwa. Malalamiko haya na manung'uniko yanafanywa na kundi kubwa la watu matajiri wanaodai kuamini Ukweli. Kama yule mtumishi asiye mwaminifu wanaogopa kwamba kuongezeka kwa talanta ambayo Mungu amewapa itapata wito wa kutolewa ili kuendeleza uenezaji wa Ukweli; kwa hivyo wanaifunga kwa kuwekeza katika hazina za kidunia na kuizika ulimwenguni, na hivyo kufanya haraka katika mchakato wa kuonekana hawana chochote, au karibu na kutokuwa na chochote, cha kuwekeza kwa ajili ya Mungu. Wameizika, wakiogopa kwamba Mungu angewataka kiasi cha riba au waongezewe. Wakati Bwana wao anapohitaji, wanaleta kiasi walichopewa, wanakuja na

visingizio vya kukosa shukrani kwa kutoweka mali walizopewa na Mungu kwa wabadilishanaji, kwa kuwekeza katika kusudi Lake ili kutekeleza kazi Yake. 3T 386.1

Yeye anayefuja mali ya Bwana wake sio tu anapoteza talanta aliyopewa na Mungu, lakini hupoteza uzima wa milele. Kuhusu yeye inasemwa kwake: "Mtupeni yule mtumishi asiye na faida kwenye giza la nje." Mtumishi mwaminifu, ambaye anawekeza pesa zake kwa sababu ya Mungu kuokoa roho za watu, hutumia mali zake kwa utukufu wa Mungu na atapokea sifa ya Bwana: “Vema, mtumishi mwema na mwaminifu:... ingia katika furaha ya Bwana wako.” Furaha hii ya Bwana wetu itakuwa nini?
Itakuwa furaha ya kuona roho zilizookolewa katika ufalme wa utukufu. "Ambaye kwa furaha iliyowekwa mbele Yake alivumilia msalaba, akidharau aibu, na ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu." 3T 387.1

Wazo la uwakili linapaswa kufanywa kwa vitendo kwa watu wote wa Mungu. Mfano wa talanta, ulioeleweka vyema, utazuia tamaa, ambayo Mungu huita ibada ya sanamu. Ukarimu wa kivitendo utawapa maisha ya kiroho maelfu ya wanaokiri kwa mdomo Ukweli kwa jina tu ambao sasa wanaomboleza juu ya giza lao. Itawabadilisha kutoka katika ubinafsi,waabudu mali wenye tamaa na kuwa wafanya kazi na Kristo waaminifu na wenye bidii katika wokovu wa wenye dhambi. 3T 387.2

Msingi wa mpango wa wokovu ulisimikwa kwa kafara. Yesu aliondoka katika nyua za kifalme na kuwa maskini, ili sisi kwa umaskini Wake tupate kutajirika. Wote wanaoshiriki wokovu huu, ulionunuliwa kwao kwa dhabihu isiyo na kikomo na Mwana wa Mungu, watafuata mfano wa njia ya Kweli. Kristo alikuwa Jiwe kuu la Pembeni, na lazima tujenge juu ya Msingi huu. Kila mmoja lazima awe na roho ya kujikana na kujitolea. Maisha ya Kristo hapa duniani hayakuwa ya ubinafsi; yaliwekwa alama ya udhalilishaji na dhabihu. Je! Watu, washiriki wa wokovu mkuu ambao Yesu alikuja kutoka mbinguni kuwaletea, watakataa kumfuata Bwana wao na kushiriki katika kujikana Kwake na kujitolea? Kristo anasema: "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi." "Kila tawi ndani Yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa matunda." Kanuni muhimu sana, utomvu wa mti ambao hutiririka kupitia mzabibu, huyapa lishe matawi, ili yastawi na kuzaa matunda [maji na lishe, xylem and phloem]. Je! Mtumwa ni mkuu kuliko Bwana wake? Je! Mkombozi wa ulimwengu atajikana nafsi na kujitolea kwa niaba yetu, na washiriki wa mwili wa Kristo kufanya kwa kujifurahisha/kujiridhisha wenyewe? Kujikana nafsi ni kigezo muhimu cha kuwa mfuasi. 3T 387.3

"Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi Wake, Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake, anifuate." Ninaongoza njia katika njia

ya kujikana. Sitaki chochote kutoka kwenu, wafuasi Wangu, lakini kile ambacho Mimi, Bwana wako, ninakupa mfano katika maisha Yangu Mwenyewe. 3T 388.1

Mwokozi wa ulimwengu alimshinda Shetani katika jangwa la majaribu. Yeye Alishinda ili kumuonesha mwanadamu jinsi anavyoweza kushinda. Alitangaza katika sinagogi la Nazareti: "Roho wa Bwana Yu juu Yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiria maskini injili; Amenituma Mimi kuponya waliovunjika mioyo, kuwahubiria waliofungwa ukombozi, na vipofu kuona tena, kuwaweka huru wale waliopondwa, kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubalika." 3T 388.2

Kazi kubwa ambayo Yesu alitangaza kwamba alikuja kuifanya walikabidhiwa wafuasi Wake duniani. Kristo, kama kichwa chetu, anaongoza katika kazi kuu ya wokovu na Yeye anatuamuru tufuate mfano Wake. Ametupa ujumbe duniani kote. Ukweli huu lazima uenezwe kwa mataifa yote, lugha, na watu. Nguvu za Shetani zilipaswa kushindwa, na alipaswa kushindwa na Kristo na pia wafuasi Wake. Vita kubwa ilipaswa kudumishwa dhidi ya nguvu za giza. Na ili kufanya kazi hii kwa mafanikio, mali zitahitajika. Mungu hajapendekeza kutuma njia moja kwa moja kutoka mbinguni, lakini Yeye huipa mikononi mwa wafuasi Wake talanta ya njia za kutumia kwa kusudi la kuendeleza vita hivi. 3T 388.3

Bwana Amewapa watu Wake mpango wa kukusanya kiasi cha kutosha kuifanya kazi hii iwe imara. Mpango wa Mungu katika mfumo wa kutoa zaka ni mzuri kwa unyenyekevu na usawa. Wote wanaweza kuushika kwa imani na ujasiri, kwani asili yake ni ya Mungu. Ndani yake umeunganishwa unyenyekevu na ugavi/matumizi, na hauitaji kina cha ujifunzaji kuelewa na kutekeleza. Wote wanaweza kuhisi kwamba wanaweza kuchukua sehemu katika kuendeleza mbele kazi ya thamani ya wokovu. Kila mwanamume, mwanamke, na kijana anaweza kuwa mweka hazina wa Bwana na anaweza kuwa wakala wa kukidhi mahitaji ya hazina. Mtume anasema: "Kila mmoja wenu ajiwekee akiba, kama vile Mungu alivyomfanikisha." 3T 388.4

Mambo mema, malengo makuu yanatimizwa na mfumo huu. Ikiwa mmoja na wote wangekubali, kila mmoja angefanywa mlinzi na mtunza hazina mwaminifu kwa Mungu, na hakungekuwa na uhaba wa mali za kuendeleza kazi kuu ya kupeleka ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu. Hazina itajaa ikiwa wote watachukua mfumo huu, na wachangiaji hawataachwa maskini. Kupitia kila uwekezaji uliofanywa watakuwa wamejifungamanisha zaidi kwa sababu ya Ukweli wa sasa. Watakuwa "wakijiwekea akiba ya msingi mzuri dhidi ya wakati ujao, ili waweze kushikilia uzima wa milele." 3T 389.1

Kwa kuwa wavumilivu, wafanyakazi wa utoaji wa mpango kwa ukarimu, wanaona kuwa mwelekeo wa juhudi zao nzuri ni kukuza upendo kwa Mungu na watu wenzao,

na kwamba juhudi zao za kibinafsi zinaongeza uwanja wao wa manufaa, watatambua kuwa ni baraka kubwa kuwa washirika- watenda kazi pamoja na Kristo. Kanisa la Kikristo, kama jambo la jumla, linakataa madai ya Mungu juu yao kutoa sadaka ya vitu ambavyo wanavyokusaidia vita dhidi ya giza la maadili ambalo linafurika duniani. Kazi ya Mungu haiwezi kamwe kusonga mbele kama inavyopaswa hadi wafuasi wa Kristo wawe watenda-kazi wenye bidii na hai. 3T 389.2

Kila mtu ndani ya kanisa anapaswa kuhisi kwamba Ukweli anaoukiri ni halisi, na wote wanapaswa kuwa wafanyakazi wasio na upendeleo. Baadhi ya matajiri wanajihisi kunung'unika kwa sababu kazi ya Mungu inapanuka na kuna mahitaji ya pesa. Wanasema kuwa hakuna mwisho wa wito wa kutoa fedha. Kitu kimoja baada ya kingine kinatokea kila wakati, kikihitaji msaada. Kwa hilo tunaweza kusema kwamba tunatumai kuwa kusudi la Mungu litaenea sana kwamba kutakuwa na hafla kubwa, na wito wa mara kwa mara na wa haraka, kwa ajili ya kutoa kutoka kwenye hazina ili kuendeleza kazi hiyo. 3T 389.3

Ikiwa mchakato wa utoaji kwa mpango ungepokelewa na kila mtu na kutekelezwa kikamilifu, kutakuwa na ugavi wa daima katika hazina. Mapato yatatiririka kama mkondo wa kutosha unaotolewa kila wakati na chemchemi zinazofurika za ukarimu. Kutoa sadaka ni sehemu ya dini ya injili. Je! Kuzingatia kwa bei isiyo na kipimo iliyolipwa kwa ukombozi wetu hakuachi juu yetu majukumu mazito kwa hiari, na vile vile kudai madai kwa nguvu zetu zote kujitolea kwa kazi ya Bwana? 3T 389.4

Tutakuwa na deni la kulipa kwa Bwana hatimaye siku ya hukumu, wakati atakaposema: "Toa hesabu ya uwakili wako." Ikiwa watu wanapendelea kuweka kando madai ya Mungu na kukumbatia mali kwa ubahili na kwa ubinafsi kuhifadhi/kubakiza kila kitu Anachowapa, Yeye atakaa kimya kwa sasa na ataendelea mara kwa mara kuwajaribu kwa kuongeza fadhila Zake kwa kuruhusu baraka Zake zitiririke, na watu hawa wanaweza kuendelea kupokea heshima za watu na bila kukemewa kanisani; lakini siku ile ya mwisho ya hukumu: "Toa hesabu ya uwakili wako." Kristo anasema: "Kama vile ambavyo hamkumtendea mmoja wa hawa walio wadogo, hamkunitendea Mimi." "Nyinyi si mali yenu wenyewe, kwa maana mmenunuliwa kwa bei kubwa," Basi mtukuzeni Mungu kwa mali yenu na pia kwa miili yenu na kwa roho yenu, ambayo ni Yake. "Mmenunuliwa kwa bei," " si kwa vitu viharibikavyo, kama fedha na dhahabu," "lakini kwa damu ya Kristo." Yeye Anatuomba kurudisha katika zawadi ambazo ametukabidhi, kusaidia katika wokovu wa roho. Ametoa damu Yake; Anaomba fedha zetu. Ni kupitia umaskini Wake ndio tunatajirika; na Je! tutakataa kumrudishia zawadi Zake Mwenyewe? 3T 390.1

Mungu hamtegemei mwanadamu kumsaidia katika kazi Yake. Angeliweza kutuma mali moja kwa moja kutoka mbinguni ya kuleta katika hazina Yake, ikiwa uongozi Wake ungeona kuwa hii ilikuwa bora kwa mwanadamu. Labda angebuni njia ambazo malaika wangetumwa kutangaza Ukweli kwa ulimwengu bila wakala wa wanadamu. Yeye Angeweza kuandika Ukweli juu ya mbingu, na basi hiyo itangaze kwa ulimwengu matakwa Yake katika herufi zilizo hai. Mungu hategemei dhahabu au fedha ya mtu yeyote. Anasema: "Kila mnyama wa mwitu ni Wangu, na ng'ombe juu ya milima elfu." "Kama ningekuwa na njaa, nisingekuambia: kwa maana ulimwengu ni Wangu, na utimilifu wake." Umuhimu wowote uliopo kwa wakala wetu katika maendeleo ya kazi ya Mungu, Yeye amekusudia kwa faida yetu. Ametuheshimu kwa kutufanya watenda kazi-washirika pamoja Naye. Ameweka kwamba kutakuwa na ulazima wa ushirikiano wa wanadamu, ili tuweze kuendelea kufanyia mazoezi/kazi wema na ukarimu wetu. 3T 390.2

Mungu katika hekima ya uweza Wake ameweka masikini daima pamoja nasi, kwamba wakati tunapaswa kushuhudia aina mbalimbali ya uhitaji na mateso ulimwenguni, tunapaswa kujaribiwa na kudhibitishwa, na kuletwa katika nafasi za kukuza tabia ya Kikristo. Yeye Ameweka masikini kati yetu kuita kutoka kwetu huruma ya Kikristo na upendo. 3T 391.1

Wenye dhambi, wanaoangamia kwa kukosa maarifa, lazima waachwe katika ujinga na giza isipokuwa watu wawapelekee nuru ya Ukweli. Mungu hatatuma malaika kutoka mbinguni kufanya kazi ambayo amemwachia mwanadamu afanye. Amewapa kazi yote ya kufanya, kwa sababu hiyo hiyo ili aweze kuwathibitisha na kwamba wapate kufunua tabia yao halisi. Kristo anaweka maskini kati yetu kama wawakilishi Wake. "Nilikuwa na njaa," anasema, "nanyi hamkunipa chakula; nilikuwa na kiu, nanyi hamkunipa maji." Kristo anajitambulisha Yeye Mwenyewe na ubinadamu unaoteseka katika nafsi za watoto wa watu wanaoteseka. Yeye hufanya mahitaji yao kuwa Yake Mwenyewe na huchukua kifuani Mwake huzuni/ole yao. 3T 391.2

Giza la kimaadili la ulimwengu ulioharibiwa huwasihi wanaume na wanawake wa Kikristo kufanya bidii ya kibinafsi, kutoa uwezo, mali zao na ushawishi wao, ili waweze kufanana na sura ya Yeye ambaye, ingawa alikuwa na utajiri usio na kipimo, lakini kwa ajili yetu akawa maskini. Roho wa Mungu hawezi kukaa na wale ambao Ametuma ujumbe wa Ukweli Wake lakini ambao wanahitaji kusukumwa kabla ya kuwa na hisia yoyote ya wajibu wao wa kuwa wafanya kazi pamoja na Kristo. Mtume anasisitiza wajibu wa kutoa kutoka kwa misingi ya juu kuliko huruma ya kibinadamu tu kwa sababu hisia zinahamishwa. Anasisitiza kanuni kwamba tunapaswa kufanya kazi bila ubinafsi na jicho likite/likodolee macho utukufu wa Mungu tu. 3T 391.3

Wakristo wanatakiwa na Maandiko kuingia katika mpango wa ukarimu ulio hai ambao utaweka mazoezi ya kila wakati maslahi katika wokovu wa wanadamu wenzao. Sheria ya maadili iliamuru utunzaji wa Sabato, ambayo haikuwa mzigo isipokuwa wakati sheria hiyo ilipovunjwa na wakafungwa na adhabu zinazohusiana na kuivunja. Mfumo wa kutoa zaka haukuwa mzigo kwa wale ambao hawakutoka kwenye mpango huo. Mfumo ulioamriwa kwa Waebrania haujafutwa au kulegezwa na Yule aliyeuanzisha. Badala ya kutokuwa na nguvu sasa, ulipaswa kutendwa kikamilifu na kupanuliwa zaidi, kwani wokovu kupitia Kristo peke yake unapaswa kufichuliwa kikamilifu katika zama za Ukristo. 3T 391.4

Yesu alimjulisha mwanasheria kwamba kigezo cha yeye kuwa na uzima wa milele ilikuwa kutekeleza maishani mwake mahitaji maalum ya sheria, ambayo yalikuwa kumpenda Mungu wake kwa moyo wake wote, na roho, na akili, na nguvu, na jirani kama yeye mwenyewe. Dhabihu za kawaida zilipokoma wakati wa kifo cha Kristo, sheria ya asili, iliyochorwa kwenye meza za mawe, haikubadilika, ikishikilia madai yake kwa mwanadamu katika kila zama/kizazi. Na katika zama za Ukristo jukumu la mwanadamu halikuwa na kikomo (halikuondolewa), lakini lilifafanuliwa zaidi na kuelezewa kwa urahisi. 3T 392.1

Injili, kupanua na kupanuka, ilihitaji matoleo zaidi ili kudumisha vita baada ya kifo cha Kristo, na hii ilifanya sheria ya utoaji wa sadaka iwe ya hitaji la dharura/haraka zaidi kuliko chini ya serikali ya Waebrania. Sasa Mungu anahitaji, sio kidogo, lakini zawadi kubwa kuliko wakati mwingine wowote wa ulimwengu. Kanuni iliyowekwa na Kristo ni kwamba karama na sadaka zinapaswa kuwa sawa na nuru na baraka zinazofurahiwa. Amesema: "Kwake yule aliyepewa vingi, kwake atadaiwa vingi." 3T 392.2
Baraka za zama Ukristo ziliitikiwa na wanafunzi wa kwanza katika kazi za hisani na ukarimu. Kumwagwa kwa Roho wa Mungu, baada ya Kristo kuwaacha wanafunzi Wake na kupaa mbinguni, kulisababisha kujikana na kujitolea kwa wokovu wa wengine. Wakati watakatifu maskini huko Yerusalemu walipokuwa na ufukara, Paulo aliwaandikia Wakristo wa Mataifa kuhusu kazi za ukarimu, na kusema: “Basi kama mlivyo mbele sana katika yote:katika imani, katika kutamka, katika juhudi na katika kutupenda, hakikisheni kuwa mnakuwa wa kwanza pia katika neema hii ya kutoa” Hapa wema na ukarimu huwekwa na upande wa imani, upendo, na bidii ya Kikristo. Wale wanaofikiria kuwa wanaweza kuwa Wakristo wazuri na kufunga masikio na mioyo yao kwa wito wa Mungu kwa ukarimu wao, wako katika udanganyifu wa kutisha. Kuna wale ambao wana utaalam mwingi wa upendo mkubwa wa Ukweli, na, kwa kadiri maneno yanavyohusika, wana hamu ya kuona Ukweli ukisonga mbele, lakini hawafanyi chochote kwa maendeleo yake. Imani ya hao imekufa, isiyokamilishwa kwa matendo. Bwana hakuwahi kufanya kosa kama kuongoa roho na kuiacha chini ya nguvu ya kutamani. 3T 392.3

Mfumo wa utoaji wa zaka unarudi nyuma zaidi ya siku za Musa. Wanaume walihitajika kumtolea Mungu zawadi kwa madhumuni ya kidini kabla ya mfumo maalum kupewa Musa, hata zamani kama siku za Adamu. Kwa kufuata matakwa ya Mungu, walipaswa kuonesha katika kutoa shukrani zao za rehema na baraka Zake kwao. Hii iliendelea kupitia vizazi vilivyofuata, na ilifanywa na Ibrahimu, ambaye alimpa zaka Melkizedeki, kuhani wa Mungu aliye juu. Kanuni hiyo hiyo ilikuwepo katika siku za Ayubu. Yakobo, akiwa Betheli, mkimbizi/mhamishwa na mtembezi asiye na pesa, alilala usiku, katika faragha na peke yake, na mwamba kama mto wake, na hapo alimuahidi Bwana: "Kati ya yote utakayonipa hakika nitakupa sehemu ya kumi.” Mungu hawalazimishi watu kutoa. Yote ambayo wanatoa lazima yawe ya hiari. Hatakuwa na hazina Yake iliyojazwa matoleo yasiyo ya moyo wa kupenda au hiari. 3T 393.1

Bwana amekusudia kumleta mwanadamu katika uhusiano wa karibu na Yeye Mwenyewe na katika huruma na upendo kwa binadamu wenzake kwa kumpa majukumu katika matendo ambayo yatapinga ubinafsi na kuimarisha upendo wake kwa Mungu na mwanadamu. Mchakato wa utoaji wa mpango kwa ukarimu, Mungu aliutengeneza kwa faida ya mwanadamu, ambaye ana mwelekeo wa kuwa mbinafsi na kufunga moyo wake kwa matendo ya ukarimu. Bwana anahitaji vipawa kufanywa kwa nyakati zilizotajwa, ikiwa kwa mpangilio kwamba kutoa itakuwa tabia na ukarimu kuhisiwa kama jukumu la Kikristo. Moyo, uliofunguliwa na zawadi moja, hautakuwa baridi na mbinafsi na kufunga kabla ya ijayo kutolewa. Mto unapaswa kuendelea kutiririka, na hivyo kuweka wazi kituo kwa vitendo vya ukarimu. 3T 393.2

Kuhusu kiasi kinachohitajika, Mungu ameainisha sehemu moja ya kumi ya ongezeko. Hii imeachwa kwa dhamiri na ukarimu wa watu, ambao hukumu yao katika mfumo huu wa kutoa zaka inapaswa kuwa huru. Na wakati imeachwa huru kwa dhamiri, mpango umewekwa wazi vya kutosha kwa wote. Hakuna kulazimishwa kunakohitajika. 3T 394.1

Mungu aliwaita wanaume katika kipindi cha Musa kutoa sehemu ya kumi ya mazao yao yote. Alijitolea katika uaminifu wao vitu vya maisha haya, kuboreshwa kwa talanta na kumrudishia kidogo tu. Amehitaji sehemu ya kumi, na hii anadai kama ndogo kabisa kwamba mtu amrudishie. Anasema: Ninakupa tisa ya kumi 9/10, wakati nahitaji moja ya kumi 1/10; hiyo ni Yangu. Wakati watu wanazuia sehemu moja ya kumi, humpora Mungu kwa nguvu. Sadaka za dhambi, sadaka za amani, na matoleo ya shukrani pia zilihitajika kama nyongeza ya sehemu ya kumi ya ongezeko. 3T 394.2

Yote ambayo yanazuiliwa kwa yale ambayo Mungu anadai, sehemu ya kumi ya ongezeko, yameandikwa katika vitabu vya mbinguni dhidi ya wazuiaji, kama

uporaji wa nguvu. Vivyo hivyo humdanganya Muumba wao; na wakati dhambi hii ya kupuuza imeletwa mbele yao, haitoshi kwao kubadili njia yao na kuanza kufanya kazi kuanzia muda huo kwa kanuni sahihi. Hii haitasahihisha hesabu/takwimu zilizofanywa kwenye rekodi ya mbinguni ya wizi wa mali waliyokabidhiwa kwa amana ya kurudishwa kwa Mkopeshaji. Toba yakutofanya kwa uaminifu kwa Mungu, na kwa kutokuwa na shukrani ya msingi, inahitajika. 3T 394.3

Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia Mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la." Ahadi imetolewa hapa kwamba, ikiwa zaka zote zitaletwa ghalani, baraka kutoka kwa Mungu itamwagwa juu ya watiifu. 3T 394.4

"Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema BWANA wa majeshi." Ikiwa wote wanaoiamini Kweli watafikia matakwa ya Mungu kwa kutoa sehemu ya kumi, ambayo Mungu anasema ni Yake, hazina hiyo isheheni kwa wingi mapato ya kuendeleza kazi kuu ya wokovu wa mwanadamu. 3T 395.1

Mungu humpa mtu tisa ya kumi, wakati anadai moja ya kumi kwa madhumuni matakatifu, kwani amempa mtu siku sita kwa kazi zake mwenyewe na ameweka na kutenga siku ya saba Kwake Mwenyewe. Kwa maana, kama ilivyo Sabato, sehemu ya kumi ya faida ni takatifu; Mungu ameihifadhi kwa ajili Yake Mwenyewe. Yeye Ataendeleza kazi Yake duniani kwa kuongezeka kwa mapato ambayo amemkabidhi mwanadamu. 3T 395.2

Mungu aliwataka watu Wake wa zamani/kale mikusanyiko mitatu ya kila mwaka. "Mara tatu kwa mwaka wanaume wako wote watatokea mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua; katika Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, na Sikukuu ya Wiki, na Sikukuu ya Vibanda; nao hawatatokea mbele za Bwana mikono mitupu; kila mtu atatoa kadiri awezavyo, kwa baraka ya Bwana, Mungu wako, Aliyokupa." Sio chini ya theluthi moja ya mapato yao yalitolewa kwa malengo matakatifu na ya kidini. 3T 395.3

Wakati wowote ambao watu wa Mungu, katika kipindi chochote cha ulimwengu, wamefanya kwa moyo mkunjufu na kwa hiari mpango Wake katika mpango wa

utoaji wa ukarimu na katika zawadi na sadaka, wamegundua ahadi ya kudumu kwamba mafanikio yatakuja katika kazi zao zote kwa kadiri tu wanavyotii matakwa Yake. Walipokubali madai ya Mungu na kutii matakwa Yake, wakamheshimu Yeye kwa mali zao, ghala zao zilijazwa na vingi. Lakini walipomnyang'anya Mungu katika zaka na katika matoleo walifanywa watambue kwamba hawakuwa wakimwibia Yeye tu bali wao wenyewe, kwani aliweka baraka Zake kwao kwa kadiri tu vile walivyoweka dhabihu zao Kwake. 3T 395.4

Wengine watatamka hii kama moja ya sheria ngumu/kali zinazowafunga Waebrania. Lakini hii haikuwa mzigo kwa moyo wenye nia ya kupenda ambao ulimpenda Mungu. Ilikuwa tu wakati tabia zao za ubinafsi zilipoimarishwa kwa kuzuia kwamba watu walipoteza maono katika kufikiria uzima wa milele na kuthamini hazina zao za kidunia juu ya roho. Kuna mahitaji ya dharura zaidi kwa Israeli wa Mungu katika siku hizi za mwisho kuliko ilivyokuwa kwa Israeli ya zamani. Kuna kazi kubwa na muhimu kutimizwa kwa muda mfupi sana. Mungu hakuwahi kubuni kwamba sheria ya mfumo wa kutoa zaka haifai kuwa ya maana au ipuuzwe kati ya watu Wake; lakini, badala ya hii, Alipanga kwamba roho ya kujitolea inapaswa kupanuka na kuongezeka kwa kazi ya mwisho-kabla ya kufunga kazi ya Mungu. 3T 396.1

Mfumo wa ukarimu kwa mpango haupaswi kufanywa kuwa mfumo wa kulazimisha watu, msukumo wa kutoa bila hiari yao. Kwani ni sadaka za hiari ndizo ambazo zinakubaliwa na Mungu. Ukarimu wa Kweli wa Kikristo unatokana na kanuni ya upendo wa shukrani. Upendo kwa Kristo hauwezi kuwepo bila upendo unaoendana sambamba kama mwitikio kwa wale ambao Yeye alikuja ulimwenguni kuwakomboa. Upendo kwa Kristo lazima uwe kanuni ya kutawala ya nafsi, kudhibiti hisia zote na kuongoza nguvu zote. Upendo Unaokomboa unapaswa kuamsha mapenzi yote nyororo, kujali, huruma na kujinyima, na kujitoa nafsi, ambayo yanaweza kuwepo katika moyo wa mwanadamu. Wakati hii ni kesi, hakuna rufaa au kuwasihi watu ili kuwachochea moyo kutahitajika kuvunja ubinafsi wao na kuamsha huruma zao zilizolala, ili kutoa matoleo mazuri kwa sababu umuhimu wa Ukweli wenye thaman. 3T 396.2

Yesu ametununua kwa dhabihu isiyo na mwisho. Uwezo wetu wote na ushawishi wetu kwa ile Kweli ni wa Mwokozi wetu kwa hakika, na unapaswa kutolewa kwa huduma Yake. Kwa kufanya hivi tunaonesha shukrani zetu kwamba tumekombolewa kutoka katika utumwa wa dhambi na damu ya Kristo. Mwokozi wetu anafanya kazi daima kwaajili yetu. Amepanda juu na kusihi kwa niaba ya ununuzi wa damu Yake. Yeye husihi mbele ya Baba Yake mateso ya kusulubiwa. Anainua mikono Yake iliyojeruhiwa na kuliombea kanisa Lake, ili wazuiwe wasianguke chini ya majaribu. 3T 396.3

Ikiwa mitazamo yetu ingeweza kuhuishwa na Roho Mtakatifu ili kuchukua kazi hii nzuri na ya ajabu ya Mwokozi wetu kwa wokovu wetu, upendo, wa kina na wenye bidii, ungewaka mioyoni mwetu. Kutojali kwetu na kutojali ubaridi kungetuogopesha na kuweka katika tahadhari. Kujitolea kabisa na ukarimu, unaosababishwa na upendo wa shukrani, utatoa kwa hata sadaka ndogo kabisa, dhabihu ya hiari, harufu nzuri, na kuifanya zawadi hiyo kuwa ya thamani kubwa. Lakini, baada ya kujitoa kwa hiari kwa Mkombozi wetu yote tunayoweza kutoa, yawe ya thamani kubwa kwetu, ikiwa tunaona deni letu la shukrani kwa Mungu kama lilivyo haswa, yote ambayo huenda tukatoa yataonekana kwetu hayatoshi na duni. Lakini malaika huchukua sadaka hizi, ambazo kwetu huonekana duni, na huziwasilisha kama sadaka yenye harufu nzuri mbele ya kiti cha enzi, na zinakubaliwa. 3T 396.4

Sisi, kama wafuasi wa Kristo, hatutambui nafasi yetu halisi. Hatuna maoni sahihi juu ya majukumu yetu kama watumishi wa Kristo walioajiriwa. Yeye Ametuongezea mshahara katika maisha Yake ya mateso na damu iliyomwagika, kutufunga katika utumishi wa hiari Kwake. Vitu vyote vizuri tulivyonavyo ni mkopo kutoka kwa Mwokozi wetu. Ametufanya mawakili. Sadaka zetu ndogo zaidi, huduma zetu za unyenyekevu, zinazotolewa kwa imani na upendo, zinaweza kuwa zawadi zilizowekwa wakfu kuongoa roho kwa kazi ya Bwana na kukuza utukufu Wake. Maslahi na ustawi wa ufalme wa Kristo unapaswa kuwa kipaumbele/kwanza katika kila jambo lingine. Wale ambao hufanya raha zao na masilahi ya ubinafsi kuwa vitu muhimu vya maisha yao sio mawakili waaminifu. 3T 397.1

Wale ambao hujikana wenyewe kufanyia wengine mema, na wanaojitolea wenyewe na kila kitu walicho nacho kwa huduma ya Kristo, watatambua furaha ambayo mtu mwenye ubinafsi/mchoyou hutafuta bure. Alisema Mwokozi wetu: "Yeyote aliye miongoni mwenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi Wangu." Upendo "hautafuti yake wenyewe." Haya ni matunda ya upendo wenye ukarimu usio na ubinafsi ambao ulionesha maisha ya Kristo. Sheria ya Mungu mioyoni mwetu italeta masilahi yetu wenyewe kwa kujitiisha kwa hali ya juu na ya milele. Tumeamriwa na Kristo kuutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake. Hili ni jukumu letu la kwanza na la juu zaidi. Bwana wetu aliwaonya wazi watumishi Wake wasiweke hazina duniani; kwani kwa kufanya hivyo mioyo yao ingekuwa juu ya mambo ya kidunia badala ya vitu vya mbinguni. Hapa ndipo roho nyingi masikini zilipofanya ajali ya imani-angamiza imani. Wameenda moja kwa moja kinyume na agizo la wazi la Bwana wetu, na wameruhusu upendo wa pesa kuwa shauku ya kutawala ya maisha yao. Hawana kiasi katika juhudi zao za kupata mali/mapato. Wameleweshwa sana na hamu yao ya wendawazimu wa utajiri kama vile yule anayekunywa pombe. 3T 397.2

Wakristo wanasahau kuwa wao ni watumishi wa Bwana; kwamba wao wenyewe, wakati wao, na kila kitu walicho nacho ni mali Yake. Wengi hujaribiwa, na wengi wanashindwa, na vishawishi vya udanganyifu ambavyo Shetani anawasilisha kuwekeza pesa zao ambapo itawapa faida kubwa kwa dola na senti. Kuna wachache tu ambao huzingatia madai ya lazima ambayo Mungu anayo juu yao kuifanya iwe biashara/shuguli yao ya kwanza kukidhi mahitaji kwa ajili Yake na kuruhusu tamaa zao wenyewe kutumikiwa mwishoni. Kuna wachache tu ambao wanawekeza katika kusudi la Mungu kwa kadiri ya uwezo wao. Wengi wamefunga pesa zao katika mali ambayo lazima wauze kabla ya kuwekeza kwa ajili ya Mungu na hivyo kuiweka kwenye utendaji halisi. Lakini wanafanya hii kuwa kisingizio cha kufanya kidogo katika kusudi la kazi ya Mkombozi wao. Wamezika pesa zao ardhini kwa ufanisi kama mtu wa Mfano wa Biblia-Mathayo 25:14-25. Wanamnyang'anya Mungu sehemu ya kumi, ambayo anadai kuwa ni Yake Mwenyewe, na kwa kumuibia Yeye wanajinyang'anya hazina ya mbinguni. 3T 398.1

Mpango wa mfumo wa ukarimu haumkandamizi sana mtu mmoja. “Na sasa kuhusu matoleo kwa ajili ya kuwasaidia watu wa Mungu. Kama nilivyoagiza makanisa ya Galatia, fanyeni vivyo hivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mmoja wenu atenge kiasi cha fedha, kulingana na mapato yake, na fedha hiyo aiweke ili nitakapokuja pasiwepo na haja ya kufanya mchango.” Masikini hawatengwi na upendeleo wa kutoa. Wao, pamoja na matajiri, wanaweza kushiriki katika kazi hii. Somo ambalo Kristo alitoa kuhusu sarafu mbili za mjane linatuonesha kwamba sadaka ndogo zaidi, iliyotolewa kwa hiari ya maskini, ikiwa zimetolewa kutoka kwa moyo wa upendo, zinakubalika kama michango mikubwa zaidi ya matajiri. 3T 398.2

Katika mizani ya Patakatifu zawadi za maskini, zilizotolewa kutoka kwa upendo kwa Kristo, hazikadiriwi kulingana na kiwango kilichotolewa, lakini kulingana na upendo uliopelekea hiyo sadaka. Ahadi za Mungu hakika zitatambuliwa na maskini mkarimu, ambaye ana kidogo cha kutoa, lakini ambaye hutoa hicho kidogo bure, kama vile tajiri anayetoa kwa wingi wake. Mtu maskini hutoa dhabihu yake ndogo, ambayo anaihisi Kweli. Anajinyima mwenyewe kwa baadhi ya vitu ambavyo anahitaji kwa raha yake mwenyewe, wakati tajiri hutoa kwa wingi wake, na hahisi kukosa, hajinyimi kitu chochote ambacho anakihitaji kwa dhati/kweli. Kwa hivyo kuna utakatifu katika toleo la mtu masikini ambao haupatikani katika zawadi ya tajiri, kwa matajiri hutoa kwa wingi wao. Utoaji wa Mungu umepanga mchakato mzima wa mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu kwa faida ya mwanadamu. Utoaji wake hausimami kamwe. Ikiwa watumishi wa Mungu wanafuata mwongozo wake wazi wa utoaji, wote watakuwa watendakazi wenye bidii. 3T 398.3

Wale ambao wanazuia hazina ya Mungu na wanahifadhi mali zao kwa watoto wao, wanahatarisha masilahi ya kiroho ya watoto wao. Wanaweka mali yao, ambayo ni kikwazo kwao wenyewe, katika njia ya watoto wao, ili watoto wapate kujikwaa

juu na kupotea. Wengi wanafanya makosa makubwa kuhusu mambo ya maisha haya. Wanajinyima wakijibana kiuchumi, wakijizuia wao wenyewe na wengine mema wanayoweza kupata kutokana na matumizi sahihi ya mali ambazo Mungu amewapa, na kuwa wabinafsi na wenye tamaa. Wanapuuza masilahi yao ya kiroho na kuwa duni katika ukuaji wa kidini, yote kwa sababu ya kujilimbikizia mali ambayo hawawezi kutumia. Wanawaachia watoto wao mali zao, na mara tisa kati ya kumi ni laana kubwa zaidi kwa warithi wao kuliko ilivyo kwao wenyewe. Watoto, wakitegemea mali ya wazazi wao, mara nyingi hushindwa kufanikiwa katika maisha haya, na kwa jumla wanashindwa kabisa kupata maisha yajayo ya umilele. Urithi bora kabisa ambao wazazi wanaweza kuwaachia watoto wao ni ujuzi wa kazi muhimu na mfano wa maisha yenye sifa ya ukarimu usio na ubinafsi na usiojifikiria wenyewe. Kwa maisha kama hayo wanaonesha thamani halisi ya pesa, kwamba ni ya kuthaminiwa kwa uzuri ambayo itatimiza katika kupunguza mahitaji yao na mahitaji ya wengine, na katika kuendeleza kusudi la Mungu. 3T 399.1

Wengine wako tayari kutoa kulingana na kile walicho nacho, na wanahisi kuwa Mungu hana madai zaidi juu yao, kwa sababu hawana uwezo mkubwa. Hawana mapato ambayo wanaweza kubakiza katika mahitaji ya familia zao. Lakini kuna wengi wa daraja hili ambao wanaweza kujiuliza swali: Je! Ninatoa kulingana na kile ningeweza kuwa nacho? Mungu alipanga kwamba nguvu zao za mwili na akili zitumike. Wengine hawajaboresha kwa kiwango bora cha uwezo ambao Mungu amewapa. Kazi ni sehemu ya maisha ya mwanadamu [tangu uumbaji]. Iliunganishwa na laana, kwa sababu ililazimishwa na dhambi. Ustawi wa mwili, akili, na maadili ya mwanadamu hufanya maisha ya kazi muhimu yawe ya lazima. "Msiwe wavivu katika biashara," ni agizo la mtume aliyeongozwa na roho ya Mungu. 3T 400.1

Hakuna mtu, awe tajiri au maskini, anayeweza kumtukuza Mungu kwa maisha ya uvivu. Mtaji wote ambao wanaume masikini wengi wanao ni wakati na nguvu ya mwili, na hii hupotezwa mara kwa mara kwa kupenda raha, maisha rahisi na kwa uvivu wa hovyo ili wasiwe na chochote cha kumletea Bwana wao kwa zaka na katika matoleo. Ikiwa wanaume Wakristo wanakosa hekima ya kufanya kazi kwa kiwango bora na kufanya mgawanyo wa busara wa nguvu zao za mwili na akili, wanapaswa kuwa na upole na unyenyekevu wa akili kupokea ushauri na ushauri wa ndugu zao, ili uamuzi wao bora uweze kutoa mapungufu yao . Masikini wengi ambao sasa wanaridhika kutokufanya chochote kwa faida ya wenzao na kwa maendeleo ya kazi ya Mungu wanaweza kufanya mengi ikiwa wangefanya. Wanawajibika kwa Mungu kwa mtaji wao wa nguvu ya mwili kama vile yule tajiri kwa mtaji wa pesa. 3T 400.2

Wengine ambao wanapaswa kuweka mali katika hazina ya Mungu watakuwa wapokeaji kutoka Kwake. Kuna wale ambao sasa ni masikini ambao wangeweza

kuboresha hali zao kwa kutumia busara ya wakati wao, kwa kuepukana na haki za hataza (patents), na kwa kuzuia mwelekeo wao wa kushiriki katika dhana ili kupata mapato kwa njia rahisi kuliko kwa kazi ya subira, ya kudumu. Ikiwa wale ambao hawajafanikiwa kimaisha wangekuwa tayari kufundishwa, wangeweza kujizoeza wenyewe mazoea ya kujinyima na uchumi madhubuti, na kuwa na kuridhika kwa kuwa watoaji/wagawaji, badala ya wapokeaji wa hisani [charity]. Kuna watumishi wengi wavivu. Ikiwa wangefanya kile kilicho katika uwezo wao kufanya wangepata baraka kubwa sana katika kusaidia wengine hivi kwamba wangegundua kweli kwamba "ni heri kutoa kuliko kupokea." 3T 400.3

Ukarimu ulioelekezwa kwa haki hutumia nguvu za kiakili na za maadili za wanaume, na huwafurahisha na kuwahamasisha kwa hatua nzuri zaidi katika kuwabariki wahitaji na katika kuendeleza kazi ya Mungu. Ikiwa wale walio na mali watatambua kuwa wanawajibika kwa Mungu kwa kila senti ambayo wanatoa, mahitaji yao yanayodhaniwa yatakuwa kidogo. Ikiwa dhamiri ingekuwa hai, ingeshuhudia juu ya matumizi yasiyo ya lazima kwa kuridhisha hamu ya kula, kiburi, ubatili, na kupenda burudani, na ingetoa taarifa juu ya ulafi wa pesa za Bwana, ambazo zingetakiwa kujitolea kwa sababu Yake Bwana. Wale wanaopoteza bidhaa za Bwana wao hatimaye siku ya hukumu watatoa hesabu ya mwelekeo wao kwa Bwana. 3T 401.1

Ikiwa wale wanaojiita Wakristo wangetumia utajiri wao kidogo katika kupamba mwili na kupamba nyumba zao wenyewe, na wangetumia fedha kidogo katika anasa za kupindukia, zinazoharibu afya kwenye meza zao, wangeweza kuweka kiasi kikubwa zaidi katika hazina ya Mungu. Kwa hivyo wangemwiga Mkombozi wao, aliyeacha mbingu, utajiri Wake, na utukufu Wake, na kwa ajili yetu akawa maskini, ili sisi tupate utajiri wa milele. Ikiwa sisi ni maskini sana kuweza kumtolea Mungu kwa uaminifu zaka na matoleo ambayo Yeye huhitaji, hakika sisi ni maskini sana kuweza kuvaa kwa gharama kubwa na kula anasa; kwa hivyo tunapoteza pesa za Bwana wetu katika anasa za kujeruhi ili kujipendeza na kujitukuza sisi wenyewe. Tunapaswa kujiuliza kwa bidii sisi wenyewe: Je! Tumewekeza hazina gani katika ufalme wa Mungu? Je, sisi ni matajiri kwa Mungu? 3Tsw 401.2

Yesu aliwapa wanafunzi Wake somo juu ya tamaa. “Kisha akawaambia mfano, “Shamba la tajiri mmoja lilizaa sana. Akawaza moyoni mwake, Je, ‘Nifanye nini? Maana sina mahali pa kuweka mavuno yangu.’ Kisha akasema, ‘Nitafanya hivi: nitabomoa maghala yangu na kujenga maghala makubwa zaidi na huko nitaweka mavuno yangu yote na vitu vyangu. Na nitasema moyoni, ‘Hakika nina bahati! Ninayo mali ya kunitosha kwa miaka mingi. Sasa nitapumzika: nile, ninywe na kustarehe.’ Lakini Mungu akamwambia, ‘Mjinga wewe! Usiku huu huu utakufa-maisha yako yatatakiwa kukomea hapa! Sasa hivyo vitu ulivyojiwekea vitakuwa

vya nani?’ Hivi ndivyo itakavyokuwa kwa mtu ye yote anayehangaika kujikusanyia utajiri duniani lakini si tajiri mbinguni kwa Mungu.” 3T 401.3

Urefu na furaha ya maisha haimo katika kiwango cha mali zetu za kidunia. Tajiri huyu mpumbavu kwa ubinafsi wake mkuu alikuwa amejiwekea hazina ambazo hangeweza kutumia. Alikuwa akiishi kwa ajili yake tu. Alikuwa amepunja na kudhulumu wengine katika biashara, alikuwa amefanya majadiliano kubembeleza bei ishuke na kuumiza wengine (bargain), na hakuwa ameonesha rehema au upendo wa Mungu. Alikuwa amewabia yatima na mjane, na aliwatapeli wenzake, ili kuongeza hisa yake ya mali za ulimwengu. Angeweza kuweka hazina yake mbinguni katika mifuko ambayo haichakai; lakini kwa kutamani kwake alipoteza ulimwengu wa hapa na ule wa milele. Wale ambao kwa unyenyekevu hutumia kwa utukufu wa Mungu mali ambazo amewakabidhi hatimaye siku ya hukumu, watapokea hazina yao kutoka kwa Bwana na baraka: "Vema, mtumishi mwema na mwaminifu: ... ingia katika furaha ya Mola wako.” 3T 402.1

Tunapofikiria dhabihu isiyo na kikomo/mwisho iliyotolewa kwa wokovu wa watu tunapotea kwa mshangao. Wakati ubinafsi unapopigania ushindi kwa mayowe katika mioyo ya wanadamu, nao wanajaribiwa kuzuia kiwango chao kinachostahili katika kazi yoyote nzuri, wanapaswa kuimarisha kanuni zao za haki kwa wazo kwamba Yeye ambaye alikuwa tajiri katika hazina isiyokadirika ya mbinguni aliiacha yote na kuwa maskini. Masihi Hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Na dhabihu hii yote ilikuwa kwa ajili yetu, ili tupate utajiri wa milele. 3T 402.2

Kristo aliweka miguu Yake Mwenyewe katika njia ya kujikana nafsi na kujitolea dhabihu, ambayo wanafunzi Wake wote lazima wasafiri ikiwa watainuliwa pamoja Naye mwishowe. Alichukua moyoni Mwake Mwenyewe huzuni ambazo mtu lazima apate. Akili za watu wa ulimwengu mara nyingi hujazwa na ubaya. Wanaweza kuona vitu vya kidunia tu, ambavyo huzinga ule utukufu na thamani ya vitu vya mbinguni. Wanadamu watazunguka nchi kavu na baharini kwa faida ya kidunia, na watavumilia shida na mateso kupata kitu chao, lakini wataacha vivutio vya mbinguni na hawatazingatia utajiri wa milele. Wanaume walio katika umaskini kwa kulinganisha hao kawaida ndio wanaofanya zaidi ili kutegemeza/kudumisha kusudi la Mungu. Wao ni wakarimu na kidogo chao. Wameimarisha misukumo yao ya ukarimu na kuendelea kutoa kwa ukarimu. Wakati matumizi yao yalipokaribia mapato, shauku yao ya utajiri wa kidunia haikuwa na nafasi au nafasi ya kuimarishwa. 3T 402.3

Lakini wengi, wanapoanza kukusanya utajiri wa kidunia, wanaanza kuhesabu ni muda gani utapita kabla ya kuwa na kiasi fulani. Katika wasiwasi wao wa kujikusanyia mali kwa ajili yao wanashindwa kuwa matajiri kwa Mungu. Ukarimu wao hauendani na mkusanyiko wao. Kadiri shauku yao ya utajiri inavyoongezeka,

mapenzi yao yanafungwa na hazina yao. Ongezeko la mali zao linaimarisha hamu ya kutaka zaidi, mpaka wengine hufikiri kwamba kumpa Bwana sehemu ya kumi ni ushuru mkali, na usio wa haki, wanadhulumiwa. Uvuvio umesema: "Utajiri ukiongezeka, usiwekee moyo wako juu yake." Wengi wamesema: "Ikiwa ningekuwa tajiri mtu huyo, ningeongeza zawadi zangu kwa hazina ya Mungu. Singefanya kitu kingine chochote na utajiri wangu lakini nitumie kwa maendeleo ya kazi ya Mungu." Mungu amewajaribu wengine hawa, kwa kuwapa utajiri, lakini pamoja na utajiri ulikuja jaribu kali, na ukarimu na wema wao ulikuwa mdogo sana kuliko siku za umaskini wao. Tamaa ya kushika utajiri mkubwa ilivuta akili na mioyo yao kwa ukali, na wakaabudu sanamu. 3T 403.1

Yeye ambaye atawasilisha kwa watu utajiri usio na mwisho na maisha ya milele ya heri katika ufalme wake kama tuzo ya utii mwaminifu, hatakubali moyo uliogawanyika. Tunaishi katikati ya hatari za siku za mwisho, ambapo kuna kila kitu cha kugeuza akili na kushawishi mapenzi kutoka kwa Mungu. Wajibu wetu utatambuliwa na kuthaminiwa tu wakati utakapozingatiwa katika nuru inayoangaza kutoka kwa maisha ya Kristo. Kama vile Jua linapochomoza mashariki na kupita kuelekea magharibi, likiujaza ulimwengu nuru, ndivyo mfuasi wa Kweli wa Kristo atakuwa nuru kwa ulimwengu. Ataenda ulimwenguni kama nuru inayong'aa, ili wale ambao wako gizani wapatiwe nuru na kupashwa moto na miale inayoangaza kutoka Kwake. Kristo anasema juu ya wafuasi Wake: “Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Jiji lililowekwa juu ya mlima haliwezi kufichwa.” 3T 403.2

Mfano wetu Mkuu alikuwa anajikana Mwenyewe, na je! Mwendo wa wanaojiita wafuasi Wake utakuwa tofauti kabisa na Wake? Mwokozi alitoa vyote kwa ajili ya ulimwengu unaoharibika, bila kujizuia hata Yeye Mwenyewe. Kanisa la Mungu limelala. Washiriki wanadhoofishwa na kutotenda-ulivu. Sauti zinatujia kutoka kila sehemu ya ulimwengu, "Njoo utusaidie;" lakini hakuna jibu la kwenda. Kuna juhudi dhaifu mara kwa mara; wachache wanaonesha kuwa watakuwa watendakazi-wenza na Bwana wao; lakini hao mara nyingi huachwa wakitaabika kufanya kazi karibu peke yao. Lakini kuna mmishonari mmoja tu kutoka kwa watu wetu katika uwanja wote katika nchi za kigeni. 3T 404.1

Ukweli ni wenye nguvu, lakini haufanywi kwa vitendo. Haitoshi kuweka pesa peke yake juu ya madhabahu. Mungu anatoa wito kwa watu, kujitolea (kihali na mali), kupeleka Ukweli kwa mataifa mengine na lugha na watu. Sio idadi yetu wala utajiri wetu ambao utatupa ishara ya ushindi; lakini ni kujitolea kwa kazi, ujasiri wa maadili, upendo wa bidii kwa roho, na bidii yenye nguvu isiyochoka, bila ya uvivu. 3T 404.2

Kuna wengi ambao wameliona taifa la Kiyahudi kama watu wa kuhurumiwa kwa sababu walitozwa ushuru kila wakati kwa kusaidia wa dini yao; lakini Mungu,

ambaye alimuumba mwanadamu na kumpatia baraka zote anazofurahia, alijua ni nini ilikuwa kwa faida yake. Na kupitia baraka Yake, aliwafanya sehemu yao ya tisa ya kumi kuwa na thamani zaidi kwao kuliko kiwango chote bila baraka Zake. Ikiwa yeyote, kwa ubinafsi, alimwibia Mungu au alimletea sadaka isiyokamilika, hakika maafa na hasara zilikuwa zikiwafuata. Mungu anasoma nia za moyo. Yeye anafahamiana na madhumuni ya moyo wa wanadamu na atawashirikisha kwa wakati Wake mzuri kama walivyostahili. 3Tsw 404.3

Mfumo maalum wa kutoa fungu la kumi ulianzishwa kwa kanuni ambayo ni ya kudumu kama sheria ya Mungu. Mfumo huu wa kutoa fungu la kumi ulikuwa baraka kwa Wayahudi, la sivyo Mungu asingewapa. Kwa hivyo pia itakuwa baraka kwa wale ambao wanautekeleza hadi mwisho wa wakati. Baba yetu wa mbinguni hakuanzisha mchakato wa utoaji kwa mpango na ukarimu ili Ajitajirishe Yeye, bali kuwa baraka kubwa kwa mwanadamu. Aliona kuwa mfumo huu wa ukarimu/wema ni kile tu mwanadamu alihitaji. 3T 404.4

Makanisa ambayo yana mpangilio na ukarimu zaidi katika kudumisha kusudi la Mungu ndio yanayofanikiwa zaidi kiroho. Ukarimu wa Kweli katika mfuasi wa Kristo hutambulisha nia yake na ile ya Bwana wake. Katika kushughulika na Mungu na Wayahudi na watu Wake hadi mwisho wa wakati, Anahitaji mfumo wa ukarimu kulingana na mapato yao. Mpango wa wokovu uliwekwa na dhabihu isiyo na mwisho ya Mwana wa Mungu. Nuru ya injili inayoangaza kutoka katika msalaba wa Kristo inakemea ubinafsi na inahamasisha ukarimu na wema. Haipaswi kuwa Ukweli uliolalamikiwa kwamba kuna wito unaoongezeka wa kutoa. Mungu katika uongozi Wake anawaita watu Wake kutoka katika nyanja ndogo ya hatua na kuingia kwenye shuguli/biashara kubwa. Jitihada zisizo na kikomo zinahitajika wakati huu wakati giza la maadili linafunika ulimwengu. Mambo ya udunia/ulimwengu na kutamani, yanakula miili ya watu wa Mungu. Wanapaswa kuelewa kuwa ni rehema Yake Bwana, ndiyo ambayo huzidisha mapato kwa mahitaji yao. Malaika wa Mungu huweka vitendo vya fadhili karibu na maombi. Alimwambia Kornelio: "Maombi yako na sadaka zako zimepanda kuwa ukumbusho mbele za Mungu." 3T 405.1

Katika mafundisho ya Kristo alisema: "Kwa hivyo ikiwa hamkuwa waaminifu kwa mali isiyo ya haki, ni nani atakayewakabidhi mali yenu ya Kweli?" Afya ya kiroho na ustawi wa kanisa hutegemea kwa kiwango kikubwa juu ya mfumo wa ukarimu wake kwa mpango. Ni kama damu ya uhai ambayo lazima itiririke kwa kiumbe chote, ikimuhimizana kumtia nguvu kila mshiriki wa mwili. Inaongeza upendo kwa roho za wenzetu; kwani kwa kujikana na kujitoa dhabihu tumeletwa katika uhusiano wa karibu na Kristo, Ambaye kwa ajili yetu akawa masikini. Kadri tunavyowekeza zaidi katika sababu ya Mungu kusaidia katika wokovu wa roho, ndivyo zitakavyoletwa karibu na mioyo yetu. Je! Idadi yetu ingekuwa kubwa kama nusu, na tukawa na hawa wafanyakazi wote waliojitolea, hakika tunapaswa kuwa

na nguvu ambayo itafanya ulimwengu utetemeke. Kwa watenda kazi Kristo amewaambia Maneno haya: "Tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu." 3T 405.2

Tutakutana na upinzani unaotokana na nia za ubinafsi, upendeleo na ubaguzi; hata hivyo, kwa ujasiri usio na hofu na imani iliyo hai, tunapaswa kupanda mbegu kando kando ya maji yote. Mawakala wa Shetani ni wa kutisha; tutakutana nao na lazima tupigane nao. Kazi zetu hazipaswi kufungiwa katika nchi yetu wenyewe (Marekani). Shamba ni ulimwengu; mavuno yameiva. Amri iliyotolewa na Kristo kwa wanafunzi kabla tu hajapaa ilikuwa: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. 3T 406.1

Tunahisi uchungu kupita kiasi kuona baadhi ya wachungaji wetu wakizungukazunguka makanisani, inaonekana wakifanya juhudi kidogo, lakini ni wanakaribia kutokuwa na lolote la kuonyesha kwa kazi zao. Uwanja ni ulimwengu. Hebu watoke nje waende kwenye ulimwengu usioamini na wafanye bidii kugeuza roho kwa ukweli. Tunawaelekeza kaka na dada zetu kwa mfano wa Ibrahimu kupanda Mlima Moria kumtoa Mwanawe wa pekee kwa amri ya Mungu. Hapa palikuwa na utii na dhabihu. Musa alikuwa katika nyua za kifalme, na taji iliyotarajiwa lilikuwa mbele yake. Lakini aliiacha ile rushwa ya kumjaribu, na “akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona afadhali kuteswa pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu kushutumiwa kwake kwaajili ya Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri.” 3T 406.2

Mitume hawakuyahesabu maisha yao kuwa ya thamani kwao wenyewe, wakafurahi kwamba wamehesabiwa kuwa wamestahili kuteswa kwa ajili ya Jina la Kristo. Paulo na Sila walipata hasara ya vitu vyote. Waliteseka kwa kupigwa mijeledi, na hawakutupwa kwa njia ya upole juu ya sakafu baridi ya shimo katika hali yenye uchungu sana, miguu yao ikiwa imeinuliwa na kufungwa kwenye nguzo. Je, kuudhika, mayowe na malalamiko yalilifikia sikio la mlinzi wa gereza? Lo, hapana! Kutoka katika gereza la ndani, sauti zilivunja ukimya wa usiku wa manane kwa nyimbo za shangwe na sifa kwa Mungu. Wanafunzi hawa walishangiliwa na upendo wa dhati na bidii kwa ajili ya kazi ya Mkombozi wao, ambayo kwa ajili yake waliteseka. 3T 406.3

Ukweli wa Mungu unapojaza mioyo yetu, na kufyonza mapenzi yetu, na kudhibiti maisha yetu, sisi pia tutahesabu kuwa ni furaha kuteseka kwa ajili ya Ukweli. Hakuna kuta za gereza, hakuna kigingi cha mfia imani, kinachoweza kututisha au kutuzuia katika kazi hiyo kuu. Njoo, ee nafsi yangu, mpaka Kalvari. Yawekee alama maisha duni ya Mwana wa Mungu. Yeye Alikuwa “mtu wa huzuni nyingi, ajuaye huzuni.” Tazama fedheha Yake, uchungu Wake katika Gethsemane, na ujifunze

kujinyima-kujikana nafsi ni nini. Je, tunapungukiwa au tu fukara ? ndivyo alivyokuwa Kristo, Ukuu wa mbinguni. Lakini umaskini Wake ulikuwa kwa ajili yetu. 3T 406.4

Je, tunaorodheshwa miongoni mwa matajiri? vivyo hivyo na Yeye. Lakini alikubali kuwa maskini kwa ajili yetu, ili sisi kwa umaskini Wake tupate kuwa matajiri. Katika Kristo tuna mfano wa kujikana nafsi. Dhabihu Yake haikutia ndani kuacha tu nyua za kifalme za mbinguni, kuhukumiwa na watu waovu kama mhalifu na kutangazwa kuwa na hatia, na kutolewa ili afe kama mhalifu, bali kubeba uzito wa dhambi za ulimwengu. Maisha ya Kristo yanakemea kutojali kwetu na ubaridi. Tunakaribia mwisho wa wakati, ambapo Shetani ameshuka chini akiwa na ghadhabu nyingi, akijua kwamba wakati wake ni mfupi. Adui anafanya kazi kwa madanganyo yote ya udhalimu ndani yao wanaopotea. Vita vimeachwa mikononi mwetu na Kiongozi wetu mkuu ili tuendeleze kwa nguvu. Hatufanyi sehemu ya ishirini ya kile tunachoweza kufanya ikiwa tungekuwa macho 1/20. Kazi imezuiwa na upendo wa urahisi na ukosefu wa roho ya kujikana ambayo Mwokozi wetu ametupa kielelezo katika maisha Yake. Watenda kazi pamoja na Kristo, wanaume wanaohisi hitaji la juhudi kubwa, wanatafutwa. Kazi ya uchapaji/matbaa zetu isipunguzwe, bali iongezwe maradufu. Shule zianzishwe sehemu mbalimbali ili kuwaelimisha vijana wetu kujitayarisha kwa bidii yao kuendeleza Ukweli.3T 407.1

Tayari muda mwingi umepotea, na malaika wanabeba mbinguni kumbukumbu ya kutokujali kwetu. Hali yetu ya kusinzia na kutowekwa wakfu imetupotezea nafasi/fursa za thamani ambazo Mungu ametutumia katika nafsi za wale waliostahili kutusaidia katika hitaji letu la sasa. Lo, ni kiasi gani tunamhitaji Hana Moore wetu Zaidi kutusaidia wakati huu katika kufikia mataifa mengine! Ujuzi wake wa kina wa maeneo ya umishonari ungetupatia fursa ya kuwafikia wale wa lugha nyingine ambao hatuwezi kuwafikia sasa. Mungu alileta zawadi hii kati yetu ili kukabiliana na dharura yetu ya sasa; lakini hatukuithamini zawadi, naye akamchukua kutoka kwetu. Amepumzika sasa kutokana na taabu zake, lakini kazi zake za kujinyima zinamfuata. Ni jambo la kusikitisha kwamba kazi yetu ya umishenari inapaswa kucheleweshwa kwa kukosa maarifa jinsi ya kupata ufikiaji wa mataifa na maeneo mbalimbali katika shamba kubwa la mavuno. 3T 408.1

Tunahisi uchungu wa roho kwa sababu karama zingine zimepotea kwetu ambazo tungeweza kuwa nazo kama tungekuwa macho. Vibarua wamezuiliwa kutokana na mavuno ya weupe. Inakuwa watu wa Mungu kunyenyekea mioyo yao mbele zake, na katika unyonge wa ndani kabisa kumwomba Bwana atusamehe kutojali kwetu na ubinafsi wetu, na kufuta rekodi ya aibu ya majukumu yaliyopuuzwa na mapendeleo ambayo hayajaboreshwa. Katika kutafakari juu ya msalaba wa Kalvari, Mkristo wa Kweli ataachana na wazo la kuweka kikomo matoleo yake kwa yale yasiyomgharimu chochote na atasikia kwa sauti za tarumbeta: 3T 408.

Nendeni mkafanye kazi katika shamba La mizabibu; Kuna kupumzika mwishowe siku moja-huko mbinguni. 3T 408.2

Yesu alipokuwa karibu kupaa juu, Alielekeza kwenye mashamba ya mavuno na kuwaambia wafuasi Wake: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili.” “Mmepokea bure, toeni bure.” Je, sisi tujikane nafsi zetu ili kwamba mavuno yanayoharibiwa na kupotea shambani yaweze kukusanywa? 3T 408.3

Mungu anaitaka vipaji vya ushawishi na uwezo. Je, tutakataa kutii? Baba yetu wa mbinguni hutoa zawadi na kuomba sehemu nyingine, ili apate kutujaribu kama tunastahili kupata zawadi ya uzima wa milele. 3T 408.4

SURA YA 34

UTOAJI KWA UKARIMU KWA MPANGO

Ikiwa wote ambao Mungu amewafanikisha kwa utajiri wa dunia watatekeleza mpango Wake kwa kutoa kwa uaminifu sehemu ya kumi ya mazao yao yote, na ikiwa hawatazuia sadaka zao za hatia na sadaka zao za shukrani, hazina hiyo ingejazwa kila wakati. Usahili wa mpango wa utoaji kwa mpango/mfumo haujiondoi kwenye faida zake, bali unainua hekima ya Mungu katika mpangilio Wake. Kila kitu kilicho na muhuri wa mbingu kinaunganisha uzuri na faida. Ikiwa utoaji kwa ukarimu na mpangu utakubaliwa ulimwenguni pote kulingana na mpango wa Mungu, na mfumo wa kutoa fungu la kumi ukafanywa kwa uaminifu na matajiri kama ilivyo kwa watu masikini, hakungekuwa na haja ya miito ya mara kwa mara ya dharura/haraka kwa ajili ya vitu katika mikusanyiko yetu mikubwa ya kidini. Kumekuwa na kupuuzwa/kukataliwa katika makanisa katika kuufuata

mpango wa neema wa utoaji, na matokeo yake kumekuwa na upungufu katika hazina na kanisa kurudi nyuma. 3T 408.6

“Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmeniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Nanyi mmelaaniwa kwa laana; kwa kuwa mmeniibia Mimi, naam taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mnijaribu wa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi, muone kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha au la. Nami kwajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake mashambani, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; kwa maana mtakuwa nchi ya kupendeza, asema Bwana wa majeshi.” 3T 409.1

Mungu ameibiwa katika zaka na sadaka/dhabihu. Ni jambo la kuogofya kuwa na hatia ya kuzuia kuleta kitu kwenye hazina au kumwibia Mungu. Wahudumu wanaohubiri neno kwenye mikusanyiko yetu mikubwa wanahisi dhambi ya kupuuza kumtolea Mungu vitu ambavyo ni Vyake. Wanajua kwamba Mungu hatawabariki watu Wake wakati wanapuuza mpango Wake wa utoaji kwa ukarimu. Wanatafuta kuwaamsha watu katika wajibu wao kwa hotuba zilizoelekezwa, za vitendo, kuonesha hatari na dhambi ya ubinafsi na tamaa. Ushawishi huishika akili, na baridi kali yenye ubarafu wa ubinafsi inaanza kuvunjwavunjwa. Na wakati wito unatolewa kwa ajili ya michango kwa upande wa Mungu, wengine, kwa sababu ya ushawishi wa mikutano, wanaamshwa kutoa ambao bila hivyo wasingetoa chochote. Kwa kadiri tabaka hili linavyohusika, matokeo mazuri yameonekana. Lakini kwa sababu ya wito wa kushinikiza wengi huhisi mguso wa ndani zaidi ambao hawajawashwa mioyo yao iliyoganda ubaridi . Kwa uangalifu wameweka mali zao kuendelea kutolewa ili kuendeleza kazi ya Mungu. Utu wao wote umechochewa na maombi ya dhati yaliyotolewa, na hao hao hujibu ambao wanaweza kuwa wametoa yote ambayo mambo yao maishani yangehitaji (wanatoa wale waliokwishatoa! Tukitoa kwa mpango maalumu huu, kila mtu atawajibika na si wale-wale daima). 3T 409.2

Lakini hawa waamini walio huru, wenye moyo wote, wakichochewa na upendo wa bidii kwa ajili ya hiyo na hamu ya kuchukua hatua haraka, wanajihesabu wenyewe kuwa wenye uwezo wa kufanya zaidi ya vile Mungu anavyowataka wafanye, kwa kuwa umuhimu wao hauna uwezo katika mwelekeo mwingine. Wale walio tayari wakati mwingine huahidi kukusanya pesa wakati hawajui ni chanzo gani zitatoka, na wengine huwekwa katika mazingira ya kusikitisha ili kutimiza ahadi zao. Wengine wanalazimika kuuza mazao yao kwa hasara kubwa, na wengine wameteseka kwa kukosa mahitaji ya maisha ili kutimiza ahadi zao. 3T 410.1

Kulikuwa na wakati mwanzoni mwa kazi yetu ambapo dhabihu kama hiyo ingehesabiwa haki, wakati Mungu angewabariki wote ambao walijitokeza kufanya kwa ajili Yake. Marafiki wa Ukweli walikuwa wachache na uwezo wa mali, mdogo sana. Lakini kazi imekuwa ikiongezeka na kuimarishwa mpaka kuwe na mali ya kutosha mikononi mwa waamini kudumisha kazi hiyo katika idara zake zote bila kuleta aibu au kumwaibisha yoyote, ikiwa wote wangebeba sehemu yao sawia. Njia ya Mungu haifai kuwa kilema hata kidogo. Ukweli wa thamani umewekwa wazi sana na kwamba wengi wameushikilia ambao mikononi mwao kuna mali ambayo Mungu amewakabidhi kuitumia katika kuendeleza makusudi ya Ukweli. Ikiwa watu hawa wenye mali na watafanya wajibu wao, hakuna haja ya kushinikizwa kwa ndugu maskini. 3T 410.2

Tuko katika ulimwengu wa vitu vingi. Ikiwa sadaka na matoleo yatakuwa sawa na kile ambacho kila mmoja amepokea kutoka kwa Mungu, kusingekuwa na haja ya wito wa dharura kwa ajili ya mali/vitu katika mikusanyiko yetu mikubwa. Nina hakika kabisa kuwa sio mpango bora wa kuleta shinikizo juu ya kupata fedha kwenye mikutano yetu ya makambi. Wanaume na wanawake wanaopenda kusudi la Mungu kama wanavyopenda maisha yao wataahidi katika hafla hizi, wakati familia zao zinapaswa kuteseka kwa ajili ya fedha zile ambazo wameahidi kutoa kuendeleza kusudi la Mungu. Mungu wetu sio msimamizi mwenye roho mbaya na hahitaji mtu masikini kutoa mali ile ambayo ni kwa ajili ya familia yake na ambayo inapaswa kutumiwa kuwaweka katika hali bora na faraja na siyo kuishi kwa dhiki na uhitaji 3T 410.3

Miito kwa ajili ya fedha/mali katika mikutano yetu mikubwa ya makambi hadi sasa imeonekana kuwa na matokeo mazuri kuhusiana na matajiri. Lakini tunaogopa matokeo ya juhudi zilizoendelea ili kujaza hazina hiyo. Tunaogopa kwamba kutakuwa na athari/mwitikio. Jitihada kubwa inapaswa kufanywa na watu wenye kuwajibika/dhamana katika makanisa tofauti ili wote wafuate mfumo wa utoaji kwa ukarimu kwa mpango kama vile Mungu alivyoagiza. Ikiwa mfumo wa utoaji kwa ukarimu kwa mpango utafanywa, mito ya dharura/haraka kwenye mikutano ya makambi kwa ajili ya fedha matumizi anuwai haitakuwa ya lazima. 3T 411.1

Mungu amepanga mpango ambao wote wanaweza kutoa kama alivyowafanikisha, na ambao utafanya utoaji kuwa mazoea bila kusubiri wito maalum. Wale ambao wanaweza kufanya hivyo, lakini sio kwa sababu ya ubinafsi wao, wanamuibia Muumba wao, ambaye amewapa vitu vya kuwekeza katika kusudi Lake ili kuendeleza matakwa/maslahi Yake. Mpaka wote watakapotimiza mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu, kutakuwa na kushindwa kufikia kanuni ya kitume. Wale wanaohudumu kwa Neno na mafundisho wanapaswa kuwa watu wa kupambanua. Wanapaswa, wakati wanatoa wito kwa ujumla, wafahamu uwezo wa wale wanaoitikia wito wao, na hawapaswi kuwaruhusu masikini kutoa ahadi kubwa.

Baada ya mtu mara moja kuweka ahadi ya kiasi fulani kwa Bwana, anatambua kuwa ni sehemu takatifu, iliyowekwa wakfu kwa matumizi matakatifu. Hii ni kweli, na kwa hivyo ndugu zetu wanaohubiri wanapaswa kujifahamisha vizuri kwamba ni nani wataikubali ahadi [usichukue ahadi kutoka kwa yule masikini sana, kwa vile tu umehubiri watu watoe kiasi fulani, naye akasema ndiyo na kumbe hana kitu]. 3T 411.2

Kila mshiriki wa familia tofauti katika makanisa yetu ambaye anaamini Ukweli anaweza kufanya sehemu katika maendeleo yake kwa kuutumia kwa moyo mkunjufu mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu. "Kila mmoja wenu ajiwekee akiba [peke yake nyumbani], ... ili kusiwe na mikusanyiko nitakapokuja." Mzigo wa kusisitiza na kushinikiza watu binafsi kutoa pesa zao haujakusudiwa kuwa kazi ya wahudumu wa Mungu. Wajibu unapaswa kuwa juu ya kila mtu anayefurahia imani ya Ukweli. Hebu "Kila mmoja wenu ajiwekee akiba mwenyewe, kwa kadiri Mungu alivyomfanikisha." Kila mwanachama wa familia, kuanzia mkubwa hadi mdogo, anaweza kushiriki katika kazi hii ya utoaji. 3T 411.3

Sadaka za watoto wadogo zinaweza kukubalika na kumpendeza Mungu. Kulingana na roho inayosukuma kitu kitolewe itakuwa thamani ya sadaka hiyo. Masikini, kwa kufuata kanuni ya mtume na kwa kuweka kiwango kidogo kila wiki, husaidia kuongeza hazina, na matoleo yao yanakubalika kabisa kwa Mungu; kwani wanatoa dhabihu kwa ukubwa sawa na tena kubwa zaidi kuliko hata ndugu zao matajiri. Mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu, utathibitisha ulinzi kwa kila familia dhidi ya vishawishi vya kutumia pesa kwa ajili ya vitu visivyo vya lazima, na haswa itakuwa baraka kwa matajiri kwa kuwalinda wasiingie katika kuridhisha/kuendekeza ubadhirifu. 3T 412.1

Kila wiki madai ya Mungu kwa kila familia huletwa akilini kwa kila mmoja wa washiriki wake kutekeleza mpango huo; na kwa vile wamejikana wenyewe kupita kiasi ili wapate kitu cha kuweka kwenye hazina, masomo ya thamani kwa sababu ya kujikana nafsi kwa utukufu wa Mungu yamejazwa moyoni. Mara moja kwa wiki kila mmoja huletwa ana kwa ana na matendo ya juma lililopita — mapato ambayo angekuwa nayo ikiwa angekuwa mchumi na fedha ambazo hana kwa sababu ya anasa na kujiridhisha. Dhamiri yake inaamshwa, kama ilivyokuwa, mbele za Mungu, na inamridhisha au kumshutumu. Anajifunza kwamba ikiwa atabaki katika utulivu wa akili na ukubali wa Mungu lazima ale na anywe na avae kwa utukufu Wake Bwana. 3T 412.2

Utoaji wa mpango kwa ukarimu na huria kulingana na mpango huweka njia ya moyo wazi. Tunajiweka katika uhusiano na Mungu, ili atutumie kama mifereji ambayo vipawa vyake vinaweza kupita kwenda kwa wengine. Masikini hawatalalamika juu ya mfumo wa utoaji, kwani huwagusa kidogo. Hawapuuzwi na kuachwa, bali wanapendelewa kwa kushiriki na kufanya sehemu kama watenda kazi pamoja na Kristo, na watapata baraka za Mungu vivyo hivyo na matajiri.

Katika mchakato wa kuweka kando walio wadogo kama wanavyoweza kuwaepusha, wanajikana nafsi zao na kukuza ukarimu wa moyo. Wanajielimisha kwa matendo mema, na kwa ufanisi wanakutana na muundo wa Mungu katika mpango wa mfumo wa utoaji kwa mpango na ukarimu, kama ilivyo matajiri zaidi ambao hutoa kwa wingi wao. 3T 412.3

Katika siku za mitume, watu walikwenda kila mahali wakihubiri Neno. Makanisa mapya yalianzishwa. Upendo na bidii yao kwa Kristo iliwaongoza katika vitendo vya kujikana sana nafsi na kujitolea. Makanisa haya mengi ya watu wa Mataifa yalikuwa maskini sana, lakini mtume anatangaza kwamba ukubwa wa umaskini wao ulizidiwa na utajiri wa ukarimu wao. Matoleo yao yalikuwa makubwa zaidi ya uwezo wao wa kutoa. Watu walihatarisha maisha yao na waliteseka kwa kupoteza vitu vyote kwa ajili ya Ukweli. 3T 413.1

Mtume anapendekeza siku ya kwanza ya juma kama wakati mwafaka wa kukagua mwelekeo wa mlichojaliwa na mafanikio yaliyopatikana, na kwa kumcha Mungu, na shukrani ya dhati/kweli ya moyo kwa baraka ambazo ametoa, kuamua ni kiasi gani, kulingana na Mpango wake mwenyewe uliobuniwa, utarudishwa mwenyewe. 3T 413.2

Mungu anapanga kwamba zoezi la utoaji litakuwa la hiari kabisa, bila kuwa na kulazimishwa na hata kwa ushawishi sana ili kuamsha huruma. "Mungu anapenda anayetoa kwa moyo wa ukunjufu." Hafurahii kuwa hazina Yake ijazwe tena na vitu vya kulazimishwa. Mioyo miaminifu ya watu Wake, wakifurahi katika Kweli inayookoa kwa wakati huu, kupitia upendo na shukrani Kwake kwa nuru hii ya thamani, watakuwa wenye bidii na wenye hamu ya kusaidia kwa vitu vyao katika kupeleka Ukweli kwa wengine. Njia bora kabisa ya kuonesha upendo wetu kwa Mkombozi wetu ni kutoa sadaka ili kuleta roho kwenye ufahamu wa Ukweli. Mpango wa ukombozi ulikuwa wa hiari kabisa kwa upande wa Mkombozi wetu, na ni kusudi la Kristo kwamba wema wetu wote uwe sadaka za hiari. 3T 413.3

SURA YA 35

UHURU WA MTU BINAFSI

Mpendwa Ndugu A,

Akili yangu inawaza/inashugulishwa sana kuhusu jambo lako. Nimekuandikia vitu ambavyo vimeoneshwa kwangu kuhusiana na hali yako ya zamani, ya sasa, na ya baadaye. Ninahisi kuwa na wasiwasi juu yako kwa sababu nimeona hatari zako.

Uzoefu wako wa zamani kwenye umizimu unakuweka kwenye majaribu na mapambano/migogoro mikali. Pale tu akili inapokuwa imesalimishwa kwenye uongozi wa moja kwa moja wa adui kupitia malaika waovu, mtu huyo hapaswi kabisa kuamini mawazo na hisia ambazo zingempeleka kwenye njia huru, mbali na kanisa la Kristo. Hatua ya kwanza ambayo mtu huyo angechukua nje ya kanisa inapaswa kuchukuliwa kama kifaa cha adui kudanganya na kuharibu. Mungu amelifanya kanisa Lake kuwa mfereji wa nuru, na kupitia kwake huwasilisha makusudi Yake na mapenzi Yake. Hampi mtu uzoefu nje ya kanisa. Hampi mtu mmoja maarifa ya mapenzi Yake kwa kanisa lote, wakati kanisa, mwili wa Kristo, limeachwa gizani. 3T 414.1

Ndugu A, unahitaji kutazama kwa uangalifu mkubwa sana jinsi unavyojenga. Kuna dhoruba inakuja ambayo itajaribu matumaini yako yote. Unapaswa kuchimba kwa kina zaidi na kuweka msingi wako thabiti. “Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; Mvua ikanyesha, na mafuriko yakaja, na pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile; isianguke, kwa maana misingi take imewekwa juu ya mwamba. ” Kwa uthabiti mjenzi huweka jiwe moja juu ya lingine mpaka jengo husimama jiwe juu ya jiwe. Mjenzi wa injili mara nyingi huendelea na kazi yake kwa machozi na katikati ya majaribu, dhoruba za mateso, upinzani mkali, upinzani mchungu na dhuluma mbaya (kukosewa haki); lakini hujisikia kuogeza bidii zaidi , kwa maana anajenga kwa ajili ya umilele. Kuwa mwangalifu, Ndugu A, ya kwamba msingi wako ni mwamba imara, na kwamba umesimama juu yake, Kristo akiwa Ndiye mwamba huo. 3T 414.2

Una nia yenye ukaidi wenye nguvu, thabiti, roho ya kujitegemea mwenywe sana, ambayo unahisi kuwa ni lazima uisimamie wakati wa hatari zote. Na umechukua roho hiyo hiyo katika uzoefu wako na katika maisha yako dini. Mara nyingi umekuwa haupatani na kazi ya Mungu kama inavyofanywa na ndugu zako wa Marekani. Hujaona kama wao wanavyoona wala haukuungana na njia yao ya kuendelea mbele. Umekuwa na ujuzi mdogo sana wa kazi katika idara zake mbalimbali. Hujahisi wasiwasi kabisa kujishughulisha na nyanja mbalimbali za kazi. Umeangalia kwa kushuku na kutokuamini kazi hiyo, na juu ya viongozi waliochaguliwa na Mungu kuiendeleza mbele. Umekuwa tayari zaidi kuhoji na kushuku na kuwaonea wivu wale ambao Mungu amewapatia majukumu mazito ya kazi Yake, kuliko kujichunguza na kujiunganisha na makusudi ya Mungu ili ujue utendaji na maendeleo yake. 3T 414.3

Mungu aliona kuwa haukustahili kuwa mchungaji, mhudumu wa haki kutangaza Ukweli kwa wengine, hadi utakapokuwa mtu aliyebadilishwa kweli kweli. Aliruhusu upite katika majaribu dhahiri na ujisikie umasikini na uhitaji, ili uweze kujua jinsi ya kutumia huruma, sikitiko na rehema, na upendo wa huruma nyororo,

na kujali kwa wasiostahili na walioonewa, na kwa wale waliogubikwa na uhitaji na kupita kwenye jaribu na shida. 3T 415.1

Wakati ulipoomba katika shida yako kwa amani katika Kristo, wingu la giza lilionekana kufunika kwenye akili yako. Pumziko na amani halikuja kama vile ulivyotarajia wewe. Wakati mwingine imani yako ilionekana kujaribiwa kabisa. Ulipotazama nyuma katika maisha yako ya zamani, uliona huzuni na kukatishwa tamaa; ulipoangalia siku zijazo, yote yalikuwa kutokuwa na uhakika. Mkono wa Mungu ulikuongoza kimuujiza kukuleta msalabani na kukufundisha kwamba Mungu alikuwa Kweli mruzuku wa wale wanaomtafuta kwa bidii. Wale wanaoomba sawa sawa au kwa usahihi watapokea. Yule atafutaye kwa imani atapata. Uzoefu unaopatikana kutoka katika tanuru la majaribu na mateso ni wa thamani zaidi kuliko usumbufu wote na uzoefu mchungu unavyogharimu. 3T 415.2

Maombi ambayo ulitoa katika upweke wako, katika uchovu wako na jaribu, Mungu alijibu, sio mara zote kulingana na matarajio yako, lakini ni kwa faida yako. Hukuwa na mtazamo sawa na sahihi juu ya ndugu zako, wala haukujiona kuwa katika nuru sahihi. Lakini, katika majaliwa, mipango na wema wa Mungu, Yeye amekuwa kazini kujibu maombi uliyotoa katika shida yako, kwa njia ya wewe na kulitukuza Jina Lake Mwenyewe. Katika ujinga/kutojitambua kwako uliomba vitu ambavyo havikuwa bora kwako. Mungu alisikia maombi yako ya dhati, lakini baraka uliyopewa ilikuwa kitu tofauti kabisa na matarajio yako. Mungu alikusudia, katikawa uongozi Wake, kukuweka moja kwa moja katika uhusiano na kanisa Lake, ili ujasiri wako uwe mdogo kwako mwenyewe na uwe mkubwa kwa wengine ambao Yeye Anawaongoza kuendeleza kazi Yake. 3T 415.3

Mungu husikia kila ombi la dhati. Yeye Angekuweka katika uhusiano na kazi Yake ili akulete moja kwa moja katika nuru. Na endapo usingeona muhuri maono yako dhidi ya ushahidi na nuru utashawishika kwamba ikiwa ungejiamini zaidi na usiwaamini sana ndugu zako ungefanikiwa zaidi kwa Mungu. Ni Mungu ambaye amekuongoza kupitia njia nyofu/nyembamba. Alikuwa na kusudi katika hili, ili dhiki iweze kufanya kazi ndani yako ya uvumilivu, na uzoefu wa uvumilivu, na upate tumaini. Aliruhusu majaribu kuja juu yako ili kupitia hayo, uweze kupata matunda ya amani ya haki. 3Tsw 416.1

Petro alimkana Mtu wa huzuni katika kupatwa kwake na uchungu katika saa ya mateso na kufedheheshwa kwake. Lakini baadaye alitubu na akaongoka tena. Alikuwa na majuto ya kweli ndani ya moyo na akajitoa tena kwa Mwokozi wake. Kwa machozi yenye kupofusha anaenda kwenye upweke wa Bustani ya Gethsemane na na huko anasujudu na pale aliona umbo la Mwokozi wake wakati jasho la damu lilipolazimishwa kutoka kwenye vinyweleo vyake kwa uchungu Wake mkubwa. Petro akakumbuka kwa majuto kwamba alikuwa amelala wakati Yesu

akisali wakati wa masaa hayo ya kutisha. Moyo wake wa kiburi ukavunjika, na machozi ya toba yakabubujikia kwenye udongo ambao hivi karibuni ulikuwa umedondokewa na matone ya jasho la damu la Mwana mpendwa wa Mungu. Aliondoka kwenye bustani hiyo akiwa mtu aliyeongoka. Alikuwa tayari basi kuwahurumia waliojaribiwa. Alinyenyekezwa na angeweza kuhurumia wanyonge na wakosefu. Angeweza kuwapa tahadhari na kuwaonya wenye kiburi, na alikuwa amejiandaa kikamilifu kuwaimarisha ndugu zake. 3T 416.2

Mungu alikuongoza kupitia katika shida na majaribu ili uweze kuwa na uaminifu kamili na ujasiri katika Yeye na usifikirie zaidi uamuzi wako mwenyewe. Unaweza kustahimili shida zaidi kuliko mafanikio. Jicho la Yehova linaloona kila kitu liligundua ndani yako kuna takataka nyingi ambazo uliona kuwa ni dhahabu na ya thamani sana kuitupa. Nguvu ya adui juu yako wakati mwingine ilikuwa ya moja kwa moja na yenye nguvu sana. Udanganyifu wa umizimu ulikuwa umeshika imani yako, ukapotosha uamuzi wako, na kukanganya uzoefu wako. Mungu katika majaliwa Yake akakujaribu, kukutakasa, kama wana wa Lawi, ili uweze kumtolea sadaka kwa haki. 3T 416.3

Ubinafsi umechanganywa sana na kazi zako zote. Mapenzi yako lazima yapatanishwe na mapenzi ya Mungu, la sivyo utaangukia kwenye vishawishi vya kutisha. Niliona kwamba wakati unafanya bidii katika Mungu, ukitupilia ubinafsi mbali nawe, utagundua nguvu kutoka Kwake ambayo itakupa kuifikia mioyo. Malaika wa Mungu watafanya kazi na juhudi zako wakati wewe ukiwa mnyenyekevu na mdogo machoni pako mwenyewe. Lakini ukiwa unafikiria wewe unajua zaidi ya wale ambao Mungu amekuwa akiwaongoza kwa miaka mingi, na ambao amekuwa akiwafundisha Ukweli na ili wafae kupanua kazi Yake, utakuwa unajiinua mwenyewe na utaanguka katika majaribu. 3T 417.1

Unahitaji kukuza fadhili, wema na upole-huruma nyororo, upendo mwanana. Unahitaji kuwa mwenye huruma, sikitiko na adabu. Kazi yako inaashiria ukali sana na roho ya ukatili, ya kidikteta, yenye nguvu. Wewe hauangalii hisia za wengine, na unasababisha majaribu na mitanziko isiyo ya lazima. Upendo zaidi katika kazi yako, na huruma zaidi yenye fadhili, ingekupa daraja la kuifikia mioyo na ingeweza kuongoza roho kwa Kristo na ukweli. 3T 417.2

Unapendelea sana uhuru binafsi kila wakati. Hautambui kuwa uhuru ni jambo baya ikiwa linakupelekea katika kujitumaini sana mwenyewe na kujiamini katika uamuzi wako mwenyewe badala ya kuheshimu mashauri na kuanza kudadisi sana maamzi ya ndugu zako, haswa ya wale walioko kwenye ofisi ambazo Mungu amewateua kwa kuokoa watu Wake. Mungu amewekeza katika kanisa Lake mamlaka na nguvu maalum ambayo hakuna mtu anayeweza kuhesabiwa haki kwa

kupuuza na kudharau, kwani kwa kufanya hivyo mwanadamu hudharau sauti ya Mungu. 3T 417.3

Sio salama kwako kuamini mivuto na hisia. Imekuwa bahati mbaya sana kwako kuja chini ya nguvu ya upotovu huo wa kishetani, umizimu. Ugonjwa huu wa kifo umekufunika, na fikra zako na mishipa yako imekuwa chini ya udhibiti wa mashetani; na unapojiamini mwenyewe na haushikamani na ujasiri usioyumba kwa Mungu uko katika hatari haswa. Unaweza, na mara kwa mara hufanya, kujiacha wazi na kumwalika adui aingie, na anatawala mawazo na matendo yako, wakati unakuwa umedanganywa hakika na wewe mwenyewe unajidhania kwamba unampendeza Mungu au una kibali chake. 3T 418.1

Shetani amejaribu kukuzuia usiwe na imani na ndugu zako wa Marekani. Umewaangalia na harakati zao na uzoefu wao kwa mashaka, wakati wao ndio wangeweza kukusaidia wewe na wangekuwa baraka kwako. Itakuwa ni juhudi ya hali ya juu ya Shetani kukutenganisha na wale ambao ni kama mifereji ya nuru, ambaye kupitia Yeye Mungu amewasilisha mapenzi Yake na kupitia Yeye amefanya kazi katika kujenga na kupanua kazi Yake. Mitazamo yako na hisia zako na uzoefu wako ni finyu sana, na kazi zako zina hali hiyo hiyo. 3T 418.2

Ili kuwa baraka kwa watu wako, unahitaji kuboresha katika mambo mengi. Unapaswa kukuza adabu na kuonesha huruma safi kwa wote. Unapaswa kuwa na neema ya Mungu, ambayo ni upendo. Unashutumu sana na sio mvumilivu kama vile unavyopaswa kuwa ili kuongoa roho. Ungeweza kuwa na ushawishi mkubwa zaidi ikiwa ungekuwa kawaida tu na rahisi na ukasukumwa zaidi na Roho Mtakatifu. Hofu yako ya kuongozwa na watu ni kubwa mno. Mungu hutumia watu kama vyombo Vyake na atawatumia kwa muda mrefu kadiri ulimwengu utakavyodumu. 3T 418.3

Malaika walioanguka walikuwa na wasiwasi wa kuwa na uhuru kutoka kwa Mungu. Walikuwa wazuri sana, wenye utukufu sana, lakini walimtegemea Mungu kwa furaha yao na kwa nuru na akili waliyofurahia. Walianguka kutoka kwenye sehemu yao ya juu kwa kutotii. Kristo na kanisa Lake hawatenganishwi. Kupuuza au kudharau wale ambao Mungu amewateua kuongoza na kubeba majukumu yanayohusiana na kazi Yake na kwa maendeleo na kueneza Ukweli ni kukataa vyombo ambavyo Mungu ameviweka wakfu kwa ajili ya msaada, faraja na nguvu za watu Wake. Kupuuzia haya na kufikiria kwamba nuru yako haiwezi kupitia njia nyingine yoyote isipokuwa moja kwa moja kutoka kwa Mungu hukufanya wewe kujiweka mahali ambapo unaweza kudanganywa na kupinduliwa/kuondoshwa. 3T 418.4

Mungu amekuweka katika uhusiano na msaada Wake aliouoteua Yeye katika kanisa Lake ili upate kusaidiwa nao. Uhusiano wako wa zamani na umizimu hufanya hatari

yako kuwa kubwa kuliko vile ingekuwa, kwa sababu uamuzi wako, hekima, na upambanuzi wako umepotoshwa. Kwa wewe mwenyewe huwezi kusema au kupambanua mapepo/roho kila wakati; kwa sababu Shetani ni mjanja sana. Mungu amekuweka wewe katika uhusiano na kanisa Lake ili wakusaidie. 3T 419.1

Wakati mwingine wewe ni mtu unahusiana na watu urasmi [formal, rigid], baridi, na asiye na huruma. Lazima ukutane na watu mahali walipo, na usijiweke mbali sana juu yao na ukahitaji kupita kiasi kutoka kwao. Unahitaji kulainishwa na kutiishwa na Roho wa Mungu wakati unahubiri kwa watu. Unapaswa kujifunza kuhusu njia bora ya kufanya kazi ili kupata hitimisho linalotarajiwa. Kazi yako lazima ijawe na upendo wa Yesu uliojaza moyo wako, kulainisha maneno yako, kuumba hulka tabia yako, na kuinua nafsi yako. 3T 419.2

Mara kwa mara huwa unazungumza kwa muda mrefu sana wakati hauna ushawishi muhimu wa Roho wa mbinguni. Unawachosha wale wanaokusikia. Wengi hukosea katika kuhubiri kwao kwa kutosimama wakati shauku ingalipo. Wanaendelea kuongea tena na tena, hadi shauku iliyokuwa imeamshwa akilini mwa wasikilizaji inaondoka na watu wanakuwa wamechoshwa na maneno yasiyo na uzito maalum au hamasa/maslahi/kupendeza. Katisha/Simama kabla ya kufika hapo. Acha wakati unapoona hauna chochote cha umuhimu zaidi kukisema. Usiendelee na maneno makavu ambayo husisimua ubaguzi tu, na wala hayaulainishi moyo. Unahitaji kuunganishwa kabisa na Kristo ili kwamba maneno yako yayeyushe na kuchoma njia yao hadi katika moyo. Mazungumzo ya kawaida tu hayatoshi kwa wakati huu. Hoja ni nzuri, lakini kunaweza kuwa na hoja/mabishano mengi sana ila ni kidogo sana yahusuyo juu ya Roho na maisha ya Mungu. 3T 419.3

Bila nguvu maalum ya Mungu kufanya kazi na juhudi zako, roho yako kuwa imesalimishwa na kunyenyekezwa kwa Mungu, moyo wako kuwa umelainishwa, maneno yako yakitiririka kutoka kwa moyo wa upendo, kazi zako zitakuwa zitakupa uchovu mwenyewe na hazitaleta matokeo yenye baraka. Kuna pointi ambayo mhudumu wa Kristo anafikia, ambayo maarifa ya kibinadamu na ustadi havina nguvu. Tunapambana na makosa makubwa, na maovu ambayo hatuna uwezo wa kuyarekebisha au kuwaamsha watu waone na kuelewa, kwani hatuwezi kuubadilisha moyo. Hatuwezi kuhuisha roho kutambua ubaya wa dhambi na kuhisi hitaji la Mwokozi. Lakini ikiwa kazi yetu inabeba mhuri/mguso wa Roho wa Mungu, ikiwa kwa nguvu ya juu, nguvu ya Mungu inaongoza juhudi zetu za kupanda mbegu ya injili, hakika tutaona matunda ya kazi yetu kwa utukufu wa Mungu. Yeye peke yake Ndiye anayeweza kumwagilia mbegu iliyopandwa. 3T 419.4

Ndivyo na wewe, Ndugu A. Haupaswi kuingia kwa haraka sana na utarajie akili nyingi zilizotiwa giza. Lazima uchukue tumaini la unyenyekevu kwamba Mungu kwa na ukarimu, atasambaza ushawishi wa ajabu, na wa kuhuisha wa Roho Wake, ambaye kwa Yeye peke yake kazi yako haitakuwa bure katika Bwana. Unahitaji

kushikamana na Mungu kwa imani hai, kila wakati ukitambua hatari zako na udhaifu wako, na kutafuta kila wakati uwezo na nguvu ambayo ni Mungu peke Yake anaweza kutoa. Hata ujaribu kadri uwezavyo, wewe mwenyewe huwezi kufanya chochote. 3T 420.1

Unahitaji kujifunza, ili uwe na hekima ya kushughulika na akili. Unapaswa kuwa na huruma na wengine, ukifanya utofauti, wakati wengine unaweza kuwaokoa kwa hofu, ukiwanyangua kwenye moto. Baba yetu wa mbinguni mara nyingi hutuacha tukiwa na uhakika kuhusiana na juhudi zetu wenyewe. Tunapaswa kupanda kando ya maji yote, bila kujua ni kipi/yupi atafanikiwa, huyu au yule. Tunaweza kuchochea imani na nguvu zetu kutoka kwa Chanzo cha nguvu zetu, na kutegemea kwa kumtegemea Yeye kabisa. 3T 420.2

Ndugu A, unahitaji kufanya kazi kwa bidii kubwa kudhibiti ubinafsi na kukuza tabia kulingana na kanuni za Neno la Mungu. Unahitaji kujielimisha na kujizoeza ili uwe mchungaji aliye na mafanikio. Unahitaji kukuza tabia nzuri — fadhili, mchangamfu, mcheshi, mkarimu, mwenye huruma mwungwana, mwenye adabu, tabia ya kusikitikia wengine. Unapaswa kushinda tabia mbaya za kutowasiliana vizuri imani zenye ubaguzi, ufinyu wa mawazo, kutafuta makosa, na kutawala wengine, una hulka mbaya, na unakuwa na huzuni saa yote. Ikiwa umeunganishwa na kazi ya Mungu unahitaji kupambana na nafsi yako mwenyewe kwa nguvu na kuunda tabia yako kupatana na Mfano wa Mungu. 3T 420.3

Bila kuendelea kujitahidi mara kwa mara kwa sehemu yako, maendeleo fulani, chini ya ushawishi wa akili yenye ufisadi, yatatokea na kuzuia njia yako, ambayo ni kizuizi ambacho utapenda kuwapakazia/kuwasingizia wengine kuliko sababu yenyewe ilivyo kweli/kimsingi. Unahitaji nidhamu binafsi-Jinidhamishe. Uchamungu wetu haupaswi kuwa na ugwadu, ubaridi, na kuwa na huzuni na kujitenga na watu na mudi-mudi/moody; bali unaopendeza na kufundishika. Roho ya kukosoa na kuwahukumu wengine, ukiwafikiria uovu itafunga njia yako na kufunga ya watu dhidi yako. Ikiwa haumtegemei Mungu kwa unyenyekevu, mara nyingi utafunga njia yako kwa vizuizi na kushitaki wengine kwamba nao wamefanya hivi. 3T 421.1

Unahitaji kujilinda mwenyewe, kwamba haufundishi Ukweli au kutekeleza majukumu kwa roho ya ubaguzi, ya kuona mawazo yako tu ndiyo yanastahili, ambayo itasisimua chuki. Unahitaji kujifunza jinsi unavyoweza kujionesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtendakazi ambaye hahitaji kulaumiwa/kuaibika. Jiulize mwenyewe tabia yako ya asili ni ipi, Je, umekuwa na tabia gani. Hii inapaswa kuwa mada/somo lako, na pia la kila mhudumu wa Kristo, ili kuwa na uangalifu mkubwa ili kutokuonesha mazoea ya kutenda, au mielekeo ya akili na maadili, ambayo hautaki kuona ikionekana kati ya wale unaowaleta kwenye Ukweli. 3T 421.2

Wachungaji/Wahudumu wa Kristo wanatakiwa kuwa mifano kwa kundi la Mungu. Ushawishi wa mchungaji/mhudumu unaweza kufanya mengi juu ya kuunda tabia ya watu wake. Ikiwa mhudumu ni mvivu, ikiwa sio safi moyoni na maishani, na ikiwa ni mkali, mkosoaji, na mwenye kwa kutafuta makosa, ana ubinafsi, anajitegemea mwenyewe, na hana kujizuia, na kiasi,atakuwa na mambo kama haya yasiyofurahisha kwa kiwango kikubwa kuyaona na kuyashughulikia kwa watu wake, na ni kazi ngumu kuweka mambo sawa pale ambapo ushawishi mbaya umefanya mkanganyiko. Kile kinachoonekana kwa mchungaji/mhudumu wao kitafanya mabadiliko makubwa kwa kuzingatia ukuzaji wa wema/ya Kikristo kwa watu. Ikiwa maisha yake ni muunganiko wa ubora, wale ambao yeye huwaleta kwenye ujuzi wa Ukweli kupitia kazi Yake, kwa kiwango kikubwa, ikiwa wanampenda Mungu kweli, wataonesha mfano na ushawishi wake, kwani yeye ni mwakilishi wa Kristo. Kwa hivyo mchungaji/mhudumu anapaswa kuhisi jukumu lake kupamba Mafundisho ya imani ya Mungu Mwokozi wetu katika vitu vyote. 3T 421.3.

Juhudi kubwa kwa mhudumu wa injili lazima iwe ni kutoa talanta zote kwa ajili ya kuokoa roho; ndipo atafanikiwa. Nidhamu na hekima makini na uangalifu ni muhimu sana kwa kila anayeliitia Jina la Kristo; lakini kwa hali ya namna kubwa zaidi inahitajika kwa mhudumu wa injili, ambaye ni mwakilishi wa Kristo. Mwokozi wetu aliwavuta watu kwa usafi Wake na maadili ya juu, wakati upendo , upole na unyenyekevu Wake uliwatia moyo kwa shauku. Masikini na wanyenyekevu hawakuogopa kumkaribia; hata watoto wadogo walivutiwa Naye. Walipenda kupanda juu ya mapaja Yake na kubusu uso huo wa kuvutia uliokuwa makini katika kutafakari, wenye moyo mzuri, ukarimu na upendo. Upendo huu mwanana, na kujali wewe unauhitaji. Unapaswa kukuza upendo. Maneno ya huruma na matendo ya adabu, staha, uungwana na heshima kwa wengine hadhi/utu wako hata chembe moja, lakini utakufungulia mioyo mingi ambayo sasa imefungwa dhidi yako. 3T 422.1

Kristo alikuwa kile kila mchungaji/mhudumu anapaswa kujitahidi kuwa. Tunapaswa kujifunza kuiga tabia Yake na kuchanganya haki thabiti, usafi, uadilifu, upendo, na ukarimu bora. Sura ya kupendeza ambayo upendo unaoneshwa, na tabia nzuri, uungwana na adabu, itatenda zaidi, kando na juhudi za mimbari, kuliko kazi katika dawati/ofisi inavyoweza kufanya bila hizi. Inakuwa ni sisi kukuza sifa ya maamuzi ya watu wengine, wakati, kwa kiwango kikubwa au kidogo, tunawategemea kabisa. Tunapaswa kukuza adabu ya kweli ya Kikristo na huruma nyororo na kujali, hata kwa watu wenye mioyo yenye mikwaruzo, migumu zaidi ya kibinadamu. Yesu alikuja kutoka nyua safi za mbinguni kuokoa watu kama hao. Unaufunga moyo wako kwa urahisi sana kwa wengi ambao inaonekana hawana shauku na ujumbe unaobeba, lakini ambao bado ni raia wa neema nao ni wa thamani machoni pa Bwana. "Na mwenye hekima huvuta roho za watu." Paulo

alikuwa kila kitu kwa watu wote ikiwa kwa njia hiyo anaweza kuwaokoa wengine. Lazima uwe katika nafasi sawa. Lazima uiname kidogo kutoka kwenye uhuru wako binafsi. Unakosa unyenyekevu wa akili. Unahitaji ushawishi laini wa neema ya Mungu juu ya moyo wako, ili usikasirishe au kuudhi watu, bali uyeyushe mwenendo wako kwenye mioyo ya wanadamu, ingawaje mioyo hii inaweza kuathiriwa na na ubaguzi. 3T 422.2

Kazi ya Mungu inahitaji sana watu wenye juhudi, watu ambao wana bidii, ari, tumaini, imani, na ujasiri. Sio watu wenye mapenzi ya kibinafsi, au wale wasisitizao nia zao binafsi, ndio ambao wanaweza kukidhi mahitaji ya wakati huu, lakini wanaume walio dhati na bidii. Tunao wachungaji/wahudumu wengi ambao ni nyeti/dhaifu katika uzoefu, wamepungukiwa na neema za Kikristo, hawajajitoa wakfu na wanaweza kuvunjika moyo kwa urahisi; ambao wapo dhati na wenye bidii kutosheleza mapenzi yao wenyewe na wanasisitiza juhudi zao za kutimiza malengo yao ya ubinafsi. Watu kama hao hawatatimiza mahitaji ya wakati wa sasa. Tunahitaji watu walio macho daima, walio na kasi na walio dhati na utayari wakati wote katika siku hizi za mwisho, wale ambao daima wako makini. Watu wanatafutwa ambao ni waaminifu katika upendo wao kwa ile Kweli na wako tayari kufanya kazi kwa kujitolea ikiwa wanaweza kuendeleza kazi ya Mungu na kuokoa roho za thamani. Wanaume wanatafutwa katika kazi hii ambao hawatanung'unika au kulalamika wakati wa shida au majaribu, wakijua kwamba hii ni sehemu ya urithi ambao Yesu amewaachia. Wanapaswa kuwa tayari kwenda nje ya kambi na kupata aibu na kubeba mizigo kama askari wazuri wa Kristo. Watabeba msalaba wa Kristo bila malalamiko, bila manung'uniko au kuudhika, kupata wasiwasi, na watakuwa wavumilivu katika dhiki. 3T 423.1

Ukweli makini, wa kujaribu kwa siku hizi za mwisho umetolewa kwetu, na tunapaswa kuufanya uwe halisi. Ndugu A, unapaswa kuepuka kujifanya mwenyewe kuwa kigezo. Epuka, ninakuomba, kutumia radhi zako mwenyewe. Yote ambayo tunaweza kuteseka, na yote ambayo tunaweza kuitwa kuumia, kwa ajili ya Ukweli yataonekana kuwa madogo sana yakilinganishwa na kile Mwokozi wetu alivumilia kwa ajili yetu wenye dhambi. Haupaswi kutarajia kila wakati kuchukuliwa kuwa sahihi au kuwakilishwa kwa usahihi. Kristo anasema kwamba ulimwenguni tutapata dhiki, lakini katika Yeye tutakuwa na amani. 3T 423.2

Umesitawisha roho ya malumbano/kupigana/ugomvi. Wakati njia yako inaingiliwa, unajiweka haraka sana kwenye nafasi ya kujihami; na, ingawa unaweza kuwa kati ya ndugu zako ambao wanapenda Ukweli na wamejitolea maisha yao kwa ajili ya Mungu, utajihesabia haki mwenye, huku ukiwa unawakosoa na kuwa na wivu kwa maneno yao na kushuku nia zao, na hivyo kupoteza baraka kubwa ambayo ni fursa yako kupata kupitia uzoefu wa ndugu zako. 3T 423.3.

Mijadala Iepukwe [Discussion and Debates to be avoided]

Umependa midahalo ya Ukweli na umependa mijadala (kubishana kwenye debate); lakini mashindano haya yamekuwa kikwazo kwako kuunda tabia ya Kikristo yenye utulivu, kwani katika hii ndio kuna fursa ya kuonesha vinasaba haswa vya tabia ambazo unapaswa kuzishinda kama daima utangia mbinguni. Mijadala si nyakati zote itaepukwa. Katika mazingira ambayo kuna maovu mawili chaguo huwa ni lile ambalo ni nafuu, nalo ni mjadala. Lakini katika nyakati ambazo inaweza kuepukwa, na iwe hivyo, kwani matokeo yake huwa ni nadra sana kumheshimu Mungu. 3T 424.1

Watu wanaopenda kuona wapinzani wakipambana wanaweza kupiga mayowe/kelele wakati majadiliano yakiendelea. Wengine wenye shauku ya kusikia ushahidi wa pande zote mbili, wanaweza kuchochea mjadala wakiwa na makusudi yote ya uaminifu; lakini wakati wowote ambao mijadala inaweza kuepukwa, na iwe hivyo. Kwa ujumla huimarisha mapambano/ugomvi na kuudhofisha upendo ule halisi na huruma yenye kicho/takatifu ambayo inapaswa kuwa daima katika moyo wa mkristo ijapokuwa wanaweza kutofautiana katika maoni. 3T 424.2

Mijadala katika enzi hii ya ulimwengu sio ushahidi wa Kweli wa shauku ya dhati kwa upande wa watu ya kuchunguza Ukweli lakini huja kupitia kupenda mambo mapya na misisimko ambayo kwa ujumla huhudhuria mijadala. Mungu kwa kawaida hutukuzwa kwa udogo sana au Ukweli husonga mbele kwa nadra sana katika mapambano haya. Ukweli ni mzito sana, ni wa maana sana katika matokeo yake, kuufanya kuwa jambo dogo kwamba haijalishi unapokelewa au unakataliwa. Kuujadili Ukweli ili kutafuta kuwaonesha wapinzani ustadi/ujuzi wa mapambano daima ni sera duni, kwani hutenda lakini kidogo sana katika kuuendeleza Ukweli. 3T 424.3

Wapinzani wa Ukweli wataonesha ustadi wao wa kupotosha wapinzani wao. Wataufanya Ukweli mzito, Ukweli uliotakaswa somo la dhihaka/mizaha. Kwa ujumla watacheza na kudhihaki Kweli takatifu ya thamani na kuweka huo katika nuru ya uongo mbele ya watu kiasi kwamba akili zilizotiwa giza na upotovu na kuchafuliwa na dhambi hazitambui nia na shabaha za watu hawa wa kubuni, kwa hivyo kuficha na kupotosha Ukweli wa thamani na u. Kwa sababu ya watu wanaojihusisha nayo, kuna lakini mijadala michache ambayo inawezekana kufanyika katika kanuni sahihi. Msukumo au maneno makali hutolewa mara kwa mara na pande zote mbili, haiba au vitabia vya watu huendekezwa, mara nyingi pande zote mbili huingia kwenye kejeli, kushushua na mizaha ya kuonyesha uhodari wa kutumia maneno [witticism]. Upendo kwa roho hupotezwa na shauku kubwa ya ubwana yaani kutawala mambo huwepo, na kutaka kushinda. Ubaguzi wa kina na wenye uchungu, mara nyingi huwa ni matokeo ya majadiliano. 3T 424.4

Nimeona malaika wakihuzunishwa wakati vito vya thamani zaidi vya Ukweli vikiletwa mbele ya watu wasioweza kabisa kuelewa uthibitisho unaounga mkono Ukweli. Uwepo wao wote upo vitani dhidi ya kanuni za Ukweli; asili zao zimekuwa na uadui na huo. Lengo lao katika majadiliano halikuwa kwamba wapate uthibitisho wa Ukweli wenyewe au kwamba watu wapate uthibitisho wa Ukweli wenyewe au kwamba watu wapate ufahamu wa haki wa msimamo wetu wa Kweli, bali kwamba watu wapate kuchanganya ufahamu huo kwa kuuweka Ukweli katika nuru potovu mbele ya watu. Kuna watu ambao wamejielimisha kama wapiganaji/wapambanaji. Ni sera yao kupotosha wapinzani wao na kufunika hoja zilizo wazi kwa mijadala isiyo ya uaminifu. Wamejizatiti kutumia nguvu walizopewa na Mungu katika kufanya kazi hii isiyo ya uaminifu, kwani hakuna kitu katika mioyo yao cha uaminifu kinachopatana na kanuni takatifu za Ukweli. Wanashika hoja zozote wanazoweza kupata za kuwaangusha watetezi wa Ukweli, wakati wao wenyewe hawaamini mambo wanayohimiza dhidi yao. Wanajiinua katika nafasi zao walizochagua, bila kujali haki na Ukweli. Hawazingatii kwamba kabla yao kuna hukumu na kwamba Ushindi uliopatikana vibaya pamoja na matokeo yake yote mabaya, yataonekana katika tabia yake halisi. Makosa katika sera zake zote za ulaghai ni mizunguko na mipindano na kugeuka ili kubadilidsha Ukweli kuwa uongo ndipo itaonekana katika ulemavu wake wote. Hakuna ushindi utakao simama katika siku ya Mungu, isipokuwa Ukweli ulio safi, uliochaguliwa, ulioinuliwa na Ukweli takatifu utashinda mbele ya utukufu wa Mungu. 3T 425.1

Malaika wanalia kuona Ukweli wa thamani wenye asili ya mbinguni unapotupwa mbele ya nguruwe, ili waukamate na kukanyagwa na matope na uchafu. Msitupe lulu yenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao tena kuwararua" haya ni Maneno ya mkombozi wa ulimwengu 3T 425.2

Watumishi wa Mungu wasihesabu fursa za kujishughulisha na mijadala kwamba ndiyo upendeleo mkubwa. Vipengele/Pointi zote za imani yetu zisibebwe na kuwasilishwa mbele ya umati watu wenye ubaguzi. Yesu alizungumza mbele ya mafarisayo na masadukayo kwa mafumbo, akificha uwazi wa Ukweli chini ya ishara, alama, na takwimu kwa sababu wangeutumia vibaya Ukweli uliwasilishwa mbele yao; lakini kwa wanafunzi wake alisema waziwazi. Tunapaswa kujifunza kutoka kwa njia za Kristo na kuwa makini tusikate masikio ya watu kwa kuwasilisha Ukweli, ambao bado haujafafanuliwa vya kutosha, na hawako tayari kuupokea.3T 426.1

Kweli ambazo tunazishikilia kwa pamoja zinapaswa kuzingatiwa kwanza na ujasiri wa wasikilizaji upatikane; kisha kama watu wanavyoweza kuletwa tunaweza kusonga mbele polepole na jambo lilowasilishwa. Busara kubwa inatakiwa kuwasilisha Ukweli usio maarufu kwa wengi mbele ya watu wenye ubaguzi kwa tahadhari zaidi ili kupata njia ya kuifikia mioyo. Mijadala huweka mbele ya watu,

ambao hawajaangaziwa kuhusina na msimamo wetu na ambao ni wajinga kuhusiana na Kweli za Biblia, seti ya hoja zilizoinuka kwa ustadi na kupangwa kwa uangalifu ili kufunika mambo yaliyo wazi ya Ukweli. Baadhi ya watu wamefanya biashara yao kuwa kufunika maelezo ya wazi ya Kweli katika Neno la Mungu kwa nadharia zao potofu, ambazo wanazifanya kuwa sahihi kwa wale ambao hawajazifanyia uchunguzi wao wenyewe. 3T 426.2

Mawakala wa Shetani ni vigumu kupatana nao na ni vigumu kuwavumilia, bali utulivu, na kujitawala nafsi ni sifa ambao kila mhudumu wa Kristo lazima aikuze. Wapambanaji wa Ukweli wamejielimisha kwa vita vya kisomi. Wamejitayarisha kuwasilisha kwa ujanja wa udanganyifu na madai kuwa ni Neno la Mungu. Wanazichanganya akili zisizo na shaka na kuweka Ukweli katika giza wakati hekaya zenye kuvutia zinawasilishwa mbele ya watu mahali pa Kweli safi za Biblia. 3T 426.3

Wengi huchagua giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Lakini kuwa wale ambao kama Ukweli ungewasilishwa kwa njia tofauti, katika mazingira tofauti, wakipewa fursa ya haki ya kupima hoja wao wenyewe na kulinganisha Andiko kwa Andiko wangechangamshwa na uwazi wake na wangeuzingatia na kuushikilia. 3T 426.4

Imekuwa jambo la kukosa busara sana kwa wachungaji wetu kuchapa na kutangaza kwa ulimwengu ule ujanja na udanganyifu wa makosa, unaobuniwa na watu ili kufunika na kufanya Ukweli safi wa Yehova usitoe matokeo. Watu hawa wajanja wanaovizia kwa hila na walaghai na ujanja ili kuwahadaa wasio na tahadhari wanatoa nguvu zao za akili kupotosha Neno la Mungu. Wanadamu wasio na uzoefu na wasioshuku wanadanganyika kwa uharibifu wao. Imekuwa ni makosa sana kuzichapisha hoja zote ambazo wapinzani hupigana na Ukweli wa Mungu, kwani kwa kufanya hivyo akili za kila tabaka huja na hoja ambazo wengi wao hawakuzifikiria. Lazima mtu mmoja atoe hesabu kwa ujemedari huu usio wa busara. Mabishano dhidi ya Kweli takatifu, yenye hila katika uvutano, huathiri akili ambayo haijafahamiswa vizuri kuhusiana na nguvu ya Ukweli. Hisia za kimaadili za jamii kwa ujumla zimefanywa butu na mazoea ya dhambi. Ubinafsi, kukosa uaminifu, na dhambi za kila aina zinazotatawala katika kizazi hiki kilichozorota kimaadili, na kuzima hisia kwa mambo ya milele hivyo kwamba Ukweli wa Mungu hautambuliwi. Kwa kuyapa nguvu ya umma makosa ya hoja ya wapinzani wetu, Ukweli na makosa huwekwa katika hali sawa katika akili zao, wakati, kama Ukweli ungewekwa mbele yao katika usafi wake kwa muda wa kutosha kuona na kutambua utakatifu wake na umuhimu, wangeshawishiwa na hoja zake nzito kwa upande wake na wangekuwa wamejianda kukabiliana na hoja zinazochochewa na wapinzani. 3T 427.1

Wale wanaotafuta kujua Ukweli na kufahamu mapenzi ya Mungu, walio waaminifu kwa nuru na wenye bidii katika kutenda majukumu yao ya kila siku, kwa hakika watajua Mafundisho ya imani, kwani wataongozwa katika Kweli yote. Mungu haahidi, kwa matendo na majaliwa Yake ya Ukuu, kuwaleta watu kwenye Ukweli bila kikwazo, wakati hawautafuti Ukweli na hawana shauku ya kuujua Ukweli. Watu wana nguvu ya kuzima roho wa Mungu; nguvu ya maamuzi imeachwa kwao. Wameruhusiwa uhuru wa matendo. Wanaweza kuwa watii kwa Jina na rehema ya Mkombozi au wanaweza kutokutii na kupokea matokeo. Mwanadamu anawajibika kwa kuupokea au kutoupokea Ukweli mtakatifu wa milele. Roho wa Mungu huendelea kusadikisha wakati wote, na watu wanafanya maamuzi ya kuufuata au kuwa dhidi ya Ukweli. Msimamo, maneno, matendo ya wahudumu wa Kristo yanaweza kuleta msawaziko kwa roho kuwa kwa Ukweli au kuwa dhidi ya Ukweli. Ni muhimu kiasi gani kwamba kila tendo la maisha liwe hivi kwamba halihitaji kutubi. Hususani ni muhimu miongoni mwa mabalozi wa Kristo, wanaotenda mahali pa Kristo. 3T 427.3

Mamlaka Ya Kanisa.

Mkombozi wa ulimwengu amewekeza nguvu na uwezo mkubwa kwa kanisa Lake. Anataka kanuni zitumike katika masuala ya majaribu ya washiriki wake. Baada ya kuwa ametoa mwelekeo wa wazi wa njia inayopaswa kufuatwa anasema “amini nawaambieni, yoyote mtakayofunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote {katika nidhamu ya kanisa} mtakayofungulia duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.” Hivyo hata mamlaka ya mbinguni huidhinisha nidhamu ya kanisa kwa kuzingatia washiriki wake, kama kanuni za Biblia zimefuatwa. 3T 428.1

The word of God does not give license for one man to set up his judgment in opposition to the judgment of the church, neither is he allowed to urge his opinions against the opinions of the church. If there were no church discipline and government, the church would go to fragments; it could not hold together as a body. There have ever been individuals of independent minds who have claimed that they were right, that God had especially taught, impressed, and led them. Each has a theory of his own, views peculiar to himself, and each claims that his views are in accordance with the word of God. Each one has a different theory and faith, yet each claims special light from God. These draw away from the body, and each one is a separate church of himself. All these cannot be right, yet they all claim to be led of the Lord. The word of Inspiration is not Yea and Nay, but Yea and Amen in Christ Jesus.

Our Saviour follows His lessons of instruction with a promise that if two or t

Neno la Mungu halitoi kibali/leseni kwa mtu mmoja kufanya hukumu yake kwa kupinga hukumu ya kanisa au kwenda kinyume, wala kuchochea maoni yake dhidi ya maoni ya kanisa. Kama kusingekuwa na nidhamu ya kanisa na serikali yake, kanisa lingesambaratika vipande vipande; lisingeshikamana kama mwili wa Kristo. Daima kumekuwa na watu binafsi wenye akili za kujitegemea wanaosisitiza kwamba wako sahihi, kwamba Mungu amewafundisha kwa njia maalumu, amewagusa moyo kwa jambo fulani na amewaongoza. Kila mmoja ana nadharia

yake mwenyewe, mitazamo ambayo ni ya kipekee kwake mwenyewe, na kila mmoja anasisitiza kuwa maoni yake yanapatana na Neno la Mungu. Kila mmoja ana nadharia na imani tofauti, na bado kila mmoja anadai nuru yake hiyo tofauti na ya kanisa, hutoka kwa Mungu. Haiwezekani kwa hawa wote kuwa sahihi, hata hivyo wote wanadai kuongozwa na Bwana. Watu hawa hujitenga na mwili wa Kristo, na kila moja hujifanya kuwa kanisa la pekee yake mwenyewe. Neno la Uvuvio si "Ndiyo" na "Hapana," bali ni "Ndiyo" na "Amina" katika Kristo Yesu. 3T 428.2

Mwokozi wetu hufuata masomo Yake ya mafundisho yenye ahadi kwamba ikiwa wawili au watatu wataungana katika kuomba chochote kwa Mungu watapewa. Kristo hapa anaonesha kuwa lazima kuwa na umoja na wengine, hata katika shauku yetu ya lengo fulani. Umuhimu mkubwa umeshikamanishwa na maombi ya pamoja, umoja wa kusudi [united prayer]. Mungu husikia maombi ya mtu mmoja-mmoja, lakini katika muktadha huu Yesu alikuwa anatoa masomo muhimu ambayo yangebeba maana ya pekee kwa kanisa lake lilopangwa upya duniani. Lazima pawepo mapatano katika mambo wanayoyatamani na kuyaombea. Sio tu mawazo au utendaji wa akili moja, inayoweza kudanganywa, lakini ombi hilo linapaswa kuwa nia ya dhati ya akili ya watu kadhaa tofauti, ikijikia kwenye pointi moja [wakiafikiana]. 3T 429.1

Katika uongofu wa kushangaza wa Paulo tunaona uwezo wa kimuujiza wa Mungu. Mwangaza ulio zaidi ya utukufu wa jua la mchana uliangaza kumzunguka pande zote. Yesu ambae Jina Lake kati ya wengine wote alilichukia na kulidharau zaidi, alijidhihirisha kwa Paulo kwa kusudi la kukamata kazi yake ya kiwazimu lakini mwaminifu, ili aweze kukifanya chombo hiki kisicho na matumaini kuwa chombo kilichochaguliwa kupeleka injili kwa watu wa mataifa. Kwa dhamiri yake alikuwa amefanya mambo mengi kinyume na Jina la Yesu wa Nazareti, katika usongo wake alikuwa mtesi mstahimilivu, mwenye bidii wa kanisa la Kristo. Usadikisho wake wa daraka lake la kutokomeza fundisho hili lenye kutisha, ambalo lilikuwa limeenea kila mahali, kwamba Yesu alikuwa Mkuu wa Uzima ulikuwa wa kina na wenye nguvu. 3T 429.2

Paulo aliamini hakika kwamba imani katika Yesu ilibatilisha sheria ya Mungu, huduma ya kidini ya matoleo ya dhabihu, na desturi ya tohara, ambayo katika enzi zote zilizopita ilipokea kibali kamili cha Mungu. Lakini ufunuo wa kimiujiza wa Kristo ulileta nuru katika vyumba vyenye giza vya akili yake. Yesu wa Nazareti ambae amejipanga dhidi Yake ni Kweli Mkombozi wa ulimwengu. 3T 429.3

Paulo aliona bidii yake potofu na akapaza sauti: “Bwana Je, wataka nifanye nini?” Yesu hakumwambia hapo hapo kama angeweza kufanya kazi aliyokuwa amemkabidhi. Paulo lazima apokee mafundisho katika imani ya Kikristo na kusonga kwa ufahamu. Kristo anamtuma kwa wanafunzi walewale ambao alikuwa

akiwatesa sana, ili kujifunza kutoka kwao. Nuru ya mwangaza wa mbinguni ilikuwa imeondoa uwezo wa kuona wa Paulo; lakini Yesu Mponyaji mkuu wa vipofu, harudishi kuoana kwake. Anajibu swali la Paulo kwa Maneno haya: “Ondoka uende mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kufanya” Yesu angeweza tu kumponya Paulo upofu wake, pia angeweza kumsamehe dhambi zake na kumwambia wajibu wake kwa kuweka alama katika njia yake ya wakati ujao. Kutoka kwa Kristo nguvu zote na rehema zilipaswa kutiririka; lakini hakumpa Paulo uzoefu, katika uongofu wake kwa Ukweli, huru na kanisa Lake lililoundwa hivi karibuni duniani. 3T 429.4

Nuru ya ajabu aliyopewa Paulo wakati huo ilimstaajabisha na kumfadhaisha. Alitiishwa kabisa. Sehemu hii ya kazi ambayo mwanadamu asingeweza kumfanyia Paulo, lakini bado kulikuwa na kazi ambayo bado watumishi wa Kristo wangeweza kuifanya. Yesu anamwelekeza kwa mawakala Wake katika kanisa kwa ajili ya ujuzi zaidi wa wajibu. Hivyo yeye hutoa mamlaka na idhini kwa kanisa Lake lililopangwa. Kristo alikuwa amefanya kazi ya ufunuo na kusadikisha, sasa Paulo alikuwa katika hali ya kujifunza juu ya wale ambao Mungu alikuwa amewaweka kufundisha Ukweli. Kristo anamwelekeza Paulo kwa watumishi Wake wateule, hivyo kumweka katika uhusiano na kanisa Lake. 3T 430.1

Watu wale wale ambao Paulo alikuwa akitaka kuwaangamiza, walipaswa kuwa walimu wake katika dini ile ile ambayo Paulo alikuwa ameidharau kuitesa. Zilipita siku tatu bila chakula wa kuona, akienda kwa watu ambao, kwa bidii yake ya upofu, alikuwa akikusudia kuwaangamiza. Hapa Yesu anamweka Paulo katika mahusiano na wawakilishi Wake duniani. Bwana akampa Anania maono ya kwenda kwenye nyumba moja huko Dameski na kumwita Sauli wa Tarso; “kwa maana tazama anaomba” 3T 430.2

Sauli alipoagizwa Dameski, wale watu waliofuatana naye walimsindikiza ili wamsaidie kuwaleta wanafunzi wa Yesu kule Yerusalemu wakiwa wamefungwa, ili wahukumiwe na kuuawa. Sauli alikaa pamoja na Yuda huko Damasko, akitumia wakati wake kwa kufunga na kuomba. Hapa imani ya Sauli ilijaribiwa. Siku tatu alikuwa katika giza la akili kwa sababu ya kile alichotakiwa kufanya, na kwa siku tatu alikuwa haoni. Alikuwa ameagizwa aende Dameski kwa maana huko alipaswa kuambiwa kile alichopaswa kufanya. Hana uhakika naye anamlilia Mungu kwa dhati na bidii. Malaika anatumwa kwa Anania, akimwelekeza aende kwenye nyumba fulani ambako Sauli anaomba ili afundishwe jambo analopaswa kufanya baada ya hapo. Kiburi cha Sauli kimetoweka. Muda mfupi kabla ya hapo alikuwa na roho ya kujiamini, akifikiri kuwa alikuwa akijishughulisha na kazi nzuri ambayo anapaswa kupokea thawabu kwayo; lakini sasa yote yamebadilika. Ameinamishwa chini na kunyenyekea mavumbini kwa toba na aibu, na dua zake ni nyingi sana za kusamehewa. Bwana akamwambia Anania kupitia malaika Wake: Tazama, anaomba. Malaika alimfunulia mtumishi wa Mungu kwamba amemfunulia Sauli katika maono mtu anayeitwa Anania akiingia na kuweka mkono wake juu yake ili

apate kuona. Anania hawezi ni kama hawezi kuamini Maneno ya malaika, na anarudia yale ambayo amesikia juu ya mateso makali ya Sauli kwa watakatifu huko Yerusalemu. Lakini amri kwa Anania ni ya lazima: “nenda zako kwa maana yeye ni chombo kiteule Kwangu, alichukue Jina Langu mbele ya mataifa na wafalme na wana wa Israeli.” 3T 430.3

Anania alitii Maneno ya malaika. Aliweka mikono yake juu ya mtu ambae hivi karibuni alikuwa na chuki kubwa zaidi, akipumua vitisho dhidi ya wote walioamini Jina la Kristo. Anania kamwambia Sauli: “Ndugu Sauli, Bwana Yesu, Yeye aliyekutokea katika njia uliyoiijia, amenituma ili upate kuona tena, na kujazwa Roho mtakatifu. Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona mara, akasimama akabatizwa. 3T 431:1

Yesu angeweza kuwa amemfanyia Paulo kazi hii yote moja kwa moja lakini huu haukuwa mpango Wake. Paulo alikuwa na jambo la kufanya katika mstari wa kuungama kwa watu ambao alikuwa alikuwa amewaza mapema uharibifu wao, na Mungu alikuwa nakazi ya kuwajibika kwa watu ambao alikuwa amewaweka kutenda badala yake. Paulo alipaswa kuchukua hatua hizo muhimu katika uongofu. Alitakiwa kuungana na watu walewale aliowatesa kwa ajili ya dini yao. Kristo hapa anawapa watu Wake wote mfano wa namna ya kufanya kazi Yake kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Mwana wa Mungu alijitambulisha mwenyewe na ofisi na mamlaka ya kanisa lililoundwa [organized church]. Baraka Zake zilipaswa kuja kupitia mashirika au mawakala ambao amewaweka, hivyo kumuunganisha mwanadamu na njia ambayo kwayo Baraka Zake huja. Umakini wa dhamiri yake Paulo katika kazi yake ya kuwatesa watakatifu hakumfanyi awe na hatia wakati ujuzi wa kazi yake ya kikatili unapotiwa ndani ya moyo wake na Roho wa Mungu. Anapaswa kuwa mjifunzaji kwa wanafunzi wa Yesu. 3T 431.2

> Anajifunza kwamba Yesu ambae katika upofu wake alimwona kuwa mdanganyifu, kwa hakikaNdiye mwanzilishi na msingi wa dini zote za wateule wa Mungu tangu siku za Adamu, na mkamilishaji wa imani, sasa ni wazi sana kwa maono yake yenye nuru. Alimuona Kristo kuwa mtetezi wa Ukweli, mtimizaji wa unabii wote. Kristo alikuwa amechuliwa kuwa amebatilisha sheria ya Mungu; lakini maono yake ya kiroho yalipoguswa na kidole cha Mungu, alijifunza kutoka kwa wanafunzi kwamba Kristo alikuwa mwanzilishi na msingi wa mfumo mzima wa dhabihu wa Kiyahudi, na kwamba Kristo halisi ilikutana na mfano [type met antitype], na kwamba Kristo alikuja katika ulimwengu kwa kusudi dhahiri ya kuhalalisha sheria ya Baba Yake 3T 432.1 [Hitaji la Daima wa Upatanisho na Maombezi ya Kristo.—Kristo alikuwa msingi wa mfumo mzima wa dini ya Kiyahudi na uelewa wote wa wokovu ulikita Kwake Masihi [The Messiah was the Foundation of whole Jewish economy]. Katika huduma ya ukuhani wa Kiyahudi tunakumbushwa daima juu ya dhabihu na maombezi ya Kristo. Wote wanaokuja kwa Kristo leo wanapaswa kukumbuka kwamba sifa na stahiki Yake ni uvumba unaochanganyikana na maombi ya wale wanaotubu dhambi zao na kupokea msamaha, rehema na neema. Hitaji letu la maombezi ya Kristo ni ya kudumu. Siku baada ya siku, asubuhi na jioni, moyo mnyenyekevu unahitaji kutoa maombi ambayo

yatarudishiwa majibu ya neema na amani na furaha. “Basi, kwa njia Yake Yeye, na tumtolee Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo Jina Lake. Lakini msisahau kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo zimpendezazo Mungu.” (MS 14, 1901). **{6BC 1078.6}**

(Ephesians 5:2; Hebrews 7:25-27; 9:23-26; 13:15; Revelation 8:3, 4.) Constant Need of Christ's Intercession—Christ was the foundation of the whole Jewish economy. In the service of the Jewish priesthood we are continually reminded of the sacrifice and intercession of Christ. All who come to Christ today are to remember that His merit is the incense that mingles with the prayers of those who repent of their sins and receive pardon and mercy and grace. Our need of Christ's intercession is constant. Day by day, morning and evening, the humble heart needs to offer up prayers to which will be returned answers of grace and peace and joy. “By him therefore let us offer the sacrifice of praise to God continually, that is, the fruit of our lips giving thanks to his name. But to do good and to communicate forget not: for with such sacrifice God is well pleased” (Manuscript 14, 1901).

.

3T 432.1

Katika mwanga wa sheria Paulo anajiona mwenye dhambi. Sheria hiyohiyo ambayo alidahani amekuwa akiitunza kwa bidii na usongo sana anaona amekuwa akiivunja. Anatubu na kuifia dhambi, anakuwa mtiifu kwa madai ya sheria ya Mungu, na ana imani katika Kristo kama Mwokozi wake, anabatizwa na kumhubiri Yesu kwa dhati, usongo na kwa juhudi kama vile alivyo mhukumu hapo awali. Katika wongofu wa Paulo tumepewa kanuni mhimu ambazo tunapaswa kukumbuka kila wakati. Mkombozi wa ulimwengu hauidhinishi uzoefu na kujishughulisha katika mambo ya kidini bila kutegemea kanisa Lake lililopangwa na kutambuliwa, ambapo Yeye ana kanisa 3T 432.2

Wengi wanawaza kwamba wanawajibika kwa Kristo peke yake kwa ajili ya nuru na uzoefu wao, bila kutegemea wafuasi Wake wanaotambulika ulimwenguni. Lakini hii inashutumiwa na Yesu katika mafundisho Yake na katika mifano, Ukweli, ambao Yeye ametoa kwa ajili ya mafundisho yetu. Huyu alikuwa ndiye Paulo ambae Kristo angemfaa kwa ajili ya kazi ya maana sana, yule ambae alipaswa kuwa chombo kilichochaguliwa Kwake, akiletwa moja kwa moja katika uwepo wa Kristo; Na bado Yeye hamfundishi masomo ya Ukweli. Anasimisha safari na mwenendo wake na kumtia hatiani; na anapouliza “unanitaka nifanye nini?” Mwokozi hamwambii moja kwa moja, bali anamuweka katika uhusiano na kanisa Lake. Watakuambia unachopaswa kufanya. Yesu ni Rafiki wa mwenye dhambi, moyo wake huwa wazi kwa mwanadamu, daima huguswa na ole wa mwanadamu; ana uwezo wote mbinguni na duniani; lakini Yeye Anaheshimu njia mabazo ameziweka kwa ajili ya na wokovu wa wanadamu. Anamwelekeza Sauli kwa kanisa, hivyo akikiri uwezo ambao amewekeza ndani yake kama njia ya nuru kwa ulimwengu. Ni mwili wa Kristo aliopangwa duniani; na heshima inahitajika kutolewa kwa maagizo yake. Kwa habari ya Sauli Anania anamwakilisha Kristo, na pia anawakilisha wahudumu wa Kristo duniani ambao wamekwa rasmi kutenda badala ya kristo. 3T 433.1.

Sauli alikuwa mwalimu msomi, mtu aliyeelimika sana katika Israel; lakini akiwa chini ya ushauwishi wa makosa ya upofu na ubaguzi, Kristo anajidhihirisha Mwenyewe kwake, na kisha kumweka katika mawasiliano na kanisa Lake, ambao ni nuru ya ulimwengu. Wanapaswa kumfundisha msemaji huyu alieelimika,

maarufu, katika dini ya Kikristo. Badala ya Kristo, ni Anania ndiye anagusa macho yake ili yapate kuona; badala Kristo anaweka mikono Yake juu yake, anaomba katika Jina ka Kristo, na Sauli anapokea Roho mtakatifu. Yote yanafanyika kwa Jina na mamlaka ya Kristo. Kristo Ndiye chemichemi. Kanisa ni mkondo wa mawasiliano. Wale wanaojivunia uhuru wa kibinafsi wanahitaji kuletwa katika uhusiano wa karibu zaidi na Kristo kwa kuunganishwa na kanisa lake duniani. 3T 432.2

Ndugu A, Mungu anakupenda na anatamani kukuokoa na kukuleta katika utaratibu wa kufanya kazi. Iwapo utakuwa mnyenyekevu na mwenye kufundishika, na kufinyangwa na Roho Wake, Yeye atakuwa nguvu yako, haki yako, haki yako, na thawabu yako kuu sana. Unaweza kutimiza mengi kwa ajili ya ndugu zako ikiwa utajificha ndani ya Mungu na kuruhusu roho Wake kulainisha roho yako. Una tabaka gumu la kulifikia. Wamejawa na chuki kali na ubaguzi, ila sio zaidi ya Sauli. Mungu anaweza kufanya kazi kwa nguvu kwa ajili ya ndugu zako ikiwa hautajiruhusu kuingia katika njia na kuifunga njia yako mwenyewe. Acha upendo unaoyeyusha, huruma na upole ukae ukae ndani ya moyo wako unapofanya kazi. Unaweza kubomoa kuta za chuma za ubaguzi ikiwa tu utashikamana na Kristo na uko tayari kushauriwa na ndugu zako wenye uzoefu zaidi. 3T 434.1

Wewe kama mtumishi wa Mungu usikatishwe tamaa kirahisi au upinzani mgumu zaidi. Ondoka si kwa jina lako mwenyewe, bali katika uweza na nguvu za Mungu wa Israeli. Vumilia ugumu kama askari mwema wa msalaba wa Kristo. Yesu alistahimili mabishano ya wenye dhambi dhidi Yake. Yatafakari maisha ya Kristo na ujipe moyo, na songa mbele katika imani, ujasiri na tumaini. 3T 434.2

SURA YA 36

UMOJA NDANI YA KANISA

Katika maono yangu ya mwisho nilioneshwa utangulizi wa Ukweli, na muendelezo maendeleo wa kusudi la Mungu, katika ya pwani ya Pasifiki. Niliona kuwa kazi nzuri ilikuwa imefanywa kwa watu wengi huko California, lakini walikuwepo wengi ambao waliukiri Ukweli ila hawakuwa tayari kuichukua kazi ya Mungu na kuifanya kwa wakati sahihi na kutoka kwenye mwongozo wa awali wa Mungu kama unavyoonesha wajibu wao. Kazi kubwa inaweza kufanywa katika pwani hii ili kuongoa roho nyingi kwenye Kweli Yake endapo kutakuwa na umoja. 3T 434.3

Ikiwa wale wote wenye ushawishi wangeuona ulazima wa ushirikiano na wangetafuta kulijibu ombi la Kristo, ya kwamba wawe wamoja kama Yeye alivyo na Umoja na Baba, kusudi la Ukweli wa sasa lingekuwa na nguvu katika pwani hii. Lakini watu wa Mungu wamelala, na hawayaoni mahitaji halisi ya wakati huu. Hawahisi umuhimu wa kujikita katika kufanya kazi kwa umoja. Shetani anatafuta kugawanya imani na mioyo ya watu wa Mungu kila siku. Anajua vizuri ya kuwa umoja ndiyo nguvu yao, na utengano ni udhaifu wao. Ni muhimu wafuasi wote wa Kristo wazitambue mbinu zote za Shetani na kwa ushirikiano mkuu wakabiliane na mashambulizi yake na kumshinda. Wanahitaji kufanya juhudi endelevu na kuhimizana kwa pamoja hata kama ikiwa ni kwa kujitoa mhanga wenyewe. 3T 434.4

Watu wa Mungu, walio na hulka na mifumo tofauti, wameletwa pamoja ndani ya kanisa. Ukweli wa Mungu, uliopokelewa mioyoni mwao, utafanya kazi yake ya kusafisha, kuinua, na kutakasa maisha na kuyashinda maoni ya kipekee na, ubaguzi na upendeleo wa kila mmoja. Wote wanapaswa kufanya kazi kwa ukaribu zaidi. Wote wanaompenda Mungu na kuzishika amri Zake katika Kweli watakuwa na ushawishi kwa wasioamini na wataongoa roho kwa ajili ya Kristo, ili kuleta mrindimo wa nyimbo za furaha na ushindi mbele ya kiti cha enzi kikubwa cheupe. Ubinafsi utashindwa, na upendo uliofurika kwa Kristo utadhihirishwa katika hatia wanayoihisi ya kuongoa roho kwa ajili ya Yeye aliyekufa kwa ajili yetu. 3T 435.1

Nilioneshwa familia nyingi ambazo haziishi katika misingi ya Kristo kama ambavyo Yeye angetaka; wanayo kazi ya kufanya katika nyumba zao kabla ya kupiga hatua katika maisha ya Ukristo/utauwa/Kiungu. Nilioneshwa kisa cha Ndugu B na kuoneshwa hapo awali alipoukubali Ukweli. Wakati ule Ukweli ulikuwa na ushawishi uliobadili maisha yake. Ubinafsi ulipotea na aliupatia Ukweli kipaumbele zaidi. Alitafuta kuonesha imani yake kwa matendo yake, na masilahi yake binafsi yalifanywa kuwa ya pili. Aliipenda kazi ya Bwana na kwa furaha alikuza maslahi ya

kusudi Lake Mungu; Bwana alizikubali juhudi zake za kumtumikia, na mkono wa Bwana ulimbariki. 3T 435.2
Nilioneshwa kuwa Ndugu B alimchukiza Mungu na kujiletea giza kuu wakati alipoamua kuweka maamuzi yake yaliyo kinyume na yale ya ndugu zake kuhusu njia ya Kweli ya utunzaji wa Sabato. Masilahi ya kaka B yalikuwa hatarini, na alikataa kulizingatia swali lililokuwa na majibu sahihi. Asingeweza kuchukua maamuzi hayo baada ya kurudi kutoka Mashariki, endapo angekuwa katika nuru. Kisha nilioneshwa hatua nyingine katika historia yake na kumwona akisafiri. Akiwa katikati ya watu wasioamini hakuiruhusu nuru yake iangaze mbele ya watu ili wao kwa kuyaona matendo yake mema wamtukuze Baba yetu aliye mbinguni. Alimsahau Mungu na wajibu wake wa kumwakilisha Mwokozi Wake kwa usahihi mahali popote na kwa nyakati zote na matukio yote. 3T 435.3

Ndugu B ni dhaifu sana katika nyanja kadha wa kadha; anapenda sifa na majivuno; anapenda anasa/starehe, kubembelezwa, kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo, na kuheshimiwa. Alijiinua na kuongea sana huku akiwa na maombi ya nadra, na Mungu akamwacha katika udhaifu wake; kwa kuwa hakuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Katika safari ile alikuwa na fursa ya kufanya mengi mazuri, lakini hakutambua kuwa alitakiwa kuwajibika kwa Mungu kwa talanta zake na ya kuwa kama wakili wa Mungu ataulizwa kutoa hesabu kwamba alitumia uwezo wake kujifurahisha mwenyewe au kumtukuza Mungu. Endapo Ndugu B angehisi nguvu ya upendo wa Kristo moyoni mwake, angeihisi hamu ya wokovu wa wale ambao alikutana nao, ya kwamba angezungumza nao maneno ambayo yangewafanya wafikirie kuhusu masilahi yao ya milele. 3T 436.1

Alikuwa na nafasi ya kupanda mbegu ya Ukweli, lakini hakuiboresha kama ilivyopaswa. Alipaswa kuibeba dini yake hata alipokuwa pamoja na jamaa zake. Kukiri kwake kwa mdomo kwa utakatifu na Ukweli wa Mungu vilipaswa kuungana na mawazo yake yote, hisia, maneno, na matendo. Kristo anawaagiza wafuasi Wake watembee katika nuru. Maana ya kutembea ni kusonga mbele, kufanya jitihada, kutumia uwezo wetu na kushiriki kikamilifu. Kama tusiposhiriki katika kazi njema ambayo Mwokozi wetu ametuita, na kuuona umuhimu wa juhudi binafsi katika kazi hii, tutakuwa na dini dhaifu, iliyodumaa. Tunapata ushindi mpya kutokana na uzoefu wetu katika kufanya kazi. Tunapata nguvu hai na kazi kwa kutembea katika nuru, ili tuweze kuwa na nguvu za kukimbia katika njia ya amri za Mungu. Tunaweza kupata ongezeko la nguvu katika kila hatua tunayosonga kuelekea mbinguni. Mungu huwabariki watu Wake pale tu wanapojaribu kuwa mbaraka kwa wengine. Neema katika maisha yetu hukua na kuendelea tunapoifanyia kazi. 3T 436.2

Nilioneshwa wakati Ndugu B alipokuwa mjini Battle Creek hakuwa na maadili mazuri. Hakutafuta kushikamana na Mungu na kuihifadhi roho yake katika mawazo

na matendo yaliyo safi, hivyo aliachwa aifuate akili yake na kupata mawazo ambayo hayakuwa sahihi na ya uharibifu kwa masilahi yake ya kiroho. Alikutana na watu wapotosha Ukweli na kumwongoza kuamini vitu ambavyo vilikuwa si vya Kweli; alipokubali kumfungulia mlango adui na kumpokea kama malaika wa nuru, alishindwa na majaribu kwa urahisi. 3T 437.1

Akawa na chuki mbaya na kuwa na shaka juu ya wale ambao Mungu aliwaleta Kwake ili amwamini. Aliviona vitu katika nuru potovu, na mikutano ambayo ingepaswa kuwa chanzo kikuu cha nguvu kwake ilimjeruhi. Hivi ndivyo Shetani alivyohitaji kuwa, ya kwamba, Ndugu B apoteze imani kwa watu ambao Mungu alikuwa amewateua kuisimamia kazi Yake. Alitofautiana nao kabisa hata katika moyo wa kuifanya kazi. Alikuwa kama chombo baharini bila nanga au usukani. Kama hakuweza kuwaamini viongozi asingekuwa na imani kwa mtu yeyote. 3T 437.2

Ndugu B hakuwaheshimu wenzake; alifikiri kuwa uamuzi, ujuzi na uwezo wake ni bora kuliko wao; hivyo hatoweza kupokea lolote kutoka kwao, kuuamini uamuzi wao, wala kutafuta ushauri kutoka kwao, isipokuwa Yeye ndiye awezaye kuwaongoza na kuwafundisha. Angefanya kulingana na maamuzi yake, bila kujali hisia za ndugu zake, huzuni yao, kusihi kwao, au maombi yao. Alipoamua kuitenganisha usadikisho wake na moyo wa kuifanya kazi, Shetani alitambua ya kwamba pasipo imani yake kurejeshwa katika Bwana, hakika ni wake hadi pale imani hiyo itakaporejeshwa. Manufaa na maslahi ya milele ya ndugu B yatategemea ukubali wake na kuiheshimu misaada na uongozi ambao umempendeza Mungu kuuweka kanisani. Ikiwa ataufuata uchaguzi wake mwenyewe hatimaye atagundua ya kuwa amekuwa katika njia potovu kabisa na ya kwamba amejidanganya na kupelekea uharibifu wake. Anaweza kuchukua hatua ya kwanza, kisha nyingine, na baada ya hapo kuipoteza njia ya Kweli na ya ya pekee inayoongoza kuelekea mbinguni. 3T 437.3

Kuna maelfu wanaosafiri katika njia ya giza na yenye makosa na upotovu, barabara pana inayoongoza kwenye mauti, ambao hujidanganya na kujibembeleza kwamba wao wako katika njia ya furaha ya mbinguni; lakini hawataifikia furaha hiyo wala kuipata katika njia hiyo. Ndugu B anahitaji msaada ambao Mungu ameuweka ndani ya kanisa, kwani yeye hawezi kutengeneza kanisa lake mwenyewe, na bado hatua yake inaonesha kwamba anaridhika kuwa kanisa kamili, bila kumtegemea yoyote. Tangu muda mrefu ndugu B alipopoteza hali ya kujitoa wakfu kwake kwa Mungu; hakuhifadhi njia ya nafsi yake dhidi ya maoni ya Shetani [macho, masikio, pua, mdomo, hisia-avenue of the soul]. Niliona malaika wa Mungu wakiandika maneno na matendo yake. Alikuwa akienda mbali zaidi na zaidi kutoka kwenye nuru ya mbinguni. Wakati neema ya Mungu inapokosa kukudhibiti, Ndugu B, wewe ni mtu mgumu kuunganishwa nayo. Unajiamini sana na kujiona imara, hali ambayo

inahisiwa katika familia yako na kanisani. Una utu na heshima kidogo kwa mtu yeyote. Hauna neema ya unyenyekevu. 3T 438.1

Ndugu B alirudi pwani wakati wa giza kuu; alikuwa amepoteza upendo wake kwa ajili ya Kweli na upendo wake kwa Mungu. Hisia zake za asili zilimdhibiti, na alikuwa na kiburi. Alijipenda mwenyewe, na alipenda pesa kuliko alivyoupenda Ukweli na Mkombozi wake. Nilioneshwa kuwa kazi yake baada ya kurudi pwani ilikuwa ni fedheha kwa jina la Kikristo. Nilimwona akiunganisha mikono na wapenda anasa wanaongua vicheko vikali vya raha. Aliwahuzunisha ndugu zake na kumjeruhi Mwokozi wake na kumdhalilisha mbele ya wasioamini. Niliona kuwa tangu wakati huu hakufurahia huduma ya Mungu au maendeleo ya Ukweli. Alionekana kuwa na bidii ya kuchunguza Maandiko na waandishi tofauti, sio kwamba ili apate kujua Ukweli juu ya mambo muhimu na kusimikwa katika Kweli ya sasa ambayo uongozi na majaliwa ya Mungu ilimpatia kupitia watu aliowachagua, la hasha, bali ili kupata nafasi mpya na kukuza maoni mapya yaliyo kinyume na imani ya kanisa. Utafiti wake haukufanywa kwa utukufu wa Mungu, bali kukuza ubinafsi. 3T 438.2

Pindi Ndugu B, anapoamua kuchukua msimamo kwa upande usiofaa au wenye makosa, asili yake siyo kuona kosa lake na kulikiri kosa hilo, bali kulipigania hadi mwisho, bila kujali matokeo yake. Roho hii ni ya kuangamiza kanisa Lake Bwana na huangamiza pia kwa familia yake. Anahitaji kulainisha moyo wake na kuruhusu upole, unyenyekevu, na upendo. Anahitaji ukarimu, uungwana, ubora na utauwa ulio bora. Kwa kifupi, anahitaji kuongoka kabisa, kuwa mtu mpya katika Kristo Yesu. Ndipo ushawishi wake kanisani utakapokuwa sahihi na atakuwa msaada unaohitajika. Atakuwa na heshima pamoja na upendo kwa familia yake na ataiongoza nyumba yake wamfuate. Wajibu na upendo kama mapacha, vitakuwa msaada kwake katika usimamizi wa watoto wake. 3T 438.3

Niliona kwamba dada B alikuwa na huzuni nyingi juu ya hatua ambayo mumewe alikuwa ameifuata kwa ajili yake; kwamba maisha yake yalikuwa ya kusikitisha sana, wakati angeweza kufurahia maisha. Alionekana kukata tamaa na kuhisi kabisa kwamba alikuwa amepuuzwa na hapendwi na mumewe. Kwa kukosekana kwa mumewe wakati mwingine alihisi karibu kuvurugwa na kuwa na wivu na kutokumwamini. Shetani alikuwepo na majaribu yake, na Dada B aliangalia vitu kadhaa na kuvikuza kuliko kawaida. Haya yote yangeokolewa ikiwa Ndugu B angehifadhi kujitolea kwake kwa Mungu. Nilichukuliwa kwenda mbele zaidi na kuona kwamba alikuwa akitembea katika kutoamini katika giza wakati alikuwa akijifariji na kujidanganya kwamba yeye peke yake ndiye mwenye nuru ya Kweli. Kadiri alivyozidi kujitenga na Mungu ndivyo upendo wake kwa ndugu zake na kwa ajili ya Kweli ulivyopungua. 3T 439.1

Nilioneshwa Ndugu B akiuliza kuhusu baadhi ya mambo kuhusiana na imani yetu ambayo imetutoa kutoka ulimwenguni na kutufanya kuwa watu wa tofauti na wa kipekee, tukilitazamia tumaini lenye baraka na kuonekana kwa utukufu wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Kutokuamini kwake na giza lake havijatikisa nguzo kuu za imani yetu. Ukweli wa Mungu haujaufanya kuwa si kitu kwaajili yake, kwani Unabaki kuwa Ukweli, ijapokuwa amekuwa na ushawishi juu ya akili za ndugu zake. Ripoti za midomo ya uongo kuhusu mimi na mume wangu, aliyoileta kutoka Mashariki, ilikuwa na ushawishi wa kujenga mashaka na dukuduku katika akili za wengine. Wale ambao hawakutufahamu, wasingeweza kusimama kututetea. Katika kanisa la -----, niliona lingeweza kuwa na idadi mara tatu zaidi ya ilivyo sasa, na ingekuwa na nguvu mara kumi zaidi, ikiwa Ndugu B asingecheza mikononi mwa adui ibilisi. Katika upofu wa kutokuamini kwake amefanya kila awezalo kuwakatisha tamaa na kuwatawanya waumini katika Ukweli. Katika upofu wake, hakutambua kwamba mwenendo wake ulikuwa wa kutisha mbele za Mungu. Kukatisha tamaa na giza ambalo amelisababisha kumefanya kazi ya Ndugu C kuwa ngumu mara mbili zaidi, kwani ushawishi wake haukusikiwa tu na kanisa la huko -----, bali hata katika makanisa mengine. 3T 439.2

Ndugu, B ameimarisha kutokuamini na ushawishi wa kupinga baina ya watu ambao Ndugu C amelazimika kukutana nao. Niliona kwamba tutakutana na mambo sawa na kwamba itachukua muda kumaliza mzizi wa zamani wa uchungu ambao wengi wametiwa unajisi; kwamba kuna wakati wa kusema na wakati wa kunyamaza; Wakati Mungu anapotupatia jukumu la kusema na kuzungumza hebu tusisite, hata kama wanadamu watasikia au hawatasikia; na kwamba tunapaswa kushinikiza jambo hilo, hata ikiwa litawaacha wengine nje ya kanisa na nje ya Ukweli. Mungu anayo kazi kubwa na muhimu kwa kila mtu kuifanya huko -----, na kwa wakati unaofaa itafanywa, na Ukweli utashinda. 3T 440.1

Ndugu zetu wale ambao walikuwa hawajapata uzoefu wao wenyewe katika Ukweli wa sasa hawakuweza kujibu hoja za Ndugu B, na ingawa hawakuweza kupokea maoni aliyoyasimamia, waliathiriwa kiasi ama kwa mazungumzo yake na hoja zake. Wengine hawakusikia Roho ya uhuru walipokutana kwa ibada. Waliogopa siku ya Sabato kusema hisia zao halisi na imani, wakitarajia kwamba mtu huyu atawakosoa kwa kile watakachosema. Kumekuwa na roho ya mauti na ukimya katika mikutano na uhuru mdogo tu. 3T 440.2

Ndugu B anatamani kwamba wengine wamuangalie yeye tu kama mtu anayeweza kuelezea Maandiko, lakini nilioneshwa kuwa amedanganywa na haelewi chochote. Ameanza katika njia potovu huku akitafuta kupata imani mpya, nadharia ya asili ya imani. Angeweza kung'oa na kuharibu alama hizo ambazo zinatuonesha nanga/nguzo zetu sahihi, ya kwamba tuko karibu na mwisho wa historia ya dunia hii. Anaweza kujidanganya kwamba anaongozwa na Bwana, lakini hakika ni roho

nyingine. Mpaka pale atakapobadilisha njia zake kabisa, na kuwa tayari kuongozwa na kujifunza, ataachwa afuate njia zake mwenyewe na kuanguka katika imani yake. 3T 440.3

Wengine wamepofushwa sana na kutokuamini kwao hata hawawezi kutambua roho ya Ndugu B. Wangeweza kusaidiwa naye ikiwa tu angekuwa amesimama katika shauri la Mungu. Angeweza kuwaongoza kwenda kwenye nuru badala ya kuzidisha mkanganyiko wa imani, fadhaa na mashaka yao. Lakini amekuwa kikwazo, kiongozi kipofu wa vipofu. Laiti angefanya njia iliyonyooka kwa ajili ya miguu yake basi, vilema wasingeweza kuzuiwa, bali wangeponywa. Amekataa kutembea katika nuru ya Ukweli ambayo Mungu amewapatia watu Wake, na wale ambao walipaswa kutembea katika nuru yeye amewazuia. 3T 441.1

Anahisi kuwa ni heshima kupendekeza mashaka na kutokuamini juu ya imani iliyowekwa kwa watu wa Mungu wanaozishika amri. Ukweli ambao hapo awali aliufurahia, sasa ni giza kwake, na asipobadilisha njia yake, atarudi katika mchanganyiko wa maelekezo ya madhehebu tofauti, lakini kwa ujumla hatakubaliana na hata mmoja kati yao; atakuwa kanisa tofauti akiwa mwenyewe, bila kuwa chini ya usimamizi Mkuu wa Kanisa. Kwa kuleta mapendekezo yake kinyume na imani ya kanisa, analivunja moyo kanisa na kulikatisha tamaa kanisa. Anaona kwamba ikiwa umoja wa watunza Sabato una Ukweli yeye yuko gizani, na hili hawezi kulikubali. Ukweli unamhukumu, na badala ya kutafuta kuifanya roho yake ipatane nao Ukweli, kujisalimisha kwa madai yake na kufa kwa nafsi yake, anatafuta nafasi ambayo hatakuwa chini ya hukumu. 3T 441.2

Nilioneshwa kwamba ikiwa ataendelea na mwenendo wake wa sasa, akipofushwa na hali yake halisi, atafurahi kwa muda baada ya kupata kisingizio cha kutokutunza Sabato. Kwa hakika Shetani hakika anamwongoza, kama alivyowaongoza wengine wengi, mbali na umoja wa mwili wa Kristo kwa njia ya udanganyifu na makosa. Ni salama zaidi kwa Ndugu B kuileta roho yake ipatane na Ukweli kuliko kutafsiri vibaya Maandiko ili ayapatanishe kuendana na matakwa yake pamoja na matendo yake. Ikiwa anataka kuyafanya matendo yake yapatane na kanuni za sheria ya Mungu ana jukumu mikononi mwake ambalo bado hajaliotea ndoto au kuliweka mawazoni. Moyo wa mwanadamu wenyey tamaa za mwili una uadui na Mungu. Hauitii sheria ya Mungu, wala hauwezi kuitii. 3T 441.3

Mazungumzo na hotuba za wazi za wale ambao ni maadui zetu huko Battle Creek zilipokelewa na Ndugu B wakati wa safari yake ya Mashariki, na alirudi na hisia kali ya uchungu na uovu moyoni mwake dhidi ya wale walio katika kiini cha kazi na hasa dhidi yangu na kazi yangu. Hakuwa na sababu nzuri ya hisia alizopenda na maoni aliyoyatoa kuhusu kazi yangu na shuhuda zangu. Kutokuamini na chuki ambayo ilikuwa imeharibu roho yake mwenyewe alijaribu kuiingiza ndani ya akili

za wengine. Alifanya hivyo kwa athari kubwa. Mwanzoni, wengi waliathiriwa na ustadi wake wa udanganyifu na giza, kwani angeweza kutoa madai na kuteka maoni kana kwamba alikuwa akishughulikia Ukweli chanya. Anajua jinsi ya kushinikiza mambo na yuko tayari kuzungumza. Maneno yake yalikuwa na ushawishi kwa wengine ambao walikuwa hawajawekwa wakfu na ambao walitamani hali iwe kama alivyoiwakilisha kuhusu kazi yetu na wito wetu. Alikuwa na ushawishi na uwezo wa kusisimua katika mawazo ya wengine ambao tungeweza kuwasaidia, alifanya hivi ili kufunga njia ya kuwafikia wengine. Ndani ya kundi hili walikuwapo Ndugu na Dada D. 3T 442.1

Katika hili Ndugu B anaweza kuona matunda ya kazi yake, na kuna wengine ambao walishawishiwa vivyo hivyo, na kwa matokeo sawa, kwa kadiri walivyohusika katika imani zao na ujasiri wao. Mara tu Ndugu B au miongoni mwa wengine, watakapotambua kuwa watu ambao walikuwa na mengi ya kufanya katika kuleta hoja ya Ukweli wa sasa kufikia hali yake ilivyo sasa hawaongozwi na Mungu, bali wanabuni mafundisho yao, wakiwarubuni, na kuwawadanganya watu, ndipo watajua kwamba, kazi yao ni kutafuta njia ya kuwa thabiti katika kupinga kazi yote na kuifanya yote kuwa udanganyifu na uongo/fraud. Ili kuwa thabiti, lazima watose na kutupa kila kitu nje ya mashua ya Neno la Mungu. Ndugu B huyu amekuwa akifanya hivi bila kujua, na wengine wamefanya hivyo pia. Nyakati zijazo, atazichunguza kazi zake kwa hisia tofauti na ilivyo sasa. Ataona kazi na matokeo yake ambayo amekuwa akiifanya katika miaka michache iliyopita na kama vile Mungu anavyoiona, yeye pia hataiona kwa kuridhika kama anavyohisi sasa. Atakapoona kazi ya huzuni ambayo amekuwa akijishughulisha kwa miaka michache iliyopita, kujivunia kwake na kiburi juu ya hekima na maarifa bora, utakuwa ni mwisho wake, na atatubu kwa uchungu, kwani damu ya roho zilizopotea ziko kwenye mavazi yake. 3T 442.2

Ikiwa Ndugu B alikuwa anataka kuona mambo kwa usahihi na alikuwa amehisi uwezekano wa kudanganywa, angekuja kwa Ndugu na Dada White na taarifa hizo zenye kujeruhi/kudhuru sifa yao na angewapa nafasi ya kusema wao wenyewe. Taarifa hizo alizoleta kutoka mbali nyanda za Pwani ya Pasifiki zilibeba ushahidi wa uwongo, na hivyo kuvunja sheria ya Mungu. Siku moja atakutana na hotuba ngumu, pamoja na werevu wa udanganyifu uliochochewa na Shetani, ambao ameuingiza ndani ya akili za watu na kudhuru ushawishi wangu mimi na mume wangu. Jambo hili haliko kati ya Ndugu B na mimi, bali kati yake na Mungu. 3T 443.1

Mungu ametupatia kazi yetu, na ikiwa Yeye ametupatia ujumbe wa kufikisha kwa watu wake, watu ambao watatuzuia katika kazi hiyo na kudhoofisha imani ya watu Wake katika Ukweli na haki Yake, wao hawapigani na chombo hicho, bali dhidi ya Mungu Mwenyewe, na watalazimika kuwajibika Kwake kwa matokeo ya maneno na

matendo yao yote. Wote walio na utambuzi wa kiroho wanaweza kuuhukumu mti kwa matunda yake. Ndugu B anasimama kama mtu aliyeangaziwa na Mungu kuwasahihisha na kuondoa uongo miongoni mwa watu kuhusu kazi na utume wetu. Wote wanaweza kuona, ikiwa watataka, matunda yanayokua juu ya mti huu. Ndugu B, je haya yote ni kwa uzima wa milele, au kifo? 3T 443.2

Baada ya Ndugu B kupokea mafundisho na maarifa maalum kutoka Battle Creek, ambayo yalimpelekea kuamua kufanya kazi ya kuudharau na kuudhalilisha utume wetu, alijiona yuko huru kujiunga na wasioamini katika kula anasa za ulimwengu huu, na kwa uaminifu wake wa mwenendo huo alileta aibu juu ya Kristo na kusababisha maumivu makali kwa mke wake. Je alikuwa amepofuka sana kiasi kwamba alikuwa akibomoa kile ambacho Mungu alikuwa akikijenga? Je, hakufikiri kwamba alikuwa anapigana na Mungu? Kazi ambayo amekuwa akiifanya malaika wameinakili mbinguni, na atalazimika kuijibu pale ambapo kila kazi italetwa hukumuni ili aweze kujibu mashtaka kwa Mungu wa milele. Katika upofu wake Ndugu B amekuwa akiinua mkono wake mdogo kupigana na Mungu huku akiidanganya nafsi yake iliyoaminishwa kwamba alikuwa akifanya huduma kwa Mungu. Kazi ya kila mtu ni kujaribiwa na moto wa siku ya mwisho, na dhahabu, fedha, na vito vya thamani tu ndivyo vitasimama katika siku hii ya mwisho. 3T 443.3
Mungu hadanganywi wala hachezewi. Yeye Anaweza kuwa mvumilivu kwa wanadamu, lakini hataacha kuzuru makosa yao na kumlipa kila mtu kulingana na kazi yake ilivyo. Ijapokuwa watu wanaweza kuzungumza kwa kujigamba na kujivunia hekima zao, pumzi moja kutoka katika kinywa cha Mungu inaweza kushusha heshima na majivuno yao yote mavumbini. Nilioneshwa kuwa Ndugu B hatakuwa na udhuru katika siku ya Mungu, wakati kila kisa kitakapopimwa katika mizani ya Patakatifu. Anajua kufanya bora kuliko alivyofanya sasa. Ana ushahidi wa kutosha kujua tabia ya kazi ambayo Mungu ametupatia. Matunda ya kazi hii yako mbele, ambayo anaweza kuyaona na kuyaelewa ikiwa atapenda kufanya hivyo. 3T 444.1

Kujiamini kwa Ndugu B ni kwa ajabu sana, na ni mtego wa kutisha kwake. Ikiwa hataweza kuishinda tabia hii hatarishi maishani mwake, itathibitisha uharibifu wake. Mara nyingi huwa yuko katika hali yake ya asili anapopambana na hoja zenye ubishani za mafundisho; atahoji na kuleta utata, na pia atakuwa na ugomvi na ndugu zake mpaka inafikia hatua ambayo Shetani anaidhibiti akili yake na kuamini kwamba kweli anao Ukweli na ndugu zake wamekosea. Hasimami kwenye nuru na wala hana baraka za Mungu, kwa maana dini yake hujumuisha kupinga hoja zenye mashiko za watu wa Mungu wanaoshika amri Zake. Je! Wote hawa wamedanganywa? na je, ni ndugu B peke yake tu ambaye Mungu amempatia Ukweli sahihi? Je! Mungu Hayuko tayari kuwapatia watumishi Wake waliojitolea,

na kujikana nafsi ufahamu sahihi wa Maandiko mpaka ampe yote ndugu B kwa ajili yao? 3T 444.2

Je! Ndugu B anajaribu kazi yake kwa mtihani huu rahisi: “Je! nuru na maarifa haya ambayo nimeyapata, na ambayo yananipa utofauti na ndugu zangu, yananivuta karibu zaidi kwa Kristo? Je, yanamfanya Mwokozi wangu awe wa thamani zaidi kwangu na kufanya tabia yangu ifanane kwa karibu zaidi na Yake?” Ni tabia ya asili, lakini si ya kupendeza, katika tabia zetu, kuwa makini na mawazo/fikra zetu, na kuwa hodari katika kukumbuka kwetu, kwa makosa na kasoro za wengine. 3T 444.3

Ndugu B hajishughulishi kwa jitihada zozote kuwa na umoja na ndugu zake; kujiamini kwake kumemfanya asione umuhimu maalumu wa umoja. Anahisi kuwa akili zao zimetupwa katika ukungu duni kuliko akili zake na kwamba kupokea maoni na ushauri wao kama unaostahili kuzingatiwa kungekuwa kujishusha sana. Kujiamini huku mwenyewe kumemfungia mbali kwa upendo na huruma za ndugu zake na kutokuwa na umoja nao. Anajiona kuwa ana busara sana na ni mzoefu kuhitaji tahadhari ambazo ni muhimu kwa wengi. Anajiamini kuwa na maoni ya juu sana ya uwezo wake na kutegemea mafanikio yake mwenyewe kuwa amejiandaa kwa ajili ya dharura yoyote. Malaika wa mbinguni walisema, wakimwelekeza Ndugu B: Hebu yule "Anayejifikiria kuwa amesimama aangalie asianguke." Kujiamini kunasababisha kupuuza kukesha na uangalifu wa sala ya unyenyekevu, na toba. Kuna majaribu ya nje yanayopaswa kuzuiliwa na maadui wa ndani wa mashaka wanaopaswa kushindwa, kwani Shetani hubadilisha jaribu lake kwa wahusika kulingana na hali tofauti na hulka za watu. 3T 445.1

Kanisa la Mungu liko katika hatari mara kwa mara. Shetani anatafuta kuwaangamiza watu wa Mungu, na akili ya mtu mmoja, uamuzi wa mtu mmoja, hautoshi kuaminiwa. Kristo angewafanya wafuasi Wake wakusanyike pamoja katika kanisa, wakifuata utaratibu, wakiwa na sheria pamoja na nidhamu, na wote wakitiana moyo wao kwa wao, wakiwachukulia wengine kuwa bora kuliko wao. Muungano na ujasiri ni nyenzo muhimu kwa ajili ya ustawi wa kanisa. Ikiwa kila mshiriki wa kanisa atahisi yuko huru kusonga mbele na kuwaacha wengine, akikaza tabia na mwenendo wake wa kipekee, kanisa litawezaje kuwa katika usalama nyakati hizi mbaya na hatari? Ustawi na uwepo wa kanisa hutegemea hatua za haraka, zenye umoja na imani ya washiriki wake. Wakati mgumu wa dharura, mtu anapopiga kengele ya hatari, kuna haja ya kufanya kazi kwa haraka na bidii, bila kusimama na kuhoji na kutafuta mada yote kutoka mwanzo hadi mwisho, na hivyo kutomruhusu adui kupata kila faida kwa kanisa kuchelewa. Ikiwa kuna umoja, matendo yanaweza kuokoa roho nyingi kutoka katika uharibifu. 3T 445.2

Mungu anahitaji watu Wake waungane katika vifungo vya umoja zaidi katika ushirika wa Kristo; imani kwa ndugu zetu ni muhimu kwa ajili ya ustawi wa kanisa; umoja katika matendo ni muhimu katika kutatua dharura na migogoro ya kidini. Hatua moja isiyo na busara, hatua moja ya kutojali, inaweza kulitumbukiza kanisa katika shida na majaribu ambayo litaweza kupona baada ya muda mrefu kupita. Mshiriki mmoja wa kanisa aliyejazwa na kutokuamini anaweza kutoa faida kwa adui mkubwa ambaye ataathiri ustawi wa kanisa lote, na roho nyingi zinaweza kupotea kama matokeo. Kristo akiwa na wafuasi Wake wanaowajibika kwa kila mmoja na wanaoaminiana; Ndipo, Mungu anaweza kuwatumia kama vyombo kuokoana wao kwa wao; kwa kuwa mtu anaweza asitambue hatari ambazo jicho la mwingine ni haraka kuzigundua; lakini ikiwa wasio na ufahamu watatii maonyo kwa ujasiri, wanaweza kuokolewa kutoka katika mashaka na majaribu makubwa. 3T 446.1

Wakati Yesu alipokuwa karibu kuwaacha wanafunzi Wake, aliwaombea kwa namna ya pekee sana na yenye kugusa moyo sana, na kwa kicho ili wote wawe kitu kimoja “kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, na Mimi ndani Yako, ili wao pia wawe wamoja ndani Yetu, ili ulimwengu upate kuamini kwamba Wewe umenituma Mimi. Na utukufu ulionipa nimewapa; ili wawe kitu kimoja, kama vile Sisi tulivyo umoja: Mimi ndani yao, na wao ndani Yangu, ili wawe wakamilifu katika mmoja; na ulimwengu ujue ya kuwa Wewe umenituma, na uliwapenda, kama vile ulivyonipenda Mimi.” Mtume Paulo katika waraka wake wa kwanza kwa Wakorintho anawahimiza wawe na umoja: “Sasa nawasihi, ndugu, kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyinyi nyote semeni sawa, na kwamba kusiwe na mafarakano kati yenu; bali muunganishwe kikamilifu katika nia moja, maamuzi na hukumu moja." 3T 446.2

Mungu anawaongoza watu kutoka ulimwenguni kwenda kwenye viwango vya juu vilivyoinuliwa vya Ukweli wa milele, ambavyo ni amri za Mungu na imani ya Yesu Kristo. Yeye atawanidhamisha na Atawaelekeza na kuwafanya watu Wake kuwafaa mahali hapo. Hawatakuwa na utofauti, mmoja akiamini jambo moja, na mwingine akiwa na imani na maoni tofauti kabisa na mwili wa Kristo, kila mmoja akienda njia yake. Kupitia utofauti wa karama na talanta ambazo ameweziweka kanisani, zote zitakuja kwa umoja wa imani. Ikiwa mtu mmoja atakuwa na mawazo yake juu ya Ukweli wa Biblia bila kuzingatia mapendekezo ya ndugu zake, na kuhalalisha mwenendo wake, akidai kwamba ana haki ya maoni yake ya kipekee, kisha akayashinikiza kwa wengine, Je, anawezaje kulitimiza ombi la Kristo? Na ikiwa mwingine atatokea na mwingine tena, kila mmoja akidai haki yake ya kuamini na kuzungumza anachopenda bila kurejelea imani ya kanisa, umoja uliopo kati ya Kristo na Baba Yake utakuwa wapi, na ambao Kristo aliomba uweze kuwepo ndani ya ndugu Zake? 3T 446.3

Mungu anawaongoza watu na kuwasimamisha kwenye jukwaa kubwa la imani, amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo. Yeye Amewapa watu Wake mnyororo /mlolongo ulio sawa wa Ukweli wa Biblia, ulio wazi na uliounganishwa. Ukweli huu ni wa asili ya mbinguni na umetafutwa kama hazina iliyofichwa. Iliyochimbwa ili kuitafuta, kwa uangalifu kupitia Maandiko, na maombi mengi. 3T 447.1

Ndugu B ana mashaka juu ya imani yetu. Ikiwa yuko sahihi katika nadharia zake mpya, umoja wa watunza Sabato uko kimakosa. Je! imani iliyosimikwa katika misimamo thabiti ya nafasi yetu, ambayo imetuongoza kutoka ulimwenguni na kutuunganisha kama watu tofauti na wa kipekee, itachukuliwa kama makosa? Je! Tutapokea imani ya mtu huyu mmoja, pamoja na ushuhuda anaotupatia wa matunda ya tabia yake ya kidini? Au Ndugu B atayasalimisha maamuzi na mapendekezo yake, na kuja kwa mwili wa Kristo? Ikiwa asingepofusha roho yake kwa kupokea ubaguzi, na kwa kuthamini upinzani mbaya kwa kazi ya Mungu, basi asingeachwa kwenye giza kama hilo na udanganyifu. 3T 447.2

Yeye ni mtu rahisi kuzungumza wakati wote ana maneno mengi na atasisitiza mapendekezo yake kila wakati na hatakubali uzito wa ushahidi dhidi yake. Ni ukatili kwa yeye kusimama katika njia ya ustawi wa kanisa, kama alivyofanya. Dunia ni kubwa; B ana fursa zote ambazo anaweza kudai kutoka kati ya wasioamini na kuwageuza kufuata nadharia zake; na anapoweza kuwasilisha tungo zake zilizopangwa vizuri basi yeye amekuwa njia ya kugeuza wa kutoka kwenye dhambi na kuwa haki, basi, na sio kabla, anapaswa kushinikiza mapendekezo ya upekee wake juu ya kanisa la Mungu, ambalo lina uchungu na kuvunjika moyo kwa sababu ya giza na makosa yake. Hana haki ya kujenga juu ya msingi wa mtu mwingine kwa kuni zake, nyasi, na mabua ya kuliwa na moto wa siku ya mwisho. 3T 447.3

Nilioneshwa kuwa nafasi pekee salama kwa Ndugu B ni kukaa miguuni pa Yesu na kujifunza njia ya uzima kwa ukamilifu zaidi. Mafundisho Yake ya imani yatashuka kama mvua, na hotuba yake itamwaga kama umande, juu ya moyo wa wanyenyekevu na wanaofundishika. Ndugu B lazima awe na tabia inayoweza kufundishika. Hapaswi kukaa kama hakimu, bali kama mwanafunzi; si kwa kutoamini, lakini kuamini; siyo kuuliza na kupata makosa na kupinga, bali kusikiliza. Kiburi lazima kibadilishwe kuwa unyenyekevu, na ubaguzi lazima ubadilishwe kuwa uaminifu, la sivyo Maneno ya neema ya Kristo yatakuwa bure kwake. Ndugu yangu, unaweza kuwaza kwa uamuzi wako kipofu na akili isiyojitakasa mpaka siku ya mwisho ya Mungu na usiwe umepiga hatua hata moja kuelekea mbinguni; unaweza kujadili, kuchunguza na kutafuta waandishi wasomi, na hata Maandiko, na bado ukazidi kujidanganya zaidi na zaidi, na kuwa katika giza totoro zaidi, kama vile walivyokuwa Wayahudi kwa uelewa finyu juu ya Kristo. Je, kosa lao lilikuwa lipi? Walikataa nuru ambayo Mungu alikuwa tayari amewapatia na walikuwa wakitafuta nuru mpya hata kutafsiri Maandiko ili kutegemeza matendo yao. 3T 448.1

Unafanya vivyo hivyo; unaiacha nuru ambayo Mungu ameona inafaa kukupatia kupitia kwenye machapisho mbalimbali juu ya Ukweli wa sasa na katika Neno Lake, na unatafuta mafundisho yako mwenyewe, nadharia ambazo haziwezi kudumishwa na Neno la Mungu. Utakapoamua kuwa kama mtoto mdogo, mwenye nia ya kuongozwa, na ufahamu wako unapotakaswa na mapenzi yako na chuki zikasalimishwa, nuru kama hiyo itatolewa nje ya moyo wako kama itakavyoangazia Maandiko na kukuonesha Ukweli uliopo kwa upatano wake mzuri. Utaonekana kama mnyororo wa dhahabu, kiunganishi, kilichounganishwa kuungana kwa ukamilifu. "Msipobadilika, na kuwa kama watoto wadogo, hamtaingia katika ufalme wa mbinguni." "Jifunzeni kutoka Kwangu," asema Kristo; "Kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu." 3T 448.2

Ikiwa Kweli umeamua kuingia katika shule ya Kristo, ZYeyeAnakutarajia udhihirishe tabia yako, mwonekano na unyenyekevu ambao umeoneshwa vizuri sana katika tabia Yake. Kristo hawezi kuwafundisha wanaojiona kuwa wenye haki, wanaojitegemea, wanaojidanganya na wenye mapenzi binafsi. Ikiwa watu kama hao watamjia na kumuuliza, Ukweli ni nini? Hatawapatia majibu. Ni wapole tu ndioambao atawaongoza katika hukumu; atawafundisha wapole njia yake. Ni Kweli Sulemani alipewa Maarifa na uwezo mkubwa wa kufikiria, lakini alijitambua mbele za Mungu kama mtoto mdogo. Alitafuta hekima kutoka kwa Mungu kwa unyenyekevu, na hakutafuta bure. Ikiwa unautafuta Ukweli kwa nia njema, kwa moyo mkunjukufu utakuja katika umoja wa hitimisho sawa, kwani humo kuna Ukweli. Ikiwa unatafuta Maandiko na waandishi anuwai ili upate mafundisho ambayo yatapatana na mapendekezo yako mwenyewe unayodhania, na ikiwa tayari umejiamria imani yako mwenyewe, basi utakuwa na kiburi, mbinafsi, usiyekubali kuacha mawazo yako na utakakosa matunda. 3T 448.3

Kujiamini Ni Mtego

Ndugu B, kwa roho uliyonayo sasa yenye kujali mapenzi yako mwenyewe, na ukaidi, utajikuta uko mbali zaidi na Ukweli; na usipobadilika utaonekana kuwa kikwazo kikubwa kwa kusudi la Mungu mahali popote ambapo wewe una ushawishi. Unapendelea kubeba hoja zako mbaya mwenyewe. Roho yako ya ubinafsi lazima itolewe kabla ya kuona kwa uwazi chochote. Umemwongoza mke wako kufikiri kwamba uliujua Ukweli kuliko wachungaji na wahudumu wetu wote; umebeba ufunguo wa maarifa mikononi mwako, kwa kadri anavyojali, na umemweka gizani. Mungu amelipatia kanisa Lake watu wenye maamuzi, uzoefu, na imani. Wanaijua njia ya Ukweli ya wokovu, kwani wameitafuta kwa uchungu kwa sababu ya upinzani waliokutana nao kutoka kwa watu ambao waligeuza Ukweli wa Mungu na kuwa uongo; na faida ya kazi ya watumishi hawa waaminifu wa Mungu hutolewa kwa ulimwengu. 3T 449.1

Ni baadhi tu ya watu ambao wanatambua hali ya kuinuliwa sana na kutukuzwa kwa kazi ya Mungu kulivyo, ikilinganishwa na biashara za muda katika maisha yetu. Yesu, Mwalimu wa mbinguni, ametupatia masomo na mafundisho kupitia wanafunzi Wake. Alipowatuma wale kumi na wawili, aliwaamuru kwamba katika miji yote au mji ambao wangeingia na kugundua kama kuna mtu aliye ndani yake ambaye angestahili umakini wa ziara yao na kwenda kumuona; na ikiwa mahali pazuri patapatikana ambapo watu hawa wangethamini baraka walizotumwa, - fursa ya kuwakaribisha wajumbe wa Kristo, —hapo walipaswa kukaa na kupumzika mpaka walipoondoka katika mji huo. hawakuagizwa kutembelea nyumba yoyote kiholela, wakiwataka uwepo wao kwa watu ikiwa wanakaribishwa au la; lakini ikiwa hawakukaribishwa, ikiwa amani yao isingeweza kutulia ndani ya nyumba hiyo, walipaswa kuiacha na kutafuta nyumba ambayo washiriki walistahili na mahali ambapo wangeweza kupumzisha roho zao. 3T 449.2

Wakati wajumbe wa Kristo ambao huenda kufundisha Ukweli kwa wengine wanapokataliwa na maneno yao kukosa nafasi moyoni, Kristo hukataliwa na Neno Lake linadharauliwa na kuchukiwa kupitia kwa wajumbe Wake wenye Ukweli ambao amewachagua na kuwatuma. Jambo hili lina matumizi kamili katika wakati huu wa ulimwengu kama ilivyokuwa wakati Kristo alipotoa maagizo kwa wajumbe Wake wateule. 3T 450.1

Wakati Kristo akiwa ulimwenguni, kulikuwa na watu ambao hawakuwa na heshima na kicho kwa wajumbe wa Mungu na hawakujali sana maonyo yao dhidi ya kuwahukumu wenyewe; pia katika zama hizi za ulimwengu kuna wale ambao hawaheshimu ushuhuda wa watumishi waliochaguliwa na Mungu kana kwamba ni mapendekezo yao wenyewe. Watu kama hao hawawezi kufaidika na kazi ya watumishi wa Mungu, na hatupaswi kupoteza muda katika kudhalilisha kazi ya Mungu ili tu kufikia fikra za namna hiyo. Kristo aliwaambia watumishi aliowatuma: "Yeye awasikiaye ninyi anisikia Mimi; na yeye anayewadharau ninyi ananipuuza Mimi; naye anidharauye Mimi anamkataa Yeye aliyenituma.” 3T 450.2

Kristo anaipatia nguvu sauti ya kanisa. "Amin Amin nawaambieni, Lolote mtakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni pia; na lo lote mtakalolifungua duniani litafunguliwa na mbinguni pia." Hakuna kitu kama hicho kinachohesabiwa haki ikiwa mtu mmoja atachukua jukumu lake binafsi na kutetea hoja zake alizojiamulia mwenyewe, na kupendekeza bila kujali maamuzi ya kanisa. Mungu amelipatia kanisa Lake mamlaka ya juu kabisa chini ya mbingu. Ni sauti ya Mungu ndani ya watu Wake walio na umoja katika uwezo wa kanisa ambayo inapaswa kuheshimiwa. 3T 450.3

Mungu amewapa kanisa Lake watu ambao wana uzoefu, wale ambao wamefunga, wamelia na kuomba, hata usiku kucha, ili Bwana awafungulie Maandiko, kwa unyenyekevu watu hawa wameudhihirishia ulimwengu namna walivyokomaa. Je! Nuru hii ni ya mbingu, ama ya wanadamu? Je! ina thamani yoyote, au haina

thamani? Ndugu B anafanya kazi katika kusambaza maono potofu ya Ukweli wa Biblia ambayo siku moja atataka kuyatengua; lakini itakuwa kazi bure. Ni Kweli anaweza kutubu, na anaweza kuokolewa kama kijinga kutoka kwenye moto; lakini, lo! Ni muda wa thamani kiasi gani ambao utakuwa umepotea ambao kamwe ambao hauwezi kuokolewa. Ni mbegu kiasi amepanda zilizojaa mbigili, vichomi na miiba pekee! Ni roho ngapi zimepotea ambazo zingeweza kuokolewa ikiwa angejaribu kwa bidii kuiruhusu nuru ya Kweli iangaze kama alivyojibidisha kutawanya giza lake! Je! Jambo lipi asingeweza kufanya ikiwa angewekwa wakfu, na kutakaswa kupitia Kweli! Ndugu B anahisi kuwa anajitosheleza, ametajirika na ameongezeka sana kimaendeleo, hata kuhisi kuwa hahitaji kitu chochote. Shahidi wa Kweli alimwonesha na kusema: "Mpaka utakapogeuzwa na kuwa kama mtoto mdogo, kamwe hauwezi kuuona ufalme wa mbinguni." Haiheshimu nuru ya Kweli iliyoletwa kwa uangalifu katika vitabu na majarida mbalimbali; bali anainua maamuzi na hukumu yake mwenyewe juu ya nuru ya thamani zaidi, na nuru hii itainuka katika hukumu na kumhukumu yeye mwenyewe. 3T 451.1

Niliona kwamba angewasumbua kwaa kuwahoji watu ambao Mungu ameona ni sawa kuweka jukumu la kazi yake mikononi mwao. Angeibua mawazo na mapendekezo yake juu ya nuru ambayo Mungu alikuwa ameitoa kupitia kwao, na angejivunia maarifa yake; pia angekuwa mshtaki wa ndugu zake, hata bila kuwakubali mabalozi wa Kristo. Ushawishi huu wote wa kudhalilisha na kudharau maamuzi ya watumishi wa Mungu na kuwasingizia juu ya udhaifu na makosa yao, huku akiibua maoni yake juu ya mafundisho yao, hakika ikiwa hatatubu, yatakuwa yameandikwa dhidi yake katika vitabu vya hukumu, ambayo atayashuhudia kwa aibu katika siku ya Mungu. 3T 451.2

Mungu atawashikilia watumishi Wake, na atawahifadhi wale anaowapenda; lakini ole wake yule ambaye hatauufanya ujumbe wake usiwe na ufanisi, ambao unaletwa kupitia mabalozi Wake Kristo, wanaopokea Neno kutoka katika kinywa cha Mungu mwenyewe ili kuongea na watu na ambao huwaambia watu kuwa upanga unakuja na kuwaonya kujiandaa kwa ajili ya siku kuu ya Bwana. Ndugu B atagundua kuwa si kazi nyepesi au ndogo ambayo amehusika mayo; ni suala ambalo litakuwa zito moyoni mwake na kumsagasaga. Roho yake imeongoza katika jitihada za kumpinga Mungu. Ana kazi ngumu mbele yake. Kristo alisema, "Makwazo hayana budi kutokea; lakini ole wake mtu yule anayeyasababisha.” 3T 452.1

Ndugu B mwenendo ambayo umekuwa ukipitia nilioneshwa miaka mitatu iliyopita. Niliona kuwa alikuwa amekosea karibu kila tendo, na bado ulijaribu kuutumia Ukweli kwa ajili ya matakwa yake badala ya kufuata matakwa ya Ukweli. Haukuwa nuru hata kwa watu wa Mungu, bali ulikuwa mzigo mzito. Haukuinua wakati ulipohitajika, bali uliwakatisha tamaa wengine kutoka kwenye umoja wa vitendo. Unatafuta lawama kila wakati na kuzungumza mabaya juu ya ndugu zako, na

wakati ambao umekuwa ukihoji juu ya mwenendo wa wengine, ukuaji wa kiwango cha magugu yenye sumu umeshamiri na kuimarisha mizizi ndani ya moyo wako mwenyewe. Mizizi hii ya uchungu iliyochipuka imewachafua wengi na itawachafua wengi zaidi kama hutaona umuhimu wa kuing'oa. 3T 452.2

Nilioneshwa kuwa roho kali na jeuri na ya kifarisayo ingeibuka juu ya Ndugu B na kumdhibiti mpaka pale atakapoona kasoro katika tabia yake na kupata neema kutoka kwa Mungu kurekebisha uovu wake. Kabla ya kupokea Ukweli, mkono wake ulionekana kuwa dhidi ya kila mtu; roho yake ya kupigana na malumbano iliimarika zaidi, na kwamba kujithamini kwake mwenyewe kwa hali ya juu kungeumizwa; Alikuwa mtu mgumu, mwenye kujiingiza na kuleta shida. Ukweli wa Mungu ulifanya matengenezo ndani yake. Mungu alimkubali, na mkono wa Bwana ukamshika. Lakini kwa kuwa Ndugu B amepoteza roho ya kujitoa wakfu na uchaji, roho yake ya zamani, yenye msukosuko, kwa kujitofautisha na wengine, imekuwa ikiimarisha na kutafuta kupata umiliki kwa nguvu zake; Atakapoifia nafsi na kuunyenyekeza moyo wake wenye kiburi mbele za Mungu atatambua jinsi alivyo dhaifu, atajisikia kuwa na uhitaji wa mbingu ili kumsaidia na atalia kwa uchungu: "Najisi! Najisi! mbele zako, Ee Mungu." Majivuno yake yote ya kiburi katika nafsi yake yatafikia mwisho. 3T 452.3

Maisha katika ulimwengu huu wenye dhoruba, ambapo giza la kimaadili linashinda Ukweli na fadhila na wema, hukuwa mzozo kwa Wakristo kadri muda tunavyoendelea. Mkristo atagundua kuwa ni lazima aendelee kuzivaa silaha za nuru, kwani atalazimika kupigana na vikosi ambavyo havichoki na maadui wasiolala kamwe. Tutajikuta tukikumbwa na majaribu yasiyo na idadi, na lazima tupate nguvu katika Kristo kuyashinda au vinginevyo tutashindwa na roho zetu ziishie kuangamia. Tunayo kazi kubwa adhimu na nzito ya kufanya, Je tutakuwa na hasara kiasi gani kama tutashindwa? Ikiwa kazi ambayo Bwana wetu ametuachia na kukuta hatujaimaliza, hatutapewa nafasi ya pili ya rehema. Lazima itabaki bila kufanywa milele. 3T 453.1

Nilioneshwa maisha ya Ndugu B katika familia yake. Malaika walilia walipotazama mwenendo wake nyumbani, kama walivyokuwa wakimwona mke asiyependwa, ambaye hapokei heshima yoyote kutoka kwake ambaye jukumu lake ni kumpenda na kumthamini kama mwili wake mwenyewe, kama vile Kristo anavyolipenda na kulitunza kanisa. B anahenyeka kwa maumivu katika kufanya kasoro za mkewe zionekane maarufu na kuinua hekima yake mwenyewe, uamuzi na kumfanya ahisi kuwa kwake chini akiwa na wenzake na hata akiwa peke yake. Pamoja na kwamba hajui kusoma wala kuandika, roho yake inakubalika zaidi kwa Mungu kuliko roho ya mumewe. Mungu anamwangalia dada B kwa hisia za sikitiko kubwa mno. Anaziishi kanuni za Kweli, kwa kadiri alivyo na nuru bora zaidi kuliko mumewe. Mke hatawajibika kwa nuru na maarifa ambayo mumewe amekuwa nayo wakati yeye hakuwa nayo. Mumewe angeweza kuwa nuru, faraja na baraka kwake, lakini

ushawishi wake mume hutumiwa kwa njia mbaya. Anamsomea yale anayopenda, ambayo yatampa nguvu kutoa mapendekezo yake na fikra zake, akiyaficha yale ya nuru ambayo hataki mke wake ayasikie. 3T 453.2

Yeye hamuheshimu mkewe, na huwafanya watoto wake pia wasimheshimu. Kama wana wa Eli, watoto hawa wameachwa kuwa juu zaidi ya mama yao. Hawazuiliwi, na upuuzaji huu wote utajirudia kwake wenyewe na kile ambacho Ndugu B anapanda sasa atakivuna kwa hakika. Dada B, katika mambo mengi, yuko karibu na ufalme wa mbinguni kuliko mumewe. Watoto hawa wasiotii, wasiothibitiwa na wenye kiburi na ambao hawafundishwa kujidhibiti, watapanda miiba mioyoni mwa wazazi wao ambayo hawawezi kuizuia; na kisha katika hukumu Mungu atawaita wazazi wawajibike kwa kuleta watoto ulimwenguni na kuwaacha wakue bila mafunzo, wasio na upendo, na ambao hawawapendeki kirahisi. Watoto hawa hawawezi kuokolewa katika ufalme wa mbinguni bila mabadiliko makubwa katika tabia zao. 3T 453.3

Ndugu B anatamani kumfanya mkewe aamini kama anavyoamini yeye, na angemtaka afikiri kwamba yote anayofanya ni sahihi na kwamba anajua zaidi ya wachungaji wote na ni mwenye busara kuliko watu wote. Nilioneshwa kuwa katika hekima yake ya kujivunia anashughulika na miili ya watoto wake kama alivyo na roho ya mkewe. Amekuwa akifuata mwenendo kulingana na hekima yake mwenyewe, ambayo inaharibu afya ya watoto wake. Anajiaminisha kwa kujidanganya kuwa sumu ambayo ameiingiza katika mfumo wake inamfanya awe hai. Ni kosa la namna gani hili! Anapaswa kuelewa kuwa ingekuwa bora zaidi kama angemwacha na asimnyanyase kutokana na asili yake. Mtoto huyu kamwe hawezi kuwa na mfumo wa mwili wenye ubora, kwani mifupa yake na mkondo wa damu kwenye mishipa yake vimetiwa sumu. Miili iliyovunjwavunjwa ya watoto wake na maumivu yao yenye kusumbua yatatoa sauti zao dhidi ya hekima yake anayojivunia, ambayo ni upumbavu. 3T 454.1

Lakini cha kusikitisha zaidi ya mengine yote ni kwamba, kama alivyokuwa, ni kwamba ameacha mlango wa upotevu wazi kwa watoto wake kuingia na kupotea. Hulka na asili za watoto wake itabidi zibadilishwe, tabia zao zibadilishwe na kufanywa kuwa mipya, vinginevyo hakutakuwa na tumaini kwao. Je, Malaika wanaweza kuiangalia familia yako kwa upendo, Ndugu B? Je! Wanaweza kufurahi kukaa katika nyumba yako? Jengo ni zuri, lakini nyumba haitengenezi furaha ndani. Wale wanaoishi ndani ya kuta zake huifanya kuwa mbingu au kuzimu. Wewe humuheshimu mama wa watoto wako. Unawaruhusu watoto pia kutotii na kukosa heshima. 3T 454.2

Unaweza kusema: “Kwa nini Dada White anakuja kwangu na hili jambo? Sina imani na maono yake haya.” Nilijua haya kabla ya kujaribu kuandika, lakini nahisi wakati umefika wa kuweka mambo haya mbele yako. Lazima nikuambie Ukweli, kwani natarajia kukutana na hukumu kwa yale ambayo nimeandika hapa bila ukamilifu.

Nimesubiri, nikitumaini kwamba ningeweza kusema kitu ambacho kingeweza kuufikia moyo wako na kuulainisha kwa maneno yale ambayo nimeyaandika hapa. Lakini nimepoteza tumaini kabisa kwa mwelekeo huo, kwani umeimarishwa na ngao isiyoweza kupenyeka kama chuma. Haukubali chochote ambacho hakikidhi akili yako. Nilioneshwa kuwa ingekuwa bora kwa sababu ya Ukweli wa sasa kama hungekuwa umeipokea Sabato maishani mwako. Dhamiri yako haiko makini sana; kwa sababu umepofushwa na adui. 3T 454.3

Nimekosa tumaini la kufanya yote katika kanisa huko ----- wakati wewe ni kikwazo kwao. Uliwahi kuipenda Kweli, na kama ungeifuata katika njia yake na utakatifu wake, sasa ungekuwa balozi wa Kristo. Utakuwa na hesabu kubwa na ya kutisha kwa ajili ya kutoa katika siku kuu ile ya Bwana Mungu kwa talanta zako ambazo haukuzitendea kazi. Ulikuwa na uwezo mzuri. Mungu alikukabidhi talanta hizi ili uweze kuwajibika vizuri, lakini umetumia vibaya talanta hizi. Kama ungekuwa umetumia uwezo ambao Mungu alikuwa amekupa, kwa upande sahihi, ungefanya mengi ili kuzileta roho kwa Kristo, na ungeweza kukutana nazo katika ufalme wa mbinguni, roho ambazo ziliokolewa kupitia wewe. Lakini umezitawanya mbali badala ya kuzikusanya kwa Kristo. Ndugu zako wamevunjika moyo katika kujaribu kuinuka na kusonga mbele, kwa sababu wewe, umekuwa kipingamizi kwao, unapinga mema ambayo wangefanya. 3T 455.1

Moyo wa Mungu haukuwahi kuwa na matamanio na watoto Wake ulimwenguni kwa upendo wa mwanana wa kina na huruma nyororo, na kujali zaidi kuliko sasa. Hakukuwa na wakati ambapo Mungu alikuwa tayari anasubiri kufanya zaidi kwa watu wake kuliko sasa. Naye atawafundisha na kuwaokoa wote wanaochagua kuokolewa kwa njia Yake aliyoweka Mwenyewe. Wale walio wa kiroho wanaweza kutambua vitu vya kiroho na kuona ishara za uwepo wa kazi ya Mungu kila mahali. Shetani, kutokana na mkakati wake wa ustadi na uovu, aliwaongoza wazazi wetu wa kwanza kutoka kwenye bustani ya Edeni — kutoka kwa kutokuwa na hatia na usafi mpaka kuingia dhambini kwa unyonge, uharibifu na uovu mkubwa sana. Mpaka sasa adui bado anaharibu; nguvu zote anazoziamuru zinatumika kwa bidii katika siku hizi za mwisho kuzunguka na kusababisha uharibifu wa roho. Anatumia kila usanii au sanaa ambayo kwayo anaweza kuwadanganya, kuwatatanisha, na kuwachanganya watu wa Mungu. 3T 455.2

Amekutumia wewe kama wakala wake kueneza giza na machafuko, na anaona kuwa unafanya kazi nzuri mikononi mwake. Wewe ndiye chombo ambacho hukitumia ili kuathiri kwa uzito, kuumiza, kukatisha tamaa, na kubomoa. Hauna bidii ya kuweka bega lako chini ya mzigo pamoja na watu wa Mungu; lakini wakati wakisogea, wewe unajitupa mwenyewe kama mzigo wa ziada kuwazuia kufanya kile wangeweza kufanya katika kusonga mbele katika njia inayofaa. Shetani anafanya kazi ili kuwapinga wale wanaozishika amri za Mungu na wana imani ya Yesu Kristo. Chuki kuu yenye jazba ipo moyoni mwake dhidi ya wote ambao ni

waaminifu kwa Mungu na wanaotii amri Zake. Adui hasinzii; na wala hatulii kwa uangalifu wake hata kwa dakika moja. Laiti wale wanaodai kuwa wafuasi wa Mungu wangekuwa wenye busara, bidii, na wavumilivu katika kazi ya Mungu hata kama ni nusu ya vile Shetani alivyo katika kazi yake. 3T 456.1

Endapo wewe, Ndugu B, ungeendelea kufuata na kusonga mbele wakati ulipoweka mkono wako kwenye plau, na usitazame nyuma, sasa ungekuwa mjumbe wa nuru ili kubeba Ukweli kwa wale walio gizani. Lakini Mungu hawezi kukutumia katika utukufu Wake mpaka pale utakapojifunza kushauriana na ndugu zako na siyo kufikiri kwamba unajua mambo yote ambayo yalistahili kujulikana. Shetani amefanikiwa kukuzuia usitende mema. Ulianza vizuri kwa msimu, lakini majaribu ya Shetani yalikushinda. Ulipenda kuwa wa kwanza na kusifiwa-sifiwa-kubembelezwa. Ulipenda nguvu ambayo pesa huitoa. Shetani anaelewa na kuujua udhaifu wa watu na ana ujuzi ambao ameukusanya kwa miaka mingi na ni mashuhuri katika kazi yake (6000!) Ujanja na udanganyifu wake umekomaa vizuri, na mara nyingi hufanikiwa kwa sababu watu wa Mungu si werevu kama nyoka. 3T 456.2

Mara nyingi Shetani huonekana kama malaika wa nuru, akiwa amevaa mavazi ya kimbingu; yeye hujifanya kuwa rafiki wa kweli, akidhihirisha utakatifu mkubwa wa tabia na heshima kubwa kwa wahanga wake, roho ambazo huzidanganya na kuziharibu. Hatari iko katika njia anayoialika roho kusafiri kwayo, lakini anafanikiwa kuificha na kutoa vivutio tu. Nahodha mkuu wa wokovu wetu ameshinda kwa niaba yetu, ili kupitia Yeye tupate kushinda, kama ambavyo tungeshinda wenyewe. Lakini Kristo hamlazimishi mtu yeyote ili aweze kumuokoa mpaka pale atakapoamua na kuchagua mwenyewe; Hamlazimishi mtu yeyote kumtii. Alitoa dhabihu isiyo na kikomo ili waweze kushinda kwa Jina Lake na haki Yake ihesabiwe kwao. 3T 456.3

Lakini ili uokolewe ni lazima ukubali nira ya Kristo na uondoe nira ambayo umejitengenezea na kuvaa shingoni mwako. Ushindi ambao Yesu aliupata jangwani ni ahadi kwako juu ya ushindi ambao unaweza kuupata kupitia Jina Lake. Tumaini lako pekee/tu na wokovu wako ni kushinda kama Kristo alivyoshinda. Hasira ya Mungu sasa inaning'inia juu yako. Unapenda anasa za ulimwengu huu dhidi ya hazina za mbinguni. Tamaa ya jicho, na kiburi cha ya maisha vimekutenganisha na Mungu. Ujasiri wako katika umaskini wako mwenyewe, udhaifu, lazima vivunjike. Lazima ujisikie kuwa udhaifu kabla ya kushuka, pamoja na mzigo wako, mikononi mwa Mungu. Nafsi inayomtegemea kabisa na kujitoa kikamilifu kwa Mungu haitaaibika kamwe. 3T 457.1

Mungu hatatutaka tujipunguzie masumbufu yetu tunavyotaka mwenyewe, pasipo kumtii. Kristo hakujifurahisha mwenyewe pindi alipokuwa akiishi kama mwanadamu miongoni mwa watu ulimwenguni. Alikuwa mtu wa huzuni na aliyejawa na majonzi. Mkuu wa mbinguni hakuwa na mahali pa kulaza kichwa

Chake, na hakukuwa na mahali ambapo angeweza kudai kuwa Pake. Alifanyika maskini kwa ajili yetu, ili kupitia Yeye tuwe matajiri wa kwelikweli. Hebu tusizungumze juu ya dhabihu, kwani hatujui nini maana ya kujitoa kwa ajili ya Kweli. Kwa kuwa bado hatujauinua msalaba kwa ajili ya mpendwa wetu Kristo. Tusitafute njia ambayo ni rahisi kuliko njia ambayo Mkombozi wetu amesafiri mbele yetu. Je! Wewe una uwezo gani, na hekima yako yote ya kujivunia, kujiongoza? Unawajibikaje kufuata maagizo na dhamiri iliyodanganywa, kukimbilia katika njia ya makosa, na kuwaburuza wengine pamoja nawe! 3T 457.2

Tabia yako ya asili hufanya utii na unyenyekeaji kwa matakwa ya Mungu kuwa mgumu sana. Kujiamini kwako bila mipaka, chuki, ubaguzi na hisia zako hukuongoza kwa urahisi kuchagua njia mbaya. Kristo atakuwa Mwongozo wako usiokosea ikiwa tu utamchagua awe juu ya uamuzi wako wenye upofu. Katika shuguli zako haujakaza jicho lako kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Umekuwa na shida nyingi na umekutana na magumu mengi, na ikiwa ungemwamini Mshauri wa Kweli badala ya uamuzi wako mwenyewe, ungeweza kuongozwa katika shida zako na shughuli na biashara zako za kazi daima. 3T 457.3

Una kazi muhimu mbele yako ambayo huwezi kuifanya bila msaada maalum kutoka kwa Mungu. Unao uwezo wa kupata ushirika wa malaika na kuwa mrithi wa Mungu, mrithi pamoja na Yesu Kristo; na ili uweze kufanya kazi ya kuminya mipaka ya tumaini na shauku ndani ya dira nyembamba ya unafuu wako, litakuwa kosa la maisha yote. Ni makosa makubwa sana kuishi tu kwa ajili ya ulimwengu huu. Unatazama nyuma na kuhisi kulaaniwa kwa njia zako mbaya, na unatafuta kujihesabia haki kwa kutafuta kujilinganisha na wengine na kutafuta makosa yao. Haijalishi njia yoyote au hatua zile ambazo watu wengine wanaweza kuifuata, au hata iwe mbaya kiasi gani, makosa yao hayatafunika kamwe moja ya makosa yako; na siku ya kutoa hesabu ya mwisho hutathubutu kuomba mbele ya Mungu kama kitulizo kwa kupuuza kwako wajibu wako. 3T 458.1

Mungu anapendekeza kukukubali kama mtoto Wake na kukufanya wewe uwe mshiriki wa familia Yake ya kifalme, mtoto wa Mfalme wa mbinguni, kwa masharti ambayo utajitenga kutoka ulimwenguni na kuwa tofauti na usiguse kitu kilicho najisi. Mfalme wa mbinguni angependa umiliki na ufurahie kila kitu kinachoweza kukuza, kupanua, na kutukuza utu wako na kukupa stahiki/sifa kukaa Naye milele, kuishi kwako kuendane na maisha ya Mungu, yaani uishi milele kama Yeye. Maisha yajayo yana matarajio ya ajabu iliyoje! Yanafurahisha kiasi gani ndani yake! Jinsi upendo wa Mungu ulivyo mpana na wa kina na usio na kipimo umeoneshwa kwa mwanadamu! Hakuna maneno yanayoweza kuelezea upendo huu; unazidi fikira na mawazo yote, lakini ni Uhalisia ambao wewe unaweza kujifunza kwa uzoefu; unaweza kufurahi ndani yake kwa furaha isiyoelezeka na iliyojaa utukufu. 3T 458.2

Ukiwa na matarajio kama hayo mbele yako, unawezaje kuifanya akili yako kuwa finyu katika dira ya mawazo ya ulimwengu na katika kazi za ulimwengu, ukitafuta

mali, na ubatili na kusalimisha pointi moja baada ya nyingine ya Ukweli wa sasa. Ukweli, kanuni, na dhamiri ni muhimu na za kutamanika kubaki kwako. Neema na kibali cha Mungu ni bora kuliko nyumba za fedha na dhahabu. Furaha ya ndani kabisa ya moyo hutoka katika kujidhili kwa ndani kabisa. Kuamini na kujitiisha kwa Mungu huleta nguvu na utu, na ubora wa tabia. Machozi siyo katika kila hali hudhibitisha udhaifu. Ili uweze kujenga tabia ambayo inakubaliwa mbele za Mungu, tabia safi na takatifu ni lazima uanzie kwenye msingi. Moyo lazima uvunjike mbele za Mungu, na toba ya Kweli kwa dhambi lazima ioneshwe, mpaka utimize mahitaji ya Ukweli na wajibu. Kisha utakuwa na heshima ya kweli kwako mwenyewe na ujasiri wa kweli kwa Mungu. Utakuwa na huruma na hisia nyeti. Roho yote ya majigambo itakuwa imetoweka. Mahali pa ukali na ujeuri kutakuwa na huruma kubwa iliyochanganywa na uthabiti wa kusudi, kusimama kwa Ukweli katika matukio yote. Ndipo utakapoona mengi ulimwenguni na moyoni mwako ya kukufanya ulie machozi. 3T 458.3

SURA YA 37

USAFISHWAJI WA KWELI KATIKA HUDUMA

Ndugu E, nilikusudia kukuandikia kwa muda mrefu, lakini sikupata fursa ya kufanya hivyo hadi sasa. Wakati nilipokuwa nikizungumza na waumini Sabato iliyopita, nilihisi kugusa moyo sana na kesi yako kiasi kwamba nilishindwa kujizuia kuliita jina lako hadharani. Sasa nitaifungua akili yangu na kukuandikia. Katika maono yangu ya mwisho nilioneshwa upungufu wa wale wanaodai kufanya kazi kwa Maandiko na Mafundisho ya imani. Niliona ya kwamba uwezo wako haukuzidi

kuboreka/kuimarika, lakini ulizidi kupungua mara kwa mara katika ufanisi wa kuufundisha Ukweli. Unahitaji uongofu kamili, una nia isiyotaka kubadilishwa ndani yako ambayo huonekana katika tabia ya ukaidi. Endapo ungekuwa si mtu wa kujiinua na kujiamini, ukawa mnyenyekevu na mpole wa roho, ungekuwa umeshafaa kupata stahiki ya kufanya kazi maalum ya kuufikisha ujumbe wa Ukweli kwa wengine. 3T 459.1

Hupendi kujituma wala kuwekeza jitihada katika kazi zinazoendelea. Hujawa mwanafunzi wa kudumu wa Neno la Mungu, wala kuwa mfanyakazi mwenye bidii katika kazi ya Mungu. Maisha yako yamekuwa mbali na uwakilishi wa maisha ya Kristo. Hupambanui mambo. Wewe siyo mfanyakazi mwenye maamuzi ya busara. Hujifunzi kuongoa roho kwa Kristo, kama ambavyo kila mtenda kazi wa Kristo anapaswa. Una njia ulizojipangia mwenyewe, viwango vyako mwenyewe, ndizo unatamani uzitumie kuwaleta watu; lakini unashindwa kuzitumia hizi kwa sababu hawatakikubali kiwango chako. Wewe ni mtu mwenye itikadi kali na mara nyingi hubeba vitu kupita kiasi, hivyo basi unaliharibu sana kusudi la Mungu na kupotosha roho katika Kweli badala ya kuongoa. 3T 459.2

Nilioneshwa kuwa umeharibu fursa kadhaa nzuri kwa njia yako mbaya ya ufanyaji kazi, nami nitasema nini kwako kuhusu jambo hili? Roho zimepotea kwa sababu ya kukosa kwako hekima katika kuwasilisha Kweli na kushindwa kuupamba wito wako kama mhubiri wa injili kwa adabu, wema, na uvumilivu. Heshima ya Kweli na uungwana wa Kikristo inapaswa kuonesha matendo yote ya mhudumu wa Kristo. Oh, ni kwa ubaya wa kiasi gani umemwakilisha vibaya sana Mkombozi wetu Mwenye huruma, ambaye maisha Yake yalikuwa mfano wa wema na usafi wa Kweli. Umezitoa nje ya njia roho katika Kweli kwa roho ya ukali, ukosoaji, na udhalimu. Maneno yako hayakuwa katika uungwana, ulaini na upole wa Kristo, bali katika nguvu na roho ya ndugu E. Kwa asili huna adabu, jeuri na hujastaarabika, na kwa sababu haujawahi kuuhisi umuhimu wa utakaso wa Kweli na upole wa Kikristo, maisha yako hayajawahi kuinuliwa kama ipasavyo. 3T 460.1

Umebaki katika korongo la mazoea yasiyo na tija. Elimu na mafunzo yako hayakuwa sahihi, hivyo basi juhudi zako zingepaswa kuwa za dhati na bidii zaidi ili kustawi, kuboresha, kurekebisha, kutengeneza na kufanya mabadiliko na uamuzi thabiti. Mpaka utakapogundua na kuamua kuongoka kweli kweli katika kila nyanja ndipo utakapostahili kuuhubiri Ukweli, na pasipo kuwa na tabia ifaayo, iliyoinuliwa na sifa njema, vizuri katika mwenendo, na utakuwa na uwezo wa kufanya madhara tu zaidi ya mema. Hujafanya kazi nzuri katika kuueneza Ukweli, kwani umekuwa ukirandaranda na kujikalisha-kalisha katika makanisa kwa muda mrefu wakati hukuweza kufanya jema katika makanisa hayo, bali ni kujeruhi tu. Njia zako, adabu na mazoea yako yahitaji kusafishwa na kutakaswa. Hupaswi tena

kuiharibu kazi ya Mungu kwa mapungufu yako, kwani haujaonesha azimio lolote la kuboreshwa ili uwe mfanyakazi katika kusudi la Mungu. 3T 460.2
Haiwezekani kwako wewe kuwainua wengine katika kiwango chochote cha juu kuliko kile ulichonacho wewe. Ikiwa huimariki au huboreki na kusonga mbele, unawezaje kuliongoza kanisa la Mungu mbele kwa kiwango cha juu cha utauwa na utakatifu? Wahubiri wote walio kama ulivyokuwa wewe kwa miaka kadhaa sasa ni laana kuliko baraka kwa kazi ya Mungu, na kadiri wanavyozidi kuwa wachache ndivyo kazi ya injili ya Ukweli wa leo itakavyozidi kustawi. 3T 461.1

Mawazo yako na kazi zako, hazijaboreshwa wala kuvutia. Umeridhika kuwa wa kawaida na kuwa mchungaji usiye na thamani wa ovyo hovyo tu {cheap Pastor}. Hauutamani ukamilifu wa tabia ya Kikristo na ile nafasi katika kazi ambayo Kristo anahitaji kila mmoja wa watumishi Wake waliochaguliwa kuifikia. Hakuna mtu yeyote anayedai kuubeba Ukweli kwa wengine anafaa katika kazi ya utume isipokuwa anakuwa katika ufahamu na kujitolea kwa kazi hiyo, na kuendelea kuborea na kuimarika kitabia na hulka, na kukua katika hekima ya Kweli siku hadi siku. Ushirika wa karibu na Mungu ni muhimu kwa kila mtu ambaye ataongoza roho katika Kweli. Wale wanaochukua jukumu la kuziongoza roho kutoka katika giza la asili hadi kwenye nuru ya ajabu wanapaswa kusonga mbele kwa kuzingatia kila siku ya kwamba nao wanakuwa katika nuru, vinginevyo wangewezaje kuwaongoza wengine? Ikiwa nao wanatembea gizani, wafahamu kuwa wamejiingiza katika jukumu la kuogofya zaidi ambalo wanadhani kwa kuigiza huwafundisha wengine njia. 3T 461.2

Umejiingiza kufanya kazi mahali ambapo hukuwa na uwezo wa kuifanya kazi kwa haki. Hukufanya kazi kwa busara. Ulijaribu kujificha kwenye kichaka cha ukosefu wako wa maarifa kwa kuyakemea madhehebu mengine, kuwadharau wengine, na kuikosoa mienendo yao na hali zao kwa ukali na uchungu. Endapo moyo wako ungemulikwa siku zote kwa roho wa Kweli, kama ungekuwa umetakaswa na Mungu na kutembea katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru, ungetembea katika hekima na ungekuwa na njia, mali, mbinu na uwezo za kutosha ndani ya uwezo wako katika kukusaidia kubaki katika Kweli bila kukosea njia na kwenda kinyume na kazi yako maalum kwa kuwakashifu wengine wanaodai kuwa ni Wakristo. 3T 461.3

Wasioamini wamechukizwa; wanafikiri kuwa Waadventista Wasabato wamewakilishwa na wewe kikamilifu, na wameamua ya kuwa sasa inatosha, na hawahitajii tena mafundisho ya imani kama hayo. Imani yetu haipendwi kabisa na watu wengi na ni tofauti kabisa na imani na mazoea ya madhehebu mengine. Ili kuwafikia wale walio katika giza la upotofu na nadharia za uwongo, lazima tuwafikie kwa tahadhari kubwa na kwa hekima kubwa, tukikubaliana nao kwa kila pointi tuyoweza kwa dhamira zenye uangalifu. 3T 462.1

Tunapaswa kuwafikia karibu na kwa tahadhari na umakini wale walio katika makosa, na kuwapa sifa stahiki kwa uaminifu wao katika vile vipengele wanavyofanya vyema. Tunapaswa kujenga uhusiano wa karibu iwezekanavyo na watu hawa, ili waweze kupata faida ya nuru na Kweli tuliyo nayo. Hata hivyo, Ndugu E—kama ilivyo kwa wachungaji wengi miongoni mwetu—huanzisha vita mara moja dhidi ya makosa ambayo wengine wanayashikilia katika imani zao; kwa kufanya hivyo, anachochea roho yao ya kupambana, malumbano na ukaidi wa matakwa yao wanayoyaamini. Hali hii huwafanya kujivika kinga na silaha za chuki-binafsi, ambayo hata tuwe na ushahidi mwingi kiasi gani wa Maandiko, hauwezi kuondoka. 3T 462.2

Je, ni nani kama si wewe mwenyewe utakayewajibika kwa ajili ya roho ambazo umezipotosha katika Kweli kwa sababu ya kazi zako za utume zisizotakaswa? Ni nani awezaye kuvunja kuta za ubaguzi ambazo kazi yako isiyo ya busara imezijenga? Siijui dhambi yoyote iliyo kubwa zaidi dhidi ya Mungu kama watu kushiriki katika utume wakijitumikia wenyewe na si katika Kristo. Wanaonekana kama wawakilishi wa Kristo, wakati hawaiwakilishi Roho Yake katika kazi zao zozote. Hawaoni wala kuzitambua hatari zinazoambatana na juhudi zinazofanywa na watu wasiowekwa wakfu na kuongoka. Huishi kama vipofu, wakipungukiwa karibu kila kitu lakini bado wakijiamini na kujitosheleza wenyewe, wakitembea wenyewe gizani na kujikwaa katika kila hatua. Wao ni miili ya giza- wao ni giza tu. 3T 462.3

Ndugu E, una mawazo finyu sana, na kazi yako ina tabia ya kuuhafifisha Ukweli badala ya kuuinua. Hii si kwa sababu hauna uwezo. Ungewezakuwa mfanyakazi mzuri u, ila wewe ni mvivu sana wa kufanya jitihada zinazohitajika kufikia malengo hayo. Kwako ni heri kuwashukia watu kwa ukali na jeuri pale wanaotofautiana nawe kuliko kuikubali shida ya kuiinua kiwango cha kazi yako ya utume. Unajichukulia misimamo fulani, na unapohojiwa juu ya hiyo misimamo, wewe siyo mnyenyekevu vya kutosha katika kuyaacha maoni yako ingawa huwa si sahihi; lakini wamama huru na wengine, ukijitegemea na kushupaa sana kwa maoni yako wakati jukumu linalohitajika kwako na la muhimu ni kukubali na kubadilika. Kwa ukaidi na kutokukubali kushindwa umeushikilia uamuzi wako binafsi na maoni yako kwa dhabihu ya uangamivu wa roho za watu. 3T 462.4

Ndugu E, misimamo yako isiyobadilika na maoni yako na nia yako thabiti, ya kusimamia maoni yako kwa namna yoyote ile ya hatari bila kujali gharama, ilihisiwa na kumchukiza mke wako, na afya yake ilidhoofika na hilo. Hukumhurumia wala kumjali binti huyu wa pekee mwenye moyo nyeti wa Mungu mwenye hisia nyeti; roho yako ya ukali iliizidi tabia yake ya upole. Alihuzunika juu ya mambo mengi. Ungeweza kuyafanya maisha yake kuwa ya furaha zaidi endapo

ungejaribu; lakini ulihitaji akubaliane na fikra zako kama ulivyoona, na, badala ya kujaribu kujistaarabisha mwenyewe katika mwenendo wake uliyosafishwa, ulijaribu kumuongoza katika hali yako na mawazo yako mabaya na jeuri. Alipotoshwa na hukuweza kusimama katika imani mwenyewe. Aliinamana na kukauka kama mmea uliopandikizwa kwenye ardhi isiyo na rutuba au isiyofaa ukuaji mwema kwa mmea. 3T 463.1

Usijaribu kubadili akili/fikra na tabia za watu vile utakavyo, bali ruhusu tabia yako itengenezwe na kuwa kama ile ya mbingu. Endapo hii dunia ingekuwa na wanaume wenye tabia na silika kama yako, ole! Ingejaa na masikitiko. Mahali popote ambapo ungepita, ungekutana na maudhi ya watu wenye tabia kama zako na ungetamani usiwepo duniani. 3T 463.2

Unajigamba na kujisifu. Oh, ni kwa namna gani hali hii haifai kwa mwanadamu yeyote, hata ikiwa ana sifa na uwezo mzuri wa kufikiri na ushawishi wa hali ya juu! Wanaume wenye sifa nzuri wana ushawishi mkubwa kwa sababu hawaijui thamani yao na ni mambo mangapi mazuri wanayoyatimiza ulimwenguni. Lakini yote hayafai kwa wanaume wa aina ya tabia kama yako wanaotafuta kujikweza na na kujisifu wenyewe. 3T 463.3

Mara nyingi kazi yako huanza vizuri katika utendaji, unapohubiri injili; unainua shauku za watu, na kuwasadikisha watu kuwa hoja zinazotumika haziwezi kupingwa; lakini katika nyakati ambazo roho za watu kiko katika mizani na zinautafakari Ukweli, ubinafsi huanza kuonekana kwa uwazi kabisa, kiasi kwamba yote ambayo wangeweza kuyapata na kujifunza, endapo Yesu angeangaza katika maneno na mwenendo wako, hupotea.3T 464.1

Unakosa neema zile ambazo ni muhimu katika kuongoa roho kwa Kristo na Ukweli. Una uwezo wa kujenga hoja vizuri na kufanya mabishano; lakini huna ujuzi wa kutosha wa mapenzi ya Mungu, na kwa kukosa uzoefu mzuri wa kidini hauwezi kuwaongoza wengine kwenye chemchemi ya maji ya uzima. Nafsi yako haijashikamana na Mungu, bali ipo gizani; na hakuna chochote kinachoweza kutambua na kujaza mahali panapoonekana kuwa na upungufu wa roho zinazopapasa gizani, isipokuwa nuru ya Kweli. Pasipo kuongoka kabisa, juhudi zako za kuwaongoa wengine bora zikome sasa, kuliko kufanya kazi kwa muda mrefu, huku ukiharibu na kuipotosha misingi viwango vya dini kwa mawazo yako hafifu, finyu, na misimamo mikali. Huna uzoefu mzuri wa mapenzi ya Mungu; haki na uadilifu wako mwenyewe huonekana kuwa ya thamani sana kwako, wakati hayana

thamani. Unahitaji kubadilishwa kabla ya kutumika kwa manufaa katika kusudi la Mungu. Utakapoongoka ndipo utakapoweza kufanya kazi inayokubalika. 3T 464.2

Humiliki dini ya Kristo. Wapaswa kuulainisha moyo wako na kujikana nafsi, na Kristo lazima aishi ndani yako; ndipo utakapotembea katika nuru kama Yeye alivyo katika nuru, nawe utaacha nyayo angavu kuelekea mbinguni ili kuwaangazia wengine kwenye nuru. Umeridhika sana na namna ulivyo. Wapaswa kuelimika na kuishinda roho yako yenye itikadi kali na ya kutafuta makosa. Unapaswa kujisalimisha mwili na kuutiisha, isije, baada ya kuwahubiria wengine, nawe ukakataliwa. 3T 464.3

Unachukua mawazo madogo katika mambo kadha wa kadha [kuchuma majani/pick straws], kukosoa na kuyapinga na kuhoji mambo ya wengine, wakati ambao ungekuwa bora zaidi kwako kuzishinda kasoro zilizo katika tabia na maisha yako, ukifanya kazi kwa mtazamo wa Kikristo, kuitafuta nuru kutoka kwa Mungu, na kujiandaa kuungana na malaika safi katika ufalme wa mbinguni. Kwa jinsi ulivyo, unaweza kuiharibu mbingu yote. Huna tabia njema, hujaboreshwa, haujasafishwa wala kutakaswa. Hakuna nafasi mbinguni kwa tabia kama hii unayoimiliki sasa. 3T 464.4

Ikiwa utaifanya kazi kwa bidii na, bila kuwa na udhuru wa kutenda dhambi, utakapoilaani dhambi katika mwili na kufikia imani na matumaini ya neema ya Mungu na hukumu sahihi, unaweza kuyashinda mapungufu yaliyo katika tabia yako ambayo hayakupi stahiki kuifanya kazi ya Mungu. Haujaendelea wala kuwa bora kwa miaka mingi. Hivi leo uko mbali zaidi kutoka katika kiwango cha ukamilifu wa Kikristo, katika kuwa na sifa ambazo zinapaswa kupatikana kwa mchungaji/mtumishi wa injili, kuliko vile ulivyokuwa miezi michache baada ya kuupokea Ukweli. 3T 465.1

Mungu huchukizwa na wale ambao hawaendi kwa akili katika masuala ya dini ya Kikristo na bado wanajaribu kuwaongoza wengine. Wewe unawakilishwa kwa usahihi kabisa na yule mtu aliyejaribu kutoa kibanzi katika kwa jicho la ndugu yake wakati alikuwa na boriti katika jicho lake. Rekebisha kwanza moyo wako, na kuisalimisha na kuitengeneza tabia yako; tafuta muunganiko/uhusiano na Mungu, na uupate uzoefu wa kila siku wa Kikristo; ndipo utakapoweza kuibeba mizigo ya roho zisizomjua Kristo.3T 465.2

Wapo baadhi ya ndugu wanaochukua muda mwingi kusoma nakala za waandishi tofauti kuliko wewe, na bado huna sifa zinazohitajika kuihubiri injili. Hujui kunukuu, wala kusoma Maandiko kwa usahihi. Jambo hili si sahihi, haipaswi kuwa hivi. Hujastawisha utamaduni wa akili naneema ndani ya nafsi yako ambayo ingemulika katika maneno na mwenendo wako haijakua. Bado hujauhisi umuhimu wa kufikia mafanikio ya hali ya juu ya utakatifu. 3T 465.3

Kukimbiza-kimbiza vitabu kwa kuvisoma soma kwa juu juu tu huziba na kupumbaza akili na husababisha kuvimbiwa kwa ubongo (kudhuru ubongo kwa kulundika vitu

vingi visivyocheuliwa vyema). Huwezi kumeng'enya na kutumia moja na nusu ya kile ulichosoma endapo unahitaji kusoma kwa sababu ya lengo moja tu la kuboresha akili basi wapaswa kusoma na kuongeza maarifa kwa wingi, kiasi akili inavyoweza kuhimili, ndipo utakapoweza kuwa mvumilivu na kustahimili katika zoezi hilo la usomaji, kisha utakuwa na matokeo na maendeleo mazuri. Wewe, pamoja na wachungaji wengine, mnatakiwa kuhudhuria shule na kuanza kujifunza kama mtoto ili kuelewa matawi ya awali vya maarifa RRR
[Reading, Riting, Rithmetic]. Bado huna uwezo wa kusoma, kuandika, wala kutamka kwa usahihi maneno, lakini bado wapo wachache walio na mizigo michache na majukumu ya kukabiliana nayo kuliko wewe. 3T 465.4

Nafasi ya wachungaji au watumishi wetu inahitaji afya ya mwili na nidhamu ya akili. Fikra nzuri zenye hekima, ujasiri, hulka ya mishipa ya fahamu yenye utimamu, na moyo mchangamfu vitamfaa mtumishi wa injili mahali popote. Haya yanapaswa kufuatwa na kudumu kuendelezwa. 3T 466.1

Maisha yako hadi sasa yamekuwa hayana faida. Una mawazo kadhaa mazuri sana, lakini Roho wa Mungu haishi ndani ya moyo wako. Hauhuishwi na nguvu Yake, na huna imani ya Kweli, tumaini, na upendo. Roho wa Kristo akikaa ndani yako atakuwezesha kuibeba nuru ya Mungu na kuwafunulia wengine. Huwezi kuwa na faida yoyote katika kazi ya Mungu mpaka pale kazi ya mchungaji mwaminifu wa Kristo itakapotukuzwa zaidi akilini mwako. Unahitaji madhumuni/kusudi maishani mwako la kutenda mema, kama Yesu. Kujikana nafsi na upendo ambao utauonesha katika kazi hii utayaelezea maisha na tabia yako kwa wengine. 3T 466.2

Unapaswa kuuundoa haraka tabia yako ya urasimi ambao una ubaridi, roho isiyo ya kirafiki, uliouzoea haraka iwezekanavyo. Unapaswa kukuza hisia za upole, huruma nyororo, kujali na urafiki katika maisha yako ya kila siku. Unapaswa kuonesha staha, adabu ya kweli na uungwana wa Kikristo. Moyo unaompenda Yesu kweli kweli huwapenda na wale Yeye aliowafia. Kama vile sindano inavyoelekeza katika ncha kwenye dira (compass), ndivyo ilivyo kwa mfuasi wa Kweli wa Kristo, kwa roho ya dhati na bidii ya kazi, avyotatafuta kuokoa roho ambazo Kristo amezifia kwa kutoa maisha yake. Kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa wale walio dhambini kutauhifadhi upendo wa Kristo ndani ya moyo na kutaupatia huo upendo maendeleo na ukuaji mzuri. Bila uelewa sahihi wa mapenzi ya Bwana kutakuwa na ukosefu wa maendeleo mazuri yenye ulinganifu katika tabia ya Mkristo. 3T 466.3
Ninakusihi, ndugu yangu, mfahamu Mungu. "Hatua za mtu mwema huongozwa na Bwana." Malaika huchukua rekodi ya kila hatua ya maendeleo yetu. Lakini nia na mapenzi yako hayajasalimishwa kwa Mungu; mawazo yako siyo matakatifu. Unaendelea, na kujikwaa gizani, bila kujua mahali pa kuweka miguu yako. Bwana hufunua mapenzi Yake kwa wale walio dhati na bidii na wanaotamani kuongozwa. Sababu ya kushidwa kwako ni kwamba umeliacha wazo la kumjua Mungu na

kufanya mapenzi Yake, Hivyo basi hujui lolote kwa usahihi. Japo u kipofu, unashiriki katika kuwaongoza vipofu. 3T 466.4

Oh masikini, Je, uko katika nafasi gani wewe na wachungaji/watumishi wengine wengi! Baada ya kumwacha Mungu, chemchemi ya maji yaliyo hai, wewe pamoja na wao mmejichimbia visima vilivyovunjika visivyoweza kutunza maji. Ninakusihi uamke, chukua tahadhari na umrudie Bwana kwa toba ya dhati ambayo itakupa msamaha Wake na nguvu ya kudumu ya Uweza Wake, ili ujazwe kwelikweli na utimilifu wote wa Mungu. Bwana Anachukizwa na kazi zako, kwa maana umekuwa kama kikwazo kwa roho za watu. Umezitegemea kazi zako mwenyewe na haki yako katika mafanikio, na huna maarifa ya mapenzi ya mbingu. 3T 467.1

Acha Bwana na akufunulie tabia yako ya Kweli nawe uyaone mapungufu yako halisi. Utakapoangaziwa na Roho wa Mungu kuyaelewa haya utaifahamu hali yako ya kupuuzia dhambi na maisha yako yasiyoboreshwa kwani utapata hofu moyoni mwako na huzuni ambavyo itapelekea toba ambayo haitaleta majuto. 3T 467.2

SURA YA 38

UMUHIMU WA KAZI

Januari 3, 1875, nilioneshwa vitu vingi vinavyohusisha maslahimakubwa na muhimu huko Battle Creek katika Shirika la Uchapishaji, shule, na Taasisi ya Afya. Endapo taasisi hizi zingeendeshwa vizuri, zingeendeleza sana kusudi la Mungu katika uenezwaji wa Ukweli na wokovu wa roho. Tunaishi katikati ya hatari za siku za mwisho. Kujiweka wakfu kwa Mungu pekee ndiko kunakoweza kumfaa yeyote kati yetu kushiriki katika kazi ya utume na ya muhimu katika nyakati hizi za mwisho. Wapo watu wachache tu wasio na ubinafsi wanaoweza kuwajibika katika nafasi hizi, wachache waliojitoa kikamilifu kwa Mungu ili kuisikia sauti Yake na kujifunza utukufu Wake. Wapo watu wachache tu ambao, ikiwa watahitajika, watayatoa maisha yao ili kuendeleza kusudi la Mungu. Walakini ni ibada na kujitoa kama huko ambako Mungu anaihitaji. 3T 468.1

Watu wanadajinganya wenyewe kwa kudhani ya kuwa wanamtumikia Mungu wakati wanajitumikia wao wenyewe na kulifanya kusudi la kazi ya Mungu kuwa jambo la pili. Mioyo yao haijawekwa wakfu. Bwana hazifurahii huduma za watu wa namna hii. Kwa nyakati tofauti kadiri kusudi la injili linavyozidi kukua, Yeye kwa hekima Zake amewateua watu kujaza nafasi mbalimbali huko Battle Creek. Watu hawa wangeweza kujaza nafasi muhimu kama wangejiweka wakfu kwa Mungu na kutoa wakfu nguvu zao kwa kazi Yake. Watu hawa ambao ndio uchaguzi wa Mungu, walihitaji nidhamu ambayo kujitolea kwa kazi Yake kungewapa. Angewaheshimu kwa kuwaunganisha naye na kuwapa Roho Wake Mtakatifu ili awastahilishe kwaajili ya majukumu waliyoitiwa. Wasingeweza kuwa upana na uzoefu wa kupokea na kuvumilia fikra tofauti na maarifa ya mapenzi ya Mungu hadi watakapokuwa na uwezo wa kubeba mizigo na majukumu. 3T 468.2

Asiwepo wa kudanganywa kwa kufikiria kuwa kwa kuungana na kazi ya Mungu huko Battle Creek watakuwa na masumbufu madogo, kazi nyepesi, na majaribu machache. Shetani yupo hai na hujibidisha sana mahali ambapo kazi ya Mungu inafanywa sana ili kukuza Ukweli na kuongoa roho. Anaielewa asili ya binadamu, na hatawaacha watu hawa peke yao ikiwa kuna matarajio yoyote ya kuwa kama Kristo na wafanyakazi wanaofaa zaidi katika kusudi la Mungu. Shetani huweka mipango yake na kushinikiza majaribu juu ya watu hao hao ambao Mungu amewachagua na kuwakubali kushiriki katika kazi Yake. Ni somo na utafiti mkuu wa Shetani kujua ni jinsi gani anaweza kupambana vizuri zaidi na kuyashinda makusudi ya Mungu. Ana uzoefu na udhaifu vile vile na uthabiti wa tabia ya wanadamu. Na kwa hila anafanya kazi kwa udanganyifu na udhalimu wote ili kuyakwamisha malengo ya Mungu kwa kushambulia vipengele dhaifu katika tabia zao; na baada ya hilo, njia huandaliwa ili ashambulie na kuvishinda vipengele vyao thabiti. Huidhibiti akili na kuupofusha ufahamu. Huwaongoza wanadamu waliotatanishwa na kushindwa na hila na mitego yake katika kujiamini na kujitosheleza huku wakiwa ni dhaifu sana kimaadili. Hujidanganya wenyewe na kufikiri kuwa wako katika hali nzuri ya kiroho. 3T 469.1

Adui atapokonya kila fursa anayoweza kupata ili atumie kwa manufaa yake na kuharibu roho. Shuhuda zimetolewa kwa niaba ya watu wanaoshika nyadhifa muhimu. Huanza vizuri kazi ya kuiinua mizigo na kutenda kwa nafasi yao wakishikamana na kazi ya Mungu. Lakini Shetani huwaandama na majaribu yake, na mwishowe hushindwa. Wakati wengine wakitazama mienendo yao mibaya, Shetani huleta pendekezo akilini mwao kuwa kuna makosa katika shuhuda zinazotolewa na hao watu, la sivyo watu hao wasingejidhihirisha kuwa hawafai kushiriki katika kazi ya Mungu. 3T 469.2

Hivi ndivyo Shetani alivyopanga iwe. Huweka shaka katika nuru aliyoitoa Mungu. Watu hawa wangeweza kuhimili vishawishi vya Shetani endapo wangekuwa waangalifu na wenye ulinzi wakikesha, wakihisi kutojitosheleza kwao, na kuliamini Jina na nguvu za Yesu kusimama kwa uaminifu katika majukumu. Lakini inapaswa kuwekwa akilini kwamba masharti wanayopewa watu hawa huenda sambamba na masharti kadha wa kadha, ya kwamba kama wangeidumisha roho ya kutokuwa na ubinafsi, kama wangeuhisi udhaifu wao na kumtegemea Mungu, bila kuitegemea hekima na uamuzi wao, lakini wakimfanya Yeye kuwa nguvu yao, wangeweza kuwa mbaraka mkubwa katika kusudi na kazi Yake. Lakini Shetani amekuja na majaribu yake na ameshinda karibu kila wakati. Adui amepanga mazingira ya kushambulia sehemu dhaifu katika tabia za watu hawa, na wameshindwa. Ni aibu kiasi gani wameliharibu kusudi la Mungu! Ni kwa namna gani wamejitenga Naye kabisa kwa kufuata mioyo yao fisadi, roho zao zinaweza kujibu haya! Lakini siku ya Mungu itadhihirisha sababu za Kweli za masikitisho yetu

yote na kukatishwa tamaa. Mungu hana makosa. Aliwapa ahadi za kutia moyo juu ya masharti yote, lakini hawakutii masharti haya. Waliziamini nguvu zao wenyewe, nao wakaanguka majaribuni. 3T 469.3

Yanayowezwa kusemwa juu ya binadamu katika hali fulani hayawezi kusemwa juu yao katika mazingira mengine. Binadamu ni dhaifu katika nguvu za maadili na wana ubinafsi wa hali ya juu, hujitosheleza wenyewe na hujazwa kwa kiburi kwa urahisi na majivuno ya bure, kiasi kwamba Mungu hawezi kufanya kazi pamoja nao, hivyo huachwa watembee kama vipofu na kudhihirisha udhaifu na upumbavu mkubwa sana kiasi kwamba wengi hushangazwa na watu kama hao kwamba imekuwaje wakubaliwe na watambuliwe kuwa na stahiki ya kushiriki au kuunganishwa katika kazi ya Mungu yoyote. Hiyo ndiyo mipango ya Shetani. Hili ndilo lililokuwa lengo lake tangu alipojaribu kulishutumu kusudi la Mungu na kutupia lawama juu ya Shuhuda. Laiti wangebaki mahali ambapo nguvu yao ya ushawahi isingehusika katika kukinzana na kusudi la Mungu, Shetani asingeweza kuwashambulia kwa ukali; kwani asingeweza kutimiza kusudi lake kwa kuwatumia kama vifaa vyake vya kufanya kazi maalum. 3T 470.1
Katika maendeleo ya kazi ya Mungu, yale yanayowezwa kusemwa katika Kweli na watu binafsi kwa wakati fulani inawezekana yasisemwe kwa usahihi wakati mwingine. Sababu ya hii ni kwamba ndani ya mwezi mmoja wanaweza wakawa wamesimama bila hatia, wakiishi katika nuru bora waliyokuwa nayo, wakati mwezi uliofuata ulikuwa mfupi sana kwao kushindwa na hila za Shetani na, na kwa kujiamini, huanguka katika dhambi mbaya na kutofaa tena kwa kazi ya Mungu. 3T 471.1

Akili zinaweza kubadilishwa kupitia majaribu na hila za Shetani, ya kuwa si busara kwangu au mume wangu kuchukua jukumu la hata kusema maoni yetu juu ya sifa za watu wanaopaswa kushika nyadhifa tofauti, kwa sababu nasi tumewekwa kuwajibika katika kusudi hilo hilo ambalo wengine wamo. Hata hivyo, wangeuendeleza unyenyekevu na imani thabiti kwa Mungu ambayo walikuwa nayo wakati walipopendekezwa kuchukua majukumu, wao ndio wangeweza kuwa wasimamizi wa nafasi hii. Watu hawa hubadilika, lakini hawayatambui mabadiliko ndani yao. huanguka majaribuni, uthabiti wao hupotoshwa mbali, na kukata uhusiano wao na Mungu. Baada ya hapo hudhibitiwa na adui na hufanya na kusema vitu ambavyo humvunjia Mungu heshima na kulifedhehesha kusudi Lake. Ndipo Shetani hujisifu anapowaona ndugu na dada zetu wakitutazama sisi kwa mashaka kwa sababu tuliwapatia watu hawa matumaini na ushawishi. 3T 471.2

SURA YA 39

HALI YA ULIMWENGU

Nilioneshwa hali ya ulimwengu, ya kwamba inajaza kikombe cha uovu wake kwa haraka. Vurugu na uhalifu wa kila namna umejaa katika ulimwengu wetu, naye Shetani anatumia kila njia kuufanya uhalifu na uovu vionekane kuwa maarufu na kupendwa. Vijana wanaotembea mitaani wamezungukwa na vipeperushi pamoja na matangazo ya uhalifu na dhambi, machapisho yanayowasilishwa katika riwaya kadhaa au yatakayoigizwa kwenye kumbi za michezo. Akili zao zimefundishwa na kuelekezwa katika mazoea na dhambi. Mwenendo wa watu waovu na wachafu ndio unaofuatwa na kuonekana za msingi na kuwekwa katika ratiba zao za vipindi vya siku, na yote yanayoweza kuvutia udadisi na kuamsha tamaa za mwili huletwa mbele zao kama hekaya za kusisimua, kuvutia na kufurahisha. 3T 471.3

Fasihi zinazoendelezwa na wasomi waovu huharibu akili za maelfu katika ulimwengu wetu. Dhambi inaonekana ya kawaida tu, na si kitu kibaya sana. Husikia na kusoma sana kuhusu uhalifu na uovu wa kudhalilisha, kiasi kwamba dhamiri ya Kweli ambayo hapo awali ilikuwa nyeti na yenye huruma ambayo ingerejeshwakwa Bwana kwa msisitizo na hofu kubwa, hupindishwa ili iweze kuishi katika fedheha na maneno maovu kwa shauku pamoja na matendo mabaya ya watu wanaoendekeza ufisadi. 3T 472.1

"Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku za Mwana wa Adamu." Mungu atakuwa na watu wenye bidii ya matendo mema, watakaosimama imara katikati ya kizazi kilichoharibika kwenye uchafuzi. Kutakuwa na watu ambao watashikilia sana nguvu za mbinguni nao watakuwa imara dhidi ya kila jaribu. Vipeperushi vya mialiko mbalimbali vinavyochochea uovu vinaweza kujaribu kuteka fahamu zao na mawazo yao; lakini watakuwa wameshikamana sana na Mungu pamoja na malaika kiasi kwamba watakuwa kama wasioona wala kusikia. Wana kazi ya kufanya ambayo hakuna mtu anayeweza kuwafanyia, kazi hiyo ni kupigana vita vizuri vya imani, na kuushikilia uzima wa milele. Hawatakuwa watu wa kujiamini na kujitosheleza wenyewe. Kwa kuufahamu udhaifu wao, watauunganisha ujinga wao katika hekima ya Kristo, na udhaifu wao katika nguvu Zake. 3T 472.2

Vijana wanao uwezo wa kuwa na kanuni thabiti kiasi kwamba hata vishawishi vyenye nguvu zaidi vya Shetani havitaweza kuwavuta mbali na utii wao. Samweli alikuwa ni mtoto aliyezungukwa na vishawishi vya ufisadi mbaya zaidi. Aliona na kusikia vitu ambavyo viliihuzunisha nafsi yake. Wana wa Eli, waliokuwa wakihudumu hekaluni walikuwa wakitawaliwa na Shetani. Watoto hawa waliyachafua mazingira yote yaliyowazunguka. Wanaume kwa wanawake kila siku walivutiwa na dhambi na makosa, lakini Samweli alitembea na kuishi bila mawaa. Mavazi yake ya tabia hayakuwa na doa. Hakushiriki wala kufurahi katika dhambi zilizoijaza Israeli yote na taarifa za kutisha. Samweli alimpenda Mungu; Aliiweka roho yake katika uhusiano wa karibu sana na mbingu hata malaika alitumwa kuzungumza naye kuhusu dhambi za wana wa Eli, ambazo zilikuwa zinaichafua/zinaiharibu Israeli. 3T 472.3

Uchu na tamaa ya mwili vinashinda maelfu ya watu wanaodai kuwa ni wafuasi wa Kristo. Akili zao zinakuwa butu kwa sababu ya kufanya mazoea na dhambi kiasi kwamba hawaichukii, bali huwavutia. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Mungu hataendelea kuvumilia uhalifu na uovu unaodhalilisha wa watoto wa wanadamu. Hakika maovu yao yamefika hadi mbinguni na hivi punde yatajibiwa na tauni na mapigo ya kutisha ya Mungu juu ya dunia. Watakinywea kikombe cha ghadhabu ya Mungu kisichochanganywa na rehema. 3T 473.1

Nimeona kuwa kuna hatari ambayo hata wale wanaojiita watoto wa Mungu wataharibiwa. Ufisadi, ulevi, ulafi, uchafu wa ngono, unawafunga wanaume kwa wanawake kama mateka. Wanaonekana kupumbazwa na kutokuwa na nguvu za kupinga na kuishinda tamaa za mwili, na ulafi wa chakula. Katika Mungu kuna uwezo; ndani yake kuna nguvu. ikiwa wataitumainia, nguvu ya Yesu iletayo uhai itamuamsha kila mtu aliyelitaja Jina la Kristo. Hatari kubwa na hali ya kutisha imetuzunguka; lakini tunaweza kuwa salama tu endapo tutauhisi udhaifu wetu na kumng'ang'ania Mwokozi wetu mkuu kwa imani. Tunaishi katika nyakati za kutisha. Hatupaswi kuacha kuwa waangalifu katika kuomba hata kidogo. Roho zetu zisizoweza kusimama pekee lazima zimtegemee Yesu, Mkombozi wetu Mwenye huruma. 3T 473.2

Nilioneshwa ukuu na umuhimu wa kazi iliyo mbele yetu. Lakini ni wachache wanaotambua hali halisi ya mambo. Wote waliolala, na wasioweza kuutambua umuhimu wowote wa kuwa makini na kukesha,tayari watashindwa. Vijana wadogo wanaamka kushiriki katika kazi ya Mungu, baadhi yao wakiwa na ufahamu mdogo sana juu ya kuifanya kazi hiyo takatifu. Wana uzoefu mdogo tu katika kuonyesha imani na katika njaa ya dhati ya roho kwa Roho wa Mungu, ambaye hunufaisha. . Baadhi ya watu wenye uwezo mzuri, wanaoweza kujaza nyadhifa muhimu, hawafahamu ni roho gani waliyonayo. Huenenda kama maji yanavyosongea, huku wakiwa na furaha kama maji yanavyotiririka mwambani [gravity]. Huzungumza mambo ya kipuuzi, na kucheza na mabinti wadogo, huku karibu kila siku

wakisikiliza ibada zenye mguso wa ile Kweli. Watu wa namna hii huwa na dini ya kichwani, lakini mioyo yao haijatakaswa na zile Kweli wanazosikia. Watu wa namna hiyo kamwe hawawezi kuwaongoza wengine kwenye chemchemi ya maji yaliyo hai mpaka wenyewe watakapoyanywa hayo maji kwanza. 3T 473.3

Huu si wakati wa kawaida na wa kudharau. Matukio ya historia ya dunia hii yatafungwa hivi karibuni. Akili zilizo hafifu yanapaswa kubadilishwa. Mtume Petro anasema: “Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi, mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa kwenu katika ufunuo wake Yesu Kristo; kama watoto watiifu msijifananishe na tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu; bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu; kwa kuwa Mimi nilivyo mtakatifu.” 3T 474.1

Mawazo yaliyotapakaa, yanapaswa kukusanywa mbele za Mungu. Mawazo yanapaswa kutii mapenzi ya Mungu. Sifa hazipaswi kupewa nafasi; kwani zitapelekea na kukuza tabia ya kujiamini badala ya kuongeza unyenyekevu, uharibifu badala ya utakaso.
Watu wenye sifa za Kweli zinazostahili na wanaohisi kuwa wana sehemu ya kutenda katika kazi ya Mungu watahisi wamewekwa chini ya kazi takatifu na ya kuheshimika, kama mkokoteni chini ya miganda. Sasa ni wakati wa kufanya juhudi za dhati kabisa kuzishinda hisia za asili za tamaa za mwili. 3T 474.2

SURA YA 40

HALI YA KANISA

Kuna umuhimu mkubwa wa matengenezo kati ya watu wa Mungu. Hali ya sasa ya kanisa inaleta maswali mengi: Je! Huu ni uwakilishi sahihi wa Yeye aliyeutoa uhai Wake kwa ajili yetu? Je, hawa ndio wafuasi wa Kristo na ndugu wa wale ambao hawakuyahesabu maisha yao kuwa ya thamani? Wale wanaovifikia viwango vya Biblia, maelezo ya Biblia ya wafuasi wa Kristo, watakuwa wachache hakika, nadra kukutana nao. Wengi wakiwa wamemwacha Mungu, chemchemi ya maji yaliyo hai, watakuwa wamechimba visima, "visima vilivyovunjika, visivyoweza kutunza maji." Malaika anasema ya kuwa: "Ukosefu wa upendo na imani ni dhambi kubwa ambazo watu wa Mungu sasa wana hatia." Ukosefu wa imani hupelekea uzembe na kujipenda wenyewe pamoja na ulimwengu. Wale ambao hujitenga na Mungu na kuanguka majaribuni huendekeza maovu mabaya, kwani moyo wenye tamaa za mwili husababisha uovu mkubwa. Na hali hii hupatikana kati ya wengi wanaokiri kuwa ni watu wa Mungu. Wakikiri ya kwamba wanamtumikia Mungu huku kwa namna na hali zote wakizipotosha njia zao mbele Zake Bwana. Tamaa za mwili na shauku huendekezwa wengi, bila kuujali mwangaza halisi wa Ukweli unaoonesha hatari na kuiinua sauti Yake yenye nguvu na maonyo: Jihadharini, jizuieni, kataeni. "Mshahara wa dhambi ni mauti." Japokuwa mfano wa wale ambao imani yao imevunjika husimama kama taa na kuwaonya wengine wasiufuate mwenendo kama huo, ila wengi hukimbilia huko. Shetani ana udhibiti wa akili zao na anaonekana kuwa na nguvu juu ya miili yao. 3T 474.3

Oh, ni wangapi wanaojidanganya kwamba ni wema na wa haki, wakati nuru ya Kweli ya Mungu inadhihirisha kuwa maisha yao yote wameishi wakijifurahisha wenyewe! Mwenendo wao wote ni machukizo kwa Mungu. Ni wangapi wanaoishi bila sheria! Wanajitazama na kujiridhisha katika giza lao kuu kwa wanaishika sheria; hebu sheria ya Mungu ifunuliwe katika dhamiri zao, kama ilivyokuwa kwa Paulo, ndipo watakapoona ya kwamba wameuzwa chini ya dhambi na lazima tamaa na mawazo ya mwili yafe. Ubinafsi lazima ufe. 3T 475.1

Ni huzuni ya kiasi gani kwa yale makosa yanayofanywa na wengi, hakika yanasikitisha na kuogopesha! Wanajenga juu ya mchanga, lakini wanajibembeleza kuwa wameshikamana na Mwamba wa milele. Wengi wanaodai kuwa ni watauwa huenenda bila tahadhari, kwa uzembe, na kwa hatari na hawajali kuhusu hatari yao, kana kwamba hakuna hukumu inayokuja mbele. Adhabu ya kutisha inawangojea, lakini bado wanakubali kudhibitiwa na misukumo na hisia za tamaa kali; wanajaza rekodi ya maisha ya giza kwaajili ya hukumu. Ninaipaza sauti yangu kuwaonya wale wote wanaolitaja Jina la Kristo waachane na uovu wote. Jitakaseni

nafsi zenu kwa kuutii Ukweli. Jitakaseni dhidi ya uchafu wote wa mwili na roho, mkiukamilisha utakatifu kwa kumcha Mungu. Wewe unayehusika katika haya unaelewa ninachomaanisha. Hata nawe uliyeziharibu njia zako mbele za Bwana, ukishiriki uovu uliojaa, na ukaizimisha roho yako na weusi dhambi, Yesu bado anakualika wewe ugeuke kutoka katika njia zako, uzitumainie nguvu Zake, na uipate hiyo amani, nguvu, na neema ndani Yake ambayo itakufanya muwe zaidi ya washindi katika Jina Lake. 3T 475.2

Uovu wa nyakati hizi mbaya za uharibifu, umechafua roho nyingi ambazo zimekuwa zikikiri kwamba zinamtumikia Mungu. Lakini hata sasa bado hujachelewa, yale makosa kusahihishwa, nafasi ipo ya makosa kurekebishwa katika damu ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka kufanya upatanisho kwa niaba yako ikiwa utatubu na kuhitaji msamaha. Tunahitaji kuwa waangalifu na kuomba kuliko hapo awali, tusije tukaanguka katika nguvu ya majaribu na kuishi mfano wa maisha yenye uharibifu mbaya na huzuni. Hatupaswi, kama watu, kuwa wazembe na kuitazama dhambi bila kujali. Kambi inahitaji kusafishwa. Wote wanaolitaja Jina la Kristo wanahitaji kuwa waangalifu, kukesha kwa maombi na kuzilinda njia za roho; kwani Shetani yupo kazini kwa ajili ya kupotosha na kuharibu ikiwa atapewa nafasi hata ndogo. 3T 476.1

Ndugu zangu, Mungu anawaita ninyi kama wafuasi Wake mtembee katika nuru. Amkeni mnahitaji kushtula. Dhambi iko kati yetu, na haionekani kuwa yenye madhara sana na uovu sana. Akili za watu wengi zimehafifishwa na uendekezaji wa hamu na mazoea ya dhambi. Tunahitaji kusonga mbele karibu na mbingu. Ili tukue katika neema na katika ujuzi wa Ukweli. Kutembea katika nuru, kukimbia katika njia ya amri za Mungu, haimaanishi kuwa tunaweza kusimama imara bila kufanya lolote. Lazima tusonge mbele. 3T 476.2

Katika kujipenda nafsi, kujikweza, na kiburi kuna udhaifu mkubwa; lakini katika unyenyekevu kuna nguvu kubwa. Utu wetu halisi hautunzwi tunapojifikiria sisi wenyewe, lakini ni pale tu Mungu anapokuwa katika mawazo yetu yote na mioyo yetu inapomulika upendo kwa Mkombozi wetu na upendo kwa wanadamu wenzetu. Unyenyekevu na usahili wa tabia na moyo utatoa furaha, wakati majivuno yataleta kutoridhika, kujidanganya, malalamiko na maudhi endelevu. Ni kwa kupitia kujifunza kutojipa kipaumbele sana na kufikiri zaidi kuwapa furaha wengine ndipo kutatupatia nguvu za kimbingu. 3T 476.3

Katika kujitenga kwetu na Mungu, katika kiburi chetu na giza, tunatafuta kujiinua kila wakati, na kusahau kuwa unyenyekevu wa moyo ni nguvu. Nguvu za Mwokozi wetu hazikuwa katika utoaji wa maneno makali ambayo yangechoma nafsi; ulikuwa ni upole Wake, unyororo [gentleness] na tabia Zake zilizo za kujionyesha-onyesha, utulivu,na muungwana [unassuming character], heshima isiyo ya

kufikirika iliyomfanya awe mshindi wa mioyo. Kiburi na kujiona kuwa bora, vikilinganishwa na unyenyekevu, hakika ni udhaifu. Tunaalikwa kujifunza kutoka Kwake aliyekuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo; ndipo tutaipata ile raha na amani ambayo inatamaniwa sana. 3T 477.1

SURA YA 41

KUIPENDA DUNIA

Jaribu lililowasilishwa na Shetani mbele ya Mwokozi wetu akiwa juu ya mlima mrefu sana, ni moja kati ya majaribu makuu yanayoongoza ambayo mwanadamu lazima akutane nayo. Falme za ulimwengu katika utukufu wake ziliwekwa mbele ya Kristo na Shetani kama zawadi kwa sharti kwamba Kristo asalimishe kwa adui heshima ya ukuu. Mwokozi wetu alihisi nguvu ya jaribu hili, lakini alikabiliana nalo kama mbadala wetu na alishinda. Kristo Asingeliweza kujaribiwa katika kipengele hiki kama mwanadamu asingelijaribiwa kwa jaribu hili duniani {Alishinda kile mwanadamu alishindwa Edeni, jaribu la hamu ya chakula Edeni]. Katika ukinzani Wake, Yeye alitupatia wanadamu kielelezo ambacho tunapaswa kukifuata Shetani anapokuja kwetu binafsi kutuongoza kutoka kwenye uadilifu. 3T 477.2

Hakuna mtu awezaye kuwa mfuasi wa Kristo na bado akaweka mapenzi yake katika mambo ya ulimwengu. Yohana katika waraka wake wa kwanza anaandika: “Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.” Mwokozi wetu, aliyekutana na jaribu hili katika nguvu yake kuu, anaijua hatari aliyonayo mwanadamu ya kujisalimisha katika jaribu la kuipenda dunia. 3T 477.3

Kristo anajitambulisha na ubinadamu Wake Yeye Mwenyewe kwa kukabiliana na jaribio kwa kiasi hiki na kulishinda kama mbadala wa mwanadamu. Ameyalinda kwa kuyawekea maonyo maeneo yote ambayo Shetani angeliweza kufanikiwa ayaletapo majaribu yake kwa wanadamu. Alijua kuwa Shetani angelipata ushindi dhidi ya mwanadamu kama asingeliwekewa ulinzi katika maeneo ya uchu wa chakula pamoja na mapenzi kwa utajiri wa dunia na taadhima yake. Anasema: “Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.” “Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.” 3T 477.4

Hapa Kristo ameweka mbele yetu mabwana wawili, Mungu na dunia, na amewasilisha wazi Ukweli kuwa ni vigumu kwetu kuwatumikia wote. Kama shauku, maslahi na mapenzi yetu, kwa ulimwengu huu ndivyo vinavyotawala, hatuwezi kupokea na kuthamini mambo, ambayo, ni ya thamani mno kuliko mengine na yanastahili umakini wetu. Upendo kwa dunia utaondoa upendo kwa Mungu na kuyafanya yale ya muhimu kwetu au matamanio yetu ya juu sana yawe chini ya mambo ya ulimwengu. Hivyo Mungu hatapewa nafasi iliyotukuka katika mapenzi yetu na kujitoa kwetu kama ilivyo kwa mambo ya dunia. 3T 478.1

Matendo yetu yataonesha kiwango halisi ambacho hazina za ulimwengu zimeshikilia mapenzi yetu. Umakini wa hali ya juu, kujali, shauku, na utendaji kazi vimeelekezwa katika mambo ya ulimwengu, wakati mambo ya umilele yakifanywa kuwa ya pili. Hapa Shetani anapokea toka kwa mwanadamu ibada ile ambayo aliidai kwa Kristo lakini akaikosa. Ni upendo wa ulimwengu ulio na ubinafsi ambao unaharibu imani ya waitwao kuwa ni wafuasi wa Kristo na kuwafanya kuwa dhaifu katika nguvu ya kimaadili. Kwa kadiri wanavyozidi kupenda utajiri wao wa kidunia, ndivyo wanavyozidi kutanga mbali na Mungu, na ndivyo wanavyozidi kupungukiwa na asili ya mbingu/Kiungu ambayo ingeliwapatia utambuzi kwa vichocheo vinavyoharibu vilivyo katika ulimwengu na hatari wanazoanikwa kwazo. 3T 478.2

Katika majaribu yake Shetani ni dhumuni lake kuufanya ulimwengu uwe wa kuvutia sana. Kupitia kupenda utajiri na taadhima ya kiulimwengu anayo nguvu ya kuloga hata wale wanaokiri imani, na kupata wale wa ulimwengu wa Kikristo. Tabaka kubwa la wale wajiitao kuwa ni Wakristo watatoa dhabihu yoyote kwa kadiri wawezavyo ili kupata utajiri, na kwa kadiri wanavyofanikiwa zaidi katika dhumuni lao ndivyo wanavyozidi kupunguza upendo walio nao kwa Kweli za thamani na ndivyo wanavyopunguza pia shauku yao katika maendeleo yake. Wanapoteza upendo wao kwa Mungu na kuwa kama wendawazimu. Kwa kadiri wanavyozidi kufanikiwa katika kuwa na utajiri ndivyo wanavyozidi kujihisi kuwa ni masikini kwa kuwa hawatoshelezwi, na ndivyo wanavyowekeza kidogo zaidi katika kazi ya Mungu. 3T 478.3

Matendo ya watu hao ambao wana upendo wa kiwendawazimu kwa utajiri yanaonesha kuwa haiwezekani kuwatumikia mabwana wawili, Mungu na mali. Pesa ndiye mungu wao. Wanaabudu uweza wake. Wanautumikia ulimwengu kwa dhamiri, nguvu na makusudi yao yote. Heshima yao, ambayo ndiyo haki yao ya uzaliwa, inatolewa dhabihu kwa ajili ya manufaa ya kiulimwengu. Nguvu hii iongozayo inatawala akili zao, na watakiuka sheria ya Mungu ili wapate kuyatumikia matamanio yao binafsi, kwa ajili ya kuongeza hazina yao ya kidunia. 3T 479.1

Wengi wanaweza kukiri kuwa wanayo dini ya Kristo na huku hawapendi na hawasikilizi waraka au kanuni za mafundisho ya Kristo. Wanawekeza nguvu zao zote katika masumbuko ya kidunia na kusujudia mali. Inatisha kwamba watu walio wengi wanadanganywa na Shetani na mawazo yao yanasisimuliwa kwa matarajio yao makubwa katika mafanikio ya kidunia. Wanapumbazwa kwa matarajio ya furaha kamili kama watatimiza lengo lao katika kuhodhi adhama na utajiri katika dunia. Shetani anawajaribu kwa hongo yenye kuvutia, “haya yote nitakupa wewe,” uweza huu wote, mali hizi zote, ambazo kwazo waweza kufanya mengi yaliyo mazuri. Lakini mara tu lengo walilolihangaikia linapotimia, wanakosa muunganiko na Mwokozi ajikanaye nafsi, ambaye angeliwafanya wawe washirika wa asili ya Kiungu. Wanashikilia hazina zao za kidunia na kupuuza kujikana nafsi na kujitoa binafsi kunakohitajika kwa ajili ya Kristo.
Hawana shauku ya kuachana na hazina zao pendwa ambazo mioyo yao imejikita kwazo. Wamebadilisha mabwana; wamekubali mali kama mbadala wa Kristo. Mali ni mungu wao, na mali ndizo wanazozitumikia. 3T 479.2

Shetani amejilimbikizia yeye mwenyewe ibada ya hizi nafsi zilizodanganywa kupitia mapenzi yao ya mali na utajiri. Badiliko limekuwa likitokea kidogo kidogo sana, na nguvu ya Shetani ni yenye udanganyifu, inahadaa, ina hila, kiasi kwamba wanafanana na ulimwengu pasipo kutambua kuwa wamejitenga na Kristo na sio watumishi Wake tena isipokuwa katika jina. 3T 479.3

Shetani anashughulika na wanadamu kwa uangalifu mno kuliko alivyoshughulika na Kristo katika jangwa la majaribu, kwa sababu anachukizwa kwa kuwa pale alipoteza. Ni adui aliyeshindwa. Haji kwa mwanadamu moja kwa moja na kutaka aweze kusujudiwa kwa ibada ya nje. Kwa urahisi anamwambia wanadamu aweke matamanio yao kwa vitu vizuri vya ulimwengu huu. Kama anafanikiwa kuhusisha akili na mapenzi, mivuto ya kimbingu inafunikwa kwa wingu. Anachotaka kwa mwanadamu ni ili aweze kuanguka katika nguvu ya udanganyifu wa majaribu yake, kuipenda dunia, kupenda madaraka na wadhifa, kupenda pesa, na kuweka matamanio yake kwenye hazina za kidunia. Kama akilipata hili, amepata yote aliyoyatarajia kwa Kristo. 3T 480.1

Mfano wa Kristo unatuonesha kuwa tumaini letu pekee la ushindi liko katika upinzani endelevu dhidi ya mashambulio ya Shetani. Yeye aliyeshinda dhidi ya adui wa wanadamu katika mgogoro wa jaribu, anaelewa nguvu ya Shetani dhidi ya jamii ya wanadamu na amemshinda adui kwa niaba yetu. Kama mshindi ametupatia sisi manufaa ya ushindi Wake, kwamba katika jitihada zetu za kupambana na majaribu ya Shetani tunaweza kuunganisha udhaifu wetu na nguvu Yake Bwana, kutokuwa kwetu na thamani na kutostahili kwetu na sifa na stahiki Yake. Na, tukiwezeshwa

na kutegemezwa na uweza wake udumuo, tunaweza kupambana kupitia Jina Lake lenye nguvu na kushinda kama Yeye alivyoshinda. 3T 480.2

Ni kupitia mateso/maonjo yasiyoelezeka, Mwokozi wetu alitupatia wokovu karibu nasi. Katika ulimwengu huu hakuheshimiwa na hakufahamika, ili kwamba kupitia kujishusha Kwake kwa pekee na kudhalilika kwake aweze kumwinua mwanadamu apate kupokea heshima ya kimbingu na furaha ya milele katika nyua zake za kifalme. Je, mwanadamu aliyeanguka atanung'unika kwa sababu mbingu yaweza kupatikana tu kwa kupitia mgogoro, kujikana nafsi, na kutaabika? 3T 380.3

Maswali ya wengi walio na moyo wa kiburi ni haya: Kwa nini ninahitaji kupitia kujidhili na kuwa na majuto makuu na kutubu kabla ya kuwa na uhakika kuwa nimekubaliwa na Mungu, na kupata tuzo ya milele? Kwa nini njia ya mbinguni isiwe rahisi na nzuri zaidi, na yenye kuvutia? Tunawarejesha wote hawa wenye mashaka na manung'uniko Kwake aliye kielelezo kikuu alipopitia maumivu chini ya mzigo wa hatia ya mwanadamu na kuvumilia maumivu makali ya njaa. Yeye Hakuwa na dhambi, na zaidi ya hili, Yeye alikuwa mfalme wa mbinguni; lakini kwa niaba ya mwanadamu akafanyika dhambi kwa ajili ya wanadamu. "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." 3T 480.4

Kristo alitoa mhanga kila kitu kwa ajili ya mwanadamu ili iwe rahisi kwa mwanadamu kupata mbingu. Sasa ni zamu ya mwanadamu aliyeanguka kuonesha kile anachoweza kukitoa mhanga yeye mwenyewe kwa ajili ya Kristo, ili aweze kupata utukufu wa milele.Wale wote ambao wana hisia za Kweli kuhusu ukubwa wa wokovu na gharama yake kamwe hawatanung'unika kwamba wanapanda kwa machozi na kwamba mgogoro na kujikana nafsi ni sehemu ya Mkristo katika maisha haya. Masharti ya wokovu kwa mwanadamu yamewekwa na Mungu. Kujikana nafsi na kubeba msalaba vimewekwa ili kupitia hivyo mdhambi atubuye aweze kupata faraja na amani. Mawazo kwamba Yesu alisalimisha yote aliyokuwa nayo kama matokeo ya kudhalilishwa Kwake na kafara ambayo mwanadamu kamwe hatoweza kupewa mtihani kuvumilia, vinapaswa kunyamazisha kila minong'ono. Furaha iliyo tamu inakuja kwa mwanadamu kupitia toba yake ya dhati kwa Mungu kwa sababu ya uasi kwa sheria Yake, na imani katika Kristo kama Mwokozi, Mtetezi, Mwombezi na Wakili wa mdhambi. 3T 481.1

Wanadamu wanahangaika kwa gharama kubwa ili wapate hazina za maisha haya. Wanataabika na kuvumilia magumu na ufukara ili waweze kupata baadhi ya manufaa ya kidunia. Kwa nini mdhambi awe na utayari mdogo kuvumilia, kuumia, na kujitoa mhanga ili aweze kupata hazina isiyoharibika, maisha ambayo yapo sambamba na maisha ya Mungu (milele), taji ya utukufu wa milele ambao haiwezi kuchuja au kufifia? Hazina zisizopimika za mbinguni, urithi wenye thamani isiyo

na kifani, ambao unamaanisha utukufu wa milele, lazima tuvipate kwa gharama yoyote. Hatupaswi kunung'unikia kuhusu kujikana nafsi, kwa kuwa Bwana na uzima na utukufu alipitia hayo kabla yetu. Hatuwezi kuepuka maonjo na ufukara, kwa kuwa Mtukufu wa mbinguni aliyakubali haya kwa niaba ya wadhambi. Kujitoa mhanga kuacha maisha rahisi ya mtelemko/bwerere, kuacha raha na utulivu havipaswi kuwa chanzo cha malalamiko, kwa sababu Mwokozi wa ulimwengu aliyakubali haya yote kwa niaba yetu. Kufanya makadirio ya juu zaidi kwa kujikana nafsi kwetu, ufukara, na kujitoa mhanga, haitugarimu sana kuliko ilivyokuwa kwa Mfalme wa amani. Kujitoa kafara kokote kule ambako tunaweza kufanya hakuna maana yoyote ile kunapolinganishwa na kile ambacho Kristo amefanya kwa niaba yetu. 3T 481.2

SURA YA 42

KIBURI

Kuna wale wenye roho ya ujasiri wa kutojali na hatarishi, ambayo wanaiita kuwa ni ujasiri na ushujaa. Pasipo na msaada wanajiweka wenyewe katika matukio yenye majanga na hatari kubwa, hivyo wanajihatarisha kwa majaribu ambayo kwayo utahitajika muujiza wa Mungu ili uweze kuwatoa pasipo kuumizwa na wala kuchafuliwa. Jaribu la Shetani kwa Mwokozi wa ulimwengu kujitupa chini toka katika kilele cha mlima lilikabiliwa kwa ujasiri na kupingwa. Shetani alinukuu ahadi ya Mungu kama ulinzi kwamba Kristo aweza kufanya hili na kuwa salama kwa sababu ya nguvu ya ahadi. Kristo alikabiliana na jaribu kwa andiko: "Imeandikwa,….Usimjaribu Bwana Mungu wako." Njia pekee iliyo salama kwa Wakristo ni kulikabili na kulipiga teke jaribu kwa Neno la Mungu. Shetani anawasukumiza wanadamu katika maeneo ambayo Mungu hataki waende, na anawapatia Maandiko ili kuthibitisha mapendekezo yake. 3T 482.1

Ahadi za Mungu za thamani hazijatolewa ili kumtia nguvu mwanadamu katika kusudi lake lenye dhana ya ujuvi (presumption) au kwa ajili yake ili azitegemee anapokimbilia pasi na ulazima kwenye hatari. Bwana anatutaka sisi kuenenda mbele kwa unyenyekevu huku tukitegemea majaliwa na maongozi Yake. "Kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu." Katika Mungu ndipo kuna ustawi wetu, mafanikio na maisha yetu. Hakuna chochote kinachoweza kufanywa kikastawi pasipo ruhusa na mbaraka wa Mungu. Anaweza kuweka mkono Wake ili apate kustawisha na kubariki, au anaweza kuugeuza mkono wake dhidi yetu. "Umkabidhi Bwana njia yako, pia umtumaini, Naye atafanya." Tunahitajika, kama watoto wa Mungu, kudumisha tabia thabiti ya Kikristo. Tunapaswa kuifanyia kazi hekima, tahadhari, na unyenyekevu, na kuenenda kwa umakini kwa wale ambao

hawana. Na bado hatupaswi kwa namna yoyote ile kusalimisha au kulegeza kanuni. 3T 482.2

Usalama wetu upo katika kutompa ibilisi sehemu yoyote ya kukanyaga, kwa kuwa mapendekezo yake na madhumuni yake ni kutuumiza sisi daima na kutuzuia ili tusimtegemee Mungu. Anajibadilisha yeye mwenyewe afanane na malaika wa nuru na usafi wa moyo ili kwamba kwa majaribu yake ya werevu, apate kuanzisha mbinu zake kwa namna ambayo hatuwezi kutambua hila zake. Kwa kadiri tunavyojisalimisha, ndivyo ambavyo madanganyo yake yatakavyokuwa na nguvu zaidi kwetu. Si salama kuingia katika malumbano au mazungumzo naye. Kwa kila faida ambayo tunampatia adui, atataka zaidi. Usalama wetu pekee u katika kukataa kwa ujasiri hatua ya kwanza ya kuelekea kwenye dhana ya ujuvi/presumption. Mungu ametupatia kupitia kwa sifa na stahiki Kristo neema toshelevu kwa ajili ya kumkabili Shetani na kuwa zaidi ya washindi. Upinzani ni mafanikio. “Mpingeni Shetani naye atawakimbia.” Upinzani unapaswa kuwa imara na thabiti. Tunapoteza yote tunayoyapata kama tunapinga leo halafu kesho tujisalimishe. 3T 482.3

Dhambi ya zama hizi ni kupuuza amri za Mungu zilizo wazi. Nguvu ya mvuto kuelekea uelekeo potofu ni kubwa sana. Hawa alikuwa na yote ambayo aliyataka. Hakukuwa na chochote kilichokosekana kumpatia yeye furaha, bali uchu usio na kiasi au kuthibitiwa, ukatamani tunda la mti pekee ambao Mungu aliukataza. Hakuwa na uhitaji wa tunda la mti wa ujuzi, bali aliruhusu uchu wake na shauku yake kuendesha fikra zake. Alikuwa na furaha kamilifu katika makazi yake ya Edeni akiwa pembeni ya mumewe; lakini, kama akina Hawa wenye wahaka (restless) wa kizazi kipya, alishawishika kuona kuwa kuna eneo la juu zaidi ya lile ambalo Mungu alipatia. Lakini kwa kujaribu kupanda juu zaidi kuliko mahali pake pa awali, akaanguka mbali mno chini yake. Na haya ndiyo yatakuwa matokeo ya uhakika mno kwa akina Hawa wa kizazi hiki kama watapuuza kutimiza majukumu yao ya maisha ya kila siku kwa uchangamfu kulingana na mpango wa Mungu. 3T 483.1

Kuna kazi kwa wanawake ambayo ni ya muhimu zaidi na yenye kutukuka kuliko majukumu ya mfalme katika kiti Zhake cha enzi. Wanaweza kuumba/kutengeneza akili za watoto wao na kuchonga tabia zao ili waweze kutumika katika ulimwengu huu na kwamba wapate kuwa wana na binti za Mungu. Muda wao unapaswa kuchukuliwa kuwa ni wa thamani mno kupotezwa katika kumbi za dansi au katika kazi za kipuuzi. Kuna kazi ya kutosha iliyo na umuhimu na ya lazima katika ulimwengu huu wa uhitaji na maonjo pasipo kupoteza nyakati za thamani kwa ajili ya mapambo au maonesho. Binti za mfalme wa mbinguni, washirika wa familia ya kifalme, watahisi uzito wa jukumu walilonalo la kufikia maisha matakatifu, ili waweze kuwa na muunganiko wa karibu na mbingu na kufanya kazi kwa pamoja na Mwokozi wa ulimwengu. Wale wote wanaojishughulisha katika kazi hii hawatatosheka na mitindo na mambo ya kipuuzi yanayofyonza akili na matamanio

ya wanawake katika siku hizi za mwisho. Kama kweli ni binti za Mungu watakuwa washiriki wa asili ya mbingu/Kiungu. Watajawa na huruma ya pekee, kama alivyokuwa Mwokozi wao, wanapoona mivuto miovu katika jamii. Watakuwa na huruma pamoja na Kristo, na katika duru lao, kwa kadiri wanavyopata uwezo na fursa, watatenda kazi kuokoa nafsi zinazopotea kama Kristo alivyotenda kazi katika duru Yake lililotukuka kwa ajili ya faida ya mwanadamu. 3T 483.2

Upuuziaji katika sehemu ya mwanamke kufuata mpango wa Mungu katika kuumbwa kwake, jitihada ya kufikia nyadhifa muhimu ambazo Yeye [Mungu] hakumstahilisha azijaze, kunaacha nafasi wazi katika nafasi ambayo angeliijaza kwa ukubali wake. Kwa kutoka nje ya eneo lake, anapoteza utu wake kama mwanamke na heshima yake. Mungu alipomuumba Hawa, alikusudia kuwa asichukue nafasi ya chini sana wala nafasi ya juu sana kwa mwanamume, bali katika mambo yote anapaswa kuwa wa kufanana naye. Jozi hii takatifu ilipaswa kutokuwa na shauku binafsi kutoka kwa kila mmoja wao; na bado kila mmoja alikuwa na upekee katika kuwaza na kutenda. Lakini baada ya dhambi ya Hawa, kwa vile alikuwa wa kwanza katika kuasi, Bwana akamwambia kuwa atatawaliwa na Adamu. Alipaswa kuonesha utii kwa mumewe na kujisalimisha kwa mume, na hili lilikuwa sehemu ya laana. Katika nyanja mbalimbali laana imeifanya sehemu ya mwanamke kuwa ya majonzi na maisha yake kuwa mzigo mzito. Ukuu ambao Mungu alimpatia mwanamume ameutumia vibaya kwa namna mbalimbali kwa kutumia nguvu kiholela. Hekima isiyo na ukomo ikaunda mpango wa ukombozi, ambao ukawapatia wanadamu kipindi cha pili cha matazamio kwa kuwapa jaribio lingine. 3T 484.1

Shetani anatumia wanadamu kama mawakala wake kuwaongoza kwenye dhana ujuvi wale wanaompenda Mungu; hasa katika suala hili la wale ambao wamedanganyika na umizimu. Wanaoamini umizimu kwa ujumla hawamkubali Kristo kama Mwana wa Mungu, na kupitia upotofu wao wameongoza nafsi nyingi kuelekea dhambi za ufidhuli. Wanadai hata ukuu juu ya Kristo kama ambavyo Shetani alifanya aliposhindana na Mfalme wa uzima. Wanaoamini umizimu ambao nafsizao zimetapakaa dhambi za tabia ya uasi, na machukizo na ambao dhamiri zao zinachomwa, wanadiriki kulitaja Jina la Mwana wa Mungu asiye na waa katika midomo yao michafu na kwa kufuru wanajumuisha Jina Lake lililotukuka sana pamoja na uovu wa kufisha unaotambulisha asili zao zilizo na uchafuzi. 3T 484.2

Watu wanaoingiza ndani mafundisho haya ya uongo yaliyo mabaya sana watathubutu kuingia katika malumbano na wale wanaofundisha Neno la Mungu, na baadhi ya wanaofundisha Kweli hawana ujasiri wa kuhimili changamoto toka katika tabaka hili, ambao ni wahusika muhimu katika Neno la Mungu. Baadhi ya wachungaji wetu hawana ujasiri wa kimaadili kusema kwa watu hawa: Mungu ametuonya sisi katika Neno Lake kuhusu ninyi. Ametupatia sisi maelezo

yanayoaminika kuhusu tabia yenu na ya uzushi mlio nao. Baadhi ya watumishi, badala ya kuachana na tabaka hili au kuwashutumu kwa woga, wamekutana nao katika mijadala ya wazi. Lakini katika mjadala pamoja na waamini umizimu hawakutani na mwanadamu tu bali Shetani na malaika zake. Wanajiweka wenyewe katika mawasiliano na nguvu za giza na kuwachochea malaika waovu wawazingire. 3T 485.1

Watu wanaoamini umizimu wanadhamiria kutangaza mafundisho yao ya uongo; na watumishi ambao ni mawakili wanaotetea Kweli ya Biblia wanawasaidia kufanya hili wanapoamua kujumuika katika mjadala pamoja nao. Wanaboresha fursa zao ili wapate kuyafikisha mafundisho yao ya uongo kwa watu, na katika kila mjadala pamoja nao baadhi ya watu watadanganywa. Namna bora zaidi kwetu ni kuwaepuka (wengi wa uongo hupenda kufanya hivi hata wale wa ushoga wana vyombo vya habari kutangaza mambo yao bila ushuru). 3T 485.2

SURA YA 43

NGUVU YA UCHU WA CHAKULA

Mojawapo ya majaribu yenye nguvu mno ambayo mwanadamu anapaswa kukutana nayo ni katika uchu wa chakula-hamu ya kula. Akili na mwili vina uhusiano uliositirika na wa ajabu. Vinaitikiana kwa pamoja. Kutunza afya ya mwili ili uendelee kuwa na nguvu, na kwamba kila sehemu ya mashine hai iweze kufanya kazi kwa upatanifu/umoja, linapaswa kuwa somo la kwanza la maisha yetu. Kuupuuza mwili ni kuipuuza akili. Haiwezi kuwa ni kwa utukufu wa Mungu kwamba watoto Wake wawe na miili dhaifu au akili zilizodumaa. Kuendekeza hamu na kuigharimu afya ni matumizi mabaya na maovu ya hisia. Wale wanaojihusisha katika aina yoyote ya kutokuwa na kiasi, aidha katika kula au kunywa, wanapoteza nguvu zao za kimwili na kudhoofisha nguvu ya kimaadili. Watapata adhabu ambayo inafuata kwa kuasi sheria ya mwili. 3T 485.3

Mwokozi wa ulimwengu alijua kuwa kuendekeza uchu wa chakula kungelileta unyonge wa kimwili, na hivyo kufisha milango ya fahamu kiasi kwamba mambo matakatifu na ya umilele hayatatambuliwa. Kristo alijua kuwa ulimwengu umeelemewa na ulafi na kwamba uendekezaji huu ungeliharibu nguvu za kimaadili. Kama uendekezaji wa uchu ulikuwa mkubwa mno miongoni mwa jamii yawanadamu kiasi kwamba, ili kuvunja nguvu yake, Mwana wa Mungu, kwa niaba ya mwanadamu, alipaswa kufunga karibia majuma sita, ni kazi kubwa kiasi gani iliyo mbele ya Mkristo ili aweze kushinda kama Kristo alivyoshinda! Nguvu ya jaribu

la kuendekeza uchu mbaya inaweza tu kupimwa kwa uchungu usioelezeka wa Kristo alipokuwa katika saumu ndefu jangwani. 3T 486.1

Kristo alijua kuwa ili afanikiwe katika mpango wa ukombozi anapaswa kuanza kazi ya kumkomboa mwanadamu mahali pale ambapo anguko/uharibifu ulianzia. Adamu alianguka kwa kuendekeza hamu ya chakula. Ili aweze kumwonesha mwanadamu wajibu wake wa kutii sheria ya Mungu, Kristo alianza kazi Yake ya ukombozi kwa kutengeneza upya tabia za kimwili za mwanadamu. Mmomonyoko wa maadili na kuzorota kwa wa jamii yanadamu ni matokeo makubwa ya kuendekeza uchu mbaya. 3T 486.2

Kuna wajibu wa adhimu na wa dhati kwa wote, hasa kwa wachungaji/watumishi ambao wanafundisha Kweli, kuushinda uchu wa chakula. Kutumika kwao kungekuwa kukubwa na kwa manufaa kama wangedhibiti uchu wao na hisia zao kali, na nguvu zao za kiakili na kimaadili zingeimarika zaidi kama wangeuganisha kwa pamoja kazi za mikono au za mwili, na jitihada za kiakili. Kwa tabia zilizo madhubuti za kiasi, na muunganiko wa mazoezi ya kimwili na kiakili, wangelikamilisha kiasi kikubwa mno cha kazi na kuhifadhi usafi wa akili. Kama wangelifanya hivyo, mawazo na maneno yao vingelitiririka kwa ulaini/urahisi, shughuli zao za kidini zingelitiwa nguvu, na mivuto wanayoionesha kwa wasikilizaji ingelikuwa dhahiri. 3T 486.3

Kukosa kiasi katika kula, hata chakula kilicho na ubora ulio sahihi, kutaleta hali ya kudhoofu katika mfumo na kuzifanya hisia makini na takatifu kuwa butu. Kiasi kilicho makini katika kula na kunywa ni muhimu sana kwa utunzaji wa afya na na uwajibikaji wenye ari wa viungo vyote vya mwili. Tabia zilizo makini katika kiasi, zikiunganishwa na mazoezi ya misuli pamoja na ya akili, vitahifadhi nguvu za akili na mwili, na kuleta nguvu ya kustahimili kwa wale waliojihusisha katika huduma, kwa wahariri, na kwa wengine wote ambao kazi zao ni za kukaa. Kama watu, huku tukiwa na taaluma yote ya matengenezo ya afya, tunakula kupita kiasi. Kuendekeza ulafi ni moja ya sababu kubwa za udhaifu wa kimwili na kiakili, na ndio msingi wa udhaifu unaoonekana kila mahali. 3T 487.1

Kukosa kiasi kunaanzia katika meza zetu tunapotumia vyakula visivyo vya kiafya. Baada ya muda, kwa kuendelea kuendekeza kula bila kiasi, mfumo wa kumeng'enya chakula iunadhoofishwa, na chakula kinacholiwa hakitoshelezi tena hamu. Masharti yasiyo ya kiafya hujitokeza, na panakuwa na hamu kali ya chakula chenye kusisimua zaidi. Chai, kahawa, na nyama nyekundu vinaleta madhara ya moja kwa moja. Kwa kuchochewa na sumu hizi, mfumo wa fahamu unasisimuliwa, na, kwa nyakati fulani, baada ya muda kupita, akili inaonekana kuwa na nguvu na kuchangamka na mawazo kuwa wazi zaidi. Kwa kuwa vichocheo hivi kwa muda huo vinaleta matokeo hayo yanayokubalika, wengi wanahitimisha kuwa

wanavihitaji mno na kuendelea kuvitumia hatimaye. Lakini siku zote kuna athari na mwitikio. Mfumo wa fahamu, kwa vile ulivyosisimuliwa isivyo halali, unakopa nguvu kwa ajili ya matumizi ya sasa kutoka katika vyanzo vya nguvu za wakati ujao. Nguvu hizi zote ni za kitambo tu na baadaye sonona au moyo kuvunjika hufuata. Kwa kiwango kile kile, kwa namna ambavyo vichocheo hivi vimeupa nguvu mfumo kwa muda ndivyo nguvu ya ogani zilizosisimuliwa itakaposhuka mara baada ya kichocheo kupoteza nguvu yake. Hamu inafundishwa kuwa na hamu kubwa ya kitu kilicho na nguvu zaidi ambacho kitakuwa na na kuchochea na kuongeza msisimko unaokubalika, mpaka hali ya kuendekeza inapokuwa tabia, na panakuwa na shauku kali ya kutaka kichocheo chenye nguvu zaidi muda wote kama tumbaku, mvinyo, na pombe. Kwa kadiri uchu unavyoendekezwa kilema kutokea, ndivyo shauku inavyozidi kuongezeka na kuwa ngumu zaidi kuidhibiti. Kwa kadiri mfumo unavyodhoofika zaidi ndivyo unavyoshindwa kufanya kazi pasipo vichocheo visivyo vya asili, na ndipo shauku kwa vitu hivi inaongezeka maradufu, mpaka nguvu ya nia inazidiwa nguvu, na hapo ndipo inapoonekana kuwa hakuna nguvu yoyote iliyosalia ili kuweza kukataa shauku isiyo ya asili kwa vitu hivi vya anasa. 3T 487.2

Njia pekee ya usalama ni kutogusa, kutoonja, kutotengeneza, chai, kahawa, vileo, tumbaku, afyuni/bangi/madawa ya kulevya, na pombe ya aina yoyote [touch not, taste not, handle not- Kol 2:21]. Umuhimu wa wanadamu wa kizazi hiki kuomba ili waweze kupata msaada wa nguvu ya nia, iliyotiwa nguvu kwa neema ya Mungu, ili waweze kukabiliana na majaribu ya Shetani na kupingana na uendekezaji wowote mdogo wa uchu mbaya ni mkubwa mara mbili zaidi ya ilivyokuwa kwa vizazi kadhaa vilivyopita. Lakini kizazi cha sasa kina nguvu ndogo mno ya kujidhibiti kuliko waliyokuwa nayo hao walioishi kabla. Wale ambao wameendekeza uchu kwa vichocheo hivi wameambukiza uchu wao ulio potofu pamoja na shauku kali kwa watoto wao, na nguvu kubwa ya kimaadili inahitajika ili kupingana na hali ya kukosa kiasi katika namna zake zote. Njia pekee iliyo kamilifu ni kusimama imara upande wa kuwa na kiasi na kutojitosa katika njia ya hatari. 3T 488.1

Hatima kuu ya kwa nini Kristo alivumilia saumu ile ndefu jangwani, ilikuwa ni kwa ajili ya kutufundisha umuhimu wa kujikana nafsi na kuwa na kiasi. Kazi hii inapaswa kuanzia katika meza zetu na inapaswa kuoneshwa kwa uthabiti katika nyanja zote za maisha. Mwokozi wa ulimwengu alikuja toka mbinguni apate kumsaidia mwanadamu katika udhaifu wake, ili katika nguvu hiyo ambayo Kristo alikuja kumpa, apate kuwa imara na kuweza kushinda uchu na shauku kali, na kuwa mshindi katika kila hatua. 3T 488.2

Wazazi wengi wanalea na kustawisha hamu za watoto wao na kuunda uchu wao wa chakula. Wanawaendekeza kula nyama nyekundu na kunywa chai na kahawa. Nyama nyekundu zilizowekwa vichocheo na viungo vingi pamoja na chai na

kahawa, ambavyo baadhi ya akina mama wanawahamasisha watoto ili waweze kuvitumia, vinaandaa njia ya wao kuwa na njaa kali ya vichocheo vyenye nguvu zaidi kama tumbaku. Matumizi ya tumbaku yanachochea hamu ya pombe, na matumizi ya tumbaku pamoja na pombe yanadhoofisha nguvu za neva. 3T 488.3

Kama hisia za kimaadili za Wakristo zingekuwa hai katika suala la kiasi katika mambo yote, kwa kuonesha mfano, wangelianzia katika meza zao, kuwasaidia wale walio dhaifu katika kujidhibiti, ambao hawana nguvu za kupambana na shauku kali ya hamu ya chakula. Kama tungelitambua kuwa tabia tunazoziunda katika maisha haya zitaathiri maslahi/mambo yetu ya umilele, kwamba hatima yetu ya umilele inategemea tabia zilizo thabiti katika kiasi, tungelipambana kuhakikisha kuwa tunakuwa na kiasi kilicho thabiti katika kula na kunywa. Kwa mfano wetu na jitihada zetu binafsi tunaweza kuwa njia ambazo kwazo nafsi nyingi zitaokolewa kutoka katika mmomonyoko wa kukosa kiasi, makosa ya jinai, uhalifu na kifo. Dada zetu wanaweza kufanya zaidi katika kazi iliyo kuu ya kuokoa wengine kwa kuzijaza meza zao kwa vyakula vyenye afya na vyenye kurutubisha pekee. Wanaweza kutumia muda wao wa thamani katika kuwafundisha watoto wao shauku sahihi na hamu, katika kuwahamasisha/kuwaundia tabia za kiasi katika mambo yote, na katika kuwahimiza kujikana nafsi na ukarimu ulio mwema kwa wengine. 3T 489.1

Walakini mbali na mfano ambao Kristo ametupatia alipokuwa katika jangwa la majaribu kwa kukataa uchu wa chakula na kuishinda nguvu yake, kuna akina mama wengi wa Kikristo ambao kwa mfano wao na kwa elimu wanayoitoa kwa watoto wao wanawaandaa kuwa walafi na walevi kupindukia. Watoto mara kwa mara wanaendekeza tabia ya kula wanachokichagua wao na kwa wakati wanaoutaka wao, pasipo kuzingatia afya. Kuna watoto wengi ambao ni walafi waliofunzwa tangu utotoni. Kwa kupitia kuendekeza uchu wamekuwa na matatizo ya chakula kutomeng'enywa chakula vyema katika matumbo yao wangali na umri mdogo * kuvembewa/Dyspeptic. Hali ya kuendekeza uchu na kukosa kiasi katika kula inakua na kuimarika kuenda na umri wao. Nguvu za kiakili na kimwili zinadhoofishwa kama matokeo ya wazazi wao kuendekeza uchu wa chakula. Ladha inaundwa kwa baadhi ya aina za chakula ambacho hakina manufaa yoyote, bali kinajeruhi; na kwa kadiri mfumo unavyochoshwa, mwili unadhoofika mno [Pizza, pilipili, nyama]. 3T 489.2

Wachungaji,watumishi, walimu, na wanafunzi si wenye akili mahiri au werevu kama wanavyopaswa kuwa katika suala la umuhimu wa mazoezi ya viungo katika sehemu ya wazi yenye hewa. Wanapuuzia wajibu huo, ambao ni wa muhimu zaidi katika utunzaji wa afya. Wanatumikisha akili zao katika vitabu na kula mshahara wa mtu aliyefanya kazi. Kwa tabia hizo baadhi wananenepa ovyo (obese), kwa kuwa mfumo umeziba. Wengine wanakuwa wakengeufu, wembamba, wanyonge, na wadhaifu kwa sababu nguvu zao za asili zimeharibiwa kwa ulafi wa chakula; ini

linaelemewa na hatimaye linashindwa kuondoa uchafu kwenye damu, na matokeo yake ni ugonjwa. Kama mazoezi ya mwili yangejumuishwa pamoja na mazoezi ya kiakili, mzunguko wa damu ungeongezeka, utendaji kazi wa moyo ungekuwa mkamilifu zaidi, takataka zingelitolewa nje, na maisha mapya na nguvu/ari vingeonekana katika kila sehemu ya mwili. 3T 489.3

Wakati akili za wachungaji, watumishi, walimu mashuleni, zinapozidi kusisimuliwa katika masomo, na mwili kuachwa bila kazi, neva za hisia zinaelemewa, wakati neva za mwendo zinaachwa bila kazi. Huku uchovu ukiwa katika ogani za kiakili, wanashughulika kupita kiasi na kudhoofika, na ilhali misuli inapoteza nguvu na uwezo wake kwa kukosa shuguli. Hakuna mwelekeo wa kufanya mazoezi ya misuli kwa kuhusika katika shughuli za kimwili kwa sababu kufanya hivyo kunaonekana kuchosha. 3T 490.1

Wachungaji/watenda kazi wa Kristo, wanaodai kuwa ni wawakilishi Wake, wanapaswa kufuata mfano Wake, na zaidi ya yote wanapaswa kutengeneza tabia za uthabiti katika kiasi. Wanapaswa kudumisha maisha na kielelezo cha Kristo mbele za watu kwa maisha yao ya kujikana nafsi, kujitoa sadaka, na ukarimu ulio hai (usio na ubinafsi). Kristo alishinda uchu kwa niaba ya mwanadamu, na kwa niaba yake wanapaswa kuonesha mfano wa kuigwa kwa wengine. Wale ambao hawaoni umuhimu wa kuhusika katika kazi ya kushinda tamaa ya chakula watashindwa kupata ushindi wa thamani ambao wangeweza kuupata, na watakuwa watumwa wa uchu na tamaa mbaya za mwili, ambavyo vimejaza kikombe cha maasi ya wote wakaao duniani. 3T 490.2

Watu wanaojihusisha na kupeleka ujumbe wa mwisho wa maonyo kwa ulimwengu, ujumbe ambao utaamua hatima ya nafsi za watu, wanapaswa kufanyia kazi kwa vitendo katika maisha yao wenyewe Kweli wanazozihubiri kwa wengine. Wanapaswa kuwa mifano kwa watu katika kula kwao, kunywa kwao, na katika mazungumzo yao na mwenendo na mwonekano. Ulafi, kuendekeza shauku zisizo na thamani za kumshusha mtu chini, na dhambi za kuhuzunisha vimesitirika chini ya mwamvuli wa utauwa kwa wengi wanaojiita kuwa wawakilishi wa Kristo kote ulimwenguni. Kuna watu walio na uwezo wa asili ulio bora sana ambao utendaji kazi wao haufiki hata nusu ya vile ambavyo ingelikuwa kama wangelikuwa na kiasi katika mambo yote. Kuendekeza uchu na shauku kali hudhoofisha akili, vinapunguza nguvu ya kimwili, na kudhoofisha nguvu ya kimaadili. Mawazo yao sio ya wazi. Maneno yao hayazungumzwi katika nguvu, hayatiwi nguvu ya uweza wa Roho wa Mungu ili yapate kuifikia mioyo ya wanaosikiliza. 3T 490.3

Kama vile wazazi wetu wa kwanza walivyoipoteza Edeni kwa kuendekeza tamaa ya chakula yaani matamanio yamwili, tumaini letu pekee la kuirejeza Edeni liko katika kujizuia kuliko thabiti katika tamaa ya chakula na shauku kali. Kujizuia katika chakula na kutawala shauku zote kutadumisha ubora wa kiakili na kuleta nguvu ya kiakili na ya kimaadili, inayowawezesha watu kuweka hali zao za asili

chini ya utawala wa nguvu za juu zaidi na kutofautisha kati ya lililo baya na lililo jema, lililo takatifu na la kawaida. Wale wote ambao wana utambuzi wa Kweli kuhusu kafara iliyotolewa na Kristo kwa kuacha makazi Yake mbinguni kuja katika ulimwengu huu ili apate kumwonesha mwanadamu jinsi ya kuyapinga majaribu kupitia maisha Yake Mwenyewe kwa uchangamfu watajikana nafsi na kuchagua kuwa washirika pamoja na Kristo katika mateso Yake. 3T 491.1

Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima. Wale wanaoshinda kama Kristo alivyoshinda watahitaji kudumu katika kujilinda wao wenyewe dhidi ya majaribu ya Shetani. Uchu na shauku kali vinapaswa kuzuiwa na kuwekwa chini ya utawala na dhamiri ya Kweli, iliyoangaziwa ili kwamba akili iwe imara pasipo kulemaa, na nguvu ya utambuzi iwe safi, ili kwamba matendo ya Shetani na mitego yake visije vikatafsiriwa kuwa ni mibaraka na majaliwa ya ya Mungu. Wengi wanatamani ijara ya mwisho na ushindi ambavyo watapewa walioshinda, lakini hawapo tayari kuvumilia taabu, ufukara, na kujikana nafsi, kama alivyofanya Mwokozi. Ni kupitia utii tu na jitihada endelevu peke yake ndipo tutashinda kama Kristo alivyoshinda. 3T 491.2

Nguvu ya uchu wa chakula inayotawala itashuhudia kuleta uharibifu kwa maelfu ya watu, wakati ambapo, kama wangelipata ushindi katika hili, wangelipata nguvu ya kimaadili ambayo ingeliwafanya kuwa washindi katika kila jaribu la Shetani. Lakini wale ambao ni watumwa wa hamu ya chakula watashindwa kuwa wakamilifu wa tabia ya Kikristo. Uasi endelevu wa mwanadamu kwa miaka elfu sita umeleta ugonjwa, maumivu, na kifo kama matunda yake. Na kwa kadiri tunavyokaribia mwisho wa wakati, jaribu la Shetani la kuendekeza uchu litakuwa na nguvu kubwa zaidi na gumu zaidi kulishinda. 3T 491.3

SURA YA 44

UONGOZI

Kaka A uzoefu wako kuhusu uongozi miaka miwili iliyopita ulikuwa ni kwa ajili ya manufaa yako mwenyewe na ulikuwa wa muhimu mno kwako. Ulikuwa na mawazo ya msingi yaliyo wazi, uliyoyaamua kuhusu uhuru binafsi na haki binafsi ya kuamua. Mawazo haya uliyonayo yanakuwa yamepitiliza. Unafikiri kuwa ni lazima uwe na nuru na uthibitisho kwa ajili yako mwenyewe kuhusu wajibu wako. 3T 492.1

Nimekuwa nikioneshwa kwamba hakuna maamuzi ya mtu yanayopaswa kusalimishwa kwa mtu awaye yote. Lakini wakati maamuzi ya Konferensi Kuu (General Conference), ambayo ni mamlaka ya juu kabisa ya Mungu hapa duniani, yanapotolewa, uhuru binafsi na maamuzi binafsi hayapaswi kusalia, bali kusalimishwa. Kosa lako lilikuwa katika kushinikiza kuendeleza maamuzi yako binafsi kuhusu wajibu wako kinyume na sauti ya mamlaka ya juu kabisa ambayo ni ya Bwana hapa duniani. Baada ya kujitafutia muda wako mwenyewe, na baada ya kazi kuwa imekwamishwa kwa kiasi kikubwa kwa kuchelewa kwako, ulikuja Battle Creek kuitia miito iliyojirudia na ya ghafla iliyotumwa kwako toka Konferensi Kuu. Uliendelea kungang'ania kwamba ulikuwa sahihi katika kufuata msimamo wako mwenyewe katika kutenda wajibu. Uliona ya kuwa ni vyema kwako kuendelea kung'ang'ania msimamo wako wa uhuru. Haukuonekana kuwa na hisia ya kweli juu ya mamlaka ambayo Mungu ameyatoa kwa kanisa Lake kupitia sauti ya Konferensi

Kuu. Ulifikiri ya kuwa kwa kuitikia mwito uliopewa na Konferensi Kuu ulikuwa unajisalimisha kwa maamuzi na akili ya mtu mmoja. Ulidhihirisha wazi uhuru, roho yenye nia iliyokazwa, ambayo haikuwa sahihi. 3T 492.2

Mungu alikupatia uzoefu wa thamani kwa wakati ule ambao ulikuwa wa maana mno kwako, na ambao ulikuongezea mafanikio ya kwako kama mchungaji/mtumishi wa Kristo. Nia yako ya kiburi na kutokubali kushindwa ilitiishwa. Ulikuwa na uongofu halisi. Hii iliakisiwa pia katika wadhifa wako wa uongozi. Kanuni zako kuhusu uongozi ni sahihi, bali hauzitumii ipasavyo. Kama ungeliacha mamlaka ya kanisa, sauti na maamuzi ya Konferensi Kuu, visimame mahala ambapo umemuweka mume wangu, pasingelikuwa na kosa lolote lile ambalo lingelipatikana katika nafasi yako. Lakini unakosea sana kwa kuvipatia akili na maamuzi ya mtu mmoja mamlaka na mvuto ule ambao Mungu amewekeza kwa kanisa Lake kupitia maamuzi na sauti ya Konferensi Kuu. 3T 493.1

Wakati uwezo huu ambao Mungu alilipatia kanisa unapoidhinishwa kwa mtu mmoja, na kukabidhiwa mamlaka ya kutoa maamuzi kwa ajili ya wengine, ndipo mpangilio wa Kweli wa Biblia unapobadilishwa. Jitihada za Shetani kwa akili ya mtu kama huyu itakuwa ya hila sana na wakati mwingine yenye nguvu ya kulemea sana, kwa sababu kupitia akili ya namna hii anafikiri kuwa anaweza kuwaathiri wengine. Nafasi yako kwenye uongozi ni sahihi, kama unaipa mamlaka ya juu sana kimuundo kile ulichompatia mtu mmoja pekee. Mungu kamwe hakuunda kwamba kazi Yake ibebe muhuri wa akili ya mtu mmoja na maamuzi ya mtu mmoja. 3T 493.2

Sababu kubwa ya kwa nini Ndugu B na C wamepungukiwa uzoefu waliopaswa kuwa nao sasa ni kuwa hawajitegemei. Wamekimbia wajibu wao kwa sababu kama wangelitimiza mapungufu yao yangeliwekwa katika nuru. Wameridhia kwamba mume wangu aongoze na kubeba majukumu, na wameruhusu yeye awe kwao mhimili wa akili na maamuzi. Ndugu hawa ni dhaifu wakati ambapo walipaswa kuwa imara. Hawajathubutu kufuata uhuru wa maamuzi yao wenyewe, wasije wakafanya makosa na kulaumiwa kwayo, na ili hali wapo tayari kujaribiwa na kumwajibisha mume wangu kama walidhani kuwa wataona makosa katika njia yake. Hawajabeba majukumu pamoja naye. Wameendelea kuyarudisha kwa mume wangu, na hivyo kumfanya abebe majukumu ambayo walipaswa kushirikiana naye, mpaka wanakuwa dhaifu kwa vigezo ambavyo kwavyo walipaswa kuwa imara. Ni dhaifu wa nguvu za kimaadili wakati wanaweza kuwa miamba, walio na sifa kusimama kama nguzo katika kazi ya Mungu. 3T 493.3

Ndugu hawa hawana uwezo wa kujitegemea wao binafsi, au ujasiri kwamba Mungu atawaongoza kabisa kama wanafuata mwangaza ambao amewapatia. Mungu kamwe hakukusudia kuwa watu wenye nguvu, walio na uwezo mkubwa ulio huru

wa kiakili wawategemee wengine ili wapate kusaidiwa kama mmea wa mwefeu utambaavyo mwaloni (mfano passion fruit-mpasheni unavyotambaa kwenye miti mingine). Magumu yote, vikwazo, vizuizi, na kukatishwa tamaa ambako watumishi wa Mungu watapitia katika kutenda kazi vitawatia nguvu tu katika kutengeneza tabia sahihi. Kwa kuweka nguvu zao wenyewe za kiakili katika utumishi, makwazo wanayokutana nayo yatageuka kuwa baraka chanya. Wataongezekewa misuli ya kiakili na ya kiroho kwa ajili ya kutumika katika matukio muhimu na kuleta matokeo bora sana. Watajifunza kujitegemea wao wenyewe na watapata ujasiri kwa uzoefu wao wenyewe kuwa Mungu anawaongoza na kuwaonesha njia kwelikweli. Na kwa kadiri wanavyokutana na hatari na kuwa na uchungu rohoni wanawiwa kutafakari na wanawezeshwa kuhisi umuhimu wa sala katika jitihada yao ya kusonga mbele kwa ufahamu na kuwajibika kwa ajili ya manufaa ya kazi ya Mungu; wanatambua kuwa migogoro na mfadhaiko ni kwa ajili ya kufanyia zoezi imani na tumaini katika Mungu, na kwa ajili ya uimara ambao unaleta nguvu. Shida zinaendelea kuibuka kwa namna na mbinu mbalimbali tena kwa ghafla. Tunaitwa kutumia uwezo ambao ungelidumaa kama haukukutana na shida zisongazo katika kazi ya Mungu. Hii inaleta uzoefu mbalimbali ili kwamba pasiwepo na kutumika kwa watu wenye wazo moja tu na wale ambao wana ukuaji hafifu au nusunusu. 3T 494.1

Watu wenye uweza na nguvu katika suala hili, ambao Mungu atawatumia kwa utukufu Wake, ni wale ambao wamekuwa wakipingwa, wakichanganywa, na kuzuiwa katika mipango yao. Ndugu B na C wangeliweza kugeuza kushindwa kwao kuwa ushindi wa muhimu; lakini, badala ya hili, wamekimbia/wameacha majukumu ambayo kupitia kwayo makosa yangelipata utatuzi. Ndugu hawa wa thamani wameshindwa kuipata elimu ambayo inaimarishwa kupitia uzoefu ambayo haipatikani kwa kusoma na kujifunza pamoja na faida nyinginezo zote. 3T 494.2

Wewe, Kaka A, umekuwa na uimara wa kubeba baadhi ya majukumu. Mungu amekubali kazi zako zenye nguvu na kubariki jitihada zako. Umefanya makosa katika baadhi, lakini kwa sababu ya huko kushindwa katika baadhi ya sehemu kamwe usitilie shaka uwezo wako wala kushindwa kuamini nguvu unayoweza kuipata katika Mungu. Umekosa utayari wa kuyabeba majukumu. Una mwelekeo wa asili wa kuyakwepa majukumu na kuchagua wadhifa mwepesi, kuandika na kuishughulisha akili mahali ambapo hakuna vitu maalumu au vya msingi vinaendelea. Unafanya makosa kwa kutegemea mume wangu akuambie cha kufanya. Hii sio kazi ambayo Mungu amempatia mume wangu. Unapaswa kujua nini cha kufanya na kubeba mizigo isiyokubalika wewe mwenyewe. Mungu atakubariki kwa kufanya hivyo. Unapaswa kubeba mizigo inayohusiana na kazi ya Mungu kulingana na uamuzi wako mzuri. Lakini unapaswa kujihadhari uamuzi wako usije ukachochewa na mawazo ya wengine. Kama ni dhahiri ili kuwa umefanya makosa, ni fursa kwako kugeuza kushindwa huku kuwe ushindi kwa kuyaepuka

hayo wakati ujao. Kwa kuambiwa nini cha kufanya kamwe hautaongezekewa uzoefu wowote wa muhimu kwa ajili ya wadhifa maalumu. 3T 495.1

Vivyo hivyo kwa wote wale walioaminiwa kushika nyadhifa tofauti tofauti katika ofisi mbalimbali Battle Creek. Hawapaswi kubembelezwa, kudekezwa na kusaidiwa kila wakati, kwa kuwa kufanya hivyo hakutawafanya wajipatie uwezo wa kushika nyadhifa maalumu. Vikwazo ndivyo vinawafanya watu kuwa imara. Sio misaada, bali ni magumu, migogoro, kukataliwa, kunakowafanya watu wawe na nguvu za kimaadili. Urahisi wa kupindukia na kukwepa majukumu vimewafanya wawe wadhaifu na waliodumaa wakati ambapo wangelikuwa watu wanaowajibika wenye nguvu za kimaadili na misuli imara ya kiroho. 3T 495.2

Watu waliotarajiwa kuwa wa Kweli katika kila dharura kama ncha ya kaskazini na dira ya compasi, wamekuwa wasio na ufanisi na wazembe kwa jitihada zao za kuepuka shutuma na kwa kuyakabili majukumu huku wakiwa na hofu ya kushindwa. Watu wenye uwezo wa hali ya juu wa kiakili wanakuwa vitoto tu katika kazi kwa sababu ni waoga kushika na kubeba mizigo waliyopaswa kuibeba. Wanapuuza kuwa na ufanisi hodari. Kwa muda mrefu wamemtumaini na kumwachia mtu mmoja kupanga kwa ajili yao na kuwaza kwa ajili yao wakati ambapo wana uwezo mkubwa wa kufanya wao wenyewe kwa maslahi ya kazi ya Mungu. Katika kila hatua tunakutana na upungufu wa kiakili. Watu wanaoridhika kuwaacha wengine wapange na kuwafanyia kazi ya kufikiri kwa ajili yao hawajapevuka vya kutosha. Kama wangeliachwa wapange mambo kwa ajili yao wenyewe wangelionekana kuwa ni watu wenye busara na wafuatiliaji. Lakini wakiwekwa kwenye muunganiko na kazi ya Mungu, ni kitu kingine tofauti kabisa kwao; wamepoteza uwezo huu wote kabisa. Wametosheka kubakia kama watu wasio na ujuzi na wasio na uwezo kana kwamba wengine wanapaswa kuweka mipango na kufikiri kwa niaba yao. Baadhi ya watu wanaonekana kwa kusemwa kuwa hawawezi hata kutengeneza njia kwa ajili yao wenyewe. Je, ni lazima wawategemee wengine kuwawekea mipango na mambo yao na kuwafanya kuwa fikra na maamuzi yao? Mungu anaaibishwa kwa askari wa namna hiyo. Hafurahishwi/aheshimiwi kwa wao kuwa na sehemu yoyote ya kutenda katika kazi yake na huku wao ni mashine tu. 3T 495.3

Wanahitajika watu wasio tegemezi na wenye jitihada za dhati, sio watu wanaobadilika shepu kama unga uliokandwa wa maandazi yanayoenda kupikwa. Wale wanaotaka wafanyiwe kazi yao, wanaotaka kiwango maalumu cha kazi ya kufanya na mshahara maalumu, ambao wanatamani kuthibitisha kuwa wanachukuliana na hali kabisa pasipo kuwa na matatizo yatokanayo na kutozoea kazi au kujifunza, hao si watu ambao Mungu anawaita kwa ajili ya kushughulika katika kazi yake. Mtu ambaye hawezi kuuzoeza uwezo alionao na kuchukuliana na mambo, ili aweze kufaa katika kila sehemu iwapo umuhimu utahitajika si mtu wa

wakati huu. Watu ambao Mungu atawaunganisha katika kazi Yake si wasionyumbulika/viwete na wadhaifu, wasio na msuli au nguvu ya kimaadili katika tabia. Ni kwa kupitia utendaji kazi ulio endelevu na wa kudumu ndipo watu wanaweza kunidhamishwa kubeba jukumu katika kazi ya Mungu. Watu hawa hawapaswi kuvunjika moyo katika hali na mazingira si rafiki sana. Hawapaswi kukata tamaa katika lengo kwamba wameshindwa kabisa mpaka wameshawishika bila shaka yoyote kuwa hawawezi wakafanya zaidi kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kwa ajili ya nafsi. 3T 496.1

Wapo watu wanaojisifu mno kuwa wangefanya makubwa na mazuri kama wangeliwekwa katika mazingira tofauti, na ilihali hawatumii uwezo walionao tayari kwa kuwajibika katika nyadhifa ambazo wamejaliwa. Mtu aweza kutengeneza mazingira yake, lakini kamwe mazingira hayapaswi kumtengeneza yeye. Mtu anapaswa kuyakamata mazingira kama vyombo vyake vya kufanyia kazi. Anapaswa kuyatawala mazingira, lakini asiruhusu kamwe kutawaliwa nayo. Kujitegemea binafsi na uwezo binafsi ni sifa zinazohitajika sasa. Tabia ya kujitegemea binafsi haipaswi kufishwa, bali inapaswa kurekebishwa, kusafishwa, kukuzwa na kuratibiwa. 3T 496.2

Nilioneshwa kuwa ni wajibu wa mume wangu kuachana na majukumu ambayo wengine wangelifurahi kumwona akiyabeba kwa kuwa inawaepusha na kuwatolea udhuru, kufanya mambo mengi yaliyo magumu. Uamuzi uliyo tayari na utambuzi ulio bayana wa mume wangu, ambavyo amevipata kupitia kujifunza kwake na mazoezi, vimemsababishia kubeba majukumu mengi ambayo yalipaswa kubebwa na wengine. 3T 497.1

Kaka A, unaenda polepole mno. Unapaswa kukuza sifa nyinginezo. Kazi ya Mungu inahitaji watu ambao wanaoweza kuona haraka na kutenda papo hapo kwa wakati sahihi na kwa nguvu. Kama utangoja kupima kila jambo lililo gumu na kulinganisha kila mfadhaiko unaokutana nao utafanya machache. Utakuwa na vikwazo na magumu ya kupambana nayo kila mara, na unapaswa kwa ujasiri kuamua kuyashinda, la sivyo yatakushinda wewe. 3T 497.2

Wakati mwingine njia na makusudi mbalimbali, namna tofauti za kutenda kazi kuhusiana na kazi ya Mungu, vinakuja akilini na vina msawaziko mzuri; lakini ni katika wakati huu ambapo upambanuzi yakinifu ni wa muhimu. Na kama lolote linakamilishwa lazima lifanyike kwa wakati sahihi na muafaka. Kuyumbayumba kwa mizania hata kuwe kudogo kwa namna gani kunapaswa kuonekane na tatizo lapaswa kugundulika mara moja. Kuchelewachelewa kwa muda mrefu kunawachosha malaika. Ni bora hata kufanya maamuzi na kukosea wakati mwingine kuliko kuwa katika hali ya kuyumbayumba, kusitasita, na wakati mwingine kuegemea upande mmoja, na kisha upande mwingine. Mfadhaiko na

unyonge mwingi ni matokeo ya kusitasita na kutilia shaka zaidi kuliko wakati mwingine kusonga mbele kwa haraka. 3T 497.3

Nimekuwa nikioneshwa kuwa ushindi wa ajabu mno na kushindwa/vipigo vya kutisha vimetokea kufumba na kufumbua tu, kwa dakika chache. Mungu anataka wepesi katika kutenda. Kukawia, mashaka, kusitasita, na hali ya kushindwa kufanya maamuzi mara kwa mara vinampatia adui kila faida. Ndugu yangu unahitaji kufanya matengenezo. Kupangilia mambo kunaweza kueleza mengi kuhusu Ukweli. Mara kwa mara kushindwa kunatokana na ucheleweshaji. Patakuwepo na migogoro katika kazi hii. Tendo la haraka na la kimaamuzi likitendwa kwa wakati sahihi ushindi wa kishindo utapatikana, wakati kusuasua na kupuuza kutaleta anguko kuu na fedheha kali kwa Mungu. Kutenda kwa kasi katika nyakati dharura/muhimu mara zote kumemdhoofisha adui, na anakatishwa tamaa na kushindwa, kwa kuwa angelitarajia kuweka mipango na kutenda kwa werevu mno kutokana na muda uliopo. 3T 497.4

Mungu anataka watu wanaojihusisha na kazi yake waliopo Battle Creek ambao wana uwezo wa kufanya wajibu wa maamuzi sahihi wakati wa dharura, ambao panapokuwa na umuhimu, akili zao zitatenda kwa kasi ya umeme/radi. Kuwa mwepesi bila kusita muhimu mno katika saa ya janga na hatari. Kila mpango waweza kuwekwa vizuri kabisa ili kukamilisha matokeo au malengo fulani, na bado ucheleweshaji wa muda mfupi sana unaweza kuyafanya mambo yawe tofauti kabisa, na malengo makuu ambayo yangeliweza kufikiwa yanapotea kwa kukosa wepesi wa kuona kabla na kuitikia kwa wepesi. Mengi yanaweza kufanywa ili kuizoeza akili iepukane na uvivu. Kuna nyakati ambapo tahadhari na tafakari ya kina ni vya muhimu; kutokuwa na subira na kuharakisha bila kufikiri kunaweza kuwa ni upumbavu. Lakini hata hapa, mengi yamepotea kwa kusuasua kwa hali ya juu. Tahadhari, kwa kiwango fulani, inahitajika; lakini kusitasita na kuendekeza sera ya kuwa na busara kupita kiasi katika matukio fulani vimeleta hatari zaidi kuliko ambayo inaweza kuletwa kwa kuharakisha mambo. 3T 498.1

Ndugu yangu unahitaji kukuza wepesi. Achana na tabia yako ya kusitasita. Unafanya kazi kwa polepole sana unasita kusogea taratibu na unapuuzia kuikamata kazi na kuikamilisha. Unapaswa kuachana na tabia hii finyu ya utendaji kazi; kwa kuwa si njema. Wakati ambapo kutoamini kumeijaza nafsi yako, utendaji kazi wako unakuwa wa kusitasita, kusimama, wa kulinganisha kiasi kwamba hakuna unalokamilisha na umekwamisha wengine wasifanye lolote. Shauku yako i katika kuona magumu na kuanzisha mashaka, lakini hauna shauku au ujasiri wa kuyashinda magumu au kuondoa mashaka. Katika nyakati kama hizo unahitaji kujisalimisha kwa Mungu. Unahitaji nguvu ya tabia, kutokuwa na ubishi pamoja na utayari. Huku kuwa taratibu na tepetepe kama konokono katika kutenda, au kutegea ni moja ya kasoro kubwa katika tabia yako na kunakuzuia usisonge mbele na usiwe na manufaa. 3T 498.2

Hali ya kusuasua polepole katika kufanya maamuzi unayoionesha katika kusudi na kazi ya Mungu wakati mwingine inaumiza. Wala si ya muhimu kabisa. Kuamua kutenda kwa wepesi kutaleta matokeo makuu. Umekuwa ukionesha utayari wa kutenda unapojisikia kufanya hivyo, tayari kufanya unapoona lipaswalo kufanywa kwa wazi; lakini unashindwa kuwa faida ambayo ungekuwa kama ungelikuwa mwenye utayari na mwenye maamuzi katika wakati muhimu, na kushinda silika ya kusitasita na uchelewaji ambavyo vimekuwa ndiyo tabia yako na kuzorotesha kwa kiasi kikubwa kazi ya Mungu. Kasoro hii, isiposhughulikiwa, italeta hatari kubwa katika nyakati za migogoro kwenye kazi na kuihatarisha nafsi yako mwenyewe kwa kifo. Lazima ujali muda na utende kwa maamuzi sahihi na kwa wakati sahihi, kwa kuwa huna sifa hizi. Katika vita na mapambano ya mataifa mara zote kuna faida ipatikanayo kwa kutawala vema tendo la haraka kuliko kupambana na adui kizembe ukiwa umedhamiria. 3T 499.1

Uwezo wa kufanya shuguli/kazi ikamalizika na bado ikafanyika kwa ukamilifu ni uwezo mkuu. Ndugu yangu, umekuwa ukihisi moyoni kabisa, kuwa uelekeo wako wenye hadhari, na kusita ulistahili kusifiwa, na kwamba ni wema zaidi kuliko kosa. Lakini kutokana na kile ambacho Bwana amenionesha kuhusiana na suala hili, la kufanya vitu polepole kama konokono ambayo ni sehemu yako limefanya ukwamishe kwa kiasi kikubwa kazi ya Mungu na kusababisha mambo mengi kutofanyika ambayo kwa haki yangefanyika kama yangelitendwa kwa wakati na kasi. Itakuwa vigumu sasa kwa wewe kufanya mabadiliko ya tabia ambayo Mungu anakutaka uyafanye, kwa kuwa tangu ujana haukujali muda na kutenda kwa kasi inayohitajika. Tabia inapoundwa, na mazoea huthibitika, na uwezo wa kiakili na kimaadili kuimarika, ni vigumu zaidi kuondoa mazoea yenye makosa, na kuwa na wepesi katika kutenda. Unapaswa kutambua thamani ya wakati. Huna kisingizio kwa kuacha kazi iliyo ya muhimu sana, japo haivutii, huku ukitarajia kuikwepa kabisa, au ukifikiri kuwa kuna wakati itakuwa na unafuu na kufurahisha, na ili hali unatumia muda wako kwa mambo yafurahishayo yasiyotumia nguvu nyingi au juhudi. Unapaswa kwanza kufanya kazi ambayo ni lazima ifanyike na inayohusisha maslahi makuu katika kazi, na kisha kushughulikia mambo yenye umuhimu mdogo mara baada ya kuwa yale yaliyo ya msingi yamekwishakamilika. Uzingatiaji wa muda na uwezo wa kufanya maamuzi katika kazi na kusudi la Mungu ni vipengele vya msingi mno. Uchelewesho katika kutenda kwa hakika ni kushindwa au maanguko. Dakika ni za thamani mno na zinapaswa kutumika vizuri kabisa. Mahusiano ya kidunia na maslahi binafsi yanapaswa kuwa ya pili. Kamwe kazi ya Mungu isiachwe ikazorota, hata mara moja, kwa sababu ya marafiki zetu wa kidunia au ndugu zetu wapendwa. 3T 499.2

“Akamwambia mwingine, Nifuate. Akasema, Bwana, nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe

enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Mtu mwingine pia akamwambia, Bwana, nitakufuata; lakini, nipe ruhusa kwanza nikawaage watu wa nyumbani mwangu. Yesu akamwambia, Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu." 3T 500.1

Hakuna vifungo vya kidunia, hakuna fikra na uzingatiaji wowote wa kidunia, unaoweza hata kwa mara moja kuwekwa katika mizania dhidi ya wajibu tulionao kwa kusudi na kazi ya Mungu. Yesu alihatarisha mahusiano Yake na vitu vyote ili apate kuuokoa ulimwengu uliopotea, na Yeye anatutaka na sisi tujitoe wakfu kweli kweli. Kuna mambo ya kujitoa mhanga kwa ajili ya maslahi ya kazi ya Mungu. Kafara ya hisia ni jitihada kubwa tunayopaswa kuifanya; na bado hata hivyo ni kafara ndogo. Unao marafiki wengi, na kama hisia zimetakasika, hutahisi kuwa unatoa kafara kubwa. Humwachi mke wako miongoni mwa wapagani. Hupewi wito kwenda kukanyaga jangwa ya Afrika lichomalo au kwenda gerezani na kupitia majaribu kila hatua. Kuwa makini na namna unavyozitegemea hisia zako na kuziitikia na kuruhusu hisia za kibinadamu na fikra binafsi vichangamane na jitihada zako na nguvu kazi unayoiweka katika kazi ya Mungu. Bwana Anahitaji huduma isiyo na ubinafsi na ya utayari wa moyo. Unaweza ukaitoa hii na bado ukafanya majukumu yako yote kwa familia yako; ila ulichukulie hili kama suala la kipaumbele cha pili. 3T 500.2

Mume wangu na mimi mwenyewe tumefanya makosa kwa kuidhinisha kufanya majukumu ambayo yalipaswa kufanywa na wengine. Mwanzoni mwa kazi hii mtu alihitajika kushauri, kutekeleza maamuzi, na kuongoza kupigana vita dhidi ya uovu, makosa na kuvishinda vikwazo. Mume wangu alibeba mzigo mzito na kukutana na upinzani mkuu ulioazimiwa. Lakini tulipokuwa taasisi iliyosajiliwa na yenye kupangwa kikamilifu, na baadhi ya watu wakachaguliwa kuwajibika katika nyadhifa zao, ndio ulikuwa muda muafaka kwa mume wangu kukoma kuwajibika kama vile yupo peke yake na kubeba majukumu na mizigo mizito. Kazi hii ilihusisha watu zaidi ya mmoja. Hapa ndipo kosa lilipofanyika kwa nduguze kumhimiza, na yeye mwenyewe kuidhinisha, kubeba mizigo na wajibu ambao amekuwa akiubeba peke yake kwa miaka mingi. Angeliacha majukumu haya miaka kadhaa iliyopita, na yangeligawiwa kwa watu wengine ili waweze kufanya kwa niaba ya watu Shetani angelifurahishwa kuona akili ya mtu mmoja na uamuzi wa mtu mmoja kutawala akili na maamuzi ya wale ambao wanaamini Ukweli wa sasa. 3T 500.3

Mara kwa nyingi mume wangu amekuwa akiachwa mwenyewe mara nyingi, katika kuona na kuhisi mahitaji ya kazi ya Mungu na kutenda kwa wepesi. Viongozi wenzake hawakuwa na upungufu wa uwezo wa akili, lakini walikosa uwezo wa nia ya kusimama katika nafasi ambayo mume wangu amekuwa nayo. Pasipo kufuata utaratibu wameruhusu mwenye kupooza kubeba mizigo na majukumu ya kazi hii, ambayo hakuna hata mmoja kati yao angeweza kuvumilia katika hali yao ya uimara

wa neva na misuli. Wakati fulani amekuwa akiongea kwa ukali na ameongea kwa namna hiyo ili kuonesha kosa. Wakati alipowaona wengine ambao wangelishirikiana katika kubeba majukumu wanakwepa majukumu, ilimuumiza mno moyoni, na akazungumza kwa mihemko/harara. Hakuwekwa katika nafasi hii ya kijinga na Bwana, bali na ndugu zake. Maisha yake yamekuwa ya aina fulani ya utumwa. Majaribu yasiyokoma, hali ya taabu ya kunyanyasika, kuchoka sana kutokana na ubongo kufanya kazi kubwa, havijathaminiwa na ndugu zake. Amekuwa na maisha yasiyo na furaha, na ameongeza huzuni yake kwa kulalamika juu ya wachungaji na watumishi wenzake ambao wamepuuza kufanya yale ambayo wangeliyafanya. Amekuwa na asilia ya kukasirishwa tena na tena. Wakati wenzake wameona hitilafu iliyotokea kwa yeye kushughulika kupita kiasi, hawajaja kuchukua sehemu ya majukumu yao, bali wameamua kumwajibisha kwa kila kitu. Ulikuja kwa uelekevu kubeba majukumu wakati ambapo hakuna wengine ambao wangeliyabeba. Kama wenziwe katika huduma wangelikuza utayari wa kubeba mizigo ambayo walipaswa kuibeba, mume wangu asingeliona na kufanya kazi nyingi ambazo zilitakiwa zifanyike na ambazo alifikiri kuwa hazipaswi kuzipuuziwa. 3T 501.1

Mungu hajayaacha maisha ya mume wangu yafikie mwisho kwa aibu na hali duni namna hii. Yeye Ameendelea kumtegemeza. Lakini mtu anayefanya kazi mara mbili zaidi, anayejaza kazi ya miaka miwili kwa mwaka mmoja, anauteketeza mshumaa wake pande zote mbili (maisha yapunguzwa). Na bado kuna kazi ambazo mume wangu anapaswa kuzifanya ambazo angelizifanya miaka kadhaa iliyopita. Anapaswa kupunguza mapambano, magomvi, mkanganyiko adha, na majukumu ya maisha sasa, ili apate kunawiri, kutulia, kulainishwa tabia na kuimarika na kukomaa kwaajili ya hatua yake ya mwisho ya mabadiliko ya tabia kabla ya kungojea mbingu. Anapaswa kuhifadhi nguvu zake. Hapaswi kuruhusu majukumu ya kazi yamlemee mno, bali anapaswa kuwa huru, mahali ambapo kubaguliwa, chuki, mashaka na tuhuma za ndugu zake havitamwondolea amani. 3T 502.1

Mungu ameruhusu nuru ya kweli ya thamani ing’ae katika Neno Lake na kuangaza akilini mwa mume wangu. Anaweza kuakisi miale ya nuru kutoka katika uwepo wa Kristo kwenda kwa wengine kwa mahubiri yake na nyaraka zake. Lakini wakati akihudumu mezani, akifanya shughuli zihusuzo kazi za kawaida tu za kila siku, amenyimwa, kwa kiwango kikubwa, fursa ya kutumia kalamu na kuhubiri watu. 3T 502.2

Amehisi kuwa aliitwa na Mungu kusimama kuitetea Kweli, na kukaripia, wakati mwingine kwa ukali, wale ambao hawakutendea haki kazi. Shinikizo la kazi, masumbuko na mateso ya ugonjwa mara zote yamemkatisha tamaa, na wakati mwingine amekuwa akiyatazama mambo kwa kuyaongeza chumvi. Wenzake wamechukua manufaa kwa maneno yake, na kwa hulka zake za harara, ambavyo vimekuwa kinyume na utendaji wao wa kusuasua katika kazi na mipango yao finyu

ya utendaji. Wamemsababishia mume wangu matilaba na hisia ambazo hakuwa nazo. Tofauti kubwa kati yao wenyewe na yeye inaonekana kuwa kama ghuba; lakini hii ingelizibika kwa urahisi, kama watu hawa wenye uwezo kiakili wangeliweka maslahi yao pembeni na mioyo yao yote katika kazi ya kuijenga na kuiendeleza kazi iliyo ya Mungu iliyo ya thamani. 3T 502.3

Tunaweza kuweka ushawishi endelevu katika sehemu hii kweny uongozi, mwanzoni mwa kazi, ambao utaendeleza ustawi wa taasisi zetu. Lakini mwenendo wa wengine ambao hawafanyi wanachoweza kufanya, ambao wapo katika hatari ya kujaribiwa na kushindwa, na ambao, kama njia yao ikizuiliwa, hupinga jitihada zetu za dhati kwa ajili ya ustawi wa kusudi la Mungu, inatusukuma sisi kutafuta kimbilio popote pale ambapo tunaweza kufanya kazi bora zaidi na yenye manufaa pasipo kuwa katika hatari ya kuelemewa na mizigo mizito. Mungu ametupatia sisi uhuru mkubwa na mamlaka pamoja na watu Wake hapa Battle Creek. Tulipokuja sehemu hii wakati wa majira ya joto, kazi yetu ilianza kwa dhati, na tangu hapo imekuwa ikindelea hivyo. Changamoto moja baada ya nyingine zimekuwa zikifuatana, na tukawajibika kwa dhati katika kuweka mambo sawa. 3T 503.1

Wakati Bwana alipoonesha kuwa Kaka D aweza kuwa mtu sahihi katika nafasi husika, kama akidumu kuwa mnyenyekevu na mwenye kutegemea nguvu Zake, hakuboronga na kumchagua asiyestahili. Kwa muda huo Kaka D alikuwa na mapenzi ya dhati na alishughulika kama baba katika taasisi ya Afya. Lakini alianza akajikweza yeye mwenyewe, na kujiona kuwa anajitosheleza mwenyewe. Akawa katika njia njia isiyo sahihi. Akajiweka katika hatari ya kujaribiwa. Udhuru ambao viongozi waliutoa kwa wao kupuuzia majukumu yalikuwa ni makosa tu. Kukwepa kwao majukumu na kuwaachia kaka na dada White kumehesabiwa dhidi yao. Ni kusema tu kwamba walipuuzia majukumu yao kwa sababu hayakuwapendeza. 3T 503.2

Niliona kuwa msaada ulikuwa ukihitajika katika ukanda wa Pwani ya Pasifiki. Lakini Mungu asingelipenda kuona tunachukua majukumu au kubeba mikanganyiko ambayo inawahusu watu wengine. Tunaweza kubakia kuwa kama washauri na kuwasaidia kwa mvuto wetu na uwezo wetu wa kufanya maamuzi. Tunaweza kufanya mengi kama hatutaambukizwa na kubebeshwa mzigo ambao unapaswa kubebwa na wengine, na ambao ni muhimu kwa wao kuubeba ili kupata uzoefu ulio wa muhimu. Tunalo jambo la muhimu la kuandikia watu ambalo wanalihitaji sana. Tunayo nuru ya thamani katika Kweli za Biblia ambayo tunapaswa kuiongea kwa watu. 3T 503.3

Nilioneshwa kuwa Mungu hakukusudia kwamba mume wangu abebe mizigo aliyoibeba kwa miezi mitano iliyopita. Sehemu ya utendaji kazi inayohusiana na kazi ya Mungu imeachwa ili imuelemee/imwangukie. Hili limeleta mkanganyiko, kuchakaa, na udhaifu wa neva, ambavyo vimepelekea kukatishwa tamaa na

msongo wa mawazo (sonona). Tangu kuanza kwa kazi pamekuwa na kukosa muafaka katika utendaji kwa upande wa wenzake. Ndugu zake katika huduma wamependa uhuru. Hawajabeba majukumu ambayo wangeliyaweza, na wameshindwa kupata uzoefu ambao wangeliupata ili kuwawezesha kusimama katika nyakati za maamuzi kuhusiana na maslahi yaliyo muhimu ya kazi ya Mungu katika wakati wa sasa na kuwajibika. Wametumia huko kupuuza kwao kubeba majukumu kama kisingizio kwa kuogopa kuakisiwa baada yake. 3T 503.4

Dini tunayodai kuwa nayo imejawa na tabia zetu za asili, tabia na hulka; hivyo basi ni muhimu sana kuimarisha sehemu zetu za tabia zilizo dhaifu kupitia mazoezi na kudhoofisha sifa zote zisizofaa zilizo na nguvu kwa kutenda kinyume chake na kwa kuimarisha sifa kinzani. Hata hivyo baadhi ya ndugu hawajafanya ambayo wangeweza na wanayopaswa kufanya, jambo ambalo lingemtia moyo vya kutosha mume wangu na kumsaidia kubeba baadhi ya majukumu katika katika uongozi wa makao makuu. Watenda kazi wenzake hawakuenenda kwa kujitegemea, kwa kumtazama Mungu ili wapate nuru na majukumu kwa ajili yao wenyewe; hawakufuata majaliwa yake Bwana yaliyo bayana na kushauriana kwa pamoja kuhusu mipango ya utendaji na kuungana katika mipango yao na namna ya kutenda kazi. 3T 504.1

Tangu tulipokuja Michigan majira ya joto yaliyopita, Bwana amebariki hasa kazi za mume wangu. Ametegemezwa kwa namna ya ajabu kufanya kazi kubwa sana iliyotakiwa kufanywa. Kama wale ambao ni washirika pamoja naye wangeamka na kuona na kuelewa mahitaji yaliyopo katika kazi ya Mungu katika kambi letu la mwisho lililofanyika Michigan, mambo mengi ambayo hayakufanyika yangelikuwa yamekamilka. Ilishindikana kukamilisha mahitaji ya tukio. Kama Kaka A angelisimama kwa uchangamfu katika Mungu, akitembea katika nuru, tayari kuona kile ambacho kilitakiwa kufanyika, na kufanya kazi kwa ukamilifu, tungelikuwa na maendeleo kwa miezi sasa katika kazi yetu, na tungeliweza kuanzisha kiwanda cha uchapaji Pwani ya Pasifiki muda mrefu uliopita. Mungu hawezi kutukuzwa kwa kuanguka kwetu katika wingu/giza lilelile na kuendelea kubaki katika wingu. Nuru inaangaza, ijapokuwa tunaweza tusitambue mbaraka wake; lakini kama tunafanya kwa bidii yote kuifikia nuru, na kama tunasonga mbele kadri nuru inavyoangaza, kitambo kidogo tutalipita giza na kuifikia nuru ya kutosha ituangazayo na kutuzunguka kila mahali. 3T 504.2

Katika mkutano wa kambi letu lililopita malaika wa Mungu kwa namna ya pekee walikuja na uweza wao kuwaangazia, kuwaponya, na kuwabariki mume wangu na ndugu Waggoner. Ushindi wa thamani ulipatikana pale ambao haupaswi kupoteza mvuto wake. Nimekuwa nikioneshwa kuwa Mungu kwa namna ya ajabu amekuwa akimpatia mume wangu ishara za upendo Wake na kujali Kwake, pamoja na neema yake endelevu inayotegemeza. [Mungu] amezingatia ari yake na kujitoa kwake katika kusudi na kazi Yake. Hili linatuongoza kwenye unyenyekevu na

shukrani kwa hicho ambacho Mungu amekifanya kwa upande mume wangu. 3T 505.1

Mungu anahitaji wanamgambo, watu ambao wana utayari kwa wakati wowote. Anataka watu ambao, wakati maamuzi ya muhimu yanapohitajika kufanyika, ni waaminifu wa Kweli kama vile mshale wa dira unavyoelekea daima kwenye ncha ya sumaku; watu ambao maslahi yao wenyewe ya muhimu na ubinafsi vimemezwa, kama ilivyokuwa kwa Mwokozi, alipojikita na jukumu moja kuu la wokovu wa roho za wanadamu. Shetani anacheza na akili ya mwanadamu kila apatapo nafasi kwa yeye kufanya hivyo anaporuhusiwa; na anateka muda na sehemu ambayo aweza kuitumia maradufu kwa ajili yake mwenyewe na kusababisha maumivu/madhara makuu katika kazi ya Mungu. Kupuuzia kufanya kile tunachoweza kufanya, na kile ambacho Mungu anatutaka tukifanye katika kazi Yake, ni dhambi isiyoweza kufunikwa kwa kisingizio cha mazingira au hali yoyote, kwa maana Yesu ametoa majaliwa na uwezo kwa wote katika hali na dharura. 3T 505.2

Ndugu yangu, katika kufanya kazi ya Mungu utakutana na mazingira tofauti tofauti ambayo yatahitaji kuhodhi, utulivu na kujitawala nafsi, lakini yatakuandaa wewe kuyakabili mazingira hayo na upekee wa hali husika. Ndipo utaweza kutenda kwa ujasiri na bila aibu. Haupaswi kujikadiria kuwa una uwezo mdogo wa kutenda katika miito mbalimbali maishani. Unapotambua mapungufu, nenda kafanyie kazi ili kuyaondoa mapungufu hayo. Usitegemee wengine wakuondolee mapungufu yako, na ilihali unaenenda tofauti kana kwamba taasisi yako ni lazima ibakie hivyo hivyo. Jitahidi katika kuponya haya mapungufu yako, ili uwe kamili katika Kristo Yesu, na usiyepunguka katika lolote. 3T 505.3

Ukijiona mwenyewe kuwa u bora kupita kiasi, utadhani kuwa kazi unazofanya zina umuhimu mkubwa kuliko uhalisia wake, na utadai uhuru binafsi ambao unafanana na kiburi. Kama ukienda upande mwingine ukaweka wazo la chini mno kuhusu mwenyewe, utajihisi mnyonge na utaacha mwonekano duni ambao utahafifisha kwa kiwango kikubwa mvuto ambao ungelikuwa nao kwa wema. Unapaswa kuepuka ncha hizo zote. Unaweza kuheshimiwa pasipo kujiamini kwa ubatili; unaweza kutosheka na kujishusha pasipo kupoteza heshima yako binafsi au uhuru binafsi, na maisha yako yatakuwa na mvuto mkubwa kwa watu wenye nafasi za juu pamoja na wenye hali ya chini kimaisha. 3T 506.1

Kaka A, hatari uliyonayo sasa ni kuathiriwa na taarifa mbalimbali. Kazi zako ni za kivitendo, ufuatiliaji, na zenye kukata-kata watu. Unawatawala watu kwa kuwapa majaribio kwa ukaribu pamoja na kuwakata-kata (ukali). Hili ni la muhimu katika nyakati fulani; lakini kazi zako zinakuwa ni za namna hii tu, na zinapoteza msukumo wake kama hazitachanganyika na neema ya upole/ulaini, yenye kutia moyo na ya Roho wa Mungu. Unaruhusu maneno ya ndugu zako na marafiki zako maalumu kuathiri maazimio na maamuzi yako. Unawathamini sana na kuwarejelea

na unaingiza maoni yao katika mawazo yako na mara zote unapotoshwa. Unatakiwa kuwa makini na kujilinda. Familia ambazo, watu wake wamekuwa na uhusiano mkubwa zimekuwa na msukumo na ushawishi. Maamuzi yako, maoni yako, hisia zako, vimeathiri, na, matokeo yake, wamekuathiri na wewe pia; na mkondo wenye nguvu utafanyika ambao utakuwa na uelekeo potofu kama hautanyenyekea na kujiweka wakfu kwa Mungu. Kila mambo ya mahusiano haya ya kifamilia kwa asili yanajitegemea na ni ya kuangalia sana, na, kama hayatakuwa na msawaziko (hayana balance) na kutawaliwa na Roho wa Mungu, yanaweza kupitiliza mpaka. 3T 506.2

Kamwe, kamwe usije ukachochewa au kushawishiwa na taarifa. Kamwe usiruhusu mwenendo wako uchochewe na jamaa/ndugu zako wapendwa. Muda umefika ambapo hekima kuu inapaswa kutumika kuhusiana na kusudi pamoja na kazi ya Mungu. Hekima inatakiwa ili kufahamu wakati wa kuongea na wakati wa kukaa kimya. Kutafuta huruma mara zote kunaendekeza ujinga wa tabia potofu kwa kufungua hisia kwa wengine. Mwonekano wako unaita huruma wakati ambapo ingelikuwa bora kwako kama usingelipokea huruma. Ni wajibu ulio wa muhimu kwa wote kufahamu mwenendo wa matendo yao siku kwa siku na nia inayosukuma matendo yao. Wanahitaji kufahamu nia hasa ambayo inachochea matendo fulani. Kila tendo la maisha yao linahukumiwa, sio kwa mwonekano wa nje, bali kwa nia inayochochea tendo hilo. 3T 506.3

Wote wanapaswa kulinda milango ya fahamu, ili Shetani asije akajitwalia ushindi dhidi yao; kwa kuwa hii ndiyo barabara ya kuelekea nafsini/moyoni [masikio, macho, mdomo nk]. Tunaweza kuwa makini/wakali kama tunavyojinidhamisha wenyewe, lakini tunapaswa kuchukua tahadhari tusije tukaziongoza nafsi kukata tamaa. Baadhi hufikiri kuwa Ndugu White ni mtu aliyeazimia kuwa mkali katika kuongea hasa miongoni mwa watu, katika kukemea kile anachofikiri kuwa ni kosa kwao. Anaweza kuwa katika hatari ya kutokuwa mwangalifu kwa namna anavyokemea na kutoakisi mambo; lakini baadhi ya wale wanaolalamika kuhusu namna anavyokemea wametumia lugha inayoumiza, kali, na ya kuhukumu, isiyofaa hata kuongewa kwenye kutaniko, na wamehisi kabisa kuwa wamesuuza nafsi zao na kufanya kazi njema. Lakini malaika wa Mungu mara zote hawaafiki kazi ya namna hiyo. Kama Ndugu White akimfanya mtu mmoja ajisikie kuwa hafanyi lililo jema, kama ni mkali kwa kupitiliza dhidi yake na anahitaji kufundishwa kurekebisha tabia zake, kulainisha roho yake, kuwa mpole, je ni muhimu kiasi gani kwa watumishi wenzake kujiona kuwa wanapotoka kwa kulifanya kutano kubwa liumie kwa makatazo yanayoumiza na shutuma kali, wakati yeye asiye na hatia anaumizwa moyoni na yule aliye na hatia. 3T 507.1

Ni mbaya zaidi, tena sana, kuonesha hisia katika kutaniko kubwa, kumfokea yeyote na kila mtu, kuliko kwenda kwa mtu mmoja mmoja ambaye amefanya kosa na kuwakemea wao binafsi. Kukereka huku kunakoletwa kwa kuongea kwa ukali,

kufoka, na kukemea katika kutaniko kubwa ni tabia ya kuogofya mno machoni pa Mungu kuliko kumkemea mtu mmoja mmoja, binafsi, kwa kuwa watu ni wengi na lawama ni ya ujumla zaidi. Ni rahisi zaidi sana kuonyesha hisia mbele ya kutaniko, kwa kuwa wapo wengi, kuliko kwenda moja kwa moja kwa waliokosa na, uso kwa uso pamoja nao, kwa uwazi, kwa Ukweli, pasipo kuficha kueleza makosa yao. Lakini kupeleka hisia kali za shutuma katika nyumba ya Mungu dhidi ya watu, na kuwafanya wasio na hatia kuumia pamoja na wenye hatia, ni tabia ambayo Mungu haifurahii na inaleta maumivu kuliko kuponya. Imezoeleka kuwa mijadala ya kukosoa na shutuma inafanywa mbele ya kutaniko. Hili halitii moyo roho ya upendo miongoni mwa ndugu. Haiwakuzi kiroho na kuwaongoza kuufikia utakatifu na mbingu, bali roho ya uchungu inaamshwa mioyoni. Mahubiri haya yenye nguvu ambayo yanamkatakata mtu vipande vipande wakati mwingine ni muhimu kuamsha, kutisha, na kuchoma roho. Lakini kama hayatafanyika chini ya uongozi wa Roho wa Mungu, yataumiza zaidi kuliko kuhuisha. 3T 507.2

Nilioneshwa kuwa mwelekeo wa mume wangu si mkamilifu. Mara kadha wa kadha amekosa kwa kulalamika na kukemea kwa ukali mno. Lakini kwa kile nilichokiona, hakukosea sana kwa mwelekeo huu kuliko wengine wanavyochukulia kama nilivyohofia mara kadhaa. Ayubu hakueleweka kwa rafiki zake. Aliwatupia shutuma na kashfa zao wenyewe. Akawaonesha kwamba kama wamemtetea Mungu kwa kuweka wazi imani yao kwake na utambuzi wao wa dhambi, kwa hakika yeye ana ufahamu wa kina na wa kutosha wa jambo hilo kuliko walionao wao. “Ninyi nyote ni wafariji wenye kutaabisha,” ndilo jibu alilolitoa baada yao kukosoa na kushutumu. “Mimi pia”, Ayubu anasema “ningeweza kunena kama ninyi: kama roho zenu zingekuwa mahali pa roho yangu, Ningeweza kutunga maneno juu yenu, Na kuwatikisia ninyi kichwa changu.” Lakini akathibitisha kwamba asingeweza kufanya hili. “Mimi,” anasema, “Ningewatia nguvu kwa kinywa changu na maneno ya midomo yangu ungewatuliza.” 3T 508.1

Ndugu na dada wenye nia njema, lakini wana uelewa finyu na kuangalia kwa nje, wanaweza kujaribu kutoa msaada katika masuala ambayo hawana ufahamu nayo wa kina. Kutokuwa kwao na uzoefu hakuwezi kutambua hisia za mtu aliyesukumwa na wito wa Roho wa Mungu, ambaye amepitia uzoefu mkubwa wa upendo wa dhati na usioelezeka na kuwa na shauku ya kazi ya Mungu na ya kuongoa nafsi ambazo hazijapitia kamwe uzoefu huu, na ambaye amebeba mizigo katika kazi ya Mungu ambayo wengine hawajawahi kuibeba. 3T 509.1

Baadhi ya marafiki wenye matatizo ya kuona, wasio na uzoefu kamili hawawezi, kwa uoni wao hafifu, kutambua na kuthamini hisia za yule ambaye amekuwa na muafaka wa karibu zaidi na nafsi ya Kristo kwa kuhusika katika wokovu wa wengine. Nia yake haieleweki na matendo yake yanasomwa vibaya na wale ambao wangelikuwa marafiki zake, mpaka, kama Ayubu, anaomba ombi la dhati: Niokoe kutoka kwa marafiki zangu. Mungu anashughulikia suala la Ayubu Yeye Mwenyewe.

Uvumilivu wake umejaribiwa vikali; lakini Mungu anapozungumza, mawazo yake yote ya madogomadogo ya upuuzi yanabadilika. Kujihesabia haki alikokua nako kulikuwa ni kwa ajili ya kuhimili shutuma za marafiki zake na si muhimu mbele ya Mungu. Kamwe hakuhukumu vibaya; kamwe hakukosa. Bwana akamwambia Ayubu, “Basi vifunge viuno kama mwanamume,” na Ayubu akasikia haraka sauti toka mbinguni wakati nafsi yake iliposujudu kwa kuhisi hatia ya dhambi zake, na akamwambia Mungu, “najichukia nafsi yangu, na kutubu katika mavumbi na majivu” 3T 509.2

Mungu alipoongea, Mume wangu alisikia sauti sauti Yake; lakini kubeba malaumu na shutuma za rafiki zake ambao hawana uwezo wa kupambanua limekuwa jaribu zito. Wakati nduguze watakaposimama katika mazingira kama hayo, na kubeba majukumu aliyobeba huku wakitiwa moyo kwa kiwango kidogo na kusaidiwa kwa kiwango kidogo kama alivyofanyiwa, ndipo watakapoweza kuelewa namna ya kusaidia, kutegemeza kutambua kutia moyo, kubariki, pasipo kuumiza hisia zake kwa malaumu na shutuma ambazo hakustahili kwa namna yoyote. 3T 509.3

SURA YA 45

MIITO KWA AJILI YA UCHANGISHAJI WA FEDHA/MALI

Nilioneshwa kuwa pamekuwa na matokeo ya kuhuzunisha kutokana na miito ya ghafla/dharura kwa ajili ya uchangishaji wa fedha katika mikutano yetu ya makambi. Suala hili limekuwa likipelekwa kwa kutumia nguvu mno. Watu wengi walio na mali wasingelifanya lolote kama mioyo yao isingelilainishwa na kuyeyushwa kama matokeo ya shuhuda zilizosimuliwa kwao. Lakini walio masikini wameathirika mno na, kwa unyofu wa mioyo yao wameahidi kutoa fedha/mali ambazo moyo ulitamani kuzitoa ila, lakini wakashindwa kuzitoa. Katika mifano mingi miito ya ghafla ya uchangishaji wa fedha imeacha mvuto mbaya kwa baadhi ya watu. Baadhi wamefikiri kuwa pesa ndio kilikuwa kiini cha ujumbe wetu. Wengi wamerudi katika majumba yao huku wakiwa wamebarikiwa kwa kuwa waliifadhili kazi ya Bwana. Lakini kuna mbinu bora zaidi za uchangishaji wa mali, kwa kutoa sadaka ya hiari, kuliko miito ya ghafla katika mikusanyiko yetu mikubwa. Ikiwa wote wataukubali mfumo wa kutoa kwa ukarimu na mpango, na kama washiriki wetu pamoja na watenda-kazi wa utume ni waaminifu katika eneo lao la kazi, hazina itatosheleza pasipo miito hii ya ghafla katika mikusanyiko mikubwa. 3T 510.1

Lakini pamekuwa na upuuzaji mkubwa wa wajibu. Wengi wamezuia fedha ambazo ni za Mungu, na kwa kufanya hivyo wamemnyang'anya Mungu. Mioyo yao ya ubinafsi haijatoa sehemu ya kumi ya mapato yao yote, ambayo Mungu ameidai. Wala hawafika katika mikutano ya mwisho wa mwaka wakiwa na sadaka yao ya hiari, sadaka yao ya shukrani, na sadaka yao ya hatia. Wengi wamekuja mbele za Bwana wakiwa mikono mitupu. "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia Mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia Mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni Baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la." 3T 510.2

Tutakuwa na dhambi sisi kama watu/washiriki, kama hatufanyi jitihada za dhati kuhakiki wale ambao wamechangia katika maeneo mbalimbali na huku wakiwa masikini wasioweza kutoa chochote. Vyote ambavyo, kwa ukarimu wa nafsi zao, wamevitoa vinapaswa virudishwe, tena pamoja na zawadi za ziada kupoza mahitaji yao. Uchangishaji wa pesa umezidi kupita kiasi (umepitiliza). Umeacha mvuto mbaya miongoni mwa walio wengi. Kufanya miito ya ghafla sio mpango ulio bora zaidi wa uchangishaji wa mali. Pamekuwa na hali ya kutojali kuchunguza masuala ya masikini na kuwasaidia, ili kwamba wasiteseke kwa kukosa mahitaji muhimu ya maisha. Kupuuzia jukumu letu kwa namna hii, la kuyafahamu mahitaji ya wale walio wahitaji na kupoza changamoto za mahitaji yao kwa kurudisha mali

zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo ya kazi ya Bwana, itakuwa ni tumempuuza Mwokozi Wetu aliye katika nafsi za watakatifu Wake. 3T 510.3

SURA YA 46

WAJIBU KWA WANAOTESEKA au WATU WALIOPATWA NA MAJANGA

Nilioneshwa baadhi ya mambo kuhusiana na jukumu tulilo nalo kwa walio wanaoteseka/wahitaji ambayo ninajisikia kuwiwa kuwaandikia kwa wakati huu. 3T 511.1

Niliona kuwa ni majaliwa ya Mungu kwamba wajane na yatima, vipofu, viziwi, viwete, na watu wenye matatizo na changamoto mbalimbali, wamekuwa wakiwekwa katika uhusiano wa Kikristo ulio wa karibu kwa kanisa Lake; kwa ajili ya kuwathibitisha watu Wake na kuboresha tabia yao ya Kweli. Malaika wa Mungu wanatazama kuona namna tunavyoshughulika na watu hawa ambao wanahitaji huruma yetu, upendo, na ukarimu wa kweli usio na ubinafsi. Hili ni jaribio la Mungu kwa tabia yetu. Kama tunayo dini ya kweli ya Biblia tutahisi kuwiwa kuonesha upendo, utu wema, shauku, na ukaribu ni kwa ajili ya Kristo kwa niaba ya ndugu zake; na tunaweza kufanya kwa kiwango kikubwa kuonesha shukrani yetu kwa upendo Wake usiopimika kwetu tulipokuwa wenye dhambi tusiostahili neema Yake, kwa kuonesha shauku na ukaribu wa hali ya juu na upendo usio na ubinafsi kwa wale ambao ni ndugu zetu na walio wahitaji zaidi kuliko sisi. 3T 511.2

Kanuni mbili kubwa za sheria ya Mungu ni upendo mkuu kwa Mungu na upendo usio na ubinafsi kwa jirani zetu. Amri nne za kwanza na zile sita za mwisho zimeshikiliwa kwa, au zinachomoza, kutoka katika kanuni hizi mbili. Kristo alielezea kwa mwanasheria nani aliyekuwa jirani yake katika kielelezo cha mtu ambaye alikuwa anasafiri toka Yerusalemu kwenda Yeriko na kuanguka kati ya wezi na wakamnyang'anya na kumpiga na kumwacha karibu na kufa, yaani akichungulia kaburi. Kuhani na mlawi walimwona mtu huyu akiteseka, lakini mioyo yao haikuonesha mwitikio kwa mahitaji yake. Wakamkwepa kwa kupita kando. Msamaria akapita njia ile, na alipoona hitaji la msaada kwa yule msafiri hakuhoji kwamba alikuwa ndugu yake au raia mwenzake au wa imani yake; bali alikwenda kufanya kazi ya kumsaidia aliyekuwa akiteseka kwa sababu kulikuwa na kazi iliyotakiwa kufanywa. Akamhudumia vizuri mno kwa kadiri alivyoweza, akampandisha juu ya punda wake, na kumpeleka katika nyumba ya wageni na kumpatia yaliyokuwa mahitaji ya yule mtu kwa gharama yake mwenyewe. Yesu akasema, msamaria huyu, alikuwa jirani kwa yule aliyeanguka katikati ya wanyang'anyi. Mlawi na kuhani wanawakilisha tabaka katika kanisa ambalo linaonesha kutojali kwa wale wanaohitaji huruma na msaada toka kwao. Hili tabaka pasipo kujali wadhifa wao katika kanisa, ni wavunjaji wa amri. Msamaria

anawakilisha tabaka ambalo ni wakarimu wa Kweli pamoja na Kristo na wanaoiga mfano Wake katika kutenda mema. 3T 511.3

Wale walio na huruma kwa wanaoteseka, vipofu, viwete, wanaoteseka, wajane, yatima, na wenye uhitaji, Kristo anawaita kama watunzao amri, ambao wataurithi uzima wa milele. Ndani kuna-ukosefu mkubwa wa dini binafsi na ukosefu wa kuhisi deni binafsi la kuguswa kwa huzuni za wengine na kushughulika kwa ukarimu usio na ubaguzi kwa ajili manufaa yao wanaoteseka na kuudhiwa. Baadhi hawana uzoefu katika majukumu haya. Wamekuwa na maisha kama ya mlawi na kuhani siku zote, ambao walipita kando. Kanisa linalo kazi ya kufanya, ambayo, kama isipofanyika, giza litatanda kwao. Kanisa kwa ujumla na kwa mtu mmoja mmoja linapaswa kuchunguza kwa uaminifu nia zao na kuyalinganisha maisha yao na mafundisho yaliyo sahihi ya Mfano wetu pekee. Kristo anaheshimu matendo yote ya rehema, ukarimu, na kujali wanayotendewa watesekao, vipofu, viwete, wanaoumwa, wajane, na yatima kama vile yanatendwa Kwake Mwenyewe; na matendo haya yanahifadhiwa katika kumbukumbu za mbinguni na yatatunukiwa. Kwa upande mwingine, kumbukumbu itaandikwa katika kitabu dhidi ya wote walioonesha kutokujali kama walivyofanya kuhani na mlawi kwa wanaoteseka, na wale ambao wanajinufaisha kwa namna yoyote kupitia matatizo ya wengine na kuwaingiza katika tabu ili waweze kufaidika wao wenyewe. Mungu hakika atalipa kila tendo lisilo la haki na kila udhihirisho wa kutokujali na kupuuza wanaoteseka walio miongoni mwetu. Kila mmoja hatimaye atapata thawabu kulingana na matendo yake. 3T 512.1

Nilioneshwa kuhusu kaka E kwamba hakutendewa kwa haki na ndugu zake. Ndugu F, G na wengine walimtendea jambo ambalo halikuwa lenye kufurahisha mbele za Mungu. Kaka F hakuwa na maslahi maalum kwa Kaka E, isipokuwa tu alifikiri angelijinufaisha kupitia yeye. Nilioneshwa kuwa baadhi walimtazama Kaka E kama masikini na asiye mwaminifu. Mungu hapendezwi na mtazamo huu au hukumu hii. Kaka E asingelikuwa na tatizo na angekuwa na mali nyingi za kumtosha yeye mwenyewe kama isingekuwa kusudi lenye ubinafsi la ndugu zake ambao walikuwa na uwezo wa kuona na mali, na kushughulika kinyume naye kwa kutafuta kutumia vipaji alivyonavyo kwa manufaa yao wenyewe yaliyo na ubinafsi. Wale wanaotumia ugumu wa kusoma alionao kipofu na kutafuta kujifaidisha wenyewe kwa mavumbuzi yake, wanafanya unyang’anyi na ni wavunjaji wa amri. 3T 513.1

Kuna baadhi kanisani wanaodai kuwa wanaitunza sheria ya Yehova, lakini ni waasi wa sheria hiyo. Wapo watu wasiotambua madhaifu yao wenyewe. Wana roho ya ubinafsi, na ufukara na wamepofusha macho yao wenyewe kwa dhambi yao ya kutamani, ambayo Biblia imeifafanua kama ibada ya sanamu. Watu wa tabia hii wanaweza kuchukuliwa na ndugu zao kuwa ni Wakristo wa vielelezo bora kweli kweli; lakini jicho la Mungu linausoma moyo na kuyatambua mawazo. Anaona kile ambacho mwanadamu hawezi kukiona katika mawazo na tabia. Kwa majaliwa yake

anawapatia watu hawa nyadhifa ambazo kwazo baada ya muda madhaifu waliyonayo katika tabia yatajifunua, ili kwamba kama wanatamani kuyaona na kuyasahihisha waweze kufanya hivyo. Kuna baadhi ambao maisha yao yote wamekuwa wakishughulikia maslahi/manugaa yao wenyewe na huku wakimezwa na mipango yao ya kibinafsi na kuwa na tamaa ya kujinufaisha wao wenyewe pasipo kujali kuwa wengine wanaweza kufadhaishwa na kusononeshwa kwa mipango au matendo yoyote wayafanyayo. Maslahi yaliyo na ubinafsi yana nguvu kuliko rehema na upendo wa Mungu. Bwana wakati mwingine anaruhusu tabaka hili kuendelea na upofu wa kiroho katika ubinafsi wao mpaka madhaifu yao yatakapodhihirika kwa wote ambao wana utambuzi wa kiroho na kuthibitisha kwa matendo yao kuwa si Wakristo wa kweli. 3T 513.2

Watu wenye mali na afya njema, na ambao wanafurahia mbaraka usiopimika wa uwezo wa kuona, wana manufaa yote kwa kulinganisha na vipofu. Njia nyingi zimefunguka kwao katika biashara zao ambazo zimefungwa kwa mtu asiye na uwezo wa kuona. Watu wanaofurahia matumizi ya viungo vyao vyote hawapaswi kutafuta faida yao wenyewe kwa ubinafsi na kumnyima nduguye aliye kipofu hata chembe moja ya fursa ya kupata mali. Kaka E ni masikini. Ni mdhaifu; na pia ni kipofu. Amekuwa na shauku ya dhati ya kutaka kujisaidia mwenyewe, na, ingawa anaishi chini ya kongwa zito la kasoro zenye kukatisha tamaa, madhaifu yake hayajakausha msukumo wa ukarimu uliopo ndani ya nafsi yake. Kwa ufinyu wa wa hali yake aliyonayo amekuwa akiwa na moyo wa kufanya na amefanya zaidi mbele ya macho ya Mungu kwa wale waliokuwa na uhitaji wa msaada kuliko wengi wa ndugu zake ambao wamebarikiwa kuwa na uwezo wa kuona na kuwa na mali nzuri. Kaka E ana mtaji katika kitivo chake cha mahesabu ya kibiashara na uvumbuzi. Amekuwa akifanya kazi kwa kwa dhati, akijituma huku akiwa na matumaini ya kuvumbua biashara ambayo inaweza kumsaidia yeye mwenyewe asije akawa tegemezi kwa ndugu zake. 3T 514.1

Natamani kwamba wote tuweze kuona kama Mungu aonavyo. Natamani wote tungelitambua namna ambavyo Mungu anawatazama watu wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo, ambao wamebarikiwa uwezo wa kuona na upendeleo waliopewa wa kuwa na mali mikononi mwao, na huku wakiwa na wivu juu ya ustawi mdogo alionao kipofu ndugu yao masikini na ambao wangelijinufaisha wenyewe, kuongeza hazina ya mali, kupitia kasoro ya ndugu yao anayeteseka. Hii inahesabiwa na Mungu kama ubinafsi mbaya zaidi na unyang'anyi/wizi, na ni dhambi inayoudhi, ambayo ni hakika kuwa itaadhibiwa. Mungu hasahau kamwe. Yeye Hatazami mambo haya kwa macho ya kibinadamu na kwa mtazamo wa kibinadamu ulio wa dharau, ubaridi na kutokujali. Yeye Hatazami mambo, kwa mtazamo wa kiulimwengu, bali kwa mtazamo wa rehema, huruma, sikitiko na upendo usio kifani. 3T 514.2

Kaka H alijaribu kumsaidia kaka E, lakini si kwa misukumo yenye ubinafsi. Mwanzoni alijawa na huruma na sikitiko. Aliona kuwa kaka E alihitaji msaada. Lakini ghafla akapoteza shauku, na hisia zilizojawa na ubinafsi zikatiwa nguvu, mpaka kusudi la wenzake kwamba Kaka E awe na mapungufu kuliko faida likazaliwa. Mambo haya yamemkatisha tamaa kwa kiwango kikubwa Kaka E na yamekuwa yakitikisa imani aliokuwa nao kwa nduguze. Matokeo yake akahusishwa na madeni ambayo asingeweza kuyalipa. Alipotambua hisia za kibinafsi zilizokuwa zikioneshwa na baadhi ya nduguze kumwelekea yeye, hilo likamhuzunisha sana na wakati mwingine lilimkasirisha mno. Hisia zake kwa wakati fulani zimeshindwa kutawalika alipotambua hali yake aliyokuwa nayo ya kukosa msaada, pasipo kuwa na uwezo wa kuona, pasipokuwa na mali, pasipokuwa na afya njema, na huku baadhi ya nduguze wakifanya kazi kinyume naye. Hili limechangia sana kuongezeka kwa taabu yake na kuchangia katika kuzorota kwa afya yake. 3T 515.1

Nilioneshwa kuwa Kaka E anazo sifa njema za kiakili ambazo zingelitambulika na kuthaminiwa vizuri zaidi kama angelikuwa na uwezo wa kujidhibiti na kutokuwa na mihemko. Kila onesho la kukosa subira na ukali linamharibia sifa, na linafanywa kuwa kubwa na baadhi ambao wana hatia ya dhambi mbaya zaidi mbele za Mungu, kanuni za Kaka E ni njema. Ni muadilifu. Si mtu asiye mwaminifu. Asingelimtapeli yeyote yule kwa kujua. Lakini anayo makosa na dhambi ambazo ni lazima azishinde. Yeye pia, kama ilivyo kwa wengine, anapaswa kushughulika na asili ya kibinadamu. Mara zote si mvumilivu na wakati mwingine ni mdhalimu. Anapaswa kuwa na roho ya utu na heshima na anapaswa kukuza moyo wa shukrani kwa wale ambao wameonesha shauku/nia katika suala lake. Kwa asili ana harara anapoamshwa kwa ghafla au kuchokozwa bila sababu. Lakini, ukiachilia mbali hili, anayo shauku ya kutenda mema, anahisi toba ya dhati kwa Mungu wakati anapoangalia makosa yake. 3T 515.2

Kama anaona nduguze wanamtendea iliyo haki atakuwa tayari kusamehe na kwa unyenyekevu kuitaka amani, hata kama anapaswa kujitoa mhanga maradufu ili aipate. Lakini anasisimka kwa urahisi mno; ana silika ya wahaka. Analo hitaji la nguvu ya utiisho ya Roho wa Mungu. Kama wale ambao wapo tayari kumshutumu na kumkosoa wangeliangalia makosa yao wenyewe na kwa wema kupuuza makosa yake kwa ukarimu kwa kadiri wanavyopaswa, wangelidhihirisha roho ya Kristo. Kaka E anayo kazi ya kufanya ili kushinda. Maneno yake na mwenendo wake kwa wengine vinapaswa kuwa vya kiungwana, laini, vya wema, upole, na uzuri. Anapaswa kujikinga dhidi ya kila kitu chenye harufu ya roho ya udikteta au chenye tabia au maneno ya majivuno, na kuwakanyaga wengine. 3T 515.3

Ingawa Mungu ni rafiki wa vipofu na wanaoteseka, Yeye hatolei udhuru au kupuuza dhambi zao. Anawataka washinde na kukamilisha tabia ya Kikristo katika Jina la Yesu, ambaye alishinda kwa niaba yao. Lakini Yesu anasikitikia madhaifu yetu, na Yupo tayari kutupatia nguvu ya kustahimili majaribu na kupingana na majaribu ya

Shetani, kama tu tutapeleka mizigo yetu Kwake. Malaika wanatumwa kuwahudumia watoto wa Mungu walio vipofu kimwili. Malaika wanalinda hatua zao na kuwaokoa kutoka katika hatari elfu, ambazo, pasipo wao kujua, zinawazingira njiani mwao. Lakini Roho Yake haitakuwa pamoja nao kama hawatathamini roho ya wema na kutafuta kwa bidii kudhibiti asili zao na kusalimisha shauku zao na kila nguvu kwa Mungu. Wanapaswa kukuza roho ya upendo na kutawala maneno na matendo yao. 3T 516.1

Nilioneshwa kuwa Mungu anawataka watu Wake kuwa wenye huruma zaidi na wenye moyo wa kujali kwa wale wanaoteseka kuliko walivyo sasa. “Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” Hapa dini iliyo safi imefafanuliwa. Mungu anataka kwamba kujali kulekule ambako kunapaswa kuoneshwa kwa wajane na wasio na baba kuoneshwe pia kwa vipofu na wale wanaoteseka kwa madhaifu mbalimbali ya kimaumbile. Ukarimu huu usio na ubinafsi, au kujifikiria mwenyewe umeadimika sana katika ulimwengu wa zama hizi. 3T 516.2

Nilioneshwa, katika suala la Kaka E, kwamba wale ambao wangelishughulika naye isivyo haki na kumkatisha tamaa katika jitihada zake za kujisaidia yeye mwenyewe, au ambao, wanatamani utajiri wa masikini kipofu, na kujinufaisha kupitia udhaifu wake alio nao, wangelijiletea wao wenyewe laana ya Mungu, ambaye ni rafiki wa mtu kipofu. Maagizo maalumu yalitolewa kwa wana wa Israeli kuhusiana na vipofu: “Usimdhulumu jirani yako, wala kumnyang’anya mali yake; ijara yake aliyeajiriwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi. Usimlaani kiziwi, wala usitie kwazo mbele ya kipofu, bali umche Mungu wako; Mimi Ndimi BWANA. Msitende yasiyo haki katika hukumu, usimpendelee mtu maskini, wala kumstahi mwenye nguvu; bali utamhukumu jirani yako kwa haki.” “Na alaaniwe aondoaye mpaka wa jirani yake. Na watu wote waseme, Amina. Na alaaniwe ampotezaye kipofu akakosa njia. Na watu wote waseme, Amina. Na alaaniwe apotoaye hukumu ya mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe. Na watu wote waseme, Amina.” 3T 516.3

Ni ajabu kuwa wanadamu wanaojiita Wakristo wanapuuza mafundisho yaliyo wazi, yenye uhakika na chanya ya Neno la Mungu na hawana majuto ya dhamiri. Mungu ameweka kwao wajibu wa kuwatunza wanaoteseka, waliopata maafa, vipofu, viwete, wajane, na wasio na baba; lakini wengi hawafanyi jitihada kuzingatia hilo. Ili kuokoa hilo, Mungu mara kwa mara anawatia katika fimbo ya mateso na kuwaweka mahali pafananapo na pale pa wale ambao walikuwa na uhitaji wa msaada na huruma yao, lakini wakaukosa kutoka kwao. 3T 517.1

Mungu ataliwajibisha kanisa, kama mwili, kwa mambo maovu ya waumini wake. Kama roho ya ubinafsi na kutokuwa na huruma kwa wanaoteseka, wajane, yatima, vipofu, viwete, au wale wanaoumwa kimwili na kiakili ikiachwa ikawepo katika

mmojawapo wa waumini wake, Yeye [Mungu] ataficha uso wake kutoka kwa watu Wake mpaka watakapofanya wajibu wao na kuondoa kosa au uovu uliopo miongoni mwao. Kama wowote wale waitwao kwa Jina la Kristo wanamwakilisha vibaya mwokozi wao kwa kutojali wajibu walionao kwa wanaoteseka, au kama kwa namna yoyote wanatafuta kujinufaisha wao wenyewe kupitia maumivu ya wanadamu wanaoteseka na hivyo kuwanyang'anya mali zao, Bwana ataliwajibisha kanisa kwa dhambi ya waumini wake mpaka wawe wamefanya yote wanavyoweza kutibu uovu uliopo. Yeye Hatasikiliza sala ya watu Wake na ili hali yatima, wasio na baba, viwete, vipofu, na wagonjwa wanapuuzwa miongoni mwao. 3T 517.2

Kuna maana zaidi kwa "kuwa upande wa Bwana" kuliko tu kusema hivyo katika mkutano. Upande wa Bwana daima ni upande wa fadhili, huruma, na kuwajali watesekao, kama itakavyoonekana kwa kielelezo tulichopewa katika maisha ya Yesu. Tunatakiwa kuiga kielelezo chake. Bali kuna baadhi ambao hawapo upande wa Bwana katika mambo haya; hawa wapo upande wa adui. Ili kuwapa wasikilizaji Wake kielelezo kuhusu somo hili, Yesu alisema: 3T 518.1

"Kwa kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Kisha atawaambia na wale walioko mkono Wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona Wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea Mimi. Na hao wataenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki wataenda katika uzima wa milele." 3T 518.2

Hapa katika hubiri Lake Kristo anajitambulisha Yeye Mwenyewe kama mwanadamu anayeteseka na anatuonesha wazi sisi sote kwamba kutokujali au matendo yasiyo haki wanayotendewa watakatifu Wake walio wadogo anatendewa Yeye. Huu ndio upande wa Bwana, na yeyote atakayekuwa upande wa Bwana, na aje pamoja nasi. Mwokozi mpendwa anaumizwa pale tunapomuumiza mmoja wa watakatifu Wake wanyeyekevu. 3T 518.3

Ayubu mwenye haki analia kwa sababu ya mateso yake na kusihi kuhusu hali yake pale alipotiwa hatiani na mmoja wa wafariji wake. Anasema: "Nalikuwa macho kwa kipofu, Nalikuwa miguu kwa aliyechechemea. Nalikuwa baba kwa mhitaji, na daawa ya mtu nisiyemjua naliichunguza. Nami nilizivunja taya za wasio haki, na kumpokonya mawindo katika meno yake." 3T 518.4

Dhambi ya mtu mmoja ililisumbua jeshi lote la Israeli. Kusudio ovu lifanywalo na mtu mmoja dhidi ya nduguye litaondoa nuru ya Mungu kutoka kwa watu Wake mpaka uovu huo utakapochunguzwa na kugundulika na dawa ya anayedhulumiwa kuthibitika. Mungu anataka watu wake wawe wema wenye huruma nyororo, kujali na mwanana, katika hisia na upambanuzi, wakati mioyo yao inapaswa kutanuka, hisia zao zinapaswa kuwa pana na zenye kina kirefu, sio finyu, zenye ubinafsi, ubahili na masikini. Huruma iliyotukuka, ukubwa wa nafsi, na ukarimu usio wa kimaslahi vinahitajika. Ndipo kanisa linaweza kushinda katika Mungu. Lakini kama vile kwa kadiri kanisa linavyosumbuliwa na ubinafsi ukaushao huruma njema na wema, kujali, ulaini wa moyo, upendo mwanana wa kina na maslahi kwa ajili ya ndugu zao, kila sifa itaharibiwa kwa kuliwa na kutu. Saumu ya Isaya inapaswa kujifunzwa na uchunguzi binafsi wa kina kufanywa katika roho ili kutambua iwapo ndani yao kuna kanuni ambazo watu wa Mungu wanapaswa kuwa nazo ili waweze kupokea mibaraka ya utajiri iliyoahidiwa. 3T 519.1

Mungu anataka kwamba watu Wake wasiruhusu masikini na wanaoteseka kudhulumiwa. Kama wanavunja kila nira na kuwafungulia wanaonyanyaswa, na kutokuwa wabinafsi na kuonesha kuwajali wahitaji, ndipo mibaraka iliyoahidiwa itakapokuwa ya kwao. Kama wapo katika kanisa wale ambao wangelisababisha vipofu kujikwaa, wanapaswa kuhukumiwa kwa haki, kuleta mahakamani; kwa kuwa Mungu ametufanya sisi kuwa walezi wa vipofu, wanaoteseka, wajane, na wasio na baba. Jiwe la kujikwaa linalotajwa katika Neno la Mungu halimaanishi kisiki kinachowekwa mbele ya miguu ya kipofu ili kumsababisha apate kujikwaa, bali lina maana kubwa zaidi ya hiyo. Linamaanisha jambo lolole linaloweza kufanywa na kuumiza mvuto wa ndugu yao aliye kipofu, kutenda kinyume na maslahi yake, au kukwamisha ustawi wake. 3T 519.2

Ndugu aliye kipofu na masikini na mgonjwa, na anayefanya kila jitihada kujisaidia mwenyewe asije kuwa tegemezi, anapaswa kutiwa moyo na nduguze kwa kila namna iwezekanavyo. Lakini wale ambao wanajidai kuwa ndugu zake, ambao wana viungo vyote vya mwili, ambao si tegemezi, bali wanasahau wajibu wao kwa kipofu huku wakimfedhehesha na kumsononesha na kumzuia katika njia, wanafanya shughuli ambayo itahitaji toba na urejeshwaji kabla Mungu hajaafiki sala zao. Na kanisa la Mungu ambalo limeruhusu ndugu yao anayeteseka kutendewa kimakosa, litakuwa katika hatia ya dhambi mpaka watakapofanya yote katika uwezo wao kurekebisha kosa lao. 3T 519.3

Wote bila shaka wanafahamu suala la Akani. Kisa hiki kimmerekodiwa katika historia takatifu kwa ajili ya vizazi vyote, lakini mahususi zaidi kwa wale ambao kwao miisho ya ulimwengu imewajia. Yoshua akaanguka kifudifudi mbele za Mungu kwa sababu watu walirudi nyuma kwa fedheha mbele ya maadui zao. Bwana akamwambia Yoshua Inuka. “Haya! Inuka, mbona umeanguka kifudifudi hivi?” Je

hakuna sababu yoyote iliyonifanya nijishushe kwa kuondoa uwepo Wangu kwako? Je, Mungu aweza kuwaacha watu Wake bila sababu? Hapana; Anamwambia Yoshua kuwa kuna jambo analopaswa kufanya kabla ombi lake halijajibiwa. “Israeli wamefanya dhambi, naam, wamelivunja agano Langu nililowaagiza; naam, wametwaa baadhi ya vitu vilivyowekwa wakfu; tena wameiba, tena wameficha na kuvitia pamoja na vitu vyao wenyewe.” Bwana Anatangaza: “Mimi sitakuwa pamoja nanyi tena, msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu.” 3T 520.1

Hapa katika kielelezo hiki tunapata wazo la wajibu uliopo kwa kanisa na kazi ambayo Mungu anawataka waifanye ili wawe na uwepo Wake. Ni dhambi iliyopo katika kanisa lolote kutokutafuta sababu ya giza walilonalo na mateso ambayo yapo miongoni mwao. Kanisa------ haliwezi kuwa hai, na lenye kustawi mpaka mpaka watakapoamka na kuyaona makosa yaliyopo miongoni mwao, ambayo yanazuia mbaraka wa Mungu usiwajilie. Kanisa halipaswi kuwatia ndugu zao katika mateso ili liwe hatiani. Hawa ni wale ambao wanapaswa kuamsha huruma ya mioyo ya wote na kuamsha roho ya kutendea kazi hisia za bora za unyofu na ukarimu kwa wafuasi wote wa Kristo. Wanafunzi wa Kweli wa Kristo watatenda kazi katika muafaka na Yeye na, kwa kufuata kielelezo Chake watawasaidia wale wanaohitaji msaada. Upofu wa Kaka E ni mateso ya kutisha, na wote wanapaswa kutafuta macho kwa kipofu na hivyo kumfanya aone upungufu alionao kuwa ni mdogo kwa kadiri iwezekanavyo. Kuna baadhi ambao wanaimarisha macho yao ili wapate kuona fursa za kufanyia kazi kwa ajili ya kujinufaisha wao wenyewe, lakini Mungu anaweza kuwapatia mkanganyiko kwa namna wasiyotarajia. 3T 520.2

Kama Mungu kwa rehema Zake amempatia kipofu uwezo wa uvumbuzi ambao aweza kuutumia kwa manufaa yake mwenyewe, Mungu apishe mbali kwamba yeyote asije akawa na kisasi/kinyongo juu yake dhidi ya fursa aliyonayo na kumnyang’anya faida ambazo anaweza kuzipata kutokana na zawadi ya Mungu kwake. Mtu kipofu ana matatizo ya kushindwa kufikia kila upande kutokana na kukosa kwake uwezo wa kuona. Moyo huo ambao hauna sikitiko au huruma na usiojali unapomwona kipofu akipapasa-papasa njiani katika ulimwengu na kumweka gizani, ni mgumu mno na unapaswa kulainishwa kwa neema ya Mungu. Hakuna hata uso mmoja ambao kipofu aweza kuutazama na kusoma huruma njema na ukarimu wa kweli. Hawezi kutazama uzuri wa asili na kuuona mkono wa Mungu katika viumbe vyake. Uzuri wao uliochangamka hauzungumzi naye na kumpatia faraja na kumbariki wakati hali ya kukata tamaa inapomjia. Ni kwa haraka kiasi gani angelibadilisha upofu wake na baraka za kitambo kwa mbaraka wa uwezo wa kuona. Bali amefungiwa katika ulimwengu wa giza, na haki zake alizopewa na Mungu zimekanyagwa ili wengine wapate kunufaika. 3T 521.1

SURA YA 47

WAJIBU WA MWANADAMU KWA WENZAKE

Nimeoneshwa vitu kadhaa kuhusu familia ya ndugu I ambavyo vimenisukuma akilini mwangu kwa nguvu tangu nilipokuwa mahali hapa na ninajitosa kuviandika. Nimeoneshwa, Ndugu I, kwamba kuna kipengele cha ubinafsi katika familia yako ambacho kinakushikilia kama ukoma. Ubinafsi huu lazima uonekane na ushindwe, kwani ni dhambi mbaya mbele za Mungu. Kama familia kwa muda mrefu mmefanya matakwa yenu wenyewe, raha, faraja na anasa zenu, hata hamhisi kuwa wengine wana madai juu yenu. Mawazo yenu, mipango yenu, na juhudi zenu ni kwa ajili yenu wenyewe. Mnaishi kwa ajili ya ubinafsi; hamkuzi ukarimu usiojifikiria wenyewe, usio na ubinafsi, ambao, ikiwa ungetumiwa, ungeongezeka na kuimarika hadi iwe raha yenu kuishi kwa ajili ya faida na wema kwa wengine. Mngehisi kuwa mna kitu maishani, kusudi ambalo lingewaletea faida kubwa kuliko pesa. Mnahitajika kuwa na shauku maalum zaidi kwa ubinadamu, na kwa kufanya hivyo mngezileta roho zenu katika uhusiano wa karibu na Kristo na mngejazwa sana na Roho Wake na kushikamana Naye kwa uthabiti mkali sana kiasi kwamba hakuna kitu kinachoweza kuwatenganisha na upendo Wake. {3T 521.2}

Kristo Ndiye Mzabibu ulio hai na kama ninyi ni matawi ya Mzabibu huo, lishe ya maisha inayotiririka ndani Yake itawalisha, ili msiwe tasa au msiozaa matunda. Kama familia na kama watu binafsi, mnajidai kuwa mmejiunganisha na huduma ya Kristo; lakini mmepimwa katika mizani ya Patakatifu na kuonekana kuwa mmepungua. Ninyi nyote mnahitaji kuwa na mabadiliko kamili kabla ya kufanya mambo ambayo Wakristo wasio na ubinafsi na kujitolea wanapaswa kuyafanya. Hakuna chochote isipokuwa uongofu kamili kinachoweza kuwapa hisia sahihi ya kasoro zenu za tabia. Ninyi nyote mna roho na upendo wa ulimwengu kwa kiwango kikubwa. Anasema mtume Yohana: "Mtu yeyote aupendaye ulimwengu, upendo wa Baba haumo ndani yake." Roho zenu za ubinafsi hupunguza na kudumaza mawazo yenu kwa maslahi yenu wenyewe. Mnahitaji dini safi na isiyo na unajisi. Unyenyekevu wa Ukweli, na usahili utawafanya mjisikie huruma kwenye shida za wengine. Kuna wale ambao wanahitaji huruma yenu na upendo. Kufanyia mazoezi

sifa hizi za tabia ni sehemu ya kazi ya maisha ambayo Kristo ametupatia sisi sote kufanya. {3T 522.1}

Mungu hatawasamehe kwa kutobeba msalaba na kujinyima wenyewe kwa ajili ya kuwatendea wengine mema kwa nia isiyo ya ubinafsi. Ikiwa mtajitahidi kujikana nafsi, kwa namna ile inayohitajika kwa Wakristo, mnaweza, kwa neema ya Mungu, kustahili kuleta roho kwa Kristo. Mungu ana madai juu yenu ambayo hamjawahi kuyaitikia. Kuna watu wengi wanaotuzunguka ambao wana njaa ya huruma na upendo. Lakini, kama wengine wengi, mmekaribia kukosa upendo huo wa unyenyekevu ambao kawaida hutiririka kwa huruma na upendo kwa maskini, wanaoteseka, na wahitaji. Sura ya mwanadamu yenyewe ni kioo cha roho, kinachosomwa na wengine, na kuwa na ushawishi mzuri juu yao kwa mema au kwa mabaya. Mungu hamuhitaji yeyote kati yetu kuwatazama ndugu zetu na kutubu dhambi zao. Yeye Ametuachia sisi kazi ya kufanya, na anatuita kuifanya kwa uthabiti, kwa hofu Yake, tukiwa na jicho letu limekodoa/limekita kwajili ya utukufu Wake. {3T 522.2}

Kila mtu, awe ni mwaminifu au vinginevyo, lazima ampe Mungu hesabu yake mwenyewe, siyo ya wengine. Kuona makosa kwa wengine na kulaani kazi yao haitatoa udhuru au kumaliza kosa letu hata moja. Hatupaswi kuwafanya wengine kuwa kigezo chetu wala kutoa udhuru wowote katika kazi yetu kwa sababu wengine wamekosea. Mungu ametupatia dhamiri kwa ajili yetu wenyewe. Kanuni kubwa zimewekwa katika Neno Lake, ambazo zinatosha kutuongoza katika hatua zetu za Kikristo na tabia kwa ujumla. Ninyi, rafiki zangu wapendwa, kama familia, hamjashika kanuni za sheria ya Mungu. Hamjawahi kuhisi mzigo wa jukumu linalomzunguka mwanadamu kwa wanadamu wenzake. {3T 523.1}

"Na tazama, wakili mmoja akasimama akamjaribu, akisema, Mwalimu, nifanye nini ili nipate kuurithi uzima wa milele? Akamwuliza, Je, Imeandikwaje katika torati? Unasomaje? Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili yako yote, na jirani yako kama nafsi yako. "Akamwambia, Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi. "Lakini yeye, akitaka kujihesabia haki, akamwuliza Yesu," Na jirani yangu ni nani? "Yesu akajibu akasema, {3T 523.2}

"Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando. Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi

nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi? Akasema, Ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia, Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo. "{3T 523.3}

Hapa masharti ya kuurithi uzima wa milele yameelezewa wazi na Mwokozi wetu kwa njia rahisi kabisa. Mtu aliyejeruhiwa na kuibiwa anawakilisha wale walio chini ya maslahi yetu, shauku, huruma, na upendo. Ikiwa tutapuuza kesi za wahitaji na wale wanaopata maafa yanayoonekana kwetu, bila kujali ni akina nani, hatuna uhakika wa uzima wa milele; kwani hatujibu madai ambayo Mungu anayo juu yetu. Hatuna huruma na upendo kwa wanadamu, kwa sababu wanaweza kuwa siyo jamaa au ndugu zetu. Mmepatikana kuwa wakosaji wa amri kuu ya pili, ambayo inategemewa na amri sita za mwisho. Yeyote anayekosea katika nukta moja, ana hatia katika yote. Wale ambao hawatafungua mioyo yao kwa ajili ya mahitaji na mateso ya wanadamu hawatafungua mioyo yao kwa madai ya Mungu kama ilivyoelezwa katika maagizo manne ya kwanza ya Dekalojia- Amri kumi. Sanamu hudai moyo na mapenzi, na Mungu haheshimiwi na wala hana utawala kabisa. {3T 524.1}

Kama familia, mmeshindwa kwa kiasi cha kusikitisha. Ninyi kwa namna yenye mashiko kabisa, siyo watunza sheria kabisaa. Mnaweza kuwa sahihi kabisa katika mambo mengine, lakini mnasahau mambo mazito zaidi - hukumu, rehema, na upendo wa Mungu. Ingawa desturi za ulimwengu siyo kigezo kwetu, lakini nimeoneshwa kuwa huruma na ukarimu wa ulimwengu kwa wale wanyonge katika visa vingi huwaaibisha wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Wengi huonesha kutowajali wale ambao Mungu ametupatia kati yao kwa kusudi la kuwajaribu na kuwathibitisha, na kukuza yaliyomo katika mioyo yao. Mungu anasoma. Anaona kila tendo la ubinafsi, kila tendo la kutowajali walio taabika, wajane, na yatima; na anaandika mbele ya majina yao: "Wenye hatia, wamepungukiwa, wavunja sheria." Tutapewa tuzo kama kazi zetu zilivyo. Utelekezaji wowote wa wajibu kwa wahitaji na kwa walio na shida ni upuuziaji wa wajibu kwa Kristo katika nafsi ya watakatifu Wake. {3T 524.2}

Wakati kesi za wote zinapoletwa mbele za Mungu kwa mapitio, swali ni hili, Je! Walikiri nini? hawataulizwa, bali, Je! wamefanya nini? Je! Wamekuwa watendaji wa neno? Je! Wameishi kwa ajili yao wenyewe, au wametumiwa katika kazi za wema, kwa matendo ya fadhili na upendo, wakiwapendelea wengine kabla yao, na kujikana kiasi kwamba wanaweza kuwabariki wengine? Ikiwa rekodi inaonesha kuwa haya yamekuwa maisha yao, kwamba tabia yao imewekewa alama ya upole, kujinyima, na ukarimu, watapokea uhakikisho wenye baraka na baraka kutoka kwa Kristo: "Vema" "Njooni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa ulimwengu." Kristo amehuzunishwa na kujeruhiwa na upendo wako wa ubinafsi uliotiwa alama na kutokujali kwako kwa maafa/ole na mahitaji ya wengine. {3T 525.1}

Mara nyingi juhudi zetu kwa wengine zinaweza kupuuzwa na kupotea. Lakini hiki hakipaswi kuwa kisingizio kwetu kuchoka katika kutenda mema. Ni mara ngapi Yesu amekuja kuangalia matunda kwenye mimea ya uangalizi Wake na hakupata tunda lolote isipokuwa majani! Tunaweza kuvunjika moyo kama matokeo ya juhudi zetu bora, lakini hili halipaswi kutufanya kuwa watu wasiojali shida za wengine na tusiofanya chochote. "Ulaaniwe Merozi, alisema malaika wa Bwana, Walaanini kwa uchungu wenyeji wake; Kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, Kumsaidia Bwana juu ya hao wenye nguvu." Waamuzi 5. Ni mara ngapi Kristo hukatishwa tamaa na wale wanaodai kuwa watoto Wake! Yeye Amewapatia ushuhuda wa upendo Wake. Akawa maskini, ili kupitia umaskini wake tuwe matajiri. Yeye Alikufa kwa ajili yetu, ili tusiangamie, bali tuwe na uzima wa milele. Vipi kama Kristo angekataa kubeba uovu wetu kwa sababu alikataliwa na wengi na kwa sababu ni wachache waliothamini upendo Wake na baraka nyingi ambazo alikuja kuwaletea? Tunahitaji kuhamasisha juhudi yenye kuhenyesha na uvumilivu usiochoka. Ujasiri ni sasa ndiyo unahitajika, siyo kukata tamaa kwa uvivu, kuudhika na manung'uniko mabaya. Tuko katika ulimwengu huu kufanya kazi kwa ajili ya Bwana na siyo kusoma mwelekeo wetu na raha, zetu kujitumikia na kujitukuza sisi wenyewe. Kwa nini, basi, tuwe watu wasio na utendaji hai, wenye kuvunjika moyo kwa sababu hatuoni matokeo ya haraka tunayoyatamani? {3T 525.2}

Kazi yetu ni kujitaabisha katika shamba la Bwana, siyo tu kwa ajili yetu wenyewe, bali kwa faida ya wengine. Ushawishi wetu ni baraka au laana kwa wengine. Tuko hapa kuunda tabia kamilifu za mbinguni. Tunalo la kufanya zaidi ya kulalamika na kunung'unika kwa mahitaji ya Mungu, na kuandika mambo machungu dhidi yetu wenyewe. Mpinzani wetu hataturuhusu kupumzika. Ikiwa kweli sisi ni watoto wa Mungu tutasumbuliwa na kuteswa sana, na hatuhitaji kutarajia kwamba Shetani au wale walio chini ya ushawishi wake watatutendea mema/vizuri. Lakini kuna malaika ambao wana nguvu zaidi ambao watakuwa pamoja nasi katika mizozo yetu yote ikiwa tu tutakuwa waaminifu. Kristo alimshinda Shetani kwa niaba yetu katika jangwa la majaribu. Yeye ni mwenye nguvu kuliko Shetani, na hivi karibuni atamponda chini ya miguu yetu. {3T 526.1}

Ninyi, kama familia na kama watu binafsi, mmejitolea udhuru kwa huduma ya dhati na ya juhudi katika kusudi la Bwana wenu. Mmekuwa wavivu sana na mmewaacha wengine kubeba mizigo mingi mizito ambayo mngeiweza na mngeibeba. Nguvu zako za kiroho na baraka zitakuwa sawia na kazi ya upendo na matendo mema mnayoyafanya. Amri ya mtume Paulo ni hii: "Chukulianeni mizigo, na kwa hivyo muitimize sheria ya Kristo." Kuzishika amri za Mungu kunahitaji matendo mema kutoka kwetu, kujikana nafsi, kujitolea, na kujitoa kwa faida ya wengine, siyo kwamba kazi zetu nzuri pekee zinaweza kutuokoa, lakini hakika hatuwezi kuokolewa bila matendo mema. Baada ya kufanya yote ambayo tunaweza kufanya, basi tutasema: Hatujafanya zaidi ya wajibu wetu, sisi ni

watumwa tusio na faida, tusiostahili upendeleo hata mdogo kutoka kwa Mungu. Kristo lazima awe haki yetu na taji ya furaha yetu. {3T 526.2}

Kujiona kuwa mwadilifu na usalama wa matendo ya mwili umewafunga kama ukuta. Kama familia mna roho ya kujitegemea na kiburi. Kipengele hiki kinawatenga na Mungu. Ni kosa, kasoro ambayo inapaswa kuonekana na kushinda. Haiwezekani kwenu kuona makosa na mapungufu yenu. Mna maoni mazuri sana juu yenu wenyewe, na ni vigumu kwenu kuona na kuondoa kwa kukiri makosa katika maisha yenu. Mna mwelekeo wa kuhalalisha na kutetea hatua zenu karibu katika kila kitu, iwe ni sawa au si sawa. Kungali hamjachelewa kwa ajili ya kurekebisha makosa, ileteni mioyo yenu karibu na Yesu kwa kujidhili na maombi, na mtafute kujitambua. Lazima mpojipoteze wenyewe ikiwa hamtaamka na kufanya kazi pamoja na Kristo. Mnajifunga kwa silaha duni, isiyo na hisia, isiyo na huruma. Kuna maisha na joto kidogo katika ushirika wenu na wengine. Mnaishi kwa ajili yenu wenyewe, siyo kwaajili ya Kristo. Ninyi ni wazembe msiojali mahitaji na hali za wengine wasio na bahati kama ninyi. Kote karibu na wewe wapo wale ambao wana njaa ya roho na ambao wanatamani upendo uliooneshwa kwa maneno na matendo. Huruma ya kirafiki na hisia za Kweli za kupendeza kwa wengine zingeziletea roho zenu baraka ambazo hamjawahi kupata na zitawaleta katika uhusiano wa karibu na Mkombozi wetu, ambaye kuja Kwake ulimwenguni kulikuwa kwa kusudi la kutenda mema na sisi ni wajibu wetu kuunakili huo mfano. Mnamfanyia nini Kristo?"Jitahidini kuingia kwa kupitia mlango mwembamba; kwa maana nawaambia, wengi watatafuta kuingia, lakini wasiweze." {3T 526.3}

Upendo na Huruma Nyumbani

Kuna wengi katika ulimwengu wetu ambao wanakufa kwa njaa ya upendo na huruma ambayo wangepaswa kupewa. Wanaume wengi wanawapenda wake zao, lakini ni wabinafsi sana kuudhirisha upendo huo. Wana hadhi ya uwongo na kiburi, na hawataonesha upendo wao kwa maneno na matendo. Kuna wanaume wengi ambao hawajui jinsi moyo wa mke ulivyo na njaa ya maneno ya shukrani mwanana/nyororo, kujali, na mahaba/mapenzi. Wanawazika wapendwa wao kutoka katika macho yao na kuunung’unikia uweza wa Mungu ambao umewaondoa wenzi wao, wakati, kama wangeweza kuangalia ndani ya maisha ya wenzi hao, wangeona kuwa mwenendo wao wenyewe ndio uliosababisha kifo chao cha mapema. Dini ya Kristo itatuongoza kuwa wema na wenye adabu na siyo wenye kushikilia maoni yetu. Tunapaswa kuifia nafsi na ubinafsi, na kuwahesabu wengine kuwa bora kuliko sisi. {3T 527.1}

Neno la Mungu ndicho kipimo/kiwango chetu, lakini watu Wake wanaodai kuliamini wameliacha mbali kwa kiwango kikubwa sana! Imani yetu ya kidini lazima iwe isiyo ya nadharia tu, bali ya vitendo. Dini safi na isiyo na uchafu haitaturuhusu kukanyaga haki za hata wale viumbe wadogo sana wa Mungu, achilia mbali haki ya washiriki wa mwili Wake na washiriki wa familia zetu wenyewe.

Mungu ni upendo, na kila mtu akaaye ndani Yake anakaa katika upendo. Ushawishi wa ubinafsi wa ulimwengu, ambao umebebwa na wengine kama wingu, linaloleta ubaridi katika angahewa ambayo wengine hupumua, na kusababisha ugonjwa wa roho na mara nyingi husababisha baridi kali inayoleta kifo. {3T 528.1}

Itakuwa ni msalaba mzito kwako kukuza upendo safi, usio na ubinafsi au kutafuta faida binafsi na ukarimu usiojifikiria wenyewe. Kusalimisha maoni na mawazo yako, kuachana na maamuzi yako, na kufuata ushauri wa wengine utakuwa msalaba mkubwa kwako. Washiriki kadhaa wa familia yako sasa wana familia zao. Lakini roho ile ile ambayo ilikuwepo kwa kiwango kikubwa au kidogo katika nyumba ya baba yao inachukuliwa kwa mazungumzo na makazi yao pale wanapoota moto wao wenyewe (mazungumzo ya familia) na kuhisiwa na wale walio nje ya duru za familia zao. Hawana unyenyekevu mwema, upole, kujali, huruma nyororo na upendo mwanana kama wa Kristo, na upendo usio na ubinafsi na usiojifikiria. Wana kazi ya kufanya kushinda sifa hizi za ubinafsi wa tabia ili kuwa matawi yenye matunda ya Mzabibu wa Kweli. Kristo alisema: "Hivyo, Baba Yangu ametukuzwa, ninyi mkizaa matunda mengi." Unahitaji kumleta Yesu karibu nawe, ili uwe naye nyumbani mwako na moyoni mwako. Hupaswi tu kuwa na maarifa ya kipi kilicho sawa, bali unapaswa kuyatenda kutoka katika nia nzuri, ukiwa na jicho lako limekita kwenye utukufu wa Mungu. Unaweza kuwa msaada, ikiwa utazingatia masharti yaliyotolewa katika Neno la Mungu. {3T 528.2}

Dini ya Kristo ni zaidi ya kuongea au mazungumzo tu. Haki ya Kristo inajumuisha matendo sahihi na matendo mema kutoka katika nia safi, isiyo na ubinafsi. Uadilifu wa nje, wakati mapambo ya ndani ni duni, hayatakuwa na faida yoyote. Na hii ndiyo habari tuliyoisikia Kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lolote hamna ndani Yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana Naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo Kweli; bali tukienenda nuruni, kama Yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu Yake Yesu, Mwana Wake, yatusafisha dhambi yote. "Ikiwa hatuna nuru na upendo wa Mungu sisi siyo watoto Wake. Ikiwa hatukusanyi pamoja na Kristo tunatawanya ng'ambo. Sisi sote tuna ushawishi, na ushawishi huo unaelezea juu ya hatima ya wengine kwa faida yao ya sasa na ya baadaye au kwa hasara yao ya milele. {3T 528.3}

J na K wote wanapungukiwa na huruma na upendo kwa wale walio nje ya familia zao. Wako katika hatari ya kuangalia kuona kasoro kwa wengine wakati ndani yao kuna maovu makubwa yasiyotambuliwa na wenyewe. Ikiwa roho hizi pendwa zitaingia mbinguni, basi sharti zifie nafsi zao na kupata uzoefu wa kutenda mema. Wana masomo ya kujifunza katika shule ya Kristo ili kukamilisha tabia za Kikristo na kuwa na umoja na Kristo. Kristo alisema kwa wanafunzi Wake: "Msipobadilika, na kuwa kama watoto wadogo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni." Aliwaelezea maana yake. Hakutaka wawe watoto katika ufahamu, bali katika

matamanio ya uovu. Watoto wadogo hawadhihirisha hisia za kujiinua na umwinyi. Wako rahisi na asili katika mwonekano wao. Kristo angewataka wafuasi Wake kukuza tabia isiyoathiriwa, ili kuzaa kwao kote kuwe kwa unyenyekevu kama Kristo. Yeye Amelifanya kuwa jukumu letu kuishi kwa faida ya wengine. Alikuja kutoka katika nyua za Kifalme za mbinguni kuja ulimwenguni kuonesha jinsi alivyokuwa na shauku kubwa kwa mwanadamu, na bei isiyo na kipimo iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu inaonesha kuwa mtu ana thamani kubwa sana kiasi cha Kristo kuweza kujitolea utajiri na heshima Yake katika nyua za Kifalme kumwinua mwanadamu, yaani mimi, kutoka kwa uharibifu wa dhambi. {3T 529.1}

Ikiwa Mfalme wa mbinguni angeweza kufanya mengi ili kuonesha upendo Wake kwa mwanadamu,Je, ni kitu gani ambacho wanadamu hawawezi kuwa tayari kukifanya ili kusaidiana kutoka katika shimo la giza na mateso! Kristo alisema, "Pendaneni kama vile Mimi nilivyowapenda ninyi;" siyo kwa upendo mkuu; kwa kuwa "hakuna aliye na upendo mkuu kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai Wake kwa ajili ya marafiki Zake. "Upendo wetu mara nyingi ni wa ubinafsi, kwani tunajifungia katika mipaka iliyowekwa. Tunapoingia katika umoja wa karibu na ushirika na Kristo, upendo wetu na huruma na kazi zetu za fadhila ukarimu zitashuka chini zaidi na kupanuka na kuimarishwa kwa mazoezi. Upendo na masilahi ya wafuasi wa Kristo lazima viwe vipana kama ulimwengu. Wale ambao wanaishi tu kwa ajili ya "mimi na yangu mwenyewe" watashindwa kufika mbinguni. Mungu anakuita kama familia kukuza upendo, kupunguza hali ya kuwa wepesi kuhusiana na mambo yenu wenyewe na kuhisi zaidi huzuni na majaribu ya wengine. Roho hii ya ubinafsina uchoyo ambayo mmeiendekeza katika maisha yenu yote inawakilishwa kwa usahihi na kuhani na mlawi aliyepita upande wa pili alipomwona mtu aliyepata majanga. Wakaona kwamba anahitaji msaada, lakini kwa makusudi walimuepuka. {3T 529.2}

Kila mmoja wenu anahitaji kuamka na kukabili kishujaa na uso kwa uso hali hii na kutoka nje ya toroli la ubinafsi. Boresha muda mfupi, wa majaribio uliopewa kwa kufanya kazi kwa nguvu zako kukomboa kushindwa kwa maisha yako ya zamani. Mungu amekuweka katika ulimwengu wa mateso ili kukuthibitisha, ili aone ikiwa utaonekana kustahili zawadi ya uzima wa milele. Kuna wale wanaokuzunguka ambao wana ole, uharibifu, na huzuni ambao wanahitaji maneno ya huruma, upendo, na upole, na maombi yetu ya unyenyekevu, ya masikitiko na huruma. Wengine wanateseka chini ya mkono wa chuma wa umaskini, wengine na magonjwa, na wengine na maumivu ya moyo, kukata tamaa, na huzuni. Kama Ayubu, unapaswa kuwa macho kwa vipofu na miguu kwa vilema, na unapaswa kuuliza juu ya sababu ambayo huijui na utafute majibu ukiwa na lengo la kupunguza uhitaji wao na kusaidia mahali ambapo wanahitaji msaada zaidi. {3T 530.1}

Ndugu L anahitaji kukuza upendo kwa mkewe, upendo ambao utadhihirishwa kwa maneno na matendo. Anapaswa kukuza upendo mwema. Mkewe ana asili ya hisia za karibu, za kushikamana na anahitaji kutunzwa. Kila neno la upole, kila neno la shukrani na kutiwa moyo kwa upendo, litakumbukwa na yeye na litaakisi baraka juu ya mumewe. Asili yake isiyo na huruma inahitaji kuletwa katika uhusiano wa karibu na Kristo, ili kwamba ugumu huo na upuuziaji na ubaridi huo wa kukosa moyo wa kirafiki, uweze kutiishwa na kulainishwa na upendo wa Mungu. Hautakuwa udhaifu au kafara ya uanaume na hadhi kumpa mkewe maonesho ya huruma nyororo, kujali na upendo mwanana kwa maneno na matendo; na hebu hiyo isiishie kwenye mduara wa familia, bali isambae kwa wale walio nje ya familia. Ndugu L ana kazi ya kufanya mwenyewe ambayo hakuna mtu anayeweza kuifanya kwa niaba yake. Anaweza kukua katika nguvu ndani ya Bwana kwa kubeba mizigo katika kusudi Lake. Upendo na mapenzi yake vinapaswa kuwa na kiini katika Kristo na vitu vya mbinguni, na anapaswa kuunda tabia ya uzima wa milele. {3T 530.2}

Mpendwa K ana maoni machache na yenye mipaka juu ya kile kinachomfanya mtu kuwa Mkristo. Amejiweka huru kutoka katika mizigo ambayo Kristo ameibeba kwa ajili yake. Yeye hayuko tayari kubeba msalaba na hajatumia vizuri uwezo na talanta alizopewa na Mungu. Hajawa na nguvu katika uvumilivu wa maadili na ujasiri, wala hakuhisi uzito wa jukumu la mtu binafsi. Hapendi kubeba lawama kwa ajili ya Kristo, kwa kuzingatia ahadi hii: "Ikiwa mnashutumiwa kwa ajili ya Jina la Kristo, heri yenu; kwa maana Roho wa utukufu na wa Mungu amekaa juu yenu." "Ikiwa tutavumilia, tutatawala pia pamoja Naye." Bwana ana kazi kwa ajili ya kila mmoja wetu KUFANYA. Hakuna anayeweza kuwa mvivu, hakuna anayeweza kuwa mzembe na mwenye ubinafsi, na bado akawa na tabia kamili ya Kikristo. Yeye Anataka familia yako yote ifungue mioyo yao kwa ushawishi mzuri wa upendo na neema Yake, ili huruma yao kwa wengine ifurike mipaka ya nafsi na maboma ya kuta za familia, kama ilivyokuwa kwa Msamaria juu ya yule maskini, mgeni anayeteseka ambaye alikuwa amepuuzwa na kuachwa na kuhani na Mlawi afe. Nilioneshwa kuwa kuna wengi ambao wanahitaji huruma na ushauri wetu; na tunapofikiria kuwa tunaweza kupita katika ulimwengu huu mara moja, kwamba hatuwezi kurudi kurekebisha makosa na mapungufu ambayo tumeyafanya, ni muhimu kiasi gani kwamba tunapaswa kuupitia ulimwengu kama tunavyostahili kufanya -[kutokana na maagizo ya Mungu]! {3T 531.1}

Wakati fulani uliopita nilioneshwa kesi ya dada J. Makosa na mapungufu yake yalianikwa wazi kwa uaminifu mbele yake; lakini kwa maono ya mwisho niliyopewa niliona kuwa makosa hayo bado yapo, kwamba alikuwa na moyo baridi na asiyeonyesha huruma kwa watoto wa mumewe. Mama huyu hutoa marekebisho na makaripio sio tu kwa makosa makubwa tu, bali hata kwa mambo madogo yasiyo na maana ambayo yanapaswa kupitishwa bila kutambuliwa. Kulaumu na kutafuta makosa mara kwa mara ni makosa, ni jambo baya, na Roho wa Kristo hawezi kukaa

katika moyo wa aina hii ambapo tabia hii ipo. Ana mwelekeo wa kuyapuuzia mema wanayofanya watoto wake na kuyaacha yapite tu bila neno la ukubali au pongezi (yanapita tu mawazoni bila yeye kuwatia moyo), lakini yuko tayari kuwakemea na kulaani vikali iwapo atagundua kuna makosa yoyote. Hii huwavunja moyo watoto na kusababisha wawe na tabia ya kutokuzingatia. Inachochea uovu ulio moyoni na kuufanya moyo huo kuktoa matope na uchafu. Watoto ambao wamekemewa na kulaumiwa kwa kawaida huwa na roho ya "Sijali," na mielekeo na tamaa mbaya zitaoneshwa mara nyingi bila kujali matokeo. {3T 531.2}

Wakati wowote ambao mama anaweza kupata nafasi ya kusema neno la kumsifu mtoto wake au kumpa pongezi kwa mwenendo mzuri, anapaswa kufanya hivyo. Anapaswa kuwatia moyo kwa maneno ya ukubali na mwonekano wa sura iliyojaa upendo. Maneno haya yatakuwa kama jua kwenye moyo wa mtoto na yatasababisha kukuza heshima binafsi, kujistahi, uungwana na fahari ya kuwa na tabia njema. Dada J anapaswa kukuza upendo na huruma. Anapaswa kuonesha upendo mwanana na kujali kwa watoto wasio na mama walio chini ya uangalizi wake. Hili litakuwa baraka kwa watoto hawa wa upendo wa Mungu na litaonekana tena juu yake katika mapenzi na upendo. {3T 532.1}

Watoto wana asili ya hisia za haraka na nyeti, za upendo. Wanafurahishwa kwa urahisi na kufanywa kuwa wasio na furaha kwa urahisi pia. Kwa nidhamu laini na upole kwa maneno na matendo ya upendo, akina mama wanaweza kuwafunga watoto wao katika mioyo yao. Kudhihirisha ukali na kuwa wakorofi au wakali kwa watoto ni makosa makubwa. Uimara sawia na udhibiti usiotegemea hisia ni muhimu kwa nidhamu ya kila familia. Sema unachomaanisha kwa utulivu, songa mbele kwa kuzingatia, kujali wengine, na fanya kile unachosema bila kupotoka. {3T 532.2}

Italipa kuonesha mapenzi katika ushirika wako na watoto wako. Usiwafukuze kwa kukosa huruma katika michezo yao ya kitoto, furaha, na huzuni. Kamwe usikubali mikunjo usoni pako au neno kali likatoka midomoni mwako. Mungu huandika maneno haya yote katika kitabu Chake cha kumbukumbu. Maneno makali huamsha hasira, hubadilisha mwenendo kwa kuleta ugwadu na kuumiza mioyo ya watoto, na wakati mwingine vidonda hivi ni vigumu kupona. Watoto wanaathiriwa sana na uonevu huu mdogo, na wengine hukata tamaa na wasiweze kuisikiliza sauti kubwa (ya juu), yenye hasira ya kuamuru au kujali vitisho vya adhabu. Uasi umewekwa mara kwa mara mioyoni mwa watoto kupitia nidhamu isiyo sahihi ya wazazi, wakati endapo kanuni sahihi ingechukuliwa, watoto wangeunda tabia nzuri na zenye usawa. Mama ambaye hana udhibiti kamili wa yeye mwenyewe hastahili kuwa na usimamizi wa watoto. {3T 532.3}

Ndugu M amejengwa na tabia yenye uhakika ya mkewe. Amekuwa mwenye ubinafsi/mchoyo kama yeye. Akili yake karibu imechukuliwa na "mimi na cha kwangu mwenyewe," na ameondoa vitu vingine vyenye umuhimu zaidi. Hachukui

msimamo wake katika familia yake kama baba wa kundi lake na, bila ubaguzi na asiyeshawishika, akifuata hatua sawia kwa watoto wake. Mkewe siyo mama wa kweli kwa watoto wasio na mama, na bila mabadiliko kamwe hawezi kuwa mama wa kweli kwa watoto wake wasio na mama. Ndugu M, kama baba kwa watoto wake, hajasimama katika nafasi yake kama ambavyo Mungu angemtaka. Hawa watoto wasio na mama ni watoto wadogo wa Mungu, wenye thamani machoni Pake. Kwa asili au kawaida ndugu M ana tabia nyororo, yenye kujali, mwanana, iliyosafishwa, ya upendo, ya ukarimu, yenye hisia, wakati mkewe ni kinyume kabisa. Badala ya kuitengeneza na kuilainisha tabia ya mkewe, yeye ndiye anayebadilishwa na mkewe. {3T 533.1}

Anafikiri kuwa ili kuwa na amani lazima aache vitu vinavyosumbua akili yake vipite tu. Amejifunzakutii na kuyasalimisha maoni ya mke wake havitarajiwi. Mkewe atatawala; atapitisha maoni yake kwa gharama yoyote. Ikiwa wote hawatakuwa dhati na bidii katika juhudi zao za kurekebisha, hawatapata uzima wa milele. Wamekuwa na nuru, lakini wamepuuza kuifuata. Upendo wa ubinafsi wa ulimwengu umepofusha maoni yao na kuifanya mioyo yao kuwa migumu. Dada J anahitaji kuona kuwa ikiwa hataacha ubinafsi wake, na akashinda nia/mapenzi yake, mihemko na hulka yake, hawezi kufika mbinguni. Angeziharibu mbingu zote kwa vitu hivi vilivyomo katika tabia yake. Namuonya dada J atubu. Ninamwita kwa Jina la Bwana wangu kuamka haraka kutoka katika usingizi na upumbavu wake wa kutojali, kutii ushauri wa Shahidi wa Kweli, na kutubu kwa bidii; kwa maana anaihatarisha nafsi yake. {3T 533.2}

Mungu ni Mwenye huruma. Sasa ataikubali sadaka ya moyo uliovunjika na roho iliyopondeka. Je! dada J ataweka udhuru kama yule Mlawi na kuhani, kwa kutoona na kuhisi maafa/ole za wengine, na kupita upande wa pili? Mungu humwajibisha huyu mama kwa kupuuza wajibu, kwa kutoonesha huruma na wema kwa wenye shida. Hazitii amri za Mungu ambazo zinaonesha wazi wajibu wake kwa jirani yake. Kristo alimwambia wakili: "Fanya hivi, nawe utaishi." Kwa hivyo kupuuza wajibu kwa jirani yetu kutatusababishia kupoteza uzima wa milele. {3T 533.3}

Utengwaji Wa Familia

K, mtoto masikini, kama wengine wengi, ana kazi ya kufanya ambayo hajawahi kuiota. Amerudi nyuma kutoka kwa Mungu. Anajiwazia mengi kuhusu mwenyewe, na anatafuta kuufurahisha ulimwengu, siyo kwa upendo wa roho usiojifikiria binafsi na kwa kutafuta kuzigeuza kwa Kristo, bali kwa ukosefu wake wa kiroho, na kufanana kwake na ulimwengu kwa roho na matendo. Anapaswa kuifia nafsi na kupata uzoefu wa kufanya mema. Yeye ni mpuuziaji na hana huruma. Roho hii ya barafu, isiyoweza kufikiwa, inapaswa kutiishwa, kuyeyushwa na mwangaza wa jua la upendo wa Kristo. Anajifungia sana kwake mwenyewe. Mungu aliona kuwa yeye ni mmea masikini uliodumaa, usiozaa matunda, bali majani. Mawazo yake

yalikuwa karibu kabisa na "mimi na cha kwangu (me, my, myself na mine)." Kwa rehema Mungu amekuwa akipogoa mmea huu wa upendo wake, akikata matawi, ili mizizi iweze kuzama zaidi. Amekuwa akitafuta kumvuta kwake mtoto huyu. Maisha yake ya kidini yamekaribia kukosa matunda. Anawajibika kwa talanta aliyopewa na Mungu. Anaweza kuwa mwenye faida; anaweza kuwa mfanyakazi mwenza na Kristo ikiwa atavunja ukuta wa ubinafsi ambao umemfunga mbali na nuru na upendo wa Mungu. {3T 534.1}

Wapo wengi ambao wanahitaji huruma na ushauri wetu, lakini siyo ushauri huo ambao unaashiria ubora katika mtoaji na udhalilishaji kwa mpokeaji. K anahitaji upole, huruma nyororo, kujali, na upendo wa Mungu unaoyeyusha moyoni mwake. Mwonekano wake pale anapomtazama mtu na toni za sauti zinapaswa kurekebishwa kwa zingatio la uangalifu na upendo mwanana, kujali, na heshima. Kila muonekano na kila toni ya sauti inayomaanisha, "mimi ni bora zaidi yako," huleta ubaridi wa uwepo wake na ni kama barafu kuliko mwale wa mwanga wa jua unaotoa joto. Dada yangu, ushawishi wako una nguvu. Unawajenga wale unaoshirikiana nao, vinginevyo huwezi kukubaliana nao. Hauna mawazo hata kidogo ya kujengwa mwenyewe kwa ushawishi bora wa wengine na kusalimisha maoni na maamuzi yako kwao. Utaamua na kufikiri kama uonavyo na kudhibitisha maoni yako na hatua yako. Usipoweza kuwashawishi wengine utarudia tena na tena katika kipengele kile kile. Sifa hii katika tabia yako itakuwa ya thamani ikiwa itatakaswa kwa Mungu na kudhibitiwa na Roho Wake Mtakatifu; lakini ikiwa sivyo, itathibitisha laana kwako na laana kwa wengine. Madai, kauli na ushauri wenye harufu ya roho ya udikteta, yaani kulazimisha mambo siyo matunda mazuri. Unahitaji upole, kulainishwa na upendo wa Kristo moyoni mwako unaoyeyusha, ambao utaonekana katika matendo yako yote kwa familia yako na kwa wale wote walio chini ya ushawishi wako. {3T 534.2}

Ninaogopa, ninaogopa sana, kwamba J mbingu itamshinda kuipata. Anaupenda ulimwengu na vitu vya ulimwengu sana kiasi kwamba hana upendo uliobaki wa kumwachia Yesu. Amejifungia sana katika ukoko wa ubinafsi kiasi kwamba nuru inayoangaza kutoka mbinguni haiwezi kupenya kwenye ukuta baridi, na mweusi wa kujipenda mwenyewe na kujithamini kuwa bora ambao amekuwa akiujenga katika maisha yote. Upendo ni ufunguo wa kufungua mioyo, lakini mmea wa thamani wa upendo haujathaminiwa. J amepofusha macho yake kwa muda mrefu kwa ubinafsi wake kiasi kwamba sasa hawezi kuutambua. Amekuwa na dini ndogo sana ya uhalisia/kweli kiasi kwamba moyoni yeye ni wa ulimwengu, na ninaogopa kuwa ulimwengu huu ndio mbingu pekee ambayo atakuwa nayo. Ushawishi wake kwa mumewe siyo mzuri. Mumewe anayumbishwa nao na wala haoni umuhimu wa kuimarishwa na neema ya Mungu kusimama kwa haki na ujasiri wa kweli wa kimaadili. Siyo tu kwamba mwanamke huyo anashindwa kutambua na kufanya kazi ambayo Mungu anaitaka kwake, bali pia ana ushawishi mkubwa wa kumzuia

mumewe na kumfunga mikono. Na amefanikiwa kwa kiwango kikubwa. Amempofusha mumewe. {3T 535.1}

Ndugu M anapaswa kuzingatia kwamba Mungu ana madai juu yake ambayo yako juu ya kila uhusiano wa kidunia. Anahitaji dawa ya kupaka macho, mavazi meupe, na dhahabu, ili awe na tabia ya ulinganifu na nafasi kubwa ya kuingia katika ufalme wa Mungu. Hakuna chochote pungufu ya uongofu kamili kinachoweza kufungua roho ya mkewe ili aone makosa yake na kuyakiri. Ana mabadiliko makubwa anayopaswa kuyafanya, ambayo hajayafanya kwa sababu hakutambua hali yake ya kweli na hakuweza kuona umuhimu wa matengenezo. Hadi sasa badala ya kuwa tayari kujifunza juu ya Bwana wa mbinguni, ambaye alikuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo, yeye anachukulia upole kama utumwa; na kuwa mtu wa roho, mnyenyekevu wa akili kwa kuwachukulia wengine bora kuliko yeye mwenyewe, anaona kama ni kujishusha na kujidhalilisha. {3T 535.2}

J ana roho isiyofaa kwa uhakika, ya kiburi, yenye kunuia kufanyayale anayoyataka tu. Haoni kitu chochote cha kuhitajika katika roho ya upole na utulivu ambayo anapaswa kuitamani. Pambo hili la thamani linayo dhamana ndogo sana kwake kiasi kwamba hawezi kukubali kulivaa. Mara nyingi, ana roho ya chuki ambayo ni kinyume na Roho wa Mungu kama mashariki ilivyo mbali na magharibi. Upole na uungwana wa kweli ni vito la thamani kubwa machoni pa Mungu. Roho ya upole na yenye utulivu haitakuwa ikitafuta furaha kwa ajili yake yenyewe, bali itatafuta kujisahau yenyewe na kupata mambo matamu na kuridhika kwa Kweli katika kuwafanya wengine wawe na furaha. {3T 536.1}

Kwa majaliwa ya Mungu, dada N ametengwa na familia ya baba yake. Ingawa, pamoja na wengine, anashiriki sifa za ushirika wa familia, kubeba majukumu mazito kumemwondoa kutoka kwake na kumpa hamu ya shida za wengine. Kwa kiwango fulani ameufungua moyo wake kwa huruma na upendo kwa familia ya Mungu, akipendezwa na kuwa shauku na wengine. Kazi na kusudi la Mungu vimeteka umakini wake. Amehisi, kwa kiwango fulani, kwamba watu duni walioanguka ni ndugu zake wakubwa. Amelazimika kujielimisha kufikiri kwa ajili ya wengine, kuwafanyia wengine, na kuisahau nafsi; na bado hajakuza kama ambavyo angepaswa, maslahi, huruma, na mapenzi kwa wengine, mambo ambayo ni muhimu kwa wafuasi wa Kristo. Anahitajika kuwa na huruma zaidi na ukali kidogo tu, haki isiyobadilika. Kwa kuwa ametoa shauku yake na muda katika somo kubwa la matengenezo ya afya amefika mbali zaidi ya nafsi yake. Kwa vile amefanya hivi amebarikiwa. Kadri anavyofanya zaidi kwa faida ya wengine, ndivyo anavyozidi kuona kufanya zaidi na ndivyo anavyohisi kuwa na shauku ya kufanya. {3T 536.2}

Kazi yake kwa wengine mara nyingi humleta pale ambapo zoezi la imani linahitajika kumleta katika nafasi ngumu na zenye kujaribu. Lakini majibu ya maombi ya dhati hutekelezwa, na imani, upendo, na ujasiri kwa Mungu huimarishwa. Kupitia shida na majaribu mara kwa mara, uzoefu hupatikana. Mungu anaufinyanga moyo uwe kama Yeye Mwenyewe. Na bado nafsi hupiga mayowe kila wakati kwa ajili ya ushindi. Dada N anahitaji kukuza upole zaidi na uangalifu wa kifikra katika uhusiano wake wa kila siku na wengine. Anahitaji kujifunza namna ya kujitiisha. Ikiwa kweli yeye ni Mkristo atahisi kwamba lazima atoe sehemu bora zaidi, na ikiwa kuna haja atoe nzima, ya maisha yake kwa bidii isiyo na ubinafsi, bidii ya uvumilivu na hivyo kuonesha upendo wake kwa Bwana. Bila uzoefu huu angeanguka mbali na ukamilifu wa tabia ya Kikristo. {3T 537.1}

Dada N amechukua hatua kadhaa za mapema, na familia wanahisi kuwa amewaacha, na huu ni msalaba kwao. Hawahisi kuwa sasa ana shauku namaslahi sawa na mapenzi na vitu maishani kama wao wenyewe. Wanahisi kuwa hawawezi kufurahia kama zamani, ushirika wa dada yao. Wanahisi kuwa yeye ndiye anayepaswa kulaumiwa, kwamba amebadilika, na kwamba huruma yake haiko nao tena. Sababu ya ukosefu huu wa hisia ni kwamba dada N amekuwa akiendelea mbele katika kuhisi shida za wengine, wakati wao wamekuwa watumishi wavivu, hawafanyi kazi ambayo Mungu amewapatia kuifanya duniani. Kwa hivyo wamekuwa wakirudi nyuma. Familia kwa sababu ya ubinafsi imejifungia mapenzi na masilahi kwao wenyewe na upendo wa ulimwengu. {3T 537.2}

N amekuwa mtendakazi katika kusudi jema. Matengenezo ya afya kwake yamekuwa mada yenye umuhimu mkubwa, kwani uzoefu wake umemwonesha umuhimu wake. Familia ya baba yake hawajaona umuhimu wa matengenezo ya afya. Hawajaona sehemu yake katika kazi ya kufunga ya siku hizi za mwisho, kwa sababu hawajataka kuona. Wameangukia kwenye gari la desturi, na ni kazi ngumu kufanya bidii inayohitajika kutoka nje ya gari hilo. Wanaona ni afadhali wangeachwa. Ni jambo baya kuchakaa kwa kutofanya kazi. Lakini familia hii hakika itapimwa katika mizani na kuonekana imepungua isipokuwa waanze kufanya kitu mara moja. "Sasa ikiwa mtu yeyote hana Roho wa Kristo, huyo si Wake." Hii ni lugha kali. Ni nani anayeweza kuhimili mtihani huu? Neno la Mungu kwetu ni mfano wa picha ya akili ya Mungu na ya Kristo, pia ya mwanadamu aliyeanguka, na ya mtu aliyefanywa upya kwa Mfano wa Kristo, mwenye akili ya mbingu/Bwana. Tunaweza kulinganisha mawazo yetu, hisia zetu, na nia yetu na picha ya Kristo. Hatuna uhusiano Naye isipokuwa tukiwa tayari kufanya kazi za Kristo. {3T 537.3}

Kristo alikuja kufanya mapenzi ya Baba Yake. Je! Tunafuata hatua Zake? Wote ambao wameitwa kwa Jina la Kristo wanapaswa kutafuta kila wakati urafiki wa karibu na mwanana zaidi Naye, ili watembee kama Yeye alivyotembea, na kufanya kazi za Kristo. Tunapaswa kuelekeza masomo ya maisha Yake kwa maisha yetu.

Kristo "alijitoa Mwenyewe kwa ajili yetu, ili atukomboe kutoka katika uovu wote, na kuwatakasa ndani Yake watu wa pekee, wenye bidii ya matendo mema." "Katika hili twajua upendo wa Mungu, kwa kuwa Yeye aliutoa uhai Wake kwa ajili yetu; nasi tunapaswa kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya ndugu." Hapa kuna kazi ya kujikana nafsi ambayo lazima tuifanye kwa uchangamfu, kwa kuiga mfano wa Mkombozi wetu. Maisha ya Mkristo lazima yawe ya mizozo/changamoto na kujitolea. Njia ya wajibu inapaswa kufuatwa, na siyo njia ya mwelekeo na uchaguzi. {3T 538.1}

Wakati familia ya ndugu I itakapoona kazi iliyo mbele yao, na kufanya kazi ambayo Mungu amewaachia wafanye, hawatatenganishwa sana kutoka kwa ndugu na dada O na dada N, na wale ambao wanafanya kazi kwa umoja na Bwana. Inaweza kuchukua muda kufikia unyenyekevu kamili kwa mapenzi ya Mungu, lakini hatuwezi kuacha katikati na hivyo tusifaekwa ajili ya mbingu. Dini ya Kweli itamwongoza mwenye nayo kufikia ukamilifu. Mawazo yako, maneno yako, na matendo yako, pamoja na shauku yako na tamaa zako, lazima vyote viletwe chini ya mapenzi ya Mungu. Lazima uzae matunda kwa utakatifu. Ndipo utakapoongozwa kumtetea maskini, yatima, na mtu anayeteseka. Utamtendea haki mjane na utawasaidia wahitaji. Utashughulika kwa haki, utapenda rehema, na utaenenda kwa unyenyekevu mbele za Mungu. {3T 538.2}

Lazima tumruhusu Kristo aingie ndani ya mioyo na nyumba zetu ikiwa tunataka kutembea katika nuru. Majumba yetu yanapaswa kufanywa yote yanayomaanishwa na neno. Inapaswa kuwa mbingu ndogo juu ya dunia, mahali ambapo upendo/mapenzi yanakuzwa badala ya kukandamizwa kwa kupania. Furaha yetu inategemea palizi hili la upendo, huruma, na adabu ya kweli kwa kila mmoja. Sababu ya kuwa na wanaume na wanawake wengi wenye mioyo migumu katika ulimwengu wetu ni kwamba mapenzi ya Kweli yamezingatiwa kama udhaifu na yamekatishwa tamaa na kukandamizwa (wakati wakiwa watoto). Sehemu bora ya asili ya watu wa kundi hili ilipotoshwa na kudhoofishwa utotoni, na ikiwa miale ya nuru ya Kiungu haitayeyusha ubaridi wao na ubinafsi wenye mioyo migumu, furaha ya watu kama hao huzikwa milele. Ikiwa tunataka kuwa na mioyo laini, kama alivyokuwa Yesu wakati alipokuwa duniani, na huruma iliyotakaswa, kama waliyonayo malaika kwa wanadamu wenye dhambi, lazima tukuze huruma za utoto, ambazo ni usahili wenyewe. Ndipo tutasafishwa, kuinuliwa, na kuongozwa na kanuni za mbinguni. {3T 539.1}

Akili iliyokuzwa ni hazina kubwa; lakini bila ushawishi laini wa huruma na upendo uliotakaswa, siyo ya thamani kubwa zaidi. Tunapaswa kuwa na maneno na matendo ya kuwajali wengine kwa upole. Tunaweza kudhihirisha umakini mara elfu kwa maneno ya urafiki na mwonekano mwema, ambayo yataonekana kwetu tena. Wakristo wasio na fikra njema kwa wengine hudhihirisha kuwa hawako katika umoja na Kristo kwa kuwapuuza wengine. Haiwezekani kuwa katika umoja na

Kristo na bado kuwa watu wasio na fadhili kwa wengine na kusahau haki zao. Wengi hutamani sana huruma ya kirafiki. Mungu amempatia kila mmoja wetu utambulisho wake, ambao hauwezi kuunganishwa na ule wa mwingine; lakini tabia zetu binafsi hazitaonekana sana ikiwa kweli sisi ni wa Kristo na mapenzi Yake ni yetu. Maisha yetu yanapaswa kuwekwa wakfu kwa ajili ya mema na furaha ya wengine, kama ilivyokuwa kwa Mwokozi wetu. Tunapaswa kusahau nafsi zetu, kila wakati tukitafuta fursa, hata katika vitu vidogo, kuonesha shukrani kwa neema tulizopokea kutoka kwa wengine, na tukitafuta fursa za kuwachangamsha wengine na kupunguza uzito na huzuni na mizigo yao kwa matendo ya wema, huruma nyororo, upendo mwanana, kujali na hata kwa yale matendo madogo ya upendo. Heshima hizi ndogo na uungwana, ambazo zinaanzia katika familia zetu, husambaa nje ya mzunguko wa familia, husaidia kutengeneza jumla ya furaha za maisha; na kupuuzwa kwa vitu hivi vidogo hufanya jumla ya uchungu na huzuni ya maisha. {3T 539.2}

Ni kazi tunayofanya au tusiyofanya ambayo inaelezea kwa nguvu kubwa juu ya maisha yetu na hatima yetu. Mungu anatuhitaji kuboresha kila fursa kwa faida ambayo tunapewa. Kupuuza kufanya hivyo ni hatari kwa ukuaji wetu wa kiroho. Tunayo kazi kubwa ya kufanya. Tusipitishe siku kwa uvivu na kupoteza masaa ya thamani ambayo Mungu ametupatia ambayo kwayo tunakamilisha tabia za mbinguni. Hatupaswi kuwa wavivu au walegevu katika kazi hii, kwani hatuna muda wa kutumia bila kusudi au lengo. Mungu atatusaidia kushinda makosa yetu ikiwa tutaomba na kumwamini. Tunaweza kuwa zaidi ya washindi kupitia Yeye ambaye ametupenda sisi. Wakati maisha mafupi katika ulimwengu huu yanapokuwa yamekamilika, nasi tukaona jinsi tunavyoonekana na kujua jinsi tunavyojulikana, ni kwa jinsi gani muda utaonekana kuwa mfupi na vitu vya ulimwengu huu vitaonekana kwetu kuwa vidogo vikilinganishwa na utukufu wa ulimwengu bora! Kristo asingeacha nyua za Kifalme na kutwaa ubinadamu, na kufanyika dhambi kwa ajili ya wanadamu, kama asingeona kwamba mwanadamu anaweza, kwa msaada Wake, kuwa na furaha isiyo na kikomo na kupata utajiri wa kudumu na maisha ambayo yangeenda sawa na maisha ya Mungu (milele). Yeye Alijua kwamba bila msaada Wake mtu mwenye dhambi asingeweza kuyapata haya. {3T 540.1}

Tunapaswa kuwa na roho ya maendeleo. Lazima tujilinde daima dhidi ya kudumu katika maoni yetu, hisia zetu, na matendo yetu. Kazi ya Mungu inasonga mbele. Matengenezo lazima yafanyike, na lazima tushikilie usukani na kusaidia kuendelea na gurudumu la matengenezo. Nishati, hulka na uvumilivu na shauku iliyosawazishwa kwa hekima, sasa inahitajika kwa kila Mkristo. Kazi ya kuokoa roho bado imeachwa kwetu, wanafunzi wa Kristo. Hakuna hata mmoja wetu aliyepewa udhuru. Wengi wamekuwa dhaifu na kudumaa katika maisha yao ya Kikristo kwa sababu ya kutotenda. Tunapaswa kutumia muda wetu kwa uadilifu na bidii tukingali katika ulimwengu huu. Ni kwa kiasi gani tunapaswa kuboresha kwa bidii kila fursa ya kutenda matendo mema, ya kuwaletea wengine ujuzi wa Ukweli!

Kauli mbiu yetu inapaswa kuwa, "Tunasonga mbele, juu zaidi," hakika, kusonga mbele katika jukumu na ushindi. {3T 540.2}

Nimeoneshwa kwa habari ya watu waliotajwa kwamba Mungu anawapenda na angewaokoa ikiwa wangeokolewa kwa njia Yake aliyoiweka. "Naye ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, Naye atawatakasa wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki. Wakati ule ndipo dhabihu za Yuda na Yerusalemu zitakapopendeza mbele za Bwana, kama katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani." Huu ndio mchakato, mchakato wa utakaso, wa usafishaji, ambao unapaswa kufanywa na Bwana wa majeshi. Kazi inajaribu sana roho, lakini ni kupitia mchakato huu tu kwamba taka na uchafu unaochafua vinaweza kuondolewa. Majaribu yetu yote ni muhimu kutuleta karibu na Baba yetu wa mbinguni, kwa kuyatii mapenzi Yake, ili tumpatie Bwana sadaka kwa haki. Kwa kila mmoja ambaye jina lake limetajwa hapa, Mungu amewapa uwezo, talanta zinazopaswa kuboreshwa. Kila mmoja anahitaji uzoefu mpya na unaoishi katika maisha ya Mbingu ili afanye mapenzi ya Mungu. Hakuna kiwango cha uzoefu wa zamani kitakachotosha kwa sasa au kutatuimarisha kushinda taabu katika njia yetu. Lazima tuwe na neema mpya na nguvu mpya kila siku ili tuweze kushinda. {3T 541.1}

Huwa ni nadra sana kwetu, katika mambo yote, kuwekwa katika mazingira sawa mara mbili. Ibrahimu, Musa, Eliya, Danieli, na wengine wengi wote walijaribiwa vikali, lakini siyo kwa njia ile ile. Kila mtu ana majaribio/changamoto na mitihani yake binafsi katika mfululizo wa drama au matukio ya maisha, lakini majaribu yale yale ni mara chache sana yatakuja mara mbili. Kila mmoja ana uzoefu wake mwenyewe, wa kipekee katika tabia na mazingira yake, ili kufanikisha kazi fulani. Mungu ana kazi, kusudi, katika maisha ya kila mmoja wetu. Kila tendo, japo dogo, lina nafasi yake katika uzoefu wetu wa maisha. Lazima tuwe na nuru na uzoefu endelevu kutoka kwa Mungu. Sisi sote tunahitaji haya, na Mungu Yuko tayari zaidi kwamba tuwe nayo ikiwa tutayachukua. Bwana Hajafunga madirisha ya mbinguni kwa maombi yako, lakini umehisi kuridhika kupita bila msaada wa Bwana ambao weew unauhitaji sana. {3T 541.2}

Ni kiasi kidogo namna gani unaelewa ushawishi wa matendo yako ya kila siku juu ya historia ya wengine. Unaweza kufikiria kuwa kile unachofanya au kusema kina matokeo kidogo, wakati matokeo muhimu zaidi kwa mema au mabaya ni matokeo ya maneno na matendo yetu. Maneno na matendo yanayoonekana kama madogo na yasiyo muhimu ila ndivyo ni viungo katika mlolongo mrefu wa matukio ya wanadamu. Hujahisi hitaji la kudhihirisha mapenzi ya Mungu kwetu katika matendo yote ya maisha yetu ya kila siku. Pamoja na wazazi wetu wa kwanza tamaa ya kuridhisha hamu moja ya chakula ilifungua milango ya ole na dhambi duniani. Laiti ninyi, dada zangu wapendwa, mngeweza kuhisi kwamba kila hatua mnayochukua inaweza kuwa na ushawishi wa kudumu na wenye udhibiti juu ya

maisha yenu wenyewe na tabia za wengine. Ah, ni hitaji kubwa kiasi gani, basi la ninyi kuwa na ushirika na Mungu! Ni hitaji kubwa kiasi gani la neema ya Mungu ituongozayo kila hatua na kutuonesha jinsi ya kukamilisha tabia za Kikristo! {3T 542.1}

Wakristo watakuwa na mandhari mpya na majaribu mapya ya kupita ambapo uzoefu wa zamani hauwezi kuwa mwongozo wa kutosha. Tuna hitaji kubwa la kujifunza juu ya Mwalimu wa Mbinguni sasa kuliko wakati mwingine wowote wa maisha yetu. Na kadri tunavyopata uzoefu, ndivyo tunavyokaribia zaidi kuelekea nuru safi ya mbinguni, na ndivyo tutakavyogundua zaidi ndani yetu hitaji la matengenezo. Sote tunaweza kufanya kazi nzuri katika kuwabariki wengine ikiwa tutatafuta ushauri wa Mungu na kufuata kwa utii na imani. Njia ya mwenye haki ni endelevu, inasonga mbele, kutoka nguvu hadi nguvu, kutoka kwa neema hadi neema, na kutoka utukufu hadi utukufu. Mwangaza wa Bwana utaongezeka zaidi na zaidi, unaolingana na harakati zetu za kusonga mbele, kutufanya tufuzu kufikia majukumu na dharura zilizoko mbele yetu. {3T 542.2}

Wakati majaribu yanapowashinikiza, wakati hali ya kukata tamaa na giza la kutokuamini linapoyadhibiti mawazo yenu, wakati ubinafsi unapoumba matendo yenu, hamuoni hitaji la Mungu kwenu na ufahamu wa kina na kamilifu wa mapenzi Yake. Hamyajui mapenzi ya Mungu, wala hamwezi kuyajua wakati bado mnaishi kwa ajili ya nafsi yenu wenyewe. Mnategemea nia zenu njema na maamuzi yenu mazuri, na jumla kuu ya maisha inaundwa na maamuzi yaliyofanywa pamoja na maamuzi yaliyovunjwa. Mnachohitaji wote ni kuifia nafsi, kuacha kushikamana nayo, na kujisalimisha kwa Mungu na kumng'ang'ania. Kwa furaha ningewafariji ikiwa ningeweza. Kwa furaha napenda kusifu tabia zenu nzuri, malengo mazuri, na matendo mema; lakini Mungu hakupenda kunionesha haya. Aliwasilisha mbele yangu vizuizi vinavyowakosesha kupata bora na sifa nzuri, ile iliyoinuka ya utakatifu mnayohitaji kuwa nayo ili msipoteze pumziko la mbinguni na utukufu wa milele ambao angependa muufikie. Mwangalieni Yesu na siyo nafsi zenu. Yeye Ndiye yote na katika yote. Faida ya damu ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka itatumika kuwasafisha kutoka katika dhambi ndogo na kubwa. Kwa imani wekeni nafsi zenu kwa Mungu kama kwa Muumba Mwaminifu. Usiwe na hofu na mashaka kila wakati kwamba Mungu atakuacha wewe. Yeye hatakuacha kamwe isipokuwa ukimwacha. Kristo ataingia na kukaa nawe ikiwa utamfungulia milango ya mioyo yenu Kwake. Kunaweza kuwa na upatanifu/maelewano kamili kati yako na Baba na Mwanawe ikiwa utaifia nafsi yako na kuishi kwa ajili ya Mungu. {3T 542.3}

Ni wachache kiasi gani wanaotambua kuwa wana sanamu vipenzi, zile wazipendazo, na wameendekeza dhambi! Mungu huona dhambi hizi ambazo unaweza kupofushwa, na Yeye hufanya kazi na kisu Chake cha kupogoa ili kukwangua kwa kina na kutenganisha dhambi hizi za kupendeza kutoka kwako. Ninyi nyote mnahitaji kuchagua wenyewe mchakato wa utakaso. Ni vigumu kiasi

gani kwenu kujisalimisha katika usulubishwaji wa nafsi; lakini wakati matendo na kazi zote zinapowasilishwa kwa Mungu, Kwake Yeye anayejua udhaifu wetu na dhambi zetu, Yeye huchukua njia bora kabisa ya kuleta matokeo yanayotarajiwa. Ilikuwa kupitia mapigano ya kila wakati na imani yakinifu kwamba Henoko alitembea na Mungu. Mnaweza wote kufanya vivyo hivyo. Mnaweza kuongoka kabisa na kubadilishwa, na kuwa kweli watoto wa Mungu, haufurahii tu maarifa ya mapenzi Yake, bali kwa mfano wako, ukiwaongoza wengine katika njia ile ile ya utii mnyenyekevu na uchaji Mungu, yaani kujitoa wakfu. Utauwa wa Kweli unaenea na kujulikana. Mwandishi wa Zaburi anasema: "Sikusitiri haki Yako moyoni mwangu; Nimetangaza uaminifu Wako na wokovu Wako. Sikuficha fadhili Zako wala kweli Yako Katika kusanyiko kubwa."Popote penye upendo wa Mungu, kuna shauku ya kuuonesha kila wakati. {3T 543.1}

Hebu Mungu awasaidie nyote kufanya bidii za dhati ili kupata uzima wa milele na kuwaongoza wengine katika njia ya utakatifu. {3T 544.1}

SURA YA 48

DHAMBI YA TAMAA

Ndugu mpendwa P: Ningependa kufanya juhudi moja zaidi kukuonya kuwa na bidii ya kuupata ufalme. Onyo baada ya onyo limetolewa kwako, na haukujali. Lakini, loo, ikiwa hata sasa utatubu njia zako mbaya za zamani na kumgeukia Bwana, unaweza kuwa hujachelewa sana kwa makosa kurekebishwa. Nguvu zote za akili yako zimewekwa katika kujipatia pesa. Umeabudu pesa. Imekuwa mungu wako. Fimbo ya Mungu inaning'inia juu yako. Hukumu Zake zinaweza kukufikia wakati wowote na utashuka kaburini ukiwa hauko tayari, nguo zako zimejipatia madoa na kuchafuliwa na uharibifu wa ulimwengu. Kumbukumbu yako ni ipi mbinguni? Kila fedha uliyoikusanya imekuwa kama kiunga cha ziada kwenye mnyororo unaokufunga kwa ulimwengu huu masikini. Shauku yako ya kupata faida imekuwa ikiimarishwa kila wakati. Mzigo wa mawazo yako umekuwa ni jinsi gani unaweza kupata mali zaidi. Umekuwa na uzoefu wa kutisha, ambao unapaswa kuwa onyo kwa wale wanaoruhusu upendo wa ulimwengu kuchukua milki ya roho zao. Umekuwa mtumwa wa mungu mali (mamoni). Je, utasema nini wakati Bwana atakapokuuliza hesabu ya uwakili wako? Umeruhusu kupenda pesa kuwa shauku ya kutawala ya maisha yako. Umelewa sana katika kupenda fedha kama mlevi na pombe yake. {3T 544.2}

Yesu ameomba kwamba ule mti ambao hauzai matunda uachwe kidogo; na ninatoa ombi moja zaidi kwako usiwe na bidii ndogo, bali ujitahidi sana, kwa ajili ya ufalme. Jikomboe mwenyewe kutoka kwenye mtego wa Shetani kabla maneno, "Yeye amejiunga na sanamu, achana naye," hayajatamkwa juu yako kuhusiana na mbingu. Wapenda fedha wote, kama wewe, siku moja watalia kwa uchungu wenye maumivu makubwa: "Ah, udanganyifu wa utajiri! Nimeuza roho yangu kwa ajili ya pesa." Tumaini lako pekee sasa ni kutotembea kwa udhaifu, bali ugeuze hatua haraka na kwenda upande tofauti. Kwa dhati kabisa omba msaada wako, nguvu ya mapenzi ambayo umeitumia kwa muda mrefu katika mwelekeo mbaya, na sasa fanya kazi kwa mwelekeo mwingine-nyuzi 180. Hii ndiyo njia pekee ya wewe kushinda tamaa. {3T 544.3}

Mungu amefungua njia ambazo tamaa inaweza kushindwa - kwa kutenda matendo mema. Kwa maisha yako unasema kwamba unathamini hazina za ulimwengu kuliko utajiri wa milele. Unasema: "Kwaheri, mbingu; kwaheri, maisha ya kutokufa; mimi nimeuchagua ulimwengu huu." Unafanya biashara ya kubadilishana, lulu ya ya thamani kubwa kwa faida ya muda mfupi ya sasa. Wakati ukionywa hivi na Mungu, wakati akiwa katika uangalizi Wake ameweka miguu yako katika mto mweusi wenye giza, Je! Utathubutu kuendeleza tabia yako ya kupenda pesa? Je! kama

matokeo ya kitendo chako cha mwisho cha maisha yaliyotumika vibaya, ulaghai na kujaribu kujinufaisha kwa njia isyo halali na kubaki na kile ambacho ni haki ya mtu mwingine? Je! Utajihesabu kuwa unaamini kwamba unatenda haki kwa ndugu yako? Je! Utaongeza kitendo kingine cha hila, na unyang'anyi na kukazana kujitwalia mali na kuishi uongo kwa orodha ya matendo yako ambayo tayari yameandikwa dhidi yako kwenye rekodi zilizo hapo juu mbinguni? Je! pigo la hukumu ya kisasi cha Mungu litakuangukia na uitwe bila onyo kupita katika maji ya giza? {3T 545.1}

Mwokozi wetu mara kwa mara na kwa bidii alikemea dhambi ya kutamani. "Akawaambia, Angalieni, jihadharini na tamaa; kwa maana uzima wa mtu hauko katika wingi wa vitu alivyo navyo. Akawaambia mfano, akisema, Shamba la mtu mmoja tajiri lilikuwa limezaa sana; akaanza kuwaza moyoni mwake, akisema, Nifanyeje? Maana sina pa kuyaweka akiba mavuno yangu. Akasema, Nitafanya hivi; nitazivunja ghala zangu, nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kisha, nitajiambia, Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi. Lakini Mungu akamwambia, Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu." {3T 545.2}

Mungu ameweka sheria kwa watu Wake kwamba sehemu ya kumi ya maongeo yote yatakuwa Yake. Nimekupa, asema Mungu, fungu la kumi; Nataka moja ya kumi ya maongeo yote. Hiyo sehemu ya kumi tajiri alikuwa amemnyima Mungu. Kama asingefanya hivi, kama angempenda Mungu kuliko chochote badala ya kujipenda na kujitumikia mwenyewe, asingekusanya hazina kubwa sana kiasi cha kukosa nafasi ya kuhifadhi mazao. Laiti kama angekuwa ameiweka mali yake katika kusaidia ndugu zake wahitaji ili kuwapatia mahitaji yao, kusingekuwa na haja ya kubomoa na kujenga ghala kubwa zaidi. Lakini alikuwa amepuuza kanuni za sheria ya Mungu. Hakuwa amempenda Bwana kwa moyo wake wote na jirani yake kama nafsi yake.
Kama angeutumia utajiri wake kama fadhila aliyokopeshwa na Mungu kwa kufanya mema angeliweka hazina mbinguni na kuwa tajiri wa matendo mema. {3T 546.1}

Urefu na kufaa katika maisha haya haijumuishi katika kiwango cha mali zetu za kidunia. Wale wanaotumia utajiri wao kufanya mema hawataona ulazima wa ulimbikizaji mkubwa katika ulimwengu huu; kwa kuwa hazina ambayo hutumiwa kuendeleza kazi ya Mungu na ambayo hupewa wahitaji kwa Jina la Kristo imetolewa kwa Kristo, na Yeye hutuwekea katika benki ya mbinguni katika mifuko ambayo haichakai. Yeye anayefanya hivi ni tajiri kwa Mungu, na moyo wake utakuwa mahali ambapo hazina zake zinasitiriwa. Yeye ambaye hutumia kwa unyenyekevu kile ambacho Mungu amempatia kwa heshima ya Mpaji, akitoa huru/bure kama alivyopokea, anaweza kuhisi amani na uhakikisho katika biashara

yake yote kwamba mkono wa Mungu uko juu yake kwa wema, na yeye mwenyewe atakuwa na mvuto na mguso wa Mungu, akiwa na tabasamu la Babaye. {3T 546.2}

Wengi wamewaonea huruma Israeli wa Mungu kwa kulazimishwa kutoa kwa mpango na ukarimu, kando na kutoa sadaka za ukarimu kila mwaka. Mungu Mwenye hekima yote alijua zaidi ni mfumo gani wa fadhili ungekuwepo kulingana na uweza Wake, na amewapa watu Wake maagizo juu Yake. Daima imethibitika kuwa tisa ya kumi ina thamani zaidi kwao kuliko kumi ya kumi. Wale ambao wamefikiria kuongeza faida yao kwa kumnyima Mungu, au kwa kumletea sadaka duni, - vilema, vipofu, au vile dhaifu, - wamehakikishiwa kupata hasara. {3T 546.3}

Majaliwa, ingawa hayaonekani, yanaendelea kufanya kazi katika mambo ya wanadamu. Mkono wa Mungu unaweza kufanikisha au kuzuia, na Yeye mara nyingi huzuia kutoka kwa mtu wakati akionekana kumfanikisha mwingine. Yote haya ni kuwajaribu watu na kuwadhihirisha na kufunua moyo. Yeye huruhusu msiba umfike ndugu mmoja wakati akiwafanikisha wengine ili kuona kama wale anaowapendelea wana uchaji Mungu, na hofu Yake mbele ya macho yao na watatekeleza jukumu alilowaamuru katika Neno Lake kuwapenda jirani zao kama nafsi zao na kumsaidia ndugu yao maskini kwa upendo kufanya mema. Matendo ya ukarimu na wema yaliwekwa na Mungu ili kuifanya mioyo ya watoto wa watu kuwa yenye kujali, upendo mwanana na huruma nyororo, na kuhimiza ndani yao kujaliana na kupendana kwa kumuiga Mwalimu, ambaye kwa sababu yetu alikua masikini, ili kwamba sisi kupitia umaskini wake tuweze kutajirika. Sheria ya kutoa fungu la kumi ilijengwa juu ya kanuni ya kudumu na iliundwa kuwa baraka kwa mwanadamu. {3T 547.1}

Mfumo wa ukarimu usio na ubinafsi ulipangwa ili kuzuia uovu huo mkubwa, yaani tamaa ya mali. Kristo aliona kuwa katika ufanyaji wa biashara, upendo wa utajiri ndio itakaokuwa sababu kuu ya kung’oa utauwa wa kweli kutoka moyoni. Yeye Aliona kuwa kupenda pesa kungeingia ndani sana na kuleta ubaridi na kupenya ndani ya roho za watu, hivyo kuzuia mtiririko wa misukumo ya ukarimu na kufunga hisia zao kwa mahitaji ya wanadamu wanaoteseka na kusumbuka. "Jihadharini," lilikuwa onyo Lake mara kwa mara, "na jihadharini na tamaa." "Hamwezi kumtumikia Mungu na mali." Maonyo yanayorudiwa-rudiwa na ya kushangaza ya Mkombozi wetu ni tofauti kabisa na vitendo vya wale wanaodai kuwa wafuasi Wake ambao wanaonesha katika maisha yao shauku kubwa ya kuwa matajiri na ambao wanaonesha kwamba Maneno ya Kristo yamepotea juu yao. Tamaa ni moja wapo ya dhambi za kawaida na maarufu za siku za mwisho, na huwa na athari ya kupooza juu ya roho. {3T 547.2}

Ndugu P, hamu ya utajiri imekuwa wazo kuu la akili yako. Shauku hii moja ya kupata pesa imeua kila zingatio la uadilifu wa hali ya juu, na imekufanya usijali mahitaji na masilahi ya wengine. Umejifanya kutoguswa moyo karibu kuwa sawa na kipande cha chuma. Dhahabu na fedha zako zimeliwa, na zimekuwa kama kuvu

inayoitafuta nafsi. Laiti ukarimu wako ungekua pamoja na utajiri wako, ungeiona pesa ni kama tu njia ambayo unaweza kufanya mema. Mkombozi wetu, ambaye alijua hatari ya mwanadamu kuhusu tamaa, ametoa kinga dhidi ya uovu huu mbaya. Amepanga mpango wa wokovu ili uanze na kumalizika kwa ukarimu. Kristo alijitoa Mwenyewe, dhabihu isiyo na mwisho. Hii, yenyewe, hushuhudia moja kwa moja dhidi ya tamaa na huinua ukarimu na kutojifikiria. {3T 547.3}

Ukarimu wa kujinyima kwa uendelevu ni suluhisho la Mungu kwa dhambi za kutisha za kansa za ubinafsi na tamaa. Mungu amepanga utoaji wa mpango ili kudumisha kusudi Lake na kupunguza mahitaji ya wanaoteseka na wahitaji. Ameamuru kwamba utoaji uwe mazoea ya mtu, ili iweze kukabiliana na dhambi ya hatari na ya udanganyifu ya tamaa. Utoaji endelevu huangamiza tamaa, yaani tamaa hufa kabisa. Utoaji kwa mpango na ukarimu umeundwa kwa mpangilio wa Mungu ili kung'oa hazina kutoka kwa wale wanaotamani kwa haraka kadri wanavyopata na kuwaweka wakfu kwa Bwana, ambaye wao ni mali Yake. {3T 548.1}

Mfumo huu umepangiliwa vema kwamba watu wanaweza kutoa kitu kutoka kwenye mshahara yao kila siku na kumpatia Bwana wao sehemu ya faida ya kila uwekezaji. Mazoezi endelevu ya mpango wa Mungu wa utoaji kwa mpango hupunguza uchoyo na kuimarisha ukarimu. Utajiri ukiongezeka, watu, hata wale wanaodai kuwa na utauwa, huiweka mioyo yao juu yake; na kadiri wanavyopata vingi, ndivyo wanavyotoa kidogo kwenye hazina ya Bwana. Kwa hivyo utajiri huwafanya watu kuwa wabinafsi, na kujilimbikizia huzalisha tamaa; na maovu haya huimarika kwa kuzoezwa. Mungu anajua hatari yetu na Yeye ametuzingira njia zinazozuia uharibifu wetu. Anahitaji mazoezi ya kila mara ya ukarimu, ili nguvu ya tabia katika kazi nzuri iweze kuvunja nguvu ya tabia katika mwelekeo mwingine ulio kinyume. {3T 548.2}

Mungu anahitaji utengaji wa mali kwa ajili ya vitu vya ukarimu kila juma, ili katika mazoezi ya mara kwa mara ya ubora huu moyo ufunguliwe kama mto unaotiririka na usiruhusiwe kufunga. Kwa kutenda na kujizoeza, ukarimu hupanua na kuimarisha, mpaka inakuwa kanuni nakutawala ndani ya nafsi. Ni hatari sana kwa roho kuruhusu ubinafsi, tamaa na uchoyo vipate nafasi hata ndogo moyoni. {3T 548.3}

Neno la Mungu lina mengi ya kusema juu ya kutoa dhabihu. Utajiri unatoka kwa Bwana na ni Wake. "Utajiri na heshima hutoka kwako." "Fedha ni Yangu, na dhahabu ni Yangu, asema Bwana wa majeshi." "Kwa maana kila mnyama wa msitu ni Wangu, na wanyama juu ya milima elfu." "Dunia na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana; Ulimwengu na wote wakaao ndani Yake." Ni Bwana Mungu wako anayekupa uwezo wa kupata utajiri. {3T 549.1}

Utajiri wenyewe ni wa muda mfupi, hupita tu na hautoshelezi. Tunaonywa tusitegemee utajiri usio na uhakika. "Maana bila shaka mali hujifanyia mabawa,

kama tai arukaye angani" "Msijiwekee hazina duniani, ambapo nondo na kutu huharibu, na ambapo wezi huvunja na kuiba." {3T 549.2}

Utajiri hauleti unafuu katika dhiki kuu ya mwanadamu. "Utajiri haufaidii kitu siku ya ghadhabu." "Fedha zao wala dhahabu zao hazitaweza kuwaokoa katika siku ya ghadhabu ya Bwana." Kwasababu kuna ghadhabu ya Bwana, "Basi ujitunze, isije hasira ikakuvuta hata ukafanya mzaha; Wala usikubali ukuu wa ukombozi ukugeuze." Onyo hili, ndugu yangu, linakufaa. {3T 549.3}

Ndugu P, umewekeza nini kwa ajili ya uzima wa milele? Je! Unao msingi mzuri dhidi ya wakati ujao, ambao utajihakikishia furaha ya milele? Hebu Mungu na akuamshe! Hebu ndugu yangu mpendwa, sasa, sasa hivi, anza kufanya kazi kwa bidii ili kupata faida na utajiri wako katika hazina ya Mungu. Hakuna hata senti yoyote iliyo yako. Yote ni ya Mungu, na umedai kuwa ni ya kwako mwenyewe yale ambayo Mungu amekukopesha wewe kujitolea kwa matendo mema. Wakati wako ni mfupi sana. Fanya kazi kwa nguvu zako zote. Kwa toba sasa unaweza kupata msamaha. Lazima ulegeze mguso wako kwa mali za kidunia na uweke upendo wako kwa Mungu na kushikilia kwa nguvu hapo. Lazima uwe mtu uliyeongoka. Huzunika na Mungu. Usiridhike kuangamia milele, bali fanya juhudi ya wokovu kabla hujachelewa milele. {3T 549.4}

Bado hujachelewa kurekebisha makosa. Onesha toba yako kwa makosa ya zamani kwa kuukomboa wakati. Pale ambapo umemkosea mtu yeyote, fanya matengenezo upya kwa kadri unavyokumbuka. Hili ndilo tumaini lako pekee la msamaha wa upendo wa Mungu. Itakuwa kama kuling'oa jicho la kulia au kukata mkono wa kulia, lakini hakuna njia nyingine kwako. Umefanya juhudi za mara kwa mara, lakini umeshindwa kwa sababu umependa pesa, ambazo zingine hazijapatikana kwa uaminifu. Hujajaribu kukomboa yaliyopita kwa kufanya marekebisho. Unapoanza kufanya hivyo, kutakuwa na tumaini kwako. Ikiwa kipindi cha siku chache zilizobaki za maisha yako unachagua kuendelea kama ulivyofanya, kesi yako haitakuwa na tumaini; utapoteza malimwengu yote mawili; utawaona watakatifu wa Mungu wakitukuzwa katika mji wa mbinguni na wewe mwenyewe ukitupwa nje; hautakuwa na sehemu katika maisha hayo ya thamani ambayo yalinunuliwa kwa ajili yako kwa gharama isiyo na kipimo, lakini ambayo uliyathamini kiasi kidogo sana hata kuyauza kwa ajili ya utajiri wa kidunia. {3T 549.5}

Sasa umebaki na muda mchache. Je, Utafanya kazi? Je! Utatubu? Au utakufa bila kujiandaa, ukiabudu pesa, ukijisifu kwa utajiri wako, na ukimsahau Mungu na mbingu? Hakuna mapambano dhaifu au juhudi dhaifu zitakazokomesha mapenzi yako kutoka kwa ulimwengu. Yesu atakusaidia wewe. Katika kila juhudi ya dhati unayofanya, atakuwa karibu nawe na atabariki juhudi zako. Lazima ujitahidi kwa dhati na bidii la sivyo utapotea. Ninakuonya usikawie hata kidogo, bali anza sasa hivi. Kwa muda mrefu umelidhalilisha jina la Kikristo kwa tamaa yako na shughuli

ndogo ndogo zenye tamaa ya pesa. Sasa unaweza kuiheshimu kwa kufanya kazi katika mwelekeo tofauti na kwa kuwaacha wote waone kwamba kuna nguvu katika Ukweli wa Mungu iwezayo kubadilisha asili ya mwanadamu. Kwa nguvu ya Mungu, unaweza kuiokoa nafsi yako ikiwa utataka. {3T 550.1}

Unayo kazi ya kufanya ambayo unapaswa kuianza mara moja. Shetani atasimama kando yako, kama vile alivyofanya kwa upande wa Kristo katika jangwa la majaribu, kukushinda kwa hoja, kupotosha hukumu yako, na kudhoofisha maoni yako ya haki na usawa. Ukitenda haki katika tukio moja, haupaswi kungojea Shetani azidi kushinda msukumo wako mzuri kwa hoja yake. Kwa muda mrefu umedhibitiwa na ubinafsi, tamaa na uchoyo kiasi kwamba huwezi kujiamini. Sitaki wewe upoteze mbingu. Nimeoneshwa matendo ya ubinafsi ya maisha yako, mipango na fikra zako, biashara zako na faida ambayo umechukua kutoka kwa ndugu zako na washiriki wenzako. Mungu ameandika kila tukio katika kitabu. Je! wewe Utamwomba Mungu ili aiangazie akili yako kusudi uone ni wapi umedhulumu au kupunja, halafu utatubu na kukomboa yaliyopita? {3T 550.2}

Ndugu P, Mungu akusaidie kabla hujachelewa. {3T 551.1}

SURA YA 49

UCHAPAJI KAZI, TASNIA KATIKA HUDUMA

Nimeoneshwa kuwa kuna hatari ya vijana wetu wahudumu kuingia shambani na kushiriki katika kazi ya kufundisha Ukweli kwa wengine wakati hawajafaa au kupata stahiki kwa kazi takatifu ya Mungu. Hawana hisia ya utakatifu wa kazi kwa wakati huu. Wanahisi hamu ya kuunganishwa na kazi hiyo, lakini wanashindwa kubeba mizigo iliyolala moja kwa moja kwenye njia yao ya wajibu. Wanafanya yale ambayo huwagharimu kwa nguvu kidogo na kujitaabisha kidogo, na wanapuuzia kuweka roho zao zote kazini. {3T 551.2}

Wengine ni wavivu sana kuweza kufanikiwa katika maisha katika masuala ya biashara na hawana uzoefu unaohitajika kuwafanya Wakristo wazuri katika hali ya kibinafsi; lakini wanajiona wana uwezo wa kushiriki katika kazi ambayo ni ngumu zaidi ya zingine zote, ile ya kushughulika na akili na kujaribu kubadilisha roho kutoka kwenye makosa na kwenda kwenda Ukweli. Mioyo ya baadhi ya wahudumu hawa haijatakaswa na Ukweli. Wote hawa ni kikwazo tu kwa wenye dhambi na wamesimama katika njia ya watendakazi wa Kweli. Itachukua kazi ngumu zaidi kuwaelimisha katika maoni sahihi, ili wasiijeruhi kazi ya Mungu, kuliko kuiacha kazi hiyo. Mungu hawezi kutukuzwa au kusudi Lake likaendelezwa na wafanyakazi wasiojitolea ambao hawana kabisa sifa zinazohitajika kuwafanya kuwa wahudumu wa injili, yaani wachungaji. Wahudumu wengine wachanga ambao huenda kufanya kazi kwa wengine wanahitaji wao wenyewe kugeuzwa kabisa kuwa na dini ya Kweli ya Biblia. {3T 551.3}

Nilioneshwa kesi ya Ndugu R wa -----, ambayo kwa njia nyingi inawakilisha kesi za wengine. Nilioneshwa kuwa Ndugu R hana faida ya kweli katika kazi ya Mungu na kamwe hawezi kuwa isipokuwa ana uongofu kamili. Ana kasoro nyingi katika tabia yake ambayo lazima azione kabla ya kukubaliwa na Mungu kama mfanyakazi katika shamba Lake la mizabibu. Kazi ya Mungu ni takatifu. Kwanza kabisa, Ndugu R hajawahi kukutana na mabadiliko hayo ya moyo ambayo humbadilisha mtu huyo

na kuitwa muongofu. Ana dini ya kichwani, lakini anahitaji kazi ya neema ya Mungu juu ya moyo ifanyike maishani kabla ya kuwaongoza wengine kwa usahihi kwa Mwana-Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu. Kazi ya wakati huu ni nzito sana na ni muhimu, kushughulikiwa na mikono na mioyo michafu. {3T 552.1}

Ndugu R ana hulka isiyo nzuri sana ya kutokuwa na furaha. Hii humletea shida yeye na marafiki zake wa karibu. Kwa asili ni mwenye wivu, mtu anayeshuku wengine, na anayetafuta makosa. Wale ambao wameunganishwa naye kwa karibu watalihisi hili kwa undani zaidi. Anajipenda sana na anajithamini kuliko wengine, na ikiwa hatambuliwi na kuthaminiwa anahisi kana kwamba kuna mtu anastahili kulaumiwa. Kosa lipo ndani yake mwenyewe. Anapenda ubatili wake usifiwe kwa madanganyo. Yeye anashuku nia ya wengine na katika hisia hizi anaonesha akili finyu sana, ya ubinafsi. Anafikiria kuwa anaona mengi ya kuuliza, kutafuta makosa, na kukemea katika mpango wa kazi za wengine, wakati uovu halisi upo ndani ya moyo wake mwenyewe usio na unyenyekevu, usiotakaswa. Nafsi/umimi, ndani yake, lazima ife, na lazima ajifunze kwa Yesu, ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, la sivyo atashindwa kukamilisha tabia ya Kikristo na kuikosa mbingu hatimaye. {3T 552.2}

Ndugu R ameshindwa katika njia yake ya kutafuta kufundisha Ukweli kwa wengine. Roho yake haiongoi. Ubinafsi umechanganywa na juhudi zake zote. Yeye yuko makini katika mambo ya mwonekano wa nje, kwa kadiri mavazi yake yanavyohusika, kana kwamba hili lingemteua kama mchungaji/mhudumu wa Kristo; lakini amepuuza mapambo ya ndani ya roho. Hajahisi ulazima wa kutafuta tabia nzuri, yenye ulinganifu, inayofanana na tabia ya Kristo, Mfano sahihi. Upole na unyenyekevu ambao ulionesha maisha ya Yesu yangeshinda mioyo na kumpa ufikiaji wa roho; lakini wakati ndugu R anaponena kutokana na roho yake mwenyewe, watu wanaona maonesho mengi ya umimi, na roho ndogo sana ya unyenyekevu, na hata mioyo yao haiguswi, bali inakua migumu na baridi kwa mahubiri yake, kwa sababu hayana mwaliko wa Kiungu/mbingu. {3T 552.3}

Roho ya kujiamini, iliyojiinua ya ndugu R lazima iwekwe mbali, na lazima ajione kwamba yeye ni mwenye dhambi na anahitaji neema na nguvu ya Mungu kila wakati ili kupitiliza giza la maadili la kizazi hiki kilichoharibika na kufikia roho ambazo zinahitaji kuokolewa. Kwa nje amevaa vazi la mchungaji/mhudumu wa injili, wakati hajahisi kwamba uzoefu halisi katika siri na fumbo la utauwa na ujuzi wa mapenzi ya Mungu vilikuwa muhimu ili kufanikisha uwasilishaji wa Ukweli. {3T 553.1}

Ndugu R ni mtu baridi sana na hana huruma. Hafikii mioyo ya watu moja kwa moja kwa unyenyekevu wa Kikristo, usahili. upole, na upendo ambao ulioneshwa katika maisha ya Kristo. Kwa hali hii ni muhimu kwamba kila mtu anayefanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho aige kielelezo alichopewa katika maisha ya Kristo. Ikiwa

watu watashindwa kujielimisha kuwa wafanyakazi katika shamba la mizabibu la Bwana, ingekuwa bora kama wangeachwa tu, wahurumiwe, na watoke shambani mwa Bwana. Itakuwa sera mbaya kutoa rasilimali kutoka katika hazi ya ya Mungu wale ambao kwa hakika wanaharibu sana kazi ya Mungu na kudhoofisha kazi Yake, na ambao kila wakati wanashusha kiwango cha Ukristo. {3T 553.2}

Ili mtu awe mtendakazi mwenye mafanikio, kuna kitu muhimu zaidi ya ujuzi wa elimu ya vitabuni. Mfanyakazi wa roho anahitaji uadilifu, akili, uchapaji kazi na ustadi, nguvu, na busara. Sifa zote hizi ni muhimu sana kwa mafanikio ya mhudumu wa Kristo. Hakuna mtu aliye na sifa hizi anayeweza kuwa duni, bali atakuwa na ushawishi wenye kuamuru. Ikiwa mfanyakazi katika kusudi la Mungu hawezi kupata ujasiri/imani ya wale anaowafanyia kazi yaani kuwahudumia, basi anaweza kufanya kazi yenye mchango mdogo tu. Mfanyakazi katika shamba la Bwana lazima kila siku apate nguvu kutoka juu ili kupinga maovu na kudumisha unyofu kupitia majaribu anuwai ya maisha, na pia roho yake lazima iwe na mapatano kamili na Mkombozi wake. Anaweza kuwa mtendakazi mwenza na Yesu, akifanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi, akipenda kama Yeye alivyopenda, na akimiliki nguvu za maadili ili kustahimili na kushinda majaribu ya nguvu ya tabia kama Yeye. {3T 553.3}

.

Ndugu R anapaswa kukuza unyenyekevu. Anapaswa kuweka kando hadhi yake ya bandia na kumruhusu Roho wa Mungu aingie na kutakasa, kuinua, kuboresha, kusafisha, na kuadilisha maisha yake. Kisha anaweza kubeba mzigo kwa ajili ya roho ambao mhudumu wa Kweli wa injili anapaswa kuuhisi wakati akiwasilisha ujumbe wa onyo kali kwa wale walio hatarini, ambao lazima waangamie katika giza lao ikiwa hawataukubali nuru ya Ukweli. Heshima hii aliyoazimwa kutoka kwa Mkombozi wake itapambwa na neema ya Bwana, kwani kupitia hiyo yeye huletwa katika umoja wa karibu na Yesu Kristo. {3T 554.1}

Nilichukuliwa mbele katika maisha ya ndugu R, na kisha nikarudishwa nyuma ili kukagua/kutathmini matokeo ya kazi yake wakati alipokuwa akijaribu kuwafundisha wengine Ukweli. Niliona kwamba kuna wachache ambao wangesikiliza, na kadiri ambavyo maneno ya kichwani yangeendelea kutolewa, wangeweza kushawishika; lakini Ndugu R hana ujuzi yakinifu (wenye matendo), ujuzi binafsi wa kila siku, ulio hai wa neema ya Mungu na nguvu Yake inayookoa, na hawezi kufikisha au kuwapa wengine kile ambacho yeye mwenyewe hana. Hana uzoefu wa mtu aliyeongoka Kweli. Je! Mungu anawezaje kumfanya kuwa baraka kwa wenye dhambi? Yeye mwenyewe ni kipofu, wakati anajaribu kuwaongoza vipofu wengine. {3T 554.2}

Nilioneshwa kuwa kazi yake imeharibu eneo zuri kwaajili ya wengine. Baadhi ya watu ambao walikuwa wamejiweka wakfu kwa Mungu na ambao walihisi mzigo wa kazi hiyo wangefanya vizuri na kuleta roho kwenye Ukweli mahali ambapo alijaribu kufanya kazi bila mafanikio, lakini baada ya kazi yake ya juu juu nafasi ya dhahabu ilikuwa imepotea. Akili ambazo zingeweza kusadikishwa, na mioyo ambayo ingekuwa imelainishwa, imekuwa ngumu na yenye chuki na ubaguzi mbaya, kwa sababu ya jitihada zake. {3T 554.3}

.

Niliangalia kuona ni roho gani za thamani zilizokuwa zimeshikilia Ukweli kama matokeo ya kazi yake. Nilifuatilia kwa karibu kuona ni huduma gani ya kulinda roho na kujali aliyokuwa nayo kwa ajili ya roho, ili kuziimarisha na kuzitia moyo, kazi ambayo daima inapaswa kuambatana na huduma ya Neno. Sikuweza kumwona hata mtu mmoja ambaye asingekuwa katika hali bora zaidi kama asingepokea maoni ya kwanza ya Ukweli kutoka kwake. Haiwezekani kwa mkondo wa maji kupanda juu kuliko chanzo chake cha chemchemi. Mtu anayebeba na kupeleka Ukweli kwa wenye dhambi anasimama katika nafasi ya uwajibikaji wa kutisha. Aidha ataziongoa roho kwa Kristo au juhudi zake zitawasukuma katika mwelekeo usio sahihi. {3T 554.4}

Nimeoneshwa kuwa ndugu R ni mtu mvivu. Anapenda raha, maisha rahisi na starehe yake. Hapendi kazi za mwili, wala hapendi matumizi makubwa ya akili kwa ajili ya kusoma Neno. Anapenda kuchukulia mambo kwa uvivu. Huenda mahali na kujaribu kuanzisha Ukweli hapo, wakati moyo wake haumo ndani yake. Hahisi uzito wa kazi, hakuna mzigo wa Kweli kwa ajili ya roho moyoni mwake. Hana upendo wa roho moyoni. Anaacha mwelekeo wake umwondoe kazini, anaruhusu hisia zake zimdhibiti, na huacha kazi na kurudi kwa familia yake. Hana uzoefu wa kujikana, kwa kutoa dhabihu raha yake na mwelekeo wake. Yeye hufanya kazi sana kwaajili ya kupata heshima na mshahara. Hatumiki kwa ukaribu katika kazi yake, bali huigusa tu hapa na pale bila uvumilivu wala bidii, na kwa hivyo hafanikiwi kwa chochote. Mungu huwakasirikia watendakazi wote wa aina hiyo, wanaojiita watendakazi wa majina tu. Siyo watu wa kuaminika katika kila kitu. Dhamiri zao si nyeti na nyororo/mwanana. {3T 555.1}

Kuutambulisha Ukweli katika maeneo na kisha kukosa ujasiri, nguvu, na busara ya kuendeleza misheni hiyo kosa kubwa, kwani kazi imebaki bila juhudi kamili na ya kudumu inayofanywa ambayo ni muhimu sana katika maeneo haya. Ikiwa mambo yatakuwa magumu, upinzani ukijitokeza, hufanya mtu arudi nyuma kwa woga badala ya kukimbilia kwa Mungu kwa kufunga na kuomba na kulia, na kwa imani kushikamana na Chanzo cha nuru, uwezo na nguvu mpaka mawingu yatoke na giza litawanyike. Imani hukua na inaimarika kwa kuletwa katika mgongano na mashaka

na ushawishi wa upinzani. Uzoefu uliopatikana katika majaribu haya ni wa thamani zaidi kuliko vito vya gharama kubwa zaidi. {3T 555.2}

Matokeo ya kazi yako, Ndugu R, yanapaswa kukufanya uone aibu. Mungu hawezi kuyakubali. Ingekuwa bora endapo ungeiacha kazi ya Mungu ya kuhubiri, na kuchukua kazi ambayo inahusisha uwajibikaji mdogo au majukumu machache. Ingekuwa bora kwako kwenda kufanya kazi kwa mikono yako. Nyenyekeza moyo wako mbele za Mungu; kuwa mwaminifu katika mambo ya muda mfupi; na unapoonesha kuwa wewe ni mwaminifu katika majukumu madogo, Mungu anaweza kukukabidhi amana za juu. "Yeye aliye mwaminifu katika lililo dogo zaidi atakuwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na yeye aliye dhalimu katika lililo dogo atakuwa dhalimu katika lililo kubwa pia." Unahitaji uzoefu zaidi katika mambo ya kidini. Ninakushauri uende kufanya kazi kwa mikono yako na umsihi sana Mungu kwa ajili ya uzoefu wako. Shikamana na Yesu na kamwe, usithubutu kuchukua majukumu ya mhudumu wa injili au uchungaji, mpaka uwe mtu uliyeongoka na uwe na roho ya upole na yenye amani. Unahitaji kukaa mbali na kazi ya Mungu mpaka upewe nguvu kutoka juu. Hakuna mtu anayeweza kufanikiwa kuokoa roho isipokuwa Kristo anafanya kazi na juhudi zake na ubinafsi havionekani. {3T 555.3}

Mhudumu wa Kristo anapaswa kuwa ameandaliwa kikamilifu kwa kazi zote njema Umefanya kosa, Umeshindwa/umefeli vibaya sana. Lazima uoneshe katika familia yako umakini mzuri, kujali, fadhili, uungwana, upole, upendo, utaratibu huruma, uvumilivu bora, na adabu ya Kweli, hivyo ndivyo inavyopaswa kwa kichwa cha familia, kabla hujaweza kufanikiwa kuongoa roho kwa Kristo. Ikiwa huna busara ya kuratibu au kusimamia kundi dogo za watu ambao umeunganishwa nao kwa karibu, unawezaje basi kufanikiwa kusimamia kundi kubwa, ambalo halivutiwi nawe? Mke wako anahitaji kuongoka kikamilifu na kiukweli kwa Mungu. Hakuna yeyote kati yenu aliye katika hali ya kuwakilisha imani yetu kwa usahihi. Wote wawili mnahitaji uongofu kamili. {3T 556.1}

Kustaafu kutoka kwenye kazi ya Mungu kwa sasa ni bora kwako. Ndugu R, hauna uvumilivu wala uti wa mgongo wa maadili. Umepungukiwa sana na tabia hizo ambazo ni muhimu kwa kazi ya Mungu kwa wakati huu. Hujapata elimu hiyo katika maisha ya vitendo ambayo ni muhimu kwako ili kufanikiwa kama mhudumu wa Kristo wa vitendo. Elimu yako imekuwa na upungufu katika mambo mengi. Wazazi wako hawajaitambua tabia yako, wala kukufundisha kushinda kasoro zake, hadi upate kukuza tabia iliyokamilika na yenye uwiano ili uwe na uthabiti, mwenye kujikana nafsi, kujikana nafsi, kujinyima, kujizuia, kujidhibiti, mnyenyekevu, na mwenye nguvu ya maadili. Unajua kidogo sana kuhusu maisha ya vitendo au uvumilivu katika shida na magumu. Una hamu kubwa ya kupinga maoni ya wengine na kusukuma mbele maoni yako mwenyewe. Haya ni matokeo ya hisia zako za

kujiona unajitosheleza na kufuata mwelekeo wako mwenyewe katika ujana. {3T 556.2}

Hujioni wewe mwenyewe na makosa yako. Hauko tayari kuwa mwanafunzi, bali una shauku kubwa ya kufundisha. Unaunda maoni yako mwenyewe kisha unang'ang'ania na maoni yako ya kipekee na msisitizo unaochosha. Una hamu ya kubeba hoja zako kwamba zikubalike, na machoni pako maoni yako ni ya muhimu zaidi kuliko uamuzi wenye uzoefu wa watu wenye thamani ya maadili ambao wamethibitishwa kwa kazi hii. Umedanganywa na wazo kwamba una uwezo ambao utathaminiwa na kukufanya uwe mtu wa thamani; lakini sifa hizi hazijapimwa, hazijajaribiwa na kuthibitishwa. Una elimu ya upande mmoja. Huna mwelekeo au upendo kwa majukumu ya nyumbani, ya kila siku katika maisha. Uvivu wako ungetosha kukuondoa katika kazi ya uchungaji, yaani huduma ya kiroho kama kungekuwa hakuna sababu zingine kwanini usiweze kushiriki. Kazi hii haihitaji wahubiri kama inavyowahitaji watendakazi. Kati ya kazi zote za maisha, hakuna kazi inayohitaji watendakazi wenye bidii, waaminifu, wavumilivu, wenye kujitolea kama kazi ya Mungu katika siku hizi za mwisho. {3T 557.1}

Mkakati au mradi wa kupata uzima wa milele iko juu ya kila jambo lingine. Mungu hataki wavivu katika kusudi Lake. Kazi ya kuwaonya wenye dhambi kukimbia hasira inayokuja, inahitaji watu wenye bidii ambao wanahisi mzigo wa roho na ambao hawatakuwa tayari kutafuta visingizio vya kuepuka majukumu ya mizigo au kuacha kazi hiyo. Kukatishwa tamaa kidogo, kama hali ya hewa isiyofaa au udhaifu wa kufikirika, inaonekana kuwa yatosha kwa Ndugu R kumtetea au kumpa kisingizio, asifanye bidii. Atajifariji hata kwa huruma zake, kwa kujihurumia mwenyewe; na majukumu yanapoibuka ambayo hajisikii nia ya kutekeleza, wakati uzembe wake ukipiga mayowe kwa za kujifurahisha, mara nyingi hutoa kisingizio kwamba ni mgonjwa, wakati hakuna sababu ya kwanini anapaswa kuwa mgonjwa, isipokuwa kupitia tabia yake ya uvivu na kuendekeza tamaa zake na uchu wa chakula, mfumo mzima umeziba kwa kukosa shuguli. Anaweza kuwa na afya njema ikiwa atazingatia kwa ukamilifu sheria za maisha na afya, na kutekeleza nuru juu ya matengenezo ya afya katika tabia zake zote.{3T 557.2}

Ndugu R siyo mtu anayefaa kwaajili ya kazi katika siku hizi za mwisho isipokuwa kama atabadilika kabisa. Mungu hahitaji wachungaji au wahudumu ambao ni wavivu kushiriki katika kazi za mwili au mikono, kubeba ujumbe unaojaribu na wa onyo kwa ulimwengu. Anahitaji watendakazi katika kusudi Lake. Watendakazi wa Kweli, wenye bidii, wenye kujinyima nafsi zao, watatimiza jambo fulani. {3T 558.1}

Ndugu R, kufundisha kwako Ukweli kwa wengine limekuwa kosa kabisa. Ikiwa Mungu atamwita mtu, hatafanya kosa kubwa hata kuchukua yule mwenye uzoefu mdogo sana katika maisha ya vitendo na mambo ya kiroho kama vile ulivyo navyo. Una uwezo wa kuzungumza, kwa kadiri hilo linavyohusika, lakini kazi ya Mungu inahitaji watu wenye kujitolea kikamilifu na wenye nguvu. Sifa hizi wewe unaweza kuzikuza, na kuzipalilia; unaweza kuzipata ukitaka. Kwa kuendelea kukuza tabia tofauti na zile ambazo sasa zinakuangusha, unaweza kujifunza kushinda mapungufu katika tabia yako ambayo yameongezeka tangu ujana wako. Kwenda nje tu na kuzungumza na watu hapa na pale, siyo kufanya kazi kwaajili ya Mungu. Hakuna kazi ya kweli ndani yake. {3T 558.2}

Wale ambao hufanya kazi ya Mungu ndiyo wameanza tu kazi wakati ambao wametoa hotuba wakiwa kwenye mimbari. Baada ya hili inakuja kazi halisi ya uinjilisti, kutembelea nyumba kwa nyumba, kuzungumza na watu wa familia, kuomba nao, na kusogea karibu kwa huruma ya dhati kwa wale ambao tunatamani wafaidike. Halitaondoa hadhi ya mchungaji/mhudumu wa Kristo kuwa macho ili kuona na kutambua mizigo ya muda na huduma za familia anazotembelea, na kuwa msaada kwao, akitafuta kupunguza mizigo kadri awezavyo kwa kusaidia kazi za mikono. Kwa njia hii anaweza kuwa na nguvu ya ushawishi wa kunyang'anya silaha za upinzani na kuvunja chuki au dhana potofu, jambo ambalo angeshindwa kulifanikisha hata ikiwa angekuwa hodari kwa kila jambo lingine kama mhudumu hodari wa Kristo. {3T 558.3}

Wachungaji wetu wachanga hawana mzigo wa kuandika ambao wazee na wenye uzoefu zaidi wanao. Hawana msururu wa majukumu ambayo huchosha akili na kudhoofisha nguvu za mtu. Lakini ni mizigo hii ya masumbufu ndiyo ambayo uzoefu kamili wa Kikristo, hutoa nguvu ya maadili, na kuwakamilisha kwa kuwa watu wenye nguvu, wenye ufanisi, wale wote wanaohusika katika kazi ya Mungu. Kuepuka mizigo na majukumu yasiyokubalika hakutawafanya wahudumu wetu kuwa watu wenye imara na nguvu, ambao wanaweza kutegemewa wakati wa mgogoro na zahama za kidini. Wengi wa wachungaji na wahudumu wetu wachanga ni dhaifu kama watoto wachanga katika kazi ya Mungu. Na wengine ambao wamekuwa wakishiriki katika kazi ya kufundisha Ukweli kwa miaka bado hawajawa watendakazi stadi, ambao wasiohitaji kujipatia aibu. Hawajaimarika kupitia uzoefu wa kuitwa nje na ushawishi pinzani. Wamejiondolea zoezi hilo ambalo lingeimarisha misuli ya maadili, likitoa nguvu za kiroho. Lakini huu ndio uzoefu wanaouhitaji ili kufikia kimo kamili cha wanadamu katika Kristo Yesu. Hawana nguvu ya kiroho kwa kukwepa majukumu na wajibu, na kujitoa kwa ajili ya uvivu/uzembe na kupenda starehe, na raha kwa ubinafsi. {3T 558.4}

Ndugu R hana upungufu wa uwezo wa kuyavika maneno mawazo yake, bali anakosa hali ya kiroho na utakatifu wa Kweli wa moyo. Hajanywa kabisa kutoka kwenye chemchemi ya Ukweli. Ikiwa angeboresha muda wake wa thamani au dhahabu katika kujifunza juu ya kazi ya Mungu labda sasa angekuwa mfanyakazi stadi, mwenye uwezo, lakini yeye ni mvivu sana kuweza kutumia akili na kujifunza kwa ajili yake mwenyewe sababu za tumaini letu. Anaridhika kuchukua vitu ambavyo

akili zingine na kalamu zingine zimejitahidi kutayarisha na kutoa, na kutumia mawazo yao, ambayo yameandaliwa tayari na kuweka mikono mwake, bila jitihada au bidii ya akili yake yeye mwenyewe, mawazo makini, au kutafakari kwa sala yeye mwenyewe binafsi. {3T 559.1}

Ndugu R hapendi kujituma kwa dhati, iwe katika kujifunza Maandiko au kazi za mikono. Anapendelea njia rahisi, na bado hajajua chochote kuhusu majaribu ya mzigo wa kazi ya Mungu. Ni rahisi kwake kurudia mawazo ya wengine kuliko kutafuta Ukweli kwa bidii yake mwenyewe. Ni kwa njia ya juhudi ibinafsi tu, kutumia akili kwa umakini, na kujitoa nafsi kikamilifu kwa kazi ndipo watu wanakuwa na sifa, stahiki na uwezo kwa ajili ya huduma. {3T 559.2}

*****

Kristo anasema: "Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini ikiwa chumvi imepoteza ladha yake, itatiwa nini hata ikolee?" Harufu/ladha ya chumvi ni neema ya Bwana. Jitihada zote zinazofanywa kuendeleza Ukweli zina thamani ndogo isipokuwa tu kama Roho wa Mungu ataambatana nazo. Umefanya kazi ya kufundisha Ukweli iwe tu kama mchezo wa watoto. Akili yako imekuwa kwenye starehe naraha yako mwenyewe, kufuatia matakwa na mwelekeo wako tu. Wewe na mkeo hamna ufahamu halisi wa utakatifu wa kazi ya Mungu. Ninyi wawili mnajali zaidi jinsi ya kupendeza matamanio yenu na kujifunza ili kutosheleza hamu yenu ya raha na starehe kuliko kushiriki katika majukumu mazito n amagumu ya maisha, hasa majukumu yanayohusiana na kazi ya kuuonya ulimwengu juu ya hukumu ijayo. {3T 559.3}

Umemuona ndugu S akiwa amelemewa na mizigo na amechoshwa na kazi za kimwili/mikono; lakini umekuwa na upendo mkubwa sana kwa raha zako na starehe na hamu ya kudumisha umuhimu wako binafsi, na kujiwekea ubaridi na udhuru wa kushiriki katika majukumu ambayo mtu mwingine alilazimika kuyatekeleza. Umepoteza siku nyingi kwa uvivu bila kumnufaisha mtu yeyote, na kisha dhamiri yako ikakuruhusu bila hata kusikia hatia au majuto, kuhusu muda uliotumiwa katika uvivu na kupokea malipo kutoka katika hazina ya Mungu. {3T 560.1}

Umeonesha kwa hatua yako kwamba haukuwa na staha na uelewa wa juu wa mambo matakatifu. Umemwibia Mungu, na sasa unapaswa kutafuta kufanya kazi kamili ya toba. Wala usijaribu kuwafundisha wengine. Unapoongoka, ndipo unaweza kuwaimarisha ndugu zako; lakini Mungu hapati manufaa kwa watu wa aina ya tabia zako katika shamba Lake la mizabibu. Unapoondoa tabia hii, na

kubeba mvuto wa Kiungu/mbingu, basi unaweza kufanya kazi katika kusudi la Mungu. Una karibu kila kitu cha kujifunza, lakini ni kwa muda mfupi ambao unaweza kujifunza masomo haya. Acha Mungu akusaidie kufanya kazi kwa bidii na kwa uhakika katika kila pointi. Nimeandika mengi zaidi juu ya kanuni za jumla, lakini kwa sasa sijapata wasaa wa kukupatia. {3T 560.2}

SURA YA 50

WAZAZI KAMA WANAMATENGENEZO

Januari 3, 1875, nilioneshwa kwamba hakuna hata mmoja wetu anayejua hatari ambazo hututembelea kila hatua. Tuna adui aliye macho, na bado wala hatujaamka kwa dhati, na kwa bidii katika juhudi zetu za kupinga vishawishi vya Shetani na kushinda hila zake. {3T 560.3}

Mungu ameruhusu nuru ya matengenezo ya afya ituangazie katika siku hizi za mwisho, ili kwa kutembea katika nuru, na hivyo tuepuke hatari nyingi tutakazokutana nazo. Vishawishi vya Shetani vina nguvu juu ya familia ya kibinadamu kuwaongoza kutosheleza uchu, kuridhisha mwelekeo, na kuishi maisha ya upumbavu wa kutotii. Adui anawasilisha vivutio katika maisha vya raha ya kibinafsi, na katika kutafuta kuridhisha silika ya mwili. Ulevi na uasherati unatawala kwa kiwango cha kutisha na unaharibu nguvu za maisha; na siyo hizi tu, bali pia nguvu za maadili zinatolewa kafara. Kujiendekeza kwa kutokuwa na kiasi hupunguza nguvu muhimu za mwili na akili. Humweka mtu aliyeshindwa kwenye ule uwanja wa adui, ambapo Shetani anaweza kumjaribu, kumkasirisha, na mwishowe kudhibiti mapenzi yake kwa urahisi. {3T 561.1}

Wale ambao wameshindwa katika suala la hamu/uraibu na wanatumia tumbaku kwa uhuru, wanapunguza nguvu zao za kiakili na kimaadili na kuwafanya watumwa wa mwili. Na hamu ya kunywa pombe inapoendekezwa, yule mtu kwa hiari huweka kwenye midomo yake maneno ambayo hufikia kiwango cha ukatili wa mnyama pori, kwa mtu aliyefanywa kwa mfano wa Mungu. Ufahamu umepooza, akili imechoka, shauku za tamaa za mwili za kinyama zinachochewa, na kisha hufuata uhalifu mbaya zaidi wa tabia. Kama watu wangekuwa na kiasi katika kila kitu, kama wasingegusa, wala kuonja, wala kushika vileo na dawa za kulevya, hekima ingeshikilia utawala wa serikali mikononi mwake na kudhibiti uchu na tamaa za kinyama (animal appetite). Katika kizazi hiki kinachoenda haraka, chakula kisichochochea tamaa/hamu ndicho bora zaidi. Kiasi katika mambo yote na kukataa kabisa uchu/tamaa zinazoleta uraibu ndiyo njia pekee ya usalama. {3T 561.2}

Shetani humjia mwanadamu, kama alivyokuja kwa Kristo, na majaribu yake yenye nguvu ya kukidhi uchu wa chakula. Adui anaijua vizuri nguvu yake ya kumshinda mwanadamu juu ya hatua hii. Aliwashinda Adamu na Hawa huko Edeni kwa uchu wa chakula, na wakapoteza makazi yao yenye furaha. Kile kilichokusanya taabu na uhalifu kimeujaza ulimwengu wetu kama matokeo ya anguko la Adamu. Miji mizima imefutwa kutoka kwenye uso wa dunia kwa sababu ya uhalifu wa kudhalilisha na uovu wa uasi ambao uliwafanya wafutwe/waondolewe ulimwenguni. Uendekezaji wa uchu wa chakula ulikuwa msingi wa dhambi zao zote. Kupitia hamu ya kula, Shetani alimdhibiti mwanadamu na akili yake. Maelfu ambao wangeweza kuishi, wameenda mapema ndani ya makaburi yao, wakiwa na uharibifu wa mwili, akili, na maadili. Walikuwa na nguvu nzuri, lakini walitoa dhabihu zote kwenye uchu -tamaa za mwili, ambao uliwaongoza kuweka hatamu kwenye shingo ya tamaa. Ulimwengu wetu ni hospitali kubwa ya wakoma. Tabia mbaya za uovu zinaongezeka. {3T 561.3}

Haipendezi, kama siyo hatari kabisa, kubaki kwenye garimoshi au kwenye chumba kilichojaa watu ambacho hakina hewa ya kutosha, mahali ambapo anga limejazwa na sifa za pombe na tumbaku. Wenyeji hutoa ushahidi kwa pumzi na mhemko kutoka mwilini kwamba mfumo umejazwa na sumu ya pombe na tumbaku. Kutumia tumbaku ni tabia ambayo huathiri mfumo wa neva mara nyingi kwa njia ya nguvu zaidi kuliko matumizi ya pombe. Inamfunga mwathirika katika vifungo vikali vya utumwa kuliko kikombe cha kileo; tabia hii ni ngumu zaidi kuishinda. Mwili na akili, mara nyingi zimelewa na kusumishwa kabisa na utumiaji wa tumbaku kuliko vileo, kwani ni sumu yenye hila zaidi. {3T 562.1}

Hali ya ukosefu wa kiasi inaongezeka kila mahali, bila kujali juhudi za dhati zilizofanywa katika mwaka uliopita [USHUHUDA HUU ULICHAPISHWA KWANZA MWAKA 1875] ili kuendelea mbele na maendeleo yake. Nilioneshwa kuwa nguvu kubwa ya kukosa kiasi haitadhibitiwa na juhudi zozote kama zile zilizofanywa. Kazi ya kujizuia lazima ianzie katika familia zetu, kwenye meza zetu. Akina mama wana kazi muhimu ya kufanya ili waweze kuupatia ulimwengu, kupitia nidhamu sahihi na elimu, watoto ambao wataweza kujaza karibu nafasi yoyote, na ambao pia wanaweza kuheshimu na kufurahia majukumu ya maisha ya nyumbani. {3T 562.2}

Kazi ya mama ni ya muhimu sana na takatifu. Anapaswa kuwafundisha watoto wake tangu utotoni wakiwa wachanga kujizoesha hali ya kujinyima, kujikana nafsi na kujidhibiti. Ikiwa muda wake unashikiliwa na watu wasio na maana katika kizazi hiki kibaya, ikiwa mavazi na sherehe zinatumia muda wake wa thamani, watoto wake watashindwa kupata elimu hiyo muhimu wanayopaswa kuwa nayo ili waweze kuunda tabia sahihi. Wasiwasi au Shauku ya mama Mkristo haipaswi kuzingatia

mambo ya nje tu, bali pia watoto wake wawe na miili yenye afya na maadili mema. {3T 562.3}

Akina mama wengi ambao wanashutumu ukosefu wa kukosa kiasi ambao upo kila mahali hawatazami kwa kina cha kutosha kuona sababu. Kutayarisha kwao kila siku sahani kadhaa na chakula kilichopikwa kupitiliza ambacho hujaribu hamu ya kula na kuhamasisha kula kupita kiasi. Meza za watu wetu wa Marekani kwa ujumla zimeandaliwa kwa namna ya kuandaa walevi wa chakula (uraibu wa chakula). Uchu wa chakula ni kanuni inayotawala kwa watu wengi. Yeyote anayeendekeza hamu ya kula mara nyingi, tena chakula kisicho na ubora, anapunguza uwezo wake wa kupinga mayowe ya uchu na shauku katika mambo mengine kwa uwiano kwani ameimarisha tabia ya kula vibaya. Akina mama wanahitaji kuvutiwa na kuguswa moyo na wajibu wao kwa Mungu na kwa ulimwengu kuipatia jamii watoto walio na tabia zilizokuzwa vizuri. Wanaume na wanawake wanaofikia hatua ya maamuzi kwa kanuni thabiti watafanywa kufaa kusimama katikati ya uchafuzi wa maadili ya kizazi hiki kibovu. Ni jukumu la akina mama kuboresha fursa zao za dhahabu/thamani kuwafundisha watoto wao kwa usahihi kwa manufaa na wajibu. Muda wao ni mali ya watoto wao kwa namna maalumu. Wakati wa thamani haupaswi kutumiwa kwa kazi isiyo ya lazima juu ya mavazi ya maonesho, bali unapaswa kutumiwa katika kuwaelekeza kwa subira na kuwafundisha watoto wao kwa uangalifu umuhimu wa kujikana nafsi na kujidhibiti nafsi. {3T 563.1}

Meza za wanawake wengi wanaojiita Wakristo kila siku zinawekwa milo ambayo huharibu tumbo na kuzalisha hali ya homa ya mfumo. Nyama zinachangia kiasi kikubwa cha chakula kwenye meza za familia nyingi, hadi damu zao inajazwa na vichocheo vya saratani, uvimbe na hata mitoki kuonekana. Miili yao inaundwa na kile wanachokula. Lakini wakati mateso na magonjwa yanapowajia, inachukuliwa kuwa ni majaliwa ya Mungu. {3T 563.2}

Tunarudia: Ukosefu wa kiasi huanzia kwenye meza zetu. Uchu huendekezwa mpaka kuwa asili ya pili. Kwa kutumia chai na kahawa hamu hutengenezwa kwa ajili ya tumbaku, na hii huhimiza hamu ya pombe. {3T 563.3}

Wazazi wengi, kwa kuepuka jukumu la kuwafundisha watoto wao tabia za kujinyima, kujikana nafsi na kuwafundisha jinsi ya kutumia vizuri baraka zote za Mungu, wanawaendekeza katika kula na kunywa wakati wowote wanaopenda. Tamaa na uchu ubinafsi, ikiwa havitazuiliwa vema, hukua na ukuaji na kuimarika kwa nguvu. Watoto hawa wanapoanza maisha yao na kuchukua nafasi zao katika jamii, huwa hawana nguvu ya kupinga majaribu. Usafi wa maadili na uovu wa kutisha umeenea kila mahali. Jaribu la kuendekeza ladha ya chakula na kuridhisha mwelekeo halijapungua kwa kadri ambapo miaka imeongezeka, na vijana kwa jumla wanatawaliwa na msukumo na ni watumwa wa uchu wa chakula. Kwa sababu

ya ulafi, mtumiaji wa tumbaku, mnywaji wa divai, na mlevi, tunaona matokeo mabaya ya elimu yenye kasoro. {3T 564.1}

Tunaposikia maombolezo ya kusikitisha ya wanaume na wanawake wa Kikristo juu ya maovu mabaya ya kutokuwa na kiasi, maswali mara moja huibuka akilini: Ni nani aliyewafundisha vijana na kuwapa muhuri wao wa tabia? Ni nani amekuza ndani yao hamu ya kula waliyoipata? Je, ni nani amepuuza jukumu zito kabisa la kuunda akili zao na tabia zao kwa faida katika maisha haya, na kwa jamii ya malaika wa mbinguni katika maisha yajayo? Jamii kubwa ya wanadamu ambao kila mahali tunakutana nao ni laana hai kwa ulimwengu. Hawaishi kwa kusudi lingine isipokuwa kujifurahisha kwa hamu na shauku, na tamaa za mwili na kuharibu roho na mwili kwa tabia mbaya. Hili ni kemeo kali kwa akina mama ambao wamejitolea katika mitindo, ambao wameishi kwa mavazi na maonesho, ambao wamepuuza kupamba akili zao wenyewe na kuunda tabia zao kwa mfano wa Mungu, na ambao pia wamepuuza amana takatifu iliyowekwa kwao, kuwalea watoto wao katika malezi na maonyo ya Bwana. {3T 564.2}

Niliona kwamba Shetani, kupitia vishawishi vyake, anaanzisha mitindo inayobadilika kila wakati na tafrija za kupendeza na burudani, ili akina mama waongozwe kutumia wakati wao wa mlango wa rehema ulio wazi waliopewa na Mungu kwa mambo ya kipuuzi ili wapate nafasi ndogo tu ya kuwaelimisha na kuwafundisha vizuri watoto wao. Vijana wetu wanawahitaji akina mama ambao watawafundisha tangu utotoni mwao kudhibiti shauku, kukataa uchu, na kushinda ubinafsi. Wanahitaji mstari juu ya mstari na amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo. {3T 564.3}

Maelekezo yalitolewa kwa Waebrania jinsi ya kufundisha watoto wao ili kuepukana na ibada ya sanamu na uovu wa mataifa ya kipagani: "Kwa hiyo yawekeni Maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili/ishara juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu." {3T 565.1}

Tunayo shauku ya dhati kwamba mwanamke atajaza nafasi ambayo Mungu aliikusudia mwanzoni, kama ilivyo sawa kwa mumewe. Tunahitaji sana akina mama ambao ni mama siyo kwa jina tu, bali kwa kila maana ambayo neno hilo linamaanisha. Tunaweza kusema kwa usalama kwamba hadhi na umuhimu wa utume wa mwanamke na majukumu tofauti ni ya tabia takatifu kuliko majukumu ya mwanamume. {3T 565.2}

Kuna dhana kuhusu haki na wajibu wa mwanamke kuhusu upigaji kura. Wengi hawana nidhamu yoyote kuelewa uelewa wa maswali muhimu. Wameishi maisha ya kujiridhisha kwa sasa kwa sababu ilikuwa mtindo. Wanawake ambao wanaweza kukuza akili nzuri na kuwa na maadili ya Kweli sasa ni watumwa tu wa mitindo.

Hawana upana wa fikira wala akili iliyokuzwa. Wanaweza kuzungumza kwa uelewa juu ya mitindo ya hivi karibuni, mitindo ya mavazi, sherehe hii au ile au michezo ya kupendeza. Wanawake kama hao hawako tayari kuchukua nafasi nzuri katika masuala ya kisiasa. Wao ni viumbe tu wa mitindo na matukio. Hebu utaratibu huu wa mambo ubadilishwe. Hebu mwanamke atambue utakatifu wa kazi yake na kwa nguvu na hofu ya Mungu, abebe utume wake wa maisha. Hebu awaelimishe watoto wake kwa manufaa katika ulimwengu huu na kwa ajili ya kupata stahiki na kufaa kwa ulimwengu bora. {3T 565.3}

Tunawahutubia akina mama Wakristo. Tunasihi kwamba mhisi jukumu lenu kama akina mama na kwamba hamuishi ili kujipendeza wenyewe, bali kwa ajili ya kumtukuza Mungu. Kristo hakujipendeza Yeye Mwenyewe, bali alichukua mfano wa mtumwa. Yeye Aliacha nyua za kifalme na kujidhalilisha/kujishusha ili kuuvisha ubinadamu Uungu Wake, ili kusudi kwa kujishusha Kwake na mfano Wake wa kujitolea mwenyewe atufundishe jinsi tunavyoweza kuinuliwa hadi kwenye nafasi ya wana na binti wa familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni. Lakini yapi ni masharti ya baraka hizi takatifu, zilizoinuliwa? "Tokeni kati yao, mkatengwe, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami nitawakaribisha, Nami nitakuwa Baba yenu, nanyi mtakuwa wana Wangu na binti Zangu, asema Bwana Mwenyezi." {3T 565.4}

Kristo alijishusha kutoka kwenye mamlaka ya juu kabisa, kutoka kwa mtu aliye sawa na Mungu, hadi mahali pa chini kabisa, pa mtumwa. Nyumba Yake ilikuwa Nazareti, mji uliokuwa umekithiri kwa uovu wake. Wazazi Wake walikuwa miongoni mwa maskini wa hali ya chini. Kazi yake ilikuwa ya useremala, na alifanya kazi kwa mikono yake ili kufanya sehemu Yake katika kudumisha familia. Kwa miaka thelathini alikuwa chini ya wazazi wake. Hapa maisha ya Kristo yanatuelekeza kwenye jukumu letu, kuwa na bidii na uadilifu katika kazi na kuwasaidia na kuwafunza wanyonge na wajinga. Katika masomo Yake ya kuwaelekeza wanafunzi Wake, Yesu aliwafundisha kwamba ufalme Wake haukuwa ufalme wa ulimwengu, ambao wote walikuwa wakipambana kwa ajili ya nafasi ya juu. {3T 566.1}

Mwanamke anapaswa kujaza nafasi takatifu zaidi na iliyoinuliwa katika familia kuliko hata mfalme kwenye kiti chake cha enzi. Kazi yake kubwa ni kufanya maisha yake kuwa mfano hai ambao angependa watoto wake wauige. Kwa amri na mfano, anapaswa kuhifadhi akili zao kwa maarifa muhimu na kuwaongoza kwenye kazi ya kujitolea kwa faida ya wengine. Kichocheo kikubwa kwa mama anayesumbuka, mwenye mzigo kinapaswa kuwa kila mtoto aliyefundishwa vizuri, na aliye na mapambo ya ndani, pambo la roho ya upole na tulivu, atafaa kwa mbingu na atang'aa katika nyua za Bwana. {3T 566.2}

Ni wachache kiasi gani wanaoona chochote kinachovutia katika unyenyekevu wa Kweli wa Kristo! Unyenyekevu Wake haukuwa na makadirio ya chini ya tabia na sifa Zake, bali katika Kunyenyekea Kwake Yeye Mwenyewe kwa ubinadamu ulioanguka ili aweze kuwainua pamoja Naye kwa ajili ya maisha ya juu. Walimwengu hujaribu kujiinua juu ya msimamo wa wale walio juu yao au kuwa bora zaidi yao. Lakini Yesu, Mwana wa Mungu, alijinyenyekeza ili kumuinua mwanadamu; na mfuasi wa Kweli wa Kristo atatafuta kukutana na watu mahali walipo ili kuwainua. {3T 566.3}

Je! Akina mama wa kizazi hiki watahisi utakatifu wa utume wao na wasijaribu kushindana na majirani zao matajiri kwa mwonekano, bali watafute kuwa bora kuliko wao katika kutekeleza kwa uaminifu kazi ya kuwafundisha watoto wao kwaajili ya maisha bora? Ikiwa watoto na vijana wangefundishwa na kuelekezwa tabia ya kujikana, Kujikana nafsi na kujidhibiti, ikiwa wangefundishwa kwamba wanakula ili waishi badala ya kuishi ili kula, kungekuwa na magonjwa kidogo na uharibifu mdogo wa maadili. Kungekuwa na ulazima mdogo wa vita ya kujizuia, ambayo ni kidogo sana, ikiwa ndani ya vijana ambao huunda jamii, kanuni sahihi kuhusu upole ingepandikizwa. Kwa hiyo wangekuwa na thamani ya maadili na uadilifu wa maadili kupinga, kwa nguvu ya Yesu, uchafuzi wa siku hizi za mwisho. {3T 567.1}
Ni jambo gumu zaidi kuondoa tabia ambazo zimeingizwa na kuendekezwa na hata kufurahiwa kwa njia ya maisha na kuhamasisha uchu. Pepo la kutokuwa na kiasi halishindwi kwa urahisi. Lina nguvu kubwa na ni vigumu kulishinda. Lakini hebu wazazi waanzishe vita dhidi ya ukosefu wa kiasi katika maeneo yao ya kukota moto wakati wa mazungumzo sebuleni, katika familia zao, kwa kanuni wanazowafundisha watoto wao kuzifuata tangu utoto wao, na wanaweza kutumaini kufanikiwa. Itawalipa ninyi akina mama kutumia masaa ya thamani ambayo mmepewa na Mungu katika kuunda, kukuza, na kufundisha tabia za watoto wenu, na kuwafundisha kuzingatia kanuni za kiasi kwa umakini katika kula na kunywa. {3T 567.2}

Wazazi wanaweza kuwa wamewaambukiza watoto wao mielekeo ya hamu ya kula na tamaa, ambayo itafanya kazi ya kuwafundisha na kuwaelekeza watoto hawa kuwa ngumu zaidi na kuwa na tabia safi na nzuri. Ikiwa hamu ya chakula kisicho na afya na vichocheo na dawa za kulevya vimepitishwa kwao kama urithi kutoka kwa wazazi wao, ni jukumu zito la kuogofya lililoko juu ya wazazi ili kuipiku/kukabiliana na mielekeo mibaya ambayo wamewapatia watoto wao! Wazazi wanapaswa kufanya bidii na juhudi kiasi gani ili kutimiza wajibu wao, kwa imani na matumaini, kwa watoto wao wasio na bahati! {3T 567.3}

Wazazi wanapaswa kuifanya kazi yao ya kwanza kuelewa sheria za maisha na afya, kwamba kusiwe na kitu watakachofanya katika kuandaa chakula, au kupitia

mazoea mengine yoyote, ambacho kitakuza tabia mbaya kwa watoto wao. Ni kwa uangalifu kiasi gani, akina mama wanapaswa kujifunza jinsi ya kuandaa meza zao na chakula rahisi na chenye afya, ili viungo vya umeng'enyaji visiweze kudhoofika, nguvu za neva hazina usawa, na maagizo ambayo wanapaswa kuwapatia watoto wao yanakabiliwa na chakula kilichowekwa mbele yao. Chakula hiki aidha hudhoofisha au huimarisha viungo vya tumbo na kinahusiana sana na kudhibiti afya ya mwili na maadili ya watoto, ambao ni mali ya Mungu iliyonunuliwa kwa damu. Ni dhamana takatifu iliyoje iliyowekwa kwa wazazi kulinda kanuni za mwili na maadili ya watoto wao ili mfumo wa neva uweze kuwa sawa na roho isiwe hatarini! Wale ambao huendekeza uchu wa watoto wao, na kushindwa kudhibiti tamaa zao, wataona kosa baya walilolifanya, kwa mtumwa anayependa tumbaku, anayekunywa pombe, ambaye akili zake zimekufa ganzi na ambaye midomo yake inanena uongo na matusi. {3T 568.1}

Wakati wazazi na watoto wanapokutana katika hesabu ya mwisho, ni tukio gani litakalooneshwa! Maelfu ya watoto ambao wamekuwa watumwa wa uchu wa chakula na tabia mbaya, ambao maisha yao yamekuwa na maadili yaliyopotoka na uharibifu kama majeruhi, watasimama uso kwa uso na wazazi ambao waliwafanya hivyo walivyo. Je, ni akina nani isipokuwa wazazi ambao wanapaswa kubeba jukumu hili la kutisha? Je! Ni Bwana aliyewafanya vijana hawa kuwa wabaya? Lo, hapana! Yeye Aliwaumba kwa mfano Wake, pungufu kidogo tu kwa malaika. Ni nani, basi, aliyefanya kazi ya kutisha ya kuunda tabia ya maisha? Ni nani aliyebadilisha tabia zao ili wasiwe na maoni ya Mungu, na lazima watenganishwe milele na uwepo Wake kama wasio safi wasio na nafasi yoyote pamoja na malaika wasafi katika mbingu takatifu? Je! Dhambi za wazazi zilipitishwa kwa watoto juu ya uchu mbaya na tamaa? Je! Kazi hiyo ilikamilishwa na mama anayependa raha kwa kupuuza kuwafundisha vizuri kulingana na mfano aliopewa? Akina mama hawa wote watapita mbele za Mungu kama vile walivyo. Shetani yuko tayari kufanya kazi yake na kuwasilisha vishawishi ambavyo hawana nia au nguvu ya maadili ya kuvipinga. {3T 568.2}

Watu wetu wanarudi nyuma kila wakati juu ya matengenezo ya afya. Shetani huona kuwa hawezi kuwa na nguvu ya udhibiti juu yao kama ambavyo angeweza ikiwa uchu wa chakula ungeendekezwa. Chini ya ushawishi wa chakula kisicho na afya dhamiri inashikwa na butwaa, ufahamu wa akili inatiwa giza, na uwezekano wake wa kuona unapungua. Lakini kwa sababu dhamiri iliyovurugwa na kunyanyaswa inafifia na kutohisi chochote, hatia ya mkosaji haipungui. {3T 569.1}

Shetani anavuruga akili na kuharibu roho kupitia majaribu yake ya hila. Je! Watu wetu wataona na kuhisi dhambi ya kuendekeza hamu mbaya au ulafi wa chakula na vileo/vichocheo? Je! Wataacha chai, kahawa, nyama, na vyakula vyote vya kusisimua, na kuwekeza mali iliyotumika kwa vitu hivi vinavyodhuru katika kueneza Ukweli? Vichocheo hivi kazi yake ni kudhuru tu, na bado tunaona kwamba

idadi kubwa ya wale wanaodai kuwa Wakristo wanatumia tumbaku. Watu hawa watashutumu uovu wa kukosa kiasi, na wakati wakisema dhidi ya matumizi ya vileo watatoa sharubati ya tumbaku kutoka kwenye midomo yao na kuitupa kama mate. Wakati hali nzuri ya akili inategemea hali ya kawaida ya nguvu muhimu, ni uangalifu gani unapaswa kutekelezwa kwamba hakuna vichocheo au dawa za kulevya zinazopaswa kutumiwa. {3T 569.2}

Tumbaku ni sumu ya taratibu, inayodhuru kwa siri, na athari zake ni ngumu kusafishwa kutoka kwenye mfumo kuliko ile ya pombe. Ni nguvu gani ambayo mwathirika wa tumbaku anaweza kuwa nayo ili kubaki katika maendeleo ya ukosefu wa kiasi? Lazima kuwe na mapinduzi katika ulimwengu wetu juu ya mada ya tumbaku kabla ya shoka kuwekwa kwenye shina la mti. Tunasogeza mada karibu zaidi. Chai na kahawa zinakuza hamu ya kula ambayo inakua kwa sababu ya vichocheo vikali, kama tumbaku na pombe. Na tunakuja karibu zaidi nyumbani, kwenye chakula cha kila siku, meza zinazotayarishwa mbele ya kaya za Kikristo. Je! Kujizuia kunatekelezwa katika vitu vyote? Je! Matengenezo ambayo ni muhimu kwa afya na furaha hufanywa huko? Kila Mkristo wa Kweli atakuwa na udhibiti wa hamu yake na tamaa. Isipokuwa tu yuko huru kutoka kwenye kifungo na utumwa wa hamu ya chakula hawezi kuwa mtumwa wa Kweli wa Kristo. Ni kwa kuendekeza hamu na tamaa ambavyo huufanya Ukweli kutokuwa na matokeo yoyote moyoni. Haiwezekani kwa roho na nguvu ya Ukweli kumtakasa mtu, nafsi, mwili, na roho, wakati anadhibitiwa na uchu wa chakula na tamaa. {3T 569.3}

SURA YA 51

"SIWEZI KUSHUKA CHINI"

"Hii ni kazi kubwa ninayoifanya mimi," anasema Nehemia, "hata nisiweze kushuka: kwa nini kazi niiache ikome, nishuke kwenu?" {3T 570.1}

Nilioneshwa, Januari 3, 1875, [Ni Furaha Hapa Kueleza Juu Ya Udhihirisho Wa Neema Ya Roho Mtakatifu Kwa Mama Ellen White Jioni Ya Januari 3, 1875, Kwamba Alikuwa Anaumwa Mafua Makali (Influenza), Na Kujifungia Chumbani Kwake Kitandani Kwa Juma Moja, Mpaka Matabibu Katika Taasisi Ya Afya Walikuwa Na Wasiwasi Juu Ya Hali Yake. Katika Hali Hii Alifuata Maelekezo Yaliyotolewa Katika Sura Ya Tano Ya Barua Ya Yakobo, Na Baada Ya Kuonesha Imani Kubwa, Kama Yule Mtu Katika Injili Aliyenyosha Mkono Wake Uliopooza, Yeye Naye Alifikia Kiwango Cha Ukombozi Wa Maumivu Na Magonjwa. Na Ilikuwa Hivi Karibuni Kwenye Maono, Yaliyodumu Kwa Dakika Kumi. Basi Akavaa Kwa Ajili Ya Mkutano, Akatembea Kuelekea Kanisani, Na Akanena Na Umati Uliosongamana Kwa Muda Wa Dakika Ishirini, Kisha Akatembea Kurudi Nyumbani. Tangu Wakati Huo Ameandika Sana, Na Amenena Na Watu Kwa Uhuru. Sasa Anajiandaa Kwa Safari Ndefu Kwenye Pwani Ya Pasifiki. J. W, Katika Toleo La Kwanza] Nilionyeshwa Kwamba Watu Wa Mungu Hawapaswi Hata Kwa Muda Mchache Kupumzika Kutoka Katika Lindo/Kesha Lao Au Umakini Wao. Shetani Yuko Njiani Kwetu. Amedhamiria Kuwashinda Watu Wa Mungu Kwa Majaribu Wale Wanaozishika Amri. Tusipompa Nafasi, Badala Yake Tukazipinga Hila Zake, Tukiwa Thabiti Katika Imani, Tutakuwa Na Nguvu Ya Kuachana Na Uovu Wote. Wale Ambao Wanazishika Amri Za Mungu Watakuwa Nguvu Katika Nchi Ikiwa Wataishi Kulingana Na Nuru Na Fursa Yao. Wanaweza Kuwa Mifano Ya Uchaji, Watakatifu Moyoni Na Katika Mazungumzo. Hatutapata Urahisi au maisha Bwerere, Ili Tuache Kukesha Na Kuomba. Kadri Wakati Unavyokaribia Kwa Kristo Kufunuliwa Katika Mawingu Ya Mbinguni, Majaribu Ya Shetani Yataletwa Kwa Nguvu Kubwa Juu Ya Wale Wanaozishika Amri Za Mungu, Kwani Anajua Kuwa Wakati Wake Ni Mfupi. {3T 570.2}

Kazi ya Shetani itaendelea kupitia mawakala. Wachungaji wanaoichukia sheria ya Mungu watatumia njia yoyote kuongoza roho kutoka kwenye uaminifu wao kwa Mungu. Maadui zetu wakubwa watakuwa miongoni mwa Waadventista wa siku ya kwanza. Mioyo yao imeamua kabisa kufanya vita dhidi ya wale wanaozishika amri za Mungu na walio na imani ya Yesu. Kundi hili linahisi kuwa ni fadhila au wema, kuzungumza, kuandika, na kuonesha chuki iliyo kali zaidi dhidi yetu. Hatuna haja

ya kutafuta kushughulika kwa haki mikononi mwao. Wengi wao wameongozwa na Shetani na wenda-wazimu dhidi ya wale wanaozishika amri za Mungu. Tutatukanwa na kuwasilishwa isivyo; nia na matendo yetu yote yatahukumiwa vibaya, na tabia zetu zitashambuliwa. Hasira ya joka itaoneshwa kwa namna hii. Lakini niliona kwamba hatupaswi kuvunjika moyo hata kidogo. Nguvu zetu ziko kwa Yesu, Wakili wetu. Ikiwa kwa unyenyekevu tunamtegemea Mungu na kuzishikilia ahadi Zake, Yeye atatupatia neema na hekima ya mbinguni ili tuhimili hila zote za Shetani na kutoka tukiwa washindi. {3T 571.1}

Kwa maoni yangu ya hivi karibuni niliona kuwa haitaongeza ushawishi wetu, au kutuletea kibali kwa Mungu, kulipiza kisasi au kushuka kutoka kwenye kazi yetu kubwa hadi kufikia kiwango chao katika kukutana na kashfa zao. Kuna wale ambao wataamua aina yoyote ya udanganyifu na uongo wa kuchukiza ili kupata kitu chao na kudanganya roho, na kuitupia lawama sheria ya Mungu na wale wanaopenda kuitii. Watarudia uongo usio na muafaka na mbaya, tena na tena, mpaka watajifanya waamini kuwa wao ni wakweli. Hizi ndizo hoja zenye nguvu ambazo wanapaswa kuzitumia dhidi ya Sabato ya amri ya nne. Hatupaswi kuruhusu hisia zetu kututawala na kutuondoa kwenye kazi ya kuuonya ulimwengu. {3T 571.2}

Kesi ya Nehemia iliwasilishwa mbele yangu. Alikuwa akijishughulisha na kujenga kuta za Yerusalemu, na maadui wa Mungu walikuwa wameamua kwamba kuta hizo zisijengwe. "Lakini ikawa, Sanbalati, na Tobia, na Waarabu, na Waamoni, na Waashdodi, waliposikia ya kuwa kazi ya kuzitengeneza kuta za Yerusalemu inaendelea, na ya kuwa mahali palipobomoka panaanza kuzibwa, basi wakaghadhibika mno; wakafanya shauri wote pamoja kuja kupigana na Yerusalemu, na kufanya machafuko humo." {3T 571.3}

Katika kesi hii roho ya chuki na upinzani kwa Waebrania iliunda kifungo cha umoja na kuunda huruma ya pamoja kati ya wanaume wenye tofauti ambao kwa kawaida wangeweza kupigana wao kwa wao. Hii inaonesha vema kile tunachoshuhudia mara kwa mara katika siku zetu katika umoja uliopo wa watu wa madhehebu tofauti kupinga Ukweli wa sasa, watu ambao umoja wao pekee huonekana kuwa wa kishetani katika asili yake, ukionesha uchungu na chuki dhidi ya masalio ambao hutii amri ya Mungu. Hii inaonekana hasa kwa waadventista wa siku ya kwanza, na siku zote, ambao wanaonekana kuwa maarufu kwa kuchukiana na kusingizana, wakati wanaweza kuokoa muda kutoka katika juhudi zao za kupotosha, kusingizia, kuharibiana tabia na katika kila unyanyasaji kwa Waadventista wa Sabato. {3T 572.1}

"Bali sisi tulimwomba dua Mungu wetu, tena tukaweka walinzi, mchana na usiku, kwa sababu yao, ili kuwapinga." Tuko katika hatari ya kila wakati ya kujitosheleza wenyewe, kutegemea hekima yetu wenyewe, badala ya kumfanya Mungu kuwa nguvu yetu. Hakuna kitu kinachomsumbua Shetani kama ujuzi wetu juu ya hila zake. Ikiwa tunahisi hatari zetu tutahisi hitaji la maombi, kama vile Nehemia, na

kama yeye tutapata ulinzi na utetezi wa uhakika ambao utatupa usalama katika hatari. Ikiwa sisi ni wazembe na wasiojali, hakika tutashindwa na hila za Shetani. Lazima tuwe macho. Wakati, kama Nehemia, tunapoamua kuomba, tukapeleka shida zetu zote na mizigo kwa Mungu, hatupaswi kuhisi kuwa hatuna la kufanya. Tunapaswa kukesha, kuwa macho na kuomba pia. Tunapaswa kuangalia kazi ya wapinzani wetu, wasije wakapata faida katika kudanganya roho. Tunapaswa, kwa hekima ya Kristo, kufanya bidii kushinda malengo yao, na wakati huo huo, tusiwaruhusu watushushe kutoka kwenye kazi yetu kubwa. Ukweli una nguvu kuliko makosa. Haki itashinda ubaya. {3T 572.2}

Watu wa Bwana wanatafuta kuponya ufa/mvunjiko ambao umefanyika katika sheria ya Mungu. "Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo." {3T 573.1}

Hii inawasumbua maadui wa imani yetu, na kila hali na mali hutumika kutuzuia katika kazi yetu. Na bado ukuta uliovunjika unaendelea kujengwa. Ulimwengu unaonywa, na wengi wanageuka kutoka katika kuikanyaga Sabato ya Yehova chini ya miguu yao. Mungu Yuko katika kazi hii, na mwanadamu kamwe hawezi kuizuia. Malaika wa Mungu wanafanya kazi pamoja na juhudi za watumishi Wake waaminifu, na kazi inakua kwa kasi na uthabiti. Tutakutana na upinzani wa kila aina, kama ilivyokuwa kwa wajenzi wa kuta za Yerusalemu; lakini ikiwa tunakesha na kuomba na kufanya kazi, kama walivyofanya, Mungu atapigana vita vyetu na kutupatia ushindi wa thamani. {3T 573.2}

Nehemia "alishikamana na Bwana, wala hakuacha kumfuata Yeye, bali alizishika amri Zake, ambazo Bwana alimwagiza Musa. Naye Bwana alikuwa pamoja naye." Wajumbe walitumwa mara kwa mara, wakiomba wawe na mkutano na Nehemia; lakini alikataa kukutana nao. Vitisho vya ukaidi/ujasiri vilifanywa kwa kile walichopendekeza kufanya, na wajumbe walitumwa kuwalaghai watu wanaohusika katika kazi ya ujenzi. Hawa waliwasilisha vishawishi vya kupendeza. Kuwasifia kwa kutia chumvi na wakawaahidi wajenzi uhuru kutoka katika kujizuia, na marupurupu mazuri, ikiwa wangeunganisha nia yao pamoja nao na kusitisha kazi yao ya ujenzi. {3T 573.3}

Lakini watu hawa waliamriwa wasishiriki katika mabishano na maadui zao na wasiwajibu neno hata moja, ili isiwepo faida ya maneno ambayo wangepewa. Vitisho na kejeli vilielekezwa kwao. Wakasema: "Hata kile wanachojenga, ikiwa

mbweha angepanda, angeuvunja ukuta wao wa mawe." Sanbalat "alikasirika, akapata ghadhabu kubwa, na kuwakejeli Wayahudi." Nehemia aliomba: "Sikia, Ee Mungu wetu; kwa maana tumedharauliwa, na uigeuze aibu yao juu ya kichwa chao." {3T 573.4}

"Na mimi nikatuma wajumbe kwao, nikasema, Hii ni kazi kubwa ninayoifanya mimi, hata nisiweze kushuka; mbona kazi ikome, hapo ninapoiacha, niwashukie? Nao wakaniletea maneno kama hayo mara nne; nikawajibu maneno kama yale. Ndipo Sanbalati akamtuma kwangu mtumwa wake vile vile mara ya tano, na barua wazi mkononi mwake." {3T 574.1}

Tutapokea upinzani mkali kutoka kwa Waadventista wanaoipinga sheria ya Mungu. Lakini, kama wajenzi wa kuta za Yerusalemu, hatupaswi kugeuzwa na kuzuiliwa kutoka kwenye kazi yetu kwa sababu ya taarifa, na wajumbe wanaotaka mazungumzo au ubishi, hata kwa vitisho vikali, kuchapishwa kwa uwongo, au hila zozote ambazo Shetani anaweza kuvitumia kushawishi . Jibu letu linapaswa kuwa: Tunajishughulisha na kazi kubwa, na hatuwezi kushuka. Wakati mwingine tutashangaa kujua ni njia gani tunapaswa kufuata ili kulinda heshima ya kazi ya Mungu na kuutetea Ukweli Wake. {3T 574.2}

Kisa na Hatua ya Nehemia inapaswa kuwa na matokeo makubwa juu ya akili zetu katika namna ya kukutana na wapinzani wa aina hii. Tunapaswa kupeleka vitu hivi vyote kwa Bwana katika maombi, kama Nehemia alivyoomba dua kwa Mungu, wakati roho yake mwenyewe ikishushwa/ikinyenyekezwa. Alishikamana na Mungu kwa imani isiyoyumba. Hii ndiyo hatua ambayo tunapaswa kuifuata. Muda ni wenye thamani sana kiasi cha kutotumiwa na watumishi wa Mungu katika kuonesha tabia zao, zilizotiwa giza na wale wanaoichukia Sabato ya Bwana. Tunapaswa kusonga mbele kwa ujasiri usioyumba, tukiamini kwamba Mungu ataupatia Ukweli Wake ushindi mkubwa na wa thamani. Kwa unyenyekevu, upole, na usafi wa maisha, tukimtegemea Yesu, tunapaswa kubeba nguvu ya kusadikisha pamoja nasi inayoonesha kwamba tuna Ukweli. {3T 574.3}

Hatuelewi, kama upendeleo wetu ulivyo, imani na ujasiri tunaoweza kuwa nao katika Mungu, na baraka kuu ambazo imani itatupatia. Kazi muhimu iko mbele yetu. Tunapaswa kufaa kimaadili kwa ajili ya mbingu. Maneno yetu na mfano vinapaswa kuuambia ulimwengu. Malaika wa Mungu wanahusika kikamilifu katika kuwahudumia watoto wa Mungu. Ahadi za thamani zimeandikwa na zote zinatusubiri kwa sharti la kutii kwetu matakwa ya Mungu. Mbingu imesheheni baraka tajiri zaidi, zote zikisubiri kuwasilishwa kwetu. Ikiwa tunahisi hitaji letu, na tunamjia Mungu kwa unyofu na kwa imani ya dhati, tutaletwa katika uhusiano wa karibu na mbingu na tutakuwa mifereji ya nuru kwa ulimwengu. {3T 574.4}

Onyo linahitaji kusikika mara nyingi: "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze." {3T 575.1}

MAMBO YA 36 AMBAYO KILA MWAMINI anapaswa kuombea



• HATA WATOTO WAKO WAJIFUNZE KUOMBEA WENGINE •

Kama ningewauliza waumini mia moja swali, "Je, mmeridhika na maisha yenu ya maombi?" Nadhani kungekuwa na wachache tu ambao wangesema kwa ujasiri kwamba wameridhika. Hiyo ni kwa sababu wengi wetu tunajitahidi kuomba. Tunajitahidi kupata muda. Tunajitahidi kubaki makini na macho katika maombi. Tunapofanya hivyo, muda wetu wa maombi mara nyingi huwa mfupi na wa juujuu, au tunajikuta tunaomba mambo yaleyale machache mara kwa mara. Je, kuna njia ya kubadilisha hili? Je, tunawezaje kukuza maisha ya maombi ya kina zaidi?

Vipi kama tungeangalia Biblia kwa mwongozo wa nini cha kuomba? Vipi kama tungeomba kutokana na Maandiko?

Wiki hii niliamua kuchimba zaidi ndani ya Biblia na nikatafuta kauli kuhusu maombi na kufusu mambo ambayo Mungu anasema tuyafuate kama waumini.

Haya ndiyo matokeo: Mambo 36 ya kibiblia ambayo kila Mkristo anapaswa kuombea.

Omba kwa ajili ya...

1. Jina la Mungu liheshimiwe na kutukuzwa (Mt.6:9).
2. Ufalme wa Mungu usonge mbele (Mt.6:10).
3. Ujuzi wa mapenzi ya Mungu (Kol.1:9), na utii Kwake (Mt.6:10).
4. Kukua kwa maarifa ya Mungu (Kol.1:10) yanayotokana na Neno Lake (Matendo 17:11).
5. Kumtegemea Mungu ili akupatie kila hitaji lako (Mt.6:11, Flp.4:19).
6. Furaha iliyojikita katika Yesu (Flp.4:4, 1 Thes.5:16).
7. Moyo usiogawanyika unaomcha Mungu (Zaburi 86:11, Mithali 9:1).
8. Chuki ya dhambi na uovu (Rum.16:19, Zab.97:10, Rum.12:21) na hamu ya haki (Mathayo 5:6).
9. Msaamha kutoka kwa Mungu unapotenda dhambi (1 Yohana 1:9).
10. Ushirika wa Karibu na Mungu (1 Yohana 1:6)
11. Moyo unaowasamehe wengine (Efe.4:32, Kol.3:13).
12. Mtazamo wa shukrani kwa wokovu wa Mungu (1 Petro 1:3-5) na matayarisho yake mengi (1 Wathesalonike 5:18, Zaburi 9:1-2).
13. Uwezo wa kuonyesha rehema na neema (Hosea 6:6, Mathayo 5:7).
14. Maadui zenu na wale wanaowatesa (Mathayo 5:44).
15. Moyo wa unyenyekevu na toba (Yakobo 4:6-10).
16. Utambuzi wa kujua mema na mabaya (Wafilipi 1:9-10, 1 Yohana 4:1).
17. Ukombozi kutoka majaribuni (Mt.6:13, 1 Kor.10:13, Mathayo 26:41).
18. Uhuru kutoka kwa uongo wa Shetani (Yohana 8:32, 44) na ushindi katika vita vya kiroho na vita (Waefeso 6:12).
19. Mguso wa uponyaji wa Mungu na/au neema ya kuvumilia mateso, chochote kile ambacho kingeleta utukufu zaidi kwa Yesu (Matendo 4:30, Yakobo 5:14-16, 2 Kor. 12:7-10).
20. Ujasiri katika kushiriki injili (Efe.6:18-19, Rum.1:16, Matendo 4:29).
21. Mungu kuondoa upofu wa kiroho wa wasioamini (Yohana 12:40, 2 Kor.4:3-4) na kuwaleta kwenye toba (2 Petro 3:9) na wokovu (Rum.10:1).
22. Mungu kuinua wafanyakazi zaidi kwa ajili ya shamba la mavuno (Mt.9:38).
23. Wamishenari (Rum.15:30-31) kwamba Mungu angewategemeza na kuwatumia watoto kuendeleza kuenea kwa injili.
24. Viongozi wa kanisa, kuhubiri kwa bidii na kufuata Ukweli (Ebr.13:7, Efe.6:19, 2 The.3:1).
25. Mamlaka zinazoongoza na viongozi kufanya maamuzi ya busara na ya haki ambayo yatawanufaisha waumini (1 Tim.2:1-4, Mit.21:1).
26. Imani kubwa zaidi kwa Mungu (Marko 9:24, Luka.22:32).
27. Hekima ya kuelewa nyakati na kujua jinsi ya kuishi kwa uaminifu kwa ajili ya Bwana (1 Mambo ya Nyakati 12:32, Yakobo 1:5).
28. Umoja na ukuaji katika kanisa (Yoh. 17:20-21, Matendo 2:47).
29. Kujitoa kwa kazi ya Mungu na kujitakasa ili kutufanya ufanane zaidi na Kristo (Rum. 8:29, 2 Kor. 3:18, 1 The. 4:3).
30. Bidii katika kuwafundisha watoto wako Neno la Mungu na kumpenda na kumtumikia Mungu wa Neno (Kum. 6:4-7).
31. Uelewa wa kina wa upendo wa Kristo (Efe. 3:14).
32. Upendo wa kweli zaidi kwa wengine unaoonekana kwa maneno na matendo (Yohana 13:34-35, 1 Kor. 13:4-8).
33. Uvumilivu na uaminifu katika kumtumikia Mungu kwa wakati wako, talanta, na pesa (1 Kor. 15:58, Mathayo 25:21,23).
34. Utimilifu wa Roho Mtakatifu (Luka 11:13) ili kuzaa matunda ya Roho (Gal. 5:22-23).
35. Njaa na kiu ya Neno la Mungu (Mt. 4:4).
36. Uwezo wa kuvumilia mateso na magumu kwa uaminifu na furaha ya subira (Kol. 1:11, Yakobo 1:2-4)

MaarifaMtandaoni.com | RohoYaUnabii.Org

MAANDIKO YA BIBLIA YENYE MSAADA *kwa Wazee*



MAANDIKO YANAYOTOA HESHIMA, FARAJA, HEKIMA NA MSAADA KWA WAZEE

NENO LA MUNGU NI NGUVU NA FARAJA KATIKA KILA HATUA YA MAISHA.

Nawe utakwenda kwa baba zako kwa amani; utazikwa katika uzee mwema.

— Mwanzo 15:15

(SWAHILI BIBLIA)

Wazee ndio walio na hekima, Na katika kuishi siku nyingi iko fahamu.

— Ayu 12:12

(SWAHILI BIBLIA)

Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana Wewe upo pamoja nami; gongo lako na fimbo yako vyanifariii.

— Zaburi 23:4

(SWAHILI BIBLIA)

Ee Mungu, umenifundisha tokea ujana wangu; Nimekuwa nikitangaza miujiza Yako hata leo. Na hata nikiwa ni mzee mwenye mvi, Ee Mungu, usiniache. Hata niwaeleze watu wa kizazi hiki nguvu Zako, Na kila atakayeıkuja uweza Wako.

— Zaburi 71:18

(NEW WORLD TRANSLATION)

Moffatt: "Do not forsake me, O God, even in old age..."

Waliopandwa katika nyumba ya Bwana Watasitawi katika nyua za Mungu wetu. Watazaa matunda hadi wakati wa uzee, Watajaa utomvu, watakuwa na ubichi.

— Zaburi 92:14, 15 (SWAHILI BIBLIA)

HESHIMA KWA WAZEE

Mwondokeeni mtu mwenye mvi; heshimuni uso wa mtu mzee; na mche Mungu wako, Mimi Ndimi Bwana.

— 1 Wafalme 19:32

(SWAHILI BIBLIA)

Usinitupe wakati wa uzee, Nguvu zangu zipungukapo usiniache.

— Zaburi 71:9

(SWAHILI BIBLIA)

Siku za miaka yetu ni miaka sabini, Na ikiwa tuna nguvu miaka themanini; Na kiburi chake ni taabu na ubatili, Maana chapita upesi tukatokomea mara..... Basi, utujulishe kuzihesabu siku zetu, Tujipatie moyo wa hekima.

— Zaburi 90:10, 12

(SWAHILI BIBLIA)

USHAURI WA WAZEE NI WA THAMANI

1 Wafalme 12:6-8, 13, 14, 19

6 Mfalme Rehoboamu akataka shauri kwa wazee waliokuwa wakisimama mbele ya Sulemani, baba yake, alipokuwa hai, akasema, Mwanipa shauri gani ili niwajibu watu hawa?

7 Wakamwambia wakasema, Ukikubali kuwa mtumishi wa watu hawa leo, na kuwatumikia, na kuwajibu, na kuwapa maneno mazuri, basi watakuwa watumishi wako daima.

8 Lakini akaliacha shauri iile la wazee, walilompa, akataka shauri kwa wale vijana waliokua pamoja naye, na kusimama mbele yake.

10 Akawaambia, Mwanipa shauri gani ili tuwajibu watu hawa, waliosema nami, wakinena Utufanyie jepesi kongwa lile alilotutwika baba yako?

11 Wale vijana waliokua pamoja naye wakamwambia, Uwaambie hivi watu wale waliokuambia, wakisema, Baba yako alilifanya zito kongwa letu, bali wewe utufanyie jepesi, uwaambie hivi, Kidole changu cha mwisho ni kinene kuliko kiuno cha baba yangu.

Basi kama vile baba yangu alivyowatwika kongwa zito, mimi nitaongeza kongwa lenu; baba yangu aliwapiga kwa mijeledi, bali mimi nitawapigeni kwa nge.....

19 Kwa hiyo Israeli wakaasi juu ya nyumba ya Daudi mpaka leo.

(SWAHILI BIBLIA)

SIFA ZOTE KWA BWANA

Msifuni Bwana kutoka duniani,... Vijana na wanawali; wazee na watoto: Msifuni Bwana kutoka nchi, Enyi nyangumi na vilindi vyote. Vijana waume, na wanawali, Wazee, na watoto; Na walisifu Jina la Bwana, Maana Jina Lake peke Yake limetukuka; Adhama Yake i juu ya nchi na mbingu.

— Zaburi 148:7, 12, 13

(SWAHILI BIBLIA)

Wana wa wana ndio taji ya wazee, Na utukufu wa watoto ni baba zao.

Fahari ya vijana ni nguvu zao, Na uzuri wa wazee ni kichwa chenye mvi.

Kweli nuru ni tamu, tena ni jambo la kupendeza macho kutazama jua (ni jambo zuri kuwa hai).

Naam, mtu akiishi miaka mingi, na aifurahie yote; lakini na azikumbuke siku zijazo za giza, kwa maana zitakuwa nyingi. Mambo yote yajayo ni ubatili.



NUKUU za RYU AFYA

Nukuu za afya za Kalamu ya matumaini:

Imetolewa na Dkt Calvin Dence na Mlei Grace Momadi-Masaka

Berrien Springs Michigan, 1994.

1. **Ikiwa tunashinda** hamu ya kula tunaweza kushinda juu ya yote. CD145
2. Soma waandishi bora juu ya sheria za maisha, uzima na afya. Kisha utii hoja yako. GW 242
3. Edeni ilipotea kwa hamu ya kula, na itarejeshwa kwa kushinda hamu ya kula. 161
4. Wale wanaotenda dhambi dhidi ya maarifa ya afya, na kutegemea dawa watapoteza maisha. MM224
5. Dawa za famasia zimefanya madhara zaidi na kuua zaidi ya zilivyosaidia. MM 27
6. Dawa za famasia nyingi zinapaswa kutupwa. MS 162
7. Ushawishi wa Roho Mtakatifu ni dawa bora kabisa kwa wagonjwa. MM 12
8. Vitu vya asili ni bora kwa afyaa kuliko dawa zote ulimwenguni. CH 169
9. Dawa ni dutu ya kigeni na yenye asili ya sumu. 134
10. Ugonjwa ni adhabu ya kukiuka sheria za asili. CH 347
11. Zula magonjwa kwa usafi na kutii sheria za afya. 4 SG 140
12. Magonjwa ni juhudi ya mwili na maumbile kuondoa uchafu wa mwili. CH 61
13. Kufanya vizuri ni dawa bora ya magonjwa. HH 447
14. Ugonjwa hauji kamwe bila sababu. 469.
15. Kusoma Biblia na kufanya kazi ni tiba bora kwa mili na akili za wagonjwa. 2T 325
16. Kufunga siku moja au mbili ni bora kuliko dawa za Famakia. CH 477
17. Kuacha kula kwa muda mfupi, au kuacha kabisa pombe na sigara ndiyo njia ya kuelekea kwenye afya 310
18. Pika kidogo na kula matunda mengi katika hali ya asili. 134
19. Imani katika Kristo na utii ni sayansi ya kweli ya uponyaji. CH 346
20. Tutakapochukua mpango wa asili wa bustani ya Edeni mapema, afya yetu itarejeshwa mapema. CH 174
21. Kwa kutii sheria za maisha TUNAHAKIKISHA AFYA YETU kuwa bora. CH 49
22. Maisha ya nje ya nyumba, hurejesha afya. 231
23. Imani ya mtu mgonjwa imekufa isipokuwa iiskiwa yuko tayari kubadilisha tabia zake. MM 262
24. Ikiwa una afya mbaya, wasaidie wengine na utajikuta unaanza kupona. 442
25. Panda juu katika Matengenezo ya Afya tunapokaribia mmisho. CH 467
26. Chochote kinachopunguza nguvu ya mwili, hufanya akili iwe dhaifu. KOL 346
27. Bila Matengenezo ya Afya matumaini yote ya mbinguni ni bure. CH 574-9
28. Tutakutana mbinguni na wale ambao tumewafanyia kazi katika Matengenezo ya afya. KOL 373
29. Hakuna usalama katika bidhaa za wanyama au samaki. CD1 411
30. Hakuna chakula kimoja kinachopaswa kupita kati ya midomo kati ya chakula CH 408
31. Kula chakula ganzi ubongo na husababisha njaa ya uwongo. 2T 212-3
32. Sukari huziba mifumo na inazuia mitambo. CH 149
33. Ikiwa wagonjwa wangeelimishwa kutumia mimea, hawatakufa kama vile dawa za kulevya. 308
34. Kuelewa utumiaji sahihi wa mimea na mizizi inmsaanisha hakuna haja ya daktari. 306
35. Matumizi ya mimea huafikiana na zoezi la imani.HL 305
36. Njia ya kweli ya kuponya wagonjwa ni kutumia mimea (herbs). HL 310
38. Chakula cha nyama na samaki, huunda magonjwa. KK 1: 1112
38. Wale walioongoka nusu-nusu kwenye ulaji wa nyama wataliacha kanisa. Ch 575
39. Dhima ya magonjwa ni mara 10 zaidi kwa wale wanaokula nyama, HL 62
40. kula nyama ni sababu ya moja kwa moja ya magonjwa. 2 SM 418-9
41. Wafanyakazi wa kimishenari wa tiba wanatoa wito wa mwisho. UT 71
42. Ufaharnu wa kutenda haki ni dawa bora kwa mgonjwa. 502
43. Vitu vya maumbile ni matabibu wa MUNGU; watio bora kwa afya kuliko dawa za mfamasia. CH 169-170
44. Kutii sheria za asili ni njia ya moja kwa moja kwenda mbinguni. CH
45. Kuna silika ya uponyaji katika zeri za mpaini, mierezi na miti ya miberoshi. 7T 77
46. Waganga wanashughulikia dawa na mgonjwa anauawa. SM 441
47. Daktari mwenye busara ataweza kugundua ugonjwa kwa kuchunguza mzizi au sababu yake. HL269
48. Mishipa ya fahamu bora, inaweza kupatikana tu kwa njia ya kujiikana nafsi, na kuwa na kiasi. KK 3: 1165
49. Tiba ya maji huleta matokeo mazuri ya asili (hydrotherapia). KK 7: 938
50. Lazima tuwe na afya kamilifu au hatuwezi kumpendeza MUNGU. KK 1: 1102
51. Huzuni hupunguza nguvu muhimu na mishipa ya fahamu. KK 3: 1146
52. Mazoezi ya asubuhi katika hewa safi ni kinga dhidi ya magonjwa yote. MLT
53. Masaa yasiyo ya kawaida ya kula na kunywa hupunguza nguvu za ubongo. YT 5/3/9
54. Wengi hufa kutokana na magonjwa ambayo ni ya kufikirika kabisa. HH 171
55. MUNGU aliiondoa nyama na akawapa mana ili kuamsha nguvu za akili. KK 1: 1113
56. Kuhusu matengenezo ya afya, zezeta hawawajibiki. MM 289
57. Wokovu hauwezekani bila Matengenezo ya Afya. 137
58. Madaktari wa Kikristo hawawezi kutoza bei kubwa kama vile waganga wa kidunia. MM 125
59. Dawa za BWANA mwenyewe ni hewa, maji na jua. 228
60. Amani ya ndani, na upendo kwa MUNGU vitaimarisha akili. 2T 327



MaarifaMtandaoni.Com **SamaritanLaymenMinistries.Org**